

# FASIRI YA BIBLIA ISIYOGHARAMIWA

**UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!**

***Mwandishi Luka:Kitabu cha Matendo***

Na Dr. Bob Utley,  
Profesa mstaafu wa kanuni za ufasiri  
(utafasili wa Biblia)

*STUDY GUIDE COMMENTARY SERIES  
OLD TESTAMENT, VOL.3B*

Copyright © 2013 [Bible Lessons International](http://www.freebiblecommentary.org). Haki zote zimehifaziwa. Nukuu au usambazaji wowote wa sehemu ya maandishi haya lazima utolewe pasipo malipo yoyote. Nukuu au usambazaji huo lazima pongezi zimwendee mwandaaji Dr. Bob Utley na ikijumuisha nukuu toka [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org)

Msingi wa Mandiko ya Kibiblia yaliyotumika katika fasihi hii yametoka katika toleo la: New American Standard Bible (lililoboreshwa, 1995)  
Copyright ©1960, 1962, 1963, 1968, 1971, 1972, 1973, 1975, 1977, 1995 by The Lockman Foundation, P. O. Box2279, La Habra, CA  
90632-2279

# ORODHA YA YALIYOMO

Neno Toka kwa Mwandishi: Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia! .....	7
Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika .....	9
Vifupisho Vilivyotumika Katika Fasihi Hii .....	16
Fasiri:	
Utangulizi wa Matendo ya Mitume .....	17
Matendo ya Mitume 1 .....	25
Matendo ya Mitume 2 .....	53
Matendo ya Mitume 3 .....	95
Matendo ya Mitume 4 .....	116
Matendo ya Mitume 5 .....	136
Matendo ya Mitume 6 .....	160
Matendo ya Mitume 7 .....	172
Matendo ya Mitume 8 .....	190
Matendo ya Mitume 9 .....	203
Matendo ya Mitume 10 .....	221
Matendo ya Mitume 11 .....	235
Matendo ya Mitume 12 .....	246
Matendo ya Mitume 13 .....	256
Matendo ya Mitume 14 .....	277
Matendo ya Mitume 15 .....	289
Matendo ya Mitume 16 .....	302
Matendo ya Mitume 17 .....	315
Matendo ya Mitume 18 .....	330
Matendo ya Mitume 19 .....	341
Matendo ya Mitume 20 .....	354
Matendo ya Mitume 21 .....	368
Matendo ya Mitume 22 .....	379
Matendo ya Mitume 23 .....	388
Matendo ya Mitume 24 .....	398
Matendo ya Mitume 25 .....	405
Matendo ya Mitume 26 .....	412
Matendo ya Mitume 27 .....	425

Matendo ya Mitume 28 .....	435
Viambatisho:	
Maelezo Mafupi ya Muundo wa Kisarufi Cha Kiyunani .....	444
Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi.....	453
Simulizi za kihistoria .....	457
Ufafanuzi/Farahasa .....	459
Maelezo ya Kimaandiko .....	468

## VIELELEZO VYA MADA MAALUM

Kupaa .....	27
Nafsi ya Roho .....	27
Kuonekana kwa Yesu Baada ya Ufufuo.....	29
Uwakilishi wa Namba Katika Maandiko.....	30
Ufalme wa Mungu .....	32
Majina Ya Uungu.....	35
Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH .....	37
Kuja Juu Mawinguni .....	39
Chati ya Majina ya Mitume.....	40
Yuda Iskarioti .....	43
Wanawake Waliofuatana na Yesu na Wanafunzi Wake.....	44
Uvuvio .....	46
Uainishi .....	46
Namba Kumi na Mbili .....	49
Moyo.....	51
Roho ( <i>Pneuma</i> ) .....	55
Moto .....	56
Mtazamo wa Biblia Kuhusiana na Kilevi na Ulevi .....	60
Mafundisho ya Kanisa la Mwanzo .....	63
Nyakati Hizi na Nyakati Zijazo .....	64
Wanawake Katika Biblia.....	65
Fasihi ya Matukio ya Siku za Mwisho.....	68
Maneno kwa Ujio wa Mara ya Pili .....	69
Jina la Bwana.....	70
Yesu wa Nazareti.....	71
Tumaini .....	74
Wafu Wako Wapi? .....	75
Masihi .....	76
Mwili ( <i>sarx</i> ) .....	77
Uungu.....	78
Mungu Kuelezewa Kama Mwanadamu .....	79
Toba (Agano la Kale) .....	82
Ubatizo.....	83

Imani ya Mungu Mmoja.....	86
Wokovu (Njeo za Vitenzi vya Kiyunani Vilivyotumika) .....	88
<i>KOINŌNIA</i> (Ushirika) .....	90
Uchaguzi/Maamuzi ya Kabla na Hitaji la Usawa wa Kithiolojia .....	92
Agano .....	92
Kuwasaidia Wahitaji.....	97
Utukufu ( <i>DOXA</i> ) .....	101
Pontio Pilato.....	103
Aliye Mtakatifu.....	104
Haki .....	105
Mwanzishaji/Kiongozi ( <i>archgēos</i> ) .....	108
Imani, Amini au Kusadiki.....	109
Masadukayo.....	117
Wakuu wa baraza la Sinagogi .....	120
Jiwe kuu la pembeni .....	124
Kutiwa mafuta katika Biblia .....	129
Familia ya Herode Mkuu.....	130
Ujasiri .....	132
Barnaba .....	134
Shetani .....	138
Uovu binafsi .....	139
Utaratibu wa mazishi .....	142
Maneno ya Kiyunani yaliyotumika kupima na vidokezo Vyake.....	143
Kanisa ( <i>Ekklesia</i> ).....	144
Malaika na pepo .....	147
Upungaji pepo.....	148
Mafarisayo .....	155
Gamalieli .....	156
Kusadiki, Amini, Imani na uaminifu katika Agano la Kale .....	163
Kuweka mikono katika Biblia .....	167
Tarehe ya kuondoka kwa Waisrael kule Misri .....	178
Mahali ulipo Mlima Sinai .....	181
Mtindo ( <i>Topos</i> ) .....	184
Miujiza .....	193

Watakatifu ( <i>hagios</i> ) .....	208
Mwana wa Mungu .....	211
Utakatifu wa Agano Jipya/utakaso .....	216
Toba katika Agano la Kale .....	217
Kuhukumu, Hukumu, na Haki katika Isaya .....	232
Mkono (Ulivyoielezwa toka kitabu cha Ezekiel) .....	241
Unabii wa Agano Jipya .....	242
Maombi ya Kusihi .....	249
Yakobo, Nduguye Yesu .....	253
Nuru .....	258
Kufunga .....	259
Kanoni za Kiebrania.....	264
Wazawa wa Israel walioishi Palestina kabla .....	266
Maoni ya Paulo Kuhusu Sheria ya Musa.....	272
Kutumwa ( <i>Apostellō</i> ).....	280
Hitaji la Ustahimilivu .....	285
Sila/Silvanus .....	297
Uhuru wa Mkristo dhidi ya Wajibu wa Mkristo.....	298
Yesu na Roho .....	306
Mji wa Korintho .....	331
Fasihi ya Kimashariki.....	345
Malaika katika maandiko ya Paulo .....	347
Kutubu(Agano Jipya).....	348
Uovu na Maadili katika Agano Jipya .....	360
Uasi ( <i>APHISTĒMI</i> ) .....	364
Kuadilisha.....	366
Mapenzi ( <i>thelēme</i> ) ya Mungu.....	371
Nadhiri ya Mnazareti .....	375
Ibada kwa walio katika huzuni.....	386
Watakatifu ( <i>hagios</i> ).....	392
Laana (ANATHEMI).....	394
Bernike.....	409
Mamlaka ( <i>exousia</i> ).....	418
“kweli” katika maandiko ya Paulo.....	422
Mabaki (BDB 984, KB 1375), maana tatu.....	440

# **NENO TOKA KWA MWANDISHI NI KWA NAMNA GANI FASIHI HII ITAKUSAIDIA?**

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoka na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

## **KANUNI YA KWANZA**

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni—ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

## **KANUNI YA PILI**

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafasiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtizamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara, kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua, kueleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafasiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima. Tafasiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafasiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la (UBS<sup>4</sup>). Andiko hili liliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.

2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama “Upokeaji wa Maandishi”. Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.
3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafasiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today’s English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS<sup>4</sup> na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafasiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoriki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasiri ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## **KANUNI YA TATU**

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafasiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafasiri nyingine hutusaidia tusiwe ving’ang’anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafasiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley

June 27, 1996

Haki Miliki © 2013 [Bible Lessons International](http://www.biblelessons.org)



# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

## UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIO THIBITIKA

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa. Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliunganishwa, una uweo wa kukabilia na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko. Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru, lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:


## I. DHANIO

1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
  - Wapokeaji wa mwanzo
  - Ujumbe ulioandikwa
  - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
  - a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
  - b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
  - c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
  - d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
  - e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
  - f. Maana zilichaguliwa kuwakilisha ujumbe


Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

## II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-historia wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji” (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.



Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:



Kwa kweli vitu hivi nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya “mwitikio wa msomaji” (unamaanishwa nini kwangu). Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasih, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

### III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: “Biblia inaangazia zaidi katika fasihi”. Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

#### 1. Mduara wa kwanza wa usomaji

- a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
  - 1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
  - 2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
  - 3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
- b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.

- c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
- d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
  - 1) Agano la kale
    - a) Simulizi za waebrania
    - b) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
    - c) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
    - d) Alama za siri za ki-sheria
  - 2) Agano jipya
    - a) Simulizi (Injili, matendo)
    - b) Hadithi za mafumbo (Injili)
    - c) Barua/nyaraka
    - d) Fasihi za mafunuo

## 2. Mduara wa pili wa usomaji

- a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
- b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
- c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

## 3. Mduara wa tatu wa usomaji.

- a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
- b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
  - 1) Mwandishi
  - 2) Tarehe
  - 3) Wapokeaji
  - 4) Kusudu mahsusi la uandishi
  - 5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
  - 6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
- c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
- d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

## 4. Mduara wa nne wa usomaji

- a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
  - 1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
  - 2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
  - 3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
- b. Angalia fahisi au muundo wa kisarufi
  - 1) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
  - 2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
  - 3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
- c. Taja vipengele vifuatavyo:-
  - 1) Istilahi muhimu
  - 2) Istahili zisizo za kawaida
  - 3) Muundo muhimu wa kisarufi
  - 4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
- d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
  - 1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
    - a) Vitabu vya thiolojia
    - b) Biblia za marejeo
    - c) Itifaki

- 2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana na uthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.
  - 3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kile kile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.
- e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
- 1) Soma biblia
  - 2) Ensiklopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
  - 3) Tangulizi za biblia
  - 4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

#### **iv. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.**

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama “uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi”. Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!

Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji≠3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafasiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema “asema Bwana” lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni “zetu” na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Biblia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

#### **v. Sura ya utafasiri wa kiroho.**

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18  
 “Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni.”
2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm, *Protestant Biblical Interpretation (tafsiri ya biblia ya ki-protestanti)* Uk.75:  
 Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.
3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:  
 Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## VI. Njia hizi za Fasiri

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji)* wa fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya “mduara wa usomaji #3” angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
  - a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
  - b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
  - c. The New King James Version (NKJV)
  - d. The New Revised Standard Version (NRSV)
  - e. Today’s English Version (TEV)
  - f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa “mada ya sentensi” au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
  - a. Mazingira ya fasihi

- b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
  - c. Habari za kisarufi
  - d. Usomaji wa neno
  - e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
- a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswada wa “Upokeaji wa Maandiko halisi”.
  - b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
  - c. The Today’s English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
  - d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
- a. Tofauti za mswada
  - b. Maana ya maneno mbadala
  - c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
  - d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII

AB	Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman
ABD	Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman
AKOT	Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens
ANET	Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard
BDB A	Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs
IDB	The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick
ISBE	International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr
JB	Jerusalem Bible
JPSOA	The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America)
KB	The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner
LAM	The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa
LXX	Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970
MOF	A New Translation of the Bible by James Moffatt
MT	Masoretic Hebrew Text
NAB	New American Bible Text
NASB	New American Standard Bible
NEB	New English Bible
NET	NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition
NRSV	New Revised Standard Bible
NIDOTTE	New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem A. VanGemeren
NIV	New International Version
NJB	New Jerusalem Bible
OTPG	Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith
REB	Revised English Bible
RSV	Revised Standard Version
SEPT	The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970
TEV	Today's English Version from United Bible Societies
YLT	Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young
ZPBE	Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney



# UTANGULIZI WA MATENDO YA MITUME

## MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Matendo ya Mitume inatengeneza muunganiko wa kipekee kati ya historia ya maisha ya Yesu (Injili) na fasiri ya wanafunzi wake, mahubiri, na matumizi ya matendo yake na maneno katika barua za Agano Jipya.
- B. Kanisa la kwanza lilianzisha na kuzungusha makusanyo ya nyaraka mbili za Agano Jipya: (1) injili (Injili nne) na (2) Mtume (barua za Paulo). Hata hivyo, pamoja na uvumi wa kwanza kuhusu upakwa Mafuta wa Kristo wa karne ya pili, thamani ya kitabu cha matendo ya Mitume kilikuja kuwa dhahiri. Matendo ya Mitume kinafunua maudhui na kusudi la mahubiri ya Kitume (kerygma) matokeo ya ajabu ya injili.
- C. Usahihi wa kihistoria wa Matendo ya Mitume umetiwa mkazo na kuthibitishwa na gunduzi akiolojia, hasa kuhusiana wadhifa wa serikali ya Kiruni
1. *stratēgoi*, Mdo.16:20,22,35,36 (pia linatumika kwa nahodha wa meli, Luka 22:4,52; Mdo. 4:1; 5:24-26)
  2. politarchas, Mdo. 17:6,8; na prōtō, Mdo. 28:7, kama vile A. N. Sherwin-White, Roman Society and Roman Law in the New Testament  
Kumbukumbu ya Luka inaandika juu ya mvutano ndani ya kanisa la kwanza, hata mapigano kati ya Paulo na Barnaba (kama vile Mdo. 15:39). Hii inaaksi usawa, uwiano, Historia iliyofanyiwa utafiti/maandiko ya kithiolojia.
- D. Kichwa cha habari cha kitabu kinapatikana katika muundo tofauti kidogo katika a
1. Machapisho  $\kappa$  (Sinaiticus), Tertullian, Didymus, na Eusebius wana "Mdo" (ASV, NIV)
  2. Machapisho B (Vaticanus), D (Bezae) katika kuungwa mkono na, Irenaeus, Tertullian, Cyrian, na Athanasius ana "Matendo ya Mitume" (KJV, RSV, NEB)
  3. Machapisho A<sup>2</sup> (masahihisho ya kwanza ya Alexandrinus), E, G, na Chrysostom wana "Matendo ya Mitume Watakatifu "  
Inawezekana kwamba maneno ya Kiyunani praxeis, praxis (matendo, njia, tabia, matendo, mazoezi) inaaksi aina ya uandishi wa kifasihi wa Shamu ambayo inaashiria maisha na matendo ya watu mashuhuri na wenye ushawishi (mfano Yohana, Petro, Stefano, Filippo, Paulo). Kitabu yawezekana kwa asili hakikuwa na jina (kama injili ya Luka).
- E. Kuna desturi mbili za kipekee za kimaandiko. Ile fupi ni ya Kiiskanderia (MSS P<sup>45</sup>, P<sup>74</sup>,  $\kappa$ , A, B, C). Familia ya Magharibi ya Machapisho (P<sup>29</sup>, P<sup>38</sup>, P<sup>48</sup> na D) inaonekana kujumuish maelezo mengine mengi zaidi. Haijulikana kama zinatoka kwa mwandishi au zilikuwa ni maingizo ya baadae ya mwandishi, yakijikita katika desturi za kanisa la kwanza. Wanataaluma wengi wa kimaandiko wanaamini kwamba machapisho ya magharibi yana maingizo ya baadae kwasababu
1. kufanya iteleze au kutengeneza vitu visivyo vya kawaida au vigumu
  2. kuongeza maelezo ya ziada
  3. kuongeza tungo Fulani ili kutia mkazo Yesu kama Kristo
  4. hayanukuliwi na waandishi wowote wa kwanza wakati wowote katika karne tatu za kwanza (kama vile F. F. Bruce, Acts: Greek Text, ukurasa 69-80)  
Kwa ajili ya mjadala wa ziada tafuta A Textual Commentary on the Greek New Testament kilichoandikwa na Bruce M. Metzger, kilichochapishwa na the United Bible Societies, ukurasa 259-272. Kwasababu ya maingizo/maelezo yaliyoongezwa baadae, Fasiri hii haitajishughulisha na mbadala yote ya kimaandiko. Ikiwa kuwepo kwa tofauti za kimaandiko ni muhimu kwa fasiri, hivyo na hapo tu ndipo tu tutakapojishughulisha na fasiri.

## MWANDISHI

- A. Kitabu hakijulikani, lakini uandishi wa Luka unaonekana kwa nguvu zote.

1. Cha kipekee na kustaajabisha "sisi" sehemu (Mdo. 16:10-17 [safari ya pili ya kimishionari katika Filipi]; Mdo 20:5-15; 21:1-18 [mwishoni mwa safari yake ya tatu ya umishionari] na Mdo. 27:1-28:16 [Paulo alitumwa Rumi kama mfungwa]) kwa nguvu inamaanisha Luka kama mwandishi.
  2. Muunganiko kati ya Injili ya tatu na Mdo ni dhahiri mtu anapolinganisha Luka 1:1-4 pamoja na Mdo. 1:1-2.
  3. Luka, Daktari wa Mataifa, anatajwa kama rafiki/mtenda kazi wa Yesu Kol. 4:10-14, Filemoni 24, na 2 Timotheo 4:11. Luka ni mwandishi wa mataifa pekee katika Agano Jipya
  4. Shahidi asiyejulikana wa kanisa la kwanza ilikuwa ni kwamba mwandishi alikuwa anamjua.
    - a. kisehemu cha wakina Murato (a.d. 180-200 B.K kutoka Rumi anasema, "kilitungwa na tabibu Luka")
    - b. maandiko Irenaeus (130-200 B.K)
    - c. maandiko ya Klement wa Alexandria (156-215 B.K)
    - d. maandiko ya Tertullian (160-200 B.K)
    - e. maandiko ya Origen (185-254 B.K)
  5. Ushahidi wa ndani wa muundo na misamiati (hasa maneno ya kitabibu) anathibitisha kuwa Luka ndiye mwandishi (Sir William Ramsay na Adolph Von Harnack).
- B. Tuna vyanzo vitatu vya taarifa kuhusu Luka.
1. Kuna vifungu vitatu katika Agano Jipya (Kol. 4:10-4; Filemoni 24; 2 Tim. 4:11) na kitabu cha Matendo ya Mitume.
  2. Dibaji ya mpinga-Marcion ya karne ya pili kwa Luka (160-180 B.K.)
  3. Wanahistoria wa kanisa la kwanza wa karne ya nne Eusebius, katika andiko lake la *Ecclesiastical History*, 3:4, anasema "Luka, kwa kabila lake alikuwa mzaliwa wa Antiokia, na kwa taaluma, tabibu, akiisha kujiweka karibu na Paulo na akiisha kuambatana na mitume wengine waliobaki waliokuwa hawako karibu, ametuachia mfano wa uponyaji wa nafsi ambao aliupata kutoka kwao katika vitabu viwili vilivyovuviwa, Injili na Matendo ya Mitume."
  4. Huu ni utunzi kamili wa wasifu wa Paulo.
    - a. Mtu wa mataifa (anaorodheshwa katika Kol. 4:12-14 akiwa na Epafa na Dema, sio pamoja na wasaidizi wa Kiyahudi)
    - b. kutoka aidha kwa Antiokia ya Siria (Dibaji ya Mpinga-Marcion kwa Luka) or Philippi of au Filipi ya Makedonia (Sir William Ramsay kwenye Mdo. 16:19)
    - c. Tabibu (kama vile Kol. 4:14), au angalau mtu aliyeelimika vizuri
    - d. alikuwa mwongokaji katika utu uzima wake baada ya kanisa kuanza katika Antiokia (Dibaji ya Mpinga-Marcion)
    - e. mtendakazi aliyesafiri na Paulo ("sisi" sehemu za Matendo ya Mitume)
    - f. hakuwa ameo
    - g. aliandika Injili ya tatu na Matendo ya Mitume (utangulizi unaofanana na mtindo uleule na misamiati)
    - h. alikufa akiwa na umri wa miaka 84 akiwa Boeotia
- C. Changamoto za uandishi wa Luke
1. Mahubiri ya Paulo akiwa Mars Hill huko Athens anatumia vipengele vya kifalsafa vya kiyunani na maneno kuunda msingi unaojulikana (kama vile Mdo. 17), lakini Paulo, katika Warumi 1-2, anaonekana kufanya "misingi inayojulikana" (asili, shahidi wa ndani wa kimaadili) kama isiyo na manufaa.
  2. Mahubiri ya Paulo na maoni katika Matendo ya Mitume yanamuonesha kama mkristo wa Kiyahudi anayamaanisha kwa Musa, lakini barua za Paulo zinashusha thamani ya sheria kama tatizo na zinazopit
  3. Mahubiri ya Paulo katika Matendo ya Mitume hayana shabaha ya mwisho wa nchi ambayo vitabu vyake vyake vya kwanza vinafanya (yaani I na 2 Wathesalonike).
  4. Haya maneno ya mvutano yanashangaza, muundo, na na msisitizo wake vinashangaza, lakini havitoi hitimisho. Pale vigezo vilevile vinapotumika kwenye Injili, Yesu wa Vitabu vine vya Injili anazungumza

tofauti sana kuliko Yesu wa Yohana. Bado, wanataaluma wachache wangekataa kwamba wote wanaaksi maisha ya Yesu.

- D. Tunapojadili uandishi wa Matendo ya Mitume ni muhimu kwamba tujadili vyanzo vya Luka kwasababu wanataaluma (mfano C. C. Torrey,) ananaamini Luka alitumia chanzo cha nyaraka za kiaramu (au vya desturi za kinywa) kwa sura zake kumi na tano za mwanzo. Ikiwa hii ndiyo kweli, Luka ni mhariri wa nyaraka hizi na sio mwandishi. Hata katika mahubiri yake ya Paulo, Luka anatoa tu muhtasari wa maneno ya Paulo, na sio ripoti ya kinywa. Matumizi ya vyanzo ya Luka ni swali muhimu kama ilivyo kwa uandishi wake.

## TAREHE

- A. Kuna mjadala mkubwa na hali ya kutoelewana kuhusu muda Matendo ya Mitume kilipoandikwa, lakini kwa tukio yenyewe yanafunika kutokea kipindi cha 30-63 B.K (Paulo aliachiliwa kutoka gerezani katika Rumi katikati ya miaka ya 60 na kukamatwa tena na kuhukumiwa chini ya Nero, yawezekana katika mateso ya miaka ya 65 B.K).
- B. Ikiwa mtu atadhania asili ya kitabu cha msamaha kuhusu selikari ya Kirumi, alafu tarehe (1) Kabla ya 64 B.K (Mwanzo wa dhiki ya mateso ya Nero ya Wakristo katika Rumi) na/au (2) inayohusiana na mapinduzi ya 66-73 B.K.
- C. Ikiwa mtu atajaribu kufananisha Injili ya Luka katika taratibu, hapo tarehe ya kuandikwa kwa Injili kunashawishi tarehe ya kuandikwa kwa Matendo ya Mitume. Toka kuanguka kwa Yerusalemu mpaka Tito katika miaka ya 70 B.K kulitabiriwa (yaani Luka 21), lakini haikuelezewa, kunaonesha kuhitaji tarehe kabla ya mwaka 70 B.K. Ikiwa ndivyo, hapo Matendo ya Mitume, liliandikwa kama matukio ya baadae, lazima iwekewe tarehe wakati mwingine baada ya Injili.
- D. Ikiwa mtu atasumbuka na kuisha ghafla (Paulo akiwa bado yuko gerezani Rumi, F. F. Bruce), hapo tarehe unayofanana na mwisho ya kifungo cha kwanza cha Paulo cha Kirumi, 58-63, inapendelewa.
- E. Baadhi ya tarehe za kihistoria zinazohusiana na matukio yaliyowekewa kumbukumbu katika Matendo ya Mitume.
1. kuenea kwa njaa chini ya Claudius (Mdo. 11:28, 44-48 B.K)
  2. kifo cha Herode Agrippa I (Mdo. 12:20-23, 44 B.K [kiangazi])
  3. baraza la Sergius Paulus (Mdo. 13:7, kuteuliwa katika 53 B.K)
  4. Ufukuzwaji wa Wayahudi kutoka Romi na Claudius (Mdo. 18:2, 49 B.K [?])
  5. Baraza la Gallio, Mdo. 18:12 (51 au 52 B.K [?])
  6. Baraza la Felix (Mdo. 23:26; 24:27, 52-56 B.K [?])
  7. kusimikwa mbadala kwa Felix na Festus (Mdo. 24:27, 57-60 B.K [?])
  8. urasimishaji wa Rumi ya Kiyudea
    - a. Mwakili/Waendesha mashitaka
      - (1) Pontio Pilato, 26-36 B.K
      - (2) Marcellus, 36-37 B.K
      - (3) Marullus, 37-41 B.K
    - b. Katika mwaka wa 41 B.K mbinu ya uwakili ya utawala wa Kirumi ilibadilishwa kuwa ya mfano wa matendo jarabati. Mtawala wa Kirumi aitwaye Claudius, aliteuliwa na Herode Agrippa I katika mwaka 41 B.K.
    - c. Baada ya Herode Agrippa I, 44 B.K, mbinu za uwakili zilianzishwa upya mpaka mwaka 66 B.K

- (1) Antonio Felix
- (2) Porcius Festo

## KUSUDI NA MUUNDO

- A. Kusudi moja la kitabu cha Matendo ya Mitume ilikuwa ni kuweka katika maandishiule ukuaji wa haraka wa wafuasi wa Yesu kutoka katika mizizi mpaka kuelekea huduma ya dunia nziama, kutoka katika kujifungia chumba cha juu kwenda kwenye hekalu la Kaisari:
1. Utaratibu huu wa Kijiografia unafuata Matendo ya Mitume 1:8, ambayo ni Agizo Kuu la Matendo ya Mitume (Mt. 28:19-20).
  2. Huku kupanuka kwa Kijiografia kunaielezwa katika baadhi ya njia.
    - a. Kutumia majiji makubwa na mipaka ya kitaifa. In Acts there are Katika Matendo ya mitume kuna nchi 32, majiji 54 na visiwa vya Shamu 9 vilivyotajwa. Majiji makubwa matatu makubwa ni Yerusalkemu, Antiokia na Rumi (kama vile Mdo. 9:15).
    - b. Kutumia watu muhimu. Matendo ya Mitume inawezekana kugawiwa katika nusu mbili: huduma za Petro na Paulo. Kuna zaidi ya watu 95 waliotajwa katika Matendo ya Mitume, lakini wakubwa ni Stefano, Philipo, Barnaba, Yakobo na Paulo.
    - c. Kuna miundo miwili au mitatu ya kifasihi ambayo inajitokeza kwa kurudia rudia katika Matendo ya Mitume ambayo inaonekana kuaksi kujitambua kwa mwandishi katika jaribio kwenye muundo:

(1)Kauli za Muhtasari	(2) kauli za ukuaji	(3) matumizi ya namba
Mdo. 1:1 – 6:7 (katika Yerusalem)	2:47	2:41
Mdo. 6:8 – 9:31 (katika Palestina)	5:14	4:4
Mdo. 9:32 – 12:24 (kuelekea Antiokia)	6:7	5:14
Mdo. 12:25 – 15:5 (Kuelekea Asia ndogo)	9:31	6:7
Mdo. 16:6 – 19:20 (kuelekea Ugiriki)	12:24	9:31
Mdo. 19:21 – 28:31 (Kuelekea Rumi)	16:5	11:21, 24
	19:20	12:24
		14:1
		19:20

- B. Matendo ya Mitume kwa dhahiri inahusiana kwa uelewa ambao ulizunguka kifo cha Yesu kwa uhaini. kwa dhahiri, Luka anawaandikia Mataifa (Theofilo, yawezekana Mrumi rasmi). Yeye anatumia (1) Hotuba za Petro, Stefano na Paulo kuonesha hila za Wayahudi na (2) Hali chanya ya wafanyakazi rasmi wa kiserikali kuhusu Ukristo. Warumi hawakuwa na kitu cha kuhofia kutoka kwa wafuasi wa Yesu.
1. hotuba ya viongozi wa Kikristo
    - a. Petro, Mdo. 2:14-40; 3:12-26; 4:8-12; 10:34-43
    - b. Stefano, Mdo 7:1-53
    - c. Paulo, Mdo. 13:10-42; 17:22-31; 20:17-25; 21:40-22:21; 23:1-6; 24:10-21; 26:1-29
  2. Mawasiliano na wafanyakazi waliorasmi wa kiserikali
    - a. Pontio Pilato, Luka 23:13-25
    - b. Sergius Paulus, Mdo 13:7,12
    - c. Mahakimu wakuu wa Filipi, Mdo. 16:35-40
    - d. Gallio, Mdo. 18:12-17
    - e. Asiarchs wa Efeso, Mdo. 19:23-41 (hasa mstari wa 31)
    - f. Claudius Lysias, Mdo. 23:29

- g. Felix, Mdo. 24
  - h. Porcius Festus, Mdo. 24
  - i. Agrippa II, Mdo. 26 (hasa 32)
  - j. Publius, Mdo. 28:7-10
3. Mtu mmoja anapolinganisha mahubiri ya Petro, ni wazi kwamba Paulo sio mvumbuzi lakini mtangazaji wa injili ya kweli ya kitume, Mwaminifu. Ikiwa mtu yeyote ataiga yoyote hapo huyo atakuwa Petro (kama vile 1 Petro) ambaye anatumia tungo za Paulo na misamiati. Mafundisho ya kanisa la kwanza (*kerygma*) yanaunganisha!
- C. Luka sio tu kwamba aliulinda Ukristo kabla ya serikali ya Kirumi, lakini pia alimtetea Paulo mbele ya kanisa la Mataifa. Paulo alikuwa akivamiwa kwa kurudiwa rudiwa na Wayahudi (Wayahudi wadini wa Kigalatia, hao "Mitume wakuu" wa 2 Wakorintho 10-13); na kikundi cha Kiyunani (Elimu ya ujuzi ya Kolosai na efeso). Luka anaonesha umahiri wake kwa kuufunua moyo wake vizuri na thiolojia katika kusafiri na hotuba.
- D. Japokuwa Matendo ya Mitume hakikusudiwa kuwa kitabu cha mafundisho ya kidhehebu, haiweki kumbukumbu kwa ajili yetu vipengele vya mahubiri ya kwanza ya mitume ambayo C. H. Dodd has called anayaita "the *Kerygma*" (Mafundisho ya awali) (kweli muhimu kuhusu Yesu). Hii inatusaidia sisi kuona nini walihisi kuwa muhimu kwa injili hasa kama zinavyofanana na kifo cha Yesu na ufufuo

### **MADA MAALUM: MAFUNDISHO YA KANISA LA KWANZA**

Kuna maoni mengi kuhusu Ukristo. Siku zetu hizi ni siku za wingi wa dini, kama ilivyokuwa karne ya kwanza. Binafsi, kwa pamoja nayajuisha na kuyakubali makundi yote yale yanayodai kumfahamu na kumwamini Yesu Kristo. Wote hatukubaliani kuhusu hili au lile lakini kimsingi ukristo ni kumhusu Yesu. hata hivyo, kuna makundi yanayodai kuwa wapo wakristo ambao wanaonekana "kufanana." Ni kwa vipi naweza kuelezea tofauti ?

Sawa, kuna njia mbili:

- A. Kitabu kinachoweza kusaidia kujua kile makundi ya madhehebu ya kisasa yanaamini (kutoka katika maandiko yao) *The Kingdom of the Cults* na Walter Martin.
- B. Hotuba ya makanisa ya awali, hasa wale kupitia Mtume Petro na Paulo katika kitabu cha Matendo, wanatupatia maelezo ya msingi kwa vipi waandishi wa karne ya kwanza waliovuwiwa waliueleza Ukristo kwenye makundi. "matamko" haya ya awali au "mafundisho" (ambacho kitabu cha matendo ni mhusari wake) yanaendana na neno la Kiyunani *Kerygma*. Ufuatao ni ukweli halisi wa injili kuhusu Yesu katika Matendo ya Mitume:
  1. Kutimiliza nabii nyingi za Agano la Kale- – Mdo 2:17-21,30-31,34; 3:18-19,24; 10:43; 13:17-23,27; 33:33-37,40-41; 26: 6-7,22-23
  2. Alitumwa na YHWH kama alivyoahidi- Mdo. 2:23; 3:26
  3. Miujiza iliyotendeka kuthibitisha ujumbe wake na kudhihilisha huruma ya Mungu- – Mdo 2:22; 3:16; 10:38
  4. Waliofunguliwa, wasiomilikiwa- Mdo. 3:13-14; 4:11
  5. Kusurubishwa - Mdo 2:23; 3:14-15; 4:10; 10:39; 13:28; 26:23
  6. Alifufuliwa kuja uzimani- Mdo. 2:24,31-32; 3:15,26; 4:10; 10:40; 13:30; 17:31; 26;23
  7. Ameinuliwa mkono wa kulia wa Mungu Baba- Mdo 2:33-36; 3:13,21
  8. Atakuja tena mara ya pili - Mdo 3:20-21
  9. Alichaguliwa kuwa hakimu- Mdo 10:42; 17:31
  10. Akamtuma Roho Mtakatifu- Mdo 2:17-18,33,38-39; 10:44-47
  11. Mwokozi wa kila aaminiye- Mdo 13:38-39
  12. Hakuna mwingine aliye mwokozi- Mdo 4:12; 10:34-36

Hapa kuna baadhi ya njia za kukubali kwenye hizi nguzo za ukweli:

1. Tubu – Mdo. 2:38; 3:19; 17:30; 26:20
2. Amini – Mdo. 2:21; 10:43; 13:38-39
3. Ubatizwe – Mdo.2:38; 10:47-48
4. Mpokee Roho – Mdo 2:38; 10:47
5. Yote yatakujilia- Mdo.2:39; 3:25; 26:23

Mpango huu ulitumika kama tamko la kanisa la mwanzo, ingawa waandishi tofauti wa Agano Jipya wanaweza kuacha sehemu au wakasisitiza wengine hasa katika maandiko yao. Injili yote ya Marko kwa karibu inafuata dhana ya mafundisho. Marko kiutamaduni anaonekana kama kuitengeneza hotuba ya Petro, iliyohubiriwa huko Roma, katika injili iliyoko kwenye maandishi. Injili zote za Mathayo na Luka zinafuata muundo wa Marko.

- E. Frank Stagg katika Fasiri yake, *The Book of Acts, the Early Struggle for an Unhindered Gospel*, kinaelezea kusudi la msingi la mtembeo wa ujumbe wa Yesu (injili) kutoka katika utafuati wa dhambi kabisa wa dini ya kiyahudi kuelekea katika ujumbe wa kiulimwengu wa wanadamu wote. Fasiri ya Stagg inalenga katika kusudi la Luka katika kuandika Matendo ya Mitume. Muhtasari mzuri na uchambuzi wa nadharia mbalimbali unapatikana katika ukurasa wa 1-18. Stagg anachagua kuweka shabaha katika neno "bila kufichwa" katika Mdo. 28:31, ambayo ni njia isiyo ya kawaida kumaliza kitabu, kama ufunguo kuelewa mkazo wa Luka kwenye kueneza Ukristo na kushinda vikwazo vyote.
- F. Japo Roho Mtakatifu anatajwa zaidi ya mara 50 katika kitabu cha Matendo ya Mitume, bado sio "Matendo ya Roho Mtakatifu." Kuna sura 11 ambapo Roho hatajwi kabisa. Anatajwa mara nyingi zaidi katika nusu ya kwanza ya Matendo ya mitume ambapo Luka ananukuu kutoka vyanzo vingine (yaweze kana kwa uasili wake ni kutoka katika kuandikwa Kiaramu). Matendo ya Mitume sio kwa Roho ambavyo Injili ziko kwa ajili ya Yesu! Hii haimaanishi kushusha hadhi ya nafasi ya Roho, lakini kutulinda kutoka katika kujenga thiolojia ya Roho kimsingi au tukiacha Matendo ya Mitume.
- G. Matendo ya Mitume imekusudiwa kufundisha fundisho (kama vile Fee na Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukurasa 94-112). Mfano wa hili ingekuwa kujaribu kujenga msingi wa thiolojia ya kugeuka kutoka katika Matendo ya mitume ambayo itashindwa tu. Msingi na vipengele vya kugeuka kunatofautiana katika Matendo ya Mitume; Hivyo utaratibu ni usanifishaji? Hatutakiwi kuangalia kwenye nyaraka za Yohana kwa msaada. Hata hivyo, inashangaza kwamba baadhi ya wanataaluma (Hans Conzelmann) wamemuangalia kwa kusudi wa kumfanya wa kawaida tena kwa yake matukio ya siku za mwisho ya karne ya kwanza yadumuyo yakiwa na makabiliano ya huduma ya kigonjwa kwa *Parousia* iliyochelewa. Ufalme wa Mungu upo hapa sasa, ukibadilisha maisha. Kanisa linafanya kazi sasa kufanyika kuwa shabaha na sio tumaini la siku za mwisho wa nchi.
- H. Uwezekano mwingine wa kusudi la Matendo ya Mitume ni sawa na Warumi 9-11: kwanini Wayahudi walikataa Masihi na kanisa likawa la watu wa Mataifa zaidi? Maeneo mengi katika Matendo ya Mitume asili ya kiulimwengu mzima ya injili ni wazi kuwa imeshapigiwa tarumbeta. Yesu anawatuma ulimwenguni kote (kama vile Mdo. 1:8). Wayahudi wanamkataa yeye lakini Mataifa wanampokea. Ujumbe huu unaifikia Rumi.
- Inawezekana kwamba kusudi la Luka ni kuonesha kwamba Ukristo wa Kiyahudi (Petro) na Ukristo wa kimataifa (Paulo) vinaweza kuishi pamoja na kukua pamoja! Haviko katika mashindano, bali wanajiunga katika uinjilishaji wa dunia.
- I. Kulingana na kusudi, nakubaliana pamoja na F. F. Bruce (*New International Commentary*, ukurasa wa 18) kwamba tangu Luka na Matendo ya Mitume ambao kwa asili vilikuwa toleo moja, dibaji ya Luka (1:1-4) inafanya kazi pia kama dibaji ya Matendo ya Mitume. Luka hata hivyo sio shahidi wa jicho la moja kwa moja kwa matukio yote, kwa kuyatafiti kwa uangalifu na kuyawekea kumbukumbu kwa usahihi, ikitumika historia yake, fasihi na muundo wa kazi.
- Luka hivyo katika pote Injili na masimulizi, anataka kutuonesha ukweli wa kihistoria na uaminifu wa kithiolojia (kama vile Luka 1:4) wa Yesu na Kanisa. Inawezekana kwamba shabaha ni maudhui ya

kutimilizwa (bila kufichwa, kama vile Mdo. 28:31, ambapo ni neno la mwisho la kitabu). Maudhui yanapelekwa mbele na maneno tofauti kadhaa na tungo (kama vile Walter L. Liefeld, *Interpreting the Book of Acts*, ukurasa 23-24). Injili si jambo la mbadala, mpango B, au jambo jipya. Ni mpango ulioamriwa kabla (kama vile Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29).

## AINA YA UWASILISHAJI WA FASIHI

- A. Matendo ya Mitume kwa Agano Jipya ni kile ambacho Yoshua katika 2 Wafalme kilivyo kwa Agano la Kale: Masimulizi ya Kihistoria (angalia kiambatanisho cha tatu). Masimulizi ya kihistoria ya Kibiblia ni ya kweli, lakini shabaha haipo katika mfululizo au kuwekwa kwa kumbukumbu vizuri kwa matukio. Linachagua matukio kadhaa ambayo yanaelezea Mungu ni nani, sisi ni nani, kwa namna gani tunahesabiwa haki na Mungu, na Mungu anatumaitaji tuishi kwa namna gani.
- B. Tatizo katika kutafsiri Masimulizi ya Biblia ni kwamba waandishi huwa hawatoi maandiko (1) nini makusudi yao, (2) kweli kuu ni nini au (3) kwa nama gani tunaweza kuiga vitu vilivyoandikwa. Wasomaji lazima wafikirie vitu vifuatavyo:
  - 1. tukio gani limewekwa kumbukumbu?
  - 2. Kwa namna gani linafanana na mambo ya kibiblia yaliyopita?
  - 3. Kweli kuu ya kithiolojia ni nini?
  - 4. Je kuna umuhimu wa muktadha wa kifasihi? (Ni matukio gani yaanza na yapi yanafuata? Je somo hili liliwahi kusungumzwa mahali popote?)
  - 5. Muktadha wa Kifasihi ni mkubwa kiasi gani? (Wakati mwingine kiasi kikubwa ya masimulizi kinatengeneza maudhui au kusudi la kithiolojia moja.)
- C. Masimulizi ya kihistoria hayatakiwi kuwa na chanzo kimoja cha mafundisho. Mara kwa mara vitu vinavyowekeka kumbukumbu kwamba vinapelekea kwenye kusudi la mwandishi. Masimulizi ya Kihistoria yanaweza kuelezea kweli zilizowekeka kumbukumbu sehemu zingine katika Biblia. Kwasababu jambo fulani limetokea haimaanishi kuwa ni mapenzi ya Mungukwa waaminio katika vizazi vyote (mfano kujiua, ndoa za mitaala, vita vya kidini, kushika nyoka, n.k.).
- D. Mjadala bora na wa kimuhtasari wa namna gani ya kufasiri masimulizi ya kihistoria ni kunatolewa na Gordon Fee na Douglas Stuart katika kitabu kiitwacho *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukurasa 78-93 na 94-112.

## BIBLIOGRAFIA YA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

Vitabu vipya vya kuiweka Matendo ya Mitume katika mazingira yake ya karne ya kwanza vimezalishwa na wanazuoni wenye utamaduni na elimu ya Wayunani na Warumi (classicists). Mbinu ya kulizungumzia jambo hili imesaidia kiukweli uelewa wa Agano Jipya. Mfululizo wa vitabu vifuatavyo vimehaririwa na Bruce M. Minter.

- A. *The Book of Acts in Its Ancient Literary Setting*
- B. *The Book of Acts in Its Graeco-Roman Setting*
- C. *The Book of Acts and Paul in Roman Custody*
- D. *The Book of the Acts in Its Palestinian Setting*
- E. *The Book of Acts in Its Diaspora Setting*
- F. *The Book of Acts in Its Theological Setting*

Pia vingine vyenye msaada ni kama

- 1. A. N. Sherwin-White, *Roman Society and Roman Law in the New Testament*
- 2. Paul Barnett, *Jesus and the Rise of Early Christianity*
- 3. James S. Jeffers, *The Greco-Roman World*

## **MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" \("A Guide to Good Bible Reading"\)](#))**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Taja dhamira kuu ya kitabu kizima katika maneno yako mwenyewe.

1. Maudhui ya kitabu kizima
2. Aina ya Fasihi (mbinu ya uwasilishaji)

## **MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" \("A Guide to Good Bible Reading"\)](#))**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri

Soma kitabu kizima cha Biblia kwa mara ya Pili kwa mkao mmoja. Ainisha masomo makuu na yaelezee masomo katika sentensi moja.

1. Somo la kipengele cha kwanza cha fasihi
2. Somo la kipengele cha pili cha fasihi
3. Somo la kipengele cha tatu cha fasihi
4. Somo la kipengele cha nne cha fasihi
5. N.k



# MATENDO YA MITUME 1

<b>MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA*</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Ahadi ya Roho	Dibaji	Utangulizi;Kristo	Utangulizi	Dibaji
Mtakatifu		mfufuka		
1:1-5	1:1-3	1:1-5	1:1-5	1:1-5
	Roho Mtakatifu			
	Aliyehaidiwa			
Kupaa kwa Yesu	1:4-8	Kupaa	Yesu anapandishwa	Kupaa
			Juu mbinguni	
1:6-11		1:6-11	1:6	1:6-8
	Yesu anapaa mbinguni		1:7-9	
	1:9-11			1:9-11
			1:10-11	
Uchaguzi mrithi wa	Mkutano wa maombi	kukutana kwa	Mrithi wa Yuda	Kundi la Mitume
Yuda	wa chumba cha juu	kumi na mbili		
1:12-14	1:12-14	1:12-14	1:12-14	1:12-14
	Mathiya anachaguliwa			Mbadala wa
nafasi				Ya Yuda
1:15-26	1:15-26	1:15-26	1:15-17	1:15-20
			1:18-19	
			1:20	
			1:21-22	1:21-22
			1:23-26	1:23-26

\* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari. Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.

Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: [Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani \(Brief Definitions of Greek Grammatical Structure\)](#), [Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi \(Textual Criticism\)](#), [Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko \(Glossary\)](#).

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" \("A Guide to Good Bible Reading"\)](#))

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 1:1-5**

<sup>1</sup> Kitabu kile cha kwanza nalikiandika, Theofilo, katika habari ya mambo yote aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha, <sup>2</sup> hata siku ile alipochukuliwa juu, alipokuwa amekwisha kuwaagiza kwa Roho Mtakatifu wale mitume aliowachagua; <sup>3</sup> wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyouhusu ufalme wa Mungu. <sup>4</sup> Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu; <sup>5</sup> ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache.

**1:1 "Kitabu kile cha kwanza nalikiandika"** Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu, kidhahiri, "naliandika." Luka ni wazi kuwa ndiye mwandishi wa vitabu vyote Injili ya Luka na Matendo ya Mitume (linganisha Luka 1:1-4 na Mdo. 1:1-2). Neno "toleo" lilitumika katika masimulizi ya kihistoria ya Kiyunani. Kwa namna yake (yaani katika kipindi cha elimu ya Kiyunani) ilimaanisha moja kati ya kazi tatu angalau. Hakika ni kweli yawezekana kwamba kumalizika kusiko kwa kawaida kwa Matendo ya Mitume inaweza kuelezewa na mpango wa Luka wa kuandika toleo la tatu. Baadhi wanadhania kwamba kile tukiitacho nyaraka za kichungaji (1Timotheo, 2 Timotheo, na Tito) inawezekana kuwa kimeandikwa na Luka.

▣ **"Theofilo"** Jina hili linatengenezwa kutoka kwa (1) Mungu (*Theos*) na (2) upendano wa kiundugu (*philos*). Inaweza ikafasiriwa "mpenzi wa Mungu," "rafiki wa Mungu," au "apendwaye na Mungu." Jina "bora zaidi sana" Luka 1:3 inawezakuwa cheo/jina la kiheshima kwa wafanyakazi wa kiserikali ya Kirumi (kama vile Mdo. 23:26; 24:3; 26:25), yawezekana alitumia amri ya kirumi ya panda farasi wa kijamii. Anawezekana akawa kuwa mfaidikaji wa fasihi kwa uandishi, kuiga na kusambaza vitabu viwili vya Luka. Desturi za majina ya kanisa yanamuita yeye T. Flavius Clemens, mpwa wa Domitian (24-96 B.K).

▣ **"yote aliyoanza Yesu kufanya"** Hii inamaanisha Injili ya Luka. Inashangaza kwamba Luka "yote" kwamba Yesu alifanya, kwasababu ya Injili ya Luka (kama Injili zote nne) ni chaguzi sana katika kile kinachowekewa kumbukumbu kuhusu maisha ya Yesu na mafundisho.

**1:2 "hata siku ile alipochukuliwa juu"** Hii inatajwa katika Luka 24:51. Angalia Mada Maalumu inayofuata

### **MADA MAALUMU: KUPAA**

Yesu alipaa kwenda mbinguni (kama vile Flp. 2:6-7; 2 Kor. 8:9). Na sasa amerejeshwa katika utukufu Wake wa awali (kama vile Yohana 1:1-3; 17:5; Efe. 4:10; 1 Tim. 3:16; I Yohana 1:2). Yeye amekaa mkono wa kuume wa Mungu (kama vile Zab. 110:1; Luka 22:69; Mdo. 2:33; Rum. 8:34; Efe. 1:20; Kol. 3:1; Ebr. 1:3; 8:1; 10:12; 12:2; 1 Pet. 3:22). Huu ni uthibitisho wa ukubalifu wa Baba kwa uhai na maisha yake!

Kuna idadi tofauti tofauti ya maneno ya Kiyunani yaliyotumika kuelezea juu ya kupaa kwa Yesu mbinguni:

1. Mdo. 1:2,11,22; *analambanō*, kunyakuliwa (kama vile 1 Tim. 3:16)
2. Mdo. 1:9, *epairō*, kutazama juu, kuinua, kunyakua
3. Luka 9:51, *analēpsis* (kwa mtindo wa #1)
4. Luka 24:51, *diistēmi*, kusambaa

Katika Injili ya Yohana kuna vidokezo mbali mbali vya akurudi mbinguni kwa Yesu (kama vile Yohana 7:33; 8:14,21; 12:33-34; 13:3,33,36; 14:4,5,12,28; 16:5,10,17,28; 26:7)

5. Yohana 3:13; 20:17, *ana BeBēken*, amekwenda zake

6. Yohana 6:62, *anabainō*, kupaa

Tukio hili halikuchukuliwa kumbukumbu katika Injili ya Mathayo au mwishoni mwa Ijili ya Marko katika 16:8, lakini moja wa maongezeko ya waandishi wa baadaye inaeleza tukio katika Marko 16: 19 (yaani, *analambanō* ). Katika Matendo Kuna vidokezo kadha wa kadha kumhusu Yesu kurudi huko mbinguni.

1. Petro – Mdo. 2:33; 3:21
2. Stefano –Mdo. 7:55-56
3. Paulo –Mdo. 9:3,5, 22:6-8; 26:13-15

▣ **"alikuwa na Roho Mtakatifu"** Angalia Mada Maalum.

### **MADA MAALUMU: NAFSI YA ROHO**

Kwenye Agano la Kale “Roho wa Mungu” (yaani *ruach*) ilikuwa nguvu iliyotimiza kusudi la YHWH, lakini kuna kidokezo kwamba alikuwa mtu binafsi (yaani Mungu mmoja, tazama Mada Maalumu: U-Mungu mmoja). Hata hivyo kwenye Agano Jipya ukamilifu wa nafsi ya ubinadamu na utu wa Roho umefunuliwa:

1. Anaweza kufanyiwa kufuru (kama vile Mt. 12:31; Marko 3:29)
2. Hufundisha (kama vile Luka 12:12; Yohana 14:26)
3. Hushuhudia (kama vile Yohana 15:26)
4. Ana hukumu, anaongoza (kama vile Yohana 16:7-15)
5. Anaitwa “ambaye” (yaani, *hos*, kama vile Efe 1:14)
6. Anaweza kuhuzunishwa (kama vile Efe. 4:30)
7. Anaweza kuzimishwa (kama vile 1 The. 5:19)
8. Anaweza kupingwa (kama vile Mdo. 7:51)
9. Anawatetea waaminio (kama vile Yohana 14:26; 15:26; 16:7)
10. Humtukuza Mwana (kama vile Yohana 16:14)

Maandiko ya utatu (hapa yapo matatu mioongoni mwa mengi, tazama Mada Maalumu: Utatu) pia anazungumza juu ya watu watatu.

1. Mt. 28:19

2. 2 Kor. 13:14

3. 1 Pet. 1:2

Ingawa neno la Kiyunani "roho" (*pneuma*) ni sio na jinsi wakati linapohusika Roho, Agano Jipya kila mara hutumia KIVUMISHI KIONYESHI CHA JINSIA YA KIKE (kama vile Yohana 16:8,13-14).

Roho anahusishwa na shughuli za binadamu.

1. Mdo. 15:28

2. Rum. 8:26

3. 1 Kor. 12:11

4. Efe. 4:30

Mwanzoni kabisa mwa matendo, jukumu la roho lina sisitizwa (kama katika injili ya Yohana). Pentekoste haikuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali, sura mpya. Yesu kila wakati alikuwa na Roho. Ubatizo wake haukuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali mwanzo wa sura mpya. Roho ndio njia yenye nguvu ya makusudi ya Baba kwa sura yake (tazama Mada Maalumu: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH)!

▣ **"Kutoa amri"** Hii inamaanisha taarifa zilizowekwa katika kumbukumbu katika Injili ya Luka 24:44-49, katika Mt. 28:18-20, na katika Mdo. 1:8.

▣ **"amri"** Hii ni kauli ya kati ya wakati uliopita usiotimilifu (yenye ushahidi) endelevu. Wanataaluma baadhi wanaona hii kama inarejerea 1:8 (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:45-47 au Luka 24:49). Kanisa lina kazi kubwa mbili kama uma:

1. Uinjilishaji na makuzi ya kufanana na Kristo; kila mwamini lazima asubirie nguvu ya Mungu na kuwezesha kufikia haya
2. Wengine wanaona kama ikimaanisha "subiri Yerusalemu kwa ajili ya kuja kwa roho na kuwezesha" (kama vile Mdo 1:4; Luka 24:49)

▣ **"Mitume"** Angalia jedwali la majina ya mitume katika Mdo. 1:13.

▣ **"aliowachagua"** "waliochaguliwa" (*eklegō*, kauli ya kati elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu) inatumika katika namna mbili. Sikuzote Agano la Kale inamaanisha huduma, sio wokovu, lakini katika Agano Jipya inamaanisha wokovu wa kiroho. Hapa inaonekana kumaanisha mawazo yote mawili (kama vile Luka 6:13).

**1:3 "Yeye alijitoa mwenyewe kuwa hai"** Hii yawezekana inamaanisha kutokea kwa Yesu mara tatu katika chumba cha juu kwa kundi lote zima la mwanafunzi katika siku tatu mfululizo za Jumapili, lakini inawezekana kumaanisha pia kuonekana kwingine (kama vile 1 Kor. 15:5-8). Ufufuo wa Yesu ni muhimu kuelekea ukweli wa Injili (kama vile Mdo. 2:24,32; 3:15,26; 4:10; 5:35; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; na hasa 1 Kor. 15:12-19,20). Ifuatayo ni jedwali ya kuonekana kwa Yesu baada ya Ufufuo kutoka kwa Paul Barnett, katika kitabu chake cha *Jesus and the Rise of Early Christianity*, ukurasa wa 185.

Yohana	Mathayo	Luka	1 Wakorintho
<b>Kutokea Yerusalemu</b>			
Maria (Yn. 20:15)	Wanawake (Mt. 28:9)	Simoni (Luka 24:34)	Kefa (1 Kor. 15:5)
Wanafunzi kumi (Yn		Wawili barabarani kwa	Kumi na mbili (1 Kor.

20:19)		Emmau (Luka 24:15)	15:5)
Wanafunzi kumi na moja (Yn 20:26)		Wanafunzi (Luka 24:36)	
<b>Kutokea Galilaya</b>			
Wanafunzi saba (Yohana 21:1)	Wanafunzi (Mathayo 28:16-20)		Waamini zaidi ya 500 (1 Kor. 15:6; yawezekana inaunganishwa na Mt. 28:16-20) Yakobo (1 Kor. 15:7)
<b>Kutokea Yerusalemu</b>			
		Kupaa (Luka 24:50-51)	Mitume wote (1 Kor. 15:7)

**NASB, NRSV**

**NIV** "kwa udhibisho mwingi wa ushawishi"

**NKJV** "kwa udhibitisho mwingi wa kweli"

**TEV** "mara nyingi katika njia nyingi ambazo zilipita wasiwasi"

**NJB** "kwa udhihirisho mwingi"

Neno *tekmērion* linatumika hapa tu katika Agano Jipya. Kuna mjadala mzuri wa maneno yanayotumika katika Fasihi ya Kiyunani ya kina Moulton na Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament*, ukurasa wa 628, ambapo inamaanisha "ushahidi unaoelezea." Neno hili pia linatumika katika Hekima za Sulemani 5:11; 19:3 na III Maccabees 3:24.

▣ **"baada ya Mateso yake"** Ilikuwa ni kwa ugumu mkubwa kwamba waamini wa Kiyahudi kuamini hiki kipengele cha injili (kama vile 1 Kor. 1:23). Mateso ya Masihi yanatajwa katika Agano la Kale (kama vile Mwanzo 3:15; Zaburi 22; Isaya 53; Zekaria 10:12; na tazama katika Luka 24:45-47). Hii ilikuwa ni ukiri mkubwa wa kithiolojia wa mahubiri ya Kitume (*kerygma*; angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:14).

Luka mara nyingi anatomia kauli tendaji ya wakati uliopita usiotimilifu usio na kikomo wa *paschō* (kuteseka) kumaanisha usulubishwaji wa Yesu (kama vile Luka 9:22; 17:25; 22:15; 24:26,46; Mdo. 1:3; 3:18; 9:16; 17:3). Luka anaweza kuwa alipata hii kutoka kwa injili ya Marko (kama vile Mdo. 8:31).

▣ **"akiwatokea"** Tuna namna kumi au kumi na moja za kutokea kwa Yesu baada ya Ufufuo kunakowekwa katika kumbukumbu katika Agano Jipya. Hata hivyo hivi ni viwaakilishi tu na sio kama ndio alitokea mara hizo pekee na sio zaidi ya hapo. Kiuhalisia Yesu alikuja na aliondoka wakati wa kipingi, lakini hakuwahi kukaa na kundi lolote.

**MADA MAALUMU: KUONEKANA KWA YESU BAADA YA UFUFUO**

Yesu alijionesha kwa watu kadhaa kuthibitisha kufufuka kwake.

1. Wanawake kaburini, Mt. 28:9
2. Wanafunzi kumi na moja kwenye mkutano ulioandaliwa Galilaya, Mt. 28:16
3. Simoni, Luka 24:34
4. Wale wawili njiani kuelekea Emau, Luka 24:15
5. Wanafunzi gorofani, Luka 24:36
6. Maria Magdalena, Yohana 20:15
7. Wanafunzi kumi ghorofani, Yohana 20:20
8. Wanafunzi kumi na moja ghorofani, Yohana 20:26
9. Wanafunzi saba kwenye bahari ya Galilaya, Yohana 21:1
10. Kefa (Petro), 1 Kor. 15:5
11. (Mitume) kumi na wawili, 1 Kor. 15:5
12. Ndugu 500, 1 Kor. 15:6 pamoja na mathayo Mt. 28:16-17
13. Yakobo (mtu wa familia yake), 1 Kor. 15:7
14. Mitume wote, 1 Kor. 15:7
15. Paulo, 1 Kor. 15:8 (Mdo. 9)

Bila shaka baadhi ya haya mengine yanarejelea kuonekana kulekule. Yesu alitaka wao wajue kwa hakika kwamba alikuwa hai!

▣ **"siku arobaini"** Hii ni nahau ya Agano la Kale kwa ajili ya muda usio na kikomo maalumu, ndefu sana kuliko zunguko wa mwezi. Hapa inahusianishwa na muda kati ya sikukukuu za mwisho za kiyahudi za Oasaka na Pentekoste (ambazo ni siku 50). Luka ni chanzo cha taarifa. Toka tarehe ya kupaa kwake hata sio kitu kikubwa (hata haikugunduliwa na waandishi mpaka karne ya nne B.K), lazima kuna sababu nyingine kwa ajili ya hesabu. Inaweza ikahusianishwa na Mlima Sinai, Israeli katika jangwa, uzoefu wa jaribu la Yesu, au tunakuwa hatujui, lakini ni wazi kwamba tarehe yenyewe sio jambo kubwa.

### **MADA MAALUM: UWAKILISHI WA NAMBA KATIKA MAANDIKO**

- A. Namba fulani zilitenda kazi maeneo yote kama tarakimu na ishara.
  1. Moja – Mungu (yaani, Kumb. 6:4; Efe. 4:4-6)
  2. Nne – dunia nzima (yaani, pembe nne, nchinne za dunia, yaani, Isa. 11:12; Yer. 49:36; Dan. 7:2; 11:4; Zek. 2:6; Mt. 24:31; Marko 13:27; Ufu. 7:1)
  3. Sita – kutokamilika kwa mwanadamu (moja chini ya 7, m.f, Ufu. 13:18)
  4. Saba – itimilifu wa Kiungu (siku saba za uumbaji). Tambua matumizi ya kiishara katika Ufunuo:
    - a. vinara vya taa saba, Ufu. 1:12,20; 2:1
    - b. nyota saba, Ufu. 1:16,20; 2:1
    - c. makanisa saba, Ufu. 1:20
    - d. Roho saba za Mungu, Ufu. 3:1; 4:5; 5:6
    - e. taa saba, Ufu. 4:5
    - f. Mihuri saba, Ufu. 5:1,5
    - g. pembe saba na macho saba, Ufu. 5:6
    - h. malaika saba, Ufu. 8:2,6; 15:1,6,7,8; 16:1; 17:1
    - i. baragumu saba, Ufu. 8:2,6
    - j. ngurumo saba, Ufu. 10:3,4
    - k. elfu saba, Ufu. 11:13
    - l. vichwa saba, Ufu. 13:1; 17:3,7,9
    - m. mapigo saba, Ufu. 15:1,6,8; 21:9
    - n. vitasa saba, Ufu. 15:7; 21:9
    - o. wafalme saba, Ufu. 17:10
  5. Kumi– ukamilifu
    - a. matumizi katika Injili

- 1) Mt. 20:24; 25:1,28
- 2) Marko 10:41
- 3) Luka 14:31; 15:8; 17:12,17; 19:13,16,17,24,25
- b. matumizi katika Ufunuo
  - 1) Ufu. 2:10, siku kumi dhiki
  - 2) Ufu. 12:3; 17:3,7,12,16, pembe kumi
  - 3) Ufu. 13:1, vilemba kumi
- c. Vigawe vya kumi katika Ufunuo
  - 1)  $144,000 = 12 \times 12 \times 1000$ , kama vile Ufu. 7:4; 14:1,3
  - 2)  $1,000 = 10 \times 10 \times 10$ , kama vile Ufu. 20:2,3,6
6. Kumi na Mbili – ushirika wa mwanadamu
  - a. Wana kumi na wawili wa Yakobo (yaani, makabila kumi na mbili ya Israeli, Mwa. 35:22; 49:28)
  - b. nguzo kumi na mbili, Kut. 24:4
  - c. mawe kumi mawili katika juu ya kifua cha Kuhani Mkuu, Kut. 28:21; 39:14
  - d. mikate kumi na miwili, ju ya meza Mahali Patakatifu (ishara ya utoaji wa Mungu wa kwa makabila kumi na mawili), Law. 24:5; Kut. 25:30
  - e. Watu kumi na wawili, Kumb. 1:23;
  - f. mawe kumi na mawili, Jos. 4:2,3,4,8,9,20
  - g. miktume kumi na wawili, Mt. 10:1

matumizi katika Ufunuo

- 1) makakabila kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri, Ufu. 7:5-8
- 2) nyota kumi na mbili, Ufu. 12:1
- 3) milango kumi na miwili, malaika kumi na wawili, makabila kumi na mawili, Ufu. 21:12
- 4) misingi ya mawe kumi na mawili, majina ya Mitume kumi na mawili, Ufu. 21:14
- 5) Yerusalemu mpya ilikuwa vipimo vya mraba elfu kumi na mbili, Ufu. 21:16
- 6) milango kumi na miwili ilitotengenezwa kwa lulu kumi na mbili Ufu. 21:21
- 7) mti wa uzima uzao matunda, aina kumi na mbili, Ufu. 22:2
7. Arobaini –namba za nyakati
  - a. wakati mwingine ni halisi (kuhamishwa na kutangatanga nyikani, m.f. Kut. 16:35); Kumb. 2:7; 8:2
  - b. inaweza kuwa halisi au ya kiishara
    - 1) mafuriko, Mwa. 7:4,17; 8:6
    - 2) Musa juu ya Ml. Sinai, Kut. 24:18; 34:28; Kumb. 9:9,11,18,25
    - 3) mgawanyo wa maisha ya Musa:
      - a) miaka arobaini ndani ya Misri
      - b) miaka arobaini jangwani
      - c) miaka arobaini ya kuiongoza Israeli
    - 4) Yesu alifunga siku arobaini, Mt. 4:2; Marko 1:13; Luka 4:2
  - c. Tambua (kwa maana ya Upatanisho) tarakimu za wakati hii tarakimu inajitokeza katika wakati wa uteuzi ndani ya Bibia!
8. Sabini – namba ya jumla ya watu
  - a. Israeli, Kut. 1:5
  - b. wazee sabini, Kut. 24:1,9
  - c. matukio ya siku za mwisho, Dan. 9:2,24
  - d. kundi la huduma, Luka 10:1,17
  - e. msamaha (70x7), Mt. 18:22

A. Marejeo mazuri

1. John J. Davis, *Biblical Numerology*
2. D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks*

▣ "Kuzungumza vitu vihusu vyuo ufalme wa Mungu" Wajuzi walidai kwamba Yesu alifunua taarifa za siri za makundi yao wakati wa nyakati kati ya Pasaka na Pentekoste. Hii hata hivyo hakika ni uongoe. Hata hivyo suala la wawili katika barabara ya Emmau ni mfano mzuri wa mafundisho ya Yesu baada ya Kufufuka kwake. Nafikiri Yesu, Mwenyewe, alionesha viongozi wa kanisa kutoka Agano la Kale, utabiri na maandiko yahasuyo maisha yake, kifo, ufufuo na Kuja kwa Mara ya Pili. Angalia [MADA MAALUMU: UFALME WA MUNGU](#) ikifuatia.

## MADA MAALUMU: UFALME WA MUNGU

Katika Agano la Kale Mungu alifikiriwa kama mfalme wa Israel (kama vile 1 Sam. 8:7; Zab. 10:16; 24:7-9; 29:10; 44:4; 89:18; 95:3; Isa. 43:15; 44:6) na Masiha akawepo kama mfalme aliyedhaniwa/kutegemewa (kama vile Zab. 2:6; Isa. 9:6-7; 11:1-5). Na kuzaliwa kwa Yesu pale Betlehemu (mwaka wa 6-4 K.K) ufalme wa Mungu ukavunjiliwa ndani ya historia ya mwanadamu kwa nguvu mpya na ukombozi ("Agano Jipya," kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:27-36).

1. Yohana Mbatizaji akatangaza kukaribia kwa ufalme (kama vile Mt. 3:2; Mk 1:15).
2. Yesu wazi wazi akafundisha kwamba ufalme ulikuwa tayari ndani yake mwenyewe na mafundisho yake (kama vile Mt. 4:17,23; 10:7; 12:28; Luka 10:9,11; 11:20; 17:21; 21:31-32). Na bado ufalme unakuja (kama vile Mt. 16:28; 24:14; 26:29; Marko 9:1; Luka 21:31; 22:16,18).

Katika usambamba wa mihitasari kwenye Marko na Luka tunakipata kifungu, "ufalme wa Mungu." Hii ilikuwa mada ya kawaida katika mafundisho ya Yesu yakijumisha utawala wa Mungu uliopo kiatika miyo ya watu, ambao siku moja utakamilishwa katika ulimwengu wote. Hii unaakisishwa kwenye maombi ya Yesu katika Mt.6:10. Mathayo, akiwaandikia Wayahudi, alipendelea kifungu kile ambacho hakitumii jina la Mungu (yaani Ufalme wa Mbinguni), wakati Marko na Luka, akiwaandikia watu wa mataifa, anatumia usanifu wa kawaida, akiweka jina la Uungu.

Hiki ni kile kifungu cha mfano katika mihitasari ya injili. Hotuba za kwanza na za mwisho za Yesu, na zaidi mafumbo yake, yanashughulika na mada. Zinarejerea utawala wa Mungu katika miyo ya wanadamu sasa! Inashangaza kuona kwamba Yohana anatumia kifungu hiki mara mbili tu (na kamwe sio kwenye mafumbo ya Yesu). katika injili ya Yohana "uzima wa milele" ni sitiari muhimu.

Mvutano na kifungu hiki unasababishwa na ujio mara mbili wa Kristo, Agano la Kale linatazamisha kwenye ujio mmoja wa Masiha wa Mungu kama afisa wa kijeshi, ujio wa kitukufu-lakini Agano Jipya linaonyesha kuwa alikuja kwanza kama mtumishi mwenye mateso katika Isaya 53 na mfalme mnyenyekevu katika Zak. 9:9. Enzi mbili za Kiyahudi (angalia mada maalumu: Enzi hii na Enzi inayokuja), enzi ya uovu na enzi mpya ya haki, zimeingiliana. Kwa sasa Yesu anatawala ndani ya miyo ya waumini, lakini siku moja atatawala juu ya uumbaji wote. Atakuja kama Agano la Kale lilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19)! Waamini wanaishi ndani ya ulimwengu wa Mungu "uliotayari" dhidi ya "ule ambao bado" (kama vile Gordon D. Fee na Douglas Stuart's *How to Read The Bible For All Its Worth*, kurasa za. 131-134).

1:4

NASB	"mkiwakusanya wao pamoja"
NKJV	"kukusanyika nao kwa pamoja"
NRSV	"wakati mkikaa nao"
TEV	"wakati walipokuja pamoja"
TEV <sup>b</sup>	"wakati alikuwa akikaa pamoja nao"
NIV	"wakati akila pamoja nao"
NJB	"wakati wakiwa mezani pamja nao"

Mistari ya 4-5 inatumia moja ya kutokea kwa Yesu kama mfano mmoja wa kutokea kwake kadhaa na uthibitisho. *Nenosunalizomenos* linaweza kuandikwa vingine. Neno linabadilisha maana.



1. a ndefu – kukusanyika/kukutana pamoja
2. a fupi – kula na (Ikiuhalisia "kwa kutumia chumvi")
3. au (mfuatano wa sauti irabu) – kukaa pamoja na

Haijulikana kipi kilikusudiwa, lakini Luka 24:41-43 (kama vile Yohana 21) inamuelezea Yesu akila na kundi lake la mitume, ambalo lingekuwa ushahidi kwamba angefufuka kwa mwili wake wa nyama (kama vile Mdo. 1:3).

▣ **"msiondoke Yerusalemu"** Hii inaandikwa katika Luka 24:49. Sehemu ya kwanza ya Matendo ya Mitume ni upitiaji wa mwisho wa injili ya Luka, yawezekana kifasihi kama njia ya kuunganisha vitabu viwili.

▣ **"kububiri ahadi ya Baba aliyohaidi"** Katika Mdo. 2:16-21 Petro anafanisha unabii wa siku za mwisho wa Yoeli 2:28-32. Walisubiri siku kumi mpaka Pentekoste. Luka kwa uwazi anaeleza "Ahadi ya Baba" kama Roho Mtakatifu (kama vile Luka 24:49; Mdo. 2:33). Yesu kabla alikuwa amezungumzia wao kuhusu kuja kwa Roho katika Yohana 14-16. Hata hivyo inawezekana kwamba Luka anaelewa ahadi ya Baba kwamba sio jambo moja tu (i.e., yaani Roho Mtakatifu), lakini pia kwamba Agano la Kale lihaiidi wokovu utaletwa kwa Israeli kupitia mtu aitwaye Mashi (kama vile Mdo. 2:39; 13:23,32; 26:6).

▣ **"Baba"** Agano la Kale linatambulisha sitiari inayofahamika ya uhusiano wa karibu:

1. Taifa la Israeli mara nyingi linaelezwa kama "mtoto" wa YHWH (kama vile Hosea 11:1; Malaki 3:17)
2. katika kumbukumbu la Torati uzao wa Mungu kama baba unatumika (1:31)
3. katika Kumbukumbu la Torati. 32:6 Israeli inaitwa "watoto wake" na Mungu anaitwa "Baba yako"
4. Masimulizi haya yanafanyika katika Zaburi 103:13 na kukuzwa katika Zaburi 68:5 (Baba wa Yatima)
5. ilikuwa kawaida kwa manabii (kama vile Isaya 1:2; 63:8; Israeli kama mtoto, Mungu kama Baba, 63:16; 64:8; Yereemia 3:4,19; 31:9)

Yesu aliongea Kiaramu, ambayo maana yake ni kwamba maeneo mengi "Baba" inatokea kutoka katika Kiyunani *Pater* inaaksi kwamba Kiaramu *Abba* (kama vile Mdo. 14:36). Hili neno lilalijulikana "Baba" au "papa" ina-aksi ukaribu wa kimahusiano wa Yesu na baba; Yeye anafunua haya kwa wafuasi wake pia kututia moyo kwenye ukaribu wetu sisi wenyewe kwa Baba. Neno "Baba" lilitumika mara chache chache katika Agano la Kale (na mara nyingi katika fasihi za kiuahim) kwa YHWH, lakini Yesu mara nyingi linatumika kwa kuenea kote kote. Ni ufunuo mkubwa wa mahusiano mapya ya waamini na Mungu wao kupitia Kristo Yesu (kama vile Mt. 6:9).

**1:5 "Yohana"** Injili zote nne (kama vile Mt. 3:1-12; Marko 1:2-8; Luka 3:15-17; Yohana 1:6-8,19-28) kuzungumzia huduma ya Yohana Mbatizaji. "Yohana" lilifupishwa kutoka katika muundo wa jina lakiebrania Johanan (BDB 220), ambalo lilimaanisha "YHWH ni mwenye neema" au "zawadi kwa YHWH." Jina lake lilikuwa la muhimu kwasababu ni kama jina la kibiblia, lilikuwa likimuelekea kwenye kusudi la Mungu kwa ajili ya maisha yake. Yohana alikuwa nabii wa mwisho katika manabii wa Agano la Kale. Kulikuwa hakujawahi kuja nabii katika Israeli toka Malaki, katika miaka ya 430 k.k. Uwepo wake mwenyewe ulisababisha uchangamfu mkubwa wa kiroho kati ya watu wa Israeli.

▣ **"kubatizwa kwa maji"** Ubatizo ulikuwa jambo la kawaida katika kuanzisha utamaduni kwa Wayahudi wa karne ya kwanza na ya pili, lakini katika muunganiko tu wa waongofu wa dini. Ikiwa mtu kutoka katika mazingira ya mataifa alitaka kuwa mtoto kamili wa Israeli, alitakiwa kukamilisha majukumu matatu:

1. tohara, ikiwa ni mwanaume
2. ubatizo binafsi kwa kuzamishwa, katika uwepo wa mashahidi watatu
3. sadaka katika hekalu ikiwa inawezekana

Katika kikundi cha dini cha karne ya kwanza katika Palestina, kama vile kina Essenes, ubatizo kwa dhahiri ulikuwa kawaida, uzoefu wa kurudia. Hata hivyo, to mainline ili kuweza kunyoosha Uyahudi, matukio ya kwanza ya kiibada yalianza na yanaweza kuainishwa kwa sherehe za kuoshwa:

1. ishara ya kuoshwa kiroho (kama vile Isaya 1:16)
2. ibada ya kawaida inayofanywa na makuhani (kama vile Kutoka 19:10; Walawi 15)
3. taratibu za kawaida za ibada zilizofanywa kabla ya kuingia hekaluni kuabudu

▣ **"Mtajazwa na Roho Mtakatifu"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati ujao. Kauli tendwa irabu ya sauti inaweza kurejerea kwwa Yesu sababu ya Mt. 3:11; Luka 3:16. Kihusishi ev kinaweza kumaanisha "katika," "pamoja," au "na" (yaani chombo, kama vile Mt. 3:11). Kifungu hiki cha habari kinaweza kumaanisha matukio haya mawili kufanyika mkristo, (kama vile 1 Kor. 12:13) au (2) katika muktadha huu, ahadi ya kujazwa nguvu ya kiroho kwa ajili ya ufanisi wa huduma. Yohana Mbatizaji mara kwa mara alizungumza juu ya huduma ya Yesu katika kifungu hiki, (kama vile Mt. 3:11; Marko 1:8; Luka 3:16-17; Yohana 1:33).

Hii iko katika mvutano na ubatizo wa Yohana. Masihi ataanzisha kizazi kipya cha Roho. Ubatizo wake utakuwa na (au "ndani" au "kwa") Roho. Kumekuwa na mjadala mkubwa kati ya madhehebu juu ya tukio gani linaloamaanishwa katika uzoefu wa kikristo. Wengine wanalichukulia kama uzoefu wa kupewa uwezo baada ya wokovu, namna fulani baraka. Binafsi ninafikiri inamaanisha kufanyika mkristo (kama vile 1 Kor. 12:13). Sikatai kujazwa kwa baadaye na kujengewa uwezo, lakini ninaamini kuna ubatizo mmoja wa kiroho wa kuanzia ndani ya Kristo ambamo waamini wanatambulikana kwa kifo cha Yesu na ufufuo (kama vile Rum. 6:3-4; Efe. 4:5; Kol. 2:12). Hii kazi ya kuanzia ya Roho katika kueleze kiufasaha katika Yohana 16:8-11. Katika uelewa wangu wa kazi ya Roho Mtakatifu ni:

1. kushuhudia juu ya dhambi
2. kufunua ukweli kuhusu Kristo
3. kupelekea kukubaliwa ya injili
4. kubatizwa katika Kristo
5. kushuhudia waamini juu ya dhambi inayoendelea
6. kumtengeneza mwamini katika hali ya kufanana na Kristo

▣ **"si siku nyingi tokea sasa"** Hii ni rejea kwa sherehe za kiyahudi za Pentekoste ambazo zilitokea wiki saba baada ya Pasaka. Ilitambua umiliki wa Mungu wa mavuno ya ngano (kama vile Mambo ya Walawi 23:15-31; Kutoka 34:22; Kumbukumbu la Torati 16:10).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 1:6-11**

<sup>6</sup> Basi walipokutanika, wakamwuliza, wakisema, Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme? <sup>7</sup> Akawaambia, Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. <sup>8</sup> Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi. <sup>9</sup> Akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao. <sup>10</sup> Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, <sup>11</sup> wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni.

**1:6 "walikuwa wakimuuliza Yeye"** Hii kauli isiyotimilifu inamaanisha aidha kitendo cha kurudia kwa wakati uliopita au mwanzo wa kitendo. Kwa dhahiri wanafunzi hawa walikuwa wamemuuliza hili mara nyingi

▣ **"Bwana"** Neno la Kiyunani "Bwana" (*kurios*) linaweza kutumika katika namna ya jumla au kukuzwa kithiolojia. Linaweza kumaanisha "mkuu," "mshemiwa," "mwenye mamlaka juu ya," "mmiliki," "mume" au "mtu mwenye

Mungu kamili" (kama vile Yohana 9:36, 38). Agano la Kale (Kiebrania, *adon*). Matumizi ya neno hili yalitokana na hali ya Wayahudi ya kutotaka kutamka jina la Mungu, YHWH, ambalo lilikuwa ni muundo wa kitenzi cha kiebrania "kuwa" (kama vile Kutoka 3:14).

Walikuwa na hofu ya kuvunja amri ailiyosema, "usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako" (kama vile Kutoka 20:7; Kumbukumbu la Torati 5:11). Hivyo, walifikiri kuacha kulitaja wangukuwa wamekwepa. Hivyo wakawa na mbadala wa neno la Kiebrania *adon*, ambalo lilikuwa na maana sawa na neno la Kiyunani *kurios* (Bwana). Waandishi wa Agano Jipya walilitumia jina hili kuelezea uungu wote wa Kristo. Tungo "Yesu ni Bwana" ilikuwa ni ukiri wa wazi wa imani na kanuni iliyobatizwa na kanisa la kwanza (kama vile Rum. 10:9-13; 1 Kor. 12:3; Flp. 2:11).

## MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

Huu ulikuwa ni usemi wa kawaida wa Agano Jipya kwa uwepo binafsi na nguvu itendayo kazi ya utatu wa Mungu katika kanisa. Haikuwa kanuni ya miujiza, bali rufaa kwa tabia ya Mungu. Daima, usemi huu unamhusu Yesu kama Bwana (kama vile Flp.2:11)

1. Weredi wa imani ya mtu katika Yesu wakati wa ubatizo (kama vile Rum 10:9-13; Mdo. 2:38; 8:12,16; 10:48; 19:5; 22:16; 1 Kor 1:13; 15; Yak. 2:7)
2. katika upungaji pepo, (kama vile Mt. 7:22; Mk. 9:38; Luka 9:49; 10:17; Mdo. 19:13)
3. katika uponyaji (kama vile Mdo. 3:6,16; 4:10; 9:34; Yak. 5:14)
4. katika tendo la huduma (kama vile Mt. 10:42; 18:5; Luka 9:48)
5. katika muda wa kutekeleza nidhamu kanisani (kama vile Mt. 18:15-20)
6. wakati wa kuhubiria watu wa Mataifa (kama vile Luka 24:47; Mdo. 9:15; 15:17; Rum.1:5)
7. katika maombi (kama vile Yn.14:13-14; 15:2,16; 16:23; 1 Kor 1:2)
8. kama njia ya kurejea Ukristo (kama vile Mdo. 26:9; 1 Kor 1:10; 2 Tim 2:19; Yak. 2:7; 1 Pet. 4:14)

Chohote tukifanyacho kama wahudumu, wasaidizi, waponyaji, watoa mapepo, n.k, tunafanya hivyo kwa tabia yake, nguvu Zake, upaji Wake - katika jina Lake.

▣ **"Je ni kwa wakati huu utawarejeshea ufalme Israeli"** Walikuwa bado wana mtazamo wa kizalendo (kama vile Zaburi 14:7; Yermia 33:7; Hosea 6:11; Luka 19:11; 24:21). Walikuwa wanaweza hata kuuliza kuhusu nafasi zao za kiutawala.

Hili ni swali la kithiolojia ambalo bado linasababisha utata mkubwa. Nataka kujumuisha hapa sehemu ya fasiri kwenye ufunuo (angalia [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org)) ambayo inajadili jambo hilihili.

"Manabii wa Agano la Kale walitabiri urejesho wa ufalme wa Kiyahudi katika Palestina ikiwela kati katika Yerusalemu, lakini Mitume wa Agano hawakuwahi kuweka lengo katika ajenda hii. je Agano la Kale halijavuviwa (kama vile Mt. 5:17-19)? Je waandishi wa Agano Jipya wameondoa matukio ya nyakati za mwisho?"

kuna vyanzo kadhaa vya taarifa kuhusu mwisho wa ulimwengu:

1. manabii wa Agano la Kale
2. waandishi wa nyakati za mwisho za Agano la Kale (kama vile Ezekieli 37-39; Danieli 7-12)
3. nyakati za kati za maagano, waandishi wa maandiko ya nyakati za mwisho za kiyahudi zisizo za kikanoni (kama I Enoch)
4. Yesu mwenyewe (kama vile Mt. 24; Marko 13; Luka 21)
5. maandiko ya Paulo (kama vile 1 Kor. 15; 2 Kor. 5; 1 The. 4; 2 The. 2)
6. maandiko ya Yohana (kitabu cha ufunuo).

Je haya yote kwa usahihi yanafundisha juu ya ajenda ya nyakati za mwisho (matukio, mtiriko, watu)? ikiwa sio, kwanini? je si kwamba yote yana uvuvio (isipokuwa maandiko ya kati ya maagano ya kiyahudi)?

Roho alifunua ukweli kwa waandishi wa Agano la Kale kutumia misamiati na vipengele walivyoweza kuvielewa. Hata hivyo, kupitia ufunuo endelevu Roho amepanua dhana hizi za Agano la Kale juu ya siku za mwisho kwa namna ya uelewa wa kiulimwengu (kama vile Efe. 2:11-3:13). Hapa ni baadhi ya mifano:

1. Jiji la Yerusalemu linatumika kama sitiari ya watu wa Mungu (Sayuni) na linaangazwa kwenye Agano Jipya kama neno linaloelezea kukubaliwa kwa Mungu kwa wote watubuo, wanadamu waaminio (Yerusalemu mpya ya Ufunuo 20-22). Upanuzi wa kithiolojia ni dhahiri, mji wa mwili kwenda katika watu wa Mungu unaaksiwa kwa mbele katika ahadi ya Mungu kuwakomboa wanadamu walioanguka katika Mwanzo 3:15 kabla hata hapajawa na Myahudi au mji mkuu wa kiyahudi. Hata wito wa Ibrahimu (kama vile Mwanzo 12:3) ulijumuisha Mataifa.
2. Katika Agano la Kale waadui wanazunguka mataifa ya kale ya Near East, lakini katika Agano Jipya wamepanuliwa kwa wasiamini wote, mpinga-Mungu, watu waliovuviwa na shetani. Vita imehama kutoka katika jiografia, migogoro ya kikanda mpaka kwenye migogoro ya kiulimwengu.
3. Ahadi ya ardhi ambalo ni jambo muhimu katika Agano la Kale (ahadi ya uzao wa ki-baba) sasa imefanyika kwa dunia yote. Yerusalemu mpya inakuja kama dunia iliyotengenezwa upya, sio Near East tu au isiyojumuishwa (kama vile Ufunuo 20-22).
4. Baadhi ya mifano mingine ya dhana za kinabii za Agano la Kale ikipanuliwa. Mbegu ya Ibrahimu sasa imefanyiwa tohara kiroho (kama vile Rum. 2:28-29); (2) watu wa agano sasa wanajumuishwa Mataifa (kama vile Hosea 1:9; 2:23; Rum. 9:24-26; pia Mambo ya Walawi 26:12; Kutoka 29:45; 2 Kor. 6:16-18 na Kutoka 19:5; Kumbukumbu la Torati 14:2; Tito 2:14); (3) hekalu sasa ni kanisa la nyumbani (kama vile 1 Kor.3:16) au waamini mmoja mmoja(kama vile 1 Kor. 6:19); na (4) hata Israeli na tungo zake za tabia ya kufunua sasa zinamaanisha watu wote wa Mungu(kama vile Gal. 6:16; 1 Pet. 2:5, 9-10; Ufunuo 1:6)

Mfano wa kinabii umetimilizwa, umepanuliwa, na sasa umekuwa jumuishi. Yesu na wandishi wa kinabii hawawasilishi nyakati za mwisho katika namna ambayo manabii wa Agano la Kale walifanya (kama vile Martin Wyngaarden, *The Future of The Kingdom in Prophecy and Fulfillment*). Wafasiri wa kisasa wanaojaribu kutengeneza mifano ya Agano la Kale iwe dhahiri au katika namna ya kawaida ya maadili yalivyozoeleka wanageuza ufunuo kwenda katika kitabu cha kiyahudi kabisa na kulazimisha maana kwenda katika kishemu kidogo kabisa, tungo tata za Yesu na Paulo! Waandishi wa Agano Jipya hawakatai manabii wa Agano la Kale, lakini wanaonesha kilele cha namna ya utenda kazi wao."

#### 1:7

**NASB** "si kazi yenu kujua majira na nyakati au wakati ambao baba ameuweka kwa mamlaka yake mwenyewe"

**NKJV** "sio kazi yenu kujua wakati na majira"

**NRSV** "sio kazi yenu kujua nyakati na vipindi"

**TEV** "nyakati na mazingira"

**NJB** "sio kazi yenu kujua nyakati na tarehe"

Neno "nyakati" (*chronos*) maana yake "vipindi" au "nyakati" (yaani kule kupita kwa muda), wakati neno "majira yanayojulikana kwa matukio fulani" (*kairos*) maana yake "muda wa tukio fulani au majira" (kama vile Tito 1:2-3). Louw na Nida: *Greek-English Lexicon*, wanasema kuwa kuna visawe ambavyo vinaonesha vipindi vya muda (kama vile 1 The. 5:1). Ni dhahiri kwamba waamini hawajaribu kupanga tarehe za kudumu; hata Yesu hakujua muda wa kurudi kwake (kama vile Mt. 24:36; Marko 13:32). Waamini wanaweza kujua muda wa kiujumla wa majira (kama vile Mt. 24:32-33). Pacha wake anasisitiza juu ya Agano Jipya kuhusu kurudi kwa mara ya pili na kuwa **wakae** katika hali **utayari**. Mengineyo ni juu ya Mungu!

**1:8 "lakini mtapokea nguvu"** Angalia kuwa kuja kwa Roho Mtakatifu kunaunganishwa na nguvu na ushuhuda. Matendo ya Mitume ni kuhusu "ushuhuda" (yaani *martus*). Maudhui yanatawala kitabu (kama vile Mdo. 1:8,22; 2:32; 3:15; 5:32; 10:39,41; 13:31; 22:15,20; 26:16). Kanisa limekuwa likimpatia kazi ushuhuda wa injili ya Kristo (kama vile Luka 24:44-49)! Mitume walikuwa mashuhuda wa maisha ya Yesu na mafundisho, sasa walikuwa mashahidi kuhusu maisha yake namafundisho. Ushuhuda wa kiufanisi unatokea tu kwa namna ya nguvu ya Roho.

Inashangaza kwamba *The Jerome Biblical Commentary* (ukurasa wa 169) anatambua hali ya Luka kuelezea "kucheleweshwa kwa siku ya mwisho." Hii ni nukuu.

"Roho ni mbadala wa *Parousia*. Hii ni nguvu ya *alla*, 'lakini,' viunganishi ambavyo vinaunganisha sehemu mbili za majibu ya Yesu. Roho ni Kanuni ya kuendelea kuwepo kwa Ukristo, nyakati ya kanisa na umisheni. Kweli hizi lazima zitokee mapema *Parousia* kama sehemu ya shabaha ya kujua kwa mkristo. Roho katika kanisa ni jibu la injili ya Luka kwa tatizo la kuchelewa kwa *Parousia* na mwendelezo wa historia."

▣ "Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." Hili ni Ainisho la kijiografia kwa Matendo:

1. Yerusalemu, Mdo. 1-7
2. Yudea na Samaria, Mdo. 8-12
3. mwisho wa nchi (yaani Rumi), Mdo. 13-28.

Ainisho hili linaweza kumaanisha muundo na kusudi wa fasihi ya mwandishi. Ukristo sio dhehebu la kiyahudi, lakini maandamano ya kiulimwengu ya Mungu mmoja wa kweli anayetimiza ahadi zake za Agano la Kale kurejesha mwanadamu nuasi katika ushirika na Yeye (kama vile Mwanzo 12:3; Kutoka 19:5; Isaya 2:2-4; 56:7; Luka 19:46).

Tungo "katika miisho ya dunia" linatumika tena katika Mdo. 13:47, ambapo ni nukuu kutoka Isaya 49:6, andiko la kimasihhi ambalo pia inatajwa "mwanga kwa ajili ya mataifa." Mkombozi (kama vile Mwanzo 3:15) kwa ajili ya mataifa (kama vile Mwanzo 12:3; Kutoka 19:5-6; Isaya 2:2-4) siku zote imekuwa mpango wa Mungu.

Wakijua tafsiri ya Agano la Kale na ahadi nyingi za kinabii za YHWH, ikiinuliwa yerusalemu, kuuleta ulimwengu Yerusalemu, ikitarajiwa haya kutimizwa kidhahiri. Walikaa katika Yerusalemu (kama vile Mdo. 8:1). Lakini injili ilipunduliwa na kupanuliwa katika dhana za Agano la Kale. Mamlaka ya kiulimwengu (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8) kuwaambia waaminio kwenda duniani kote, sio kusubiri ulimwengu kuwaendea. Yerusalemu ya Agano Jipya ni sitiari ya mbinguni (kama vile Ufunuo 21:2), sio jiji katika Palestina.

## **MADA MAALUM: MPANGO WA UKOMBOZI WA MILELE WA YHWH**

Nalazimika kukubali kwako kiongozi kuwa ninao upendeleo juu ya hoja hii. Mpangilio wangu wa kithiolojia sio wa ufuasi wa Calvin au mfumo wa kidini, bali ni agizo kuu la kiunjilisti (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Naamini Mungu ana mpango wa milele kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (mf., Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Jer. 31:31-34; Eze. 18; 36:22-39; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Rum. 3:9-18,19-20,21-31), wale wote walio umbwa kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26-27). Maangano yote yameunganishwa katika Kristo (kama vile Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Yesu ni fumbo la Mungu, lilijificha ambalo halijafunuliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13)! Injili ya Agano Jipya, sio Israel, ni ufunguo wa maandiko.

Huu uelewa wangu wa kabla unanakshi tafasiri zangu zote za maandiko. Nasoma maandiko kwa kuyapitia yote! Hakika ni upendeleo (walionao watafsiri wote), lakini ni dhahanio za utaarifishwaji wa kimaandiko. Mtizamo wa Mwanzo 1-2 ni YHWH akiandaa mahali ambapo Yeye na Uumbaji wake ulio juu, mwanadamu, waweza kuwa na ushirika (kama vile Mwanzo. 1:26,27; 3:8). Uumbaji wake wa vitu ni hatua kwa ajili ya ajenda ya ki-Ungu kati ya watu wawili.

1. St. Augustine anauanisha kama tundu lenye muonekano wa ki-Ungu katika kila mtu ambaye anaweza kujazwa tu na Mungu mwenyewe.
2. C.S. Lewis aliita sayari hii "sayari inayoshikika," (yaani., iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu).

Agano la Kale lina vidokezo vingi vya ajenda hii ya ki-Ungu.

1. Mwanzo 3:15 ni ahadi ya kwanza kuwa YHWH hatamwacha mwanadamu katika hali tete ya dhambi na

uasi. Hii hairejelei kwa Israel kwa sababu hapakuwepo na Israel, wala watu wa agano, mpaka pale Ibrahimu alipoitwa katika Mwanzo 12

2. Mwanzo 12:1-3 ni wito wa awali wa YHWH na ufunuo kwa Abraham ambao ndio ulikuja kuwa watu wa agano, Israel. Lakini hata katika huu wito wa awali, Mungu alikuwa anaangalia ulimwengu wote. Angalia Mwanzo 12:3!
3. Katika Kutoka 20 (Kumbu kumbu la Torati 5) YHWH alimpa Musa sheria ili kuwaongoza watu wake maalum. Tambua kuwa katika Kutoka 19:5-6, YHWH alidhihirisha kwa Musa uhusiano wa kipekee ambao Israel itakuwa nao. Lakini pia tambua kuwa wao walichaguliwa, kama Ibrahim, kuubariki ulimwengu (kama vile Kut. 19:5, "kwa vile vitu vyote vya Dunia ni mali yangu"). Israel ilipaswa kuwa chombo kwa mataifa kumjua YHWH na kuvutwa kwake. Kwa masikitiko makubwa wakashindwa (kama vile Eze. 36:22-38)
4. Katika 1 Wafalme 8 Sulemani aliliwakilisha hekalu ili wote waje kwa YHWH (kama vile 1 Fal. 8:43,60).
5. Katika Zaburi– 22:27-28; 66:4; 86:9 (Ufu. 15:4)
6. Kupitia kwa manabii wa YHWH kuendelea kudhihilisha mpango wake wa ukombozi kwa watu wote.
  - a. Isaya – 2:2-4; 12:4-5; 25:6-9; 42:6,10-12; 45:22; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:18,23
  - b. Yeremia – 3:17; 4:2; 16:19
  - c. Mika 4:1-3
  - d. Malaki 1:11

Msisitizo huu wa wote umerahisishwa na uwepo wa "agano jipya" (kama vile Yer.31:31-34; Ezek. 36:22-38), ambao unaangazia juu ya huruma ya YHWH, na sio utendaji wa mwanadamu aliyeanguka. Kuna "moyo mpya," "mawazo mapya," na "roho mpya." Utii ni kitu cha muhimu lakini ni cha ndani, na sio mfumo wa nje tu (kama vile Rum. 3:21-31).

Agano Jipya linaimalisha mpango wa ukombozi wa wote kwa njia mbali mbali.

1. Agizo kuu – Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8
2. Mpango wa Mungu wa milele (yaani ulio amuliwa kabla) – Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29
3. Mungu anawataka wanadamu wote waokolewe – Yohana 3:16; 4:42; Mdo. 10:34-35; 1 Tim. 2:4-6; Tit. 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14
4. Kristo anaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya – Gal. 3:28-29; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11. Mipaka yote na tofauti zote za mwanadamu zimeondolewa katika Kristo. Yesu ni "fumbo la Mungu," lililofichika lakini sasa limedhihilishwa (Efe. 2:11-3:13).

Agano Jipya linaangazia juu ya Yesu, na sio Israel. Injili, sio utaifa wala eneo la kijiografia, ni kitu cha muhimu. Israel ilikuwa ndio ufunuo wa mwanzo lakini Yesu ni hatma ya ufunuo huo (kama vile Mt. 5:17-48).

Natumai utapata wasaa wa kusoma [Mada Maalum: kwa nini ahadi za Agano la Kale zinaonekana kuwa tofauti toka ahadi za Agano Jipya](#). Waweza kupata katika mtandao [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org).

**1:9 "aliinuliwa"** Tukio hili linajulikana kama kupaa. Yesu mfufuka anarudishwa katika nafasi yake ya utukufu uliokuwako kabla (kama vile Luka 24:50-51; Yohana 6:22; 20:17; Efe. 4:10; 1 Tim. 3:16; Ebr. 4:14; na 1 Pet. 3:22). Wakala ambaye hajaelezewa wa kauli tendwa irabu ya sauti ni Baba. Angalia [MADA MAALUM: KUPAA](#) katika Mdo. 1:2. Tazama tofauti katika kitenzi kilichotumika kufunua kupaa huku.

1. "kupandishwa juu," Mdo. 1:2 – kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usio timilifu
2. "kuinuliwa juu," Mdo. 1:9 – kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usio timilifu
3. "ameinuliwa," Mdo. 1:11 (kama vile Mdo. 1:2) – kauli tendwa endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu
4. "alipandishwa kwenda mbinguni," Luka 24:51 (textual variant utofauti wa kimaandiko) – kauli tendwa elekezi ya wakati usiotimilifu.

Angalia [MADA MAALUM: KUPAA](#) katika Mdo. 1:2.

▣ **"mawinguni"** Mawingu yalikuwa alama muhimu ya nyakati za mwisho muhimu. Angalia Mada Maalum inayofuata.

## **MADA MAALUM: KUJA MAWINGUNI (Maneno kadhaa ya Kiebrania, hasa *anan*, BDB 777, KB 857)**

Huu ujio wa mawinguni ulikuwa ishara muhimu sana ya matukio ya siku za mwisho. Huu ulitumika katika njia tatu tofauti ndani ya Agano la Kale.

1. Kuonyesha mwonekano wa uwepo wa Mungu, *Shekinah* wingu la Utukufu kama vile Kut. 13:21; 14:19,20,24; 16:10; 19:9; Hes. 11:25; Neh. 9:19)
2. kuufunika Utakatifu Wake ili kwa mwanadamu asimuone na kufa (kama vile Kut. 33:20; Isa. 6:5)
3. kuupandisha Uungu (kama vile Zab. 18:9; 104:3; Isa. 19:1; Nah. 1:3; Mdo. 1:9; 1 The. 4:17)

Katika Danieli 7:13 mawingu yalitumika kama usafirishaji wa uungu, Masihi aliye mwanadamu (tazama Mada Maalum: Masihi). Unabii huu ulio ndani ya Danieli unadokezwa mara 30 katika Agano Jipya. Uhusiano huu huu wa Masihi pamoja na mawingu ya mbinguni unaweza kuonekana katiaka Mt. 24:30; 26:64; Marko 13:26; 14:62; Luka 21:27; Mdo. 1:9,11; 1 The. 4:17; Ufu. 1:7.

**1:10 "Walipokuwa wakikaza macho"** Hii ni kauli isiyotimilifu yenye mafumbo. Walikuwa wakiendelea kukaza macho kumuangalia Yesu kadiri inavyowezekana. Hata baada ya kupoteza kuona, waliendelea kuangalia. Neno hili ni tabia ya maandiko ya Luka (kama vile Luka 4:20; 22:56; Mdo. 1:10; 3:4,12; 6:15; 7:55; 10:4; 11:6; 13:9; 14:9; 23:1, inapatikana katika Agano Jipya nje, in 2 Wakorintho 3). Ilimaanisha "kukazia macho," "kuangalia sana," au "kuweka macho katika kuangalia."

▣ **"katika anga"** Watu wa kale waliamini mbingu ilikuwa juu, lakini katika siku zetu za maarifa kamili ya ulimwengu, juu ina uhusiano. Katika Luka 24:31, Yesu alipotea. Hii inaweza kuwa mfano bora kwa desturi. Mbingu haipo juu na huko nje, lakini yawezekana kipimo kingine cha muda na nafasi. Mbingu sio katika uelekeo lakini katika nafsi!

▣ **"watu wawili katika mavazi meupe"** Agano Jipya mara nyingi zinatambua malaika, (kama vile Luka 24:4; Yohana 20:12). Malaika walitokea wakati wa kuzaliwa kwake, majaribu yake, katika Gethsamane, katika kaburi, and here na hapa katika kupaa kwake.

**1:11 "watu wa Galilaya"** Mara kadhaa katika Mdo Luka anawekakumukumbu ya uasili wa wanafunzi wa Galilaya (kama vile Mdo. 2:7; 13:31). Kumi na mbili wote, isipokuwa Yuda Iskarioti, walikuwa wanatokea Galilaya. Eneo hili lilikuwa likidharauliwa na wakazi wa Yudea kwasababu lilikuwa na idadi kubwa ya watu na ilikuwa na "kosher" (yaani makini) katika utenda kazi wake wa desturi za midomo (Talmud). Mtu anaweza kushangaa ikiwa Luka alitengeneza mabadilishano haya kujibu maswali ya baadae kuhusu kuchelewa kwa ujio wa mara ya pili. Wakristo hawatakiwi kuweka mkazo kwenye *Parousia* lakini katika huduma, evangelismuinjilisti, na misheni!

▣ **"Yesu.....atakuja"** Baadhi ya wana thiolojia wanajaribu kuweka tofauti kati ya "Yesu" na "tuhakiki." Malaika hawa wanakiri kwamba ni Yesu ambaye walimjua angerudi. Kristo aliyetukuzwa na, aliyepaa Kristo bado ni Yesu wa Nazareth aliyetukuzwa.

Yesu atakuja tena kama alivyoondoka, katika mawingu (Angalia Mada maalumu katika Mdo. 1:9, kama vile Mt. 10:23; 16:27; 24:3,27,37,39; 26:64; Marko 8:38-39; 13:26; Luka 21:27; Yohana 21:22; 1 Kor. 15:23; 1 The. 1:10, 4:16; 2 The. 1:7, 10; 2:1,8; Yak. 5:7-8; 2 Pet. 1:16; 3:4,12; 1 Yohana 2:28; Ufunuo 1:7). Kuja kwa Mara ya Pili kwa Yesu ni maudhui kubwa na inayotokea na dhamira kubwa ya Agano Jipya. Sababu kuu ya injili ilichukua muda mrefu kuwekwa katika muundo wa mategemeo ya kurudi karibuni kwa Kristo kwa kanisa la mwanzo. Kuchelewa

kwake huku kunakoshangaza, kufa kwa mitume, na kuinuka kwa uvumi yote hatimaye yalilifanya kanisa kuweka kumbukumbu la maisha na mafundisho ya Yesu katika muundo wa maandishi..

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 1: 12-14**

<sup>12</sup> Kisha wakarudi kwenda Yerusalemu kutoka mlima ulioitwa wa Mizeituni, ulio karibu na Yerusalemu, wapata mwendo wa sabato. <sup>13</sup> Hata walipoingia, wapakanda orofani, walipokuwa wakikaa; Petro, na Yohana, na Yakobo, na Andrea, Filipo na Tomaso, Bartholomayo na Mathayo, Yakobo wa Alfayo, na Simoni Zelote, na Yuda wa Yakobo. <sup>14</sup> Hawa wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali, pamoja nao wanawake, na Mariamu mama yake Yesu, na ndugu zake.

**1:12 "wakarudi"** Luka 24:52 inaongeza "kwa furaha kubwa."

▣ **" mlima ulioitwa wa Mizeituni "** Hii inapingana na Luka 24:50 (yaani Bethania); Hata hivyo, linganisha Luka 19:29 na 21:37 pamoja na Marko 11:11-12 na 14:3. Kimpando kijulikanacho kama Mlima wa Mzeituni ulikuwa kama maili 2.5 kama 300-400 futi juu ya Yerusalemu mkabala na Bonde la Kidron, kupitia katika Hekalu. Imetajwa katika unabii wa matukio ya siku za mwisho ya Agano la Kale (kama vile Zekaria 14:4). Yesu alikuwa amekutana na wanafunzi mara nyingi kuomba na yawezekana kwenda nje kuweka kambi pamoja.

▣ **"mwendo wa sabato"** Mwendo wa Myahudi ambao angeweza kutembea siku ya Sabato ulipangwa na waalimu (kama vile Kutoka 16:29; Hesabu 35: 5). Ulikuwa ni mwendo kama wa hatua (miguu) 2,000, ambao walimu walipanga umbali mrefu zaidi ambao mtu angetembea katika sabato na kutovunja sheria ya Musa.

**1:13 "chumba cha juu orofani"** Hii yawezekana ilikuwa sehemu ileile kama ya Karamu ya Mwisho (kama vile Luka 22:12; Marko 14:14-15). Desturi zinasema kilikuwa ni chumba cha juu (ghorofa ya pili au ya tatu) ya nyumba ya Yohana Marko (kama vile Mdo. 12:12), aliyaandika kumbukumbu za Petro katika Injili ya Marko. Lazima kilikuwa chumba kikubwa na uwezo wa kupokea watu 120.

▣ **"wao"** Hii ni moja ya orodha nne za mitume (kama vile Mt. 10:2-4; Marko 3:16-19; na Luka 6:14-16). Orodha hazifanani. Majina na mpangilio unabadilika. Hata hivyo, walikuwa siku zote watu walewale waliotajwa katika makundi manne yay a watatu. Petro siku zote huwa ni wa kwanza na Yuda huwa ni wa mwisho. Makundi haya matatu ya wane yawezekana walikuwa na kusudi la kuruhusu watu kurudi nyumbani kwa vipindi kupata mahitaji na kuangalia mahitaji ya familia zao. Angalia Mada Maalum inayofuata.

**MADA MAALUMU: CHATI YA MAJINA YA MITUME**

	<b>Mathayo 10:2-4</b>	<b>Marko 3:16-19</b>	<b>Luka 6:14-16</b>	<b>Mdo. 1:12-18</b>
<b>Kundi la kwanza</b>	Simoni (Petro) Andrea (Petro nduguye) Yakobo (mwana wa Zebedayo) Yohana (nduguye Yakobo)	Simoni (Petro) Yakobo (mwana wa `Zebedayo) Yohana (nduguye Yakobo) Andrea	Simoni (Petro) Andrea (Petro nduguye) Yakobo Yohana	Petro Yohana Yakobo Andrea
<b>Kundi la pili</b>	Filipo Bartholomayo Thomaso Mathayo (mtunza ushuru)	Filipo Bartholomayo Mathayo Thomaso	Filipo Bartholomayo Mathayo Thomaso	Filipo Thomaso Bartholomayo Mathayo



<b>Kundi la tatu</b>	Yakobo (mwana wa Alfayo) Thadayo Simoni (Mkananayo) Yuda (Iskariote)	Yakobo (mwana wa Alfayo) Thadayo Simoni (Mkananayo) Yuda (Iskariote)	Yakobo (mwana wa Alfayo) Simoni (Zelote) Yuda (wa Yakobo) Yuda (Iskariote)	Yakobo (mwana wa Alfayo) Simoni (Zelote) Yuda (wa Yakobo)
----------------------	---	---	--	--

Kutoka katika muhtasari wa Luka 6:14:

☐ **“Simoni, aliyemwita jina la pili Petro”** Kuna orodha nyingine tatu za mitume kumi na wawili. Kwa kawaida Petro ni wa kwanza; Yuda Iskariote ni wa mwisho daima. Kuna makundi matatu kati ya manne ambayo yamebaki kwa usawa, hata kama mtiririko wa majina ndani ya makundi unageuzwa mara kwa mara (kama vile Mathayo. 10:2-4; Marko 3:16-19; Mdo. 1:13).

☐ **“Andrea”** Neno la Kiyunani linamaanisha “mwenye sifa za kiume.” Kutoka Yohana 1:29-42 tunajifunza kwamba Andrea alikuwa mwanafunzi wa Yohana Mbatizaji na kwamba alimtambulisha nduguye, Petro, kwa Yesu.

☐ **“Yakobo”** Hili ni jina la Kiebrania “Jacob” (BDB 784), ambalo linamaanisha “chukua nafasi ya,” kama vile Mwa. 25:26). Kuna wanaume wawili wanaitwa Yakobo katika katika orodha ya wale Kumi na wawili. Ni nduguye Yohana (kama vile Marko 3:17) na sehemu ya mzunguko wa ndani (yaani, petro, yakobo, na yohana). Huyu ni nduguye Yohana.

☐ **“Yohana”** Huyu alikuwa nduguye Yakobo na moja wa mzunguko wa ndani wa wanafunzi. Aliandika vitabu vitano katika Agano Jipya na aliishi kipindi kirefu kuliko mtume ye yote yule.

☐ **“Filipo”** Jina la Kiyunani linamaanisha “mpenda farasi” Wito wake umeandikwa katika Yohana 1:43-51.

☐ **“Bartolomayo”** Jina linamaanisha “mwana wa mtawala wa Misri” Anaweza kuwa Nathanaeli wa Injili ya Yohana (kama vile Yohana 1:45-49; 21:20).

☐ **“Mathayo”** Jina la Kiebrania (kutoka *Mattithiah*, kama vile 1 Nya. 9:31; 15:18,21; 16:5; 25:3,21; Neh. 8:4) linamaanisha “karama ya YHWH.” Hii inarejea katika Lawi (kama vile Marko. 2:13-17).

☐ **“Tomaso”** Jina la Kiebrania linamaanisha “pacha” au Didimus (kama vile Yohana 11:16; 20:24; 21:2).

☐ **“Yakobo wa Alfayo”** Hili ni jina la Kiebrania “Jacob.” Kuna wanaume wawili walioitwa kwa jina la Yakobo katika wale Kumi na wawili. Mmoja ni nduguye Yohana (kama vile Luka 6:17) na sehemu ya mzunguko wa ndani (yaani, Petro, Yakobo, na Yohana). Huyu anajulikana kama “Yakobo aliye mdogo” (kama vile Marko 3:17).

☐ **“Simoni aitwaye Zelote”** Maandishi ya Kiyunani ya Marko yana “Mkananayo” (pia Mathayo. 10:4). Marko, ambaye Injili iliandikwa kwa Warumi, asingetakiwa kutumia “maneno makali” ya kisiasa, Zelote, ambalo linarejea juu ya Wapigania Mabadiliko wa Kiyahudi Waishio mstuni walio kinyume na utawala wa Kirumi. Luka anamtaja kwa istilahi hii (kama vile Mdo. 1:13). Istilahi ya Mkananayo ina minyumbuo mbali mbali.

1. kutoka eneo la Galilaya lijulikanalo kama Kana
2. kutoka matumizi ya Agano la Kale ya Wakanaani kama mfanyabiashara
3. kutoka jina la jumla kama mwenyeji wa Kanaani.

Kama jina la jumla alilolitumia Luka ni sahihi, basi Zelote linatokana na neno la Kiaramu “*enthusiast*” (kama vile Mdo. 1:17). Uchaguzi wa Yesu wa wanafunzi kumi na wawili walikuwa wametoka makundi shindani tofauti na mbalimbali. Simoni alikuwa mmoja wa kundi la kizalendo ambalo lilipigania kupinduliwa kwa ghasia za mamlaka ya Kirumi. Mara nyingi Simoni na Lawi (yaani, Mathayo, mtoza ushuru) na kila mmoja .wasingekuwa katika chumba kile kile

☐ "Yuda wa Yakobo" Pia aliitwa "Lebbeus" (kama vile Mt. 10:3) au "Yuda" (kama vile Yohana 14:22). Yote Thadayo na Lebbeus inamaanisha "mtoto apendwaye.

☐ "Yuda Iskariote," Kuna Simoni wawili, Yakobo wawili, na Yuda wawili. Jina Iskariote lina uwezekano wa minyumbuo miwili:

1. mtu wa Kerioth (mji) katika (kama vile Jos. 15:23, ambapo ingemaanisha yeye alikuwa wa Yudea pekee)
2. jina la baba yake (kama vile Yohana 6:71; 13:2,26)
3. "mtu wa uadui" au mwuaji, ambapo ingemaanisha yeye pia alikuwa Zelote, kama Simoni

☐ "**Petro**" Wayahudi wengi wa Galilaya walikuwa na yote majina ya kiyahudi (mfano Simoni au Simeoni [BDB 1035, kama vile Mwanzo 29:33], ikimaanisha "kusikia") na jina la Kiyunani (ambalo halikuwahi kutolewa). Yesu alimuita jina maarufu "mwamba." Katika Kiyunani ni *petros* na ni Kiaramaiki ni *cephas* (kama vile Yohana 1:42; Mt. 16:16).

☐ "**Andrea**" Neno la Kiyunani linamaanisha "ya kiume." Kutoka Yohana 1:29-42 Tunajifunza kwamba Andrea alikuwa mwanafunzi wa Yohana Mbatizaji na kwamba alimtambulisha nduguye Petro kwa Yesu

☐ "**Filipo**" Neno la Kiyunani "apendaye farasi." Wito wake unaelezwa katika Yohana 1:43-51.

☐ "**Tomaso**" Neno la Kiebrania linamaanisha "mapacha" au Didymus (kama vile Yohana 11:16; 20:24; 21:2).

☐ "**Batholomayo**" Neno linamaanisha "Mwana wa Ptolemy." Aliwezekana akawa Nathanaeli ("zawadi ya Mungu," BDB 681 na 41) ya Injili ya Yohana (kama vile Yohana 1:45-49; 21:20).

☐ "**Mathayo**" Yawezekeka linahusiana na jina la kiebrania *Mattenai*, linaloamaanisha "zawadi ya YHWH" (BDB 683). Haya ni maelezo mengine kwa Walawi (kama vile Marko 2:14; Luka 5:27).

☐ "**Yakobo**" Hii ni neno la Kiebrania "Yakobo" (BDB 784, kama vile Mwanzo 25:26) Kuna wanaume wawili walioitwa Yakobo katika orodha ya kumi na mbili. Mmoja wapo ni Yohana (kama vile Marko 3:17) na sehemu ya mzunguko wa ndani (yaani Petro, Yakobo, and Johnna Yohana). Hili linajulikana kama Yakobo wa chini.

☐ "**Simoni Zelote**" Andiko la Kiyunani la Marko "Mkanaani" (pia Mt. 10:4). Marko, ambao injili iliandikwa kwa Warumi, yumkini kuyatumia kisiasa "kifungo-cha moto" neno "Zelote," ambalo lilimaanisha kikundi cha kiasi kilichoipinga serikali ya Kirumi. Luka hajiiti kwa jina hili (kama vile Luka 6:15 na Mdo. 1:13). Neno "Mkanaani" linaweza kuwa na vihusishi vyake.

1. Eneo la Galilaya lililojulikana kama Kana
2. kutoka katika matumizi ya Mkanaani ya Agano la Kale kama wafanya biashara
3. Kutoka katika maelezo ya jumla kama mkanaani mzawa.

Kama maelezo ya Luka yako sawa, hivyo "Zelote" inatoka katika neno la kiaramaiki "mwenye shauku" (kama vile Luka 6:15; Mdo. 1:17). Wanafunzi kumi na mbili wa Yesu waliochaguliwa walitoka katika vikundi mbali mbali vinyoshindana. Simoni alikuwa mwanachama wa kikundi cha kizalendo ambacho kilikuwa kinatetea kupinduliwa kwa mamlaka ya Kirumi. Kawaida Simoni Mlawi (yaani Mathayo mtoza ushuru) asingekuwa katika chombo kimoja na wengine.

☐ "**Thadeo**" Pia alikuwa akiitwa "Lebbeus" ("mtu wa moyo," kama vile Mt. 10:3) au "Yuda" (kama vile Luka 6:16; Yohana 14:22; Mdo. 1:13). Thadeo linamaanisha "mtoto mpendwa" (kidhahiri "kutoka katika matiti").

☐ "**Yuda Iskarioti**" Kuna Simoni wawili na Yuda wawili. "Iskarioti" na wana vihusishi viwili vinyowezekeka: (1) mtu wa kerioth katika Yuda (kama vile Joshua 15:23) au (2) "mtu mwenye bisu" au muuaji wa kuajiriwa, ambaye ingemaanisha kwamba pia alikuwa Zelote, kama Simoni.

## MADA MAALUMU: YUDA ISKARIOTI

Yuda alikwisha sikia, akachunguza, na kufanya ushirika na Bwana Yesu kwa karibu sana kwa miaka mingi, lakini dhahili kabisa hakuwa na ushirika binafsi na Yeye katika imani (k.v. Mt. 7:21-23). Petro naye alipitia uzito ule ule wa jaribu kama alilolipitia Yuda, lakini yakiwa na matokeo yenye athari kubwa (k.v.Mt. 26:75). Majadiliano mengi yalifanyika juu ya mwenendo wa usaliti wa Yuda:

1. Kimsingi yalikuwa ni mambo ya fedha (k.v.Yoh.12:6)
2. Kimsingi yalikuwa ni mambo ya kisiasa (k.v William Klassen, *Judas Betrayer or Friend of Jesus?*)
3. Yalikuwa ni mambo ya kiroho (kama vile Luka. 22:3; Yoh. 6:70; 13:2,27)

Juu ya somo la ushawishi wa kishetani au kumilikiwa na pepo (angalia Mada Maalumu: hali ya kimapepo katika agano jipya) kuna vyanzo mbali mbali vya kimapato (vilivyo oredheshwa katika mpangilio wa wale ninao waamini)

1. Merrill F. Unger, *Biblical Demonology, Demons in the World Today*
2. Clinton E. Arnold, *Three Crucial Questions About Spiritual Warfare*
3. Kurt Koch, *Christian Counseling and Occultism, Demonology Past and Present*
4. C. Fred Dickason, *Demon Possession and the Christian*
5. John P. Newport, *Demons, Demons, Demons*
6. John Warwick Montgomery, *Principalities and Powers*

Uwe mwangalifu juu ya udanganyifu wa kitamaduni na miiko. Shetani anamwathuri Petro katika Mt. 16:23 kumjaribu Yesu katika njia zile zile-kifo chake mbadala. Shetani anaendelea. Anajaribu kutumia kila liwezekanalo kuzuia kazi ya Yesu ya ukombozi kwa niaba yetu.

1. Jaribu la Yesu, Luka 4
2. Akamtumia Petro
3. Akamtumia Yuda Iskarioti na wakuu wa Sinagogi

Yesu hata anamwelezea Yuda kama shetani katika Yohana 6:70. Biblia haizungumzii somo la kushawishiwa na kumilikiwa na shetani kama inahusiana na waumini. Lakini, waumini wazi kabisa wanaathiriwa na maamuzi binafsi na uovu binafsi (angalia Mada Maalumu: Uovu Binafsi)

Asili ya "Yuda Iskarioti" kwa kiasi Fulani haieleweki; hata hivyo, kuna uwezekano mbali mbali:

1. *Kerioth*, mji wa Yuda (k.v. Yosh. 15:25)
2. *Kartan*, mji wa Galilaya (k.v. Yosh. 21:32)
3. *Karōides*, walipomlaki na matawi ya mitende huko Yerusalemu au Yeriko
4. *scortea*, aproni au begi la ngozi (k.v. Yoh. 13:29)
5. *ascara*, kujinyonga (Waebrania) toka Mt. 27:5
6. kisu cha kujiulia (Kiyunani), ikimaanisha alikuwa mkereketwa kama simion(k.v. Luka 6:15)

**1:14 "wote hawa kwa moyo mmoja"** Neno hili ni ambatani ya "hili lilelile" (*homo*) na "hisia za ufahamu" (*thumos*). Haikuwa kigezo kama vile ingekuwa mazingira ya mategemeo. Mtazamo huu unatajwa tena na tena katika Mdo. (yaani ya waaminio, kama vile Mdo. 1:14; 2:46; 4:24; 5:12; 15:25; na ya wengine katika Mdo. 7:57; 8:6; 12:20; 18:12; 19:29).

NASB	"wakiendelea kujitoa"
NKJV	"kuendelea"
NRSV	"wakidumu katika kujitoa"
TEV	"wakikusanyika mara kwa mara"
NJB	"wakidumu katika kuungana"

Neno hili (*pros* na *kaptereō*) linamaanisha kuwa makini au kwa bidii au kuhusika kwa nia dhabiti. Luka analitumia mara nyingi (kama vile Mdo. 1:14; 2:42,46; 6:4; 8:13; 10:7). Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo yenye mafumbo.

▣ **"pamoja nao wanawake"** Kulikuwa na kikundi cha wanawake waliosafiri pamoja na kujitolea na kuwahudumia Yesu na mitume (kama vile Mt. 27:55-56; Marko 15:40-41; Luka 8:2-3; 23:49; na Yohana 19:25). Angalia Mada Maalum inayofuata.

## MADA MAALUM : WANAWAKE WALIOFUATANA NA YESU NA WANAFUNZI WAKE

### Mathayo. 27:55-56

Maria Magdalene

Mariamamu, mama yao

Yakobo na Yusufu

Mama wa wana wa  
Zebedayo (Yakobo na  
Yohana)

### Marko 15:40-41

Maria Magdalene

Mariamamu, mama wa

Yakobo Mdogo na, Yose

Salome

### Luka 8:2-3; 23:49

Maria Magdalene

Yoana, mkewe Kuza (wakili  
wa Herode)

Susana na wengine wengi

### Yohana 19:25

Mariamamu, mama wa Yesu

Umbu la mamaye

Mariamamu, wa Klopa

Mariamamu Magdalene

Yafuatayo ni maelezo yahasuyo hawa wanawake kutokana na maoni yangu kuhusu Marko 15:40-41:

**"Palikuwepo na wanawake wakitazama kwa mbali."** Kundi la kimitume lilisaidiwa na wanawake kadhaa wanawake waliohudumia kwa vyote kiuchumi na kimwili (yaani, kupika, kusafisha, nk. Kama vile Marko 15:41; Mt. 27:55; Luka 8:3).

**"Mariamu Magdalene."** Magdala ulikuwa mji mdogo katika fukwe za Bahari ya Galilaya, umbali wa maili tatu kaskazini mwa Tiberia. Mariamu alimfuata Yesu kutoka Galilaya baada ya Yeye kumkomboa kutoka katika pepo kadhaa waliokuwa wachafu (kama vile Luka 8:2). Pasipokuwa na usawa huyu alitambuliwa kama kahaba lakini hakuna ushahidi wa Agano Jipya wa jambo hili.

**"Mariamu, mama yao Yakobo na Yusufu."** Katika Mt. 27:56 huyu anaitwa "mama yao Yakobo na Yusufu." Katika Mt. 28:1 huyu anaitwa "Mariamu yule wa pili." Swali la muhimu ni hili, huyu alikuwa mke wa nani? Katika Yohana 19:25 bila shaka huyu alikuwa mke wa Klopa, bado mwanaye Yakobo, aliyesemekana kuwa "mwana wa Alfayo" (kama vile Mt. 10:3; Marko 3:18; Luka 6:15).

**"Salome."** Huyu alikuwa mama wa Yakobo na Yohana, ambao walikuwa sehemu ya mzunguko wa ndani wa mwanafunzi wa Yesu, na mke wa Zebedayo (kama vile Mt. 27:56; Marko 15:40; 16:1-2).

Yafuataayo ni maelezo yangu kuhusu wanawake hawa kutokana na maoni yangu ya Yohana 19:25:

**"Na penye msalaba wake Yesu walikua wamesimama mamaye, na umbu la mamaye, Mariamu wa Klopa, na Mariamu Magdalene"** Kuna mjadala mwingi kuhusu kwa vyovyote kuna majina mane hapa au majina matatu.

Inawezekana kwamba kuna majina matatu kwa sababu hapawezi kuwa na maumbu mawili wanaoitwa Mariamu. Umbu la Mariamu, Salome, limetajwa katika Marko 15:40 na Mt. 27:56. Ikiwa ndivyo ilivyo, hii ingemaanisha Yakobo, Yohana na Yesu walikuwa jamaa wa karibu. Karne ya pili ya desturi (Hegesippus) inasema kwamba Klopas alikuwa ndugu wa Yusufu. Mariamu wa Magdala alikuwa mmoja wa wale ambao Yesu aliwaondolea pepo saba, na wa kwanza aliyemchagua kujionyesha kwake baada ya ubatizo Wake (kama vile Yohana 20:1-2; 11-18; Marko 16:1; Luka 24:1-10).

▣ **"ndugu zake"** Tunawajua baadhi ya ndugu wa Yesu: Yuda na Yakobo (Angalia Mada maalum katika Mdo. 12:17), na Simoni (kama vile Mt. 13:55; Marko 6:3 na Luka 2:7). Walikuwa hapo kabla wasioamini (kama vile Yohana 7:5), lakini sasa ni sehemu ya kundi la ndani la wanafunzi. Kufuatilia mjadala mzuri wa kimuhtasari wa ukuaji wa historia ya mafundisho ya "ubikra wa kudumu" wa Maria, angalia F. F. Bruce, *New International Commentary, Acts*, kur. 44, kidokezo namba 47.

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 1:15-26

<sup>15</sup> Siku zile akasimama Petro kati ya hao ndugu (jumla ya majina ilipata mia na ishirini), akasema, <sup>16</sup> Ndugu, ilipasa andiko litimizwe, alilolinena Roho Mtakatifu zamani kwa kinywa cha Daudi, katika habari za Yuda aliyewaongoza wao waliomkamata Yesu; <sup>17</sup> kwa sababu alikuwa amehesabiwa pamoja na sisi, akapata sehemu ya huduma hii. <sup>18</sup> (Basi mtu huyu alinunua konde kwa ijara ya udhalimu; akaanguka kwa kasi akapasuka matumbo yake yote yakatoka. <sup>19</sup> Ikajulikana na watu wote wakao Yerusalemu; hata konde lile likaitwa kwa lugha yao Akeldama, maana yake, konde la damu.) <sup>20</sup> Kwa maana imeandikwa katika chuo cha Zaburi, Kikao chake na kiwe ukiwa, Wala asiwepo mtu mwenye kukaa humo; <sup>21</sup> Basi katika watu waliofuatana nasi wakati wote Bwana Yesu alipokuwa akiingia na kutoka kwetu, <sup>22</sup> kuanza tangu ubatizo wa Yohana, hata siku ile alipochukuliwa kwetu kwenda juu, inapasa mmoja wao awe shahidi wa kufufuka kwake pamoja nasi. <sup>23</sup> Wakaweka wawili, Yusufu, aitwaye Barsaba, aliyekuwa na jina la pili Yusto, na Mathiya. <sup>24</sup> Kisha wakaomba, wakasema, Wewe, Bwana, ujuaye mioyo ya watu wote, tuonyeshe ni nani uliyemchagua katika hawa wawili, <sup>25</sup> ashike mahali katika huduma hii na utume huu, alioukosa Yuda, aende zake mahali pake mwenyewe. <sup>26</sup> Wakawapigia kura; kura ikamwangukia Mathiya; naye akahesabiwa kuwa pamoja na mitume kumi na mmoja.

**1:15 "Siku zile"** Kiuhalisia hii ni "katika siku hizi" (*en tais hēmerais*) Kifungu hiki kinatumika mara nyingi katika sura za ufunguzi za Matendo ya Mitume (kama vile Mdo. 1:15; 2:18; 5:37; 6:1; 7:41; 9:37; 11:27; 13:41). Luka anatomia vyanzo vingine vya ushahidi mwingine wa macho. Pia anatomia aya ya "kutoka siku hadi siku" (*kath hēmeran*) kama kwaida, kiashiria cha wakati wenye utata katika sura za awali za kitabucha Matendo ya Mitume (Kama vile Mdo. 2:46, 47; 3:2; 16:5; 17:11,31; 19:9). Baada ya Mdo. 15, Luka kwa upekee anafahamika kwa wingi wa matukio aliyo yaandika. Bado anaendelea kutumia neno "siku" mara kwa mara, lakini si mara kwa mara kama katika utata huu, vifungu vya kinahau.

▣ **"akasimama Petro"** Kwa uwazi Petro ni msemaji wa Mitume (kama vile Mathayo 16). Alihubiri mahubiri yake ya kwanza kwa kanisa kwanza baada ya ujio wa Roho (kama vile Matendo ya Mitume 2) na hotuba ya pili katika Matendo ya Mitume 3. Yesu alijionyesha kwake kwa mara ya kwanza baada ya mionekano ya ufufuo (kama vile Yohana 21 na 1 Kor. 15:5). Jina lake la Kiebrania ni "Simoni" (kama vile Matendo ya Mitume 15:14; 2 Pet. 1:1). Jina hili linatamkika "Simoni" katika Kiyunani. Neno "Petro" ni neno la Kiyunani (*petros*) kwa maana ya "mwamba uliojitenga." Hii ni "Kefa" au "msingi wa mwamba" katika lugha ya Kiaramu (kama vile Mt. 16:18).

▣ **"jumla ya majina ilipata mia na ishirini"** Hiki kifungu kimetengwa ndani ya mabano katika Tafsiri ya UBS<sup>4</sup> ya Kiyunani (lakini si Matendo ya Mitume 1:18-19). Kundi hili lazima litakuwa limehusisha wale Mitume kumi na wawili, wale wanawake waliokuwa wakifuatana na Yesu, na wanafunzi wengine waliotokana na mahubiri ya Yesu na huduma ya uponyaji.

**1:16 "andiko"** Marejeleo yote yanayohusu "Andiko" katika kitabu cha Agano Jipya (isipokuwa 2 Pet. 3:15-16) yanarejelea juu ya kitabu cha Agano la Kale (mfano Mt. 5:17-20; 2 Tim. 3:15-17). Kifungu hiki pia kinaeleza juu ya ule uvuvio wa Roho Mtakatifu (kama vile 2 Pet. 1:21) kupitia Daudi. Pia kifungu kinaeleza idhinisho la sehemu ya "Mandiko" ya Biblia ya Kiebrania.

## MADA MAALUM: UVUVIO

Haya ni maelezo ya imani kwamba Mungu alikuwa anahusika kwa bidii katika kuweka kumbukumbu ya matukio Yake, promisesahadi, and will for mankind na mapenzi yake kwa binadamu. Hii "ni" kujifungua kibinafsi kiungu! Kufungua huku kunaitwa "ufunuo." Kuweka kumbukumbu huku kwa baadaye kunaitwa "uvuvio."

Neno pekee linalotumika "uvuvio" katika Biblia liko katika 2 Tim. 3:16 na kiuhalisia "Mungu alipumulia." Tazama "maandiko" katika Agano Jipya siku zote yanarejerea Agano la Kale (yaani 2 Tim. 3:15 ikimaanisha makuzi ya kiyahudi ya Timotheo). Angalia kusudi la maandiko liko sehemu mbili.

1. hekima inayopelekea wokovu, 2 Tim. 3:15
2. mafunzo ya haki, 2 Tim. 3:16

Tazama namna Yohana 5:39; 1 Kor. 15:3-4; na 1 Pet. 1:10-12 Angalia Agano la Kale linatuelekeza katika Kristo. Yesu mwenyewe anakiri katika Luka 24:25-27! Roho aliwaongoza waandishi wa Agano la Kale (kama vile 2 Pet. 1:20-21). Kanisa lilikubali Kanoni (angalia Mada Maalum: Kanoni) ya Agano la Kale. Waliliona kama lililojaa uvuvio (kama vile Mt. 5:17-19). Hata hivyo, waligundua pia katika Agano Jipya, ambalo lilijumuisha maneno ya Yesu na matendo (kama vile Mt. 5:21-48; Ebr. 1:1-2). Yesu yu kamili, mwisho, na kukamilisha ufunuo wa YHWH (kama vile Yohana 1:1-5,14; Kol. 1:15-16). Yeye anatimiza ahadi ya Agano la Kale ya Masihi (yaani Mt. 26:31,56; 14:27,49; Luka 20:17; Yohana 12:14-16; 13:18; 15:25; 17:12; 19:24-36; Mdo.1:16; 3:18,21-26; 4:25-28).

Roho lazima afungue ufahamu na moyo ili mtu aweze kuelewa (kama vile Mdo. 8:34-35; 13:27). Roho aliwaongoza waandishi wa kibiblia kuelezea maneno kibinadamu, nahau, na ufafanuzi wa kweli za ufunguzi binafsi wa Mungu katika Yesu (kama vile Yohana 14:26; 15:26-27; 1 Kor. 2:10-11,13-16).

Mjadala mzuri wa kimuhtasari unapatikana katika Millard J. Erickson, *Christian Theology*, 2nd ed., ukurasa. 224-245. Pia mjadala mzuri wa kifasihi wa mchakato kutoka "ya kinywa" yaliyojikita katika jamii ya nyaraka zilizoandikwa ni H. Walton na D. Brent Sandy, *The Lost World of Scripture* (2013).

▣ **"ilipasa"** Hili ni neno *dei*, ambalo linamaanisha umuhimu. Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati usiotimilifu ambayo inarejelea juu ya ile nukuu ya kwanza katika Matendo ya Mitume 1:20. Hili neno ni sifa bainifu ya maana ya Luka kuhusu maisha ya Yesu na kanisa la kale lililo upana wa Maandiko ya kitabu cha Agano la Kale (kama vile Luka 18:31-34; 22:37; 24:44). Luka analitumia neno hili mara kwa mara (kama vile Luka 2:49; 4:43; 9:22;11:42; 12:12; 13:14,16,33; 15:32; 17:25; 18:1; 19:5; 21:9; 22:7,37; 24:7,26,44; Matendo ya Mitume 1:16,21; 3:21; 4:12; 5:29; 9:6,16; 14:27; 15:5; 16:30; 17:3; 19:21,36; 20:35; 23:11; 24:19; 25:10,24; 26:9; 27:21,24,26). Hili neno linamaanisha "linaunganisha," "ni muhimu," "haiepukiki." Injili na ukuaji wake havikutokea kwa bahati mbaya, bali mpango wa Mungu wa awali na utimilifu wa Agano la Kale (Matumizi ya Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiyunani LXX ).

▣ **"litimizwe"** Mtu asomapo nukuu hizi za kitabu cha Agano la Kale (Matendo ya Mitume 1:20), usaliti wa Yuda halikuwa kusudio la mwandishi wa Zaburi (yaani, Zab. 69:25; 109:8). Mitume walikitafsiri kitabu cha Agano la Kale ndani ya nuru ya uzoefu wao pamoja na Yesu. Hii inaitwa fasiri ya kiufanisi (kama vile Mdo. 1:20). Yesu Mwenyewe anaweza kuwa ameweka mpangilio wa mtazamo huu kama alivotembea na kunena na wale wawili katika barabara ya kuelekea Emmau (kama vile Luka 24:13-35, hasa Matendo ya Mitume 1:25-27). Wafasiri wa mwanzo wa Kikristo waliona ufanano kati ya matukio ya Agano la Kale na maisha ya Yesu na mafundisho. Hawa walimuona Yesu kama utimilifu wa kinabii wa kitabu chote cha Agano la Kale. Waamini wa sasa yawapasa kujiadhari na mtazamo huu! Wale waandishi wa Agano Jipya waliovuviwa walikuwa chini ya kiwango na walikuwa na ukaribu binafsi na maisha na mafundisho ya Yesu. Tunaikiri ile kweli na mamlaka ya ushahidi wao lakini hatuwezi kuifuatisha njia yao.

## MADA MAALUM: UAINISHI

Philo na kanisa la kwanza katika matumizi yake ya isitiari na matumizi ya Paulo ya mbinu hiyo zinatofautiana kiumuhimu. Ya kwanza ilipuuza kabisa mazingira ya kiistoria, kukuza mafundisho ambayo kwa sehemu kubwa yote yalikuwa ya kigeni kwa kusudio la mwandishi wa awali (yaani kuendana na mawazo ya Plato). Mbinu ya

Paulo ina tabia za kama "uanishi." Paulo alichuliamazngira ya kihistoria ya Mwanzo na umoja wa Kale na Maagano Mapya, hivyo alipata uwezo wa kujenga mfanano kati yao kwasababu walikuwa na mwandishi mmoja—Mungu. Katika Mukhtadha huu hasa (yaani, Wagalatia 3-4), Paulo analinganisha agano la Ibrahimu na agano la Musa na kuweka utendaji kazi wake katika Agano Jipya ya Yeremia 31:31-34 na Agano Jipya Muunganiko wa aina nne katika Wagalatia 4:21-31 unaweza kuchorwa

1. Mama wawili wanasimama kwa niaba ya familia mbili; moja kwa namna ya asili, na nyingine kwa ahadi ya kiungu
2. Kulikuwa na mvutano kati ya wamama hawa wawili na watoto wao kama kulivyokuwa na mvutano kati ya jumbe za wayahudi na injili ya Paulo
3. makundi yote mawili yalidai kuwa wazao wa Ibrahimu , lakini moja lilikuwa katika kifungo kwa sheria ya Musa na lingine huru katika kazi ya Kristo iliyomalizika
4. Milima miwili ilikuwa imeunganishwa na maagano haya tofauti tofauti, Mlima Sinai pamoja na Musa na Mlima Sayuni na pamoja na Ibrahimu. Mlima Sayuni, au Mlima Moria, ndipo Ibrahimu alipomtoa Isaka (kama vile Mwanzo 22), ambayo baadaye ilikuja kuwa Yerusalemu. Ibrahimu alikuwa akiutazamia mji wa mbinguni (Ebr. 11:10; 12:22; 13:14, Yerusalemu mpya, Isaya 40-66) sio yerusalemu ya duniani.

Paulo yawezekana aalitumia uanishi huu kwasababu

1. Walimu wa uongo walikuwa wametumia mbinu hii hii kwa ajili ya faida yao wenyewe, wakidai kuwa mbegu ya kweli ya Ibrahimu.
2. Walimu wa Uongo wangukuwa wametumia mbinu kutoka katika maandiko ya Musa kuendesha thiolojia yao ya maagano ya kiyahudi hivyo Paulo alitumia baba wa iman ya Kiyahudi, Ibrahimu.
3. Paulo yawezekana alitumia kwasababu ya Mwanzo. 21:9-10, ambayo inanukuu mstari wa 30 and saysna kusema, "endesha" mwana wa asili; katika maandiko ya Paulo, hili lilimaanisha wana dini la Kiyahudi.
4. Paulo yawezekana aliutumia kwasababu ya kutaka kuwaacha nje baadhi ya walimu wa iongo wa kiyahudi, hasa katika hali yao ya kutoridhika kwa mafia: katika uainishi wa Paulo Mataifa yanakubaliwa na wale wanaojiona ufahari na ujasiri kwa rangi zao wanakataliwa na Mungu (kama vile Mt. 8:11-12)
5. Paulo inawezekana alitumia aina hii ya uanishi kwasababu amekuwa akisisitiza katika "uana" na "urithi" katika Wagalatia 3 & 4. Huu ulikuwa ni moyo wa hoja zake: kuchukuliwa kwetu na kukaribishwa katika familia ya Mungu kwa imani kupitia Kristo pekee, sio kwa asili

▣ **"Yuda"** Ulikuwa uasi wa Yuda, si kifo chake, ambacho kilisababisha uchaguzi huu wa Mtume aliye ishika nafasi yake. Katika Matendo ya Mitume 1:20b, matendo ya Yuda yalionekana kama utimilifu wa unabii. Kitabu cha Agano Jipya hakikunukuu uchaguzi mwingine wa kiutumie baada ya kifo cha Yakobo (kama vile Matendo ya Mitume 12:2). Kuna siri na huzuni nyingi ndani ya maisha ya Yuda. Bila shaka huyu alikuwa Mtume pekee ambaye hakuwa Mgalilaya. Huyu alifanywa mhazini wa kundi la kimitume (kama vile Yohana 12:6). Huyu alishutumwa kuiba fedha zao kwa kipindi chote cha Yesu kuwa nao. Huyu anasemekana kuwa utimilifu wa kinabii na chombo cha shambulizi la Kishetani. Shauku yake haielezwi kamwe, bali huzuni yake ilileta matokeo katika kuutoa uhai wake baada ya kuiurudisha ile hongo.

Kuna makisio mengi yanayomhusu Yuda na makusudi yake. Huyu anatajwa na kukashifiwa mara nyingi katika Injili ya Yohana (Yohana 6:71; 12:4; 13:2,26,39; 18:2,3,5). Neno la sasa la utani "Yesu Kristo ni Mashuhuri" linamweleza kama mwaminifu, lakini mtu aliyeishiwa imani, mfuasi aliyejaribu kumlazimisha Yesu katika kutimiza dhima ya Masihi wa Kiyahudi —hiii ni, kuwapindua Warumi, kuwaadhibu wale walio dhalimu, na kuitangaza Yerusalemu kama makazi ya ulimwengu. Hata hivyo, Yohana anazifanua shauku zake kama za kiuchoyo na za hila. Tatizo kuu ni suala la kitheolojia la ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu. Je! Mungu au Yesu ndiye aliyemtawala Yuda? Je! Yuda anawajibika kwa ajili ya matendo yake ikiwa Shetani alimtawala au Mungu alimtabiri na kumsababisha yeye kumsaliti Yesu? Biblia haielezi juu ya maswali haya moja kwa moja. Mungu yu ndani ya

utawala wa historia; Yeye ayajua matukio yajayo, lakini mwanadamu anawajibika kwa ajili ya uchaguzi na matendo. Mungu ni wa haki, si mwenye hila.

Kuna kitabu kipya ambacho kinajaribu kumtetea Yuda—*Judas Betrayer or Friend of Jesus?* na William Klassen, Fortress Press, 1996. Mimi sikubaliani na kitabu hiki, bali kinatia shauku sana na kinachokonoa fikra.

▣ **"aliyefanyika kiongozi wa wao waliomkamata Yesu"** Hapa ni nukuu inayotokana na maoni yangu juu ya Mathayo 26:47-50 (angalia [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org)). "Kumekuwa na mjadala mwingi kuhusiana na nia ya Yuda. Haswa kusemekana kwamba hili linabaki bila uhakika/kujulikana. Lile busu lake kwa Yesu katika Matendo ya Mitume 1:49 kwa vyovyote (1) ilikuwa ishara kwa askari kwamba huyu alikuwa mtu wa kukamatwa (kama vile Mt. 26:48); au (2) inatoa msaada kwa nadharia ya sasa kwamba huyu alikuwa akijaribu kuuulazimisha mkono wa Yesu kutenda kazi, (kama vile Mt. 27:4). Vifungu vingine vya Injili vinaeleza kwamba huyu alikuwa mnyang'anyi na asiyeamini kuanzia mwanzo (kama vile Yohana 12:6). Kutokana na Luka 22:52 tunayafahamu makusudi ya umati huu. Kulikuwa na askari wa Kirumi waliohusishwa kwa sababu ya hawa ndio watu pekee ambao wangebeba mapanga kisheria. Pia majemedari wa Hekalu waliohusishwa kwa sababu mara nyingi walikuwa wakibeba marungu. Wawakilishi kutoka kwa Wakuu wa Sinagogi pia walikuwepo katika kukamatwa (kama vile Mt. 26:47, 51)."

**1:17** Yuda alichaguliwa na Yesu, alimsikia Yesu akinena, aliiona miujiza ya Yesu, alitumwa kwa ajili ya kazi maalum na kwa ajili ya Yesu, alikuwepo huko ghorofani na alishiriki katika matukio haya na, bado, alimsaliti Yesu!

**1:18**

**NASB, NKJV**

**NRSV, NJB**

**NIV** "akaanguka kwa kasi akapasuka matumbo yake yote yakatoka"

**TEV** "akaanguka chini, akapasuka na matumbo yake yakamwagika nje"

Inawezekana kwamba "kuanguka chini" lilikuwa neno la kitabibu la neno "kuvimba" (kama vile Moulton na Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament*, kur. 535-536), ambalo linapatikana katika baadhi ya tafsiri za Kiingereza (yaani, Phillips, Moffatt na Goodspeed). Kwa mjadala nzuri wa matoleo mbalimbali ya kifo cha Yuda (Mt. 27:5 dhidi ya Matendo ya Mitume 1:18) angalia *Hard Sayings of the Bible*, Kur. 511-512.

▣ **"mtu huyu alinunua konde"** Mistari ya 18-19 ni ya kimabano (kama vile NASB, NKJV, NRSV, NJB, NIV). Mwandishi aliileta habari hii kwa ajili ya uelewa wa msomaji. Kutokana na Mt. 27:6-8 twajifunza kwamba makuhani walinunua konde kakika utimilifu wa unabii wa Agano la Kale (kama vile Mt. 27:9). Hii ilikuwa fedha ya Yuda, ambayo makuhani walifikiri kwa haikuwa safi na ilitumika kununua konde kwa ajili ya kuzika wageni. Mistari 18-19 inatwambia kuwa hili lilikuwa shamba hili hili ambapo Yuda alifika. Taarifa hii ya kifo cha Yuda haijarudiwa sehemu nyingine yoyote.

**1:19 "kwa lugha yao"** Wayahudi wengi wa siku za Yesu hawakusoma wala kuzungunza lugha ya Kiebrania, bali lugha ya Maana ile ile, Kiaramu, ambayo walijifunza miaka hadi miaka chini ya utawala wa Kiajemi. Watu waliosoma wangeweza kuzungumza na kusoma lugha ya Kiebrania. Yesu alitumia sana lugha hii wakati aliposoma Maandiko ndani ya Masinagogi. Watu wengi katika Palestina wangukuwa wanazungumza lugha mbili (lugha ya Koine ya Kiyunani na Kiaramu) au lugha tatu (lugha ya Koine ya Kiyunani, Kiaramu, na Kiebrania).

Yesu alizungumza Kiaramu muda mwingi. Vifungu na maneno katika Injili vinavyonukuliwa vyote ni vya Kiaramu.

**NASB, NRSV** "Akeldama, maana yake, konde la damu"

**NKJV** "Akel dama, ambalo ni, Konde la Damu"

**TEV** "Akeldama, ambalo linamaanisha Konde la Damu"

**NJB** "Hekali yenye Damu. . .Hakel-dama"



Hii ni tafsiri ya Kiyunani ya neno la Kiaramu. Mara nyingi ni vigumu kuibadili kwa ufanano kutoka lugha moja kwenda nyingine. Pamoja na utofauti wa herufi za Kiyunani, lugha ya Kiaramu inamaanisha "konde la damu." Hili linaweza kumaanisha

1. konde lililonunuliwa kwa fedha ya damu (kama vile Mt. 27:7a)
2. konde ambapo damu ilimwagika (kama vile Mdo. 1:18)
3. konde ambapo wauaji wa kigeni walizikwa (kama vile Mt. 27:7b)

**1:20** Hizi ni nukuu mbili zinazotoka katika Zaburi. Zaburi ya kwanza 69:25. Kihalisia huu ulikuwa wingi. Hii inafanya kazi kama kanuni ya laana inayohusiana na Yuda. Nukuu ya pili inatoka katika Zab. 109:8 (Maandiko ya Kale ya Kiyunani. Hii inatoa mwongozo wa kinabii wa mbadala wa Yuda uliojadiliwa katika Mdo. 1:21-26.

Waamini wa sasa hawawezi kuinakili hii njia ya uainishi wa ufasiri wa ki-Biblia kwa sababu kati yetu hakuna waliovuviwa katika kipindi hiki cha historia. Roho aliwaongoza hawa waandishi wa Biblia /waandishi weledi katika kiwango ambacho hakukifanya kwa waamini wa baadaye. Tunaangazwa Naye lakini kwa wakati mwingine hatukubali (angalia [MADA MAALUM: UVUVIO](#) katika Mdo. 1:16).

**NASB, NKJV,**

**NJB**

"ofisi"

**NRSV**

"eneo la askofu"

**TEV**

"mahari pa huduma"

Katika Machapisho ya Kale ya Kiyunani neno *episkopē* linabeba maana nyingine ya gharama za huduma ya afisa (kama vile Num. 4:16; Zab. 109:8). Hili lilikuja kumaanisha ofisi katika mfumo wa kikarani wa Kanisa Katoliki la Kirumi, lakini katika Kiyunani hili lilikuwa neno la dora ya mji fulani wa kiongozi (kama vile NIV), kama "mzee" (*presbuteros*) lilikuwa neno la Kiyahudi la kiongozi (mfano Mwa. 50:7; Kut. 3:16,18; Hes. 11:16,24,25,39; Kumb. 21:2,3,4,6,19,20 na mengine). Hivyo kwa uwezekano wa upekee wa Yakobo, "askofu" na "mzee" baada ya kifo

**1:21"ni muhimu"** Hili ni neno *dei* (tazama maelezo kamili katika Mdo. 1:16). Kwa uwazi kabisa Petro alihisi kuwa Mitume kumi na wawili kwa kiasi fulani waliwakilisha makabila ama baadhi ya ishara ambazo hazipaswi kutoweka.

**1:21-22** Hizi ni sifa za Utume (angalia Mada Maalum: Kutumwa [*apostellō*] katika Mdo. 14:4). Tambua kwamba hi inaonyesha uwepo wa waamini wengine zaidi ya wale Kumi na Wawili waliomfuata Yesu kipindi chote cha huduma Yake ya hapa duniani. Hizo sifa baadaye zilitumiwa na baadhi kuukataa Utume wa Paulo.

Luka kwa uwazi kabisa aniweka mistari hii miwili kuonyesha umuhimu wa ushahidi wa Mitume, si uchaguzi wa Mathiya, kuhusu nani tunayemsikiliza na si mwingine. Kanisa na Maandiko ya Kitabu cha Agano Jipya litajengwa juu ya maisha na mafundisho ya Yesu, lakini inasuruhishwa kupitia ushahidi wa macho, ushahidi wa kimamlaka, ushahidi wa kithiolojia uliochaguliwa, Kitabu cha Agano Jipya. Hili ni suala la kithiolojia, si ishara ya wale "kumi na wawili"!

### **MADA MAALUMU: NAMBA KUMI NA MBILI**

Kumi na mbili mara nyingi imekuwa kiishara (angalia [Mada Maalumu: Namba za Kiishara katika Andiko](#) namba ya shirika

A. Nje ya biblia

1. Ishara kumi na mbili za ukanda
2. Miezi kumi na miwili ya mwaka

B. Katika Agano la Kale (BDB 1040 kuongeza 797)

1. wana wa Yakobo (Makabila ya Kiyunani)
2. waliotazamishwa kwenye
  - a. Nguzo kumi na mbili za madhabahu katika Kut. 24:
  - b. Vito kumi na viwili juu ya kifua cha kuhani mkuu (ambayo vinasimama kwa niaba ya makabila) katika Kut. 28:21
  - c. unga mwembamba wa mkate kimi na miwili katika sehemu takatifu ya kibanda katika Law. 24:5
  - d. wapelelezi kumi na wawili waliotumwa huko Kanaani katika idadi ya kabila (mmoja kutoka katika kila kabila)
  - e. fimbo kumi na mbili (viwango vya kikabila) katika uhasi wa Kora katika Hes. 17:2
  - f. mawe kumi na mawili ya Yoshua katika Yos. 4:3,9,20
  - g. majimbo kumi na mawili ya kiutawala katika utawala wa Suleimani katika 1 Fal. 4:7
  - h. mawe kumi na mawili ya madhabahu ya YHWH katika 1 Fal. 18:31

C. Katika Agano Jipya

1. Mitume kumi na wawili waliochagulwa
2. Vikapu kumi na viwili vya mikate (kimoja kwa kila Mtume) katika Mt. 14:20
3. Viti kumi na viwili vya enzi ambapo Wanafunzi wa Agano Jipya wamekaa (vinayorejea juu ya makabila 12 ya Israeli) katika Mt. 19:28
4. Majeshi kumi na mmawili ya malaika wa kumsaidia Yesu katika Mt. 26:53
5. Ishara ya Ufunuo
  - a. Wazee 24 juu ya viti 24 4:4
  - b. 144,000 (12x12,000) katika 7:4; 14:1,3
  - c. nyota kumi na mbili juu ya taji la mwanamke katika 12:1
  - d. malango kumi na mawili, malaika kumi na wawili wakiakisi makabila kumi na mawili katika 21:12
  - e. Mawe kumi na mawili ya misingi ya Yerusalemu mpya na juu yao majina ya mitume kumi na mawili katika 21:14
  - f. Mianzi kumi na mbili elfu katika 21:16 (kipimo cha mji mpya, Yerusalemu Mpya)
  - g. kuta ni dhira 144 katika 21:17
  - h. malango kumi na mawili ya lulu katika 21:21

miti mipya katika Yerusalemu yenye aina aina kumi na bili za tunda (moja kwa kila mwezi) katika 22:2

**1:23 "Wakaweka wawili"** Kuna utofauti wa Machapisho ya Kiyunani ambao unaonyesha suala la kithiolojia katika kifungu hiki:

1. *estēsan* ("wakaweka") katika MSS , $\mathcal{N}$ , A, B, C, D<sup>1</sup>, E
2. *estesēn* ("akaweka") katika MS D\* (karne ya tano), Orodha ya vitabu katika Biblia au visehemu vilivyotengwa kusomwa katika ibada ya kimungu 156 (karne ya kumi ), machapisho mawili ya kale ya Kilatini (karne ya tano na karne ya kumi na tatu), na Augustine (b.k. 354-430)

Ikiwa namba moja, huu ni mfano wa kundi zima la wanafunzi waliopiga kura juu ya uwezekano wa kuondolewa kwa Yuda (mfumo wa dora ya kusanyiko (kama vile Matendo ya Mitume 15:22), lakini namba 2, kisha huu ni ushahidi wa uwezo wa Petro (kama vile Matendo ya Mitume 15:7-11,14). Kama ulivyo ushahidi wa machapisho ya Kiyunani, maneno ya namba moja ni yumkini (toleo la UBS<sup>4</sup> lilipata daraja "A").

▣"Yusufu. . Mathiya" Hatufahamu chochote kuhusu watu hawa kutoka kitabu cha Agano Jipya. Yatupasa kukumbuka kuwa Injili na kitabu cha Matendo ya Mitume si historia za magharibi, bali ni maandishi ya kithiolojia kwa ajili ya kumtambulisha Yesu na kuonyesha namna ujumbe Wake ulivyoleta matokeo katika ulimwengu.

**1:24**

**NASB** "ujuaye mioyo ya watu wote"

**NKJV** "ajuaye mioyo ya wote"

**NRSV** "ujuaye moyo wa kila mtu"  
**TEV** "ujuaye mawazo ya kila mtu"  
**NJB** "uwezaye kuusoma moyo wa kila mtu"

Hili ni neno ambatani, "mioyo" na "kujulikana" (kama vile Mdo. 15:8). Hili lina aksi ile kweli ya Agano la Kale (kama vile 1 Sam. 2:7; 16:7; 1 Fal. 8:39; 1 Nya. 28:9; 2 Nya. 6:30; Zab. 7:9; 44:21; Mit. 15:11; 21:2; Yer. 11:20; 17:9-10; 20:12; Luka 16:15; Mdo. 1:24; 15:8; Rum. 8:27). Mungu anatufahamu fika na bado anatupenda (kama vile Rum. 8:27). Wanafunzi wanakiri kwamba YHWH anazifahamu nia zao pamoja na maisha ya wale wawili waliochaguliwa. Wanayataka mapenzi ya Mungu katika uchaguzi huu (kauli ya kati ya wakati usio timilifu). Yesu aliwachagua wale Kumi na Wawili, lakini sasa Yeye anamjua Baba

## **MADA MAALUMU: MOYO (AGANO JIPYA)**

Neno la Kiyunani *kardia* limetumika katika maandiko ya kale ya Kiyunani na Agano Jipya kuashiria neno la Kiebrania *lēb* (BDB 523, KB 513). Limetumika kwa njia tofauti kadhaa (kama vile Bauer, Arndt, Gingrich na Danker, *A Greek-English Lexicon*, 2nd Ed. kur. 403-404).

1. Kitovu/Kituo cha maisha ya kimwili, neno mbadala kwa mtu (kama vile. Matendo 14:17; 2 Kor. 3:2-3; Yakobo 5:5)
2. Kitovu cha maisha ya kiroho (yaani, adilifu)
  - a. Mungu anatumia mioyo (kama vile Luka 16:15; Rum. 8:27; 1 Kor. 14:25; 1 The. 2:4; Ufu. 2:23)
  - b. Imetumika kwa maisha ya kiroho ya mwanadamu (kama vile. Mt. 15:18-19; 18:35; Rum. 6:17; 1 Tim. 1:5; 2 Tim. 2:22; 1 Pet. 1:22)
3. Kitovu cha maisha ya kifikra (yaani, uwezo wa kufikiri, kama vile. Mt. 13:15; 24:48; Matendo 7:23; 16:14; 28:27; Rum. 1:21; 10:6; 16:18; 2 Kor. 4:6; Efe. 1:18; 4:18; Yakobo 1:26; 2 Pet. 1:19; Ufu. 18:7; moyo ni sawa na mawazo katika 2 Kor. 3:14-15 na Flp. 4:7)
4. kitovu cha maamuzi binafsi (yaani, matakwa, kama vile. Matendo 5:4; 11:23; 1 Kor. 4:5; 7:37; 2 Kor. 9:7)
5. Kitovu cha hisia za ndani (kama vile. Mt. 5:28; Matendo 2:26, 37; 7:54; 21:13; Rum. 1:24; 2 Kor. 2:4; 7:3; Efe. 6:22; Flp. 1:7)
6. Mahali pa pekee kwa shughuli za kiroho (kama vile. Rum. 5:5; 2 Kor. 1:22; Gal. 4:6 [yaani, Kristo katika mioyo yetu, Efe. 3:17])
7. Moyo ni njia mbadala ya ki-sitiari ya kumrejerea mtu (kama vile. Mt. 22:37, kwa kunukuu Kumb. 6:5). Mawazo, sababu, na matendo vikichangia kikamilifu kwenye moyo kubainisha kikamilifu mtu alivyo. Agano la Kale lina baadhi ya matumizi ya maneno ya kushangaza.
  - a. Mwa. 6:6; 8:21, "Mungu alihuzunishwa katika moyo," pia tazama Hosea 11:8-9
  - b. Kumb. 4:29; 6:5; 10:12, "kwa moyo wako wote na nafsi yako yote"
  - c. Kumb. 10:16; Yer. 9:26, "Roho zisizo na tohara" na Rum. 2:29
  - d. Ezek. 18:31-32, "moyo mpya"
  - e. Ezek. 36:26, "moyo mpya" dhidi ya "moyo wa jiwe" (kama vile Ezek. 11:19; Zak. 7:12)

**1:25 "mahali pake mwenyewe"** Hii ni tafsida ya "ulaanifu." Shetani alimtumia kwa makusudi yake (kama vile Luka 22:3; Yohana 13:2; 27), lakini Yuda anawajibika kwa uchaguzi na matendo yake (kama vile Gal. 6:7).

**1:26 "Wakawapigia kura"** Hili lina usuli wa kitabu cha Agano la Kale uliohusiana na matumizi ya Makuhani Wakuu kuvaa Urimand Thummim (vitu vilivyovalwa katika kifua cha makuhani visivyojulikana asili yake vilivyotumika kwa ajili ya ibada ya kiungu) (katika Mambo ya Walawi. 16:8, au watu kutumia baadhi ya aina njia inayofanana (kama vile Mit. 16:33; 18:18). Askari wa Kirumi pia waliyapiagia kura mavazi ya Yesu (kama vile Luka 23:34). Hata hivyo, huu ni wakati wa mwisho hii ni njia ya mwisho ya kuyaju a maopenzi ya Mungu yaliyotajwa katika kitabu cha Agano Jipya. Ikiwa mtu anaelekea kuyachunguza maandiko, njia hii ingeweza kuwa sanifu kwa namna ya kufanya uamuzi wa kiroho, ambao ungeweza kuwa wa bahati mbaya (mfano kuifunua Biblia na kukiweka kidole cha mtu

juu ya mstari kwa ajili ya kuyatafuta mapenzi ya Mungu). Waamini wanapaswa kuishi kwa imani, si kwa kwa ufanisi wa kuyatafuta mapenzi ya Mungu (mfano ngozi ya kondoo, kama vile Waamuzi 6:17,36-40).

▣ **"Mathiya"**Eusebius anasema huyu alihusishwa katika wajumbe wale sabini (kama vile Luka 10). Baadaye desturi zilidai kuwa huyu alikuwa shahidi aliyeifia dini huko Ethiopia.

### **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa mfasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. kwa nini Yesu aliendelea kukaa na wanafunzi wake kwa siku 40?
2. nii maana ya "ubatizo wa roho?"
3. kwa nini mstari wa 7 ni wa muhimu sana?
4. kwa nini kupaa ni muhimu?
5. kwa nini Petro alihisi kuijaza nafasi ya yuda?
6. ni kwa namna gani paulo alikuwa mtume wakati hakukamilisha zile sifa? (1:21-22)

## MATENDO YA MITUME 2

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>USB<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Ujio wa Roho Mt	Ujio wa Roho Mt	Siku ya Pentekoste	Ujio wa Roho Mt	Pentekoste
2:1-4	2:1-4	2:1-4	2:1-4	2:1-4
	Mawingu yanaitikia			
2:5-13	2:5-13	2:5-13	2:5-13	2:5-13
Kauli ya Petro siku Ya Pentekoste	Hotuba ya Petro	Hotuba ya Petro	Hotuba ya Petro	Petro ahutubia umati
2:14-21	2:14-39	2:14-21	2:14-21	2:14-21
2:22-28		2:22-28	2:22-28	2:22-28
2:29-36		2:29-36	2:29-35 2:36	2:29-35 2:36
		Wito wa toba		Kuongoka kwa mara ya kwanza
2:37-42		2:37-42	2:37	2:37-41
	Hitaji la makuzi ya Kanisa		2:38-39	
	2:40-47		2:40-42	Badiliko la awali La Mkristo
Maisha kati ya Wakristo			Maisha kati ya Wakristo	2:42
2:43-47		2:43-47	2:43-47	2:43 2:44-45 2:46-47

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" \("A Guide to Good Bible Reading"\)](#))

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii Mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Hii ni hotuba ya kwanza ya zama mpya. Tambua nukuu za Agano la Kale na vidokezo vyake katika Matendo 2. Petro anahubiri kwa Wayahudi toka kwa ulimwengu wote wa shamu. Maandiko anayopenda kuyatumia yanaaksi mafundisho ya Yesu kwa wale watu wawili wakielekea Emmau (kama vile Lk. 24:21-32) na pale alipowatokea wanafunzi wake baada ya kufufuka (kama vile Lk 24:45).
1. Mdo.2:1 6-21 – Yoeli 2:28-32
  2. Mdo. 2:25-28 – Zaburi 1 6:8-1 1
  3. Mdo. 2:30 – kidokezo kwa 2 Sam. 7:11 -16 na Zab.. 89:34 au 1 32:1 1
  4. Mdo.2:34-35 – Zaburi 1 1 0:1
- B. Utimilifu wa unabii ya Yoel kuhusu matukio ya siku ya mwisho unadhihilisha wazi kuwa hukumu ya Mungu ambayo ilimwondoa Roho wake toka Israeli baada ya Malaki (au mwandishi wa Mambo ya Nyakati) imefikia tamati! Roho amekwisha rudi katika agizo kuu la nguvu na lililokusudiwa
- C. Mkanganyiko wa lugha toka kwenye mnara wa Babeli (kama vile Mwanzo 11) sasa umegeuzwa (kwa wastani kiishara). Zama mpya imeanza.
- D. Kwa sasa “ndimi” wa kwenye kitabu cha Matendo ni wa tofauti na ile wa kwenye Korintho. Hakuna uhitaji wa mfasiri. Ujumbe hakika ni wa kiinjalisti.
- Ndimi katika matendo ni kwa Wayahudi wanaoamini kutambua kuwa Mungu tayari amekwisha kukubali kikundi cha jamii ya watu kuingia katika ufalme (yaani wasamalia wema, Warumi, n.k).
- Ndimi za ki-Korintho zinafaa aina ya tamaduni ya unabii wa Delphi. Walimweleza Mungu kama sio mwanadamu (kama vile 1 Kor. 14:2). Walimjenga msemaji (kama vile 1 Kor. 14:4). Tafadhali usichukue huu uchunguzi kama ulio kinyume kwa namna yeyote ile kwa namna ya watu wa Korintho (kama vile 1 Kor. 14:5,18). Ninaamini bado ni uendeleu wa karama za rohoni. Hata hivyo, kwa sababu ya swali la 1 Kor. 12:28-29, linalotarajia jibu la “hapana,” si la kila mwamini! Angalia maelezo kamili juu ya somo katika 1 Wakorintho 12 na 14 katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 2:1-4

<sup>1</sup> Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. <sup>2</sup> Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. <sup>3</sup> Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. <sup>4</sup> Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.

**2:1 "Pentekoste"** Hii sikukuu ya mwaka ya Kiyahudi pia ilijulikana kama “sikukuu ya majuma” (kama vile Kut. 34:22; Kumb. 1 6:1 0). Neno “Pentekoste” linamaanisha “hamsini.” Sikukuu hii iliandaliwa kwa siku hamsini (majuma saba) baada ya sikukuu ya Pasaka (yaani ikihesabiwa toka siku ya pili ya sikukuu ya mikate isiotiwa chachu). Ilikuwa na makusudi matatu katika siku za Yesu:

1. Kuadhimisha kumbukumbu ya upewaji wa sheria za Musa (kama vile *Jubilees* 1 :1 )
2. Shukurani kwa Mungu kwa ajili ya mavuno

3. Matoleo ya matunda ya kwanza (yaani, alama ya YHWH ya umiliki wa mavuno yote) ya mavuno ya nafaka. Mazingira ya nyuma ya Agano la Kale katika Kut. 23:1 6-1 7; 34:22; Law. 23:1 5-21 ; Hes. 28:26-31 na Kumb.1 6:9-1 2.

NASB, NRSV	"hata ilipotimia"
NKJV	"imekwisha kutimia"
TEV	"ilipotimia"
NJB	"imekusha kuwa karibu"

Hii kifasihi "imekwisha kutimia." Ni kauli tendwa isio na kikomo ya wakati uliopo. Hii ilikuwa ni ahadi ya ki-Ungu na utimilifu wa kusudi la ki-Ungu. Kinatumika kwa maandishi ya Luka tu (kama vile Luka 8:23; 9:51; hapa; na sitiri mfanano katika Luka 2:6). Historia ya mwanadamu inawekewa kumbukumbu na YHWH. M. R. Vincent, *Word Studies*, juzuu. 1, uk. 224, inakumbusha sisi kuwa Wayahudi waliangalia siku hii kama chombo cha kujazwa. Kipindi cha Pentecoste kimekwisha kuja tayari! Pia ilikuwa ni muda muhimu wa Mungu kuzindua rasmi enzi ya Roho, mwanzo wa kanisa.

☐ **"walikuwako wote mahali pamoja"** Kifungu hiki kinamaanisha umoja wa sehemu zote na fikra (kama vile Mdo. 1:1 4). haijulikani hili lilitokea wapi. Yumkini ilikuwa kwenye "chumba cha juu" (kama vile Mdo. 1 :1 3; "nyumba," Mdo. 2:2), lakini kwa hoja nyingine hekalu linaingizwa kwenye uzoefu huu (kama vile Luka 24:53; wingi wa kundi katika Mdo. 2:47).

**2:2 "kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo"** Katika kipengere hiki kizima msisitizo upo juu ya uvumi, na sio upepo au moto. Hii inafanana na Mwa. 3:8. Katika Agano la Kale neno *ruah* (BDB 924) linatumika kwa ajili ya pumzi, upepo, na Roho (kama vile Ezek. 37:9-1 4); katika Agano Jipya *pneuma* linatumika kama upepo na Roho Mtakatifu (kama vile Yn. 3:5-8). Neno upepo katika mstari huu ni *pnoē*. Linatumika hapa tu na katika Mdo. 17:25. Neno *pneuma* linatumika kwa ajili ya Roho Mdo.2:4.

## MADA MAALUM: ROHO (PNEUMA) KATIKA AGANO JIPYA

Neno la Kiyunani "roho" limetumika katika njia mbali mbali kwenye Agano Jipya. Hapa kuna baadhi ya maelezo yenye upambanuzi na mifano.

- A. Mungu wa Utatu (angalia [Mada Maalumu: Utatu](#))
  1. wa Baba (kama vile Yohana 4:24)
  2. wa Mwana (kama vile Rum. 8:9-10; 2 Kor. 3:17; Gal. 4:6; 1 Pet. 1:11)
  3. wa Roho Mtakatifu (kama vile Marko 1:11; Mat. 3:16; 10:20; Yohana 3:5,6,8; 7:39; 14:17; Matendo 2:4; 5:9; 8:29,35; Rum. 1:4; 8:11,16; 1 Kor. 2:4,10,11,13,14; 12:7)
- B. wa nguvu ya maisha ya mwanadamu
  1. wa Yesu (kama vile Marko 8:12; Yohana 11:33,38; 13:21)
  2. wa mwanadamu (kama vile Mt. 22:43; Mdo. 7:59; 17:16; 20:22; Rum. 1:9; 8:16; 1 Kor. 2:11; 5:3-5; 7:34; 15:45; 16:18; 2 Kor. 2:13; 7:13; Flp 4:23; Kol. 2:5)
  3. mambo ambayo Roho huzalisha ndani na kupitia roho za wanadamu
    - a. isio roho ya utumwa dhidi roho ya kuasili - Rum. 8:15
    - b. roho ya unyenyekevu – 1 Kor. 4:21
    - a. roho ya imani – 2 Kor. 4:13
    - b. roho ya hekima na ufunuo katika maarifa Yake – Efe. 1:17
    - c. isio roho ya woga dhidi ya nguvu, pendo, na heshima – 2 Tim. 1:7
    - d. roho ya ukungeufu dhidi ya roho ya ukweli – 1 Yohana 4:6
- C. wa ulimwengu wa kiroho
  1. viumbe vya kiroho

- a. walio wazuri (yaani, malaika, kama vile Mdo. 23:8-9; Ebr. 1:14)
  - b. walio waovu (yaani, pepo wabaya, kama vile. Mat. 8:16; 10:1; 12:43,45; Matendo 5:16; 8:7; 16:16; 19:12-21; Efe. 6:12)
  - c. pepo (kama vile Luka 24:37)
  2. roho ya utambuzi (kama vile Mt. 5:3; 26:41; Yohana 3:6; 4:23; Mdo. 18:25; 19:21; Rum. 2:29; 7:6; 8:4,10; 12:11; 1 Kor. 14:37)
  3. mambo ya kiroho (kama vile Yohana 6:63; Rum. 2:29; 8:2,5,9,15; 15:27; 1 Kor. 9:11; 14:12)
  4. karama za kiroho (kama vile 1 Kor. 12:1; 14:1)
  5. uvuvio wa Roho (kama vile Mt. 22:43; Luka 2:27; Efe. 1:17)
  6. Viungo ya kiroho (kama vile 1 Kor. 15:44-45)
- D. uainishaji
1. mtazamo wa ulimwengu (kama vile Rum. 8:15; 11:8; 1 Kor. 2:12)
  2. mchakato wanadamu wa kufikiri (kama vile Mdo. 6:10; Rum. 8:6; 1 Kor. 4:2)

E. wa ulimwengu wa kimwili

1. wingu (kama vie. Mat. 7:25,27; Yohana 3:8; Matendo 2:2)
2. pumzi (kama vile Matendo 17:25; 2 The. 2:8)

Ni dhahiri kwamba neno hili linapaswa kufasiriwa katika upande wa mazingira ya sasa. Kuna maana mbalimbali ya vivuli ambavyo vinaweza kurejerewa (1) ulimwengu wa kiroho; (2) ulimwengu usioonekana; (3) pamoja na watu wa ulimwengu huu wa kiroho au ulimwengu dhahiri.

Roho Mtakatifu ni sehemu ile ya Utatu ambaye ni mtendaji mkuu katika hatua hii ya historia. Enzi mpya za Roho zimekuja. Vyote vilivyo vizuri, vitakatifu, vya haki, na vinavyohusiana Naye kweli kweli. Uwepo Wake, karama, na huduma ni muhimu katika ukuzaji wa injili na mafanikio ya Ufalme wa Mungu (kama vile Yohana 14 na 16). Havutii upande wake Mwenyewe, bali kwa Kristo (kama vile Yohana 16:13-14). Anasadikisha, hushawishi, hubatiza, anabatiza, na anawakomaza waamini wote (kama vile Yohana 16:8-11).

**2:3 "kukatokea ndimi za moto zilizogawanyikana"** Andiko linatokea kuelezea tukio la uvumi na mwanga. Ndimi kama ndimi za moto kwa mara ya kwanza ziliunganikana, lakini zikagawanyika katika udhihilisho tofauti na kutua kwa kila mwamini. Kila mmoja aliyekuweko katika chumba cha juu-Mitume, washirika toka familia ya Yesu, na wanafunzi –walishuhudia uthibitisho wa kujumuishwa kwao. Kanisa lilikuwa moja! Sikukuu ya Pentecoste ilikuwa huko Uyahudi kama sherehe ya Musa kupewa sheria kwenye Mlima Sinai (ni lini hii mila ilikua haijulikani, bila shaka ilikuwa katika karne ya pili B.K., lakini huenda mapema zaidi). Kwa hiyo, sauti kubwa ya ngurumo na umeme yawezekana kuwa ukumbusho wa kumheshimisha YHWH alipotemka juu ya Mlima (kama vile Kut. 19:16). Katika Agano la Kale moto ulimaanisha (1) uwepo wa Uungu ;(2) hukumu (kama vile Isa. 66:15-18); au (3) kutakaswa (kama vile Kut. 3:2; Kumb. 5:4 na Mt. 3:11). Luka anatomia mfanano kujaribu kuelezea utokeaji wa kipekee wa Roho kujidhihilisha wazi. Angalia Mada Maalum inafuata.

## MADA MAALUM: MOTO

Moto unavyo vidokezo chanya na hasi katika maandiko.

- A. Chanya
1. Husisimua (kama vile Isay 44:15; Yohana 18:18)
  2. Huwasha nuru (kama vile Isaya 50:11; Mt 25:1-13)
  3. Hupikia (kama vile Kutok 12:8; Isay 44:15:16; Yohana 21:9)
  4. Husafisha (kama vile Hes 31:22-23; Mith 17:3; Isaya 1:25; 6:6-8; Yer 6:29; Malaki 3:2-3)
  5. Utakatifu wa Mungu (kama vile. Mwz 15:17; Kutoka 3:2; 19:18; Ezek 1:27; Waebrania 12:29)
  6. Uongozi wa Mungu (kama vile Kutoka 13:21; Hes 14:14; Wafalme 1. 18:24)
  7. Uwezeshaji wa Mungu (kama vile Matendo 2:3)
  8. Ulinzi wa Mungu (kama vile Zekaria 2:5)



- B. Hasi
  1. Huunguza (kama vile. Yos 6:24; 8:8; 11:11; Mt. 22:7)
  2. Huangamiza (kama vile. Mwz 19:24; Walawi 10:1-2)
  3. Hasira (kama vile. Hes 21:28; Isay 10:16; Zek 123:6)
  4. Adhabu (kama vile. Mwz 38:24; Walawi 20:14; 21:9; Yoshua 7:17)
  5. Ishara ya mbaya ya siku ya mwisho (kama vile. Ufunuo 13:13)
- C. Hasira ya Mungu dhidi ya dhambi mara nyingi hudhihirishwa kwa tanuru ya moto.
  1. Hasira yake huunguza (Kama vile. Hos 8:5; Sefania 3:8)
  2. Humimina moto (kama vile. Nah 1:6)
  3. Moto wa milele (kama vile. Yer 15:14; 17:4; Mt.25:41; Yuda aya ya 7)
  4. Hukumu ya siku ya mwisho (kama vile. Math 3:10; 5:22; 13:40; Yohana 15:5; Thes 2. 1:7; Petro 2. 3:7-10; Ufu 8:7; 16:8; 20:14-15)
- D. Moto mara nyingi huonekana katika tanuru
  1. Mwz 15:17
  2. Kutoka 3:2
  3. Kutoka 19:18
  4. Zaburi 18:7-15; 29:7
  5. Ezek 1:4, 27; 10:2
  6. Ebr 1:7; 12:29
- E. Kama sitiari yingi katika Biblia (yaani chachu, simba) moto unaweza kuwa Baraka au kufuatana na mazingira au muktadha.

☐ **"kila mmoja wao"** Hapakuwepo na utofauti uliojitokeza kati ya mitume na wanafunzi; wanaume au wanawake (kama vile Yoeli 2:28-32; Mdo. 2:1 6-21 ).

**2:4 "wote walijazwa na Roho Mtakatifu"** Tukio hili limetajwa katika Luka 24:49 na kuitwa "ahadi ya Baba." "kujazwa" ni kitendo cha kujirudia (kama vile Mdo. 2:4; 4:8,31 ; 6:3,5; 7:55; 9:1 7; 1 1 :24; 1 3:9). Kinamaanisha maisha ya kila siku ya kufanana na Yesu (kama vile Efe. 5:18 ikilinganishwa na Kol. 3:1 6). Hii ni tofauti na ubatizo wa Roho, ambao unamaanisha uzoefu wa awali wa Mkristo au ushirikishwaji ndani ya Kristo (kama vile 1 Kor. 1 2:1 3; Efe. 4:4-5). Kujazwa ni uwezeshwaji wa kiroho kwa ajili ya huduma madhubuti (kama vile Efe. 5:18-20), hapa uinjilisti! Angalia maelezo katika Mdo. 3:10. Kwa njia nyingi tofauti baadhi ya vipengere vya kilokole vimeonyesha hisia kwa kile kilichoonekana kuwa zaidi katika eneo la uzoefu wa Kiroho na limeweza kushusha thamani ta msisitizo wa Agano Jipya juu ya Roho Mtakatifu. Vitabu viwili vilivyonisadia mimi kulishughulikia jambo hili ni vya Gordon Fee

1. *Gospel and Spirit*
2. *Paul, the Spirit, and the People of God*

Angalia maelezo kamili katika Mdo. 5:17.

**NASB, NKJV** "wakaanza kusema kwa lugha nyingine"  
**NRSV** "wakaanza kuongea kwa lugha nyingine"  
**TEV** "kuzungumza kwa lugha nyingine"  
**NJB** "wakaanza kusema kwa lugha tofauti"

Kiuhalisia ni "kwa lugha nyingine" (*heterais glōssais*). Tafasiri ya "lugha nyingine" inaaksi uwelewa wa neno hili ulioegamia juu ya muktadha wa Mdo. 2:6 na 11. Tafasiri zingine zinazowezezana ni "kunena kwa furaha isiyokuwa na kifani," inayosimamia juu ya 1 Wakorintho 12-14 na yumkini Mdo. 2:13. Haijulikani ni lugha ngapi tofauti ziliongelewa pale, lakini zilikuwa nyingi. Ukijaribu kuongeza mataifa yote na mikoa yote ya Mdo. 2:9-11 lazima ifikie ishirini. Waamini mbali mbali kati ya wale 120 lazima waliongea lugha ya kufanana.

Saa nyingine Mungu ni wa ajabu na mwenye nguvu kuweza kukivuvia hiki kikundi kidogo chenye wanaume na wanawake wenye kujaa hofu walingojea katika chumba cha juu kilichofungwa ili wawe wapiga mbiu wa injili

walioshikamana (wote wanaume na wanawake). Haijarishi hii alama ya mwanzo ya kuja kwa Roho Mtakatifu aliye ahidiwa, Mungu pia alitumia kuthibitisha ukubarifu wake wa makundi mengine (yaani., wasamalia wema, na watu wa mataifa). “ndimi” katika matendo siku zote ilikuwa ni alama kwa waamini kwamba injili imeweza kuikabili mipaka ya kijiografia na ukabila. Kuna utofauti wa kipekee kati ya ndimi za kwenye kitabu cha Matendo na huduma ya Paulo ya baadaye huko Korintho (kama vile 1 Wakorintho 12-14).

Kithiolojia inawezekana kuwa siku ya Pentekoste moja kwa moja ilikuwa kinyume na mnara wa Babeli (kama vile Mwanzo 10-11). Kama watu wenye kuasi, wenye majivuno walivyodai uhuru wao (yaani., katazo la kugawanyika na kuijaza dunia), Mungu akaanzisha mapenzi yake kwa kuingiza lugha nyingi. Sasa, katika zama mpya ya Roho, utaifa ambao unamzorotesha mwanadamu kutokuungana (yaani., kutengeneza serikali moja ya kidunia ya matukio ya siku ya mwisho) upo kwawaamini waliokwisha geuzwa. Ushirika wa Kikristo pande zote za mipaka ya mwanadamu (yaani umri, jinsi, daraja, mazingira, lugha) ni kinyume cha matokeo ya Mwanzo 3.

☐ **"kwa kadri Roho alivyowajalia kutamka"** Kitenzi ni kauli isio timilifu tendaji alekezi, ikimaanisha Roho ameanza kuwapa. Neno “kutamka” (*apophthegomai*) ni kauli tendwa (shahidi) isio na ukomo ya wakati uliopo. Neno hili limetumia tu na Luka katika Matendo (kama vile Mdo. 2:4,14; 26:25).

Inatumika katika tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani kwa ajili ya kuwazungumzia manabii (yaani., kauli zilizovuviwa na Roho, kama vile Kumb.32:2; 1 Nya. 25:1; Ezek. 13:9,19; Mik. 5:11; Zak. 10:2). Napendelea tafasiri hii kwa maana ya asili ya neno la Kiyunani la daraja la juu “kuongeza sauti,” “kuongea kwa msisimko” au “ufasaha wa kusema.” Luka alikwisha tambua tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani na alivutiwa na rahaja zake. Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani yalikuwa ni Biblia ya huko ulimwengu wa Mediterania na yakaja kuwa ni Biblia ya kanisa.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 2:5-13**

<sup>5</sup> Na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu. <sup>6</sup> Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe. <sup>7</sup> Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, Tazama, hawa wote wasemao si Wagalilaya? <sup>8</sup> Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyojaliwa nayo? <sup>9</sup> Warparthi na Wamedi na Waelami, nao wakaao Mesopotamia, Uyahudi na Kapadokia, Ponto na Asia, <sup>10</sup> Frigia na Pamfilia, Misri na pande za Libia karibu na Kirene, na wageni watokao Rumi, Wayahudi na waongofu, <sup>11</sup> Wakrete na Waarabu; tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu. <sup>12</sup> Wakashangaa wote wakaingiwa na shaka, wakiambiana, Maana yake nini mambo haya? <sup>13</sup> Wengine walidhihaki, wakisema, wamelewa kwa mvinyo mpya.

**2:5 "watauwa"** Neno hili linamaanisha “kushikilia kitu fualani kwa umakini” (kama vile tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani [LXX] Law. 1 5:31 ; Mika 7:2). Kwa suala la dini ya Kiyahudi la karne ya kwanza, ilimaanisha heshima iliyotolewa kwa Mungu na desturi za wazee (yaani., simulizi za kimila, ambazo zikaja kuwa sheria na taratibu za Kiyahudi). Hawa walikuwa watu wa dini, waadilifu (kama vile Mdo 8:2; 22:12; Lk 2:25). Hii ina maan sawa na neno “asiye na lawama” lililotumia na Nuhu na Ayubu.

☐ **"kila taifa chini ya mbingu"** Wanaume wote wa Kiyahudi waliamuliwa kwa nguvu kuhudhulia zile siku tatu muhimu za sikukuu ya mwaka (kama vile Walawi) pale hekaluni (kama vile Kumb. 16:16). Walikuwa

1. Huenda mahojaji toka pande zote za Shamu waliokuja Yerusalemu kwa ajili ya sikukuu ya pasaka na kuamua kukaa mpaka siku ya Pentecoste
2. Wakazi wa kudumu waliotoka sehemu zingine nje ya Yerusalemu (kama vile matumizi ya neno katika Mdo. 4:16; 7:24; 9:22,32)

Hili lilikuwa na vidokezi vya kithiolojia (kama vile Mt. 28:19-20; Lk. 24:47; Mdo. 1:8)

**2:6 "basi sauti hii iliposikiwa"** Hili lingaliweza kurejea (1) kelele za upepo uliokuwa ukivuma (kama vile Mdo. 2:2) au (2) waamini waliokuwa wakisema kwa lugha nyingine (kama vile Mdo 2:4)

**NASB, NKJV**

**NRSV** "walitatanishwa"

**TEV** "walichanganyikiwa"

**NJB** "walisisimka"

Neno kama hili limetumika katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani katika Mwa. 11:7,9, yakihusianishwa na mkanganyiko wa lugha katika mnara wa Babel. Nafikiri Pentecoste ni alama iliyo kinyume na utaifa ulioanza pale kwenye mnara wa Babel, moja ni kuiadhibu dhambi ya mwanadamu aliyekataa mapenzi ya Mungu ili isienee na pili kwa ajili ya ulinzi toka serikali moja ya kiulimwengu. *Jerome Biblical Commentary*, juzuu. 2, uk. 1 72, zaidi inaimalisha mtizamo huu kwa utumiaji wa *diamezizō* katika Mdo. 2:3, ambalo ni neno adimu, lakini pia linatumika katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani ya Kumb. 32:8 kwa ajili ya kuwachanganya pale kwenye mnara wa Babel. Waamini hawatengwi teana na utaifa! Angalia maelezo katika Mdo. 9:22

☐ **"makutano walikutanika"** Hii inamaanisha kuwa hili lilitokea katika eneo la hekalu kwa vile ule umati mkubwa usingeweza kutoshereza kwenye kile chumba kidogo cha juu au kwenye mitaa midogo ya Mji wa Yerusalem.

☐ **"kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe"** Huu ungeweza kuwa muujiza wa kusikia, sio kuongea kusiko epukika (kama vile Mdo. 2:8 na 11). Kama watu hawa wengi, wote wanaongea kwa lugha tofauti, wakaongea kwa wakati mmoja kungalikuwa na mkanganyiko. Hii ni thiolojia iliyo na kinyume ya mnara wa Babel (kama vile Mwanzo 11).

Hili ni neno la Kiyunani *dialektos* (kama vile Mdo. 2:8), ambapo tunapata neno la kiingereza "lahaja." Luka analitumia neno hili mara nyingi katika Mdo (kama vile Mdo. 1 :1 9; 2:6,8; 21 :40; 22:2; 26:1 4). Lilitumika kwa maana ya "lugha." Hata hivyo, katika muktadha huu, lahaja yaweza kuwa ni maana iliyokusudiwa. Wayahudi hawa walimsikia Yesu katika lahaja za mama. Hili lilimaanisha kuwa alama ya uthibitisho kwao ya ukweli wa ujumbe mpya kumhusu Mungu na ujumuishaji wa wote!

**2:7,12** Tambua tofauti zote za maneno yenye kuelezea hisia kali katika muktadha huu.

1. *sunechō*, "walitatanishwa" (Mdo. 2:6)
2. *existēmi*, "walistaabishwa" (Mdo. 2:7)
3. *thaumazō*, "walishangazwa" (Mdo. 2:7)
4. *diaporeō*, "waliduwazwa" (Mdo. 2:1 2)

☐ **"tazama, hawa wote wasemao si Wagalilaya"** Haya maswali yenye ustadi (yaliyo tarajia jibu la "ndiyo") yaliulizwa kwa sababu ya matamshi yao ya ki-Kaskazini (yaani lahaja, kama vile Mt. 26:73). Neno "kwa nini" linaaksi neno la Kiyunani *idou* (tazama), lililotumika mara ishirini na tatu katika Matendo ya mitume na Luka.

**2:9 "Waparthi, Wamedi, Waelami, na wale wakao Mesopotamia"** Makundi haya yote yalikuwa toka Uislamu uliokomaa (Mesopotamia), mahali pale Abraham alitwa toka (Uru wa Wakalidayo, kama vile Mwa. 11:28) na toka mahali pale Israel na Yuda walipokimbilia kama mateka (Ashuru na Babel).

☐ **"Yudea"** Kwa nini Yudea inaorodheshwa kati ya nchi mbili zisizohusiana? Kwa nini inaorodheshwa pasipo kibainishi, ambacho kingalikuwa sahihi kisarufi? Ni kwa ninin kingaliwashangaza watu wa Yudea kuwa Wagalilaya wanaongea Kiarama? Kwa sababu ya maswali haya wengi wao wanapaswa kuwa na makosa ya kiuandishi yaliyotokea na neno hili linarejea kwa taifa linguine

1. Tertullian, Augustine – Armenia
2. Jerome – Syria
3. Chrysostom, Erasmus – India
4. Kwa maoni mbali mbali ya kisasa angalia Bruce M. Metzger, *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, uk. 293.

**2:9-10 "Kapadokia, Ponto na Asia, Filigia na Pamfilia"** Haya yalikuwa ni makundi toka Uturuki ya leo.

**2:10 "Misri na pande za Libia karibu na Kirene"** Haya yalikuwa makundi toka Africa Kaskazini.

☐ **"toka Rumi"** Wale mahojaji wa Kiyahudi walioongoka katika tukio hili wanaweza kuwa waanzilishi wa kanisa huko Rumi

☐ **"waongofu"** Hili linarejelea watu wa mataifa walibadilika toka kwa dini ya Kiyahudi waliopaswa

1. Kuitunza sheria ya Musa
2. Kuwa wanaume wafanye tohara
3. Kubatizwa wao wenyewe kabla ya kushuhudia
4. Ikiwezekana waweze kutoa dhabihu katika hekalu

Walikuweko kule Yerusalem kwa vile wanaume wote wa Kiyahudi walitakiwa kuhudhulia sikukuu tatu muhimu za kila mwaka (kama vile Kutoka 23 na Walawi 23).

**2:11 "Wakrene"** Hiki kilikuwa ni kisiwa kikubwa huko Shamu karibia na Uturuki. Lingaliweza kusimama kama neno la ujumla kwa visiwa vyote vya Augeni.

☐ **"Warabu"** Hili lingaliweza kurejerea kwenye kizazi cha Esau. Palikuwepo na kabila nyingi za kiarabu zilizotawanyika sehemu za Kusini Mashariki ya karibu. Hii orodha iliwasilishwa kwa watu wa Kiyahudi wa karne ya kwanza waliojulikana kote. Yawezakuwa ni sitiari mfanano kwa kabila sabini za ulimwengu kama alama ya Kiyahudi kwa wanadamu wote (kama vile Luka 10). Wazo lile lile linaelezewa katika Kumb. 32:8 katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani.

**2:12** Mahujaji hawa walitambua haya matukio muhimu kama alama yenye umuhimu. Petro aliachana na kipindi cha kuyajibu maswali yao.

**2:13 "walikuwa wamelewa"** Hii ni kauli timilifu tendwa yenye kuarifu iliyo na mafumbo, inayodai kuwa hawa wanafunzi walikuwa wamekunywa wakiwa katika hali ya ulevi kama walivyoonekana wakiwa wamelewa.

☐ **"mvinyo mpya"** Maelezo Fulani ya hali hii ni kuwa hawa wafuasi wa Yesu walikuwa wamelewa (kama vile Efe.5:8a). ni kwa namna gani ulevi unaelezea uwezo wa lugha? Nina uhakika palikuwepo pia na mazingira ya shangwe na furaha.

## **MADA MAALUM: MTAZAMO WA KIBIBLIA KUHSIANA NA KILEVI NA ULEVI**

### I. Maneno ya Kibiblia

#### A. Agano la Kale

1. Yayin – Hili ni neno la jumla la divai (BDB 406, KB 409), ambalo limetumika mara 141. Asili ya neno hili si yumkini kwa sababu haitokani na mzizi wa Kiebrania. Hii mara nyingi inamaanisha juisi ya matunda iliyochacha, mara nyingi tunda aina ya balungi. Baadhi ya vifungu bainishi ni Mwa. 9:21; Kut. 29:40; Hes. 15:5,10.
2. Tirosh – Hii ni "divai mpya" (BDB 440, KB 1727). Kwa sababu ya tabia ya nchi ya Mashariki ya Karibu, uchachu unaanza ndani ya masaa sita baada ya kutengeneza juisi. Neno hili hurejerea juu ya divai katika hatua ya kuchachusha. Kwa vifungu vibainishi tazama Kut. 12:17; 18:4; Isa. 62:8-9; Hos. 4:11.
3. Asis – Kwa uhalisia hiki ni kinywaji aina ya kileo ("divai mpya," BDB 779, KB 860, m.f. Yoeli 1:5; Isa. 49:26).
4. Sekar – Hili ni neno "kinywaji kikali" (BDB 1016, KB 1500). Mzizi wa Kiebrania unatumika ndani ya neno "kulewa" au "mlevi." Mara nyingi huu unaongezwa katika ndani yake ili kukifanya kileweshe

zaidi. Hiki ni sawa na yayin (kama vile Mit. 20:1; 31:6; Isa. 28:7).

B. Agano Jipya

1. Oinos – neno lililo sawa kimaana na yayin
2. Neos oinos (divai mpya) – neno linalofanana la Kiyunani sawa na tirosh (kama vile Marko 2:22).
3. Gleuchos vinos (divai mpya, asis) – ni ile divai inayotengenezwa katika hatua za mwanzo kabla ya kuchachushwa (kama vile Matendo ya Mitume 2:13).

II. Matumizi ya Kibiblia

A. Agano la Kale

1. Mvinyo ni zawadi ya Mungu (Mwa. 27:28; Zab 104:14-15; Mhu. 9:7; Hos. 2:8-9; Yoeli 2:19,24; Amosi 9:13; Zek. 10:7).
2. Divai ni swehemu ya sadaka ya kuteketeza (Kut. 29:40; Law. 23:13; Hes. 15:7,10; 28:14; Kumb. 14:26; Amu. 9:13).
3. Divai inatumika kama tiba (2 Sam. 16:2; Mit. 31:6-7).
4. Divai inaaweza kuwa chanzo cha tatizo (Nuhu – Mwa. 9:21; Lutu – Mwa. 19:33,35; Samsoni – Waamuzi 16; Nabali – 1 Sam. 25:36; Uria – 2 Sam. 11:13; Amnon i – 2 Sam. 13:28; Ela – 1 Fal. 16:9; Ben-hadad i – 1 Fal. 20:12; Watawala – Amosi 6:6; na Wanawake – Amos 4).
5. Divai inaweza kutumika vibaya (Mit. 20:1; 23:29-35; 31:4-5; Isa. 5:11,22; 19:14; 28:7-8; Hosea 4:11).
6. Divai ilizuiliwa kwa makundi fulani (makuhani waliokuwa katika zamu, Law. 10:9; Eze. 44:21; Wanazareti, Hesabu 6; na watawala, Mit. 31:4-5; Isa. 56:11-12; Hosea 7:5).
7. Divai ilitumika katika mpangilio wa matukio ya siku za mwisho (Amosi 9:13; Yoeli 3:18; Zek. 9:17).
  1. Kipindi cha uwazi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya
  2. Divai katika upatanisho ina msaada (Ecclesiasticus 31:27-33).
  3. Walimu wa Sheria za Kiyahudi wanasema, "Divai kuu kuliko tiba zote, mahali palipo na uhaba wa divai, madawa yalevyayo yanahitajika." (BB 58b).

B. Agano Jipya

1. Yesu alikibadili kiwango kikubwa cha maji katika divai (Yohana 2:1-11).
2. Yesu alikunywa divai (Mt. 11:18-19; Luka 7:33-34; 22:17 na kuendelea)
3. Petro alidhihakiwa kwa ulevi "mvinyo mpya" siku ya Pentekoste (Mdo. 2:13).
4. Divai inaweza kutumika kama matibabu (Marko 15:23; Luka 10:34; 1 Tim. 5:23).
5. Watawala hawatakiwi kuwa watumiaji wabaya. Hii haimaanishi kujinyima molja kwa moja (1 Tim. 3:3,8; Tito 1:7; 2:3; 1 Pet. 4:3).
6. Divai ilitumika katika kupangili matukio ya siku za mwisho (Mathayo 22:1 na kuendelea; Ufu. 19:9).
7. Divai ililaaniwa (Mt. 24:49; Luka 12:45; 21:34; 1 Kor. 5:11-13; 6:10; Gal. 5:21; 1 Pet. 4:3; Rum. 13:13-14).

III. Utambuzi wa ndani wa Kithiolojia

A. Mkazo wa Kiupembuzi

1. Divai ni zawadi kutoka kwa Mungu.
2. Ulevi ni tatizo kubwa.
3. Waamini katika baadhi ta tamaduni yawapasa kuweka uhuru wa mipaka yao kwa ajili ya injili (Mt. 15:1-20; Marko 7:1-23; 1 Wakorintho 8-10; Warumi 14).

B. Mwelekeo wa kwenda nje ya mipaka

1. Mungu ndiye mwanzilishi wa mambo yote.
  - a. chakula – Marko 7:19; Luka 11:44; 1 Kor. 10:25-26
  - b. mambo yote yasiyo najisi – Rum. 14:14,20; 1 Tim. 4:4
  - c. mambo yote ya halali – 1 Kor. 6:12; 10:23
  - d. mambo yote yaliyo safi – Tito 1:15
2. Mwanadamu aliyeanguka ametumia vibaya zawadi ya Mungu kwa kuzitumia nje ya mipaka ya Mungu aliyoitoa.

C. Matumizi mabaya yako ndani yetu, si ndani ya vitu. Hakuna kilicho kiovu ndani ya uuumbaji wa vitu vinanyoonekana (tazama B. 1. Hapo juu).

- IV. Utamaduni wa Karne ya kwanza ya Kiyahudi na Chachu
- A. Chachu hunza ndani ya muda mfupi, takribani ndani ya masaa 6 baada ya barungi kusagwa
  - B. Desturi ya Kiyahudi inasema kwamba povu linapoonekana juu yake (dalili ya uchachu), hii huelekea kuwa sehemu ya divai iliyo na uchachu (Ma aseroth 1:7). Hiii iliitwa "divai mpya" au "divai tamu."
  - C. Chachu ya kwanza iliyo kali uilikamilishwa baada ya juma moja.
  - D. Chachu ya pili ilichukuwa sku zipatazo 40 . Katika hatua hii tendo hili lilifikiriwa kama "divai kukuu" na ingweza kutolewa madhabahuni (Edhuyyoth 6:1).
  - E. Divai ambayo iliyobakizwa ndani ya machicha (divai kongwe) ilifikiriwa kuwa nzuri, lakini ilitakiwa kuchujwa vizuri kabla ya kutumiwa.
  - F. Divai ilifikiriwa kuwa kuukuu kwa usahihi baada ya kutunzwa vema kwa ajili ya kuchachushwa. Miaka mitatu kilikuwa kipindi cha muda mrefu ambapo divai ingetunzwa kwa usalama. Hii iliitwa "divai kuuku" na ilitakiwa kuchanganywa na maji.
  - G. Ni katika miaka 100 ya mwisho pekee ya ukame wa mazingira na ongezeko la madawa uchachu umetoweka. Ulimwengu wa kale usingeweza kustisha tendo la asili la kuchachusha.
- V. Maelezo ya Kiufungaji
- A. Hakikisha uzoefu wako, thiolojia, na fasiri ya kibiblia havimkashifu Yesu na ile karne ya kwanza ya Kiyahudi/Utamaduni wa ki- Kristo! Hawa kwa uwazi hawakujinyima moja kwa moja.
  - B. Mimi sitetei matumizi haya ya kilevi kwa jamii. Hata hivyo, wengi huchochea nafasi ya Biblia juu ya somo hili na sasa wanadai keki kuu iliyojikita katika utamaduni/ubaguzi wa kimadhehebu.
  - C. Kwangu mimi, Warumi 14 na 1 Wakorintho 8-10 zimetoa utambuzi na mwongozo uliojikita katika upendo na heshima kwa waamini wenetu na kuieneza injili ndani ya utamaduni wetu, si uhuru binafsi au ukosoaji wa hukumu. Ikiwa Biblia ni chanzo pekee cha imani na matendo, bila shaka yatupasa wote kufikiria upya juu ya jambo hili.
  - D. Ikiwa tunahimiza kujinyima moja kwa moja kama mapenzi ya Mungu, nini tunachokimaanisha juu ya Yesu, pamoja na zile tamaduni za sasa ambazo kwa hali ya mazoea hutumia divai (m.f. Ulaya, Israeli, Argentina).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO 2:14-21**

<sup>14</sup>Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti yake, akawaambia, Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu. <sup>15</sup>Sivyo mnavyodhani; watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana; <sup>16</sup>lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli, <sup>17</sup>Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto. <sup>18</sup>Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Roho yangu, nao watatabiri. <sup>19</sup>Nami nitatoa ajabu katika mbingu juu, na ishara katika nchi chini, damu na moto, na mvuke wa moshi. <sup>20</sup>Jua litageuka kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla ya kuja ile siku ya Bwana iliyo kuu na iliyo dhahiri. <sup>21</sup>Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa.

**2:14 "Petro"** Jaribu kufikiri, kati ya wanafunzi wote, Petro ndiye alikuwa wa kwanza kuhubiri ujumbe wa Kikristo! Yeye Yule aliyemkana Yesu mara tatu kuwa hamjui (kama vile Luka 23)! Petro anabadilika toka kwenye uwoga na ukanaji na kuwa mtu aliyeshikamana na mwenye utambuzi wa kiroho ni ushahidi kuwa zama za Roho zimeshushwa zikiwa na nguvu ya mabadiliko ya maisha. Hii ni hotuba ya kwanza iliyowekwa kama kumbukumbu katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Inatuonyesha sisi kilichomo na msisistizo wa mahubiri ya mitume. Haya mafundisho ya kitume yanaunda sehemu muhimu ya Matendo ya Mitume.

## MADA MAALUM: MAFUNDISHO YA KANISA LA MWANZO

Kuna maoni mengi kuhusu Ukristo. Siku zetu hizi ni siku za wingi wa dini, kama ilivyokuwa karne ya kwanza. Binafsi, kwa pamoja nayajuisha na kuyakubali makundi yote yale yanayodai kumfahamu na kumwamini Yesu Kristo. Wote hatukubaliani kuhusu hili au lile lakini kimsingi ukristo ni kumhusu Yesu. hata hivyo, kuna makundi yanayodai kuwa wapo wakristo ambao wanaonekana "kufanana." Ni kwa vipi naweza kuelezea tofauti ?

Sawa, kuna njia mbili:

- C. Kitabu kinachoweza kusaidia kujua kile makundi ya madhehebu ya kisasa yanaamini (kutoka katika maandiko yao) *The Kingdom of the Cults* na Walter Martin.
- D. Hotuba ya makanisa ya awali, hasa wale kupitia Mtume Petro na Paulo katika kitabu cha Matendo, wanatupatia maelezo ya msingi kwa vipi waandishi wa karne ya kwanza waliovuviwa waliueleza Ukristo kwenye makundi. "matamko" haya ya awali au "mafundisho" (ambacho kitabu cha matendo ni mhasari wake) yanaendana na neno la Kiyunani *Kerygma*. Ufuatao ni ukweli halisi wa injili kuhusu Yesu katika Matendo ya Mitume:
  - 1. Kutimiliza nabii nyingi za Agano la Kale- – Mdo 2:17-21,30-31,34; 3:18-19,24; 10:43; 13:17-23,27; 33:33-37,40-41; 26: 6-7,22-23
  - 2. Alitumwa na YHWH kama alivyoahidi- Mdo. 2:23; 3:26
  - 3. Miujiiza iliyotendeka kuthibitisha ujumbe wake na kudhihilisha huruma ya Mungu- – Mdo 2:22; 3:16; 10:38
  - 4. Waliofunguliwa, wasiomilikiwa- Mdo. 3:13-14; 4:11
  - 5. Kusurubishwa - Mdo 2:23; 3:14-15; 4:10; 10:39; 13:28; 26:23
  - 6. Alifufuliwa kuja uzimani- Mdo. 2:24,31-32; 3:15,26; 4:10; 10:40; 13:30; 17:31; 26;23
  - 7. Ameinuliwa mkono wa kulia wa Mungu Baba- Mdo 2:33-36; 3:13,21
  - 8. Atakuja tena mara ya pili - Mdo 3:20-21
  - 9. Alichaguliwa kuwa hakimu- Mdo 10:42; 17:31
  - 10. Akamtuma Roho Mtakatifu- Mdo 2:17-18,33,38-39; 10:44-47
  - 11. Mwokozi wa kila aaminiye- Mdo 13:38-39
  - 12. Hakuna mwingine aliye mwokozi- Mdo 4:12; 10:34-36

Hapa kuna baadhi ya njia za kukubali kwenye hizi nguzo za ukweli:

- 1. Tubu – Mdo. 2:38; 3:19; 17:30; 26:20
- 2. Amini – Mdo. 2:21; 10:43; 13:38-39
- 3. Ubatizwe – Mdo.2:38; 10:47-48
- 4. Mpokee Roho – Mdo 2:38; 10:47
- 5. Yote yatakujiilia- Mdo.2:39; 3:25; 26:23

Mpango huu ulitumika kama tamko la kanisa la mwanzo, ingawa waandishi tofauti wa Agano Jipya wanaweza kuacha sehemu au wakasisitiza wengine hasa katika maandiko yao. Injili yote ya Marko kwa karibu inafuata dhana ya mafundisho. Marko kiutamaduni anaonekana kama kuitengeneza hotuba ya Petro, iliyohubiriwa huko Roma, katika injili iliyoko kwenye maandishi. Injili zote za Mathayo na Luka zinafuata muundo wa Marko.

☐ **"pamoja na wale kumi na mmoja"** Hili linaonyesha mambo mawili (1) Petro anakuwa mnenaji, lakini bado anakuwa sehemu ya kundi la kitume. Haongei mwenyewe au kwa kutumia mamlaka yake mwenyewe. Roho anaongea mwenyewe kipekee kupitia kundi hili linaloitwa mashahidi wa macho na (2) Mathayo, ingawa hajui kitu chochote kuhusiana na huduma yake, rasmi akawa sehemu ya kundi la kitume.

☐ **"enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalem"** Watu waliokuwa wakielezwa hapa wanaonekana kuwa tofauti na wale mahojaji walio elezwa kinagaubaga kwa utaifa wao katika Mdo 2:7-11.

☐ **"Ilijueni jambo hili mkasikie maneno yangu"** Maneno haya yote ni yenye kushurutisha na la pili ni kauli ya kati (shahidi) ya wakati uliopita usiotimilifu. Petro anahitaji usikivu usiogawanyika. Inavyoonekana kifungu hiki ni nahau ya Kisemitiki. Kimetumika mara mbili kuitambulisha hotuba ya Petro (kama vile Mdo 2:14; 4:10) na mara mbili kwa Paulo (kama vile Mdo. 13:38; 28:28). Luka alikuwa mtu wa mataifa wa umri mkubwa aliyeongoka. Alama hii ya nahau ya Kisemitic inaonyesha kuwa Luka hakuiandaa hotuba ile ya Matendo ya Mitume kwa ajili ya kusudi lake la kithiolojia, lakini kwa uaminifu akakielezea kwa ufupi chanzo chake.

**2:15 "watu hawa hawakulewa"** Petro, akivutika kwenye mabadiliko katika Mdo. 2:13, anasema ilikuwa ni mapema mno kwa hawa Wakristo wa Kiyahudi kulewa kwa mvinyo. Hili linfuatisha tafasiri ya kiuualimu wa dini ya Kiyahudi ya Kut. 16:8 (kama vile (cf. E. M. Blaiklock, Tyndale NT Commentary Series, Acts, uk. 58).

☐ **"ni saa tatu ya mchana"** Hii ingaliweza kuwa ni saa 3:00 ya asubuhi. Ulikuwa ni muda wa kila siku wa asubuhi wa utoaji sadaka dhabihu ya hekalu. Ulikuwa umekwisha kuwa muda muafaka wa maombi kwa Wayahudi. "saa ya tatu mchana" ni ishara ya muda wa Kiyahudi. Waandishi wa Agano Jipya (hasa Yohana) anatumia ishara zote za Kiyahudi na Kirumi.

**2:16 "jambo hili ni lile lililonenwa na kinywa cha nabii Yoel"** Hii ni nukuu toka kwa Yoel 2:28-32 toka kwenye tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani. Yesu mwenyewe anawezakuwa ndiyo chanzo cha kutambua sura hii ya kinabii kama imekwisha kutimilizwa (kama vile Luka 24:27,45).

**2:17 "katika siku za mwisho"** Kifungu hiki ni marekebicho ya Luka ya andiko la tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani na hakitakiwi kuwa katika herufi kubwa. Katika Agano la Kale kifungu hiki kilirejelea wakati wa mwisho na ujio wa zama mpya za Masihi. Katika Agano Jipya "siku za mwisho" zinarejelea mwendelezo wa enzi za Kiyahudi. Enzi mpya ilianza kwa Yesu alipobadilika katika umbo la kibinadamu pale Bethlehem na kitadumu mpaka ujio wake wa mara ya pili. Tunaishi kwenye mvutano kati ya ufalme wa Mungu "uliokwisha timia" na "ule ambao bado." angalia Mada Maalum ifuatayo.

### **MADA MAALUM: NYAKATI HIZI NA NYAKATI ZIJAZO**

Manabii wa Agano la Kale waliutazama wakati ujao kama upanuzi wa wakati uliopo. Kwao wakati ujao utakuwa marejesho ya Israeli ya kijiografia. Hata hivyo, hata wao waliuona kama siku mpya (kama vile Isa. 65:17; 66:22). Kwa kwendelea kukataliwa YHWH kwa makusudi na uzao wa Abraham (hata baada ya uhamisho) ni kielelezo kiliicho dhihirika ndani ya hati ya Kiyahudi ya fasili ya mambo ya ufunuo wa matukio ya siku za mwisho (yaani, I Enoch, IV Ezra, II Baruch). Maandishi haya yanatengeneza utofauti kati ya zama hizi mbili: zama za uovu za sasa zinazomilikiwa na Shetani na zama zijazo za haki zinazomilikiwa na Roho na zilizozinduliwa na Masihi (apiganaye mwenyewe mara kwa mara).

Katika eneo hili la theolojia (hukumu, kifo na peponi) kuna maendeleo ya dhairi. Wanatheolojia wanalihita hili "ufunuo endelevu." Agano Jipya linakubaliana na ukweli huu mpya wa kiulimwengu wa zama hizi mbili (yaani, nyakati mbili

<b>Yesu</b>	<b>Paulo</b>	<b>Webrania (Paulo)</b>
Mt. 12:32; 13:22,39	Warumi 12:2	Ebr.1:2; 6:5; 11:3
Marko 10:30	1 Kor. 1:20; 2:6,8; 3:18	
Luka 16:8; 18:30; 20:34-35	2 Kor. 4:4	
	Wagalatia 1:4	



Efe. 1:21; 2:2,7; 6:12

1 Timotheo 6:17

2 Timotheo 4:10

Tito 2:12

Katika theolojia ya Agano Jipya zama hizi za Kiyahudi zimekuwa zikipishana kwa sababu ya tabiri zisizotarajiwa na ambazo hazikutiliwa maanani zilizohusu kuja kwa Masihi. Kuonekana kwa Yesu katika umbile la mwili kulitimiza unabii mwingi wa Agano la Kale uliohusu utambuzi wa zama mpya (Dan. 2:44-45). Hata hivyo, Agano la Kale pia liliutazama ujio Wake kama Hakimu na Mshindi, bado alikuja kwa mara ya kwanza kama Mtumishi Ateswaye (kama vile Isaya 53; Zek. 12:10), mnyenyekevu na mpole (kama vile Zekaria 9:9). Atarudi katika nguvu ile ile kama Agano la Kale lilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19). Utimilifu wa zama hizi mbili ulisababisha Ufalme kuwepo (uliotambuliwa), lakini zile zijazo (hazijatimilika ipasavyo). Huu ni mvutano wa Agano Jipya wa uliopo tayari, lakini bado!

☑ **"asema Mungu"** Kitabu cha miswaada wa ya kale ya Kiyunani na Kilatini (Codex Bezae, MS D, ina neno *kurios* (Bwana). Je neno *kurios linarejea kwa YHWH wa Agano la Kale au kwa Yesu, Masihi?* Haswa yawezekana kuwa neno *Theos* (Mungu) lilikuwa jaribio la waandishi kumwelezea kwa ufasaha mnenaji.

☑ **"nitawamwagia watu wote Roho yangu"** Tambua kipengere cha wote (kama vile Mdo. 2:39). Mipaka yote ya desturi za kale imeondolewa katika Kristo (kama vile 1 Kor. 1 2:1 3; Gal. 3:28; Efe. 3:6; Kol. 3:1 1 ).ingawa hakuna tofauti kati ya Myahudi na Mtu wa mataifa iliyotajwa katika Yoeli 2, tambua Mdo 2:38, ambayo inadokeza kutokuwepo na tofauti. YHWH anagawana Roho Wake na wanadamu wote aliowaumba kwa sura yake (kiuhalisia, "mwili wote"), ambao unatetewa katika Mwa. 1:26-27.

☑ **"wana na binti watatabiri. .waume kwa wake, nitawamwagia Roho yangu"**Hili lawezakuwa ni utimilifu maalumu wa Hes. 11:29. Tambua kuwa hapana utofauti wa jinsia.

## MADA MAALUM: WANAWAKE KATIKA BIBLIA

- I. Agano la Kale
  - A. Katika mila na desturi wanawake walichukuliwa kama ni mali kwa aliyenaye
    1. Walijumuishwa katika orodha ya mali (Kutoka 20:17)
    2. Walivyotendewa wanawake watumwa (Kutoka 21:7-11)
    3. Nadhiri za wanawake kufutwa na waume wenye madaraka (Hesabu 30)
    4. Wanawake kama mateka wa vita (kumbukumbu 20:10-14; 21:10-14)
  - B. Kiutendaji palikuwa na ushirikiano
    1. Mwanaume na mwanamke waliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:26-27)
    2. Heshima kwa baba na mama (Kutoka 20:12 [Kumb. 5:16])
    3. heshima kuu kwa baba na mama (Mambo ya Walawi 19:3; 20:9)
    4. mwanaume na mwanamke wangeweza kuwa Wanazareti (Hesabu 6:1-2)
    5. mabinti wana haki ya urithi (Hesabu 27:1-11)
    6. ni sehemu ya watu wa agano (Kumbu kumbu. 29:10-12)
    7. wanapata mafundisho ya baba na mama (Mithali 1:8; 6:20)
    8. wana wa kiume na mabinti wa Hemani (nyumba ya Kilawi) waliongoza muziki ndani ya Hekalu (1 Mambo ya Nyakati 25:5-6).
    9. Wana wa kiume na wa kike watatoa unabii katika enzi mpaya (Yoeli 2:28-29)
  - C. Wanawake katika dhima ya uongozi
    1. Dada yake Musa, Miriamu, alitwa nabii wa kike (Kutoka 15:20-21 vile vile nukuu Mika 6:4)
    2. Wanawake walikirimiwa toka kwa Mungu kusokota nguo za aina mbalimbali kwa ajili ya

Vibanda(Kutoka 35:25-26)

3. Mwanamke aliyeolewa, Debora, pia nabii (kama vile Waamuzi. 4:4), aliyaongoza makabila yote (Amu. 4:4-5; 5:7)
4. Hulda alikuwa nabii ambaye mfalme Yosia alimsihi kusoma na kutafsiri kitabu kipya kilichotolewa "*Book of the Law*" (2 Falme 22:14; 2 Nya. 34:22-27)
5. Malkia Esta, mwanamke aliyemcha Mungu, aliwaokoa Wayahudi katika Uajemi

## II. Agano Jipya

- A. Kwa utamaduni wa dini za Kiyahudi na ulmwengu wa kale wa Kiyunani na Rumi, wanawake walikuwa raia wa daraja la pili wenye haki na vipaumbele vichache (isipokuwa Makedonia).
- B. Wanawake katika dhima ya uongozi
  1. Elizabeti na Mariamu, wanawake waliomcha Mungu kwa kujihudhuria mbele za Mungu (Luka 1-2)
  2. Ana, nabii mwanamke akihudumu katika Hekalu (Luka 2:36)
  3. Lidia, mwamini na kiongozi wa kanisa la nyumbani (Matendo 16:14,40)
  4. Mabinti Filipo wanne waliokuwa mabikra na manabii (Matendo 21:8-9)
  5. Fibii, shemasi wa kike wa kanisa katika Kenkrea (Rum. 16:1)
  6. Priska (Prisila), mtendakazi pamoja na Paulo na mwalimu wa Apolo (Matendo 18:26; Rum. 16:3)
  7. Maria, Trifaina, Trifosa, Persisi, Yulia, dada wa Nerea, wanawakae kadhaa watenda kazi amoja na Paulo (Rum. 16:6-16)
  8. Yunia (KJV), bila shaka mwanamke mtume (Rum. 16:7)
  9. Euodia na Sintike, watenda kazi pamoja na Paulo (Flp. 4:2-3)

## III. Ni kwa namna gani mwamini wa sasa atailinganisha mifano hii tofauti ya kibiblia?

- A. Ni kwa namna gani mtu ataupambanua kweli wa kihistoria na kiutamaduni, anaoutumia katika mazingire asilia pekee, kutoka katika ukweli wa milele ulio halali kwa makanisa yote, waamini wa rika zote?
  1. Kwa umakini yatupasa kuchukuliana na kusudio la mwandishi asilia aliyevuviwa. Biblia ni neno la Mungu na njia na chanzo pekee cha imani na matendo.
  2. Yatupasa kushughulika dhahiri na maandiko yenye masharti na kihistoria yaliyovuviwa.
    - a. Utaratibu wa ibada (yaani, utaratibi na liturujia) wa Israeli (kama vile Matendo 15; Wagalatia 3)
    - b. dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza
    - c. semi dhahiri za Paulo zenye masharti kihistoria na katika 1 Wakorintho
      - 1) mfumo wa kisheria wa wapagani katika Rumi (1 Wakorintho 6)
      - 2) kubaki katika hali ya utumwa (1 Kor. 7:20-24)
      - 3) ujane/useja (1 Kor. 7:1-35)
      - 4) mabikra (1 Kor. 7:36-38)
      - 5) chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu (1 Kor. 8; 10:23-33)
      - 6) matendo yasiyofaa katika Karamu ya Bwana (1 Wakorintho 11)
  3. Kwa uwazi na kwa ukamilifu Mungu alijifunua kwa utamaduni maalumu, siku maalumu. Yatupasa kuuchukua ufunuo kwa umakini mkubwa, sio kufanya marekebisho kwa kila kipengele. Neno la Mungu liliandikwa katika maneno ya mwanadamu, likaelezwa katika utamaduni maalumu kwa wakati maalumu .
- B. Tafsiri za kibiblia inapaswa kutafuta kusudi la asilia la mwandishi, nini alichokuwa akikizungumzia katika sihu zake zile? Hili ndilo jambo la kimsingi na la muhimu sana la tafsiri sahihi. Lakini basi yatupasa tulitumie hili kwa wakati wetu huu tulio nao. Tatizo kubwa la kiutafsiri linaweza kuelezea maana ya neno. Je! Ni wapi palikuwa na huduma nyingi kuliko wachungaji ambao walionekana kama viongozi? Je! Ni wapi wahudumu au mashemasi wa kike na manabii wa kike walionekana kama viongozi? Ni dhahiri sana kuwa Paulo, katika 1 Kor.

14:34-35 na 1 Tim. 2:9-15, anadai kuwa wanawake wasishike nafasi katika ibada ya hadharani! Lakini alitumie kwa namna gani katika siku kama hizi? Nisingetaka utamaduni wa Paulo au utamaduni wangu kunyamazisha neno la Mungu na mapenzi yake. Bila shaka katika siku zile za Paulo palikuwa na mipaka sana, lakini pia katika siku zangu hizi inaweza kuwa wazi mno. Najisikia kukosa amani sana kusema kwamba kuwa maneno na na mafundisho Paulo ni ya kimasharti, karne ya kwanza, ukweli unaoendana na mazingira ya wenyeji hao. Mimi ni nani hata niweze kusababisha akili yangu au utamaduni wangu kumpinga mwandishi aliyevuviwa?!

Hata hivyo, nitafanya nini ikiwa kuna mifano ya kibiblia ya wanawake waliokuwa viongozi (hata katika maandiko ya Paulo, kama vile Warumi 16)? Mfano mzuri wa hili ni mjadala wa Paulo kuhusu ibada ya hadharani katika 1 Wakorintho 11-14. Katika 1 Kor. 11:5 anaonekana kuyaruhusu mahubiri na maombi ya wanawake katika ibada za hadharani huku vichwa vyao vikiwa vimefunikwa, lakini bado katika 14:34-35 anawahitaji wawe kimya! Kulikuwa na watoa huduma wanawake (kama vile Rum. 16:1) na manabii wa kike (kama vile Matendo 21:9). Ni utofauti huu unaonipa uhuru wa kutambua maoni ya Paulo (kama inavyohusiana na maagizo kwa mwanamke) kama ilivyozuiliwa huko Korintho na Efeso katika karne ya kwanza. Katika makanisa yote mawili palikuwa na matatizo kwa wanawake katika kutumia uhuru wao mpya uliopatikana (kama vile Bruce Winter, *After Paul Left Corinth*), ambapo ingeweza kusababisha ugumu kwa kanisa kuifikia jamii kwa ajili ya Kristo. Uhuru wao ulibidi kupunguzwa ili kwamba injili iweze kuleta matokeo mazuri.

Siku zangu ziko kinyume na siku za Paulo. Katika siku zangu injili inaweza kuwekewa mipaka ama ikiwa wanawake wenye uwezo wa kusema, waliofunzwa hawaruhusiwi kuchangia katika injili, hawaruhusiwi kuongoza! Ni nini hatima ya lengo la ibada ya hadharani? Si uinjilisti na nidhamu? Je! Mungu anaweza kuheshimiwa na kufurahishwa na viongozi wa kike? Biblia kwa ujumla wake inaonekana kusema "ndiyo"!

Nataka kukubaliana na Paulo; theolojia yangu kimsingi ni ya Kipauline. Sitaki kuathiriwa kwa kiwango kikubwa au kugeuzwa kifikra na sera za kisasa za kupigania haki za wanawake. Hata hivyo, nahisi kwamba kanisa limeenda pole pole katika kuitikia ukweli ulio wazi wa kibiblia, kama matendo yasiyo stahili kuhusu utumwa, ubaguzi, itikadi kali, na ubaguzi wa kijinsia. Hili pia limechelewa kwa kutoitikia vyema masuala ya uzalilishaji wa wanawake katika ulimwengu wa kisasa. Mungu katika Kristo amemweka huru mtumwa na mwanamke. Si thubutu kuruhusu maandiko yenye utamaduni unaopingana na haya.

Hoja moja zaidi: kama mtafsiri ninafahamu kuwa Korintho lilikuwa ni kanisa lililoharibiwa sana. Vipawa vilivyotolewa vilikuwa vya majivuno. Wanawake wangeweza kuwa wameshikwa katika hili. Pia ningeweza kuamini kuwa Efeso ilikuwa imeathiliwa na walimu wa uongo waliofanikiwa kutumia wanawake kama wasemaji mbadala ndani ya makanisa ya Efeso.

C. Mapendekezo kwa usomaji zaidi

1. *How to Read the Bible For All Its Worth* by Gordon Fee and Doug Stuart (kur. 61-77)
2. *Gospel and Spirit: Issues in New Testament Hermeneutics* by Gordon Fee
3. *Hard Sayings of the Bible* by Walter C. Kaiser, Peter H. Davids, F. F. Bruce, na Manfred T. Branch (kur. 613-616; 665-667)

☐ **"unabii"** Kiwastani kuna njia mbili za kulielewa neno hili (1) katika waraka wa Wakorintho neno hili linarejea kwenye kugawana au kuitangaza injili (kama vile Mdo. 14:1 ; Mdo. 2:1 7) (2) kitabu cha Matendo kinawataja (kama vile Mdo. 12:27; 13:1 ; 15:32; 22:10, hata manabii wa kike, 21 :9), ambao walitabiri mambo ya mbeleni (angalia Mada Maalum katika Mdo. 1 1 :27).

Tatizo lililopo kwenye neno hili ni, ni kwa namna gani karama ya unabii ya Agano Jipya inahusiana na manabii wa Agano la Kale? Katika Agano la Kale manabii ndio waandishi wa maandiko. Katika Agano Jipya kazi hii imepewa kwa mitume kumi na wawili wa mwanzo na wasaidizi wao. Kama vile neno “Mtume” linavyochukuliwa kama karama endelevu (kama vile Efe. 4:11) lakini likiwa na kazi mbadala baada ya vifo vya wale kumi na wawili, hivyo pia nasi, ofisi ya nabii. Uvuvio umekwisha koma, hapana tena maandiko yaliyovuviwa (kama vile Yuda 3,20). Manabii wa Agano Jipya kazi yao ya msingi ni kuitangaza injili, bali pia kazi tofauti, yumkini ni kwa namna gani kuutumia ukweli wa Agano Jipya kwa hali ya sasa na uhitaji

☐ **"vijana wenu. . .wazee"** Tambua kuwa hakuna tofauti ya umri.

**2:18 "hata watumishi wangu"** Tambua kuwa hapana ubaguzi kwenye uchumi wa kijamii. Petro anaongeza neno “unabii” kwa unabii wa Yoeli. Halipo kwenye andiko la Kiebrania au tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani, bali linadokezwa toka katika Mdo. 2:17. Kama ilivyo Luka 24 (Mdo. 2:3,6,1 2,1 7,32,36,40,51 ) ina tofauti mbali mbali za kimaandiko, vivyo hivyo pia, matendo (yaani., 2:11, 18, 37, 44). Tofauti hizi mara nyingi zinahusiana kwenye andiko fupi linalopatikana katika MS D (mswaada wa kale wa kiyunani na kilatini toka karne ya 5) na katika matoleo baadhi ya Kilatini ya kale (toka karne ya 5). Mara nyingi hizi familia za ki-Magharibi za machapisho ya Kiyunani yanaongezea vifungu, lakini katika Luka/Matendo kuna maandiko mafupi. Wengi wa watafasiri wa Kiingereza wanajumuisha familia yote ya Iskanda ya machapisho yenye matoleo marefu. Angalia utangulizi wa Matendo, “maelezo ya ufunguzi,” E.

**2:19-20** Hii lugha ya kiyama, ambayo ni dhahili kwa sababu Petro anadai kuwa hili lilikwisha timilizwa, hapana tabia hizi maalumu za kiasili zikitokea, isipokuwa yumkini giza lilipotanda pindi Yesu akiwa msalabani. Inazungumza kwa lugha ya kitamathali juu ya ujio wa Muumba na Mwamuzi. Katika Agano la Kale ujio wake waweza kuwa wa Baraka au hukumu. Uumbaji wote unachanganyikiwa namna ya kuukabili (kama vile Isa. 13:6 na kuendelea na Amo. 5:18-20). Katika unabii wa Agano la Kale hakuna utofauti wa wazi kati ya umbo la kibinadamu (ujio wa kwanza na *Parousia* (ujio wa mara ya pili). Wayahudi walitegemea ujio mmoja tu na mwamuzi/mwokozi mwenye nguvu. Kitabu chenye msaada juu ya lugha za kiyama ni D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks: Rethinking Prophetic and Apocalyptic Language*.

### **MADA MAALUM: FASIHI YA MATUKIO YA SIKU ZA MWISHO (kutoka Utangulizi wa kitabu cha Ufunuo)**

Kitabu cha Ufunuo ni aina ya kipekee ya fasihi ya Kiyahudi, matukio ya siku za mwisho. Mara nyingi hii ilitumika katika nyakati zilizojaa mvutano uyakini kwamba Mungu alikuwa katika mamlaka ya historia na angeleta ukombozi kwa watu Wake. Hii aina ya fasihi inabainishwa na

1. maana nzito ya ukuu wa Mungu kiulimwengu (Mungu aliye mmoja na kuashiliwa)
2. mapambano kati ya wema na uovu, zama hizi na zama zijazo (dhana ya uwili)
3. matumizi ya mfumo wa maneno ya siri (mara nyingi kutoka Kitabu cha Agano la Kale au fasihi ya Kiyahudi ya matukio ya siku za mwisho katika Kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya)
4. matumizi ya rangi, namba, wanyama, wakati mwingine wanyama/wanadamu
5. matumizi ya upatanisho wa kimalaika kwa maana ya maonona ndoto, lakini mara nyingi kupitia upatanisho wa kimalaika
6. mitazamo ya mwanzo juu ya nyakati za mwisho (zama mpya)
7. matumizi ya muonekano wa ishara, si ukweli, ili kupasha habari ya nyakati za mwisho
8. Baadhi ya mifano ya hii aina hii ya fasihi ni
  - a. Agano la Kale
    - 1) Isaya 24-27, 56-66
    - 2) Ezeieli 37-48
    - 3) Danieli 7-12
    - 4) Joeli 2:28-3:21

- 5) Zekaria 1-6, 12-14
- b. Agano Jipya
  - 1) Mathayo 24, Maro 13, Luka 21, na 1 Wakorintho 15 (katika njia nyingine)
  - 2) Ufunuo (sura 4-22)
- c. isiyo ya umbo- mwili (ilichukiliwa kutoka D. S. Russell, *The Method and Message of Jewish Apocalyptic*, kr. 37-38)
  - 1) I Enoch, II Enoch (the Secrets of Enoch)
  - 2) The Book of Jubilees
  - 3) The Sibylline Oracles III, IV, V
  - 4) The Testament of the Twelve Patriarchs
  - 5) The Psalms of Solomon
  - 6) The Assumption of Moses
  - 7) The Martyrdom of Isaiah
  - 8) The Apocalypse of Moses (Life of Adam and Eve)
  - 9) The Apocalypse of Abraham
  - 10) The Testament of Abraham
  - 11) II Esdras (IV Esdras)
  - 12) Baruch II, III

Kuna maana ya uwili katika fasifi hii. Hii inauangalia ukweli kama mtiririko wa uwili, tofauti, au mvutano (ni awaida sana katika maandiko ya Yohana) kati ya:

- a. mbingu – dunia
- b. zama za uovu (wanadamu wa uovu na malaika wa uovu) – zama mpya za wenye haki (watu wa Mungu na malaika wa Mungu)
- c. Kuwepo kwa sasa – kuwepo kwa baadaye

Hizi zote zinaelekea utimilifu ulioletwa na Mungu kumhusu Mungu. Huu si ulimwengu alioukusudia Mungu kuwa, bali Yeye azidi kutenda kazi na kuonyesha mapenzi yake kwa ajili ya urejesho wa uhusiano wa karibu ulionzia ndani ya Bustani ya Edeni. Tukio la Kristo ni mpango wa Mungu wa umwagaji maji, lakini ujio mbili unasababisha uwili wa sasa.

**2:20 "ile siku ya Bwana iliyo kuu na iliyo dhahili"** Neno "dhahili" ni kutoka katika mzizi mmoja wa neno *epiphaneia*, ambalo mara nyingi linatumiwa juu ya ujio wa Yesu wa mara ya pili (kama vile 1 Tim. 6:1 4; 2 Tim. 4:1 ; Tit. 2:1 3). Angalia Mada Maalum ifuatayo.

### **MADA MAALUM: MANENO KWA UJIO WA MARA YA PILI**

Kuna maneno na vifungu kadhaa ambavyo vinarejea juu ya kurudi kwa Yesu.

1. *parousia*" yaani, Yakobo 5:7), ambalo linamaanisha "kuwepo," lililotumika kifalme(kama vile Mt. 24:3,27,37,39; 1 Kor. 15:23; 1 The. 2:19; 3:13; 4:15; 5:23; 2 The. 2:1,8; 2 Pet. 1:16; 3:4,12; 1 Yohana 2:28)
2. *epiphaneia*, "mwonekano wa ana kwa ana" (yaani, 1 Tim. 6:14; 2 Tim. 1:10; 4:1,8; Tito 2:13)
3. *apokalupis*, "kufunua" au "konyesha" (yaani, 1 Kor. 1:7; 2 The.1:7; 1 Pet. 1:5,13; 4:13; 5:1)
4. "siku ya Bwana" na mabadiliko ya kifungu hiki (angalia Mada Maalum: Siku ya Bwana)

Kitabu cha Agano Jipya kama kilivyo kizima kimeandikwandani ya mtazamo wa ulimwengu wa Agano la Kale, ambao unadai kwamba

1. uovu wa sasa, zama za uasi
2. zama mpya za haki zijazo
3. hii ingeletwa na ushirika wa Roho kupitia kazi ya Masihi (Mpakwa Mafuta; tazama Mada Maalum: Masihi)

Dhanio la kithiolojia la uhusiano endelevu linahitajika kwa sababu waandishi wa Agano Jipya kwa uchache

wanabadilisha matarajio ya Israeli. Badala ya jeshi, ilitazamiwa kitaifa (Israeli) ujio wa Masihi, kuna ujio wa mara ya pili. Ujio wa mara ya kwanza ulikuwa wa umbo-mwili la Uungu katika kutungungwa mimba na kuzaliwa kwa Yesu Mnazarethi. Yeye alikuja kama mtu asiye na majeshi, si mtu wa sheria "mtumwa ateswaye" wa Isaya 53; pia aliyejifanya mdogo juu ya juu ya mngongo wa punda (si farasi wa vita au nyumbu wa vita), wa Zek. 9:9. Ujio wa kwanza ulizitambulisha Zama Mpya za Kimasihi, ufalme wa Mungu hapa duniani (tazama Mada Maalum: Ufalme wa Mungu). Katika maana moja ufalme wa Mungu uko hapa, lakini kwa jinsi hiyo, katika maana nyingine huu bado u mbali. Huu ni mvutano kati ya ujio wa aina mbili wa Masihi ambao, katika maana, huku ni kupishana kwa zama za Kiyahudi ambazo zilikuwa hazikuonekana, au hata kutokuwa sawa, kutoka Agano la Kale (tazama Mada Maalum: Zama hizi na Zama Zijazo). Katika ukweli, ujio ulio katika uwili unasistiza juu ya ahadi za YHWH za kuwakomboa watu wote (kama vile Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5 na kuhubiri kwa manabii, hasa Isaya na Yona; tazama Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukumbozi wa Milele).

Kanisa halisubirii ule utimilifu wa Agano la Kale kwa sababu unabii ulio mwingi unarejea juu ya ujio wa kwanza (kama vile *How to Read the Bible For All Its Worth*, uk. 165-166). Nini waamini wanakitarajia ndani ya ujio wa utukufu wa Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana, historia ya utimilifu wa zama mpya za haki zilizotarajiwa hapa duniani bado iko mbinguni (kama vile Mt. 6:10). Uwasilishaji wa Agano la Kale haukuwa sahihi, bali haukukamilika. Yeye atakuja tena kama manabii walivyotabiri, katika uweza na mamlaka ya YHWH (tazama Mada Maalum: Kwa nini Ahadi za Kiagano Zinaonekana Tofauti Sana Ahadi za Agano Jipya Agano Jipya?).

Ujio wa Mara ya Pili si neno la kibiblia, bali ni muundo wa dhana ya matazamo wa ulimwengu na sura ya Agano Jipya lote. Mungu atayaweka mambo yote sawa. Ushirika na kati ya Mungu na mwanadamu aliyeumbwa kwa sura na mfano Wake utajejeshwa (kama vile Ufuunuo 21-22). Waovu watahukumwa na kuondoshwa (kama vile Ufu. 20:11-15). Makusudi ya Mungu ataweza, hawezi, atashindwa!

**2:21 "kila mmoja"** Hapa pana kipengere cha wote tena (kama vile Mdo. 2:1 7 na 39). Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote (kama vile Yn 1 :1 2; 3:1 6; 4:42; 1 Tim. 2:4; Tit. 2:1 1 ; 2 Pet. 3:9; 1 Yn 2:1 ; 4:1 4). Tambua Roho amekwisha kutolewa kwa wanadamu wote (kama vile Mdo. 2:1 7).

☑ **"alitajaye"** Hii ni kauli ya kati tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Mwitikio wa mwanadamu ni sehemu ya mpango wa Mungu kwa ajili ya wokovu (kama vile Yoeli 2:32; Yn 1 :12, 3:16; na Warumi 10:9-13). Wanadamu pekee wameitwa (kama vile Mdo. 2:39) kwenye toba (kama vile Mdo. 2:38) na kuiamini injili, na kuingia katika uhusiano binafsi na Mungu kupitia Kristo (kama vile Mdo. 3:1 6,1 9; 20:21 ; Mk 1 :1 5). Yesu alikufa kwa ajili ya ulimwengu mzima; fumbo ni kuwa kwa nini baadhi wanaitika kwenye kumtafuta Roho (kama vile Yn. 6:44,65) na baadhi hapana (kama vile 2 Kor.4:4).

☑ **"jina la Bwana"** Hii inarejea kwenye tabia ya Yesu au mafundisho kumhusu Yeye. Kuna vyote kipengere binafsi na cha kimafundisho.

## **MADA MAALUM: JINA LA BWANA**

Hii ilikuwa aya ya kawaida kwenye Agano Jipya kwa ajili ya uwepo binafsi na nguvu ya tendaji ya nafsi tatu za Mungu kanisani. Haikuwa kanuni ya kichawi, bali kupeleka hitaji kwa tabia ya Mungu kama inavyoonekana ndani ya Yesu. Mara nyingi aya hii humhusisha Yesu kama Bwana (kama vile Wafilipi 2:11)

1. Katika ukiri wa imani ya mtu kwa Yesu (kama vile Warumi 10:9-13; Matendo 2:21, 30; 8:12 16:10, 48; 19:5; 22:16; 1 Wakorintho 1:13, 15, Yakobo 2:7)
2. Kwenye kukemea pepo (kama vile Mt. 7:22 Marko 9:38; Luka 9:49; 10:17 ; Matendo 19:13)
3. Kwenye uponyaji (kama vile Mdo 3:6, 16:4 10:9 34; Yakobo 5:14)

4. Kwenye tendo la kufanya huduma (kama vile Mathayo 10:42; 18:5; Luka 9:48)
  5. Kwenye wakati wa nidhamu kanisani (kama vile Mathayo 18:15-20)
  6. Wakati wa kuwahubilia mataifa (kama vile Luka 24:47; Matendo 9:15 15:17 Warumi 1:5)
  7. Kwenye maombi (kama vile Yohana 14:13-14 15:7, 16, 16:23 1 Wakorintho 1:2)
  8. Njia ya kuhusisha Ukristo (kama vile Matendo 26:9; 1 Wakorintho 1:10; 2 Tim 2:19, Yakobo 2:7; 1 Pet. 4:14)
- Lolote tulifanyalo kama watangazaji, wachungaji au wahubiri watoa misaada, waponyaji watoa mapepo n.k tufanye katika tabia yake, uweza, utoaji wake kwa jina lake (yaani, Wafilipi 2:9-10)!

☐ **"wataokolewa"** Katika muktadha huu, hii inarejea juu ya wokovu wa kiroho, wakati katika Yoeli yumkini inamaanisha ukombozi wa mwili toka ghadhabu ya Mungu (kama vile Mdo. 2:40). Neno "okolewa" limetumika katika Agano la Kale juu ya kukombolewa kimwili (kama vile Mt. 9:22; Mk 6:56; Yakobo 5:1 4,20). Hata hivyo, katika Agano Jipya lilitumika ki-sitiari kwenye wokovu wa kiroho au ukombozi toka katika ghadhabu ya Mungu ( Yakobo1 :21 ; 2:1 4; 4:1 2). Moyo wa Mungu unadunda kwa ajili ya wokovu wa watu wote wake kwa waume walioumbwa kwa sura yake (kama vile Mwa. 1 :26-27); wakaumbwa kwa ajili ya ushirika!

### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 2:22-28**

<sup>22</sup> Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua; <sup>23</sup> mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani, ninyi mkamsulibisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamwua; <sup>24</sup> ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao. <sup>25</sup> Maana Daudi ataja habari zake, Nalimwona Bwana mbele yangu siku zote, Kwa kuwa yuko upande wa mkono wangu wa kuume, nisitikisike. <sup>26</sup> Kwa hiyo moyo wangu ukapendezewa, ulimi wangu ukafurahi; Tena mwili wangu nao utakaa katika matumaini. <sup>27</sup> Kwa maana hutaiacha roho yangu katika kuzimu; Wala hutamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu. <sup>28</sup> Umenijuvisha njia za uzima; Utanijaza furaha kwa uso wako.

**2:22 "waume wa Israel"** Hawa wasikiaji walikiwa ni mashuhuda wa macho kwenye matukio ya wiki ya mwisho ya maisha ya Yesu hapa duniani. Walikuwa na maarifa binafsi ya kile Petro alikuwa akikizungumza. Wale waliokuwa na utambuzi wa kiroho waliitikia kwenye injili, yapata watu elfu tatu walihudhulia kwenye hutuba ya kwanza (kama vile Mdo. 2:41).

☐ **"sikilizeni"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Udhihilisho wa wazi wa Roho ulikata usikivu wao; sasa ukaja ujumbe wa injili.

☐ **"Yesu Mnazareti"** Mara nyingi inafikiliwa kuwa kwa wastani huu ni mfanano na "Yesu wa Nazareti." Lakini, hii kwa namna Fulani sio njia ya kawaida ya kulielezea hili. Hii sasa inawezekana kuwa kifungu hiki kinaaksi wadhifa wa Kimasihi, "ambalo ni shina" (BDB 666, kama vile Isa. 4:2; 6:1 3; 1 1 :1 ,1 0; 1 4:1 9; 53:2; Yer. 23:5; 33:1 5-1 6; Zak. 3:8; 6:1 2-1 3). Neno la Kiebrania la neno "shina" ni *nezer*.

### **MADA MAALUM: YESU MNAZARETI**

Kuna maneno mbalimbali ya Kiyunani ambayo Agano Jipya hutumia kumzungumzia Yesu.

A. Haya ni maneno ya Agano Jipya

1. Nazarethi – mji katika Galilaya (kama vile Luka 1:26; 2:4,39,51; 4:16; Matendo 10:38). Mji huu hautajwi katika vyanzo vya wakati huu, bali umekutwa katika kumbukumbu ya maandishi ya

baadaye. Kwa upande wa Yesu kuwa alitoka Nazarethi haikujitosheleza (cf. Yohana 1:46). Alama ya msalaba wa Yesu ambayo imeliweka jina la eneo hili ilikuwa alama ya aibu kwa Wayahudi.

2. Nazarēnos – pia inataja maeneo ya kijiografia (cf. Luka 4:34; 24:19).
3. Nazōraios – inaweza kuurejea juu ya mji, lakini pia ingeweza kuwa mwaminifu na mtenda haki Masihi wa Kiebrania "Utanzu" (netzer, BDB 666, KB 718 II, cf. Isa. 11:1; maana zinazokaribiana, BDB 855, Yer. 23:5; 33:15; Zek. 3:8; 6:12; iliyodokezwa katika Ufu. 22:16). Luka akilitumia hili kumhusu Yesu katika 18:37 na Matendo 2:22; 3:6; 4:10; 6:14; 22:8; 24:5; 26:9.
4. Iliyohusiana na #3 nāzir (BDB 634, KB 684), ambalo linamaanisha "aliyewakifishwa kwa maana ya nadhiri."

B. matumizi ya Kihistoria ya neno nje ya Agano Jipya.

1. Lilimaanisha kundi la ausi la Kiyahudi (Mkristo wa awali) (nāsōrayyā ya Kiaramu).
2. Lilitumika katika mzunguko wa Kiyahudi kuwatambulisha waamini katika Kristo (cf. Matendo 24:5,14; 28:22, nosri).
3. Lilikuja kuwa neno la kawaida katika kumaanisha waamini katika makanisa ya Kisiria (Kiaramu). "Mkristo" lilitumika katika makanisa ya Kyunani kumaanisha waamini.
4. Wakati mwingine baada ya kuanguka kwa Yerusalemu, Wafarisayo walikusanyika huko huko Jamnia na walichochea utengano rasmi kati ya sinagogi na kanisa. Mfano wa aina ya maapizo ya mazungumzo dhidi ya Wakristo unapatikana katika *"the Eighteen Benedictions" from Berakoth 28b-29a*, ambayo "Wanazarethi." "Wanazarethi na awaasi waliweza kutoweka kwa muda mfupi; walifutwa kutoka katika kitabu cha uzima na kutoandikwa kuwa walikuwa na imani."
5. Ilitumiwiwa na Justin Martyr, Dial. 126:1, ambaye alitumia netzer ya (Isa. 11:1) kumhusu Yesu.

C. Maoni ya Mwandishi

Nashangazwa sana na herufi za maneno, Ingawa nafahamu kwamba hili ni jambo geni kusikika katika Agano la Kale "Yoshua" ina herufi mbalimbali katika Kiebrania. Maelezo yafuatayo yananisababisha kubaki na mashaka kama maana yake dhahiri :

1. kama vile maana yake ya karibu na neno la Kimasihi "tawi" (netzer) au neno lililo sawa nāzir (aliyekwa mafuta kwa maana ya nadhiri)
2. vidokezo hasi vya eneo la Galilaya kuyahusu mataifa
3. uchache au kutokuwepo kwa uthibitisho wa fasili za sasa kukusu mji wa Nazarethi katika Galilaya
4. inatoka katika kinywa cha pepo katika maana ya hukumu (yaani, "Umekuja kutuungamiza?").

Kwa wasifu kamili wa masomo ya kundi la neno hili, tazama Colin Brown (ed.), *New International Dictionary of New Testament Theology*, juzuu. 2, uk. 346 au Raymond E. Brown, *Birth of the Messiah*, kur. 209-213, 223-225.

☐ **"mtu alidhihilishwa kwenu na Mungu"** Yesu ni mwanadamu pasipo shaka (yaani Mdo. 2:23; Rom. 1 :3), vile vile pia ni Mungu ( kama vile 1 Yn 4:1 -3). Hii ni kauli timilifu tendwa ya hali ya kuendelea. Neno linamaanisha "kuonyeshwa kwa uthibitisho." Mungu kwa uwazi na kwa kurudia mara kwa mara amejidhihilisha mwenyewe katika maneno ya Yesu, matendo na maisha. Wasikilizaji wa Yerusalemu wamekwisha ona na kusikia!

☐ **"kwa miujiza na ajabu na ishara"** Hawa wasikilizaji walikuwa ni mashuhuda wa macho kwa yale yote Yesu aliyafanya katika Yerusalemu wiki yw mwisho ya maisha yake. Neno "miujiza" (teras) lilimaanisha ishara zisizo za kawaida, mara nyingi zilitokea mbinguni, kama Mdo. 2:19-20. Neno "ishara" (sēmeion) linadokeza tukio maalumu linaloelezea maana au umuhimu. Hili ni neno muhimu katika injili ya Yohana (ishara saba muhimu, kama vile Mdo. 2:1 -1 1 ; 4:46-54; 5:1 -1 8; 6:1 -1 5,1 6-21 ; 9:1 -41 ;1 1 :1 -57). Mara zote ishara hazionekani katika mtazamo chanya (kama vile Yn 2:1 8; 4:48; 6:2). Hapa linatumika kama mlolongo wa udhihilisho wa nguvu ambao unafunua kuwa zama mpya imekwisha anza! Inafurahisha kuwa Petro hakutumia muda wowote katika hotuba yake ya mwanzo (kwa wastani muhtasari katika Matendo 2) kuhusu maisha ya awali ya Yesu na mafundisho yake. Uutilizaji wa unabii wa Agano la Kale, kifo chake cha kidhabihu kilichopangwa kabla na ufufuko wake wenye utukufu ni hoja zilizo kuu



**2:23 "mtu huyu"** Hii inawezakuwa ni nahau yenye dharau (kama vile Mdo. 5:28; 6:1 3; Luka 23:1 4; Yn 9:1 6; 1 8:29), lakini katika Mdo. 23:9 na 20:31-32 sio nahau iliyo kinyume. Tena ubinadamu wa Yesu umesisistizwa (kama vile Mdo. 2:22)

▣ **"alipotolewa kwa"** Neno hili (*ekdotos*) linapatikana hapa tu katika Agano Jipya.

**NASB** "shauri lililokusudiwa"

**NKJV** "mwongozo uliokusudiwa"

**NRSV** "mpango bainifu"

**TEV** "mpango wa Mungu mwenyewe"

**NJB** "kusudi lililopangwa"

Hili ni neno *horizō* katika muundo wake wa kauli timilifu tendwa yenye hali ya kuendelea. Maana yake ya kimsingi ni kuamua, kuchagua, au kuweka sawa. Katika Agano la Kale limetumika kwa ajili ya kuweka mipaka ya nchi au mahitaji. Luka aliliumia mara nyingi (kama vile Luka 22:22; Mdo. 2:23; 10:42; 11:29; 17:26,31). Msalaba hakikuwa kitu cha mshangao mbele za Mungu, bali siku zote kilikuwa ni chombo alichokichagua (yaani., muundo wa kidhabihu wa Walawi 1-7) kwa ajili ya kuleta ukombozi kwa mwanadamu *aliyeasi* (kama vile Mwa. 3:1 5; Isa. 53:1 0; Mk 1 0:45; 2 Kor. 5:21 ). Kifo cha Yesu kilikuwa sio cha bahati mbaya. Ulikuwa ni mpango wa Mungu wa ukombozi, wa milele (kama vile Luka 22:22; Mdo. 3:18; 4:28; 13:29; 26:22-23). Yesu alikuja kufa (kama vile Mk. 10:45)! Msalaba haukuwa wa bahati mbaya!

▣ **"kwa kujua kwake Mungu mapema"** Hili ni neno *prognosis* (kufahamu kabla), limetumika hapa tu katika 1 Pet. 1 :2. Hii dhana ya Mungu kutambua historia yote ya mwanadamu ni ngumu kwetu kupanisha na mapenzi huru ya mwanadamu. Mungu ni kiumbe wa kiroho, wa milele ambaye hazuiliwi na mfuatano wa kitambo kidogo. Ingawa hudhibiti na kuitengeneza historia, wanadamu wanawajibika kwa ajili ya mienendo na matendo yao. Kujua mapema hakuathiri upendo wa Mungu na uchaguzi. Kama ndivyo, ingalikuwa ni yenye masharti juu ya bidii ya mwanadamu na thamani yake. Mungu ni mwenye mamlaka na amechagua kuwa wafuasi wake wa Agano wawe na baadhi ya uhuru wa kuchagua namna ya kujongea kwake (kama vile Rum. 8:29; 1 Pet. 1 :20). Kuna mipaka miwili kwenye eneo hili la thiolojia: (1) uhuru ulisukumia mbali: baadhi wanasema Mungu hajui kuhusu uchaguzi wa mbeleni na matendo ya mwanadamu (imani ya wazi kuwa Mungu yupo, ambao ni mwendelezo wa kifalsafa wa mchakato wa kifikra) na (2) ukuu wa Mungu umetupiliwa mbali, ambayo ikaja kuwa Mungu anawachagua baadhi kwenda mbinguni na wengine kwenda kuzimu (kuwa na pande mbili za ufuasi wa Calvin). Napendelea Zaburi 139!

▣ **"ninyi"** Petro anadai kuwepo na kosa na unafiki kwa ajili ya kifo cha Yesu kwa wale wasikiaji wa Yerusalem (kama vile Mdo. 3:1 3-1 5; 4:1 0; 5:30; 1 0:39; 1 3:27,28). Hawakuwa miongoni mwa lile kusanyiko walioitwa kwa ajili ya kusulubiwa; hawakuwa washirika baraza la wakuu wa hekalu waliomleta kwa Pilato; hawakuwa miongoni mwa wale maafisa wa Kirumi au maaskari waliomsulubisha, lakini walihusika, kama nasi tunavyohusika. Dhambi za mwanadamu na uasi zililazimisha mauti yake!

▣ **"mkamsulubisha"** kiuhalisia neno hili ni "kukaza kwa nguvu" (*prospēgnumi*). Limetumika hapa tu katika Agano Jipya. Linamaanisha kupigilia misumari na kumbana kwenye msalaba. Katika matendo 5:30 mchakato wa aina ile ile umeelezewa kama "kutungikwa juu ya mti." Viongozi wa Kiyahudi hawakutaka Yesu apigwe mawe kwa ajili ya kukufuru kama Stefano alivyofanyiwa (kama vile Matendo 7), bali walitaka Yeye (Louw and Nida say this *hapax legomenon* lawezekana kufanana na *stauroō*, sulubisha, [kur. 237 tanbihi 9]). Yumkini hili lilihusianishwa na laana ya Kumb. 21:23. Mwanzoni laana hii ilihusishwa na mazuko yasio sahihi, lakini siku ya Yesu walimu wa dini ya Kiyahudi wameihusianisha na kusulubiwa. Yesu aliwaondolea waamini wote ile sheria ya laana ya agano la kale (kama vile Gal. 3:1 3; Kol. 2:1 4).

▣ **"watu wabaya"** kiuhalisia hii inamaanisha "watu wasiofuata sheria" na inawarejea Warumi.

**2:24 "Mungu alimfufua"** Agano Jipya linathibitisha kuwa watu wote watatu wa Utatu walikuwa kwenye utendaji katika ufufuko wa Yesu:

1. Roho (kama vile Rum. 8:1 1 )
2. Mwana (kama vile Yohana 2:1 9-22; 1 0:1 7-1 8)
3. Kwa kiasi kikubwa mara zote Baba (kama vile Mdo. 2:24,32; 3:1 5,26; 4:1 0; 5:30; 1 0:40; 1 3:30,33,34,37; 1 7:31 ; Rum. 6:4,9)

Matendo ya Baba yalikuwa uthibitisho wa ukubalifu wa maisha ya Yesu, kifo na mafundisho. Hii ilikuwa dhana kuu ya mafundisho yake ya awali kwa mitume wake. Angalia Mada Maalum: *Mafundisho* katika Mdo. 2:14.

▣ **"akiufungua uchungu wa mauti"** Neno hili laweza kumaanisha (1) kiuhalisia, maumivu wakati wa kujifungua (tamaduni na elimu za Kiyunani, kama vile Rum. 8:22) (2) ki-isitiari matatizo kabla ya ujio wa pili (kama vile Mt. 24:8; Mk. 1 3:8; 1The. 5:3). Yumkini linaaksi neno la Kiebrania "mtego" au "kitanzi" katika Zaburi 18:4-5 na 116:3, ambayo yalikuwa ni isitiari za Agano la Kale juu ya hukumu (kama vile Isa. 1 3:6-8; Yer. 4:31 ).

▣ **"kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao"** Yohana 20:9 pia inaunganisha ufufuko wa Yesu kwenye unabii wa Agano la Kale (kama vile Mdo. 2:25-28). Yesu alikwenda kuzimu kwa makusudi (kama vile 1 Pet. 3:1 9; 4:6). Alipoondoka aliwachukuwa waamini wenye haki (kama vile 2 Kor. 5:6, 8)!

**2:25 "maana Daudi ataja habari zake"** Hii ni nukuu toka Zaburi 16:8-11. Petro anadai kuwa Zaburi 16 ni ya ki-Masihi (kama alivyofanya Paulo katika Mdo. 13:36; hizi ni nukuu mbili za Zaburi 16 katika Agano Jipya) na kwamba linarejea moja kwa moja kwa Yesu. Ufufuo wa Yesu ni tumaini la mtunga zaburi na tumaini la mwamini wa Agano Jipya

**2:26 "tumaini"** Neno hili halitumiki ndani ya injili, lakini linatumika katika Matendo kuelezea imani ya mwamini katika utimilifu wa wakati ujao wa ahadi ya injili (kama vile Mdo. 23:6; 24:1 5; 26:6, 7; 28:20). Linatumika mara nyingi katika maandiko ya Paulo, lakini kwa maana mbali mbali linahusiana na mpango wa Mungu wa ukombozi. Angalia Mada Maaalum ifuatayo.

## **MADA MAALUM: TUMAINI**

Paulo alilitumia neno hili mara nyingi kwa namna tofauti lakini katika maana zinazoshabihiana. Mara nyingi lilihusiana na utimilifu wa imani ya waamini (mfano 1 Tim. 1:1). Hili laweza kuellezewa kama utukufu, maisha ya milele, hatma ya wokovu, ujio wa mara ya pili, n.k. Utimilifu huu unajulikana, bali sula la muda ni mbeleni na halijulikani. Tumaini mara nyingi lilihusiana na "imani" na "upendo" (kama vile 1 Kor. 13:13; 1 The. 1:3; 2 The. 2:16). Orodha ya muda ya baadhi ya matumizi ya Paulo ni:

1. Ujio wa mara ya pili, Gal. 5:5; Efe. 1:18; 4:4; Tit. 2:13
2. Yesu ni tumaini letu, 1 Tim. 1:1 (Mungu ni tumaini letu, 1 Tim. 5:5; 1 Pet. 3:5)
3. Waamini kuwasilishwa mbele ya Mungu, Kol. 1:22-23; 1 The. 2:19
4. Tumaini likewekwa mbinguni, Kol. 1:5
5. Imani katika injili, Kol. 1:23; 1 The. 2:19
6. Hatma ya wokovu, Kol. 1:5; 1 The. 4:13; 5:8
7. Utukufu wa Mungu, Rum. 5:2, 2 Kor. 3:12; Kol. 1:27
8. Wokovu wa watu wa mataifakupitia Kristo, Kol. 1:27
9. Uhakika wa wokovu, 1 The. 5:8
10. Maisha ya milele, Tit. 1:2; 3:7
11. matokeo ya ukomavu wa Mkristo, Rum. 5:2-5
12. ukombozi wa uumbaji wote, Rum. 8:20-22
13. kukubali utimilifu, Rum. 8:23-25
14. wadhifa wa Mungu, Rum. 15:13

15. shauku ya Paulo kwa waamini, 2 Kor. 1:7

16. agano la Kale kama mwongozo wa waamini wa Agano Jipya, Rum. 15:4

**2:27 "kuzimu"** Hili ni neno la Kiyunani kwa ajili ya sehemu inayowahifadhi wafu. Linaelekeana na neno la Kiebrania *Sheol* katika Agano la Kale. Katika agano la Kale maisha baada ya kifo lilielezwa kwa angalizo la uwepo familia ya mtu, lakini hapakuwepo na furaha au ushirika. Ufunuo endelevu pekee wa Agano Jipya kwa uwazi zaidi unaelezea maisha baada ya kifo (yaani mbinguni na kuzimu)

### **MADA MAALUM: Wafu Wako Wapi?**

Paulo alilitumia neno hili mara nyingi kwa namna tofauti lakini katika maana zinazoshabihiana. Mara nyingi lilihusiana na utimilifu wa imani ya waamini (mfano 1 Tim. 1:1). Hili laweza kuellezwa kama utukufu, maisha ya milele, hatma ya wokovu, ujio wa mara ya pili, n.k. Utimilifu huu unajulikana, bali sula la muda ni mbeleni na halijulikani. Tumaini mara nyingi lilihusiana na "imani" na "upendo" (kama vile 1 Kor. 13:13; 1 The. 1:3; 2 The. 2:16). Orodha ya muda ya baadhi ya matumizi ya Paulo ni:

1. Ujio wa mara ya pili, Gal. 5:5; Efe. 1:18; 4:4; Tit. 2:13
2. Yesu ni tumaini letu, 1 Tim. 1:1 (Mungu ni tumaini letu, 1 Tim. 5:5; 1 Pet. 3:5)
3. Waamini kuwasilishwa mbele ya Mungu, Kol. 1:22-23; 1 The. 2:19
4. Tumaini likewekwa mbinguni, Kol. 1:5
5. Imani katika injili, Kol. 1:23; 1 The. 2:19
6. Hatma ya wokovu, Kol. 1:5; 1 The. 4:13; 5:8
7. Utukufu wa Mungu, Rum. 5:2, 2 Kor. 3:12; Kol. 1:27
8. Wokovu wa watu wa mataifakupitia Kristo, Kol. 1:27
9. Uhakika wa wokovu, 1 The. 5:8
10. Maisha ya milele, Tit. 1:2; 3:7
11. matokeo ya ukomavu wa Mkristo, Rum. 5:2-5
12. ukombozi wa uumbaji wote, Rum. 8:20-22
13. kukubali utimilifu, Rum. 8:23-25
14. wadhifa wa Mungu, Rum. 15:13
15. shauku ya Paulo kwa waamini, 2 Kor. 1:7
16. agano la Kale kama mwongozo wa waamini wa Agano Jipya, Rum. 15:4

▣ **"wala hutamtoa mtakatifu wako aone uharibifu"** Hii ilikuwa nukuu ya wazi ya ki-Masihi iliyohusiana na kifo, na sio uharibifu wa ahadi, wa mapakwa mafuta, aliye Mtakatifu (kama vile Zab. 49:15 na 86:13).

**2:28 "utanijaza furaha kwa uso wako"** Kifungu hiki kinadokeza uzoefu binafsi, wenye furaha na Baba (matendo 2:22-28) mbinguni kwa njia ya kifo cha Masihi (kama vile Isa. 53:10-12). Mtazamo huu chanya wa ushirika binafsi tukiwa na Mungu katika maisha baada ya kifo umenukuliwa katika Ayubu 14:4-15; 19:25-27.

### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 2:29-36**

<sup>29</sup> Waume, ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo. <sup>30</sup> Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapa kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi; <sup>31</sup> yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu. <sup>32</sup> Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake. <sup>33</sup> Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia. <sup>34</sup> Maana Daudi

**hakupanda mbinguni; bali yeye mwenyewe anasema, Bwana alimwambia Bwana wangu, Keti upande wa mkono wangu wa kuume.<sup>35</sup> Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako.<sup>36</sup> Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo.**

**2:29-31** Sio rahisi kwa viongozi wa sasa wa ki-Magharibi kuufuatisha uchunguzi wa Petro wa Zaburi hii kwa sababu anatumia utaratibu wa kanuni za ufasiri wa kiuhalimu wa dini ya Kiyahudi (hili pia ni la kweli kwenye kitabu cha Waebrania). Yawezekana Petro alisikia ubishi huu ndani ya hekelu kwa ajili ya ujio wa Measihi na sasa inajulikana inarejea kwa Yesu wa Nazareti

**2:29** Petro anaonyesha kuwa Zaburi 16, ingawa kwa namna Fulani inarejelea kwa Daudi (hasa 16:10b), moja kwa moja haiwezi kurejelea kwa Daudi.

**2:30 "kwa kuwa ni nabii"** Wayahudi waliamini kuwa Mungu alizungumza kupitia manabii. Musa anaitwa nabii (kama vile Kumbu. 18:18). Vitabu vya Agano la Kale Yohua, Waamuzi, 1 na 2 Wafalme na 1 na 2 Samweli vilijulikana katika sheria za kanisa kama "manabii wa awali." baada ya kifo cha nabii wa mwisho, Malaki, walimu wa dini ya Kiyahudi walifikilia kama ufunuo umekoma. Ilikuwa katika maana hii ya neno la Kiyahudi (yaani, mwandishi wa andiko) kuwa Daudi alifikiliwa kuwa nabii. Mapema katika Agano la Kale Mungu alikwisha jidhahilisha kwa Musa (kama vile Mwanzo 49) kuwa Masihi angalikuja toka katika kabila la Yuda. Katika 2 Samwel 17 Mungu anadhahilisha kuwa angalitoka katika uzao wa kifalme wa Daudi. Katika Zaburi 110 zaidi Mungu anajidhahilisha kuwa pia angalitoka katika uzao wa kikuhani wa Melchizedeki (kama vile Mdo. 2:34-35)

▣ **"akijua ya kuwa Mungu amemwapa kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi"** Huu ni muhtasari au nukuu zilizotungwa pamoja kwenye 2 Sam. 7:1 1 -1 6; Zab. 89:3-4; or 1 32:1 1 . Hii inaonyesha kuwa kusudi la kale la Mungu lapasa litimilizwe katika Yesu wa Nazareti. Kifo chake na ufufuko haukuwa na mpango B, lakini ni maamuzi ya kabla ya Mungu, ni mpango wake wa uumbaji wa kabla wa ukombozi (kama vile Efe. 2:1 1 -3:1 3).

**2:31 "Kristo"** Hii ni tafasiri ya Kiyunani ya neno "Masihi" au kiuhalisia "Mpakwa mafuta." Sio tu kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Daudi, Mfalme wa Israel, bali Mwana wa Mungu na amekaa katika kiti cha Enzi (kama vile Zaburi 110).

## **MADA MAALUM: MASIHI**

Ugumu katika kutafasiri neno hili ni kwa sababu ya matumizi tofauti kuhusiana na neno lenyewe "Masihi" au "aliyetiwa mafuta" (BDB 603, KB 645). Neno lilitumika katika kumwekea mtu mafuta maalumu kuonyesha wito wa Mungu na kumkabidhi majukumu ya uongozi.

1. Lilitumika kwa wafalme wa Kiyahudi (mf. 1 Sam. 2:10; 12:3; 24:6, 10; 2 Sam. 19:21; 23:1; Zab. 89:51; 132:10, 17; Wim. 4:20; Hab. 3:13; "Malkia mtiwa mafuta" katika Dan. 9:25)
2. Lilitumika kwa makuhani wa Kiyahudi (yaani, "makuhani walitiwa mafuta," Kut. 29:7; mf. Law. 4:3, 5, 16; 6:15; 7:36; 8:12; bila shaka Zab. 84:9-10; na 133:2)
3. Lilitumika kwa makasisi, na Manabii (kama vile. Mwa. 26:7; 1 Nya. 16:22; Zab. 105:15, iliyomaanisha watu wa Agano kwa pamoja; yumkini Hab. 3:13)
4. Lilitumika kwa manabii (kama vile. 1 Fal. 19:16; yumkini 1 Nya. 29:22)
5. Lilitumika juu ya Koreshi (kama vile. Isa. 45 :1)
6. # 1 na # 2 umeunganishwa katika Zab. 110 na Zekaria 4.
7. Lilitumika kwa ujio maalumu wa Mungu, Ufalme wa Daudi kuleta enzi mpya ya haki
  - a. uzao wa Yuda (kama vile. Mwanzo 49:10)
  - b. nyumba ya Yesse (kama vile. 2 Sam 7)

c. utawala wa ulimwengu (kama vile. Zaburi 2; Isa. 9:6; 11:1-5; Mik. 5:1- 4 na kuendelea)

d. Huduma kwa wahitaji (kama vile Isa. 61:1-3)

Mimi binafsi nimevutiwa na utambulisho wa neno "aliyetiwa mafuta" na Yesu wa Nazareti (kama vile. Yn. 1:41; 4:25) kwa sababu

1. kutambulishwa kwa ufalme wa milele katika Danieli 2 kipindi cha utawala wa nne
2. kutambulishwa kwa "mwana Adamu" katika Dan. 7:13 akipewa ufalme wa milele
3. maneno ya ukombozi wa Dan. 9:24, ambayo yanaashiria mwisho wa historia ya ulimwengu ulioanguka
4. matumizi ya Yesu ya kitabu cha Danieli katika Agano Jipya (kama vile Mt. 24:15; Marko 13:14)

Lazima kukiri kuwa hii ni mada nadra katika Agano la Kale, bila shaka Dan. 9:25. Lazima pia ifahamike kuwa Yesu haingii sana katika maelezo ya jumla kuhusu Masihi katika Agano la Kale

1. hakuwa kiongozi katika Israeli
2. hakutiwa mafuta rasmi na kuhani
3. sio kama mwokozi wa Israeli
4. sio tu "mwana wa Adamu" lakini kwa mshangao "Mwana wa Mungu"

▣ **"kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu"** Hili halikuondolewa kama nukuu ya Agano la Kale katika andiko la NASB (lililoboreshwa) 1995. kwa wazi kabisa inarejelea KWA Zaburi 16. Kwa ajili ya neno "mwili" angalia Mada Maalum hapa chini

### **MADA MAALUM: MWILI (*sarx*)**

Neno hili limetumiwa mara kwa mara na Paulo kwa Wagalatia na makuzi yake kithiolojia katika Warumi. Wasomi wana tofautiana juu ya namna gani dokezo la maana ya maneno haya ibainishwe. Kuna uhakika wa baadhi ya mipishano katika maana. Lifuatalo ni jaribio tu la kunukuu uwanja mpana wa maana ya neno.

- A. mwili wa binadamu, Yohana 1:14; Rum. 2:28; 1 Kor. 5:5; 7:28; 2 Kor. 4:11; 7:5; 12:7; Gal. 1:16; 2:16,20; 4:13; Flp. 1:22; Col. 1:22,24; 2:5; 1 Tim. 3:16
- B. kushuka kibinadamu, Yohana 3:6; Rum. 1:3; 4:1; 9:3,5,8; 11:14; 1 Kor. 10:18; Gal. 4:23,29
- C. mwanadamu, Rum. 3:20; 7:5; 8:7-8; 1 Kor. 1:29; 2 Kor. 10:3; Gal. 2:16; 5:24
- D. kuzungumza kibinadamu, Yohana 8:15; 1 Kor. 1:26; 2 Kor. 1:12; 5:16; 10:2; Gal. 6:12
- E. udhaifu wa kibinadamu, Rum. 6:19; 7:18; 8:5-6,9; 2 Cor. 10:4; Gal. 3:3; 5:13,16,19-21; Kol. 2:18
- F. ghasia ya wanadamu kumwelekea Mungu, inayohusiana na matokeo ya Anguko, Rum. 7:14; 13:14; 1 Kor. 3:1,3; Efe. 2:3; Kol. 2:18; 1 Petr. 2:11; 1 Yohana 2:16

Inasisitizwa ya kwamba "mwili" hautazamwi kama uovu katika Agano Jipya, ni katika fikira za Kiyunani. Kwa wanafalsafa wa Kiyunani "mwili" ulikuwa chanzo cha matatizo ya wanadamu; kifo kilimweka huru mtu kutoka kwenye matakwa yake. Lakini katika Agano Jipya, "mwili" ni uwanja wa mgogoro wa mapambano ya kiroho (kama vile. Efe. 6:10-18), tena usio na upande. Mwingine anaweza kutumia umbile lake la mwili kwa mazuri au mabaya.

**2:32-33 "Yesu. . Mungu. . Roho"** Ingawa neno "Utatu" kamwe halitumiki ndani ya Biblia, dhana ya Mungu wa Utatu inahitajika kwa (1) Uungu wa Yesu na (2) hali ya nafsi ya Roho. Biblia inawasilisha dhana hii kwa kutaja nafsi tatu za utatu katika mazingira ya aina moja (kama vile Mdo. 2:32-33; Mt. 28:19; 1 Kor. 12:4-6; 2 Kor. 13:14; 13:14; Efe. 4:4-6 na 1 Pet. 1:2).

### **MADA MAALUM: UTATU**

Angalia kazi za watu hawa wote watatu katika mazingira ya pamoja. Neno "utatu," kwanza lilibuniwa na

Tertallian, sio neno la Kibiblia, lakini dhana yake imesambaa sana.

- A. Injili
  - 1. Mt. 3:16-17; 28:19 (na nyingine zinazoendana nazo)
  - 2. Yohana 14:26
- B. Matendo-Mdo. 2:32-33, 38-39
- C. Paulo
  - 1. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
  - 2. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
  - 3. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
  - 4. Gal. 4:4-6
  - 5. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6
  - 6. 1 The. 1:2-5
  - 7. 2 The. 2:13
  - 8. Tit. 3:4-6
- D. Petro – 1 Pet. 1:2
- E. Yuda-kur. 20-21

Uwingi wa Mungu umedokezwa katika Agano la Kale

- A. Matumizi ya uwingi kumhusu Mungu
  - 1. Jina Elohim liko katika wingi (angalia mada maalumu: majina ya Uungu), lakini linapotumika kumhusu Mungu mara zote unakuta lina kitenzi kilichoko katika umoja.
  - 2. “Sisi” katika Mwa. 1:26-27; 3:22; 11:7
- A. “Malaika wa Bwana” (angalia mada maalumu: Malaika wa Bwana) alikuwa mwakilishi wa Uungu aliyeonekana
  - 1. Mwanzo 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16
  - 2. Kutoka 3:2,4; 13:21; 14:19
  - 3. Waamuzi 2:1; 6:22-23; 13:3-22
  - 4. Zakaria 3:1-2
- B. Mungu na Roho wake ni nafsi tofauti, Mwa. 1:1-2; Zab. 104:30; Isa. 63:9-11; Ezek. 37:13-14
- C. Mungu (YHWH) na Masiha (Adonai) nao ni nafsi tofauti, Zab. 45:6-7; 110:1; Zak. 2:8-11; 10:9-12
- D. Masihi na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, Zak. 12:10
- E. Wote watatu wametajwa katika Isa. 48:16; 61:1

Uungu wa Yesu na nafsi/haiba ya Roho vimesababisha matatizo kwa uhalisia, kwa wale wanaamini uwepo wa Mungu mmoja (angalia mada maalumu: wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja), kwa waumini wa awali

- 1. Tertellian-ilimshusha Mwana kwa Babaye
- 2. Origin-aliishusha nafsi ya Uungu wa Mwana na Roho
- 3. Arius-anaukana Uungu wa Mwana na Roho
- 4. Watawa-waliamini katika ufanisi wa udhahiri wa matukio ya Mungu mmoja kama Baba, Mwana, na Roho

Utatu ni kanuni anzilishi ya kihistoria iliyoelezewa na maneno ya Kibiblia.

- 1. Uungu kamili wa Yesu, ambao ni sawa na wa Baba, ulithibitishwa katika mwaka wa 325 B.K na baraza la Nicea (kama vile Yoh.1:1; Fil. 2:6; Tit. 2:13)
- 2. Nafsi kamili na Uungu wa Roho ambao ni sawa na wa Baba na Mwana ulithibitishwa katika mwaka 381 B.K na baraza la Konstantino
- 3. Mafundisho ya Uungu yameelezwa kiundani katika kazi ya Augustine De Trinitate

Hakika kuna muujiza hapa. Lakini Agano Jipya linathibitisha nafsi moja ya Kiuungu (wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja) ikiwa na udhahiri wa nafsi tatu za umilele (Baba, Mwana, na Roho)

**2:32 "Yesu huyo Mungu alimfufua"** Angalia maelezo kamili katika Mdo.2:24.

▣ **"na sisi sote tu mashahidi wake"** Hili linawarejelea wale wote waliomwona Kristo aliyefufuka. Angalia jedwali la Yesu kuwatokea baada ya kufufuka toka kwa Paul Barnett, *Jesus and the Rise of Early Christianity*, uk. 185, katika Mdo. 1:3 (uk. 9).

**2:33 "mkono wa kuume wa Mungu"** Hii ni sitiari ya Mungu kuzungumzwa kama mwanadamu kwa ajili ya nafasi ya nguvu, mamlaka, na kusihi (kama vile 1 Yn 2:1 ), ilichukuliwa toka Zab. 110:1 (lililonukuliwa zaidi ya Zaburi zingine katika Agano Jipya) au Zab. 118:16. Mungu ni Roho wa Milele, iliyokuwepo wakati wote wa uumbaji kimwili na kiroho. Wanadamu wanalazimishwa kutumia lugha ya dunia iliyoungana pamoja na mawazo ya kumunena Yeye, lakini vyote (1) vimekanushwa (2) vinafanana au (3) sitiari. Hata neno lenyewe "Baba" kumwelezea Mungu au "Mwana" kumwelezea Yesu ni la ki-sitiari. Sitiari zote zinaharibika katika baadhi ya hoja. Zinamaanisha kuelezea ukweli wa ndani au wazo kuhusu Uungu. Uwe mwangalifu kwenye uhalisia! Hakika hutarajii kuona mtu mzee, kijana juu ya kiti cha Enzi na ndege mweupe akiwa amemzunguka utakapofika mbinguni. Angalia Mada Maalum ifuatayo.

### **MADA MAALUM: MUNGU KUELEZWA KAMA MWANADAMU (lugha ya kibinadamu)**

- I. Aina hii ya lugha (yaani., Uungu kuelezewa katika maneno ya kibinadamu) ni wa kawaida katika Agano la Kale (baadhi ya mifano)
  - A. Viungo vya mwili
    1. Macho - Mwa. 1:4,31; 6:8; Kut. 33:17; Hes. 14:14; Kumb. 11:12; Zak. 4:10
    2. Mikono – Kut. 15:17; Hes. 11:23; Kumb. 2:15
    3. Viganja – Kut. 6:6; 15:16; Kumb. 4:34; 5:15
    4. Masikio – Hes. 11:18; 1 Sam. 8:21; 2 Fal. 19:16; Zab. 5:1; 10:17; 18:6
    5. Uso – Kut. 33:11; Law. 20:3,5,6; Hes. 6:25; 12:8; Kumb. 31:17; 32:20; 34:10
    6. Vidole – Kut. 8:19; 31:18; Kumb. 9:10; Zab. 8:3
    7. Sauti – Mwa. 3:9,11,13; Kut. 15:26; 19:19; Kumb. 26:17; 27:10
    8. Miguu – Kut. 24:10; Ezek. 43:7
    9. Umbo la mtu – Kut. 24:9-11; Zaburi 47; Isa. 6:1; Ezek. 1:26
    10. Malaika wa Bwana – Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:4,13-21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22
  - B. Matendo ya mwili (angalia mifano)
    1. Kuongea kama moja ya mfumo wa uumbaji- Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24,26
    2. Kutembea (yaani., sauti ya)- Mwa. 3:8; Law.26:12; Kumb. 23:14; Hab. 23:14
    3. Kufunga mlango wa safina ya Nuhu – Mwa. 7:16
    4. kunukia dhabihu – Mwa. 8:21; Law. 26:31; Amo. 5:21
    5. kurudi chini – Mwa. 11:5; 18:21; Kut. 3:8; 19:11,18,20
    6. maziko ya Musa – Kumb. 34:6
  - C. Mihemuko ya kibinadamu (baadhi ya mifano)
    1. Majuto/toba- Mwa. 6:6,7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:29,35; Amo. 7:3,6
    2. Hasira- Kut. 4:14; 15:7; Hes. 11:10; 12:9; 22:22; 25:3,4; 32:10,13,14; Kumb. 6:15; 7:4; 29:20
    3. Wivu - Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15; 32:16,21; Yosh. 24:19
    4. Karaha/chuki- Law. 20:23; 26:30; Kumb. 32:19
  - D. Maneno ya kifamilia (baadhi ya mifano)
    1. Baba
      - a. Wa Israel- Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 31:9; Hos. 11:1
      - b. Wa Wafalme- 2 Sam. 7:11-16; Zab. 2:7
      - c. Sitiari za vitendo vya kibaba- Kumb. 1:31; 8:5; 32:6-14; Zab. 27:10; Mith. 3:12; Yer. 3:4,22;

31:20; Hosea 11:1-4; Mal. 3:17

2. Mzazi – Hosea 11:1-4
3. Mama- Isa. 49:15; 66:9-13 (mshabihiano wa unyonyeshaji wa mama)
4. Kijana mpendwa mwaminifu-Hosea 1-3

II. Sababu za kutumia aina hii ya lugha

- A. Ni muhimu kwa Mungu kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu. Hakuna misamiati mingine kuliko ile ya maneno ya kiulimwengu, ulioanguka. Dhana iliyosambaa ya Mungu kuwa wa jinsia ya kiume ni mfano mmoja wa lugha ya kumwelezea binadamu kwa sababu Mungu ni Roho!
- B. Mungu anachukulia dhana ya maana halisi ya maisha ya mwanadamu na kuwatumia ili kujidhihirisha mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka (Baba, Mama, Wazazi, Wapendwa)
- C. Ingawa ni muhimu kwa wakati mwingine (yaani., Mwa. 3:8), Mungu hahitaji kuwekewa pingamizi kwa aina yeyote juu ya umbo la kibinadamu (kama vile Kut. 20; Kumbu. 5)
- D. Hatima ya Mungu kuelezewa kama mtu ni kubadilika kwa Yesu katika umbo la kibinadamu! Mungu akawa mtu, mwenye kugusika (kama vile Yohana 1:1-18).

- III. kwa umakinika wa maelezo, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, ukurasa 10, "Tabia ya mwanadamu kwa Mungu," katika *The International Standard Bible Encyclopaedia*, kurasa za. 152-154

▣ **"ahadi ya Roho Mtakatifu"** Agano la Kale liliahidi siku mpya ya haki ya kuongozwa na Roho, iliyowekwa itende kwa kazi ya Masihi.

1. Yohana 7:39, siku mpya imewadia
2. Gal. 3:1 4, Baraka za Abraham (kama vile Gen. 1 2:3) sasa zinapatikana katika ulimwengu wote
3. Efe. 1 :1 3, waamini katika nyakati hizi mpya wamepigwa muhuri na Roho.

▣ **"mnachokiona sasa na kukisikia"** Huu ni msisitizo endelevu katika hotuba hii juu ya asili ya mashuhuda wa macho ya wale waliosikia (nakala 1 4,22,32,33,36). Wanafahamu kile Petro alichosema kilikuwa ni kweli kwa sababu walikuwepo. Wanasheria wanaliita hili kama kiini cha ushahidi wa msingi.

**2:34 "Bwana alimwambia bwana wangu"** Hii ni nukuu toka Zaburi 110:1 (YHWH...Adon). Yesu analitumia katika Mt.22:41-46. Katika Agano Jipya inaonyesha dhana mbili za Ufalme,; Yesu tayari yupo katika haki ya Mungu, lakini maadui wake bado sio sehemu yake ya kuweka miguul. Angalia Mada Maalum: Ufalme Wa Mungu katika Mdo. 1 :3.

**2:36 "na nyumba yote ya Israel"** Hii inarejea kwenye uongozi wa Kiyahudi na watu, ule ambao Petro alikuwa akiuelezea. Anadai kuwa unabii wa Agano la Kale umekwisha timilika na kufikia kilele ndani ya Yesu wa Nazareti. Mada Maalum: Ufalme Wa Mungu katika Mdo. 1 :3.

**NASB "wajue kwa yakini"**

**NKJV "wajue hakika"**

**NRSV "wajue wakiwa na hakika"**

**TEV "wajue kwa uhakika"**

**NJB "yawezakuwa yakini"**

Hili linaaksi maneno mawili ya Kiyunani, kielezi *aphalōs*, kinachomaanisha "kukaza kwa uhakika" (ki-sitari kukiwa na uhakika, kama vile Mdo.16:23) na kauli shurutishi ya wakati uliopo ya *ginōskō*, "kufahamu." Waha mashuhuda wa macho wa wiki ya mwisho ya Yesu, kifo, na ufufuko wasingalikuwa na mashaka kuhusu ukweli wa maneno ya Petro.

▣ **"Bwana na Kristo"** Neno "bwana" (*kurios*) laweza kutumika katika maana ya ujumla au katika maana maalum ya kithiolojia (kama vile Mdo. 2:21 ). Laweza kumaanisha "bwana," "mzee," "Mkuu wa kaya," "mmiliki," "mme," au



"Mungu-Mtu kamili." Matumizi ya Agano la Kale ya neno hili (*adon*) lilitoka kwa Wayahudi wazembe wenye kushindwa kutamka jina la agano la Mungu, YHWH, toka kitenzi cha Kiebrania "kuwa" (kama vile Kut. 3:1-4). Walikuwa wakiogopa kuvunja sheria iliyosema "usilitaje jina la Mungu wako bure" (kama vile Kut. 20:7, Kumb. 5:1-1). Walifikiri kama wasipolitaja, wasingaliweza kulitamka bure. Kwa hiyo, walitumia neno mbadala *adonai*, lililokuwa na maana sawa na neno la Kiyunani, *Kurios* (Bwana). Waandishi wa Agano Jipya walilitumia neno hili kuelezea Uungu kamili wa Yesu. Kifungu "Yesu ni Bwana" ulikuwa ni ukiri wa wazi wa imani na kanuni ya kiubatizo ya kanidsa la mwanzo (kama vile Rum. 1 0:9-13; 1 Kor. 1 2:3; Fil. 2:1-1). Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika Mdo. 1:6. Neno "Kristo" lilikuwa neno la Kiyunani lenye kulingana na neno la Kiebrania *messiah*, lililomaanisha "mpakwa mafuta" (kama vile Mdo. 2:31, 36; 3:1 8,20; 4:26; 5:42; 8:5; 9:22; 1 7:3; 1 8:5,28; 26:23). Lilidokeza "mtu aliyeitwa na kuwezesha na Mungu kwa ajili ya kazi maalum." Katika Agano la Kale makundi matatu ya viongozi: makuhani, wafalme, na manabii walitiwa mafuta. Yesu alitimizwa haya makundi yote (kama vile Ebr. 1 :2-3). Angalia Mada Maalum: Masihi katika Mdo. 2:31. Kwa kutumia nyazifa zote tatu za Agano la Kale kwa ajili ya Yesu wa Nazareti, Luka anatetea Uungu wake wote (kama vile Flp. 2:6-11, angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:32) na u-Masihi wake (kama vile Luka 2:1-1). Hii inatengeneza hatua kwa ajili ya kutamka (*kerygma*) katika hotuba zingine kwenye Matendo ya Mitume! Angalia Mada Maalum: *Mafundisho* Ya Kanisa La Mwanzo katika Mdo. 2:14.

▣ **"Yesu huyo mliyemsulubisha"** Petro aliwashutumua hawa wakazi wa Yerusalemu waliokuwa ndumilakuwili juu ya kifo cha Yesu. Wanadamu wote walioanguka wanahusika sawa katika kulitenda kosa. Angalia maelezo katika Mdo. 2:23.

▣ **"huyo Yesu"** Usanifishaji wa neno "huyo Yesu" (kama vile 2:23,32,36) unahusianisha tamko la Petro la Kristo aliyeinuliwa, Yesu wa kihistoria kwenye ufufuko. Dhana zote ni kweli. Hakuna utofauti wa kibiblia kati ya Yesu Yule wa mwanzo na Yesu wa imani!

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 2:37-42**

<sup>37</sup> Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu? <sup>38</sup> Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. <sup>39</sup> Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjje. <sup>40</sup> Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, Jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. <sup>41</sup> Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu. <sup>42</sup> Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.

**2:37 "wakachomwa mioyo yao"** Hili ni neno la Kiyunani *kata* likiongezeka na neno *nussō*. Mzizi wa neno umetumika katika Yohana 1 9:34 kwa ajili ya Yesu kuangikwa pale msalabani. Ujumbe wa Petro uliwaangika wale wasikiaji pale msalabani kwenye ukweli wa injili. Inavyoonekana unarejelea kwenye badiliko muhimu la Roho Mtakatifu aliyeutangulia wokovu (kama vile Yn 1 6:8-11; Rum. 3:21-31).

**2:38 "Tubuni"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita, ikimaanisha maamuzi muhimu. Neno la Kiebrania kwa ajili a toba linamaanisha kubadili tabia. Neno la Kiyunani kubadili mawazo. Toba ni matakwa ya badiliko. Haimanishi kuacha dhambi moja kwa moja, bali shauku ya kumpendeza Mungu, na sio mtu mwenyewe. Kama mwanadamu aliyeanguka tunaishi kwa ajili yetu wenyewe, lakini kama waamini tunaishi kwa ajili ya Mungu! Toba na imani ni mahitaji ya Mungu kwa ajili ya wokovu (kama vile Mk 1 :15; Mdo. 3:16, 19; 20:21). Yesu akasema "msipotubu, mtaangamia" (kama vile Luka. 1 3:3,5). Toba ni mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka (kama vile 2 Pet. 3:9, Ezek. 1 8:23, 30, 32). Siri ya ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu kwa wazi yaweza kuonyeshwa kwa toba kama sharti la wokovu. Hata hivyo, fumbo au jozi ya upembuzi ni kuwa pia ni zawadi ya Mungu (kama vile Mdo. 5:31; 1 1 :18 na 2 Tim. 2:25). Mara nyingi pana mvutana katika uwasilishaji wa

kibiblia wa neema iliyoanzishwa na Mungu na mwitikio wa kimaagano uliohitajika kwa mwanadamu. Agano Jipya, kama lilivyo Agano la Kale, lina muundo wa "kama.....kwa hiyo."gano Jipya ambayo yanahusiana na dhana ya toba.

## **MADA MAALUM: TOBA (AGANO LA KALE)**

Dhana hii ni ya muhimusana lakini ni vigumu kuitolea ufafanuzi. Wengi wetu tunao ufafanuzi ambao unatokana na ushirikishwaji wa kimadhehebu. Hata hivyo, mara nyingi huu "mwelekeo" wa ufafanuzi wa kithiolojia unalazimisha maneno kadhaa ya Kiebrania (na Kiyunani) amabayo kwa upekee wake hayamaanishi "elekea" ufafanuzi huu. Lazima ikumbukwe kwamba waandishi wa kitabu cha Agano la Kale (isipokuwa Luka) walikuwa wanafikra wa Kiebrania waliotumia maneno ya lugha ya Koine ya Kiyunani, hivyo sehemu ya kuanzia ni ile ya maneno yenyewe ya Kiebrania, ambayo kimsingi ni mawili.

1. *nacham* ( BDB 636, KB 688)
2. *shub* ( BDB 996, KB 1427)

Neno la kwanza, *nacham*, kiuhalisia linaonekana kumaanisha "kueleza pumzi ya ndani" linatumika katika maana kadhaa.

- a. "kupumzika" au "kufariji" (m.f. Mwa. 5:29; 24:67; 27:42; 37:35; 38:12; 50:21; mara nyingi linatumika katika majina, kama vile 2 Fal. 15:14; 1 Nya. 4:19; Neh. 1:1; 7:7; Nahumu 1:1)
- b. "kuhuzuka" (m.f. Mwa. 6:6,7)
- c. "kughairi" (m.f. Kut. 13:17; 32:12,14; Num. 23:19; Ayubu 42:5-6)
- d. "huruma" (m.f. Kut. 32:36)

Tambua kwamba haya yote yanahusisha hisia za ndani! Hapa ndipo palipo na ufubuzi: hisia za ndani ambazo huelekea katika tendo. Badiliko hili la tendo mara kwa mara huelekezwa kwa watu wengine, lakini pia kuelekea kwa Mungu. Ni hili badiliko la mtazamo na tendo kumwelekea Mungu ambalo hukazia neno hili kwa umuhimu huu wa kithiolojia. Lakini hapa ungalifu lazima ufanyiwe kazi. Mungu anasemekana "kutubu" (kama vile Mwa. 6:6, 7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:11, 35; Zab. 106:45), lakini hili si matokeo ya sononeko juu ya dhambi au makosa, bali ni njia ya kiaandiko ya kuonyesha huruma ya Mungu na uangalifu (kama vile Hes. 23:19; 1 Sam. 15:29; Zab. 110:4; Yer. 4:27-28; Eze.24:14). Adhabu istahiliyo dhambi na uasi inasamehewa ikiwa mtenda dhambi ameamua kwa usahihi kuongoka kutoka dhambini kwake/kwao na kurudi kwa Mungu. Huu ni uthamanisho mpya wa maisha.

Neno la pili, *shub*, linamaanisha "kurudi" (kurudi kutoka, kurejea, kurudi kwa). KITENZI *shub* (BDB 996, KB 1427) kimsingi kinamaanisha "kugeuka" au "kurejea tena" Kitenzi hiki kinaweza kutumika kwa

1. kumuelekea Mungu, Hes. 14:43; Yos. 22:16,18,23,29; Amu. 2:19; 8:33; 1 Sam. 15:11; 1 Fal. 9:6; Yer. 3:19; 8:4
2. kumrudia Mungu, 1 Fal. 8:33,48; 2 Nya. 7:14; 15:4; 30:9; Zab. 51:13; 116:7; Isa. 6:10; 10:21,22; 31:6; Yn. 4:6,8-11 (tambua hasa Yeremia 7 na Amosi 4)
3. YHWH anamwambia Isaya hapo awali kwamba Yuda haitaweza/isingeweza kutubu (kamavile Isa. 6:10), lakini si mara ya kwanza katika kitabu hiki, Yeye anawahita warudi Kwake.

Toba si hisia nyingi sana kama ulivyo mtazamo kumwelekea Mungu. Huu uthamani mpya wa maisha kutoka upekee kuelekea Kwake. Hii inadokeza utayari wa kubadilika na kubadilishwa. Si ukomavu kamili kuihusu dhambi, bali ukomavu wa uasi unaojulikana! Huu ni ukinyume wa matokeo yaliyo kitovu Anguko la Mwanzo 3. Hiii inadokeza kwamba sura na ufanano wa Mungu (Mwa. 1:26-27), ingawa iliharibika, umerejeshwa! Ushirika pamojana Mungu kupitia mwanadamu aliyeanguka inawezakana kurejeshwa tena.

Toba katika Agano la Kale kimsingi inamaanisha "badiliko la tendo," ambapo "toba" katika Agano Jipya inamaanisha "badiliko la fikra" (tazama Mada Maalum: Toba [AJ]). Yote haya ni muhimu kwa ajili ya toba ya kweli ya kibiblia. Pia ni muhimu kutambua kwamba toba ni vyote tendo la awali na hatua endelevu. Tendo la awali linawezakuonekana katika Marko 1:15; Matendo ya Mitume 3:16 na 19; 20:21, ambapo hatua endelevu inaweza kuonekana katika 1 Yohana 1:9; Ufunuo 2 na 3. Toba si uchaguzi (kama vile Luka 13:3,5)!

Ikiwa ni kweli kwamba mahitaji ya maagano mawili ni "toba" na "imani" (m.f. Mt. 3:2; 4:17; Maro 1:4,15; 2:17; Luka 3:3,8; 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3), kisha neno *nachamr* linarejea juu ya hisia zenye nguvu za kutambaua dhambi ya mtu na kugeuka kutoka ndani ya hiyo dhambi, ambapo neno *shub* lingaliweza kurejea juu ya kurudi toka dhambini na kumwelekea Mungu (moja ya mfano wa haya matendo ya kiroho uko katika Amosi 4:6-11, "hamkunirudia mimi" [mara tano] ana Amosi 5:4,6,14, "Nitafuteni mimi. . .Mtafuteni Bwana. . .Tafuteni mema, wala si mabaya").

Mfano wa kwanza ulio mkuu wa nguvu ya toba ni ile dhambi ya Daudi's sin with Bathsheba (kama vile 2 Samuel 12; Zaburi 32,51). Kulikuwa na matokeo endelevu kwa Daudi, familia yake, na Israeli, lakini Daudi alirejeshwa katika ushirika pamoja na Mungu! Hata Manase aliyekuwa dhalimu aliweza kutubu na kusamehewa (kama vile 2 Nya. 33:12-13).

Maneno yote haya yanatumika kwa usawa katika Zab. 90:13. Lazima kuwepo na utambuzi wa dhambi na nia iliyokusudiwa, kurudi kwa mtu binafsi kuto dhambini, pamoja na shauku ya kumtafuta Mungu na haki Yake (kama vile Isa. 1:16-20). Toba ni hatua tambuzi, hatua binafsi, na hatua ya kimaadili. Haya yote yanahiajika, yote ni kwa ajili ya kuanza uhusiano mpya pamoja na Mungu na kuushikilia uhusiano huo mpya. Hisia za ndani za majuto hurejesha ndani ya utele wa uaminifu kwa Mungu na kwa ajili ya Mungu!

▣ **"mkababatizwe"** Hii ni kauli nyingine tendwa shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Angalia Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUM: UBATIZO

- I. Ubatizo katika maisha ya Kiyahudi
- II. Ubatizo ulikuwa utaratibu wa kawaida miongoni mwa Wayahudi wa karne ya kwanza nay a pili.
  1. maandalizi ya kuabudu hekaluni (yaani, utatibu wa kujitakasa)
  2. ubatizo wa kujibatiza mwenyewe kwa kubadili dini  
Ikiwa mtu aikuwa na histori ya kuwa mtu wa Mataifa ilimlazimu kuwa mtotokamili wa Israeli, huyu ilimpsa kutimiza majukumu matatu:
    - a. tohara, ikiwa nimwanamume
    - b. kujibatiza mwenyewe kwa kuzama majini, katika uwepo wa mashahidi watatu
    - c. dhabihu ndani ya Hekalu
  3. Tendo la utakaso (kama vile Mambo ya Walawi 15)

Iakundi ya kimadhehebu ya karne ya kwanza ya ki- Palestina, kama vile Essenes, kwa uwazi kabisa ubatizo lilikuwa jambo la kawaida, zoezi lililorudiwa rudiwa. Hata hivyo, to kuifanya dini ya kiyahudi iwe rasmi, Ubatizo wa Yohana wa toba ungeweza kuwa wa ungemnyenyekeza mtoto wa asili kuyafanya Mataifa kuzikubali taratibu hizi.

1. baadhi ya vigezo vya kitabu cha Agano la kale vinaweza knukuliwa vinaweza kuonekana kupitia sherehe

za kuosha

2. Kama taratibu za zilivyofanywa na makuhani kwa ukawaida (kama vile Kutoka 19:10; Mambo ya Walawi16)

lazima itambuliwe kwamba batizo nyingine zote katika karne ya kwanza ya utaduni wa Kiyahudi zilikuwaq ni za kujiendesha zenyewe. Wito pekee wa Yohana Mbatizaji kwa ajili ya ubatizo ndiyo uliomhusisha yeye kama mtathimini (kama vile Mt. 3:7-12) na mwendehaji wa tendo hili la toba (kama vile Mt. 3:6).

### III. Ubatizo ndani ya Kanisa

#### A. Sababu za Kithiolijia

1. msamaha wa dhambi – ya Mitume 2:38; 22:16
2. upokeaji wa Roho Mtakatifu – Matendo ya Mitume 2:38 (Matendo ya Mitume 10:44-48)
3. ushirika pamoja na Kristo – Gal. 3:26-27
4. ushirika ndani ya kanisa – 1 Kor. 12:13
5. dalili za kurudi kwa roho – 1 Pet. 3:20-21
6. dalili za kifo cha kiroho na ufufuo – Rum. 6:1-5

B. Ubatizo ulikuwa fursa ya kanisa la kale kwa ajili ya ukiri wa umati wa watu (au ungamo). Huiu haukuwa/si kwa maana ya wokovu, bali tukio la ukili kwa maneno ya imani (yaani, bila shaka, "Yesu ni Bwana"). Kumbuka kanisa la kale halikuwa na majengo na hawa walikutana majumbani au walikutana katika maeneo ya maficho mara kwa mara kwa sababu ya kuteswa.

C. Watoa maoni wengi wamekuwa wakidai kuwa 1 Petro ni hotuba ya kiubatizo. Ijapokuwa hili linawezekana, huu si uchaguzi wa kipekee. Ni kweli kuwa Petro mara nyingi alitumia ubatizo kama tendo muhimu la imani (kama vile Matendo ya Mitume 2:38,41;10:47). Hata hivyo, hili lilikuwa/ ni tukio la kisakramenti, lakini tukio la imani, linaashiria mauti kuzikwa, na ufufuo kama mwamini atambuavyo kwa uzoefu wa mara kwa mara (kama vile Rum. 6:7-9; Kol. 2:12). Tendo ni la kiishara, si la kisakramenti; tendo ni tukio la ukiri, si kwa maana ya wokovu.

#### IV. Ubatizo na Toba katika Matendo ya Mitume 2:38

Curtis Vaughan, Kitabu cha Matendo ya Mitume kina tambuhi inayoshawishi katika uk p. 28 unahusiana na Matendo ya Mitume 2:38.

"Neno la Kiyunani la 'kubatizwa' ni nafsi ya tatu shurutishi; neno la 'kutubu,'ni nafsi ya pili shurutishi. Hii inabadilika moja kwa moja kutoka nafsi ya pili shurutishi hadi nafsi ya tatu ya chini ya moja kwa moja ya neno 'kubatizwa' linalomaanisha kwamba dai la msingi la Peto ni kwa ajili ya toba."

Hili linafuata ule msistizo wa Yohana Mbatizaji (kama vile Mt. 3:2) na Yesu (kama vile Mt. 4:17). Toba inaonekana kuwa ufunguzi wa kiroho na ubatizo uko nje ya sura ya madiliko hili la kiroho. Kitabu cha Agano Jipya hakifahamu lolote juu ya waamini wasiobatizwa! Kwa kanisa la kale ubatizo ulikuwa ungamo la imani ya wengi. Hili ni tukio la ungamo la imani ya walio wengi katika Kristo, si kwa maana ya wokovu! Inahitajika kukumbuka kwamba ubatizo hautajwi ndani ya hotuba ya pili ya Petro, ijapokuwa toba ipo (kama vile Matendo ya Mitume 3:19; Luka 24:17). Ubatizo ulikuwa mfano uliowekwa na Yesu (kama vile Mt. 3:13-18). Ubatizo uliamriwa na Yesu (kama vile Mt. 28:19). Swali la sasa la umuhimu wa ubatizo kwa ajili ya wokovu hauelezwi abu cha Agano Jipya; waamini wote wanatarajiwa kubatizwa. Hata hivyo, mtu lazima pia ajiulinde dhidi sifa ya kisakramenti! Wokovu ni suala la imani, si si sehemu ya haki, haki ya maneno, haki ya suala la utaratibu!

▣ **"katika jina la Yesu Kristo"** Hii ni nahau ya Kiebrania (iliyozalishwa toka Yoel 2:32) inayorejelea kwenye ubinadamu au tabia ya Yesu. Yawezakuwa kanuni ya mwanzo ya kiubatizo ya kanisa, yumkini iliyokuwa ikirudiwa na mtahiniwa, ilikuwa "naamini Yesu ni Bwana" (kama vile Rum. 10:9-13; 1 Kor. 1 :13,15). Hii ulikuwa ni

uthibitisho wa kithiolojia na uthibitisho wa mtu kuamini kibinafsi. Katika agizo kuu la Mt. 28:19-20 jina la Uungu ni kanuni ya kiubatizo. Tena tunalazimika kujilinda dhidi ya mbinu za ki-sakramenti! Cheo au kanuni sio kitu cha msingi, bali moyo wa Yule aliyebatizwa. Kwa ajili ya “Kristo” angalia Mada Maalum kwenye Mdo. 2:31

<b>NASB, NJB, NIV</b>	<b>"mpate ondoleo la dhambi zenu"</b>
<b>NKJV</b>	<b>"kwa ajili ya ondoleo la dhambi"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"kwamba dhambi zenu zisamehewe"</b>
<b>TEV</b>	<b>"kwamba dhambi zenu zipate kusamehewa"</b>

Swali la kithiolojia ni kwa namna gani neno “kwa ajili”(eis) linatenda kazi? Je neno msamaha linaambatanishwa na neno “tubu” au “mkabatizwe”? je neno msamaha ni tegemezi ya neno toba na/au ubatizo? Uwezekano wa kutumia neno eis ni wa namna nyingi. Utumiaji wa kawaida ni ule “kukiwa na mtazamo wa” au “kwa kusudi la.” Wasomi wengi wa ki-Baptist wanachagua neno “ kwa sababu ya” kwa minajili ya kithiolojia, lakini ni sababu iliyo ndogo. Mara nyingi dhahaniao zetu hata huweza kutenda kazi katika hatua ya upembuzi wa kisarafu. Lazima tuisababisha biblia iongee katika muktadha; baadaye angalia ufanano; baadaye utengeneze utaratibu wa kithiolojia. Wafasiri wote kihistoria, kimadhehebu, kiuzoefu wamewekewa masharti. Msamaha kupitia katika Kristo ni dhamira inayojirudia katika jumbe hizi katika Mdo. (yaani Petro 2:38; 3:1 9;5:31 ; 1 0:43; na Paulo 13:38).

▣ **"mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"** Hii ni kauli ya kati (shahidi) elekezi ya wakati ujao. Kipawa cha Roho Mtakatifu kilikuwa

1. Wokovu uliohakikiwa
2. Uwepo ulio ndani
3. Kuiwezesha huduma
4. Kuendeleza mfanano wa Kristo

Hatupaswi kulazimisha vipengere au mpangilio wa matukio ya wokovu kwa sababu mara nyingi yako tofauti katika Matendo ya Mitume. Kitabu cha Matendo hakikumaanisha kufundisha kanuni maalum au mtiririko wa kithiolojia (kama vile *How To Read the Bible for All Its Worth*, kur. 94-1 1 2), lakini weka kumbu kumbu kwa yale yaliotokea. Je ni lazima mfasiri atumie andiko hili kudai mtiririko matendo ya wokovu: tubu, mkabatizwe, msamaha, na baadaye kipawa cha Roho? Thiolojia yangu inadai Roho kuwa hai toka mwanzo (kama vile Yn 6:44,65) na kufanya muhimu yote kupitia mchakato wa badiliko na muhimu (kama vile Yn 1 6:8-1 2), toba (kama vile Mdo. 5:31 ;11 :18; 2 Tim. 2:25), na imani. Roho ni wa msngi na muhimu (kama vile Rum. 8:9) toka mwanzo hadi mwisho.

Bila shaka hawezi kuwa wa mwisho katika huo mtiririko! Moja ya kitabu kilichonisaidia kufunika mafundisho yangu ya kidini na kuiacha biblia iongee kwa nguvu ni F. F. Bruce, *Answers to Questions*. Ndani yake kinatengeneza maoni mbali mbali mazuri kuhusu matendo 2:38. Moja ya yale yaliyonivutia ni: "upokeaji huu wa roho waweza kuzoeleka hata kabla ya ubatizo (Mdo. 2:38), au baada ya ubatizo *kuongeza* na uwekewaji wa mikono ya kitume (Mdo.8:16;19:54)" (kur. 167).watu wa kisasa wanataka mafundisho yenye maelezo ya wazi yanayoweza kuthibitishwa, lakini mara zote yenye kutoa jawabu la njia ya utafasiri kwenye “uhakiki wa andiko” na kuyatenga yale tu maaandiko yenye kuufaa uelewa wao wa kabla, upendeleo (angalia semina juu ya utafasiri wa Biblia, [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org) )

**2:39 "ahadi ni kwenu na watoto wenu"** Huu ulikuwa ni ushirika wa Agano la Kale, vizazi vingi, dhana iliyozoeleka (kama vile Kut. 20:5-6 and Kumb. 5:9-1 0; 7:9). Imani ya watoto iliathiriwa na wazazi na ulikuwa ni wajibu wa wazazi (kama vile Kumb. 4:9; 6:6-7; 20-25; 1 1 :1 9; 32:46). Huu ushawishi wa ushirika pia ulikuwa na dhana ya uoga kutokana na Mt. 27:25 (“na damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu”). Ahadi ya ushawishi wa imani ya vizazi vingi ilinisaidia mimi kuamini kuwa Mungu atatumia imani yangu kushawishi, kubariki, na kulinda vizazi vyangu (kama vile Kumb. 7:9). Imani yangu na huduma ya kuaminika katika Kristo inaweza kuleta matokeo ya familia yangu na familia za wengine na kadhalika (kama vile Kumb.7:9).ni tumaini lenye kuleta faraja lililoje na ahadi ya kihamasa. Imani hupita mpaka kwenye familia! Katika Matendo ahadi (2:39) ya Mungu inajumuisha vipengere mbali mbali ikiwa na viunganishi vya Agano la Kale:

1. Msamaha wa dhambi– Mdo. 2:38; 3:19; 5:31 ; 10:43; 13:38-39; 26:18

2. wokovu – Mdo. 2:21 ; 4:12; 11:14; 13:26; 16:31
3. roho – Mdo. 2:38-39; 3:19; 5:32; 8:15-18; 10:44-48; 19:6
4. muda wa kuburudika – Mdo. 3:1 9

▣ **"kwa watu wote walio mbali"** Petroa anawahutubia Wayahudi. Kifungu hiki mwanzoni kabisa kilirejea kwa wale Wayahudi waliokimbilia uhamishoni ambao wangerudi katika nchi yao ya ahadi (kama vile Isa. 57:19). Hata hivyo, pia, katika baadhi ya sura, inaonekana kurejea kwa watu wa mataifa waliokuwa mbali na ufahamu wa YHWH (kama vile Isa. 49:1; Zak. 6:15). Habari njema ya injili ni kuwa Mungu mmoja wa kweli (yaani, imani ya Mungu mmoja) aliyewaumba wanadamu wote katika sura yake (kama vile Mwa. 1:26-27), ana shauku kuwa nao ushirika kwao wote (kama vile 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9). Hili ni tumaini la umoja wa wanadamu wote katika Kristo. Ndani yake hapana zaidi Myahudi-mtu wa mataifa, mtumwa wala aliye huru, mme-mke wote ni wamoja (kama vile Efe. 2:11-3:13). Paulo anatumia nukuu hii kuwaelezea watu wa mataifa katika Efe.2:13 na 17. Enzi mpya ya Roho imekwisha leta umoja usiotarajiwa!

## **MADA MAALUM: IMANI YA MUNGU MMOJA**

M wanadamu amehisi kuwa kuna ukweli zaidi kuliko ule wa kimaumbile (yaani, yanayoathiriwa na mambo yaliyo nje ya uwezo, kama vimbunga, mfumo wa kupatwa kwa jua au mwezi, kimondo, hali ya hewa, matukio, vifo, n.k.). Wataalamu wa Elimu ya Mwanadamu wanatwambia kuwa walivikuta vitu ndani ya makaburi ya kale ya hominoids ambavyo vilikuwa kwa ajili ya maisha ya baadaye, ambavyo vilionekana kama nyongeza ya maisha haya. Utamaduni wa kwanza ulioandikwa ulikuwa Sumer (Tigri ya kusini, Mto wa Eufrate), ulianza mnamo 10,000 - 8,000 K.K. Hawa waliandika mashairi kuyaeleza maoni yao ya miungu na ushirika wao. Kisha, zaidi ya hayo kama wanadamu na udhaifu wao. Mila zao zilianza kuwepo katika mtindo wa masimulizi marefu kabla ya wao kuandika.

Kulikuwa na kukua kwa theolojia kutokana na

1. imani juu ya vitu vyote ni hai
2. miungu wengi wa
3. mungu mkuu (au wa uwili)

Dhana ya "Mungu mmoja" (aliye mmoja na nafsi ya kwanza, Mungu wa maadili asiye na mahusiano ya mke), si "mungu mkuu" miungu wengi au mungu mzuri wa uwili w ki-Irani (Wafuasi wa Zoroaster, ni wa pekee kwa Israeli (Abrahamu na Ayubu, 2000 K.K.). Ni mmoja pekee huko Misri (Amenhotep IV, pia anajulikana kama Akhenaten, 1367-1350 au 1386-1361 K.K. AMBAYE ALIABUDU Atemi, mungu jua, kama mungu pekee). Tazama J. Assmann, *The Mind of Egypt*, kr. 216-217.

Dhana hii inaelezwa katika vifungu kadhaa ndani ya Agano la Kale.

1. "hakuna aliye kama HWH Elohim, wetu" Kut. 8:10; 9:14; Kumb. 33:26; 1 Fal. 8:23
2. "hapana mwingine zaidi Yake," Kumb. 4:35,39; 32:39; 1 Sam. 2:2; 2 Sam. 22:32; Isa. 45:21; 44:6,8; 45:6,21
3. "YHWH ni mmoja" Kumb. 6:4; Rum. 3:30; 1 Kor. 8:4,6; 1 Tim. 2:5; Yakobo 2:19
4. "hakuna aliye kama Wewe," 2 Sam. 7:22; Yer. 10:6
5. "Wewe ni Mungu wa pekee," Zab. 86:10; Isa. 37:16
6. "kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwepo mwingine," Isa. 43:10
7. "hapana mwingine; zaidi ya mimi. . .hapana mwingine," Isa. 45:5,6,22
8. " Yeye ni chanzo cha vitu vyote," Isa. 45:7 (kama vile. Amosi 3:6)
9. "hapana mwingine, hapana Mungu tena," Isa. 45:14,18
10. "hapana mwingine zaidi ya mimi," Isa. 45:21
11. "hapana mwingine;. . .hakuna aliye kama mimi," Isa. 46:9

Lazima ikubalike kwamba haya mafundisho ya muhimu yamefunuliwa katika njia endelevu. Semi za kale

zingeweza kueleweka kama "mungu mmoja" au Mungu mmoja wa matendo (kuna miungu wengine, yaani, Yoshua. 24:15; 1 Fal. 18:21), lakini Mungu mmoja kwetu (kama vile Kut. 15:11; 20:2-5; Kumb. 5:7; 6:4,14; 10:17; 32:12; 1 Fal. 8:23; Ps. 83:18; 86:8; 136:1-9).

Maandiko ya kwanza ambayo yalianza kudokeza juu ya umoja (Mungu mmoja wa kifalsafa) ni ya kale (kama vile Kut. 8:10; 9:14; 20:2-3; Kumb. 4:35,39; 33:26). Madai kamili na yenye mashindano yanapatikana katika Isaya 43-46 (kama vile 43:10-11; 44:6,8; 45:7,14,18,22; 46:5,9).

Kitabu cha Agano la Kale kinaishusha thamani ya miungu ya mataifa kama

1. uumbaji wa mwanadamu – Kumb. 4:28; 2 Fal. 19:18; Zab. 115:4-8; 135:15-18; Isa. 2:8; 17:8; 37:19; 40:19; 41:7,24,29; 44:10,12; 46:6-7; Jer. 10:3-5; Ufu. 9:10
2. pepo wabaya– Kumb. 32:17; Zab. 106:37; Isa. 8:19; 19:3c; 1 Kor. 10:20; Ufu. 9:20
3. majivuno, tupu – Kumb. 32:21; 2 Fal. 17:15; Zab. 31:6; Isa. 2:18; 41:29; Yer. 2:5; 10:8; 14:22; Yer. 2:5; 8:19
4. kisicho mungu – Kumb. 32:21; 2 Nya. 13:9; Isa. 37:19; Yer. 2:11; 5:7; 1 Kor. 8:4-5; 10:20; Ufu. 9:20

Kitabu cha Agano Jipya kinadokeza juu ya Kut. 6:4 katika Rum. 3:30; 1 Kor. 8:4,6; Efe. 4:6; 1 Tim. 2:5; na Yakobo 2:19. Yesu analinukuu hili kama amri ya katika Mt. 22:36-37; Marko 12:29-30; Luka 10:27. Kitabu cha Agano la Kale, pamoja na Agano Jipya, kinadai kwamba ukweli wa viumbe vingine vya kiroho (pepp wabaya, malaika), lakini muumbaji mmoja wa pekee/ Mungu mwokozi (YHWH, Mwa. 1:1).

Mungu mmoja wa Kibiblia anabainishwa na

1. Mungu ni mmoja na wa pekee (asili ya uhai wake ni dhahania, haidhirishwi)
2. Mungu ni nafsi (kama vile Mwa. 1:26-27; 3:8)
3. Mungu ni wa maadili (kama vile Kut. 34:6; Neh. 9:17; Zab. 103:8-10)
4. Mungu aliwaumba wanadamu kwa sura na mfano wake (Mwa. 1:26-27) kwa ushirika (yaani., #2). Yeye ni Mungu mwenye wivu (kama vile Kut. 20:5-6)

Kutoka kitabu cha Agano Jipya

Mungu ana umilele wa aina tatu, uthahirisho wa nafsi (tazama Mada Maalum: Utatu)

1. Mungu amefuliwa kwa ukamilifu na utimilifu katika Yesu (kama vile Yohana 1:1-14; Kol. 1:15-19; Ebr. 1:2-3)
2. Mpango wa Mungu wa milele kwa ukombozi wa mwanadamu aliyeanguka ni kujitoka dhabihu kwa Mwana Wake wa pekee (Isaya 53; Marko 10:45; 2 Kor. 5:21; FIP. 2:6-11; Webrania)

▣ **"na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie "** Hii ni kauli ya kati (shahidi) tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Mwanzoni ilikuwa ikiwarejea Wayahudi waliotawanyika. Siku zote Mungu hutumia fursa (sauti irabu ya kati, kama vile, Yn. 6:44,65). Toka Ezek. 1 8:32; Yn 3:1 6; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9 tunafahamu kuwa huwaita wanadamu wote, kwenda kwake. Lakini, lazima waitikie (yaani., dhamira tegemezi). Maneno "wengi" na "wote" kibiblia yanafanana (linganisha Isa. 53:6, "wote" na Isa. 53:11,12, "wengi" au Rum. 5:18, "wote" na Rum. 5:19, "wengi"). Moyo wa Mungu unadunda kwa ajili ya mwanadamu aliyepotea aliyemuumba kwa sura yake (kama vile Mwa. 1:26-27), akawaumba wawe na ushirika nae (kama vile Mwa. 3:8)!

**2:40 "kwa maneno mengine mengi"** Huu ni ushahidi wa kimaandiko kwamba ujumbe ulionukuliwa katika Matendo ya Mitume ni mihtasari. Hii pia ni kweli kwa mafundisho ya Yesu na mahubiri katika injili. Ki-dhahania tunathibitisha uvuvio na usahihi wa mihtasari hii. Ulimwengu wa karne ya kwanza ulijizoeza kwenye uwasilishaji wa mdomo/simulizi na uzuiji wake.

▣ **"akawashuhudia"** Neno la Kiyunani (*dia* likiongezea na *marturomai*) linafahamika na Luka (kama vile Mdo. 2:40; 8:25;10:42; 1 8:5; 20:21 ,23,24; 23:1 1 ; 28:23; Luka 1 6:28). Injili ina uwakala na hatimaye kuwa isingeweza kuchwa kwenye tamko au usikilizaji.

▣ **"akiendelea kuwaonya"** Mtu anapaswa kuitika kwenye zawadi ya Mungu katika Kristo (kama vile Yn 1:12;3:16; Rum. 10:9-13). Hili ni fumbo la ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu (kama vile Flp. 2:1 2-1 3).

**NASB, NKJV "jiokoeni"**

**NRSV, TEV**

**NJB "jiokoeni mwenyewe"**

Muundo huu wa neno uliobadilishwa ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu, lakini kama unavyoweza kutuambia, NRSV, TEV,NA NJB yanalitafasiri kama sauti irabu ya kati. Huu ni mvutano wa kithiolojia kuhusiana na wokovu (kama vile Flp 2:12-13). Yote ni kwa minajili ya Mungu au inawapasa wasikiaji wamuruhusu Mungu atende katika maisha yao.? Neno la Kiyunani "okoa" (*sōsō*) linaaksi dhana ya Kiebrania (*yasha*, BDB 446, kama vile Kut. 1 4:30) ya ukombozi wa mwili (kama vile Yakobo 5:15,20) wakati katika matumizi ya Agano Jipya unachukulia katika vidokezo vya ukombozi wa kiroho au (kama vile Yakobo 1 :21 ; 2:1 4; 4:1 2).

### **MADA MAALUM: WOKOVU (NJEO ZA VITENZI VYA KIYUNANI VILIVYOTUMIKA)**

Wokovu siyo kitu, bali ni uhusiano. Haiishii hapo mtu anapomwamini Kristo; ndiyo safari imeanza! Siyo Sera ya bima ya moto, wala tiketi ya kwenda mbinguni, bali ni kukua kumfanana Kristo. Tunao usemi katika Amerikaunaosema, kadiri wawili katika ndoa wanavyoendelea kuishi, ndiyo wanaendelea kufanana. Hili ndilo lengo la wokovu!

#### **WOKOVU KAMA KITENDO KILICHO KAMILISHWA (WAKATI ULIOPIA USIOTIMILIFU)**

- Matendo 15:11
- Warumi 8:24
- 2 Timotheo 1:9
- Tito 3:5
- Warumi 13:11(inajumuisha WAKATI ULIOPIA USIOTIMILIFU ukiwa na mazingira ya WAKATI UJAO )

#### **WOKOVU KAMA HALI YA KUWA (TIMILIFU)**

- Waefeso 2:5,8

#### **WOKOVU KAMA MCHAKATO UNAOENDELEA (WAKATI ULIOPO)**

- 1 Wakorintho 1:18; 15:2
- 2 Wakorintho 2:15
- 1 Petro 3:21

#### **WOKOVU KAMA UKAMILISHO WA WAKATI UJAO (WAKATI UJAO KATIKA NJEO YA KITENZI au MAZINGIRA)**

- Warumi 5:9, 10; 10:9,13
- 1 Wakoritho 3:15; 5:5
- Wafilipi 1:28;
- 1 Wathesalonike 5:8-9
- Waebrania 1:14; 9:28



- 1 Petro 1:5,9

Kwa hivyo, wokovu unaanza na uamuzi wa imani ya awali (cf. Yohana 1:12; 3:16; Rom 10:9-13), lakini hili lazima liendane na mchakato wa imani katika mtindo ya maisha (cf. Rom. 8:29; Gal. 3:19; Efe.1:4; 2:10), ambao siku moja utakuja kukamilishwa kwa kuonekana (cf. 1Yoh. 3:2). Hatua hii ya mwisho inaitwa utukufu. Hili linaweza kuelezwa kama.

1. Utukufu wa awali – udhihirisho (kukombolewa kutoka katika adhabu ya dhambi)
2. Wokovu endelevu–utakaso (kuokolewa toka katika nguvu ya dhambi)
3. Wokovu wa mwisho – utukufu (kuokolewa kutoka katika uwepo wa dhambi)

▣ **"katika kizazi hiki kikaidi"** Hili linaweza kuwa dokezo la Kumb.32:5 na Zab. 78:8. Mzizi wa Agano la Kale kwa ajili ya neno "kweli," "haki," "mwadilifu," "kutenda haki" lilikuwa ni "tete la kwenye mto" (angalia Mada Maalum katika Mdo. 3:14). Ikajakuwa muundo wa sitiari, futi kamba, au kipimo kilicho nyooka. Mungu aliichagua sitiari hii kuelezea tabia yake. Mungu ndiye kipimo! Mengi ya maneno kwa ajili ya dhambi katika Kiebrania na Kiyunani yanarejea kwenye mchepuko unaotokana na kipimo hiki (yaani., kilichopinda, kikaidi). Wanadamu wote wanahitajika waokolewe na kurejeshwa.

**2:41**

**NASB** "waliolipokea"

**NKJV** "waliolipokea kwa furaha"

**NRSV** "waliolikaribisha"

**TEV** "walioliamini"

**NJB** "waliolikubali"

Hii ni kauli ya kati yenye hali ya kuendelea ya wakati uliopita usiotimilifu *apodechomai*. Louw and Nida, *Greek-English Lexicon*, anaorodhesha matumizi matatu ya neno hili (kama vile juzuu ya 2, uk.28).

1. kumkaribisha mtu
2. kukubaliana na kitu Fulani au mtu kuwa ni kweli na kuitikia inavyopaswa
3. kukubaliana na ukweli au thamani ya kitu au mtu

Luka anatumia neno hili mara nyingi (kama vile Luka 8:40; 9:1 1 ; Mdo. 2:41 ; 1 8:27; 24:3; 28:30). Injili ni mtu anayepaswa kukaribishwa, ukweli kuhusu mtu wa kuamini, na maisha ya mtu yampasayo kuishi. Yote matatu ni muhimu.

▣ **"wakabatizwa"** Ubatizo ulikuwa ni tumaini la kidini kwa Wayahudi mara walipoingia hekaluni. wabadili itikadi walijibatiza wenyewe. Hili lilikuwa ni tukioa lililotarajiwa la kidini kwa hawa wasikiaji lakini wakiwa na maana mpya. Yesu alibatizwa (Mt. 3:13-17); Yesu alitumru tubatize (Mt. 28:18) —wale wanaoamua kuwa! Agano Jipya halijui chichote kuhusu mwamini asiyebatizwa. Inaonyesha kwangu kuwa huu ulikuwa mvunjiko wa wazi wa dini ya Kiyahudi na mwanzo wa watu wapya wa Mungu (yaani., kanisa, kama vile Gal.6:16).

▣ **"watu wapatao elfu tatu"** Hii ni hesabu ya ujumla, lakini ni hesabu kubwa. Ujumbe wa Petro ukabisha nyumbani mwa hawa mashuhuda wa macho. Walikuwa tayari kukiri imani kwa vinywa vyao kulikohitaji kuamini.

1. Yesu alikuwa Masihi
2. Masihi ilimaanisha kupata mateso
3. Imani ndani yake ilikuwa njia pekee ya msamaha
4. Ubatizo ulikuwa ukifaa

Hili linahitaji maamuzi ya haraka, maamuzi ya kubadili maisha (kama ifanyikavyo leo)! Angalia Mada ,Maalum: *Kerygma* katika Mdo. 2:1 4.

**2:42 "wakawa wakidumu katika fundisho la Mitume"** Luka anatumia dhana hii mara nyingi (kama vile Mdo. 1 :14;2:42,46; 6:4; 8:1 3; 1 0:7). Tambua vitu walivyofanya wakiwa pamoja:

1. mafundisho (kama vile Mdo. 2:42; 4:2,1 8; 5:21 ,25,28,42)
2. ushirika
3. wakiumegea mkate (yaani., inawezekana hii inarejea kwenye chakula cha Bwana, angalia maelezo katika Mdo. 2:46)
4. Maombi (kama vile Mdo. 2:43-47)

Haya ndio mambo yanayotupasa kiuwafundisha waumini wapya! Hawa waaumini wapya walikuwa na njaa ya ukweli. Angalia Mada Maalum ifuatayo

### **MADA MAALUM: KOINŌNIA (USHIRIKA)**

Neno "ushirika" (*koinōnia*) unamaanisha

1. Ushirika wa karibu na mtu
  - a. na Mwana (kama vile 1 Kor 1:9; 1 Yohana 1:6)
  - b. na Roho (kama vile. 2 Kor. 13:14; Flp. 2:1)
  - c. na Baba na Mwana (kama vile. 1 Yohana 1:3)
  - d. na ndugu wa agano wa kiume/kike (kama vile. Matendo 2:42; 2 Kor. 8:23; Gal. 2:9; Philemon aya. 17; 1 Yohana 1:3,7)
  - e. usio na uovu (kama vile. 2 Kor. 6:14)
2. ushirika wa karibu na vitu ama makundi
  - a. na injili (kama vile Flp. 1:5; Philemon aya. 6)
  - b. na damu ya Kristo (kama vile 1 Kor. 10:16)
  - c. usio na giza (kama vile 2 Kor. 6:14)
  - d. na mateso (kama vile. 2 Kor. 1:7; Flp. 3:10; 4:14; 1 Pet. 4:13)
3. Zawadi ama changizo zilizotolewa kwa mtindo wa ukarimu (kama vile Rum. 12:13; 15:26; 2 Kor. 8:4; 9:13; Flp. 4:15; Ebr. 13:16)
4. Kipawa cha Mungu cha neema, kupitia Kristo kinachorejesha ushirika wa mwanadamu na yeye na ndugu zake wa kiume na kike

Hii inatangaza uhusiano wa ulalo (mwanadamu kwa mwanadamu) ambao unaletwa kwa uhusiano wa kweli (mwanadamu na muumbaji). Pia unasisitiza hitaji na furaha ya jumuiya ya Kikristo (yaani, Ebr. 10:25).

### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 2:43-47**

<sup>43</sup> Kila mtu akaingwiwa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume. <sup>44</sup> Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika, <sup>45</sup> wakiuza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja. <sup>46</sup> Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimegea mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, <sup>47</sup> wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.

**2:43-47** Hili linaonekana kuwa moja kati ya maoni mengi ya kiuandishi ya Luka (yaani., Mdo. 6:7; 9:31 ; 1 2:24; 1 6:5; 1 9:20). Angalia utangulizi, madhumuni na muundo, "A.

**2:43 "kila mtu akaingwiwa na hofu"** Hii ni kauli isiotimilifu tendwa (shahidi) yenye hali ya kuelekeza. Tunapata neno la kiingereza "woga" toka kwenye neno "hofu" au "wasiwasi." Uwepo wa Mungu na nguvu ulisababisha kuwepo na mazingira ya utakatifu, hata wale wenye dhambi ambao hawajaokoka walikuwa wakijua utakatifu wa muda na mahali!

**2:44 "wote wliokwisha amini"** Angalia maelezo katika Mdo. 3:16.

▣ **"na kuwa na vitu vyote shirika"** Jaribio hili la mwanzo katika "jamii" halikufanikiwa (Mdo. 4:32-5:11). Haikumaanisha kuwa kanuni ya wote, bali jaribio la upendo, imani au jamii yenye msaada wa karibu . huu ni mfano mzuri ambao si kila kitu kilichoandikwa kwenye biblia kinamaanisha kuwa cha wote! Hawa waamini wa mwanzo walikuwa na upendo mkubwa kati yao. La,hasha tunaweza kuurejesha tena upendo huu na kuhisi uwepo na nguvu ya Mungu kati yetu. (kama vile Yn 1 7:1 1 ,21 ,22,23)!!

**2:46 "kwa moyo mmoja"** Kanisa la mwanzo liliainishwa kwa kusudi hili la umoja (kama vile Mdo. 1 :1 4; 2:46; 4:24; 5:1 2). Hii sio kusema kwamba walikubaliana kwa kila kitu, bali mioyo na fikra zao ziliunganika pamoja katika vipaumbele vya ufalme badala ya upendeleo binafsi.

▣ **"ndani ya hekalu"** Yumkini walikutana katika "tao la Suleimani" (kama vile Mdo. 3:1 1 ; 5:1 2). Yesu alifundisha huko (kama vile Yn 1 0:23). Tao la suleimani au kibaraza ilikuwa ni sehemu wa uwazi iliyofunikwa pamoja na sehemu uwanda wa nje wa watu wa mataifa katika hekalu la Herode (kama vile Josephus' *Antiq.* 1 5.1 1 .3). walimu wa dini walifundisha huko. Mara nyingi watu walikusanyika huko kusikiliza mafundisho. Tambua kanisa la mwanzo lilihudhulia hekaluni na yawezekana masinagogi ya mahala mpaka walimu wa dini walipoanzisha utaratibu wa apizo (yapata miaka 70 B.K), iliyowalazimisha washirika wa sinagogi kumlaani Yesu. Hili lilisababisha mgawanyiko kati ya kanisa na dini ya kiyahudi. Waamini wa mwanzo waliendeleza ibada zao za kati kati ya juma, lakini pia walikutana siku ya Jumapili kukumbuka ufufuko wa Yesu. Kumbuka, Yesu mwenyewe alikutana na wanafunzi, Jumapili tatu mfululizo.

▣ **"wakiuemea mkate nyumba kwa nyumba"** Kama "kuumea mkate" lilikuwa ni azimio la kiufundi kwenye karamu ya (kama vile Luka 22:19 na hasa chakula cha upendo [1 Kor. 1 1 :1 7-22; 2 Pet. 2:1 3-1 4; Yuda 1 2] katika kanisa la mwanzo , Mdo. 20:7), hivyo hili linarejea kwenye ushirika wa kila siku majumbani kwetu (lakini inapaswa kueleweka kuwa pia linatumika kwenye chakula cha kila mara katika Luka 24:30,35). Uwe mwangalifu na desturi zako za imani ya kimadhehebu kuhusu lini, wapi, mara ngapi, na muundo wa karamu ya Bwana. Moyo ndiyo msingi!

<b>NASB</b>	<b>"kwa furaha na moyo mweupe"</b>
<b>NKJV</b>	<b>"kwa furaha na usafi wa moyo"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"furaha na ukarimu wa moyo"</b>
<b>TEV</b>	<b>"furaha na moyo wa kupondeka"</b>
<b>NJB</b>	<b>"furaha na ukarimu"</b>

Aina mbali mbali za utafasiri wa neno la pili unaonyesha ugumu wa kulitafasiri neno *aphelotēs*. Kiuhalisia linamaanisha kitu laini au tambarare, lakini lilitumika ki-sitari kwa minajili ya "rahisi," "aminifu," au "nyenyekevu" (Louw and Nida). Angalia Mada Maalumu : Moyo katika Mdo. 1 :24.

**2:47**

<b>NASB, NKJV</b>	<b>"wakiwapendeza watu wote"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"wakiwatakia mapenzi mema watu wote"</b>
<b>TEV</b>	<b>"wakifurahia mapenzi mema kwa watu wote"</b>
<b>NJB</b>	<b>"waliangaliwa na kila moja"</b>

Kifungu hiki kinarejea kwenye ukubalifu wa Wakristo wa mwanzo na watu wa Yerusalemu. Aina zote za utofauti na ngazi za kijamii waliwafikilia vizuri hawa waamini wa mwanzo. Wakristo hawakuwa tishio kwenye utawala wa Kirumi (kusudi moja la Matendo). Hapakuwepo na matengano na walimu wa dini ya Kiyahudi mwanzoni mwa kanisa.

▣ **"Bwana akazidisha "** Hii ni kauli tendaji isiotimilifu yenye kuarifu. Biblia inasisitiza juu ya ukuu wa Mungu. Hakuna kinachoweza fanyika mbali na mapenzi ya Mungu. Hakuna kinachomshangaza Mungu. Hata hivyo, hii njia ya Agano la Kale ya kutetea imani ya Mungu mmoja (yaani., angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:39) limeeleweka vibaya. Ningalipenda kuingiza Mada Maalum mbili, moja ya hitaji juu ya hitaji kwa ajili ulinganifu na moja juu ya agano. Natumai hili linaleta mwanga, sio joto!

### **MADA MAALUM: Uchaguzi/Maamuzi ya kabla na Hitaji la Usawa wa Kithiolojia**

Uchaguzi ni fundisho la ajabu. Hata hiyo, si wito ulio na upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa jili ya huduma; katika Agano Jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia hipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguziwa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile.Warumi10:11,13).

Umuhimu wa huu mvutano wa kithiolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni mwandamu mchaguzi wa Mungu na wote ni uwezo wa kuchaguliwa ndani yake (Karl Barth). Yesu ni Mungu. Yesu "ndio" kwa mahitaji ya mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo). Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu(uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milelele!

Mafundisho huja kuhusiana na ukweli mwingine, sio mmoja tu, ukweli usiohusiana. Hali au tabia nzuri inakuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika mashariki na sio magharibi, mtindo. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja(fumbo la maneno) za kweli za mafundisho:

1. majaaaliwa/mchaguzi dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu
2. . Usalama wa wanaoamini dhidi ya mahitaji ya uvumilivu
3. DHAMBI YA ASILI DHIDI YA DHAMBI YA HIARI
4. KUTOTENDA DHAMBI DHIDI YA KUTENDA DHAMBI KIDOGO
5. UDHIHILISHO NA UTAKASO WA PAPO KWA PAPO DHIDI YA UTAKASO ENDELEVU
6. Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo
7. Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Munngu wa asili
8. Mungu kama hatimaye isiyojulikana dhidi ya Mungu anayejulikana katika maandiko
9. Ufalme wa Mungu kama sasa dhidi ya kukamilishwa baadaye
10. Kutubu kama zawadi ya Mungu dhidi ya jibu muhimu la Agano la kibinadamu
11. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama mwanadamu
12. Yesu ni sawa na Mungu Baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu Baba

Dhana ya kitheolojiaya "agano" inaunganisha Ufalme wa Mungu (ambaye daia huchukua hatua kwa kuweka mswada) pamoja na mamlaka ya mwanzo imani ya kuendelea kutubu kujibiwa kutoka kwa mwanadamu(k.v. Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21). Kuwa mwangalifu wa maandishi ya uthibitisho wa upande mmoja wa fumbo la maeneo na punguza kwa mwingine! Kuwa mwangaliu wa kuthibitisha mafundisho yako ya mapenzi tu au mfumo wa theolojia!

### **MADA MAALUM: AGANO**

Neno la Agano la Kale *berith* (BDB 136, KB 157), "Agano," sio rahisi kulielezea. Hakuna KITENZI kinachoshabihiana katika Kiebrania. Yote yanajaribu kupata ile asili ya neno au maana inayofanana inayodhihilisha kutoleta ushawishi. Yumkini ubashiri mzuri ni "kukata" ikimaanisha sadaka ya mnyama

inayojumuishwa kwenye agano(kama vile Mwa. 156:10,17). Hata hivyo, kiini dhahili cha dhana yenyewe kimetizamishwa kwa wasomi kuchunguza matumizi ya kidunia katika jaribio la kupima maana yake ya kiutendaji. Agano ni namna ambayo Mungu wa kweli (angalia Mada Maalum: Uwepo wa Mungu Mmoja) anavyoshughulika na uumbaji wake wa Mwanadamu. Dhana ya Agano, mkataba, au makubaliano ni ya muhimu katika kuuelewa ufunuo wa Mungu. Mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu kwa wazi unaonekana katika dhana ya Agano. Baadhi ya maagano yanaegamia moja kwa moja juu ya tabia ya Mungu na matendo.

1. Uumbaji wenyewe (kama vile Mwanzo 1-2)
2. Utunzaji na ahadi ya Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9)
3. Wito wa Abrahamu (kama vile Mwanzo 12)
4. Agano pamoja na Abraham (kama vile Mwanzo 15)

Hata hivyo, ile asili ya Agano inahitaji mwitikio.

1. Kwa imani Adamu anapaswa kumtii Mungu na kutokula lile tunda la mti wa katikati ya Edeni
2. Kwa imani Nuhu anapaswa kutengeneza safina mbali na maji na kuwakusanya wanyama wote
3. Kwa imani Abraham anapaswa kuiacha familia yake, na kumfuata Mungu, na kuamini katika kizazi kijacho
4. Kwa imani Musa anawatoa wana wa Israeli toka Misri kwenda Mlima Sinai na kupokea maagizo maalum kwa ajili ya maisha ya kidini na kijamii yakiwa na ahadi ya Baraka na laana ( kama vile Walawi 26, Kumbu kumbu la Torati 27-28)

Mvutano ule ule unaohusiana na ushirika wa Mungu kwa mwanadamu unaelezewa katika “agano jipya” (kama vile. Yer. 31:31-34; Ebr. 7:22; 8:6,8,13; 9:15; 12:24). Mvutano kwa wazi unaweza kuonekana katika kulinganisha Ezek. 18:31 na Ezek. 36:27-38 (tendo la YHWH). Je agano linasimamia juu ya matendo ya neema ya Mungu au mamlaka ya mwitikio wa mwanadamu? Hili ni suala mtambuka kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Lengo la yote ni sawa:

1. Urejesho wa ushirika na YHWH uliopotea katika Mwanzo 3
2. Uimalishaji wa watu wa haki ambao wanaaksi tabia ya Mungu

Agano jipya la Yer. 31:31-34 linatutua mvutano kwa kuondoa utendaji wa kibinadamu kwa maana ya kupata ukubarifu. Sheria za Mungu zikaja kuwa shauku ya ndani badala ya sheria ya nje. Lengo la ki-Mungu, watu wenye haki linabaki vile vile, lakini njia zinabadilika. Wanadamu waliyoanguka wanathibitisha wao wenyewe pasipo utosherevu kwa kuaksi taswira ya Mungu. Tatizo halikuwa agano la Mungu, bali ni udhaifu na dhambi za mwanadamu (kama vile Mwanzo 3; Warumi 7; Wagalatia 3).

Mvutano wa aina ile ile kati ya maagano ya Agano la Kale yasiyo na masharti na yenye masharti yanabaki katika Agano Jipya. Wokovu ni wa bure katika kazi aliyokwisha kuimaliza Yesu Kristo, lakini unahitaji toba na imani (mwanzoni na kuendelea, angalia Mada Maalum: Kuamini katika Agano Jipya). Yesu anaita ushirika wake mpya na waamini “agano jipya” (kama vile Mt. 26:28; Marko 14:24; Lk 22:20; 1 Kor. 11:25). Yote ni matamko ya kisheria (ya kimahakama) na wito wa kumfanana na Kristo (kama vile Mt. 5:48; Rum. 8:29-30; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23; 1 Pet. 1:15), maelezo elekezi ya ukubalifu (Warumi 4) wito wa ushurutishi wa kuwa mtakatifu (kama vile Mt. 5:48)! Waamini hawaokolewi kwa utendaji kazi wao, lakini ni katika utii (kama vile (kama vile Efe. 2:8-10; 2 Kor. 3:5-6). Maisha ya ki-Mungu yamekuwa ni ushuhuda wa wokovu, na sio njia ya wokovu (yaani., Yakobo na 1Yohana). Hata hivyo, maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika! Mvutano huu unaonekana kwa wazi katika maonyo yanayoonekana katika Agano Jipya (angalia Mada Maalum: Uasi)

NASB, NRSV "akalizidisha idadi"  
NKJV "akalizidisha kanisa"  
TEV "akalizidisha kundi"  
NJB "katika jamii"

Kifungu *epi to auto* linatumika katika Kiyunani cha daraja la juu na lugha ya Koine ya daraja la juu (tafasiri ya agano la kale la Kiyunani na Mdo.1 :15; 2:1 ,47;1 Kor. 1 1 :20; 1 4:23), ikimaanisha “kuwa pamoja” (Metzger, *Textual Commentary*, p. 305). Hapa katika Agano Jipya linarejea kusanyiko la kanisa. Kwa hiyo, Bwana akaliongeza kanisa (yaani., kusanyiko) kila siku. Hii inaonyesha kuwa stadi ya maisha ya uinjilist wa hiki kizazi cha waamini!

▣ **"kwa wale waliokolewa"** Kifungu "Bwana (Mungu na Kristo) waliongezeka, "kilichotumika mwanzoni katika Mdo. 2:46, ni kauli tendaji isiotimilifu yenye kuarifu, lakini kifungu hiki ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo. Sauti irabu tendwa iliyoelezewa ni ya Bwana. “waliokolewa” wako katika mchakato. Wokovu unianza na kusadiki/kuamini /imani (yaani., Yn 1 :1 2; 3:1 6; Rum. 1 0:9-1 3). Wokovu ni uhusiano ulioanzishwa na Mungu/Roho (kama Yn. 6:44,65), bali unapaswa kuwa katika uzoefu endelevu. Sio tiketi ya kwenda mbinguni au bima ya maisha; uhusiano wa imani ya kila siku, na inayokua. Angalia Mada Maalum: Njeo za Vitenzi vya Kiyunani yaliyotumika kwenye wokovu katika Mdo. 2:40.

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Elezea kwa mifano hotuba ya Petro
2. Nini lilikuwa kusudi la Pentekoste
3. Ni kwa namna gani unabii wa Yoel unahusiana na muktadha huu
4. Elezea matumizi ya Petro ya sura za Agano la Kale

## MATENDO YA MITUME 3

<b>MGAWANYO WA AYA ZA TAFSRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Mtu aliyekuwa Kiwete Aponywa Katika Mlango wa Hekalu	Mtu Aliyekuwa Kiwete Aponywa	Uponyaji katika Mlango Mzuri	Aliyekuwa Kiwete na Ombaomba Aponywa	Tiba ya Mtu Kiwete
3:1-10	3:1-10	3:1-10	3:1-10	3:1-0
Usemi wa Petro Ndani ya Tao la Suleimani	Mahubiri ndani ya Tao la Suleimani	Mahubiri ya Petro	Ujumbe wa Petro ndani ya Hekalu	Maelezo ya Petro kwa Watu
3:11-26	3:11-26	3:11-16 3:17-26	3:11-26 3:17-26	3:11-16 3:17-26 3:25-26

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("A Guide to Good Bible Reading"))

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

#### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

Katika Matendo 3-5 kuna mvutano katika Yerusalemu juu ya mafundisho ya Yesu na miujiza ya Mitume. Mwonekano wa sura tano za mwanzo yapata mwaka mmoja.

- A. Petro na Yohana wanamponya mtu aliyekuwa kiwete, Matendo ya Mitume 3:1-4:31 (mfano wa Matendo ya Mitume 2:43)
  - 1. uponyaji wenyewe
  - 2. hotuba ya pili ya Petro inayoeleza kuhusu uponyaji
  - 3. upinzani na kesi (hotuba ya tatu ya Petro, aliyoitoa kwa Wakuu wa Sinagogi)
  - 4. mateso yake yanaanza
- B. Jaribio la maisha ya ushirika, Matendo ya Mitume 4:32-5:11
  - 1. umoja wa waamini wa kale (mfano wa Matendo ya Mitume 2:43-47)
  - 2. matatizo ya Anania na Safira
- A. mahusiano ya kanisa la kale kati Walimu wa Sheria za Dini ya Kiyahudi Matendo ya Mitume 5:12-42
  - 1. maisha ya kanisa
  - 2. wivu wa Wakuu wa Sinagogi
  - 3. utetezi wa malaika
  - 4. hotuba ya nne ya Petro
  - 5. upinzani na adahabu

### MAJINA YA YESU KATIKA SURA ZA 3-4

- A. Yesu Kristo Mnazarethi, Matendo ya Mitume 3:6; 4:10
- B. Mtumishi Wake Yesu, Matendo ya Mitume 3:13,26; 4:27
- C. Mtakatifu na Mwenye haki, 3:14 (kama vile Matendo ya Mitume ya Mitume 2:27)
- D. Mkuu wa Uzima, Matendo ya Mitume 3:15
- E. Kristo, Matendo ya Mitume 3:18,20; 4:10 (kama vile "Bwana na Kristo," Matendo ya Mitume 2:36)
- F. Nabii, Matendo 3:22
- G. Bila shaka hili ni dokezo la jina la "Uzao wa Abrahamu," Matendo ya Mitume 3:25-26
- H. Jiwe lililodharauliwa, Matendo ya Mitume 4:11

### USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

#### ANDIKO LA NASB ( LILIBORESHWA ): MATENDO YA MITUME 3:1-10

<sup>1</sup>Basi Petro na Yohana walikuwa wakikwea pamoja kwenda hekaluni, saa ya kusali, saa tisa. <sup>2</sup>Na mtu mmoja aliyekuwa kiwete toka tumboni mwa mamaye alichukuliwa na watu, ambaye walimweka kila siku katika mlango wa hekalu uitwao Mzuri, ili aombe sadaka kwa watu waingiao ndani ya hekalu. <sup>3</sup>Mtu huyu akiwaona Petro na Yohana wakiingia hekaluni aliomba apewe sadaka. <sup>4</sup>Na Petro, akimkazia macho, pamoja na Yohana, akasema, Tutazame sisi. <sup>5</sup>Akawaangalia, akitaraji kupata kitu kwao. <sup>6</sup>Lakini Petro akasema, Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende. <sup>7</sup>Akamshika mkono wa kuume, akamwinua, mara nyayo zake na vifundo vya miguu yake vikatiwa nguvu. <sup>8</sup>Akaondoka upesi akasimama, akaanza kwenda; akaingia ndani ya hekalu pamoja nao, akienda, akiruka-ruka, na kumsifu Mungu. <sup>9</sup>Watu wote wakamwona akienda, akimsifu Mungu. <sup>10</sup>Wakamtambua, ya kuwa yeye ndiye aliyekuwa akiketi na kuomba sadaka penye mlango Mzuri wa hekalu; wakajaa ushangao wakastaajabia mambo yale yaliyompata.

**3:1**"Petro na Yohana walikuwa wakikwea pamoja kwenda hekaluni" Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usiotimilfu. ilikuwa tabia ya wanafunzi wa kale kwenda hekalu kila siku (kama vile Luka 24:53; Matendo 2:46). Wafuasi halisi wa Yesu katika Palestina waliabudu

- 1. ndani ya Hekalu walau katika siku maalum kama si kila siku)



2. ndani ya masinagogi ya mahali (kila siku ya Sabato)

3. pamoja na waamini siku ya Jumapili

Huu ulikuwa mpangilio wa kipindi cha muda mrefu. Hawa waamini hawakuona mgawanyiko kati ya imani yao ndani ya Yesu kama Masihi aliyehaidiwa na Dini ya Kiyahudi. Hawa walijiona kama "watu wa kusanyiko la Israeli." Ndio maana waliichagua jina la *eklesia* kwa ajili ya kundi lao. Katika Maandikko ya Kale ya Kiyunani hiki ni kifungu cha kimaagano, "kusanyiko (*qahal*) la Israeli" kilichotafsiriwa.

Wayahudi walichukua hatua ya kiserikali baada ya kuanguka kwa Yerusalemu na kuanzishwa kwa kanuni ya kiapo (kumkataa Yesu kama Masihi) ili kuzuia ushirika ndani ya masinagogi. Hapa ndipo kanisa lilipoimarisha siku yake ya ibada kama siku ya Jumapili (siku ya kuadhimisha ufufuo wa Yesu; ile siku Yesu alipoonekana mara tatu kwa wanafunzi kule Ghorofani).

Yohana mara nyingi anatambulishwa na Petro katika Matendo (kama vile Matendo ya Mitume 1:13; 3:1,3,4,11; 4:13,19; 8:14). Kwa hakika inawezekana kwamba kanisa la kale la huko Yerusalemu lilikuwa na kundi la viongozi ambao waliwakilisha vipengele tofauti na kusistiza juu ya injili. Bila shaka Petro na Yohana walikuwa wazi zaidi kwa ajili ya injili ya Mataifa (kama vile Matendo 3:8,10), ambapo Yakobo (nduguye Yesu) alitambulishwa zaidi na ishara za Kiyahudi za kushikilia tamaduni a kale. Yote haya yalibadilika kwa kiasi fulani baada ya Baraza la Yerusalemu la Matendo 15.

☑ **"saa ya kusali, saa tisa"** Hili linaweza kuashiria masaa manane mchana kutwa. Wayahudi (yaani, Mafarisayo) walikuwa na maombi ya kidesturi kila siku saa 9 asubuhi, 12 aduhuri na 3 alasiri bila shaka walijikita katika Zab.55:17). Andiko hili linarejelea ule wakati wa dhabihu ya jioni, ambapo ilikuwa saa 3 alasiri (dhabihu ya asubuhi ilikuwa saa 9 asubuhi). Watu wengi wangukuwa hekaluni kwa wakati huu (kama vile Mdo. 10:30).

**3:2 "mtu mmoja aliyekuwa kiwete toka tumboni mwa mamaye"** Wale wote waliokuwa na kawaida ya kuhudhuria hekaluni waliifahamu hali ya mtu huyu ("aliwekwa na watu kila siku" ni kauli tendewa ya wakati uliopita usiotimilifu); hivyo, hakukuwa na nafasi ya udanganyifu uliohusishwa katika uponyaji huu (kama vile 3:10; 4:22). Huu ulikuwa utimilifu wa unabii wa Kimasihi wa Agano la Kale (kama vile Isa. 35:6). Wayahudi walitaka ishara; Yesu aliwapa ishara nyingi, sasa wanazo nyingine ikiwa walikuwa na macho ya kuona tu.

Hapa kuna fumbo lenye kuogopesha la yule mgonjwa aliyekuwa akikaa katika nyumba ya Mungu. Kama ilivyo kawaida, kulikuwa na katazo pia dhidi ya watu wa aina hii kuhusika kwa ukamilifu katika ibada (yaani, kutumika kama makuhani, (kama vile Law. 21:16-24). Injili hutoa siku mpya. Hata towashi wa ki-Ethiopia (hakuna vizuizi vya rangi) (hakuna vizuizi vya kimwili) anakaribishwa katika ufalme mpya (kama vile Matendo 8:26-40).

☑ **"katika mlango wa hekalu uitwao Mzuri"** Eneo kamaili la mlango huu halijulikani kwa usahihi. Bila shaka huu ulikuwa Mlango wa Nicanor ambao ulitengenezwa kwa shaba ya ki-Korintho (Flavius Josephus, *Antiq.* 15.11.3; *Wars* 5.5.3). Huu ulianzai Mahakama ya Mataifa hadi Mahakama ya Wanawake. Huu ulikuwa upande wa mashariki wa hekalu, uliokuwa umeangaliana na Mlima Mizeituni, karibu na Tao la Suleimani.

☑ **"ili aombe sadaka kwa watu waingiao ndani ya hekalu "** Utoaji au kuwapa wahitaji, ilikuwa sehemu ya imani ya Kiyahudi iliyohitajika (kama vikle Mt. 6:1-4; Luka 11:41; 12:33; Matendo ya Mitume 10:2,4,31; 24:17). Mara nyingi fedha ilikusanywa kwa kila juma katika masinagogi ya mahali na chakula kiligawiwa, lakini kwa uwazi kabisa baadhi yao waliombaomba kila siku ndani ya eneo la Hekalu lenyewe.

## **MADA MAALUM: KUWASAIIDIA WAHITAJI**

- I. Neno lenyewe
  - A. Neno hili lilikuwa ndani ya Uyahudi.
  - B. Ili linarejelea kuwapa wahitaji na/ama maskini.
  - C. Neno la Kiyunani, kueasaidia wahitaji, linatokana na ufupisho wa neno la Kiyunani *eleēmosunē*.
- II. Dhana ya Agano la Kale

- A. Dhana ya kuwasaidia wahitaji ilihidhinishwa katika torati ya kale
1. muktadha unaofanana, Kumb. 15:7-11
  2. kusaza," kubakiza sehemu ya mavuno kwa wahitaji, Law. 19:9; 23:22; Kumb. 24:20
  3. "sabbath year," allowing the poor to eat the produce of the seventh, fallow year,
- B. Dhana hii iliendelezwa katika Hekima ya Fasihi (mifano iliyoteuliwa)
1. Ayubu 5:8-16; 29:12-17 (yule dhalimu anaelezwa katika 24:1-12)
  2. Zaburi, 11:7
  3. Mithali 11:4; 14:21,31; 16:6; 21:3,13
- III. Uendelezwaji katika Uyhudi
- A. Mgawanyo wa kwanza Mishnah unashughulika na kuwatunza wahitaji, maskini, na Walawi wa mahali palepale.
- B. Nukuu zilizoteuliwa
1. Kitabu cha Mhubiri (pia kinajulikana kama Hekima ya Bin Sira) 3:30, "kama maji yazimishavyo ndimi za moto, ndivyo kuwasaidia wahitaji kulipiavyo dhambi" (NRSV)
  2. Tobiti 4:6-11, <sup>6</sup>"Maana ukitenda vitu kwa uaminifu utafanikiwa katika mambo yako yote. <sup>7</sup>Toa sehemu ya mali yako kuwapa maskini. Kamwe usimpe kisogo mtu maskini naye Mungu hatakupa kisogo. <sup>8</sup>Toa ulicho nacho. Ukiwa na zaidi, toa zaidi. Hata kama unacho kidogo tu, toa sehemu yake <sup>9</sup> Kwa kufanya hivyo utajiwekea hazina bara kwa wakati wa shida . <sup>10</sup> Kwa maana kusaidia maskini huokoa mtu kifoni na kumkinga asiingie katika makao ya giza. <sup>11</sup> Naam! Kusaidia maskini, kwa wale wanaofanya hivyo, ini sadaka bora mbele ya Mungu Mkuu." (NRSV)
  3. Tobiti 12:8-9, <sup>8</sup>"Afadhali sala pamoja na ukweli na kusaidia maskini pamoja na kutenda haki kuliko kuwa tajiri na kukosa uaminifu. <sup>9</sup>Sadaka kwa maskinihumwoko mtu na kifo na kumtakasa dhambi zake. Wale wanaowasaidia maskini watajaliwa uhai." (NRSV)
- A. Nukuu ya mwisho kutoka Tobiti 12:8-9 inaonyesha uendeleu wa tatizo. Matendo ya mwanadamu/ faida za mwanadamu zilionekana kama utaratibu kwa misamaha yote na utele.
- B. Dhana hii iliendelea baadaye katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani amabapo nenola Kiyunani la "kuwasaidia wahitaji" (*eleēmosunē*) lilikuja kuwa kisawe cha "mwenye haki" (*dikaio sunē*). Haya yangeweza kubadili kila kitu katika kutafsiri Kiebrania "mwenye haki" (BDB 842, agano la upendo wa Mungu na uaminifu, kama vile Kumb. 6:25; 24:13; Isa. 1:27; 28:17; 59:16; Dan. 4:27).
- C. Matendo ya mwanadamu ya huruma huwa kusudi ndani yake ili kufanikisha utele wa mtu binafsi hapa na wokovu wakati wa kifo. Tendo lenyewe, badala ya nia iliyo nyuma ya tendo, huwa sifa ya kitheolojia. Mungu huangalia mioyo, kisha hupima kazi ya mikono. Hili lilikuwa fundisho la Walimu wa sheria za Kiyahudi, lakini kwa kiasi fulani hii imepotezwa katika haki binafsi (kama vile Mika 6:8).
- IV. Agano Jipya
- A. Neno hili linapatikana katika
1. Mt. 6:1-4
  2. Luka 11:41; 12:33
  3. Matendo ya Mitume 3:2-3,10; 10:2,4,31; 24:17
- B. Yesu anaelezea uelewa wa kitamaduni kuhusu haki kama (kama vile II Clement 16:4)
1. kuwasaidia wahitaji
  2. kufunga
  3. Maombi

Katika hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7), Kimsingi Yeye alieaelekeza upya mtazamo wa desturi iliyohusu haki (yaani, kusadiki katika matendoya mtu). Lile "agano jipya" la Yer. 31:31-34 lilikuja kuwa kipimo cha haki pamoja na Mungu (kama vile Rum. 3:19-31). Mungu hutoa moyo mpya, akili mpya, roho mpya. Tazamio haliko juu ya utendaji wa mwanadamu bali utendaji wa ki-Ungu (yaani, Eze. 36:26-27).

**3:3** Shauku ya mtu huyu kwa uhalisia ilikuwa ya kifedha (kama vile Matendo ya Mitume 3:5).

**3:4"akimkazia macho"** Tazama maelezo katika Matendo 1:10.

☑️**"Tutazame sisi"** Walihitaji usikivu kamili (*blepō* ni muundo wa kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu).

**3:5** Mitume hawakuwa watu wa utajiri wa kipesa, bali walikuwa njia ya rasilimali za kiroho kwa Mungu Mungu (kama vile Matendo ya Mitume 3:6).

**3:6"Kwa jina la Yesu Kristo "** "Jina" ni nahau ya Kiebrania ambayo inazungumzia sifa ya mtu (kama vile Luka 9:48,49; 10:17; 21:12,17; 24:47, tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:21). Hili lazima lingekuwa jambo la kuogopesha kwa mtu huyu. Yesu alikuwa ameshtumiwa na kusulibishwa kama mharifu hivi karibuni, ambapo mgeni huyu (yaani, Petro) alimuita "Mashi" (yaani, "Kristo," ambapo hii ni tafsiri ya Kiyunani, tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:31).

☑️**"wa Nazareti"** Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:22.

☑️**"simama uende"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Petro na Yohana, kama Yesu, alitumia nafasi ya kukutana kwa ajili ya kuudhihirisha upendo wa Mungu na nguvu na pia kuuhimarisha ujumbe wa injili (kama vile Matendo 3:9). Huu uponyaji uliongeza umakini kwa waamini wa Kiyunani (kama vile Matendo ya Mitume 3:12 na kuendelea).

**3:7** Hii ni taarifa ya ushahidi wa macho ya matukio kadhaayenye kuhusiana. Mtu mmoja aliyekuwepo pale akamwambia Luka kuhusu hili kwa uhakika, maneno ya undani.

☑️**"mara"** Hili ni neno la Kiyunani *parachrēma*. Luka amelitumia mara kumi ndani ya Injili na mara sita katika kitabu cha Matendo (kama vile Matendo ya Mitume 3:7; 5:10; 12:23; 13:11; 16:26 ,33). Hili limetumika mara mbili katika Mathayo na hakuna sehemu nyingine katika Agano Jipya. Neno hili linatumika mara kadhaa ndani ya Maandiko ya Kale ya Kiyunani. Mara nyingi Luka anatumia nahau na maneno kutoka katika tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania. Huyu alipaswa kuwa analifahamu vema, bila shaka ni mawasiliano yake na Mtume Paulo au kushiriki katika katekismu pamoja na waamini wapya.

**3:8"Akaondoka upesi akasimama"** Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakatgi uliopo (kama vile Matendo 3:9). Mtu huyu alianza kutembea kulizunguka eneo hili la Hekalu. Ni fursa gani tilionayo ya kuishiriki Habari Njema!

**3:10** Walimjua mtu huyu (kauli tendaji elekezi ya wakati usio timilifu, walianza kumtambua). Huyu hakuwa mgeni wala mtembeleaji. Walikuwa wakimwona mlangoni siku hadi siku, na walikuwa wakimpita! Hata hivyo, wawakilishi wa Yesu hawakutumika, walitenda kazi katika nguvu za ki- Pentekoste!

☑️**"wakajaa"** Luka analitumia neno hili mara nyingi (angalia maelezo kamili katika Matendo 5:17). Wanadamu wanaweza "kujawa" na vitu vingi (yaani, kubainishwa na):

1. Roho Mtakatifu, Luka 1:15,41,67; Matendo ya Mitume 2:4; 4:8,31; 9:17; 13:9
2. ghadhabu, Luka 4:28; 6:11
3. woga, Luka 5:26
4. mshangao na kustaajabu, Matendo ya Mitume 3:10
5. wivu, Matendo ya Mitume 5:17; 13:45
6. ghasia, Matendo ya Mitume 19:29

Petro na Yohana waliwataka wale waliojawa na mshangao (aliuona uzingativu wao) wajawe na injili!

☑️**"ushangao wakastaajabia"** Mambo haya pia ni ya kawaida katika maandiko ya Luka.

1. ushangao, *thambos*, Luka 3:6; 5:9; Matendo ya Mitume 3:10 na *ekthambos* katika Matendo ya Mitume 3:11
2. kustaajabu

- a. *ekstasis*, Luka 5:26; Matendo ya Mitume 3:10; 10:10; 11:5; 22:17
- b. *existēmi*, Luka 2:47; 8:56; 24:22; Matendo ya Mitume 2:7,12; 8:9,11; 9:21; 10:45; 12:16

Upendo na matendo ya Mungu mara nyingi husababisha kustaajabu (maneno haya ya Kiyunani yalitumika katika Maandko ya Kale ya Kiyunani kwa ajili ya kumcha na kumhofu Mungu, kama vile Mwa. 15:12; Kut. 23:27; Kumb. 28:28).

### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 11-16**

<sup>11</sup> Basi alipokuwa akiwashika Petro na Yohana, watu wote wakawakusanyikia mbio katika tao lile lililoitwa tao la Sulemani, wakishangaa sana. <sup>12</sup> Hata Petro alipoyaona haya akawajibu wale watu, Enyi Waisraeli, mbona mnastaajabia haya, au mbona mnatukazia macho sisi, kana kwamba tumemfanya huyu aende kwa nguvu zetu sisi, au kwa utauwa wetu sisi? <sup>13</sup> Mungu wa Ibrahimu na wa Isaka na wa Yakobo, Mungu wa baba zetu, amemtukuza mtumishi wake Yesu, ambaye ninyi mlimsaliti na kumkana mbele ya Pilato, alipokuwa ametoa hukumu yake afunguliwe. <sup>14</sup> Bali ninyi mlimkana yule Mtakatifu, yule Mwenye haki, mkataka mpewe mwuaji; <sup>15</sup> mkamwua yule Mkuu wa uzima, ambaye Mungu amemfufua katika wafu; na sisi tu mashahidi wake. <sup>16</sup> Na kwa imani katika jina lake, jina lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo kwake yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote.

**3:11"alipokuwa akiwashika Petro"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo. Ningefikiri kwamba huyu alikuwa ameshikwa na Petro kama Mariamu alivyokuwa amemshika Yesu ndani ya bustani (kama vile Yohana 20:16-17).

☐ **"tao la Sulemani"** Hili lilikuwa eneo refu lenye kuzunguka kandokando ya upande wa mashariki ya mahakama ya Kimataifa (kama vile Josephus' Antiq. 20.9.7). Mzizi umetegemezwa na safu nyingi. Hili ilipata jina lake kutokana na ukweli kwamba misingi ya kale ya hekalu la Suleimani ilikuwa ndani ya maeneo yale yale ya kwa ujumla. Mara nyingi Yesu alikuwa akifundisha mahahali pale (kama vile Yohana 10:23).

**3:12"Hata Petro alipoyaona haya"** Waliona maajabu na uchunguzi wa umati na akachukulia kama faida (kama vile Kol. 4:3; 2 Tim. 4:2) ya fursa ya kuishirikisha injili (yaani, hotuba ya pili ya kanisa jipya).

☐ **"Waisraeli"** Petro aliwahita hivi katika Matendo ya Mitume 2:22. Petro anaendelea kuwahubiria Wayahudi.

☐ **"mbona. . . mbona"** Petro aliuliza mbona kwa kuwa hawa walishangazwa na uponyaji wa kimuujiza. Je! Yesu hakufanya miujiza ya aina hii wakati wa juma la mwisho la uhai Wake? Pia, kwa nini hawa waliwaangalia Petro na Yohana kwa kustaajabu sana, kana kwamba wao ndiyo walilifanya hili? Hii ilikuwa ishara ya uaminifu wa injili na uweza wa Masihi mfufuliwa.

Roho alilitenda muujiza huu kwa sababu kadhaa.

1. kuuthibitisha uongozi wa Petro na Yohana
2. kumsaidia mtu aliyekuwa mhitaji
3. kumshuhudia kwa Wayahudi waliokuwa Hekaluni

**3:13"Mungu wa Ibrahimu na wa Isaka na wa Yakobo"** Hili linaonyesha kwamba huduma ya Yesu na injili zilikuwa zimeungamanishwa na Agano la Mungu na watu wa kimaagano ya Agano la Kale kwa umuhimu kama vile Kut. 3:6, 15; Luka 20:37). Lazima Ukristo utambuliwe kama utimilifu wa kweli wa Dini ya Kiyahudi (kama vile Mt. 5:17-19). Wayahudi wengi wangeliona hili kama ukaidi, lakini waandishi wa Agano Jipya wanaliona hili kama utimilifu. Wafuasi wa Yesu wanahaidiwa ukomavu wa "agano jipya" la Yer. 31:31-34 (kama vile Gal. 6:16). Israeli haikukamilisha kazi yake ya umisheni ya kuwa ufalme wa makuhani kwa ulimwengu (kama vile Kut. 19:5-6; 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6).

Kanisa limepewa mamlaka (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Matendo 1:8). Kusudi la Mungu li katika kuirejeha sura na mfano Wake ndani ya mwanadamu, hivyo hilo ndilo kusudi la ushirika unaoweza kukamilishwa. Ikiwa kuna Mungu mmoja pekee (yaani, Mungu aliye mmoja, tazama Mada Maalum katika Matendo 2:39), tena hapawezi kuwepo na watu wa kipekee, ni watumishi tu wayatumikiao makusudi ya Mungu kwa ulimwengu pamoja na wanadamu wote (tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mtume 1:8).

☐ "amemtukuza" Neno hili linaweza kueleweka katika njia kadhaa.

1. muktadha wa papo kwa papo juu ya uponyaji wa mtu aliyekuwa kiwete kwa jina Lake
2. upana wa muktadha wa hotuba ya Petro kuhusu Yesu aliyefufuka na kutukuzwa
3. muktadha wa Agano la Kale juu ya Yesu kama Masihi ajaye
4. Katika Injili ya Yohana neno hili mara nyingi linatumiwa na Yesu Mwenyewe kuhusu kusulibiwa Kwake (kama vile Matendo 7:39; 12:10,23; 13:31-32; 16:14; 17:1).

## MADA MAALUMM : UTUKUFU

- I. Maana yake kubwa  
Kuna maneno yapatayo ishirini yaliyo litafasiri neno "utukufu" (*doxa*) na agano la kale la Kiyunani, lakini neno la Kiebrania lililo muhimu sana ni *kabod* (BDB 458-459, 455-458). Maana yake ya msingi ni ile ambayo ni nzito. Lilikuwa ni neno la kibiashara lililotumika kwenye ununuzi wa miamala (yaani .vipimo). likaja kuwa na elimu-maana kubwa ambapo dhana ya uzito ikajitokeza katika kilo, watu wenye nazo, mahali na vitu.
- II. Utumiaji wa neno YHWH
  - A. ikajakuwa ndo njia ya kuelezea uwepo binafsi wa YHWH. Ilijumuisha nguvu zake, uweza (yaani, uliopita mipaka) akiwa na u-mtu wake na uwepo katika umbo la kirahisia.
  - B. Iliidokeza YHWH katika uumbaji, kama vile Zab. 19:1; 29:3,9; 104:31
  - C. Lilitumika katika udhahiri wa wazi wa Mungu kwa mwanadamu likijiungamanisha na utengenezaji wa agano la watu wake. Yeye ni "utukufu wa Israel", kama vile. 1Sam. 15:29
    - 1) Safari yao ya kutoka Misri kama vile Hes. 14:22 (ilitabiliwa katika Mwa. 15:12-21)
    - 2) Katika wingu la utukufu lililowafunika na kuwaongoza kama vile Kut. 16:7,10
    - 3) Utoaji wa sheria zake katika mlima Sinai
    - 4) Matendo yake ya utoaji na hukumu wakati wa kutangatanga nyikani
      - a. Uwasi wa awali uliohusiana na taarifa ya wapelelezi kumi na mbili, kama vile Hes. 14:9-10
      - b. Uingiliaji kati wa Musa kwa niaba yao kama vile Hes. 14:20-21
      - c. Uasi wa Kola kama vile Hes. 16:19
      - d. Mgogora wa maji, kama vile Hes. 26:6
  - D. Ombi la Musa kutaka kumwona Mungu, kama vile Kut. 33:18-23
  - E. Lilitumika na YHWH mwenyewe
    - 1) 1Nya. 29:11
    - 2) Zab. 106:20; Yer. 2:11; Hos. 4:7; Rum. 1:23
    - 3) Isa. 42:8; 45:7; 48:11; 58:8; 60:1-2,19 (Ufu. 21:23; 22:5)
    - 4) Zek. 2:5,10
  - F. Lilitumika katika muunganikano wa uwepo wa YHWH na/ katika
    - 1) Hema takatifu, kama vile Kut. 16:7,10; 29:43; 40:34-35; Law. 9:6,23
    - 2) Hekalu, kama vile 1 Fal. 8:11; 2 Nya. 5:14; 7:1-3; Isa. 6:3; Hag. 2:3,9
    - 3) Sanduku la agano, kama vile 1 Sam. 4:22; Zab. 63:2; 78:61
  - G. Lilitumika katika ufalme wa YHWH, kama vile 1 Nya. 29:12-13; Zab. 24:7-10; 45:3
  - H. Lilitumika na YHWH katika hali ya kuadilisha (yaani, haki), kama vile Zab. 29:3; 97:6; Isa. 42:8; 48:11; 58:8; Hab. 2:14

- III. Lilitumika kwa wanadamu na mataifa
  - A. Binadamu
    - 1) Likiendana na “nafsi” (yaani, *nephesh*) kama vile. Mwa. 49:6; Zab. 16:9; 108:1
    - 2) Mali, kama vile Mwa. 31:1; Zab. 49:16,17; Isa. 10:3; 61:6; 66:11-12
    - 3) Heshima, kama vile Mwa. 45:13; Zab. 8:6; Hag. 2:7
    - 4) Sifa njema, kama vile Ayu. 19:9; 29:20; Zab. 4:2; 49:17
    - 5) Uzuri, kama vile 1 Nya. 29:12,28; 2 Nya. 17:5; 18:13; 32:27
  - B. Mataifa
    - 1) Misri,
    - 2) Ephrahim, kama vile Hos. 9:11
    - 3) Samaria, kama vile Hos. 10:5
  - C. Wafalme
    - 1) Ahausuero, kama vile Esta 1:4
    - 2) Israeli, kama vile Zab. 21:6
    - 3) Antiochus IV, kama vile. Dan. 11:39
  - D. Majeshi ya mataifa
    - 1) Syria, kama vile Isa. 8:7
    - 2) Israel, kama vile Isa. 17:4
    - 3) Kedar, kama vile Isa. 21:16
- IV. Lilitumika kwenye maelezo ya siku za mwisho
  - A. YEHOVA atarudi kwenye hekalu lake jipya, kama vile Eze. 43:2,4,5; 44:4
  - B. YHWH atauvutwa ulimwengu wote kwake, kama vile Isa. 40:5; 59:19; 60:1-3; 66:18-19
  - C. YHWH ataishusha Yerusalem “mpya” kama vile Isa. 66:10; Zek. 12:7
- V. Kusudi la uumbaji ni kumtukuza YHWH
  - A. Aliumba kwa ajili ya utukufu wake, kama vile Isa. 43:7
  - B. Utukufu ni juu yake, kama vile 1 Nya. 16:29
  - C. Imba/sifu utukufu wake, kama vile Zab. 66:2; 96:8; 115:1
  - D. Yote tuyatendayo twayatenda katika yeye, kwa ajili ya utukufu wake, kama vile 1 Kor. 10:31; 2 Kor. 4:15; Efe. 5:22; 6:5; 1 Pet. 2:12
  - E. Maelezo ya kwanza ya katekismu

●"mtumishi wake" Neno "mtumishi" (*pais* lililotumika kwa ukawaida kikatika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiyunani- LXX)

1. jina la heshima katika Agano la Kale lililotumika kwa Yakobo, Musa, Yoshua, na Daudi (kama vile Zaburi 105; Luka 1:69)
2. katika Nyimbo za Mtumishi za Isaya (yaani, Isa. 42:1-5; 49:1-7; 50:4-11; 52:13-53:12)
3. taifa la Israeli (kama vile Matendo 41:8-9; 42:19; 43:10; 44:1,21; pia Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiyunani (LXX) zinaonekana katika Luka 1:54)
4. Masihi wa Mungu (kama vile Matendo 42:1; 52:13; 53:11)
5. Neno *Pais* linatumika juu ya Yesu kama Mtumishi /Masihi katika Matendo ya Mitume 3:13,26; 4:27,30 Hakuna tofauti sahihi kati kipengele cha ushirika na kile cha kibinafsi, hasa katika wimbo wa Mwisho (yaani, Isa. 52:13-53:12). Katika muktadha hili linaweza kuirejelea Israeli.
  1. taifa haliwezi kukosa hatia kwa yule aliyelewa wokovu kwa kuwa hili taifa lilikaikaidi hukumu (kama vile Isa. 41:18-22; 53:8d)

2. Maandiko ya Kale ya Kiyunani yanaliabadili neno "wewe" katika Isa. 52:14 "Yeye" (pia katika Matendo ya Mitume 3:15). Watafsri wa Kiyahudi waliokuwepo kabla ya kuzaliwa kwa Yesu (bila shaka 250-150 k.k.) walilionga andiko hili kama la ki-Masihi na nala kipekee.

☑ "Yesu" Jina la Yesu linapotumika kwalo, mara kwa mara linasistiza juu ya ubinadamu Wake (kama vile Matendo 3:6).

☑ "ambaye ninyi mlimsaliti na kumkana" neno "ninyi" ni la kimsistizo! Si viongozi wa Kiyahudi pekee waliowajibika kwa ajili ya kifo cha Yesu (kama vile Matendo ya Mitume 3:17; 2:23). Petro alinatengeneza kumbukumbu maalum kwa ule mwikio wa umati kabla ya Pilato (kama vile Luka 23:18-25). Inawezekana kwamba baadhi ya hawa yawezekana kuwa walikuwepo pale, lakini Petro anahutubia umati huu kana kwamba waliwajibika kama kundi (kama vile Matendo ya Mitume 3:15). Watu wa Mungu waliochaguliwa (Wayahudi) "walimsaliti" na "kumkana" Masihi wa Mungu (kama vile Yohana 1:11).

☑ "Pilato" Tazama Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUMU: PONTIO PILATO

- A. Mahali na wakati alipozaliwa havijulikani
- B. Wa daraja au tabaka la Waendesha farasi (daraja la juu ngazi ya kati la jamii ya Warumi)
- C. Aliaoa, lakini watoto hawajulikani
- D. Teuzi za kiutawala wa awali (ambazo lazima zilikuwa nyingi) hazijulikani

### I. Nafsi ya mtu

- A. Mitazamo miwili tofauti
  1. Philo (Legatio na Gaium, 299-305) na Josephus vitabu vya historia za kale 18.3.1 na vita vya kiyahudi 2.9.2-4) wanamweleza mtawala wa ..... asiye na huruma na katili.
  2. The NT (Injili, Matendo) linamtoa kama wakili wa Kirumi dhaifu ambaye anaweza kuendeshwa kwa urahisi.
- B. Paul Barnett, Yesu na kuinuka kwa Ukristo wa kwanza, kur. 143-148, kinatoa maelezo yenye kukubalika kuhusu mitazamo hii miwili.
  1. Pilato aliteuliwa kuwa wakili mwaka 26 b.k chini ya Tiberia ambaye alikuwa anaunga mkono Wayahudi (kama vile Philo, Legatio and Gaium, 160-161).
  2. Tiberius alipata hasara ya kukosa nguvu za kisiasa L. Aelius Sejanus, kiranja wake mlinzi wa jumba la kifalme ambaye alikuwa nguvu halisi nyuma ya kiti chake cha kifalme na aliye wachukia Wayahudi (Philo, Legatio land Gaium, 159-160).
  3. Pilato alikuwa mfuasi wa Sejanus nana alijaribu kumvutia
    - a. Kuleta viwango vya kirumi kwenye mji wa Yerusalemu (26 B.K), ambavyo mawakiri wengine hawakuwa wamefanya. Hizi alama za Miungu wa Kirumi iliwachochea Wayahudi (kama vile Josephus' Antiq. 18.3.1; Vita vya Kiyahudi 2.9.2-3).
    - b. Kuchapa sarafu (29-31 B.K) ambayo ilikuwa na picha za Warumi wakiabudu zimechongwa juu yake. Josephus anasema alikuwa kwa makusudi kabisa anajaribu kupindua sheria za kiyahudi na desturi (kama vile Josephus, Kitabu cha mabo na historia ya kale 18.4.1-2).
    - c. Kuchukua fedha kutoka hazina ya hekalu kujenga mfereji Yerusalemu (kama vile Josephus, Antiq. 18.3.2; Vita vya Kiyahudi 2.9.3).
    - d. kupata Wagalilaya baadhi na kuwaua wa kutoa dhabihu siku ya pasaka mjini Yerusalemu.
    - e. Kuleta ngao za Kirumi mjini Yerusalemu katika mwaka 31 b.k., mwana wa Herode mkuu aliyempelekea ombi kwake waondolewe. Lakini asingefanya hivyo walimwan dikia Tiberia ambaye aliwataka warejeshwe kaisaria kwa bahari (kama vile Philo, Legatio na Gaium, 299-305).

- f. Kupata Wasamaria wengi wachinjwe juu ya mlima Gerizim (mwaka 36/37b.k) walipokuwa wanalifuta vifaa vyao vitakatifu vya dini yao, ambavyo vilikuwa vimekwisha potea. Jambo hili lilimsababisha mkuu wake Pilato wa mahali pale (Vitellius, kiranja wa Ashuru) amwondoe kutoka ofsini na kumtuma Roma (kama vile. Josephus, Antiq. 18.4.1-2).
- 4. Sejanus alihukumiwa katika mwaka 31 b.k na Tiberia alirejeshwa kwenye mamlaka ya kisiasa kwahiyoy, #a, b, c, na d pengine zilifanywa na Pilato kupata imani kwa Sejanus' ; #e zingeweza kuwa ni majaribio ya kupata imani kwa Tiberia lakini yawezekana yakawa yamelipuka na kuharibika.
- 5. Ni dhahiri kwa amiri jeshi mfalme anayeunga mkono Wayahudi aliyerejeshwa pamoja na barua rasmi kwa mawakili kutoka Tiberia kuwa mwema kwa Wayahudi (kama vile Philo, Legatio na Gaium, 160-161), kwamba uongozi wa Kiyahudi katika Yerusalemu walichukua fursa ya udhaifu wa kisiasa wa Pilato na Tiberia na wakamrubuni ili amsababishe Yesu kusulubiwa. Nadharia ya Barnett inaleta pamoja mitazamo hiyo miwili ya Pilato katika njia inayoonekana kuwa yenye mantiki.

II. Hatma yake

- A. Aliitwa tena na alifika Roma mara tu baada ya kifo cha Tiberia (mwaka 37 b.k).
- B. Hakuteuliwa tena.

Mke wake hajulikani baada ya hili. Kuna nadharia nyingi za baadaye, lakini hakuna kweli zilizo salama.

☐"alipokuwa ametoa hukumu yake afunguliwe"Aya hii inarejelea juu ya "alipomkuta hana hatia," pamoja na kujaribu mara tatu kumwachilia (kama vile Luka 23:16,20,22). Wasomi wengi wanaamini kuwa kitabu cha Matendo kiliandikwa kuonyesha kwamba maafisa wa Kirumi hawakumkuta Yesu na hatia yoyote. Pilato alilazimishwa na uongozi wa Kiyahudi kufanya kile ambacho yeye mwenyewe alikikaidi.

**3:14"yule Mtakatifu, yule Mwenye haki"** Hili linaeleza dhahiri hali ya Yesu ya kutokuwa na hatia na dhambi. Mashtaka yalikuwa ya kipuuzi. Hili ni jina lingine la Kimasihi la Agano la Kale (kama vile Isa. 53:11; Matendo 7:52; 22:14; Yohana 6:69). Wale pepo wabaya walimwita Yesu mtakatifu wa Mungu katika Marko 1:24; Luka 4:34. Tazama Mada Maalum ifuatayo.

**MADA MAALUM : ALIYE MTAKATIFU**

- I. "Aliye Mtakatifu wa Israeli" ni jina la Uungu lililoshamiri katika Isaya (kama vile Isa. 1:4; 5:19; 10:17,20; 12:6; 17:7; 29:19,23; 30:11,12,15; 31:1; 37:23; 40:25; 41:14,16,20; 43:3,14,15; 45:11; 47:4; 48:17; 49:7; 54:5; 55:5; 60:9,14). Kwa sababu Yeye ni "mtakatifu," watu Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; 1 Pet. 1:16).

Jina hili, katika maana, linaeleza mvutano usiowezekana wa wenye dhambi, watu walioanguka kutii na kuingia katika kiwango cha utakatifu. Agano la Musa halikuwa na uwezekano wa kuutunza (kama vile Yos. 24:19; Matendo 15; Wagalatia 3; kitabu cha Waebrania). Agano la kale lilikuwa ni njia ya kuonyesha kutowezekana kwa wanadamu kukitii kiwango cha Mungu (Wagalatia 3), bado alikuwa pamoja nao, kuwaandaa kwa ajili ya jibu Lake katika hali ya kuanguka kwao (yaani, "Agano Jipya katika Yesu"). Akishusha kiwaango Chake, bali alikitoa kupitia Masihi Wake. Agano Jipya (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38) ni agano la imani na toba, na si utendaji wa mwanadamu, ingawa linatoa Ufanano wa Kristo (kama vile Yakobo 2:14-26). Mungu anamtaka mtu anaeangaza tabia yake kwa mataifa (kama vile Mt. 5:48).



II. "alivyo mtakatifu" inaweza kurejea juu ya

1. Mungu Baba (kama vile vifungu vingi vya Agano la Kale juu ya "aliye Mtakatifu wa Israeli")
2. Mungu Mwana (kama vile Mk 1:24; Luk. 4:34; Yohana 6:69; Matendo 3:14; 1 Yohana 2:20)
3. Mungu Roho (jina Lake, "Roho Mtakatifu" kama vile Yohana 1:33; 14:26; 20:22).

Matendo 10:38 ni mstari ambapo watu wote wa asili ya Mungu wanahusishwa katika kupakwa mafuta. Yesu alipakwa mafuta (kama vile Luka 4:18; Matendo 4:27; 10:38). Dhana imepanuka ili kuwajumuisha waamini wote (kama vile 1 Yohana 2:27). Aliyepakwa mafuta amekuwa mpakwa mafuta! Hii inaweza kuwa sambamba na Mpinga Kristo au wapinga Kristo (kama vile 1 Yohana 2:18). Katika Agano la Kale lilikuwa ni tendo la kiishara la kimwali la kumiminia mafuta (kama vile Kut. 29:7; 30:25; 37:29) inahusiana na wale ambao waliitwa na kuandaliwa na Mungu kwa ajili ya kuifanya kazi yake maalumu (yaani, manabii, makuhani, na wafalme). Neno "Kristo" ni tafsiri ya neno la Kiebrania "aliye pakwa mafuta" au Masihi.

## **MADA MAALUMU: HAKI**

"Haki" ni mada muhimu ambayo mwannafunzi wa Biblia yampasa kufanya upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana. Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinaelezwa kama "halali" au "haki" (kitenzi, BDB 842, KB 1003; nomino jinsia ya kiume, BDB 841, KB 1004; nomino jinsia ya kike, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na "mafungo ya mto" ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalumu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kistiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii anatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu. Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wawili halisi walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21). Mungu aliahidi kufanya marekebisha na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu: Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanae. Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko, hatua ya kwanza ya Mungu kuuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3). Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya aagano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

1. kutangaza haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, mahakama ya haki)
2. kwa kutoa haki huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kusingiziwa)
3. kumtoa Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu
4. kurejesha ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwitikio wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi 5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

1. Toba
2. Imani
3. Utii wa mtindo wa maisha
4. Ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, iliyojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinafsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo. Dhana inaitwa "haki kwa neema kupitia imani" (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani "mwenye haki" katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara 100.

Paulo, akiwa rabbi aliyefundishwa, anatumia neno *dikaiousunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiq* lililotumika katika Tafsihi za Maandiko ya Kale ya Kiyunani, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu, Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyingi limendwa katika maneno ya kimaagano (tazama Mada Maalumu: Agano). YHWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipya ili kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipya (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana). Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utofauti huu unaelezwa katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Kiingereza kama "haki" (yakihusiana na jamii) na "mwenye haki" (ikihusiana na dini).

Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufuo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msistizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungu [ utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakathoriki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoeleka].

Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenye kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu wa Edeni. Biblia inaanza kati Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (kama vile Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!

Ili kuthibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochgululiwa vya Agano Jipya vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

1. Mungu ni haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)
  - a. Warumi 3:26
  - b. 2 Wathesalonike 1:5-6
  - c. 2 Timotheo 4:8
  - d. Ufunuo 16:5
2. Yesu ni haki
  - a. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
  - b. Mathayo 27:19

- c. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
- 3. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki. Mambo ya Walawi 19:2
  - a. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
- 4. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki
  - a. Warumi 3:21-31
  - b. Warumi 4
  - c. Warumi 5:6-11
  - d. Wagalatia 3:6-14
- 5. Iliyotolewa na Mungu
  - a. Warumi 3:24; 6:23
  - b. 1 Wakorintho 1:30
  - c. Waefeso 2:8-9
- 6. Iliyopokelewa kwa imani
  - a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
  - b. 2 Wakorintho 5:7,21
- 7. kupitia matendo ya Mwana
  - a. Warumi 5:21
  - b. 2 Wakorintho 5:21
  - c. Wafilipi 2:6-11
- 8. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki
  - a. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
  - b. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
  - c. Waefeso 1:4; 2:10
  - d. 1 Timotheo 6:11
  - e. 2 Timotheo 2:22; 3:16
  - f. 1 Yohana 3:7
  - g. 1 Petro 2:24
- 9. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
  - a. Matendo 17:31
  - b. 2 Timotheo 4:8

Haki ni atabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenye dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

- 1. agizo la Mungu
- 2. zawadi ya Mungu
- 3. tendo la Kristo
- 4. maisha yapasayo kuyaishi

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudi, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana Naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohana 3:2) katika kifo au ujio wa pili!

Hapa kuna dondoo nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na Barua Zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa na kipengele cha kuachiliwa. Calvin anasistiza asili ya ajabu ya mawasiliano

au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

1. injili ni mtu (msistizo wa Kanisa la Mashariki na Calvin)
2. injili ni ukweli (msistizo wa Augustine na Luther)
3. injili ni maisha yaliobadilishwa (msistizo wa Katoliki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuungamanishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasisitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.

Yatupasa kumkaribisha Yesu!

Yatupasa kuiamini injili!

Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo!

☛"**mkataka mpewe mwuaji**" Hii ni kejeli kubwa kwamba Baraba ndiye aliyekuwa mtuhumiwa wa uhalifu halisi ambao walimshtumu Yesu kuhusiana na —uovu (kama vile Luka 23:18-19,23-25).

**3:15"mkamwua"** Inashangaza kwaba katika maandiko mengi yaliotaja juu ya kifo cha Yesu (kama vile Matendo ya Mitume 2:23,36; 3:15; 4:10; 5:30; 7:52; 10:39; 13:28) katika Matendo ya Mitume kwa uchache sana yameendelezwa karibu na mistari ya Mwa. 3:15 au Isaya 53. Pia kuna utofauti katika namna kifo Chake kilivyoelezwa.

1. alitundikwa msalabani – Matendo ya Mitume 2:23
2. alisuliibiwa msalabani – Matendo ya Mitume 2:36; 4:10
3. aliuawa – Matendo ya Mitume 3:15; 13:28
4. aliwekwa kifoni kwa kumtundika msalabani – Matendo 5:30; 10:39
5. aliuawa – Matendo ya Mitume

Ufufuo unasistizwa lakini si upatanisho ulio mbadala.

**NASB, NKJV** "Mkuu wa uzima"

**NRSV, NIV** "Muumbaji wa uzima"

**TEV** "Auongozaye uzima"

**NJB** "Mtawala wa uzima"

**Moffatt** "Mwongozaji wa uzima"

Jina hili inaakisi moja ya maana zile tatu zenye uhakika za neno *archēgos*:

1. muumbaji au mwanzilishi (kama vile NRSV, Ebr. 2:10; 12:2)
2. wakili wa uumbaji (kama vile Yohana 1:3; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2)
3. yule aendaye kwanza, muacha alama (kama vile TEV, NEB, Moffatt, Mdo. 5:3)

Hili neno kwa uwazi linatofautiana na "muuaji" (Matendo ya Mitume 3:14). Angalia Mada Maalum hapa chini.

## **MADA MAALUM : MWANZISHAJI/KIONGOZI (*archēgos*)**

Neno "mwandishi" au "kiongozi" nineno la Kiyunani *archēgos*. Hili linatokana na mzizi wa Kiyunan "mwanzo" (*archē*) na "kwenda" au "kuongoza" (*agō*). Huu uambatani ulikuja kutumika kwa kiongozi, mkuu, au kiongozi (mwanadamu au kimalaika). Neno hili halitumiki mara nne pekee katika Agano Jipya kurejea juu ya Yesu:

1. Mkuu wa uzima katika Matendo ya Mitume 3:15
2. Mkuu na Mwokozi Matendo ya Mitume 5:31

3. Kiongozi Mkuu wa wokovu wao katika Ebr. 2:10
  4. Aliyeanzisha (au mtangulizi) na mkamilishaji wa imani katika Ebr. 12:2
- Yesu nimwanzilishi, mtoaji, na mmalizaji wa wokovu.

☐ **"Mungu amemfufua katika wafu"** Mara nyingi katika Agano Jipya Baba ndiye aliyemfufua Mwana kutoka katika wafu kama alama ya ukubalifu wa maisha ya Yesu, mafundisho, na kifo cha mbadala. Pia Kitabu cha Agano Jipya kinathibitisha kwamba nafsi zote tatu za Utatu zilikuwa zikitenda kazi ndani ya ufufuo wa Yesu:

1. Roho (kama vile Rum. 8:11)
2. Mwana (kama vile Yohana 2:19-22; 10:17-18)
3. Baba (kama vile Matendo ya Mitume 2:24,32; 3:15,26; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 6:4,9)

Hiki ni kipengele kikuu cha kitheolojia cha neno *Kerygma* (tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:14). Ikiwa hili si la kweli, haya yote si ya kweli (kama vile 1 Kor. 15:12-19).

☐ **"mashahidi wake"** Kwa vyovyote hii ni

1. msisitizo katika vyanzo vya msingi vya vitu; wasikilizaji hawa walikuwa mashahidi wa macho (kama vile Matendo ya Mitume 2:22)
2. rejea inayowahusu Mitume na wanafunzi katika Chumba cha Juu (kama vile Matendo ya Mitume 1:22; 2:32)

Katika muktadha namba mbili inaonekana bora zaidi.

**3:16 "kwa imani"** Kifungu hiki kimetokea katika Flp.3:9. Neno la Kiyunani "imani" (*pistis*) linaweza kutafsiriwa katika lugha ya Kiiingereza kama "fimani," "sadiki," au "amini." Hii ni amri ya mwitikio wa kibinadamu kwa neema ya Mungu ya bure (kama vile Efe. 2:8-9). Kimsingi huku ni kusadiki kwa mwamini katika uaminifu wa Mungu (yaani, sifa Yake, Ahadi Zake, Masihi Wake) ama kuuamini uaminifu wa Mungu!

Ni vigumu katika maelezo ya Injili na kitabu cha Matendo kutoa ufafanuzi wa tukio (yaani, kimaagano) lililo upande wa kiroho. Wale wanaokolewa mara nyingi "hawaokolewi" (kama vile Yohana 5). Tazama Mada Maalum hapa chini. Kihisishi cha Kiyunani kilichotumika ndani ya kifungu hiki, *eis* (kama vile Flp. 3:9), ni haba pale kinapotumika kwa imani ya mtu katika Kristo (maelezo haya haya katika Matendo 2:38). Mara nyingi moja ya vihusishi kinatumika.

1. *dia* – Rum. 3:22, 25, 30; Gal. 2:16; 3:14,26; Efe. 2:8; 3:12,17; Kol. 2:12; 2 Tim. 3:15; 1 Pet. 1:5
2. *ek* – Rum. 9:30; 14:23; Gal. 3:8,9,22; 5:5; Yakobo 2:24
3. *en* – 1 Kor. 16:13; 2 Kor. 13:5; Gal. 2:20; 1 Tim. 3:13
4. maneno yote *eis* na *ek* yanatumika katika Rum. 1:1

Hiki hakikuwa kifungu sanifu "imani iokoayo."

## **MADA MAALUM : Imani, Amini, au Sadiki – (*Pistis* [nomino], *Pisteuō*, [kitenzi], *Pistos* [kivumishi])**

- A. Hili ni aina ya neno muhimu katika Biblia (kama vile. Ebr. 11:1,6). Lilikuwa ni somo la Yesu katika mahubiri ya awali (kama vile. Mk. 1:15). Kiwastani kuna mahitaji mapya mawili ya agano: toba na imani (Mk. 1:15; Mdo. 3:16, 19; 20:21)
- B. Asili na historia yake ya maneno haya
  1. Neno "imani" katika Agano la Kale lilimaanisha mtiifu, mwaminifu au mwaminifu wa kutumainiwa na yalikuwa ni maelezo ya asili ya Mungu na si yetu.
  2. Linatokana na neno la Kiebrania (*emun, emunah*, BDB 53, yaani., Hab. 2:4), ambalo mwanzo kabisa lilimaanisha "kuwa na uhakika au imara." Kuitumikia imani ni

- a. Kumkaribisha mtu (yaani., imani binafsi, sadiki, kama vile. E.1.hapo chini)
  - b. Kuamini imani kuhusu mtu (yaani., maandiko, kama vile. E.5.hapo chini)
  - c. Kuishi maisha kama ya mtu huyo (yaani., mfano wa Kristo)
- C. Matumizi yake katika Agano la Kale  
Lazima isisitiziwe kuwa imani ya Ibrahim ilikuwa si kwa ajili ya Masiha ajaye, lakini ni kwa ahadi ya Mungu ya kwamba atapata mototo na uzao (kama vile Mwa. 12:2-5; 17:4-8; Rum. 4:1-5). Ibrahim aliikubali ahadi hii kwa kumwamini Mungu (angalia Mada Maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika Agano la Kale) na neno lake. Bado anamashaka na kuhusika juu ya ahadi hii, ambayo ilimchukua miaka kumi na mitano kutimizwa. Imani yake isiyo kamili, hata hivyo, alikubaliwa na Mungu. Mungu anapenda kufanya kazi na mwanadamu mwenye mapungufu anayejongea kwake na katika ahadi zake kwa imani, hata kama kwa kipimo cha chembe ya haradari (kama vile. Mt. 17:20) au imani mchanganyiko (kama vile. Mark 9:22-24)
- D. Matumizi yake katika Agano Jipya  
Neno “kuamini” linatoka katika neno la Kiyunani *pisteuō* au nomino *pistis*, ambayo yanatafasiliwa kwa Kiingereza “kuamini” “amini” au “imani.” Kwa mfano, nomino haijitokezi katika injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna uwalakini katika uhalisia wa uwajibikaji wa kundi kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha. Mifano mwingine wa matumizi ya kubabiya ya neno hili “kuamini” ni katika Yohana 8:31-59 na Matendo 8:13, 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi ya uwajibikaji wa awali. Lazima ifuatishwe na mchakato wa uwanafunzi (kama vile Mt. 13:20-23, 31-32; 28:19-20)
- E. Matumizi yake ikiwa na vivumishi
1. *eis* inamaanisha “ndani ya.” Muundo huu wa kipekee unasisitiza waumini kuweka imani zao kwa Yesu
    - a) ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
    - b) ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45,48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Fil. 1:29; 1 Petr. 1:8)
    - c) ndani yangu (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
    - d) ndani ya mwanaye (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
    - e) ndani ya Yesu (Yohana 12:11; Mdo. 19:4; Gal. 2:16)
    - f) ndani ya nuru (Yohana 12:36)
    - g) ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
  2. *ev* inamaanisha “katika” kama ilivyo katika Yohana 3:15; Mark 1:15; Mdo. 5:14
  3. *epi* ikimaanisha “katika” au “juu ya” kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo. 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6
  4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10
  5. *hoti* likimaanisha “kuamini kwamba,” inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
    - a) Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
    - b) Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
    - c) Yesu katika Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
    - d) Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
    - e) Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
    - f) Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
    - g) Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
    - h) Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30)
    - i) Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye “Mimi ndiye” (Yohana 8:24; 13:19)
    - j) Tutaishi naye (Rum. 6:8)
    - k) Yesu alikufa na kufufuka tena (1The. 4:14)

## ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 3: 17-26

<sup>17</sup>Basi sasa, ndugu, najua ya kuwa mliyatenda haya kwa kutokujua kwenu, kama na wakuu wenu walivyotenda. <sup>18</sup>Lakini mambo yale aliyohubiri Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote, ya kwamba Kristo wake atateswa, ameyatimiza hivyo. <sup>19</sup>Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; <sup>20</sup>apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani; <sup>21</sup>ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu. <sup>22</sup>Kwa maana Musa kweli alisema ya kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi. <sup>23</sup>Na itakuwa ya kwamba kila mtu asiyemsikiliza nabii huyo ataangamizwa na kutengwa na watu wake. <sup>24</sup>Naam, na manabii wote tangu Samweli na wale waliokuja baada yake, wote walionena, walihubiri habari za siku hizi. <sup>25</sup>Ninyi mmekuwa watoto wa manabii na wa maagano yale, ambayo Mungu aliagana na baba zenu, akimwambia Ibrahimu, Katika uzao wako kabila zote za ulimwengu zitabarikiwa. <sup>26</sup>Mungu, akiisha kumfufua mtumishi wake Yesu, alituma kwenu ninyi kwanza, ili kuwabarikia kwa kumwepusha kila mmoja wenu na maovu yake.

**3:17 "najua ya kuwa mliyatenda haya kwa kutokujua kwenu"** Aya hii inaakisi maneno ya Yesu alipokuwa msalabani (kama vile Luka 23:34). Hata hivyo, hata katika kutokujua kwao, watu hawa kiroho wallipaswa kuwajibika! Kwa namna nyingine sababu hii ilikuwa njia ya kuwasaidia watu kukubali jukumu lao wenyewe (kama vile Matendo 13:27; 17:30; 26:9; 1 Kor. 2:8). Kwa mjadala mzuri wa dhana hii tazama Millard Erickson, *Christian Theology*, toleo la 2, kr. 583-585.

☐ **"kama na wakuu wenu walivyotenda"** Luka mara nyingi anatengeneza tofauti kati ya watu na viongozi wao (kama vile Luka 7:29-30; 23:35; Matendo ya Mitume 13:27; 14:5). Jambo la uhakika katika kujaribu kulifanya hili linaweza kuwa jukumu la makundi yote mawili. Mara nyingi inaelezwa kwamba Yesu hakuwashutumu Wayahudi kama kundi zima, bali ule ukinyume wao (yaani, sio wa uzao wa Aruni) viongozi. Hakika ni vigumu kufahamu kama kulaani mti wa mtini (kama vile Marko 11:12-14,20-24) na ule mfano wa wakulima waovu ndani ya shamba la mizabibu (kama vile Luka 20:9-18) ni shtutuma za Dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza au viongozi wake pekee. Luka anatoa maelezo kuhusu mifano yote miwili!

**3:18"aliyohubiri Mungu tangu zamani"** Injili haikuwa wazo mbadala la Mungu, bali umilele Wake, mpango wa makusudi (kama vile Mwa. 3:15; Marko 10:45; Luka 22:22 Matendo ya Mitume 2:23; 3:18; 4:28; Rum. 1:2, angalia Mada Maalum katika Matendo 1:8). Hotuba za kale katika Matendo ya Mitume (*kerygma*, tazama Mada Maalum 2:14) yanamwonyesha Yesu kama utimilifu wa ahadi za Agano la Kale na unabii.

Kuna vipengele kadhaa vya *Kerygma* (yaani, vipengele vikuu vilivyovya vya kitheolojia vya zile hotuba katika Matendo) vinaelezwa katika mistari hii.

1. imani katika Yesu ni muhimu
2. nafsi ya Yesu na kazi vilitabiriwa na manabii wa Agano la Kale
3. itampasa Masihi kuteswa
4. yawapasa kutubu
5. Yesu atarudi tena.

☐ **"Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote"** Yesu alitimiza ubabii wa Agano la Kale (kama vile Matendo ya Mitume 3:34, Mt. 5:17-48). Nafikiri Yesu mwenyewe alijionyesha katika barabara ya kwenda Emau (kama vile Luka 24:13-35) unabii wa Agano la Kale ambao unaendana na mateso Yake, na ufufuo. Walilishiriki hili

pamoja na Mitume, ambao walilifanya sehemu ya mahubiri yao (kama vile Luka 24:45).

☐ **"Kristo"** Hii ni Tafsiri ya Kiyunani ya neno la Kiebrania "Masihi" (tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:31), ambalo linamaanisha Mpakwa Mafuta. Neno hili linarejelea juu ya nguvu ya Mungu ya kipekee ambayo maisha na kifo vinatambulisha zama mpya za haki, zama za Roho.

Uthibisho kwamba Yesu alikuwa/ ni Kristo/Masihi aliyehaidiwa na YHWH imekuwa dhamira ya mara kwa mara ya mahubiri ya Matendo.

1. Petro – 2:31; 3:18; Matendo ya Mitume 5:42; 8:5
2. Paulo – 9:22; 17:3; Matendo ya Mitume 18:5,28

☐ **"atateswa"** Hili lilidokezwa katika maandiko kadhaa ya Agano la Kale (kama vile Mwa. 3:15; Zaburi 22; Isaya 53; Zek. 12:10). Kipengele hiki cha Masihi ateswaye kiliwashangaza Wayahudi (kama vile 1 Kor. 1:23). Walikuwa wakitarajia Kamanda atshindaye (kama vile Ufu. 20:11-16). Hii ilikuwa dhamira ya mara kwa mara ya hotoba za Kitume katika Matendo

1. Paulo (kama vile Matendo ya Mitume 17:3; 26:23)
2. Petro (kama vile Matendo ya Mitume 3:18; 1 Pet. 1:10-12; 2:21; 3:18)

**3:19**"**Tubuni basi, mrejee**" Neno la Kiyunani "kutubu" linamaanisha kubadili fikra. Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu wa neno *metanoeō*. Neno la Kiebrania toba linamaanisha "kubadili tendo" ("kurejea" neno [*emistrephō*] linaweza kuakisi neno la Kiebrania "kurudi" *shub*, kama vile Hes. 30:36; Kumb. 30:2,10) katika Maandishi ya Kale ya Kiyunani.

Toba ni kipengele cha agano muhimu ndani ya wokovu pamoja na imani (kama vile Marko 1:15 na Matendo ya Mitume 3:16,19; 20:21). Kitabu cha Matendo kinalitaja hili mara kwa mara (kama vile Petro – 2:38; 3:19,26 na Paulo – 14:15; 17:30; 20:21; 26:20). Toba ni muhimu (kama vile Luka 13:3 na 2 Petro 3:9). Kimsingi huu ni utayari wa kubadilika. Hili ni tendo la hiari na neema ya Mungu (kama vikle Matendo ya Mitume 5:31; 11:18; 2 Tim. 2:25). Tazama Mada Maalum katika Matendo 2:38.

☐ **"ili dhambi zenu zifutwe"** Hili neno linamaanisha "kupangusa"; "kuondoa waa"; au "kufuta" (kama vile Kol. 2:14; Ufu.3:5; 7:17; 21:4). Ni ahadi iliyoje! Katika ulimwengu wa kale wino ulikuwa tindikali na ndivyo ilivyokuwa, hivyo, isingewezekana kuufuta. Huu ni muujiza wa kweli wa neema ya Mugu (kama vile Zab. 51:1; 103:11-13; Isa. 1:18; 38:17; 43:25; 44:22; Yer. 31:34; Mika 7:19). Mungu anaposamehe, Mungu husahahu (hufuta)!

☐ **"nyakati za kuburudishwa"** Neno la Kiyunani (*anapsuchō, anapsuxis*) kimsingi linamaanisha "mahali pa kupumzikia, ulegezaji, tulizo" (Baker, Arndt, Gingrich, na Danker, *A Greek-English Lexicon*, uk. 63), "kuchangamka kutokana na upepo mwanana," au "kutibu majeraha kwa kutulizwa" (Kittle, *Theological Dictionary of the New Testament*, juzuu. 9, uk. 663). Upanuzi wa kistiari ni wa kimwonekano au kiburudisho au urejesho. Katika Maandiko ya Kale neno hili linatumika katika kupata nguvu za kimwili upya baada ya mapambano (kama vile Kut. 23:12; Amu. 15:19; 2 Sam. 16:14) au burudani ya kihisia kama katika 1 Sam. 16:23. Marejeleo ya Petro yanaonekana kuwa ahadi za Agano la Kale, lakini kifungu hiki hakitumiki katika Agano la Kale.

Kwa watu wa eneo la jangwani walitambuliwa kwa uhuru na furaha, walipokaribia katika maeneo haya kulikuwa na ishara za mateso na taabu. Mungu alikuwa anakwenda kuleta upanuzi, nyakati za burudani ya kazi ya kiroho. Hii kazi ya ki-Masihi imekuja katika injili. Zile "nyakati za burudani" zimekuja ndani ya Yesu wa Nazarethi. Hata hivyo, ujio wa utimilifu ungeleta nyakati mpya za Roho. Katika muktadha huu wa kipekee Petro anarejelea ule Ujio wa mara ya Pili. Kifungu hiki kinaonekana kufanana na "kipindi cha urejesho" (Matendo ya Mitume 3:21). Tazama Mada Maalum: Mafundisho ya Awali (Kerygma) katika Matendo ya Mitume 2:14.

**3:20**"**apate kumtuma Kristo Yesu** " Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu, ambayo inadokeza ishara zisizotarajiwa. Matendo ya wasikilizaji wa Petro, katika maana nyingine, yalitambulisha nyakati za utimilifu



wa kiroho (kama vile F. F. Bruce, *Answers to Questions*, ambapo anaunganisha Matendo ya Mitume 3:19-21 na Rum. 11:25-27, uk.201).

Usambamba wa jina "Yesu" baadaye "Kristo/Masihi" unaonekana kumaanisha kwamba kwa upekee Petro anaeleza u-Masihi wa Yesu wa Nazarethi. Baadaye katika Agano Jipya, jina "Bwana," "Yesu," na "Kristo" limetokea mara kwa mara zaidi kama rejeo lililounganishwa kwa Yesu (yani, Bwana Yesu Kristo) kuliko ule msistizo wa jina la Masihi. Hili ni kweli hasa katika makanisa ya mataifa makuu.

☐"**mliyewekewa tangu zamani**" Kitenzi hiki ni kauli tendewa endelevu ya wakati timilifu. Neno kama hili linatumika kuwazungumzia mashahidi waliochaguliwa na Mungu katika Matendo ya Mitume 10:41; 22:14; 26:16; Ujio na kufa kwa Yesu mara nyingi umekuwa mbango wa Mungu wa ukombozi a milele (kama vile Matendo ya Mitume 2:23; 3:18; 4:28; 13:29).

Katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani neno hili linaakisi chaguo, lakini bila utambuzi wa awali (yaani, kwa Luka neno "kabla ya" linamaanisha kabla, kama vile Kut. 4:13 na Yos. 3:12), ambalo linaonekana wazi katika matumizi haya ya maneno ndani ya Matendo. Inaeleza kwamba kumtuma Yesu ulikuwa uchaguzi wa Mungu wa baraka na ukombozi!

### 3:21

<b>NASB, NKJV</b>	<b>"ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"ambaye ilimpasa kukaambinguni"</b>
<b>TEV, NIV</b>	<b>"Iimpasa kukaa mbinguni"</b>
<b>NJB</b>	<b>"ambaye mbingu ilimpasa kumtunza"</b>

Kiima cha kifungu hiki ni "mbinguni";kiarifu ni "ambaye (yaani, Yesu). Kuna vitenzi viwili katika kifungu hiki. Cha kwanza ni *dei*, kutokana na *deō*, amabacho kinamaanisha "hili ni muhimu" au "ihili ni sahihi" Tazama maelezo kamaili katika Matendo ya Mitume 1:16.

Cha pili ni ile kauli ya kati ya wakati uliopita usio timilifu (yenye ushahidi) kitenzi jina cha neno *dechomai*. Harold K Moulton, *The Analytical Greek Lexicon Revised* anasema katika muktadha huu hiki kitenzi kinamaanisha "kupokea na kutunza" (uk. 88). Unaweza kuona ni kwa jinsi gani tafsiri za Kiingereza zinajieleza katika kipengele cha kimuktadha. Luka analitumia neno hili zaidi ya mwandishi mwingine wa Agano Jipya (mara 13 katika Luka na mara 8 katika Matendo ya Mitume ). Lazima maneno yatolewe ufafanuzi katika nuru ya matumizi ya kimuktadha na maana, si asili ya neno. Misamiati (kamusi) inadokeza matumizi tu. Haiweki mpangilio wa ufafanuzi!

<b>NASB</b>	<b>"hata"</b>
<b>NKJV, NRSV,</b>	
<b>TEV</b>	<b>"mpaka"</b>
<b>NJB</b>	<b>"hadi"</b>

Neno hili liko katika maandiko ya Kiyunani ya Toleo la UBS<sup>4</sup>. Sifahamu ni kwa nini tafsiri ya NASB, toleo la mwaka 1995, inaweka maandishi katika mtindo wa mlazo, ambayo ni njia ya kuonyesha kuwa hili halipo katika maandiko ya Kiyunani, bali yalitolewa kwa wasomaji wa Kiingereza kwa kusudi la kuelewa. Katika toleo la mwaka 1970 la tafsiri ya NASB, kibainishi "hiki" kiko katika mtindo wa mlazo na si "hata," ambacho ni sahihi.

☐"**zamani za kufanywa upya vitu vyote**" Aya hii inarejelea juu ya uumbaji mpya (kama vile Mt. 17:11; na hasa Rum.8:13-23). Uhasi wa uovu wa mwanadamu katika Mwanzo 3 unathibitishwa na uumbaji unarejeshwa; ushirika pamoja na Mungu unahimarishwa. Kusudi asilia la uumbaji hatimaye linakamilishwa.

☑ **"zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu"** Injili ya Marko inaanza na nukuu kutoka Mal. 3:1. Mathayo 1:22-23 inayorejelea juu ya unabii wa Isa. 7:14. Luka anakitumia kifungu hiki hiki katika Luka 1:70. Moja ya kipengele cha *Kerygma* {Mafundisho ya Awali} (yaani, kweli za kitheolojia za mara kwa mara ndani ya hotuba katika Matendo tazama Mada Maalum katika, Matendo ya Mitume 2:14) ni kwamba kuzaliwa kwa Yesu, uhai, kifo, na ufufuo vilitimizwa na unabii wa Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-19). Huduma ya Yesu haikuwa wazo mbadala au Mpango B. Huu ulikuwa uamuzi wa Mungu wa kabla (kama vile Matendo ya Mitume 2:23; 3:18; 4:28; 13:29, tazama Mada Maalum katika Matendo yaume Mit1:8). Mambo yote yanatenda kazi nje ya utimilifu wa urejesho wa jumla wa mapenzi ya Mungu kwa ajili ya uumbaji.

**3:22 "Musa kweli alisema"** Jina "Nabii" lilitumika kumaanisha yule Masihi (kama vile Kumb. 18:14-22; hasa.15,18; Yohana 1:21,25). Kumbukumbu hii ya Yesu kutoka Sheria ya Musa (yaani, sehemu ya kimamlaka zaidi ya kanuni za kanisa la Agano la Kale kwa Wayahudi, wote Masadukayo na Mafarisayo) zingekuwa za muhimu kwa hawa wasikilizaji wa Kiyahudi. Yesu amekuwa mpango wa Mungu wa ukombozi mara kwa mara (yaani, Mwa. 3:15). Alikuwa kwa ajili ya kutufia (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21).

**3:23** Hili lilikuwa neno la maonyo lenye maana kubwa. Hili ni dokezo la Kumb. 18:19. Kukataliwa kwa Yesu kulikuwepo, na bado kupo, kuna maana kubwa, ni suala la milele.

Dokezo hili la Kumb. 18:14-22 pia lina umuhimu wa tambuzi za ndani za kitheolojia.

1. Tambua vipengele vyote vya binafsi na vile vya ushirika. Kila nafsi ya mtu kibinafsi lazima iwe na mwitikio kwa Masihi. Inatosha kuwa sehemu ya ushirika wa mwili wa Israeli.
2. Kifungu "ataangamizwa na kutengwa" ni dokezo la "vita takatifu." Mungu ataondoa mzabibu wake Mwenyewe (yaani, Israeli, kama vile Yohana 15; Rum. 9-11). Wale wanaomkataa "Nabii" wanakataliwa na Mungu. Suala la wokovu ni mwitikio wa imani ya mtu kwa Masihi wa Mungu. Familia, rangi, maadili, na uangalifu wa utendaji wa sheria si vigezo vya agano la wokovu, bali imani katika Kristo (kama vile 1 Yohana 5:12).

**3:24 "Samweli"** Katika sheria za kanisa la Kiyahudi huyu (yaani, 1 Samueli) anafikiwa kama moja ya "Manabii wa Mwanzo," mbali na mgawanyo wa pili wa sheria za kanisa la Kiebrania. Samueli aliitwa nabii katika 1 Sam. 3:20 na pia mwonaji (yaani, kwa neno lingine nabii) katika 1 Sam. 9:9; 1 Nya. 29:29.

☑ **"siku hizi"** Zile "nyakati za burudani" (Matendo 3:20) na "nyakati za urejesho wa mambo yote" (Matendo 3:21) rejea juu ya utimilifu wa Ufalme wa Mungu katika kurudi kwa Kiristo, lakini kifungu hiki kinarejelea juu ya uanzilishi wa Ufalme wa Kimasihi, ambao ulitokea katika umbo-mwili la Yesu huko Bethlehemu au yapata kipindi kizima cha siku za baadaye, ambacho ni nyakati kati ya mionekano miwili ya Kristo katika sayari ya dunia. Kitabu cha Agano la Kale kimsingi kiliumtambua ujio mmoja pekee wa Masihi kama "Mtumishi Ateswaye" (Matendo 3:18) hii ilishangaza; Ujio Wake wa utukufu kama kiongozi wa kijeshi na hakimu ulitarajiwa.

**3:25** Petro anawaeleza hawa Wayahudi kama wana wa Abrahamu, watu wa agano. Hata hivyo, maagano haya lazima yaitikiwe katika imani na toba kwa Yesu na injili ama hawa watakaliwa (Matendo ya Mitume 3:23)! Kitabu cha Agano Jpya (agano jipya) kinatazamia undani wa mtu, si ubaguzi wa kimakundi. Katika wito wa mkuu wa Abram kuikuwa na ishara za kuilimwengu (kama vile Mwa. 12:3). Kujitoka kiulimwengu kumekuja katika Kristo na kunapatikana kwa wote (yaani, Luka kwa msingi wa Mataifa. Injili yake na Kitabu chake cha Matendo kiliufanya mwaliko huu kurudiwa rudiwa na kwa upekee).

☑ **"maagano"** Tazama [MADA MAALUM: AGANO](#) katika Matendo 2:47.

☑ **"uzao wako kabila zote za ulimwengu zitabarikiwa"** Hii aya inarejerea juu ya ahadi ya Mungu kwa Abrahamu katika Mwa. 12:1-3. Tambaua ishara ya kiulimwengu pia katika Mwa. 22:18. Mungu alimchagua Abrahamu ili awachaague watu, kuuchagua ulimwengu (kama vile Kut. 19:5-6; Efe. 2:11-3:13). Tazama Mada Maalum katika Matendo1:8.

**3:26"kwenu ninyi kwanza"** Wayahudi, kwa sababu ya urithi wa Kimaagano, wanayo fursa ya kwanza ya kuusikia na kuelewa ujumbe wa injili (kama vile Rum. 1:16; 9:5). Hata hivyo, hawa lazima waitikie katika njia ile ile kama ilivyo kwa kila mtu: toba, imani, ubatizo, utii, na ustahimilivu.

☑ **"akiisha kumfufua mtumishi wake"** Tazama maelezo katika Matendo ya Mitume 2:24 na 3:13.

☑ **"kuwabarikia"** Hivi ndivyo Mungu anavyotaka kwa wanadamu wote (kama vile Mwa. 12:3). Hata hivyo, Yeye alimtuma Yesu kwanza kwa kondoo nyumba ya Israeli waliopotea!

☑ **" kwa kumwepusha kila mmoja wenu na maovu yake"** Wokovu unahusisha mabadiliko ya fikra kuhusu dhambi pamoja na matokeo ya mabadiliko ya matendo na vipaumbele. Haya mabadiliko ni ushahidi wa mageuzi ya kweli! Maisha ya milele yana sifa zenye kuitazamika!

### **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa mfasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini maana ya "mfululizo"?
2. Kwa nini uponyaji huu una nguvu sana"
3. Kwa nini Masihi mwenye kuteswa alikuwa hofu sana kwa Wayahudi?
4. Kwa nini Luka anainukuu Mwa. 12:3?
5. Je! Wayahidi waliokolewa tofauti na watu wa Mataifa?

## MATENDO YA MITUME 4

<b>MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Petro na Yohana Mbele ya baraza 4:1-4	Petro na Yohana wanakamatwa 4:1-4	kukamatwa na kuachiwa kwa Petro na Yohana 4:1-4	Petro na Yohana mbele ya baraza 4:1-4	Petro na Yohana mbele ya Wakuu wa Sinagogi 4:1-4
4:5-22	Kuhutubia baraza la Sinagogi 4:5-12 Kukatazwa kwa Jina la Yesu 4:13-22	4:5-12  4:13-22	4:5-7 4:8-12  4:13-17 4:18-22	4:5-12  4:13-17 4:18-22
Waamini waomba Kwa ujasiri 4:23-31	maombi ya ujasiri 4:23-31	4:23-31	waamini waomba kwa ujasiri 4:23-30  4:31	maombi ya mitume ktk mateso 4:23-26 4:27-31
Vitu vyote Ktk shirika 4:32-37	kushirikishana vitu vyote 4:32-37	kushirikishana vitu  (4:32-5:6) 4:32-5:11	waamini wakishiri- kishana mali zao 4:32-35  4:36-37	jamii ya kanisa la kwanza 4:32 4:33 4:34-35 Ukarimu wa Barnaba 4:36-37

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" ("A Guide to Good Bible Reading"))

### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Ni dhahiri kwamba mgawanyo wa sura sio sawa katika Matendo ya Mitume. Kumbuka, mgawanyo wa Sura, mgawanyo wa mistari, uwekaji wa Huanza kwa herufi kubwa, mgawanyo wa aya, na uwekaji wa alama mbali mbali vyote sio jambo la kiasili katika maandiko ya Kiyunani na hivyo ni kazi ya kamati za fasiri za kisasa.
- B. Mistari ya 1-31 inazungumzia habari ya uponyaji wa mtu aliyekuwa kiwete katika Matendo ya Mitume 3 na madhara yake.
- C. Mistari ya 32-37 lazima iende na Matendo ya Mitume 5:1-11.
- D. Tatizo la kanisa la kwanza linazidi kuendelea na kukua lakini pia neema na nguvu ya Roho.
- E. Katika kushughulikia msisitizo wa Luka, wafasiri wa kisasa wa Magharibi lazima wafanye ulinzi dhidi ya ubaguzi wa "kibepari". Luka anaonekana kukiri ufanano wa kujitolea. Matendo ya Mitume haiwezi kusaidia ujamaa wala ubepari kwasababu haikuwa ikijulikana wakati wa muda huo. Andiko lazima lifasiriwe kwa uwazi, kusudio la mwandishi na ulimwengu wa wasikiaji.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 4:1-4

<sup>1</sup> Hata walipokuwa wakisema na watu wale, makuhani na akida wa hekalu na Masadukayo wakawatokea, <sup>2</sup> wakifadhaika sana kwa sababu wanawafundisha watu na kuhubiri katika Yesu ufufuo wa wafu. <sup>3</sup> Wakawakamata, wakawaweka gerezani hata asubuhi; kwa kuwa imekwisha kuwa jioni. <sup>4</sup> Lakini wengi katika hao waliosikia lile neno waliamini; na hesabu ya watu waume ikawa kama elfu tano.

**4:1 "makuhani"** Hili ni neno linalotumika katika maandiko ya kale ya Kiyunani,  $\kappa$ , A, D, na E, lakini MS C ina "makuhani wakuu" (*archiereis*). Toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa neno "makuhani" alama ya B (karibu na hakika). Muktaadha wa Matendo ya Mitume 4 inaonesha kwamba upinzani haukutoka kwa Makuhani wakuu (kama vile Matendo ya Mitume 4:6). Katika Agano la Kale kabila la Walawi (yaani kabila la Musa na Aruni) walichaguliwa na YHWH badala ya "wazaliwa wa kwanza" (kama vile Kutoka 13). Ndani ya kabila hili walikuwa na familia Fulani zilizotumika kama

1. walimu wa sheria wa mahali
2. watumishi wa Hekaluni
3. makuhani waliofungua hekalu rasmi na hasa ikijumuisha taratibu za utoaji wa sadaka (kama vile Mambo ya Walawi 1-7)

Familia Maalum ambayo Kuhani Mkuu ilikuwa lazima atoke katika familia ya Musa na Aruni. Hili kabila lote halikupokea gawio la ardhi kama makabila mengine. Walikuwa na majiji fulani yaliyogawiwa kwa kiasi Fulani (yaani 48 miji ya kikuhani, kama vile Joshua 20). Hizi familia za kikuhani zilitegemea makabila mengine kuwasaidia kupitia malipo ya Zaka na zaka ya mwaka wa tatu. Mambo yote haya yalibadilika wakati Rumi ilipoichukua Palestina. Ofisi ya Kuhani Mkuu ilinunuliwa kutoka Rumi. Haikuendelea kuwa ofisi ya kiroho ya Agano la Kale, lakini ya kibiashara, ofisi ya nguvu ya kisiasa. Kuhani Mku wakati huu alikuwa ni Kayafa (kama vile Mt. 26:3; Luka 3:2; Yohana 18), Lakini nguvu halisi ilikuwa nyuma ya ofisi ya Kuhani Mkuu aliyepita (kama vile Luka 3:2; Yohana 18:13,24; Mdo. 4:6). Familia hii ilikuwa ya dhehebu la Masadukayo ya dini ya kiyahudi.

▣ **"akida wa hekalu"** Hii ilikuwa ni ofisi maalum ya kikuhani ambayo ilikuwa inafuatia kimamlaka baada ya ofisi ya kuhani Mkuu (kama vile Josephus, *Wars* 6.5.3). Angeweza kutawala juu ya maakida wa hekaluni (kama vile 1 Nyakati 9:11; Neh. 11:11; Luka 22:4,52; Mdo. 5:24,26). Katika kiebrania alitwa "mtu wa mlima wa nyumba."

▣ **"Masadukayo"** Hawa walikuwa matajiri, viongozi wa kisiasa wa wakuu wa sinagogi

## MADA MAALUM: MASADUKAYO)

- I. Chimbuko la Kundi
  - A. Wasomi wengi wanaamini kuwa jina hili linatokana na Sadoki, mmoja wa makuhani wakuu wa Daudi (kama vile 2 Sam. 8:17; 15:24). Baadaye, Suleimani alimhamisha Abiathari kwa kuunga mkono uasi wa Adonia (kama vile 1 Flp. 2:26-27) na alimtambua Sadoki kama Kuhani Mkuu pekee (kama vile 1 Flp. 2:35). Baada ya uhamisho wa Babeli huu mpangilio wa kikuhani uliimarishwa tena katika Yoshua (kama vile Hag. 1:1). Hii familia ya Kilawi ilichaguliwa kwa ajili ya kusimamia hekalu. Baadaye wale waliokuwa miongoni mwa haya mapokeo ya kikuhani na wale wasaidizi wao waliitwa Wasadoki au Masadukayo.
  - B. Ile karne ya tisa B. K. mapokeo ya Walimu wa Kisheria kwa Dini ya Kiyahudi neno (*Aboth* Mwalimu wa Sheria) anasema Sadoki alikuwa mwanafunzi wa Antigonos wa Sokho (karne ya pili K.K.). Sadoki hakuelewa usemi maarufu wa mshauri wake, "baada ya kifo thawabu," na kuiendeleza thiolojia ambayo ilipingwa hapo nyuma na, ambapo pia ufufuo wa mwili ulipingwa.
  - C. Baadaye ndani ya Dini ya Kiyahudi Masadukato walitambuliwa na wafuasi wa Boethus. Boethus pia alikuwa mwanafunzi wa Antigonos wa Sokho. Huyu aliikuza theolojia ile ile ya Sadoki, ambayo ilipingwa hapo nyuma.
  - D. Hili jina Masadukayo halikuonekana hadi siku za Yohana Hyrcanus (135-104 B.K.), ambapo lilinukuliwana Josephus (kama vile *Antiquities* 13.10.5-6). Katika *Antiquities* 13.5.9 Josephus anasema hawa wanaishi "shule tatu za," Mafarisayo, Masadukayo, na Wa-Essene.
  - E. Kuna nadharia za uamsho ambazo zilitokana na kile kipindi cha juhudi za utawala wa Selucid kuwafanya wawe wayunani ukuhani uliokuwa chini ya Antiokio IV Epiphanes (175-163 K.K.). Wamakabayo walipoasi ukuhani mpya ulianza katika Simoni Makabayo (142-135 K.K.) na uzao wake (kama vile I Mak. 14:41). Hawa makuhani wakuu wapya wa Hasmonia bila shaka walikuwa mwanzo wa makuhani wakuu yawezekana ulikuwa mwanzo wa utawala wa Masadukayo wa kimakabila. Mafarisayo walihimarika katika kipindi hiki kutoka Hasidim (yaani, "waliotengwa," kama vile I Mak. 2:42; 7:5-23).
  - F. Kuna nadharia mpya (yaani, T. W. Manson) ambayo "Sadukayo" ni tafsiri ya neno la Kiyunani *sundikoi*. Hili neno lilirejea juu ya mamlaka za mahali pale pale ambazo zilijitokeza pamoja mamlaka ya Kirumi. Hili linaweza kueleza kwanini baadhi ya Masadukayo hawakuwa makuhani wa utawala wa kimakabila, bali walikuwa mojawapo ya Wakuu wa baraza la Sinagogi.
- II. Upekee wa Imani
  - A. Haya yalikuwa makundi madogo madogo ya kikuhani yasiyobadili msimamo (hawa walikubali kuwa Torati pekee kama iliyovuviwa) wa madhehebu ya maisha ya Kiyahudi wakati Hasmonian na vipindi vya Kirumi.
  - B. Hawa hasa walihusika na matukio ya hekalu, hitifaki, taratibu za dini, na liturujia.
  - C. Hawa walishikilia Torati iliyoandikwa yaani, Mwanzo – Kumbukumbu la Torati) kama utawala wa kikabila, lakini waliipinga desturi ya Orad (yaani, Buku la Sheria za Kiyahudi).
  - D. Hawa, kwa hiyo, walipinga mafundisho mengi yaliyotunzwa na kuendelezwa Mafarisayo
    1. ufufuo wa mwili (kama vile Mt. 22:23; Marko. 12:18; Luka 20:27; Matendo ya Mitume 4:1-2; 23:8)
    2. kufa kwa nafsi (kama vile *Antiquities* 18.1.3-4; *Wars* 2.8.14)
    3. uwepo wa kueleza mpangilio wa malaika (kama vile Matendo ya Mitume 23:8)
    4. hawa walichukulia "jino kwa jino" (yaani, *lex talionis*) kiuhalisi na waliunga mkono adhabu ya kimwili na adhabu za kifo (badala ya mapatano ya kifedha)
  - E. Eneo lingine la kithiolojia ilikuwa ni upinzani dhidi ya wazo la awali dhidi ya mapenzi huru. Ni makundi matatu yaliyotajwa na Josephus
    1. Wa-Essene walikubali aina ya nadharia ya maamuzi
    2. Masadukayo waliuondoa ule msisitizo juu ya mapenzi huru ya mwanadamu (kama vile *Antiquities* 13.5.9; *Wars* 2.8.14)

3. Mafarisayo walishikilia namna fulani ya usawa wa uelekeo kati ya haya mawili
- F. Katika maana moja ya migogoro kati ya makundi mawili (yaani, Masadukayo – Mafarisayo) yaliyoangalia mvutano kati ya makuhani na manabii wa Kitabu cha Agano la Kale. Mvutano mwingine ulizuka kutokana na ukweli kwamba Masadukayo waliwakilisha daraja la kijamii na umiliki wa ardhi. Hawa walikuwa wenye mamlaka (kama vile Josephus' *Antiquities* 13.10.6; 18.1.4-5; 20.9.1), ambapo Mafarisayo na waandishi walikuwa wasomi na wacha Mungu miongoni mwa watu wa mahali pale. Mvutano huu ungeweza kubainishwa kama hekalu humo Yerusalemu dhidi masinagogi ya maeneo yote.

Mvutano mwingine unaweza kuwakilisha ule ukaidi wa Masadukayo wa ushawishi wa mafundisho ya Zorostra juu ya thiolojia ya kifarisayo. Mifano ya thiolojia yao ni (1) elimu ya juu ya kimalaika iliyokuzwa sana; (2) ule uwili kati ya HWH na Shetani; na (3) maelekezo mapendekezo ya maisha ya nyuma katika kukua kwa maneno ya wazi. Haya mazidi ya wa-Essene na Mafarisayo walisababisha mwitikio wa kithiolojia wa Masadukayo. Walirudi kwenye kushikiria nafasi yao ya thiolojia yao ya Musa tu katika kujaribu kuzuia mawazo mengine ya makundi mengine ya kiyahudi.

### III. Chimbuko la Taarifa

- A. Josephus ndiye chimbuko kuu la taarifa kuhusu Masadukayo. Alikuwa mbaguzi wa kujitoa kwake kwa Mafarisayo na nia katika kuweka wazi taswira chanya ya maisha ya kiyahudi ya Warumi.
- B. vyanzo vingine vya taarifa ni fasihi ya kiualimu. Hata hivyo, hapa, pia, ubaguzi wa nguvu ni dhahiri. Masadukayo walikataa uhusiano na mamlaka ya desturi ya kinywa cha Wazee (yaani, Talmud). Maandiko haya ya Kifarisayo kwa uwazi yanafunua upinzani wao katika hali hasi, yawezekana ikiwa imetiwa chumvi (yaani mpinzani wa kubuni, mbinu) njia.
- C. Hakuna maandiko yanayojulikana ya Kisadukayo yenyewe ambayo yamedumu. Pamoja na uharibifu wa Yerusalemu na hekalu katika miaka ya 70 B.K nyaraka zote na ushawishi wa usomi wa kikuhani uliharibiwa.

Walitaka kuendeleza amani ya kimkoa na njia pekee ya kufanya hivyo katika karne ya kwanza ilikuwa ni kushirikiana na Rumi (kama vile Yohana 11:48-50).

#### 4:2

NASB, NKJV

“wakifadhaika sana”

NRSV

“wakifadhaishwa sana”

TEV

“walifadhaishwa”

NJB

“wakifahaishwa kupitiliza”

Hili ni neno nadra la Kiyunani (hapa ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo [yenye ushahidi] ikimaanisha "kufanyia kazi kwa bidii kitu fulani." Inapatikana sehemu moja tu ya kitabu cha Matendo ya Mitume (16:18). Haipatikani katika Tafsiri ya Agano la Kale wala katika mafunjo ya lugha ya Koine, huko Misri.

Uongozi wa Kisadukayo ulikatishwa tamaa kwasababu viongozi wa Kikristo walikuwa wakifundisha umati ndani ya hekalu katika jina la Yesu na kutangaza ufufuo wake (jambo ambalo Masadukayo walikataa na pia dhana ya thiolojia ya ufufuo kwa ujumla). Pia inawezekana kutokana na maneno ya Matendo ya Mitume 4:2 kwamba Mitume si tu kwamba walikuwa wanaelezea ufufuo wa Yesu, bali kumaanisha ukweli wa ufufuo wa waaminio wote (kama vile 1 Wakorintho 15).

**4:3 "wao"** Katika Mdo. 4:2 inamaanisha ni Petro, Yohana na hata yawezekana yule kiwete aliyeponywa. Katika Mdo. 4:3 kinachotangulia ni makuhani na maakida wa hekalu.

▣ **"wakawawekea mikono"** Kitenzi hiki cha kiyunani kina upana mkubwa wa kimaana, lakini Luka anakitumia katika maana ya kukamatwa (kama vile Luka 20:19; 21:12; Mdo. 5:18; 12:1; 21:27).

▣ **"mpaka kesho yake"** Sheria ya kiyahudi ilikataza kuendesha kesi na mashitaka baada ya kuandama kwa mwezi Viongozi hawa walitaka mahubiri haya na mafundisho haya kuachwa mara moja. Hivyo waliwafunga kwa usiku mmoja mahali fulani chini kwa sababu za kihekalu, badala ya kuwaweka jela ya umma ya watu wote (kama vile Mdo.5:18).

**4:4 "wale waliosikia . . .waliamini"** Vitenzi hivi vyote ni njeo ya wakati uliopita usiotimilifu. Imani inaanza na kusikia (kama vile Rum. 10:17). Kusikia matokeo ya injili (kwa msaada wa Roho mtakatifu kama vile Yohana 6:44,65; 16:8-11) katika kuamini injili. Angalia **MADA MAALUM: WOKOVU (NJEUYA KITENZI YA KIYUNANI)** katika Mdo. 2:40.

▣ **"na hesabu ya watu waume ikawa kama elfu tano "** Angalia kwamba namba hii haijumuishi wanawake na watoto. Mara kwa mara katika Agano Jipya inamaanisha kwamba imani ya baba ilikuzwa na kujumuishwa kwa familia nzima (kama vile Mdo. 11:14; 16:15,31,33). Kundi lililokuwa chumba cha juu kilikuwa na hesabu ya watu kama 120. Wakati wa Pentekoste watu 3,000 waliongezeka (kama vile Mdo. 2:41); sasa hesabu yao sasa ya waamini ilifikia 5,000! Kanisa la Yerusalemu lilikuwa likikua kwa kasi!

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 4:5-12**

<sup>5</sup> Hata asubuhi wakubwa na wazee na waandishi wakakusanyika Yerusalemu, <sup>6</sup> na Anasi Kuhani Mkuu, na Kayafa pia, na Yohana na Iskanda, na wote wale waliokuwa jamaa zake Kuhani Mkuu. <sup>7</sup> Walipowaweka katikati wakawauliza, Kwa nguvu gani na kwa jina la nani ninyi mmefanya haya? <sup>8</sup> Ndipo Petro, akijaa Roho Mtakatifu, akawaambia, Enyi wakubwa wa watu na wazee wa Israeli, <sup>9</sup> kama tukiulizwa leo habari ya jambo jema alilofanyiwa yule mtu dhaifu, jinsi alivyoponywa, <sup>10</sup> jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulibisha, na Mungu akamfufua katika wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu. <sup>11</sup> Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. <sup>12</sup> Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.

**4:5 "watawala wao na wazee na waandishi"** Wakuu wa masinagogi (yaani baraza, 5:21, kutoka eneo la Yerusalemu; baraza la wazee, 22:5) lilikuwa linaundwa na viongozi wa kiyahudi sabini. Kilikuwa ni chombo cha kisiasa na kidini (ambacho Rumi ilikiruhusu) ndani ya siku za Yesu. Dhana ilianzwa (yaani, desturi za kiyahudi) kwa Ezra na "Watu wa sinagogi kuu." Mara zote inatambuliwa katika Agano Jipya kwa tungo, "waandishi, wazee na makuhani" (kama vile Luka 23:13; Mdo. 3:17; 4:5,8; 13:27). Angalia Mada Maalum.

#### **MADA MAALUMU: WAKUU WA BARAZA LA SINAGOGI**

- I. chanzo cha habari
  - A. Agano Jipya lenyewe
  - B. Flavian Yusufu wa mambo ya kale ya Kiyahudi
  - C. Sehemu ya Mishna juu ya sheria za kiibada za Kiyahudi (yaani eneo la watu wa Sinagogi kuu).

Bahati mbaya Agano Jipya na Yusufu hawakubaliani na maandiko ya sheria za Kiyahudi, ambazo zinaonekana kuwathibitisha watu wawili wa Sinagogi kuu katika Yerusalemu, kuhani mmoja (yaani., Msadukayo), akidhibitiwa na kuhani mkuu na akishughulika na haki za jamii na uhalifu na wa pili ikidhibitiwa na mafarisayo na waandishi, waliohusiana na mambo ya kidini na kitamaduni. Hata hivyo, tarehe za maandiko ya sheria za Kiyahudi toka mwaka 200 B.K na kuangazia hali ya kitamaduni baada ya Yerusalemu kuangukia mikononi mwa kamanda Tito wa Rumi, mwaka wa 70 B.K. wayahudi (yaani., uongozi wa kifarisayo) waliimarisha tena makao makuu yao kwa minajili ya maisha ya kidini katika mji uitwao Jamnia na baadaye (yaani mwaka wa 118 B.K) wakaondoka kwenda Galilaya.



## II. Istilahi

Tatizo la kumtambua mtu wa kimahakama unahusisha majina tofauti yanayojulikana. Kuna maneno mengi yaliyotumika kuelezea watu wa kimahakama ndani ya jamii ya Kiyahudi ya Yerusalemu.

- A. *Gerousia*-“senati” au “baraza.” Hili ni neno la zamani lililotumika kwenye kipindi cha mwisho cha Uajemi (kama vile vitu vya asili ya kale vya Yusufu 12.3.3 na II Wamakabayo 11:27). Linatumiwa na Luka katika Mdo 5:21 pamoja na “watu wa Sinagogi kuu.” Yaweza kuwa ni njia ya kuelezea neno kwa viongozi wanaoongea Kiyunani (kama vile Wamakabayo 12:35)
- B. *Synedrion*- “watu wa Sinagogi kuu.” Huu ni muunganikano toka *syn* (pamoja na) na *hedra* (nafasi). Cha kushangaza neno hili linatumiwa katika lugha ya Kiarama, lakini likitazamisha neno la Kiyunani mwishoni mwa kipindi cha Wamakabayo hili likajakuwa ni neno linalokubalika kuunda mahakama kuu ya Kiyahudi katika Yerusalemu (kama vile Mt. 26:59; Marko 15:1; Luka. 22:66; Yohana 11:47; Mdo 5:27). Tatizo hapa linakuja wakati maneno yale yale yanatumika katika mabaraza ya kimahakama ya mahali fulani nje ya Yerusalemu (kama vile Mt. 5:22; 10:17)
- C. *Presbyterion*- “baraza la wazee” (kama vile Luka 22:66). Huu ni mfumo wa Agano la Kale la viongozi wa kikabila. Hata hivyo, ilikuja kurejerea mahakama kuu katika Yerusalemu (kama vile Mdo. 22:5)
- D. *Boulē* –neno hili “baraza”lilitumiwa na Yusufu (yaani vita 2.16.2; 5.4.2, lakini sio agano jipya) kuelezea watu mbali mbali wa kimahakama:
  - 1. Seneti kwenye mji wa Rumi
  - 2. Mahakama za kawaida za Rumi
  - 3. Mahakama kuu ya Kiyahudi katika Yerusalemu
  - 4. Mahakama za kawaida za KiyahudiYusufu wa Arimataya ameelezewa kama mwanajumuiya ya watu wa Sinagogi kuu kwa muundo wa neno hili (yaani., *bouleutē*, likimaanisha “mkuu wa baraza” kama vile Marko 15:43; Luka 23:50)

## III. Maendeleo ya kihistoria

Mwanzoni kabisa Ezra alisema kulitengeneza Sinagogi kuu (kama vile Targum katika Wimbo ulio Bora 6:1)katika kipindi cha uhamisho, ambacho kilikuja onekana kuwa watu wa sinagogi kuu katika siku za Yesu.

- A. Mishna (yaani., sheria za kiibada za Kiyahudi) zimeweka kumbu kumbu kwamba palikuwepo mahakama mbili kuu katika Yerusalemu (kama vile Sanh. 7:1)
  - 1. Moja iliyokuwa imeundwa na wanajumuiya 70 (au 71) (sand. 1:6 hata inaelezewa kuwa Musa alitengeneza hilo baraza la kwanza la watu wa Sinagogi kuu (Sanhedrin) la watu 11, kama vile Hes.11:16-25)
  - 2. Lingine lililokuwa limeundwa na wanajumuiya 23 (lakini yawezekana inarejerea mabaraza ya Sinagogi ya kawaida).
  - 3. Baadhi ya wasomi wa Kiyahudi waliamini kuwa palikuwepo na wanajumuiya 23 waliounda sinagogi kuu huko Yerusalemu. Wakati watatu wanaungana, pamoja na viongozi wawili, likiteua wanajumuiya 71 toka “watu wa sinagogi kuu.”(yaani Nasi na Av Bet Din).
    - a. Kuhani mmoja (yaani Sadukayo)
    - b. Mwanasheria mmoja (pharisayo)
    - c. Mtu wa ukoo bora mmoja (yaani., wazee)
- B. Wakati wa ukimbizi toka mahali pao, kizazi cha Daudi kilichorudi ni Zurubabeli na kizazi cha Aroni alikuwa Yoshua. Baada ya kifo cha Zerubabeli, hapakuwepo na kizazi cha Daudi kilichoendelea, kwa hiyo joho la kimahakama lilipitishwa pasipo kuwajumuisha makuhani(kama vile I Macc. 12:6) na wazee wa mahali (cf. Neh. 2:16; 5:7).
- C. Jukumu la kuhani katika mahakama lilithibitishwa na Diodorus 40:3:4-5 wakati wa

- D. Jukumu hili la kuhani katika serikali liliendelea mpaka kipindi cha Selucid. Yusufu anamnukuu Antiokia “mkuu III” (223-187 K.K) katika mabo ya kale 12.138-142.
- E. Mamlaka ya kuhani yaliendelea mpaka kipindi cha Wamakabayo kutokana na mambo ya kale ya Yusufu 13.10.5-6; 13.15.5
- F. Wakati wa kipindi cha utawala wa Warumi gavana wa Syria (yaani Gabinus toka 57-55 K.K) akaanzisha “sinsgogi kuu” za Kimikoa (kama vile mambo ya kale ya Yusufu 14.5.4; na Vita 1.8.5), lakini baadaye ilitenguliwa na Rumi (yaani., mwaka wa 47 K.K)
- G. Watu wa Sinagogi kuu walikuwa na mkabiliano wa kisiasa na Herode (yaani mambo ya kale 14.9.3-5) ambao, mwaka 37 K.K, wakalipiza kisasi na watu wengine wa baraza kuu wakauwawa (kama vile mambo ya kale ya Yusufu 14.9.4; 15.1.2)
- H. Chini ya wakili wa Kirumi (yaani., 6-66 B.K) Yusufu anatuambia (kama vile mambo ya kale 20.200,251) kuwa watu wa Sinagogi kuu tena wakapata nguvu na umaarufu (kama vile Marko 14:55). Kuna majaribu matatu yalioandikwa katika Agano Jipya pale watu wa siagogi kuu, chini ya uongozi wa familia ya kuhani mkuu, walitenda haki.

- 1. Jaribu la Yesu (kama vile Marko 14:53-15:1; Yohana 18:12-23,28-32)
- 2. Petro na Yohana (kama vile Mdo 4:3-6)
- 3. Paulo (kama vile Mdo. 22:25-30)

- I. Wakati Wayahudi walipoasi katika mwaka wa 66 K.K, Warumi baadaye wakaiharibu jamii yote ya Kiyahudi na Yerusalemu katika mwaka wa 70 K.K. watu wa sinagogi kuu moja kwa moja wakatenguliwa, ingawa Mfarisayo pale Jamnia wakajaribu kurudisha tena baraza kuu la kisheria (yaani Beth Din) katika maisha ya dini ya Kiyahudi (lakini sio kwenye jamii au siasa)

#### IV. Uanachama

- A. La kwanza Kibiblia kutajwa kwenye baraza kuu huku Yerusalemu ni lile la 2Nya. 19:8-11. Liliundwa na
  - 1. Walawi
  - 2. Makuhani
  - 3. Wakuu wa familia (yaani., wazee, kama vile I Wamak. 14:20; II Wamak.4:44)
- B. Wakati wa kipindi cha Wamakabayo lilimilikiwa na (1) familia ya kikuhani ya Masadukayo na (2) familia ya ukoo bora wa mahali Fulani (kama vile I Wamak. 7:33; 11:23; 14:28). Baadaye katika kipindi hiki “waandishi” (wanasheria wa Musa, ambao mara nyingi walikuwa mafarisayo) waliongezwa, inaonekana na mke wa Alexanda Jannaesus, yaani Salome (76-67 B.K). Hata hivyo alisema kuwafanya mafarisayo kuwa kikundi cha maarufu (kama vile Yusufu, vita vya Wayahudi 1.5.2).
- C. Wakati wa siku za Yesu baraza liliundwa na
  - 1. Familia ya kuhani mkuu
  - 2. Watu wa kawaida toka kwenye familia ya watu wenye uwezo
  - 3. Waandishi (kama vile Luka 19:47)

#### V. Vyanzo vya maoni vikatafuta toka

- A. Dictionary of Jesus and the Gospels, IVP, kurasa 728-732
- B. The Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible, vol. 5, kurasa 268-273
- C. The New Schaff-Herzog Encyclopedia of Religious Knowledge, vol. 10, kurasa 203-204
- D. The Interpreter’s Dictionary of the Bible, vol. 4, kurasa 214-218

**4:6 "Annasi"** Jina lake kwa Kiyunani ni Hannas; Josephus alimuita Hannanos (Yonathan). Jina linaonekana kutoka katika kiebrania "mwenye rehema" au "mwenye neema" (*hānān*, BDB 336). Katika Agano la Kale ukuhani mkuu ulikuwa wa maisha na ulikaa katika uzao wa Aaruni. Hata hivyo Warumi wamegeuza ofisi hii kuwa uwanja wa kisiasa wakinunuliwa na familia ya kikuhanu. Kuhani Mkuu alisimamia na kufanya kazi katika mahakama ya wanawake. Kusafisha hekalu kwa Yesu kulitia hasira familia hii

Kulingana na Flavius Josephus, Annasi alikuwa Kuhani Mkuu miaka ya 6-14 b.k. aliteuliwa na Quirinius, mtawala wa Shamu na kuondolewa na Valerius Gratus. Ndugu zake ( watoto 5 wa kiume na mjuukuu wa kiume) walichukua nafasi yake baada yake. Kayafa (18-36 b.k, mkwilima wake (kama vile Yohana 18:13), alikuwa mrithi wake wa mara moja. Annasi alikuwa nguvu kubwa nyuma ya ofisi. Yohana anamuelezea kama mtu wa kwanza ambaye Yesu anapelekwa kwake (kama vile Mdo. 18:13,19-22).

▣ **"Kayafa"** Alichaguliwa kama Kuhani Mkuu na Valerius Gratus, mwendesha mashitaka wa Yudea (kama vile MS D, *'Iōnathas*, matoleo ya NEB, NJB) kutoka mwaka 18-36. B.k

▣ **"Yohana"** Hii inaweza kummaanisha "Yonathan," ambaye Josephus alitwambia kuwa alikuwa mmoja wa watoto wa Anna ambaye alikuja kuwa Kuhani Mkuu mwaka 36 b.k baada ya Kayafa. Hata hivyo toleo la UBS<sup>4</sup> lina *'Iōannēs* (yaani Yohana) kama iliyopewa alama ya A (hakika); hata toleo la REB linamrejerea "Yohana."

▣ **"Iskanda"** Hakuna kinachojulikana kuhusu mtu huyu, lakini kama Yohana, yawezekana alikuwa mmojawapo ya wanafamilia ya Anna au mwanafamilia kiongozi wa chama cha masadukayo.

**4:7 "Walipowaweka katikati"** Wajumbe wa baraza la wakuu wa sinagogi wakakaa nusu duara juu ya kilima.

▣ **"wakaanza kuwauliza"** Hii ni njeo ya wakati usiotimilifu, ambalo ilimaanisha aidha (1) kitendo kinachoendelea wakati wa nyuma au (2) mwanzo wa kitendo.

▣ **"kwa nguvu gani na jina la nani"** Walianza kukebehi kuwa uponyaji ulikuwa unafanyika kwa nguvu za giza (kama vile Mdo. 19:13). Walijaribu mbinu hii kwa Yesu (kama vile Luka 11:14-26; Marko 3:20-30). Wasingeweza kupinga miujiza hivyo walianza kukebehi na kupindisha mbinu au chanzo cha nguvu.

**4:8 "wakijaa Roho Mtakatifu"** Roho alikuwa chanzo cha hekima na ujasiri kwa Mitume (kama vile Luka 12:11-12; 21:12-15). Kumbuka kuwa huyu hakuwa mwanaume yule yule ambaye siku chache zilizopita alikuwa amemkana Yesu kwa hofu (kama vile Mdo. 4:13). Tazama Petro "alijazwa" (kama vile Mdo. 2:4; 4:8,31). Hii inaonekana kuwa kilikuwa ni kitendo kinachojirudia (kama vile Efe. 5:18). Angalia kidokezo kamili katika Mdo.5:17.

**4:9 "ikiwa"** Hii ni sentensi ya daraja la kwanza lenye masharti ambayo ilidhaniwa kuwa kweli kwa kusudi la mwandishi.

▣ **"kiwa tutashitakiwa leo"** Hili neno la Kiyunani kidhahiri linamaanishas "kupitia kwa mahakama" (kama vile Mdo. 12:19; 24:8; 28:18; Luka 23:14). Lilikuwa likitumika na Wayahudi wa Beroya katika kuyachunguza maandiko kuona kama Paulo alikuwa sahihi katika kuyafasiri (kama vile Mdo. 17:11).

▣ **"kwa ajili ya faida ya mgonjwa"** Petro anaelezea kutokuwa sahihi kwa mashitaka haya ya kiofisi katika mazingira yenye uadui ya namna hii juu ya miujiza mizuri ya uponyaji na rehema. Badala yake walitakiwa kumsifu Mungu!

▣ **"imeeleweka"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliotimilifu ikiwa na maana ya afya timilifu na urejesho wa miguu yake.

**4:10 "Na ijulikane kwa watu wote wa Israeli na ninyi nyote"** Hii ni kauli timilifu tendaji shurutishi. Roho alimtia nguvu Petro. Hakutishwa na mazingira ya kimahakama. Viongozi hawa hawakuweza kumficha Kristo katika kaburi na hawakuweza kukataa kuwa mtu aliyeponywa alikuwa akisimama mbele yao!

▣ **"Kwa jina la Yesu Kristo Mnazareti"** Petro anaanzia juu ya swali na majibu hasa ya namna gani muujiza ule umetokea. Angalia MADA MAALUM: YESU MNAZARETI katika Mdo. 2:22.

▣ **"ambaye mlisulubisha"** Huu ulikuwa ukweli ulio wazi. Walichochea Kifo chake. Angalia "kwa ninyi" katika Mdo. 4:11, ambayo pia ilielezea dhamiri ya kushitakiwa kwao.

▣ **"ambaye Mungu alimfufua"** Agano Jipya linakiri kwamba nafsi zote tatu za Utatu Mtakatifu zilikuwa kazini zikifanya kazi wakati wa ufufuo wa Yesu:

1. Roho, Rum. 8:11
2. Yesu, Yohana 2:19-22; 10:17-18
3. Baba, Mdo. 2:24,32; 3:15,26; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 6:4,9

Huu ulikuwa ukiri wa kweli wa maisha ya Yesu na mafundisho kuhusu Mungu na pia ukubarifu kamili wa Baba wa kifo mbadala cha Yesu. Hii ilikuwa sehemu kubwa ya *mafundisho* (yaani mahubiri katika Mdo, angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:14).

▣ **"Mtu huyu anasimama hapa"** Hii ni dhahaka juu ya neno "kusimama." Mlemavu anasimama na anasimama mbele zao wote.

**4:11** Hii ni nukuu kutoka Zaburi 118:22, lakini sio maandiko ya Masoreti au Tafsihi ya Agano la Kale (kama vile Efe. 2:20; 1 Pet. 2:4 na kuendelea). Yesu anatumia hili mwenyewe katika Marko 12:10 na Luka 20:17, akichukua kutoka katika Tafsihi ya Agano la Kale. It Inamaanisha kutimilizwa kwa unabii wa Agano la Kale wa Masihi aliyekataliwa aliyefanyika moyo wenyewe wa mpango wa milele wa Mungu kwa ajili ya ukombozi (angalia Mada Maalum katika Mdo. 1:8) wa Israeli na ulimwengu. Hii ilikuwa ni kauli ya kushitua kwa viongozi hawa wa Kiyahudi (kama vile 1 Tim. 2:5).

**NASB** "Jiwe kuu la pembeni"  
**NKJV** "jiwe kuu la pembeni"  
**NRSV, NJB** "jiwe la pembeni"  
**TEV** "jiwe.....la muhimu kati ya yote"

### **MADA MAALUM: "JIWE" (BDB 6, KB 7) na "JIWE KUU LA PEMBENI" (BDB 819, KB 944)**

- I. Matumizi ya Agano la Kale
  - A. Dhana ya jiwe kama kitu kigumu mkinachodumu ambacho kilitumika kutengeneza msingi kilitumika kuelezea YHWH (kama vile Ayubu 38:6; Zaburi 18:2 inatumia maneno mawili ya "mwamba," BDB 700, 849).
  - B. Alafu baadae lilikuzwa kuwa cheo cha Kimasihi (kama vile Mwanza 49:24; Mwanzo 118:22; Isaya 28:16).
  - C. Neno "jiwe" au "mwamba" lilikuja kuwakilisha hukumu kutoka kwa YHWH Masihi (kama vile Isaya 8:16 [BDB 6 KUTENGENEZA BDB 103]; Danieli 2:34-35,44-45 [BDB 1078]).
  - D. Hii ilikuzwa mpaka kuwa sitiari ya kiujenzi (hasa Isaya 28:16).
    1. linalowekwa la kwanza, ambalo lililuwika linahakikisha usalama na kuweka vipimo vya jengo lote linalosalia liliitwa "jiwe kuu la pembeni"
    2. Ingeweza pia kumaanisha jiwe la mwisho linalowekwa sehemu yake likishikilia kuta pamoja (kama vile Zekaria 4:7; Efe. 2:20, 21), liliitwa "jiwe kifuniko," kutoka katika Kiebrania *rosh* (yaani kichwa)
    3. Linaweza kumaanisha "jiwe la msingi," ambalo linakuwa katikati ya njia ya kuingilia na kushikilia

uzito wa jengo la kuta nzima.

II. Matumizi ya Agano Jipya

- A. Yesu alinukuu Zaburi 118 mara kadhaa katika kujizungumzia mwenyewe (kama vile Mt. 21:41-46; Marko 12:10-11; Luka 20:17)
- B. Paulo alitumia Zaburi 118 akiunganisha kukataliwa kwa YHWH na Waisraeli wasioamini na wenye kuasi (kama vile Rum. 9:33)
- C. Paulo anatumia dhana ya "jiwe kuu la pembeni" katika Efe. 2:20-22 kama urejereo kwa Kristo
- D. Petro anatumia dhana hii ya Yesu 1 Petro 2:1-10. Yesu ni jiwe kuu la pembeni na waamini ni mawe yaliyo hai (yaani waamini kama mahekalu, kama vile 1 Kor. 6:19), yakijengwa juu yake (yaani Yesu ni Hekelu jipya, kama vile Marko 14:58; Mt. 12:6; Yohana 2:19-20). Wayahudi walikataa msingi wa tumaini lao pale walipomkataa Yesu kama Masihi.

III. Kauli za Kithiolojia

- A. YHWH alimruhusu Daudi/ Sulemani alijenge hekalu. Aliwaambia kwamba iwapo wangelitunza agano angeliwabariki na kuwa pamoja nao (kama vile 2 Samueli 7), lakini ikiwa wasingelishika agano, hekalu lingeliharibiwa (kama vile 1 Wafalme 9:1-9)!
- B. Walimu wa kiyahudi waliweka mkazo katik muundo na ibada na kuachana na kipengele cha imani binafsi (kama vile Yeremia 31:31-34; Ezekieli 36:22-38). Mungu anatafuta uhusiano wa kila siku, wa binafsi na wa kiungu pamoja na wale walioumbwa kwa sura na mfano wake (kama vile Mwanzo 1:26-27). Luka 20:17-18 inajumuisha maneno ya kutisha ya hukumu kama ilivyo kwa Mathayo 5:20, kuelekezwa kwa uyahudi.
- C. Yesu alitumia dhana ya hekalu kuwakilisha mwili wake mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22). Hii inaendelea na kupanuka kwa dhana ya imani binafsi katika Yesu kama masihi ni msingi wa mahusiano pamoja na YHWH (yaani Yohana 14:6; 1 Yohana 5:10-12).
- D. Wokovu umemaanishwa kurejesha sura ya Mungu iliyoharibika katika wanadamu (Mwanzo 1:26-27 na Mwanzo 3) ili kwamba ushirika pamoja na Mungu uwezekane. Lengo la Ukristo ni kufanana na Kristo kwa sasa. Waamini wanatakiwa kuwa mawe yaliyohai (mahekalu madogo yaliyojengwa/kwa mfano wa Kristo).
- E. Yesu ni msingi wa Imani yetu na jiwe letu la imani (yaani the Alfa na Omega). Bado, pia jiwe la kujikwaa na mwamba wa hatia (Isaya 28:16). Kumkosa Yeye ni kukosa kila kitu. Kunaweza kusiwe na ardhi nyingine ya kati hapa!

**4:12 "hakuna wokovu kwa mwingine awaye yote yule"** Hii ni kauli hasi ya mara mbili yenye nguvu. Hakuna wokovu katika Ibrahimu au Musa (kama vile Yohana 14:6; 1 Tim. 2:5; 1 Yohana 5:10-12). Madai gani ya kushangaza ya namna hii! Hii ni ya mipaka lakini pia dhahiri sana kwamba Yesu aliamini kuwa kupitia uhusiano binafsi tu pamoja na ye ndipo mtu anaweza kumjua Mungu. Petro kwa ujasiri anatangaza hili kwa uongozi wa kisomi wa kiyahudi. Hii mara kwa mara imekuwa ikiitwa kashfa ya ukristo. Hakuna mazingira ya kati hapa. Kauli hii ni ya kweli au Ukristo ni uongo!

▣ **"Hakuna jina lingine chini ya mbingu ambalo wanadamu wamepewa "** Hali ya kuendelea "limekwisha tolewa" ni kauli tendwa ya wakati timilifu. Mungu ameliweka jambo hili wakfu! Yesu ni jibu kwa hitaji la kiroho la mwanadamu. Hakuna mpango B! Kwa ajili ya rejea ya kitabu cha madai juu ya Ukristo angalia H. A. Netland, *Dissonant Voices: Religious Pluralism and the Question of Truth*.

▣ **"katika wanadamu"** Angalia kipengele cha kiulimwengu (kama vile Yohana 3:16; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9).

▣ **"ambalo litupasalo kuokolewa"** Tungo hii ina vitenzi viwili.

1. *dei*, kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo, "ni lazima tu" (angalia kidokezo kamili *dei* katika Mdo.1:16)

2. *sōthēnai*, kauli tendwa ya wakati uliopita usio timilifu isiyo na kikomo *sōzō*, "kuokolewa"

Neno kwa "kuokoa" lina matumizi mawili katika Agano Jipya.

1. kuokoa kimwili (namna ya Agano la Kale, kama vile Mt. 9:22; Marko 6:56; Luka 1:71; 6:9; 7:50; Mdo.27:20,31; Yakobo 1:21; 2:14; 4:12; 5:20)
2. wokovu wa kiroho (matumizi ya Agano Jipya, kama vile Luka 19:10; Mdo. 2:21,40,47; 11:14; 15:11; 16:30-31)  
Mtu kiwete alikuwa anapitia vyote. Viongozi wa kidini walihitaji kumwamini Yesu kama tumaini lao la pekee kwa ajili ya kukubaliwa na msamaha! Wanadamu wanahitaji kuokolewa (kama vile Rum. 1:18-3:20) na Yesu ni njia pekee kwa ajili ya hili kutimilizwa (kama vile Rum. 3:21-31). Nukuu ya Agano la Kale katika Mdo. 4:12 linaonesha kuwa siku zote ulikuwa Mpango wa Mungu (kama vile Isaya. 8:14-15; 28:14-19; 52:13-53:12).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 4:13-22**

<sup>13</sup> Basi walipoona ujasiri wa Petro na Yohana, na kuwajua ya kuwa ni watu wasio na elimu, wasio na maarifa, wakastaajabu, wakawatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu. <sup>14</sup> Na wakimwona yule aliyeponywa akisimama pamoja nao hawakuwa na neno la kujibu. <sup>15</sup> Wakawaamuru kutoka katika baraza, wakafanya shauri wao kwa wao, <sup>16</sup> wakisema, Tuwafanyie nini watu hawa? Maana ni dhahiri kwa watu wote wakao Yerusalemu ya kwamba ishara mashuhuri imefanywa nao, wala hatuwezi kuikana. <sup>17</sup> Lakini neno hili lisije likaenea katika watu, na tuwatishe wasiseme tena na mtu awaye yote kwa jina hili. <sup>18</sup> Wakawaita, wakawaamuru wasiseme kabisa wala kufundisha kwa jina la Yesu. <sup>19</sup> Petro na Yohana wakawajibu wakawaambia, Kwamba ni haki mbele za Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe; <sup>20</sup> maana sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia. <sup>21</sup> Nao walipokwisha kuwatisha tena wakawafungua, wasione njia ya kuwaadhibu, kwa sababu ya watu; kwa kuwa watu wote walikuwa wakimtukuza Mungu kwa hayo yaliyotendeka; <sup>22</sup> maana umri wake yule mtu aliyefanyiwa ishara hii ya kuponya ulipita miaka arobaini.

**4:13 "ujasiri"** Angalia Mada Maalum: ujasiri (*parrhēsia*) katika Mdo. 4:29.

▣ **"wasiokuwa na elimu"** Neno ni *agrammatos*, ambalo ni neno "maandiko" yakiwa na herufi ya kwanza ya kiyunani ya hasi. Hii inamaanisha kuwa walikuwa

1. wajinga au wasiokuwa na elimu (kama vile Moulton, Milligan, *Vocabulary*, ukurasa wa 6)
2. wasiokuwa na mafunzo katika shule za sheria za kidini (kama vile A. T. Robertson, *Word Pictures in the Greek New Testament*, vol. 3, ukurasa wa 52 na Louw na Nida, *Lexicon*, vol. 1, ukurasa wa 328)

▣ **"wasiokuwa na mafunzo"** Hili ni neno *idiōtēs*, ambalo mara nyingi limekuwa likifasiriwa "wasiokuwa na elimu" au "wasiokuwa na ujuzi katika eneo fulani." Kiasili lilimaanisha mtu wa kawaida ikilinganisha dhidi ya kiongozi au msemaji. Lilitokea kutumika na mtu wa nje dhidi ya mjumbe wa kundi (kama vile 1 Kor. 14:16,23-24; 2 Kor. 11:6). Angalia namna fasiri mbalimbali za kingereza zinavyozungumzia tungo hii.

**NASB, NKJV** "watu wasiokuwa na elimu wala maarifa"  
**NRSV** "wasiokuwa na elimu na watu wa kawaida"  
**TEV** "watu wa kawaida wasiokuwa na elimu"  
**NJB** "watu wasiokuwa na elimu"

▣ **"walistaajabu"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati usiotimilifu (kama ilivyo vitenzi viwili vinavyofuata). Inamaanisha aidha mwanzo wa kitendo au tukio linalojirudia rudia katika wakati uliopita (hali ya elekezi). Luka

anatumia neno hili mara kwa mara (mara 18 katika Luka na katika Mdo); mara nyingi lakini sio siku zote huwa lina visawe chanya (kama vile Luka 11:38; 20:26; Mdo. 4:13; 13:41).

▣ **"wakaanza kuwatambua kuwa walikuwa na Yesu"** Huu ulikuwa ni ukweli wa kupongeza. Yesu pia hakuwa ana mafunzo katika shule za sheria za kidini lakini bado alilifhamu Agano la Kale vizuri. Alikuwa amesoma shule za kisinagogi kama ilivyokuwa desturi ya watoto wote wa kiyahudi (kama ilivyokuwa kwa Petro na Yohana) walivyokuwa wanatakiwa kufanya. Viongozi hawa walitambua ujasiri na nguvu ya Petro na Yohana. Walikuwa wameona hivyo hivyo ndani ya Yesu.

**4:14** Kila mtu alimfahamu kiwete huyu kwasababu kila mara alikuwa akikaa katika lango la uzuri wa hekalu. Lakini siku hiyo hakuwa amekaa tena (kama vile Mdo. 4:16,22).

**4:15** Waliuliza watatu wao kuondoka wakati wakiendelea na tafakari zao na kupanga mikakati ya kukataa na udanganyifu (kama vile Mdo. 4:17-18).

**4:17-18** Huu ndio ulikuwa mpango wao! kuacha kumzungumzia Yesu na kuacha kusaidia watu kwa Jina lake! Je vipi watu wote waliokuwa wakimsifu Mungu kwa ajili ya uponyaji (kama vile Mdo. 3:8-9; 4:16)?

**4:19 "kama"** Hii ni sentensi ya daraja la kwanza lenye masharti, ambayo inatumika ila si kwa uhalisia bali kwa ajili ya hoja. Petro na Yohana hawakufikiria juu ya amri zao kama zilikuwa sawa (kama vile Mdo. 5:28).

▣ **"haki"** Angalia [MADA MAALUM: HAKI](#) katika Mdo. 3:14.

▣ **"Hukumuni nyie wenyewe"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiokuwa timilifu. Viongozi hawa walijihukumu wenyewe kwa maneno yao, nia zao na matendo.

**4:20** Petro na Yohana walielezea kuwa hawawezi kukataa kile walichokiona na kukishuhudia na hawataacha kuwashirikisha watu!

**4:21 "walipokuwa wamewatisha sana"** Najaribu kuwaza kwa kushangaa kuwa sijui walikuwa wamewatisha kuwa wangewafanyia nini. Yesu alifufuka kutoka katika wafu. Mtu huyu aliinuliwa kutoka katika kitanda; Viongozi hawa walikuwa wanaenda kuwafanyia nini Petro na Yohana?

▣ **"(hawakupata sababu ya kuwaadhibu)"** Hii inaweza kuwa imeelekeza nia ya Luka kuandika. Ukristo haukuwa kitisho kwa Rumi au amani ya Yerusalemu. Hata wakuu wa baraza la sinagogi hakupata sababu ya kuwahukumu viongozi wake.

▣ **"juu ya watu"** Washuhudiaji wa macho wa matukio wa Yerusalemu waliliona kanisa la kwanza kwa heshima na taadhima kubwa (kama vile Mdo. 2:47). Viongozi wa kiyahudi walikuwa wametishwa na umaarufu huu (kama vile Mdo. 5:13,26)

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 4:23-31**

<sup>23</sup> Hata walipofunguliwa, wakaenda kwa watu wao, wakawapasha habari ya mambo yote waliyoambiwa na wakuu wa makuhani na wazee. <sup>24</sup> Nao waliposikia, wakampazia Mungu sauti zao kwa moyo mmoja, wakisema, Mola, wewe ndiwe Mungu, ndiwe uliyefanya mbingu na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo; <sup>25</sup> nawe ulinena kwa Roho Mtakatifu kwa kinywa cha babaetu Daudi, mtumishi wako, Mbona mataifa wamefanya ghasia, Na makabila wametafakari ubatili? <sup>26</sup> Wafalme wa dunia wamejipanga, Na wakuu wamefanya shauri pamoja Juu ya Bwana na juu ya Kristo wake. <sup>27</sup> Maana ni kweli, Herode na Pontio Pilato pamoja na Mataifa na watu wa Israeli, walikusanyika katika mji huu juu ya Mtumishi wako mtakatifu Yesu,

uliyemtia mafuta,<sup>28</sup> ili wafanye yote ambayo mkono wako na mashauri yako yamekusudia tangu zamani yatokee.<sup>29</sup> Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao; ukawajalie watumwa wako kunena neno lako kwa ujasiri wote,<sup>30</sup> ukinyosha mkono wako kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa jina la Mtumishi wako mtakatifu Yesu.<sup>31</sup> Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.

**4:23** Walienda tena chumba cha juu kukutana na wanafunzi.

**4:24 "kwa nia moja"** Huu umoja wa moyo na akili ilikuwa ni tabia ya kanisa la kwanza (kama vile Mdo. 1:14; 2:46; 4:24; 5:12; 15:25). Kuna nguvu kubwa ya kiroho na matendo yenye shabaha katika hali ya umoja kwa ajili ya kusudi fulani.

▣ **"Bwana"** Hili ni neno la Kiyunani *despota*, ambalo kutokana na huko tunapata neno la Kingereza despot (dikteta/mtawala). Lilimaanisha mamlaka kamili! Hapa linamaanisha Mungu Baba (kama vile Luka 2:29 na Ufunuo 6:10). Pia linatumika kwa Yesu (kama vile 2 Pet. 2:1 na Yuda na Mdo. 4:4).

▣ **"aliyefanya mbingu na nchi na bahari na vyote vilivyomo ndani yake"** Haya yanaweza yakawa ni maelezo ya Kutoka 20:11. Yananukuliwa katika Mdo. 14:15 na ukweli unatajwa katika Mdo.17:24. YHWH ndiye muumbaji!

**4:25** Kuna utofautiano mwingi wa maandiko katika sehemu hii ya kwanza. Maandiko ya kale P<sup>74</sup>,  $\kappa$ , A, na B tayari yanajumuisha utofauti wa utata. Japo maneno yanatofautiana, na nguvu ya maandiko ni dhahiri. Kwa ajili ya kujua matukio yote ya kinadharia yaliyotokea angalia Bruce M. Metzger, *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, kurasa 321-323).

▣ **"ambaye kwa Roho Mtakatifu kupitia kinywa cha baba yetu Daudi"** Hii inaelezea uvuvio wa Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-19). Hii ni nukuu kutoka katika Tafsiri la Agano la Kale ya Zaburi 2:1-2, Zaburi ya Masihi wa kifalme. Ukristo sio kitu kipya bali ni kutimilizwa kwa Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-48). Upinzani wa kiulimwengu lazima utarajiwe lakini pia ushindi wa YHWH.

**4:25-26 "Mataifa . .Watu. . .Wafalme ....watawala."** Inaonekana kama vile wanafunzi wanafanya ulinganifu wa maneno ya kiuahali "watawala" Katika namna wanawaita wakuu wa baraza la sinagogi *Goyim* (yaani mataifa) au angalau kuoanisha majina haya ya Agano la Kale na vikundi vya kisasa (yaani Pilato, Herode, Wakuu wa baraza la sinagogi na makundi ya kiyahudi) ambao walishiriki katika mashitaka usulubishaji wa Yesu.

▣ **"hasira"** Hii kiuahalisia "kutoa pumzi puani." Hii inamaanisha majivuno ya kiburi.

**4:26 "Bwana. . .Kristo wake"** Angalia kuwa YHWH na Masihi wote wanazungumziwa kwa pamoja. Ninashangazwa kwamba hawakunukuu Zaburi 110:1. Ni ngumu sana kuwa mtu wa imani ya mungu mmoja (Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:39) na kuelezewa Uungu kamili wa Kristo na unafsi wa Roho (kama vile Mdo. 4:25, Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:32). Bado nafsi hizi za kiungu tatu za kimilele zinatokea zikiwa zimeunganishwa kimuktadha mara nyingi katika Agano Jipya. Kumbuka kwamba waandishi wote isipokuwa Luka ni Wakristo wa kiyahudi waabudu Mungu mmoja. Kitu fulani kimesababisha wao kukubaliana na utatu (yaani Injili).

Angalia [MADA MAALUM: UTATU](#) katika Mdo. 2:32.

**4:27 "Mtumishi mtakatifu wako Yesu, ambaye ulimpaka Mafuta"** Angalia vyeo na majina haya ya Kimasihi.

1. mtakatifu (kama vile Mdo. 3:14; 4:30)
2. mtumwa (*pais*, kama vile Mdo. 3:13,26; 4:25,27,30. angalia kidokezo katika Mdo. 3:13)
3. mpakwa mafuta (*chriō*, ambalo kutoka huko Kristo linatoka, kama vile Luka 4:18; Mdo. 4:27; 10:38)



Mstari huu unaeleza mambo kadhaa tofauti tofauti kwamba Yesu alitumwa na kupewa mamlaka na YHWH. Yesu ni mpango wa Mungu wa milele na mbinu ya ukombozi na urejesho (Kama vile Mdo. 4:28, angalia Mada Maalum katika Mdo. 1:8).

## **MADA MAALUMU: "KUTIWA MAFUTA KATI KA BIBLIA" Hata hivyo kitenzi, BDB 602, KB 643 I; nomino, BDB 603)**

(kitenzi cha Kiebrania, BDB 602, KB 643 I; nomino, BDB 603)

- A. Yaliyumika kwa ajili ya urembeshaji (BDB 691 I. kama vile Kumb. 28:40; Ruthu 3:3; 2 Sam. 12:20; 14:2; 2 Nya. 28:15; Dan. 10:3; Mik. 6:15)
- B. Yalitumika kwa ajili ya wageni (BDB 206, kama vile Zab. 23:5; Luka 7:38,46; Yohana 11:2)
- C. Yalitumika kwa ajili ya uponyaji (BDB 602, kama vile Isa. 61:1; Marko 6:13; Luka 10:34; Yakobo 5:14) [yalitumika kwa maana ya tiba na kinga katika Eze. 16:9]
- D. Yalitumika katika maandalizi ya mazishi (kama vile Marko 16:1; Yohana 12:3,7; 19:39-40; 2 Nya. 16:14, lakini likiwa bila kitenzi "kutiwa mafuta")
- E. Yalitumika katika maana ya kidini (ya jambo, BDB 602, cf. Mwa. 28:18; 31:13 [nguzo]; Kut. 29:36 [madhabahu]; Kut. 30:26; 40:9-16; Law. 8:10-13; Hes. 7:1 [hema])
- F. Yalitumika kuwasimika viongozi
  - 1. Makuhani
    - a. Haruni (Kut. 28:41; 29:7; 30:30)
    - b. Wana wa Haruni (Kut. 40:15; Law. 7:36)
    - c. waliowekwa wakfu (Hes. 3:3; Law. 16:32)
  - 2. Wafalme
    - a. Na Mungu (kama vile 1 Sam. 2:10; 2 Sam. 12:7; 2 Fal. 9:3,6,12; Zab. 45:7; 89:20)
    - b. Na manabii (kama vile 1 Sam. 9:16; 10:1; 15:1,17; 16:3,12-13; 1 Fal. 1:45; 19:15-16)
    - c. Na makuhani (kama vile 1 Fal. 1:34,39; 2 Fal. 11:12)
    - d. na wazee (kama vile Amu. 9:8,15; 2 Sam. 2:7; 5:3; 2 Fal. 23:30)
    - e. juu ya Yesu kama mfalme wa Kimasihi (kama vile Zab. 2:2; Luka 4:18 [Isa. 61:1]; Matendo 4:27; 10:38; Heb. 1:9 [Zab. 45:7])
    - f. wafuasi wa Yesu (kama vile 2 Kor. 1:21; 1 Yohana 2:20,27 [mafuta])
  - 3. Juu ya manabii kadri iliyowezezana (kama vile 1 Fal. 19:16; Isa. 61:1)
  - 4. Kuvikomboa vyombo visivyoaminika vya ki-Uungu
    - a. Koreshi (kama vile Isa. 45:1)
    - b. Mfalme wa Tiro (kama vile Eze. 28:14, ambapo alitumia stirahi za Bustani ya Edeni)
  - 5. Neno au cheo "Masihi" maana yake ni "Mtiwa mafuta" (BDB 603), kama vile Zab. 2:2; 89:38; 132:10

Matendo 10:38 ni msitari ambapo nafsi tatu za Uungu zinazwekwa pamoja katika kutiwa mafuta. Yesu alipakwa mafuta (kama vile Luka 4:18; Matendo 4:27; 10:38). Dhana inapanuliwa ili kuwajumuisha waamini wote (kama vile 1 Yohana 2:27). Mpakwa mafuta anakuwa wapakwa mafuta! Hii inaweza kuwa sambamba na Mpinga Kristo na wapinga Kristo (kama vile 1 Yohana 2:18). Tendo la ishara ya Agano la Kale la kumiminiwa mafuta mwilini (kama vile Kut. 29:7; 30:25; 37:29) linahusiana na wale walioitwa na kuandaliwa na Mungu kwa kazi maalumu (yaani, manabii, makuhani, na wafalme). Neno "Kristo" ni tafsiri ya neno la Kiebrania "mpakwa mafuta" au Masihi.

▣ **"walikusanyika kwa pamoja kinyume na mtumishi wako mtakatifu"** Hapa ni orodha ya wapinzani wa Yesu katika Yerusalemu.

- 1. Herode, Warumi walimteuwa Edumean mtawala wa Palestina (angalia Mada Maalum hapa chini)
- 2. Pontio Pilato, Uongozi wa kiutawala wa kirumi kiongozi wa Palestina (Angalia Mada Maalum katika Mdo.3:13)

3. Mataifa, ambalo linaweza kuwa linamaanisha jeshi la Kirumi au wabadili dini wa kiyahudi
4. "watu wa Israeli," ambayo ingemaanisha mamlaka ya kiyahudi mna vikundi vya kiyahudi ambao walimuomba Baraba aachiwe na Yesu asulubishwe

## **MADA MAALUM: FAMILIA YA HERODE MKUU**

### **A. Herode Mkuu**

1. Mfalme wa Yudea (37-4 k.k.), Idumean (kutoka Edom), ambao kupitia ujanja wa kisiasa na msaada wa Marko Antoni, waliweza kuteuliwa mtawala wa sehemu kubwa ya Palestina (Kanaani) kwa seneti ya kirumi katika 40 k.k.
2. Anatajwa katika Mt. 2:1-19 na Luka 1:5
3. Watoto wake
  - a. Herode Filipo (mwana wa Mariamne wa Simoni)
    - (1) mume wa Herodia (4 k.k. – 34 b.k)
    - (2) Anatajwa katika Mt. 14:3; Marko 6:17
  - b. Herode Filipo I (mwana wa Cleopatra)
    - (1) Mtawala wa eneo kaskazini na Magharibi ya bahari ya Galilaya (4 k.k. – 34B. k)
    - (2) anatajwa katika Luka 3:1
  - c. Herode Antipa
    - (1) Mtawala wa Galilaya na Perea (4 k.k. – 39 b.k)
    - (2) Anatajwa katika Mt. 14:1-12; Marko 6:14,29; Luka 3:1,19; 9:7-9; 13:31; 23:6-12,15; Mdo. 4:27; 13:1
  - d. Archelaus, Herode wa Ethnarch
    - (1) Mtawala wa Yudea, Samaria, na Idumea (4 b.c. – a.d. 6)
    - (2) anatajwa katika Mt. 2:22
  - e. Aristobulus (mwana wa Mariamne)
    - (1) ametajwa kama Baba wa Herode Agrippa I aliyekuwa
      - (a) Mfalme wa Yudea (37-44 B.K)
      - (b) anatajwa katika Mdo. 12:1-24; 23:35
        - (i) mwana wa Herode wa Agrippa II  
– Tetrarch ngome ya kaskazini (50-70 B.K)
        - (ii) mtoto wake wakike alitwa Bernice  
– mwenza wa kaka yake  
– anatajwa katika Mdo. 25:13-26:32
        - (iii) mtoto wake Drucilla  
– mke wa Felix  
–anatajwa katika Mdo.24:24

### **B. Rejea za kibiblia kuhusu Herode**

1. Herode Mtawala, inanatajwa katika Mathayo 14:1 na kuendelea; Luka 3:1; 9:7; 13:31, na 23:7, alikuwa mtoto wa Herode Mkuu . Wakati wa kifo cha Herode Mkuu, ufalme wake uligawanywa kwa watoto wake wa kiume. Neno "Tetrarch (mtawala)" lilimaanisha "kiongozi wa sehemu ya nne." Herode huyu alijulikana kama Herode Antipa, ambalo limefupishwa kutoka katika Antipater. Alikuwa akitawala Galilaya na Perea. Hii ilimaanisha kiasi hiki katika huduma ya Yesu iliyokuwa katika mipaka ya kizazi hiki cha pili cha Mtawala Idumean.
2. Herodia alikuwa mtoto wa kike wa kaka wa Herode Antipa aliyetwa Aristobulus. Lakini kabla alikuwa ameolewa na Filipo ambaye ni ndugu ayekuwa wa ukoo wa Herode Antipa. Huyu hakuwa Filipo Mtawala aliyeeongoza eneo tu la kaskazini ya Galilaya, lakini ndugu mwingine alikuwa Filipo, aliyeshi katika Rumi. Herodia alikuwa na binti mmoja na Filipo. Katika safari ya Herode Antipa kutembelea Rumi alikutana na alitongozwa na Herodita, aliyekuwa akitafta kutanuka kisiasa. Hivyo,

Herode Antipa alimtaliki mkewe aliyekuwa Malkia wa Nabatean, na Herodia alimtaliki Filipo ili kwamba Herode Antipa aweze kuolewa. Yeye alikuwa pia ni dada wa Herode Agrippa I (kama vile Mdo. 12).

3. Tunajifunza juu ya jina la mtoto wa kike wa Herodia, Salome, kutoka katika kitabu cha Flavius Josephus, Mambo ya Kale ya Wayahudi 8:5:4. Yawezekana lazima alikuwa na umri kati ya kumi na mbili na kumi na saba kwa wakati huu. Kwa dhahiri alikuwa akiongozwa na kurubuniwa vibaya na mama yake. Baadaye aliolewa na Filipo Mtawala, but was soon widowed.
  4. Kama miaka kumi baada ya kukamatwa kwa Yohana Mbatizaji, Herod Antipa alikwenda Rumi katika sherehe ya mke wake Herodia, kutafuta cheo cha mfalme kwakuwa Agrippa I kaka yake alikuwa hapo mwanzo amepewa cheo hicho. Lakini Agrippa I aliwaandikia Rumi na kuwashutumu Antipa kwa kushirikiana na Wa-Parthia, adui wa Rumi mwenye kuchukiwa kutoka katika Crescent ya rutuba (Mesopotamia). Mtawala kidhahiri aliamini Agrippa I na Herode Antipa, pamoja na mkewe Herodia, walikuwa wameenda uhamishoni Uhispania
  5. Inaweza ikawa rahisi kukumbuka hawa wakina Herode tofauti tofauti kama wanavyowasilishwa katika Agano Jipya kwa kukumbuka kwamba Herode Mkuu aliuwa watoto katika Betlehemu; Herod Antipa aliuwa Yohana Mbatizaji; Herode Agrippa I aliuwa Mtume Yakobo; na Herode Agrippa II alisikia kukata rufaa juu ya Paulo iliyowekwa katika kumbukumbu katika kitabu cha Matendo ya Mitume.
- C. Kwa ajili ya usuli wa taarifa juu ya familia ya Herode Mkuu, tazama kielezo cha Flavius Josephus in Kumbukumbu ya Kale ya Wayahudi.

**4:28 "Mkono wako na kusudi lako lililoamriwa kufanyika"** Hata kabla ya uumbaji Mungu alikuwa na mpango wake kabla wa Ukombozi (kama vile Mt. 25:34; Yohana 17:24; Efe. 1:4; 1 Pet. 1:20; Ufunuo 13:8; Mdo. 2:13; 3:18; 13:29). Maadui hawa wote wa Kristo walifanya tu kwamba Mungu aliwataka wafanye. Yesu alikuja ili afe (kama vile Marko 10:45). Neno linalofasiriwa hapa ni "kuamuliwa" ni ambatani ya kihisishi cha neno "kabla" na "kuweka mipaka" (kama vile Rum. 8:29,30; 1 Kor. 2:7; Efe. 1:5,11).

Kifungu cha kimaielezo juu ya maamuzi ya kabla katika Agano Jipya ni Warumi 8:28-30; Rum. 9; na Efe. 1:3-14. Maandiko haya kidhahiri yalikuwa yanaweka msisitizo kwamba Mungu ni Mtawala Juu ya yote. Yeye anashughulikia hayo yote, ikiwemo historia ya mwanadamu. Kuna mpango wa ukombozi wa ki-Ungu unaofanyiwa kazi katika muda. Hata hivyo mpango huu sio wa kibaguzi bila ya sababu. Unajikita sio tu katika ukuu na utawala wa Mungu na maarifa yake y akabla lakini pia katika tabia yake isiyobadilika ya upendo, rehema na neema isiyostahiliwa

Lazima tuwe makini na ubinafsi wetu wa ki-Magharibi (U-marekani) au shauku yetu ya kiinjili inayopamba ukweli huu. Lazima pia tujilinde dhidi ya migogoro ya kudhoofishwa katika historia, thiolojia kati ya Augustine na Pelegius au kuamliwa kwanza na dhana pinzani inayokataa kuamriwa kabla.

Kuamriwa kabla sio findisho linalokusudiwa kuweka mipaka ya upendo wa Mungu, neema na rehema wala kuweka kando baadhi ya injili. Inamaanisha kutia nguvu waamini kwa kuwatengeneza kwa mtazamo wa kiulimwengu. Upendo wa Mungu ni kwa ajili ya wanadamu wote (kama vile 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9). Mungu anashughulikia mambo yote. Nani au nini kinachotutenga mbali naye (kama vile Warumi 8:31-39)? Kuamriwa kabla ni kutengeneza muundo mmoja wa njia mbili za kuyaangalia Maisha. Mungu anayaangalia maisha yote kama yanatokea sasa. Wanadamu wanamipaka. Mitazamo yetu na uwezo wetu wa akili ina kikomo. Hakuna mgongano kati ya ukuu wa Mungu na utashi huru wa mwanadamu. Ni muundo wa kiagano. Huu ni mfano wa ukweli wa kibiblia unaotolewa katika hali ya mafumbo, kilahaja, na jozi zenye mvutano. Mafundisho ya kibiblia yanawasilishwa kutoka katika mitazamo mbalimbali. Mara nyingi yanatokea kimafumbo. Ukweli ni ulali kati ya jozi mkabala. Lazima tuondoe mvutano kwa kuchukua moja ya kweli. Hatutakiwi kutenga kweli yoyote ya kibiblia katika chumba chake peke yake yenyewe.

Ni muhimu tuongeze kwamba lengo la uchaguzi si tu kwa ajili ya kwenda mbinguni tunapokufa, lakini kufanana na Kristo sasa (kama vile Efe. 1:4; 2:10)! Tulichaguliwa tuwe "watakatifu na tusio na laumu." Mungu anachagua kutubadilisha sisi ili kwamba tuweze kuona mabadiliko na kuitikia kwa imani kwa Mungu. Kuamuliwa kwanza sio nafasi ya upendeleo bali jukumu la kiagano! Tumeokolewa ili tutumikie! Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:47. **4:29 "nena neno lako"** Hii ni kauli tendaji ya wakati uliopo usiokuwa na kikomo. Hii ni sala kwa ajili ya mwendelezo wa ujasiri (kama vile Efe. 6:19 na Kol. 4:3) na ukiri wa uvuvio (kama vile 2 Tim. 3:15-17).

**NASB** "kwa ujasiri wote"  
**NKJV, NRSV**  
**TEV** "kwa ujasiri wote"  
**NJB** "kwa hali ya kutoogopa"

Angalia Mada Maalum inayofuata.

### **MADA MAALUMU: UJASIRI (*parrhēsia*)**

Neno hili la Kiyunani ni muungano wa maneno "yote" (*pan*) na "*(rhēsis)*". Uhuru huu au ujasiri katika usemi mara nyingi una maana nyingine ya ushujaa katikati ya upinzani au ukataliwaji (kama vile Yohana 7:13; 1 The. 2:2). Katika maandiko ya Yohana (limetumika mara 13) mara nyingi huonesha tangazo la wazi wazi (kama vile Yohana 18:20, pia katika maandiko ya Paulo, Kol. 2:15). Hata hivyo, wakati mwingine kwa maana ya kawaida ni "kwa uwazi" (kama vile Yohana 10:24; 11:14; 16:25,29).

Katika Matendo Mitume wanazungumzia ujumbe unaomhusu Yesu katika namna ile ile (kwa ujasiri) kama Yesu alivyozungumza kumhusu Baba na mipango na ahadi Zake (kama vile Mdo. 2:29; 4:13,29,31; 9:27-28; 13:46; 14:3; 18:26; 19:8; 26:26; 28:31). Pia Paulo ilihitaji msaada wa maombi ambapo kwa ujasiri angeliweza kuihubiri injili (kama vile Efe. 6:19; 1 The. 2:2) na kuiishi injili (kama vile Flp. 1:20).

Tumaini la Paulo la mambo yahasuyo kifo, hukumu na pepo katika Kristo lilimpa ujasiri na kijiamini katika kuihubiri injili katika zama hizi za sasa za uovu (kama vile 2 Kor. 3:11-12). Pia alikuwa na iamani kwamba wafuasi wa Kristo wangepanya kazi kwa namna ya kufaa sana (kama vile 2 Kor. 7:4).

Kuna kipengele kimoja zaidi cha neno hili. Kitabu cha Waebrania kinatumia neno hili katika maana ya kipekee ya ujasiri wa mwamini, kumwendea Mungu na kuzungumza Naye (kama vile Heb. 3:6; 4:16; 10:19,35). Waamini wanakubaliwa na kwa ukamilifu na kukaribishwa katika ukaribu na Baba kupitia Mwana (kama vile 2 Kor. 5:21)!

Katika Agano Jipya linatumika katika njia kadhaa.

1. imani, ujasiri, au moyo wa kujiamini inahusiana na
  - a. wanaume (kama vile Mdo. 2:29; 4:13,31; 2 Kor. 3:12; Efe. 6:19)
  - b. Mungu (kama vile 1 Yohana 2:28; 3:21; 4:12; 5:14; Ebr. 3:6; 4:16; 10:19)
2. kuzungumza wazi, dhahiri, au bila na utata (kama vile Marko 8:32; Yohana 7:4,13; 10:24; 11:14; 16:25; Mdo. 28:31)
3. kwa kuzunza hadharani (kama vile Yohana 7:26; 11:54; 18:20)
4. muundo uhusiano (*parrhēsiazomai*) unatumika kuhubiri kwa ujasiri katikati ya mazingira magumu (kama vile Matendo 18:26; 19:8; Efe. 6:20; 1 The. 2:2)

**4:30 "wakati ukinyoosha mkono wako kuponyal"** Hii ilikuwa ni tungo yenye tabia za ubinadamu (Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:33) zinatumika kuelezea Mungu akifunua huruma yake na nguvu. Ishara zilikuwa njia ya kuthibitisha ujumbe wa Injili. Ilikuwa ni ujumbe tofauti kutoka katika kile walichokisikia maisha yao yote katika Sinagogi.

**4:31 "Mahali walipokuwa pakatikiswa"** Mungu aliwatia nguvu washuhudiaji hawa kwa udhahirisho mwingine wa kimwili wa nguvu na uwepo, kama alivyofanya siku ya Pentekoste. Neno aliloliumia kwa upepo kuvuma juu ya chombo cha baharini kinachotembea

▣ **"wote wakajazwa na Roho Mtakatifu"** Angalia tena hapa wakajazwa wote (kama vile Mdo. 2:4; 4:8,31; 9:17; 13:9,52, angalia kidokezo kamili katika Mdo. 5:17). Ujazo huu ulikuwa wa kutangaza injili. Pia kwamba ndimi hazikutajwa. Katika Matendo ya Mitume ndimi zinatajwa, siku zote huwa kuna muktadha wa kiinjili unaoshindana na vizuizi vya desturi za kikabila au kijiografia.

▣ **"neni la Mungu"** Fasiri ya Biblia ya Jerome (ukurasa wa 180) una maelezo mazuri juu ya tungo hii, "Hii ni namna nzuri ya Luka ya kuelezea ujumbe wake wa kikristo (angalia Mdo. 6:2,7; 8:14; 11:1; 13:5,7,44,46,48; 16:32; 17:13; 18:11). Utofauti wa hii ni "neni la Bwana" (Matendo 8:25; 13:49; 15:35,36; 19:10,20; 20:35) au kirahisi "neni" (Mdo. 4:29; 6:4; 8:4; 10:44; 11:19; 14:25; 16:6)." Hii ni swali kuu la kiimani, "Je injili inayowasilishwa katika Agano Jipya ni Neni la Mungu?" Imani inayotiwa nguvu na Roho inasema "ndio"!!

▣ **"kwa ujasiri"** Angalia Mada maalumu katika Mdo. 4:29

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 4:32-35**

<sup>32</sup> Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu cho chote alichochacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika. <sup>33</sup> Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote. <sup>34</sup> Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu watu wote waliokuwa na viwanja au nyumba waliviuza, wakaileta thamani ya vitu vile vilivyozwa, <sup>35</sup> wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji.

**4:32 "walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja"** Roho alikuwa na umoja kati ya waaminio (kama vile Mdo. 1:14) aliaksi umoja wa utatu wa Mungu (kama vile Yohana 17:11,21,23; Efe. 4:4-6). Maneno haya haya yalitumika katika Marko 12:30 kuaksi amri ya kwanza katika Kumbu. 6:4-5.

▣ **"walikuwa na vitu vyote shirika"** Walijisikia kufanya kazi kama familia. Hii ilikuwa ni jaribio la kwanza la kanisa kusaidia huduma kifedha. Ilikuwa ni kwa kupenda na kwa kuwiwa wala si kwa lazima au kushurutishwa. Upendo na kujali sio kwa namna ya kijamii ya kiserikali kwamba nia zao zilisukumwa kutoka huko!

**4:33 "wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu"** Hii ilikuwa kweli kuu ya ukweli wa ujumbe wake (kama vile 1 Wakorintho 15). Yesu alikuwa hai!

▣ **"na neema nyingi ikawa juu yao wote"** Tunajifunza kutoka katika barua za Paulo kwamba katika nyakati za hivi punde kanisa hili lilikuwa maskini (kama vile Rum. 15:3; Wagalatia 2:10). Neema tele, kama maisha tele (Kama vile Yohana 10:10) ina vitu vichache vya kufanya. Angalia utele huu ulikuwa na watu wote si kwa viongozi tu pekee yao kwamba ndio walikuwa wamiliki wa mali Fulani au wali wenye hadhi Fulani za kiuchumi.

**4:34** Kanisa liliona umuhimu wa kubebeana jukumu. Wale waliokuwa navyo walitoa kwa uhuru kwa wale waliokuwa na mahitaji (ama vile Mdo. 4:35). Huu sio ujamaa bali upendo uliopo kazini.

**4:35 "wakaiweka miguuni pa mitume"** Hii ni nahau ya kidesturi ya kutoa kitu. Waliweka vitu na pesa katika miguu ya mitume kwasababu walikuwa wameyatoa maisha yao katika miguu ya Yesu.

▣ **"akagawiwa"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati usiotimilifu, ambayo inaonesha matendo yanayoendelea wakati uliopita. Hii inafuatia utaratibu wa Sinagogi wa kusaidia maskini na wahitaji.

▣ **" kwa kadiri ya alivyohitaji."** Kuna maoni mazuri sana kwa Klein, Blomberg, na Hubbard's *Introduction to Biblical Interpretation*, kurasa za 451-453, kwamba Marx's manifesto inajumuisha nukuu mbili kutoka Mdo:

1. "kulingana na uwezo wake kwa kila mtu" – Mdo. 11:29
2. "kwa kila mtu kulingana na uhitaji wake"

Tatizo la Tafsiri za Biblia ni kwamba watu wa kisasa wanajaribu kutumia Biblia kuhalalisha kile ambacho Biblia haijawahi kukizungumzia wala kukielezea. Biblia haiwezi ikamaanisha kile ambacho hakikuwahi kukusudiwa na mwandishi wa asilia au wasikiaji. Tunaweza kutumia maadiko katika namna nyingi kwenye mazingira yetu ya kitamaduni na yale tuliyopo lakini katika kutumia kwetu lazima kutenganishwa kwa muunganiko wa maana iliyokusudiwa na mwandishi wa asili. Kila andiko la Biblia lina maana moja tu, lakini matumizi au umuhimu ni mwingi sana. (Angalia Semina za Fasiri zangu za kibiblia katika [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org))

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 4:36-37**

<sup>36</sup> Na Yusufu, aliyelitwa na mitume Barnaba, (maana yake, Mwana wa faraja), Mlawi, asili yake ni mtu wa Kipro, <sup>37</sup> alikuwa na shamba akaliuza, akaileta fedha, akaiweka miguuni pa mitume.

**4:36 "Yusufu, Mlawi"** Agano la Kale lilipiga marufuku makuhani kumiliki ardhi lakini mamlaka ya Kirumi yalikuwa yamebadili vitu vingi katika Palestina.

▣ **"aliyelitwa Barnaba na Mitume (ambalo lilifasiriwa kama mwana wa kutia moyo)"** Hii ni maana inayojulikana sana ya "Barnaba." Katika kiaramu ingeweza kuwa inamaanisha "mwana wa unabii" au katika kiebrania yawezekana "mwana wa Nebo" (AB, toleo la 1). Alikuwa kiongozi wa kwanza katika kanisa la Yerusalemu na rafiki wa Paulo na mwenza mtendakazi wa kimishonari. Eusebius na Mwanahistoria wa kanisa la kwanza anasema kwamba alikuwa mmoja wa wale sabini katika Luka 10.

#### **MADA MAALUM: BARNABA**

- I. Kuhusu mtu mwenyewe
  - A. kiasili aliyelitwa Yusufu (kama vile Mdo. 4:36)
  - B. alizaliwa Cipro (kama vile Mdo. 4:36)
  - C. wa kabila la Lawi (kama vile Mdo. 4:36)
  - D. aliyelitwa jina maarufu "mwana wa faraja" (kama vile Mdo. 4:36; 11:23)
  - E. aliyelitwa "mtu mwema" (kama vile Mdo. 11:24)
  - F. muumini wa kanisa la Yerusalemu (kama vile Mdo. 11:22) na alitumwa kama mwakilishi kuangalia hali ya maendeleo ya kanisa jipya linalokua la Antiokia, Ashuru (kama vile Mdo.11:19-28)
  - G. ilisemekana kujazwa na Roho Mtakatifu (kama vile Mdo. 11:24)
  - H. alisemekana kujawa na imani (kama vile Mdo. 11:24)
  - I. alikuwa na karama za rohoni kama nabii na mwalimu (kama vile Mdo. 13:1)
  - J. aliyelitwa mtume (kama vile Mdo 14:14)
- II. Huduma yake
  - A. Ndani ya Yerusalemu
    1. aliuzia mali zake na kuwapa pesa zote mitume kusaidia maskini (kama vile Mdo. 4:37)
    2. kiongozi wa kanisa la Yusaumu (kama vile Mdo. 11:22)
  - B. pamoja na Paulo
    1. alikuwa ni mmojawapo wa wa kwanza kumwamini Sauli/kuongoka kwa Paulo (kama vile

Mdo. 9:27)

2. alikwenda Tarso kumtafuta Paulo/kumpata Paulo kutoa msaada wa kanisa jipya la Antiokia (kama vile Mdo. 11:24-26)
3. Kanisa pale Antiokia lilituma Barnaba na Sauli kwenda kanisani huko Yerusalemu pamoja na msaada kwa maskini (kama vile Mdo. 11:29-30)
4. Barnaba na Paulo wanakwenda katika safari yao ya kimishenari ya kwanza (kama vile Mdo. 13:1-3)
5. Barnaba alikuwa kiongozi wa timu huko Cipro(katika kisiwa chake cha nyumbani), lakini hivi karibuni uongozi wa Paulo ulitambulika (kama vile Mdo. 13:13)
6. Walitoa taarifa kwa kanisa la Yerusalemu kuelezea na kuandika habari ya kazi yao ya umisheni kati ya mataifa (kama vile Mdo. 15:1-21, aliita baraza la Yerusalemu).
7. Barnaba na Paulo walikuwa na hali ya kutoelewana kuhusu sheria ya kiyahudi ya chakula na ushirikawa kimataifa uliowekwa katika kumbukumbu katika Wagalatia 2:11-14
8. Barnaba na Paulo walipanga safari ya pili ya kimishenari lakini mgogoro uliibuka kati yao na mpwa wa Barnaba, Yohana Marko (kama vile Kol. 4:10), alielekeza kazi katika safari yao ya kimisheni ya kwanza (kama vile Mdo. 13:13). Paulo alikataa kuambatana nae katika safari ya kimisheni ya pili, hivyo timu ikaharibika (kama vile Mdo. 15:36-41). Hii ilipelekea timu mbili (yaani Barnaba na Yohana Marko, na Paulo na Sila).

III. Desturi za kanisa (Eusebius)

- A. Barnaba alikuwa miongoni mwa wale sabini waliotumwa na Yesu (kama vile Luka 10:1-20).
- B. Alikuwa kama shujaa wa Kikristo nyumbani kwake, Cipro (kutoka katika Matendo ya Barnaba).
- C. Tertullian anasema aliandika kitabu cha Waebrania
- D. Klement wa Alexandria anasema aliandika kitabu kisichokuwa cha wakanoni cha Waraka wa Barnaba.

**4:37 "aliyekuwa akimiliki ardhi"** Alikuwa nai mtu wa njia zake nyingi (kama Nikodemo na Yusufu wa Arimathaya). Mdo. 5 inaonesha uwezekano wa kutumiwa vibaya mbinu hii ya kuwezesha huduma kifedha (mfano, wivu, uongo, na kifo).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Masadukayo ni akina nani? Kwanini wanakuwa wamerukwa na akili?
2. Wakuu wa baraza la Sinagogi ni nini?
3. Nini umuhimu wa Zaburi 118?
4. Kwanini Mdo. 4:12 ni muhimu sana?
5. Je kule kutajwa kabla kwa Mdo. 4:28 inamaanisha mtu mmoja mmoja au mpango wa ukombozi wa Mungu? Kwanini?
6. Je Luka anajaribu kupanga na kuweka mwongozo kwa ajili ya kanisa katika Mdo. 4:32-5:11?

## MATENDO YA MITUME 5

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Anania na Safira	Kumdanganya Roho Mtakatifu	Kugawana Mavuno (4:32-5:11) 4:32-5:6	Anania na Safira	Udanganyifu wa Anania na Safira
5:1-11	5:1-11	5:7-11	5:1-6 5:7-8	5:1-6 5:7-11
Ishara nyingi na Maajabu Yaliyofanyika	Nguvu endelevu ndani ya kanisa	Kukamatwa mara ya pili kwa Mitume	Miujiza na Maajabu	Hali kwa Ujumla
5:12-16	5:12-16	5:12-21a	5:12-16	5:12-16
Mateso ya Mitume	Mitume Waliotiwa Gerezani Waachiliwa Huru		Mitume Wanateswa	Kukamatwa kwa Mitume na Kombolewa
5:17-26	5:17-21			5:17-18 5:19-21a Hotuba ziliendelea Kabla ya Masadukayo
	Mitume Wakishtakiwa Tena	5:21b-26	5:21b-26	5:21b-26
	5:22-32			
5:27-32		5:27-32	5:27-28	5:27-33
	Ushauri wa Gamalieli	Gamalieli	5:29-32	
5:33-42	5:33-42	5:33-39a	5:33-39a	Kuingilia kati kwa Gamalieli
		5:39b-42	5:39-42	5:34-39a 5:39-41 5:42

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (kutoka "[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)")

**KUFUATIA KUSUDIO ASILIA LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni [mwongozo](#) kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya



Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembelee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB ( LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 5:1-6

<sup>1</sup> Lakini mtu mmoja jina lake Anania, pamoja na Safira mkewe, aliuza mali, <sup>2</sup> akazuia kwa siri sehemu ya thamani yake, mkewe naye akijua haya, akaleta fungu moja akaliweka miguuni pa mitume. <sup>3</sup> Petro akasema, Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja? <sup>4</sup> Kilipokuwa kwako, hakikuwa mali yako? Na kilipokuwa kimekwisha kuuzwa, thamani yake haikuwa katika uwezo wako? Ilikuwa hata ukaweka neno hili moyoni mwako? Hukuwambia uongo mwanadamu, bali Mungu. <sup>5</sup> Anania aliposikia maneno haya akaanguka, akafa. Hofu nyingi ikawapata watu wote walioyasikia haya. <sup>6</sup> Vijana wakaondoka, wakamtia katika sanda, wakamchukua nje, wakamzika.

**5:1"Anania"** Jina kamili la Kiebrania lingekuwa Ananiah, ambalo linamaanisha "YHWH ametoa kwa neema" au "YHWH ni wa neema" (BDB 337).

☐ **Safira"** Huyu alikuwa mke wa Anania. Jina hili katika lugha ya Kiaramu linamaanisha "mrembo" Wote walikuwa waamini.

**5:2 akazuia kwa siri"** Hiki ni kitenzi kile kile kilicho adimu (*nosphizomai*) kinatumika katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani (LXX) ya Yoshua 7:1 kueleza ile dhambi ya Akani. F. F. Bruce, katika maoni yake juu ya kitabu cha Matendo ya Mitume (NIC) ametengeneza maoni kuwa Anania alikuwa wa kanisa la mwanzo ambapo Akani alikuwa Mateka. Dhambi hii alikuwa na uwezekano wa kulidhuru kanisa zima. Neno hili pia linatumika katika Tito 2:10 juu ya watumwa wawaibiao mabwana zao.

☐ **"akaleta fungu moja akaliweka miguuni pa mitume"** Hili linafanana na kile alichokifanya Barnaba katika Matendo ya Mitume 4:37. Wawili hawa walikuwa na uhuru wa kuuza au kuuza mali yao binafsi (kama vile Matendo ya Mitume 5:4). Hawa walikuwa na uhuru wa kumpa mtu mwingine au kutoa vyote kwa ajili ya kazi ya Bwana. Hawakuwa na haki ya kutoa sehemu, bali walidai kutoa yote. Nia na matendo yao ya kinafiki yaliifunua mioyo yao (kama vile Matendo ya Mitume 5:4c; Luka 21:14). Mungu huangalia moyo (kama vile 1 Sam. 16:7; 1 Fal. 8:39; 1 Nya. 28:9; Mit. 21:2; Yer. 17:10; Luka 16:15; Matendo ya Mitume 1:24; Rum.8:27).

**5:3"Shetani. . . Roho Mtakatifu"** Hili linaonyesha uwepo wa nguvu mbili za kiroho ambazo zinatenda kazi katika ulimwengu wetu na ndani ya maisha yetu. Katika Efe. 2:2-3 (kama vile Yakobo 4) wameorodheshwa maadui watatu baada ya uwepo wa mwanadamu:

1. mfumo wa ulimwengu ulioanguka
2. tabia binafsi

### 3. asili yetu iliyoanguka

## **MADA MAALUM: SHETANI**

Hili suala gumu sana kutokana na sababu kadhaa.

1. Kitabu cha Agano la Kale hakimfunui adui mkuu apingaye mema, bali mtumishi wa YHWH (angalia A. B. Davidson, OT Theology, kr. 300-306), ambaye anampa mwanadamu uchaguzi wa bure na pia kumlaumu mwanadamu juu ya kutokuwa kwake mwenye haki. Kuna Mungu mmoja pekee (angalia Mada Maalum: Mungu aliye mmoja, uweza wa aina moja, sababu moja iliyo ndani ya Agano la Kale—YHWH (kama vile Isa. 45:7; Amosi 3:6).
2. Hii dhana ya huyu adui mkuu wa Mungu wa kipekee ilikuwa katika kipindi cha ukimya wa fasihi ya Agano la Kale na Agano Jipya (pasipo sheria za kikanisa) chini ya ushawishi wa pande mbili za dini za Kiajemi (Dhana ya Zoroaster). Hii, katika kurudia, kwa kiwango kikubwa hizi ziliwashawishi viongozi wa dini za Kiyahudi na jamii ya Essene (yaani, Magombo ya Kale ya Bahari ya Chumvi).
3. Kitabu cha Agano Jipya kiliikuza dhana ya Agano la Kale katika namna yaugumu wa kushangaza, lakini wa kipekee, wa aina nyingi.

Ikiwa moja ya mitazamo ya somo la uovu kutokana na kipengele cha theolojia ya kibiblia (kila kitabu au mwandishi au aina ya somo lililofundishwa na maelezo ya kimuhtasari yaliotengwa), tena ni mawazo tofauti sana ya uovu unaofunuliwa. Ikiwa, kwa vyo vyote, moja ya mitazamo ya somo la uovu kutoka mtazamo usio wa kibiblia au mtazamo wa ziada wa kibiblia wa dini za ulimwengu au dini za mashariki, tena maendeleo mengi ya kitabu cha Aagano Jipya yanatabiriwa katika ule uwili wa Kiajemi na ukiroho wa utawala wa Wagiriki-Waroma.

Ikiwa wazo la awali lilijikita juu ya Andiko la mamlaka ya Kiungu (kama Mimi Niko!), kasha ukuaji wa kitabu cha Agano Jipya lazima uonekane kama ufunuo endelevu. Yawapasa Wakristo kujilinda dhidi ya kuyaruhusu mafunzo ya mila na desturi za Kiyahudi au fasihi ya mashariki (Dante, Milton) kwa ajili ya ushawishi wa dhana ya baadaye. Kuna siri fulani na utata katika eneo hili la ufunuo. Mungu amechagua kutovifunua vipengele vyote vya uovu, chimbuko lake (angalia Mada Maalum: Lusfa), uendelevu wake, sababu yake, lakini Yeye amelifunua ondoleo lake!

Katika neno la Agano la Kale "shetani" au "mshtaki" (BDB 966, KB 1317) anaweza kuhusiana na makundi matatu taliyojitenga.

1. washtaki wa mwanadamu (kama vile 1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 11:14,23,25; Zab. 109:6)
2. washtaki wa kimalaika (kama vile Hes. 22:22-23; Ayubu 1-2; Zek. 3:1)
3. washtaki wa kimapepo (kama vile 1 Nyak. 21:1; 1 Fal. 22:21; Zek. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha ukimya wa Agano la Kale na Agano Jipya tu ndipo yule nyoka wa Mwanzo 3 alipotambujishwa kama Shetani (kama vile Book of Wisdom 2.23-24; II Enoch 31:3), na baadaye hili lilikuja kuwa uchaguzi wa sheria za Kiyahudi. Sot 9b na Sanh. 29a). Wale "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 walikuja kuwa malaika katika I Enoch 54:6. Nalitaja hili, si usahihi wa kitheolojia, bali hili linaonyesha maendeleo yake. Katika Kitabu cha Agano Jipya kazi hizi linapewa kundi la kimalaika, uovu wa kibinadamu (kama vile 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9). Chimbuko la uovu wa kibinadamu ni gumu au haliwezekani (linategemeana na hoja ya mtazamo wako) kuibainisha kutokana na kitabu cha Agano la Kale. Moja ya sababu ya hili ni kuwepo kwa Mungu wa Israeli Aliye mmoja (angalia Mada Maalum: Mungu Aliye Mmoja; pia nukuu 1 Fal. 22:20-22; Mhu. 7:14; Isa. 45:7; Amosi 3:6). Usababishi wote (kama vile Isa. 45:7; Amosi 3:6) alikpewa YHWH ili kuonyesha upekee na ubora Wake (kama vile Isa. 43:11; 44:6,8,24; 45:5-6,14,18,21,22).

Chimbuko la uhakika wa habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo Shetani ni mmoja wa "wana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14 na Ezekieli 28, ambapo wafalme wenye majivuno waliokuwa karibu na mashariki (Babeli

na Tiro) kwa hakika wanatumika kueleza juu ya majivuno ya Shetani (kama vile 1 Tim. 3:6). Nimechanganywa kihisia kuhusu mtazamo huu. Ezekieli anatomia stiari za Bustani ya Edeni, si kwa mfalme wa Tiro pekee kama Shetani (kama vile Eze. 28:12-16), bali pia kwa mfalme wa Misri kama Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya (Ezekieli 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa mist. ya. 12-14, anaonekana kuufafanua uasi wa kimalaika kupitia majivuno. Ikiwa Mungu alitaka kuifunua kwetu ile asili ya kipekee na chimbuko la Shetani, hii ni njia isiyo wazi na ni sehemu ya kulifanya hili. Yatupasa kujilinda dhidi ya uelekeo wa theolojia ya mfululizo wa kuchukulia mambo madogo madogo, sehemu za utata wa semi mbalimbali, waandishi, vitabu, aina na kuziunganisha kama vipande vya mafumbo ya Uungu.

Nakubaliana na Alfred Edersheim (The Life and Times of Jesus the Messiah, juzuu. 2, viambaisho XIII [kr. 748-763] na XVI [kr.770-776]) kwamba Sheria za Dini ya Kiyahudi kwa kiasi kikubwa zimepewa ushawishi na zile pande mbili za Kiajemi na kisiko la kimapepo. Hawa Walimu wa sheria za Kiyahudi si chimbuko zuri la ukweli ndani ya eneo hili. Kimsingi Yesu anaachana na mafundisho ya Masinagogi ndani ya eneo hili. Nafikiri kwamba ile dhana ya adui wa YHWH aliyekuwa katika umbo la kimalaika iliendelezwa kutokana na miungu mikuu miwili ya pande mbili za ki-Irani, Ahkiman na Ormaza, ambapo iliendelezwa tena na Walimu wa Sheria katika pande mbili za YHWH na Shetani.

Kuna uhakika wa ufunuo endelevu katika kitabu cha Agano Jipya kama sifa ya, lakini si kama wanavyoeleza Walimu wa Sheria za Kiyahudi. M fano mzuri wa utofauti huu ni "vita ya mbinguni." Anguko la Shetani kimantiki lina umuhimu, lakini ubatana haokutolewa (angalia Mada Maalum: Anguko la Shetani na Malaika Zake). Hata kile kilichotolewa kinafunikwa katika aina ya ukiyama (kama vile Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa Shetani anaondolea kwa Yesu na kutupwa duniani, bado anafanya kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile Mt. 4:1; Luka 22:31-32; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20). Katika eneo hili yatupasa kuzuia uchunguzi. Kuna nguvu binafsi ya ushawishi na uovo, lakini bado kuna Mungu mmoja pekee na bado tunawajibika kwa ajili ya chaguzi zetu. Kuna mapambano ya kiroho, wakati wote kabla na baada ya wokovu. Ushindi unaweza kuja tu na kubaki pale pale kupitia Mungu wa Utatu. Uovu emeshindwa na utaondoshwa kama vile Ufu. 20:10)!

## **MADA MAALUMU: UOVU BINAFSI**

### **I. Somo kuhusu shetani ni ngumu sana**

A. Agano la Kale halibainishi adui mkubwa wa (Mungu), bali mtumishi wa YHWH ambaye anawapa wanadamu mbadala na kutuhumu huyu mwanadamu kwa kutokuwa na haki (A. B. Davidson, *A Theology of the OT*, kr. 300-306).

B. Dhana ya adui mkubwa wa Mungu ulianza wakati wa fasili kati ya Biblia (zisizo na taratibu za kikanisa) katika kipindi cha dini ya kiislamu iliyoanzishwa na Zoroaster huko Uajemi. Hii kwa namna nyingine, kwa kiwango kikubwa ilisababisha sheria ya dini ya Kiyahudi (yaani, waliokuwa wametengwa na kuishi nje ya Israel yaani Babiloni, na Persia).

C. Agano Jipya linaunda dharura ya Agano la Kale katika ugumu wa ajabu lakini makundi yaliyochaguliwa kama mtu anaanza kusoma habari za uovu katika mtizamo wa thiolojia ya biblia (kila kitabu au mwandishi au michoro alisoma na kuandika kwa kifupi kwa kutenganisha) basi mawazo mbalimbali kuhusu uovu yangeibuliwa. hata hivyo, mtu ataanza kusoma kuhusu uovu lakini kwa njia isiyo ya kibiblia au nje zaidi ya biblia mfano dini za kiulimwengu au dini za mashariki, basi sehemu kubwa ya mambo mengi ya maendeleo ya agano jipya yalionyeshwa katika pande mbili za uajemi na tabia za uyunani na kiroma.

Kama mtu alidhaniwa kujitoka kwa uwezo wa kiungu neno la Mungu (lama nilivyo!),kwa hiyo mambo ya Agano Jipya lazima yaonekane kama ufunuo endelevu. Wakristo yawapasa wajilinde dhidi ya kuruhusu simulizi za Kiyahudi au fasihi za Kiingereza (yaani, Dante, Milton) kufafanua zaidi dhana hiyo bila shaka miujiza na maana tofauti tofauti katika eneo hili la wokovu. Mungu amechagua kutobainisha mambo yote ya uovu, asili yake

(tazama Mada Maalumu: Lusifa), kusudi lake, lakini amebainisha kushindwa kwake!

## II. SHETANI KATIKA AGANO LA KALE

Katika Agano la kale neno "Shetani" (BDB 966, KB 1317) au "mshitaki" linaonekana kuhusiana na makundi matatu tofauti.

A. Washtaki wa wanadamu (1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 5:4, 11:14,23,25; Zab. 109:6,20,29)

B. Washtaki wa kimalaika (Hes. 22:22-23; Zak. 3:1)

1. Malaika wa Bwana – Hes. 22:22-23

2. Shetani – 1 Nya. 21:1; Ayubu 1-2; Zak. 3:1

C. Washtaki wa kimapapo (bila shaka shetani) (1 Fal. 22:21; Zak. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha kuingia agano jipya ibilisi wa Mwanzo 3 alijulikana ni shetani (kama vile. Kitabu cha Hekima 2:23-24; II Enoch 31:3), na hata baadaye ambapo anakuja kuwa chaguo la viongozi wa kidini wa Uyahudi (kama vile. Sot 9b na Sanh. 29a). "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 wanakuwa malaika wa uovu katika I Enoch 54:6. Wanakuwa waanzilishi wa uovu katika thiolojia ya viongozi wa kidini wa Kiyahudi. Nalitaja hili sio kwa kuonyesha usahihi wake wa kithiolojia, bali kuonyesha maendeleo yake katika Agano Jipya, shuguli hizi za Agano la Kale zinachangia katika uovu wa malaika wa nuru (yaani shetani,)katika 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9.

Asili ya uovu wa yule aliyejigeuza kuwa malaika wa nuru ni mgumu au haiwezekani (kutegemea maoni yako) kuupima toka katika Agano la Kale. Sababu moja wapo ni ile imani ya ni 3:6). Majeruhi wote walipelekea YHWH kuonyesha kwa vitendo alivyo wa pekee na mkuu (kama vile. Isa. 43:11; 44:6,8,24; 45:5-6,14,18,21,22).

Uwezekano wa vyanzo vya habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo shetani ni mojawapo wa wana wa Mungu "mwana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14; Ezekieli 28, ambapo ujivuni karibu na wafalme wa mashariki (Babiloni na Uturuki) wamekuwa wakielezea sifa au ujivuni wa shetani (kama vile. 1 Tim. 3:6). Nimechanganya mihemko kuhusu kuliendea suala hili. Ezekieli anatumia bustani ya Edeni kama neno mbadala sio tu kwa mfalme wa Uturuki kama shetani (kama vile. Eze. 28:12-16), lakini pia kwa ufalme wa Misri kama mti wa maarifa wa mema na mabaya (Ezekieli 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa kurasa 12-14, anaonekana kuelezea uasi wa malaika kupitia majivuno kama Mungu alivyotaka kubainisha kwetu jinsi alivyo hasa na asili ya shetani hii ni njia isiyo elezea moja kwa moja na mahali pa kuifanya (tazama Mada Mada Maalumu: Lusifa). Lazima tujilinde dhidi ya mwenendo wa Theolojia wa kuchukua sehemu ndogo ndogo, tata toka kwenye maeneo yenye maana mbalimbali ya maandishi, vitabu, na kuviunganisha kama vipande vipande vya fumbo la Kiungu.

## III. SHETANI KATIKA AGANO JIPYA

Alfred Edersheim (*The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII [kur.. 748-763] na XVI [kur. 770-776]) anasema mafundisho ya sheria za Kiyahudi yameathiriwa wazi kabisa na umiliki wa pande mbili za Uajemi na mtizamo wa kimapapo. viongozi hawa wa kidini sio vyanzo vizuri vya ukweli katika eneo. Yesu kimsingi anakwepa kutoka kwenye mafundisho ya sinagogi. Nafikiri kuwa dhana ya viongozi wa dini ya kiyahudi ya upatanisho wa kimalaika (kama vile. Matendo 7:53) na upinzani katika kutoa sheria za Musa kwenye mlima Sinai ilifungua mlango kwa dhana ya adui mkuu wa YHWH kadhalika na mwanadamu. Palikuwa na Mungu wawili wa pande mbili za Iran (ufuasi wa Zoroaster).

1. *Ahura Mazda*, baadaye akaitwa *Ohrmazd*, aliyekuwa mungu muumbaji, mungu mwema

2. *Angra Mainyu*, baadaye aliitwa *Ahriman*, roho aangamizaye, mungu mwovu,

Vita juu ya ukuu na dunia ikawa kama uwanja wa vita. Umiliki wa pande mbili ukajengeka ndani ya pande mbili za Kiyahudi zenye ukomo kati ya YHWH na shetani.

Hakika kuna mafunuo endelevu katika agano Jipya kama ilivyo kwenye uovu, lakini sio kama ilivyo elezewa kama walimu wa dini ya Kiyahudi wanavyodai mfano mzuri wa utofauti huu ni "vita vya mbinguni." Kuanguka kwa shetani (Mwovu) ni mantiki yenye umuhimu, lakini sehemu husika haikutolewa (Tazama Mada Maalumu:

Kuanguka kwa shetani na malaika wake). Hata hivyo kile kilichotolewa kimefichika kwenye mafunuo tanzu (k.v. Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa shetani ameshindwa na kutupwa duniani, bado anatenda kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile. Mt. 4: 1; Luka 22: 31-32; 1 Kor. 5: 5; 1 Tim. 1: 20).

Lazima tuthibiti kiu yetu katika eneo hili. Kuna nguvu binafsi ya majaribu na uovu lakini bado kuna Mungu mmoja tu na mwanadamu bado anawajibika kwa uchaguzi wake. kuna vita ya kiroho kabla na baada ya wokovu. Ushindi wawezakuja tu na kubakia ndani na kupitia Mungu wa Utatu. Uovu umekwisha shindwa na utaondolewa (kama vile. Ufu. 20:10)!

☐ **"amekujaza"** Hili ni neno sawa linatumika kwa Roho (kama vile Efe. 5:18). Kujazwa kunahitaji ushirika! Tunajazwa na kitu fulani (tazama maelezo kamili katika Matendo ya Mitume 5:17)! Shetani anahusishwa, lakini tuwajibika (kama vile Luka 22:3-6). Nilipendekeza kitabu cha *Three Crucial Questions About Spiritual Warfare*, na Clinton E. Arnold. Kwa mshangao kuna ushawishi wa kishetani unaoendelea ndani ya maisha ya waamini (kama vile Efe. 6:10-19; 1 Yohana 5:18-19). Tazama maelezo kamili katika Matendo ya Mitume 2:4 na 3:10. Kifungu hiki (yaani, moyo wako uliojazwa") kinaweza kuwa nahau ya Kiebrania (kama vile Esta 7:5; Mhu. 8:11; 9:3). Wasomi wengi wanadhani kuwa hiki ni kiaramu halisi kwa sura za kale za kitabu cha matendo ya maitume.

☐ **"kumwambia uongo Roho Mtakatifu"** Hawa walimdanganya Petro na kanisa, lakini katika ukweli hawa walimdanganya Roho. Kitheolojia hili linafanana sana na Yesu alivyomuuliza Paulo akiwa barabarani kwenda Dameski, "Mbona waniudhi?" (kama vile Matendo ya Mitume 9:4). Paulo aliliwatesa waamini, lakini Yesu alilichukulia hili kwa upekee, kama anavyofanya Roho hapa. Hili linapaswa kuwa neno la maonyo kwa waamini wa sasa.

**5:4** Mstari huu una maswali mawili ambayo yanatarajia jibu la "ndiyo". Hii ni sifa ya kisarufi, si jambo la kiufasiri.

☐ **"Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu"** Si kwamba hawa walitunza sehemu ya fedha, bali kwamba waliongea uongo kwa kujifanya wako kiroho. Tambua kwamba hata namna, tendo la kiwivu, ambalo linafanywa kwa nia mbaya, ni dhambi (kama vile Rum. 14:23c). Tambua kwamba Roho Mtakatifu anayetajwa katika Matendo ya Mitume 5:3 hapa anaitwa Mungu.

**5:5** **"akaanguka, akafa"** Katika maneno ya kale mtu kuanguka chini na kufa ulikuwa ushahidi kwamba roho ya mtua imebaki (kama vikle Amu. 4:2; Eze. 21:7 katika tafasiri ya Maandiko ya Kale ya Kiyunani LXX). Neno hili linapatikana katika Agano Jipya pekee katika kitabu cha Matendo ya Mitume (kama vile Matendo ya Mitume 5:4,10; 12:23). Huu ni mfano wa humu ya wakati huu. Hili li sawa na hukumu ya Mungu juu ya wana wa Aaroni katika Mambo ya Walawi 10. Dhambi ni suala zito kwa Mungu. Inagharimu maisha (kama vile 2 Fal. 14:6; Eze. 18:4,20).

☐ **"Hofu nyingi ikawapata watu wote"** Hii huenda ilikuwa sababu ya hofu ya wakati huo. Hili linaweza kushabihiana na vifo vya Agano la Kale vya Nadabu na Abihu wa Mambo ya Walawi 10 na Uzzah wa 2 Samueli 6. Kwa kujikita katika 1 Kor. 11:30; yakobo 5:20; na 1 Yohana 5:16-17, inawezekana kudhani kuwa dhambi zingine zinazotendwa na waamini zinaleta matokeo ya kifo cha papo kwa papo. Ni vigumu kuulinda usawa kati ya utakatifu wa Mungu (wenye kuvuka mipaka) na Ubaba wa Muungu (kuwepo kila mahali siku zote).

**5:6"wakamzika"** Wayahudi wa karne ya kwanza hawakuwa na zoezi la utiaji dawa maiti (bado hawafanyi hivyo), huenda ni kwa sababu ya Mwa. 3:19 (kama vile Zab. 103:14; 104:29). Mtu alitakiwa kuzikwa haraka, mara nyingi ilikuwa ndani ya siku moja. Hii ni kwa sababu ya hatia kwani hakukua na huduma ya ukumbusho au taratibu za maziko ya Kikristo.

### **MADA MAALUMU: UTARATIBU WA MAZISHI**

- I. Mesopotamia
    - A. Mazishi sahihi yalikuwa muhimu sana kwa maisha ya baadae yenye furaha ambayo daima yalitazamwa kama mwendelezo wa maisha yaliyopo hapa, (tazama Mada Maalumu:\_Wafu wako wapi?).
    - B. Mfano wa laana ya watu wa Mesopotamia ni, "Ardhi haiwezi kuzipokea maiti zenu "
  - II. Agano la Kale
    - A. Mazishi yaliyo sahihi yalikuwa muhimu sana (kama vile Mhu. 6:3).
    - B. Yalifanyika haraka sana (kama vile Sara katika Mwanzo 23 na Raheli katika Mwa. 35:19 na tazama Kumb. 21:23).
    - C. Mazishi yasiyo sahihi yalikuwa ni ishara ya kukataliwa na dhambi.
      1. Kumbukumbu la torati 28:26
      2. Isaya 14:20
      3. Yerima 8:2; 22:19
    - D. Mazishi yalifanyika kama iwezekanavyo, katika vyumba vya familia vya ndani kwa ndani katika maeneo ya nyumbani (yaani , alilala na babazake").
    - E. Hapakuwa na mafuta ya kupaka maiti isioze kama ilivyo kuwa Misri. Mwanadamu alitoka mavumbini na atarudi mavumbini (mf. Mwa. 3:19; Zab. 103:14; 104:29 Pia angalia Mada\_Maalumu: Kuchoma maiti.
    - F. Katika sheria za dini za Kiyahudi ilikuwa vigumu kuweka usawa wa heshima kamili na kuukabili mwili katika dhana ya kuinajisi sherehe kunakohusishwa na maiti.
  - III. Agano Jipya
    - A. Mazishiya haraka yalifuatia kifo, kwa kawaida ilikuwa ndani ya masaa ishirini na nne.Wayahudi kwa kawaida walilinda kaburi kwa siku tatu, wakiamini kuwa nafsi ingeweza kuurudia mwili ndani ya siku hizo (kama vile Yohana 11:39).
    - B. Mazishi yalijumuisha kuosha na kufunika maiti kwa manukato (kama vile Yohana 11:44; 19:39-40).
- Hapakuwa na utofauti katika taratibu za maziko kati ya Wayahudi na Wakristo (au kitu kilichowekwa kaburini) katika karne ya kwanza huko Palestina

**5:7" muda wa saa tatu"** Hili linaonyesha udhahiri wa kiwango kupitia ushahidi wa macho. Maandiko ya Luka yanabainishwa na umakini huu kwa undani. Hili linaaksi vyote mtindo wa uandishi na njia za utafiti (yaani., mahojiano pamoja na ushahidi wa macho).

**5:8 Udanganyifu**, masingiziano yanaendelea!

**5:9"ikumjaribu"** Katika mzunguko wa kutafuta maana, hili lilikuwa jaribu la uwepo na uweza wa Roho Mtakatifu, Mungu ni uwepo pekee wa Baba duniani (tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 1:2). Kuna matokeo ya papo kwa papo, pamoja na matokeo ya milele kwa kumkashifu Roho! Haya mawili hayaelezi kwamba huyu alikuwa Roho ambaye walikuwa wanamwambia uongo, bali Petro alinena hivyo. Kuna maneno mawili ya Kiyunani yaliyotumika kudokeza juu ya jaribu. Hii ni moja ya maana nyingine ya "kujaribu kwa kutazamia uharibifu." Bila shaka hili linaaksi Kut. 17:2 na Kumb. 6:16, ambapo maandiko haya yanaonya dhidi ya kumshawishi/kumjaribu YHWH (kama vile Zab. 78:18,41,56).

## MADA MAALUMU: MANENO YA KIYUNANI YAHUSUYO KUPIMA NA VIDOKEZO VYAKE NYINGINE

Kuna manaeno mawili ya Kiyunani ambayo yana kidokezo kwa ajili ya kumpima mtu kwa kusudi fulani.

### 1. *Dokimazō, Dokimion, Dokimasia*

Neno hili ni neno la mtu yule afuaye vyuma kwa ajili ya kujaribu uhalisia wa kitu fulani (yaani, kistiari mtu fulani) kwa moto (tazana Mada Maalumu: Moto). Moto hudhihilisha chuma halisi na huteketeza (yaani, husafisha) dongo la chuma. Kitendo hiki cha kifizikia kinakuwa nahau yenye nguvu kwa Mungu na/au Ibilisi na/au binadamu kuwajaribu wengine. Neno hili linatumika tu katika maana chanya ya kujaribu kwa kuangalia hadi kuufikia ukubalifu (tazama Mada Maalumu: Mungu Huwajaribu Watu Wake [Agano la Kale]).

Linatumika katika Agano la Kale kwa ajili ya

- a. Madume ya ng'ombe – Luka 14:19
- b. sisi wenyewe – 1 Kor. 11:28
- c. imani yetu – Yakobo 1:3
- d. hata Mungu –Ebr. 3:9

Matokeo ya majaribu hayajafikiwa kuwa chanya (kama vile. Rum. 2:18; 14:22; 16:10; 2 Kor. 10:18; 13:3,7; Flp. 2:27; 1 Pet. 1:7), hivyo, neno husilisha wazo la mtu aliyepimwa na kuhakikishwa

- a. kuwa wa thamani
- b. kuwa wazuri
- c. kuwa halisi
- d. kuwa wa maana
- e. kuwa wa kuheshimiwa

### 2. *Peirazō, Peirasmus*

Neno hili mara nyingi lina maana nyingine ya kupimwa kwa kusudi la utafutaji au ukataaji. Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu ya Yesu nyikani.

- a. Linabeba jaribio la kumtega Yesu (kama vile Mt. 4:1; 16:1; 19:3; 22:18, 35; Marko 1:13; Luka 4:2; Ebr. 2:18).
- b. Neno hili (*peirazōn*) linatumika kama wadhifa kwa Ibilisi katika Mt. 4:3; 1 The. 3:5 (yaani, "mjaribu").
- c. Matumizi
  - 1) Lilitumiwa na Yesu alipokuwa akiwaonya wanadamu kutomjaribu Mungu (kama vile Mat. 4:7; Luka 4:12, [au Kristo kama vile 1 Kor 10:9]).
  - 2) Pia linamaanisha jaribio la kufanya kitu fulani ambacho kimeshindikana (kama vile Ebr.11:29).
  - 3) Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu na masumbufu ya waamini (kama vile 1 Kor. 7:5; 10:9, 13; Gal. 6:1; 1 The. 3:5; Ebr. 2:18; Yakobo. 1:2, 13, 14; 1 Pet. 4:12; 2 Pet 2:9).

**5:10** Hili neno linatumika kueleza "watu wachanga" (*neōteroi*) katika Matendo ya Mitume 5:6 ni tofauti na neno *neanikoi* katika Matendo ya Mitume 5:10. Hili yumkini kwa vyovyote vile ni namna nyingine ya kimamlaka au kundi tofauti la watu wachanga ndani ya kanisa. Maneno yote ya Kiyunani yanatokana na mzizi wa neno lile lile (*neos*).

**5:11**"Hofu nyingi. . . wote walioyasikia haya" Luka anatumia neno la kawaida *phobos* mara kadhaa katika maana ile ile ya jumla (kama vile Luke 1:69; 3:37; Matendo ya Mitume 19:17). Kwa waamini hili lina maana ya

unyenyekavu, heshima, na ukuu, lakini kwa wale wasioamini hili lina maana ya utabiri, hofu, na utisho (kama vile Luka 12:4-5; Ebr. 10:31).

☐ **"kanisa"** Hii ni mara ya kwanza neno hili kutumika katika Matendo ya Mitume, japokuwa lipo katika upokeaji wa maandiko katika Matendo ya Mitume 2:47. Tazama Mada Maalum ifuatayo.

### **MADA MAALUM: KANISA (*ekklesia*)**

Neno hili la Kiyunani, *ekklesia*, linatokana na maneno mawili, "nje ya" na "kuitwa." Neno hili linatumika kidunia (yaani, jamii iliyoitwa kwenye kikao, k.v Mdo. 19:32, 39, 41) na kwa sababu ya utumiaji wa maandiko ya kale ya Kiyunani ya neno hili kwa ajili ya "kusanyiko" la Israel (Qahal, BDB 874, KB 1078, k.v. Hes. 16:3; 20:4; Kumb. 31:30), na matumizi ya kidini. Kanisa la mwanzo walijiona wao kama mwendelezo wa Agano la Kale la watu wa Mungu. Walikuwa Waisraeli wapya (k.v. Rum. 2:28-29; Gal. 3:29; 6:16; 1 Pet. 2:5,9; Uf. 1:6), utimilizo wa kusudi la Mungu kidunia (k.v. Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8; angalia Mada Maalum: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH)

Neno lililotumika kwa maana nyingi katika injili na matendo.

1. Mikusanyiko ya kidunia, Mdo. 19:32,39,41
2. Watu wa Mungu ulimwenguni katika Kristo, Mt. 16:18 na Waefeso
3. Kusanyiko la waumini wa mahali katika Kristo, Mt. 18:17; Mdo. 5:11 (katika aya hii, ni kanisa huko Yerusalemu); Mdo. 13:1; Rum. 16:5; 1 Kor. 16:19; Kol. 4:15; Filemoni uk. 2
4. Watu wa Israeli kwa ujumla, Mdo. 7:38, katika hotuba ya Stephano
5. Watu wa Mungu kwenye Miji, Mdo. 8:3; Gal. 1:2 (Yuda au Palestina)

Kanisa ni watu waliokusanyika, na sio jengo. Hapakuwepo na majengo ya kanisa kwa muda wa miaka mingi. Katika Y akobo (moja ya kitabu cha mwanzo ni kabisa cha Wakristo) kanisa lilitajwa kwa neno "*synagōgē*" (kusanyiko). Neno kanisa limetokea tu kwa Yakobo (k.v. Yakobo 2:2; 5:14).

**5:12-16** Huu ni muhtasari mfupi, ambao ni kibainishi kikuu cha kitabu cha Matendo ya Mitume (kama vile Matendo ya Mitume 2:43-47 na 4:32-35).

**5:12** "ishara na maajabu mengi" Hii ni kauli tendewa elekezi (yenye ushahidi) ya wakati usio timilifu. Haya maneno mawili yanaonekana ndani ya nukuu za Petro kutoka Yoeli 2 katika Matendo ya Mitume 2:19. Miujiza ilifanyika kwa kujirudiarudia (kama vile Matendo ya Mitume 2:43; 4:30; 5:12; 6:8; 7:36; 14:3; 15:20). Kumbuka kwamba maajabu si alama ya Uungu unaojiendesha yenyewe (kama vile Mt. 24:24; na 2 The. 2:9), bali ilikuwa na ni njia ya kuthibitisha ujumbe wa Kikristo, ambao kwa muhimu sana ulikuwa tofauti na mtazamo na msistizo wa Dini ya Kiyahudi.

☐ **"nia moja"** Tazama Maelezo kamili katika Matendo ya Mitume 1:14. Ni muhimu kwa Luka kusistiza hili kwa mara nyingine tena. Huu ulikuwa ukweli kwamba halikuwa na mwisho!

☐ **"katika ukumbi wa Sulemani"** Hii ilikuwa safu ya nguzo iliyokuwa wazi ndani ya eneo la Hekalu kandokando ya ukuta wa mashariki wa Mahakama ya Mataifa. Yesu mara nyingi alifundisha hapo pia (kama vile Yohana 10:23). Hili lilikuwa eneo la Petro na Yohana kukamatwa kwa mara ya kwanza.



### 5:13

**NASB** "hapana hata mmoja aliyethubutu kuambatana nao"

**NJIV, NRSV** "hapana hata mmoja aliyethubutu kuungana nao"

**TEV** "Hapana hata mmoja nje ya kundi aliyethubutu kuungana nao"

**NJB** "Hapana hata mmoja zaidi ya hao aliyethubutu kuungana nao"

Hiki si kifungu cha kawaida. Hiki kinaonekana kueleza upande hasi wa neno "hofu." Kuna makundi kadhaa yanayoonyeshwa undani wa maandiko haya (kama vile Matendo ya Mitume 5:12-16). Kwa walio wengi, matukio yalikuwa kielelezo cha imani katika Kristo (kama vile #5 na bila shaka #6 na #7) au uthibitisho wa imani katika Kristo (yaani., #3).

1. Mitume, Matendo ya Mitume 5:12
2. watu, Matendo ya Mitume 5:12,13
3. waamini (yaani, ndani ya makubaliano ya aina moja katika ukumbi wa Suleimani), Matendo ya Mitume 5:12
4. hata mmoja (yaani, uongozi wa Kiyahudi), Matendo ya Mitume 5:13
5. waamini wapya, Matendo ya Mitume 5:14
6. wagonjwa wa Yerusalemu, Matendo ya Mitume 5:15
7. wagonjwa na walioudhiwa na pepo wachafu kutoka kando kando ya miji, Matendo ya Mitume 5:16

Kitenzi jina cha kauli ya kati ya wakati uliopo ya neno "kuambatana" kiuhalisia ni "kuganda." Luka analitumia neno hili mara nyingi, lakini katika tofauti iliyo na maana pana. Hapa hili neno linarejea juu ya kutokuwa sehemu ya kundi jipya (yaani, tofauti ya waamini ndani ya Kristo kama Masihi aliyehaidiwa).

**5:14"walioamini"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo ambyo inamaanisha tendo endelevu. Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:40 na 3:16.

**NASB,TEV**

**NJB, NIV** "katika Bwana"

**NKJV, NRSV** "kwa Bwana"

Huu muundo wa kisarafu (yaani, mfumo wa uhusika nane) unaweza kueleweka kama wakati ("kwa") au wa mahali ("katika"). Nafikiri hii ni njia ya kuonyesha kwamba waamini ni wa Bwana. Sisi tunamilikiwa Naye, na Yeye ni wetu!

☉**"wanawake"** Luka kwa upekee anasistiza "wanawake," pote katika Injili na Matendo ya Mitume (yaani, Matendo ya Mitume 1:14; 8:12; 16:1,13; 17:4,12,34; 18:2; 21:5). Yesu alnaleta maana mpya ya utu na thamani ya wanawake na watoto.

☉**"wakazidi kuongezeka"** Mara nyingi Luka alitumia semi za ufupisho wa ukuaji wa kanisa (kama vile Matendo ya Mitume 2:47; 5:14; 6:7; 9:31; 12:24; 16:5; 19:20).

**5:15" ili Petro akija, ngawa kivuli chake"** Miujiza katika kiwango hiki ilikuwa ya kawaida kama njia ya kuithibitisha injili. Kwa uwazi alikuwa msemaji wa Mitume. Kwa aina hii ya uthibitisho, uponyaji ulitokea kupitia Paulo (kama vile Matendo ya Mitume 19:12).

Kama wafasiri yatupasa kukumbuka kwamba ishara za miujiza hii zilitolewa kwa ajili ya

1. kuonyesha huruma ya Mungu
2. kuionyesha kweli ya injili
3. kuonyesha ni viongozi gani walioitwa na Mungu

Ishara hizi zilitolewa ndani ya utamadni maalum, kwa ajili ya kusudi binafsi. Kwa kuwa Mungu alilifanya hili mahali pale, moja kwa moja haimaanishi kwamba Yeye atafanya jambo lilile katika kila kipindi cha historia katika kila utamaduni. Siyo kwamba Mungu si mtendaji katika kila zama ama si mwenye huruma, bali wale watu wa Mungu yawapasa kuenenda kwa imani na si kwa utambuzi! Miujiza inaendelea, lakini wokovu wa mwenye dhambi lazima uwe shabaha kuu, si uponyaji wa mwili kwa wale watakaendelea kufa! Kwangu mimi inaonekana kwamba Mungu habadiliki. Sifa yake, uweza wake, huruma yake, na shauku ya wote kuokolewa inabaki palepale, lakini kwa kuangalia historia kithiolojia, kuna vipindi vikuu viwili vyenye nguvu, ishara za nguvu ya asili, vyote vyatoka kwa Mungu na kwa Shetani.

1. Mazingira wakati wa kubadilika katika umbo la kibinadamu na maendeleo ya kanisa la awali
2. Matukio ya awali ya nyakati za mwisho pale waamini watakapokuwa chini ya mateso ya kutisha Ningependa kumnukuu A. T. Robertson, *Word Pictures in the New Testament*, juzuu. III, uk. 62 "Hakikia, kulikuwa na, ukosefu wa maadili au nguvu ndani ya kivuli cha Petro. Hii ilikuwa imani yenye kuchanganyikana na ushirikina, hakika, haya mambo ni sawa na yale yaiyotokea katika Injili (Mt. 9:20; Marko 6:56; Yohana 9:5) na matumizi ya kitambaa cha mkononi cha Paulo (Matendo ya Mitume 19:12). Mungu huiheshimu hata imani ya kishirikina ikiwa ni imani ya kweli katika yeye. Watu wachache ni waoga kabisa wa imani ya ushirikina."

**5:16"nao wote wakaponywa"** Hii ni kauli tendewa elekezi ya wakati usiotimilifu, ambayo inaeleza kuwa kila mtu aliponywa (hiyo nguvu ya ajabu iliyotumika kufanya mambo hayo haielezwi, lakini yaweza kuwa Roho) mtu mmoja kwa wakati huo huo, hakuna hata mmoja aliyebaki! Hii ni aina ya usemi mfupi. Je! Tunalichukulia hili kwa uhalisia (yaani, kila mmoja mmoja)? Yesu alihitaji imani au alitumia uponyaji ili (1) kuwapatia mafunzo wanafunzi au (2) kuusababisha umati kuwa na usikivu. Hii kwangu inanitisha kwamba si kwamba wote walioponywa katika Agano Jipya "waliokolewa"papo kwa papo (yaani, kumwamini Kristo na kuwa na maisha ya milele). Uponyaji wa mwili unachukua nafasi kidogo kwa wokovu wa kiroho.

Miujiza inakuwa na msaada pale tu inapotuleta kwa Mungu. Wanadamu wote wanaishi katika ulimwengu ulioanguka. Mambo mabaya hutokea. Mara nyingi Mungu huchagua kutoingilia kati, lakini usemi huu hauseremi cho chote kulihusu pendo na uhusiano Wake. Jiahadhari na dai kwamba Mungu hutenda kazi kimiujiza kila wakati katika zama hizi za uovu. Yeye ni mkuu na hatufahamu maana kamili za hali yo yote inayojitokeza. Kwa kiwango hiki ningependa kuongeza maelezo ya maoni yangu kutoka 2 Tim. 4:20 kumhusu Paulo na uponyaji wa mwili (tazama [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org)) : "Kuna maswali mengi sana ambayo tungependa kuwauliza waandishi wa kitabu cha Agano Jipya. Jambo moja ambalo waamini wote wanafikiri kulihusu ni uponyaji wa mwili. Katika kitabu cha Matendo ya Mitume (kama vile Matendo ya Mitume 19:12; 28:7-9) Paulo anaweza kuponya, lakini hapa na katika 2 Kor. 12:7-10 na Flp. 2:25-30, anaonekana kutoweza. Kwa nini baadhi yao waliponywa na si wote, na kuna wakati mlango unafunguliwa kwa ajili ya uponyaji ambao umefungwa? Kwa uhakika naamini katika ushirikina, Baba mwenye huruma ambaye huponya kimwili pamoja na kiroho, lakini kwa nini kipengele cha uponyaji kinaonekana kuwepo na kisha kinaonekana kutokuwepo? Sifikiri kwamba hili limeunganishwa na imani (kama vile 2 Wakorintho 12).

Nahisi kwamba uponyaji na kuamini miujiza kulithibitisha uaminifu na uthabiti wa injili, ambayo bado inafanya kazi katika maeneo ya ulimwengu ambamo ilienezwa kwanza. Hata hivyo, Nafikiri kwamba Mungu anatutaka tuenende katika imani na si kwa mtazamo. Pia, maradhi ya mwili mara nyingi huachiliwa ndani ya maisha ya mwamini (1) kama adhabu ya maisha kwa ajili ya dhambi; (2) kama matokeo ya maisha katika ulimwengu ulioanguka; na (3) kuwasaidia waamini kukua kiroho. Tatizo langu ni kwamba kamwe siwezi kufahamu kitu gani kinahusishwa! Ombi langu juu ya mapenzi ya Mungu kufanyika katika kila jambo si uhaba wa imani bali ni jaribio la unyenyekevu kwa ajili ya kuruhusu hali ya neema, Mungu mwenye huruma huyafanya mapenzi yake katika

☐ "pepo wachafu" Tazama Mada Maalum hapa chini.

### MADA MAALUM: MALAIKA NA PEPO (PEPO WACHAFU)

- A. Watu wa kale waliamini kwamba viumbe vyote vina uhai. Walifikiri kwamba sifa za mwanadamu ni sawa na nguvu ya asili, wanyama, na viumbe vya asili. Maisha yalielezeka kupitia mwingiliano wa uwepo wa vitu/viumbe hivi na wanadamu.
- B. Mifano hii wakati mwingine ilileta matokeo ya kuabudu miungu mingi (miungu wengi). Kwa kawaida mapepo (*genii*) ilikuwa miungu midogo au nusu miungu (mizuri au miovu) ambao ilileta matokeo kadha wa kadha katika maisha ya watu binafsi.
1. Machufuko na migogoro huko Mesopotamia,
  2. Mpangilio na kazi huko Misri,
  3. Kanaani, tazama W. F. Albright's *Archaeology and the Religion of Israel*, Toleo la Tano, kur. 67-9
- C. Agano la Kale halielezi sana au kukuza jambo la miungu wadogo, malaika, au pepo, huenda ni kwa sababu ya msistizo wake mkali unaozungumzia Imani ya Mungu mmoja (tazama Mada Maalumu : Mungu mmoja\_ Imani ya Mungu mmoja kama vile Kut. 8:10; 9:14; 15:11; Kumb. 4:35,39; 6:4; 33:26; Zab. 35:10; 71:19; 86:8; Isa. 46:9; Yer. 10:6-7; Mik. 7:18). Haliizungumzii miungu ya uongo ya mataifa ya wapagani (*Shedim*, BDB 993, kama vile Kumb. 32:17; Zab. 106:37) na halitaji majina au kufananisha baadhi yao.
1. *Se'im* (mazimwi au majitu yenye manyoya, BDB 972 III, KB 1341 III, kama vile Law. 17:7; 2 Nya. 11:15; Isa. 13:21; 34:14)
  2. *Lilith* (pepo jike, pepo apotoshaye kizinifu nyakati za usiku, BDB 539, KB 528, kama vile Isa. 34:14)
  3. *Mavet* (neni la Kiebrania liliotumika kumtaja mungu mwovu wa Wakanani, Mot, BDB 560, KB560, kama vile Isa. 28:15,18; Yer. 9:21; na kwa kadri iwezekavyo Kumb. 28:22)
  4. *Resheph* ( mahali, moto, au mawe yenye kutiririsha mvua ya mawe, BDB 958, KB 958, kama vile Kumb. 32:24; Zab. 78:48; Hab. 3:5)
  5. *Dever* (uharibifu, BDB 184, cf. Zab. 91:5-6; Hab. 3:5)
  6. *Az'azel* (jina halina uhakika, lakini huenda akawa pepo wa jangwani au jina la mahali, BDB 736, KB 736, kama vile Law. 16:8,10,26)
- (Mifano hii inachukuliwa kutoka *Encyclopedia Judaica*, juzuu I. 5, uk. 1523.). Hata hivyo, hakuna imani ya Mungu wawili au uhuru wa malaika kutoka kwa YHWH katika Agano la Kale. Ibilisi chini ya YHWH (kama vile Ayubu 1-2; Zekaria 3), hayuko huru, ni adui anayejiongoza (kama vile A. B. Davidson, *A Theology of the Old Testament*, kr. 300-306).
- D. Dini ya Kiyahudi iliendelezwa kipindi cha uhamisho wa Babeli (586-538 b.k). Kitheolojia iliathiriwa aina mbili za Kiajemi zilizochukua nafasi kwa wafuasi wa Zoroaster, mungu mkuu na mzuri alitwa Mazda au Ormazd na mpinga uovu aitwaye Ahriman. Huyu aliruhusiwa ndani ya dini ya Kiyahudi baada ya uamisho na kuwa mfano wa aina mbili kati ya YHWH na malaika Zake na Ibilisi malaika zake au pepo.
- Theolojia ya dini ya Kiyahudi yenye kutoa mfano wa uovu inaelezwa na kunakiliwa vema katika Edersheim ya Alfred *The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII (kur. 749-863) na XVI (kur. 770-776). Dini ya Kiyahudi ilitoa mifano ya uovu katika njia tatu.
1. Ibilisi au Malaika wa maangamizi
  2. kusudi la uovu (yetzer hara) ndani ya mwandamu
  3. Malaika wa Mauti

Edersheim anayabainisha haya kama

1. Mshitaki
2. Mjaribu
3. Mwadhibishaji (juzuu. 2, uk. 756)

Kuna tofauti zinazodhihirika kitheolojia kati ya dini ya Kiyahudi iliyokuwepo baada ya uhamisho na namna uwasilishaji na maelezo ya uovu inavyofanyika ndani ya Agano Jipya.

- E. Agano Jipya, haswaa Injili, linadai uwepo na upinzani wa uovu wa viumbe vya kiroho kwa mwanadamu na kwa YHWH (katika dini ya Kiyahudi, Ibilisi alikuwa adui wa mwanadamu, lakini si kwa Mungu). Hawa wanayapinga mapenzi ya Mungu, amri, na ufalme.

Yesu alikabiliana na kuvifukuza hivi viumbe vya kimapepo, pia viliitwa (1) roho mchafu (kama vile. Luka 4:36; 6:18) au (2) roho za uovu kama vile Luka 7:21; 8:2), kutoka kwa wanadamu. Yesu kwa udhihirisho alitengeneza tofauti kati ya maradhi (kimwonekano na kiakili) na hali ya kimapepo. Aliithibitisha nguvu Yake na mtazamo wa ndani wa kiroho kwa kuwatambua na kuwafahamu hawa pepo wabaya. Mara nyingi walimtambua na kumwita, lakini Yesu alikataa ushuhuda wao, alihitaji wawe kimya, na kuyafukuzia mbali. Utambuzi wa pepo hawa ni ishara ya kuvunja ufalme wa Ibilisi.

Kuna upungufu wa ajabu wa habari ndani ya barua za Kitume za Agano Jipya kuhusiana na somo hili. Utambuzi huu kamwe haukuorodhesha karama za kiroho, wala methodolojia au hatua yake iliyotolewa kwa ajili ya vizazi vijavyo vya huduma au waamini.

- F. Mwovu yu dhahiri; mwovu ni mtu binafsi; mwovu yupo. Si asili yake wala kusudi lake linalofunuliwa. Biblia inatetea ukweli wake na kwa ukali inapinga ushawishi wake yule mwovu. Ndani ya ukweli hakuna hatima yenye mitazamo yenye uwili ndani yake. Mungu yu ndani ya utawala wake mwenyewe; mwovu anaangamizwa na kuhukumiwa na ataondolewa kutoka katika uumbaji.
- G. Watu wa Mungu yawapasa kumpinga mwovu (kama vile Yakobo 4:7). Hawawezi kutawaliwa na naye (kama vile 1 Yohana 5:18), bali wanaweza kujaribiwa na ushuhuda na ushawishi wake kuangamizwa (kama vile Efe. 6:10-18). Mwovu ni sehemu ya mtazamo wa ulimwengu kwa wakristo uliofunuliwa. Wakristo wa sasa hawana haki ya kueleza wazi kwa mara nyingine (kutafasiri upya maandishi ya Rudolf Baltmann); kuyaua maovu (miundo ya kijamii ya Paul Tillich), wala kujaribu kuelezea kwa ukamilifu katika namna ya kisaikolojia (Sigmund Freud). Ushawishi wake umeenea kote, lakini umeangamizwa. Waamini wanahitaji kuenenda ndani ya ushindi wa Kristo!

## **MADA MAALUM : UPUNGAJI PEPO)**

Upungaji Pepo yalikuwa mambo ya kawaida katika siku za Yesu, lakini njia za Yesu zilikuwa tofauti sana (kama vile Mt. 8:16; Marko 1:27). Upungaji Pepo Wake ilikuwa ishara ya Zama Mpya (kama vile Luka 9:1). Walimu wa Sheria za Kiyahudi (kama vile Mt. 12:27; Matendo ya Mitume 19:13) walitumia njia za nguvu za giza (tazama Alfred Edersheim, *The Life and Times of Jesus, The Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII, uk. 748-763; XVI, kur. 770-776), lakini Yesu alitumia mamlaka yake Mwenyewe. Kuna mkanganyiko mkubwa na habari mbaya zinazoenea kwa sasa kuhusu upungaji pepo na pepo wachafu. Sehemu ya tatizo hili ni kwamba Agano Jipya haijadili juu ya mambo haya. Kama mchungaji natumaini ninayo habari zaidi kuhusu jambo hili. Hapa kuna baadhi ya vitabu ninavyoviamini.

1. Christian Counseling and the Occult, Kurt E. Koch

2. Demons in the World Today, Merrill F. Unger
3. Biblical Demonology, Merrill F. Unger
4. Principalities and Powers, John Warwick Montgomery
5. Christ and the Powers, Hendrik Berkhof
6. Three Crucial Questions About Spiritual Warfare by Clinton Anton

Hii inanishangaza kwamba upungaji pepo haukuorodheshwa kama moja ya karama za kiroho na suala hilo halielezwi ndani ya barua za ki-Utume. Naamini katika mtazamo wa kiulimwengu kibiblia unahusisha ufalme wa kiroho (yaani, mema na mabaya), wakati uliopo na tendaji katika ufalme wa kiroho (yaani, Ayubu 1-2; Danieli 10; Efe. 6:10-18). Hata hivyo, Mungu amechagua kutofunua ule ubaya. Sisi kama waamini habari zote, tunahitaji kuishi ki-Ungu, maisha yenye manufaa Kwake! Lakini mambo mengine hayajafunuliwa kwa ukamilifu au kuimarishwa. Waamini wanahitaji kukumbuka kwamba upungaji pepo ni ushahidi unaonekana juu ya ushindi wa Yesu dhidi ya uovu (kama vile Luka 10:17-20). Kitabu cha Agano Jipya kinaunda tofauti iliyo wazi kati ya upungaji pepo na uponyaji (kama vile Mt. 8:16; Marko 1:32; Luka 4:40-41).

Tazama Mada Maalum:

1. Mada Malum: Shetani
2. Mada Maalum: Uovu Binafsi
3. Mada Maalum: Pepo Wachafu katika AK
4. Mada Maalum: Pepo Wachafu katika AJ

#### **ANDKO LA NASB (LILIOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 5: 17-26**

<sup>17</sup>Akaondoka Kuhani Mkuu na wote waliokuwa pamoja naye, (hao ndio walio wa madhehebu ya Masadukayo), wamejaa wivu, <sup>18</sup>wakawakamata mitume wakawaweka ndani ya gereza; <sup>19</sup>lakini malaika wa Bwana akafungua milango ya gereza usiku, akawatoa, akasema, <sup>20</sup>Enendeni mkasimame hekaluni mkawaambie watu maneno yote ya Uzima huu. <sup>21</sup>Nao waliposikia wakaenda alfajiri hekaluni, wakaanza kufundisha. Akaja Kuhani Mkuu nao waliokuwa pamoja naye, wakawakutanisha watu wa baraza, na wazee wote wa wana wa Israeli, wakatuma watu gerezani ili wawalete. <sup>22</sup>Hata watumishi walipofika hawakuwaona gerezani, wakarudi wakatoa habari, <sup>23</sup>wakisema, Gereza tumeikuta imefungwa salama, nao walinzi wamesimama mbele ya mlango; lakini tulipoufungua hatukukuta mtu ndani. <sup>24</sup>Basi jemadari wa hekalu na wakuu wa makuhani waliposikia haya, wakaingiwa na shaka kwa ajili yao, litakuwaje jambo hilo. <sup>25</sup>Mtu mmoja akaja akawapasha habari ya kwamba, Watu wale mliowaweka gerezani wako ndani ya hekalu, wamesimama wakiwafundisha watu. <sup>26</sup>Ndipo yule jemadari akaenda pamoja na watumishi, wakawaleta, lakini si kwa nguvu, kwa maana waliogopa watu wasije wakawapiga kwa mawe.

**5:17" wamejaa wivu"** Neno la Kiyunani kwa ukawaida linamaanisha "kuchemsha." Kwa hiyo, muktadha lazima utwambie kwamba hii ni shauku au wivu. Aya hii inaonyesha nia ya kweli ya viongozi wa kidini, wivu! Katika Injili ya Luka maadui wakubwa wa Yesu walikuwa Mafarisayo, lakini katika kitabu cha Matendo ya Mitume maadui Wake wengi waliomfuata walikuwa Masadukayo. Kitenzi "kujawa" kinatumika katika njia tofautitofauti kwa Luka kuonyesha kile kinamchobainisha au kumweleza mtu au utambulisho wa mtu.

1. Yohana Mbatizaji, hata kabla ya kuzaliwa kwake, alikuwa amejazwa na Roho Mtakatifu – Luka 1:15
2. Elizabeti alikuwa amejazwa na Roho Mtakatifu – Luka 1:41
3. Zacharia alikuwa amejazwa na Roho Mtakatifu –Luka 1:61
4. wale wote waliokuwa ndani ya Sinagogi waliosikia Yesu akizungumza kuwa alikuwa amejaa ghadhabu – Luka 4:28

5. wale waliokuwa ndani ya nyumba walikuwa wamepooza na walipitishwa juu ya paa wakiwa wamejawa na hofu – Luka 5:26
6. Mafarisayo na Waandishi wakifuatana na Yesu katika siku ya Sabato wakiwa wamejaa ghadhabu – Luka 6:11
7. Wale waliokuwa ghorofani katik sikukuu ya Pentekoste walikuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu – Matendo ya Mitume 2:4
8. Wale waliomsikia Petro akizungumza hekaluni walijawa na mshangao – Matendo ya Mitume 3:10
9. Petro akizunguza mbele ya Wakuu wa Sinagogi alikuwa amejazwa na Roho Mtakatifu – Matendo ya Mitume 4:8
10. wote waliokuwa ghorofani walikuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu – Matendo ya Mitume 4:31
11. Shetani alijaza mioyo ya Anania na Safira – Matendo ya Mitume 5:3
12. Petro na Yohana waliwaambia tena Wakuu wa Sinagogi na walijaa na wivu – Mateno ya Mitume 5:17
13. Yerusalemu ikajazwa kwa injili – Matendo ya Mitume 5:28
14. watu saba waliojawa na Roho na hekima– Matendo ya Mitume 6:3
15. Stefano alikuwa amejawa na imani na Roho Mtakatifu – Matendo ya Mitume 6:5,8; 7:55
16. Anania alimwekea mikono Sauli/Paulo na alikuwa amejawa na Roho Mtakatifu –Matendo ya Mitume 9:17
17. Paulo alihubiri akiwa amejawa na Roho Mtakatifu – Matendo ya Mitume 13:9
18. Wayahudi waliokuwa katika umati aliouhubiri Paulo walijawa na wivu – Matendo ya Mitume 13:45
19. Wanafunzi waliendelea kujaa furaha na Roho Mtakatifu – Matendo ya Mitume 13:52
20. Waefeso walijawa na ghasia – Matendo ya Mitume 19:29

Katika uwepo wa injili wewe “umejazwa” nini?

**5:18** Hizi sura tatu za mwanzo katika Matendo ya Mitume zinaonyesha matatizo yaliyoikumba kanisa la mwanzo. Matatizo yanatofautiana zama kwa zama, tamaduni kwa tamaduni, bali Mungu yu kwa ajili yetu, pamoja nasi, na anatuwezesha kushinda. Hakuna—gereza, kutendewa unyanyasaji, adha, nk.—viwezavyo kuwazuia waamini katika uwepo na amani ya Kristo (kama vile. Rum. 8:31-39).

**5:19"malaika wa Bwana"** Kifungu hiki kimetumika katika njia mbili ndani ya Agano la Kale.

1. malaika (kama vile Mwa. 24:7,40; Kut. 23:20-23; 32:34; Num. 22:22; Amu. 5:23; 1 Sam. 24:16; 1 Nya. 21:15 na kuendelea Zek. 1:28)

kama njia ya kurejea juu ya HWH (kama vile Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:2,4; 13:21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-24; 13:3-23; Zek. 3:1-2)Luka anakitumia kifungu hiki mara kwa mara (kama vile Luka 1:11,13; 2:9; Matendo ya Mitume 5:19; 7:30; 8:26; 12:7,11,23; 10:3; 27:23), lakini katika maana ya #1 hapo juu. Kitabu cha Agano Jipya hakitumii maana ya #2, isipokuwa katika Matendo ya Mitume 8:26 na 29, ambapo, "malaika wa Bwana" anafanana na Roho Mtakatifu.

☛**"akafungua milango ya gereza"** Hii ni sawa na lile tukio la katika Wafilipi (kama vile Matendo ya Mitume 16:26). Katika njia nyingi za maisha ya Petro zinafananishwa na zile za Paulo. Hili linaweza kuwa dhamirio la Luka la kimaandishi.

**5:20"nendeni mkasimame hekaluni mkawaambie"** Hizi zitatenda kazi kama kauli shurutishi tatu.

1. Enendeni, kauli ya kati shurutishi (yenye ushshidi) ya wakati uliopo
2. Mkasimame, kauli tendewa endelevu ya wakati uliopita usio timlifu ambayo inatumika kama tungo shurutishi (Friberg's, *Analytical Greek New Testament*, uk. 379)

3. Mkawaambie, kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Yule malaika alikuwa na ujumbe wa kiinjili kwa lile kanisa la mwanzo (na kwa kanisa la sasa).

☐ "mkawaambie watu" Huu ulikuwa msukumo mkuu wa huduma ya Mitume. Ujasiri (angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 4:29), si hofu, inayobainisha maisha yao mapya ya kujazwa na Roho.

NASB "maneno yote ya Uzima huu"

NKJV "habari yote ya maisha haya"

NRSV "maneno yote ya uhai huu"

TEV "yote kuhusu uzima huu mpya"

NJB "yote kuhusu Uhai huu mpya"

Kifungu hiki kinazunguzia uzima mpya (*zōe*, maisha ya milele) kinachopatikana katika injili ya Yesu Kristo pekee. Hawa walikuwa wamewekwa huru katika hali zote kiroho (wokovu) na kimwili (nje ya gereza). Sasa iliwapasa kuwaambia watu wote (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Matendo ya Mitume 1:8)!

**5:21** Tambua kwamba kuwa huru kutoka nguvu za giza hakukumaanisha kuwa hawa wasingetiwa gerezani tena. Hata gereza la Mungu halimaanishi kwamba magumu yote yatapatiwa ufumbuzi au kuondolewa ndani ya huruma (kama vile Mt. 5:10-12; Rum. 8:17; 1 Pet. 4:12-16)

☐ "baraza. . . wazee wote wa wana wa Israeli" Tazama Mada Maalum: Wakuu wa Sinagogi katika Matendo ya Mitume 4:5. Je! hawa "wazee" wanarejea juu ya nani? Curtis Vaughan, katika *Acts*, kur. 39-40, anasema hawa walikuwa wazee wa Yerusalemu ambao hawakuwa moja ya Wakuu wa Sinagogi kwa wakati huo (kama vile M. R. Vincent, *Word Studies*, Juzuu. 1, uk. 234), lakini tafsiri za NASB na NIV zinasadiki kwa mba Baraza na Wazee ni visawe.

**5:23** "imefungwa" Hii ni kauli tendewa ya wakati uliopo unaoendelea. Wazo lilikuwa kwamba milango ya gereza ilikuwa imelindwa na kuwekewa mipangilio (kauli tiomilifu tendaji ya hali ya kuendelea), lakini wafungwa walikwenda zao.

**5:24** "wakaingiwa na shaka" Luka analitumia neno hili mara kadhaa. Huu ni muundo chochezi wa neno *aporeō* (kama vile Luka 24:4; Matendo yha Mitume 25:20) pamoja na neno *dia* (kama vile Luka 9:7; Matendo ya Mitume 2:12; 5:24; 10:17). Maana yake ya msingi ni ya wasiwasi, ni ya uyumkini, au kimashaka.

☐ "litakuwaje jambo hilo" Muundo wa kisarufi wa kifungu hiki ni sentensi yenye masharti dalaja la nne isiyokamilika (*an* pamoja na kauli ya kati [yenye ushahidi] ya wakati uliopita usiotimilifu yenye uchaguzi). Dhamira ya uchaguzi inaeleza mfadhaiko (kama vile Luka 1:61-62; 3:15; 8:9; 15:26; 22:23; Matendo ya Mitume 5:24; 8:31; 10:17; 21:33, angalia James Allen Hewett, *New Testament Greek*, uk. 195).

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 5:27-32

<sup>27</sup> Walipowaleta, wakawaweka katika baraza. Kuhani Mkuu akawauliza, <sup>28</sup> akisema, Je! Hatukuwaamuru ninyi kwa nguvu, msifundishe kwa jina hili? Nanyi, tazameni, mmeijaza Yerusalemu mafundisho yenu, na mnataka kuileta damu ya mtu yule juu yetu. <sup>29</sup> Petro na mitume wakajibu, wakisema, Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu. <sup>30</sup> Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu, ambaye ninyi mlimwua mkimtundika katika mti. <sup>31</sup> Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi. <sup>32</sup> Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtii.

**5:26** "waliogopa watu wasije wakawapiga kwa mawe" Hili linaonyesha wingi wa watu wa kanisa la mwanzo (kama vile Matendo ya Mitume 5:13; 2:47; 4:21) na chanzo cha wivu endelevu wa viongozi wa Kiyahudi.

5: 28

NASB, NRSV

TEV "Hatukuwaamuru ninyi kwa nguvu"

NKJV "hatukuwashurutisha kwa nguvu"

NJB "onyo kali"

Tafsiri ya NKJV ina aya "Hatukuwasurutisha kwa nguvu msifundishe kwa jina hili," ambayo ni tofauti ya machapisho ya Kiyunani yanayopatikana ndani ya maandiko ya Kiyunani  $\alpha^2$ , D, na E, lakini si katika MSS P<sup>74</sup>,  $\alpha^*$ , A, au B. Tafsiri ya UBS<sup>4</sup> inaweka uchaguzi wa tafsiri ya NKJV ndani ya maandiko, lakini "si" katika mabano. Swali hili linatarajia jibu la "ndiyo". Mitume walionywa! Uundaji huu ni nahau ya Kisemitiki (kama vile Luka 22:15) una ufanano na uhusiano wa kushutumu katika lugha ya Koine ya Kiyunani, ambapo kitenzi (*parangellō*) na kiarifu (*parangelia*) vinatokana na mzizi ule ule. Uundaji huu unachochea maana ya msingi ya maneno. Inavutia kwamba neno hili lililo katika mafunjo yaliyotumika yaliyoandikwa lugha ya Koine yanayopatikana huko Misri lilimaanisha wito maalum au amri kutoka mahakamani (kama vile Moulton na Milligan, *Vocabulary of the Greek New Testament*, uk. 481).

☐ "mtu yule" kifungu hiki kinaonyesha dharau ya viongozi wa Kiyahudi. Kamwe hawakuthubutu kulitaja jina la Yesu. Buku la Sheria za Kiyunani pia linamuita "hivyo na hivyo" (kama vile M. R. Vincent, *Word Studies*, juzuu 1, uk. 234).

☐ "damu ya mtu yule juu yetu" Petro na Yohana waliendelea kudai kwamba viongozi wa Kiyahudi ndiyo waliosababisha kifo cha Yesu (kama vile Matendo ya Mitume 5:30; 2:33; 3:14-15; 4:10). Pia jambo hili lilikuwa shutma ya Stefano katika Matendo ya Mitume 7:52.

5:29 "Imetupasa" Neno hili dei linamaanisha umuhimu wa maadili. Hili linaonyesha wajibu wa Mitume kuihubiri kweli, pasipo kujali matokeo (kama vile Matendo ya Mitume 4:19). Angalia maelezo kamili katika Matendo ya Mitume 1:16.

5:30 "Mungu wa Baba zetu" Hawa Wakristo wa mwanzo waliamini kuwa walikuwa warithi wa kweli wa kiroho na uzao wa watu wa Mungu wa Agano la Kale (kama vile Matendo ya Mitume 3:13; Rum. 2:28-29; Gal. 6:16; 1 Pet. 3:5,9; Ufu. 1:6).

☐ "alimfufua Yesu" Kitabu cha Agano Jipya kinathibitisha kwamba Baba alimfufua Yesu (kama vile Matendo ya Mitume 2:24,32; 3:15,26; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 6:4,9) kuidhinisha kweli ya maisha ya Yesu na mafundisho. Hiki ni kipengele kikuu cha *Kerygma* (kama vile 1 Wakorintho 15). Pia inatakiwa kukumbukwa kwamba Kitabu cha Agano Jipya kinathibitisha kwamba Mwana na Roho pia walihusishwa katika tukio kuu uthibitisho huu.

1. Mwana – Yohana 2:19-22; 10:17-18
2. Roho – Rum. 8:11

☐ "ambaye ninyi mlimwua mkimtundika katika mti" Hii inarejeshajuu ya laana ya Kumb. 21:23. Hawa viongozi wa kidini walimtaka Yesu, aliyejifanya kuwa wa ki-Masihi, kubeba ile laana ya YHWH. Yesu aliiondoa laana ya sheria ya Agano la Kale (yaani, roho ile itendayo dhambi itakufa [kama vile Eze. 18:4,20] wa wanadamu wote waliotenda dhambi, kama vile Rum. 3:9-18, 23) kwetu (kama vile Gal. 3:13; Kol. 1:14). Yesu alikuwa Mwana-kondoo wa Mungu aliyezichukua dhambi za ulimwengu (kama vile Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21).

5:31 "Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume" Neno "kutukuza" linatafsiriwa katika Yohana 3:14 kama "kuinuliwa" na katika Flp. 2:9 kama "kutukuzwa sana" Msalaba wa Yesu unamaanisha kuinuliwa na ushindi (kama vile Kol. 1:15; 2 Kor. 2:14). Hiki kifungu chenye uhusiano na mwonekano wa kibinadamu "mkono wa kuume" kilikuwa sitiari ya mahali pa nguvu na mamlaka (kama vile Mt.26:64). Mungu ni Roho wa milele. Yeye hana umbo-



mwili. Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:33.

☐ **"Mkuu"** Mstari huu kwa uwazi kabisa na kwa upekee unaelezea juu ya Umasihi wa Yesu. Neno kama hili lilitumika juu ya Yesu katika Matendo ya Mitume 3:15, ambapo lingeweza kutafsiriwa kama "mwanzilishi" (NRSV). Hili linaweza kumaanisha "kiongozi mkuu," "mwasisi," au "mwana wa mfalme." Hili pia lilitumika kwa mwanzilishi wa shule au familia (kama vile Ebr. 2:10; 12:2). Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 3:15.

☐ **"Mwokozi"** Neno hili lilitumika katika karne ya kwanza ya ulimwengu wa Uyunani ya Kirumi wa Kaizari. Huyu alidai kuwa yeye ni mwokozi wa utamaduni na amani. Neno lingine ambalo watu wa majina ya Kaizari walivyoyahitaji wenyewe, lakini walilitumia kwa Yesu kwa namna ya tofauti, huyu alikuwa Bwana (*kurios*). Neno hili "Mwokozi" lilitumika katika Agano la Kale kama neno la YHWH (kama vile kama vile 2 Sam. 22:3; Zab. 106:21; Isa.43:4,11;45:15,21; 49:26; 60:16; 63:8). Waandishi wa Agano Jipya mara nyingi walieleza Uungu wa Yesu kwa kumpa sifa ya majina ya YHWH ya Agano la Kale. Tambua namna Paulo katika barua yake kwa Tito alifanya hili.

1. Tito 1:3, "Mungu Mwokozi wetu"
2. Tito 1:4, "Kristo Yesu Mwokozi wetu"
3. Tito2:10, "Mungu Mwokozi wetu"
4. Tito 2:13, "Mungu wetu mkuu na Mwokozi wetu, Kristo Yesu"
5. Tito 3:4, "Mungu Mwokozi wetu"
6. Tito 3:6, "Yesu Kristo Mwokozi wetu"

☐ **"awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi"** Hili linaonyesha makusudu ya kifo cha Yesu (kama vile Luka 24:47 na Matendo ya Matendo ya Mitume 2:38). Si kawaida waandishi wa Agano Jipya kurejerea juu ya toba na kama karama itokayo kwa Mungu (kama vile Matendo ya Mitume 11:18 [kwa Mataifa]; 2 Tim. 2:25; na kwa hakika pia Rum. 2:4). Mara nyingi hili ni moja ya mahitaji ya Agano Jipya kwa mwanadamu aliyeipokea injili (kama vile Marko 1:15 na Matendo ya Mitume 3:16,19; 20:21). Nafikiri hii ni njia ya kimaandishi ya kuonyesha kwamba Mungu anawataka wanadamu wote waliumbwa kwa sura na mfano wake kuokolewa. Hili jambo halikuhusu ukuu wa Mungu. Mara nyingi wale wanaotazamia kwa upekee sehemu ya Mungu ndani ya Agano Jipya wanautumia mstari huu kuhakikisha kwamba wokovu ni mambo yote ya Mungu na hauhusishi ushiriki wowote kwa upande wa mwanadamu. Hata hivyo, huu ni mfano mzuri wa kukihakiki kifungu cha maandiko ili kwenda sawa na mfumo wa mawazo ya mtu ya thiolojia ya awali.

Kwa uwazi kabisa Biblia inaeleza umuhimu na uhitaji wa uanzilishi wa Mungu, lakini pia inafunua kwamba ile dhana ya agano" inaeleza mfano Wake aliouchagua wa namna ya kuhusianisha utu wa muhitaji. Uhuru ni neema ambayo Mungu aliitoa kupitia uuumbaji. Mungu haibatilishi neema hii/kazi yake (kama vile Rum. 2:4; 2 Kor. 7:10). Yeye hutuvuta, hutuvumilia, hutenda kazi pamoja nasi, na kutupa njia ya wokovu (kama vile Yohana 6:44, 65). Lakini wanadam walioanguka yawapasa kuitikia na kuendelea kuitikia katika toba, imani, utii, na ustahimilivu. Hapa kuna nukuu inayovutia kutoka kwa Frank Stagg, *New Testament Theology*, uk. 119: "Watu hawawezi kufanikiwa isipokuwa wakipokea toba, bado wanatakiwa kuipokea. Kwa imani mtu humpokea Kristo na utu wa ndani; na Kristo, kama aliyesababisha kuwepo kwa mageuzi na mabadiko yaliyosababisha maisha hayo kutoka katika kujiaminisha kuelekea katika kumwamini Mungu, kutoka katika kujitetea kuelekea katika kujikana wenyewe. Badiliko hili ni urejeo wa yule Aliyeanguka, ambamo mwanadamu alitazamia kupata maana kamili ya kuwepo kwake ndani yake mwenyewe."

**5:32** Mara nyingi katika Matendo ya Mitume Peto anarejea juu ya ile kweli kwamba Mitume na wanafunzi walikuwa mashahidi wa maisha ya Yesu na kifo na ufufuo. Katika muktadha huu anaongeza, "Roho Mtakatifu" kama ushahidi. Hili linaweza kuwa njia ya kukiri njia mbili muhimu za Agano la Kale kulithibitisha jambo (kama vile

Hes. 35:30; Kumb. 17:6).

Luka/Matendo ya Mitume inazingumzia juu ya huyu Roho

1. katika ubatizo – Matendo ya Mitume 2:38
2. katika ubatizo wa injili – Matendo ya Mitume 5:32
3. hayatapatikana kwa mali – Matendo ya Mitume 8:19-20
4. kwa Mataifa – Matendo ya Mitume 10:45; 11:17
5. kutoka kwa Baba – Luka 11:13 (kama vile Yakobo 1:17)

☐ **"wote wantiio"** Utii ni uchaguzi wa maisha! Yatupasa kutii kwa kuiamini injili. Yatupasa kuendelea katika utii ili tuyafurahie matunda yake (kama vile Mt. 7:24-27; Luka 6:46-48). Hili neno adimu "kutii" (*peithomai* kuongeza *archē*, kama vile Matendo ya Mitume 27:21; Tito 3:1), lililotumika katika Matendo ya Mitume 5:29 na 32, lilikuwa muungano wa maneno "kiongozi" (*archē*) na kuitikia.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 5:33-39**

<sup>33</sup> Wao waliposikia wakachomwa mioyo yao; wakafanya shauri kuwaua. <sup>34</sup> Lakini mtu mmoja, Farisayo, jina lake Gamalieli, mwalimu wa torati, mwenye kuheshimiwa na watu wote, akasimama katika baraza, akaamuru mitume wawekwe nje kitambo kidogo, <sup>35</sup> akawaambia, Enyi waume wa Israeli, jihadharini jinsi mtakavyowatenda watu hawa. <sup>36</sup> Kwa sababu kabla ya siku hizi aliondoka Theuda, akijidai ya kuwa yeye ni mtu mkuu, watu wapata mia nne wakashikamana naye; naye aliuawa na wote waliomsadiki wakatawanyika wakawa si kitu. <sup>37</sup> Baada ya mtu huyo aliondoka Yuda Mgalilaya, siku zile za kuandikiwa orodha, akawavuta watu kadha wa kadha nyuma yake, naye pia akapotea na wote waliomsadiki wakatawanyika. <sup>38</sup> Basi sasa nawaambia, Jiepusheni na watu hawa, waacheni; kwa kuwa shauri hili au kazi hii ikiwa imetoka kwa binadamu, itavunjwa, <sup>39</sup> lakini ikiwa imetoka kwa Mungu hamwezi kuivunja; msije mkaonekana kuwa mnapigana na Mungu.

5:33

NASB "wakachomwa mioyo yao"

NKJV "wakawa hasira"

NRSV "wakaghadhabika"

TEV "wakawa na hasira"

Neno hili kifasihi linamaanisha "kukatisha usemi" au "kusaga meno" Neno hili linalofanana na lililo katika muundo huo huo pia linatumika katika Matendo ya Mitume 7:54, ambapo kifungu kilichoongezwa, "utaingia moyoni mwako," kinaonyesha maana kamili ya kistiari (pia angalia Luka 2:35). Hili neno lenye nguvu (yaani, *diaprō*) kina fanana na maana na 2:37a katika.

☐ **"wakafanya shauri kuwaua"** Hii ni kauli ya kati (yenye ushahidi) elekezi isiyotimilifu, inayomaanisha kwamba (1) hapo hapo wakaanza kufanya shauri la kuwaua au (2) huu ulikuwa mpango wao na shauku yao ya mara kwa mara. Kutokana na ufahamu wetu wa ukuaji wa kanisa la mwanzo kutoka Matendo ya Mitume, #1 inakaa vizuri zaidi. Tambua kwamba Masadukayo ndiyo walielezwa kuwa na ghadhabu na kusudi la kuuu. Inawezekana kwamba Mafarisayo (yaani, Gamalieli) waliliona kanisa la mwanzo kama mwiba uliotumika kuwachoma Masadukayo walioukataa ufufuowa Yesu kwa ujumla. Mafarisayo wasingependa kuukiri ufufuo wa Yesu, bali wangeikiri dhana au ufufuo uliyofuatiwa na maisha ya baadaye pamoja na Mungu. Inashangaza kwa viongozi wa Biblia za sasa kwamba viongozi wa kidini wangepanga mauaji. Kumbuka hawa Masadukayo walikuwa na msimamo wa maandiko ya Musa, ambayo yalishurutisha kwamba wanaokufuru yawapasa kupigwa kwa mawe hadi kufa. Viongozi hawa walifikiri kwamba walikuwa wakitenda badala ya Mungu na kwa ukubalifu wa neno Lake kama vile

**5:34" Mafarisayo" tazama mada maalum ifuatayo.**

**MADA MAALUMU: MAFARISAYO**

- I. Neno lilikuwa na uwezekano wa kuwa na asili moja kati ya hizi zifuatazo:
  - A. "Kujitenga." Kundi hili lilianza wakati wa ufuasi wa kiongozi wa Kiyahudi Yuda wa karne ya pili (hii ni mtizamo mpana sana unaokubalika), na kujitenga wao wenyewe toka kwenye umma wa watu ili kutunza tamaduni simulizi za sheria ya Musa (yaani, mienendo ya kichini chini ya Kiyahudi iliyopatikana karne ya 18).
  - B. "Kugawa" Hii ni maana nyingine toka kwenye kiini kile kile cha lugha ya Kiebrania (BDB 827, BDB 831 I, KB 976); yoye yakimaanisha "kugawanya." Baadhi ya wasomi wanasema linamaanisha mfasili (kama vile Neh. 8:8; 2 Tim. 2:15).
  - C. "Uajemi." Hii ni maana nyingine toka kwenye kiini kile kile cha lugha ya Kiarama (BDB 828, KB 970). Baadhi ya mafundisho ya mafarisayo yanaingiliana na wafuasi wa dini za Kiislamu za awali toka Uajemi zilizoanzishwa na Zoroaster (angalia maada maalumu Uovu).
- II. Pamekuwepo na nadharia nyingi nani alianzisha Ufarisayo.
  - A. Kikundi cha kithiolojia cha dini ya mwanzo ya Kiyahudi (angali, Yusufu)
  - B. Kikundi cha kisiasa toka kipindi kile cha Herode
  - C. Kikundi cha kisomi cha wafasiri wa sheria za Musa ambao walitaka kuwasaidia watu wa kawaida kuelewa Agano la Musa na tamaduni simulizi zilizowazunguka.
  - D. Mienendo ya chini kwa chini ya maandishi, kama vile Ezra na Sinagogi kuu, wakigombea uongozi wa ukuhani mkuu katika hekalu.

Yaliundwa nje ya misigishano na

1. Makabaila wasiokuwa Wayahudi (hasa Antiokia IV).
  2. jamii ya watu wakuu dhidi ya watu wa kawaida
  3. wale waliojifungamanisha kwenye maisha ya agano dhidi ya Wayahudi wa kawaida toka Palestina
- III. Habari zetu kuwahusu wao zinatoka
    - A. Yusufu, aliyekuwa mfarisayo
      1. Vitu vya kale vya Kiyahudi
      2. Vita vya Wayahudi
    - B. Agano Jipya
    - C. Asili ya awali ya Kiyahudi
  - IV. Mafundisho yao makuu
    - A. Imani ya kuja kwa Masiha, iliyoshawishiwa na maandishi wa Kibiblia wa Kiyahudi wenye fasihi ya kimaono kama vile Enock.
    - B. Imani ya kwamba Mungu yu hai katika maisha yetu ya kila siku. Hii moja kwa moja ilikuwa kinyume na Masadukayo (kama vile Mdo. 23:8). Mafundisho mengi ya Kifarisayo yalikuwa ni kijazilizo cha yale ya Masadukayo.
    - C. Imani katika maelekezo ya kimwili baada ya maisha yaliyolenga maisha ya duniani, yaliyojumuisha zawadi na adhabu (kama vile Dan.12:2)
    - D. Imani katika mamlaka ya Agano la Kale vile vile simulizi za kitamaduni (Talmud). Walitambua kuwa watiifu kwa amri za Mungu za Agano la Kale kama zilivyo tafasiliwa na shule za wasomi wa sheria za

Kiyahudi (Shammai, asiyependa mabadiliko na Hillel, anayependa mabadiliko). Watafasiri wa sheria za Kiyahudi walisimamia juu ya mazungumzo kati ya wanasheria/walimu wa falsafa mbili zinazokinzana, mmoja asiyependa mabadiliko na mwingine anayependa mabadiliko. Mazungumzo haya ya kisumulizi juu ya maana ya andiko hatimaye likaandikwa kwa miundo miwili: sheria za kiibada za Wababeli na sheria za kiibada zisizo kamili za Wapalestina. Waliamini kuwa Musa alipokea hizi sheria za mdomo kwenye Mlima Sinai. Mwanzo wa haya mazungumzo ya kihistoria yalianzishwa na Ezra na watu wa "Sinagogi kuu" (baadaye wakaitwa Sanhedrin)

- E. Imani ilioanzishwa juu ya mafundisho ya kithiolojia ya kimalaika. Haya yalijumuisha viumbe wazuri na wabaya. Hili lilianzia huko Uajemi yenye pande mbili na fasihi za Kiyahudi zenye mwingiliano na Biblia.
- F. Imani juu ya mamlaka ya kifalme ya Mungu, lakini pia mazoezi ya utashi huru wa binadamu(yetzer).
- V. Nguvu ya mabadiliko ya Kifarisayo.
  - A. Walipenda, waliheshimu, kuamini mafunuo ya Mungu (yaani., yote, yakijumuisha sheria, Manabii, Maandiko, na simulizi za kitamaduni)
  - B. Walijitolea kuwa wafuasi wenye haki (yaani., maisha ya kila siku na imani) wa mafunuo ya Mungu. Walitaka "Israel yenye haki" kutimiza ahadi ya kinabii ya siku mpya yenye mafanikio.
  - C. Walitetea kuwepo usawa na jamii za Kiyuda, ambao unajuisha ngazi zote za watu, kwa maana kuwa, walikataa uongozi wa kikuhani (yaani, masadukayo) na thiolojia(kama vile Mdo. 23:8).
  - D. Walipigania kitu halisi cha mtu kwenye agano la sheria za Musa. Walitetea au kudai mamlaka ya Mungu, lakini pia wakashikilia kwenye hitaji la utendaji huru wa mwanadamu
  - E. Agano Jipya linataja mafarisayo mbali mbali walioheshimika (yaani., Nikodemu, Mtawala tajili kijana, Yusufu wa Alimataya).

Walikuwa ni kundi hilo tu la dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza kuhimili uharibifu wa Yerusalemu na hekalu toka kwa Warumi mwaka wa 70 B.K. wakawa ni dini ya Kiyahudi ya kisasa

## **MADA MAALUM : GAMALIELI**

- I. Jina
  - A. Jina hili linamaanisha "Mungu ndiye mtoaji wangu wa thawabu."
  - B. Huyu anajulikana kama "kiongozi " au Gamalieli. Kwangu mimi kumtofautisha mtu huyu na jamaa wajao, pia huyu alikuwa mashughuli ndani ya uongozi wa Kiyunani.
- II. Mtu
  - A. Desturi zinasema huu alikuwa mjuukuu wa Hileli.
  - A. Desturi zingine zinasema huyu ameunganishwa ndani ya familia ya ufalme wa Herode (yaani, Agripa I).
  - B. Desturi zinasema huyu alikuwa kiongozi wa Wakuu wa Sinagogi, lakini huenda hili likarejea juu ya Gamalieli II.
  - C. Huyu alikuwa mmoja wa walimu wa saba wa sheria walioheshimiwa sana na waliopewa wadhifa wa Rabban.
  - D. Huyu alifariki kabala ya 70 b.k.
- III. Thiolojia yake
  - A. Huyu alikuwa mwalimu wa sheria wa siku za Yesu aliyeheshimiwa sana (kama vile Matendo ya Mitume 5:34).
  - B. Huyu alijulikana kwa kujali na kubaki katika uthibiti usambaaji wa Wayahudi waliokimbilia nje

ya nchi.

- C. Huyu alijulikana kwa kujali kwake jamii iliyonyimwa haki (usemi wake ulianza mara nyingi ulianza na "kwa manufaa ya kibinadamu").
  - 1. Yatima
  - 2. Wajane
  - 3. Wanawake
- D. Huyu alikuwa alikuwa mshauri wa walimu wa kisheria kwa Mtume Paulo ndani ya Jerusalem (kama vile Matendo ya Mitume 22:3).
- E. Katika Matendo ya Mitume 5:34-39 anatoa mawazo ya hekima na busara namna ya kulitunza kanisa humo Palestine.
- F. Kiongozi huyu alikumbukwa sana kwa sababu ya hili katika kifo chake hili lilizungumziwa, "Wakati Rabban Gamalieli mzee aliyeufia utukufu wa Torati iliyokuwa huru na utakaso na utakatifu (lit. 'utengano') uliopotea (Sot. 9:15), ilichukuliwa kutoka katika Encyclopedia Judaica, juzuu. 7, uk. 296.

Lazima ielezwe kwamba nia ya Gamalieli katika Matendo ya Mitume 5:34-39 ni ya uhakika. Huyu anaweza kuwa anaitetea hekima ya Mafarisayo dhidi ya uchochezi wa Masadukayo. Haya madhehebu mawiliyenye nguvu yalinyanyasana katika kila upenyo!

**5:36-37" Theuda. . . Yuda Mgalilaya,"** Josephus anayataja majina haya mawili yanayofanana (kama vile *Antiq.* 20.5.1). Hata hivyo, aliyasikiliza katika mpangilio uliokuwa kinyume. Taarifa zingine za kihistoria zinaonyesha kwamba kulikuwa na watu wawili wenye jina hili ambao walikuwa wakereketwa dhidi ya Rumi. Kwa hiyo, wote walioandika kitabu cha Agano Jipya na Josephus wanaweza kuwa sahihi. Mtu aliyetajwa kwa jina la Gamalieli ameandikwa katika karne ya 6 b.k, ambapo aliyetajwa na Josephus ameandikwa katika karne ya 44 b.k.

**5:37 " siku zile za kuandikiwa orodha"** Josephus (kama vile *Antiq.*18.1.1; *Wars* 2.8.1) anatwambia kwamba Augustus aliamuru kodi itozwe kwa Wayahudi, mapema tu baada ya Archelaus kujiuzulu na Quirinius kuifanywa mjumbe wa Shamu (yaani, yapataa 6-7 b.k). Hizi siku za kuandikiwa orodha zilizokuwa na makusudi ya kutoza kodi ziliendeshwa kila baada ya miaka kumi na mine, lakini zilichukuwa muda kukamilika.

☐ **" Yuda Mgalilaya"** Huyu ametajwa na Josephus mara nyingi (kama vile *Antiq.* 18.1.1-6; 20.5.2 na pia katika *Wars* 2.8.1; 2.17.8-9). Uasi Wake ulijitokeza yapata karne ya 6 au 7 b.k. Huyu alikuwa mwasisi mkereketwa wa maandamano. Hawa wakereketwa (Josephus anawahita "falsafa ya nne) na Sicarii (yaani, wauaji) kwa hakika ni maandamano sawa na ya kisiasa.

**5:38 "Jiepusheni na watu hawa"** Ni ushauri gani ushangazao! Kifungu hiki kina kauli mbili tendaji shurutishi za wakati uliopita usiotimilifu.

- 1. *aphistēmi*, jitenge, kaa mbali
- 2. *aphiēmi*, jiondoe, tawanyika

☐ **"ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la tatu, ambayo inamaanisha tukio muhimu.

**5:39 "ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza, ambayo maranyingi inadokeza ukiri wa ile kweli, lakini hapa haiwezi kuwa ya kweli. Hii inaonyesha matunmizi ya kimaandishi ya muundo huu wa kisarufi.

☐ **" msije mkaonekana kuwa mnapigana na Mungu"** Inabidi kukumbukwa kwamba hawa viongozi wa kidini walifikiri kuwa walikuwa wakitenda kwa niaba ya Mungu. Ukweli ulio mkuu ni kuwa Gamalieli alizungumzia juu ya uwezekano wa wao kuwa na utii wa kimakosa na wa kushtua (kama vile Matendo ya Mitume 11:17).

**5:40" Wakakubali maneno yake"** Kifungu hiki kimehusishwa katika Matendo ya Mitume 5:39 katika baadhi ya tafsiri (kama vile NRSV) na katika Matendo ya Mitume 5:40 katika vitabu (kama vile NASB, NKJV). The Tafsiri za TEV na NJB zinakiendeleza kifungu hiki katika Matendo ya Mitume 5:39, lakini kinaanza na aya mpya.

**ANDIKO LA NASB ( LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 5: 40-42**

<sup>40</sup> **Wakakubali maneno yake; nao walipowaita mitume, wakawapiga, wakawaamuru wasinene kwa jina lake Yesu; kisha wakawaacha waende zao. 41 Nao wakatoka katika ile baraza, wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo. 42 Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo.**

☐ **"wakawapiga"** Hili halikuwa sawa na ule upinzani wa Kirumi (*mastix*, kama vile Matendo ya Mitume 22:24-25), ambao Yesu aliustahimili. Hili linarejea juu ya upigaji wa fimbo za Kiyahudi (kama vile Kumb. 25:3; yaani, *derō*, Luka 12:47-48; 20:10-11; 22:63). Inaumiza sana, lakini si utisho wa maisha. Tatatizo lenye kufafanuliwa ni kwamba haya maneno mawili ya Kiyunani mara nyingi yanatumika katika namna ya mabadiliko. Yale Maandiko ya Kale ya Kiyunani ya Kumb. 25:3 yana neno *mastix*, lakini hili linarejea juu ya adhabu ya Kiyahudi. Luka kwa ukawaida anatomia neno *derō* kuonyesha upigaji uliokuwa unafanyika ndani ya hili sinagogi la Kiyahudi (kifasihi hii ni "kuchuna mnyama").

☐ **"wakawaamuru wasinene kwa jina lake Yesu"** Baraza hili lilikuwa limelifanaya hili mapema sana (kama vile Matendo ya Mitume 4:17,21). Kwa kipindi hiki waliwapiga na walirudia kuwapa onyo.

**5:41** Yesu ameitabiri aina hii ya utendaji (kama vile Mt. 10:16-23; Marko 13:9-13; Luka 12:1-12; 21:10-19; Yohana 15:18-27; 16:2-4).

☐ **"wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo"** Hili linaonekana kushangaza leo kwa sababu tunaishi katika jamii ambamo mateso ya kimwili ni kawaida sana, lakini hali limekuwa si suala kubwa sana kwa umati wa waamini karne zote. Kwa uwazi Yesu anasema kwamba wafuasi wake lazima watapitia mateso. Tafadhari soma Mt. 5:10-12; Yohana 15:18-21; 16:1-2; 17:14; Matendo ya Mitume 14:22; Rum. 5:3-4;; 8:17; 2 Kor. 4:16-18; Flp. 1:29; 1 The. 3:3; 2 Tim. 3:12; Yakobo 1:2-4. Pia Tambaua namna Yesu alivyopitia mateso katika 1 Petro (kama vile Matendo ya Mitume 1:11; 2:21,23; 3:18; 4:1,13; 5:1) na inavyowapasa wafuasi wake kuyapitia hayo hayo (kama vile Matendo ya Mitume 1:6-7; 2:19; 3:13-17; 4:1,12-19; 5:9-10).

**5:42" kila siku, ndani ya hekalu"** Hawa mashahidi wa Yesu wa mwanzo walikaidi kunyamazishwa, hata ndani ya kila moyo wa Viongozi wa jamii ya Kiyahudi, kwenye hekalu la Yerusalemu.

☐ **"nyumbani mwao"** Kanisa la mwanzo lilikuwa na mikusanyiko yao ndani ya nyumba binafsi zilizokuwa zimezagaa mji mzima (kama vile Matendo ya Mitume 2:46). Hapakuwa na majengo ya kanisa hadi baada ya miaka mia moja baadaye.

**NASB, NKJV "Kristo"**

**NRSV, TEV**

**REB "Masihi"**

Katika utaratibu huu wa Kiyahudi jina "Masihi" (angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:31) linafaa sana (katika Matendo ya Mitume 2:31; 3:18; 5:42; 8:5; 9:22), kama Petro alivyolitumia katika Mt. 16:16. Paulo alipowahubiri Wayahudi pia alilitumia hili kama rejeo la kile kilicho ahidiwa, mtiwa Mafuta (kama vile Matendo ya Mitume 17:3; 18:5,28).

## MASWALI YA MJADALA WA MATENDO YA MITUME 3-5

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Mitume walikaa Uyunani kwa kipindi kirefu?
2. Orodhesha majina ya Yesu na maana zake ambazo zinatumiwa katika Matendo ya Mitume 3.
3. Je! ni mahitaji gani ya chini kabisa katika wokovu?
4. Kwa nini Musa alinukuliwa mara nyingi katika kitabu cha Agano Jipya?
5. Ni umuhimu gani uliopo wa agano la ibrahimu kwenye kanisa la Agano Jipya?
6. Kwa nini Petro na Yohana walitiwa mbaroni?
7. Eleza kwa muhtasari hotuba ya tatu ya Petro.
8. Ni umuhimu gani unaohusu ombi la matendo ya Mitume 4:24-31?
9. Kwa uwazi Agano Jipya linatakiwa kuwa la kiujamaa? (kama vile Matendo ya Mitume 4:32)
10. Orodhesha sababu kwa nini Luka anahusisha maelezo ya Anania na Safira.
11. Je! Anania alitambua kama alikuwa amejazwa na Shetani? Je! Alitambua kama amemdanganya Mungu?
12. Kwa nini Mungu alionekana kuchukizwa sana?
13. Vipi kuhusu miujiza (sanasana uponyaji) katika siku za leo?
14. Kwa nini Wasadukayo walishikwa na jazba sana?
15. Kwa nini malaika waliwatoa Mitume gerezani?
16. Eleza kwa muhtasari hotuba ya nne ya Petro. Orodhesha mambo ya pamoja kati ya hotuba zake zingine zilizonukuliwa katika Matendo ya Mitume.
17. Gamalieli alikuwa nani?
18. Kwa nini Wakristo yawapasa kufurahi kwa ajili ya kuteswa kwao?

## MATENDO YA MITUME 6

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kuteuliwa kwa saba	saba wanachaguliwa	uchaguzi wa saba	wasaidizi saba	Taasisi ya wale saba
6:1-6	Kuhudumu 6:1-7	6:1-7	6:1-4 6:5-6	6:1-6
6:7			6:7	6:7
Kukamatwa kwa Stephano	Stephano ashitakiwa kwa kukufuru	Kuhubiri na Ushujaa wa Stephano (6:8-7:2a)	kukamatwa kwa Stephano	kukamatwa kwa Stephano
6:8-15	6:8-15	6:8-7:2a	6:8-15	6:8-15

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("[A Guide to Good Bible Reading](#)")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Mdo. 6 na 7 njia za historia ya kifasihi za Luka ya kuanza kujadili misheni ya Mataifa.
- B. Kanisa la Yerusalemu lilikuwa limekua kwa kasi kwa muda huu (kama vile Mdo. 6:1).
- C. Kanisa lilikuwa likiundwa na Wayahudi wanaozungumza kiaramu kutoka Palestina na Wayahudi wanaozungumza Kiyunani kutoka ughaibuni.

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 6:1-6**

<sup>1</sup> Hata siku zile wanafunzi walipokuwa wakiongezeka hesabu yao, palikuwa na manung'uniko ya Wayahudi wa Kiyunani juu ya Waebrania kwa sababu wajane wao walisahauliwa katika huduma ya kila siku. <sup>2</sup>Wale Thenashara wakawaita jamii ya wanafunzi, wakasema, Haipendezi sisi kuliacha neno la Mungu na kuhudumu mezani. <sup>3</sup>Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili; <sup>4</sup>na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno. <sup>5</sup> Neno hili likapendeza machoni pa mkutano wote; wakamchagua Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho Mtakatifu, na Filipo, na Prokoro, na Nikanori, na Timoni, na Parmena, na Nikolao mwongofu wa Antiokia; <sup>6</sup>ambao wakawaweka mbele ya mitume, na walipokwisha kuomba wakaweka mikono yao juu yao.



**6:1 "wanafunzi"** Hii kidhahiri inamaanisha "watu wanaojifunza" kutoka katika kitenzi *manthanō*. Ni muhimu kutambua kwamba Agano Jipya linaweka mkazo "kufanyika wanafunzi" (kama vile Mt. 28:19; Mdo. 14:21), sio tu kufanya maamuzi. Maelezo haya kwa waamini ni ya kipee kwa Injili na Matendo ya Mitume. Katika barua, neno "ndugu" na "watakatifu" yametumika kumaanisha wafuasi wa Yesu.

▣ **"waliokuwa wakiongezeka kwa hesabu"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo. Ukuaji siku zote unasababisha mvutano.

▣ **"manug'uniko"** Neno hili linamaanisha "kunog'onona" (yaani mazungumzo binafsi kati ya watu, Moulton, *Analytical Lexicon*, p. 81). Inatokea mara kadhaa katika LXX ya Kutoka ikielezea hali ya kutapakaa na kutangatanga Jangwani (kama vile Kutoka 16:7,8; 17:3; pia Hesabu 11:1; 14:27). Neno hili hili linapatikana katika Luka 5:30 na mara kadhaa katika Yohana (kama vile Yohana 6:41,43,61; 7:12,32).

▣ **"Wayahudi wa mafundisho ya Uongo dhidi ya Waebrania wazawa"** Hii inamaanisha Wayahudi waaminio, wao waliokuwa wakitoka Palestina na wao kimsingi walizungumza Kiaramu na wale waliokulia ughaibuni walizungumza Koine ya Kiyunani. Walikuwa hakika watu wa desturi na wanaojitazama juu ya makabila yao.

▣ **"huduma ya kuhudumia chakula kila siku"** Kanisa la kwanza ilifuata utaratibu wa kisinagogi. Kila fedha za wiki (kama vile sadaka za kifedha) zilikusanywa kusaidia maskini. Fedha hii ilitumika kununua chakula ambazo zilitolewa kila wiki kwenye sinagogi na kila siku na kanisa la nyumbani. Angalia Mada Maalum: Misaada kwa wahitaji katika Mdo. 3:2.

Inaonekana kutokana na historia kwamba Familia nyingi za Kiyahudi waliofanya kazi katika nchi zingine walirudi Palestina katika siku za baadaye za Baba ili kwamba aweze kuzikwa katika nchi ya ahadi. Hivyo kulikuwa na wajane wengi katika Palestina hasa eneo la Yerusalemu.

Dini ya Kiyahudi ilikuwa ya kitaasisi (yaani Agano la Musa) juu ya maskini, wageni, na wajane (kama vile Kutoka 22:21-24; Kumb. 10:18; 24:17). Maandiko ya Luka inaonesha kwamba Yesu pia alijali wajane (kama vile Luka 7:11-15; 18:7-8; 21:1-4). Inakuwa hivyo sasa kwa asili kwamba kanisa la kwanza walijiwekea utaratibu wao wenyewe kwa vyote katika huduma za kijamii za Sinagogi na mafundisho ya Yesu yangeweza kugeuza hali ya kujali wajane wa Kanisa.

**6:2 "kumi na mbili"** Hili lilikuwa jina la jumla kwa ajili ya Mitume. Hao walikuwa wale watendakazi hasa wa kwanza kuchaguliwa na Yesu wakati wa huduma yake hapa duniani akianzia Galilaya.

▣ **"wakawaita jamii ya wanafunzi"** Kile kinachomaanishwa hapa kwa hakika hakijulikani katika namna kwamba kanisa liliundwa na maelfu kadhaa ya watu kwa maana hii, hivyo hakuna nyumba au biashara iliyokubwa kiasi cha kupokea kundi hili. Hii yawezekana ilifanyika katika Hekalu lenyewe, yawezekana sehemu ya Sulemani (kama vile Mdo. 3:11; 5:12).

Huu ni mfano wa kwanza wa kile kilichokuja kuitwa kusanyiko (kama vile Mdo. 6:3,5; 15:22). Hizi ni njia tatu za kibiblia ambazo kanisa la kisasa linapangwa:

1. Baraza la kiaskofu (yaani kiongozi mmoja mkuu Kiongozi)
2. Wa-presbyterian (yaani kundi la viongozi)
3. kusanyiko (yaani mwili wote wa waaminio)

Yote yanaonekana katika Matendo ya Mitume 15.

▣ **"Haipendezi kwetu sisi kuacha neno la Mungu ili kuhudumia meza"** Hili sio neno la kuparanganyisha kuhusu kuhudumia lakini mwanzo wa hitaji lililohisiwa kwa ajili ya kugawana majukumu kichungaji kati ya watu wa Mungu. Hizi hazikuwa ni ofisi bali kazi za kugawiwa. Utangazaji wa injili lazima ufanye kipaumbele juu ya huduma

zinazohitajika. Mitume walikuwa wameitwa kipekee na wenye sifa ya kufanya kazi. Hakuna cha kuwaweka mbali na jukumu hilo. Hii haikuwa "aidha/au," lakini hali ya "yote/na". Neno "kuhudumia" ni neno maarufu la Kiyunani kwa ajili ya huduma, *diakonia*. Bahati mbaya wafasiri wengi wa kisasa wanaangalia mwongozo kwa ajili ya ofisi za baadae za ushemasi (kama vile Wafilipi 1:1; 1 Tim. 3:8-10,12-13), wametumia maandiko haya kutoa maana na kuhalalisha hii kazi ya huduma. Hata hivyo hawa sio "mashemasi"; ni wahudumu na wahubiri tu wa kawaida. Ni wa-eisegesis wanaoweza kupata mashemasi katika Mdo. 6. Inashangaza kwangu namna kanisa hili la kwanza lilivyoweza kufanya huduma bila majengo.

1. wakati walipokutana wote lazima ilikuwa katika Hekalu.
2. Siku ya Sabato hakika walikutana katika masinagogi yao ya mahali pamoja na siku za Jumapili yawezekana katika nyumba za makanisa.
3. Wakati wa siku za wiki (kila siku) Mitume walihama kutoka katika nyumba za waamini kwenda katika nyumba za waamini (kama vile Mdo. 2:46).

### 6:3

<b>NASB</b>	<b>"chagua"</b>
<b>NKJV</b>	<b>"tafuta"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"chagua"</b>
<b>TEV</b>	<b>"lazima kuchagua"</b>

Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu (yenye ushahidi). Baadhi ya vitu vilitakiwa vifanywe kurejesha umoja. Hili jambo la kichungaji lilikuwa na uwezo wa kuathiri kuendelea kwa Injili. Kanisa lilitakiwa kupangilia kwa ajili ya huduma. Kila mwamini anaitwa na kupewa karama ya kuwa mhudumu wa injili wa wakati wote (kama vile Efe. 4:11-16).

▣ **"wanaume saba"** Hakuna sababu ya kutumia hesabu hii isipokuwa ilikuwa ni namba ya ukamilifu iliyotumiwa mara kwa mara katika Agano la Kale kwasababu ya uhusiano wake na siku saba za uumbaji (kama vile Mwanzo 1; Zaburi 104). Katika Agano la Kale kuna tukio lililotangulia kwa mchakato huu wa kuendeleza ufuatano huu wa uongozi (kama vile Hesabu 18). Angalia Mada Maalum: uwakilishi wa hesabu/namba katika Mdo. 1:3.

<b>NASB, NJB</b>	<b>"wenye sifa njema"</b>
<b>NKJV</b>	<b>"yenye sifa njema"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"yenye kupendeza"</b>
<b>TEV</b>	<b>"wanaojulikana kuwa"</b>

Tofauti ya tafsiri hizi mbili za kingereza zina aksi matumizi tofauti mawili ya matumizi ya hili neno.

1. "kutoa ushuhuda kwa" au kutoa taarifa kuhusu (kama vile matoleo ya TEV, NIV)
2. "kumzungumzia mtu vizuri" (kama vile Luka 4:22).

▣ **"akijaa Roho"** Ujazo wa Roho ulikuwa umetajwa mara kadhaa katika Mdo, Mara nyingi katika muunganiko na kumi na mbili na mahubiri yao, mafundisho/kufikia huduma. Inaashiria nguvu kwa ajili ya huduma.

Uwepo wa Roho katika maisha ya mtu ni swala unaloweza kulishuhudia. Upo ushahidi katika mtazamo, matendo na ufanisi. Wajane ni muhimu lakini kutangazwa kwa injili ni kipaumbele (kama vile Mdo. 6:4). Angalia kidokezo kamili katika "kujazwa" katika Mdo. 5:17.

▣ **"na ya hekima"** Ziko aina mbili za hekima katika Agano la Kale.

1. Kupata maarifa (taaluma)
2. maisha ya hekima (uzoefu)

Hawa wanaume saba wote walikuwa navyo vyote!

▣ **"ambao tutawaweka juu ya kazi hii"** Walikuwa na shughuli zenye kazi ndani yake. Kifungu hiki cha habari hakiwezi kutumiwa kuelezea kwamba mashemasi wanahusika na mambo ya biashara (KJV, "biashara hii") ya kanisa! Neno "jukumu" (*chraomai*) inamaanisha "uhitaji," sio "ofisi" (Alfred Marshall, *RSV Interlinear*, ukurasa 468).

**6:4 "kujitoe wenyewe"** Neno hilo la Kiyunani lilitumika katika namna kadhaa.

1. kuhusianisha na mtu kwa ukaribu, Mdo. 8:13
2. kumuhudumia mtu kibinafsi, Mdo. 10:7
3. Kwa kuendelea kujitoe kwenye jambo fulani au mtu fulani
  - a. wanafunzi wa kwanza wao kwa wao na maombi, Mdo. 1:14
  - b. mitume wa kwanza kwa mafundisho ya mitume, Mdo. 2:42
  - c. mitume wa kwanza wao kwa wao, Mdo. 2:46
  - d. Mitume kwa huduma ya maombi na Neno, Mdo. 6:4 (Paulo anatumia neno hilo hilo kuwaita waumini kudumu katika maombi, Warumi. 12:12; Kol. 4:2).

▣ **"maombi na huduma ya neno"** Tungo hii inawekwa mbele (yaani kuwekwa mbele kwanza) katika sentensi ya Kiyunani kwa ajili ya msisitizo. Je hii si yenye utata kwamba ilikuwa hii "saba" ambae alikuwa wa kwanza kukamata mamisheni ya ulimwengu, sio mitume. Ilikuwa "wale saba" ambao mahubiri yao yalilazimisha kuvunjika kwa dini ya kiyahudi, sio mitume.

Inashangaza sana pia kwamba Mitume hawakuwa waanzilishi wa Agizo Kuu lakini hawa Wayahudi wazungumzaji wa Kiyunani. Matendo ya Mitume haikuwahi kuweka kumbukumbu yao kutimiza jukumu walilopewa na mitume lakini badala yake inawaeleza kama wahubiri wa Injili. Kuhalalishwa kwao kunaonekana zaidi katika usambamba pamoja na jukumu hili zaidi ya utawala na hali ya kujali ya kichungaji inayotakiwa na kanisa katika Yerusalemu.

Badala ya kuleta amani, huduma zao zilileta mtafaruku na dhiki!

**6:5 "Stefano"** Jina lake linamaanisha "taji ya mshindi. "wote saba" walikuwa na majina ya Kiyunani, lakini Wayahudi wengi wa ughaibuni walikuwa nayo yote jina la kiebrania na Kiyunani. Majina peke yake hayamaanishi walikuwa Wayahudi wazungumzao Kiyunani. Sababu inasema kulikuwa na vikundi vyote pamoja.

▣ **"akijaa imani"** Neno imani lilikuja kutoka katika neno la Agano la Kale (yaani *emeth*) ambalo kiasili lilimaanisha mtu ambaye miguu yake ilikuwa inaweza kukanyaka hatua kiuthabiti. Ilikuwa kutumika kisitari kwa ajili ya mtu aliyekuwa mwaminifu, wa kuaminiwa, wakutegemewa na mwema. Katika Agano Jipya neno hili linatumika kwa ajili ya mwitikio wa Ahadi ya Mungu kupitia Kristo. Tunaamini katika uaminifu wake! Tunaweka imani katika uaminifu wake. Stefano aliamini katika uaminifu wa Mungu; hivyo alikuwa amejaa tabia za Mungu (Yaani amejaa imani, uaminifu).

## **MADA MAALUMU: Kusadiki, Amini, Imani na Uaminifu katika Agano la Kale**

- I. Maelezo ya awali  
Inahitajika kuanza kwamba utumiaji wa dhana ya kithiolojia, ni wa muhimu katika Agano Jipya, hauko wazi kama ulivyochezwa katika Agano la Kale. Hakika upo, lakini umethibitishwa katika aya na watu muhimu waliochaguliwa.  
Vitu ambavyo havikupatana katika Agano la Kale
  - A. Watu binafsi na jamii
  - B. Ukabiliano binafsi na utii wa aganoImani kwa ujumla ni ukabiliano binafsi na stadi ya maisha ya kila siku! Ni rahisi kuelezea katika maisha ya mfuasi mwaminifu kuliko katika muundo wa kinahau (yaani usomaji wa neno). Dhana hii binafsi

imeelezwa vizuri katika

- A. Ibrahimu na uzao wake
- B. Daudi na Israel

Watu hawa walikutana/kukabiliana na Mungu na maisha yao yalibadilika jumla (sio maisha kamilifu kihivyo, lakini ni kuendelea katika imani). Majaribu yalifichua udhaifu na nguvu ya imani yao ya kukabiliana na Mungu, lakini hatima, uhusiano wa kuamini umeendelea muda wote! Imani ilijaribiwa na kusafishwa, lakini ikaendelea kama ushuhuda kwa moyo wao wa ibada na stadi ya maisha.

II. Asili kuu iliyotumika

A. תָּמָא (BDB 52, KB 63)

1. KITENZI

- a. Shina la neno *Qal* -kutegemeza, kustawisha (yaani 2 Fal. 10:1,5; Esta. 2:7, matumizi yasio ya kithiolojia)
- b. Shina la neno ni *phal*-kuhakikisha au fanya imara, kuanzisha, kuhakiki, kuwa mwaminifu
  - 1) Kwa watu, Isa. 8:2; 53:1; Yer. 40:14
  - 2) Kwa vitu, Isa. 22:23
  - 3) Kwa Mungu, Kumb. 7:9; Isa. 49:7; Yer. 42:5
- c. Shina la neno *Hiphil* –kusimama imara, kusadiki, kuamini
  - 1) Ibrahimu alimwamini Mungu, Mwa. 15:6
  - 2) Waisrael katika Misri walamini, Kut. 4:31; 14:31 (ilikanushwa katika Kumb. 1:32)
  - 3) Waisrael wakamwamini YHWH alipoongea kupitia Musa, Kut. 19:9; Zab. 106:12,24
  - 4) Ahazi hakuamini katika Mungu, Isa. 7:9
  - 5) Yeyote aliyeamini katika Yeye, Isa. 28:16
  - 6) Ukweli wa kuamini kuhusu Mungu, Isa. 43:10-12
- 2. NOMINO (JINSI YA KIUME) –kubaki kuwa mwaminifu (yaani., Kumb. 32:20; Isa. 25:1; 26:2)
- 3. KIELEZI-kweli kabisa, kweli, nakubali, iwe hivyo (kama vile. Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Isa. 65:16; Yer. 11:5; 28:6). Hii ni namna ya liturujia ya neno “amina” katika agano la kale na agano jipya.

B. תָּמָא (BDB 54, KB 68) nomino jinsi ya kike, uimarifu, kuwa mwaminifu, kweli

- 1. Kwa watu, Isa. 10:20; 42:3; 48:1
- 2. Kwa Mungu, Kut. 34:6; Zab. 117:2; Isa. 38:18,19; 61:8
- 3. Kwenye ukweli, Kumb. 32:4; 1 Fal. 22:16; Zab. 33:4; 98:3; 100:5; 119:30; Yer. 9:5; Zak. 8:16

C. הַנּוֹמָא (BDB 53, KB 62), uimara, kusimama imara, uaminifu

- 1. Katika mikono, Kut. 17:12
- 2. Katika muda, Isa. 33:6
- 3. Katika watu, Yer. 5:3; 7:28; 9:2
- 4. Kwa Mungu, Zab. 40:11; 88:11; 89:1,2,5,8; 119:138

III. Matumizi ya Paulo juu ya dhana ya Agano la Kale

A. Paulo anaegemea uelewa wake mpya kuhusu YHWH na Agano la Kale juu ya ukabiliano wake na Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9:1-19; 22:3-16; 26:9-18).

B. Alipatwa kuungwa mkono na Agano la Kale kwa uelewa wake mpya katika aya mbili muhimu za Agano la Kale ambazo zilitumia asili ya neno (תָּמָא).

- 1. Mwa. 15:6- ukabiliano binafsi wa Abrahamu ulioanzishwa na Mungu (Mwanzo 12) ukasababisha maisha matiifu ya imani (Mwanzo 12-22). Paulo analidokeza hili katika Rumi 4 na Wagalatia 3.
- 2. Isa.28:16- wale walioamini ndani yake (yaani., kujaribiwa kwa Mungu na uwekaji wa jiwe kuu la pembeni kwa uthabiti) kamwe hautakuwa
  - a) Rum. 9:33 “aibisha” au “katisha tamaa”
  - b) Rum.10:11, kama ilivyo hapo juu
- 3. Hab. 2:4-wale wote wanaomfahamu Mungu Yule aliye mwaminifu lazima waishi maisha ya uaminifu (kama vile Yer. 7:28). Paulo analitumia neno hili katika Rum. 1:17 na Gal 3:11 (pia angalia Hab. 10:38)

IV. Matumizi ya Petro ya dhana ya Agano la Kale

- A. Petro anaunganisha
  - 1. Isa. 8:14 – 1 Pet. 2:8 (jiwe la kujikwaa)
  - 2. Isa. 28:16 – 1 Pet. 2:6 (jiwe kuu la pembeni)
  - 3. Zab. 118:22 – 1 Pet. 2:7 (jiwe lililokataliwa)
- B. Alibadilisha lugha ya kipekee ambayo iliielezea Israel kama “jamii iliyochaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa teule, watu waliomilikiwa ya Mungu mwenyewe” toka
  - 1. Kumb. 10:15; Isa. 43:21
  - 2. Isa. 61:6; 66:21
  - 3. Kut. 19:6; Kumb. 7:6

Na sasa anatumia kwa minajili ya imani ya kanisa katika Kristo (kama vile 1 Petro 2:5,9)

V. Matumizi ya Yohana kwenye dhana hii

A. Utumiaji wake kwenye Agano Jpya

Neno “aaminiye” linatokana na neno la Kiyunani pisteuō ambalo pia laweza kutafasiliwa “kuamini,” “sadiki,” au “imani.” Kwa mfano, nomino haionekani kwenye injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna mashaka kama kwenye uhalisia wa kundi kujitoka kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha wao. Mifano mingine wa utumiaji wa kubabiababia wa neno hili “kuamini” unapatikana katika Yohana 8:31-39 na Mdo. 8:31; 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi kuliko ukubalifu wa awali. Lazima uambatane na mchakato wa uanafunzi (Mt. 13:20-22,31-32).

B. Utumiaji wake ukiwa na vivumishi

1. *eis* inamaanisha “ndani ya” muundo huu wa kipekee unasisitiza waumini kuweka imani yao kwa Yesu
  - a. ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
  - b. ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45 48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Flp. 1:29; 1 Petr. 1:8)
  - c. ndani yake (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
  - d. ndani ya mwana (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
  - e. ndani ya Yesu (Yohana 12:11; Mdo 19:4; Gal. 2:16)
  - f. ndani ya nuru (Yohana 12:36)
  - g. ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
2. *ev* inamaanisha “katika” kama ilivyo katika Yohana 3:15; Marko 1:15; Mdo 5:14
3. *epi* ikimaanisha “katika” au “juu ya” kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6
4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1 Yoh. 3:23; 5:10
5. *hoti*, likimaanisha “kuamini kwamba,” inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
  - a. Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
  - b. Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
  - c. Yesu ndani ya Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
  - d. Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
  - e. Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
  - f. Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
  - g. Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
  - h. Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30)
  - i. Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye “Mimi ndiye” (Yohana 8:24; 13:19)
  - j. Tutaishi naye (Rum. 6:8)
  - k. Yesu alikufa na kufufuka tena (1The. 4:14)

VI. Hitimisho

- A. Imani ya Kibiblia ni ukubarifu wa mwanadamu katika neno/agano la Kiungu. Mungu siku zote huanzisha (yaani., angalia Mada Maalumu: Agano)
1. Toba (angalia Mada Maalumu: Toba)
  2. Sadiki/amini (angalia Mada maalumu)
  3. Utii
  4. Usitahimilivu (angalia Mada maalumu: Usitahimilivu)
- B. Imani ya Kibiblia ni
1. Uhusiano binafsi (imani ya awali)
  2. Uthibitisho wa kweli wa Kibiblia (imani katika ufunuo wa Mungu, yaani., andiko)
  3. Kuwajibika katika utii sahihi (uaminifu wa kila siku)
- Imani ya Kibiblia sio tiketi ya kwenda mbinguni au utaratibu wa bima. Ni mahusiano binafsi. Na hili ndio kusudi la uumbaji, mwanadamu aliumbwa katika sura na mfanano (kama vile Mwa. 1:26-27) wa Mungu. Suala hapa ni kwamba “urafiki wa karibu.” Mungu anapendelea ushirika, sio msimamo fulani wa kithiolojia! Lakini ni ushirika na Mungu aliye mtakatifu anataka kuwa wana waonyeshe tabia za “kifamilia” (yaani utakatifu, kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; 1 Petro 1:15-16). Anguko (kama vile Mwanzo) liliathiri uwezo wetu kuwajibika kwa usahihi. Kwa hiyo, Mungu akatenda kwa niaba yetu (kama vile Ezek. 36:27-38), akitupatia “moyo mpya” na “roho mpya” inayotuwezesha kupitia imani na toba ili kuwa na ushirika na Yeye na kumtii Yeye! Yote haya matatu ni muhimu. Yote haya matatu yanapaswa kudumishwa. Kusudi ni kumjua Mungu (wote kwa maana ya Wayunani na Waebrania)
- C. Uaminifu wa mwanadamu ni matokea (Agano la Jipya), na sio msingi (Agano la Kale) wa uhusiano na Mungu: imani ya mwanadamu katika uaminifu wake; kusadiki kwa mwanadamu katika kuamini kwake. Moyo wa Agano Jipya katika mtazamo wa wokovu ni kwamba mwanadamu lazima mwanzoni kabisa awajibike na aendelea kuwajibika kwenye neema na rehema ya Mungu, iliyoonyeshwa katika Kristo. Alipenda, alitumwa, alitoa, lazima tuwajibike katika imani na kuamini (kama vile Efe. 2:8-9 na 10)

Mungu aliye mwaminifu anawahitaji watu waaminifu kujidhihilisha kwao kwa ajili ya ulimwengu usio na imani na kuwaleta wote kwenye imani binafsi katika Yeye.

▣ **"akijaa . .Roho Mtakatifu"** Kuna aina nyingi za tungo ambazo zinafunua huduma ya Roho kwa waaminio:

1. Kuugua kwa Roho (kama Yohana 6:44,65)
2. Ubatizo wa Roho (kama vile 1 Kor. 12:13)
3. matunda ya Roho (kama vile Gal. 5:22-23)
4. Karama ya Roho (kama vile 1 Kor. 12)
5. Kujazwa kwa Roho (kama vile Efe. 5:18).

Kujazwa kwa Roho Mtakatifu kunamaanisha vitu viwili: (1) kwamba mtu anaokolewa (kama vile Warumi 8:9) na (2) kwamba mtu anaongozwa kwa Roho (kama vile Warumi 8:14). Inaonekana kwamba "ujazo" kunahusishwa na mtu kuendelea kujazwa (kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopo ya Efe. 5:18). Kwa ajili ya "kujazwa" angalia kidokezo kamili katika Mdo. 5:17.

▣ **"Philipo"** Kuna Philipo kadhaa katika Agano Jipya. Huyu ni mmoja wa wale saba. Jina lake ni "mpenda farasi." Huduma yake inaelezwa katika Mdo.8. Alikuwa muhimu katika uvuvio wa Samaria na mshuhudiaji binafsi wa mfanyakazi wa kiserikali kutoka Kushi (Ethiopia). Anaitwa "mwinjilisti" katika Mdo. 21:8 na binti zake walikuwa watendaje katika huduma (yaani manabii wa kike, kama vile Mdo. 21:9, Angalia [MADA MAALUM: WANAWAKE KATIKA BIBLIA](#) katika Mdo. 2:17).

▣ **"Prokoro"** Machache yanajulikana juu ya mtu huyu. Katika *The International Standard Bible Encyclopedia*, vol. 4, James Orr (ed.) anasema alikuwa Askofu wa Nicomedia na alikufa kama shujaa wa kidini katika Antiokia (ukurasa wa 2457).

▣ **"Nikanori"** Katika historia ya kanisa hakuna kinachojulikana kuhusu mtu huyu. Jina lake ni la Kiyunani na linamaanisha "mshindaji."

▣ **"Timoni"** Hakuna chochote kinachojulikana kuhusu mtu huyu katika historia ya kanisa. Jina lake la Kiyunani na linamaanisha "mshimiwa."

▣ **"Parmena"** Hiki nikifupi cha *Parmenides*. Desturi za kikanisa zinasema kuwa aliwawa kishujaa katika Filipi wakati wa utawala wa Trajan (kama vile *The International Standard Bible Encyclopedia*, vol. 4, ukurasa wa 2248).

▣ **"Nikolao Mwangofu wa Antiokia"** Taarifa zingine zinaweza kuwa zilitolewa kuhusu mtu huyu kwasababu jina jiji lake linawezekana ni lilelile la nyumbani kwao na Luka. Akiwa mwongofu Myahudi ilijumuisha matendo ya taratibu matatu:

1. kwamba mtu ajibatize mwenyewe mbele ya mashuhuda
2. kwamba mtu kama ni wa kiume alitakiwa atahiriwe
3. kwamba mtu kama walikuwa na fursa, walitoa dhabihu katika hekalu

Kumekuwa na mkanganyiko kuhusu mtu huyu katika historia ya kanisa kwasababu kuna kundi lenye jina sawa lililotajwa katika Ufunuo. 2:14-15. Baadhi ya Mababa wa kanisa la kwanza (yaani Irenaeus na Hippolytus) walidhani alikuwa mwanzilishi wa kikundi cha walimu wa mafundisho ya uongo. Wengi wa mababa wa kanisa walitaja muunganiko wakati wote kundi lingejaribu kuelezea muasisi wao kuwa alikuwa kiongozi wa kanisa la Yerusalemu.

**6:6 "waliweka mikono yao juu yao"** Sarufi hii inamaanisha kwamba kanisa zima liliwawekea mikono (kama vile Mdo. 13:1-3), Ingawa kiwakilishi kinachorejerewa.

Kanisa la Kirumi limetumia maandiko kama hili kuelezea kuchukua kwa hatamu ya kitume. Katika maisha ya Kiubatizo tunatumia maandiko kama hili kuelezea kuwekwa wakfu (yaani kuweka wakfu watu katika huduma fulani). Ikiwa ni kweli kwamba waaminio wote wanaitwa, wanapewa karama na ni wahudumu wenye karama (kama vile Efe. 4:11-12), hivyo hakuna utofauti katika Agano Jipya "kichungaji" na "kuhudumu." Hali ya usomi iliandaa mazingira na kukuzwa na desturi zisizo za kibiblia za kihubiri zisizopewa mashiko zinazotakiwa kuangaliwa upya na kuchunguzwa katika nuru ya maandiko ya Agano Jipya. Kuwekea mikono kunaweza kumaanisha kazi lakini sio mamlaka yaliyo thabiti. Desturi nyingi za kidhehebu ni za kihistoria au za kidhehebu zikijikita na zisizo wazi kiefundisho ya biblia au mamlaka. Desturi sio tatizo mpaka zimekuzwa kiasi cha kuchukua mamlaka ya kimaandiko.

## **MADA MAALUM: KUWEKEA MIKONO KATIKA BIBLIA**

Hii ishara ya kujumuishwa inatumiwa sana katika njia mbalimbali katika Biblia.

1. kula kiapo (yaani mkono katika uvungu wa paja [kama vile Mwanzo 24:2,9; 47:29])
2. kuchukua uongozi wa familia (kama vile Mwanzo 48:14,17,18)
3. kutambua kifo cha dhabihu ya mnyama kama mbadala
  - a. Makuhani (kama vile Kutoka 29:10,15,19; Law. 16:21; Hes. 8:12)
  - b. kuwalaza watu (kama vile Law. 1:4; 3:2,8; 4:4,15,24; 2 Nyakati. 29:23)
4. mtu wa kukaa pembeni kumtumikia Mungu kwa ajili ya jukumu maalumu au huduma (kama vile Hes. 8:10; 27:18,23; Kumb. 34:9; Mdo. 6:6; 13:3; 1 Tim. 4:14; 5:22; 2 Tim. 1:6)
5. kushiriki katika kurusha mawe kwa kimahakama kwa kumpiga mwenye dhambi (kama vile Law. 24:14)

6. mkono katika mdomo wa mtu huashiria ukimya au tafakari (kama vile Waamuzi. 18:19; Ayubu 21:5; 29:9; 40:4; Mika 7:16)
7. Mkono wa mtu ukiwa katika kichwa chake humaanisha huzuni/ombolezo (2 Sam. 13:19)
8. kupokea Baraka za afya, furaha na utauwa (kama vile Mt. 19:13,15; Marko 10:16)
9. ikihusiana na uponyaji wa mwili (kama vile Mt. 8:3; 9:18,20; Marko 5:23; 6:5; 7:32; 8:23; 16:18; Luka 4:40; 13:13; Mdo 9:17; 28:8)
10. kupokea Roho Mtakatifu (kama vile Mdo. 8:17-19; 9:17; 19:6, angalia Kumbu. 34:9)

Kwa kushangaza kuna ukosefu wa mfanano katika vifungu ambavyo kihistoria vimekuwa vinatetea kuwekwa wakfu kwa viongozi kwa ajili ya kazi ya injili (yaani kuwekwa wakfu , angalia Mada Maalum: Kuwekwa Wakfu).

1. Katika Mdo. 6:6 Ni mitume wanaoweka mikono yao kwa ajili ya huduma ya watu saba ya kanisa la mahali pamoja.
2. Katika Mdo. 13:3 Ni Mitume na Walimu wanaoweka mikono juu ya Barnaba na Paulo kwa ajili ya huduma ya kimishenari.
3. Katika Mdo. 1 Tim. 4:14 Ni viongozi wa kanisa la nyumbani (wazee) waliojumuishwa katika wito wa kwanza na kuwekwa rasmi.
4. In Katika 2 Tim. 1:6 Ni Paulo anayeweka mikono yake juu ya Timotheo.

Mtawanyiko na utata unaonyesha kukosekana kwa mpangilio katika kanisa la karne ya kwanza. Kanisa la kwanza lilikuwa zaidi katika kuendelea na kubadilika badilika na mara zote likitumia karama na vipawa vya roho vya waamini (kama vile Wakorintho 12; 14). Agano Jipya kwa ufupi tu limeandikwa kutetea au kushusha mfano wa serikali (Angalia mtawanyiko huu katika Mdo. 15) au taratibu za kuwekwa wakfu. Mpangilio wa desturi za kikanisa ni muhimu lakini sio kibiblia. The Uuungu wa uongozi ni zaidi kiumuhimu kuliko mfumo ya uongozi (yaani dola).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 6:7**

<sup>7</sup>Neno la Mungu likaenea; na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana katika Yerusalemu; jamii kubwa ya makuhani wakaitii ile Imani.

**6:7 "Neno la Mungu"** Hii inamaanisha Injili ya Yesu Kristo. Maisha yake, kifo, ufufuo na mafundisho kuhusu Mungu yalitengeneza njia mpya ya kutazama Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-48). Yesu ni neno (Kama vile Yohana 1:1; 14:6). Ukristo ni mtu! Angalia kidokezo katika Mdo. 4:31.

▣ **"likazidi kuenea"** Vitenzi vyote vitatu katika Mdo. 6:7 viko katika njeo ya wakati usiotimilifu. Hii ni dhamira kuu katika Matendo ya Mitume. Neno la Mungu linakua kwa watu wakiamini katika Kristo na kufanyika kuwa sehemu

ya watu wapya wa agano la Mungu (kama vile Mdo. 6:7; 12:24; 19:20). Hii inaweza kuwa maelezo kwa ahadi za Mungu kwa Ibrahimu kuhusu kukua kiidadi kwa familia yake ambao wakifanyika watu wa agano la kale la Mungu (kama vile Mdo. 7:17; Mwanzo 17:4-8; 18:18; 28:3; 35:11).

▣ **"wengi wa wakuu wa mkuhani walikuwa watii kwa imani"** Hii ilikuwa ni sababu ya uongozi wa Kiyahudi (yaani Masadukayo) kutotulia kuhusu Ukristo. Wale waliojua Agano la Kale vizuri walikuwa wakishawishiwa kwamba Yesu Kristo wa Nazareti alikuwa kweli Masihi aliya ahidiwa. Mzunguko wa ndani wa dini ya Kiyahudi ulikuwa unabomoka! Maelezo ya Kimuhtasari ya ukuaji yanaweza yakawa ufunguo kwa muundo wa kitabu (kama vile Mdo. 9:31; 12:24; 16:5; 19:20; 28:31).

▣ **"imani"** Neno hili linaweza kuwa na visawe kadhaa vya upekee:

1. Katika usuli wa Agano la Kale "uaminifu" au "kuaminika"; hivyo linatumika katika kuweka kwetu imani katika uaminifu wa Mungu au kuamini katika uaminifu wa Mungu (Angalia Mada Maalum katika Mdo. 6:5)



2. kukubali kwetu au kupokea zawadi ya bure ya Mungu ya msamaha katika Kristo
3. kuishi kimungu na kwa uaminifu
4. namna ya jumla ya imani ya kikristo au ukweli wa kimafundisho kuhusu Yesu (kama vile Warumi 1:5; Gal. 1:23; na Yuda 3 & 20). Katika vifungu kadhaa kama vile 2 The. 3:2, ni ngumu kujua jambo gani ambalo Paulo alikuwa nalo katika ufahamu.

Angalia **MADA MAALUM: AMINI, SADIKI, IMANI NA UAMINIFU KATIKA AGANO LA KALE (ἰμᾶ Believe, Trust (noun, verb, adjective)** katika Mdo. 3:16.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 6:8-15**

<sup>8</sup> Na Stefano, akijaa neema na uwezo, alikuwa akifanya maajabu na ishara kubwa katika watu. <sup>9</sup> Lakini baadhi ya watu wa sinagogi lililoitwa sinagogi la Mahuru, na la Wakirene, na la Waiskanderia, na la wale wa Kilikia na Asia, wakaondoka na kujadiliana na Stefano; <sup>10</sup> lakini hawakuweza kushindana na hiyo hekima na huyo Roho aliyesema naye. <sup>11</sup> Hata wakashawishi watu waliosema, Tumemsikia mtu huyu akinena maneno ya kumtukana Musa na Mungu. <sup>12</sup> Wakawataharakisha watu na wazee na waandishi, wakamwendea, wakamkamata, wakampeleka mbele ya baraza. <sup>13</sup> Wakasimamisha mashahidi wa uongo waliosema, Mtu huyu haachi kusema maneno ya kufuru juu ya mahali hapa patakatifu na juu ya torati; <sup>14</sup> maana tumemsikia akisema kwamba Yesu huyo Mnazareti atapaharibu mahali hapa, na kuzibadili desturi tulizopewa na Musa. <sup>15</sup> Watu wote walioketi katika ile baraza wakamkazia macho yao, wakamwona uso wake kuwa kama uso wa malaika.

**6:8 "akijaa neema na nguvu"** "kujaa neema" kunamaanisha Baraka ya Mungu katika maisha na huduma. Angalia Mada Maalumu katika Mdo. 5:17. Neno "nguvu" linahusiana na tungo ya pili, "kufanya miujiza kikubwa na ishara."

▣ **"akitenda ishara kubwa na miujiza"** Hii ni njeo ya wakati usiotimilifu (kama Mdo. 6:7). Hii yawezekana ilitokea kabla ya maamuzi yake kama mmoja wa wale saba. Ujumbe wa Injili ya Stephano ilikuwa kwa mfululizo ikipendeshwa na utu wake (yaani kujaa imani) na nguvu (ishara na miujiza).

**6:9 "baadhi ya watu kutoka. . . wengine kutoka"** Kuna swali la juu ya namna gani mtu anaweza kufasiri vikundi vingapi viliinuka dhidi ya Stephano.

1. Sinagogi moja (wanaume kutoka nchi zote wanawekwa kwenye orodha)
2. masinagogi mawili
  - a. ya Wayahudi kutoka Kirene na Iskanderia
  - b. ya Wayahudi kutoka Kilikia na Asia (Paulo alikuwa akitoka Kilikia)
3. Sinagogi moja lakini nakundi mawili
4. Masinagogi matano tofauti tofauti

Kiambata cha Jinsi cha Kiyunani cha wingi cha ke (kiume) cha wingi (*tōn*) kinarudiwa mara mbili.

▣ **"kutoka katika kile kinachoitwa"** Sababu ya tungo hii "mtu huru" ni neno la Kilatini; hivyo ilitakiwa lifasiriwe vizuri. Kidhahiri Wayahudi hawa walikuwa wamepelekwa katika ardhi za nje kama watumwa (kijeshi au kiuchumi), lakini kwasasa walikuwa wameanza kurudi Palestina kama watu huru walioachiwa, lakini bado Kiyunani cha Koine ndiyo ilikuwa lugha yao ya kwanza

**6:10** Sio tu kwamba Injili ya Stephano ilitibitishwa kwa nguvu na ishara lakini kwa dhahiri ilikuwa na ushawishi wa kimaana. Mdo.7 ni mfano wa mahubiri yake.

▣ **"Roho"** Katika maandiko ya Kiyunani hakuna namna ya kutofautisha herufi kubwa; hivyo hii ni fasiri ya mfasiri. Herufi kubwa ya "R" inaweza maanisha Roho Mtakatifu, herufi ndogo ya "r" inamaanisha roho ya binadamu

(kidokezo cha matoleo ya KJV, NRSV, REB, kama vile Mdo. 7:59; 17:16; 18:25; Warumi 1:9; 8:16; 1 Kor. 2:11; 5:4; 16:18; 2 Kor. 2:13; 7:13; 12:18; Gal. 6:18; Flp. 4:23). Haya yanaweza kuwa maelezo ya Mithali. 20:27.

Angalia [MADA MAALUM: ROHO \(PNEUMA\) NDANI YA AGANO JIPYA](#) katika Mdo. 2:2.

**6:11 "kwa siri wakawarubuni watu waseme"** Neno "kurubuni" linaweza kumaanisha (1) kutoa rushwa (kama vile Louw Nida, *Lexicon*, vol. 1, kurasa 577-578) au (2) kufanya mbinu za siri (kama vile Bauer, Arndt, Gingrich, na Danker, *A Greek-English Lexicon*, ukurasa 843). Hii ni mbinu ileile inayotumika dhidi ya Yesu (kama vile Mt. 26:61) na Paulo (kama vile Mdo. 21:28). Mashitaka yao yalikuwa ni uvunjaji wa Kutoka 20:7, ambayo adhabu yake ilikuwa ni hukumu ya kifo.

▣ **"Tumemsikia akinena habari za maneno ya kufuru dhidi ya Musa"** Mahubiri ya Stephano katika Matendo 7 yanajibu mashitaka haya. Iwapo Mdo. 7 ilikuwa mahubiri ya injili ya Stepshno au mahubiri maalum yaliyomaanisha kujibu mashitaka haya hayana uhakika, lakini Yawezekana Stephano alitumia Agano la Kale mara kwa mara kuelezea U-Masihi wa Yesu.

▣ **"na dhidi ya Mungu"** Wayahudi haya walimuweka Mungu baada ya Musa! Muundo wa sentensi zao zilifunua tatizo la kimtazamo. Sheria ya Musa ilikuwa ni kilele.

**6:12 "wazee na waandishi.....Baraza"** Tungo "wazee na waandishi" mara kwa mara linaelezwa kwa kifupi kwa ajili ya wajumbe wa Baraza la wakuu wa Sinagogi, ambalo linamaanishwa kwa muktadha huu kama "Baraza." Ilikuwa ni mamlaka ya kidini ya taifa la Kiyahudi katika kipindi cha Warumi kabla ya miaka ya 70 b.k. Ilikuwa linaundwa na

1. Kuhani Mkuu(s) na familia yake
2. wamiliki wa ardhi matajiri na viongozi wa umma
3. waandishi wa mahali pamoja

Ilikuwa na jumla ya viongozi sabini kutoka katika eneo la Yerusalemu. Angalia Mada Maalum: Wakuu wa baraza la Sinagogi katika Mdo. 4:5.

**6:13 "mtu huyu"** Hii ni namna ya kebehi ya kuonesha hali ya kutoridhika. Tungo hii mara kwa mara inatumika juu ya Yesu.

▣ **"akizungumza dhidi ya mahali hapa patakatifu na sheria"** Tungo hii ni mwendelezo wa mashitaka ya Mdo. 6:11. Hii inaweza kumaanisha ukiri wa maneno ya Yesu kuhusu kuharibiwa kwa hekalu kulikowekwa katika kumbukumbu katika Luka 19:44-48 (pia Marko 13:2), au vitisho vya Yesu katika Mt. 26:61; 27:40; Marko 14:58; 15:29; Yohana 2:19 (kama vile Mdo. 6:14). Yesu alijiona mwenyewe kama "Hekalu Jipya," kituo kipya za ibada, mahali pa upya pa kukutanika katika ya Mungu na wanadamu (kama vile Marko 8:31; 9:31; 10:34). Hukumu ya Mungu ilikuwa inakuja katika jengo la Herode.

Mahubiri ya Stephano kuhusu msamaha kamili kupitia Yesu yawezekana yalikuwa na chanzo cha "kuzungumza dhidi ya sheria." Ujumbe wa Injili unapunguza "agano la Musa" kuwa ushuhuda wa kihistoria badala ya njia ya wokovu (kama vile Wagalatia 3 na kitabu cha Agano Jipya cha Waebrania).

Kwa maana Wayahudi wa karne ya kwanza wakikuwa na mafundisho ya kimsimamo, kukufuru! Hii kweli inatoka nje ya uelewa wa Agano la Kale wa Mungu mmoja, wokovu na sehemu ya kipekee ya Israeli. Agano Jipya lina Shabaha isiyopitiwa pitiwa (yaani Yesu na sio Israeli, neema na sio vigezo vya kibinadamu).

**6:14** Katika namna ambayo mashitaka haya yalikuwa ya kweli! Mashitaka haya mawili yalikuwa yanalenga kuwachochea wote Masadukayo (yaani, "kuharibu sehemu hii") na Mafarisayo (yaani "kubadili desturi ambazo Musa alizirithisha").

▣ **"huyu Yesu Mnazareti"** Angalia Mada Maalumu katika Mdo. 2:22.

**6:15 "Wakamkazia macho"** Hii ni mbinu ya kifasihi ambayo mara kwa mara inatumiwa na Luka. Inaashiria umakini ambao hauingiliwi na kizuizi wala usumbufu (kama vile Luka 4:20; 22:56; Mdo 1:10; 3:4,12; 6:15; 7:55; 10:4; 11:6; 13:9; 14:9; 23:1).

▣"**sura yake kama sura ya malaika**" Hii inaweza kuwa sawa na

1. Sura ya Musaa kug'aa baada ya kutembelewa na YHWH (kama vile Kutoka 34:29-35, 2 Kor. 3:7)
2. Sura ya Yesu na mwili kug'aa wakati wa kugeuzwa kwake (kama vile Mt. 17:2; Luka 9:29)
3. Mjumbe wa malaika wa Danieli 10:5-6

Hii ni njia ya kisitiari ya kuashiria mtu ambaye amekuwa mbele za Mungu

### **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembe katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini kanisa la kwanza lilichagua watu walio bora ili kuhudumia wahitaji?
2. Kwanini kunakuwa na mgogoro katika ukuaji wa haraka?
3. Nini kusudi la kuwekea mikono?
4. Kwanini Stephano alivamiwa/alishambuliwa?

## MATENDO YA MITUME 7

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFASIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Hotuba za Stefano	Maelekezo ya Stefano: wito wa Ibrahim	Mafundisho na kuuwawa kwa Stefano (6:8-8:1a)	Hotuba ya Stefano	Hotuba ya Stefano
7:1-8	7:1-8		7:1 7:2-8	7:1-8
	Wazee wa familia huko Misri	7:2b-8		
7:9-16	7:9-16	7:9-16	7:9-16	7:9-16
7:17-22	7:17-36	7:17-22	7:17-22	7:17-22
7:23-29		7:23-29	7:23-29	7:23-29
7:30-43		7:30-34	7:30-34	7:30-34
	Israel wanamwasi Mungu	7:35-43	7:35-38	7:35-43
	7:37-43			
	Hekalu la Mungu		7:39-43	
7:44-50	7:44-50	7:44-50	7:44-47	7:44-50
	Israel inampinga Roho Mtakatifu		7:48-50	
7:51-53	7:51-53	7:51-53	7:51-53	7:51-53
Kupigwa mawe kwa Stefano	Stefano anauawa		Kupigwa mawe kwa Stefano	Kupigwa mawe kwa Stefano, Sauli ndiye mtesaji
7:54-8:1a	7:54-60	7:54-8:1a	7:54-8:1a	7:54-8:1

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" \("A Guide to Good Bible Reading"\)](#))

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

#### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Kauli ya Stefano katika Matendo 7 ndio iliyo ndefu kuandikwa katika kitabu cha Matendo. Inaondoa mitazamo ya kithiolojia kwa ajili ya uelewa wa Paulo (pamoja na kanisa) wa uhusiano wa injili kwenye agano la kale. Hotuba ya Stefano inajibu shutuma zote zilizotengenezwa dhidi yake, kuonyesha kuwa

1. Mungu alitenda nje ya hekalu

2. Mungu anafanya kazi na watu wa mataifa
  3. Wayahudi muda wote walikataa ujumbe wa Mungu, wajumbe wake na sasa wamemkataa Masihi!
- B. Utetezi wa Stefano uliathiri moyo wa Sauli wa Tarso na thiolojia ya Paulo
- C. Stefano anadhihiliwa mwendelezo wa kutokuwepo na uaminifu wa agano kwa Wayahudi na mafunuo ya Mungu nje ya ahadi ya nchi walioahidiwa na mbali na hekalu la Yerusalem, ambalo limekuwa mtazamo wa karne ya kwanza ya ibada ya Kiyahudi.
- D. Wayahudi mara nyingi wamewakataa wale waliosema kwa niaba ya Mungu na sasa wamefanya tena kile kile. Wameendelea kwa ukali kumkataa Yesu wa Nazareti na walikaribia kwa ukali kuukataa ushuhuda wa Stefano.
- E. Stefano anahukumiwa na kikundi kile kile kwa matusi yale yale kama aliyotukanwa Yesu. Alipokuwa akipigwa mawe Stefano alisema vitu vingi akiiga maneno ya Yesu aliyoyasema pale masalabani. Je huu ulikuwa ni mpango wa kimakusudi wa kifasihi uliotumiwa na Luka? Inaonekana hivyo!
- F. Mtazamo wa Stefano juu ya uhusiano kati ya Wayahudi na Wakristo utatengeneza hatua kwa ajili ya mateso (k.v Mdo. 8:1-3) na mgawanyiko wa ndani wa haya makundi mawili. Yawezekana kuwa Mungu alimtumia Stefano, kama alivyofanya kwa Samson katika Agano la Kale, kuanzisha vita hatimaye kusababisha kuenea kwa ajili nje ya Palestina.
- G. Kauli /utetezi/hotuba ya Stefano ilikuwa na maelezo mbali mbali yanayokinzana na yale ya Kiebrania ya Agano la Kale (alinukuu toka kwenye tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani). Je wasomi wanajaribu kutetea semi za Stefano au kuziruhusu kuwa mila za Kiyahudi au hata makosa ya kihistoria? Swali hili linafunua jazba na upendeleo wa watafasiri wasomi. Naamini kuwa Biblia ni historia ya kweli, ambayo Wakristo husimama kwayo au huanguka kwenye matukio ya Biblia. Hata hivyo, mwanzo wa Biblia (yaani., Mwanzo 1:11) na mwisho wa Biblia (yaani., kitabu cha ufunuo) sio “historia yenyewe”! kwa ajili ya kuingilia kati nafikiria wako sawa. Hili linapelekea kuwajibika kuwa wakati mwingine kuna.
1. Tofauti ya kihesabu
  2. Tofauti ya kiuwasilishaji
  3. Tofauti ya maelezo
  4. Mbinu za utafasiri wa sheria za Kiyahudi (mf. Kuunganisha maandiko mawili au zaidi). Hili haliathiri uthibitisho wangu wa usahihi wa kihistoria au utegemeaji wa simulizi za kibiblia. Yawezekana Stefano aliwajibika tena kwa kile alichojifunza katika shule za Sinagogi au aliyabadilisha maandiko ili kuliwezesha kusudi lake. Kuachana na ujumbe wake kwa kuangalia juu ya maelezo moja au mawili inaonyesha maana yetu ya sasa ya uandishi wa historia na sio maana ya kihistoria ya karne ya kwanza.
- H. Maelezo ya kimsingi ya Stefano kihistoria yanaeleza namna Mungu anavyoshughulika na Israel katika Matendo 7
1. Wakuu wa kaya, Mdo. 7:2-16
  2. Kutoka kwa Waisrael Misri na kipindi cha kutangatanga jangwani, Mdo. 7:17-43
  3. Hema la kukutanikia na hekalu, Mdo. 7:44-50
  4. Matumizi ya muhtasari wa historia ya Agano la Kale kwao, Mdo. 7:51-53
- I. Stefano anatumia kumbukumbu mbalimbali za Agano la Kale (nukuu na vidokezo)
1. Mdo. 7:3 – Mwa. 1 2:1
  2. Mdo. 7:5 – Mwa. 1 2:7 au 1 7:8
  3. Mdo. 7:6-7a – Mwa. 1 5:1 3-1 4
  4. Mdo. 7:7b – Kut. 3:1 2
  5. Mdo. 7:8a – Mwa. 1 7:9-1 4
  6. Mdo. 7:8b – Mwa. 21 :2-4
  7. Mdo. 7:8c – Mwa. 25:26
  8. Mdo. 7:8d – Mwa. 35:22-26
  9. Mdo. 7:9 – Mwa. 37:1 0,28; 45:4
  10. Mdo. 7:1 0 –Mwa. 39:21 ; 41 :40-46
  11. Mdo. 7:1 1 –Mwa. 41 :54-55; 42:5
  12. Mdo. 7:1 2 – Mwa. 42:2

13. Mdo. 7:1 3 –Mwa. 45:1 -4
14. Mdo. 7:1 4 – Mwa. 45:9-1 0
15. Mdo. 7:1 5 – Mwa. 46:5; 49:33; Kut. 1 :6
16. Mdo. 7:1 6 – Mwa. 23:1 6; 50:1 3
17. Mdo. 7:1 7 – Kut. 1 :7-8
18. Mdo. 7:1 8 – Kut. 1 :8
19. Mdo. 7:1 9 – Kut. 1 :1 0-1 1
20. Mdo. 7:20 – Kut. 2:2
21. Mdo. 7:21 – Kut. 2:5,6,1 0
22. Mdo. 7:22 – Kut. 2:1 0
23. Mdo. 7:23 – Kut. 2:1 1 -1 2
24. Mdo. 7:26 – Kut. 2:1 3
25. Mdo. 7:27-28 –Kut. 2:1 4
26. Mdo. 7:30 – Kut. 3:1 -2
27. Mdo. 7:29a –Kut. 2:1 5
28. Mdo. 7:29b – Kut. 2:22; 4:20; 1 8:3-4
29. Mdo. 7:32 – Kut. 3:6
30. Mdo. 7:33-34 – Kut. 3:5,7-1 0
31. Mdo. 7:36 – Kut. 1 2:41 ; 33:1
32. Mdo. 7:37 – Kumb. 1 8:1 5
33. Mdo. 7:38 – Kut. 1 9:1 7
34. Mdo. 7:39 – Hes. 1 4:3-4
35. Mdo. 7:40 – Kut. 32:1 ,23
36. Mdo. 7:41 – Kut. 32:4,6
37. Mdo. 7:42-43 – Amos 5:25-27
38. Mdo. 7:44 – Kut. 25:31 ,36-40
39. Mdo. 7:45 –Yos. 3:1 4 na kuendelea; 1 8:1 ; 23:9
40. Mdo. 7:46 – 2 Sam. 7:8 na kuendelea
41. Mdo. 7:47 – 1 Falm 6-8; 2 Nya. 1 -6
42. Mdo. 7:49-50 –Isa. 66:1 -2

Muhtasari mwingine mzuri wa kimaandiko wa historia ya Israel ni ule wa Nehemia 9.

1. Neh. 9:6 – Mwanzo 1 -1 1
2. Neh. 9:7-8 – Mwanzo 1 2-50
3. Neh. 9:9-1 4 – Kutoka (Waisrael kutoka Misri)
4. Neh. 9:1 5-21 – Hesabu (kipindi cha kutangatanga jangwani)
5. Neh. 9:22-25 – YOSHUA (ushindi)
6. Neh. 9:26-31 – Waamuzi
7. Neh. 9:32-38 – Samuel, Wafalme, Nyakati (ufalme)

## KIFUNGU CHA NENO NA USOMAJI WA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 7:1-8

<sup>1</sup> Kuhani Mkuu akasema, Je! Mambo hayo ndivyo yalivyo? <sup>2</sup> Naye akasema, Ndugu zangu na baba zangu, sikilizeni: Mungu wa utukufu alimtokea baba yetu Ibrahimu, alipokuwa katika Mesopotamia, kabla hajakaa Harani, <sup>3</sup> akamwambia, Toka katika nchi yako na katika jamaa zako, ukaende hata nchi nitakayokuonyesha. <sup>4</sup> Ndipo alipotoka katika nchi ya Wakaldayo, akakaa Harani, akatoka huko baada ya kufa babaye, Mungu akamhamisha mpaka nchi hii mnayokaa ninyi sasa. <sup>5</sup> Wala hakumpa urithi humu hata kiasi cha kuweka mguu; akaahidi kwamba atampa, iwe milki yake, na ya uzao wake baadaye alipokuwa hana mtoto. <sup>6</sup> Mungu akanena hivi, ya kwamba wazao wake watakuwa wageni katika nchi ya watu wengine, nao watawafanya kuwa

watumwa wao, na kuwatenda mabaya kwa muda wa miaka mia nne.<sup>7</sup> Na lile taifa watakaowafanya watumwa nitawahukumu mimi, alisema Mungu; na baada ya hayo watatoka, nao wataniabudu mahali hapa.<sup>8</sup> Akampa agano la tohara; basi Ibrahimu akamzaa Isaka, akamtahiri siku ya nane. Isaka akamzaa Yakobo. Yakobo akawazaa wale kumi na wawili, wazee wetu.

**7:1 "Kuhani mkuu"** Huyu alikuwa Kayafa. Angalia maelezo katika Mdo. 4:6

**7:2 "Akasema"** Utetezi wa Stefano unafanana na ule ulioko kwenye kitabu cha Waebrania. Aliyajibu mashitaka kwa njia mbili: (1) wayahudi waliendelea kumkataa Musa kipindi cha nyuma na (2) hekalu ilikuwa njia mojawapo ya Mungu kuongea na Waisrael. Hili lilikuwa ni jibu la moja kwa moja juu ya mashitaka yaliyoletwa dhidi yake katika Mdo. 6:13

▣ **"Sikilizeni"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu ya neno la Kiyunani *akouō*. Linatumika katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani kutafasiri mchezaji maarufu wa Kiyahudi, *Shema* (kama vile Kumb. 6:4-5). Pia linatumiwa na manabii kutazamisha maana ya kifungu "sikilizeni mkapate kujitetea" (kama vile Mika 1:2; 6:1). Ni vigumu kujulikana kwa kidokezo hiki cha kiufundi kilichokuwepo kipindi wanaume wa Kiyahudi walipoelezea fikra zao za Kiebrania katika maneno ya lugha ya Koine, lakini katika baadhi ya mazingira kama haya hili linaweza kuwa kweli.

▣ **"Mungu wa utukufu"** Huyu Mungu wa utukufu (kama vile. Zab. 29:3) alijitokeza kwa Mkuu wa familia Ibrahim (kama vile. Mwa. 1 2:1 ,1 5:1 ,4; 1 7:1 ; 1 8:1 , 22:1 ), hivyo basi, ukawa mwanzo wa Wayahudi. Angalia Mada Maalum katika Mdo. 3:13.

▣ **"Ibrahim"** Ibrahim alifikiliwa kuwa baba wa Wayahudi. Alikuwa ndiye mkuu wa familia wa kwanza. Wito wake na baadaye alivyo enenda na Mungu kumeelezewa katika Mwanzo 12:1-25:11. Katika Wagalatia 3 na baadaye Warumi 4 Paulo anamtumia kama kielelezo cha kuhesabiwa haki kwa njia ya imani.

▣ **"alipokuwa Mesopotamia kabla ya kuishi Haran"** Mwanzo 1 1 :31 inadokeza kuwa Ibrahim alikuwa katika Mji wa Harani kipindi Mungu anaongea naye. Ingawa, wakati Mungu anakutana na Ibrahim haukuelezewa vizuri. Ibrahim alikuwa katika Uru wa Wakaldayo (kama vile Mwanzo. 1 1 :28,31 ), lakini baadaye alikwenda Harani (kama vile Mwa. 1 1 :31 ,32; 29:4) akifuata amri ya Mungu. Hoja ni kuwa Mungu aliongea na Ibrahim nje ya nchi ya Kaanani. Ibrahim hakuwa akimiliki sehemu yeyote ya nchi takatifu (kama vile Mdo. 7:5) kipindi cha uhai wake (isipokuwa pango kwa ajili ya kuzikia ndugu zake, kama vile. Mwa. 23:9).

Neno "Mesopotamia" linaweza kurejelea kikundi cha utamaduni Fulani:

1. Kikundi Fulani cha watu walioko katika eneo la Tigris na Euphrates (yaani., "Syria katikati ya Mito")
2. Kikundi cha watu karibia na malango ya Tigris na Euphrates

**7:3 "toka katika nchi yako na katika jamaa zako, ukaende katika nchi nitakayo kuonyesha"** Hii ni nukuu toka Mwa. 12:1. Suala la kithiolojia linalohusika kwenye nukuu hii ni wakati Mungu anasema na Abram:

1. Kipindi alipokuwa katika Uru kabla hajawachukuwa Babaye Terah na Mpwa wake Lutu kuwapeleka Harani
2. Kipindi alipokuwa Harani na akasubiri mpaka pale baba yake alipokufa kumfuata Mungu kusini mwa Kaanani?

**7:4 "ndipo alipotoka katika nchi ya Wakaldayo"** Kaldayo (BDB 505) yawezakuwa ni jina la mji karibu na malango ya Mto Tigris na Euphrates (angalia maelezo katika Mdo. 7:2). Baadaye ikajakuwa ikirejelea kwenye taifa lililoanza hapo, lililojulikana kama Babel (BDB 93). Taifa hili pia lilizalisha wasomi wengi walioanzisha kanuni za kimahesabu zilizohusiana na mwenendo wa miangaza ya usiku (yaani., sayari, nyota, vimondo, n.k). Hiki kikundi cha mamajusi (yaani., wanajimu) pia walijulikana kwa jina la Wakaldayo (kama vile Dan. 2:2;4:7;5:7-11)

▣ **"Harani"** Harani (BDB 357) ni mji ambao Terah, Ibrahim, na Lutu (kama vile Mwa. 11:31-32). Ndugu wengine wa Ibrahim walikaa huko na sehemu yenyewe iliitwa kwa jina lake (yaani., mji wa Nahori, kama vile Mwa. 24:10; 27:43). Huu mji uliopo sehemu ya juu ya Mto Euphrates (yaani., kwenye kijito cha Mto Balikh) ulianzishwa katika karne ya 3 K.K. na umebaki na jina hilo hata leo. Kama maelezo yenye kufurahisha, nduguze Ibrahim, waliopo Haran (BDB 248), hawakuapizwa kwa Kiebrania kama ilivyo kawaida ya mji.

▣ **"baada ya baba yake kufariki"** Wengi wameona mkanganyiko uliopo kati ya Mwanzo. 11:26,32 na 12:4. Kiwastani kuna ufumbuzi wa aina mbili.

1. Yawezekana Ibrahim hakuwa kijana mkubwa, lakini alikuwa kijana maarufu (yaani., aliyetajwa kwanza)
2. Torati ya Wasamalia ikiwa na miaka ya Tera 145 hadi kufikia mauti yake, na sio miaka 205, kama maandishi ya Kiebrania yanavyosema. Angalia Gleason L. Archer, *Encyclopedia of Bible Difficulties*, p. 378.

**7:5 "akaahidi kwamba atampa, iwe milki yake, na ya uzao wake baadaye alipokuwa hana mtoto"** Hili ni dokezo la Mwanzo 12:7 au 17:8. Maelezo ya kithiolojia sio tu ahadi ya Mungu, bali imani ya Ibrahim katika Mungu ya kupewa kizazi na nchi. Imani hii imesisitizwa katika Mwa. 15:6 (kama vile Gal.3:6; Rum.4:3)

**7:6** Huu unabii uliotabiliwa umeelezwa katika Mwa. 15:132,14 na kuthibitishwa tena katika Kut. 3:12. Hata hivyo, Kut. 12:40 ina "miaka 430" badala ya "miaka 400." Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX) yanaitafasiri Kut. 12:40 kama "kukaa kwa wana wa Israel, kipindi wakikaa kwa muda katika nchi ya Misri na nchi ya Kaanani ni miaka 430." walimu wa dini ya Kiyahudi waliseama kwamba "miaka 400" ilianza na pale alipotolewa Isaka kama sadaka katika Mwanzo 22. John Calvin ameiita miaka 400 kama miaka ya ujumla. Yaweza kuhusiana na vizazi vinne vya miaka 100 kila kimoja (kama vile Mwa. 15:16).

**7:7 "Na lile taifa"** Hii ni nukuu toka kwenye tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani ya Mwa, 15:14. Hii haimaanishi kuwa ni upumbavu, bali ni maelezo ya ujumla. Dhahili taifa lenyewe lilikuwa ni Misri. Mataifa mengine, hata hivyo (yaani., Filistia, Shamu, Ashuru, Babel), wanalikuwa wakandamizaji wa Israel na Mungu atawahukumu pia

▣ **"na baada ya hayo"** Kifungu hiki kizima kimenukuliwa toka Kut. 3:12. Stefano aliongea kwa wazi historia nzima ya Israel. Andiko hili linaahidi kuwa Kaanani na Yerusalemu kwa upekee patakuwa ni mahali pa YHWH. Hili linaendana na msisitizo wa kitabu cha kumbu kumbu la torati.

▣ **"Wataniabudu mahali hapa"** Katika muktadha wa nukuu toka Kut. 3:12, hili linarejelea Mlima Sinai (angalia Mada Maalum katika Mdo. 7:30), ambao pia uko nje ya nchi ya ahadi na ni moja ya eneo la matukio muhimu kwa wana wa Israel (kipindi Musa akipewa sheria

**7:8 "Agano"** Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:47.

▣ **"Tohara"** Hili lilikuwa likitendeaka kwa majirani wote wa Israel, isipokuwa tu Wafilisti Tamaduni nyingi mara nyingi zilikuwa ni taratibu za kuapishwa kuelekea utu uzima, lakini sio kwa Waisrael, ambapo ulikuwa ni uanzishaji wa utaratibu ndani ya watu wa agano. Ilikuwa ni ishara ya uhusiano maalum wa imani na YHWH (kama vile Mwa. 17:9-14). Kila mkuu wa familia aliwatahiri wanae (yaani., alitenda kama kuhani kwa niaba ya familia yake). Robert Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, uk. 214, anasema utaratibu wa tohara unaohusiana na utaratibu wa umwagaji damu pakiwepo na kitendo cha kutahiri. Damu ilihushishwa na uunganishwaji wa agano (kama vile Mwa. 15:17), uvunjaji wa agano (kama vile Mwa. 2:17), na ukombozi wa agano (kama vile Isaya 53).

▣ **"wazee kumi na wawili"** Hii mara nyingi inamrejelea Ibrahim, Isaka, na Yakobo, lakini hapa inarejelea kwa watoto kumi na wawili wa Yakobo, ambao walikuja kuwa kabira za Israel.



**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 7:9-10**

<sup>9</sup> Wale wazee wetu wakimwonea wivu Yusufu, wakamwuzwa aende Misri. Mungu akawa pamoja naye, <sup>10</sup> akamtoa katika dhiki zake zote, akampa fadhili na hekima mbele ya Farao, mfalme wa Misri; naye akamfanya awe mtawala juu ya Misri na nyumba yake yote.

**7:9 "Yusufu"** Hadithi hii inapatikana katika Mwa. 37:1 1 ,28; 45:4. Stefano anajaribu kuonyesha kuwa Wayahudi na viongozi wao mara nyingi walimkataa kiongozi aliyechaguliwa na Mungu (kama vile Musa katika Mdo. 7:35).

**7:10** Maelezo haya yanapatikana katika Mwa. 39:21 ; 41 :40-46.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 7: 11-16**

**11** Basi kukawa njaa katika nchi yote ya Misri na Kanaani, na dhiki nyingi, wala baba zetu hawakupata chakula cha kuwatosha. **12** Hata Yakobo aliposikia ya kwamba huko Misri kuna nafaka, akawatuma baba zetu mara ya kwanza. **13** Hata safari ya pili Yusufu akajitambulisha kwa ndugu zake, jamaa ya Yusufu ikawa dhahiri kwa Farao. **14** Yusufu akatuma watu akamwita Yakobo babaye na jamaa zake wote pia, watu sabini na watano. **15** Basi Yakobo akashuka mpaka Misri; akafa yeye na baba zetu; **16** wakachukuliwa mpaka Shekemu wakazikwa katika kaburi lile, ambalo Ibrahimu alilinunua kwa kima cha fedha kwa wana wa Hamori, huko Shekemu

**7:11** Maelezo haya yanapatikana katika Mwa. 41 :54-55; 42:5.

**7:12** Maelezo haya yanapatikana katika Mwa. 42:4.

**7:13** Maelezo haya yanapatikana katika Mwa. 45:1 -4.

**7:14 "Ishirini na watano"** Hii inafuatisha tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani na machapisho ya magombo ya Bahari ya Chumvi, wakati andiko la ki-Masoreti lina "Sabini" (kama vile. Mwa. 46:27; Kut. 1 :5; Kumb. 1 0:22). Mwanzoni hili lilionekana kama tatizo la machapisho kati ya tafasiri ya kale ya maandiko ya Kiyunani, ambayo Stefano alinukuu, na andiko la Kiebrania la Kut. 1:5. Kwa mtazamo mwingine yaweza kuwa katika njia mbili za kuvihesabu vizazi vya Yakobo. Tatizo lililoibuka kati ya Mwa. 46:26 na 27:1. Maandiko ya ki-Masoreti ya mstari wa 27 inaorodhesha watoto wawili waliozaliwa Misri, wakati tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX) imeandika watoto Tisa, ambapo inamaanisha kuwa Efrahimu na Manase baadaye walipata watoto wengine kati yao wawili. Katika andiko la Kiebrania Yakobo na mkewe walihesabiwa, lakini wana wa ziada wa Efrahimu na Manase hawakuhesabiwa. Katika maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX) Yakobo na Mkewe hawakuhesabiwa, lakini watoto wa ziada wa Efrahim na Manase walihesabiwa. Wote wako sawa, lakini waliongeza vizazi katika njia tofauti na wakati tofauti katika maisha ya Yakobo. Maandiko ya Kiebrania yaliyojulikana kama magombo ya Bahari ya Chumvi pia yana "watu Sabini na Watano" katika Mwa. 46:27 na Kut. 1:5. Filo wa Iskandaria alikuwa akizijua hesabu zote. Sisi wote ni wawezeshaji wa udhamini wa leo linapokuja suala la ugumu wa maandiko au tatizo la hesabu kama hili. Kuna aina mpya ya vyanzo vya kibiblia vilivyopo siku hizi ambavyo vinalenga haya maandiko yenye utata. Ninapendekeza:

1. *Hard Sayings of the Bible*, IVP
2. *More Hard Sayings of the Bible*, IVP
3. *Encyclopedia of Bible Difficulties* by Gleason Archer.

Kwa majadiliano zaidi angalia Mdo. 7:1 4-1 5 angalia #1 kur. 521 -522.

**7:15** Maelezo haya yanapatikana katika Mwa. 4+6:5; Kut. 1:6.

**7:16 "mpaka Shekemu"** Kutokana na maelezo ya kitabu cha Mwanzo ya (1) mazishi ya Yusufu yaliyoandikwa katika Yos.24:32 na (2) mazishi ya Yakobo yaliyoandikwa katika Mwa. 50:13, panaonekana kuwepo na hitilafu katika mahubiri ya Stefano. Tatizo ni (1) Mji, unapaswa kuwa Hebron, na sio Shekem, au (2) Mkuu wa familia, anapaswa kuwa Yakobo, na sio Ibrahim. Ingawa, wote Ibrahim na Yakobo walinunua ardhi (kama vile. Mwa. 23:1 6; 33:1 9). Huko Hebron ndiko Sara na Ibrahim walizikwa (kama vile. Mwa. 23:1 9; 25:9), kama alivyokuwa kwa Rebeka na Isaka (kama vile. Mwa. 49:29-31 ) na Yakobo (kama vile. Mwa. 50:1 3). Ingawa haijulikani kuhusu sehemu alipozikwa kule Shekemu, yawezekana kuwa Ibrahim aliwahi nunua sehemu alipokuwa amekaa huko kwa muda katika Mwa. 12:6-7. Baadaye Yakobo akaikomboha hiyo sehemu ya ardhi (kama vile. Mwa. 33:1 9; Yos. 24:32). Hizi zaweza kuwa ni tetesi za wazi, lakini Stefano anaonekana mtu wa maarifa mengi juu ya historia ya Agano la Kale na hili lingalikuwa ndio njia ya suluhu kwenye maelezo mbali mbali.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 7: 17-29**

<sup>17</sup> Basi wakati wa ile ahadi ambayo Mungu alimpa Ibrahim ulipokuwa unakaribia, wale watu wakazidi na kuongezeka sana huko Misri, <sup>18</sup> hata mfalme mwingine akainuka juu ya Misri, asiyemfahamu Yusufu. <sup>19</sup> Huyu akawafanyia hila kabila yetu, na kuwatenda mabaya baba zetu, akiwaamuru wawatupe watoto wao wachanga, ili wasiishi. <sup>20</sup> Wakati huo akazaliwa Musa, naye alikuwa mzuri sana, akalelewa muda wa miezi mitatu katika nyumba ya babaye. <sup>21</sup> Hata alipotupwa, binti Farao akamtwa, akamlea awe kama mwanawe. <sup>22</sup> Musa akafundishwa hekima yote ya Wamisri, akawa hodari wa maneno na matendo. <sup>23</sup> Umri wake ulipopata kama miaka arobaini akaazimu moyoni mwake kwenda kuwatazama ndugu zake Waisraeli. <sup>24</sup> Akamwona mmoja akidhulumiwa, akamtetea, akamlipia kisasi yule aliyekuwa akionewa, akampiga huyo Mmisri. <sup>25</sup> Alidhani kwamba ndugu zake watafahamu ya kuwa Mungu anawapa wokovu kwa mkono wake, lakini hawakufahamu. <sup>26</sup> Siku ya pili yake akawatokea walipokuwa wakishindana, akataka kuwapatanisha, akisema, Enyi bwana zangu, ninyi ni ndugu. Mbona mnadhulumiana? <sup>27</sup> Lakini yeye aliyemdhulumu mwenziwe akamsukumia mbali, akisema, Ni nani aliyekuweka wewe kuwa mkuu na mwamuzi juu yetu? <sup>28</sup> Je! Wataka kuniua mimi kama ulivyomwua yule Mmisri jana? <sup>29</sup> Musa akakimbia kwa neno hilo, akakaa hali ya ugeni katika nchi ya Midiani, akazaa wana wawili huko.

**7:17** Hili lingaliweza kurejelea kwenye Mwa. 1 5:1 2-1 6 (ahadi) na Kut. 1 :7 (hesabu yao kubwa).

**7:18 "hata mfalme mwingine akainuka"** Hii ni nukuu toka Kut. 1 :8. Pamekuwepo na pameendelea kuwepo na mijadala kati ya wasomi juu ya tarehe ya kuondoka kwa wana wa Isarel kule Misri. Utambulisho wa huyu Mfalme wa Misri ulipatikana ukiwa na pingamizi. Mtu anaweza kumtambua yeye kama mfalme wa Misri toka kwenye utawala wa XVIII (Mwaka 1445 k.k) au toka utawala wa XIX (mwaka 1290 K.K). Nadharia iliopo ni kuhusianisha huyu Mfalme wa Misri na mtawala mzawa wa kwanza wa Misri aliyemwangusha aliyekuwa mtawala wa Misri wa kisemiti Hyksos. Hili lingaliweza kuelezea matumizi ya *heteros* katika Mdo. 7:1 8. Mzawa wa ki-Misri asingaliwapenda Wasemiti, kama ilivyo kwa Waebrania, kwa kiasi kikubwa katika eneo, wakihofia uvamizi mwingine kama wa Hyksos

#### **MADA MAALUM: TAREHE YA KUONDOKA KWA WAISRAEL KULE MISRI**

Pamekuwepo na maoni mbali mbali ya kisomi juu ya tarehe ya kutoka kwa Waisrael Misri.

- A. Kutoka 1 Falm 6:1, "miaka 480 toka kuondoka kwa Waisrael Misri hadi ujenzi wa hekalu la Sulemani"
  1. Suleimani alianza kutawala katika mwaka 970 K.K. Hii inahesabiwa kwa kutumia vita vya Qarqar vya mwaka 853 K.K kama tarehe ya mwanzo iliyojulikana
  2. Hekalu lilijengwa katika Mwaka wake wa nne (965 K.K), na kuondoka kwa Waisrael kulitokea yapata Mwaka 1445/6 K.K
  3. Hili linaonekana kutokea katika karne ya 18 wa utawala wa ki-Misri.
    - a. Yule Farao mkandamizaji angalikuwa ni Thutmose III (1490-1436 K.K)

- b. Yule Farao aliye sababisha Waisrael kuondoka Misri angalikuwa Amenhotep II (1436-1407 K.K)
    - 1) Wengine wanaamini ushahidi toka Yeriko uliosimamia kuwa hapakuwepo na mawasiliano ya kidiplomasia kati ya Yeriko na Misri wakati wa utawala wa Amenhotep III (1413-1377 K.K).
    - 2) Maandishi ya Amarna yanaweka kumbukumbu ya mawasiliano ya kidiplomasia yaliyoandika kwenye makombe kuhusu (Habiru) wachungaji waliokuwa wakihama hama na kuenea kote nchi ya Kanani katika utawala wa Amenhotep III. Kwa hiyo, kuondoka kwa Waisrael Misri kulitokea katika utawala wa Amenhotep II.
    - 3) Kipindi cha waamuzi hakikuwa kirefu kama karne ya 13 ndio tarehe ya Waisrael kuondoka Misri.
  4. Uwepo wa tatizo juu ya tarehe hizi
    - a. Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX) yana miaka 440, na sio 480.
    - b. Yawezekana kuwa miaka 480 ni uwakilisho wa vizazi 12 vyenye miaka 40 kila kimoja, kwa hiyo, ni hesabu ya ujumla.
    - c. Kuna vizazi kumi na viwili vya makuhani kati ya Aaron na Suleiman (kama vile 1 Nyakati 6), tena kumi na viwili toka Suleimani hadi hekalu la pili. Wayahudi, kama walivyo Wayunani, walihesabu vizazi kama Miaka arobaini. Kwa hiyo, kuna kipindi cha miaka 480 nyuma na mbele (uwakilishaji wa kutumia hesabu, kama vile uhesabuji tena wa tarehe za Waisrael kuondoka Misri na kushinda wa Bimson).
  5. Pia kuna maandiko matatu yaliyotaja tarehe hizi.
    - a. Mwanzo 15:13,16 (kama vile Mdo. 7:6), miaka 400 ya ukandamizwaji
    - b. Kutoka 12:40-41 (kama vile Gal. 3:17)
      - 1) MT (maandishi ya Kimasoretic)-Miaka 430 ya kuishi kwa muda huko Misri
      - 2) LXX (Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani)-Miaka 215 ya kuishi kwa muda huko Misri
    - c. Waamuzi 11:26-Miaka 300 kati ya siku ya Yeftha na kushinda kwake (inaunga mkono tarehe 1445)
    - d. Mdo. 13:19-Kuondoka Misri, kutangatanga jangwani, na kushinda-Miaka 450
  6. Mwandishi wa kitabu cha Wafalme alitumia nukuu maalum za kihistoria na hakuweka hesabu ya ujumla (Edwin Thiele, A Chronology of the Hebrew Kings, kur. 83-85)
- B. Ushahidi wa mfano toka elimukale inaonekana kuelekeza hadi tarehe za 1290 K.K. au karne ya 18 ya utawala wa ki-Misri
1. Yusufu aliweza kuwatembelea baba yake na Farao siku moja. Farao wa kwanza mzawa aliyeanza kuondoa Mji mkuu toka Thebes na kuurudisha Nile Delta, mahali palipoitwa Avaris/Soan/Tanis, ambao ulikuwa Mji wa kale ulioitwa Hyksos, ulikuwa Seti (1309-1290 K.K). Angalikuwa ni Farao wa ukandamizaji.
    - a. Inapendeza kuoanisha vipande vya habari kuhusu kutawala kwa Hyksos huko Misri.
      - 1) Mawe yaliyowekwa kwa ajili ya mipaka yamepatikana kipindi cha Ramese wa II kuadhimisha kupatikana Mji Mkuu wa Misri, Avaris mwanzoni mwa miaka 400 kipindi cha utawala wa Hyksos mwaka 1700 K.K
      - 2) Unabii wa Mwanzo 15:13 unaongelea juu ya miaka 400 ya ukandamizaji
    - b. Hii inadokeza kuwa kuja kwa Yeftha kwenye utawala kulikuwa chini ya Hyksos. Utawala mpya wa ki-Misri unarejelewa katika Kut. 1:8
  2. Hyksos, ni neno la ki-Misri linalomaanisha “watawala wan chi ngeni,” lilikuwa ni kundi la watawala wa kisemiti huko Misri, walioidhibiti Misri kipindi cha utawala karne ya 15 na 16 (1720-1570K.K). Baadhi wanaoanisha na kuingia kwa Yeftha kwenye utawala. Tukitoa mika 430 ya Kut. 12:40 toka kwenye miaka 1700K.K, tunapata miaka takribani 1290 K.K.
  3. Mtoto wa Seti I alikuwa Ramese II (1290-1224 k.k). jina hili limetajwa kama moja ya mji ulijengwa na watumwa wa Kiebrania, Kut. 1:11. Pia Wilaya hii katika Misri karibu na Goshen Inaitwa Ramese, Mwa.47:11. Avaris/Soan/Tanis ulijulikana kama “nyumba ya Ramese” toka mwaka 1300-1100K.K
  4. Thusmoses III alijulikana kama mjenzi mkuu, kama alivyokuwa Ramese II.
  5. Ramese II alikuwa na mabinti 47 walioishi sehemu mbali mbali.
  6. Elimukale inaonyesha kuwa mingi ya miji ya Kaanani iliyozungushiwa ukuta (Hazor, Debir, Lachish)

iliharibiwa na kujengwa tena yapata miaka ya 1250 K.K. Katika kuiruhusu miaka 38 ya kutangatanga jangwani, inaendana na tarehe za 1290K.K. Wana akiolojia wamepata ushahidi wa Israel kuwa kusini mwa Kaanani juu ya mawe ya kumbu kumbu yaliyowekwa kwa ajili ya mipaka wakati wa utawala wa mrithi wa Ramese, aitwaye Merneptah (1224-1214 K.K, kama vile mawe ya mipaka ya Merneptah, yaliyoandikwa 1220 K.K).

7. Edom na Moabu inaonekana kupata utambulisho wa nguvu wa kitaifa katika mwaka 1300 K.K. nchi hizi mbili hazikuwa zimeungana katika karne ya kumi na tano.
  8. Kitabu, Redating the Exodus and Conquest by John J. Bimson, kilichochapishwa na chuo kikuu cha Sheffield, 1978, wanabishana juu ya ushahidi wa elimukale kwa ajili ya tarehe.
- C. Pamekuwepo na nadharia ambayo inaweza onekana katika historia, iitwayo "Exodus Decoded," kinachodai kuwepo na njia ya moja kwa moja upande wa Kaskazini (yaani., "njia ya Wafilisti"), hata mapema yapata miaka ya 1445 K.K., katika kipindi cha Hyksos (yaani., "wachungaji wa kifalme," 1630-1523 K.K.)

**7:19** Maelezo haya yanapatikana katika Kut. 1 :1 Ona kuendelea.

**7:20 "Musa akazaliwa"** Maelezo haya yanapatikana katika Kitabu cha Kutoka 2.

▣ **"alikuwa wa kupendeka machoni pa Mungu"** Hii ni nahau ya Kiebrania juu ya uzuri wa Musa (kama vile. Kut. 2:2). Hata Yusufu alitoa maoni juu ya uzuri wa Musa (kama vile. *Antiq.* 2.9.6).

**7:21** Haya maelezo yanapatikana katika Kut. 2:5-6,1 0.

▣ **"alipokuwa ametupwa"** Hili ni neno la Kiyunani *ektithēmi*, linalomaanisha "kuweka wazi" (kama vile. Mdo. 7:1 9) au "kuweka nje." Wamisri waliwalazimsha Waebrania kuwatelekeza watoto wao wa kiume kuwaweka kwenye vitu vya asili na wanyama wa porini ili waweze kudhibiti idadi ya watu iliyokuwa ikikua kwa kasi.

**NASB, NKJV "Binti Farao akamtwaa"**

**NRSV, NJB "Binti Farao akamuasili"**

**TEV "Binti Mfalme akamuasili"**

Neno *anaireō* kiuhalisia linamaanisha "kuokotwa." Kwa wazi Musa "aliokotwa" kando ya Mto na kwa kitendo hicho, akawa mtoto aliye asiliwa na Binti Farao.

**7:22** Musa alikuwa na mafunzo mazuri ya kijeshi na kielimu aliyoyapata katika siku zake katika baraza la Farao.

▣ **"akawa hodari wa maneno na vitendo"** Hii yawezakuwa taarifa ya maisha ya baadaye ya Musa kwa sababu alipokabiliana na YHWH kwenye kichaka kilichokuwa kikiwaka moto alidai hawezi kuongea vizuri kwa sababu ya kigugumizi (kama vile. Kut. 4:1 0-1 7).

**7:23-24** Maelezo haya yapo katika Kut. 2:1 1 -1 2.

**7:23 "Umri wake ulipopata miaka Arobaini "** Nafikiri alikuwa D. L. Moody alisema maisha ya Musa yanaweza kugawanyika katika makundi matatu yenye arobaini:

1. Miaka arobaini ya kwanza alifikiri alikuwa mtu wa kiwango fulani (yaani., aliye elimika katika baraza la Farao)
2. Miaka arobaini ya pili alifikiri kuwa si mtu tena wa hadhi yeyote (yaani., alikimbilia katika nchi ya Midiani na kujifunza njia na uwanda wa jangwa la Sinai)
3. Miaka arobaini ya tatu alipata kile Mungu anaweza kumfanyia mtu asiye kitu (yaani., aliwaongoza watu wa Mungu kwenda kwenye nchi ya ahadi)

**7:25** Mstari huu ni mawazo ya Stefano (yumkini desturi za Kiyahudi); hayajaelezewa katika kitabu cha Kutoka.

**7:26-29** Maelezo haya yanapatikana katika kitabu cha Kut. 2:1 3-1 4.

**7:28** Swali linategemea jibu la “hapana.”

**7:29 "Musa akakimbia kwa neno hilo"** Maelezo haya yanapatikana katika Kut. 2:1 5,22. Hofu ya Musa ya mauaji ya Mmisri yanaonyesha kuwa Farao hakuwa upande wa Bintiye juu ya kumuasili mtoto. Hata hivyo, Ebr. 11:27 inaweka wazi

▣ **"akakaa hali ya ugeni katika nchi ya Midiani"** Mungu alimtokea Musa katika kichaka cha moto katika nchi ya Midiani (kama vile Kutoka 3-4) na kudhihilisha sheria zake kwa Musa katika Mlima Sinai katika nchi ya Midiani (kama vile Exodus 1 9-20), ambapo inaonyesha kuwa Mungu hakuzuilika wapi ajidhihilishe mwaneyewe. Msisitizo wa aina ile ile juu ya Mungu kujidhihilisha mwaneyewe mbali na hekaluni kule Yerusalem unaonekana katika Mdo. 7:36, 44, 48, na 53.

▣ **"akazaa wana wawili huko"** Maelezo haya yanapatikana katika Kut. 2:22; 4:20; 1 8:3-4.

#### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO 7:30-34

**30** Hata miaka arobaini ilipotimia, malaika wa Bwana akamtokea katika jangwa la mlima wa Sinai katika mwali wa moto, kijitini. **31** Musa alipouona, akastaajabia maono yale, na alipokaribia ili atazame, sauti ya Bwana ikamjia, **32** Mimi ni Mungu wa baba zako, Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Musa akatetemeka, asithubutu kutazama. **33** Bwana akamwambia, Vua viatu miguuni mwako, kwa maana mahali hapa unaposimama ni nchi takatifu. **34** Yakini nimeona mateso ya watu wangu waliomo Misri, nimesikia kuugua kwao, nami nimeshuka niwatoe. Basi sasa, nitakutuma mpaka Misri.

**7:30** Maelezo haya yanapatikana katika kitabu cha Kutoka, sura ya 3 na 4

▣ **"Malaika "** Katika andiko la Agano la Kale malaika huyu hakika alikuwa YHWH. Angalia maelezo kamili katika Mdo. 5:19. Tambua namna huyu malaika alivyoainishwa.

1. Kut.. 3:2, "malaika wa Bwana akamtokea katika miale ya moto"
2. Kut. 3:4, "na Bwana (yaani., YHWH) alipoona kuwa amegeuka ili atazame"
3. Kut.. 3:4, "Mungu (yaani., *Elohim*) akamwita toka katikati ya kile kijiti"

Angalia [MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU](#) katika Mdo 1 :6.

▣ **"Mlima Sinai"** Angalia Mada Maalum hapa chini.

#### MADA MAALUM: MAHALI ULIPO MLIMA SINAI

- A. Kama Musa alikuwa akiongea kiuhalisia na sio kimethali juu ya “safari ya siku tatu” alipokwenda kumwomba Farao (Kut. 3:18; 5:3; 8:27), huo haukuwa muda wa kutosha kwao kupata mahali pa kimila katika rasi ya kusini mwa Sinai. Kwa hiyo, wasomi wengine wanaelekeza huo Mlima kuwa karibu na chemic hemi za Kadesh-Barnea (angalia video kwenye idhaa ya Historia, “The Exodus Decoded”).
- B. Mahali pa kimila palipoitwa, “Jebel Musa,” katika nyika ya uovu, pana vitu vingi ndani yake.
  1. Uwanda mkubwa kabla ya Mlima
  2. Kumbukumbu la Torati 1:2 inasema ilikuwa yapata safari ya siku kumi na moja toka Mlima Sinai mpaka Kadesh-Barnea.
  3. Neno “Sinai” (BDB 696, KB 751) ni neno lisilo la Kiebrania. Laweza kuhusianishwa na nyika ya uovu, ambalo linarejelea kwenye vichaka vidogo vidogo vya mbugani. Neno la Kiebrania la la Mlima ni Horeb (yaani., nyika, BDB 352, cf. Kut. 3:1; 17:6; 33:6).
  4. Mlima Sinai pamekuwa ni mahali pa kimila tangu karne ya Nne B.K. Upo katika “nchi ya Wamidiani,” ambayo inajumuisha sehemu kubwa ya rasi ya Sinai na Arabia
  5. Inaonekana kuwa elimukale imethibitisha mahali penyewe pa baadhi ya miji iliyotajwa katika maelezo

ya Kitabu cha Kutoka (Elim, Dophkah, Rephidim) yanavyosema kuwa upande wa Magharibi mwa Rasi ya Sinai.

- C. Wayahudi kamwe hawakupenda eneo la kijografia la Mlima Sinai. Waliamini kuwa Mungu aliwapa sheria na utimilifu wa ahadi yake toka Mwa. 15:12-21. "ambapo" halikuwa tatizo na hawakukusudia kurejea kwenye eneo hili (yaani., hapakuwepo na hija ya mwaka)
- D. Eneo la kimila la Mlima Sinai halikuweza anzishwa mpaka kwenye hija ya Silvia, iliyoandikwa yapata mwaka 385-8 B.K (k.v F. F. Bruce, Commentary on the Book of the Acts, uk. 151.

Jina jingine lililotumika katika Agano la Kale mahali ambapo YHWH aliwapa "Amri Kumi" palikuwa "Horebu" (BDB 352, KB 350, cf. Kut. 3:1; 17:6; 33:6; Kumb. 1:2,6,19; 4:10,15; 5:2; 9:8; 18:16; 29:1; 1 Falm. 8:9; 19:8; 2 Nya. 5:10; Zab. 106:19; Mal 4:4). Asili hii yaweza kuhusiana na konsonanti tatu za Kiebrania inayomaanisha "mabaki," "ukiwa," au "hame" (BDB 352, KB 349). Inaonekana kuwa "Horebu" inarejelea mkusanyiko wa Milima na "Sinai" ni moja ya kilele chake.

**7:32** Maelezo haya yanapatikana katika Kut.3:6.

▣ "**Baba zako**" Katika matoleo yote ya andiko la Kiebrania na tafasiri ya Kiyunani (yaani., tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani) neno liko katika hali ya umoja. Katika uonekanaji sehemu nyingine wa kifungu ni hali ya wingi. Mungu alitambua baba yake Musa aliyekuwa mtumwa.

**7:33** Maelezo haya yanapatikana katika Kut. 3:5. Musa alikisogelea kile kijiti akikishangaa, na sio suala la kidini. Sababu hasa ya Musa kuvua viatu vyake haijulikani.

1. Huenda viatu vyake vilikuwa vichafu (yaani., vikiwa na mavi ya ng'ombe)
2. Kuvua viatu kwa Musa huenda ilikuwa ni ishara ya urafiki wa karibu.
3. Huenda ni utendaji wa kitamaduni wa wazee wa familia au ibada za watu wa Misri

**7:34** Maelezo haya yanapatikana katika Kut. 3:7. Kwangu mimi mstari huu ni wa muhimu kithiolojia kwa sababu hiyo: YHWH alisikia kilio chao, akayaona maumivu yao, na kutenda. Alishuka chini ili awasaidie, lakini tambua msaada wake uliathiliwa na njia za kibinadamu. Mungu akamtuma Musa ambaye hakuwa tayari. Mungu aliamua kushughulika na mwanadamu kupitia mwanadamu!

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):MATENDO 7:35-43**

<sup>35</sup> Musa huyo waliyemkataa, wakisema, Ni nani aliyekuweka kuwa mkuu na mwamuzi? Ndiye aliyetumwa na Mungu kuwa mkuu na mkombozi, kwa mkono wa yule malaika aliyemtokea katika kile kijiti. <sup>36</sup> Huyu ndiye aliyewatoa, akifanya ajabu na ishara katika nchi ya Misri, na katika bahari ya Shamu, na katika jangwa muda wa miaka arobaini. <sup>37</sup> Musa huyo ndiye aliyewaambia Waisraeli, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye. <sup>38</sup> Yeye ndiye aliyekuwa katika kanisa jangwani pamoja na yule malaika aliyesema naye katika mlima wa Sinai, tena pamoja na baba zetu; ndiye aliyepokea maneno ya uzima atupe sisi. <sup>39</sup> Mtu huyo baba zetu hawakutaka kumtii, bali wakamsukumia mbali, na kwa mioyo yao wakarejea Misri, <sup>40</sup> wakamwambia Haruni, Tufanyie miungu, watakaotutangulia; maana huyo Musa, aliyetutoa katika nchi ya Misri, hatujui lililompata. <sup>41</sup> Wakafanya ndama siku zile, wakaleta dhabihu kwa sanamu ile, wakafurahia kazi za mikono yao. <sup>42</sup> Basi Mungu akaghairi, akawaacha ili waliabudu jeshi la mbinguni, kama ilivyoandikwa katika chuo cha manabii, Je! Mlinitolea mimi dhabihu na sadaka Miaka arobaini katika jangwa, enyi nyumba ya Israeli? <sup>43</sup> Nanyi mlíchukua hema ya Moleki, Na nyota za mungu wenu Refani, Sanamu mlizozifanya ili kuziabudu; Nami nitawafahamisha mwende mbali kupita Babeli.

**7:35 "Musa huyu waliyemkataa"** Mara nyingi watu wa Mungu huwakataa wasemaji wa Mungu (kama vile Mdo.7:51 -52). Hii hata yawezakuwa kusudi la Mdo. 7:27!

▣ "**kwa mkono wa yule malaika aliyemtokea katika kile kijiti**" Tena Mungu alikuja kwa wana wa Israel nje ya nchi ya ahadi. Kazi ya Mungu haikuwa na mipaka ya sehemu yeyote ile. Historia nyingi ya Waisrael ilitokea nje ya Kaanani na kabla ya hekalu huko Yerusalem. Kutokana na historia ya wana wa Israel viongozi wa Mungu walikataliwa na wenza wao (kama vile. Mdo. 7:9,27-28,35,39). Hii ni dhamira inayojirudia. malaika huyu alielezwa kama mwenye Uungu (kama vile. Kut. 3:2,4). Huu udhahili wa ki-Mungu wa dhahili pia unaweza kuonekana katika Mwa.1 6:7-1 3; 22:1 1 -1 5; 31 :1 1 ,1 3; 48:1 5-1 6; Kut. 1 3:21 ; 1 4:1 9; Waamuzi. 2:1 ; 6:22-23; 1 3:3-22; Zak. 3:1 -2.hata hivyo, lazima ikubalike kwamba "malaika wa Bwana" sio mara zote ajidhahilishe katika mwili wa ki-Ungu; wakati mwingine ni malaika aliyetumwa , (kama vile Mwa. 24:7,40; Kut. 23:20-23; 32:34; Hes. 22:22; Amu.5:23; 2 Sam. 24:1 6; 1 Nya. 21 :1 5na kuendelea; Zak. 1 :1 1 ; 1 2-1 3).

**7:36** Hii kiufupi ni miujiza ya nguvu ya Mungu (yaani., fimbo ya Musa) kupitia Musa na Haruni.

**7:37-38** Hii ni nukuu ya ki-Masihi toka Kumb.1 8:1 5. Stefano anautambua uwepo wa Mungu kipindi cha Waisrael wakitoka nchi ya Misri na kipindi cha kutangatanga jangwani kama ilivyo kote malaika wa Mungu na mrithi wa Mungu kwa Musa (yaani., Masihi, nabii). Stefano hamdharau Musa, bali kiukweli anamsikiliza Musa!

**7:38 "akiwa katika kusanyiko"** Hili ni neno la Kiyunani *ekklesia*, lakini linatumika kwa maana ya kusanyiko, na sio kanisa. Angalia Mada Maalum: Kanisa katika Mdo.5:1 1 .

▣ "**malaika aliyesema naye katika Mlima Sinai**" Thiolojia ya sheria ya Kiyahudi inadai kuwa malaika walikuwa wapatanishi kati ya YHWH na kipindi cha kupeana sheria (angalia maelezo katika Mdo.7:53). Pia yawezekana kuwa malaika anarejelea kwa YHWH mwenyewe (kama vile Kut. 3:21 ukilinganisha na 14:1 9; na pia Kut. 32:34; Hes. 20:1 6; Amu. 2:1 ).

**7:39 "baba zetu hawakutaka kumtii"** Stefano anaunganisha alama za uasi wa Agano la Kale. Uainishaji wake ni kuwa Wayahudi mara zote waliwakataa viongozi wa Mungu, na sasa wamemkataa Masihi.

▣ "**wakamsukumia mbali** " Maelezo haya yanapatikana katika Hes.14:3-4.

**7:40-41** Maelezo haya yanapatikana kwenye Kutoka 32. Hii haikuwa ibada ya sanamu, bali uumbaji wa sura ya Mungu. Baadaye ikajakuwa ibada ya kuzaa matunda.

**7:41** Stefano anatafasiri yule ndama wa dhahabu kama kinyago na kulitumia hili tukio la kihistoria kuleta nukuu toka Amosi 5, ambayo inaidokeza Israel, hata nyuma kabisa kipindi Waisrael wakitoka Misri na kipindi kile cha kutangatnga jangwani, ilikuwa ni ibada ya sanamu na uasi.

**7:42 "Bwana akaghairi, akawaacha"** Mstari wa 42 na 43 ni nukuu toka kwa Amosi 5:25-27 wakati Amosi anadai kuwa Israel mara zote walikuwa wakitoa dhabihu kwa miungu wa kigeni. Ilikuwa kawaida na mapema, kuweza kuelezea historia yao (kama vile Yos. 24:20). Hii inakumbushia moja ya maelezo ya nguvu ya upingaji katika Rum.1 :24,26,28.

▣ "**waliabudu jeshi la Mbinguni**" Hii inairejelea ibada ya kuabudu nyota ya Waashuru na Babel (kama vile Kumb. 1 7:3, maandiko ya Kiebrania, (MT) Amos 5:25-27, maandiko ya Kiyunani (LXX). Stefano:

1. Jina la mungu nyota. Maandiko ya ki-Masoreti yana *kywn* au *kaiwann*, jina la ki-Ashuru kwa ajili ya sayari ya Zohali. Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX) yana *rypn* au *raiphan*, ambalo lawezakuwa *repa*, jina la ki-Misri kwa ajili ya mungu wa sayari ya Zohali.
2. Maandiko ya Kiebrania (MT) na maandiko ya Kiyunani (LXX) yana "ng'ambo ya Dameski," wakati Stefano ananukuu "ng'ambo ya Babel." haijulikani kama kuna machapisho ya Amosi yenye kuwa na utafasiri. Stefano yawezakuwa aliongelea, pamoja na Wababeli waliokimbilia uhamishoni huko Yuda, lakini wakibadilishana eneo la uhamishoni. Ibadu ya miungu ya nyota ilianza huko Mesopotamia, lakini ikaja kuenea mpaka Shamu na Kaanani (kama vile Ayu.31 :26,27).Uvumbuzi wa elimukale katika Tell El-Amarna,

unaojumuisha mamia ya nyaraka toka Kaanani kwenda Misri katika karne ya 14 K.K pia walitumia hii miungu nyota kama jina la mahali.

▣ **"katika chuo cha manabii"** Hili linarejelea kwenye magombo yaliyo na manabii wadogo kumi na wawili (kama vile Mdo. 1 3:40). Nukuu katika Mdo. 7:42-43 ni kutoka tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani toka Amos 5:25-27. Kifungu kinachofuata katika Mdo. 7:42 ni swali linalotarajia jibu la "hapana."

**7:43 "Moleki"** Konsonanti za Kiebrania kwa ajili ya neno Mfalme ni *mlk* (BDB 574). Kuna miungu mbali mbali ya ki-Kaanani ambayo majina yake yanahusiana na konsonanti hizi, *Milcom*, *Molech*, au *Moloch*. *Moloch* ambayo ilikuwa ni miungu ya mavuno ya Waamori ambayo watoto walikabidhiwa kwayo kwa ajili ya kuhakikisha afya na ustawi kwenye jamii au taifa (kama vile. Law. 20:2-5; Kumb. 1 2:31 ; 1 Fal. 1 1 :5,7,33; 2 Fal. 23:1 0,1 3,1 4; Yer. 7:31 ;32:35). A. T. Robertson, *Word Pictures In the New Testament*, juzuu ya. 3, uk. 93, anasema *Moloch* alikuwa "ni sanamu ya kichwa cha dume la ng'ombe yenye miguu ilionyoochwahwa mahali ambapo watoto waliwekwa ikiwa na shimo chini yake kwa ajili ya kuwasha moto chini yake." Maafikiano yamesababisha baadhi ya wasomi kufikiri kuwa watoto hawakutolewa kama dhabihu kwa Moleki, bali waliwekwa wakfu kwake kama makahaba wa hekaluni, wa kiume na kike. Wazo lenyewe linafaa katika utendaji wa pamoja wa ibada ya mavuno.

▣ **"sanamu"** angalia mada maalum ifuatayo.

## MADA MAALUM: MTINDO (TUPOS)

Neno *tupos* lina elimu-maana pana.

1. Moulton and Milligan, *The Vocabulary of the Greek New Testament*, uk. 645
  - a. Sampuli
  - b. mpango
  - c. Mtindo au namna ya kuandika
  - d. Amri ya serikali ama agizo litolewalo na mtawala
  - e. Sentensi ama uamuzi
  - f. Mfano wa mwili wa binadamu kama sadaka ya kuondoa nadhiri kwa Mungu anayeponya
  - g. Kitenzi kilichotumika kwa maana ya kuongeza agizo au mwongozo wa sheria
2. Louw and Nida, *Greek-English Lexicon*, juzuu. 2, uk. 249
  - a. Kovu (kama vile. Yohana 20:25)
  - b. Sura (kama vile. Matendo 7:43)
  - c. Fanya kwa mfano (kama vile. Hebr. 8:5)
  - d. Mfano (kama vile. 1 Kor. 10:6; Flp. 3:17)
  - e. Umboasili (kama vile. Rum. 5:14)
  - f. Aina (kama vile. Matendo 23:25)
  - g. Maudhui (kama vile. Matendo 23:25)
3. Harold K. Moulton, *The Analytical Greek Lexicon Revised*, p. 411
  - a. Kipigo, chapa, alama (kama vile. Yohana 20:25)
  - b. Eleza kinaganaga
  - c. Sanamu (kama vile. Matendo 7:43)
  - d. Kanuni, mpango (kama vile. Rum. 6:17)
  - e. Muundo, kusudi (kama vile. Matendo 23:25)
  - f. Umbo, enye kufanana na kitu kingine (kama vile. 1 Kor. 10:6)
  - g. Umbo tarajiwa, aina (kama vile. Rum. 5:14; 1 Kor. 10:11)
  - h. Sampuli mfano (kama vile. Matendo 7:44; Hebr. 8:5)
  - i. Mfano adilifu (kama vile. Flp. 3:17; 1 The. 1:7; 2 The. 3:9; 1 Tim. 4:12; 1 Pet. 5:3)



Kumbuka, msamiati hauweki maana; ni matumizi tu ya maneno kwenye sentensi/aya ndiyo yanaweka maana (yaani, muktadha). Kuwa mwangalifu kugawanya rasmi kundi la fafanuzi kwa neno na kulitumia kila mahali neno hilo linapotumika katika Biblia, muktadha huamua maana!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 7:44-50**

<sup>44</sup> Ile hema ya ushahidi ilikuwa pamoja na baba zetu jangwani, kama alivyoagiza yeye aliyesema na Musa, ya kwamba aifanye sawasawa na mfano ule aliouona; <sup>45</sup> ambayo baba zetu, kwa kupokezana, wakaiingiza pamoja na Yohana katika milki ya Mataifa wale, ambao Mungu aliwafukuza mbele ya baba zetu, mpaka siku za Daudi; <sup>46</sup> aliyepata fadhili mbele za Mungu, naye aliomba ampatie Mungu wa Yakobo maskani. <sup>47</sup> Lakini Sulemani alimjengea nyumba. <sup>48</sup> Ila Yeye aliye juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono, kama vile asemavyo nabii, <sup>49</sup> Mbingu ni kiti changu cha enzi, Na nchi ni pa kuwekea miguu yangu; Ni nyumba gani mtakayonijengea? Asema Bwana, <sup>50</sup> Au ni mahali gani nitakapostarehe? Si mkono wangu uliofanya haya yote?

**7:44** Maelezo haya yanapatikana katika kitabu cha Kutoka, vifungu vya 25-31; 36-40. Mipango kamili ya hema la kukutania ilitambuliwa kwa Musa juu ya Mlima Sinai. Kitabu cha Agano Jipya cha Waebrania kinazungumza kuhusu hema la Mbinguni au madhabahu. (kama vile Mdo. 8:5-6; 9:1 1 ,23) ambayo ile iliyoko duniani ni mfano wake. Kama Stefano alivyoshughulikia kipindi cha nyuma katika sura hii maagizo ya sura ya 6 yaliyokuwa kinyume na Musa (kama vile Mdo. 6:1 1 ), sasa anaanza kushughulika na maagizo ya pili kuwa alikuwa kinyume na hekalu (kama vile. Mdo. 6:1 3).

▣ "**Ile hema**" Angalia Mada Maalum katika Mdo.7:43.

**7:45** Hili limechukua kipindi kirefu toka pale waliposhinda (huenda 1400 au 1250 K.K.) mpaka kipindi cha Daudi (+1 01 1 K.K. mpaka 971 /70 K.K., Harrison; 973 K.K., Young; 961 K.K., Bright).

**7:46** Hii inaaksi 2 Samweli 7, ambayo ni sura muhimu. Ni uimalishaji wa ki-Ungu wa ufalme wa Daudi.

**7:47 "Sulemani aliyemjengea nyumba"** Maelezo haya yanapatikana katika 12 Wafalme 6-8 na 2 Nyakati 1-6.

**7:48** Maelezo haya yanafanana na maelezo ya Sulemani katika 1 Wafalme 8:27 na 2 Nyakati 6:1-8.

**7:49-50** Nukuu hii imechukuliwa toka tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani ya Isa. 66:1 -2. Hoja ni kuwa hata Sulemani alitambua kuwa jengo lingalikuwa na Mungu wa uumbaji! Huenda mistari hii inadokeza mabishano ya ujumuishaji wa watu wa mataifa? Kama ndivyo, inaonekana kwa kiasi Fulani haliko wazi. Hata hivyo, Sulemani mwenyewe aliliangalia hekalu kama sehemu kwa ajili ya dunia kumrudia YHWH (kama vile. 1 Fal. 8:41 -43). Ilikuwa ni Wayahudi waliokuwa wakizungumza Kiyunani (yaani., saba katika Mdo. 6) ambao waliliona na kuutangazia ulimwengu wote mpango huu hata kabla ya mitume kutambua dhana hii ya mafundisho ya Yesu (kama vile. Mt. 28:1 8-20; Mdo. 1 :8).Stefano yawezakuwa akilitetea hili kwa dokezo katika Mdo.7:50.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 7:51-53**

<sup>51</sup> Enyi wenye shingo gumu, msiotahiriwa mioyo wala masikio, siku zote mnampinga Roho Mtakatifu; kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo. <sup>52</sup> Ni yupi katika manabii ambaye baba zenu hawakumwudhi? Nao waliwaua wale waliotabiri habari za kuja kwake yule Mwenye Haki; ambaye ninyi sasa mmekuwa wasaliti wake, mkamwua; <sup>53</sup> ninyi mliiopokea torati kwa agizo la malaika msiishike.

**7:51 "Enyi watu"** Stefano aligeuka toka kwenye uasi wa viongozi wa Kiyahudi na watu wa nyakati zilizopita kuwaelekea viongozi wa sasa na watu katika hekalu waliokuwa wakisisiliza ujumbe wake. Walikuwa na wanaendelea kuwa waasi dhidi ya YHWH!

▣ **"wenye shingo ngumu"** Stefano anadokeza juu ya uainishaji wa Musa wa watoto wa Yakobo/Israel (kama vile Kut.32:9; 33:3,5; 34:9; Kumb. 9:6).

▣ **"msiotahiriwa mioyo"** Nahau hii ya Kiebrania inamaanisha kutokuwa mwaminifu, mtiifu (kama vile. Law.26:41; Yer. 9:25-26; Ezek. 44:7). Hili ni kinyume na Kumb. 1 0:1 6; Yer. 4:4!

▣ **"wala masikio"** Nahau hii inarejelea juu ya kutokutaka kwao na kuwakubalia wajumbe wa Mungu (kama vile. Yer.6:1 0).

▣ **"siku zote mnampinga Roho Mtakatifu"** Hili linafanana na lile la Isa. 63:1 0. Upendo na uaminifu wa Mungu ulisifiwa sana katika Isa. 63:9,1 1 -1 4, bali majibu ya watu yalikuwa ya kutokuwa na imani!

**7:51b-52** Hii ni shutuma ya nguvu kwa uatawala uliopo wa Kiyahudi, kama ulivyokuwa utawala wa kale wa Kiyahudi! Watu wa kale wa Mungu waliwaua wale waleta habari wa Mungu na sasa wamemuua Masihi (kama vile. Mdo. 3:1 4; 5:28).

**7:52 "mwenye haki"** Hili kimetumika kama cheo kwa ajili ya Kristo katika Mdo. 3:1 4 and 22:1 4. Angalia maelezo kamili katika Mdo.3:1 4 na Mada Maalum: Haki katika Mdo.3:1 4.

**7:53 " ninyi mliiopokea torati kwa agizo la malaika "** Hii inarejelea kwenye sheria za Kiyahudi za Kumb. 33:2 toka kwenye tafasiri za maandiko ya kale ya Kiyunani pale Mungu alipompa Musa sheria kupitia mazingatio ya malaika ambayo yanaonekana kuthibitishwa na Gal. 3:1 9 na Ebr. 2:2.

▣ **"msiishike"** Stefano aliweka wazi utetezi wake ukiwa na neno "sikia" (BDB 1 033) ambao unaaksi neno la Kiebrania *Shema*, lenye kumaanisha "sikia upate kusikiza" (kama vile Kumb. 6:4). Stefano baadaye Yakobo (nduguze Yesu) wote wanadai "kuwa watendaji wa neno na sio wasikiaji tu" (kama vile. Yakobo 1 :22-23 akifuata Yesu, Mt. 7:24-27; Luka1 1 :48; Yn 1 3:1 7; kama alivyofanya Paulo, Rum. 2:1 3).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 7:54-60**

<sup>54</sup> Basi waliposikia maneno haya, wakachomwa mioyo, wakamsagia meno. <sup>55</sup> Lakini yeye akijaa Roho Mtakatifu, akakaza macho yake, akitazama mbinguni, akauona utukufu wa Mungu, na Yesu akisimama upande wa mkono wa kuume wa Mungu. <sup>56</sup> Akasema, Tazama! Naona mbingu zimefunguka, na Mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume wa Mungu. <sup>57</sup> Wakapiga kelele kwa sauti kuu, wakaziba masikio yao, wakamrukia kwa nia moja, <sup>58</sup> wakamtoa nje ya mji, wakampiga kwa mawe. Nao mashahidi wakaweka nguo zao miguuni pa kijana mmoja aliyeitwa Sauli. <sup>59</sup> Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, Bwana Yesu, pokea roho yangu. <sup>60</sup> Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, Bwana, usiwahesabie dhambi hii. Akiisha kusema haya akalala. Na Sauli alikuwa akiona vema kwa kuuawa kwake.

**7:54 "Wakachomwa"** Hili lazima lirejelee kwa washirika wa baraza kuu la sinagogi (kama vile Mdo. 6:1 5).

**NASB**"wakaumia mioyo"

**NKJV**"wakachomwa mioyo"

**NRSV**"wakajaa jazba"

**TEV**"wakawa na jazba"

## **NJB "wakakasirika"**

Hii ni kauli tendwa elekezi ya isiotimilifu. Kiuhalisia inamaanisha "kuumia mioyo" (kama vile Mdo. 5:33). Ujumbe wa Stefano hakika uliwaingia viongozi hawa, badala ya kutubu, wakageuka nyuma, kama ilivyokuwa, kwenye kukataliwa na mauaji (kama vile. Mdo. 5:33).

▣ **"wakamsagia meno"** Hii ni ishara ya hasira (kama vile Ayu.1 6:9; Zaburi 35:1 6; 37:1 2; Maombolezo. 2:1 6).

**7:55 "Roho Mtakatifu. . .Mungu. . .Yesu"** Tambua kule kutajwa kwa Mungu wa Utatu. Angalia Mada Maalum katika Mdo.2:32-33.

▣ **"akijaa Roho Mtakatifu"** Dhana ya kujazwa na Roho kwa ajili ya kuitangaza injili ni ya kipekee katika Matendo ya Mitume (yaani., *plēroō*, kama vile. Mdo. 2:4; 4:8,31 ; *plērēs*, kama vile Mdo. 6:3,5,8; 7:55; 11 :24). Angalia maelezo kamili katika Mdo. 5:1 7.

ukweli wa kibiblia unaohusianishwa na Roho unaainishwa kama:

1. Nafsi ya Roho (kama vile. Yn 1 4-1 6)
2. Ubatizo wa Roho (kama vile. 1 Kor. 1 2:1 3)
3. Tunda la Roho (kama vile. Gal. 5:22-23)
4. Karama za Roho (kama vile 1 Kor. 1 2)
5. Kujazwa na Roho (kama vile. Efe. 5:1 8)

Ndani ya yote haya, Kitabu cha Matendo kinaangazia juu ya #5. Viongozi wa kanisa la mwanzo walitiwa nguvu, wakaonekana majasiri tena na tena, na kutiwa nguvu ya kuitangaza injili ya Yesu Kristo. Katika suala la Stefano mahubiri yake ya kumaanisha yaligharimu maisha yake.

▣ **"akakaza macho"** Luka anapenda neno hili (kama vile. Luka 4:20; 22:56; Mdo. 1 :1 0; 3:4,1 2; 6:1 5; 7:55; 1 0:4;1 1 :6; 1 3:9; 1 4:9; 23:1 ). Stefano alitazama juu, kama ilivyokuwa Tabia ya Wayahudi ya maombi, lakini badala ya maombi, Mungu akamruhusu kuangalia mbinguni.

▣ **"akauona utukufu wa Mungu"** Tambua Stefano hasemekani kumwona Mungu, bali utukufu wake, hakuna awezae kumwona Mungu akaishi (kama vile Kut. 33:20-23). Ayubu aliamini angalimwona Mungu (kama vile Ayu. 1 9:25-27; Mdo. 7:55). Yesu aliahidi kuwa wale walio wasafi wa mioyo watamwona Mungu (kama vile Mt. 5:8). Angalia **MADA MAALUM: UTUKUFU (DOXA)** katika Mdo. 3:1 3.

▣ **"na Yesu akisimama mkono wa kuume wa Mungu"** Yesu kuwa upande wa kuume wa Mungu Baba ni nahau ya lugha ya kibinadamu kumwelezea Mungu (angalia Mada Maalum katika Mdo.2:33) kwa ajili ya nafasi ya nguvu ya ki-Ungu na mamlaka. Ukweli kwamba Yesu alikuwa amesimama inaonyesha umuhimu wake na kujali kwa ajili ya Wakristo wa mwanzo waliouawa. Mungu alijidhihilisha mwenyewe kwa Stefano katika umbo na tabia ambayo Stefano asingeweza kuipokea.

Hii haimaanishi kudokeza.

1. Kuwa mbinguni ni huko "juu"
2. Mungu ameketi kwenye kiti cha Enzi

Inajaribu kuelezea namna Yesu anavyojari na kuwajibika. Lazima tuwe waangalifu kushurutishwa kitamaduni na lugha zinazomwelezea Mungu kwa lugha ya kibinadamu kama chanzo cha mafundisho. Wasomaji wa sasa wa ki-Magharibi wanajaribu kuchukua kila sura kiuhalisia kama njia ya kuonyesha imani kwenye biblia kuwa ni mwenendo wa kitamaduni wa bahati mbaya. Hakika Mungu anajidhihilisha mwenyewe kwenye uumbaji wake, lakini anafanya hivyo katika njia na miundo ya kidunia ili wapate kumwelewa. Hakika kuna kipengere cha malazi. Mwanadamu kiumbe aliyeanguka, mwenye ukomo, hawezi kwa ukamilifu kuukabili ulimwengu wa kiroho. Mungu alichagua vitu toka kwenye tamaduni zetu na ulimwengu uliozoeleka kuvitumia kama mfanano na sitiari ili kuwasiliana nasi. Hakika haya ni kweli, na sio kamilifu.

**7:56 "Mwana wa Adamu"** Stefano kwa wazi anamtambua Yesu kama mtu wa "haki" kwenye Mdo. 5:52. Wasikiaji wake wasingepaswa kukosa uthibitisho huu wa ki-Masihi. Neno "Mwana wa Adam" lina matumizi mawili:

1. Ulikuwa ni msemu wa kawaida wa mtu (kama vile Ezek. 2:1 ; Zab. 8:4)
2. Lilitumika kwa mtu Fulani wa ki-Ungu (yaani., Masihi) katika Daniel 7:1 3-1 4 na Zab. 1 1 0:1. Kwa hiyo, lilikuwa na vidokezo vyote vya Ubinadamu na Uungu. Hii ndio sababu Yesu alilitumia kama utambulisho binafsi na pia kwa sababu halikuwa likitumiwa na walimu wa Kiyahudi waliojaribu kutumia nyadhifa za Agano la Kale kwa namna ya kijeshi au kitaifa. Nukuu hii iliyotumiwa na Stefano ni moja ya matumizi mawili ya msemu nje ya maneno ya Yesu (kama vile Yn 1 2:34).

**7:57-58** Hawa wasikiaji waliamini kuwa Stefano alikufuru kwa kudai kuwa Yesu ndiye Mwana wa Adamu ajaye (kama vile. Dan. 7:1 3). Kwa ajili ya hawa Wayahudi wenye imani ya Mungu mmoja (angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:39) hili lilikuwa limepita kipimo! Walitenda kwa Stefano kile Musa alichogiza kwa ajili ya makufuru (kama vile. Law. 24:1 4-1 6; Kumb. 1 3:9; 1 7:7). Uthibitisho wa Stefano huenda ukawa wa kweli au makufuru yanayostahili kifo! Panaweza pasiwepe mazingira ya kati kuhusu madai ya Yesu (kama vile. Yn 1 4:6-9).

**7:57 "wakamrukia kwa nia moja"** Hili ni neno lililotumiwa mara kwa mara na Luka kuelezea umoja uliokuwepo mwanzoni kwa wanafunzi (kama vile Mdo. 1 :1 4; 2:46; 5:1 2; 1 5:25). Wazee wa baraza kuu la sinagogi waliungana katika hasira zao na kumkataa Stefano (pia angalia 1 8:1 2, ambapo Wayahudi kule Akaya walimkataa Paulo na 1 9:29 juu ya hasira ya wapagani wa Efeso dhidi ya Wakristo).

**7:58 "wakamtoa nje ya mji"** Hakuna mtu aliyetakiwa kuuwawa ndani ya Yerusaleem kwa vile palikuwa eneo "takatifu!"

▣ **"wakampiga kwa mawe"** Mara nyingi imeelezwa kuwa Wayahudi chini ya umiliki wa Warumi hawakuwa na haki ya kutoa adhabu kali. Hili linaonyesha kwamba mara nyingi halikuwa kweli. Fujo za watu wengi hazikuweza kuzimwa kwa haraka.

▣ **"kijana mmoja aliyetwa Sauli"** Katika familia moja za Kiyahudi, mtu walimtathimini kuwa bado mdogo mpaka kwenye umri wa mika 40. Huu ndio mwanzo wa kukutana na Sauli wa Tarso kwa jina aliloitwa, na baadaye kuwa Paulo Mtume. Paulo alisikia safari ya Stefano katika Agano la Kale na yumkini alikwisha kuisikia mapema katika Sinagogi la Kilikia huko Yerusaleem (6:9). Mtu anaweza kushangaa ikiwa hili lilianza katika kipindi kisichojulikana cha Sauli, ambapo alijaribu kushughulika kwa kuwatesa Wakristo.

**7:59 "Bwana Yesu, pokea roho yangu"** Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Tambua kuwa Stefano aliamini kuwa anakwenda mbinguni kuwa na Yesu (kama vile. 2 Kor. 5:6,8) na sio kuzimu (kama vile., mahali pa kutunzia watu waliokufa kama ilivyo kwa Waebraia *sheol*, angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:27). Stefano yawezakuwa alishuhudia Yesu akisulubiwa, au kwa kiasi Fulani alisikia kulihusu hilo kwa upana kwa sababu alitumia misemo miwili iliyofanana (yaani., 7:59 na 60, kama vile. Luka 23:34,46). inafurahisha kutambua kuwa Stefano aliomba kwa Yesu, kama walivyofanaya Wanafunzi katika Mdo. 1 :24. Hata hivyo, katika maombi ya Agano Jipya yaliyobaki yanaelekezwa kwa Baba kupitia jina la Mwana.

**7:60 "akapiga magoti"** kupiga mtu mawe halikuwa suala la haraka. Andiko linadokeza kuwa lilichukua dakika nyingi hadi kutendeka.

▣ **"akalia kwa sauti kubwa "** Hili pia liliiga uzoefu wa Yesu. Hii sauti ilikuwa kubwa kwenye ule umati kama kwa YHWH. Haya maneno yawezakuwa yalisikika katika masikio ya Sauli.

▣ **"akalala"** Hii ni sitiari ya kibiblia kwa ajili ya kifo (mf. Ayu. 3:1 3; 1 4:1 2; Zab. 76:5; 2 Sam. 7:1 2; 1Fal. 2:1 0; Yer. 51 :39,57; Dan. 1 2:2; Mt. 27:52; Yn 1 1 :1 1 ; Mdo. 7:60; 1 3:36; 1 Kor. 1 5:6,1 8,20; 1The. 4:1 3; 2 Pet. 3:4). Hili halithibitishi mafundisho ya "nafsi kufa"

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri.

Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki.

Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini lilikuwa kusudi la maelezo ya Stefano? Hili linaonyesha nini kwa Wayahudi? Kwa nini walikasirika?
2. Ni vipi Yesu alifanana na Musa, mstari wa 37?
3. Kwa nini nukuu toka Isaya 66:1-2 katika mstari 49-50 ni wa muhimu?
4. Ni kipi kilikuwa cha muhimu kuhusu maono ya Stefano kwa Yesu?

## MATENDO YA MITUME 8

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Sauli analiudhi Kanisa	Sauli analiudhi kanisa	kusambaa kwa injili mpaka samaria na Pwani ya bahari	Sauli analiudhi kanisa	Stephano kupigwa mawe Sauli kama Mtesi
8:1b-3	8:1-3	8:1b-3	8:1b-2	(7:55-8:3) 8:2
Injili inahubiriwa Samaria	Kristo anahubiriwa Samaria		8:3	8:3
8:4-8	8:4-8	8:4-8	Injili inahubiriwa Samaria	Philipo Samaria
	Imani ya kazi ya Kichawi		8:4-8	8:4-8
8:9-13	8:9-13	8:9-13		Simoni Mchawi
	Dhambi ya mchawi		8:9-13	8:9-13
8:14-24	8:14-24	8:14-24	8:14-17	8:14-17
			8:18-19	8:18-24
			8:20-24	
8:25	8:25	8:25	8:25	8:25
Philipo na towashi Mkushi	Kristo anahubiriwa kwa Mkushi		Philipo na afisa Mkushi	Philipo anabatiza Towashi
8:26-33	8:26-40	8:26-40	8:26-40	8:26-33
			8:31-33	
8:34-40			8:34-37	8:34-40
			8:38:40	

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" \("A Guide to Good Bible Reading"\)](#))

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

#### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 8:1a**

<sup>1a</sup> Sauli alikuwa amefanya makubaliano yamoyo ili kumuua

**8:1 "Sauli alikuwa katika makubaliano ya kumuua"** Tungo hii inahitimisha Mdo. 7. Ni kauli tendaji ya wakati usiotimilifu yenye mafumbo. Paulo alikumbuka tukio kama hili lililowahi kumtia aibu (kama vile Mdo. 22:20; 1 Kor. 15:9; Gal. 1:13,23; Flp. 3:6; 1 Tim. 1:13). Baadhi inafana na kifungu hiki cha habari na 26:10, ambapo inadhaniwa kuwa Paulo alipiga kura katika baraza la wakuu wa sinagogi ili kuwauwa Wakristo.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 8:1b-3**

<sup>1b</sup> wote wakatawanyika katika nchi ya Uyahudi na Samaria, isipokuwa hao mitume. <sup>2</sup> Watu watauwa wakamzika Stefano, wakamfanyia maombolezo makuu. <sup>3</sup> Sauli akaliharibu kanisa, akiingia kila nyumba, na kuwaburuta wanaume na wanawake na kuwatupa gerezani.

▣ **"Siku ile kukatukia adha kuu ya kanisa lililokuwa katika Yerusalemu"** Hii yawezekana inawakilisha tukio la viongozi wa kiyahudi (zaidi Masadukayo) kwa sababu ya utawala na ukuaji wa kanisa la kwanza katika Yerusalemu. Hata hivyo ilikuwa njia ya Mungu ya kulazimisha kanisa kufanyia kazi Mdo. 1:8! If noKama sio Mdo. 1:8 basi Mdo. 8:1!

Sio bahati mbaya kwamba Luka anatumia neno *ekklesia* (angalia Mada Maalum katika Mdo. 5:11) kwa ajili ya mwili mpya wa waaminio. Watu hawa waume kwa wake hawakujiona kama kitu cha kujitenga kutoka katika ahadi za Agano la Kale, lakini kuzitimiliza! Neno lilitumika katika Tafsiri za Agano la Kale kufasiri "kusanyiko" (MT -*qahal*) la Israeli (kama vile Mdo. 7:38); sasa linatumika katika ushirika wa waamini katika Yerusalemu.

Luka anapenda sana neno hili "kubwa" (*megas*). Analitumia mara ishirini na tano katika Injili yake na mara ishirini na tisa katika Mdo. Katika Mdo. 8 he uses it foranalitumia kwa ajili ya:

1. dhiki kuu, Mdo. 8:1
2. Maombolezo kuu, Mdo. 8:2
3. Sauti kuu, Mdo. 8:7
4. mtu mkuu, Mdo. 8:9
5. kwa ukuu, Mdo. 8:10
6. miujiza mikuu, Mdo. 8:13

▣ **" wote wakatawanyika katika nchi ya Uyahudi na Samaria, isipokuwa hao mitume "** Ni jambo la kushangaza sana kwamba dhiki iliwapita kando Mitume na kushuka maradufu juu ya Wakristo wafuasi wa mafundisho ya uongo ya kiyahudi.

Kidhahiri wakati huu Mitume walikuwa wameridhika kuendelea kukaa ndani ya Uyahudi. Hili tukio lilikuwa limetukia baada ya muda kidogo wa Wanafunzi kukutana na Yesu Galilaya (kama vile Mt. 28:18-20) Pentekoste na bado uongozi wa kitume walikuwa radhi kuendelea kukaa na kuhubiri kwa Wayahudi tu au waongofu ana katika eneo moja tu la Yerusalemu.

▣ **"wakatawanyika katika nchi ya Uyahudi na Samaria"** Huku ni kutimika kwa Agizo Kuu la Luka linalotajwa katika Mdo. 1:8. Imekuwa muda sasa tokea Yesu azungumze maneno haya na kidhahiri kwa dhiki kulikuwa ni namna pekee ya kufanya kanisa kwenda katika ulimwengu wote. Kanisa bado limetulia tu!

**8:2 "Watu watauwa wakamzika Stefano,"** Neno "watu watauwa" mara nyingi linatumika kumaanisha Wayahudi wenye hisia kali za kiroho (kama vile Luka 2:25). Inawezekana kwamba linamaanisha Wakristo Wayahudi au Wayahudi tu waliokataa kufuata taratibu za kisheria (yaani uvunjifu wa amani wa umma) na kuuawa kwa Stephano. *Mishnah* wanaruhusu kuzikwa kwa wanaokufuru, lakini sio maombolezo ya sauti ya juu ya wale wanaokwenda kuzika. Watu hawa watauwa waliomboleza hadharani

1. kwa kwenda kinyume au kulaani kile kilichotendeka
2. kwa kurejea kwamba kile kilichotendeka hakikuwekewa mazingira ya kuzuliwa rasmi

**8:3 "Sauli akaliharibu kanisa"** Hiki ni kitenzi cha kauli ya kati elekezi ya wakati usiotimilifu. Hii inaweza kumaanisha mwanzo wa kitendo katika wakati uliopita (kama vile toleo la NASB, NJB) au tukio linalojirudia rudia (kama vile toleo la NKJV, NRSV, TEV). Neno "kuharibu" lilimaanisha "kuchanwa chanwa kwa mwili kunakofanywa na mnyama." Linatumika katika Tafsiri ya Agano la Kale katika Kutoka 22:13; Zaburi 74:13 na kushindwa kijeshi katika Yeremia 28:2 na 31:18. Paulo kwa wakati huu alikuwa akipambana na kweli zilizokuwa katika kauli za Stephano na labda alikuwa amejaribu kufunika mvutano wake wa ndani kwa kukazana kulitesa kanisa (kama vile Mdo. 9:1,13,21; 22:4,19; 26:10-11; 1 Kor. 15:9; Gal. 1:13; Flp. 3:6; 1 Tim. 1:13). Angalia Mada Maalum: Church at Acts Kanisa katika Mdo. 5:11.

▣ **"Sauli akaliharibu kanisa, akiingia kila nyumba,"** Tungo hii inaweza kueleweka kwa namna mbili:

1. Paulo aligundua wapi Mitume walikuwa wametembelea (kama vile Mdo. 5:42)
2. Kulikuwa na nyumba kadhaa za makanisa hata katika tarehe za hivi mwanzoni katika Yerusalemu ambapo waamini walikuwa wakikutana mara kwa mara

Wakristo wa kwanza walikuwa wanaweza kukutana katika

1. Masinagogi ya mahali pamoja kila Sabato
2. Hekaluni katika siku maalumu au hata siku zote
3. sehemu fulanifulani zilizotengwa au katika nyumba kadhaa siku za Jumapili

▣ **"kuwaburuta wanaume na wanawake"** Hiki ni kitenzi kinachotumika kumuelezea shetani kuondoa robo tatu ya nyota kutoka mbinguni katika Ufunuo 12:4. Inatumika mara kwa mara katika Mdo. (kama vile Mdo. 8:3; 14:19; 17:6). Sauli alikuwa makini bila mchezo katika kutesa kwake (kama vile Mdo. 26:10). Hii inawekwa na ushahidi wa tungo "wanaume kwa wanawake." alizivuruga vuruga na kusambaratisha familia za waamini wa kweli na kuwafunga na wengine hata kuwauwa (kama vile Mdo. 9:1,13,21; 22:4,19; 26:10,11; Gal. 1:13;23; 1 Tim. 1:13). Hii ndio maana yeye mwenyewe anajiita "mdogo wa watakatifu" (kama vile 1 Kor. 15:9; Efe. 3:8)

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 8:4-8**

<sup>4</sup> Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno. <sup>5</sup> Filipino akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo. <sup>6</sup> Na makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa na Filipino walipoyasikia na kuziona ishara alizokuwa akizifanya. <sup>7</sup> Kwa maana pepo wachafu wakawatoka wengi waliopagawa nao, wakilia kwa sauti kuu; na watu wengi waliopooza, na viwete, wakaponywa. <sup>8</sup> Ikawa furaha kubwa katika mji ule.

**8:4 "wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno"** Angalia kwa makini utaona kuwa walikuwa sio miyume maana wao walikuwa wamebaki katika Yerusalemu, lakini Wakristo wa mafundisho ya uongo wa kiyahudi walitapakaa katika maeneo yote wakawa wainjilisti wa kwanza. Ni jambo la kushangaza kwamba umisheni wa kiulimwengu wa kanisa ulichangamshwa sio na Mitume lakini Stephano na Philipo. Hili "neno" hapa kwa hakika lazima limaanishe injili, but lakini pia kuongezeka kwa ulimwengu mzima, shabaha isiyokuwa ya kiyahudi ya Stephano (Agizo Kuu, 1:8; Mt. 28:18-20; Luka 24:47).

8:5 "Philipo" Yeye ni mmoja wa "saba" wanaotajwa katika Mdo. 6:5 (kama vile Mdo. 21:8-9). Anatazamwa katika mazingira matatu ya kiinjilisti: (1) Samaria; (2) Towashi wa Kushi; na (3) huduma ya eneo la pwani ya kipalestina. Hawa "saba" walikuwa na moyo kwa ajili ya uinjilisti.

▣ "wakaenda katika mji wa Samaria" Kuna swali la kimaandiko ikiwa andiko linasomeka "Mji wa Samaria" au mjini Samaria." udhibitishwaji wa Maandiko unaunga mkono kuwepo kwa kimbata jina (kama vile MSS, P<sup>74</sup>, X, A, B). Hata hivyo jiji hili lilikuwa halijulikani kwa jina la Samaria kwa wakati huu lakini ilikuwa ukijulikana kama Sebaste. Wakati huu wa kipindi cha kirumi neno Samaria lilikuwa linatumika kama wilaya. Jiji Kubwa la Samaria lilitakiwa kuwa Shechem, wakati huo likiitwa Neapolis na leo Nablus. Limekuwa likijengewa nadharia kwamba jiji hili



linaweza kuwa Gitta kwasababu hilo ndilo lilikuwa jina la jadi la nyumba ya Lime Simon Magus. Nadharia hii inatoka kwa Justin Martyr, ambaye pia alitoke eneo hili.

▣ "na kuanza kutangaza Kristo kwao" Wasamaria walikuwa wakichukiwa na Wayahudi kwasababu walikuwa wakichukuliwa kama machotara (kama vile Ezra 4:1-3). Hii ilikuwa inafanana na uhamisho wa Ashuru wa mwaka 722 k.k. ambao ulizalisha watu wengi kwa upya eneo la kaskazini la Makabila Kumi likiwa na wapagani ambao walioleana na idadi ndogo ya wayahudi waliokuwa wamebaki (kama vile 2 Wafalme 17:24-41).

Kundi hili la watu lilikuwa pia limehudumiwa na Yesu. Yesu alidhihirisha U-masihi wake kwa mwanamke wa Samaria na kijiji chake (kama vile Yohana 4). Sasa Philipo anahubiri kuhusu "Kristo" (kiambata jina), ambalo ni fasiri ya Kiyunani "The Messiah Masihi" (angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:31). Jina la Agano la Kale la ahadi ya YHWH ya kutuma Mtu ambaye angeanzisha ufalme mpya, kuanzisha kizazi kipya cha Roho. Tukio hili linaoneshwa kwa mbele kwa kivuli katika huduma ya Yesu na hasa likitiwa mamlaka katika maneno ya Yesu ya kufunga (1:8).

8:6 "umati mzima kwa nia moja" Tungo "kwa nia moja" linatumika sana na Luka. Angalia kidokezo katika Mdo. 1:14.

▣ "Waliposikia na kuona ishara ambazo walikuwa wakizifanya" Hii inamaanisha miujiza ilidhibitisha ujumbe wa Philipo (kama vile Mdo. 8:7). Kudhihirishwa hukuhuku kwa Roho ilifuatana na Yesu, kumi na mbili, Sabini, na mahubiri ya Petro na Yohana.

8:7 Kupagawa na pepo ni halisi katika ulimwengu wetu (kama vile vitabu viwili vya Merrill F. Unger: [1] Biblical Demonology na [2] Demons in the World Today). Angalia Mada Maalum katika Mdo. 5:16.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 8:9-13**

<sup>9</sup> Na mtu mmoja, jina lake Simoni, hapo kwanza alikuwa akifanya uchawi katika mji ule, akiwashangaza watu wa taifa la Wasamaria, akisema ya kuwa yeye ni mtu mkubwa. <sup>10</sup> Wote wakamsikiliza tangu mdogo hata mkubwa, wakisema, Mtu huyu ni uweza wa Mungu, ule Mkuu. <sup>11</sup> Wakamsikiliza, kwa maana amewashangaza muda mwingi kwa uchawi wake. <sup>12</sup> Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake. <sup>13</sup> Na yeye Simoni mwenyewe aliamini akabatizwa, akashikamana na Filipo; akashangaa alipoziona ishara na miujiza mikubwa inayotendeka.

**8:9 "Na mtu mmoja, jina lake Simoni"** Iwe mtu huyu ikiwa kweli iliamini (kama vile Mdo. 8:13,18) au ilikuwa charlatan kutafuta nguvu hakuna uhakika. Ningetamani kumpa yeye faida za wasiwasi zikijikita katika Mdo. 8:24. Inashangaza kwa namna gani desturi za kwanza za kanisa la kwanza lilikua kupitia mtu huyu lakini yote ya hawa ni dhanio (kama vile *The Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible*, vol. 5, kurasa wa 442-444).

NASB, NRSV "miujiza"  
NKJV, TEV "uchawi"  
NJB "sanaa ya miujiza"

#### **MADA MAALUM: MIUJIZA**

Katika zama za kale palitokea kuwepo na aina mbali mbali ya watu binafsi na makundi yaliyojijhusisha na aina tofauti ya miujiza. Miujiza ni muundo wa utendaji wa kidini.

1. Kutokea kwa muujiza wa kwanza kunapatikana katika tamaduni za awali zilizoandikwa (yaani., sumer) katika uwepo wake wa kuundwa.
  - a. mkuu wa miungu, *Ea-enki*, anaitwa "Bwana mwenye umbo la binadamu" kwa sababu alimuua *Apsu*

- kwa msaada wa uchawi
- b. mwanae, *Marduk*, akamushinda *Tiamat* kwa sababu ya nguvu na uchawi wa baba yake
  - c. angalia Erica Reiner, *Surpu: A Collection of Sumerian and Akkadian Incantations*
2. miujiza ilikuwa ni ya muhimu sana huko Misri, ikiwahusisha *Thoth* na *Isis*. Hapakuwepo na utofauti kati ya miujiza mizuri na mibaya, kama ilivyo katika #1 na #3. Mara nyingi ulihusiana na
    - a. uponyaji
    - b. ufasiri wa ndoto
    - c. masuala ya kisiasa
    - d. ulimwengu wa vifo
  3. miujiza huko Anatolia (kwenye tamaduni za Wahiti) ilifanana na #1. Palikuwepo na miujiza mizuri na mibaya. Ya kwanza ilikubaliwa na pili ilikataliwa. Mara nyingi wabibi vizee walitumika sambamba na makuhani. Kama ilivyokuwa watu wa ANE, waliiona miujiza kama sehemu iliyokubalika kwa kampeni za kijeshi.
  4. Pana kundi la kijamii ya kikuhanu toka Medea waliojijhusisha katika utabiri wa nyota walioitwa "Wakalidayo" (kama vile Dan. 1:20; 2:2,10,27; 4:7,9; 5:11; Mt. 2:1,7,16). Herodotus aliwaita "makuhani wa Kimidiani." Walijijhusisha na utabiri na kudhibiti matukio ya mbeleni yaliyohusiana na mienendo na ushirikiano wa miungu nyota (yaani., sayari, kundi, vimondo).
  5. Kuna simulizi chache zilizopo kuhusiana na miujiza ya Kaanani (yaani., lugha ya kisemitic iliyoongelewa na watu wa Ugarit). Kwa wazi kabisa *El* alikuwa na nguvu nyingi na aliponya Mfalme wa Ugarit kwa miujiza (angalia "Hekaya za Mfalme Keret" ANET. 148b).
  6. Makundi mengi ya kimiujiza yaliundwa na watu waliodai kuwa na uwezo wa kuhadaa nguvu za miujiza (Yaani. Mwa. 41:8,24; Kut. 7:11,22; 8:7,19; 9:11). Mara nyingi hizi nguvu (au miungu) ilionekana kuwa na mtafaruku na wanadamu na ukichukulia upande wa hizi nguvu au mwenye maarifa ya kuzimiliki anaweza kuzidhibiti hizo nguvu kwa matumizi binafsi (kama vile mafunjo ya kimiujiza ya karne ya tatu na ya nne b.k). hawa watu binafsi wangaliweza:
    - a. Kutabiri mambo ya mbeleni
    - b. Kuweza kudhibiti mambo yanayokuja
    - c. Kutabairi mambo yajayo na ndoto
    - d. Kulaani au kumlinda mtu, mji, taifa, jeshi n.k
  7. Watenda miujiza, kama katika Mdo. 8:9,11 walidai kuwa na uwezo wa kuhadaa kwa nguvu za asili au za kimapepo kutenda matakwa yao. Hii mara nyingi ilihusiana na ibada ya kimiujiza. Watenda miujiza wa "kweli" mara nyingi waliwashambulia wenzao ambao hawakuweza kutenda ibada na litulujia kiusahihi. Hawa waliitwa wapotoshaji au wenye kuigiza.
  8. Nguvu ya injili inaonekana kwenye huduma ya Paulo huko Efeso ambapo wale watenda miujiza wa mwanzo walipo ongoka, na mbele za watu wakavichoma vitabu vyao vya kimiujiza (yaani., ni kwa namna gani unaweza kutenda ibada za matambiko, liturujia na kuwa na mwili wa kibinadamu, kama vile Mdo. 19:19) badala ya kiviuzi.
  9. Kwa usomaji zaidi angalia
    - a. Susan Garrett, *The Demise of the Devil*, Fortress Press, 1989
    - b. Merrill Unger, *Biblical Demonology*, Scripture Press, 1967
    - c. Hendrik Berkhof, *Christ and the Powers*, Herald Press, 1977
    - d. Waller Wink, *Naming the Powers*, Fortress Press, 1984
    - e. Clinton Arnold, *Three Crucial Questions About Spiritual Warfare*, Baker, 1997
  10. Miujiza yote hii, utendaji wa mambo ya siri ni chukizo mbele ya YHWH na imekatzwa kwa watu wake (angalia maelezo katika Kumb. 18:10-14, kwenye mtandao)

**8:10 "Mtu huyu ndiye anayeitwa Nguvu Kubwa ya Mungu"** Hiki kilikuwa ni cheo cha mungu wa kipindi kati ya Warumi-Wayunani Pantheon (yaani Zeus). Kwa Kiaramu ingekuwa "Hii ni nguvu ya mungu aitwaye mkuu." Mtu huyu alikuwa amewachezea sana mbinu watu wa eneo fulani. Yawezekana alikuwa hata amejifanyia mbinu mwenyewe (kama vile Mdo. 8:9,13).

**8:12 "waliamini"** Angalia Mada Maalum: Amini, Imani, Sadiki katika Mdo 3:16 na Kuamini kwa Agano la Kale katika Mdo. 6:5

**NASB** "kuhubiri habari njema"

**NKJV** "walihubiri vitu"

**NRSV** "walikuwa wakitangaza habari njema"

**TEV** "ujumbe wa habari njema"

Hiki kilikuwa kitenzi cha Kiyunani *euangelizō*, ambacho ni ambatani ya wema (*eu*) na ujumbe (*angelizō*). Tunapata maneno ya Kiingereza evangel (injili), evangelize (injilisha), na evangelism (uinjilisti) kutoka katika neno hili la Kiyunani. Philipo aliwasilisha hadithi ya Yesu kwa Wasamaria hawa nao wakaitikia katika kutunza imani.

▣ **"kuhusu ufalme wa Mbinguni"** Angalia Mada Maalum mbili katika somo hili katika Mdo. 1:3.

▣ **"jina la Yesu Kristo"** Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:21.

▣ **"walikuwa wakibatizwa"** Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:38.

▣ **"wanaume kwa wanawake pia"** Kimuktadha kunaweza kuwa na umuhimu wa aina mbili kwa tungo hii.

1. Paulo aliwatesa "wanaume na wanawake (kama vile Mdo. 8:3)," lakini pia injili ilikuwa inaokoa "wanaume kwa wanawake"
2. Katika Uyahudi ni wanaume peke yake walishiriki taratibu za mwanzo za tohara za Kiyahudi lakini kwa sasa katika Injili Jinsi zote zilishiriki katika taratibu za ubatizo.

**8:13 "Simoni aliamini"** Matumizi mengi ya kiinjilisti ya neno hili "kuamini" (Angalia Mada Maalum katika Mdo. 3:16) Katika namna ya kimaana sana, lakini kuna mahali katika Agano Jipya (kwa mfano Yohana 8:31) ambapo inaashiria kitu kingine cha chini tofauti na uongofu (kama vile Yohana 8:59).

Imani ya kuanzia msio kigezo pekee tu (kama vile Mt. 13:1-9,10-23; 24:13). Muendelezo na utii pia ni ushahidi wa mahusiano ya kweli na Kristo.

## **MADA MAALUMU: USTAHIMILIVU**

Mafundisho ya kibiblia yaliyohusiana na maisha ya Mkristo ni vigumu kuyaelezea kwa sababu yanawasilishwa katika namna ile ile ya mashariki, milinganyo ya kirahaja (tazama Mada Maalum: Fasihi ya Mashariki [mafumbo ya kibiblia]). Milinganyo hii inaonekana kuwa na mkanganyiko, bado mihimili yote ni ya kibiblia. Wakristo wa Mashariki walielekea kuchagua ukweli ulio mmoja na kuachana au kukashifu kweli iliyo kinyume. Baadhi ya Mifano ni:

1. Je! Wokovu ni maamuzi asilia ya kumwamini Kristo au ni maisha yenye wajibu ya kiuwanafunzi?
2. Je! Wokovu ni uchaguzi kwa maana ya neema kutoka katika mamlaka ya Mungu au imani na mwikio wa toba kwa sehemu ya mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu?
3. Je! wokovu, unapopokelewa, haiwezekani kuupoteza, au kuna uhitaji wa jitihada endelevu

Jambo hili la ustahimilivu limekuwa la kibishi katika historia nzima ya kanisa. Tatizo linaanza na muonekano wa mgogoro wa vifungu vya Agano Jipya:

1. maandiko yahasuyo uhakika
  - a. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 6:37; 10:28-29)
  - b. semi za Paulo (Rum. 8:35-39; Efe. 1:13; 2:5,8-9; Flp. 1:6; 2:13; 2 The. 3:3; 2 Tim. 1:12; 4:18)
  - c. semi za Petro (1 Pet. 1:4-5)
2. maandiko yahasuyo umuhimu wa ustahimilivu

- a. semi za Yesu katika Injili za Kimhutasari (Mt. 10:22; 13:1-9,24-30; 24:13; Marko 13:13)
- b. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 8:31; 15:4-10)
- c. semi za Paulo (Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2; 2 Kor. 13:5; Gal. 1:6; 3:4; 5:4; 6:9; Flp. 2:12; 3:18-20; Kol. 1:23; 2 Tim. 3:2)
- d. semi za mwandishi wa Kiebrania (2:1; 3:6,14; 4:14; 6:11)
- e. semi za Yohana (1 Yohana 2:6; 2 Yohana 9; Ufu. 2:7,17,26; 3:5,12,21; 21:7)

Mambo ya wokovu ndani ya biblia hutoka katika pendo, huruma, na neema ya mamlaka ya Mungu wa Utatu. Hakuna mwanadamu awezaye kuokolewa pasipo kuingiliwa na Roho (kama vile Yohana 6:44,65). Mungu alikuja na kupangilia mambo muhimu, lakini alidai kwamba wanadamu wanapaswa kuitikia katika imani na toba, katika namna zote kwa uanzilishi na kwa uendelevu. Mungu hutenda kazi na wanadamu katika uhusiano wa agano. Kuna upendeleo na majukumu!

Wokovu umetolewa kwa wanadamu wote. Kifo cha Yesu kilihusika na tatizo la dhambi ya uumbaji ulioanguka! Mungu ameleta njia na anahitaji wale wote walioumbwa kwa mfano Wake kuliitikia pendo Lake na utoaji katika Yesu. Kama ungependa kusoma zaidi juu ya somo hili tazama

1. Dale Moody, *The Word of Truth*, Eerdmans, 1981 (kur. 348-365)
2. Howard Marshall, *Kept by the Power of God*, Bethany Fellowship, 1969
3. Robert Shank, *Life in the Son*, Westcott, 1961

Biblia inashughulikia matatizo mawili tofauti katika eneo hili: (1) kuchukulia imani kama msimamo wa kuishi bila kuzaa matunda, maisha ya ubinafsi au (2) kuwatia moyo wale wanaopambana na huduma na dhambi binafsi. Tatizo ni kwamba makundi yasiyo sahihi yana uchukuwa ujumbe usio sahihi na kutengeneza mifumo ya kitheolojia yenye vifungu vya kibiblia vyenye kuwekewa mipaka. Baadhi ya Wakristo wakiwa katika hali ya kukata tamaa wanahitaji ujumbe wa kuwatia moyo, wakati wengine wanahitaji kuonywa kwa ukali kuhusiana na uvumilivu! Wewe uko ndani ya kundi lipi?

Kuna mabishano ya historia ya kitheolojia iliyomuhusisha Augustine dhidi ya Pelagius na Calvin dhidi ya Arminius (semi-Pelagian). Jambo hili lilihusisha swali la wokovu : kama mtu akiokolewa kiukweli, yampasa kustahimili katika imani na uamiifu?

Wafuasi wa Calvin wamesimama nyuma ya maandiko yale ya kibiblia ambayo yanadai kwamba mamlaka ya Mungu na nguvu idumuyo (Yohana 10:27-30; Rum. 8:31-39; 1 Yohana 5:13,18; 1 Pet. 1:3-5) na vitenzi vya nyakati kama kauli tendewa timilifu endelevu ya Efe. 2:5,8.

Wafuasi wa Arminius wamesimamia maandiko yale ya kibiblia ambayo yanamuonya yule aaminiye "kusimama imara," "kudumu," au "kuendelea" (Mt. 10:22; 24:9-13; Marko 13:13; Yohana 15:4-6; 1 Kor. 15:2; Gal. 6:9; Ufu. 2:7,11,17,26; 3:5,12,21; 21:7). Mimi binafsi siamini kwamba Waebrania 6 na 10 zinatumiwa, lakini wafuasi wengi wa Arminius wanazitumia kama onyo dhidi ya uasi. Mfano wa Mpanzi katika Mathayo 13 na Marko 4 inashughulikia suala la imani, kama inavyofanya Yohana 8:31-59. Kama wafuasi wa Calvin wanavyo nukuu vitenzi vya kauli ya wakati uliopo timilifu vilivyotumiwa kueleza wokovu, Wafuasi wa Arminius wana nukuu vifungu vya kauli ya wakati uliopo kama 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15.

- Huu ni mfano kamili wa namna mfumo wa kitheolijia unayotumiwa vibaya njia ya uhakiki wa fasiri za maandiko. Mara nyingi kanuni inayoongoza au andiko kuu linatumika kutengeneza ufito wa kitheolojia ambapo maandiko mengine yote yanatazamiwa. Kuwa makini na mfumo kutoka vyanzo vyo vyote vile. Vitokana na ufafanuzi wa mantiki ya mashariki, si ufunuo. Biblia ni kitabu cha mashariki. Inawakilisha kweli katika mvutano uliokamilishwa, ulinganifu wa mafumbo yaonekanayo. Wakristo wanamaanisha kukubaliana na yote na kuishi ndani ya mvutano huo. Agano Jipya linawasilisha vyote yaani ulinzi wa mwaamini na dai la imani endelevu na uovu. Ukristo ni mwitikio wa mwanzo wa toba na imani inayofatiwa na mwitikio endelevu wa toba na imani. Wokovu si kama matokeo (tiketia ya kwenda mbinguni au sera ya bima ya moto), bali uhusiano. Ni maamuzi na uwanafunzi. Inaelezwa katika

Agano Jipya 3:5

- utimilifu (tendo lililokamilishwa na matokeo endelevu), Efe. 2:5,8
- inawasilisha (tendo endelevu), 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15
- wakati ujao (matukio yajayo au matukio fulani), Rum. 5:8,10; 10:9; 1 Kor. 3:15; Flp. 1:28; 1 The. 5:8-9; Ebr. 1:14; 9:28

katika vitenzi vyote vya nyakati:

- kauli (tendo timilifu), Matendo 15:11; Rum. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito

▣ **"aliendelea na Philipo"** Hii ni kauli yenye mafumbo ya wakati usiotimilifu. Tazama mfuatano.

1. alisikia, Mdo. 8:6-7,12
2. aliona, Mdo. 8:6-7,13
3. aliamini, Mdo. 8:13
4. alibatizwa, Mdo. 8:13
5. alikwenda na Philipo, Mdo. 8:13

### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 8: 14-24**

<sup>14</sup> Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana; <sup>15</sup> ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu; <sup>16</sup> kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu. <sup>17</sup> Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. <sup>18</sup> Hata Simoni alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha akisema, <sup>19</sup> Nipeni na mimi uwezo huu, ili kila mtu nitakayemweka mikono yangu, apokee Roho Mtakatifu. <sup>20</sup> Lakini Petro akamwambia, Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania ya kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali. <sup>21</sup> Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili, kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu. <sup>22</sup> Basi, tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana, ili kama yamkini, usamehewe fikira hii ya moyo wako. <sup>23</sup> Kwa maana nakuona u katika uchungu kama nyongo, na tena u katika kifungo cha uovu. <sup>24</sup> Simoni akajibu, akasema, Niombeeni ninyi kwa Bwana, yasinifikilie mambo haya mliyosema hata moja.

**8:14 "Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana "** Huduma kwa Wasamaria ilikuwa ni katazo kwa wakati wa Yesu (kama vile Mt. 10:5). Kwa namna ya wazi Mitume walitaka kutoa vikwazo vyao vya kiofisi kwa namna hizi na ujio na mtembeo mpya usiokuwa wa kawaida wa Roho Mtakatifu kati ya makabila haya yenye desturi zinazochukiwa. Eneo hili kwa namna yake linatajwa katika Mdo 1:8. Kama ilivyokuwa kawaida Philipo alinasa dhana na maana ya Yesu ya kuenenda ulimwenguni kote na Injili kwa haraka zaidi ya wale kumi na mbili.

Tazama kwamba kumwamini Yesu kunaenda sambamba na "kupokea neno la Mungu." Neno la Mungu laweza kusima kwa vitu mbali mbali kadhaa.

1. Mawasiliano ya Mungu ya jumla kwa wanadamu
2. Mawasiliano ya Mungu yaliyowekwa katika kumbukumbu (yaani Maandiko)
3. Mungu Mwana (yaani Neno, kama vile Yohana 1:1) ambaye ni kilele cha ufunuo wa Mungu (Kama vile Waebrania 1:3)

Tazama kwamba Petro na Yohana walitumwa. Petro alikuwa ni kiongozi anayetambuliwa na kundi la kitume na Yohana ndiye hapo mwanzo aliyetaka kuita moto ushuke juu ya Wasamaria (kama vile Luka 9:54).

**8:15 "ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu"** Kuna matatizo ya ajabu yanayojaribu kujenga thiolojia ya wokovu kutoka Matendo ya Mitume kwa sababu zifuatazo: mpangilio wa mtukio na matukio yenyewe yanayozunguka wokovu yanatofautiana kutoka katika kifungo kimoja kwenda kingine. Roho Mtakatifu

katika kifungu hiki cha habari anamaanisha uthibitisho kama wa Pentekoste kuonesha kwamba Mungu amekubali na kuokoa hawa Wasamaria. Wasingeweza kuwa wameokolewa kiukweli ukweli hapo mwanzo (yaani kupokea ni kauli ya kati elekezi ya wakati timilifu) bila kazi ya Roho Mtakatifu (kama vile Warumi. 8:9).

Nafikiri jambo la Pentekoste lilitengeneza utaratibu ambao aliufanya Mungu katika kutambua makundi ya watu na makabila na mazingira tofauti ya kijiografia, kuonesha na kuthibitisha kwa kanisa liaminilo la kiyahudi kwamba Mungu mwenyewe alikuwa amewakubali kwa ukamilifu kundi hili jipya. Udhihirisho wa Roho (yaani Pentekoste) kithiolojia hapo ni tofauti na ndimi za Wakorintho.

Andiko haliwezi kutumika kutaka hali inayofanana na ya Wakorintho kuthibitisha wokovu (kama vile 1 Kor. 12:29-30, ambayo ni mfululizo wa maswali yanayotarajia jibu la "hapana" ). Luka anaweka kumbukumbu kile kilichotokea sio kile kinachotakiwa kutokea kila mara.

**8:16-17** Hii ni tofauti na mfululizo wa matukio na mfuatano wake unaotajwa katika Mdo. 2:38. Tofauti inasababishwa na tendo fulani la Roho Mtakatifu: (1) katika Mdo. 2:38 katika kuhusianisha na wokovu na (2) katika Mdo. 8:16 ukihusianisha na aina ya jambo kama la Pentekoste. Hili "tukio la Roho Mtakatifu" la Mdo. 2 sasa lilitokea katika Samaria. Hii haikuwa kwa ajili ya faida yao peke yake, lakini kwa ajili ya jamii nzima ya Wakristo wa Kiyahudi. Iliwaonyesha wao kwamba Mungu alikuwa amewakubali kiukamilifu! Hii haimaanishi kuelezea hatua za mara mbili za kwanza za tukio la wokovu. Tafadhali angalia kwamba ilikuwa ni Petro na Yohana waliotambua kutokuwepo kwa udhihirisho maalum wa Roho Mtakatifu kama waliokuwa nao siku ya Pentekoste. Hii haimaanishi kwamba ishara za miujiza ambazo zilifuatana na mahubiri ya Paulo hazikuwa madhihirisho ya kweli ya Roho (kama vile Mdo. 8:13). Petro na Yohana walitaka Pentekoste ya Kisamaria! Hii ni muhimu sana kwasababu Kornerio alikuwa na hali hiyo hiyo (yaani Mdo. 10), Petro alijua kwamba Mungu alikuwa amemkubali askari huyu wa Kirumi na familia yake. Injili ni kwa ajili ya watu wote. Hii ni kweli kuu ambayo tukio hili linafunua katika Mdo!

**8:16** Hii ingeweza kitwa Pentekoste ya Kisamaria.

**8:17** Hii haiwezi kuwa andiko la udhibitisho kwa ajili ya hitaji la kuwawekea watu mikono. Hatua hizi kwa ajili ya kusudi hili hazitokei tena katika Matendo ya Mitume. Inaelezea nguvu na mamlaka ya Mitume. Angalia [MADA MAALUM: KUWEKEA MIKONO](#) katika Mdo. 6:6.

**8:20** Swali letu la Kithiolojia kwetu ni swali la fundisho la wokovu kwa Simoni. Je aliokoka au la? Je maneno ya Petro yanaweza kuchukuliwa kama laana au onyo? Waamini wote wapya wana udhaifu na taarifa zisizokuwa sahihi kuhusu Injili, lakini je hili la Sinoni linamaanisha semu ya ziada ya ubinafsi wa kikwakwe kwake? Je watu wanaweza kuokolewa wakiwa na vipaumbele vya kingogoro katika maisha yao?

▣ **" karama ya Mungu "** Hapa Roho anasimama kwa ajili ya kazi zote za Mungu kwa niaba ya ubinadamu unaoasi na wenye ukaidi (kama vile Isa. 55:1-2; Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38; Luka 11:13; Mdo. 2:38).

**8:21 "Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili "** Neno la kwanza "sehemu" (yaani *meris*) linamaanisha sehemu katika ukawaida. Lina kissawe hasi hapa na 2 Kor. 6:15. Neno la pili "sehemu" (yaani *klēros*) ni neno la Agano la Kale "tele," ambalo lilikuwa na maana ya kutambua mapenzi ya Mungu (yaani *Urim* na *Thummim*). Yalikuwa yakitumiwa kugawanya Nchi ya Ahadi kati ya kabila (kama vile Yohana 12-19). Hivyo linatumika katika namna ya urithi. Neno hili lilikuja kutumika katika Kingereza kwa ajili ya "askofu/kuhani," lakini katika Agano Jipya linamaanisha waamini wote .

▣ **"moyo wako si mnyofu mbele za Mungu"** Haya yanaweza kuwa maelezo ya Zaburi. 78:37. Maneno "haki" na "usawa" (Angalia Mada Maalum katika Mdo. 3:14) na miundo yake tofauti tofauti inatoka katika neno kwa ajili ya mafunjo yanayopatikana katika mji wa Mesopotamia. Ilikuwa na urefu wa kunyooka moja kwa moja wa futi kumi na tano. Mungu alichukua neno hili, ambalo lilikuwa linatumika katika ujenzi (kuangalia unyoofu wa mshazali wa ukuta), kufunua tabia yake mwenyewe ya kimaadili. Mungu ndiye kipimo, rula na cha iliyonyooka ambayo

wanadamu wote wanahukumiwa kwa hiyo. Katika ufahamu wa hili, wote wanashindwa jaribio (kama vile Rum. 3:9-18,23).

**8:22 "tubu"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiokuwa timilifu, ambayo inamaanisha uharaka. Angalia Kidokezo na Mada Maalum katika Mdo. 2:38.

▣ **"uombe"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopita usiokuwa timilifu (yenye ushahidi). Kuzungumza na Mungu ni ushahidi wa mahusiano ya kibinafsi, uvuvio unaopelekea toba, ni ushahidi wa Roho akaaye ndani!

▣ **"ikiwa"** Hii ni sentensi ya daraja la kwanza yenye masharti, ambayo inadhaniwa kuwa kweli kwa ajili ya makusudi ya kifasihi ya kiuandishi au kutoka katika mtazamo wake. Katika sentensi hii kunaashiria kutojulikana kunakojikita katika utayari wa Simoni kutubu na kuomba kwa ajili ya msamaha. Hali yake ya ufahamu na matendo ni kuchepuka kwa dhati kutoka katika desturi ya Kikristo.

▣ **"dhamira ya moyo wako"** Dhambi inaanza na uhai wa wazo. Walimu wa Kiyahudi wanasema kwamba akili ni kama shamba lililokwisha kulimwa tayari kwa ajili ya kupanda mbegu. Tunachokiruhusu kupitia macho yetu na maskio yetu kinachukua mizizi. Ikiwa tukiendelea na jambo hili mawazo haya yanakuwa matendo. Hii ndio maana Agano Jipya linaeleza kuwa "vifungeni viuno vya nia zenu" (kama vile 1 Pet. 1:13) au "kufanywa upya ufahamu" (kama vile Rum 12:2; Efe. 4:23).

### 8:23

NASB, NRSV	"nyongo ya uchungu"
NKJV	"umewekewa sumu kwa uchungu"
TEV	"mejaa wivu wenye uchungu"
NJB	"uchungu wa nyongo"

Maneno "nyongo" (*cholē*) na "uchungu" (*pikros*) zote zinamaanisha roho yenye uchungu, ambayo siku zote inaambatana na hasira na uasi na ukanaji (kama vile Kumbu. 29:18; 32:28-33; Ebr. 12:15). Paulo anatumia neno "uchungu" mara kwa mara katika kuorodhesha vitu vya kuacha (kama vile Rum. 3:14; Efe. 4:31).

NASB	"katika kifungo cha uovu"
NKJV	"kufungwa na uovu"
NRSV	"minyororo ya uovu/ubaya"
TEV	"mfungwa wa dhambi"
NJB	"minyoro ya dhambi"

Haya yanaweza kuwa maelezo ka kazi ya Masihi (kama vile Isa. 58:6). Yesu angeweza kumuweka huru Simoni kutoka katika kifungo hiki cha uovu ili apate nguvu binafsi kama alivyomuweka huru kutoka katika adhabu ya dhambi. Dhambi ina sehemu mbili: (1) kifo katika vyote kimwili na kiroho (2) yeye aliyeshikilia maisha ya mwenye dhambi (inaweza kuathiri vyote anayeokolewa na anayepotea, kama vile 1 Kor. 3:1-3). Dhambi lazima ishughulikiwe kote ndani ya muda na milele; adhabu yake na nguvu lazima ishughulikiwe, lakini Kristo tu na Roho wanaweza kufanya hivyo, lakini sisi kama waamini lazima tuwaruhusu kufanya kazi!

**8:24 " Niombeeni ninyi kwa Bwana, nyie wenyewe "** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopita usiokuwa timilifu (wingi huu, unaweza kuwa ulimaanisha timu nzima ya umisheni). Simoni anarudia maneno aliyoyanena Petro katika Mdo. 8:22. Maneno ya Petro yamemuogopesha. Naamini Simoni japo ni Muumini ila ni mtoto mchanga kabisa.

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 8:25

<sup>25</sup> Nao walipokwisha kushuhudia na kulihubiri neno la Bwana wakarudi Yerusalemu, wakaihubiri Injili katika vijiji vingi vya Wasamaria.

8:25 "kushuhudia kwa dhati" Angalia Kidokezo katika Mdo. 2:40.

▣ "wakaihubiri Injili katika vijiji vingi vya Wasamaria." Hii inaonesha badiliko la ghafla la kimitizamo la sehemu ya Mitume kwa Wasamaria. Inaonekana kwamba "neni la Bwana" na "Injili" ni visawe.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 8:26-40**

<sup>26</sup> Malaika wa Bwana akasema na Filipino, akamwambia, Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa. <sup>27</sup> Naye akaondoka, akaenda; mara akamwona mtu wa Kushi, towashi, mwenye mamlaka chini ya Kandake malkia wa Kushi, aliyewekwa juu ya hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu, <sup>28</sup> akawa akirejea, ameketi garini mwake akisoma chuo cha nabii Isaya. <sup>29</sup> Roho akamwambia Filipino, Sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo. <sup>30</sup> Basi Filipino akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, Je! Yamekuelea haya unayosoma? <sup>31</sup> Akasema, Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipino apande na kuketi pamoja naye. <sup>32</sup> Na fungu la Maandiko alilokuwa akilisoma ni hili, Aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo, Na kama vile mwana-kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, Vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. <sup>33</sup> Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi. <sup>34</sup> Yule towashi akamjibu Filipino, akasema, Nakuomba, nabii huyu; asema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? <sup>35</sup> Filipino akafunua kinywa chake, naye, akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. <sup>36</sup> Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema, Tazama, maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe? <sup>37</sup> Filipino akasema, Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana. Akajibu, akanena, Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. <sup>38</sup> Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipino na yule towashi; naye akambatiza. <sup>39</sup> Kisha, walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipino, yule towashi asimwone tena; basi alikwenda zake akifurahi. <sup>40</sup> Lakini Filipino akaonekana katika Azoto, na alipokuwa akipita akahubiri Injili katika miji yote, hata akafika Kaisaria.

8:26 " Malaika wa Bwana akasema na Filipino "Hapa "malaika wa Bwana" na "Roho Mtakatifu" wanaonekana kutengeneza visawe (kama vile Mdo. 8:29). Hii ni kawaida katika Mdo. Angalia Kidokezo katika Mdo. 5:19.

▣ "Ondoka ukaende upande wa kusini" Hizi zote ni amri. Hii inaweza kuwa ilimaanisha moja ya barabara mbili kuelekea Misri. Ujumbe huu inawezekana ulikuwa wa kusikika kwa sauti ya juu kwa sababu ya maelekezo yake yaliyonyooka (kama ule wa Paulo).

NASB	"(Hii ni njia ya jangwani)"
NKJV	"Hili ni jangwa"
NRSV	"(Hii ndito barabara ya nyikani)"
TEV	"(Hii barabara haitumiki siku hizi)"
NJB	"barabara ya jangwani"

Ikiwa hii ni maoni ya Luka, Luka anajaribu kuainisha chanzo chake, o au je yawezekana kuwa hii kweli ni maoni ya chanzo cha Luka (yawezekana Philipo, kama vile Mdo. 21:8)? Maswali haya hayawezi kujibiwa kwa uhakika. Uuvio unafunika uzalishwaji wa Biblia bila kujali watu wangapi tofautitofauti wamejumuishwa.

8:27 "towashi, mwenye mamlaka "Neno"Rasmi" Kidhahari ni neno "towashi." Hata hivyo haijulikana kama alikuwa towashi wa mwili au kama alikuwa tu ni towashi mwenye mamlaka ya kimahakama (maana iliyozalishwa) Katika Agano la Kale Potipha naitwa towashi ila anaonekana ameoa (kama vile Mwanzo 39:1). Katika Agano la Kale, Kumb. 23:1 inakataza towashi kufanyika kuwa sehemu ya jamii ya Wayahudi; hata hivyo katika Isaya 56:3-5, katazo hili limekwisha ondolewa. Hii kwa dhahiri inaonesha kuwa kizazi kipya cha Roho kimepambazuka. Ikiwa



mtu huyu alikuwa mcha Mungu au mwongofu ni kwamba haijalekweka tu na inabaki kuwa yumkini inawezekana lakini maelezo ya tungo yanonesha kuwa alikuwa mfanyakazi mkubwa wa kiserikali

▣ **"chini ya Kandake malkia wa Kushi"** Kandake kiikuwa ni cheo kama "Farao" au "Kaisari." Sababu kwanini Malkia anatajwa ni kwasababu Mfalme wa Kushi alikuwa anachukuliwa kama ana u-mungu na, hivyo lilikuwa jambo dogo la chini sana kumfanya ashughulike na masuala madogo madogo ya kiutawala au mambo ya kisiasa.

**8:28 "akisoma chuo cha nabii Isaya"** Kwa uwazi mtu huyu alikuwa amenunua gombo la ngozi ghali sana la Isaya, ambalo lawezekana kuwalilikuwa na urefu kama wa futi 29 (yaani yalipatikana katika mabaki ya kale ya magombo ya Bahari ya Shamu). Kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, alikuwa amefungua katika kifungu cha habari cha Isaya 53:7-8 and was reading it na alikuwa akikisoma.

**8:29 "Roho akamwambia Filipino, Sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Kiuhalisia ilimaanisha "kugundishwa." Roho alikuwa anampatia Filipino kila uongozi unaohitajika.

**8:30 "Filippo akamkimbilia na kumsikia akisoma chou cha Isaya Nabii"** Maandiko ya kale yote yalitakiwa kusomwa kwa sauti hata kama mtu akiwa peke yake.

▣ **"Je! Yamekuelea haya unayosoma"** Swali zuri kwa namna gani hili! Inawezekana kusoma maandiko na kiuwazi usiweze kuona kusudio lake. Roho anamuongoza Filipino katika "kukutana kiungu" ambacho kitasababisha

1. kuonesha kizazi kipya kimeanza
2. kutoa ushuhuda mkubwa kwa kikundi kingine cha watu

**8:31** A. T. Robertson katika kitabu chake cha *Word Pictures in the New Testament* anatoa maoni yake katika mstari huu, "Hii ni hali iliyochanganywa, hitimisho linalokuja kwanza ni la daraja la nne. . .likiwa na 'an' na hali ya uchaguzi, lakini ni hali...isiyo ya daraja la kwanza... ni mazingira yanayotoshelezana sana katika Koine" (ukurasa wa 110). Hali ya daraja la kwanza katika Luka 19:40 anatumia *ean* badala ya *ei*. Hali inaamuliwa na hisia wala sio ilivyotengenezwa (kama vile Luka 19:40).

**8:32-33** Nukuu hii inatoka katika kifungu cha habari cha Tafsiri ya Agano la Kale cha Isa. 53:7-9. Ninashangaa kwamba mistari hii inasisitizwa na sio mistari mingine ya Kimasihi katika muktadha wa Agano la Kale. Hata hivyo Filipino anaanza vizuri kwa kuanza kusoma na kuelezea kifungu chote katika ufahamu wa maisha, huduma, kifu na Ufufuo wa Yesu wa Nazareth. Unabii wa Agano la Kale umekuwa ukitimizwa na msamaha kupitia Kristo anayetolewa kwa kila mtu!

**8:35 "Filippo akafunua kinywa chake"** Hii inaonesha dhamila ya kifungu cha Agano la Kale juu ya "Mtumishi atesekeaye" kwenye kutangazwa kwa injili. Naamini Yesu, mwenyewe alilionesha kanisa la mwanzo namna nabii hizi za kale zinamuhusu yeye mwenyewe (kama vile Luka 24:27).

**8:36 "Tazama, maji haya; ni nini kinachonizua nisibatizwe"** Injili ya Filipino ilijumuisha Ubatizo (kama vile Mathayo 3; 28:19; Mdo. 2:38; Rum. 6:1-11; Kol. 2:12)! Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:38. Angalia kwamba hakuhitaji kuthibitishwa kutoka kwa Mitume wa Yerusalemu kwenda kubatiza mwongofu. Ubatizo sio suala la kidhehebu bali ni suala la ufalme. Lazima tuwe makini na desturi za kimadhehebu ambazo zimetuzamisha katika tope zito na kuchafua maji ya Kibiblia! Je towashi alikuwa na wasiwasi wa kubatizwa?

1. jambo la kikabila/utaifa
2. jambo la kimwili
3. hali za kijamii na kiuchumi
4. jambo kuhusu Katekismus/ kushikiliwa kwa misimamo ya kidini

Vikwazo vyote vimeshushwa chini katika Jina la Yesu Kristo (kama vile Efe. 2:11-3:13). Mapenzi yoyote yaweza kuja (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum. 10:9-13)!

**8:37** Mstari huu unaowekwa katika kumbukumbu ya ukiri wa haujajumuishwa katika maandiko ya mafujo ya Kiyunani P<sup>45</sup> ( Mafujo ya Chester Beatty), P<sup>74</sup> (Mafujo ya Bodmer ), au maandiko ya Kiyunani ya Kale,  $\alpha$ , A, B, au C. Hakipo katika matoleo ya kale ya Vulgate, Syriac, Ki-koptik, Fasiri za Ki-kushi.

Mstari wa 37 sio wa asili katika Mdo. UBS<sup>4</sup> linatoa kuondolewa kwake alama ya "A", ikimaanisha ni hakika. Haijajumuishwa hata katika andiko la NASB (1970) lilihaririwa, Lakini haupo katika kuhuishwa kwake kwa mwaka 1995 ukuhisha kwa mabano.

**8:38-39 "wakatelemka majini.....walipopanda kutoka majini,"** Hili si andiko la udhibitisho wa kimaandiko kwa ajili ya kuzamishwa. Muktadha unamaanishwa walitembea katika mwili wa maji, na sio mbinu za ubatizaji. kuwa makini na msimamo wako na mafundisho ambayo ulishayapokea tayari kabla ya mimi kukwambia jambo hili!

**8:39 "Roho wa Bwana akamnyakua Filipo "** Ikiwa kutokea huku ni kule kwa kimiujiza kama kwa Eliya (kama vile 1 Wafalme 18:12; 2 Wafalme 2:16) au ule wa Ezekieli (kama vile Ezek. 3:14; 8:3) au ikifanya rejerea yake kwamba namna alivyopotea au kuondoka haraka hakuna uhakika. Roho kwa karibu sana alihusika katika kugeuzwa huku. Angalia pia kwamba ufuatiliaji mkubwa ka Katekisimu kwa uhalisia hakukuwepo, lakini Mwingofu alikuwa na gombo la Isaya na Roho akaaye ndani yake!

▣ **"basi alikwenda zake akifurahi"** Habari njema ni kwamba huwa inafuatana na furaha (Kama vile Mdo. 8:8). Ireaneus anaandika kwamba desturi zile ambazo Towashi huyu alikuwa mmishenari wa Injili kwa watu wake mwenyewe. Roho mwenyewe lazima alifanya ufuatiliaji na uanafunzi!

**8:40** Philipo aliendelea (kauli ya kati elekezi ya wakati usiotimilifu) huduma yake ya uinjilisti katika mji wake wa kifilisti na Ashdod (yaani *Azotus*) akiwa njiani kuelekea Kaisaria kwa njia ya bahari. Ni wazi kwamba Philipo alielewa maana ya kiulimwengu pana ya uwepo wa Wasamaria na Wa-kushi. Injili iliwajumuisha hata Wafilisti!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, hii ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Mungu aliruhusu mateso kulitokea kanisa la kwanza?
2. Kwanini Kuhubiriwa kwa Injili iliyokuwa ikihubiriwa kwa Wasamaria kulikuwa muhimu sana?
3. Je Simoni alikuwa ni Mwamini?
4. Kwanini Wasamaria hawakumpokea Roho mtakatifu wakati walipoamini?
5. Ni aina gani ya watu huyu Towashi anawakilisha?
6. Kwanini Mstari wa 37 hauandikwi katika Biblia zote?

## MATENDO YA MITUME 9

<b>MGAWANYO WA AYA ZA TAFSRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Kuongoka kwa Paulo 9:1-9	Akiwa Barabarani kuelekea Dameski: Sauli aliongoka 9:1-9	Kuongoka kwa Sauli huko Taso 9:1-9	Kuongoka kwa Sauli 9:1-2 9:3-4 9:5a 9:5b-6 9:7-9	Kuongoka kwa Sauli 9:1-2 9:3-9
9:10-19	Anania alimbatiza Sauli 9:10-19	9:10-19a	9:10a 9:10b 9:11-12 9:13-14 9:15-16 9:17-19a	9:10-12 9:13-19a
Sauli anahubiri huko Dameski 9:19b-22	Sauli Anamhubiri Kristo 9:20-22	9: 19b-22	Sauli Anahubiri humo Dameski 9:19b-20 9: 21 9:22	Mahubiri ya Sauli huko Dameski 9:19b-22
Sauli Anawakwepa Wayahudi 9:23-25	Sauli Anakikwepa Kifo 9:23-25	Ziara ya Kwanza huko Yerusalemu 9:23-25	9:23-25	9:23-25
Sauli akiwa Yerusalemu 9:26-30	Sauli akiwa Yerusalemu 9:26-30 Washindi wa Kanisa	9:26-30	Sauli akiwa ndani ya Yerusalemu 9:26-30	Ziara ya Sauli hadi Yerusalemu 9:26-30 Mfariji
9:31	9:31	9:31	9:31	9:31
Uponyaji wa Ainea 9:32-35	Ainea anaponywa 9:32-35	Safari ya Lida na Yafa 9:32-35	Petro aiona Lida kupitia Yafa 9:32-35	Petro anamponya mtu aliyepooza huko Yafa 9:32-35
Dorkasi Anarejeshewa Uhai 9:36-43	Dorkasi Anarejeshewa Uhai 9:36-43	9:36-43	9:36-43	Petro Aurudisha Uhai wa Mwanamke huko Yafa 9:36-43

## **KUSOMA MZUNGUKO WA TATU** (kutoka "[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)" ("[A Guide to Good Bible Reading](#)")

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA NDANI ZA KIMUKTADHA**

- A. Msistizo unaanza na mabadiliko ya mara ya pili toka
  1. kwa Mtume Petro hadi kwa Mtume Paulo
  2. kutoka Palestina hadi ulimwengu wa ki- Mediterranean
  3. Kutoka kwa Wayahudi hadi kwa Mataifa.
- B. Mabadiliko ya Paulo ni kipengele muhimu sana katika historia ya kanisa ambacho kimechukuliwa kumbukumbu mara tatu katika kitabu cha Matendo ya Mitume.
  1. Maelezo ya Luka, Matendo ya Mitume 9:1-30
  2. Maelezo ya Paulo mbele ya umati wa watu katika Yerusalemu, Matendo ya Mitume 22:3-16
  3. Maelezo ya Paulo mbele Agripa II huko Sisera, Matendo ya Mitume 26:4-18
  4. Pia Paulo kwa muhtasari anakitaja kipindi hiki hiki katika Gal. 1:13-1na 2 Kor. 11:32-33
- C. Ufanano uliopo kati ya ujumbe wa Stefano na ujumbe wa Paulo uko dhahiri. Paulo alianza kutawala Wayahudi wa Kiyunani ambao Stefano aliwahubiria. Paulo aliisikia hutoba ya Stefano ya Matendo ya Mitume 7 (kama vile Matendo ya Mitume 7:58; 8:1; 22:20). Inawezekana kwamba Paulo alikuwa mmoja wa viongozi wa Masinagogi ya Wayahudi wa Kiyunani humo Yerusalemu ambao walihojiana na Stefano na kumwondosha!
  1. Badhi ya sababu zenye nguvu katika mabadiliko ya Paulo ni
    1. Dini ya Kiyahudi kushindwa kuleta amani na furaha ya ndani
    2. maisha na mafundisho ya Yesu yalifahamika vema na kujadiliwa katika mizunguko ya kisheria za kidini (hasa Yerusalemu)
    3. huyu aliisikia hotuba ya Stefano na kushuhudia kifo chake (huenda hata huyu alimhoji Stefano)
    4. huyu aliuona mwenendo na imani ya Wakristo waliokuwa chini ya mateso
    5. kukabiliana kwake kiupekee na Bwana mfufuka kulibadilisha kila kitu

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 9:1-9**

<sup>1</sup>Lakini Sauli, akizidi kutisha na kuwaza kuwaua wanafunzi wa Bwana, akamwendea Kuhani Mkuu, <sup>2</sup>akataka ampe barua za kuenda Dameski zilizoandikwa kwa masinagogi, ili akiona watu wa Njia hii, waume kwa wake, awafunge na kuwaleta Yerusalemu. <sup>3</sup>Hata alipokuwa akisafiri, ikawa anakaribia Dameski; ghafula

ikamwagaza kote kote nuru kutoka mbinguni. <sup>4</sup>Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, Sauli, Sauli, mbona waniudhi? <sup>5</sup> Akasema, U nani wewe, Bwana? Naye akasema, Mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe. <sup>6</sup>Lakini simama, uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda. <sup>7</sup>Na wale watu waliosafiri pamoja naye wakasimama kimya, wakiisikia sauti, wasione mtu. <sup>8</sup>Sauli akainuka katika nchi, na macho yake yalipofumbuka, hakuona kitu; wakamshika mkono wakamleta mpaka Dameski. <sup>9</sup> Akawa siku tatu haoni; hali, wala hanywi

**9:1 "Sauli, akizidi kutisha na kuwaza kuwaua"** Kiuhalisia hili ni neno linalomaanisha "kuongeza shari." Katika Matendo ya Mitume 26:11, Paulo anajizungumzia yeye mwenyewe, kwamba akiwa na hasira sana alighadhabishwa kuwahuu. Kwa uwazi kabisa Paulo hata aliwauwa baadhi ya Wakaristo kama (vile Matendo ya Mitume 8:1).

☐ **"wanafunzi wa Bwana"** Neno hili linamaanisha wale wanaojifunza. Hili linaonekana katika Injili ya kitabu cha Matendo ya Mitume pekee. Neno hili linaweza kuwa mbadala wa neno "watakatifu." Tambua idadi ya maneno yaliyotumika ndani ya sura hii kuwabainisha watu wa Mungu:

1. wanafunzi, Matendo ya Mitume 9:1,10,19,25,26,36,38
2. Njia, Matendo ya Mitume 9:2
3. watakatifu, Matendo ya Mitume 9:13,32,41
4. ndugu, Matendo ya Mitume 9:17.

☐ **"akamwendea Kuhani Mkuu"** Kwa udhihirisho mkubwa hili ni rejeo linalorejelea juu ya Wakuu wa Sinagogi (kama vile Matendo ya Mitume 26:10). Angalia Maelezo yahusu Wakuu wa Sinagogi katika Matendo ya Mitume 4:5.

**9:2 "akataka ampe barua za kuenda Dameski"** Serikali ya Kirumi ilipewa mamlaka yenye mipaka kwa Wakuu wa Sinagogi kuendesha na kutawala matukio yaliyokuwa yakifanyika ndani ya masinagogi ama yaliyohusiana na maisha ya Wayahudi ndani ya Dora (kama vile I Mak. 15:16-21 ama Josephus, *Antiq.* 14.10.2). Dini ya Kiyahudi ni dini ya kisheria iliyotambuliwa na ulimwengu wa Wagiriki-Waroma. Inavyoonekana hizi zilikuwa ni barua za kukamatwa kwa Wakristo wa Kiyahudi waliokuwa wamekimbilia Yerusalemu katika kuepuka mateso ya Kiyahudi (kama vile Matendo ya Mitume 9:14,21; 22:5; 26:10).

☐ **"akiona"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la tatu yenye kumaanisha tendo muhimu.

☐ **"Njia hii"** Huu ndio uliokuwa utambulisho wa awali kwa waamini (kama vile Matendo ya Mitume 19:9,23; 22:4; 24:14,22 na huenda 18:25,26). Neno hili lina usuli wa kitabu cha Agano la Kale, huzungumzia maisha ya imani (kama vile Zab.1:1; 16:11; 119:105; 139:24; Mit.4:10-19). Yesu anatumia dhana hii katika Mt. 7:14 na anatumia sifa hii kujizungumzia Yeye Mwenyewe katika Yohana 14:6. Ukristo ni makabiliano binafsi yafuatiwayo na mahusiano ya kila siku.

☐ **"wake"** Kuwataja wanawake mara tatu kati ya makundi aliyoyatesa Paulo ni njia ya kuonyesha nguvu ya matendo ya Paulo (kama vile Matendo ya Mitume 8:3; 22:4). Luka analo sikitiko la kipekee kuwahuu wanawake!

**9:3 "Dameski"** Huu ulikuwa mji wa kale na makao makuu ya Jimbo la Kirumi huko Shamu ukiwa kaskazini/ama kaskazini mashariki mwa Galilaya. Ilikuwa maili 150 kutoka Yerusalemu.

☐ **"ghafula"** Hili neno pia lina maana nyingine ya kile "kisichotarajiwa"

☐ **"nuru kutoka mbinguni"** Paulo anahusianisha uzoefu wake pamoja na nuru hii iliyokuwa ya tofauti ndani ya maelezo yake ya aina tatu kutokana na ufahamu wake katika Matendo ya Mitume

1. "ikamwangaza kote kote nuru kutoka mbinguni" (Matendo ya Mitume 9:3)
2. "ghafula nuru kuu ilitoka mbinguni, ikanimulikia pande zote" (Matendo ya Mitume 22:6)
3. "naliona nuru inatoka mbinguni ipitayo mwangaza wa jua, ikinimulikia mimi, na wale waliofuatana nami pande zote" (Matendo ya Mitume 26:13)

Kwa uwazi Paulo alilikumbuka tukio hili! Yawezekana kwamba nuru hii kithiolojia/kimwonekano ilihusiana na *Shekinah wingu la utukufu la uwepo wa YHWH* pamoja na Israeli wakati wa Kipindi cha Kutangatanga Nyikani. Dhana ya kithiolojia ya neno "utukufu" inachukuwa kipengele cha nuru anga'avu kutokana na tukio (angalia [MADA MAALUM: UTUKUFU \(DOXA\)](#) katika Matendo ya Mitume 3:13). Nuru hii ingalimwonyesha Sauli mwalimu wa dini ya Kiyahudi kuwa huu ulikuwa uwepo binafsi wa Mungu.

**9:4"akasikia sauti"** Hii sauti ya mbinguni ilikuwa ni kitu ambacho dini ya Kiyahudi ilikuwa na utambuzi juu yake. Hii inajulikana kama *bathkol*. Kwa Wayahudi hii ilimaanisha kupokea ujumbe na /ama uthibitisho toka kwa Mungu (wakati wa kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya katikati ya ukimya wa Malaki [au Mambo ya Nyakati] na mwanzoni mwa huduma ya Yohana Mbatizaji). Muundo huu wa ufunuo ulikuwa wa muhimu kwa sababu hapakuwa na manabii waliovuviwa katika kipindi hiki.

☐ "Sauli, Sauli" Katika lugha ya Kiebrania kurudia rudia jina ilikuwa njia ya kuonyesha msistizo (ukali).

☐ "**mbona waniudhi**" Hili kithiolojia ni la muhimu zaidi kwa sababu linaonyesha mwendelezo na ukaribu kati ya Yesu na kanisa lake (kama vile Mt. 10:40; 25:40,45). Paulo alilitesa Kanisa, lakini Yesu alilichukulia hili kwa upekee. Kutokana na Matendo ya Mitume 26:14 tunafahamu kuwa Agano Jipya kulihusu kanisa:

1. mwili
2. familia
3. kujenga
4. watakatifu

Yote haya yanasistiza asili ya ushirika wa imani (kama vile 1 Kor. 12:7). Inaanza kwa upekee, lakini inaenda hadi kufikia kundi (utambuzi na uhusiano). Huu ushirika wa kipekee unaweza kuonekana ndani ya mjadala wa Paulo juu ya Adamu na Kristo katika Rum. 5:12-21. Moja ni sehemu ya yale yote; moja linaweza kuathiri yote (kama vile Yohana 7).

**9:5a "U nani wewe, Bwana"** Je! Paulo alimaanisha nini kwa kutumia neno "Bwana"?

1. Bwana, jina la heshima (mf. Yohana 4:11)
2. Jina YHWH, linatafsiriwa kama Bwana katika kitabu cha agano la Kale (mf. Mwa. 2:4) Ikiwa mshangao ndiyo mtazamo, kisha kwa uwezekano kabisa #1 unatumika, lakini ikiwa nuru kutoka mbinguni inadokeza tendo la Mungu, kwa hiyo #2 ndiyo wa kweli. Ikiwa #2, baadaye thiolojia ya sheria za Kiyahudi, Paulo ilibadilika ghafla. Ni aina gani ya mkanganyiko na kipindi cha kuogofya kingeweza kuwa! Angalia [MADA MAALUM: MAJINA YA MIUNGU](#) katika Matendo ya Mitume 1:6.

**9:5b-6b** Mistari hii haipatikani katika machapisho yoyote ya kale ya Kiyunani. Hii inapatikana pekee ndani ya machapisho ya Kilatini. Erasmus, akitafsiri kutoka katika Toleo la Kilatini, anaiweka mistari hii katika toleo lake la kwanza la Agano Jipya la Kiyunani katika 1516. Maneno haya yanapatikana katika Matendo ya Mitume 26:14. Kuhusishwa kwake hapa kunaonyesha uelekeo wa maandishi kufanya ufanano sawa na maelezo kamili ya undani wote.

**9:5 "Mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe"** Paulo anadai kumuona Kristo Aliyetukuzwa (kama vile Matendo ya Mitume 22:14; 1 Kor. 9:1; 15:8-9). Baadaye Paulo aliweza kuwa na ufahamu wa sehemu hii muhimu ya wito wake wa kuwa Mtume kwa Mataifa. Yule fundi seremala kutoka Nazarethi aliyesulibiwa ni Masihi aliyetukuzwa!

**9:6** Hili linaelezwa kwa undani katika Matendo ya Mitume 9:10-19

☐ **"yakupasayo kutenda"** Angalia maelezo kamili yahusuyo neno *dei* katika Matendo ya Mitume 1:16.

**9:7 "Na wale watu waliosafiri pamoja naye"** Bila shaka hili linamaanisha

1. askali wa Hekalu waliokuwa wamefuatana na Paulo
2. wakereketwa wengine wa Kiyahudi, huenda hawa wanatoka masinagogi ya wale walioshika sana mila na desturi za Kiyahudi
3. wanafunzi wengine wa kithiolojia kutoka Yerusalemu

☐ **"wakiisikia sauti, wasione mtu"** Kuna utofauti unaonekana kati ya Matendo ya Mitume 9:7 na 22:9 katika undani wa tukio hili. Kumekuwa na nadharia kadhaa zinaonyesha namna ya kulishughulikia hili:

1. Ni suala la sarufi muundo. Kitenzi "kusikia" kinaweza kuchukua umilikishi (Matendo ya Mitume 9:7) au hali ya kushutumu (Matendo ya Mitume 22:9). Hii miundo tofauti ina maana tofauti au maana nyingine. Toleo la NRSV, katika tanbihi, lina "Mapendekezo ya Kiyunani kwamba wale waliokuwa wamefuatana naye waliisikia sauti, lakini wasiyasikie maneno yaliyozungumzwa."
2. Wengine wanasema hii ni sawa na Yohana 12:29-30 kuhusu kuingia kwa Yesu humo Yerusalemu na sauti iliyotoka mbinguni.
3. Wengine wanasema kwamba ni sauti ya Paulo inayorejelewa, si Yesu. Hawa walimsikia Paulo akizungumza, lakini hawakumsikia Yesu akizungumza.
4. Wengine wanasema hili ni sawa na tatizo la Injili za Muhtasari. Waandishi tofauti wa Injili wanachukua kumbukumbu ya matukio haya haya, hotuba, na matendo ya Yesu katika kutofautisha, ambayo ni maelezo ya tofauti ya ushahidi wa macho.

**9:8 "na macho yake yalipofumbuka, hakuona kitu"** Kwa uthibitisho kabisa Paulo alikuwa na matatizo ya macho kuanzia wakati huo (kama vile Gal. 4:13-15; 6:11). Mimi, binafsi, naamini "mwiba uliokuwa ndani ya mwili" wa Paulo (kama vile 2 Kor. 12:7-10; Gal. 4:13-15; 6:11) ni ugonjwa ulioanzia Mashariki, bila shaka ulisababishwa na hali hii. Hapa kuna kejeli; Paulo alikumbana na matatizo mbalimbali. Yeye alifikiri kuwa angeona (kimwili na kiroho, kama vile Yohana 9), lakini alijikuta akiwa kipofu. Baada ya kukutana na Kristo alikuwa kipofu wa mwacho kwa kipindi fulani, lakini macho haya ya kiroho yalikuwa wazi kwa upana!

**9:9 "Akawa siku tatu haoni"** Hii ni kauli yenye msistizo isiyotimilifu. Baadhi ya watoa maoni wanaliona hili kama tukio la maono ya Paulo ya mbinguni yaliyonukuliwa katika 2 Kor. 12:1-4.

☐ **"hali, wala hanywi"** Paulo alikuwa akifunga na kuomba (kama vile Matendo ya Mitume 9:11). Ni uanzilishi wa tatizo la namna gani ambavyo lazima yangetokea ndani ya fikra za Paulo (thioljia) na moyo (shauku)! Alianza mabadiliko kutoka katika hali ya kuwa mtesaji wa injili hadi kuwa mhubiri wa injili!

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 9:10-19a**

<sup>10</sup>Basi palikuwapo Dameski mwanafunzi jina lake Anania. Bwana akamwambia katika maono, Anania. Akasema, Mimi hapa, Bwana. <sup>11</sup> Bwana akamwambia, Simama, enenda zako katika njia iitwayo Nyofu, ukaulize katika nyumba ya Yuda mtu aitwaye Sauli, wa Tarso; maana, angalia, anaomba; <sup>12</sup> naye amemwona mtu, jina lake Anania, akiingia, na kumwekea mikono juu yake, apate kuona tena. <sup>13</sup> Lakini Anania akajibu, Bwana, nimesikia habari za mtu huyu kwa watu wengi, mabaya mengi aliyowatenda watakatifu wako Yerusalemu; <sup>14</sup> hata hapa ana amri itokayo kwa wakuu wa makuhani awafunge wote wakuitiao Jina lako. <sup>15</sup> Lakini Bwana akamwambia, Nenda tu; kwa maana huyu ni chombo kiteule kwangu, alichukue Jina langu

mbele ya Mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli. <sup>16</sup>Maana nitamwonyesha yalivyo mengi yatakayompasa kuteswa kwa ajili ya Jina langu. <sup>17</sup>Anania akaenda zake, akaingia mle nyumbani; akamwekea mikono akisema, Ndugu Sauli, Bwana amenituma, Yesu, yeye aliyekutokea katika njia uliyojijia, upate kuona tena, ukajazwe Roho Mtakatifu. <sup>18</sup> Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona, akasimama, akabatizwa; <sup>19</sup>akala chakula, na kupata nguvu.

**9:10**"Anania" Jina hili linamaanisha "YHWH ni mwenye rehema." Kwa udhihirisho huyu alikuwa Myahudi mwenye sifa njema, hakuwa mkimbizi (kama vile Matendo ya Mitume 22:12).

☐"**Mimi hapa, Bwana**" Hii ni nahau ya Kiyahudi ya upatikanaji (kama vile Isa. 6:8). Mstari wa 11 kwa hakika unatolewa kwa vitendo kwa sababu ni agizo la kipekee sana.

**9:12**"naye amemwona mtu, jina lake Anania" Kifungu kielezeacho "Katika maono" hakiko katika machapisho ya kale ya Kiyunani P<sup>74</sup>, § na A, bali kiko katika MSS B na C. Toleo la UBS<sup>4</sup> linaweka usomaji mfupi sana katika maandiko lakini unalipa daraja "C" (kwa ugumu katika usomaji). Mstari huu unaonyesha kwamba ujio wa Anania, matendo, na ujumbe vilithibitisha maneno ya Yesu ya awali kwa Paulo (kama vile Matendo ya Mitume 9:6)

☐"**kumwekea mikono juu yake**" Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 6:6.

**9:13**"nimesikia habari za mtu huyu kwa watu wengi" Ni dhahiri kuwa Anania alisikia habari mbaya juu ya ukali wa mateso ya Paulo kwa waamini waliokuwa wakimbizi wa Kiyahudi kutoka Yerusalemu.

☐"**watakatifu wako**" Hili neno *hagioi linahusiana na neno la Kiyunani "takatifu" (hagios)*. Usuli wa Agano la Kale (*kadosh*) unahusiana na kitu fulani, mtu fulani, ama eneo lililotengwa na Mungu kwa ajili ya kazi maalim. Hili neno "watakatifu" mara nyingi ni wingi, isipokuwa mara moja katika Flp. 4:21, lakini pia kuna muktadha wa wingi. Kuwa Mristo ni kuwa sehemu ya familia, jamii. Katika imani hakuna walio na upweke.

## **MADA MAALUM: WATAKATIFU (*hagios*)**

Huu ni usawa wa Kiyunani wa neno la Kiebrania *kadosh* (NOUN, BDB 871; VERB, BDB 872, KB 1066-1067; tazama Mada Maalum: Takatifu), lililo na maana ya msingi ya kumweka mtu katika usawa, kitu fulani, au baadhi ya sehemu tofauti na matumizi ya YHWH yaliyojitenga. Hili linadokeza dhana ya Kiingereza ya "wekwa wakfu." Israeli lilikuwa "taifa takatifu" la YHWH (kama vile 1 Pet. 2:9, ambayo inanukuu Kut. 19:6). YHWH anaweka mbali na ubinadamu kwa kutumia asili Yake (milele, Utakatifu usioumbwa) na sifa Yake (ukamilifu wa maadili). Yeye ni kipimo ambapo vitu vyote vinapimwa na kuhukumiwa. Yeye yu kila mahali, Mtakatifu, Mtakatifu wa Watakatifu.

Mungu aliwaumba wanadamu kwa ushirika, lakini anguko (Mwanzo 3) lilisababisha kikwazo cha mahusiano na maadili kati ya Mungu Mtakatifu na mwanadamu mdhambi. Mungu alichagua kuurejesha ufahamu Wake wa uumbaji; hivyo, Anawaita watu Wake kuwa "watakatifu" (kama vile Law. 11:44; 19:2; 20:7,26; 21:8). Kwa imani uhusiano wa YHWH na watu Wake ukawa mtakatifu kwa nafasi zao za kiagano ndani Yake, lakini pia wanaitwa kuishi maisha matakatifu (tazama Mada Maalum: Utakaso, kama vile Mt. 5:48; Efe. 4:1,17; 5:2-3,15; 1 Pet. 1:15).

Huku kuishi kitakatifu kunawezekana kwa sababu waamini wamekubaliwa kwa utimilifu na kusamehewa kupitia (1) Maisha ya Yesu na (2) kazi na uwepo wa Roho Mtakatifu ndani ya fikra na mioyo yao. Hili linahimarisha hali ya ukinzani kwa waamini:

1. kuwa watakatifu kwa sababu ya haki ya Kristo iliyowekwa ndani yao (kama vile Warumi 4)
2. walioitwa kuishi kitakatifu kwa sababu ya uwepo wa Roho (tazama Mada Maalum: Utakaso)



Waamini ni "watakatifu" (*hagioi*) kwa sababu ya

1. mapenzi ya yule Aliye Mtakatifu (Baba, kama vile Yohana 6:29,40; 1 Pet. 1:15-16)
2. kazi ya Mwana aliye Mtakatifu (Yesu, kama vile 2 Kor. 5:21; 1 Pet. 1:18-21)

uwepo wa Roho Mtakatifu akaaye ndani (kama vile Rum. 8:9-11,27)

Mara nyingi katabu cha Agano Jipya kinawarejelea watakatifu kama WINGI (isipokuwa mara moja katika Flp. 4:21, lajkini muktadha unalifanya neno hili kuwa WINGI). Kuokolewa ni kuwa sehemu ya familia, mwili, ujenzi! Imani ya kibiblia huanza na mapokezi binafsi, bali suala li ndani ya ushirika wa pamoja. Kila mmoja wetu amekirimiwa kama vile 1 Kor. 12:11) kwa ajili ya afaya, ukuaji, na manufaa ya Mwili wa Kristo—kanisa (kama vile 1 Kor. 12:7). Tumeokolewa ili kutumika! Utakatifu ni sifa ya familia!

Hili linakuwa adimu kwa waamini (kama vile Matendo ya Mitume 9:13,32,41; 26:10; Rum. 1:7; 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Efe. 1:1; Flp. 1:1; Kol. 1:2) na njia ya kuonyesha huduma kwa wengine (kama vile Rum. 12:13; 16:2; Efe. 1:15; Kol. 1:4; 1 Tim. 5:10; Ebr. 6:10). Paulo alichukua wakati wa kipekee wa kujitua kwa makanisa Mataifa kwa watu wahitaji waliokuwa ndani ya Kanisa Mama ndani ya Yerusalemu (kama vile Rum. 15:25-26; 1 Kor. 16:1; 2 Kor. 8:4; 9:1).

**9:14 "wakuu wa makuhani"** Katika Agano la Kale ukuhani mkuu ulikuwa ni wa milele na ulipitia katika familia maalum ya mwana wa ki-Kuhani (kama vile Law. 8-10). Hata hivyo, wakati wa kipindi cha Kirumi nafasi hii ilipatikana kutoka kwa maafisa wa Kirumi. Kwa hiyo, kulikuwa na Makuhani Wakuu kadhaa ndani ya familia ya ki-Sadukayo ya Anasi.

☐ **"wakuitiao jina lako"** Kifungu hiki kina maana muhimu za kithiolojia. Luka anakitumia mara kadhaa katika kitabu cha Matendo ya Mitume kwa ajili ya

1. yule aliyefundisha kuhusu habari za Yesu (kama vile Matendo ya Mitume 7:59)
2. yule aliyemkubali Yesu kama Mwokozi (kama vile Matendo ya Mitume 9:14,21)
3. nukuu ya Agano la Kale kutoka Amosi 9:12, ambapo inamrejelea yule ambaye jina la YHWH linaitwa (yaani, waamini, kama vile Matendo ya Mitume 15:17)
4. Njia ya mtu kukiri kwa uwazi imani yake katika Yesu (kama vile Matendo ya Mitume 22:16) Kifungu hiki pia ni sehemu ya ombi la Paulo juu ya Israeli kutoka Yoeli 2:32 katika Rum. 10:9-13 (kama vile 2 Tim. 2:22). Petro anakitumia kifungu hiki hiki (Yoeli 2:28-32) katika hotuba yake siku ya Pentekoste na kuwaalika wale waliokuwepo "kulisihi jina la Bwana" kutoka Yoeli 2:32. Jina husimama badala ya mtu. Kwa kuliitia jina, wenye dhambi humsihi Yesu kutenda badala yao na kuwajumuisha ndani ya familia Yake. Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:22.

**9:15 "Nenda"** Hii ni kauli ya kati shurutishi (yenye ushahidi ) ya wakati uliopo. Kwa mamlaka Yesu alimtuma Anania ambaye hakuwa tayari kutumwa kwa Sauli.

☐ **"kwa maana huyu ni chombo kiteule kwangu"** Oh, hii ni neema na upendeleo mkuu wa Mungu! Paulo si kielelezo kizuri cha mfano wa kujitolea kwa hiari katika injili, mabadiliko ya hiari. Huyu alitwa kwa ushahidi!

**NASB, NKJV** "mbele ya Mataifa"

**NRSV, NJB** "kulijulisha jina langu mbele ya Mataifa"

**TEV** "kulitangaza jina langu mbele ya Mataifa"

Ni usemi gani wa mwanzo wa kumwambia Myahudi (kama vile Efe. 3:7)! Bado, mara nyingi huu umekuwa mpango wa Mungu (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5-6; Efe. 2:11-3:13, angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume

1:8). Israeli kilikuwa chombo pekee cha kuufikia ulimwengu, kilichoumbwa kwa sura na mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27), lakini kilichoanguka (kama vile Mwa. 3:15).

☑️"**na wafalme**" Paulo alikuwa akizungumza na viongozi wa kiserikali, wakubwa kwa wadogo, na hatimaye Kaizari!

☑️"**na wana wa Israeli**" Mtiririko wa utaratibu wa umisheni wa Paulo ulikuwa ni kuhubiri kwanza ndani ya sinagogi la wenyeji (kama vile Rum. 1:16) katika kila mji. Hili liliwapa nafasi Wayahudi na wale wacha- Mungu ambao waliifahamu nafasi ya Agano la Kale kuwa na mwitikio wa awali wa injili. Kisha ungerudi kwa wale ambao walikuwa hawamjui Mungu (wapagani).

**9:16"Maana nitamwonyesha yalivyo mengi yatakayompasa kuteswa kwa ajili ya Jina langu"** Kuteswa hakukwepeki, bali ni desturi ya Mristo katika ulimwengu huu ulioanguka (kama vile Mt. 5:10-12; Yohana 15:18-21; 16:1-2; 17:14; Matendo ya Mitume 14:22; Rum. 5:3-4; 8:17-18; 2 Kor. 4:7-12; 6:3-10; 11:24-33; Flp. 1:29; 1 The. 3:3; 2 Tim. 3:12; Yakobo 1:2-4; 1 Petro 4:12-16). Kuna uhusiano wa kithiolojia kati ya mateso ya Mkristo na wafuasi Wake katika ufalme huu ulioanguka. Kitabu cha 1 Petro kinaonyesha ufanano huu.

1. Kuteswa kwa Yesu, 1 Pet. 1:11; 2:21,23; 3:18; 4:1,13; 5:1
2. Wafuasi Wake, 1 Pet. 1:6-7; 2:19; 3:13-17; 4:1,12-19; 5:9-10

Ikiwa ulimwengu ulimkataa utayakataa yaliyo yake 7:7; 15:18-19; 17:14).

**9:17"akamwekea mikono"** Hakuna msingi wa kimaandiko kuhusu dhana ya "mamlaka ya kitume" katika kukirimia karama za kiroho. Anania ni mwekea mikono asiyejulikana ndani ya Dameski ambaye alikuwa

1. Msemaji wa Mungu na mwakilishi
2. Kujazwa Roho Mtakatifu kwa Paulo (kama vile Matendo ya Mitume 9:17)
3. Uponyaji wa kimwili wa Paulo (kama vile Matendo ya Mitume 9:18)
4. Ubatizo wa Paulo (kama vile Matendo ya Mitume 9:18)

☑️"**Ndugu Sauli**" Ni mfano gani ulio mkuu wa utii na pendo!

**9:18 "vikaanguka machoni pake vitu kama magamba"** Hili ni neno la kitabibu na la kiufundi la kubanduka kwa ngozi kutoka katika kidonda. Luka analitumia neno hili kueleza kile kilichojiri katika macho ya Paulo ndani ya wasaa huu wa uponyaji. Neno magamba linatumika kuzungumzia magamba ya samaki katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani (kama vile Law. 11:9,10,12; Kumb. 14:9). Upanuzi wa kistiari unaweza kuonekana katika Hes. 16:38, ambapo neno hili linatumika kuzungumzia vipande vya chuma vilivyoyeyushwa. Katika muktadha huu huenda hivi vilikuwa vipande vya ngozi au magamba ambayo yalidondoka kutoka katika macho ya Paulo.

☑️"**akabatizwa**" Kwa uwazi kabisa Anania pia alimbatiza Paulo (kama vile Matendo ya Mitume 8:36,38). Ubatizo wa Agano Jipya ulikuwa tendo la kuutii mfano wa Yesu (kama vile Mt. 3:13-17; Marko 1:9-11; Luka 3:21-22) na amri Zake (kama vile Mt.28:19.) Huu unaweka alama za badiliko la umiliki na utii.

**9:19a"akala chakula, na kupata nguvu"** Paulo alikuwa akifunga na kuoma tangu nuru ilipomwangaza kote kote (kama vile Matendo ya Mitume 9:9). Baada ya mfululizo wa siku tatu (bila kula wala kunywa), ilimpasa kuwa mdhaifu.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 9:19b-22**

<sup>19b</sup>Akawa huko siku kadha wa kadha pamoja na wanafunzi walioko Dameski. <sup>20</sup>Mara akamhubiri Yesu katika masinagogi, kwamba yeye ni Mwana wa Mungu. <sup>21</sup>Na wote waliosikia wakashangaa, wakasema, Siye huyu

**aliyewaharibu walioliitia Jina hili huko Yerusalemu? Na hapa alikuwa amekuja kwa kusudi hilo, awafunge na kuwapeleka kwa wakuu wa makuhani? <sup>22</sup>Sauli akazidi kuwa hodari, akawatia fadhaa Wayahudi waliokaa Dameski, akithibitisha ya kuwa huyu ndiye Kristo.**

**9:20"akamhubiri Yesu katika masinagogi"**Hii ni kauli tendaji elekezi. Hii inaweza kumaanisha (1) mwanzo wa tendo au (2) tendo lenye kurudiwa rudiwa. Ni kejeli ya namna iliyoje! Huyu alitangulia kupeleka barua kutoka kwa Wakuu wa Makuhani humo Yerusalemu hadi katika masinagogi yaliyoko Dameski ili kuwatesa wafuasi wa Yesu na sasa anakuja ndani ya masinagogi yale yale kwa ajili ya kumhubiri Yesu kama Masihi (kama vile mst. 21).

☐"**yeye ni Mwana wa Mungu**" Hapa ndipo palipo na matumizi pekee ya jina "Mwana wa Mungu" katika kitabu cha Matendo ya Mitume (isipokuwa kwa nukuu ya Zab. 2:7 katika Matendo ya Mitume 13:33). Usuli wake wa kitabu cha Agano la Kale unaaksi umuhimu wake: (1) taifa la Israeli (kama vile Hos.11:1); (2) Mfalme wa Israeli (kama vile 2 Sam. 7:14); na (3) Masihi (kama vile Mt. 2:15). Mkazo wa Paulo kumhusu Mungu Mmoja (angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:39) unafafanuliwa tena!

### **MADA MAALUMU: MWANA WA MUNGU)**

Hii ni moja kati ya nyadhifa kubwa alizopewa Yesu katika Agano Jipya. Ni wazi kabisa ina kidokezo cha Uungu. Inamjumuisha Yesu kama "Mwana" au "Mwana wangu," pia Mungu anaelezewa kama "Baba" (angalia Mada Maalum: Ubaba wa Mungu). Linatokea mara 124 katika Agano Jipya. Hata usanifu wa Yesu mwenyewe kama "Mwana wa Adamu" ina kidokezo cha Uungu toka Dan. 7:13-14

Katika Agano la Kale usanifu wa neno "Mwana" ingalirejea kwenye makundi maalumu manne (angalia Mada Maalum: "Wana wa.....")

- A. Malaika (mara nyingi iko katika hali ya WINGI, kama vile Mwa. 6:2; Ay. 1:6; 2:1)
- B. Mfalme wa Israel (kama vile 2 Sam. 7:14; Zab. 2:7; 89:26-27)
- C. Taifa la Israel kwa pamoja (kama vile Kut. 4:22-23; Kumb. 14:1; Hos. 11:1; Mal. 2:10)
- D. Waamuzi wa Israel (kama vile Zab. 82:6)

Ni utumiaji wa mara ya pili ambao unahusianishwa na Yesu. kwa njia hii "Mwana wa Daudi" na "Mwana wa Mungu" semi zote zinahusianishwa na 2 Samwel 17; Zaburi 2 na 89. Katika Agano la Kale neno "Mwana wa Mungu" kamwe halitumiki hasa kwa Masihi, isipokuwa kama ni mfalme wa siku za kiamama kama mmoja wa "wapakwa mafuta" wa Israel. Hata hivyo, katika magombo ya bahari ya chumvi wadhifa unaohusiana na Masihi ni wa kawaida (angalia nukuu maalumu katika Dictionary of Jesus and the Gospels, uk. 770). Pia "Mwana wa Mungu" ni wadhifa wa Kimasihi katika miingiliano miwili ya kazi za mafunuo ya Kiyahudi (kama vile II Esdras 7:28; 13:32,37,52; 14:9 na I Enoch 105:2)

Mazingira ya nyuma ya Agano Jipya kama inavyorejereka kwa Yesu kwa uzuri imefupishwa kwa namna mbali mbali.

- 1. Uwepo wake kabla (kama vile Yohana 1:15-30; 8:56-59; 16:28; 17:5; 2 Kor. 8:9; Flp. 2:6-7; Kol. 1:17; Ebr. 1:3; 10:5-8)
- 2. Kuzaliwa kwake kwa njia ya pekee (kama vile Isa. 7:14; Mt. 1:23; Luk. 1:31-35)
- 3. Ubatizo wake (kama vile Mt. 3:17; Mk 1:11; Luk. 3:22. Sauti ya Mungu toka mbinguni ikiunganisha ufalme wa kifahari wa Zaburi 2 na mtumishi mwenye mateso wa Isaya)
- 4. Majaribu ya shetani (kama vile Mt. 4:1-11; Mk 1:12,13; Luk 4:1-13. Anajaribiwa kuuwekea mashaka uwana wake au kutimiliza kusudi lake kwa njia tofauti na ile ya msalaba.)
- 5. Uthibitisho wake na wale wakiri wasiokubalika
  - a. Mapepo (kama vile Mk 1:23-25; Luk 4:31-37,41; Mk 3:11-12; 5:7; angalia Mada Maalum: Pepo

[roho wachafu]

- b. Wasioamini (kama vile Mt. 27:43; Mk 14:61; Yohana 19:7)
- 6. Uthibitisho wake kupitia wanafunzi wake
  - a. Mt. 14:33; 16:16
  - b. Yohana 1:34,49; 6:69; 11:27
- 7. Uthibitisho wake mwenyewe
  - a. Mt. 11:25-27
  - b. Yohana 10:36
- 8. Utumiaji wake wa stiari ya kawaida ya Mungu kama Baba
  - a. Utumiaji wake wa neno *abba* kwa ajili ya Mungu
    - 1) Mk 14:36
    - 2) Rum 8:15
    - 3) Gal 4:6
  - b. Utumiaji wake wa sasa wa jina Baba (*patēr*) kuelezea uhusiano wake na Uungu.

Kwa ufupi, wadhifa wa neno "Mwana wa Mungu" una maana kubwa ya kithiolojia kwa wale waliolifahamu Agano la Kale na ahadi zake, lakini waandishi wa Agano Jipya waliogopeshwa kuhusu utumiaji wao na watu wa mataifa kwa sababu ya mazingira ya nyuma ya wapagani ya "miungu" ikiwachukulia wanawake na matokea ya watoto kuwa "majitu."

**9:21** Mstari huu umo ndani ya muundo wa swali linalotarajia jibu la "ndiyo".

☐ "**aliyewaharibu**" Neno hili adimu lenye maana ya kuangamiza, kusababisha madhara, ama kuharibu moja kwa moja. Neno hili linapatikana hapa tu na katika Gal. 1:13,23 katika Agano Jipya na katika IV Mak. 4:23. Paulo alikuwa mtesajiwa kikatili sana!

**9:22**

**NASB** "Sauli akazidi kuwa hodari"

**NKJV** "Sauli akaongeza nguvu zote"

**NRSV** "Sauli akazidi kuongeza nguvu zaidi"

**TEV** "Mahubiri ya Sauli yakazidi kuwa na nguvu"

**NJB** "Nguvu ya Sauli ikaongezeka mara"

Hii ni kauli tendewa elekezi ya wakati usiotimilifu. Hii mara nyingine inachukua nafasi ya karama za Sauli na ujuzi wa kuendelea. Katika muktadha hili linarejelea juu ya mahubiri ya Paulo na ule ujuzi wa mahojiano (kama vile TEV).

☐ "**akawatia fadhaa**" Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati usiotimilifu ambayo inadokeza tendo lenye kurudiwa rudiwa katika wakati uliopita. Hili ni neno ambatani linalotokana na neno "kwa pamoja" (*sun*) na "kumimina" (*cheō*). Neno hili linapatikana katika Matendo ya Mitume pekee.

1. Matendo ya Mitume 2:6, shikwa na fadhaa
2. Matendo ya Mitume 9:22, tiwa na fadhaa
3. Matendo ya Mitume 19:32, machafuko
4. Matendo ya Mitume 21:27, taharakisha
5. Matendo ya Mitume 21:31, machafuko

Wayahudi wasingeeleza juu ya mabadiliko ya Paulo au mahubiri yake yenye nguvu yaliyomhusu Yesu kama Masihi wa Agano la Kale aliyeahidiwa.

☐ **"akithibitisha"** Neno hili linamaanisha kuhusisha (kama vile Matendo ya Mitume 16:10; 19:33) na kwa upanuzi, kuhakikisha. Mbinu ya Paulo ilifanana sana na ile ya Stefano. Wote walitumia vifungu na ukamilifu wao katika maisha ya Yesu wa Nazarethi kuthibitisha kwamba Yeye alikuwa Masihi aliyeahidiwa katika Agano la Kale.

☐ **"ndiye Kristo"** Hii ni njia ya kumrejelea Masihi (Aliyemiminiwa Mafuta, Yule Ajaye Aliyeahidiwa, angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:31). Mara nyingi katika Matendo ya Mitume kibainishi cha wazi hutangulia nomino (mf. Matendo ya Mitume 2:31,36;3:18,20). Sauli alikuwa akieleza kwa nguvu mtazamo kwamba Yesu wa Nazarethi, aliyewa humo Yerusalemu, alikuwa Mwana wa Mungu kweli, Masihi. Ikiwa hili lilikuwa la kweli, linabadilisha kila kitu kwa Wayahudi (na Mataifa)! Hawakumwelewa na pia walimkataa. Hawa wameikosa neema ya Mungu na kubaki ndani ya giza la kiroho na uhitaji.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 9:23-25**

<sup>23</sup>Hata siku nyingi zilipopita, Wayahudi wakafanya shauri ili wamwue; <sup>24</sup>lakini hila yao ikajulikana na Sauli. Wakamvizia malangoni mchana na usiku wapate kumwua. <sup>25</sup>Wanafunzi wake wakamtwaa usiku wakamshusha ukutani, wakimtelemsha katika kapu.

**9:23**"Hata siku nyingi zilipopita" Yatupasa kuyachukulia maelezo binafsi ya Paulo yanayopatikana katika Gal.1:15-24, ambapo alitumia kipindi cha muda mrefu akiwa Arabia. Katika muktadha huu, Arabia inarejelea ile himaya ya Nabataen (iliyotawaliwa na Aretas IV, ambaye alitawala kuanzia 9 k.k. hadi 40 b.k.) bado ni kusini mashariki ya Dameski. Hiki kipindi cha miaka mitatu huenda kinaaksi mahali fulani panapokaribia na miezi kumi na minane. Wayahudi waliihesabu nusu siku kama siku mzima (kama vile Matendo ya Mitume Mt. 26:61; 27:40,63); hesabu hii pia ilitumika kuhesabu miaka.

☐ **"Wayahudi wakafanya shauri ili wamwue"** Ni dhahiri kuwa Wayahudi walizichochea mamlaka za kisheria (kama vile 2 Kor. 11:32-33). Hili lazima lingekuwa fedheha kwa Paulo kwa sababu analitaja tukio hili katika kila mjadala wake uliohusu udhaifu wake katika 2 Wakorintho 11.

**9:25**"wakamshusha ukutani" Hili lazima lirejeele ule mlango uliokuwa katika nyumba binafsi ambayo ukuta wake ulikuwa sehemu ya ukuta uliokuwa umezunguka mji (kama vile 2 Kor. 11:33; Yos. 2:15; 1 Sam. 19:12).

**ADIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 9:26-30**

<sup>26</sup>Na Sauli alipofika Yerusalemu, alijaribu kujiunga na wanafunzi, nao walikuwa wakimwogopa wote, wasiadiki ya kuwa yeye ni mwanafunzi. <sup>27</sup>Lakini Barnaba akamtwaa, akampeleka kwa mitume, akawaeleza jinsi alivyomwona Bwana njiani, na ya kwamba alisema naye, na jinsi alivyohubiri kwa ushujaa katika Dameski kwa jina la Yesu. <sup>28</sup>Naye akawa pamoja nao katika Yerusalemu akiingia na kutoka. <sup>29</sup>Akahubiri kwa jina la Bwana kwa ushujaa, akinena na kuhojiana na Wayahudi wa Kiyunani. Nao wakajaribu kumwua. <sup>30</sup>Lakini ndugu walipopata habari wakamchukua mpaka Kaisaria, wakampeleka aende Tarso.

**9:26**"alipofika Yerusalemu" Kwa udhihirisho kabisa ilikuwa ni baada ya miezi therathini na sita baadaye (kama vile Gal. 1:15-24). Mstari huu unaonyesha kiwango cha nadharia ya kushuku ambapo waamini wa Yerusalemu walimtambua mtesi wao wa hapo awali. Kwa udhihirisho kitabu cha Matendo ya Mitume kinanukuu ziara kadhaa za Paulo huko Yerusalemu baadaya ushahidi wa kubadilika kwake.

1. Matendo ya Mitume 9:26, ziara ya kwanza
2. Matendo ya Mitume 11:30, ziara ya faraja
3. Matendo ya Mitume 12:25, baada ya umisheni
4. Matendo ya Mitume 15:2, Baraza la Yerusalemu
5. Matendo ya Mitume 18:22, ziara fupi kwa kanisa

6. Matendo ya Mitume 21:17, ziara iliyomuhusisha Yakobo pia na wazee wote na kusababisha watu wa Nazarethi kufurahia na pia kusababisha kukamatwa kwao

**9:27 "Barnaba"** Maana inayofahamika sana, ingawa si ile ya asili ya neno, ilikuwa "Mwana wa Faraja." Huyu alikuwa mwema sana na ametajwa huko nyuma katika Matendo ya Mitume 4:36 ambaye baadaye alikuja kuwa mfuasi wa Paulo wa kwanza wa kimisionari. Angalia maelezo kamili na Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 4:36.

☑ **"akampeleka kwa mitume"** Maelezo mengine ya kipekee ni Wagalatia 1:18.

☑ **"akawaeleza"** Barnaba alifahamu na kushiriki ushuhuda wa Sauli. Hili lilifungua mlango wa kukubalika kwake (kama vile Matendo ya Mitume 9:28).

**9:28**

**NASB** "akawa pamoja nao"

**NKJV** "akaingia na kutoka"

**NRSV** "akienda huku na huko"

**TEV** "akatembea maeneo yote"

**NJB** "akazunguka maeneo yote"

Hii ni nahau ya Agano la kale ya maisha ya kila siku au kazi (kama vile Hes. 27:17; 1 Flp. 3:7).

**9:29 "akinena na kuhojiana na Wayahudi wa Kiyunani"** Hili linarejelea juu ya kundi hilo hilo (masinagogi ya Wayahudi waliozungumza lugha ya Kiyunani humo Yerusalemu) la wale waliomuua Stefano; na sasa walikuwa wakipanga kumuua Sauli, ambaye pia alikuwa Myahudi kutoka katika mataifa mengine. Hawa lazima wangefikiri kuwa Stefano karudi!

**9:30 "ndugu walipopata habari"** Kutokana na 22:17-21 tunajifunza kwamba Yesu alijitokeza kwa Paulo kwa wakati huo kumwambia kukimbilia Yerusalemu. Yesu alijitokeza kwa Paulo mara kadhaa nyakati za huduma yake kumpa faraja na kumwongoza (kama vile Matendo ya Mitume 18:9-11; 22:17-21; na malaika wa Bwana katika 27:23).

☑ **"Kaisaria"** Jina hili linarelea ile bandari ya Kirumi iliyoko ng'ambo ya Palestina. Haya yalikuwa makao makuu rasmi ya serikali ya Kirumi.

☑ **"Tarso"** Paulo anatoweka machoni sasa kwa miaka kadhaa kutoka katika mji wa nyumbani. Tarso ulikuwa mji huru. Pia lilikuwa eneo la tatu kwa ukubwa kwa kujifunzia katika ulimwengu wa kale, nje ya Iskandria na Athens. Vyuo vya Elimu ya Juu vilivyokuwa humo Tarso vilisitiza juu ya falsafa, ufasaha wa kusema na sheria. Paulo alikuwa akijifunza vyote katika ufasaha wa kusema Kiyunani na falsafa pamoja na sheria za Dini ya Kiyahudi.

### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 9:31**

<sup>31</sup> Basi kanisa likapata raha katika Uyahudi wote na Galilaya na Samaria, likajengwa, likiendelea na kuongezeka katika kicho cha Bwana, na faraja ya Roho Mtakatifu.

**9:31** Huu ni mstari wa kimuhtasari ambao unahitimisha maelezo yakuongoka kwa Paulo na kuanza kuzungumzia safari za Petro. Luka anatomia mistari ya kimuhtasari mara nyingi katika Matendo ya Mitume. Angalia Introduction IV Purpose and Structure, A.

☑ **"kanisa"** Angalia maelezo na Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 5:11 na nukuu namna umoja wa neno "kanisa" unavyorejelea juu ya mikusanyiko mingi ya watu. Hili neno "kanisa" linaweza kudokeza kanisa la wenyeji (mf. Kol. 1:18,24; 4:15,16), makanisa yote ya mahali (mf. Efe. 1:22; 3:10,21; 5:23,24,25,27,29,32), na makanisa

yote kiulimwengu (mf. Mt.16:18).

■ *Tambua mambo aliyoyachagua* Luka kuyataja.

1. amani kwa makaisa yote
2. kukua na kuongezeka
3. faraja kutoka kwa Roho Mtkatifu

Ni mabadiliko yaliyoje yaotokanayo na mateso ya Matendo ya Mitume 8:1! Bado kuna matatizo, lakini Mungu amekutana na kila hitaji!

## MASWALI YA MJADALA

Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Paulo alikuwamkali katika katika kulitesa kanisa?
2. Kwa nini kuna maelezo mara tatu ya kuongoka kwa Paulo katika kitabu cha Matendo ya Mitume?
3. Kuna umuhimu gani wa Paulo kuzungumziwa, kuwekewa mikono, na kubatizwa na Anania?
4. Ni uhumu gani wa Paulo kumtumia Yesu kama "Mwana wa Mungu"?
5. Kwa nini Luka hakuinukuu miaka mitatu ya Paulo ya kuzuru Arabia?

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 9:32-10:48

- A. Ingawa kitabu cha Matendo ya Mitume kinaanza na mabadiliko kutoka kwa Petro hadi kwa Paulo, kitabu cha Matendo ya Mitume 9:32-12:25 kinaonyesha mzunguko wa huduma ya Petro.
- B. Sehemu hii inahusika na Petro akiwa huko Lida, Matendo ya Mitume 9:32-35; Yafa, Matendo ya Mitume 9:36-43, 10:9-23; Kaizaria, Matendo ya Mitume 10:1-8, 23-48; na huko Yerusalemu, Matendo ya Mitume 11:1-18; 12:1-17.
- C. Sehemu hii ni muhimu zaidi kwa sababu inashughulika na mapambano endelevu dhidi ya umisheni wa Mataifa na sehemu ya Petro (kama mkuu wa kundi ta ki-Utume) katika mapambano hayo. Luka anaamini kuwa maelezo ya Korineli ni ya muhimu sana kama anavyoyarudia mara tatu katika sehemu hii.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 9 :32-35

<sup>32</sup>Hata Petro alipokuwa akizunguka-zunguka pande zote akawatelemkia na watakatifu waliokaa Lida.<sup>33</sup>Akamwona mtu mmoja huko, jina lake Ainea, mtu huyo amelala kitandani miaka minane; maana alikuwa amepooza.<sup>34</sup>Petro akamwambia, Ainea, Yesu Kristo akuponya; ondoka, ujitandikie. Mara akaondoka.<sup>35</sup>Na watu wote waliokaa Lida na Sharoni wakamwona, wakamgeukia Bwana.

9:32" Petro alipokuwa akizunguka-zunguka" Kwa uwazi kabisa Mitume walikuwa wakihubiri maeneo yote ya Palestina na nchi jirani.

☐ **"watakatifu"** Neno hili linatumika katika kitabu cha Matendo ya Mitume kulieleza kanisa. Angalia [MADA MAALUM : WATAKATIFU](#) katika Matendo ya Mitume 9:13. Hili neno "wanafunzi" kwa hali ya kawaida linaondolewa na neno "watakatifu." Hili neno linahusiana na neno la Agano la Kale "takatifu" na linamaanisha, "tenga pembeni" kwa ajili ya huduma ya Mungu. Hili halitumiki kamwe katika hali ya umoja isipokuwa mara moja katika Flp. 4:21, ambayo ni muktadha shirikishi. Hili linaonyesha kwamba kuwa mtakatifu inamaanisha kuwa "ndani ya jamii." Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 9:13. Waamini wote wanaitwa "watakatifu" katika Agano Jipya! Hii ni nafasi yetu katika Kristo inayosistizwa.

## **MADA MAALUM : UTAKATIFU WA AGANO JIPYA/UTAKASO**

Agano Jipya linadai kwamba pindi mwenye dhambi anapomgeukia Yesu katika toba na imani (kama vile Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21), mara moja anahesabiwa haki na kutakaswa. Hii ni nafasi yao mpya katika Kristo. Haki yake imewekwa ndani yao (kama vile Mwa. 15:6; Warumi 4). Wanahesabiwa haki na utakatifu (mambo ya kimahakama ya Mungu)

Lakini Agano Jipya pia linataka waamini wote kuwa katika utakatifu na utakaso. Hii yote ni nafasi ya kithilojia katika kazi aliyoimaliza Kristo na kuwaita wote kufanana na Kristo katika mienendo na matendo katika maisha ya kila siku. Kama ilivyo wokovu ni zawadi ya bure na kuyaghalimia maisha, vile vile pia, utakaso.

### Mwitikio wa awali

Matendo 26:18  
 Warumi 15:16  
 1 Wakorinto 1:2-3; 6:11  
 2 Wathesolanike 2:13  
 Waebrania 2:11; 10:10,14; 13:12  
 2 Petro 1:2

### Mwendelezo wa kufanana na Kristo

Warumi 6:19  
 2 Kor. 7:1  
 Waefeso 1:4; 2:10  
 1 The. 3:13; 4:3-4,7; 5:2  
 1 Timotheo 2:15  
 2 Timotheo 2:21  
 1 Petro 1:15-16  
 Waebrania 12:14

☐ **"Lida"** Mji wa Lida ulikuwa miongoni mwa misafara ya biashara kutoka Babeli hadi Misri. Katika Kitabu cha Agano la Kale huu unafahamika kama "Bwana" (kama vile 1 Nya. 8:12). Huu ilikuwa yapata maili kumi na moja nchi kavu kutoka Bahari ya Mediterranea. Hili ni eneo hili hili lililoongelewa na Filipo. Katika Matendo ya Mitume 8:40.

9:33 **"mtu mmoja huko, jina lake Ainea"** Jina lake la Kiyunani linamaanisha "kusifu." Haijulikani kama alikuwa ni mwamini au si mwamini, lakini kwa uthibitisho Petro anayatembelea tena makanisa yaliyoanzishwa na Filipo.

☐ **"huyo amelala kitandani miaka minane; maana alikuwa amepooza"** Tafsiri hii ni tafsiri ya kifungu hiki cha Kiyunani kilicho cha kawaida sana (NASB, NKJV, NRSV, TEV, NJB). Hata hivyo, hiki kifungu cha Kiyunani kinaweza kumaanisha "miaka minane tangu kuzaliwa" (kama vile Newman na Nida, *A Translator's Handbook on The Acts of the Apostles*, uk. 199).

9:34 **"Yesu Kristo akuponya"** Hapa hakuna kibainishi, kinachomaanisha kwamba haya maneno mawili yanakuwa maelezo ya kawaida. Hii ni muundo wa kifasihi unaojulikana kama wakati uliopo usiotimilifu, ambao Unamaanisha "huyu ndiye Masihi akuponyaye kwa wakati huu."

☐ **"ondoka, ujitandikie"** Hizi ni kauli mbili tendaji shurutishi za wakati uliopita usio timilifu zinazoonyesha msistizo



na umuhimu!

☑ "**Mara akaondoka**" Hili linaonyesha imani ya mtu katika kuwa na mwitikio wa ujumbe wa Petro kuhusu injili ya Kristo Yesu.

9:35 "**Na watu wote waliokaa Lida**" Huu ni mfano mzuri wa matumizi ya kuzidisha sifa ya neno "wote" katika Biblia (kama vile Mwa. 41:37; Kumb. 2:25; Luka 2:1; Rum. 11:26).

☑ "**Sharoni**" Jina hili linarejelea ile sehemu ya uwanda wa pwani ya kaskazini ndani ya Palestina. Eneo hili lapata urefu wa maili therathini kutoka Yafa hadi Kaizaria.

☑ "**wakamgeukia Bwana**" Hili neno "kumgeukia" linaweza kuliaksi neno la Agano la Kale linalomaanisha toba (*shub*). Hili linamaanisha kugeuka kwa mtu mwenyewe kutoka dhambini (toba) na kumrudia (imani) Bwana (kama vile Matendo ya Mitume 11:21). Usemi huu wenye muhtasari mfupi umehusishwa mara kadhaa ndani ya kipengele hiki, ukionyesha mabadiliko makubwa ya Roho Mtakatifu kupitia kwa Petro na kupitia kwa Paulo. Hili tukio la kimiujiza lilifungua mlango wa kuihubiri injili.

## MADA MAALUM : TOBA KATIKA AGANO LA KALE

Dhana hii ni ya muhimusana lakini ni vigumu kuitolea ufafanuzi. Wengi wetu tunao ufafanuzi ambao unatokana na ushirikishwaji wa kimadhehebu. Hata hivyo, mara nyingi huu "mwelekeo" wa ufafanuzi wa kithiolojia unalazimisha maneno kadhaa ya Kiebrania (na Kiyunani) amabayo kwa upekee wake hayamaanishi "elekea" ufafanuzi huu. Lazima ikumbukwe kwamba waandishi wa kitabu cha Agano la Kale (isipokuwa Luka) walikuwa wanafikra wa Kiebrania waliotumia maneno ya lugha ya Koine ya Kiyunani, hivyo sehemu ya kuanzia ni ile ya maneno yenyewe ya Kiebrania, ambayo kimsingi ni mawili.

3. *nacham* ( BDB 636, KB 688)

4. *shub* ( BDB 996, KB 1427)

Neno la kwanza, *nacham*, kiuhalisia linaonekana kumaanisha "kueleza pumzi ya ndani" linatumika katika maana kadhaa.

e. "kupunzika" au "kufaraji" (m.f. Mwa. 5:29; 24:67; 27:42; 37:35; 38:12; 50:21; mara nyingi linatumika katika majina, kama vile 2 Fal. 15:14; 1 Nya. 4:19; Neh. 1:1; 7:7; Nahumu 1:1)

f. "kuhuzuka" (m.f. Mwa. 6:6,7)

g. "kughairi" (m.f. Kut. 13:17; 32:12,14; Num. 23:19; Ayubu 42:5-6)

h. "huruma" (m.f. Kut. 32:36)

Tambua kwamba haya yote yanahusisha hisia za ndani! Hapa ndipo palipo na ufubuzi: hisia za ndani ambazo huelekea katika tendo. Badiliko hili la tendo mara kwa mara huelekezwa kwa watu wengine, lakini pia kuelekea kwa Mungu. Ni hili badiliko la mtazamo na tendo kumwelekea Mungu ambalo hukazia neno hili kwa umuhimu huu wa kithiolojia. Lakini hapa ungalifu lazima ufanyiwe kazi. Mungu anasemekana "kutubu" (kama vile Mwa. 6:6, 7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:11, 35; Zab. 106:45), lakini hili si matokeo ya sononeko juu ya dhambi au makosa, bali ni njia ya kiaandiko ya kuonyesha huruma ya Mungu na uangalifu (kama vile Hes. 23:19; 1 Sam. 15:29; Zab. 110:4; Yer. 4:27-28; Eze.24:14). Adhabu istahiliyo dhambi na uasi inasamehewa ikiwa mtenda dhambi ameamua kwa usahihi kuongoka kutoka dhambini kwake/kwao na kurudi kwa Mungu. Huu ni uthamanisho mpya wa maisha.

Neno la pili, *shub*, linamaanisha "kurudi" (kurudi kutoka, kurejea, kurudi kwa). KITENZI *shub* (BDB 996, KB 1427) kimsingi kinamaanisha "kugeuka" au "kurejea tena" Kitenzi hiki kinaweza kutumika kwa

4. kumuelekea Mungu, Hes. 14:43; Yos. 22:16,18,23,29; Amu. 2:19; 8:33; 1 Sam. 15:11; 1 Fal. 9:6; Yer. 3:19; 8:4
5. kumrudia Mungu, 1 Fal. 8:33,48; 2 Nya. 7:14; 15:4; 30:9; Zab. 51:13; 116:7; Isa. 6:10; 10:21,22; 31:6; Yn. 4:6,8-11 (tambua hasa Yeremia 7 na Amosi 4)
6. YHWH anamwambia Isaya hapo awali kwamba Yuda haitaweza/isingeweza kutubu (kamavile Isa. 6:10), lakini si mara ya kwanza katika kitabu hiki, Yeye anawahita warudi Kwake.

Toba si hisia nyingi sana kama ulivyo mtazamo kumwelekea Mungu. Huu uthamani mpya wa maisha kutoka upekee kuelekea Kwake. Hii inadokeza utayari wa kubadilika na kubadilishwa. Si ukomavu kamili kuihusu dhambi, bali ukomavu wa uasi unaojulikana! Huu ni ukinyume wa matokeo yaliyo kitovu Anguko la Mwanzo 3. Hiii inadokeza kwamba sura na ufanano wa Mungu (Mwa. 1:26-27), ingawa iliharibika, umerejeshwa! Ushirika pamojana Mungu kupitia mwanadamu aliyeanguka inawezakana kurejeshwa tena.

Toba katika Agano la Kale kimsingi inamaanisha "badiliko la tendo," ambapo "toba" katika Agano Jipya inamaanisha "badiliko la fikra" (tazama Mada Maalum: Toba [AJ]). Yote haya ni muhimu kwa ajili ya toba ya kweli ya kibiblia. Pia ni muhimu kutambua kwamba toba ni vyote tendo la awali na hatua endelevu. Tendo la awali linawezakuonekana katika Marko 1:15; Matendo ya Mitume 3:16 na 19; 20:21, ambapo hatua endelevu inaweza kuonekana katika 1 Yohana 1:9; Ufunuo 2 na 3. Toba si uchaguzi (kama vile Luka 13:3,5)!

Ikiwa ni kweli kwamba mahitaji ya maagano mawili ni "toba" na "imani" (m.f. Mt. 3:2; 4:17; Maro 1:4,15; 2:17; Luka 3:3,8; 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3), kisha neno *nacham* linarejea juu ya hisia zenye nguvu za kutambua dhambi ya mtu na kugeuka kutoka ndani ya hiyo dhambi, ambapo neno *shub* lingaliweza kurejea juu ya kurudi toka dhambini na kumwelekea Mungu (moja ya mfano wa haya matendo ya kiroho uko katika Amosi 4:6-11, "hamkunirudia mimi" [mara tano] ana Amosi 5:4,6,14, "Nitafuteni mimi. . .Mtafuteni Bwana. . .Tafuteni mema, wala si mabaya").

Mfano wa kwanza ulio mkuu wa nguvu ya toba ni ile dhambi ya Daudi's sin with Bathsheba (kama vile 2 Samuel 12; Zaburi 32,51). Kulikuwa na matokeo endelevu kwa Daudi, familia yake, na Israeli, lakini Daudi alirejeshwa katika ushirika pamoja na Mungu! Hata Manase aliyekuwa dhalimu aliweza kutubu na kusamehewa (kama vile 2 Nya. 33:12-13). Maneno yote haya yanatumika kwa usawa katika Zab. 90:13. Lazima kuwepo na utambuzi wa dhambi na nia iliyokusudiwa, kurudi kwa mtu binafsi kuto dhambini, pamoja na shauku ya kumtafuta Mungu na haki Yake (kama vile Isa. 1:16-20). Toba ni hatua tambuzi, hatua binafsi, na hatua ya kimaadili. Haya yote yanahiajika, yote ni kwa ajili ya kuanza uhusiano mpya pamoja na Mungu na kuushikilia uhusiano huo mpya. Hisia za ndani za majuto hurejeshwa ndani ya utele wa uaminifu kwa Mungu na kwa ajili ya Mungu!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 9:36-43**

<sup>36</sup> Na mwanafunzi mmoja alikuwako Yafa, jina lake Tabitha, tafsiri yake ni Dorkasi (yaani paa); mwanamke huyu alikuwa amejaa matendo mema na sadaka alizozitoa. <sup>37</sup> Ikawa siku zile akaugua, akafa; hata walipokwisha kumwosha, wakamweka orofani. <sup>38</sup> Na kwa kuwa mji wa Lida ulikuwa karibu na Yafa, nao wanafunzi wamesikia ya kwamba Petro yuko huko, wakatuma watu wawili kwake, kumsihi na kusema, Usikawie kuja kwetu. <sup>39</sup> Petro akaondoka akafuatana nao. Alipofika, wakampeleka juu orofani wajane wote wakasimama karibu naye, wakilia na kumwonyesha zile kanzu na nguo alizozishona Dorkasi wakati ule alipokuwa pamoja nao. <sup>40</sup> Petro akawatoa nje wote, akapiga magoti, akaomba, kisha akaelekea yule maiti, akanena, Tabitha, ondoka. Naye akafumbua macho yake, na alipomwona Petro akajiinua, akaketi. <sup>41</sup> Akampa

**mkono, akamwinua; hata akiisha kuwaita wale watakatifu na wajane akamweka mbele yao, hali yu hai. <sup>42</sup> Ikajulikana katika mji mzima wa Yafa; watu wengi wakamwamini Bwana. <sup>43</sup> Basi Petro akakaa siku kadha wa kadha huko Yafa, nyumbani mwa mtu mmoja, jina lake Simoni, mtengenezaji wa ngozi.**

**9:36" Yafa"** Kwa sasa mji huu unajulikana kama Yaffa (*Yafo*). Huu ulikuwa na reli ya kale iliyoelekea Yerusalemu. Kwa sasa ni sehemu ya mji wa kisasa wa Tel Aviv-*Yafo*.

☐"**mwanafunzi**" Hili neno "mwanafunzi" linatumika mara nyingi katika kipengele hiki cha Matendo ya Mitume. Kwa uhalisia neno hili linamaanisha "ajifunzaye," lakini linatumika katika maana ya kuwa mwamini.

☐"**Tabitha. . .Dorkasi**" Jina hili la mwanamke wa Kiaramu lilikuwa *Tabitha*; jina lake la Kiyunani lilikuwa *Dorcas*. Wayahudi walio wengi waliokuwa na uhusiano wa kijamii au wa kibiashara na wale wasiokuwa Wayahudi walikuwa na majina mawili, moja la Kiaramu na moja la Kiyunani. Majina haya yote yakimaanisha "paa" alama ya neema na uzuri (kama vile Wimbo Ulio Bora 2:9, 17; 4:5; 7:3).

☐"**amejaa matendo mema** " Hii inarejelea kuwasaidia wahitaji. Hii ilikuwa dhana ya Kiyahudi ya msaada wa kila juma ambao uliendelezwa katika Sinagogi kwa malezi ya watu wahitaji wa Kiyahudi katika jumuiya. Katika siku za Yesu hili lilifikiriwa na Wayahudi kuwa la muhimu kiroho. Kanisa nalo lilifuta mlolongo huu (kama vile Matendo ya Mitume 6). Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mutume 3:2.

☐"**alizoitoa**" Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati usiotimilifu. Aya hii inazungumzia tendo la mara kwa mara katika wakati uliopita.

**9:37"walipokwisha kumwosha, wakamweka orofani"** Tendo la kuosha mwili lilifanana maandalizi ya Kiyahudi kwa ajili ya maziko. Katika Yerusalemu mwili ulipaswa kuzikwa siku ile ile ya mtu kukumbwa na mauti, lakini nje ya Yerusalemu, maziko yalikuwa kwa muda wa siku tatu. Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 5:6.

**9:38" wakatuma watu wawili kwake"** Waamini hawa walisikia juu ya miujiza mikuu iliyofanywa na Mungu kupitia kwa Petro na waliani kwamba alikuwa na uwezo wa kufanya jambo lingine kwa mwanamke huyu wa Kiyahudi aliyekuwa Mkristo mkuu.

**9:39 "wajane wote wakasimama karibu naye"** Kwa uthibitisho kabisa hawa walikuwa wamevaa nguo ambazo Dorkasi alikuwa amezishona kwa namna mbili: (1) nguo za ndani na (2) kanzu.

**9:40"Petro akawatoa nje wote"** Kiuhalisia aya hii inamaanisha "kupeleka nje" Tendo hili ni sawa kabisa na lile alilolifanya Yesu katika Marko 5:40. Kwa kweli, kuna ufanano mkubwa kati ya miujiza iliyofanyika katika kipengele hiki na miujiza ile iliyofanyika katika kipindi cha maisha ya Yesu. Huduma ya Yesu ndiyo mfano pekee walikuwa nao Mitume. Swali ni kwamba, "Kwa nini Petro aliwaamuru wote watoke ndani ya chumba?" Yesu alilifanya hili kwa sababu hakutaka kujulikana kama mponyaji pekee na injili ilikuwa bado haijakamilishwa. Lakini kwa nini Petro alifanya hivi? Inaonekana kwamba miujiza hii ilifungua mlango wa imani, hivyo ingeonekana kwamba kwa vyo vyote vile anataka wengi walione hili.

☐"**akapiga magoti**" Kawaida ya uombaji wa Kiyahudi ilikuwa ni kusimama na kuinua mikono na amacho mbinguni. Hata hivyo, katika Kitabu cha Matendo ya Mitume, hili limenukuliwa mara kadhaa kwamba wanafunzi walipiga magoti kuomba. Kwa uthibitisho huu ulikuwa msistizo (kama vile Matendo ya Mitume 7:60; 20:36; 21:5), kama ilivyokuwa kwa Yesu katika Bustani ya Gethsemane (kama vile Luka 22:41).

☞ **"Tabitha, ondoka"** Kwa uwazi kabisa huyu alikuwa akizungumza lugha ya Kiaramu, si Kiebrania. Hili ni la kweli hata kama ilivyo Ezra-Nehemia (kama vile Neh. 8:4-8).

**9:41 "watakatifu"** Angalia Mada Maalum: Watakatifu katika Matendo ya Mitume 9:13.

**9:42 "wengi wakamwamini Bwana"** Huu ni usemi mwingine wa kimuhtasari ambao unaoonyesha matokeo makubwa ya miujiza ya Petro na huduma ya mahubiri. Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:40 na 3:16.

**9:43 "Petro akakaa siku kadha wa kadha huko Yafa, nyumbani mwa mtu mmoja, jina lake Simoni, mtengenezaji wa ngozi"** Sheria za Kiyahudi kwa Petro lazima zilikuwa tayari zimekwisha kuvunjwa kwa sababu ya yeye kukaa na mtengeneza ngozi ambaye kwa taratibu zao hakuwa safi (ilimpasa kujihusisha na utengenezaji wa ngozi za wanyama waliokufa) kama alivyokuwa akifanya Simoni

## **MASWALI YA MJADALA**

Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini kuongoka kwa Paulo kumenukuliwa mara tatu katika Matendo ya Mitume?
2. Kwa nini maelezo ya aina tatu yazungumziayo kuongoka kwa Paulo yana utofauti kidogo?
3. Ni uchaguzi wa namna gani aliokuwa nao Paulo katika kuongoka kwake? Je! uelewa wake ulionekana kuwa sahihi?
4. Kwa nini Wayahudi wa Kiyunani walijaribu kumuua Paulo?
5. Ikiwa Petro na Paulo walitumia miujiza kufungua mlango wa kuihubiri injili, kwa nini Mungu hatumii njia nyingine zaidi siku hizi?

## MATENDO YA MITUME 10

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Petro na Kornelio 10:1-8	Kornelio anatuma Watu 10:1-8	kuongoka kwa Kornelio 10:1-8	Petro na Kornelio 10:1-3	Petro anatembelea akida wa Kirumi 10:1-2 10:3-8
10:9-16	Maono ya Petro 10:9-16	10:9-16	10:4a 10:4b-8 10:9-13 10:14	10:9-16
10:17-23a	Kuitwa Kaisaria 10:17-23	10:17-23a	10:15-16 10:17-18 10:19-21 10:22-23a	10:17-23a
10:23b-33	Petro akutana na Kornelio 10:24-33	10:23b-29  10:30-33	10:23b-29  10:30-33	10:23b-33
Petro anaongea Ktk nyumba ya Kornelio 10:34-43	Mahubiri ktk nyumba ya Kornelio 10:34-43	10:34-43	Hotuba ya Petro 10:34-43	Hotuba ya Petro ktk nyumba ya Kornelio 10:34-35 10:36-43
Mataifa wapokea Roho Mtakatifu 10:44-48	Roho Mtakatifu ashuka juu ya Mataifa 10:44-48	10:44-48	Mataifa wanakaribisha Roho Mtakatifu 10:44-48	Ubatizo wa kwanza wa Mataifa 10:44-48

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" \("A Guide to Good Bible Reading"\)](#))

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

#### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

- A. Injili inatoka katika uasili wake wa Kiyahudi
  1. Kornelio – Akida wa jeshi la Kirumi anayemcha Mungu

2. Towashi wa Kushi – Mcha Mungu wa Mataifa
- B. Kazi ya Wayahudi wazungumzao Kiyunani (saba katika Mdo. 6) imwenye ushawishi.
- C. Kujirudia kwa tukio la Kipentekoste kunakoonyesha Mungu kuwakubali watu wote.
  1. Wasamaria (Mdo. 8)
  2. Warumi (Mdo. 10)
  3. Mkushi (Mdo. 8)
- D. Jukwaa la kithiolojia linawekwa kwa Baraza la Yerusalemu katika Mdo. 15. Upatikanaji wa njia panda na mgawanyiko wa injili ya kiulimwengu unafikiwa!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 10:1-8

<sup>1</sup> Palikuwa na mtu Kaisaria, jina lake Kornelio, akida wa kikosi kilichoitwa Kiitalia, <sup>2</sup> mtu mtauwa, mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima. <sup>3</sup> Akaona katika maono waziwazi, kama saa tisa ya mchana, malaika wa Mungu, akimjia na kumwambia, Kornelio! <sup>4</sup> Akamtazama sana, akaogopa akasema, Kuna nini, Bwana? Akamwambia, Sala zako na sadaka zako zimefika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu. <sup>5</sup> Sasa basi, peleka watu Yafa, ukamwite Simoni, aitwaye Petro. <sup>6</sup> Yeye ni mgeni wa mtu mmoja, jina lake Simoni, mtengenezaji wa ngozi, ambaye nyumba yake iko pwani, atakuambia yakupasayo kutenda. <sup>7</sup> Na yule malaika aliyesema naye akiisha kuondoka, Kornelio akawaita wawili katika watumishi wake wa nyumbani, na askari mmoja, mtu mtauwa katika wale waliomhudumia daima; <sup>8</sup> na alipokwisha kuwaeleza mambo yote akawatuma kwenda Yafa.

**10:1 "Palikuwa na mtu Kaisaria"** Kuongoka kwa Kornelio kulikuwa tukio kubwa sana. Hata hivyo lazima ikumbukwe kwamba hakikuwa kikwazo cha kijamii cha injili cha kwanza kukishinda.

1. cha kwanza kilikuwa ni cha Msamaria
2. alafu kilifuatiwa na Towashi Mkushi aliyekuwa inawezekana Mcha Mungu
3. Alafu Kornelio ambaye hakuwa tu kwamba ni mtu wa mataifa, lakini alikuwa ni akida wa jeshi la Kirumi ambaye alikuwa sehemu ya jeshi lililokuwa likitawala ardhi ya Nchi ya Ahadi.

Msisitizo wa jambo hili hauko sana kwenye kuongoka kwa Kornelio kwasababu alikuwa tayari Mcha Mungu kama Towashi kutoka nchi ya Kushi, lakini idadi kubwa ya ndugu na rafiki zake, wanaotajwa katika Mdo. 10:1,24,27,44,48, ambao pia waliokoka. Petro anamaanisha jambo hili katika baraza la Yerusalemu katika Mdo.15:7-9 na kuweka jukwaa kwa ajili ya misheni ya Kanisa.

▣ **"Kornelio"** Kidokezo namba 1 katika F. F. Bruce's *Commentary on the Book of the Acts*, ukurasa wa 214, kinadai "Kornelio haswa lilikuwa jina la kawaida katika Rumi tangu utawala wa Publius Cornelius Sulla katika miaka ya 82 k.k. aliyewaweka huru watumwa 10,000 walioingizwa katika *gens Cornelia*, ambayo yeye alikuwemo." *gens* lilikuwa ni koo au kundi la familia zilizokuwa zinachangia majina sawasawa na imani ya pamoja ya mtu wa kale au shujaa (kama ilivyo hapa).

▣ **"akida"** Maakida wanatajwa mara kadhaa katika Agano Jipya na siku zote katika nuru au mwanga mwema (kama vile Mt. 8:5; Luka 7:2; 23:47; Mdo. 10:1; 22:5; 27:3; nakadhalika). Kiufundi walikuwa ni viongozi wa watu mia moja mia moja; hata hivyo walikuwa ni maafisa wasiosimikwa kitu kama makamanda majenerali.

▣ **"kikosi kilichoitwa Kiitalia"** Siku zote kikosi cha Kirumi kinaundwa na wanaume kama 600. Kikosi hiki kilikuwa

kinaundwa na warumi waliojitolea ambao walikuwa wamepangiwa sehemu yao ya kazi kuwa Ashuru. Tunafahamu kutokana na ushahidi wa kihistoria kwamba waliitwa kikosi kisaidizi. Yawezekana wao walikuwa warusha mishale. Vikosi vya Kirumi vilitakiwa kufanyia kazi Palestina kwasababu ya uasi wa Wayahudi.

**10:2 "mtu mtauwa"** Haya ni maelezo ya mafiga matatu kuhusu hali ya kujitoa kwa mtu huyu:

1. alikuwa mwenye hofu ya Mungu (angalia kidokezo katika Mdo. 10:22) yeye na nyumba yake yote
2. alikuwa siku zote ni mkarimu katika matendo yake ya misaada kwa watu
3. alikuwa na tabia ya kumuomba Mungu (kama vile Mdo. 10:22; 13:16,26).

Mtu huyu alikuwa mtu wa dini, mwenye kujishikanisha na Sinagogi kihisia na kijamii, ingawa hakuwa mwongofu kamili. Ili awe mwongofu kamili mtu alitakiwa awe na sifa hizi

1. apate tohara ikiwa ni mwanaume
2. ajiabatize mwenyewe mbele ya mashahidi
3. ikiwezekana atoe dhabihu hekaluni

Matakwa haya yaliwazuia wengi wa Mataifa waliokuwa na shauku ya kuwa waongofu kamili.

▣ **"yeye na nyumba yake yote"** Hii ni mara ya kwanza kutajwa kwa familia kama shemu ya dini ambayo tunaipata mara kwa mara katika kitabu cha Matendo ya Mitume (kama vile Mdo. 10:2; 11:14; 16:15, 31; 18:8). Inaonesha muktadha wa kifestari kwamba imani ya baba siku zote ilikuwa imani ya nyumba nzima na hata wanaukoo ambao ingejumuisha na wafanyakazi.

▣ **"sadaka nyingi"** Hii inamaanisha utoaji wa sadaka. Kwa watu wa Kiyahudi hii ingeonesha kwamba Kornelio alikuwa sehemu au kiungo muhimu cha Sinagogi la mahali fulani na kidhahiri mtu Mcha-Mungu. Angalia Mada Maalum: Utoaji wa Sadaka katika Mdo 3:2.

▣ **"na kumwomba Mungu daima"** Kuna kauli endelevu za wakati uliopo tatu hapa, zinazoonyesha kitendo kinachoendelea cha huruma ya Kornelio.

1. hofu, kauli ya kati ya wakati uliopo (yenye ushahidi)
2. kutoa sadaka, kauli tendaji ya wakati uliopo
3. kuomba, kauli ya kati ya wakati uliopo (yenye ushahidi)

Kujitoa kwa mtu huyu kulikuwa ni kwa kila siku na kwa kibinafsi. Alikuwa akifanya mambo mawili ambayo dini ya kiyahudi ya kiuahimu iliyaheshimu sana, utoaji wa sadaka na maombi.

**10:3 " kama saa tisa ya mchana,"** Hii inamaanisha muda wa jioni wa kujitoa (yaani saa 9 mchana, kama vile Kutoka 29:39, 41; Hesabu. 28:3-31; 1 Wafalme. 18:29-36; Zaburi. 55:17; 141:2; Dan. 6:10; Josephus *Antiq.* 11.4.1; Wars 1.1.1). Huu ulikuwa muda uliozoeleka wa kwenda kuomba.

**NASB, NRSV**

**TEV** "kuona vizuri"  
**NKJV** "kuona vizuri"  
**NJB, NIV** "kuona kwa upekee"

Katika Injili, kielezi *phanerōs* kinamaanisha kutokea kwa uwazi au mbele ya umma (kama vile Marko 1:45; Yohana 7:10). Maono haya yalikuja wakati wa saa za mchana na yalikuwa yanamaelekezo ya wazi na yanayoeleweka.

▣ **"Akaona katika maono .....Malaika wa Mungu,"** Kwa namna fulani kuongoka huku kwa namna fulani ni kama kule kwa Sauli. Mtu huyu alikuwa mtauwa mchaji wa kidini. Mungu anatuma kitu cha kiajabu cha kumsaidia

kumuongoza katika imani. Nani angeweza kusema "Hapana"? Huku kuongoka ni ishara ya uchaguzi wa Mungu na sio utashi wa kimwili wa kibinadamu. Watu hawa wanaitikia ushahidi uzidio na matukio ya ukweli wa injili.

**10:4** Ujumbe wa malaika umebeba maneno mawili ya kidhabihu dhabihu: "kupanda" na "ukumbusho mbele za Mungu." Inavyoonekana Mungu alikubali ibada ya mtu huyu (yaani maombi na utoaji wa sadaka) hata kabla hajasikia injili.

▣ **"Akamtazama sana,"** Angalia kidokezo katika Mdo. 1:10.

▣ **"Kuna nini, Bwana?"** Ni vigumu sana kufasiri hili neno Bwana. Linaweza kumaanisha (1) "mkuu" au "mheshimiwa" au (2) "Bwana" katika namna ya kithiolojia ya Bwana/Mmiliki/mwenye uweza wote. Kifungu kingine kizuri cha Agano Jipya kinachonyesha utata ni Yohana 4:1,11,15,19,49.

Katika Matendo ya Mitume kuna uwezekano uliongezwa. Kornelio naye anaitwa na malaika kama Bwana (kama vile Ufunuo. 7:14) Petro anahutubia "sauti" (kama vile Mdo. 10:13,15) kama Bwana (kama vile Mdo. 10:14). Hivyo neno linaweza kumaanisha nguvu yoyote ya juu na udhihirisho binafsi, kwa mrejereo wa hasa kwa Yesu. Katika Mdo. 8:26 na 29 malaika wa Bwana anatambulishwa na Roho. Huku kuelea na kugeuzwa kunatokea kati ya "sauti" na Roho katika Mdo. 10:13,14,15 and 19,20.

**10:5 "Sasa basi, peleka watu Yafa"** Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu (yenye ushahidi). angalia kwamba malaika hakuhubiri habari za injili, lakini akaagizwa Petro. Mungu anatumia watu kama vyombo (kama vile Kutoka 3:7-10). Mtu huyu, mtauwa mtu wa dini anayemaanisha (kama Sauli), alihitaji kusikia na kuitikia mwito wa injili ya Yesu Kristo.

**10:7 "akawaita wawili katika watumishi wake wa nyumbani, na askari mmoja, mtu mtauwa;"** Hii inatengeneza chama cha watatu; hata hivyo katika mastari wa 19 ni wawili tu ndio wanaotajwa. Yawezekana mwanajeshi alikuwa mlinzi na watumishi wengine wawili wa nyumbani walizungumza.

**10:8** Kornelio aliwashirikisha familia yake na marafiki zake katika imani yake. Mtu huyu aliishi katika yake aliyoyaamini. Jamii yote ingekuja kwake kwa imani kupitia yeye. Hawa wanaume watatu lazima walitembea usiku kucha na kushangaa na kujadiliana juu ya ujumbe wa malaika na bwana wao na imani ya rafiki yao.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 10:9-16**

<sup>9</sup> Hata siku ya pili, walipokuwa wakisafiri na kuukaribia mji, Petro alipanda juu darini, kwenda kuomba, yapata saa sita ya mchana; <sup>10</sup> akaumwa na njaa sana, akataka kula; lakini walipokuwa wakiandaa, roho yake ikazimia, <sup>11</sup> akaona mbingu zimefunuka, na chombo kikishuka kama nguo kubwa, inatelemshwa kwa pembe zake nne hata nchi; <sup>12</sup> ambayo ndani yake walikuwamo aina zote za wanyama wenye miguu minne, na hao watambaao, na ndege wa angani. <sup>13</sup> Kisha sauti ikamjia, kusema, Ondoka, Petro, uchinje ule. <sup>14</sup> Lakini Petro akasema, Hasha, Bwana, kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au najisi. <sup>15</sup> Sauti ikamjia mara ya pili, ikimwambia, Vilivyotakaswa na Mungu, usiviite wewe najisi. <sup>16</sup> Jambo hili likatendeka mara tatu; kisha kile chombo kikapokewa tena mbinguni.

**10:9 "kwenda kuomba, yapata saa sita ya mchana;"** Ingawa Dini ya kiyahudi ya kiuahimu ilikuwa imetenga kuwa saa 3 kamili asubuhi na saa 9 kamili mchana ndio muda wa kuomba (muda wa dhabihu za kila siku katika hekalu), Mafarisayo walikuwa wameongeza kuwa saa 6 kamili mchana ulikuwa muda mwingine mzuri wa kuomba. Inavyoonekana Petro alikuwa anatenda katika desturi za wazee za kuomba wakati wa mchana au labda alikuwa amejipumzisha kidogo akisubiri mlo wa mchana.

**10:10 "akaumwa na njaa sana"** Mazingira ya maono ya Petro yako katika muktadha wa njaa yake na maoni yake ya bahari ya Shamu kutoka katika paa la Simoni. Neno kwa ajili ya "njaa" linatumika hapa tu katika fasihi zote za



Kiyunani zinazojulikana. Visawe vyake sahihi ni ngumu kuvifahamu, lakini kwa kihisishi kinachoongezwa cha *pros*, inaweza kumaanisha "njaa kali," lakini hii inashangaza kimuktadha. Hii *hapax legomenon* (maneno yanayotumika mara moja tu katika Agano Jipya) lazima yabakie katika kutoeleweka mpaka taarifa za kisamiati zinapogundulika. Lazima ibakie katika hali ya kutoeleweka na ndio maana Luka alichagua kutumia neno hili nadra, lakini kwa maana ya jumla muktadha upo wazi.

▣ "**akataka kula**" Hii kwa dhahiri "nje yake mwenyewe" au "kuacha yeye mwenyewe," mara kwa mara linatumika katika hali ya mshangao (kama vile Marko 5:42; 16:8; Luka 5:26; na katika maandiko kadhaa ya LXX). Tunapata neno la kingereza "ecstasy (kujawa na furaha kuu)" kutoka katika neno hili la Kiyunani. Katika mstari huu na 11:5 na 22:17 linamaanisha hali ya akili kujitambua nusu ambayo inaruhusu Mungu kuzungumza kwenye akili iliyofichika. Hili ni neno tofauti na lile tunalotumia katika mstari wa 3 kuelezea maono ya Kornelio.

**10:11**

<b>NASB</b>	<b>"anga ilifunguka"</b>
<b>NKJV, TEV</b>	<b>"mbingu ilifunguka"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"mbingu ilifunguka"</b>
<b>NJB</b>	<b>"mbingu ilifunguka"</b>

Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu, literally kikawaida "mbingu baada ya na zimeendelea kufunguka." Katika Agano la Kale mbingu ziko katika wingi. Huku kufunguka kwa hali ya hewa ni nahau kwa viwango vya kiroho visivyonekana kupenya katika ukweli wa kimwili (kama vile Ezek. 1:1; Mt. 3:16; Marko 1:10; Luka 3:21; Yohana 1:51; Mdo. 7:56; 10:11; Ufunuo 4:1; 19:11).

▣ "**kama nguo kubwa**" Hili ni neno lilelile lililotumika kwa ajili ya safari za majini za meli.

**10:12 "ambayo ndani yake walikuwamo aina zote za wanyama wenye miguu minne, na hao watambao, na ndege wa angani."** Huku ni kugawanyika kulekule kwa makundi matatu ya wanyama kunakopatikana katika Mwanzo 1 na 6:20. Inavyoonekana walikuwa wanaundwa na wanyama safi na najisi kulingana na sheria za kiyahudi za vyakula katika Mambo ya walawi 11.

**10:13 "Kisha sauti ikamjia"** Kutoka katika muda wa kufunga kitabu cha Malaki mpaka kipindi cha kuja kwa Agano Jipya hakukuwa na sauti ya kimamlaka ya kinabii kutoka kwa Mungu kati ya Wayahudi. Wakati wa kipindi hiki ambapo Wayahudi walitaka kuthibitisha kitu kama kimefunuliwa na Mungu walitegemea kitu kilichojulikana kama *bath kol*. Tunaona hiki katika Agano Jipya katika Mt. 3:17; 17:5, pia katika Mdo. 9:7, na hapa.

**10:14 "Hasha, Bwana, kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au najisi."** "kwa namna yoyote" ni tungo ya kiyunani yenye nguvu inayotumika mara kadhaa katika Tafsihi ya Agano la Kale kufasiri nahau kadhaa za za Kiebrania. Petro alikuwa bado anahangaika na mafundisho yake ya Kiyahudi. Alikuwa ameweka matendo yake akijitetea kupitia Mambo ya Walawi 11. Hata hivyo Yesu anaonekana kwa hasa kushughulikia jambo hili katika Marko 7:14, hasa mstari wa 19. Inashangaza kujua kwamba Injili ya Marko inavyoonekana baadaye kama makusanyo au mahubiri ya Mtume Petro kutokea Rumi.

**10:15 "Vilivyotakaswa na Mungu, usiviite wewe najisi"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi, ambayo mara nyingi inatumika kuweka ukomo wa kitendo kinachoendelea. Mungu kwa usahihi anazitoa kauli ya uzuiaji wa sheria ya chakula ya Musa (yaani Mambo ya Malawi 11). Si yenye kufaa kwa waamini wapya wa agano. Hapa yanatumika katika njia ya masimulizi kuonesha kukubaliwa kwa wanadamu wote!

**10:16 "Jambo hili likatendeka mara tatu"** Ni jambo la kawaida katika Biblia kwa maombi muhimu, sifa au matendo kurudiwa mara tatu.

1. Maombi ya Yesu katika Bustani ya Gethsemane (kama vile Marko 14:36,39)

2. Mjadala wa Yesu na Petro baada ya kufufuka (kama vile Yonaha John 21:17)
3. Maombi ya Paulo juu ya "mwiba katika nyama" (kama vile 2 Kor. 12:8)

Ilikuwa ni katika namna ya msisitizo (kama vile Isa. 6:3; Yer. 7:4). Kwa namna hii kwa uwazi inaonesha hali ya Petro ya kutokukubaliana na sauti ya kimbungu!

A. T. Robertson, *Word Pictures In the New Testament* kina neno kali katika jambo hili. "Huu hapa ni maelezo makali ya ukaidi/usugu kwa sehemu ya yule anayetambua sauti ya Mungu kwake yeye amri ya Bwana inapita mapendeleo ya mtu mwenyewe na chuki bila sababu. Kuna mifano mingi ya kutosha leo ya jambo hili. Kwa namna halisi kabisa Petro alikuwa akiwe huruma zaidi ya mapenzi ya Bwana" (ukurasa wa 137).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 10:17-23a**

<sup>17</sup> Hata Petro alipokuwa akiona shaka ndani ya nafsi yake, maana yake ni nini maono hayo aliyoyaona, wale watu waliotumwa na Kornelio, wakiisha kuiulizia nyumba ya Simoni, wakasimama mbele ya mlango, <sup>18</sup> wakaita; wakauliza kwamba Simoni aitwaye Petro anakaa humo. <sup>19</sup> Na Petro alikuwa akiyafikiri yale maono. Roho akamwambia, Wako watu watatu wanakutafuta. <sup>20</sup> Basi ondoka ushuke ufuatane nao, usione tashwishi, kwa maana ni mimi niliyewatuma. <sup>21</sup> Petro akawashukia wale watu, akanena, Mimi ndiye mnayemtafuta. Mmekuja kwa sababu gani? <sup>22</sup> Wakasema, Kornelio akida, mtu mwenye haki, mchaji wa Mungu, aliye na sifa njema kwa taifa lote la Wayahudi, alionywa na malaika mtakatifu kutuma watu kwako, uende nyumbani kwake, apate kusikiliza maneno kwako. <sup>23</sup> Akawakaribisha wawe wageni wake. Hata siku ya pili, Petro akaondoka akatoka pamoja nao,

**10:17 "Petro alipokuwa akiona shaka ndani ya nafsi yake"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati usiotimilifu, ambayo hapa inaashiria mwanzo wa kitendo kwa wakati uliopita. Neno limetumika mara kadhaa na Luka kuonesha mkanganyiko wa kiakili (kama vile Luka 9:7; Mdo. 2:12; 5:24; 10:17). Petro hakuweza kuendelea kwa mara moja kusudi la maono.

▣ **"maono"** Neno lililotumika hapa kuelezea uzoefu wa tukio la Petro, *horama*, ni lile lile lililotumika katika maono katika Mdo.10:3 (kama vile Mdo. 10:19).

**10:19 "Roho akamwambia"** Uhusiano halisi kati ya "Roho" (Mdo. 10:19) kuzungumzia na "malaika" (Mdo. 10:3,22) akizungumza kupitia muktadha huu haujulikani (Kama vile Mdo. 10:20, "Nimewatuma Mimi Mwenyewe"). Inavyoonekana malaika alizungumza kwa niaba ya Roho Mtakatifu au wawili wanatambulishwa kama kuidhahilisha kwa miungu ya Agano la Kale (Kama vile Kutoka 3:2,4; Mdo. 8:26,29). appearance

**10:20** Mstari huu unatiliwa mkazo.

1. inuka, kauli endelevu ilivyotumika kama kauli shurutishi
2. shuka chini, kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu
3. fuatana nao, kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopo (yenye ushahidi)
4. bila wasiwasi, kauli endelevu iliyotumika kama kauli shurutishi
5. Nimewatuma Mimi mwenyewe, *ego* pamoja na kauli tendaji elekezi ya wakati timilifu

Hakukuwa na mbadala kwa Petro isipokuwa kuondoka! Huku kulikuwa ni kukutana kiungu. Roho alikuwa anawajibika kwa maono ya Kornelio, Kornelio kuwatuma watu, maono ya Petro na sasa Petro akiitikia wito wao.

**10:22** Wanafananisha kwa uaminifu kwa kile ambacho kimetokea

NASB	"mwenye haki"
NKJV	"mtu mtauwa"
NRSV, NJB	"mkamilifu"
TEV	"mtu mwema"

Neno hili linatumika katika namna ya Agano la Kale "bila shutuma." Haimaanishi hali ya kutokuwa na dhambi (kama vile Mwanzo. 6:1; Ayubu 1:1; Luka 1:6; 2:25) au kwa haki iliyoshutumiwa ya Kristo (kama vile Rum. 4). Huyu mtu aliishi yote aliyokuwa anayaelewa kuhusu mapenzi ya Mungu. Angalia [MADA MAALUM: HAKI](#) katika Mdo. 3:14.

NASB, NRSV	
NJB	"mcha Mungu"
NKJV	"yule anayemuhofu Mungu"
TEV	"anayemwabudu Mungu"

Tungo hii (au moja kama hii) inatumika mara kwa mara kumfunua Kristo (kama vile Mdo.10:2,22,35). Katika Mdo. 13:16,26,43,50 inatumika kwa wale ambao sio wayahudi kikabila na ambao sio waongofu kamili lakini wale ambao mara kwa mara wanahudhuria katika Sinagogi. Walikuwa wakiitwa "Wacha-Mungu" (kama vile Mdo. 16:14; 17:4,17; 18:7).

**10:23 "Akawakaribisha wawe wageni wake na kuwapa sehemu ya kulala"** Huu ni mfano wa mwendelezo wa Petro wa kuachana na misimamo yake ya Kiyahudi. Ni hakika kuwa askari aliyefuatana naye alikuwa Mrumi nabado Petro alimwalika ndani kwa ajili ya mlo wa jioni na ushirika. Angalia namna Mdo. 10:48 Petro atakaa katika nyumba ya Rumi kwa siku chache.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 10:23b-29**

<sup>23b</sup> na baadhi ya ndugu waliokaa Yafa wakafuatana naye. <sup>24</sup> Siku ya pili yake wakaingia Kaisaria. Na Kornelio alikuwa akiwangojea, hali amekusanya jamaa zake na rafiki zake. <sup>25</sup> Petro alipokuwa akiingia Kornelio akatoka amlaki akamwangukia miguu, akamsujudia. <sup>26</sup> Lakini Petro akamwinua, akasema, Simama, mimi nami ni mwanadamu. <sup>27</sup> Na katika kusema naye akaingia ndani, akaona watu wengi wamekusanyika. <sup>28</sup> Akawaambia, Ninyi mnajua ya kuwa si halali mtu aliye Myahudi ashikamane na mtu aliye wa taifa lingine wala kumwendea, lakini Mungu amenionya, nisimwite mtu awaye yote mchafu wala najisi. <sup>29</sup> Kwa sababu hiyo nalikuja nilipoitwa, nisikatae; basi nawauliza, ni neno gani mliloniitia?

**10:24 "na baadhi ya ndugu waliokaa Yafa wakafuatana naye."** Mdo. 11:12 inasema kuwa walikuwa sita kati yao. Petro alijua kwamba jambo hili lingeweza kusababisha matatizo kati ya baadhi ya wafuasi wa kiyahudi wa Yesu. Hivyo aliwachukua mashuhuda kadhaa pamoja naye (kama vile Mdo. 11:12).

▣ **"Kaisaria"** Kaisaria lilikuwa jiji zuri kando ya bahari. Lilipewa jina hilo kama heshima ya Kaisari wa Kirumi. Lilikuwa sehemu ya Kipalestina kwa ajili ya jeshi la kirumi linalotawala hapo. Warumi walikuwa wamefanya hivyo katika bandari ndogo.

▣ **"hali amekusanya jamaa zake na rafiki zake"** Kornelio alikuwa akitegemea mzungumzaji kutoka kwa Mungu, alikuwa amewaita rafiki zake wote wa karibu, marafiki, watumishi, na yawezekana wanajeshi wengine. Walikuwa wakisubiria kwa masaa na masaa. Roho ya matarajio sipati picha kwa namna gani ilikuwa ikijaa kwenye hii nyumba! Wote hawa ukute walikuwa wakijadili kuhusu ujumbe wa ndoto.

Hiki ndicho kilichowachanganya viongozi wa dhehebu la kiyahudi wa kanisa, kwamba kundi kubwa la mataifa wengi wao waliomcha Mungu, walikuwa wakijumuishwa katika ujazo wa Roho na ubatizo (kama vile Mdo. 10:27).

**10:25,27 "Petro alipokuwa akiingia. . . akatoka"** Inavyoonekana kuna upungufu. Hata hivyo, kwanza "kuingia" kunatajwa katika Mdo.10:25 kunaweza kuwa lango katika sehemu ya nyumba naya pili "kuingia" katika Mdo. 10:27 kunaweza kukawa ni katika nyumba ya Kornelio. Vyovyote itakavyokuwa, Petro tena anavunja taratibu za kiyahudi za ibada za sherehe kwa kuingia katika nyumba ya mtu wa mataifa.

**10:25 "akamwangukia miguu, akamsujudia."** Hii ni nahau ya mara kwa mara katika Tafsiri ya Agano la Kale na katika Injili kwa ajili ya ibada. Lakini katika muktadha huu "toa heshima" inaweza kushikilia wazo hili vizuri (kama vile toleo la NJB). Malaika alikuwa ameandaa kuja kwa Petro; japo ndio Kornelio angeheshimu na kumjali mleta ujumbe huyu (kama vile Ufunuo 19:10; 22:8-9).

**10:28 " Ninyi mnajua ya kuwa si halali mtu aliye Myahudi ashikamane na mtu aliye wa taifa lingine wala kumwendea "** Petro ananukuu kutoka katika mafunzo yake ya kiuahidi au kutoka katika Sinagogi; hata hivyo, hii haipatikani katika Agano la Kale, lakini ni fasiri tu za kiuahidi.

▣ **"mtu aliye wa taifa lingine"** Neno hili nalo ni neno lingine la kipekee linalopatikana hapa katika Agano Jipya. Luka amechagua maneno kadhaa nadra sana katika sura hii.

1. *eusebēs*, Mdo. 10:2,7, mtauwa (kama vile 2 Pet. 2:9)
2. *prospeinos*, Mdo. 10:10, mwenye njaa
3. *dienthumeomai*, Mdo. 10:19, anayeaksi
4. *sunomileō*, Mdo.10:27, waliongea
5. *athemiton*, Mdo. 10:28, isiyoruhusiwa kisheria
6. *alophulō*, Mdo. 10:28, mgeni
7. *anantirrētos*, Mdo. 10:29, bila kuinua kizuizi chochote (kama vile Mdo. 19:36)
8. *prosōpolēmpēs*, Mdo. 10:34, mpendeleaji (sawa na Rum. 2:11; Efe. 6:9; Yakobo 2:19)
9. *katadunasteuō*, Mdo. 10:38, taabisha (kama vile Yakobo 2:6)
10. *procheirotoneō*, Mdo. 10:41, kuchaguliwa kabla

Haeleweki ikiwa Luka alinukuu baadhi ya mahubiri haya ya mwanzo na matukio katika Matendo ya Mitume kutoka katika vyanzo vingine au kumbukumbu za mahojiano ya kinywa pamoja na wale waliokuwepo.

▣ **"lakini Mungu amenionya, nisimwite mtu awaye yote mchafu wala najisi"** Petro aliupata ujumbe! Wanyama katika shuka waliwakilisha binadamu wote waliofanywa kwa sura ya Mungu (kama vile Mwanzo 1:26-27). Upendo wa Mungu kwa Kornelio na familia yake na marafiki ulimuonesha Petro mtazamo wa kiulimwengu wa injili! Hii ingethibitisha ushuhuda wa Stefano na kuhubiri kwa Philipo.

#### **ANDIKO LA NASB( LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 10: 30-33**

<sup>30</sup> Kornelio akasema, Siku tatu zilizopita, katika saa ii hii, yaani saa tisa, nilikuwa nikisali nyumbani mwangu; nikamwona mtu amesimama mbele yangu, mwenye nguo zing'arazo, <sup>31</sup> akasema, Kornelio, kuomba kwako kumesikiwa, na sadaka zako zinakumbukwa mbele za Mungu. <sup>32</sup> Basi, tuma watu kwenda Yafa, ukamwite Simoni aitwaye Petro, anakaa katika nyumba ya Simoni, mtengenezaji wa ngozi, karibu na pwani; naye akija atasema nawe. <sup>33</sup> Mara nikatuma watu kwako, nawe umefanya vyema kuja. Basi sasa sisi sote tupo hapa mbele za Mungu, tupate kuyasikiliza ma

**10:30 "mwenye nguo zing'arazo"** Malaika mara kwa mara walitokea katika namna hii (kama vile Mdo. 1:10; Mt.28:3; Marko 16:5; Yohana 20:12; Luka 24:4).

**10:31** Hii ni mara ya tatu katika surah ii huruma ya Kornelio inathibitishwa (kama vile Mdo. 10:4,22). Kornelio sio kitu cha kushangaza; ni marafiki zake, watumishi, na familia ambao pia wanaamini katika Kristo.

Huu ni mmoja wa mfano kadhaa katika Mdo "wokovu wa nyumbani."

Wengine wetu ambao tumekua na mifano ya kiinjili ya kimagharibi ya uinjilisti ambao unaweka mkazo na mwitikio binafsi wa kujitolea tunashangazwa na aina hii ya mwitikio wa kipamoja wa kiujumla, lakini sehemu kubwa ya kulimwengu ina wa kimakabila, kifamilia, kimakundi. Mungu anaweza kufanya kazi kupitia mifano mingi kufikia wanadamu waliofanywa kwa sura yake. Hakuna mfano mmoja wa uinjilisti!

**10:33** Hawa watu walikuwa tayari kusikia! Waligundua kuwa walikuwa kati ya muda wa kiungu na mjumbe wakutumwa na Mungu.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 10:34-43**

<sup>34</sup> Petro akafumbua kinywa chake, akasema, Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo; <sup>35</sup> bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye. <sup>36</sup> Neno lile alilowapelekea wana wa Israeli akihubiri habari njema ya amani kwa Yesu Kristo (ndiye Bwana wa wote), <sup>37</sup> jambo lile ninyi mmelijua, lililoenea katika Uyahudi wote likianza Galilaya, baada ya ubatizo aliouhubiri Yohana; <sup>38</sup> habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye. <sup>39</sup> Nasi tu mashahidi wa mambo yote aliyoyatenda katika nchi ya Wayahudi na katika Yerusalemu; ambaye walimwua wakamtundika mtini. <sup>40</sup> Huyu Mungu alimfufua siku ya tatu, akamjalia kudhihirika, <sup>41</sup> si kwa watu wote, bali kwa mashahidi waliokuwa wamekwisha kuchaguliwa na Mungu, ndio sisi, tuliokula na kunywa pamoja naye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu. <sup>42</sup> Akatuagiza tuwahubiri watu na kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliyeamriwa na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu. <sup>43</sup> Huyu manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi.

**10:34 "ya kuwa Mungu hana upendeleo"** Huu ni mwanzo wa mahubiri ya Petro. Ni mfano mzuri wa mahubiri ya kanisa la mwanzo kwa wasio wayahudi. Katika Agano la Kale tungo hii ya kimahakama iliweka tabia za Mungu (kama vile Kumb. 10:17; 2 Mambo ya Nyakati. 19:7) na kutakiwa kwa watu wake (kama vile Kumb. 1:17; 16:19). Na pia ni wasifu wa kawaida ya Mungu katika Agano Jipya (kama vile Rum. 2:11; Wagalatia 2:6; Efe. 6:9; Kol. 3:24-25; 1 Pet. 1:17). Katika Agano la Kale tungo hii ilimaanisha "kuinua sura." Katika mahakama za kiebrania Washitakiwa waliweka vichwa vyao vikiwa vimeinamishwa ili kwamba Hakimu asiweze kutambua mtu na hivyo kutoa hukumu pendelevu.

Mungu hana upendeleo (mataifa, makabila, au watu binafsi)! Ikiwa huu ndio ukweli hivyo kuamriwa kabla kunafanyaje kazi? Au kwa namna gani Israeli ni maalum? Kuwa mwangalifu wa mifumo ya kithiolojia ya kisasa!

**10:35 "bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye"** Maelezo haya hayamaanishi dhana ya wokovu wa kiroho, lakini inavyoonekana kwa wazo la kutoa sadaka, maombi na huruma. Angalia Mada Maalum katika Mdo. 3:2. Tungo hii lazima iwekewe usawa kithiolojia na mamlaka ya kupokea injili (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum. 10:9-13).

Kweli kuu ni kwamba Mungu anawakubali Mataifa bila wao kuwa waongofu wa Kiyahudi. Hii inaweka jukwaa la kithiolojia kwa ajili ya Mdo. 15, Baraza la Yerusalemu.

**10:36-39** *The Jerome Biblical Commentary* (vol. II, ukurasa wa 188) inatengeneza maoni kadhaa mazuri.

1. yanajumuisha muhtasari wa Petro wa injili (yaani *Kerygma*)
2. yana mfumo hafifu wa kimsamiati, ambao unaoonyesha kwamba Luka kwa ufasaha aliweka kumbukumbu za vyanzo vyake na na hayabuni buni au kuyarekebisha rekebisha

**10:36 "Neno lile alilowapelekea wana wa Israeli"** Hii haimaanisha Agano la Kale, lakini mahubiri ya Yesu na wanafunzi wenzake.

▣ **"akihubiri habari njema ya amani kwa Yesu Kristo"** Haya yawezi kuwa maelezo kwa Isa. 52:7. Neno "amani" linatumika katika namna tatu katika Agano Jipya:

1. amani kati ya Mungu na wanadamu (kama vile Kol. 1:20)
2. amani ya mtu binafsi ya mwamini mmoja mmoja (kama vile Yohana 14:27; 16:33, Wafilipi 4)
3. amani kati ya vikundi vya kibinadamu wanaoitikia Kristo (kama vile Efe. 2:14-3:6; Kol. 3:16)

Vikwazo vyote vya kibinadamu vimeondolewa katika Kristo (kama vile Wagalatia 3:28; Kol. 3:11)

▣ **"(ndiye Bwana wa wote)"** Haya ni maoni ya kihariri/kiuandishi. Hapa kuna kisehemu cha ujumbe wa kiulimwengu na mwaliko wa Injili ya Yesu Kristo ambayo bado inaonekana ni ya kushikiliwa katika vinywa vya wayahudi wa kale washika dini (kama vile Mdo. 2:36; Mt. 28:18; Rum. 10:12; Efe. 1:20-22; Kol. 2:10; 1 Pet. 3:22). Yeye ni Bwana wa makabila yote na vitu vyote (yaani U-Bwana juu ya ulimwengu wote)!

**10:37,39 "jambo lile ninyi mmelijua, lililoenea"** Petro anatumia mfumo uleule wa kama mahubiri yake ya Pentekoste (kama vile Mdo. 2:22,33). Walikuwa wamesikia kuhusu Yesu na kile kilichotokea kwake katika Yerusalemu.

Mtu anaweza kushangaa kwa namna gani watu hawa walikuwa na taarifa zote hizi. Petro anatumia mtindo wa kuweka chumvi? Kwa haya angalau alishirikisha baadhi ya matukio katika Yerusalemu? Je baadhi ya wafanyakazi wake wa nyumbani walikuwa Wayahudi? Andiko ni fupi sana na hatuwezi kujua. Wengine wametumia mahubiri haya kuelezea:

1. Luka aliandika mahubiri yote katika Matendo ya Mitume (lakini Luka ni mwandishi mzuri wa Koine na Matendo ya Mitume 10:36-38 sio mzuri Myunani wa kukubalika).
2. Luka alikuwa mkweli kwa vyanzo vyake na alinukuu kwa ufasaha bila kusahihisha sarufi yake dhaifu.
3. Tungo hii inakusudiwa kueleweka na wasomaji wa baaadaye wa Matendo ya Mitume (kama vile *The Jerome Commentary*, vol. II, ukurasa wa 189).

**10:37 "baada ya ubatizo aliouhubiri Yohana"** Kwanini Yesu alibatizwa imekuwa sikuzote jambo nyeti kwa waaminio kwasababu Ubatizo wa Yohana wa toba. Yesu hakuhitaji toba au msamaha, kwavile hakuwa mwenye dhambi (kama vile 2 Kor. 5:21; Ebr. 4:15; 7:26; 1 Pet. 2:22; 1 Yohana 3:5).

Nadharia hizo zimekuwa:

1. ilikuwa ni mfano kwa ajili ya waaminio kufuata
2. ilikuwa ni utambulisho wake wa mahitaji ya waaminio
3. ilikuwa ni kuwekwa kwake wakfu na kuwezesha kwa ajili ya huduma
4. ilikuwa ni ishara ya jukumu lake la kiukombozi
5. ilikuwa ni uthibitishaji wake wa huduma na ujumbe wa Yohana Mbatizaji
6. Ilikuwa ni kuona mbali kwa kinabii kwa kifo chake, maziko na ufufuo (kama vile Rum. 6:4; Kol. 2:12).

Ubatizo wa Yohana ulionekana mwanzoni mwa Yesu kujazwa Roho Mtakatifu, huduma ya umma. Kumbukumbu zote tatu za Injili hii zilianzishwa rasmi. Marko anaanza Injili yake (hesabu ya shuhuda ya Petro) pamoja na tukio hili. Hii ilionekana na kanisa la mwanzo kama mwanzo maalum wa kizazi kipya cha Roho kama kinavyofanana na huduma ya umma ya Yesu.

**10:38 "Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu"** Tazama mambo ambayo Petro anayakiri kuhusu Yesu.

1. Mungu alimtia mafuta (kupaka mafuta ni mzizi wa kiebrania wa Masihi)
2. Pamoja na Roho Mtakatifu (kizazi kipya ni kizazi cha Roho)
3. kwa nguvu (ufanisi wa huduma)
  - a. kutenda mema
  - b. kuponya wote walioonewa na shetani (nguvu ya uovu na shetani)
4. Mungu alikuwa pamoja naye (Aliongea kwa niaba ya YHWH, kama vile Yohana 3:2; 9:33; 10:38; 14:10-11)

Inavyoonekana hii inamaanisha ubatizo wa Yesu (kama vile F. F. Bruce, *Answers to Questions*, ukurasa 171-172). Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, anatengeneza kauli ya kufurahisha:

"kitenzi *XPIEIN* kinatumika mara tano katika Agano Jipya. Katika vifungu hivi vine inamaanisha kupakwa mafuta kwa Kristo na Baba yake, ikitajwa: Luka 4. 18, ambayo inanukuliwa kutoka katika Isa. 61. 1; Ebr. 1. 9, ikinukuliwa kutoka Zaburi 45. 7; Mdo. 4. 27, ambapo inatumika kwa rejea maalum kwa nukuu kutoka katika Zaburi mbili ambayo mara moja inaitangulia; na katika Mdo. 10. 38, tunaambiwa Mungu alimpaka mafuta Yesu kwa Roho" (ukurasa wa 183).

Angalia Mada Maalum: *Kerygma* katika Mdo.2:14.

▣ **"na kuponya wote walioonewa na Ibilisi "** Angalia Mada maalum katika Mdo. 5:3 na 5:16.

**10:39 "ambaye walimwua wakamtundika mtini"** "wao" inamaanisha uongozi wa Kiyahudi, kundi lenye ghasia, na mamlaka za Kirumi. Angalia kidokezo katika Mdo 2:23. Dhana hii ya kutundikwa mtini inatajwa katika Mdo. 5:30 Na kuaksiwa katika Mdo. 21:23 (ambayo kiasili ilimaanisha kutundikwa katika nyama baada ya kifo kumfedheheshwa mtu), ambapo Yesu alichukua laana zetu za sheria la Agano la Kale lakini walimu wa Kiyahudi wa siku za Yesu waliifasiri kama kusulubishwa kwa Kristo (kama vile Isa. 53) kwa ajili yetu (kama vile Gal. 3:13).

**10:40 "Mungu alimfufua"** Inafurahisha sana kithiolojia kwamba katika katika Isa.53:4-6,10 inaelezea kwamba ni mapenzi ya YHWH na makusudi kwamba Yesu ateseke na afe (kama vile Mwanzo 3:15). YHWH alitumia uwakala wa

1. shetani
2. uongozi wa kiovu wa kiyahudi
3. uongozi uliorubuniwa wa Kirumi
4. kundi la kighasia lenye hasira la kiyahudi

Uovu upo katika mapenzi ya Mungu! Anautumia kukamilisha kilele cha kusudi lake kwa ajili ya wanadamu walioumbwa kwa sura na mfano wake. Aisee! Thiolojia ya namna gani hii ya kiutawala! Anaruhusu kifo, alafu analeta maisha ya ufufuo kwa Yesu na kwa wote!

Agano Jipya linakiri kwamba nafsi zote tatu za Utatu Mtakatifu zilikuwa zikitenda kazi katika ufufuo wa Yesu:

1. Roho (Rum. 8:11)
2. Yesu (Yohana 2:19-22; 10:17-18)
3. Baba (Mdo. 2:24,32; 3:15,25; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 27:31; Rum. 6:4,9)

Huu ulikuwa uthibitisho wa kweli ya maisha ya Yesu, kifo na mafundisho kuhusu Mungu. Hii ilikuwa sehemu kubwa ya *Kerygma* (yaani mahubiri katika Matendo ya Mitume. (Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:14).

▣ **"siku ya tatu,"** Kwasababu ya 1 Kor. 15:4, Baadhi zinafananisha hii na Zaburi 16:10 au Hosea 6:2, lakini zaidi yawezekana Yona 1:17 kwasababu ya Mt. 12:40.

**10:40-41 "akamjalia kudhihirika, si kwa watu wote"** Yesu alitokea kwa baadhi ya vikundi vilivyochaguliwa (kama vile Yohana 14:19, 24; 15:27; 16:16, 22; 1 Kor. 15:5-9).

**10:41 "tuliokula na kunywa pamoja naye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu"** Japokuwa mwili wa Yesu baada ya Kufufuka haukuhitaji matunzo ya nje ya kimwili, Yeye alikula na kunywa kuonesha mashuhuda wake maalum kwamba alikuwa ni halisi na kuelezea ushirika wake pamoja nao (kama vile Luka 24:35, 41-43; Yohana 21:9-13).

**10:42 "Akatuagiza tuwahubiri watu"** Kiwakilishi kinamaanisha Yesu (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:47-48; Yohana 15:27). Shuhuda huyu alikuwa akianza katika Yerusalemu lakini kuufikia ulimwengu wote (kama vile 1:8).

▣ **"awe Mhukumu wa walio hai na wafu"** Kristo ni wakala wa Baba katika hukumu (kama vile Dan. 7:13-14; Yohana 5:22,27; Mdo. 17:31; 2 Kor. 5:10; 2 Tim. 4:1; 1 Pet. 4:5) kama alivyokuwa wakala wa baba katika uumbaji (kama vile Yohana 1:3; Kol. 1:16; Ebr. 1:2). Yesu hakuja kuhukumu bali kukoa (kama vile Yohana 3:17-19). Tungo "waliohai na waliokufa" inamaanisha hukumu ya siku za mwisho, kuja kwa mara ya pili. Baadhi ya waamini watakuwa hai (kama vile 1 The. 4:13-18).

### **MADA MAALUM: KUHUKUMU, HUKUMU, na HAKI KATIKA ISAYA**

Hili ni neno linalotumika kwa upana zaidi (BDB 1047, KB 1622) katika Agano la Kale. NIDOTTE, juzuu ya. 4, uk. 214, limeainisha mgawanyo na umuhimu wake.

1. Torati, 13%, waamuzi wa wanadamu
2. Vitabu vya kihistoria, 34%, viongozi wanadamu
3. Fasihi ya hekima, 22%, kazi za ki-Ungu
4. Manabii, 31%, kwa kiasi kikubwa kazi za ki-Ungu

Angalia chati ifuatayo toka kwa Isaya:

YHWH kama Mwamuzi	Mesih kama mwamuzi	Waamuzi bora wa Israel	Waamuzi halisi wa Israel
2:4	9:7	1:17	1:23
3:14	11:3, 4	26:8	3:2
4:4	16:5	56:1	5:7
5:16	32:1	58:2, 8	10:2
28:6, 17, 26	40:14		59:4, 9, 11, 14, 15
30:18	42:1, 3, 4		
33:5, 22	51:4, 5		
61:8	53:8		
66:16			

Israel ilipaswa kuaksi tabia za YHWH katika mataifa. Lakini ilishindwa, kwa hiyo, YHWH akamwinua Mwisrael mmoja "aliye bora" kutimiliza ufunuo wake binafsi katika mataifa (yaani., Mesih, Yesu wa Nazareti, ambaye ni Kristo, kama vile. Isa. 52:11-53:12)!



**10:43 "Huyo manabii wote humshuhudia"** Yesu aliwaonesha wanafunzi wake wawili njiani Emmau (imewekwa kumbukumbu katika Luka 24:13-35) ambapo na namna gani Agano la Kale linammanisha mwenyewe. Hii ilioneshwa kwa wanafunzi katika chumba cha juu na taarifa hii ilikuwa njia ya mkabiliano ya ushuhudiaji (kama vile Mdo. 3:18). Yesu aliwafungua akili zao wanafunzi (kama vile Luka 24:45).

▣ **"kwa jina lake"** (kama vile Yoeli 2:32 na Luka 24:47)

▣ **"kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi."** Huu ni ujumbe wa injili:

1. kila mmoja
2. kupitia jina lake
3. yeye amwaminiye
4. anayepokea msamaha wa dhambi (kama vile Luka 24:46-47)

Imelengwa kwa Yesu na sio kulengwa katika matendo (yaani again Jipya la Yer. 31:31-34, kama vile Ezekieli 36:22-38). Vitu vyote vinavyotakiwa kufanyika kwa kila mtu, yoyote kuokolewa kumekwisha fanyika! Mungu amechagua kufanya kazi na mwanadamu aliyeanguka kupitia agano. Ameanzisha na kuweka agenda, akini anataka pia kwamba wanadamu waitikie kwa toba, imani, utii na ustahimilivu. Wanadamu lazima wapokee zawadi ya Mungu katika Kristo (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum. 10:9-13). Sio jambo la kujiamisha lenyewe.

Frank Stagg, *New Testament Theology*, wana maoni ya kupendeza sana kuhusu msamaha na mahusiano yake dhania kuelekea toba.

"Msamaha inataka ufahamu mpya ya dhambi na kugeuka kutoka huko. Uhakika unatolewa kwamba msamaha na kusafishwa dhambi hakika kutafuata juu ya ukiri wa dhambi (1 Yohana 1:9), lakini hakuna ahadi inayotolewa ambapo ukiri haupatikani. Katika nyumba ya Kornelio, Petro anahusianishwa na msamaha kwa imani, akitangaza kwamba mtu huyu (JesusYesu) manabii wote watoa ushuhuda: kwamba kupitia jina lake kila mtu anayemwamini yeye atapokea msamaha wa dhambi (Mdo. 10:43). Katika Hii imani pamoja na toba na ukiri, mmoja anamiliki vyote na na anapoteza umiliki wake wa dhambi. Hii haimaanishi kwamba toba inashinda msamaha; hata toba haifanyi mtu astahili msamaha. Kama mwingine anavyoiweka. Mwenye dhambi hasameheki mpaka anapokuwa tayari kukubali *hapana* ya Mungu ili aweze kusikia *ndio yake*" (ukurasa 94).

Kwa "kuamini katika Yeye" angalia Mada Maalum katika Mdo. 3:16.

#### **ANDIKO LA NASB(LILILOBRESHWA): MATENDO YA MITUME 10:44-48**

<sup>44</sup> Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno. <sup>45</sup> Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. <sup>46</sup> Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu. Ndipo Petro akajibu, <sup>47</sup> Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? <sup>48</sup> Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha.

**10:44** Tazama kwamba Petro hakuwa amemaliza mahubiri yake wakati Roho aliposhuka (kama vile Mdo. 8:16-17; 10:44; 11:15).

▣ **"akawashukia wote waliolisikia lile neno"** Mvutano wa kweli wa kithiolojia jhaukuwa kwa Kornelio. Alikuwa amekubalika kikamilifu na Sinagogi la mahali pamoja. Wote walikuwa marafiki zake! Inavyoonekana hakuwa na mawasiliano ya nyuma, hata dini ya kiyahudi, na sasa Mungu alikuwa amewakubali kikamilifu. Kukubaliwa huku kulioneshwa na kuthibitishwa na udhihirisho uleule wa nguvu ya roho na uwepo ulioneshwa siku ya Pentekoste. Pia tambua kwamba mpangilio wa matukio unabadilika. Roho inakuja kabla ya ubatizo wa maji sio pamoja na muunganiko wake (kama vile Mdo. 2:38) au baada yake (kama vile Mdo. 8:17). Luka anaweka kumbukumbu ya kile ambacho kimetokea, na sio "kile ambacho kingetakiwa kutokea." Kuwa mwangalifu juu ya kujaribu kugeuza

moja ya mikutaniko ya injili hizi zinazowekwa katika kumbukumbu katika Matendo ya Mitume kuelekea "kwenye" mkutaniko wa kiinjili!

**10:45** Udhihirisho uleule wa kiungu wa Roho (kama vile Mdo 10:46) ambao ulitokea siku ya Pentekoste, ulitokea tena ukijumuisha tena Warumi! Ishara hii maalum kwa Kornelio na rafiki zake tu, lakini kimsingi kwa ajili ya waamini wasiotahiriwa (kama vile Mdo. 10:47). Iionesha katika namna ya nguvu mitindo isiyoshindwa kwamba Mungu alikubali Mataifa (kama vile Mdo. 11:17), hata Warumi!

Luka anaweka jukwaa la kifasihi kwa ajili ya Mdo. 15, Baraza la Yerusalemu. Wote Petro na Paulo walikuwa wameshawishika pamoja na walimu wa mafundisho ya uongo wakiamini Wayahudi kwamba Mungu alikuwa amewakubali mataifa kiukamilifu kupitia Kristo.

▣ **"kipawa cha Roho Mtakatifu"** Huduma ya Roho inaweza kuonekana vizuri katika Yohana 16:8-14. Katika namna moja, kushuhudiwa kwa dhambi ni karama kutoka kwa Roho. Wokovu wenyewe ni karama ya Roho. Uwepo wa ndani ni karama ya Roho. Hizi ni zama mpya za Roho (kama vile Mdo. 2:38; 8:20; 11:17). Hakuna kitu cha kudumu na cha kiufanisi kinachotokea bila ya uwepo na nguvu ya Roho.

▣ **"wamemwagiwa"** Hii ni kauli tendwa ya wakati uliopo. Kujazwa kulikuwa sehemu ya mfumo wa kidhabihu wa Agano la Kale. Ilikuwa imetabiriwa katika Roho na Yoeli 2:28 na kunukuliwa na Petro katika mahubiri yake ya Kipentekoste (kama vile Mdo. 2:17,33). Roho amekuwa mzima mzima na wa kudumu aliyetolewa kwa waamini na Mungu.

**10:47** Hili ni swali lisilotegemea kujibiwa au kupata jibu la "hapana". Swali hili lilikuwa ni kupata mapatano ya waamini wa Kiyahudi waliomsindikiza Petro kutoka Joppa. Angalia [MADA MAALUM: UBATIZO](#) at katika Mdo. 2:38.

**10:48 "Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo "** Tazama kwamba Ubatizo ulikuwa wa haraka. Pia tazama kwamba ulifanywa katika Jina la Yesu katika Mdo. 2:38 and 19:5. Kanuni ya ubatizo katika Matendo ya Mitume "katika jina la Yesu," while in wakati katika Mt. 28:19 ilikuwa katika jina la utatu wa Mungu. Kanuni sio msingi, lakini moyo wa uanafunzi!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini wokovu wa Kornelio ulikuwa wa muhimu sana?
2. Ni kwa namna gani tukio la wokovu wa Kornelio lina shabihiana na lile la Paulo?
3. Nini umuhimu wa kithiolojia wa kitambaa kilichojaa wanyama na maoni ya Petro vinatoa ukihusianisha na Kornelio?
4. Kwanini uongofu wa rafiki za Kornelio ulikuwa tatizo?
5. Ainisha mahubiri ya Petro na yalinganishe na matukio mengine ya wokovu katika Matendo ya Mitume. Yote ni tofauti lakini pia ni sawa.

## MATENDO YA MITUME 11

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Petro anatoa Taarifa kwa kanisa la Yerusalemu wake	Petro anatetea Neema ya Mungu	Kujitetea kwa Petro	Petro anatoa taarifa kwa kanisa la Yerusalemu	Yerusalemu: Petro anahalalisha mwenendo
11:1-18	11:1-18	11:1-18	11:1-4 11:5-17 11:18	11:1-10  11:11-14 11:15-17 11:18
Kanisa la Antiokia	Barnaba na Sauli huko Antiokia	Misheni kwa Wayunani wa Antiokia	Kanisa la Antiokia	Msingi wa kanisa la Antiokia
11:19-26	11:19-26	11:19-26	11:19-26	11:19-21 11:22-24 11:25-26
Yerusalemu	Misaada kwa Yudea	msaada wa njaa Unatumwa kwa Yerusalemu		Barbana na Sauli wanatumwa kama wasaidizi
11:27-30	11:27-30	11:27-30	11:27-30	11:27-30

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("[A Guide to Good Bible Reading](#)")

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili

3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 11:1-18

<sup>1</sup> Basi mitume na ndugu waliokuwako katika Uyahudi wakapata habari ya kwamba watu wa Mataifa nao wamelipokea neno la Mungu. <sup>2</sup> Na Petro alipopanda kwenda Yerusalemu, wale walio wa tohara wakashindana naye, <sup>3</sup> wakisema, Uliingia kwa watu wasiotahiriwa ukala nao. <sup>4</sup> Petro akaanza kuwaeleza kwa taratibu, akasema, <sup>5</sup> Nalikuwa katika mji wa Yafa, nikiomba, roho yangu ikazimia, nikaona maono; chombo kinashuka, kama nguo kubwa inatelemshwa kutoka mbinguni kwa pembe zake nne, kikanifikilia. <sup>6</sup> Nikakitazama sana, nikifikiri, nikaona wanyama wa nchi wenye miguu minne, na wanyama wa mwituni, nao watambaao, na ndege wa angani. <sup>7</sup> Nikasikia na sauti ikiambia, Ondoka, Petro, ukachinje ule. <sup>8</sup> Nikasema, Hasha, Bwana, kwa maana kitu kilicho kichafu au kilicho najisi hakijaingia kabisa kinywani mwangu. <sup>9</sup> Sauti ikanijibu mara ya pili kutoka mbinguni, Alivyovitakasa Mungu, usivinene wewe najisi. <sup>10</sup> Jambo hili likatendeka mara tatu, kisha vitu vyote vikavutwa tena juu mbinguni. <sup>11</sup> Na tazama, mara hiyo watu watatu wakasimama mbele ya nyumba tuliyokuwamo, waliotumwa kwangu kutoka Kaisaria. <sup>12</sup> Roho akaniambia nifuatane nao, nisione tashwishi. Ndugu hawa sita nao wakaenda pamoja nami, tukaingia katika nyumba ya mtu yule; <sup>13</sup> akatueleza jinsi alivyomwona malaika aliyesimama nyumbani mwake na kumwambia, Tuma watu kwenda Yafa ukamwite Simoni aitwaye Petro, <sup>14</sup> atakayekumbua maneno ambayo yatakuokoa, wewe na nyumba yako yote. <sup>15</sup> Ikawa nilipoanza kunena, Roho Mtakatifu akawashukia kama alivyotushukia sisi mwanzo. <sup>16</sup> Nikalikumbuka neno lile la Bwana, jinsi alivyosema, Yohana alibatiza kwa maji kweli, bali ninyi mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu. <sup>17</sup> Basi ikiwa Mwenyezi Mungu amewapa wao karama ile ile aliyotupa sisi tuliomwamini Bwana Yesu Kristo, mimi ni nani niweze kumpinga Mungu? <sup>18</sup> Waliposikia maneno haya wakanyamaza, wakamtukuza Mungu, wakisema, Basi, Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.

**11:1** Mstari huu unamaanisha kwamba uongozi wa kanisa la Yerusalemu lilishangazwa na mgeuko wa matukio. Walishangazwa na hawakuwa na ushirikiano kwa ukamilifu! Wao hawakuwa wameelewa Agizo Kuu (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8) kujumuisha Wapagani. Tungo hii inatokea tena katika Mdo.8:14 wakati Msamaria anapoipokea Injili.

▣ **"ndugu"** Hili ni jina la kwanza kwa waamini wanaoweka mkazo familia yetu ya pamoja (kama vile Mdo. 1:15; 6:3; 9:30; 10:23; 11:1,12, 29; 12:17; 14:2; 15:1,3,22,23,32-33,40; 16:2,40; 17:6,10,14; 18:18,27; 21:7, 17; 22:5; 28:14-15). Kuwa Mkristo nikuwa sehemu ya familia (Kama vile 1 Kor. 12:13; Gal. 3:28; Kol. 3:11).

▣ **"Uyahudi yote"** Hii inaonesha ukomo wa kijiografia wa kanisa mpaka katika muda ule. Hata baada ya miaka mingi kanisa halikuwa limetoka katika mipaka yake ya kidesturi. Amri ya Yesu katika Mdo. 1:8 haikuwa imetekelezwa kwa utii! Ni kama "inakaribiana" sambamba na Mwanzo 10-11.

▣ **"kwamba watu wa Mataifa nao wamelipokea neno la Mungu."** Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu (yenye ushahidi). Inaonesha umuhimu wa upokeaji binafsi wa ujumbe wa Injili (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum. 10:9-13 Efe. 2:8-9). Tungo "neno la Mungu" ni sambamba na "Injili." Ahadi za Agano la Kale za kulimwengu na unabii unatimilizwa. Angalia Mada Maalum katika Mdo. 1:8.

**11:2 "Na Petro alipopanda kwenda Yerusalemu"** Kiuwazi tatizo la umisheni wa Mataifa linaloendelea katika Mdo. 15 lilikuwa linajitokeza tena katika uongozi wa Yerusalemu wa kanisa la kwanza. Waongofu wengi kwenda kwenye Ukristo walikuwa bado wazalendo (kama vile Mdo. 15:5; 21:18-26).

<b>NASB</b>	<b>“wale waliokuwa wametahiriwa”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“wale wa tohara”</b>
<b>NRSV, NJB</b>	<b>“waamini waliotahiriwa”</b>
<b>TEV</b>	<b>“wale waliokuwa wakiunga mkono kuwatahiri mataifa”</b>
<b>Williams</b>	<b>“mashujaa wa tohara”</b>

Tungo hii inaweza kutumika katika namna tofauti kadhaa:

1. Katika Mdo. 10:45 kuelezea watendakazi wenza wa Petro sita wa Kiyahudi
2. hapa inamaanisha kikundi cha waamini katika kanisa la Yerusalemu (kama vile Mdo. 11:18 au 15:5)
3. Kwa Wagalatia inamaanisha waaminio kutoka kanisa la Yerusalemu (kama vile Mdo. 2:12) na pia wasioamini wa kiyahudi (kama vile Mdo. 1:7; 2:4; 5:10,12)

Hakuna swali juu ya ukweli na udhati wa waamini hawa wala hekima ya nafasi zao. Hata hivyo asili ya kiini cha injili ilikuwa imefungua mlango kwa watu wote ambao hawajaunganishwa kabisa na sheria ya Musa (yaani Rum. 3:21-31) Huu ni ujumbe (neema wala sio matendo yanayoleta wokovu) Waamini wengi wa kisaa tunahitaji kusikia na kufanyia kazi!

<b>NASB</b>	<b>“walichukua jambo”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“wakipingana”</b>
<b>NRSV, TEV</b>	<b>“wakakosoa”</b>
<b>NJB</b>	<b>“wakapinga”</b>

Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Huu muundo wa kisarufi unaweza kuelezea tendo linalojirudiarudia wakati uliopita ao mwanzoni mwa kitendo. Tazama hawa watu waamini wa desturi walilichukua jambo pamoja na Petro. Hawakuona kwamba jambo hili lilikuwa jambo la Injili.

**11:3 "Uliingia kwa watu wasiotahiriwa ukala nao"** Kwa uwazi Petro sio kiongozi ambaye hakutani na changamoto. Kisarufi mstari huu unaweza ukawa kauli au swali (NRSV). Jambo hili la ushirika wa meza lilikuwa muhimu sana kwa watu wa Kiyahudi. Hilli jambo linaweza likawa chanzo cha sheria katika kitabu cha Mambo ya Walawi 11 kushusu vyakula. Wayahudi hawakutakiwa kushirikiana tukio lolote la kijamii na Wakanaani. Kula katika Near East na Kale lilikuwa ni jambo la ushirika wa kiagano. Yesu alikuwa ameshutumiwa na kushitakiwa kwa jambo hilo hila la kuvunja taratibu za desturi katika Mt. 9:11; 11:19; Luka 5:30; 15:2. Petro alipambana na jambo la namna hii katika huduma yake (kama vile Gal. 2:12). Hili lilikuwa jambo la muhimu sana kwa waamini hawa wa kwanza. Ni ngumu sana kufikiria kwa upya mila na desturi na upendeleo binafsi lakini injili inataka kwamba tufanye hivyo (kama vile 1 Kor. 12:13; Gal. 3:23-29; Kol. 3:11). Wayahudi dhidi ya mfano wa Mataifa wa Agano la Kale umekuwa kwa uzima uzima wake pamoja na waamini dhidi ya mfano wa wasioamini!

**11:4-18** Petro anarejerea tukio lake katika nyumba za Simoni na Kornelio (Mdo. 10) kwa viongozi wa Kiyahudi Yerusalemu. Haya ni marudio (kama vile Baraza la Yerusalemu katika Mdo. 15) ni namna ya Luka ya kuonesha umuhimu wa jambo hili (uinjilishaji wa ulimwengu) lilikuwa ndiyo uhai wa kanisa. Hili ulikuwa wakati wa njia panda/ muachano wa kithiolojia!

<b>11: 4</b>	
<b>NASB</b>	<b>“kwa mpangilio unaofuatana”</b>
<b>NKJV</b>	<b>“katika mpangilio kutokea mwanzo”</b>
<b>NRSV</b>	<b>“hatua kwa hatua”</b>
<b>TEV</b>	<b>“kwa hesabu kamili”</b>
<b>NJB</b>	<b>“kwa kina cha alama moja mpaka nyingine”</b>

Neno *kathexēs* linatumika latika Agano Jipya na Luka tu (kama vile Luka 1:3; 8:1; Mdo. 3:24; 11:4; 18:23). Lina viwsawe vya kuelezea jambo fulani katika mpangilio mzuri wa kimawazo, kwa muda mfupi na mpangilio mzuri wa utaratibu. Hii inashabihiana na mbinu ya kitafiti ya Luka (kama vile Luka 1:1-4), utanashati, na mafunzo ya kikazi (kitabibu).

**11:6 "kukaza macho yangu juu yake"** Angalia kidokezo katika Mdo. 1:10.

**11:12**

<b>NASB</b>	<b>"bila wasiwasi"</b>
<b>NKJV</b>	<b>"kutokuwa na shaka ya chochote"</b>
<b>NRSV</b>	<b>"kutofanya utofauti"</b>
<b>TEV</b>	<b>"bila kusitasita"</b>
<b>NJV</b>	<b>"kutokuwa na kusita sita"</b>

Kuna maandiko kadhaa ya Kiyunani tofauti tofauti yanayounganika na njeo ya wakati endelevu (kauli ya kati ya wakati uliopo katika Mdo. 10:20 au kauli ya kati ya wakati uliopita usiotimilifu katika MSS P<sup>74</sup>,  $\kappa^2$ , B). Hata pia imeondolewa katika maandiko ya Kiyunani P<sup>45</sup>, D, na baadhi ya Kilatini ya Zamani na toleo moja la Ki-Ashuru. Waandishi walijaribu kutengeneza mfanano au kukubaliana. Kama ilivyo kwa mengi ya aina za maandiko katika Agano Jipya, haya hayaathiri maana ya tungo. Toleo la UBS<sup>4</sup> linaweka kauli ya kati endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu katika andiko lakini linatoa alama ya "C" (ngumu katika kufanya maamuzi).

**11:14 "wataokolewa"** Huruma na ukarimu wa Kornerlio havikumfanya awe Mkristo! Yeye na familia yake na mara fiki zake wanaokolewa kwa imani katika Kristo!

**11:15** Mstari huu ni wa muhimu sana kithiolojia katika kuona kusudi la kurudia hali ya tukio la Pentekoste katika Mdo. Mungu alitumia uzoefu wa ufunguzi katika Yerusalemu na kuonesha kukubaliwa Kwake kwa makabila na makundi mengine ya watu, jiografia na desturi tofauti (kama vile Mdo.11:17). Uzoefu huu haukuwa tu kwa ajili ya Kornelio bali kwa ajili ya

1. Petro
2. waaminio wa kiyahudi waliokuwa wakisindikiza na kuwepo
3. kanisa la Yerusalemu

**11:16 "Nikakumbuka Neno la Bwana"** Haya ni maelezo ya maneno ya Yesu katika Mdo. 1:5. Hii inaonesha utaratibu wa mkabiliano wa kwanza wa Mitume juu ya thiolojia:

1. kumnukuu Yesu
2. kutumia mfano wa Yesu
3. kunukuu Agano la Kale (kama vile Mt. 3:11; Mdo.1:5)

Peter is establishing that the Lord Himself foresaw this developmentPetro anathibitisha na kuweka msingi kwamba Bwana mwenyewe aliona mambo haya (yaani ishara).

**11:17 "ikiwa"** Hii ni sentensi daraja la kwanza yenye masharti ambayo inasemekana kuwa kweli kutoka katika mtazamo wa kiuandishi au kwa ajili ya kusudi lake la kifasihi.

▣ **"Mungu amewapa wao karama ile ile"** Hii kama Mdo. 11:15, Inamaanisha uzoefu wa Pentekoste (kama vile Mdo. 2:1-4; 8:15; 10:46; 15:8). Wokovu, kama Roho, pia ni kipawa kutoka kwa Mungu (kama vile Rum. 3:24; 5:15-17; 6:23; Efe. 2:8).

▣ **"Baada ya kuamini katika Bwana"** Lazima upokelewe (kama vile Mdo. 11:1; Yohana 1:12; Efe. 2:8-9). Tazama namna Mdo.11:17 inaelezea vyote ukuu wa Mungu na mwikio wa lazima wa binadamu uliowekwa. Kuna vihisishi kadhaa katika Agano Jipya vinavyotumika kuelezea imani katika Yesu:

1. . *epi* = juu ya (hapa)

2. *eis* = ndani ya
3. *en* = ndani
4. *hoti* = kauli kuhusu Yesu
5. Uhusika wa wakati wa bila kihisishi

Aina hii inaonekana kumaanisha kwamba hakukuwa na muundo wa kisarufi uliokuwa umeunganishwa kwenye "amini" (*pisteuō*). Siku zote sehemu ya ubinafsi na ya kujitolea ndiyo inayotiliwa mkazo (isipokuwa kwa *hoti*, ambayo inamaanisha maudhui ya injili au mafundisho). Yesu ni nafsi inayotakiwa kukaribishwa! Angalia Mada Maalumu katika Mdo. 2:40 na 3:16.

**11:18 "walikaa kimya na kumtukuza Mungu"** Ushuhuda wa Petro sio tu kwamba ulinyamazisha na kuzuia hali ya hewa hasi, lakini ilisababisha sifa! Wengi wa viongozi hawa wa kwanza na waaminio walikuwa watu wanaofundishika na wenye kukubali kubadilika kutokana na mazingira, hawakuwa wenye shino ngumu. Walikuwa tayari kubadilisha thiolojia yao na kufuata uongozi wa Mungu.

▣ **"Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima"** Kuna vifungu kadhaa katika Agano Jipya vinavyomaanisha kwamba Mungu ndiye Chanzo cha toba kama ilivyo neema (kama vile Mdo. 5:31, 8:22; 2 Tim. 2:25). Suala la kithiolojia linalofanana na tungo hii ni, "Je Mungu Mkuu mtawala anahusianishwa vipi na wokovu dhidi ya mwitikio wa binadamu?" Je imani na toba (kama vile Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21) mwitikio wa mwanadamu au au karama ya Mungu? Kuna maandiko ambayo kwa nguvu yanamaanisha kwamba vyote ni vipawa vya Mungu (kama vile Mdo. 5:31; 11:18; Rum. 2:4; na 2 Tim. 2:25). Kwa kuwa naamini kuwa maandiko yote yamevuviwa (kama vile 2 Tim. 3:16) hivyo mtu lazima alinganishe maandiko yote yanayofanana na jambo la kithiolojia na sio kuvamia kithibitisho cha andiko au mbinu na mafundisho ya kimadhehebu. Ni wazi kuwa Mungu mmoja wa Kweli anatawala na kushughulikia mambo yote! Mdo. Inasisitiza jambo hili tena na tena. Hata hivyo amechagua kuhusianisha na uumbaji wake wa juu kwa namna ya agano. Mungu siku zote huchukua hatua na kuamua agenda, lakini sharti mwanadamu aitikie na aendelee kuitikia. Sio suala la kusitasita au kujishauri shauri. Siku zote ni vyote viwili na mahusiano. Angalia Mada Maalumu: Agano katika Mdo. 2:47. Kwa "toba" Angalia Mada Maalumu katika Mdo. 2:38. Michael Magill, *NT TransLine* (ukurasa wa 435, #24) kina kauli za kimutahsari juu ya nini wayahudi wa kwanza waaminio katika Yerusalemu walifikiria kingetokea.

"Waamini Wayahudi walijua ujumbe kwa ajili ya ulimwengu. Lakini kwamba Wokovu ulitakiwa uje kwa Mataifa na sio kwa dini ya Kiyahudi, kwa maana kwamba hili lilikuwa na wazo jipya kwa ajili yao. Walikuwa wanadhania kuwa wokovu ungeweza kutangazwa kwa ulimwengu kama sehemu na kupitia kweli, dini ya Kiyahudi ya kiroho; kwamba Uyahudi ungetawala na watu wote wangekuwa wayahudi kama sehemu ya kutafta maisha katika Kristo; kwamba desturi ya Israeli kwa utukufu ingekuwa desturi ya dunia nzima."

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 11:19-26**

<sup>19</sup> Basi wale waliotawanyika kwa sababu ya ile dhiki iliyotukia kwa habari ya Stefano, wakasafiri hata Foinike na Kipro na Antiokia, wasilihubiri lile neno ila kwa Wayahudi peke yao. <sup>20</sup> Lakini baadhi ya hao walikuwa watu wa Kipro na Kirene, nao walipofika Antiokia wakasema na Wayahudi wa Kiyunani, wakihubiri habari njema za Bwana Yesu. <sup>21</sup> Mkono wa Bwana ukawa pamoja nao, watu wengi wakaamini, wakamwelekea Bwana. <sup>22</sup> Habari hizo za watu hao zikafika masikioni mwa kanisa lililokuwako katika Yerusalemu; wakamtuma Barnaba, aende hata Antiokia. <sup>23</sup> Naye, alipokwisha kufika na kuiona neema ya Mungu akafurahi, akawasihi wote waambatane na Bwana kwa kusudi la moyo. <sup>24</sup> Maana alikuwa mtu mwema amejaa Roho Mtakatifu na imani; watu wengi wakaongezeka upande wa Bwana. <sup>25</sup> Kisha akatoka akaenda Tarso kumtafuta Sauli; <sup>26</sup> hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia.

**11:19-30** Mistari hii inaonekana kuwa usuli wa kihistoria na muhtasari wa kithiolojia. Inaunganishwa na 8:4.

**11:19 "wale waliotawanyika kwasababu ya dhiki na mateso"** Tunayo mifano ya mateso haya ya awali katika Mdo. (kama vile Mdo. 5:17ff; 6:8-15; 8:1-3; 9:1-2). Uelewa wa Stephano wa maana ya dhati ya injili iliwalazimisha waamini wa kiyahudi katika Palestina kupitia upya imani yao na kusudi la injili.

▣ **"Antiokia"** Antiokia lilikuwa jiji kubwa la tatu la dola ya Kirumi baada ya Rumi na Iskanderia. Lilikuwa Mji Mkuu wa Ashuru na lilikuwa na idadi kubwa ya wayu wayahudi. Lilikuwa likijulikana sana kwa maisha yake ya kidunia na uchafu wake wa kingono. Pia lilikuwa maarufu kwa mbio za magari ya farasi duniani. Hili linakuwa kituo kikubwa cha Ukristo!

▣ **"hawakuongea neno lolote isipokuwa kwa wayahudi tu"** Hii inaonesha kuwa kanisa la kwanza halikuwa na uhakika ikiwa kuhubiri kwao kwa mataifa kulikuwa ni sahihi. Watu wenye msimamo wangukuu maneno ya Yesu kutoka Mt. 10:5, Wakati waonaji wangukuu Mt. 28:18-20 au Mdo. 1:8. Jambo hili la kithiolojia litawekewa msingi wake upya katika Mdo. 15.

**11:20 "Watu wa Kipro na Kirene,"** Hawa ni wamini walewale wayahudi wanaozungumza Kiyunani katika Mdo. 6-8, walioanza kuhubiri maana ya kiulimwengu ya injili ya Kikristo katika Yerusalemu. Barnaba pia alitokea eneo hili la Kijiografia.

▣ **"kwa Wayunani"** Neno hili (*Hellēn*) mara nyingi linamaanisha kwa Mataifa (kama vile Mdo. 14:1; 16:1,3; 18:4; 19:10,17; 20:21; 21:28). Hata hivyo Mdo. 17:4 inamaanisha mataifa waliokuwa wameunganishwa na masinagogi (Wacha-Mungu), lakini si wanachama (yaani waongofu).

Swali ni hili, "Je Luka anamaanisha wakina nani walikuwa wanahubiriwa."

1. Wayahudi wazungumzao Kiyunani kama katika Mdo.6:1 and 9:29 (*walimu wa mafundisho ya uongo*)
2. Mataifa wanaouhusianishwa na Sinagogi (*walimu wa mafundisho ya uongo*)
3. Mataifa kamili (kama vile matoleo ya TEV, NJB)?

Pamoja na fujo zilizotokea na kusababishwa, yawezekana neno linamaanisha wale wote wanaozungumza Kiyunani; Baadhi wanaweza kuwa wayahudi wa ughaibuni na wengine wakiwa Mataifa kamili.

▣ **"Wakimuhubiri Bwana Yesu"** Hiki ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo ya kitenzi ambapo kupitia hiki tunapata neno la Kingereza "evangel (hubiri)" na evangelism (uinjilisti)." Ujumbe wao haukuwa ukihusu sheria za Agano la Kale na taratibu lakini kuhusu Yesu wa Nazareti kama Masihi (Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:31)!

**11:21 "Mkono wa Bwana ukawa pamoja nao, watu wengi wakaamini, wakamwelekea Bwana."** Hii ni kauli ingine ya muhtasari juu ya mtembeo mkubwa wa Mungu kupitia mahubiri ya kiinjilisti. Mwishowe Mdo. 1:8 ilikuwa ikitimilizwa (kama vile Mdo. 11:24b). Hii ni nahau ya Agano la Kale kwa ajili ya kutambua uwepo na nguvu ya YHWH kwa ajili ya kutimiliza makusudi yake katika matendo ya kibinadamu (kama vile 2 Sam. 3:12). Inashangaza kutambua kwamba neno "Bwana" (*Kurios*) inatumika katika mwanzo wa andiko hili kumaanisha YHWH (kama vile LXX Kutoka 3:14; 2 Sam. 3:12; Isa. 59:1, angalia Mada Maalum katika Mdo. 1:6). Hata hivyo katika sehemu inayofuata ya mstari inatumika kummaanisha Yesu Kristo. Huku kugeuzwa kwa vyeo na majina ni mbinu ya kifasihi ya waandishi wa Agano Jipya kuelezea Uungu wa Yesu. Tazama mahali Paulo ananukuu maandiko ya Agano la Kale ikimaanisha YHWH na kutumika kwao kwa Yesu (yaani Rum. 10:13; 1 Kor. 2:16; Flp. 2:10-11). Huu "mkono wa Bwana" nahau ya viumbe vya Agano la Kale (angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:33). YHWH ni roho ya milele iliyomo kupitia muda na uumbaji. Yeye hana mwili wa damu na nyama. Hata hivyo msamiati pekee wanadamu wanatakiwa kuzungumzia ni nafsi namna ya kibinadamu. Lazima tukumbuke ukomo wa kuanguka, muda na lugha ya kibinadamu ya duniani. Inazungumzia ulimwengu wa roho kwa namna ya sitiari, masimulizi na ukanushi. Inaelezea ukweli lakini katika njia zisizomalizika. Mungu yuko juu sana zaidi ya nguvu zetu kujua na kuelezea. Anazungumza kiukweli kwetu lakini si kwa namna ya kumaliza. Tunaweza kuiamini Biblia kama ufunuo binafsi wa Mungu lakini lazima tutambue kwamba Mungu bado ni Mkuu! Lugha ya binadamu ina vyote ufunuo na ukomo!



## MADA MAALUM: MKONO (ULIVYOELEZEWA TOKA KITABU CHA EZEKIEL

Neno "mkono" (BDB 388, KB 386) lina matumizi na vidokezo vingi.

1. Kwa maana iliyo wazi (yaani., mkono wa mtu)
  - a. Alama ya nafsi kamili, Ezek. 3:18; 18:8,17; 33:6,8
  - b. Alama ya udhaifu wa mwanadamu, Ezek.7:17,27; 21:7; 22:14
  - c. Alama ya maadui wa kigeni, Ezek. 7:21; 11:9; 16:39; 21:31; 23:9,28; 28:10; 30:12; 34:27; 38:12; 39:23
  - d. Kwa maana iliyo wazi ya mkono, Ezek. 8:11; 12:7; 16:11; 37:17,19,20
  - e. Alama ya nguvu ya kiongozi asiye wa kweli , Ezek. 13:21,22,23; 34:10
  - f. Alama ya taifa, Ezek. 23:31,37,42,45; 25:14; 27:15; 28:9; 30:10,22,24,25; 31:11; 39:3
2. Uungu wa Mungu kuelezewa kwa lugha ya kibinadamu
  - a. Utoaji mafunuo wa YHWH, Ezek. 1:3; 3:14,22; 8:1; 33:22; 37:1; 40:1 (2:9 ni sura nyingine ya mafunuo– gombo la mkononi)
  - b. Uwezo wa YHWH katika hukumu, Ezek. 6:14; 13:9; 14:9,13; 16:27; 20:33; 25:7,13,16; 35:3; 39:21
  - c. YHWH mwenyewe (uwepo wake binafsi), Ezek. 20:22
  - d. Uwezo wa YHWH wa kuokoa, 20:34 (yumkini matumizi muhimu toka kitabu cha Kutoka, kama vile. 3:20; 4:17; 6:1; 7:19; 13:3)
3. *Makerubi* wanaelezewa kwa lugha ya kibinadamu, Ezek. 1:8; 8:3; 10:7,8,12,21
4. Malaika wa maangamizo wanaelezewa kwa lugha ya kibinadamu, Ezek. 9:1-2; 21:11
5. Alama ya ahadi au kiapo, Ezek. 17:18; 20:5 (mara mbili), 6,15,23,28; 36:7; 44:12; 47:14
6. Alama ya furaha, Ezek. 25:6
7. Malaika kuelezewa kwa lugha ya kibinadamu, Ezek. 40:3,5; 47:3

**11:22 "Barnaba"** Barbaba ni Mhusika mkuu katika kitabu cha Matendo ya Mitume (kama vile Mdo. 4:36-37; 9:27). Jina lake linatumika kwa namna ya kutia moyo, jambo ambalo ni wazi katika Mdo. 11:23. Kanisa katika Yerusalemu lilikuwa bado halijafurahia suala la mataifa kujumuishwa katika injili! Angalia Mada Maalum katika Mdo. 4:36.

**11:23** Inashangaza kugundua kwamba wakati Barnaba aliona uwepo wa neema ya Mungu kupitia Roho, aliwatia moyo wote kuendelea kukaa katika imani (kama vile Mdo. 14:22). Hii kwa hakika inaonesha hitaji la bidii katika sehemu ya watu wa Mungu kwa ajili ya ustahimilivu wa kimakusudi (angalia Mada Maalum katika Mdo. 14:22). Wayahudi na kanisa walikuwa makini na muktadha za kipagani za kutokuwa na maadili ya kimila lakini wito kwa ajili ya utauwa (kama vile Mt. 5:48; Rum. 8:28-29; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 4:1; 1 The. 3:13; 4:3; 1 Pet. 1:15). Mungu anataka watu waaksi tabia yake kwenda kwenye ulimwengu uliopotea. Lengo la Ukristo sio tu kwenda mbinguni mara tunapokufa, bali kufanana na Kristo sasa ili kwamba wengine waje katika imani katika Kristo!

**11:24 "Maana alikuwa mtu mwema amejaa Roho Mtakatifu na imani;"** Melezo haya ni sawa na ya waamini wa kiyahudi wazungumzao kiyunani (wale saba) wa Mdo. 6:3, 5. Kanisa la kwanza lilikuwa na watu kama hawa! Aha kwamba hii ingekuwa kweli kwa desturi zetu na kanisa letu!

**11:25 "Nae akaondoka Tarso kwenda kumtafuta Sauli"** Kitenzi hiki katika mafunjo ya Koine ya Misri (lakini sio katika LXX) inamaanisha kuwa Sauli alikuwa si mtu mwepesi kupatikana. Ni Luka tu anayetumia neno hili katika Agano Jipya (kama vile Luka 2:44,45; Mdo.11:25). Hii miaka ya ukimya kwa uwazi inarejerea kwa Gal. 1:21. Muda kabisa kabisa haujulikani, lakini inakadiriwa ilikuwa kama miaka kumi.

**11:26 "kanisa"** Angalia Mada Maalum katika Mdo. 5:11.

▣ **"akamleta Antiokia.....Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia."** Kwa mara ya kwanza "mkristo" ilikuwa ni rejea ya kushusha hadhi kwa waamini iliyotengenezwa na wapagani. Cha kushangaza hili neno

ni nadra katika Agano Jipya. Uundwaji wa neno (inayoishia na *ianos*) unafuata utaratibu wa utengenezaji wa neno kwa wale wanaounga mkono na kufuata; Herode (na familia yake) wanaitwa "ma-Herodia" (kama vile Marko 3:6; 12:13; Mt. 22:16). Matumizi yake katika mazingira haya ya desturi za Kiyunani inaonesha namna cheo/jina kwa ajili ya Masihi (Kiebrania) lilifasiri Kristo katika Kiyunani limekuwa jina la wafuasi wa Yesu (Wa-Kristo). Katika mazingira haya ya desturi za Kiyunani, Inawezekana kwamba neno walipewa na wafanyakazi wa serikali ili kuwatofautisha Wayahudi na waamini.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 11: 27-30**

<sup>27</sup> Siku zizo hizo manabii walitelemka kutoka Yerusalemu hata Antiokia. <sup>28</sup> Na tulipokusanyika akasimama mmoja wao, jina lake Agabo, akaonyesha kwa uweza wa Roho Mtakatifu kwamba njaa kubwa itakuja karibu katika dunia nzima, nayo ikatukia katika siku za Klaudio. <sup>29</sup> Na wale wanafunzi, kila mtu kwa kadiri ya alivyofanikiwa, wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokaa Uyahudi. <sup>30</sup> Wakafanya hivyo, wakawapeleka wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli.

**11:27 "manabii"** Manabii wanatajwa mara kadhaa katika Agano Jipya (kama vile Mdo. 13:1; 15:32; 21:10; 1 Kor. 12:28; 14:1-5, 29-33; Efe. 2:20; 4:10). Huwa haijulikana siku zote kama kazi yao ya msingi ilikuwa ni kutabiri kama ilivyo hapa au kuyasema yajayo kama ilivyo katika 1 Wakorintho 14 na Mdo. 2:17 (kama vile Mdo. 13:6; 15:32; 1 Kor. 12:28; 14:1-5, 29-33; Efe. 2:20; 4:10). Katika Agano la Kale manabii wanaonekana kama wasemaji wa Mungu, wakielezea ufunuo wake; hata hivyo manabii wa Agano Jipya sio wapatanishi wa ufunuo wa Mungu. Hii imeachwa kwa maandishi wa Agano Jipya ambao wengi wao walikuwa Manabii au wale waliokuwa wakifanana na Mitume (Marko, Luka). Karama ya Agano Jipya ya unabii lazima iwe na ukomo. Ufunuo wenye uvuvio umekoma (kama vile Yuda 3 na 20).

#### **MADA MAALUMU: UNABII WA AGANO JIPYA)**

- I. Sio sawa na Unabii wa Agano la Kale (BDB 611, KB 661; tazama Mada Maalumu:Unabii [Agano la Kale]), ambao una vidokezo vya upokeaji wa sheria za Kiyahudi na kunukuu mafunuo yaliyovuviwa toka kwa YHWH (kama vile Mdo. 3:18, 21; Rum. 16:26). Ni manabii tu waliweza kuandika maandiko.
  - A. Musa alitwa nabii (kama vile kumb. 18:15-21)
  - B. Vitabu vya historia (Yoshua – Wafalme [isipokuwa Ruthu]) waliitwa “manabii wa mwanzo” (kama vile Matendo. 3:24)
  - C. Manabii wanachukua nafasi ya makuhani wakuu kama chanzo cha habari kutoka kwa Mungu. (kama vile Isaya –Malaki)
  - D. Mgawanyo wa pili wa kanuni za kanisa la Kiebrania ni “Manabii” (kama vile Mt. 5:17; 22:40; Luka 16:16; 24:25, 27; Rum. 3:21).
  
- II. Katika Agano Jipya dhana ya unabii imetumika katika njia kadhaa tofauti tofauti.
  - A. Kuwarejea manabii wa Agano la Kale na jumbe zao zilizovuviwa (kama vile Mt. 2:23; 5:12 11:13; 13:14; Rum. 1:2).
  - B. Kuurejea ujumbe kwa mtu mmoja badala ya kikundi kichoungana (yaani, manabii wa Agano la Kale kimsingi waliongelea juu ya Israeli).
  - C. Kuwarejea wote wawili Yohana mbatizaji (kama vile Mt. 11:9; 14:5; 21:26 Luka 1:76) na Yesu kama mpiga mbiu wa ufalme wa Mungu (kama vile Mt. 13:57; 21:11, 46; Luka 4:24; 7:16; 13:33; 24:19). Yesu pia alidai kuwa mkuu kuliko manabii (kama vile Mt. 11:9; 12:41; Luka 7:26).
  - D. Manabii wengine katika Agano Jipya

1. Maisha ya awali ya Yesu kama ilivyoandikwa katika injili ya Luka (yaani., kumbu kumbu za Maria)
  - a. Elizabethi (kama vile Luka 1:41-42)
  - b. Zakaria (kama vile Luka 1:67-79)
  - c. Simoni (kama vile Luka 2:25-35)
  - d. Ana (kama vile Luka 2:36)
2. Ubashiri wa kejeli (kama vile. Kayafa, John 11:51)

E. Inarejea juu ya mtu anayeitangaza injili (ikijumuishwa kwenye orodha ya kipawa cha utangazaji katika 1 Kor. 12:28-29; Efe. 14:11)

F. Ikirejea juu ya vipawa vinavyoendelea kanisani (kama vile Mt. 23:34; Mdo. 13:1; 15:32; Rum. 12:6; 1 Kor. 12:10, 28-29; 13:2; Efe. 4:11) wakati mwingine hii inaweza kumaanisha kwa wanawake (kama vile Luka 2:36; Mdo. 2:17; 21:9; 1 Kor. 14:4-5).

G. Ikirejea kwa sehemu mafunuo ya kitabu cha ufunuo (kama vile Ufu. 1:3; 22:7, 10, 18,19)

### III. Manabii wa Agano Jipya

- A. Hawatoi ufunuo uliovuviwa kwa maana sawa kama manabii wa Agano la Kale waliofanya (yaani mafundisho ya Biblia). Usemi huu unawezekana kwa sababu ya Matumizi ya kifungu cha neno “Imani” (yaani kwa maana ya injili iliyokamilika) iliyotumika katika Matendo 6:7; 13:8; 14:22; Gal. 1:23; 3:23; 6:10; Flp. 1:27; Yuda 3, 20.

Dhana hii iko wazi kutokana na fungu kamili la maneno lililotumika katika Yuda 3, “imani ya mara moja pasipo kujirudia imekabidhiwa kwa watakatifu.” Imani ya “jumla pasipo kujirudia” inarejerea kwenye ukweli, mafundisho, dhana, maoni ya dunia juu ya mafundisho ya ukristo. Msisitizo huu unaotolewa mara moja tu ni msingi wa Kibiblia kwa ajili ya kuzuia uvuvio ulio wa kithiolojia wa maandiko ya Agano Jipya na pasipo kuruhusu maandiko mengine kufikirika kimafunuo (angalia Mada Maalumu: Uvuvio). Kuna maeneo mengi yenye utata, yasiojulikana katika agano jipya (Tazama Mada Maalumu: Fasihi za mashariki [mafumbo ya Kibiblia]), lakini waamini wanathibitisha kwa imani kuwa kila kitu “kinachohitajika” kwa ajili ya imani na utendaji inajumuishwa ikiwa na utosherevu wenye uwazi wa kutosha katika Agano Jipya. Dhana hii inaelezwa kama “ufunuo pembe tatu.”

1. Mungu amejidhirisha mwenyewe katika historia kwa muda muafaka (UFUNUO)
2. Amechagua baadhi ya waandishi wa kibinadamu kuweka kumbu kumbu na kuelezea matendo yake (UVUVIO).
3. Alimtoa Roho Wake ili kufungua mawazo na mioyo ya watu wapate kuyaelewa maandishi haya, si kwa ubora tu bali kwa utosherevu wa wokovu na maisha ya Mkristo yenye kufaa (NURU, tazama Mada Maalumu: nuru). Hoja iliyopo hapa ni kuwa uvuvio umewekewa ukomo kwa waandishi wa neno la Mungu. Hakuna maandiko mengine, maono au mafunuo yenye mamlaka. Sheria za kanisa zimefungwa. Tuna ukweli wote tunaohitaji ili kuitikia vizuri kwa Mungu. Ukweli huu unaonekana vizuri katika makubariano ya waandishi wa Kibiblia dhidi ya waumini watiifu wa ki-Mungu wasiokubali. Hakuna mwandishi au mnenaji wa kisasa aliye na kiwango cha uongozi wa ki-Uungu kama ambao waandishi wa neno la Mungu waliokuwa nacho.

B.Kwa namna nyingine manabii wa Agano Jipya ni sawa na wale wa Agano la Kale.

1. Utabiri wa matukio yajayo (kama vile Paulo, Mdo. 27:22; Agabo, Mdo. 11:27-28; 21:10-11; manabii wengine wasiotajwa Mdo. 20:23).
1. Kutangaza hukumu (kama vile Paulo, Mdo. 13:11; 28, 25-28)
2. Dalili za matendo ambayo dhahili yanaonyesha matukio (kama vile Agabo Matendo 21:11).

C.Mara zote wananena kweli ya injili, wakati mwingine kwa njia ya utabiri (kama vile Matendo 11:27-28; 20-23; 21:10-11) Lakini kimsingi huu sio mtazamo wenyewe. Unenaji wa unabii katika Wakorinto wa 1 kimsingi unaibainisha injili (kama vile 1 Kor. 14:24,39).

D. Ni Roho wa wakati ule ule akimaanisha kudhihirika wakati ule ule na utumiaji wa kiutendaji wa kweli ya Mungu kwa kila hali, tamaduni mpya au kipindi cha muda (kama vile 1 Kor. 14:3).

E. Walikuwa imara katika makanisa ya mwanzo ya Paulo (kama vile 1 Kor. 11:4-5; 12:28, 29;13:2, 8, 8,9; 14:1 3,4,5,6,22,24,29,31,32,37,39; Efe. 2:20; 3:5; 4:11; 1 The. 5:20) na wametajwa katika *Didache* (iliyoandikwa katika karne ya mwisho au karne ya pili tarehe haijulikani) na wakati wa mienendo ya Kikristo ya karne ya pili na tatu katika Afrika ya kaskazini.

#### IV. Je karama za Agano Jipya zimekoma?

- A. Swali ni gumu kulijibu. Linasaidia kufafanua jambo kwa kuelezea kusudi la karama. Je wanamaanisha kuthibitisha mafundisho ya awali ya kuhubiri injili au ni njia endelevu ya kanisa kujihudumia lenyewe kwenye ulimwengu ulipotea?
- B. Je mmoja aweza kuangalia kwenye historia ya kanisa kujibu maswali au Agano Jipya lenyewe? Hakuna kiashirio chochote kinachoonyesha katika Agano Jipya kuwa karama za rohoni zilikuwa za muda tu. Wale wote wanaojaribu kutumia 1 Kor 13:8-13 kuelezea habari hii wanatukanisha kusudi la mwandishi wa aya hii, ambayo inadokeza kuwa kila kitu kitatoweka isipokuwa upendo.
- C. Nathubutu kusema kuwa tangu Agano Jipya, si historia ya kanisa, ndiyo yenye mamlaka, waamini wanapaswa kuthibitisha kuwa karama zinaendelea. Hata hivyo ninaamini kuwa mila zinaathiri tafsiri za maandiko. Baadhi ya maandiko yalioko wazi hayatumiki tena (yaani busu takatifu, Baibui, makanisa kukutana nyumbani n.k). kama mila zinaathiri maandiko, hivyo kwa vipi zisiathiri historia ya kanisa?
- D. Hili ni swali ambalo haliwezi kujibiwa. Baadhi ya waumini wanatetea kuwepo na “ukoma” na wengine watetea “kusiwepo na ukomo”. Katika eneo hili, kama ilivyo kwa mambo mengi yaliyo fasiliwa, moyo wa mwamini unabaki kuwa ndo kiini. Agano jipya ni tata na la kitamaduni zaidi. Ugumu unaweza kuamua ni maandiko yapi yanaathiriwa na mila/historia na yapi yanaathiriwa kwa wakati wote na yapi kwa mila (kama vile Fee na Stuart, *How to read the Bible for all its Worth*, kur. 14-19 na 69-77 hapa ndipo pale mjadala wa uhuru na kuwajibika, unaopatikana katika Warumi 14:1-15, 13 na Kor. 8-10 unapokuwa wenye umuhimu mkubwa. Namna tunavyojibu swali ni muhimu katika njia mbili.
1. Kila mwamini anapaswa kutembea katika imani yake kwa mwanga walio nao. Mungu anaona mioyo yetu na nia.
2. Kila mwamini yampasa aruhusu waamini wengine kutembea katika uelewa wa imani. Lazima pawepo na uvumilivu ndani ya mipaka ya kibiblia. Mungu anatumia kupendane kama anavyotupenda.

E. Kwa kuhitimisha suala hili, Ukristo ni maisha ya imani na upendo, na sio tu thiolojia kamili. Uhusiano wetu na Yeye unaosababisha kuwepo na uhusiano na wengine ni muhimu zaidi kuliko habari au imani kamili.

**11:28 "njaa kubwa duniani kote. . . Claudio"** Tungo hii ya Kijiografia inamaanisha Dola ya Kirumi (kama vile Mdo. 17:6, 31; 19:27; 24:5). Klaudio alitawala kutoka miaka ya 41-54 b.k. Alifuatiwa na Caligula na Kutanguliwa na Nero. Kulikuwa na njaa kadhaa wakati wa utawala wake (kama vile Suetonius, *Life of Caludius* 18:2). Njaa mbaya kuliko zote kwa Palestina ilikuwa muda fulani kati ya miaka ya 44-48 b.k, kulingana na Josephus, *Antiq.* 20.5.2.

**11:29 "kila mtu kwa kadiri ya alivyofanikiwa, wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokaa Uyahudi "** Huu ni mmoja wa mkakati mkubwa wa kanisa la Mataifa kukuza ushirika na kanisa dada lililoko Yerusalemu. Hii ingeanzisha utaratibu huu katika makanisa ya Paulo (kama vile Mdo. 24:17; Rum. 15:2-28; 1 Kor. 16:1-4; 2 Kor. 8-9; Gal. 2:10).

**11:30 "Wakafanya hivyo.....wakawapelekea wazee"** Hii ni mara ya kwanza ya kutajwa kwa kanisa "wazee" (kama vile Mdo. 14:23; 15:2,4, 6, 22,23; 16:4; 20:17; 21:18). Neno "wazee" lina usawe na maneno kama "waangalizi," "maaskofu," na "wachungaji" (kama vile Mdo. 20:17,28 na Tito 1:5,7). Neno mzee (*presbuteros*) lina asili ya kikabila la Agano la Kale, wakati mwangalizi (*episkopos*) lina usuli wa jimbo la kiserikali la Kiyunani. Kwa dhahiri hii inamaanisha kundi Fulani la wazee au viongozi katika kanisa la Yerusalemu (kama vile Mdo.15:2,6,22,23). Zaidi sana kisehemu cha Uyahudi cha Agano Jipya kama Yakobo na Waebrania, bado wanatumia uelewa wa Kiyahudi wa viongozi wazee na viongozi wengine wa kanisa la mahali japo sio lazima inapokuja suala la mchungaji.

▣ **"ya Barnaba na Sauli."** Kuna mjadala mkubwa kama ikiwa kutembelea Yerusalemu kunakotajwa katika Gal. 2:2,10 kunamaanisha kutembelea huku au baraza la Yerusalemu linalotajwa katika Mdo. 15. Tunafahamu kidogo juu ya maisha ya kwanza ya Paulo na huduma.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, hii ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembele katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Mataifa waliokuwa wakimpokea Kristo walikuwa tatizo kubwa la kithiolojia?
2. Je toba ni kipawa cha Mungu (Mdo. 11:18) au hitaji la Agano (Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21)?
3. Kwanini Barnaba aliondoka na kwenda kumtafuta Sauli (Paulo)?

## MATENDO YA MITUME 12

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Yakobo anauawa Na Petro anatiwa Gerezani	Vurugu za Herode kwa kanisa	Mateso ya Herode Agrippa	Mateso zaidi	Petro akamatwa na kwa miujiza aokombolewa
12:1-5	12:1-5	12:1-5	12:1-5	12:1-5
Petro atolewa Gerezani	Petro afunguliwa toka gerezani		Petro aachiliwa toka gerezani	
12:6-17	12:6-19	12:6-11	12:6-10 12:11	12:6-11
		12:12-17	12:12-15 12:16-17	12:12-17
12:18-19		12:18-19	12:18-19a 12:19b	12:18-19
Kifo cha Herode	Kifo cha Herode Mkorofi	Kifo cha Herode Agrippa	Kifo cha Herode	kifo cha yule mtesaji
12:20-23	12:20-24	12:20-23	12:20 12:21-23	12:20-23
	Barnaba na Sauli Wanachaguliwa	Barnaba na Sauli huko Kipro  (12:24-13:12)		Barnaba na Sauli wanarudi Antiokia
12:24-25		12:24-25	12:24	12:24
	12:25-13:3		12:25	12:25

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("[A Guide to Good Bible Reading](#)")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya tatu
8. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

Ukoo wa Herode Mkuu (kwa taarifa zaidi fuata mwongozo wa Flavius Josephus katika Antiquities of the Jews).

- I. Herode Mkuu
  - A. Mfalme wa Yuda (37-4 k.k.)
    - B. Mt. 2:1-19; Luke 1:5
  - II. Wanawe
    - A. Herod Philip (Mwana wa Marianne wa Simoni)
      1. Mme wa Herodia
      2. Gavana wa Iturea (4 k.k. – 34 b.k)
      3. Mt. 14:3; Marko 6:17
    - B. Herode Philip (Mwana wa Cleopatra)
      1. Gavana wa eneo la Kaskazini na Magharibi mwa Bahari ya Galilee (4 k.k. – 34 b.)
      2. Luka 3:1
    - C. Herode Antipas
      1. Gavana wa Galilee na Perea (4 k.k.- 39 b.k)
      2. Mtendaji Yohana Mbatizaji
      3. Mt. 14:1-12; Marko 6:14,29; Luka 3:19; 9:7-9; 13:31; 23:6-12,15; Mdo. 4:27; 13:1
    - D. Archelaus, Herode Mtawala
      1. Mtawala wa Judea, Samaria and Idumea (4 k.k. – 6 b.k)
      2. Mt. 2:22
    - E. Aristobulus (Mwana wa Mariam)
      1. Mwanae wa pekee alikuwa Herode Agrippa I
      2. Alitawala sehemu yote ya Palestina (41-44 b.k)
      3. Akamwua Yakobo na kumweka gerezani Petro
      4. Mdo. 12:1-24; 23:35
        - a) Mwanae alikuwa Herode Agrippa II, Mtawala wa eneo la Kaskazini ( 50-70b.k)
        - b) Binti yake alikuwa Bernice
          - (1) Mke wa nduguye
          - (2) Mdo. 25:13-26:32
        - c) Binti yake alikuwa Drusilla
          - (1) Mke wa Felix
          - (2) Mdo. 24:24

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 12:1-5

1 Panapo majira yale yale Herode mfalme akanyosha mikono yake kuwatenda mabaya baadhi ya watu wa kanisa. 2 Akamwua Yakobo, ndugu yake Yohana, kwa upanga. 3 Na akiona ya kuwa imewapendeza Wayahudi akaendelea akamshika na Petro. Siku hizo zilikuwa siku za mikate isiyochachwa. 4 Alipokwisha kumkamata, akamweka gerezani akamtia mikononi mwa vikosi vinne vya askari wanne wanne, wamlinde, akitaka baada ya Pasaka kumtoa na kumweka mbele ya watu. 5 Basi Petro akalindwa gerezani, nalo kanisa likamwomba Mungu

**12:1 "Herode"** Hii inamrejelea Herode Agrippa I. alitawala sehemu mbali mbali za Palestina toka mwaka 37-44 b.k. Alikulia Rumi na kuwa rafiki wa Gayo, aliyemfuatia Mfalme mkuu Tiberia na baadaye akawa Mfalme Mkuu Kaligula. Wayahudi bila kusita walimkubali Herode kama kiongozi wao kwa sababu bibi yao (Mariam) alikuwa Malikia wa Hasmonen/ Maccabe (yaani., Mzalendo wa Kiyahudi). Alikuwa mfuasi wa karibu wa dini ya Kiyahudi (lakini yumkini kwa sababu ya kisiasa). Kwa maelezo zaidi kuhusu huyu Herode, angalia Josephus' *Antiq.* 19.7.3; 19.8.2.

▣ **"Kanisa"** angalia Mada Maalum katika Mdo. 5:11.

▣ **"kuwatenda mabaya"** Herode alilifanya hili kupata ukubalifu na kibali toka kwenye uongozi wa Kiyahudi (kama vile Mdo. 12:3,11). Viongozi wa Kirumi walifanya kitu kile kile (kama vile Mdo. 24:27; 25:9). Luka alitumia neno hili mara kadhaa (kama vile 7:6,19; 12:1; 14:2; 18:10). Lilikuwa ni neno la kwaida katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani kwa ajili ya kutibu maradhi. Msamiati wa Luka kwa upana umeshawishiwa na tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani.

**12:2 "Akamwua Yakobo, ndugu yake Yohana, kwa upanga"** Hii inarejelea kwa Mtume Yakobo, ambaye alikuwa nduguye Yohana (kama vile Luka 5:10; 6:14; 8:51; 9:28,54). Alikuwa ni mmoja wa wale tenashara (kama vile Mt. 17:1; 26:37; Marko 5:37; 9:2; 14:33; Luka 9:28). Kwa nini Yakobo auwawe na Petro aachwe ni fumbo la Mungu. Kukatwa kichwa kwa kutumia upanga ilikuwa ni njia ya kawaida kwa ajili ya adhabu kuu kwa raia wa Kirumi, lakini inaonekana ilikuwa chukizo kwa Wayahudi. Inafurahisha kuona kuwa kipindi hiki kanisa la awali halikutambua hitaji la kumbadilisha Yakobo kwa vile walikuwa na Yuda (kama vile Mdo. 1:15-20). Sababu kwa ajili ya hili haiko wazi, lakini yumkini ilikuwa ni mbinu ya Yuda, sio kifo, kilichosabaisha badiliko (kama vile Mdo. 1:15-26). Baadhi wanaweza kudai kuwa Paulo kumwita Yakobo, nduguye Yesu na kiongozi wa kanisa la Yerusalem, mtume (kama vile Gal. 1:19) ni kufanyika mbadala. Swali linahusiana na nafasi rasmi ya wale kumi na wawili wa mwanzo dhidi ya kipawa cha Utume endelevu (kama vile Efe. 4:11). Nikisoma James D. G. Dunn, *Unity and Diversity in the New Testament* imenisababisha kufikiri kuhusu tofauti iliyokuwepo ya muundo wa kimamlaka katika kanisa la karne ile ya .

1. Mitume wa Yerusalem
2. Moja ya wale mitume (Petro, Yakobo, Yohana)
3. Yakobo nduguye Yesu, aliyeliongoza kanisa la Yerusalem
4. Wale saba (Matendo 6) ambao walikuwa ni viongozi wa Kiyunani waliokuwa wakiongea Kiyahudi
5. Baadaye Paulo na Barnaba na wale waliowapeleka kanisani huko Antiokia ya huko Shamu

Kwa hili linaweza kuongeza mgawanyiko uhusiano na Ukristo, wafuasi wa dini ya Kiyahudi (Judaizers, waliodai kuwa na ujuzi wa kipekee (Gnostics), kikundi cha Kiyahudi kilichokubali utume wa Yesu na kukataa Uungu wake (Ebionites). Kati ya haya yote pia palikuwa na uongozi wao. Ule umoja ambao Luka mara nyingi aliurejelea kati ya Wakristo ulikuwa mgumu kuuendeleza. Mahubiri ya Yesu na maandiko yalikuwa magumu kiasi cha kuruhusu ufasiri mpana. Hii ndio sababu kuwa "kuongoza kwa imani" kulianza katika karne ya kwanza. Palitakiwa kuwepo kipimo cha kupima thiolojia ya kundi. Msisitizo wa uongozi tendaji wa kiroho wa Agano Jipya uligeuka kuwa muundo wa pamoja wa vituo vya kanisa vya Mashariki na Magharibi. Imani halisi ni suala muhimu kwa kizazi kile kilichoondolewa toka kwa mwanzilishi na wale mashuhuda.

**12:3 "Akamshika na Petro"** Huku ni kukamatwa kwa Petro mara ya tatu (kama vile Mdo. 4:3; 5:18). Wakristo hawakuachwa kwenye suala la mateso.

▣ **"Siku hizo zilikuwa siku za mikate isiyotiwa chachu"** Hii inarejelea kwenye sikukuu ya pasaka (kama vile Mdo. 12:4), pamoja na sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu, iliyodumu kwa siku nane (kama vile Kut. 12:18; 23:15; Luka



22:1). Zote zilisherehekewa na Waisrael kukombolewa toka kwenye ukandamizaji. Zilisherehekewa kwenye mwezi wa Nissan ambao kwetu ungalipaswa kuwa mwezi wa tatu au Nne, kutegemeana na kalenda ya Kiyahudi.

**12:4 "Vikosi vinne vya askari"** Hii ingalimaanisha vikundi vinne vya askari mara nne kwa siku, au watu kumi na sita. Hesabu inaonyesha uhusika wa Herode juu ya uwezekano au sababu ya Petro kutoroka (kama vile Mdo. 5:19).

**12:5 "kanisa likamwomba Mungu kwa juhudi kwa ajili yake"** Kanisa linasali (kama vile Mdo. 12:12), lakini inashangaza vile Mungu anavyojibu! "kihamasa " ni kielezi chenye uzito (kama vile Luka 22:44). Limetumika mara tatu tu katika Agano Jipya (kama vile 1 Pet. 1:22)

## **MADA MAALUM: MAOMBI YA KUSIHI**

- I. Utangulizi
  - A. Maombi ni ya muhimu kwa sababu ya mfano wa Yesu
    1. Maombi binafsi, Mk 1:35; Luka 3:21; 6:12; 9:29; 22:31-46
    2. Kulisafisha Hekalu, Mt. 21:13; Mk 11:17; Luka 19:46
    3. Maombi ya kuiga, Mt. 6:5-13; Luka 11:2-4
  - B. Maombi yanaweka kuamini kwetu kwenye hali ya kugusika kwa mtu, Mungu anayejali ambaye yupo , anayependa na kutenda kwa niaba yetu na kwa ajili ya wengine, kupitia maombi yetu.
  - C. Mungu binafsi amejizuia mwenyewe kutenda juu ya maombi ya watoto wake katika Nyanja nyingi (kama vile. Yakobo 4:2)
  - D. Kusudi kuu la maombi ni ushirika na muda wetu kwa Mngu wa Utatu.
  - E. Nafasi ya maombi ni mtu yeyote au kitu chochote kinachohusiana na waumini. Tunaweza kuomba,kuamini mara moja, au zaidi na zaidi tena kama fikra zinavyojirudia.
  - F. Maombi yanaweza kuhusisha ishara/dalili mbali mbali
    1. Sifa na kuabudu kwa Mungu wa Utatu
    2. Shukrani kwa Mungu kwa ajili ya uwepo wake, ushirika, na upaji wake
    3. Ukiri wetu wa utendaji dhambi, kwa hali zote za siku zilizopita na wakati sasa
    4. Ombi la mahitaji yetu muhimu au hamu yetu
    5. Usihi wetu pale tunapoyawasilisha mahitaji ya wengine mbele za Baba
  - G. Ombi la kusihi ni la ajabu. Mungu anawapenda wale tuwaombeao zaidi kuliko tufanyavyo, na bado maombi yetu yasifanye badiliko, uajibikaji, au hitaji lolote, sio tu kwetu binafsi, lakini hata kwao.
- II. Taarifa za Kibiblia
  - A. Agano la Kale
    1. Baadhi ya mifano ya maombi ya kusihi
      - a. Ibrahim aliomba maombi ya kuitetea Sodoma, Mwa. 18:22ff
      - b. Maombi ya Musa kwa ajili ya Israel
        - 1) Kutoka 5:22-23
        - 2) Kutoka 32:9-14,31-35
        - 3) Kutoka 33:12-16
        - 4) Kutoka 34:9
        - 5) Kumbu. 9:18,25-29
      - c. Samweli akiomba Israel
        - 1) 1 Samweli 7:5-6,8-9
        - 2) 1 Samweli 12:16-23
        - 3) 1 Samweli 15:11
      - d. Maombi ya Daudi kwa ajili ya watoto wake, 2 Samweli 12:16-18
    2. Mungu anawatafuta waombeaji, Isaya 59:16
    3. Dhambi ijulikanayo, usio ikiri, tabia usizozitubia zinaathiri maombi yetu
      - a. Zaburi 66:18

- b. Mithali 28:9
- c. Isaya 59:1-2; 64:7

B. Agano Jipya

1. Huduma ya kusihi/kuombea ya Mwana na Roho

- a. Yesu
  - 1) Warumi 8:34
  - 2) Waebrania 7:25
  - 3) 1 Yohana 2:1
- b. Roho Mtakatifu, Warumi 8:26-27

2. Huduma ya Paulo ya kuombea kwa kusihi

- a. Akiomba kwa ajili ya Wayahudi
  - 1) Warumi 9:1ff
  - 2) Warumi 10:1
- b. Akiliombea kanisa
  - 1) Warumi 1:9
  - 2) Waefeso 1:16
  - 3) Wafilipi 1:3-4,9
  - 4) Wakolosai 1:3,9
  - 5) 1 Wathesolanike 1:2-3
  - 6) 2 Wathesolanike 1:11
  - 7) 2 Timotheo 1:3
  - 8) Filemon, uk. 4
- c. Paulo analiomba kanisa limwombee
  - 1) Warumi 15:30
  - 2) 2 Wakorintho 1:11
  - 3) Waefeso 6:19
  - 4) Wakolosai 4:3
  - 5) 1 Wathesolanike 5:25
  - 6) 2 Wathesolanike 3:1

3. Huduma ya kanisa ya maombi ya kusihi

- a. Kuombeana wao kwa wao
  - 1) Waefeso 6:18
  - 2) 1 Timotheo 2:1
  - 3) Yakobo 5:16
- b. Maombi yaliyohitajiwa na makundi maalumu
  - 1) Adui zetu, Mat. 5:44
  - 2) Wakristo watembeaji, Waebrania 13:18
  - 3) Watawala, 1 Timotheo 2:2
  - 4) wagonjwa, Yakobo 5:13-16
  - 5) waliorudi nyuma, 1 Yohana 5:16

III. masharti kwa ajili ya maombi yaliyotakiwa kujibiwa

A. Mahusiano yetu kwa Yesu na Roho

- 1. Kutii ndani yake, Yohana 15:7
- 2. Katika jina lake, Yohana 14:13,14; 15:16; 16:23-24
- 3. Katika Roho, Waefeso 6:18; Jude 20
- 4. Kwa kadri ya mapenzi ya Mungu, Mathayo 6:10; 1 Yohana 3:22; 5:14-15

B. Visababishi

- 1. Kutotetereka, Mathayo 21:22; Yakobo 1:6-7
- 2. Unyenyekevu na toba, Luka 18:9-14
- 3. Kuomba vibaya, Yakobo 4:3

4. Ubinafsi , Yakobo 4:2-3

C. Mitazamo mingine

- a. Usitahimilivu
- b. Luka 18:1-8
- c. Wakolosai 4:2

1. Endelea kuomba

- a. Mathayo 7:7-8
- b. Luka 11:5-13
- c. Yakobo 1:5

2. Kutoelewana nyumbani, 1 Petro 3:7

3. Kuwa huru kutoka katika dhambi zijulikanazo

- a. Zaburi 66:18
- b. Mithali 28:9
- c. Isaya 59:1-2
- d. Isaya 64:7

IV. Hitimisho la kithiolojia

- A. Ni faida ipi, fursa ipi, shughuli na uwajibikaji upi
- B. Yesu ni mfano wetu. Roho ni mwongozo wetu. Baba anasubiri kwa hamu.
- C. Inaweza kukubadilisha wewe, familia yako, rafiki zako na hata dunia

#### **ANDIKO LA NASB( LILILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 12:6-17**

6 Hata wakati Herode alipotaka kumtoa, usiku ule ule Petro alikuwa analala katikati ya askari wawili, amefungwa minyororo miwili; walenzi mbele ya mlango wakailinda gereza. 7 Mara malaika wa Bwana akasimama karibu naye, nuru ikamulika mle chumbani, akampiga Petro ubavuni, akamwamsha, akisema, Ondoka upesi. Minyororo yake ikamwanguka mikononi. 8 Malaika akamwambia, Jifunge, kavae viatu vyako. Akafanya hivyo. Kisha akamwambia, Jivike nguo yako, ukanifuate. 9 Akatoka nje, akamfuata; wala hakujua ya kuwa ni kweli yaliyofanywa na malaika; bali alidhani kwamba anaona maono. 10 Na walipopita lindo la kwanza na la pili, wakaja hata mlango wa chuma wa kuingilia mjini, ukawafungukia wenyewe. Wakatoka nje, wakapita katika njia moja; mara malaika akamwacha. 11 Hata Petro alipopata fahamu akasema, Sasa nimejua yakini ya kuwa Bwana amempeleka malaika wake na kunitoa katika mkono wa Herode na katika kutazamia kote kwa taifa la Wayahudi. 12 Na alipokuwa akifikiri haya akafika nyumbani kwa Mariamu, mamaye Yohana, ambaye jina lake la pili ni Marko; na watu wengi walikuwa wamekutana humo wakiomba. 13 Naye alipobisha kilango cha lango, kijakazi, jina lake Roda, akaja kusikiliza. 14 Alipoitambua sauti ya Petro, hakukifungua lango, kwa ajili ya furaha, bali alipiga mbio, akaingia ndani akawaambia kwamba Petro anasimama mbele ya lango. 15 Wakamwambia, Una wazimu. Lakini yeye akakaza sana, akasema ya kwamba ndivyo hivyo. Wakanena, Ni malaika wake. 16 Petro akafuliza kugonga, hata walipokwisha kumfungulia wakamwona, wakastaajabu. 17 Naye akawapungia mkono wanyamaze, akawaeleza jinsi Bwana alivyomtoa katika gereza. Akasema, Kampasheni Yakobo na wale ndugu habari hizi. Akaondoka, akaenda mahali pengine.

**12:6 "Usiku ule ule"** Maandiko ya Luka yanaainishwa na viashirio vya muda (kama vile matendo 12:3,4,5,6,7,8,10,18). Lakini uwe mwangalifu wa kuyatafasiri haya kama historia ya kimagharibi, kimfuatano, utaratibu wa kupanga matukio. Luka ana kusudi la uinjilisti wa kithiolojia.

▣ **"katikati ya maaskari wawili"** Mstari huu unaonyesha kutokuwepo uwezekano wa Petro kutoroka. Kiwastani kuwepo na tumaini la kuweza kuachiwa (kama vile Mdo. 5:19).

**12:7 "Malaika wa Bwana akasimama karibu naye"** Sio kawaida kuwa kuingilia kati kwa nguvu isio ya kawaida ya malaika wa Bwana (kama vile Mdo. 5:19; 7:30,35,38,53; 8:26; 10:3,7,22) na Roho Mtakatifu (kama vile Mdo. 8:29,39;10:19) panaonekana kuwepo mabadiliko katika kitabu chote cha Matendo ya Mitume. Inavyoonekana Roho anaongea kwa welewa, bali malaika ni udhahiri wa nje kimwili. Inafurahisha kuona muunganiko wa kiasili na nguvu zisizo za kawaida katika habari hii (ikifanana na mapigo ya Wairael kipindi wakitoka Misri).

▣ **"Ondoka upesi"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu inayomaanisha suala la muhimu. Kwa nini malaika huyu ana uharaka? Je hayuko katika kudhibiti matukio?

**12:8 "Jifunge, kavae viatu vyako"** Haya yote yako katika kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu.

▣ **"Jivike nguo yako, ukanifuata"** Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu ikifuatiwa na kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Hakika malaika alikuwa katika uharaka wa kuitenda kazi hii! Alikuwa ni mmoja wa malaika wa kuogofya!

**12:9** Petro hakujua kama haya yalikuwa maono, ndoto, au ukweli halisi(kama vile Mdo. 12:11-12; 10:17,19; 11:5).

**12:11 "Hata Petro alipopata fahamu"** Luka anatumia kifungu mfanano katika kumwelezea mtoto wa kipekee Yesu (kama vile Luka 15:17). Ghafla ukweli juu ya uzoefu na madhara yake yakawa juu yake (kama vile Mdo. 12:12).

**12:12 "Nyumbani mwa Mariaum"** Maria lilikuwa ni jina lililozoeleka. Kuna akina Maria wengi waliotajwa katika injili.

1. Mama yake na Yesu (kama vile Luka 1:27)
2. Maria Magdala, mwanafunzi toka Galilaya (kama vile Luka 8:2; 24:10)
3. Mama yake Yakobo na Yohana (kama vile Luka 24:10)
4. Dada yake na Martha na Lazaro (kama vile Luka 10:39,42)
5. Mke wa Cleophas (kama vile Yn 19:25)
6. Mama yake Yohana aitwaye Marko (hapa)

▣ **"Mamaye Yohana"** Hii inarejelea kwa mama yake Yohana aitwae Marko. Kanisa la kwanza lilikutana katika nyumba ya familia hii huko Yerusalemi (kama vile Mdo. 12:12). Palikuwa ni sehemu moja kati ya zile tatu Bwana alipojidhahilisha baada ya kufufuka na kuja kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste. Yohana aitwae Marko akaambatana na Paulo na mpwaye Barnaba (kama vile Col. 4:10) katika safari ya kwanza ya kimisionari (kama vile Mdo. 12:25-13:13). Kwa sababu Fulani Fulani aliliacha kundi na kurudi nyumbani (kama vile Mdo. 15:38). Barnaba walitaka kumjumuisha kwenye safari ya pili ya umisionari, lakini Paulo akakataa (kama vile Mdo. 15:36-41). Hii ilipelekea Paulo na Barnaba wakatengana. Barnaba akamchukua Yohana aitwae Marko wakaenda Kipro (kama vile Mdo. 15:39). Baadae, wakati Paulo akiwa gerezani, alimnena Marko vizuri (kama vile Col. 4:10) na baadae tena katika mara ya pili wakati Paulo akiwa kifungoni huko Roma, kabla ya kifo chake, alimtaja tena Marko (kama vile 2 Tim. 4:11). Inavyoonekana Marko akajakuwa sehemu ya kundi la Petro kwenye umisionari (kama vile 1 Pet. 5:13). Eusebius' *Eccl. His.3.39.12* inatupatia habari ya kufurahisha juu ya uhusiano wa Marko kwa Petro. "katika kitabu chake kitiwacho Papias kinatupatia habari juu ya semi za Bwana alizozipata toka kwa Aristion au alipata kujifunza moja kwa moja toka kwa mzee wa kanisa Yohana. Walipolileta hili mbele ya uangalizi wa wasomi, kwa hiyo nalazimika kufuatisha maelezo ambayo tayari yamekwisha nukuliwa toka kwake yakiwa na kipande kidogo cha habari ambacho alikiweka kinachomhusu Marko, aliyeandika injili:

Hili, pia mzee wa kanisa alipenda kulisema. Marko, ambaye alikuwa mfasiri wa Petro, akayaandika kwa umakini, lakini pasipo mpangilio, yote ambayo Bwana aliyasema na kuyatenda. Kwa vile hakuwahi kumsikia Bwana au kuwa mmoja wa wafuasi wake, lakini baadaye, kama nilivyokwisha kusema, mmoja wa Petro. Petro alipendelea kubadilisha mafundisho yake kwenye matukio, pasipo kufanya mpangilio wowote wa maneno ya Bwana, ili kwamba Marko apate kuyathibitisha katika kuandika vitu Fulani Fulani alivyokumbuka. Kwa vile alikuwa na kusudi moja, kutokuacha chochote alichokisikia, na kukosea kueleza kuhusu hicho" (uk 152)

Katika nukuu hii Papias anamrejelea "Yohana mwenye umri mkubwa." Irenaeus anasema "na vitu hivi vilitolewa ushahidi katika maandishi na Papias, wale wasikilizaji wa Yohana, na mwenza wa Polycarp." Hii inadokeza Papias aliyasikia toka kwa Yohana Mtume

▣ **"Watu wengi walikuwa wamekutana humo wakiomba"** Miundo ya visarufi vya maneno haya vinaonyesha kuwa kanisa lilikuwa likikusanyika na kukusudia kubaki katika maombi (kauli tendwa timilifu yenye kuendelea ikifuatiwa na kauli ya kati [shahidi] yenye kuendelea.

**12:13 "Kilango cha lango"** Hili ni lango dogo kwenye mtaa. Palikuwepo na lango kubwa orofani.

▣ **"Rhoda"** Jina lake lilimaanisha "ua la waridi." Haijulikani ikiwa alikuwa mjakazi wa nyumba ile au mmoja wa wale wana maombi.

**12:15 "Una wazimu"** Kanisa lilikuwa likiomba Mungu apate kutenda, lakini walipata mshangao mkubwa alipotenda (kama vile Mdo. 12:16).

▣ **"Wakaendelea kusema"** Kuna kauli zisizo timilifu tendaji elekezi katika muktadha huu, ambazo zinadokeza kuwa udhahilisho wa Rhoda na wale waliokuwa katika maombi katika chumba cha juu mwikio ulitokea zaidi ya mara moja.

▣ **"Ni malaika wake"** Malaika anachukua sehemu muhimu katika maandiko ya Luka. Inavyoonekana Wayahudi waliamini kuwa malaika mwangalizi mmoja angaliweza kuchukua sura yao ya kimwili (kwa maelezo mazuri juu ya asili na imani ya kiyahudi kuhusu malaika waangalizi, angalia *Encyclopaedia Judaica*, juzuu. 2, uk. 963). Hakuna msingi wa kimaandiko kwa ajili ya imani hii. Maendeleo haya kuhusu thiolojia ya malaika yawezakuwa imekuja toka kwenye dhana ya *fravashi* katika nadharia ya Zoroastrer. Mengi juu ya elimu ya dini ya Kiyahudi kuhusu thiolojia ya malaika inaweza kuangaliwa kwenye ushawishi huu wa Kiajemi. Kuna baadhi ya ushahidi wa kimaandiko kwa ajili ya malaika waangalizi kwa ajili ya waamini wapya (kama vile Mt. 18:10). Malaika ni watumishi wa wale waliokombolewa (kama vile Heb. 1:14).

**12:17 "Naye akawapungua mikono wanyamaze"** Kwa wazi kabisa haya ni maelezo ya ushahidi wa macho (kama vile Mdo.13:16). Luka anaweka kumbu kumbu ishara hizi mara kadhaa (kama vile Mdo. 13:16; 19:33; 21:40).

▣ **"Kampasheni Yakobo na wale ndugu habari hizi"** Hii inaonyesha kuwa Yakobo, nduguye Yesu, alikuwa amekwisha kuwa kiongozi wa kanisa la Yerusaleim (kama vile Mdo. 15:13-21).

## **MADA MAALUM: YAKOBO, NDUGUYE YESU**

Aliitwa "Yakobo mwenye haki" na baadaye akajulikana kwa jina maarufu "camel knees-mwenye magoti kama ngamia" kwa sababu muda mwingi alipiga magoti kuomba (toka kwa Hegesippus, imenukuliwa na Eusebius Hist. Eccl. 2.23-24; 4-18).

- A. Yakobo hakuwa mwamini mpaka baada ya ufufuo (kama vile Marko 3:21; Yn 7:5). Yesu alimtokea binafsi baada ya ufufuo (kama vile 1 Kor.15:7)
- B. Alikuwepo kwenye chumba cha ghorofani akiwa na wanafunzi (kama vile Mdo. 1:14) na yumkini pia Roho anashuka siku ya Pentekoste.
- C. Alikuwa ameo (kama vile 1 Kor. 9:5)
- D. Anarejelewa na Paulo kama nguzo ya kanisa la Yerusaleim (yumkini Mtume, kama vile Gal. 1:19; angalia Mada Maalum: Kutumwa [apostellō]) lakini hakuwa mmoja wa wale kumi na wawili (kama vile Gal. 2:9; Acts 12:17; 15:13 na kuendelea; 21:18).
- E. Katika *Antiquities of the Jews*, 20.9.1, Josephus anasema kuwa alipigwa mawe mwaka wa 62 b.k kwa amri iliyotoka Msadukayo toka baraza kuu la Sinagogi, wakati desturi zingine (waandishi wa karne ya

pili, Clement of Alexandria or Hegesippus) anasema aliondolewa nje ya ukuta wa hekalu.

- F. Kwa vizazi vingi baada ya kifo cha Yesu ndugu wa Yesu alichaguliwa kuwa kiongozi wa kanisa la Yerusalem.
- G. Alikuwa ndiye mwandishi wa kitabu cha "Yakobo" na nduguye mwandishi wa kitabu cha Agano Jipya "Yuda" (kama vile Yuda uk. 1).

▣ **"Akaenda mahali pengine"** Hakuna ajuaye wapi Petro alikwenda, lakini inavyoonekana hakwenda Rumi kama wengine wanavydhani kwa sababu yupo katika kumbu kumbu za baraza la Yerusalem katika Matendo 15. Hata kama nguvu za ajabu za Mungu zilimwokoza Petro. Hii haimaanishi kuwa asingekuwa wa kujali au kutarajia miujiza hii itokee kila wakati. Kumbuka Yakobo alikuwa amekwisha kuuwawa! Petro pia alituma ujumbe kwa kanisa kutarajia mateso zaidi kwa sababu ya ukombozi wake.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 12:18-19**

**18 Hata kulipopambauka askari wakaingiwa na fadhaa nyingi, amekuwaje Petro. 19 Na Herode alipomtafuta, asimwone, aliwauliza-uliza wale walinzi, akaamuru wauawe. Kisha akatelembia kutoka Uyahudi kwenda Kaisaria, akakaa huko**

**12:18 "Wakaingiwa na fadhaa nyingi"** Inafurahisha kuwa aliyaongea mambo kinyume, mara nyingi kwa kutoeleza kikamilifu (kama vile Mdo. 12:18; 15:2; 19:11,23,24; 20:12; 26:19,26; 27:30; 28:2, angalia tanbihi #8, uk. 134, wa G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*). Fasihi hii haijulikani katika fasihi ya Kiebrania, lakini mara nyingi inatumika katika fasihi ya Kiyunani. Luka alikuwa msomi mkubwa wa Kiyunani!

**12:19 "Aliwauliza-uliza wale walinzi, akamua wauawe"** Haya ndiyo matokeo ya andiko hili (kama vile NKJV, NRSV, TEV), lakini haijaelezewa kinagaubaga (kama vile NJB). Baadhi ya tafasiri zinatumia miandiko ya kulala kuyatambua maneno ambayo hayako katika Kiyunani. kama mlinzi akipoteza mfungwa wake, atastahili kuibeba adhabu ya mfungwa huyo (kama vile Mdo. 16:27; 27:42, Code of Justinian 9.4.4).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 12:20-23**

**20 Naye Herode alikuwa amewakasirikia sana watu wa Tiro na Sidoni; wakamwendea kwa nia moja, na wakiisha kufanya urafiki na Blasto, mwenye kukitunza chumba cha mfalme cha kulalia, wakataka amani; kwa maana nchi yao ilipata riziki kwa nchi ya mfalme. 21 Basi siku moja iliyoazimiwa, Herode akajivika mavazi ya kifalme, akaketi katika kiti cha enzi, akatoa hotuba mbele yao. 22 Watu wakapiga kelele, wakisema, Ni sauti ya Mungu, si sauti ya mwanadamu. 23 Mara malaika wa Bwana akampiga, kwa sababu hakumpa Mungu utukufu; akaliwa na chango, akatokwa na roho.**

**12:20 "Alikuwa amewakasirikiwa sana watu wa Tiro na Sidoni"** Herode alikasirika na kendelea kuwa hivyo (kauli isiotimilifu ya hali ya mafumbo). Tukio hasa la kistoria na mtu mwenyewe havijulikani katika historia, lakini eneo la Tiro na Sidoni lilitegemea mazao ya kilimo yaliyozalishwa huko Galilea (kama vile 1 Fal. 5:11; Ezra 3:7; na yumkini Ezek. 27:17).

**12:21 "Herode akajivika mavazi ya kifalme"** Hili lilitokea katika karne ya 44 b.k. kwa habari kamili kuhusu tukio hili angalia Josephus' *Antiq.* 19.8.2 ( iliyofasiliwa na William Whiston, Kregal). "katika kila tukio la kisherehe, umati mkubwa wa watu ulikusanyika pamoja kwa wale watu maarufu, na kufanya hivyo kulimheshimisha katika jimbo zima. Katika siku ya pili ilimuonyesha akiwa amevalia mwili mzima mavazi yaliyotengenezwa kwa madini ya fedha, na kimuktadha kwa kweli alionekana kustaajibisha, aliingia ukumbini mapema asubuhi; wakati ambao vazi lake la madini ya fedha lilimekameka kwa mionzi ya jua iliyolimrika,

akapendeza kwa mtindo wa kushangaza, aliweza kung'ara na kuleta mshangao kwa wale waliokuwa wakimtaazama kwa makini: na wakati huo huo wapambe wake wakapiga makelele, mmoja toka upande huu, na mwingine upande ule, (ingawa si kwa yale mazuri yake) kwamba alikuwa mungu: na wakaongeza,—'utuhemu; ingawa mpaka sasa tumeliheshimisha hili tu kama mtu, lakini bado mbeleni tutamiliki huu mwili usio haribika.' Kwa kufanya hivyo mfalme wala hakupata kuwakemea, wala kuukataa uovu wao. Lakini, baadaye akiwa ameangalia juu, akamwona bundi akiwa amekaa juu ya kamba kwa kichwa chake, na kwa haraka akatambua kuwa huyu ndege alikuwa mjumbe wa keleta habari mbaya, kama mwanzoni alivyokuwa mjumbe mzuri wa keleta habari nzuri kwake; na aliingiwa na majonzi mazito. Maumivu makali pia aliayasikia tumboni mwake, na yakaanza kwa hali ya vurugu kubwa. Baadaye akawaangalia rafiki zake, na kusema,—'mimi, ambaye munaniita mungu, nimeamriwa sasa hivi niiondoke katika uzima huu; wakati hatma inanihukumu yale maneno ya uongo mnayoniambia; na mimi, ambaye ninyi mliniita nisyekufa, pasipo kuchelewa sasa nachuliwa na mauti'" (uk. 412). Hasira ya Herode na hali ya kimwili iliyoambatana nayo pia vimeelezwa kwa undani wa maelezo ya kutisha katika *Antiq.* 17:6:5. The *Jerome Biblical Commentary* (juzuu. 2, uk. 191) inatutaarifu kuwa maelezo haya ya kuogofya ya kifo cha mtu ilikuwa ni njia ya waandishi wa kale kuonyesha kile kilichotokea kwa wale wanao mkosea Mungu

1. Antiochus IV Epiphanes – II Macc. 9:5-18
2. Herod Mkuu – Josephus, *Antiq.* 17.6.5

**12:23 "Malaika wa Bwana"** Hii inarejelea juu ya malaika aletaye mauti (kama vile Kut. 12:23; 2 Sam. 24:16; 2 Fal. 19:35). Kifo kipo katika mikono ya Mungu, na sio shetani. Huu ni mfano wa hukumu ya kiulimwengu.

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 12:24

24 Neno la Bwana likazidi na kuenea.

12:24 Hii ni tabia ya maelezo mafupi ya Luka (*kama vile Mdo. 6:7; 9:31; 12:24; 16:5; 19:20; 28:31*)

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 12: 25

25 Na Barnaba na Sauli, walipokwisha kutimiza huduma yao, wakarejea kutoka Yerusalemu, wakamchukua pamoja nao Yohana aitwaye Marko.

**12:25** Hii inaanza na habari ya safari ya kimisiaonari ya Paulo. Kuna tofauti ya maandiko katika mstari huu ukihusiana iwapo alirudi Yerusalemu (kama vile *eis*, MSS X na B) au "toka" Yerusalemu (kama vile *apo*, MS D au *ek*, MSS P74, A). Matendo 13 inaanza na Barnaba na Sauli huko Antiokia ("toka Yerusalemu hadi Antiokia," kama vile MS E na matoleo ya kale ya Kilatini, Shamu na Coptic).

▣ **"Marko"** angalia "watu waliotajwa," utangulizi wa Matendo 16

## MASWALI YA MJADALA

Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Mungu alimwacha Petro na siyo Yakobo?
2. Je kanisa lililokusanyika lilishangaa kusikia maombi yamejibiwa? Elezea madhara yake
3. Je waumini wanahitaji kuwa na malaika ikiwa wana Roho aishiye ndani yao?

## MATENDO YA MITUME 13

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Barnaba na Sauli Wanawekwa wakfu	Barnaba na Sauli wanateuliwa	Barnaba na Sauli katika Kipro	Barnaba na Sauli wanachaguliwa na kutumwa	Kutumwa katika umisheni
13:1-3	(12:25-13:3)	(12:23-13:12) 13:1-3	13:1-2 13:3	13:13
Mitume wahubiri Huko Kipro	kuhubiri katika Kipro		katika Kipro	Kipro: Mchawi Elima
13:4-12	13:4-12	13:4-12	13:4-5 13:6-11a 13:11b-12	13:4-5 13:6-12
Paulo na Barnaba Huko Antiokia Ya Pisidia	Antiokia ya Pisidia	safari ya Antiokia ya Pisidia na Ikonio	ndani ya Antiokia katika Pisidia	wakafika katika Antiokia ya Pisidia
13:13-16a 13:16b-25	13:13-41	13:13-16a 14:16b-25	13:13-16a 13:16b-20a 13:20b-25	13:13-16a 13:16b-25
13:26-41		13:26-41	13:26-41	13:26-31 13:32-37 13:38-39 13:40-41
13:42-43	Baraka na mgogoro Antiokia 13:42-52	13:42-43	13:42-43	13:42-43 Paulo na Barnaba Wanahubiri Kwa mataifa
13:44-52		13:44-47 13:48-52	13:44-47 13:48 13:49-52	13:44-47 13:48-49 13:50-52

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("[A Guide to Good Bible Reading](#)")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili



3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Haya ni maelezo ya safari ya kwanza ya umisheni ya Paulo na Barnaba. Sehemu za kitabu cha Matendo ya Mitume zilizobaki zitaachwa kwa ajili ya huduma ya Paulo.
- B. Ingekuwa jambo la msaada iwapo utaangalia ramani nyuma ya Biblia yako au Atlasi na kufuatilia maeneo ya kijiografia yanayotajwa katika Mdo. 13 and 14.
- C. Kuna mabadiliko dhahiri katika Matendo ya Mitume 13 na 14 kutoka uongozi wa Barnaba hadi uongozi wa Paulo.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB( LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 13: 1-3

<sup>1</sup>Na huko Antiokia katika kanisa lililokuwako palikuwa na manabii na waalimu, nao ni Barnaba, na Simeoni aitwaye Nigeri, na Lukio Mkirene, na Manaeni aliyekuwa ndugu wa kunyonya wa mfalme Herode, na Sauli. <sup>2</sup> Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia. <sup>3</sup> Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao.

**13:1"Antiokia"** Angalia maelezo katika Matendo ya Mitume 11:19.

☐ **"kanisa"** Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 5:11.

☐ **"manabii na waalimu"** Hizi karama mbili za Roho zimeorodheshwa katika 1 Kor. 12:28 na Efe. 4:11. Utungaji wa kisarufi ni ule ambao si yumkini aidha watu watano waliorodheshwa wote walikuwa manabii na waalimu ama ikiwa wale watatu wa mwanzo ni manabii na wale wawili wa mwisho ni waalimu.

Tatizo la neno hili ni, "Ni kwa jinsi gani karama za unabii wa Agano Jipya zinahusiana na manabii wa Agano la Kale?" Katika Agano la Kale manabii ndiyo waandishi wa Maandiko. Katika Agano Jipya kazi hii wanapewa wale Mitume kumi na wawili wa mwanzo na wasaidizi wao. Kama neno "mtume" linavyoshikiriwa kama karama endelevu (kama vile Efe. 4:11), lakini kwa kazi yenye mabadiliko baada ya kifo cha wale Kumi na Wawili, kama ilivyo, ni utawala wa nabii. Uuvio umetoweka; hakuna Andiko lililovuviwa zaidi. Kazi ya awali ya manabii wa Agano Jipya ni kuihubiri injili, lakini pia ni kazi tofauti, huenda ni kwa namna ya kuzitumia kweli za Agano Jipya katika hali ya sasa na mahitaji. Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 11:27.

Karama ya ualimu imeorodheshwa katika Matendo ya Mitume 13:1 katika muungano na unabii, lakini katika Efe. 4:11 karama hii imeunganishwa na wachungaji. Katika 2 Tim. 1:11 Paulo anasema kwamba yeye ni mhubiri, mtume, na mwalimu. Hapa inaonekana kusimama kwa upekee, kama ilivyo katika Rum. 12:7. Karama hii pia inajadiliwa katika Yakobo 3:1 na kuendelea. Hii inamaanisha kwamba karama hizi za uongozi zinaweza kuuunganishwa katika njia tofauti kwa ajili ya kukidhimahitaji ya kanisa katika siku zile au eneo lile. Kila kiongozi aliyekirimiwa kwa karama hizi (kama vile Efe. 4:11) aliihubiri injili, lakini katika njia tofauti (kwa kushurutisha, kuhubiri, kuagiza).

### MADA MAALUM: UVUVIO

Haya ni maelezo ya imani kwamba Mungu alikuwa anahusika kwa bidii katika kuweka kumbukumbu ya matukio Yake, ahadi, na mapenzi yake kwa binadamu. Hii "ni" kujifungua kibinafsi kiungu! Kufungua huku kunaitwa"

ufunuo." Kuweka kumbukumbu huku kwa baadaye kunaitwa"uvuvio."

Neno pekee linalotumika "uvuvio" katika Biblia liko katika 2 Tim. 3:16 na kiuhalisia "Mungu alipumulia." Tazama "maandiko" katika Agano Jipya siku zote yanarejerea Agano la Kale (yaani 2 Tim. 3:15 ikimaanisha makuzi ya kiyahudi ya Timotheo). Angalia kusudi la maandiko liko sehemu mbili.

1. hekima inayopelekea wokovu, 2 Tim. 3:15
2. mafunzo ya haki, 2 Tim. 3:16

Tazama namna Yohana 5:39; 1 Kor. 15:3-4; na 1 Pet. 1:10-12 Angalia Agano la Kale linatuelekeza katika Kristo. Yesu mwenyewe anakiri katika Luka 24:25-27! Roho aliwaongoza waandishi wa Agano la Kale (kama vile 2 Pet. 1:20-21). Kanisa lilikubali Kanoni (angalia Mada Maalum: Kanoni) ya Agano la Kale. Walilionga kama lililojaa uvuvio (kama vile Mt. 5:17-19). Hata hivyo, waligundua pia katika Agano Jipya, ambalo lilijumuisha maneno ya Yesu na matendo (kama vile Mt. 5:21-48; Ebr. 1:1-2). Yesu yu kamili, mwisho, na kukamilisha ufunuo wa YHWH (kama vile Yohana 1:1-5,14; Kol. 1:15-16). Yeye anatimiza ahadi ya Agano la Kale ya Masihi (yaani Mt. 26:31,56; 14:27,49; Luka 20:17; Yohana 12:14-16; 13:18; 15:25; 17:12; 19:24-36; Mdo.1:16; 3:18,21-26; 4:25-28).

Roho lazima afungue ufahamu na moyo ili mtu aweze kuelewa (kama vile Mdo. 8:34-35; 13:27). Roho aliwaongoza waandishi wa kibiblia kuelezea maneno kibinadamu, nahau, na ufafanuzi wa kweli za ufunguzi binafsi wa Mungu katika Yesu (kama vile Yohana 14:26; 15:26-27; 1 Kor. 2:10-11,13-16).

Mjadala mzuri wa kimuhtasari unapatikana katika Millard J. Erickson, *Christian Theology*, 2nd ed., ukurasa. 224-245. Pia mjadala mzuri wa kifasihi wa mchakato kutoka "ya kinywa" yaliyojikita katika jamii ya nyaraka zilizoandikwa ni H. Walton na D. Brent Sandy, *The Lost World of Scripture* (2013).

## MADA MAALUMU: NURU

Mungu ametenda hapo mwanzo ilikujidhihirisha wazi kwa wanadamu. Kithiolojia, huu unaitwa ufunuo. Alichagua watu kadhaa kuweka kumbukumbu na kueleza ufunuo wake huu. Katika thiolojia, huu unaitwa uvuvio. Ametuma Roho kusaidia wasomaji kuelewa neno lake. Katika thiolojia, huu unaitwa mwangaza. Tatizo linatokea pale tunapobisha kuwa Roho anahusika katika kuelewa neno la Mungu- Sasa, kwa nini panakuwa na tafsiri nyingine kiasi hicho? Sehemu ya tatizo ipo kwa uelewa wa nyuma wa wasomaji au uzoefu binafsi. Daima hoja binafsi inaelezwa kwa kutumia Biblia katika uthibitisho wa kimaandishi au mtindo wa kuhakiki. Daima thiolojia inachagua maneno ya kusoma Biblial ikiruhusu kusoma maneno kadha na kwa njia zilizopendekezwa. Mwangaza hauwezi kulinganishwa na uvuvio ingawa sehemu zote mbili Roho mtakatifu anahusika.

Njia rahisi ya kusoma ni kujaribu kufafanua wazo kuu katika aya, na siyo kutafsiri kila neno kwa kina katika maandiko. Ni wazo la juu tu ambalo linapeleka ukweli hasili wa mwandishi wa kwanza. Kudokezea kitabu au sehemu ya kifasihi inasaidia kufuatilia kusudio la mwandishi wa awali aliyevuviwa. Hakuna mfasili aliyevuviwa.

Hatuwezi kuzalisha njia ya tafasiri ya mwandishi wa Kibiblia. Tunaweza na lazima tujaribu kuelewa walichokuwa wakisema enzi za nyakati zao na kuwakilisha ukweli huo nyakati zetu. Kuna sehemu za Biblia ambazo ni tata au zimefichika (hadi wakati/kipindi kingine). Daima patakuwapo kutokukubaliana katika baadhi ya maandiko na masomo lakini lazima tuseme wazi kweli halisi na kuruhusu uhuru wa tafsiri binafsi ndani ya mipaka ya kusudio la mwandishi wa mwanzo. Wafasiri lazima watembe ndani ya mwanga walio nao, na siku zote wakiwa tayari kwa mwanga zaidi kutoka katika Biblia na Roho. Mungu atatuhukumu kutokana na kiwango cha uelewa wetu na jinsi tulivyoishi katika uelewa huu.

☐ "Simeoni aitwaye Nigeri" Hili nenola Kilatini *nigeris* linamaanisha eusi au eupe. Baadhi ya watoa maoni anajaribu kulihusianisha huyu Simoni na Marko 15:21.

☐ "Lukio Mkirene" Bila shaka huyu ni mmoja wa Wayahudi wa Kiyunani ambaye alihubiri katika Mataifa katika Antiokia (kama vile Matendo ya Mitume 11:20). Huenda huyu si yule Lukio anayetajwa katika Rum. 16:21.

☐ **"Manaeni aliyekuwa ndugu wa kunyonya wa mfalme Herode" Neno *Manaen*** ni muundo wa Kiyunani wa neno la Kiebrania *Manahem*, ambalo linamaanisha "mfariji." Mtu huyu kwa vyo vyote vile alikuwa ndugu wa kuzaliwa (fasihi ya Kiyunani) wa Herode Antipa (angalia Utangulizi wa Matendo ya Mitume 12) au wa kukua pamoja naye (mafunjo yaliyotumika kuandika lugha ya Koine). Luka huenda alikuwa na habari nyingi sana zilizomhusu Herode Antipa (Ndugu wa Kunyonya) kutokana na mahojiano na mtu huyu.

**13:2**

**NASB** "hudumia"

**NKJN** "walipokwisha fanya huduma"

**NRSV** "abudu"

**TEV** "wakitumika"

**NJB** "wakijitolea kwa ibada"

Hili neno la Kiyunani *leitourgia* (neno ambatani kutokanana "hadhara" na "kazi") ambapo tunalipata neno la Kiyunani liturujia. Kiuhalisia hili lilirejelea yule mtu aliyefanya huduma ya hadhara kwa ajili yao. Katika muktadha huu neno hili linamaanisha kipindi cha kuyatafuta mapenzi ya Mungu wakati wa huduma ya ibada. Kitenzi kingerejelea kanisa zima au wale watu watano aliorodheshwa.

☐ **"walipokwisha kufunga"** Katika Agano la Kale kuna siku moja tu ya kufunga kwa mwaka mzima, Siku ya Upatanisho, Mambo ya Walawi 16. Hata hivyo, katika kipindi cha karne ya kwanza, sheria za Dini ya Kiyahudi ziliboresha kwa kuweka siku mbili za kufunga ndani ya juma moja. Ijapokuwa tendo la kufunga halipendelewi na waamini, mara nyingi linasaidia katika kuyatambua mapenzi ya Mungu (kama vile Matendo ya Mitume 14:23).

## **MADA MAALUM: KUFUNGA**

Kufunga, ingawa hakujaamriwa katika Agano Jipya, kulitarajiwa katika wakati muafaka kwa ajili ya wanafunzi wa Yesu (kama vile Mt. 6:16,17; 9:15; Marko 2:19; Luka 5:35). Kufunga kunakostahili kunapatikana katika Isaya 58. Yesu alijiweka mwenyewe kuwa wa mfano (kama vile Mt. 4:2). Kanisa la mwanzo lilifunga (kama vile Mdo. 13:2-3; 14:23; 2 Kor. 6:5; 11:27). Mienendo na tabia ni vya muhimu; kwenda na wakati; umbali na jambo kutokea ni la kiuchaguzi. Kufunga katika agano la kale sio sharti la waamini wa Agano Jipya (kama vile Mdo. 15:19-29). Kufunga sio njia ya ya kuonyesha u-kiroho cha mtu (kama vile Isaya 58; Mt. 6:16-18), lakini ni njia ya kumsogeza mtu karibu na Mungu na kuhitaji mwongozo wake (yaani., Yesu, Mt. 4:2). Yaweza kuwa ni msaada wa kiroho.

Tabia ya kanisa la mwanzo dhidi ya uwazi ulisababishwa na waandishi walioingiza neno "kufunga" katika sura mbali mbali (yaani., Mt. 17:21; Marko 9:29; Mdo. 10:30; 1 Kor. 7:5). Kwa ajili ya maelezo zaidi juu ya ya maandiko haya yenye maswali mwone Bruce Metzger's *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, kilichochapishwa na United Bible Societies.

☐ **"Roho Mtakatifu akasema"** Huu ni uthibitisho mwingine wa kibiblia wa nafsi ya Roho Mtakatifu katika Matendo ya Mitume (angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 1:2). Kwa vyo vyote vile ini sauti iliyosikika wazi ama ilikuwa ilikuwa ya ndani, hii si yumkini (kama vile Matendo ya Mitume 8:29; 10:19; 11:12; 20:23; 21:11). Ni wazi kwamba huu ulikuwa ujumbe wa kipekee sana (kama vile Matendo ya Mitume 16:6-7), huenda ujumbe huu ulityolewa kupitia manabii.

☐ **"Nitengeeni"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Hili neno *aphorizō* lina maana nyingine iliyo sawa na neno "takatifu" (*hagiazō*). Hili linamaanisha kuweka kando na kuweka wakfu kwa ajili ya kazi ya Uungu iliyoelekezwa (kama vile Rum. 1:1; Gal. 1:15).

☐ Baada ya "kuwatenga" katika andiko la Kiyunani hiki ni kiambata *dē*, ambacho kinadokeza msisitizo (kama vile Luka 2:15; 1 Kor. 6:20). Tendo hili huleta arabuni kwa wito wa Roho Mtakatifu. Kuna ufanano katika usemi wa Paulo wa Matendo ya Mitume 15:36.

☐ **"kwa kazi ile niliyowaitia"** Hii ni kauli ya kati elekezi (yenye ushahidi) ya wakati timilifu. Roho Mtakatifu ndiye aitaye na kuweka wakfu kwa ajili ya huduma (kamavile 1 Kor. 12:7,11).

**13:3** Mstari huu una kauli tatu endelevu za wakati uliopita usio timilifu ambazo zinaelezea juu ya maandalizi ya kiroho kwa ajili ya kuwatuma wamisionari kutoka kanisa lililoko Antiokia.

1. walifunga
2. waliomba
3. waliwawekea mikono

Hili linaonekana kuwa muungano wa matendo ya kusanyiko zima, si manabii wengine na waalimu. Kanisa zima lilipaswa kushiriki katika kazi za Agizo Kuu!

☐ **"wakaweka mikono yao juu yao"** Huu mstari mahususi ni moja ya maandiko yenye utata ambao linafanywa katika uwekaji wetu wakfu kisasa na kujikita. Hata hivyo, hili haliendi sawa kama ulivyo msingi wa kibiblia kwa utaratibu wa sasa wa kimadhehebu. Kna mifano mingi inayoonekana kuhusu tendo la "kuwekea mikono" katika Biblia.

1. katika Agano la Kale kwa kusudi la
  - a. utambulishjo wa kujitoa dhabihu (kama vile Law. 1:4; 3:2; 4:4; 16:21)
  - b. baraka (kama vile Mwa. 48:13 na kuendelea Mt. 19:13,15)
  - c. kumwagiza mrithi (kama vile Hes. 27:23; Kumb. 34:9)
2. Katika usuli wa kitabu cha Agano Jipya ni sawa sawa na ilivyotofautiana
  - a. kwa uponyaji (kama vile Luka 4:40; 13:13; Matendo ya Mitume 9:17; 28:8)
  - b. wekwa wakfu au kuagiza kwa ajili ya kazi fulani (kama vile Matendo ya Mitume 6:6; 13:3)
  - c. iliyohusiana na kumpokea Roho Mtakatifu au karama za kiroho (kama vile Matendo ya Mitume 8:17; 19:6; 1 Tim. 4:14; 2 Tim. 1:6)
  - d. marejeleo ya mafundisho ya msingi ya Dini ya Kiyahudi au kanisa (kama vile Ebr. 6:2)

Huku kuwekea mikono halikuwa tendo la lililoanzishwa. Watu hawa tayari walikuwa wamekwisha itwa, kirimiwa, viongozi watenda kazi. Kwao hii haikuwa huduma mpya waliohitiwa, bali ulikuwa upanuzi wa kile ambacho tayari walikuwa wamekwisha kukifanya.

Kuwekwa Wakfu huchangia kuchochea tofauti miongoni mwa waamini. Kunatoa imani kwa makasisi wa kilei wasio kuwa wa kawaida unaogawanyika sehemu mbili zinazokinzana. Hilineno la Kiyunani *cleros* (kurithi kwa kubahatisha) na *laos* (Neno la Kiyunani linalomaanisha watu), linapotumika katika Agano Jipya, mara nyingi hili linarelea juu ya kundi zima la waamini. Waamini wote wanaitwa, wanakirimiwa, ni wahudumu wa injili kwa wakati wote (kama vile Efe. 4:11-12). Hakuna ushahidi wa kibiblia unaoonyesha kuwatenga waamini katika mtiririko wa kimakundi. Waamini wote wanakirimiwa huduma kwa ajili y amwili wa Kristo (kama vile 1 Kor. 12:7, 11).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 13:4-12**

<sup>4</sup>Basi watu hao, wakiisha kupelekwa na Roho Mtakatifu wakatelemkia Seleukia, na kutoka huko wakasafiri baharini hata Kipro. <sup>5</sup> Na walipokuwa katika Salami wakalihubiri neno la Mungu katika masinagogi ya Wayahudi, nao walikuwa naye Yohana kuwa mtumishi wao. <sup>6</sup> Walipokwisha kupita katikati ya kisiwa chote mpaka Pafo, wakaona mtu mmoja, mchawi, nabii wa uongo, Myahudi jina lake Bar-Yesu; <sup>7</sup> mtu huyu alikuwa pamoja na liwali Sergio Paulo, mtu mwenye akili. Yeye liwali akawaita Barnaba na Sauli waje kwake, akataka kulisikia neno la Mungu. <sup>8</sup> Lakini Elima, yule mchawi (maana ndiyo tafsiri ya jina lake), akashindana nao, akitaka kumtia yule liwali moyo wa kuiacha ile imani. <sup>9</sup> Lakini Sauli, ambaye ndiye Paulo, akijaa Roho Mtakatifu, akamkazia macho, <sup>10</sup> akasema, Ewe mwenye kujaa hila na uovu wote, mwana wa Ibilisi, adui wa haki yote, huachi kuzipotoa njia za Bwana zilizonoyoka? <sup>11</sup> Basi, angalia, mkono wa Bwana u juu yako, nawe utakuwa kipofu, usilione jua kwa muda. Mara kiwi kikamwangukia na giza, akazunguka-zunguka na kumtafuta mtu wa kumshika mkono na kumwongoza. <sup>12</sup> Ndipo yule liwali, alipoyaona

**13:4 "wakiisha kupelekwa na Roho Mtakatifu"** Muktadhahuu hauelezi juu ya mamlaka ya kanisa la mahali, bali ile malaka ya Roho. Huyu ni sehemu ya Uungu (angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:32) unaosisitizwa katika Matendo ya Mitume. Kifungu cha "zama mpya za ki- Masihi" kilijulikana kama "zama za Roho." Yeye anahita, anakirimia, anaongoza, hukumbusha, na kutia nguvu (kama vile Yohana 14:16-17,26; 15:26; 16:7-15). Hakuna huduma ya kudumu ama yenye matokeo bora ambayo inaweza kuwepo pasipo uwepo na baraka Zake.

☐"**Seleukia**" Huu ulikuwa uwanja wa mji wa Antiokia ya Shamu. Huu ulikuwa maili zipatazo kumi na tano kusinimagharibi. Jilna lake linarejea juu ya ukuu wa Iskanda mkuu (Seleukidi), ambaye alitawala eneo hili baada ya kifo cha Iskanda mkuu.

☐"**Kipro**" Hapa ndipo nyumbani kwa Barnaba (kama vile Matendo ya Mitume 4:36) ambapo kulikuwa na idadi kubwa ya watu wa Kiyahudi. Katika Agano la Kale mji huu unajulikana kama *Kittim*. Huu haukuwa ushahidi wa kwanza wa Kikristo kukihusu kisiwa hiki (kama vile Matendo ya Mitume 11:19-20).

**13:5 "Salami"** Huu ulikuwa uwanja wa mji wa kisiwa cha Kipro. Hiki kilikuwa kituo kisiwa cha kibiashara.

☐"**wakalihubiri neno la Mungu katika masinagogi**" Sababu ya tendo hili wazi

1. Wayahudi hawa tayari walikuwa wamekwisha kulijua Agano la Kale
2. Wayahudi walikuwa watu waliochaguliwa (kama vile Mwa. 12:1-3) na walikuwa na nafasi ya kwanza ya kuitikia (kama vile Matendo ya Mitume 3:26; 13:46; 17:2; 18:4,19; 19:8; Rum. 1:16)
3. Katika masinagogi huduma zilikuwa wale watu wa Mataifa ambao [a] walikuwa wamekwisha kuvutiwa na Mungu mmoja wa kweli na [b] kulijua Agano la Kale

Hii ilikuwa njia ya kawaida ya kimisionari ya Paulo popote palipokuwa na sinagogi.

☐"**Yohana**" Huyu anamrejelea Yohana Marko ambaye nyumba yake ndiyo iliyotumiwa na wanafunzi kwa ajili ya kukutanika (kama vile Matendo ya Mitume 12:12). Huyu pia ni mwandishi wa jadi wa Injili ya of Marko, ambayo inaonekana kunukuu ushuhuda wa ushahidi wa macho wa Mtume Petro. Huyu pia ni ndiye chanzo cha mabishano makubwa kati ya Paulo na Barnaba ambayo yalifungua mlango wa kupasuka kwakundi la kimisionari (kama vile Matendo ya Mitume 15:36-41). Hata hivyo, baadaye Paulo anamtaja Yohana Marko katika njia inayokubalika (kama vile Kol. 4:10; 2 Tim. 4:11 na Filemoni 24). Tazama maelezo kamili katika Utangulizi wa Matendo ya Mitume 16.

**13:6 "Walipokwisha kupita katikati ya kisiwa chote"** Bila shaka hili linamaanisha kwamba walisitisha na kuhubiri katika kila sinagogi lililokuwa katika kisiwa hiki.

☐"**Pafu**" Hili linarejelea juu ya Pafu mpya, katika matengenezo kutoka mji wa Pafu wa zamani ipatayo maili saba nje kidogo. Miji yote miwili imeitwa majina haya badala ya miungu ya Kipafu *Paphian*. Huyu alikuwa mungu wa upendo aliyejulikana kama *Aphrodite*, *Astarte*, *Venus*, n.k. Mji huu ulikuwa makazi ya kiutawala na kisiasa ya mji wa Kipro.

☐"**Bar-Yesu**" Mtu huyu alikuwa nabii wa uongo wa Kiyahudi. Jina lake lilimaanisha "mwana wa Yoshua." Tunajifunza kutoka Matendo ya Mitume 13:8 kwamba kwa sifa ya Elima yule mchawi. Neno hili mchawi linaakisi usawa wa Kiyunani wa mzizi wa Kiaramu ambao unamaanisha "mlozi" (kama vile Matendo ya Mitume 13:10). Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 8:9.

**13:7 "pamoja na liwali Sergio Paulo"** Kumekuwa na mjadala mkubwa kuhusu uhalisia wa historia ya matukio yaliyoelezwa na Luka. Hapa kuna mfano mzuri wa usahihi wa Lukea mwana historia. Huyu anamuita mtu huyu "liwali," ambapo inamaanisha Kopro lilikuwa jimbo la usenetari wa Kirumi. Tunajifunza kuwa hili lilitokea katika

miaka ya 22 b.k kwa amri kutoka kwa Augustus. Pia tunajifunza kutokana na maandishi ya Kilatini ya huko Soloi kwamba Sergio Paulo alianza uliwali wake katika 53 b.k. Habari zaidi za wagunduzi wa mambo ya kale kutoka katika ulimwengu wa Kishamu wa karne ya kwanza, usahihi zaidi wa maelezo ya Luka unakubalika.

☐"**mtu mwenye akili**" Neno hili linatumika kwa mapana tofauti ya maana nyingine. Katika muktadha huu neno hili linamaanisha kwamba hyu alikuwa na uwezo wa kutawala kwa namna ya kufaa. Pia kwa kumwelezea namna hii inaonyesha kwamba injili haikuleta matokeo kwa maskini na wale wasio na elimu, bali pia kwa matajiri na wasomi (kama vile *Manaen*13:1). Inawezekana kwamba moja ya malengo ya Luka ya kukiandika kitabu cha Matendo ya Mitume yalikuwa kuonyesha kwamba injili haikuuyumbisha utawala wa Kirumi.

**13:8 "Elima"** Inaonekana kwamba hili jina la Kiyunani ni unukuzi wa

1. neno la Kiaramu la mtu mwenye akili (mwenye busara, wa kiungu, yule awezaye kuona mbali na kuitawala kesho kwa kutumia nguvu zisozonekana /uweza wa ulimwengu usioonekana, AB, juzuu. 2, uk. 487)
2. neno la Kiaramu linaloamaanisha yule anayetafsri ndoto

☐"**yule mchawi**" Neno hili linahusiana na neno "mamajusi," ambalo lilimaanisha watu wa Kaldea-Midiani wenye hekima, kama Danieli (kama vile Dan. 2:2; 4:9; Mt. 2:1). Hata hivyo, kwa siku za Paulo, hili lilitumika kwawachawi waliokuwa wakitembea maeneo mbalimbali na maajabu ya kutisha katika ulimwengu wa kipindi cha kati ya Wayunani-Warumi. Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 8:9.

☐"**imani**" Hili neno linatumika katika namna tatu za kipekee katika Agano Jipya:

1. kuamini kwa upekee katika Yesu Kristo kama Mwokozi
2. uaminifu, kuishi ki- Mungu
3. maudhui ya thiolojia ya injili (yaani, mafundisho, kama vile Yuda 3, 20)

Utata unaofanana unaonekana katika Matendo ya Mitume 6:7. Hapa neno hili linaonekana kurejelea #3 kwa sababu ya kiambata na muktadha. Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 3:16 na 6:5.

**13:9 "Paulo"** Haya ni matumizi ya kwanza ya uweza wake wa Kirumi katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Paulo linatoka katika maneno ya Kiyunani linaloamaanisha "uchache" Baadhi wanafikiria kuwa ni kulingana na maumbile ya Paulo ya kimwili, wengine wanafikiri kuwa ni tathmini yake mwenyewe kama "mdogo wa mitume" kwa sababu ya kuliudhi kanisa. Yawezekana lilikuwa ni jina lake la pili kupewa na wazazi wake baada ya kuzaliwa.

☐"**Paulo, akijaa Roho Mtakatifu**" Nguvu ya Roho Mtakatifu ambayo ililiongoza kanisa la mwanzo inaelezwa kwa kutumia neno "kujaza" (kama vile Matendo ya Mitume 2:4; 4:8,31; 6:3; 7:55; 9:17; 13:9,52). Ie nguvu endelevu, kujazwa Roho Mtakatifu kila siku ni hali ya kawaida kwa waamini wote (kama vile Efe. 5:18). Katika Matendo ya Mitume mara kwa mara hili linahusiana na ujasiri wa kuihubiri injili.

☐"**akamkazia macho**" Angalia maelezo kamili katika Matendo ya Mitume 1:10.

**13:10** Paulo anaubainisha unabii wa uongo wa Kiyahudi kwa kutumia maneno kadhaa.

1. "wamejaa udanganyifu," inamaanisha kulaghai kwa kutumia maneno ya ushawishi (haya ni matumizi pekee ya neno hili katika maandiko ya Luka)
2. "wamejaa hila," huu ni muundo wa neno la Kiyunani unaomaanisha kufanya jambo fulani kwa mapungufu au kwa upuuzi, lakini linakuwa na maana ya uovu (kama vile Matendo ya Mitume 18:14). Neno hili linapatikana katika Matendo ya Mitume pekee (kama vile Matendo ya Mitume 13:10; 18:14).
3. "mwana wa uovu," Hii ni nahau ya Kisemitiki (kama vile Matendo ya Mitume 3:25; 4:36) kwa yule mwenye sifa ya matendo ya uovu (kama vile Mt. 13:38; Yohana 8:38,41,44, angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 5:3)

4. "adui wa haki," Neno hili limetumika mara kadhaa katika maandiko ya Luka zikiwemo nukuu za Agano la Kale (kama vile Luka 1:71,74; 20:43; Matendo ya Mitume 2:35). Yote yaliyo ya Mungu, mtu huyu alikuwa kinyume nayo. Angalia [MADA MAALUM: HAKI](#) katika Matendo ya Mitume 3:14.
5. Paulo analitumia neno jumuishi "yote" mara tatu kuonyesha utimilifu wa shauku ya udhalimu wa mtu huyu

☑️"**huachi kuzipotoa njia za Bwana zilizonyoka**" Swali hili linatarajia jibu la "ndiyo". Neno "haki" au "nyooka" katika Agano Jipya linaakisi dhana ya Agano la Kale ihusuyo haki, ambayo ilimaanisha kiwango au futi ya kupimia. Maneno ya Agano Jipya "kuposha" au "kukaidi" linaakisi maneno ya Agano la Kale yazungumziayo dhambi, ambayo yalitofautiana kulingana na viwango, ambavyo ni Mungu Mwenyew. Mtu huyu kila alichokifanya kilikuwa cha kupotosha (yaani, kinyume na haki). Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 3:14.

**13:11"mkono wa Bwana"** Hiki ni kifungu cha Kisemitiki kihusucho sifa za kibinadamu ambacho kinarejelea uweza na uwepo wa YHWH (kama vile Luka 1:66; Matendo ya Mitume 11:21). Katika Agano la Kale mara nyingi hili linarejelea hukumu yam Mungu (kama vile Kut. 9:3; 1 Sam. 5:6; Ayubu 19:21; 23:2; Zab. 32:4; 38:2; 39:10), kama ilivyo hapa.

☑️"**nawe utakuwa kipofu**" Haya maneno bainishi yenye nguvu yazungumziayo uovu na uasi ambapo Paulo anamweleza mtu huyu na muundo wa adhabu yake ya ki-Ungu ya muda yanaweza kuakisi maisha ya Paulo ya awali. Sasa anakumbuka na kujiona katika ualimu huu wa uongo wa Kiyahudi na hila yake (kama vile Matendo ya Mitume 9:8). Upofu mara nyingi unatumika katika maana ya kimafumbo ya uhaba wa kutoyapokea mambo ya kiroho (kama vile Yohana 9; Matendo ya Mitume 9; pia tazama Kumb. 28:28-29).

**13:12"alipoyaona yaliyotendeka, akaamini"** Hili ni neno lile lile la Kiyunani (*pisteuō*, nomino inaweza kutafsiriwa kama kuamini, imani, au sadiki) linalotumika katika Agano Jipya kwa ajili ya imani ya kweli. Huyu liwali aliitikia habari ya injili. Macho ya mtu huyo yakatiwa upofu (kiuhalisia); macho ya mtu huyo yalikuwa wazi (kistiari). Hii ndiyo siri ya imani na kutokuwa na imani (kama vile Yohana 9). Angalia Mada Maalum: Imani (nomino, kitenzi, na kuvumishi) katika Matendo ya Mitume 3:16 na Imani ya Agano la Kale katika Matendo ya Mitume 6:5.

#### ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 13:13-16a

<sup>13</sup> Kisha Paulo na wenziwe wakang'oa nanga wakasafiri kutoka Pafo, wakafika Perge katika Pamfilia. Yohana akawaacha akarejea Yerusalemu. <sup>14</sup> Lakini wao wakatoka Perge, wakapita kati ya nchi, wakafika Antiokia, mji wa Pisidia, wakaingia katika sinagogi siku ya sabato, wakaketi. <sup>15</sup> Kisha, baada ya kusomwa torati na chuo cha manabii, wakuu wa sinagogi wakatuma mtu kwao, na kuwaambia, Ndugu, kama mkiwa na neno la kuwafaa watu hawa, lisemeni. <sup>16</sup> Paulo akasimama, akawapungia mkono, akasema, Enyi waume wa Israeli,

**13:13 "Paulo na wenziwe"** Kwa uwazi kabisa uongozi ulibadilika. Kuanzia sasa katika kitabu cha Matendo ya Mitume jina la Paulo litaorodheswa kwanza.

☑️"**Perge katika Pamfilia**" Perge ulikuwa mji mkuu wa jimbo dogo la Kirumi pwani ya Pamfilia (kusini ya kati ya Uturuki). Mji huu ulikuwa maili kadhaa bara kwa ajili ya kuwazuia maaramia wa baharini. Kwa uwazi kabisa Paulo hakuhubiri eneo hili kwa wakati huo, bali alihubiri eneo hili kwa baadaye (kama vile Matendo ya Mitume 14:25). Hakuna ushahidi wa kihistoria wa kundi ka ki- Kristo katika eneo hili kwa miaka mia na zaidi. Alikuwa mtu wa kupita tu eneo hili.

☑️"**Yohana akawaacha akarejea Yerusalemu**" Luka analinukuu tukio hili, lakini hatoi ushahidi kwa nini (ama alivyofanya mwandishi wa Agano Jipya). Angalia Utangulizi wa Matendo ya Mitume 16, alirudi katika kuifanya kazi ya Bwana!

**13:14 "Antiokia, mji wa Pisidia"** Kiuhalisia hili linamaanisha "Antiokia hadi Pisidia" kwa sababu mji huu ulikuwa ndani ya watu wa kundi la watu wa aina moja huko Filigia Jimbo la Kirumi la Galatia. Hii ilikuwa wilaya ya kundi la watu wa aina moja, huenda kutoka Ulaya.

▣ **"katika sinagogi siku ya sabato"** Hili linaweza kudokeza kutoka machweo skiku ya Jumamosi. Wayahudi walihesabu muda kutoka asubuhi hadi jioni, kwa kufuata Mwanzo 1.

▣ **"wakaketi"** Hii inaweza kuwa nahau inayodokeza mtu ambaye alikuwa akizungumza katika sinagogi. Walimu wa Sheria za Kiyahudi mara nyingi walikuwa wakifundisha huku wamekaa (kama vile Mt. 5:1; Luka 4:20). Mara nyingi Masinagogi yaliruhusiwa kwa ajili wageni kuzunguka zunguka na kuzungumza kama walivyotaka (kama vile Matendo ya Mitume 13:15).

**13:15 "kusomwa torati na chuo cha manabii"** Hii ilikuwa sehemu ya mpangilio wa ufanano wa huduma katika sinagogi katika siku za Yesu. Kiuhalisia Sheria ya Musa pekee ndiyo iliyosomwa, lakini but Antiokio IV Epiphanes alilizuia hili katika 163 b.k. Kisha Wayahudi walikiiondoa chuo cha Manabii. Kipindi cha uasi wa Wamakabayo, Dini ya Kiyahudi ilirejeshwa na vyote Torati na chuo cha Manabii kiliendelea kusomwa kwa pamoja kama muundo muhimu wa huduma ya sinagogi (kama vile Matendo ya Mitume 13:27). Angalia Mada Maalum ifuatayo.

## **MADA MAALUM: KANONI YA KIEBRANIA**

Biblia ya Kiebrania imegawanyika kwenye migawanyo mitatu (Biblia ya Kiingereza inafuata mpangilio wa tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani).

1. Torati (vitabu vitano vya Musa), Mwanzo – Kumbu kumbu la Torati
2. Manabii (Nevi'im)
  - a. Manabii wa mwanzo, Yoshua – Wafalme (isipokuwa kitabu cha Rutu)
  - b. Manabii wa baadaye, Isaya – Malaki (isipokuwa kitabu cha Maombolezo na Daniel)
3. Maaandiko (Kethubim)
  - a. Fasihi za Hekima, Ayubu – Mithali
  - b. Kipindi cha Wayahudi baada ya kutoka uhamishoni, Ezra – Esta
  - c. Vitabu vitano vya Kiebrania (Megilloth) (vile vitabu vitano, vilivyosomwa kwenye sherehe)
    - 1) Kitabu cha Rutu (kilichosomwa siku ya Pentekoste)
    - 2) kitabu cha Mhubiri (kilichosomwa kwenye hema la kukutanikia)
    - 3) kitabu cha Wimbo ulio bora (kilichosomwa siku ya Pasaka)
    - 4) kitabu cha Maombolezo (kilichosomwa kukumbuka kuanguka kwa Yerusalem mwaka wa 586 k.k.)
    - 5) kitabu cha Esta (kilichosomwa wakati wa kupiga kura)
  - d. 1 na 2 Nyakati
  - e. Danieli

Kitabu kipya cha Kanoni ni kile cha 2 Nyakati. Tarehe kamili haijulikani kwa sababu matoleo ya kiuandishi kwa baadhi ya koo.

▣ **"wakuu wa sinagogi"** Hawa walikuwa watu wa mashtaka ya kuhimarisha ulinzi na utaratibu wa ibada (kama vile Luka 8:41,49). Mara nyingi hawa waliwapa wageni nafasi ya kuzungumza.

▣ **"kama mkiwa na neno la kuwafaa watu hawa"** Hii ni sentensi yenye amri dalaja la kwanza, ambayo inadhaniwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi wa makusudi yake ya kiuandishi. Hiki kilikuwa kipengele cha kawaida cha ibada ya sinagogi. Paulo alichukulia kama sehemu ya manufaa.



**13:16"Paulo akasimama"** Mara kwa mara walimu wa Kiyahudi walikuwa wamekaa wakati wa kufundisha; hata hivyo, hii ilikuwa desturi ya kipindi cha kati ya Wayunani-Warumi ya kusimama wakati wa kufundisha. Paulo aliiboresha namna yake na uwasilishaji wake kwa hadhira.

▣**"akawapungia mkono"** Paulo alitumia ishara kuwanyamazisha. Luka anautaja undani wa huu wa ushahidi wa macho mara kwa mara (kama vile Matendo ya Mitume 12:17; 13:16; 19:33; 21:40).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 13:16b-25**

<sup>16b</sup> nanyi mnaomcha Mungu, sikilizeni. <sup>17</sup> Mungu wa watu hawa Israeli aliwachagua baba zetu, akawatukuza watu hao, walipokuwa wakikaa kama wageni katika nchi ya Misri, na kwa mkono ulioinuliwa akawatoa, akawaongoza. <sup>18</sup> Na kwa muda wa miaka kama arobaini akawavumilia katika jangwa. <sup>19</sup> Na alipokwisha kuwaharibu mataifa saba katika nchi ya Kanaani akawapa nchi yao iwe urithi kwa muda wa miaka kama mia nne na hamsini; <sup>20</sup> baada ya hayo akawapa waamuzi hata zamani za nabii Samweli. <sup>21</sup> Hatimaye wakaomba kupewa mfalme; Mungu akawapa Sauli mwana wa Kishi, mtu wa kabila ya Benyamini, kwa muda wa miaka arobaini. <sup>22</sup> Na alipokwisha kumwondoa huyo, akamwinua Daudi awe mfalme wao ambaye alimshuhudia, akisema, Nimemwona Daudi, mwana wa Yese, mtu anayeupendeza moyo wangu, atakayefanya mapenzi yangu yote. <sup>23</sup> Katika uzao wake mtu huyo Mungu amewaletea Israeli Mwokozi, yaani, Yesu, kama alivyoahidi; <sup>24</sup> Yohana alipokuwa amekwisha kuwahubiri watu wote wa Israeli habari za ubatizo wa toba, kabla ya kuja kwake. <sup>25</sup> Naye Yohana alipokuwa akimaliza mwendo wake alinena, Mwanidhani mimi kuwa nani? Mimi siye. Lakini, angalieni, anakuja mmoja nyuma yangu ambaye mimi sistahili kumlegezea viatu vya miguu yake.

**13:16b "waume wa Israeli, nanyi mnaomcha Mungu, sikilizeni"** Kulikuwa na makundi mawili, Wayahudi na Watu wa Mataifa "wale wanaomcha Mungu" (kama vile Matendo ya Mitume 13:26; 10:2,22,35). Hotuba hii inafanana sana na hotuba ya Stefano ya Matendo ya Mitume 7. Katika namna nyingi Paulo walishawishiwa kwa undani na ufahamu wa Stefano wa Agano la Kale na injili.

**13:17** Paulo alianza mtazamo wake wa historia ya Agano la Kale kwa wito wa Mashahidi (Abraham, Isaka, na Yakobo katika Mwanzo) na ukamataji na ukombozi kutoka Misri (Kutoka-Kumbukumbu la Torati).

▣**"na kwa mkono ulioinuliwa akawatoa, akawaongoza"** Hii ni taswira ya Agano la Kale inayofanana (kama vile LXX Kut. 6;1,6) ya YHWH ya maneno yasiyojitosheleza. Hili ni sawa na kifungu cha maarifa yahasuyo elimu ya kibinadamu, "Mkono wake wa kuume." Biblia inazungumza juu ya msamiati wa Mungu mwenye kisasi (yaani, maarifa ya sifa za kibinadamu) hata kama yeye ni wa milele, asiyeonekana, Roho iliyo kila mahaliali. Hizi tofauti za kibiblia ndiyo chanzo cha kutoelewana na semi zinazopitiliza. Biblia inamzungumzia Mungu katika utofauti, stiari, na ukanaji. Mungu yu mbali sana kuliko, mipaka ya wakati, wanadamu walio na mipaka ya kidunia wanaweza kutamba au kueleza! Angalia Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:33.

**13:18 "kwa muda wa miaka kama arobaini akawavumilia katika jangwa"** Aya hii inaakisi Kumbu. 1:31 na inaweza kutafsriwa kama "kulisha kama muuguzi" (kama vile MSS A, C). Hili linaakisi vitabu vya Agano la Kale vya Kutoka na Hesabu.

Neno "arobaini" mara nyingi ni namba ya mzunguko. Kiuhalisia wakati ule wa kutoka Horebu hadi Shitimu ilikuwa miaka thelathini na nane kwa kipindi cha mika miwili huko Horebu (Sinai). Angalia Mada Maalum katika Marendo ya Mitume 1:3.

**13:19 "kuwaharibu mataifa saba" Mataifa ya Palestina** yanaweza kuelezwa katika namna kadhaa.

1. maneno ya jumla, Wakanaani (yaani, wahivi, kama vile Mwa. 10:18-29; Amu. 1:1) au Waamori (yaani, watu waishio uwanda wa juu, kama vile Mwa. 15:16)
2. mataifa mawili (Wakanaani, Waperizi, kama vile Mwa. 13:7; 34:30; Amu. 1:4-5)

3. mataifa matatu (Wahivi, Wakanaani, Wahiti, kama vile Kut. 23:28)
4. mataifa sita (Wakanaani, Wahiti, Waamori, Waperizi, Wahivi, Wayebusi, kama vile Kut. 3:8,17; 33:2; 34:11; Kut. 20:17; Yos. 9:1; 12:8)
5. mataifa saba (Wahiti, Wagirgashi, Waamori, Wakanaani, Waperizi, Wahiti, Wayebusi, kama vile Kumb. 7:1; Yos. 3:10; 24:11)
6. mataifa kumi (Mkeni, Mkenizi, Mkadmoni, Wahiti, Waperizi, Mrefai, Waamori, Wakanaani, Mgirgashi, Wayebusi, kama vile Mwa. 15:19-21)

### **MADA MAALUM: Wakazi wa Waisraeli walioishi Palestina Kabla**

#### A. Kuna orodha nyingi ya watu.

##### 1. Mwanzo 15:19-21 (10)

- |              |             |               |             |
|--------------|-------------|---------------|-------------|
| a. Wakeni    | d. Wahiti   | g. Waamori    | j. Wayebusi |
| b. Wakenizi  | e. Waperizi | h. Wakaanani  |             |
| c. Wakadmoni | f. Warefai  | i. Wagirgashi |             |

##### 2. Kutoka 3:17 (6)

- |              |             |
|--------------|-------------|
| a. Wakaanani | d. Waperizi |
| b. Wahiti    | e. Wahivi   |
| c. Waamori   | f. Wayebusi |

##### 3. Kutoka 23:28 (3)

- a. Wahivi
- b. Wahiti
- c. Wahiti

##### 4. Kumbu kumbu la Torati 7:1 (7)

- |               |              |             |
|---------------|--------------|-------------|
| a. Wahiti     | d. Wakaanani | g. Wayebusi |
| b. Wagirgashi | e. Waperizi  |             |
| c. Waamori    | f. Wahivi    |             |

##### 5. Yoshua 24:11 (7)

- |              |               |             |
|--------------|---------------|-------------|
| a. Waamori   | d. Wahiti     | g. Wayebusi |
| b. Waperizi  | e. Wagirgashi |             |
| c. Wakaanani | f. Wahivi     |             |

#### B. Asili ya majina haya haijulikani kwa sababu ya kukosa vielelezo vya kihistoria. Mwanzo 10:15-19 inajumuisha mengi kati yao kama inavyohusiana na Mwana wa Hamu.

#### C. Maelezo mafupi ya watu hawa waliotajwa

1. Wakeni — BDB 884, KB 1098  
 — wasio Waisrael  
 — jina linahusiana na "mfua chuma" au "mhunzi," ambalo lingalirejelea kazi ya kufua bati au muziki (kama vile Mwa. 4:19-22)  
 — lilihusianishwa na eneo la Mlima Sinai Kaskazini mwa Hebron  
 — jina lilihusiana na Yethro, Mkwewe Musa (kama vile Amu. 1:16; 4:11)
2. Wakenizi — BDB 889, KB 1114  
 — nduguze Wayahudi

- ukoo wa Edom (kama vile Mwa. 15:19)
- waliishi huko Negebu
- yumkini wakaishilia Uyahudi (kama vile Hes. 32:12; Yos. 14:6,14)
- 3. Wakadmoni — BDB 870 II, KB 1071 II
  - hawakuwa Waisrael, yumkini kizazi cha Ishmael (kama vile Mwa. 25:15)
  - jina linahusiana na "mtu wa Mashariki"
  - waliishi huko Negebu
  - yumkini wanahusiana na "watu wa Mashariki" (kama vile Ayu. 1:3)
- 4. Wahiti — BDB 366, KB 363
  - hawakuwa Waisrael
  - kizazi cha Sethi
  - walitokea ufalme wa Anatolia (Asia Ndogo, Uturuki)
  - walikuwepo mwanzoni kabisa huko Kaanani (kama vile Mwanzo 23; Yos. 11:3)
- 5. Waperizi — BDB 827, KB 965
  - hawakuwa Waisrael, yumkini Hurrians
  - waliishi kwenye maeneo ya misitu ya Uyahudi( kama vile Mwa. 34:30; Amu. 1:4; 16:10)
- 6. Refaimu — BDB 952, KB 1274
  - hawakuwa Waisrael, yumkini majitu (kama vile Mwa. 14:5; Hes. 33:33; Kumb. 2:10-11,20)
  - waliishi kwenye kingo za Mto Yordani (kama vile Mwa. 15:20; Yos. 12:4; 13:12; Kumb.2:8-11,20; 3:13) au Kingo za Magharibi (kama vile Yos. 15:8; 17:15; 2 Sam. 5:18,22; 23:13;1 Nya. 20:4)
  - kizazi cha wapiganaji
- 7. Waamori — BDB 57, KB 67
  - kundi la watu wa Kisemitic toka Hamu (kama vile Mwa. 10:16)
  - wakawa wenye cheo kikuu kwa kizazi cha Wakaanani (kama vile Mwa. 15:16; Kumb. 1:7; Jos. 10:5; 24:15; 2 Sam. 21:2)
  - jina laweza kumaanisha "watu wa Magharibi"
  - ISBE, juzuu. 1, uk. 119, inasema neno linamaanisha
    - a. kizazi cha Wapalestina kiujumla
    - b. idadi ya watu wa nchi ya milima waliopingwa na watu wa uwanda wa Pwani
    - c. kikundi cha watu maalum wakiwa na Mfalme wao
- 8. Wakaanani — BDB 489, KB 485
  - toka kwa Hamu (kama vile Mwa. 10:15)
  - wakawa wenye cheo kikubwa kwa kabila zote za Wakaanani Magharibi mwa Yordani
  - maana ya Kaanani haijulikani, yumkini "mfanya biashara" au "rangi ya hudhurungi"
  - kama kikundi cha watu walioishi kando ya uwanda wa Pwani (kama vile Hes. 13:29)
- 9. Wagirgashi — BDB 173, KB 202
  - toka kwa Hamu (kama vile Mwa. 10:16) au kiwastani "toka mwana wa [yaani., nchi ya] Wakaanani," ISBE, juzuu. 2, uk. 1232)
- 10. Wayebusi — BDB 101, KB 382
  - toka kwa Hamu (kama vile Mwa. 10:16)
  - toka Mji wa Wayebusi/Salemu/Yerusalem (kama vile Yos. 15:63; Yos. 19:10)
  - Ezek. 16:3,45 inadai kilikuwa kizazi mchanganyiko toka kwa Waamori na Wahiti
- 11. Wahivi — BDB 295, KB 297

- toka kwa Hamu (kama vile Mwa. 10:17)
- ikatafasiriwa na maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX) kama Waamori (kama vile Mwa. 34:2; 36:20-30; Yos. 9:7)
- yumkini toka kwenye neno la Kiebrania "pango," kwa hiyo, waishio mapangoni
- waliishi katika uwanda wa juu wa Lebanoni (kama vile Yos. 11:3; Amu. 3:3). katika 2 Sam. 24:6-7 imewaorodhesha mbele ya Tiro na Sidoni

▣"urithi " Neno ambatani lenye utatu *kata + klēros+ nemōis* ni la kawaida katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani, lakini linatumika hapa tu katika Agano Jipya (maandiko mengine yana maneno *kata + klēros + didōmi*). Hili linamaanisha kuwatangaza wale waliopotea kama njia ya kuigawa Nchi Iliyohaidiwa miongoni mwa makabila (kama vile Yos. 13-19). Hili neno *klērosis* tunalipata neno la Kiingereza "kasisi," lakini mara nyingi Agano Jipya linarejelea umoja wa waamini, si kundi la wasomi!

▣"nne na hamsini" Hii ni namba inayoonekana kufika mahali kwa:

1. miaka 400 ya kifungo ndani ya Misri (kama vile Mwanzo. 15:13)
2. miaka 40 ya jangwa na kipindi cha kutangatanga (kama vile Kutoka 16:35; Hesabu. 14:33-34; 32:13)
3. miaka 7-10 ya utawala wa kivamizi (Kama vile Yoshua 14:7,10)

Toleo la Textus Receptus (KJV) linahamisha hesabu katika Mdo. 13:20 inaonekana ili wajumuisha mahakimu (ukifatilia Josephus, *Antiq.* 8.3.1), lakini huku kuweka maneno hakuko katika lile la zamani na maandiko mazuri zaidi ya Kiyunani (kama vile X, A, B, C), ambayo inashabihiana na tarehe za 1 Wafalme 6:1. Dashi zinazopatikana katika toleo la NASB linaweka mkazo mahali sahahi pa namba.

**13:20** Hii inamaanisha kipindi kutoka Kitabu cha Waamuzi kupitia 1 Samweli 7.

**13:21** Hii inamaanisha 1 Sam. 8-10.

▣"miaka arobaini" Wakati huu haupatikani katika Agano la Kale labda mpaka tatizo la maandiko ya Agano la Kale linalounganishwa na 1 Sam. 13:1 likijumuisha "arobaini" (NIV). Josephus, *Antiq.* 6.14.9 pia inataja kwamba Sauli alitawala miaka "arobaini". Tafsiri la Agano la Kale linaondoa sentensi nzima na kuanza na 1 Sam. 3:2. "arobaini" ilikuwa destruri ya kawaida ya kiuahimili iliyozeleka.

**13:22 "Nimemwona Daudi, mwana wa Yese, mtu anayeupendeza moyo wangu"** Hii sio nukuu ya moja kwa moja kutoka Agano la Kale bali inavyoonekana ni muunganiko wa Zaburi 89:20 na 1 Samweli 13:14. Inahitajika ikumbukwe kwamba mahubiri haya ya Paulo yanafuata utaratibu wa msingi wa masimulizi ya kihistoria ya Mdo. 7. Kwamba Daudi alitwa mtu anayeupendeza moyo wa Mungu wakati alikuwa mwenye dhambi wa kutupwa (kama vile Zaburi. 32,51; 2 Samweli11), ni kutiwa moyo kukubwa kwa ajabu sana.

Muunganiko huu wa nukuu unamaanisha mambo kadhaa ya vitu.

1. Hili lilikuwa ni jambo linalofanyika kawaida na walimu wa kiyahudi, linaloelezea kunukuu Agano la Kale kusiko kwa kawaida.
2. Hii ilikuwa tayari sehemu ya Katekismu ya Kikristo. Paulo mara kwa mara ana nukuu kutoka katika tenzi za ukristo wa kwanza na yawezekana kutoka katika fasihi zingine.
3. Nukuu hii ni ya kipekee na inaonesha kwamba Luka lazima alikuwa amepata muhtasari huu wa kwamza kuwekewa kumbukumbu ya Paulo katika Matendo ya Mitume kutoka kwa Paulo mwenyewe.

NASB, NKJV	"atakayeyatenda mapenzi yangu yote"
NRSV	"atakayeyafanya mapenzi yangu yote"
TEV	"atayefanya yale yote nitakayotaka ayatende"
NJB	"atakayeyafanya mapenzi yangu yote"

Mstari huu ni muungano wa dokezo la Agano la Kale. Sehemu hii ya sentensi haimo katika vifungu vya Agano la Kale. Katika muktadha wa Agano la Kale Sauli alikuwa kaidi na alikataliwa. Lakini maisha ya Daudi pia yalikuwa na hali ya kutotii. Mungu hutenda kazi pamoja na wanadamu wasio kamilifu ili kuukamilisha mpango wake wa ukombozi.

**13:23** Hili linafanana na Matendo ya Mitume 7:52. Hoja zake zinarejelea ahadi zote za Agano la Kale.

1. ukombozi kupitia uzao wa mwanake, Mwa. 3:15
2. mtawala kutoka Yuda, Mwa. 49:10
3. mtawala ajaye kama Musa, Nabii, Kumb. 18:15,18
4. mtawala kutoka uzao wa Daudi, 2 Sam. Zab. 132:11; Isa. 11:1,10; Mt. 1:1
5. mtume ateswaye, Isa. 52:13-53:12
6. mwokozi, Luka 2:11; Mt. 1:21; Yohana 1:29; 4:42; Matendo ya Mitume 5:3

Kwa Luka #4 inajulikana (kama vile Luka 1:32,69; 2:4; 3:31; Matendo ya Mitume 2:29-31; 13:22-23). Masihi angekuwa chipukizi katika shina la Yese (kama vile. Isa. 9:7; 11:1,10; 16:5).

**13:24** Huduma na ujumbe wa Yohana Mbatizaji vinaelezwa katika Marko 1:1-8; Mt. 3:1-11; Luka 3:2-17; Yohana 1:6-8,19-28. Yohana alikamilisha unabii wa Mt. 3:1; 4:5-6. Mahubiri yake ya toba pia yaliweka mpangilio wa mahubiri ya Yesu ya awali (kama vile Mt. 4:17; Marko 1:14-15). Yohana alizungumzia juu ya Yule Ajaye, aliye mkuu kuliko yeye (kama vile Mt. 3:11; Marko 1:7; Luka 3:16; Yohana 1:27,30; Matendo ya Mitume 13:25).

**13:25" Naye Yohana alipokuwa akimaliza mwendo wake"** Mungu alikuwa kazi mahususi kwa ajili ya Yohana kuitenda. Huduma ya Yohana ya hadhara ilimalizika tu ndani ya miezi kumi na minane. Lakini, ni mwaka gani na nusu mwaka gani, alipojazwa na nguvu ya Roho Mtakatifu na kuitengeneza kuiandaa njia kwa ajili ya Masihi. Paulo alilifahamu Agano la Kale tokea ujana wake katika shule ya sinagogi na mafundisho yake kama mwalimu wa sheria za Kiyahudi chini ya Gamalieli humo Yerusalemu. Yeye aliisikia injili

1. kutoka kwa Stefano
2. kutoka kwa waamini aliokuwa akiwatesa
3. kwa maono maalum kutoka kwa Yesu
4. kutoka kwa mwekea mikono wa Kiyahudi aliyetoka Dameski
5. kupitia kwa Yesu alipokuwa Arabia
6. wakati aliposafiri pamoja na Mitume wengine

Alijaribu kumnukuu Yesu popote alipokuwa akifundisha. Hapa anayanukuu mamelezo ya Injili ya maisha Yake

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 13:26-41**

<sup>26</sup> Ndugu zangu, wana wa ukoo wa Ibrahimu, na hao miongoni mwenu wanaomcha Mungu, kwetu sisi neno la wokovu huu limepelekwa. <sup>27</sup> Kwa maana wakaa Yerusalemu, na wakuu wao, kwa kuwa hawakumjua yeye, wala maneno ya manabii yanayosomwa kila sabato, wameyatimiza kwa kumhukumu. <sup>28</sup> Na ijapokuwa hawakuona sababu ya kumfisha wakamwomba Pilato auawe. <sup>29</sup> Hata walipokwisha kumaliza yote aliyoandikiwa, wakamtelemsha katika ule mti, wakamweka kaburini. <sup>30</sup> Lakini Mungu akamfufua katika wafu; <sup>31</sup> akaonekana siku nyingi na wale waliopanda naye kutoka Galilaya hata Yerusalemu, ambao sasa ndio walio mashahidi wake mbele ya watu. <sup>32</sup> Na sisi tunawahubiri habari njema ya ahadi ile waliyopewa mababa, <sup>33</sup> ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo, kwa kumfufua Yesu; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili, Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa. <sup>34</sup> Tena ya kuwa alimfufua katika wafu, asipate kurudia uharibifu, amenena hivi, Nitawapa ninyi mambo matakatifu ya Daudi yaliyo amini. <sup>35</sup> Kwa hiyo anena na pengine, Hutamwachia Mtakatifu wako kuona uharibifu, <sup>36</sup> Kwa maana Daudi, akiisha kulitumikia shauri la Mungu katika kizazi chake, alilala, akawekwa pamoja na baba zake, akaona uharibifu. <sup>37</sup> Bali huyu aliyefufuliwa na Mungu hakuona uharibifu. <sup>38</sup> Basi, na ijulikane kwenu, ndugu zangu, ya kuwa kwa huyo mnahubiriwa msamaha wa dhambi; <sup>39</sup> na kwa yeye kila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote asiyoweza kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa. <sup>40</sup>

**Angalieni, basi, isiwajilie habari ile iliyonenwa katika manabii.** <sup>41</sup> Tazameni, enyi mnaodharau, kastaajabuni, mkatoweke; kwa kuwa natenda kazi mimi siku zenu, kazi ambayo msingeadiki kabisa, ijapo mtu akiwasimulia sana.

**13:26 "wana wa ukoo wa Ibrahimu, na hao miongoni mwenu wanaomcha Mungu"** Hii inamaanisha wasikiaji wote wa Kiyahudi (au waongofu) na mataifa (wacha -Mungu) waliojiungamanisha na kuabudu mungu mmoja dini ya Kiyahudi na kimaadili.

▣ **"wokovu"** Hii inamaanisha ahadi ya Mungu ya kuwakomboa wanadamu walioanguka kupitia Masihi (kama vile Mwanzo. 3:15). Inajumuisha mataifa (kama vile Mwanzo. 12:5; Kutoka 19:5-6; na Matendo ya Mitume 28:28 na 13:46).

**13:27** Kwa maneno ya wazi mafupi kinaweka muhtasari wa upofu wa Wayahudi katika Yerusalemu kuhusu maandiko hata kama wanayasoma kwa mfululizo. Kwa kukosa ishara za kinabii (kama vile Zaburi 22; Isaya 53; Zekaria, Malaki) na manabii (Isaya, Yona) walikuwa ishara za kinabii! Alikuwa kwenya mji wake mwenyewe lakini watu wake hawakumpokea (kama vile Yohana 1:11-12).

**13:28** Mdo inaweka kumbukumbu tena na tena uwajibikaji wa kiroho wa Wayahudi ndani ya Yerusalemu (kama vile Mdo. 2:23,36;3:13-15; 4:10; 5:30; 7:52; 10:39; 13:27-28).

**13:29 "wao.....wao"** Haya lazima yalikuwa makundi tofauti. La kwanza lilikuwa lile lililotafuta mauti Yake (yaani uongozi wa Kiyahudi, umati mbele ya Pilato). La pili lilijumuisha wale waliotaka maziko sahihi. Hii inaweza kuwa ilijumuisha watu wa Kiyahudi walioona hali ya kutotendewa haki (sawa na Matendo ya Mitume 8:2, iliyojumuisha Stephano) au wanafunzi wa sirisiri kama Yusufu wa Arimathaya na Nikodemo (kama vile Yohana 19:38-42).

▣ **"yale yote yaliyoandikwa juu yake Yeye"** Maisha ya Yesu yalikuwa ni moja ya unabii uliotimizwa. Ushahidi wenye nguvu mmojawapo kwa ajili ya uvuvio wa Biblia na U-Masihi wa Yesu wa Nazareti (kama vile Luka 22:22; Mdo.2:23; 3:18; 4:28; 10:43; 13:29; 24:14; 26:22).

Ni hakika kwamba maelezo mengi ya maisha ya Yesu, ambayo sisi katika kanisa tunayaita unabii yako kwenye namna ya uanishi. Matukio mengi yalitokea katika maisha ya Israeli ambayo baadaye yanaonekana pia kutokea kwa Yesu (Mfano mmoja, Hosea 11:1). Mara kwa mara vifungu vya habari vyenye utata na vyenye mwanga kidogo, ambavyo visingetakiwa kueleweka kimuktadha kama vya kinabii vinaonekana kuruka kwenye maisha kama moja ya maoni ya uzoefu wa Yesu wa duniani (mfano Zaburi 22; Isaya 53). Inagharimu uvuvio na namna ya mtiririko wa historia ya ukombozi ili kiukamilifu kukubali kutabiriwa kabla kwa Yesu kunakofanywa na Agano la Kale. Pia ningeweza kuongezea hiyo kwamba japokuwa waandishi waliovuviwa wa Agano Jipya, hata sitiari, kwamba hata waalimu wa kisasa na wahubiri hawatakiwi kutumia mbinu hii ya ufasiri! Angalia Semina ya Ufasiri wa Kibiblia wa Bob katika mtandao wa [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org)

▣ **"msalaba"** Angalia muhtasari katika Mdo. 5:30 and 10:29.

**13:30,33,34,37 "Lakini Mungu alimfufua katika wafu"** Agano Jipya linathibitisha kwamba nafsi zote tatu za Utatu zilikuwa zikifanya kazi katika Ufufuo wa Yesu:

1. Roho (kama vile Rum. 8:11)
2. Mwana (kama vile Yohana 2:19-22; 10:17-18)
3. Baba (kama vile Mdo. 2:24,32; 3:15,26; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 6:4,9; 10:9; 1 Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14; Gal. 1:1; Efe. 1:20; Kol. 2:12; 1 The. 1:10).

Huu ulikuwa ni uthibitisho wa Baba wa kweli ya maisha ya Yesu na mafundisho. Hiki ni kipengele cha *Kerygma* (yaani maudhui ya mahubiri katika Matendo ya Mitume). Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:14.

**13:31 "kwa siku nyingi"** Mdo. 1:3 inasema "siku arobaini" Hata hivyo siku arobaini ni kawaida katika namba za mzunguko wa Agano la Kale. Angalia Mada Maalum katika Mdo. 1:3.

▣ **"Alitokea"** Angalia Mada Maalum: Kutokea kwa Yesu baada ya kufufuka katika Mdo. 1:3

**13:32 "Ahadi iliyofanywa kwa Ma-baba"** Hii inamaanisha ahadi ya kuanzia ya YHWH kwa Ibrahimu kama mbegu (kama vile Mwanzo 12:1-3; Warumi 4). Ahadi hii hii ya uwepo wa Mungu na Baraka ilirudiwa kwa wazazi wetu wa kwanza na watoto wao (kama vile Isaya 44:3; 54:13; Yoeli 2:32). Agano la Kale linaweka shabaha katika ardhi wakati Agano Jipya linaweka shabaha katika "mbegu" Paulo anaweka maelezo kwa ahadi hii katika Warumi 1:2-3.

**13:33** Hii ni ahadi kutoka Zaburi 2:7, ambayo ni zaburi ya masihi wa kifalme kuhusu mgogoro na ushindi ahadi iliyohaidiwa ya Masihi. Yesu alikuwa ameuwawa na nguvu ya uovu (ya kibinadamu na kipepo), lakini Mungu alimfufua Yeye kwa ushindi (kama vile Warumi 1:4).

Mstari huu katika Warumi 1:4 ulitumika na wavumishaji (waasilishaji) kuelezea kuwa Yesu alifanyika Masihi wakati wa Ufufuo. Hakika kuna msisitizo wa Agano Jipya kwa Yesu kuthibitiswa na kutukuzwa kwasababu ya utii wake lakini hii lazima isichukuliwe yenyewe kutoka katika utukufu wake uliokuwepo mwanzo kabla ya yeye kuja na uungu (kama vile Yohana 1:1- 5,9-18; Flp. 2:6-11; Kol. 1:13-18; Ebr. 1:2-3).

Kitenzi hiki cha "alimfufua" (*anistēmi*), kinatumika katika Mdo. 3:26 ya Mungu kumuinua juu "Mtumishi wake"; katika Mdo.3:22 Mungu kumuinua juu nabii (kama vile Mdo. 7:37; Kumbu. 18:19). Hii inaonekana kuwa tofauti kabisa kimatumizi kutoka kwa "kumfufua" kutoka kwa wafu (kama vile Mdo. 13:30,34,37). Yesu alikuwa "akiinuliwa juu" kabla hajafa!

**13:34 "asipate kurudia uharibifu"** Kauli hii inamaanisha kifo cha Yesu na ufufuo. Alikuwa wa kwanza kufufuliwa (malimbuko ya kwanza ya waliokufa, kama vile 1 Kor. 15:20) kama kuhuishwa. Watu wengi walirejeshwa katika maisha ya mwili katika Biblia, lakini wote walitakiwa kufa tena. Henoko na Eliya walipandishwa mbinguni bila kufa, lakini hawakuishwa.

▣ **"Nitawapeni Baraka takatifu na ya hakika ya Daudi "** Hii ni nukuu kutoka Isa. 55:3 kutoka katika LXX. Nukuu inajumuisha wingi "baraka za hakika," lakini hazitoi kwa ufasaha ni nini kinamaanishwa. Ni kitu kinachopitishwa kutoka kwa Mungu kwenda kwa Daudi (wingi "wewe" katika nukuu). Mukstadha wa Agano la Kale unaonesha umuhimu wa "wewe" (kama vile Isa. 55:4-5 LXX, "Angalieni, nimemweka kuwa shahidi kwa kabila za watu; kuwa kiongozi na jemadari kwa kabila za watu. Tazama, utaita taifa usilolijua, na taifa lisilokujua wewe litakukimbilia, kwa sababu ya Bwana, Mungu wako, na kwa ajili yake Mtakatifu wa Israeli; maana amekutukuza. "Tafsiri ya Agano la Kale Zondervan, 1976, ukurasa wa 890). Baraka na ahadi kwa Daudi (yaani Wayahudi) sasa ni Baraka na ahadi kwa mataifa (yaani wanadamu wote).

**13:35-37** Hii ni hoja iliyotumika mwanzoni kabisa katika mahubiri ya Pentekoste ya Petro (kama vile Mdo. 2:24-32), pia ikichukuliwa kutoka katika Zaburi 16. Haya mahubiri ya mwanzo ya Matendo ya Mitume yanaaksi Katekisimu ya kwanza ya Mkristo. Maandiko kadhaa ya Agano la Kale ya Kimasihi tungwa kwa pamoja katika namna yake. Hivyo mara kwa mara viwakilishi na maelezo havionekani kuwa na mfanano wa kisasa kwa kusudi kuu la Agano Jipya, ambayo ilikuwa ni kuthibitisha kufufuka kimwili kwa Yesu na kupotea kwa kuzeeka kwa Daudi.

**13:38** Paulo anatumia hoja zilizoongezewa za Agano la Kale (Mdo. 2) na Stephano (Mdo. 7) kufikia wasikilizaji wa masinagogi haya. Paulo anaahidi msamaha kamili na uliokamilika ambao dini ya kiyahudi hauutoi (kama vile Mdo. 13:39), kwa wote wanaomwamini Yesu kama Kristo (yaani "Huyu Mmmoja," Mdo. 13:38,39).

**13:39 "na kupitia yeye kila mmoja"** Tazama kipengele cha kiujumla. Mungu anawapenda watu wote na wanadamu wote wana fursa ya kuitikia kwa Yeye kwa imani (kama vile Mdo. 10:43; Isa. 42:1,4,6,10-12; 55; Ezeieli 18:23,32; Yoeli 2:28,32; Yohana 3:16; 4:42; Rum. 3:22,29,30; 10:9-13; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Petro 3:9; 1 Yohana 2:1; 4:14).

▣ **"Yeye aaminiye"** Angalia Mada Maalum katika Mdo. 3:16 and 6:5.

**NASB, NKJV** "amewekwa huru na mambo yote" (Mdo. 13:39)

**NRSV** "anawekwa huru mbali na dhambi hizo" (Mdo. 13:39)

**TEV** "anawekwa huru mbali na dhambi zote" (Mdo. 13:39)

Hii kidhahiri ni "hesabiwa haki" (kauli tendwa elekezi ya wakati uliopo). Hili ni neno la kisheria ambalo linafunua na kuelezea msimamo wetu mbele za Mungu kupitia haki ya Yesu Kristo (kama vile 2 Kor. 5:21). Kwa kiebrania kiasili linamaanisha "funjo la mto" (angalia Mada Maalum katika Mdo 3:14). Linaaksi utungwaji wa neno la Agano la Kale lililotumika kisitari kwa ajili ya Mungu kama mfano au mtawala ambaye hukumu yake inafanyika.

▣"ambayo msingeweza kuwekwa huru kitipia Sheria ya Musa" Hii ilikuwa suala linalomaanisha kwa ukubwa sana na Paulo kithiolojia (kama vile Warumi 3:21-30). Sheria ya Musa ilikuwa kama mwalimu wa kutuleta katika uelewa wa dhambi binafsi na kutusababisha tumtamani Kristo (kama vile Gal. 3:23-29). Sheria ya Agano la Kale sio njia ya wokovu kwa sababu wote tulitenda dhambi (kama vile Rum. 3:9-18,23; Gal. 3:22). Ilikuwa imefanyika adhabu ya mauti, laana (kama vile Gal. 3:13; Kol. 2:14).

### MADA MAALUMU: MTAZAMO WA PAULO KUIHUSU SHERIA YA MUSA

Ni nzuri na inatoka kwa Mungu (kama vile Rum. 7:12,16).

- A. Si njia ya kuelekea haki na ukubalifu wa Mungu (inaweza hata kuwa laana, kama vile Gal. 3). Tazama Mada Maalum: Sheria ya Musa na Mkristo.
- B. Bado ni mapenzi ya Mungu kwa waaminio kwa sababu ni ufunuo wa Mungu Mwenyewe (mara nyingi Paulo amelinukuu Agano la Kale kuwasadikisha na /au kuwatia moyo waaminio).
- C. Waamini wanafahamishwa na Agano la Kale (kama vile Rum. 4:23-24; 15:4; 1 Kor. 10:6,11), lakini hawaokolewi na Agano la Kale (kama vile Matendo 15; Warumi 4; Wagalatia 3; Waebrania). Ina fanya kazi ndani ya utakaso lakini si uthibitisho.
- D. Inafanya kazi ndani ya agano jipya ili:
  - 1. kuonyesha dhambi (kama vile Gal. 3:15-29)
  - 2. kuwaongoza wanadamu ndani ya jamii waliokombolewa
  - 3. kumfahamisha Mkristo maamuzi ya kimaadili

Ni mpangilio maalumu unaomulika kithiolojia uliohusiana na Sheria, kutoka katika hali ya kulaaniwa (kama vile Gal. 3:10-13) na badala yake kuwepo baraka za kudumu, jambo ambalo linasababisha tatizo katika kujaribu kuuelewa mtazamo wa Paulo kuihusu Sheria ya Musa. Mwanadamu aliye ndani ya Kristo, James Stewart analionyesha fumbo la fikra na maadiko ya Paulo:

"Kwa kawaida ungetarajia kuwepo kwa mwanadamu anayejiendesha mwenyewe ili kuunda mfumo wa fikra na mafundisho yaliyoimarishwa na kama kitu kisichobadilishwa kama alivyotumia maneno yenye manufaa. Ungetarajia yeye kuulenga usahihi katika kutumia maneno yalioziongoza fikra zake. Ungedai kwamba neno, linapotumiwa na mwandishi wetu katika maana mahususi, linapaswa kuibeba maana hiyo kotekote. Lakini kwa kuangalia muundo huu yakupasa kutomtia moyo Paulo. Matumizi mengi ya maneno yake ni marahisi, si magumu. . . anaandika 'Basi torati ni njema', 'Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani' (Rum. 7:12,22) lakini ni dhahiri kwamba kipengele kingine cha *nomos* ndicho kinachomfanya kuzungumza hali hii pengine, 'Kristo alitukomboza katika laana ya torati' (kama vile Gal. 3:13)" (uk. 26).

**13:40-41** Paulo anawasihi wasikilizaji wake (kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo) kuitikia kwa kumwamini Yesu kama Masihi aliyehaidiwa kama njia pekee ya kupokea msamaha (kama vile Yohana 14:6; Mdo 4:12; 1 Tim. 2:5). Ananukuu Habakuki 1:5 kutoka katika Tafsiri ya Agano la Kale. Katika maeneo mengine katika maandiko ya Paul, ananukuu Habakuki 2:4 kama mwitikio sahihi (kama vile Rum. 1:17; Gal. 3:11). Paulo anahubiri kwa ajili ya maamuzi. Waidhinishaji wa kiakili hawatoshi; Kusalimu amri kibinafsi kulikokamilika kwa Yesu kama tumaini pekee kunatakiwa. Hii imani ya kuanzia na mwitikio wa toba lazimaa ifanani na kuishi kwa kila siku kama Kristo.

Mstari wa 41 inaelezea mbinu mpya za wokovu wa agano Jipya katika Kristo.



**ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 13: 42-43**

<sup>42</sup> Na walipokuwa wakitoka, wakawasihi waambiwe maneno haya sabato ya pili. <sup>43</sup> Sinagogi ilipofumukana, Wayahudi na waongofu watauwa wengi wakashikamana na Paulo na Barnaba; ambao, wakisema nao, wakawatia moyo kudumu katika neema ya Mungu.

**13:42** Hii inaonesha nguvu ya Roho (1) ukitumia mahubiri ya Paulo na (2) njaa ya msamaha na urejesho pamoja na Mungu ndani ya mioyo ya binadamu.

**13:43**

<b>NASB</b>	“waongofu wacha Mungu”
<b>NKJV</b>	“waongofu watauwa”
<b>NRSV</b>	“waongofu watauwa wa dini ya Kiyahudi”
<b>TEV</b>	“mataifa waliokuwa wameongoka kwenye dini ya kiyahudi”
<b>NJB</b>	“waongofu watauwa”

Tungo ipo dhahiri "waongofu waabuduo" Hili ni kundi tofauti "wale wamwabuduo Mungu" wa Mdo. 13:16,26 (kama vile Mdo. 10:2,22,35). Mstari wa 43 inamaanisha kwa wale Mataifa ambao kirasmi walifanyika Wayahudi. Hii ilihitaji

1. ubatizo binafsi mbele ya mashahidi
2. tohara kwa wanaume
3. kutoa sadaka hekaluni katika Yerusalemu inapowezekana

Kuna rejea chache kwa wayahudi waongofu katika Agano Jipya (kama vile Mt. 23;15; Mdo. 2:11; 6:5; 13:43).

▣"uakiwasihi wao kuendelea katika neema ya Mungu" Kutoka katika muktadha ni vigumu kutoa maana ya tungo hii.

1. baadhi ya wasikiaji hawa ukute walikuwa tayari wamekwisha itikia injili ndani ya mioyo yao
2. Wale ambao walikuwa waaminifu kwa kile walichoelewa juu ya neema ya Mungu katika Agano la Kale wanahimizwa kuendelea kumtafuta Mungu na kumsikiliza Paulo tena (kama vile Mdo. 13:44)

**ANDIKO LA NASB (LILLOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 13:44-47**

<sup>44</sup> Hata sabato ya pili, watu wengi, karibu mji wote, wakakusanyika walisikie neno la Mungu. <sup>45</sup> Bali Wayahudi, walipowaona makutano, wakajaa wivu, wakayakanusha maneno yaliyonenwa na Paulo, wakibisha na kutukana. <sup>46</sup> Paulo na Barnaba wakanena kwa ushujaa wakasema, Ilikuwa lazima neno la Mungu linenwe kwenu kwanza; lakini kwa kuwa mnalisukumia mbali, na kujiona nafsi zenu kuwa hamkustahili uzima wa milele, angalieni, twawageukia Mataifa. <sup>47</sup> Kwa sababu ndivyo tulivyoamriwa na Bwana, Nimekuweka uwe nuru ya Mataifa, Upate kuwa wokovu hata mwisho wa dunia.

**13:44** Ujumbe wa Paulo ulikuwa na matokeo ya wazi. Huku pia ni kutia chumvi. Si kwamba kila mmoja katika mji alihudhuria.

**NASB, NRSV**

**TEV** “neni la Mungu”

**NKJV, NJB,**

**REB** “neni la Mungu”

Kuna maandiko ya Kiyunani juu ya suala hili.

1. Bwana ni katika MSS P<sup>74</sup>, κ, A, B<sup>2</sup>
2. Mungu ni katika MSS B, C, E

Toleo la UBS<sup>4</sup> linaweka "Bwana" katika maandiko, akini linatoa alama ya "C" (ngumu kuamua). Kama bila utofautiutofauti, hii haibadiliki katika maana ya andiko. Injili ni ufunuo wa kiungu kuhusu Yesu, Masihi/Kristo.

**13:45 "Wayahudi, walipowaona makutano . . .wivu"** Kwa vyo vyote vile kulikuwa na kujijokeza kwa wingi au idadi kubwa ya Watu wa Mataifa katika umati uliosababisha vivu hii haijulikani katika muktadha huu. Wivu unaonekana kuwa kwa viongozi wa Kiyahudi maeneo yote katika Yerusalemu na katika mataifa yote walikokuwa Wayahudi. (kama vile Mt. 27:18; Marko 15:10; Matendo ya Mitume 17:5). Baadaye katika Warumi Paulo analikuza tatizo la kithiolojia la wale Wayahudi wasioamini (kama vile Warumi 9-11). Anaeleza kuwa Mungu ameipofusha Israeli kwa muda ili Mataifa yaokolewe. Hata hivyo, Mungu atautumia wokovu wa Mataifa kama njia (yaani, wenye wivu) ili kuisababisha Israeli kumwitikia Kristo, iliwaamini wote wawe wamoja kupitia ijili (kama vile Efe. 2:11-3:13). Tatizo ni kwamba hili lililtokea lini? Swali kama hili lingeweza kuulizwa kupitia Zek. 12:10. Je! Unabii huu unahusiana na kanisa la awali, ambalo liliundwa na Wayahudi walioamini, au kipindi kijacho? Wivu ulimaanisha kasudi la ukombozi (kama vile Rum. 10:19; 11:11,14), lakini katika andiko hili wivu ulisababisha kutokuamini!

▣"**wakajaa wivu**" Angalia maelezo katika Matendo ya Mitume 3:10.

▣"**wakayakanusha**" Kadri Wayahudi hawa walivyozitetea tamaduni zao na kuyashambulia mahubiri ya Paulo, wao kwa wao walijikuta na hatia ya ukanushi. Hapa Hakuna swala la msingi. Kwa vyo vyote Dini ya Kiyahudi au Ukristo ni mawazo sahihi ya mapenzi ya Mungu. Ni ya kipekee!

**13:46 "wakibisha na kutukana"** Katika Matendo ya Mitume hii ni moja ya alama za kujazwa Roho Mtakatifu.

▣"**Ilikuwa muhimu kwamba Neno la Mungu lihubiriwe kwenu kwanza**" Huu ulikuwa utaratibu wa mahubiri ya wamishionari wa kwanza. Wayahudi walikuwa na kipaumbele (kama vile Warumi 9-11), lakini Mungu alikuwa amekwisha jumuisha mataifa. Wali waliokuwa katika masinagogi walikuwa wanajua katika Agano la Kale unabii zilizomo. Matendo ya Mitume wana mfululizo wa maandiko juu ya dhana na utaratibu (kama vile Mdo. 3:26; 9:20; 13:5,14; 16:13; 17:2,10,17).

▣"**ninyi mnalikanusha**" Hiki ni kitenzi chenye nguvu (kauli ya kati elekezi ya wakati uliopo) inatumika katika Tafsihi ya Agano la Kale. Ni maana ya msingi "kuweka mbali." ilitumika katika mahubiri ya Stephano ya Israeli (kama vile Mdo. 7:39). Pia inatuma na Paulo katika Warumi 11:1-2 to inaelezewa kwamba Mungu hajakataa watu wake, lakini wamekataa Mtoto wake, namna yake pekee ya wokovu, ufunuo wake kamili.

▣"**kujiona nafsi zenu kuwa hamkustahili uzima wa milele,**" Ni ngumu kushikilia dhana ya kuamriwa kwanza ambayo inasisitiza mara kwa mara katika Matendo ya Mitume, na dhana ya mwitikio binafsi wa kimamlaka. Hakuna anayeweza kuja katika imani bila kuvutwa karibu na Roho (kama vile Yohana 6:44,65), Tunapimwa na kama tunaitikia au la. Kwa kutaa kwao injili iliyokuwa ikinenwa na Paulo, walijifunua wenyewe namna walivyo (kama vile Yohana 3:17- 21). Lawama kwa kukosa mwitikio hauwezi kuwekwa kwa Mungu. Yeye ametoa njia, Mwanaye, lakini yeye ndiye njia pekee! Ni siri ya "Kutokuamini"!

▣"**twawageukia Mataifa**" Hii ukajakuwa mfano wa kawaida wa tamko la injili (kama vile Mdo. 18:6; 22:21; 26:20; 28:28; Rom. 1:16).

**13:47** Hii ni nukuu toka Isa. 49:6 (kama vile Mdo.42:6) toka tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani. Simioni alitumia nukuu hii wakati wa kumbariki Yesu katika Luka 2:32 ili kuithibitisha kazi yake ya ki-Masihi ya ukombozi wa wote (angalia Mada Maalum katika Mdo. 1:8). Yawezekana kuwa "nuru" katika muktadha inarejelea kwenye mahubiri ya Paulo na Barnaba ya injili kwa hawa wa Mataifa (kama vile "matumizi ya Agano la Kale katika agano jipya," by Darrell Boch, uk. 97 in *Foundations for Biblical Interpretation*, Broadman& Holman Publishers, 1994). Sasa Paulo analitumia kuonyesha tangazo la injili kwa wote! Kifungu cha mwisho, "hadi mwisho wa nchi," chaweza kuwa ni kidokezo cha 1:8. Kinasisitiza injili ya wote.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 13:48-52**

<sup>48</sup> Mataifa waliposikia hayo wakafurahi, wakalitukuza neno la Bwana, nao waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini. <sup>49</sup> Neno la Bwana likaenea katika nchi ile yote. <sup>50</sup> Lakini Wayahudi wakawafitinisha wanawake watauwa wenye cheo na wakuu wa mji, wakawataharakisha watu wawaudhi Paulo na Barnaba; wakawatoa katika mipaka yao. <sup>51</sup> Nao wakawakung'utia mavumbi ya miguu yao, wakaenda Ikonio. <sup>52</sup> Na wanafunzi walijaa furaha na Roho Mtakatifu.

**13:48 "Mataifa waliposikia hayo wakafurahi, wakalitukuza neno la Bwana"** Wengi wa hawa walikuwa katika sinagogi kwa muda mrefu na walikuwa hawajawahi kusikia wakijumuishwa, katika ujumbe wa upendo wa Mungu na kukubaliwa kwa wanadamu wote kwa imani katika Masihi. Waliposikia waliamini (kama vile Mdo. 28:28) na kuwaambia wengine (kama vile Mdo. 13:49).

▣ **"nao waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini"** Hii ni kauli iliyowazi ya kuamriwa kabla ( iliyokuwa ya kawaida kwa walimu wa kiyahudi na katika fasihi za kati ya maagano ya kiyahudi), lakini iko katika uhusiano tata uleule kama vifungu vyote vya Agano Jipya ambavyo vinahusiana na mkanganyiko wa uchaguzi wa Mungu na utashi huru wa mwanadamu (kama vile Flp. 2:12, 13). Ni kauli tendwa ya wakati timilifu wa wazi mwenye mafumbo ambao unakuja kutoka katika neno la kijeshi (*tassō*) ambalo linamaanisha ya "kuandikisha" au "kuteuwa." Dhana hii ya kuandikisha inamaanisha vitabu viwili vya kisitiari ambavyo Mungu anatumza (kama vile Danieli 7:10; Ufunuo 20:12). Kitabu cha kwanza ni kitabu cha matendo ya wanadamu (kama vile Zaburi 56:8; 139:16; Isa. 65:6; na Mal. 3:16). Kingine ni kitabu cha Uzima (kama vile Kutoka 32:32; Zaburi 69:28; Isa. 4:3; Dan. 12:1; Luka 10:20; Flp. 4:3; Ebr. 12:23; Ufunuo 3:5; 13:8; 17:8; 20:12-15; 21:27). Angalia Mada Maalum: Uchaguzi/Kuamriwa Kabla na hitaji la ulali wa kithiolojia katika Mdo. 2: 47

**13:50 "Lakini Wayahudi wakawafitinisha wanawake watauwa wenye cheo"** Andiko hili linatoa kihistoria na mazingira ya kifestari ya kuinuliwa kwa sehemu ya wanawake katika Asia ndogo katika karne ya kwanza (kama vile Mdo. 16:14; 17:4). Katika muktadha huu inamaanisha waongofu kwa dini ya Kiyahudi ambao pia walikuwa viongozi katika jamii. A. T. Robertson, *Word Pictures in the New Testament*, vol. 3, ukurasa wa 201, anatengeneza suala kwamba Mataifa wanawake walikuwa wanavutiwa sana na dini ya uyahudi (kama vile *Strabo* 7:2 and *Juvenal* 6:542) kwasababu ya maadili.

▣ **"wakawataharakisha watu wawaudhi Paulo na"** Paulo anamaanisha hiki katika 2 Tim. 3:11.

**13:51 "wakawakung'utia mavumbi ya miguu yao "** Hii ni ishara ya kukataliwa ya Kiyahudi (kama vile Mt. 10:14; Marko 6:11; Luka 9:5; 10:11). Haijulikani bado kama hii inamaanisha (1) Mavumbi kwenye miguu yao na viatu walivyokuwa wakitembelea (2) mavumbi yaliyokuwa katika nguo zao ambayo ndiyo yaliyokung'utwa.

▣ **"Ikonio"** Huu ulikuwa mji mkuu katika mji wa Likanoi, uliokuwa katika jimbo la Kirumi la Galatia. Ilikuwa ni maili themanini mashariki, kusini-mashariki mwa Antiokia ya Pisidia na ikiungwa moja kwa moja kaskazini mwa Listra.

**13:52 "walijaa furaha "** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati usiotimilifu ambayo inaweza kumaanisha mwanzo wa kitendo au kurudia kwa kitendo kwa wakati uliopita. Toleo la NASB la mwaka 1995 lililoboreshwa linalichukulia katika namna ya pili. Ni Roho Mtakatifu tu anayeweza kutoa furaha katikati ya mateso (kama vile Rum. 5:3; Yakobo 1:2; 1 Petro 4:12). Tungo "wanafunzi" ni tata. Je linamaanisha waamini wapya, timu ya umishenari au vyote?

## MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Paulo alihubiri kwenye Sinagogi kwanza?
2. Kwanini Yohana Marko aliiacha timu ya umisheni? (kama vile Mdo.13:13)
3. Ni kwa namna gani Mdo.13:39 inahusiana na Wagalatia 3?

Elezea Mdo. 13:48b kwa kuihusianisha na kuamriwa kabla na utashi huru wa mwanadamu.

## MATENDO YA MITUME 14

MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA				
UBS <sup>4</sup>	NKJV	NRSV	TEV	NJB
Paulo na Barnaba Huko Ikonio 14:1-7	Ikonio 14:1-7	Huduma huko Mji wa Ikonio na kurudi 14:1-7	Ndani ya Ikonio 14:1-4	Uinjilisti wa Ikonio 14:1 14:2 14:3 14:4-7
Paulo na Barnaba Huko Listra 14:8-18	kuabudu sanamu huko Listra 14:8-18	14:8-18	14:5-7 Listra na Derbe 14:8-13 14:14-18	kuponywa kwa kiwete 14:8-10 14:11-18
14:19-20 Kurudi Antiokia Huko Ashuru 14:21-28	Kupigwa mawe Kukimbia mpaka Derbe 14:19-20 kuimarisha waongofu 14:21-28	14:19-20 14:21-23 14:24-28	14:19-20 kurudi Antiokia huko Ashuru 14:21-23 14:24-26 14:27-28	Mwisho wa Safari 14:19-20 14:21-23 14:24-26 14:27-28

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("[A Guide to Good Bible Reading](#)")

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

#### **Misheni ya Paulo inahusianishwa vipi kwa Wagalatia?**

- A. Vipengele hivi viwili vya usuli wa vitu sharti ushughulikiwe kwa pamoja kwasababu ya nadharia mbili zinazopingana za utambulisho wa wapokeaji unaathiri tarehe za barua. Nadharia zote mbili zina uzito wa kimantiki na ukomo wa ushahidi wa kibiblia.
- B. Nadharia mbili
  1. Nadharia ya kijadi ambayo haikuwa inajulikana mpaka karne ya kumi na nane.
    - a. Inaitwa "Nadharia ya Galatia ya Kaskazini."

- b. Inadhania kwamba "Galatia" inamaanisha kabila la Wagalatia wa uwanda wa kaskazini kati mwa Uturuki (kama vile 1 Pet. 1:1). Makabila haya ya Wagalatia yalikuwa Celts (Wayunani wa Kelti au Wa-Latino wa Gall) ambao walivamia eneo hili katika karne ya tatu K.K. Walikuwa wakiitwa "Gallograecians" ili kuwatofautisha na ndugu zao wa Ulaya Magharibi. Walishindwa mwaka 230 k.k. na Attalus I, Mfalme wa Pergamo. Ushawishi wao wa Kijiografia ulikuwa na kikomo kwa Kaskazini kati mwa Asia ndogo au Uturuki ya sasa.
  - c. Ikiwa kikundi hiki cha kikabila kinadhaniwa, hivyo tarehe inaweza kuwa katikati ya miaka ya 50 wakati wa safari ya Paulo ya kimishonari ya pili au ya tatu. Watenda kazi wa Paulo walikuwa Sila na Timotheo.
  - d. Baadhi wameunganisha maradhi ya Paulo ya Gal. 4:13 na maralia. Wanaeleza kwamba Paulo alielekea Kaskazini katika milima ili kutoka katika maeneo nyevu yenye maambukizi ya maralia ambayo yalikuwa nyanda za chini za ardhi maeneo ya pwani.
2. Nadharia ya Pili inashikiliwa na Sir Wm. M. Ramsay, St. Paul the Traveler na Raia wa Kirumi, New York: G. P. Putnam's Sons, 1896.
    - a. Ambapo nadharia ya kijadi inatoa maana ya "Galatia" kama kikundi cha kikabila, nadharia hii inataja kuwa utawala. Inavyoonekana ni kwamba Paulo mara kwa mara alitumia majina ya Kirumi ya kikanda (kama vile 1 Kor. 16:19; 2 Kor. 1:1; 8:1, nakadhalika) Jimbo la Kirumi "Galatia" lilijumuisha eneo kubwa zaidi ya eneo la kundi la kikabila la "Galatia." Haya makabila ya Celts yalisaidia Rumi mapema sana na walikirimiwa zaidi ya uwezo wao wenyewe wa mahali wa kujiendesha na kupanua mamlaka ya kimipaka. Ikiwa eneo hili lilijulikana kama "Galatia," hivyo inawezekana kwamba Safari ya kwaza ya kimishonari kwa majiji haya ya kusini mwa Antiokia katika Pisidia, Listra, Derbe and Ikonio, yanawekwa katika kumbukumbu katika Mdo. 13-14, ni mahali pa makanisa haya.
    - b. Ikiwa mtu anadhania "Nadharia ya Kikusini," tarehe ingekuwa mapema sana—ikikaribia, lakini kabla, "Baraza la Yerusalemu" la Matendo ya Mitume 15, ambayo inaelezea somo hilo kama kitabu cha Wagalatia. Baraza lilitokea katika miaka ya 48-49 b.k na barua yawezekana iliandikwa wakati wa kipindi hiki. Ikiwa hii ni kweli, Wagalatia ni barua ya kwanza ya Paulo katika Agano Jipya letu.
    - c. Baadhi ya ushahidi kwa ajili ya nadharia ya Wagalatia wa Kikusini
      - (1) Hakuna kutajwa kwa watenda kazi waliokwenda na Paulo kwa majina yao lakini Barnaba anatajwa mara tatu (kama vile Mdo. 2:1,9,13). Hii inashabihiana na safari ya kwanza ya kimishonari ya Paulo
      - (2) Inatajwa kwamba Tito hakuwa ametahiriwa (kama vile Mdo. 2:1-5). Hii inashabihiana sana kabla ya Baraza la Yerusalemu la Mdo.15.
      - (3) Kutajwa kwa Petro (kama vile Mdo. 2:11-14) na tatizo la ushirika pamoja na mataifa linashabihiana vizuri sana kabla kabla ya Baraza la Yerusalemu.
      - (4) wakati fedha ilipochukuliwa kwenda Yerusalemu, watendakazi kadhaa wa Paulo kutoka maeneo tofauti tofauti (kama vile Mdo. 20:4) wana orodheshwa. Hakuna, hata hivyo walio orodheshwa kutoka miji ya Galatia Kaskazini, japokuwa tunafahamu makanisa haya ya makabila ya Wagalatia yalishiriki (kama vile 1 Kor. 16:1). Kwa ajili ya uwasilishaji wa ndani wa hoja tofauti tofauti juu ya nadharia hizi, tafuta fasiri za kuifundi. Kila moja yake ina jambo la muhimu. Mpaka muda huu hakuna makubaliano, lakini "Nadharia ya Kusini" inaonekana kukaa vizuri zaidi ya zote kiukweli.
- C. Mahusiano ya Wagalatia kwa Matendo ya Mitume
    1. Paulo alifanya safari kuelekea Yerusalemu, inawekwa katika kumbukumbu na Luka katika kitabu cha Matendo ya Mitume
      - a. 9:26-30, baada ya kuongoka kwake
      - b. 11:30; 12:25, kupeleka misaada kutokana na njaa kutoka katika makanisa ya Mataifa
      - c. 15:1-30, Baraza la Yerusalemu.
      - d. 18:22, safari fupi
      - e. 21:15 maelezo mengine ya kazi ya mataifa

2. Kuna safari mbili kuelekea Yerusalemu inayowekwa katika kumbukumbu katika Wagalatia:
  - a. 1:18, baada ya miaka mitatu
  - b. 2:1, baada ya miaka kumi na nne
3. Inavyoonekana zaidi kwamba Mdo. 9:26 inahusiana na Gal. 1:18. Mdo. 11:30 & 15:1 ni matengenezo ya mikutano ambayo haijawekwa katika kumbukumbu ambayo inatajwa katika Gal. 2:1.
4. Kuna baadhi ya tofauti kati ya Mdo. 15 na hesabu za Gal. 2 lakini hii yawezekana ni kwasababu ya
  - a. mtazamo tofauti tofauti
  - b. makusudi tofauti tofauti ya Luka na Paulo
  - c. ukweli ambao Wagalatia 2 kinaweza kuwa kimetokea kuwa nao wakati fulani kabla ya mkutano unaoelezwa katika Mdo. 15 kwa muunganiko pamoja nayo.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 14:1-7

<sup>1</sup> Ikawa huko Ikonio wakaingia pamoja katika sinagogi la Wayahudi; na kwa vile walivyonena, kundi kubwa la Wayahudi na la Wayunani wakaamini. <sup>2</sup> Walakini Wayahudi wasioamini wakawataharakisha watu wa Mataifa na kuwatia nia mbaya juu ya ndugu. <sup>3</sup> Basi wakakaa huko wakati mwingi, wakinena kwa ushujaa katika Bwana, aliyelishuhudia neno la neema yake, akiwajalia ishara na maajabu yatendeke kwa mikono yao. <sup>4</sup> Lakini jamii ya watu wa mjini wakafarakana; hawa walikuwa upande wa Wayahudi, na hawa upande wa Mitume. <sup>5</sup> Hata palipotokea shambulio la watu wa Mataifa na Wayahudi pamoja na wakubwa wao juu yao, kuwatenda jeuri na kuwapiga kwa mawe, <sup>6</sup> wao wakapata habari wakakimbilia Listra na Derbe, miji ya Likaonia, na nchi zilizo kando kando; <sup>7</sup> wakakaa huko, wakihubiri Injili.

**14:1 "Ikonio"** Kuna kitabu cha karne ya pili kisicho kuwa katika kanoni kinachojulikana kama *The Acts of Paul and Thekla*, ambacho kilitoa taarifa juu ya shughuli za Paulo katika mji wa Ikonio. Kitabu hiki yawezekana kinajumuisha maelezo ya nje ya kimwii ya Paulo ambayo yaliwahi kuwekwa kumbukumbu: mfupi, mwenye kipara, matege na mwenye nyusi nyingi na macho makubwa yaliyotokeza nje. Si jambo la kiuvuvio na lakini bado linaaksi matokeo ambayo Mtume Paulo aliyapata katika eneo hili la Asia ndogo. Sehemu kubwa ya eneo hili ipo katika Jimbo la Kirumi la Galatia.

▣ **"wakaingia pamoja katika sinagogi"** Hii ilikuwa utaratibu wa kawaida ya Paulo na Barnaba. Wasikiaji hawa wote Wayahudi na Wayunani walikuwa wanajua ahadi na nabii za Agano la Kale.

▣ **"kundi kubwa la Wayahudi na la Wayunani wakaamini"** Tungo hii inaonesha kusudi la Matendo ya Mitume. Injili inasambaa kwa haraka katika ya watu mbalimbali. Maana za ahadi za Agano la Kale kwa wanadamu wote (kama vile Mwanzo 3:15; 12:3) sasa zinaweza kutimia. Kauli za Muhtasari huu zinazohusiana na kukua kwa kasi kwa kanisa ni tabia za maandiko ya Luka.

**14:2 "Wayahudi wasioamini"** Wokovu unawekwa sifa za "wakaamini" (kama vile Mdo. 14:1), upofu wa kiroho na ukaidi unapewa sifa za "kutotii" au "kutokuamini." Kukataa kuitikia kwa Injili kunapelekea mtu upofu na kupoteza! Luka analeta nyaraka zinazopingana vikali sana za kutokuamini kwa Wayahudi na mateso yanayoendelea. Ni kukataa kwao ambako kunafungua mlango wa imani kwa mataifa (kama vile Warumi 9-11).

▣ **"wakawataharakisha"** Hiki ni kitenzi cha kawaida katika Tafsiri za Agano la Kale kwa uasi (kama vile 1 Sam. 3:12; 22:8; 2 Sam. 18:31; 22:49; 1 Nyakati 5:26), lakini inatumika hapa katika Agano Jipya tu katika Mdo. 13:50 na hapa.

▣ **"kuwatia nia mbaya"** Hili ni neno lingine ambalo linatumiwa sana katika Tafsiri ya Agano la Kale kuelezea uovu, watu waonevu ambao wanawatenda wengine vibaya. Luka analitumia neno hili mara kwa mara katika Mdo. (kama vile Mdo. 7:6,19; 12:1; 14:2; 18:10).

**14:3** Mungu alitumia miujiza kuthibitisha tabia yake ya rehema na ukweli wa injili ya Yesu Kristo katika eneo hili jipya (kama vile Mdo. 4:29-30; Ebr. 2:4).

**14:4 "Lakini jamii ya watu wa mjini wakafarakana "** Neno la kweli siku zote hugawanyisha (kama vile Mdo. 17:4-5; 19:9; 28:24; Mt. 10:34-36). Baadhi ya Wayahudi katika Sinagogi waliamini lakini wengine wakawa waasi dhidi ya injili.

▣ **"upande wa Mitume"** Hii inawamaanisha wote Paulo na Barnaba. Katika Sura hii (yaani 14:4 na 14) ni muda wa pekee ambao Luka analitumia neno hili kumaanisha yoyote isipokuwa wale mitume wa asili wa kwanza Kumi na mbili. Barnaba anaitwa Mtume (kama vile Mdo. 14:14) Hii pia inamaanishwa katika 1 Kor. 9:5-6. Hii ni neno dhahiri kwa matumizi mapana "mtume" zaidi ya Kumi na mbili. Yakobo mwenye kutenda haki (ndugu wa ukoo wa Yesu) anaitwa mtume katika Wagalatia 1:19; Silvano na Timotheo walikuwa wakiitwa mitume katika 1 The. 1:1 ukiunganisha na 2:6; Andronicus na Yunius (Yunia katika toleo la KJV), wanaitwa mitume katika Rum. 16:6-7; na Apollo anaitwa mtume katika 1 Kor. 4:6-9.

Mitume kumi na mbili walikuwa wakipekee. Pale walipokufa hakuna aliyepatikana wakuchukua nafasi zao (isipokuwa Matthiya kwa ajili ya Yuda, kama vile Mdo. 1). Hata hivyo kuna kipawa kinachoendelea ya utume kinachotajwa katika 1 Kor, 12:28 na Efe. 4:11. Agano Jipya haitoi taarifa za kutosha kufunua kazi ya karama hii. Angalia Mada Maalum: Kutuma (*Apostellō*) inafuata.

### **MADA MAALUMU: KUTUMA (*apostellō*)**

Hili ni neno la kiyunanila kawaida kwa "upelekwa" (yaani *apostellō*). Neno hili lina matumizi kadha ya kithiolojia:

1. Katika kiyunani cha sasa na kwa Wayahudi waliokuwa na elimu na viongozi wa dini, neno hili hutumiwa kama moja inayoitwa na kutumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine, kitu kama kiingereza chetu "Balozi". (kama vile. 2 Kor. 5:20).
2. Injili daima zinatimia kitenzi hiki kwa Yesu kutumwa na baba yake, katika Yohana, linasikika zaidi kama Masihi (kama vile Mt. 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48 na hasa Yohana 5:36, 38; 6:29, 57; 7:26; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3, 8, 18, 21,23 25; 20:21 (Yote "*apostellō*" na KISAWE CHAKE *pempō* inayotumika katika mst. 21). Inatumika kwa Yesu kutuma waumini (kama vile. Yn 17:18; 20:21<sup>21</sup> [Yote "*apostellō*" na KISAWE CHAKE ni "*pempō*" katika Yohana 20:21]).
3. Agano Jipya lilituma jina "Mtume" kwa wanafunzi
  - a. Mitume kumi na wawili wa mwanzo kama mzunguko wa kwanza kati ya wanafunzi wake. (Marko 6:30; Luka 6:13; Mdo. 1:2; 26)
  - b. Kundi maalumu la msaada la Mitume na watumishi wenzie.
    - 1) Barnabasi (kama vile. Mdo. 14:4, 14)
    - 2) Andronicus na Junias (KJV, Junia , kama vile. Rum. 16:7)
    - 3) Appollo (kama vile. 1 Kor. 4:6-9)
    - 4) Yakobo ndugu wa Bwana (kama vile. Gal. 1:19)
    - 5) Silvanus na Timotheo (kama vile. 1The. 2:6)
    - 6) Bila shaka Tito (kama vile. 2 Kor. 8:23)
    - 7) Bila shaka Epafrodito (kama vile. Efe. 2:25)
  - c. Zawadi inayoendelea katika kanisa (kama vile. 1 Kor. 12:28-29; Efe 4:11)
4. Paulo anatumia cheo hiki kwa ajili yake katika barua zake nyingi kama njia ya kuonesha mamlaka yake aliyopewa na Mungu kama mwakilishi wa Kristo. (kama vile. Rum. 1:1 1 Kor. 1:1; Gal. 1:1; Efe. 1:1; Kol. 1:1; Tim. 1:1 2Tim. 1:1; Tito 1:1).
5. Tatizo tunalokumbana nalo kama waamini wa leo ni kwamba Agano Jipya halitafasiri hii zawadi inayoendelea inahusu nini au vipi inabainishwa kwa waamini. Bila shaka mtu apaswa kutofautisha kati kumi nambaili ya awali (# 3b) na matumizi ya baadaye (# 3b). Tazama Mada Maalumu: Msukumo na Mada Maalum: Mwangaza. Kama mitume wa leo hawakusukumwa kuandika maandiko mengi matakatifu (yaani, kitabu cha Wayunani kanoni kimefungwa, kama vile. Yuda mst.



3; tazama. Mada Maalumu: kanuni ya kanisa) kisha kipi wanafanya tofauti na Manabii wa Agano Jipya na Wainjilisti (kama vile. Efe. 4:11) hapa kuna uwezekano wa mambo.

- a. Waanzilishi wa kanisa la wamisionari huanza katika maeneo yasiyo ya uinjilisti (kutumika kama vile katika *Doache*)
- b. Viongozi wa Wachungaji katika eneo Fulani au madhehebu.
- c. ?

Napenda # 1.

**14:5 "pamoja na wakubwa wao juu yao"** Hii inaweza kumaanisha viongozi wa mji au viongozi wa Sinagogi. Baadhi ya wafasiri wa kwanza na wa kisasa wanatoa maelezo ya mateso mawili (1) Mdo. 14:2 na (2) na Mdo. 14:5, lakini muktadha inamaanisha mara moja.

**NASB, NRSV,**

**TEV** "kuwatenda vibaya"

**NKJV** "kuwatumia vibaya"

**NJB** "kuwavamia"

Neno la Kiyunani *hubrizō* ni zaid ya kali "kuwatendea vibaya," yawezekana "kuwafanya kichaa," au "kufanya matendo ya vurugu." Ni kawaida sana katika Tafsiri za Agano la Kale. Luka anatumia neno hili mara kwa mara katika nama tatu.

1. kutukana, Luka 11:45
2. matendo ya ghasia, Luka 18:32; Mdo. 14:5
3. Kupoteza mali za kimwili, Mdo. 27:10,21

▣ **"mawe"** Hili ni neno la pili linalofunua na kuonesha upinzani wa vurugu kupanga uvamizi kwa waamini. Yawezekana kipengele cha Kiyahudi walichagua namna hii kwasababu ya muunganiko wake wa Agano la Kale na Kufuru (yaani Mambo ya Walawi 24:16; John Yohana 8:59; 10:31-33).

**14:6 "wakakimbilia Listra na Derbe, miji ya Likaonia"** Ikonio ilikuwa Phrygia. Ilikuwa karibu na mpaka wa kundi kabila la aina yake. Maelezo haya yanaoneshwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume.

**14:7** Kitenzi ni kauli ya kati ya wakati uliotimilifu yenye mafumbo, ikiwa na maana kwamba walihubiri tena tena. Haya ndiyo maudhui ya safari za kimishonari za Paulo (kama vile Mdo. 14:21; 16:10). Wale waliomwamini Kristo chini ya mahubiri yake pia walihisi uharaka na mamlaka ya kuwasilisha injili kwa wengine. Hii ilikuwa na ndio ni kipaumbele (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8)

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 14:8-18**

<sup>8</sup> Na huko Listra palikuwa na mtu mmoja, dhaifu wa miguu, kiwete tangu tumboni mwa mamaye, ambaye hajaenda kabisa. <sup>9</sup> Mtu huyo alimsikia Paulo alipokuwa akinena; ambaye akamkazia macho na kuona ya kuwa ana imani ya kuponywa, <sup>10</sup> akasema kwa sauti kuu, Simama kwa miguu yako sawasawa. Akasimama upesi akaenda. <sup>11</sup> Na makutano walipoona aliyoyafanya Paulo wakapaza sauti zao, wakisema kwa Kilikaonia, Miungu wametushukia kwa mifano ya wanadamu. <sup>12</sup> Wakamwita Barnaba, Zeu, na Paulo, Herme, kwa sababu ndiye aliyekuwa mnenaji. <sup>13</sup> Kuhani wa Zeu ambaye hekalu lake lilikuwa mbele ya mji, akaleta ng'ombe na taji za maua hata malangoni, akitaka kutoa dhahihu pamoja na makutano. <sup>14</sup> Walakini mitume Barnaba na Paulo, walipopata habari, wakararua nguo zao, wakaenda mbio wakaingia katika makutano, wakipiga kelele, <sup>15</sup> wakisema, Akina bwana, mbona mnafanya haya? Sisi nasi tu wanadamu hali moja na ninyi; twawahubiri habari njema, ili mgeuke na kuyaacha mambo haya ya ubatili na kumwelekea Mungu aliye hai, aliyeumba mbingu na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo; <sup>16</sup> ambaye zamani zilizopita aliwaacha mataifa yote waende katika njia zao wenyewe. <sup>17</sup> Lakini hakujiacha pasipo ushuhuda, kwa kuwa

**alitenda mema, akiwapeni mvua kutoka mbinguni, na nyakati za mavuno, akiwashibisha mioyo yenu chakula na furaha.<sup>18</sup> Na kwa maneno hayo wakawazuia makutano kwa shida, wasiwatolee dhabihu.**

**14:8 "Na huko Listra"** Huu mji ulikuwa nyumba ya Timotheo (kama vile Mdo. 16:1). Hili ni Koloni lililoanzishwa na Augustus katika karne ya 6 b.k. Kunawezekana hakukuwa na Sinagogi, hivyo Paulo na Barnaba walikuwa wakifanya mahubiri ya mitaani.

▣ Hivyo hapakuwa na uwezekano wa mbinu au udanganyifu (kama vile Mdo. 3:2). Kuna tungo za maelezo maalum tatu zinazoeleza hali ya kudumu ya mtu huyu.

1. hakuwa na nguvu katika miguu yake
2. kiwete toka tumboni mwa mama yake
3. hakuwahi kutembea kabla

▣ **"dhaifu"** Neno *adunatos* siku zote linamaanisha "kutokuwezekana" au kidhahiri "kutoweza" (kama vile Luka 18:27; Ebr. 6:4,18; 10:4; 11:6), lakini hapa Luka analitumia kama mwandishi wa kidaktari katika namna ya kutozaa au dhaifu (kama vile Rum. 8:3; 15:1).

Inafurahisha kwamba, kuna mashabihiano mengi kati ya huduma za Paulo na na Petro. Petro na Yohana wanamponya kiwete katika Mdo. 3:1-10 sasa hivyo pia inatotea Paulo na Barnaba wanafanya pia.

**14:9 "akamkazia macho"** Luka anatumia tumgo hii mara kwa mara (kama vile Mdo. 3:4; 10:4). Angalia kidokezo katika Mdo.1:10. Paulo alimuona mtu huyu akiangalia kwa umakini. Hivyo, akamuamuru asimame na kutembea (kama vile mstari wa 10) na alifanya hivyo!

▣ **"na kuona ya kuwa ana imani ya kuponywa"** Hii inatumika katika namna ya Agano la Kale "kuokolewa," ikimaanisha wokovu wa kimwili. Tazama kwamba Uwezo wa Paulo kuponya ulikuwa umejikita juu ya imani ya yule mtu. Hii inatokea mara kwa mara japo sio maeneo yote katika Agano Jipya (kama vile Mdo. 5:20; Yohana 5:5-9). Miujiza ilikuwa na kazi kadhaa:

1. kuonesha upendo wa Mungu
2. kuonesha nguvu na kweli ya injili
3. kutoa mafunzo na kutia moyo waamini wengine waliopo

**14:11 "wakisema kwa Kilikaonia"** Inavyoonekana na ni wazi Paulo na Barnaba hawakuelewa kile ambacho umma ulikuwa unakisema. Hii ilikuwa ni lugha ya jadi ya eneo lile.

**14:12 "Wakamwita Barnaba, Zeu, na Paulo, Herme, kwa sababu ndiye aliyekuwa mnenaji"** Mila na desturi za jadi zilieleza kwamba miungu ya kiyunani mara kwamara iliwatembelea wanadamu katika muundo wa mwili wa kibinadamu (kama vile Ovid, *Metamorphoses* 8:626). Kutoka katika maelezo ya mahali hapa tunajifunza hii ilikuwa eneo ambapo Zeus na Hermes walikuwa wakiabudiwa (kama vile Mdo. 14:13).

Tazama kwamba Barnaba anatajwa kwanza. Hii inawezekana kwakuwa Paulo kama msemaji angeweza kuchukuliwa na hawa wapagani sawa na Hermes (Zebaki); Barnaba ambaye alikuwa kimya lazima alichukuliwa kama mungu mkuu Zeus (Jupita).

**14:13 "lango"** Hii inaweza kumaanisha jiji au zaidi yawezekana kwa hekalu la Jupita (Zeus) ambayo ilikuwa katika eneo nje kidogo tu ya lango la mji na kuangaliana nayo. Ulikuwa ni muda wa machafuko makubwa na kukosa maelewano.

**14:14 "mitume"** Angalia kidokezo katika Mdo. 14:4.

▣ **"wakachana chana mavazi yao"** Hii ni ishara ya kiyahudi ya kuomboleza na kukufuru (kama vile Mt. 26:65; Marko 14:63). Ni hakika ingekuwa imefanywa mawasiliano yake hata kwa hawa wapagani kwamba kulikuwa na tatizo.

▣ **"wakatoka"** Hili ni neno lililozoeleka katika Tafsiri ya Agano la Kale Iwa "rukia nje" au "kutoka nje kwa upesi," japo inatumika tu hapa katika Agano Jipya. Paulo na Barnaba walinyanyuka na kupotea katikati ya umati wa watu. **14:15-17** Huu hapa ni muhtasari wa hotuba ya Paulo ya kwanza kwa Wapagani. Hill Ni sawa na mahubiri yake katika kilima cha Mars (kama vile Mdo.17:22-33).

**14:15**

**NASB, NKJV** "watu wenye asili kama ninyi"

**NRSV** "tu wanadamu tupitao kama nyie"

**TEV** "sisi wenyewe ni binadamu tu kama ninyi"

**NJB** "sisi tu binadamu tu, wapitaji kama ninyi wenyewe"

Neno ni *homoioopathēs*, ambalo ni ambatani ya "ile ile" na "shauku." Neno hili linatumika hapa tu na katika Yakobo 5:17 in katika Agano Jipya. Watu wa eneo lile walifikiri kuwa Paulo na Barnaba walikuwa miungu (*homoiothentes*, kama vile Mdo. 14:11), ambayo maana yake "waliofanywa kama" wanadamu. Paulo anatumia mzizi uleule kuwaelezea ubinadamu wao wa kawaida. Luka anaonesha unyenyekevu wa Paulo na Barnaba katika kuwatofautisha mbele ya Herode Antipa katika Mdo. 12:20-23.

▣ **"ili mgeuke na kuyaacha mambo haya ya ubatili"** Neno "batili" maana yake utupu, isiyokuwepo, isiyoishi. Paulo moja kwa moja anakabiliiana na upagani wao wa kichawichawi.

▣ **"kwa Mungu aliye hai"** Huku ni kufanya matumizi mengine ya YHWH, ambayo inatoka katika kitenzi cha Kiebrania "kuwa" (kama vile Kutoka. 3:14). YHWH anaishi milele, Mungu pekee anayeishi. Angalia [MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU](#) katika Mdo. 1:6.

▣ **"aliyefanya"** Hii imenukuliwa Kutoka 20:11 au Zaburi 146:6. Neno la Kiebrania *Elohim* (kama vile Mwanzo 1:1) inaeleza Mungu kama muumbaji na mtoshelevu (kama vile *The Expositor's Bible Commentary*, vol. 1, ukurasa 468-469) kama YHWH kimfunua Yeye kama Mwokozi, Mkombozi (kama vile *The Expositor's Bible Commentary*, vol. 1, kama vile 471-472) na Mungu mfanya agano. Angalia Mada Maalum katika Mdo. 1:6.

**14:16 "ambaye zamani zilizopita aliwaacha mataifa yote waende katika njia zao wenyewe"** Tungo hii inaweza kuwa maelezo ya Kumb. 32:7-8 ambayo Musa anamueleza YHWH anayeweka mipaka ya mataifa. Kithiolojia hii inakiri hali ya kujali ya Mungu na umakini kwa mataifa (Mataifa, kama vile Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, ukurasa 258-259). Mungu alitamani kwamba wamjue Yeye, lakini anguko la mwanadamu likampelekea na kumsababishia uchawi na kuabudu sanamu (kama vile Rum. 1:18-2:29). Hata hivyo aliendelea kuwafuatilia wao (kama vile Mdo. 14:17).

Ujinga wa Mataifa unatofautishwa na maarifa ya Mungu. Kejeli ni kwamba mataifa wanaitikia katika wingi wa imani kwenye injili, wakati Wayahudi wanaitikia katika wingi wa wa kukataa na mateso kuelekea kwenye injili (kama vile Warumi 9-11).

**14:17 "Hakuondoka mwenyewe bila shuhuda"** Hii ni dhana ya ufunuo wa asili (Kama vile Zaburi 19:1-6; Rum. 1:19-20; 2:14-15). Wanadamu wote wanajua kitu kuhusu Mungu kutoka katika uumbaji na ushuhuda wa ndani wa kimaadili.

▣ **"mvua.....chakula"** Desturi za kipagani wa eneo zilizisema kuwa Zeus alikuwa mtoaji wa mvua na Hermes alikuwa mtoaji wa chakula. Paulo akifuatilia Kumbukumbu la Torati 27-29, anakiri Mungu kushughulikia asili.

Wapagani hawa hawakujua ili agano la laana la Kumbukumbu la Torati ibadilishwe na uvumilivu wa Mungu (kama vile Mdo. 17:30; Rum. 3:25; 4:15; 5:13). Paulo alikuwa chaguo la kipekee la Mungu (mtume wa mataifa) kufikia mataifa ya nchi! Paulo anatumia uumbaji wa Mungu na utoaji wa Mungu kupitia asili (kama vile Zaburi. 145:15-16; 147:8; Yer. 5:24; Yona 1:9) kama sehemu yake ya mawasiliano.

Inashangaza kwamba hakuna kitu ambacho kuhusu injili katika muhtasari huu wa mahubiri. Mtu anaweza kudhania kuwa Paulo aliendele katika mstari huu huu wa kufikiri kama alivyofanya katika mahubiri yake ya Athene katika Mdo. 17:16-34. Mtu anaweza kushangaa kama Luka alipata muhtasari huu kutoka kwa Paulo au yawezekana Timotheo (hii ilikuwa nyumbani kwake).

**14:18** Haya ni maelezo ya mtoa shuhuda

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 14:19-23**

<sup>19</sup> Lakini Wayahudi wakafika toka Antiokia na Ikonio, wakawashawishi makutano hata wakampiga kwa mawe Paulo, wakamburuta nje ya mji, wakidhania ya kuwa amekwisha kufa. <sup>20</sup> Lakini wanafunzi walipokuwa wakimzunguka pande zote, akasimama, akaingia ndani ya mji; na siku ya pili yake akatoka, akaenda zake pamoja na Barnaba mpaka Derbe. <sup>21</sup> Hata walipokwisha kuihubiri Injili katika mji ule, na kupata wanafunzi wengi, wakarejea mpaka Listra na Ikonio na Antiokia, <sup>22</sup> wakifanya imara roho za wanafunzi na kuwaonya wakae katika ile Imani, na ya kwamba imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi. <sup>23</sup> Na walipokwisha kuwachagua wazee katika kila kanisa, na kuomba pamoja na kufunga, wakawaweka katika mikono ya Bwana waliyemwamini.

**14:19** Upinzani wa Kiyahudi katika miji ambapo Paulo alikuwa amehubiri u iliunganika katika uvaizi wa sasa kwake (kama vile 2 Kor. 4:7-15; 6:3-10; 11:23-30). Tazama kwamba uvamizi ulikuwa umelenga kwa Paulo na sio Barnaba. Tazama pia ukigeugeu wa umati wa kipagani. Paulo na Barnaba baadaye wanapewa heshima kama miungu kwa wakati mmoja na baadaye wanapigwa mawe!

▣ **"wakampiga Paulo mawe"** Huku kulikuwa si kutia uhai muujiza, lakini kama hesabu ya uwezo wa kimwili wa Paulo na ujasiri (kama vile Mdo. 14:20-21). 2 Wakorintho 11:25 na Wagalatia 6:17 pia kunamaanisha tukio hili hili. Kupigwa mawe kunapangwa katika Mdo.14:5 sasa kunakuwa halisi!

**14:20 "wakati wanafunzi wamesimama wakimzunguka"** Japokuwa haijawekwa wazi kwa kusemwa, nafikiri huu ulikuwa mkutano wa maombi kwa Mungu ulioitikia kimaajabu. Tazama namna mateso yalivyoendelea kuwa mbinu kwa ajili ya kuenea kwa injili (yaani mji mpya).

**14:21 "Baada ya kuwa wameihubiri injili katika mji ule"** Hii ilimaanisha Derbe (kama vile 14:20). Mji huu pia ulikuwa ndani ya Likanoi sehemu ya jimbo la kirumi la Galatia. Hii ilikuwa mbali ya upande wa Mashariki kama Paulo na Barnaba waliosafiri katika safari hii ya kimishonari. Mji huu uliitikia vizuri Injili na wengi waliokolewa.

▣ **"wakarejea mpaka Listra na Ikonio na Antiokia"** Inavyoonekana hawakuhubiri kwa umma katika safari yao ya kurudi lakini walikuwa kwa kibinafsi wanapanga na kuwatia moyo waumini (kama vile Mdo. 14:22-23).

**14:22** Mstari huu ni muhtasari wa ujumbe wa Paulo wa kufanya wanafunzi. Tazama ilivyoweka mkazo katika (1) ustahimilivu na (2) dhiki. Waumini wanaweza kukua kutokana na majaribu (kama vile Rum. 5:3-4; 8:17-18; 1 The. 3:3; 2 Tim. 3:12; Yakobo 1:2-4; 1 Pet. 4:12-16).

- ▣ **"wakiwatia nguvu"** Neno hili linatumika mara kwa mara katika Tafsiri ya Agano la Kale katika namna "kusababisha kupumzika juu ya" au "kuimarishwa" Luka analitumia neno hili mara kadhaa kuelezea na kufuanua huduma ya Paulo ya kufuatilia hali ya uanafunzi (kama vile Mdo. 14:22; 15:32,41; 18:23).
- ▣ **"nafsi za wanafunzi"** Neno nafsi (*psuchē*) linatumika katika namna ya mtu au shughuli zao za kiakili. Hii sio dhana ya Kiyunani ya kila mtu kuwa na nafsi isiyokufa, lakini katika dhana ya Kiebrania ya nafsi (*nepshesh*, BDB 659, KB 711-713, kama vile Mwanzo 2:7) kama njia yas kumaanisha mwanadamu (kama vile Mdo. 2:41; 3:23; 7:14; 14:2,22; 15:24; 27:37).
- ▣ **"wakiwatia moyo wao kuendelea katika imani"** Angalia [MADA MAALUM: USTAHIMILIVU](#) inafuata.

## MADA MAALUM: HITAJI LA USTAHIMILIVU

Mafundisho ya kibiblia yaliyohusiana na maisha ya Mkristo ni vigumu kuyaelezea kwa sababu yanawasilishwa katika namna ile ile ya mashariki, milinganyo ya kirahaja ([angalia Mada Maalumu: Fasihi ya Mashariki \[mafumbo ya kibiblia\]](#)). Milingnyo hii inaonekana kuwa na mkanganyiko, bado mihimili yote ni ya kibiblia. Wakristo wa Mshariki walielekea kuchagua ukweli ulio mmoja na kuachana na au kukushifu kweli iliyo kinyume. Baadhi ya Mifano ni:

4. Je! Wokovu ni maamuzi asilia ya kumwamini Kristo au ni maisha yenye wajibu ya kiuanafunzi?
5. Je! Wokovu ni uchaguzi kwa maana ya neema kutoka katika mamlaka ya Mungu au imani na mwikitiko wa toba kwa sehemu ya mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu?
6. Je! wokovu, unapopokelewa, haiwezekani kuipoteza, au kuna uhitaji wa jitihada endelevu

Jambo hili la ustahimilivu limekuwa la kibishi katika historia nzima ya kanisa. Tatizo linaanza na muonekano wa mgogoro wa vifungu vya Agano Jipya:

3. maandiko yahasuyo uhakika
  - d. semi za Yesu katika Inili ya Yohana (Yohana 6:37; 10:28-29)
  - e. semi za Paulo (Rum. 8:35-39; Efe. 1:13; 2:5,8-9; Flp. 1:6; 2:13; 2 Thes. 3:3; 2 Tim. 1:12; 4:18)
  - f. semi za Petro (1 Pet. 1:4-5)
4. maandiko yahasuyo umuhimu wa ustahimilivu
  - f. semi za Yesu katika Injili za Kimhutasari (Mt. 10:22; 13:1-9,24-30; 24:13; Marko 13:13)
  - g. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 8:31; 15:4-10)
  - h. semi za Paulo (Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2; 2 Kor. 13:5; Gal. 1:6; 3:4; 5:4; 6:9; Flp. 2:12; 3:18-20; Kol. 1:23; 2 Tim. 3:2)
  - i. semi za mwandishi wa Kiebrania (2:1; 3:6,14; 4:14; 6:11)
  - j. semi za Yohana (1 Yohana 2:6; 2 Yohana 9; Ufu. 2:7,17,26; 3:5,12,21; 21:7)

Mambo ya wokovu ndani ya biblia hutoka katika pendo, huruma, na neema ya mamlaka ya Mungu wa Utatu. Hakuna mwanadamu awezaye kuokolewa pasipo kuingiliwa na Roho (cf. Yohana 6:44,65). Mungu alikuja na kupangilia mambo muhimu, lakini alidai kwamba wanadamu wanapaswa kuitikia katika imani na toba, katika namna zote kwa uanzilishi na kwa uendelevu. Mungu hutenda kazi na wanadamu katika uhusiano wa agano. Kuna upendeleo na majukumu!

Wokovu umetolewa kwa wanadamu wote. Kifo cha Yesu kilihusika na tatizo la dhambi ya uumbaji ulioanguka! Mungu ameleta njia na anahitaji wale wote walioumbwa kwa mfano Wake kuliitikia pendo Lake na utoaji katika Yesu. Kama ungependa kusoma zaidi juu ya somo hili tazama

4. Dale Moody, *The Word of Truth*, Eerdmans, 1981 (kr. 348-365)
5. Howard Marshall, *Kept by the Power of God*, Bethany Fellowship, 1969
6. Robert Shank, *Life in the Son*, Westcott, 1961

Biblia inashughulikia matatizo mawili tofauti katika eneo hili: (1) kuchukulia imani kama msimamo wa kuishi

bila kuzaa matunda, maisha ya ubinafsi au (2) kuwatia moyo wale wanaopambana na huduma na dhambi binafsi. Tatizo ni kwamba makundi yasiyo sahihi yana uchukuwa ujumbe usio sahihi na kutengeneza mifumo ya kitheolojia yenye vifungu vya kibiblia vyenye kuwekewa mipaka. Baadhi ya Wakristo wakiwa katika hali ya kukata tamaa wanahitaji ujumbe wa kuwatia moyo, wakati wengine wanahitaji kuonywa kwa ukali kuhusiana na uvumilivu! Wewe uko ndani ya kundi lipi?

Kuna mabishano ya historia ya kitheolojia iliyomuhusisha Augustine dhidi ya Pelagius na Calvin dhidi ya Arminius (semi-Pelagian). Jambo hili lilihusisha swali la wokovu : kama mtu akiokolewa kiukweli, yampasa kustahimili katika imani na uamiifu?

Wafuasi wa Calvin wamesimama nyuma ya maandiko yale ya kibiblia ambayo yanadai kwamba mamlaka ya Mungu na nguvu idumuyo (Yohana 10:27-30; Rum. 8:31-39; 1 Yohana 5:13,18; 1 Pet. 1:3-5) na vitenzi vya nyakati kama kauli tendewa timilifu endelevu ya Efe. 2:5,8.

Wafuasi wa Arminius wamesimamia maandiko yale ya kibiblia ambayo yanamuonya yule aaminiye "kusimama imara," "kudumu," au "kuendelea" (Mt. 10:22; 24:9-13; Marko 13:13; Yohana 15:4-6; 1 Kor. 15:2; Gal. 6:9; Ufu. 2:7,11,17,26; 3:5,12,21; 21:7). Mimi binafsi siamini kwamba Waebrania 6 na 10 zinatumiwa, lakini wafuasi wengi wa Arminius wanazitumia kama onyo dhidi ya uasi. Mfano wa Mpanzi katika Mathayo 13 na Marko 4 inashughulikia suala la imani, kama inavyofanya Yohana 8:31-59. Kama wafuasi wa Calvin wanavyo nukuu vitenzi vya kauli ya wakati uliopo timilifu vilivyotumiwa kueleza wokovu, Wafuasi wa Arminius wana nukuu vifungu vya kauli ya wakati uliopo kama 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15.

- Huu ni mfano kamili wa namna mfumo wa kitheolijia unayotumiwa vibaya njia ya uhakiki wa fasiri za maandiko. Mara nyingi kanuni inayoongoza au andiko kuu linatumika kutengeneza ufito wa kitheolojia ambapo maandiko mengine yote yanatazamiwa. Kuwa makini na mfumo kutoka vyanzo vyo vyote vile. Vitokana na ufafanuzi wa mantiki ya mashariki, si ufunuo. Biblia ni kitabuj cha mashariki. Inawakilisha kweli katika mvutano uliokamilishwa, ulinganifu wa mafumbo yaonekanayo. Wakristo wanamaanisha kukubaliana na yote na kuishi ndani ya ndani ya mvutano huo. Agano Jipya linawasilisha vyote yaani ulinzi wa mwaamini na dai la imani endelevu na uovu. Ukristo ni mwitikio wa mwanzo wa toba na imani inayofatiwa na mwitikio endelevu wa toba na imani. Wokovu si kama matokeo (tiketia ya kwenda mbinguni au sera ya bima ya moto), bali uhusiano. Ni maamuzi na uanafunzi. Inaelezwa katika Agano Jipya 3:5
- utimilifu (tendo lililokamilishwa na matokeo endelevu), Efe. 2:5,8
- inawasilisha (tendo endelevu), 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15
- wakati ujao (matukio yajayo au matukio fulani), Rum. 5:8,10; 10:9; 1 Kor. 3:15; Fil. 1:28; 1 The. 5:8-9; Ebr. 1:14; 9:28

katika vitenzi vyote vya nyakati:

- kauli (tendo timilifu), Matendo 15:11; Rum. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito

▣ **"ufalme wa Mungu"** Hii ni tungo ngumu kuifasiri. Yesu alitumia mara kwa mara katika muunganiko na huduma yake mwenyewe. Hata hivyo, Mitume kiudhahari hawakuelewa umuhimu wake (kama vile Mdo. 1:3,6). Katika Mdo inafanana kabisa na kismwawe na ijili (kama vile Mdo. 8:12; 19:8; 20:25; 28:23,31). Hata hivyo katika Mdo 14:22 inaelezea maana zinazomaanishwa kwa matukio ya siku za mwisho. Ni hii "tayari" (kama vile Mt. 12:28; Luka 16:16) dhidi ya "bado" (kama vile Mt. 24:14,30,36-37; 25:30,31; 2 Pet. 1:11) Mvutano ambao unapamba tabia za kizazi hiki. Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:17. Ufalme wa Mbinguni umekuja katika Yesu Kristo (yaani Kuja kwa Mara ya Kwanza), lakini kuhitimishwa katika siku za usoni (yaani Kuja kwa Mara ya Pili).

**14:23 "walikuwa wamewateua wazee"** Neno "wazee" (*presbuteros*) ni kisawe cha maneno "askofu" (*episkopos*) na "wachungaji" (*poimenos*) ndani ya Agano Jipya (kama vile Mdo. 20:17,28 na Tito 1:5,7). Neno "mzee" lina usuli wa kiyahudi (kama vile Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, ukurasa wa 244-246 na Frank Stagg, *New Testament Theology*, kurasa za 262-264), wakati neno "askofu" au "mwangalizi" lina usuli wa mji wa kiyunani. Kuna viongozi wawili tu wa kanisa wanao orodheshwa katika Agano Jipya: wachungaji na mashemasi (Kama vile Flp. 1:1).

Neno "teuwa" kunaweza kumaanisha "kuchagua kwa kunyooshewa mikono" (kama vile 2 Kor. 8:19 na Louw na Nida, *GreekEnglish Lexicon*, ukurasa wa 363, 484). Neno baadaye linatumika kwa ajili ya "kuweka wakfu" kulikofanywa na mababa wa kanisa la kwanza. Suala nyeti ni kwa namna gani "unachagua kwa kura" kunafaa na kushabihiana kimuktadha? Kura kwa makanisa haya mapya kunaonekana sio sawa (Japokuwa kanisa katika Yerusalemu lilipiga kura kwa ajili ya saba katika Mdo. 6 na kanisa linapiga kura kuthibitisha huduma ya Paulo kwa mataifa katika Mdo. 15).

F. F. Bruce, *Answers to Questions*, ukurasa wa 79 anasema, "kiasili kuteuliwa kwa kuonesha au uchaguzi wa kuonesha mikono (inavyoonekana kwa kunyoosha mkono), ilikuwa imepoteza nguvu hii husika katika nyakati za Agano Jipya na kulikuwa kumekuja kumaanisha tu 'teuwa,' licha ya taratibu za namna yoyote." Mtu hawezi kuchagiza au kukataa dol ala kidini/kikasasi kwa matumizi ya neno hili katika Agano Jipya.

Tazama kwamba Paulo anatoa maelekezo kwa Tito ili pia ateuwe "wazee" kwa Krete, lakini kwa Timotheo katika Efeso Paulo anasema waliache kanisa lichague watu wa sifa fulani (kama vile 1 Timotheo 3). Katika maeneo mapya viongozi waliteuliwa, lakini katika maeneo yaliyojijithibitisha tayari katika tabia za uongozi kulikuwa na nafasi ya kudhihirishwa na kuthibitishwa na kanisa la mahali fulani.

Tazama kwamba mbinu za kimishonari za Paulo ni kuyajenga makanisa ya mahali watacaoendeleza kazi ya uinjilisti na uanafunzi katika maeneo yao (kama vile Mt. 28:19-20). Hii ni mbinu ya Mungu ya kufikia ulimwengu mzima (yaani makanisa ya nyumbani)!

▣ **"kanisa"** Angalia Mada Maalum katika Mdo. 5:11.

▣ **"baada ya kufunga na kuomba"** Hii inaweza kimakusudi ipo sambamba na 13:2-3. Paulo alikuwa na uzoefu wa nguvu ya Roho na mwelekeo Antiokia. Aliendeleza utaratibu huu huu wa kiroho. Walitakiwa wenyewe kujiandaa kwa ajili ya Mungu kufunua mapenzi yake. Angalia [MADA MAALUM: KUFUNGA](#) katika Mdo. 13:2.

▣ **"katika yeye waliyekuwa wameamini"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliotimilifu ainishi, ambayo inaashiria kitendo kilichomalizika cha wakati uliopita. Hawa viongozi wazee walikuwa wameamini kwa kipindi cha muda na walaikuwa wamethibitisha kuwa waaminifu wakionesha sifa za uongozi.

Matengenezo haya ya kisarufi ya *eis* yanayounganishwa na *pisteuō* (kama vile Mdo. 10:43) ni tabia ya maandiko ya Yohana, lakini pia ipo kwa Paulo (kama vile Rum. 10:14; Gal. 2:16; Flp. 1:29) na Petro (kama vile 1 Pet. 1:8). Angalia Mada Maalum katika Mdo.3:16 and na 6:5.

▣ **"wakawaweka kwa Bwana"** Hii haimaanishi baadhi ya aia ya kuwekwa wakfu. Kitenzi kilekile kinatumika katika Mdo. 14:26 kwa Paulo na Barnaba, wakati katika Mdo. 20:32 kwa wale ambao tayari walikuwa ni wazee. Kuwekwa wakfu kunasaidia kwa maana kwamba kunaweka mkazo kweli kwamba Mungu anawaita watu kwenye uongozi. Inakuwa ni mbaya na sio kibiblia ikiwa inaweka utofauti kwa waaminio. Waaminio wote wanaitwa na kupewa kipawa kwa ajili ya huduma (kama vile Efe. 4:11-12). Hakuna utofauti wa kusafisha kusikokuwa kwa kawaida katika Agano Jipya.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 14:24-28**

<sup>24</sup> Wakapita kati ya Pisidia wakaingia Pamfilia. <sup>25</sup> Na baada ya kuhubiri lile neno katika Perge wakatelemka mpaka Atalia. <sup>26</sup> Na kutoka huko wakaabiri kwenda Antiokia. Huko ndiko walikoombewa neema ya Mungu

**kwa ile kazi waliyokwisha kuitimiza.<sup>27</sup> Hata walipofika wakalikutanisha kanisa, wakawaeleza mambo yote aliyoyafanya Mungu pamoja nao, na ya kwamba amewafungulia Mataifa mlango wa imani.<sup>28</sup> Wakaketi huko wakati usiokuwa mchache, pamoja na wanafunzi.**

**14:24** Uwanda wa juu wa jimbo la Pisidia lipo kaskazini mwa pwani ya jimbo la Pamphilia. Perga ulikuwa mji mkuu wa mkoa. Paulo alipita tu katika jiji hili mapema (kama vile Mdo. 13:13), lakini sasa anarudi na kuhubiri injili (kama vile Mdo. 14:25).

**14:25 "Atalia"** Hii ilikuwa ni bandari ya bahari ya Perga.

**14:26 "wakaabiri kwenda Antiokia"** Hawakurudi Cipro. Barnaba angerudi baada ya mgogoro na Paulo juu ya Yohana Marko (kama vile Mdo. 15:36-39).

▣ **"walikoombewa neema ya Mungu"** Kitenzi ni kauli tendwa timilifu ainishi yenye mafumbo. Hii safari ya kwanza ya kimishionari ilianzishwa na kushikiliwa na Roho, ilikuwa ya mafanikio sana.

**14:27 "Hata walipofika wakalikutanisha kanisa, wakawaeleza mambo yote aliyoyafanya Mungu pamoja nao"** Tazama walivyokuwa wakiwajibika kwa kanisa. "Hata mitume kwa ajili ya Mataifa" walitoa ripoti kwa kanisa la mahali (Angalia Mada Maalum katika 5:11). Pia walitambua aliyefanya jambo kubwa hili—YHWH/Roho. Hawakutoa taarifa kwa viongozi (kama vile Mdo. 13:1), lakini kwa kusanyiko na baadaye walitoa taarifa kuhusu shughuli zao kwa kusanyiko la Yerusalemu (kama vile Mdo. 15:4) na kwa namba hiyo, makusanyiko mengine huko njiani (kama vile Mdo. 15:3). Nafikiri ilikuwa ni kusanyiko zima walioweka mikono yao juu yao na kuwaweka wakfu katika safari yao.

▣ **"na ya kwamba amewafungulia Mataifa mlango wa imani"** Paulo alitumia tungo hii "mlango wa imani" mara kwa mara sana (kama vile 1 Kor. 16:9; 2 Kor. 2:12; Kol. 4:3; na pia tazama Ufunuo 3:8). Mungu alifunua mlango kwa wanadamu wote katika injili kwamba asiwepo mtu ambaye atapoteza. Maana kamili ya maneno ya Yesu katika Mdo. 1:8 sasa yapo yanatimizwa.

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, hii ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ainisha safari ya kwanza ya Paulo ya kimishionari kwa maeneo ya kijiografia.
2. Ainisha vyote mahubiri ya Paulo: kwa Wayahudi na kwa Wapagani.
3. Je ni kwa namna gani kufunga kunahusianishwa na mkristo wa kisasa?
4. Kwanini Yohana Marko aliacha timu ya kimishionari?



## MATENDO YA MITUME 15

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFASIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Baraza la Yerusalem	Mzozo juu ya tohara	Mjadala juu ya Watu wa mataifa	Mkutano huko Yerusalem	Mjadala huko Antiokia
15:1-5	15:1-5	15:1-5	15:1-2  15:3-5	15:1-2  15:3-4  Mjadala huko Yerusalem  15:5-7a
	Baraza la Yerusalem			
15:6-11	15:6-21	15:6-21	15:6-11	Hotuba ya Petro  15:7b-11
15:12-21			15:12-18  15:19-21	15:12  Hotuba ya Yakobo  15:13-18  15:19-21
Jibu la baraza	Tamko la Yerusalem		Barua kwa waamini Wa mataifa	Barua ya kitume
15:22-29	15:22-29	15:22-29	15:22-29	15:22-29
Kuiendeleza Huduma huko Shamu				Wajumbe huko Antiokia
15:30-35	15:30-35	15:30-35	15:30-34  15:35	15:30-35
Paulo na Barnaba Wanatengana	Mgawanyiko juu ya Yohana aitwaye Marko	Kuondoka kwa safari ya pili ya Umisionari	Paulo na Barnaba wanatengana	Paulo anatengana na Barnaba na kumwandaa Sila
15:36-41	15:36-41	15:36-41	15:36-41	15:36-38  15:39-40

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" \("A Guide to Good Bible Reading"\)](#))

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **UTAMBUZI WA KIMUKTADHA**

- A. Sura hii mara nyingi inaitwa "baraza la Yerusalem."
- B. Hii ilikuwa ni sehemu muhimu ya kuanzia, mgawanyiko wa kithiolojia, katika mbinu na mikakati ya kanisa la mwanzo. Kwa maana ya kugawa vituo viwili vya jamii ya Kikristo, Yerusalem na Antiokia
- C. Mageuzi ya wale wasio Wayahudi katika Matendo 8-11 yanaonekana kuruhusiwa kuwa kama ya kitofauti (hawakuwa wapagani kamili, kiutendaji), lakini sio kama sera mpya iliyotakiwa kutendwa kwa nguvu (kama vile 11:19)
- D. Uhusiano wa kifungu hiki cha Wagaratia 2 hakieleweki. Matendo 15 au Mdo. 11:27-30 ingaliweza kuwa ni mazingira ya nyuma ya Wagaratia 2. Angalia utangulizi katika Matendo 14,C.
- E. Inafurahisha kuwa ishara iliyojirudia siku ya Pentekoste ya kunena kwa lugha (Matendo 2,8 & 10; yumkini Matendo 15:8) haijatajwa kabisa kama ushahidi kwa ajili ya uthibitisho wa wokovu kwa Mataifa (yaani, wapagani)

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO 15:1-5**

<sup>1</sup> Wakashuka watu waliotoka Uyahudi wakawafundisha wale ndugu ya kwamba, Msipotahiriwa kama desturi ya Musa hamwezi kuokoka. <sup>2</sup> Basi baada ya Paulo na Barnaba kushindana na watu hawa na kuhojiana nao sana, ndugu wakaamuru kwamba Paulo na Barnaba na wengine miongoni mwao wapande kwenda Yerusalemu kwa mitume na wazee kwa habari ya swali hilo. <sup>3</sup> Basi, wakisafirishwa na kanisa, wakaipita kati ya nchi ya Foinike na Samaria, wakitangaza habari za kuongoka kwao Mataifa; wakawafurahisha ndugu sana. <sup>4</sup> Walipofika Yerusalemu wakakaribishwa na kanisa na mitume na wazee, nao wakawaeleza mambo yote Mungu aliyoyafanya pamoja nao. <sup>5</sup> Lakini baadhi ya madhehebu ya Mafarisayo walioamini wakasimama wakisema, Ni lazima kuwatahiri na kuwaagiza kuishika torati ya Musa.

**15:1 "Wakashuka watu waliotoka Uyahudi"** Aya hii inarejelea juu ya tukio lililojili huko Antiokia. "wakashuka watu" inarejelea kikundi cha waamini ambao walijitoa kote katika dini ya Kiyahudi na kwa Yesu. walimwona Yesu kama utimilifu wa imani ya Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-19), na sio mpinzani, wala mbadala wake (kama vile Mdo. 1 1 :2; 1 5:5; Gal. 2:1 2).Thiolojia ya watu hawa inahusiana na walimu wa uongo wa Kiyahudi (wafuasi wa dini ya Kiyahudi) waliorejelewa kwenye kitabu cha Wagalatia. Watu hawa kiwastani walijihusianisha na kanisa la Yerusalem (kama vile Mdo. 1 5:24), hawakuwa wawakilishi rasmi. Tambua kifungu kinasema "shuka."ukiangalia katika ramani, inaonekana kuwa "juu,"lakini kwa Wayahudi kila mahali palikuwa "chini,"kithiolojia, toka

Yerusalem (kama vile Mdo. 15:2).

☐ **"wakawafundisha"** Hii ni nje ya wakati usiotimilifu, ambayo inaweza kumaanisha(1 ) akaanza kuwafundisha au (2) akawafundisha tena na tena.

☐ **"Msipotahiriwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza, ikimaanisha tendo muhimu. Kutahiriwa ilikuwa ni ishara ya agano kwa Ibrahim na urithi wake (kama vile Mwa. 1 7:1 0-1 1 ). Hili halikuwa jambo dogo katika dini ya Kiyahudi, bali lilihusiana na wokovu. Watu hawa walifikiri kuwa njia iliyopo ya kumfikia YHWH ni kupitia dini ya Kiyahudi (kama vile Mdo. 1 5:5). Aina hii ya watu walikuja kujulikana kama wafuasi wa dini ya Kiyahudi (kama vile Gal. 1 :7; 2:4.waliamini katika Kristo na kukubali agano la Musa (kama vile Mdo. 1 5:5). Haki iliegamia juu ya utendaji wao, na sio zawadi ya bure ya Mungu. Uhusiano wa Mtu na Mungu ulifikiwa na utendaji wa mtu (kama vile Rum. 3:21 -30; Gal. 5:2-9). Suala lenyewe lilikuwa hasa ni wapi "watu wa Mungu"na ni namna gani unaweza kuwaainisha?

**15:2 "Basi baada ya Paulo na Barnaba kushindana na watu hawa na kuhojiana nao sana"** Luka anatumia maelezo ya "kuhojiana sana"kuonysha hisia nzito (kama vile Luka 23:1 9,25; Mdo. 1 5:2; 1 9:40; 23:7,1 0; 24:5). Mjadala huu ulikuwa wa muhimu! Ulielekezwa kwenye kitovu cha ujumbe wa injili:

1. Namna mtu anavyosimama vizuri na Mungu?
2. Je agano jipya lisilotengana linahusiana na agano la Musa?

kifungu katika toleo la NASB, "palikuwa na majadiliano na kuhojiana,"kiuhalisia linamaanisha "kutokukubaliana na kuhoji kwingi." *Young's Literal Translation of the Bible* (uk. 95), ina kifungu "sio mgogoro mdogo na majadiliano."Hizi mbinu za kifasihi za kuelezea kitu Fulani katika hali ya kinyume ya kutoeleza kikamilifu zinaainishwa katika maandiko ya Luka. Angalia maelezo kamili katika Mdo. 12:18.

☐ **"Ndugu wakaamuru kwamba"** Hii inalirejelea "kanisa" (kama vile Mdo. 1 5:3). Kuna makundi mbali mbali katika Matendo 15 ambayo yanahusiana na uongozi mbali mbali au aina ya dola.

1. Katika mistari ya 2,3,12, na 22 mamlaka ya kimkusanyiko inatajwa
2. Katika mistari ya 6 na 22 mamlaka ya Kitume au ki-Askofu (yaani., Yakobo) inatajwa, ambayo ni Romani Katoriki au dola ya kianglikani
3. Katika mistari ya 6 na 22 mamlaka ya wazee inatajwa. Hii inaonekana kuwa sambamba na dola ya Presibiteria

Agano Jipya linaweka kumbu kumbu yote ya muundo wa dola. Kuna maendeleo toka kwenye mamlaka ya Kitume (ambaye siku moja atakufa) kwa mamlaka ya wale wanaohudhulia ibada, wakiwa na wachungaji wenye kuchochea uongozi (kama vile Mdo. 15:19). Kwa maoni yangu muundo wa dola sio muhimu sana kama viongozi wa kiroho. Agizo kuu, viongozi waliojazwa na Roho ni muhimu kwenye injili. Muundo Fulani wa dola unaokuwepo ndani na nje kwa msaada, mara zote unaegamia juu ya aina za kisiasa za kitamaduni.

☐ **"Na wengine miongoni mwao"** A. T. Robertson, *Word Pictures in the New Testament*, uk. 224, ina hoja ya kufurahisha juu ya huu mstari, "haswa Tito (Gal. 2:1,3), Myunani na yumkini nduguye Luka ambaye hatajwi katika Matendo ya Mitume."hakika hii inawezekana, lakini inaegemea kwenye dhana mbali mbali. Lazima tuwe waangalifu kuwa kwa sababu ya andiko (likiwa na dhahanio) laweza kumaanisha au kudokeza kitu Fulani, haimaanishi kuwa linatenda! Lazima tutosheke na maandiko ya mwandishi wa mwanzo na sio dhana zetu zilizo pana.

☐ **"kwa mitume"** Muundo wa uongozi wa kanisa la Yerusalem haujakamilika. Kutokana na maandiko mbali mbali inaonekana kana kwamba Yakobo, nduguye Yesu, alikuwa kiongozi. Hili linaonekana kuwa kweli katika sura hii. Bado, palikuwepo na makundi mengine ya uongozi (kama vile Mdo. 15:4,22):

1. Wale tenashara
2. Viongozi wa mahali

Kile kisichojulikana ni jinsi Yakobo anavyohusiana na makundi haya. Amejulikana kama Mtume katika Gal. 1 :1 9. Pia inawezekana alikuwa kiongozi anayekubalika wa kundi la viongozi (kama vile Petro alijiita Mzee katika 1 Pet.

5:1; Yohana anajiita Mzee katika 2 Yohana 1 na 3 Yohana 1)

☉ **"Wazee"** Katika muktadha huu "wazee" wangelirejelea kwenye kikundi cha muda mrefu cha uongozi kilichofanywa kwa mfano wa Sinagoga. Angalia maelezo katika matendo 11:30 au 4:23

**15:3 "Kanisa"** Angalia Mada Maalum kwenye Matendo 5:1 1 .

☉ **"Wakapita kati ya nchi ya Foinike na Samaria"** Hii ni kauli ya kati elekezi isiotimilifu. Watu wa Foiniki walikuwa watu wa Mataifa, wakati Wasamaria walikuwa watu mchanganyiko Wayahudi na wa Mataifa. Haya maeneo huko nyuma tayari yalikuwa yameisha kuhubiliwa kwa injili (kama vile Mdo. 8:5na kuendelea; 1 1 :1 9).

☉ **"Wakitangaza habari za kuongoka kwao Mataifa"** Inaonekana kwamba Paulo na Barnaba waliitangaza kazi ya ajabu ya Mungu kwa "Mataifa" kwa kila kusanyiko walilokutana nalo. Kwa watu wenye maarifa wa Agano la Kale, kubadilika kwa "Mataifa" ilikuwa ni unabii uliotimia (yaani., Isa. 2:2-4; 42:6;49:6)! pia yawezekana kuwa kwa upana baada ya kutoa taarifa za kufanikisha juhudi za kazi kuwa kanisa huko Yerusalelem lisingaliweza kwa utulivu na usiri mkubwa kumaliza suala lenyewe (kama vile Mdo. 21 :1 8-20).

☉ **"Wakawafurahisha ndugu sana"** Haya yalikuwa ni maeneo ya watu wa Mataifa. Makanisa yangaliweza kuwa ni makanisa mchanganyiko. Mwitikio ni ukumbusho wa kinabii kwa kanisa la Yerusalelem. Wito wa kiulimwengu ulianzishwa na Wayunani, unathibitishwa na makanisa ya Kiyunani..

**15:4 "Kanisa na Mitume na Wazee"** Hapa makundi yote ya dola yanatajwa, kama ilivyo katika mstari 22.

☉ **"Wakawaeleza mambo yote Mungu aliyoyafanya pamoja nao"** Hili limekuja kuwa mfano!

**15:5 "lakini baadhi ya madhehebu ya Mafarisayo walioamini"** Imani (kauli timilifu tendaji endelevu) katika Yesu kama Masihi aliyeahidiwa ilikuwa msingi wa kanisa. Lakini humo kanisani palikuwepo na hoja mbali mbali kwa namna gani hii imani katika Kristo inahusiana na agano na ahadi ya Israel. Hiki kikundi cha uimbaji ("kikasimama" kinatangulizwa mbele katika Kiyunani kuonyesha msisitizo) cha Mafarisayo waliookolewa wakafikiri ya kuwa Agano la Kale lilikuwa limevuviwa kwa hiyo inapaswa kuliendelea (kama vile Mt. 5:1 7-1 9)! Mtu lazima amwamini Yesu na kumtii Musa (yaani., *dei*, ni muhimu [1 ] kutahiriwa; [2] kuwabadilisha; na [3] kuwatunza; Hizi zote tatu ni kauli zisizo na kikomo za wakati uliopo). Ni hili swali linaloleta swali la miundo ya kithiolojia ya Warumi 1-8 na Wagalatia! Angalia [MADA MAALUM: MAFARISAYO](#) katika Mdo.5:34.

☉ **"ni lazima"** Angalia maelezo kamili juu ya *dei* katika Mdo. 1 :1 6.

#### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): MATENDO 15:6-11

<sup>6</sup> Mitume na wazee wakakusanyika wapate kulifikiri neno hilo. <sup>7</sup> Na baada ya hoja nyingi Petro akasimama, akawaambia, Ndugu zangu, ninyi mnajua ya kuwa tangu siku za kwanza Mungu alichagua miongoni mwenu ya kwamba Mataifa walisikie neno la Injili kwa kinywa changu, na kuliadini. <sup>8</sup> Na Mungu, ajuaye mioyo ya watu, akawashuhudia, akiwapa Roho Mtakatifu vile vile kama alivyotupa sisi; <sup>9</sup> wala hakufanya tofauti kati yetu sisi na wao, akiwasafisha mioyo yao kwa imani. <sup>10</sup> Basi sasa mbona mnamjaribu Mungu na kuweka kongwa juu ya shingo za wanafunzi, ambalo baba zetu wala sisi hatukuweza kulichukua. <sup>11</sup> Bali twaamini kwamba tutaokoka kwa neema ya Bwana Yesu vile vile kama wao.

**15:6 "Mitume na Wazee wakakusanyika pamoja"** Hapa uongozi ulikutana kwa siri kwanza. Hii inaongelea juu ya mwongozo wa dola ya Presbiteria

**15:7 "Baada ya hoja nyingi"** Viongozi hawakufikia muafaka. Baadhi walikubaliana na maelezo katika Mdo. 15:5. Hawa walikuwa waamini waminifu. Lakini baadhi bado wanang'ang'ania kujulikana kwao wakati wakiwa wamepofushwa kwenye asili muhimu ya injili. Hata Mitume hawakuyaona madhara yake kamili (kama vile Mdo. 8:1 ). Tambua kipengere cha kufanya sera: (1 ) majadiliano binafsi; (2) majadiliano ya wazi; (3) yalipigiwa kura na kusanyiko

▣ **"Petro akasimama"** Hii ingaliweza kuwa ni njia ya kuweza kuongea kwenye kikundi kilichokuwa kimekusanyika (kama vile Mdo. 1 5:5). Hii ni mara yake ya mwisho kutajwa katika kitabu cha Matendo. Alikumbuka tena uzoefu wake akiwa na Kornelio (kama vile Mdo. 1 0-1 1 ).

▣ **"Mataifa walisikie neno la kinywa change, wapate kuliamini"** Mungu alimtumia Petro kuushuhudia upendo wake na ukubalifu wa mataifa! Mungu aliuruhusu huu uelewa muhimu kuendelea kwa hatua ya

1. Wasamalia wema kwanza, Matendo 8
2. Toashi wa Kikushi
3. Kornelio

Hawa hawakuwa wale waliokuwa wakiutenda upagani, lakini wote walihusishwa na dini ya Kiyahudi. Hata hivyo, 1 na 3 ilithibitishwa na uzoefu wa ile siku ya Pentekoste, ambao ndio ulikuwa ushahidi wa kanisa la mwanzo wa ukubalifu wa Mungu kwa kundi jingine.

**15:8 "Mungu ajuaye, mioyo ya watu"** Hii ilikuwa njia ya kuthibitisha maarifa kamili ya Mungu (kama vile 1 Sam.1 :24; 1 6:7; Zab. 26:2; 1 39:1 ; Mith. 21 :2; 24:1 2; Yer. 1 1 :20; 1 7:1 0; Luka 1 6:1 5; Rum. 8:27; Ufu. 2:23) ya imani ya hawa watu wa Mataifa walioongoka.

▣ **"akiwapa Roho Mtakatifu"** inavyoonekana hili linarejelea kwa aina ile ile ya uzoefu wa kiroho kama siku ile ya Pentekoste ("kama vile pia alivyotenda kwetu"). Uthihilisho wa aina ile ile wa Roho ulitokea katika Yerusalem, pia ulitokea huko Samaria, na Kaisaria. Ilikuwa ni ishara kwa waamini wa Kiyahudi wa ukubalifu wa Mungu kwa makundi mengine (kama vile 1 5:9; 1 1 :1 7).

**15:9 "Wala hakufanya tofauti kati yetu sisi na wao"** Hili lilikuwa ni suluhisho la kithiolojia ambalo Petro alifanya katika Mdo. 1 0:28,34; 1 1 :1 2. Mungu sio mheshimishaji wa watu (kama vile Gal. 3:28; Efe. 3:1 1 -4:1 3; Col. 3:1 1 ). Watu wote wameumbwa kwa sura yake (kama vile Mwa. 1 :26-27). Mungu anatamani watu wote wapate kuokolewa (kama vile Mwa.1 2:3; Kut. 1 9:5-6; 1 Tim. 2:4; 4:1 0; Tit 2:1 1 ; 2 Pet. 3:9)! Mungu anaupenda ulimwengu wote (kama vile Yn 3:1 6-1 7).

▣ **"Akiwasafisha mioyo yao kwa imani"** Neno hili linatumika katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani kumaanisha utakaso wa Walawi. Unamaanisha uondoaji wa kile kinachotutenganisha na Mungu. Hiki ni kile kitenzi kilichotumika katika uzoefu wa Petro juu ya wanyama waliosafi na wasiosafi katika Mdo. 1 0:1 5 na 1 1 :9 (kinachofuatisha tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani ya Mwa. 7:2,8; 8:20). katika injili ya Luka kilitumika kwa ajili ya kuwasafishwa wale wenye ukoma (kama vile Mdo. 4:27; 5:1 2,1 3; 7:22; 1 7:1 4,1 7). Ilikuwa kuwa sitiari yenye nguvu kwa ajili ya kusafishwa toka dhambini (kama vile Ebr. 9:22,23; 1 Yn 1 :7). Moyo ndiyo njia ya Agano la Kale la kumrejelea mtu. Angalia Mada maalum katika Matendo 1:24. Hawa watu wa mataifa walikuwa wamesafishika jumla na kukubaliwa na Mungu kupitia Yesu Kristo. Namna ya utakasa wao ulikuwa ni imani katika ujumbe wa injili. Waliamini, wakapokea, na kuaminiwa kamili katika nafsi na kazi ya Yesu (kama vile Rum 3:21 -5:1 1 ; Gal. 2:1 5-21 ).

**15:10 "Mbona mnamjaribu Mungu"** Mazingira ya agano la kale kuhusu maelezo haya uko katika kitabu cha Kutoka 1 7:2,7 na Kumb. 6:1 6. Hili ni neno la Kiyunani kwa ajili ya "kujaribu" (*peirazō*) lina kidokezo cha neno "kujaribu kwa mtazamo wa uharibifu."Huu ulikuwa mjadala mzito! Angalia Mada Maalum: Maneno ya Kiyunani kwa ajili ya neno "kujaribu" na vidokezo vyake katika Mdo. 5:9

▣ **"Kongwa"** Hili lilitumiwa na waalimu wa dini ya Kiyahudi kwa ajili ya uwasilishaji wa neno *Shema*, Kumb. 6:4-5; kwa hiyo, linasimama kwa ajili ya sheria, iliyoandikwa na kusimuliwa (kama vile Mt. 23:4; Luka 11:46; Gal. 5:1). Kwa sharti la Agano Jipya ndani yake

▣ **"Ambalo Baba zenu wala sisi hatukuweza kulichukua"** Hii inaaksi mafundisho ya Yesu (kama vile Luka 11:46). Somo hili linelezewa na Paulo katika Galatia 3. Lakini huyu ni Petro, ambaye ni kama Yakobo, alisia uzito uliopo kwa dini ya Kiyahudi (kama vile Gal. 2:11-21). Kifungu hiki kinakubaliana na ukweli wa thiolojia kuwa sheria haikuweza kuleta wokovu kwa sababu mwanadamu aliyeanguka asingeliweza kuitunza sheria takatifu (kama vile Warumi 7)! Wokovu usingaliweza na hauwezi kuegamia juu ya utendaji wa mwanadamu. Hata hivyo, aliokoa, alikirimia, na mwamini anahitaji kuishi maisha ya utakatifu (kama vile Mt. 11:30; Efe. 1:4; 2:10). Maisha ya utauwa (maisha ya kufanana na Kristo, yaani., 8:29; Gal.4:19; Efe. 4:13) mara zote ndio lengo la Ukristo, kwa ajili ya kusudi la kutoa fursa ya uinjilisti, na sio kiburi binafsi wala hukumu juu ya ushikaji sheria.

15:11 Muhtasari huu wa wokovu (yaani., "waliookolewa," kauli tendwa isio na ukomo ya wakati uliopita usiotimilifu) kwa neema kupitia imani (kwa ajili ya Petro. Matendo 2-3; kwa ajili ya Paulo kama vile Matendo 13:38-39; Warumi 3-8; Wagalatia3; Waefeso 1-2). Angalia namna ya wokovu ni ule ule kwa ajili ya Wayahudi na Watu wa mataifa (kama vile Rum. 3:21-31; 4; Efe. 2:1-10).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 15:12-21**

<sup>12</sup> Basi mkutano wote wakanyamaza, wakawasikiliza Barnaba na Paulo wakiwapasha habari za ishara na maajabu, ambayo Mungu aliyafanya kwa ujumbe wao katika Mataifa. <sup>13</sup> Na hao walipokwisha kunyamaza Yakobo akajibu, akisema, Ndugu zangu, nisikilizeni. <sup>14</sup> Simeoni ametueleza jinsi Mungu hapo kwanza alivyowaangalia Mataifa ili achague watu katika hao kwa ajili ya jina lake. <sup>15</sup> Na maneno ya manabii yapatana na hayo, kama ilivyoandikwa, <sup>16</sup> Baada ya mambo haya nitarejea, Nami nitajenga tena nyumba ya Daudi iliyoanguka. Nitajenga tena maanguko yake, Nami nitaisimamisha; <sup>17</sup> Ili wanadamu waliosalia wamtafute Bwana, Na mataifa yote ambao jina langu limetajwa kwao; <sup>18</sup> Asema Bwana, ajulishaye hayo tangu milele. <sup>19</sup> Kwa sababu hiyo mimi naamua hivi; Tusiwataabishe wale waliomgeukia Mungu katika Mataifa; <sup>20</sup> bali tuwaandikie kwamba wajiepushe na unajisi wa sanamu, na uasherati, na nyama zilizosongolewa, na damu. <sup>21</sup> Kwa maana tangu zamani za kale Musa anao watu wahubirio mambo yake; katika kila mji husomwa kila sabato katika masinagogi.

**15:12 "Basi mkutano wote wakanyamaza, wakawasikiliza"** Maneno ya Petro yaliweza kuunyamazisha mkutano. Kutokana na muktadha huu inaonekana kuwa kwa hoja hii wamisionari wawili waliandaa safari ya umisheni kwa mara ya pili. Kipindi hiki viongozi waliwasikiliza! *The Jerome Biblical Commentary* (juzuu ya. 2, uk.1 95) inaamini ulikuwa mkutano mwingine tofauti toka kwenye baraza la kanisa Mdo.1 5:6-11. Nafikiri ni mkutano ule ule.

▣ **"Barnaba and Paulo"** Tambua kuwa majina yamejirudia kwa sababu hili lilikuwa kanisa la nyumbani kwake Barnaba.

▣ **"Wakiwapasha habari za ishara na maajabu"** Kusudi la kithiolojia la unenaji wa lugha mpya siku ya Pentekoste katika Matendo ni ishara ya ukubarifu wa Mungu, kwa hiyo mtu anaweza shangaa ikiwa ishara hii haswa ilikuwa ikijirudia mara kwa mara kama njia ya uthibitisho. Ishara zenyewe zilitendwa na Yesu (Matendo 2:22), Mitume (kama vile Mdo. 2:43; 3:7; 4:1 6,30;5:1 2), wale saba (kama vile Mdo. 6:8; 8:6,1 3), nao Paulo na Barnaba (kama vile Mdo.1 4:3; 1 5:1 2). Mungu alikuwa anathibitisha uwepo wake na nguvu kupitia injili kwa ishara na maajabu. Huu ulikuwa ni ushuhuda zaidi kwa kikundi kile cha wafuasi wa dini ya Kiyahudi kuwa Mungu huwakubali wapagani kikamilifu kwa msingi wa neema pekee, kupitia imani.

**15:13 "Yakobo"** Huyu siyo Mtume Yakobo kwa sababu alikuwa amekwisha uwawa katika Matendo 12:1-2. Huyu alikuwa nduguye Yesu ambaye alikuja kuwa kiongozi wa kanisa la Yerusalem na mwandishi wa kitabu cha Yakobo

katika Agano Jipya. Alijulikana kama “Yakobo mwenye haki.” Wakati mwingine alijulikana kama “magoti ya ngamia” kwa sababu ya tabia yake ya kuomba kila mara, akipiga magoti. Viongozi wakuu wa Yerusaleem walipiga kelele juu ya jambo hili (Petro na Yakobo). Angalia Mada Maalum katika Matendo 12:17.

**15:14 "Simeoni"** Huyu ni namna ya yule Simeoni wa kabila la Kiarama, ambaye ni Petro (kama vile 2 Pet. 1 :1 ).

▣ **"ili achague watu katika hao kwa ajili ya jina lake"** Huu ni msisitizo kwa wote manabii wa agano la kale (mfano Isa. 2:2-4; 42:6; 45:20-23; 49:6; 52:1 0). Watu wa Mungu mara zote waliwajumuisha wote Wayahudi na watu wa Mataifa (kama vile Mwa. 3:1 5; 1 2:3; Kut. 9:1 6; Efe. 2:1 1 -3:1 3). Kifungu "kwa ajili ya jina lake" chaweza kuwa ni dokezo la Yer.13:1 1 na 32:20 au Isa. 63:1 2,1 4.

**15:15-18 "Imeandikwa"** Hii ni nukuu huru toka katika Amos 9:1 1 -1 2 katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani. Neno "mwanadamu" katika mstari wa 17 ni *Edom* (Taifa) kwa andiko la ki-Masoretic, lakini tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani yana neno *anthropos* (mwanadamu). Yakobo ananukuu tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani kwa sababu kwa namna hii kipekee linaendana na kusudi lake la kuilezea asili ya ahadi ya Mungu ya ukombozi. Tambua matendo yaliyoahidiwa ni ya YHWH. Hili linafanana na la Ezek. 36:22-38. Hii ilikuwa nukuu toka kwenye tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani (LXX), ambalo dhahili linatofautiana na maandiko ya ki-Masoteti (MT), linaonyesha kuwa suala lenyewe la imani sio andiko kamili, bali ni Mungu kamili na mipango yake kwa mwanadamu. Hakuna kati yetu kama ilivyo utofauti wa kimaandiko wa Agano la Kale au Agano Jipya, lakini hauathiri imani ya waamini katika uaminifu wa maandiko. Mungu kwa uaminifu mkubwa amejidhihilisha mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka! Maandishi ya kale yaliyo nukuliwa kwa mkono hayawezi kutumika kama sababu ya kukataa ufunuo huu. Angalia Manfred Brauch, *Abusing Scripture*, sura ya 1 , "asili ya andiko," kur. 23-32.

**15:16** Ni dhahili toka kwenye muktadha kuwa Yakobo amechagua na kubadilisha nukuu hii toka kwenye tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani ili kudai ijumuishaji wa mataifa. Je pia alichagua andiko hili kwa sababu inatetea uharibifu wa dini ya agano la kale la Musa? Agano jipya ni tofauti kabisa

1. Ni kwa neema, wala sio kwa utendaji (zawadi sio faida)
2. Mtazamo wa ki-Masihi, sio wa kihekalu (Yesu ni hekalu jipya)
3. Katika mtazamo wa kiulimwengu, na sio kwa mwelekeo wa jamii ya Kiyahudi

Mabadiliko haya ni ya kushangaza kwenye “sherehe ya tohara” kwa waamini. Sasa Mtume Mkuu (Petro), Mtume mwalimu wa dini ya Kiyahudi aliyeongoka (Paulo), na kiongozi wa kanisa la Yerusaleem (Yakobo) wote waliwapinga kama mwafaka wa kanisa mama na makanisa ya kimisionari!

**15:17** Ni ajabu kiasi gani juu ya maelezo kwa watu wote. Lakini pia kumbuka kifungu cha neno “uchaguzi” kwa ajili ya watu wa mataifa wote walioitwa kwa jina langu” (kama vile Dan. 9:1 9). Inaonyesha uzoefu wa kiibada wa namna Fulani (kama vile LXX ya Kumb. 28:1 0; pia soma Isa. 63:1 9; Yer. 1 4:9).

**15:18** Ujumuishaji wa watu wa mataifa siku zote umekuwa ni mpango wa Mungu (kama vile Gal. 3:26-29; Efe. 3:3-6, angalia Mada Maalum katika Mdo. 1:8). Njia ya wokovu itakuja toka katika uzao wa Daudi (kama vile Mdo. 1 5:1 6; 2 Nya.6:33).

**15:19** Huu ni uhitimishaji wa Yakobo.

**15:20** Miongozo aina hii ilimaanisha (1 )uhakika wa ushirika wa pamoja katika makanisa mchanganyiko na (2) kuongeza uwezekano wa kuwahubiri Wayahudi wa mahali. Mambo haya hayana kitu chochote zaidi ya wokovu binafsi wa watu wa mataifa. Miongozo hii ilielekezwa kote ikiwezekana kwa Wayahudi na zaidi kwa ibada za kipagani (kama vile Mdo.1 5:29; 21 :25). Sheria za Kilawi zilitolewa ili kuleta utofauti (jamii na dini) kati ya Wayahudi na Wakaanani. Kusudi lao kuu lilikuwa kutokujumuika pamoja, lakini hapa kusudio ni kinyume. Huu “umuhimu” ni kusaidia kuendeleza ushirika kati ya waamini na tamaduni! Pana tofauti nyingi za machapisho ya Kiyunani yanayohusiana na tamko hili la kitume. Baadhi yana vipengere viwili, vipenger vitatu, au vipengere vinne.

Kwa majadiliano kamili ya uchaguzi, angalia Bruce M. Metzger's *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, kur. za 429-434). Wengi wa watafasiri wa Kiingereza wana orodha nne zilizopo pamoja.

**NASB, NRSV,**

**REB** "na uasherati"

**NKJV, REV,**

**NET** "na zinaa"

**NJB** "toka ndoa zisizokubalika"

Ni ngumu kujua kwa uhakika ikiwa katazo hili lilielekezwa moja kwa moja kwa

1. Taratibu za ibada za kipagani zisizo na maadili (yaani., zinaa)
2. Umakini wa Kiyahudi kuhusu kujamiiana kwa ndugu wa jamaa moja (kama vile Walawi 1 8; angalia F. F. Bruce, *Answers to Questions*, uk. 43; NJB)

▣ **"Nyama zilizosongolewa na damu"** Baadhi ya watoa maoni wanalihusianisha hili na yale yote yaliyohusiana na sheria ya Musa kuhusu nyama zilizosongolewa (kama vile Law. 1 7:8-1 6). Hata hivyo, yawezekana kuwa neno "na damu" inarejelea kwenye mauaji, ambalo pia ni suala muhimu katika maandiko ya Musa

**15:21** Mstari huu unamaanisha

1. Kuwahakikishia wale washika sheria kuwa vitabu vitano vya Musa (torati) ilikuwa ni ngumu kwa wamataifa kwa kila namna au
2. Kwa vile palikuwepo na Wayahudi katika kila eneo, hofu yao lazima iheshimiwe ili kwamba waweze kuhubiliwa kwa urahisi ((kama vile 2 Kor. 3:1 4-1 5)
- 3.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO 15:22-29**

<sup>22</sup> Basi ikawapendeza mitume na wazee na kanisa lote kuwachagua watu miongoni mwao na kuwapeleka Antiokia pamoja na Paulo na Barnaba; nao ni hawa, Yuda aliyelitwa Barsaba, na Sila, waliokuwa watu wakuu katika ndugu. Wakaandika hivi na kupeleka kwa mikono yao, <sup>23</sup> Mitume na ndugu wazee, kwa ndugu zetu walioko Antiokia na Shamu na Kilikia, walio wa Mataifa; Salamu. <sup>24</sup> Kwa kuwa tumesikia ya kwamba watu waliotoka kwetu wamewasumbua kwa maneno yao, wakipotosha roho zenu, ambao sisi hatukuwaagiza; <sup>25</sup> sisi tumeona vema, hali tumepatana kwa moyo mmoja, kuwachagua watu na kuwapeleka kwenu pamoja na wapendwa wetu Barnaba na Paulo, <sup>26</sup> watu waliohatirisha maisha yao kwa ajili ya jina la Bwana wetu Yesu Kristo. <sup>27</sup> Basi tumewatuma Yuda na Sila, watakaowaambia wenyewe maneno yayo kwa vinywa vyao. <sup>28</sup> Kwa maana ilimpendeza Roho Mtakatifu na sisi, tusiwatwike mzigo ila hayo yaliyo lazima, <sup>29</sup> yaani, mjiepushe na vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na damu, na nyama zilizosongolewa, na uasherati. Mkijizua na hayo, mtafanya vema. Wasalamu.

**15:22** Ukaimishaji ulikuwa ni kwa kusudi la umoja (kama vile Mdo. 1 5:23), sio kulazimisha maafikiano.

▣ **"Yudas aliyelitwa Barsaba"** Huyu kiongozi mwaminifu, kama ilivyo wengi katika Agano Jipya, hawajulikani kwetu. Hapana chochote katika Agano Jipya kinacho zungumzia kuhusu yeye. Lakini Mungu anamtambua vizuri! Yawezekana kuwa mtu huyu alikuwa ni ndugu wa Yusufu Barsaba, ambaye alikuwa ni mmoja wa wanafunzi walio chukua nafasi ya Yuda Iskarioti katika Mado.1:23. Kama ndivyo, basi walikuwa watoto wa mtu aliyelitwa Barsaba.

▣ **"Sila"** Yeye, kama alivyo Barsaba, alikuwa ni kiongozi katika kanisa la Yerusalemi. Aliitwa na Paulo Silvanus na atachukua nafasi ya Barsaba kama ambavyo Paulo alivyomhusisha kwenye safari ya mara ya pili ya umisiaonari. Paulo angeliweza kumchagua yeye ili kwamba ikiwa mtu atamhukumu yeye juu ya (1) kuifundisha injili tofauti na wale tenashara au (2) kutokushirikiana na kanisa mama, Sila aweze kujibu malalamiko yao.



## MADA MAALUM: SILA/SILVANUS

Sila, au Silvanus, ni mtu ambaye Paulo alimchagua kwenda nae katika safari yake ya pili ya umisiaonari (yaani., Mdo. 15:40-18:5) baada ya Barnaba na Yohana kurudi Kipro (yaani., baada ya kubishana na Marko, kama vile Mdo. 15:36-39).

- A. ni wa kwanza kutajwa katika Biblia kwenye Mdo.15:22 ambapo anaitwa kiongozi kati ya wapendwa walioko katika kanisa la huko Yerusalem.
- B. Pia yeye alikuwa nabii (kama vile Mdo. 15:32).
- C. Alikuwa raia wa Kirumi kama alivyokuwa Paulo (kama vile Mdo. 16:37).
- D. Yeye na Yuda Barsaba walipelekwa Antiokia na kanisa la Yerusalem kwa ajili ya kuchunguza eneo (kama vile Mdo. 15:22,30-35).
- E. Paulo anamtaja yeye katika 2 Cor. 1:19 kama mfuasi wa kuihubiri injili.
- F. Baadaye anatambuliwa na Petro katika maandiko 1 Petro. (kama vile 1 Pet. 5:12; huenda ndo maana Petro anasikika sana kama Paulo).
- G. Wote Paulo na Petro wanamwita Silvanus, wakati Luka anamwita Sila (muundo wa Sauli wa lugha ya Kiaramu). Yawezekana Sila lilikuwa jina lake la Kiyahudi na Silvanus lilikuwa la Kilatini (kama vile F. F. Bruce, Paul: Apostle of the Heart Set Free, uk. 213).

**15:23** Barua toka kwenye baraza la Yerusalem ilielekezwa tu kwa makanisa fulani, inavyoonekana ni kwa yale yaliyokuwa na waumini wengi wa Kiyahudi. Kwa kuorodhesha maeneo fulani, Yakobo alionyesha kuwa haikumaanisha kama sheria kwa makanisa yote ya watu wa Mataifa. Barua ilikuwa tu kwa ajili ya ushirika na uinjilisti na sio kwa ajili ya miongozo ya maadili au wokovu!

Je kama mwamini wa sasa unaweza moja kwa moja kuepukana na nyama zilizosongolewa?(zenye kutimiza utaratibu wa Kiyahudi) Angalia

1. Manfred Brauch, *Abusing Scripture*, chapter 7, "The Abuse of Context: Historical Situation na Cultural Reality," kur. za 202-249
2. Gordon Fee, *Gospel and Spirit*
3. *Hard Sayings of the Bible*, "How Kosher Should Christians Live?", pp. 527-530 and "To Eat or Not to Eat," kur.za 576-578

Hivi vyote ni vifungu vyenye kuweza kusaidia. Inaleta faraja kusoma Wakristo wengine wenye taarifa, waaminifu na wanaoiamini biblia wanaoshughulika na mambo haya. Maandiko yao yanawapa waamini wengine uhuru wa kufikiri na kuishi unaosimamia juu ya nuru walio nayo. Umoja, na sio ufanano, ndio ufunguo wa ustawi, ukuaji wa makanisa yenye kulishika agizo kuu.

▣ "**Kilikia**" Hapa palikuwa ni eneo la kwao Paulo (kama vile Mdo. 22:3).

**15:24** Kifungu hiki kinaonyesha kuwa kanisa la Yerusalem lilikuja kupata taarifa kuwa baadhi ya washirika wake, wale wasio na mamlaka au msimamo rasmi (kama vile Mdo. 1 5:1 ), walikuwa (1 ) wakisafiri kwa haya makanisa ya umisionari na (2) walihitaji wakubaliane kuhusu sheria ya Musa (kama vile Mdo. 1 5:1 ). Kitenzi (*anaskeuazō*) kilichotumika ni neno la kijeshi lenye mkazo lililotumika hapa tu katika Agano Jipya kwa ajili ya kuuteka mji.

**15:25**

**NASB**"hali tumepata kwa moyo mmoja"

**NKJV**"tukikusanyika kwa shauri moja"

**NRSV,NJB**"tukiamua kwa pamoja"

**TEV**"tukikutana pamoja na kuamua mamoja"

Huu umoja kati ya waumini ulikuwa ni tabia ya uwepo wa Roho Mtakatifu (kama vile Mdo. 1 5:28). Tambua hili halimaanishi kuwa hapakuwepo na majadiliano au mabishano, lakini hayo yalikuwepo baada ya kuliweka wazi suala ili waumini wapate kuwa kitu kimoja. Haya makubaliano ya kithiolojia ya pamoja yalihatiji kuenezwa ng'ambo ili pasiwepe mivutano na mabishano tena na tena. Kanisa la Yerusalem sasa limekwisha chukua msimamo rasmi juu ya dhima ya injili na madhara yake kwa watu wa mataifa!

**15:26** Paulo na Barnaba hawakugawana tu ushindi, bali pia ugumu wa kazi ya umisheni. Huu uwazi haukuwa tu wa kupita au wa muda, bali kulikuwa ni kujitoa kwa kudumu (kauli timilifu tendaji ya hali ya kuendelea).

**15:28 "Roho Mtakatifu na sisi"** Mungu alikuwepo kwenye mkutano huu muhimu. Aliweza kuonyesha mapenzi yake katika ,mazungumzo haya! Roho Mtakatifu ndiye huleta umoja. Hapa mitizamo yote ya agano la kibiblia limetizama—kazi ya Mungu na wajibu ufaao wa mwanadamu. Tambua yalikuwa ni malidhiano; kila upande walipata kitu. Injili ya neema tu, imani tu iliweza kuthibitishwa, lakini hekima ya Kiyahudi iliheshimika. Angalia [MADA MAALUM: NAFSI YA ROHO](#) katika Mdo. 1 :2.

▣ **"tusiwatwike mizigo"** Hili halirejelei kwenye wokovu wa mtu binafsi, bali ushirika kati ya mwamini wa Kiyahudi na mwamini wa mataifa katika makanisa ya mahali.

**15:29** Hili lililenga mgawanyiko kamili uliokuwepo kati yao na ibada ya sanamu katika kipindi kilichopita. Uhuru wa Mkristo na uwajibikaji ni mgumu kuulinganisha, lakini lazima (kama vile Rum. 1 4:1 -5:1 3; 1 Kor. 8:1 -1 3; 1 O:23-28). Hizi ibada za kipagani za kipindi cha nyuma zilihusisha mambo haya matatu yaliyojumuishwa! Haya "mambo ya msingi" yameorodheshwa katika njia mbali mbali katika maandiko tofauti ya Kiyunani. swali lenyewe ni kuwa

1. Vitu vilivyotolewa kwenye ibada ya sanamu vingalirejelea nyama
2. Damu ingelirejelea au kwa
  - a. Nyama zisizosongolewa
  - b. Mauaji ya kimakusudi
3. Vitu vilivyosongolewa lazima virejeele kwenye namna ya utaraibu usio wa Kiyahudi wa kuwaua wanyama, ukidokeza kuwa zile njia mbili za nyuma pia zilihusiana na mambo ya msingi ya Wayahudi kuhusu chakula (yaani., Walawi 11)
4. Uasherati ungelirejelea kwenye
  - a. Ushirikishaji wa ibada za kipagani (vile vile na mambo ya chakula)
  - b. Sheria za ki-Lawi za agano la kale dhidi ya kujamiiiana kwa marihamu (kama vile Law. 1 7:1 0-1 4, angalia F. F. Bruce, *Answers to Questions*, uk.43)

Haya yote "mambo ya msingi" hayakuhusiana na wokovu, bali kushirikishana ndani ya makanisa yaliyochangamana na kupanua wigo kwa ajili ya kuwahubiri Wayahudi. Angalia F. F. Bruce, *Answers to Questions*, kur. za 80-81 .

## **MADA MAALUM: UHURU WA MKRISTO DHIDI YA WAJIBU WA MKRISTO**

- A. Warumi 14:1-15:13 inajaribu kuleta mlinganyo wa kutoeleweka kwa uhuru wa Mkristo na uajibikaji wake. Sehemu ya fasihi inaendelea toka Rum. 14:1-15:13.
- B. Tatizo linalowahisha kifungu hiki yumkini lilikuwa ni mvutano kati ya waamini wa Mataifa na Wayahudi katika kanisa la Rumi. Kabla ya kuongoka Wayahudi walijaribu kuwa washika sheria sana na wapagani wakawa wasio waadilifu. Kumbuka, hili lilihubiriwa kwa wafuasi waaminifu wa Yesu. kifungu hiki hakiwaelezei waamini wa mwilini. Mwenendo mkuu unatambuliwa na makundi yote. Mazungumzo haya sio leseni ya kutafutia makosa ya ushikaji wa sheria au kuonyesha wema.
- C. waamini wanapaswa kuwa makini sio kufanya thiolojia zao au maadili kuwa kipimo cha waamini wengine (kama vile 2 Kor. 10:12). Waamini wanapaswa kutembea katika nuru walio nayo lakini waelewe kuwa thiolojia yao sio thiolojia ya moja kwa moja ya Mungu. Waamini bado wanaathiriwa na

dhambi. Tunalazimika kuwatia moyo, kuwainua, na kufundishana kati ya mtu na mtu maandiko, sababu, na uzoefu, lakini siku zote katika upendo. Kwa jinsi mmoja anavyojua zaidi ndivyo mwingine asivyojua (kama vile 1 Kor. 13:12)!

- D. tabia na mwenendo wa mtu mbele za Mungu ndio kigezo cha kupima matendo ya Mkristo. Wakristo watasimama mbele ya Kristo kwa ajili ya kuhukumiwa na namna walivyo watendea wenzao (kama vile Mdo. 15:10,12 na 2 Kor. 5:10).
- E. Martin Luther alisema, "Mkristo ni Bwana wa wote wa walio huru, asiyewajibika kwa yeyote; Mkristo ni mtumishi mtenda kazi wa wote, anayewajibika kwa wote." Ukweli wa kibiblia mara nyingi unaletwa na mvutano wa kutokuelewana katika kauli (angalia Mada Maalum: Mkanganyiko katika maandiko).
- F. Somo hili lililo muhimu lakini gumu linashughulika na sehemu nzima ya fasihi ya Warumi 14:1-15:13 na pia katika 1 Wakorinto 8-10 na Wakolosai 2:8-23.
- G. Hata hivyo, inahitajika kuelezewa kuwa uwingi kati ya waamini waminifu sio kitu kibaya. Kila mwamini anao udhaifu na nguvu. Kila mmoja inampasa kutembea katika nuru aliyo nayo, akiwa wazi kwa Roho na Biblia. katika kipindi hiki cha kuona kupitia kioo kilichotiwa giza ( 1 Kor. 13:8-13) mtu anapaswa kutembea katika upendo (Mdo. 15:15), na katika amani (Mdo. 15:17,19) kwa ajili uimalishaji wa kidugu. Tofauti zetu kama waamini ni lango la Mungu lililo wazi kwa ajili ya wasio amini wengine kupata msamaha na urejesho katika Kristo. Wingi wa Kikristo, ndani ya mipaka ya kibiblia, ni kitu kizuri kwa ajili ya uinjilisti!
- H. Utambulisho wa "mwenye nguvu" na "aliye dhaifu" ambao Paulo anayapa haya makundi yanaleta ubaguzi kwetu. Hakika hili halikuwa kusudi la Paulo. Makundi yote yalikuwa yenye waamini walio waaminifu. Tusitake kujaribu kuwatengeneza wakristo wengine ndani yetu! Tunakaribishana kati yetu katika Kristo!
- I. Hoja zote zingalielezewa kama
  1. kukalibishana kati yetu kwa vile Mungu alitukaribisha nasi katika Kristo (Mdo. 15:14:1,3; 15:7)
  2. Tusihukumiane sisi kwa sisi kwa vile Kristo ndiye Bwana wetu na mwamuzi (kama vile Mdo. 14:3-12)
  3. upendo ni kitu cha muhimu kuliko uhuru binafsi (kama vile Mdo. 14:13-23)
  4. Ufuatisheni mfano wa Kristo na kuweka chini haki zenu kwa ajili ya kuwaimarisha wengine (kama vile Mdo. 15:1-13)

▣ **"ikiwa"** Kisarufi hii sio sentensi yenye masharti. Toleo la NJB "limeyaepuka haya, na kufanya kile kilicho haki."

▣ **"Wasalaam"** Hii ni kauli timilifu tendwa shurutishi ambayo ilitumika kuhitimisha ilipowatakia nguvu na afya.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): MATENDO 15:30-35**

<sup>30</sup> Hata hao wakiisha kupewa ruhusa wakatelemkia Antiokia; na baada ya kuwakusanya jamii yote wakawapa ile barua. <sup>31</sup> Nao walipokwisha kuisoma wakafurahi kwa ajili ya faraja ile. <sup>32</sup> Tena Yuda na Sila, kwa kuwa wao wenyewe ni manabii, wakawausia ndugu kwa maneno mengi, wakawathibitisha. <sup>33</sup> Na wakiisha kukaa huko muda, wakaruhusiwa na ndugu waende kwa amani kwa hao waliowatuma. [ <sup>34</sup> Lakini Sila akaona vema kukaa huko.] <sup>35</sup> Na Paulo na Barnaba wakakaa huko Antiokia, wakifundisha na kulihubiri neno la Bwana, pamoja na watu wengine wengi.

**15:30** Hili tena ni kusanyiko la pamoja. Linaonyesha umuhimu wa kusanyiko la kanisa la mahala.

**15:31** Hili ni kusanyiko la pili (yaani., kanisa la mataifa huko Antiokia) halikuweza kuyaona haya mambo ya msingi kama yenye makatazo au yaliyo kinyume.

**15:32** Huu mstari unaelezea nguvu ya unabii wa Agano Jipya. Kimsingi ni mafundisho ya injili na matumizi yake; nani ajuaye, huenda ni ushahidi wa Agano Jipya kwa ajili ya mahubiri ya muda mrefu! Angalia Mada Maalum: Unabii wa Agano Jipya katika Mdo. 11:27

**15:33 "katika amani"** Tafasiri ya toleo hili la NASB ni gumu kueleweka. Angalia NKJV na NRSV kwa njia rahisi ya kuufasiri mstari huu. Hili laweza kuaksi namna ya kutakiana amani kwa Kiebrania, *Shalom* (yaani., "amani", BDB 1 022). Hii ni njia nyingine ya kuonyesha ukubarifu wa moja kwa moja wa kanisa la Yerusalemu na viongozi wake.

**15:34** Mstari huu haukujumuishwa kwenye machapisho ya Kiyunani ya P74, x, A, B, E, wala tafasiri ya Kilatini ya Vulgate. Pia umeondolewa katika matoleo ya NRSV, TEV, NJB, na NIV. Uko katika muundo wa kurekebisha katika maandiko ya Kiyunani ya herufi kubwa (yaani., C na D). yumkini sio sehemu ile ya asili ya kitabu cha Matendo. Toleo la UBS<sup>4</sup> linapima kutojumuishwa kwake kwa alama (A)

**15:35** Huu mstari unaonyesha ni wahubiri wengine wangapi wa karne ya kwanza na walimu tunaowaita wa kisasa wasivyojua kitu kuuhusu mstari huu. Agano Jipya ni la kiuchaguzi sana katika ushahidi wake kuhusu maisha ya Mitume wengine na Wamisioanri na wahubiri. Mungu anajua! Matendo ya Mitume hakifurahishwa na wasifu wa watu.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 15:36-41**

<sup>36</sup> Baada ya siku kadha wa kadha Paulo akamwambia Barnaba, Haya! Mrejee sasa tukawaangalie hao ndugu katika kila mji tulipolihubiri neno la Bwana, wa hali gani. <sup>37</sup> Barnaba akaazimu kumchukua Yohana aliyetwa Marko pamoja nao. <sup>38</sup> Bali Paulo hakuona vema kumchukua huyo aliyewaacha huko Pamfilia, asiende nao kazini. <sup>39</sup> Basi palitokea mashindano baina yao hata wakatengana. Barnaba akamchukua Marko akatweka kwenda Kipro. <sup>40</sup> Lakini Paulo akamchagua Sila, akaondoka, akiombewa na wale ndugu apewe neema ya Bwana. <sup>41</sup> Akapita katika Shamu na Kilikia akiyathibitisha makanisa.

**15:36 "Haya! mrejee"** Lilikuwa ni kusudi la Paulo na Barnaba kurudi na kuyaimalisha makanisa ambayo waliyaanzisha wakati wa safari yao ya kwanza. Tambua hapakuwepo na udhahiri wa ki-Mungu kuhusu safari hii kama ilivyokuwa ya kwanza (kama vile Mdo. 1 3:2).

**15:38 "Paulo hakuona vema kumchukua"** Hii ni kauli isio timilifu tendaji elekezi. Inavyoonekana Paulo aliendelea kuelezea kusita kwake.

\

▣ **"huyo aliyewaacha huko"** Haswa sababu ni kwa nini Yohana aitwaye Marko aliondoka kwenye ile safari ya kwanza haijulikani (kama vile Mdo. 1 3:1 3).

**15:39 "Palitokea mashindano kati yao hata wakatengana"** Maana halisi ya neno hili "maneno makali," ikimaanisha "kuwa na makali kama kiwembe." linatumika katika maana chanya katika Ebra 10:24. Kitenzi pia kimetumika katika Mdo., 17:6 na 1 Kor. 13:5. Kwa kweli palikuwepo na mashindano!

▣ **"Barnaba akamchukua Marko wakatweka kwenda Kipro"** Sasa palikuwepo na timu mbili za umisheni.

**15:40 "Paulo akamchagua Sila"** Paulo alichagua kiongozi mwingine kutoka katika kanisa la Yerusalemu.

▣ **"akiombewa na wale ndugu apewe neema ya Bwana"** Hili lingaliweza kuhusisha aina ya huduma ya maombi ya kujitoa (kama vile Mdo. 6:6; 1 3:3 1 4:26; 20:32). Hili lilimaanisha kanisa zima, na sio kikundi fulani.

**15:41 "Kilikia"** kwa nini na namna gani makanisa yalianzishwa haijulikani. Yumkini Paulo mwenyewe aliyaanzisha kipindi cha utulivu wake huko Tarso. Kilikia palikuwa nyumbani kwao Paulo.

▣ **"Makanisa"** Angalia Mada Maalum katika Mdo.5:1 1 .

## **MASWALI YA MJADALA**

Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. kwa nini sura hii ni ya muhimu?
2. Ni akina nani wafuasi wa dini ya Kiyahudi walio Wakristo?
3. Kwa nini maoni ya Yakobo yalipewa umuhimu mkubwa?
4. Ni akina nani wazee?
5. Je maonyo ya mistari ya 28-29 yanarejelea kwenye wokovu au ushirika?

## MATENDO YA MITUME 16

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFASIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS4</b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Timotheo anafuatana Na Paulo na Sila	Timotheo anaungana na Paulo na Sila	Timotheo anaungana na Paulo	Timotheo anaambatana na Paulo na Sila	Likonia: Paulo anamfunza Timotheo 15:41-16:3
16:1-5	16:1-5	16:1-5	16:1-5	16:4
Maono ya Paulo juu Ya mtu wa Makedonia	Wito wa Makedonia	Kupia Asia Ndogo mpaka Troa	Huko Troa: Paulo anaona maono	16:5 Safari ya kupitia Asia Ndogo
16:6-10	16:6-10	16:6-10	16:6-10	16:6-8
Kuongoka kwa Lidia	Lidia anabatizwa Huko Filipi	Paulo na Sila huko Filipi	Huko Filipi: Lidia anaongoka	16:9-10 Kuingia huko Filipi
16:11-15	16:11-15	16:11-15	16:11-15	16:11-15
Awekwa gerezani Huko Filipi	Paulo na Sila wawekwa gerezani		Wakiwa gerezani huko Filipi	Kufungwa kwa Paulo na Sila
16:16-24	16:16-24	16:16-18  16:19-24	16:16-22a  16:22b-24	16:16-18  16:19-24
16:25-34	16:25-34	16:25-34	16:25-28  16:29-30 16:31-34	16:25-28  16:29-34
16:35-40	16:35-40	16:35-40	16:35  16:36 16:37 16:38-40	16:35-37  16:38-40

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("[A Guide to Good Bible Reading](#)")

### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA NDANI YA MATENDO 15:36-16:40**

#### **I. SAFARI YA PILI YA KIMISIONARI (Matendo 1 5:36-1 8:23)**

- A. safari hii ya kimisionari ilichukua muda mrefu kuliko ile safari ya kwanza, yumkini iliwachukua miaka 3-4.
- B. kimsingi safari hii iliingalia miji ya Makedonia na Akaiia, amabayo ni Ugiriki ya sasa.
- C. maelezo fasaha
  1. Barnaba and Paulo wanagawanyika, Mdo. 1 5:36-40 (wakagombana juu ya Yohana aitwaye Marko)
  2. Shamu na Kilikia, Matendo 1 5:41 (lini na namna gani makanisa haya yalianza haijulikani.)
  3. Lisitra and Derbe, Matendo 1 6:1 -5 (Timotheo anaungana na timu)
  4. Troa, Mdo.1 6:6-1 0 (Paulo anapokea maono ya kurudi Magharibi.)
  5. filipi, Acts 1 6:1 1 -40
  6. Thessalonike, Mdo. 1 7:1 -9
  7. Berea, Mdo. 1 7:1 0-1 4
  8. Athens, Mdo. 1 7:1 5-34
  9. Korinto, Mdo. 1 8:1 -1 7
  10. Akarudi Antiokia huko Shamu, Mdo. 1 8:1 8-22

### **WATENDA KAZI WENZA WA PAULO**

- A. Yohana aitwaye Marko (Yohana ni jina la Kiyahudi. Marko ni jina la Kirumi, Mdo. 1 2:25.)
  1. Alikulia Yerusalemu. Nyumba ya mama yake imetajwa katika Mdo. 1 2:1 2 kama sehemu ambayo kanisa la Yerusalemu lilikutana kwa maombi.
  2. Wengi wamedai kuwa nyumba hii ilikuwa ni mahali palipo fanyika karamu ya Bwana na kuwa yule mtu aliyekimbia uchi katika Marko 14:51-52 alikuwa Yohana aitwaye Marko. Yote kati ya haya yanawezekana, lakini ni mtizamo tu.
  3. Alikuwa umbu lake Barnaba (kama vile Kol. 4:1 0).
  4. Alikuwa rafiki wa Barnaba na Paulo (kama vile Mdo. 1 3:5).
  5. Aliiacha timu mapema na kurudi Yerusalemu (kama vile Mdo. 1 3:1 3).
  6. Barnaba alitaka kumchukua kwenye safari yake ya pili, lakini Paulo akakataa (kama vile Mdo. 1 5:36-41 ).
  7. Baadaye Paulo na Yohana aitwaye Marko inavyoonekana walipatana (kama vile 2 Tim. 4:1 1 ; Filemon 24).
  8. Inavyoonekana alikuja kuwa rafiki wa karibu na Petro (kama vile 1 Petro 5:1 3).
  9. Mila zinasema kuwa aliandika injili iliyoruhusu jina lake kurekodiwa kwenye hotuba ya Petro iliyohubiliwa huko Rumi. Injili ya Marko ina maneno ya Kilatini kuliko kitabu kingine cha Agano Jipya

na yumkini kiliandikwa kwa ajili ya Warumi. Hili linatoka kwa Papias wa Hierapoli, kama ilivyonukuliwa na Eusebio ' *Eccl. His.* 3.39.1 5.

10. Mapokeo yanasema anahusiana na uimalishaji wa kanisa la Iskanderia

B. Sila

1. Aliitwa Sila katika Matendo na Silvanus katika Nyaraka.
2. Yeye, kama alivyo Barnaba, alikuwa kiongozi kwenye kanisa la Yerusalem (kama vile Mdo. 1 5:22-23).
3. Alishirikiana kwa karibu na Paulo (kama vile Mdo. 1 5:40; 1 6:1 9 na kuendelea; 1 7:1 -1 5; 1 The. 1:1).
4. Yeye, kama alivyokuwa Barnaba na Paulo, alikuwa ni Mtume (kama vile Mdo. 1 5:32).
5. Aliitwa Mtume (kama vile 1 Thes. 2:6).
6. Yeye, kama alivyokuwa Paulo, alikuwa ni mwenyeji wa Warumi (kama vile 1 6:37-38).
7. Yeye, kama alivyokuwa Yohana aitwaye Marko, pia anahusianishwa na Petro, huenda yumkini akajifanya mwandishi (kama vile 1 Petro 5:1 2).

C. Timotheo

1. Jina lake linamaanisha "mtu aliyemheshimu Mungu."
2. Alikuwa mtoto wa mama wa Kiyahudi na baba wa Kiyunani na waliishi Lisitra. Tafasiri ya Kilatini ya Origen's commentary kwenye Rum. 1 6:21 inasema Timotheo alikuwa mkazi wa Derbe. Yumkini hili limechukuliwa toka mdo. 20:4. Alierekezwa katika imani ya Kiyahudi na mamaye na nyanya yake (kama vile 2 Tim. 1 :5; 3:1 4-1 5).
3. Aliombwa kuambatana na timu ya umisheni ya Paulo na Sila kwenye safari ya pili (kama vile Mdo. 16:1-5). Alithibitishwa na unabii (kama vile 1 Tim. 1 :1 8; 4:1 4).
4. Alitahiriwa na Paulo ili kwamba aweze kutenda kazi kote kwa Wayahudi na Wayunani.
5. Alikuwa ni rafiki aliyejitoa na mfanyakazi mwenza wa Paulo. Ametajwa kwa jina zaidi ya wasaidizi wengine wa Paulo (mara 17 katika nyaraka 1 0, kama vile 1 Kor. 4:1 7; 1 6:1 0; Fil. 1 :1 ; 2:1 9; Kol.1 :5; 1 The. 1 :1 ; 2:6; 3:2; 1 Tim. 1 :2,1 8; 4:1 4; 2 Tim. 1 :2; 3:1 4-1 5).
6. Aliitwa "Mtume" (kama vile 1 The. 2:6).
7. Nyaraka mbili kati ya tatu za kichungaji zinamzungumzia Yeye.
8. Ametajwa mara ya mwisho katika Waebrania 1 3:23.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO 16:15

<sup>1</sup>Basi akafika Derbe na Listra, na hapo palikuwa na mwanafunzi mmoja jina lake Timotheo, mwana wa mwanamke Myahudi aliyeamini; lakini babaye alikuwa Myunani. <sup>2</sup> Mtu huyo alishuhudiwa vema na ndugu waliokaa Listra na Ikonio. <sup>3</sup> Paulo akamtaka huyo afuatane naye, akamtwa akamtahiri kwa ajili ya Wayahudi waliokuwako pande zile; kwa maana wote walijua ya kuwa babaye ni Myunani. <sup>4</sup> Basi walipokuwa wakipita kati ya miji ile, wakawapa zile amri zilizoamriwa na mitume na wazee walioko Yerusalemu, ili wazishike. <sup>5</sup> Mekanisa yakatiwa nguvu katika ile Imani, hesabu yao ikaongezeka kila siku.

**16:1 "Derbe and to Listra"** Miji hii iko sehemu ya kusini mwa jimbo la Kirumi huko Galatia (Uturuki ya leo). Paulo aliitembelea miji hii kwenye safari yake ya kwanza ya umisionari (kama vile 1 6:1 4).

▣ **"Na hapo palikuwepo na Mwanafunzi"** Luka anatumia neno hili *idou* kutambulisha hiki kifungu. Ilikuwa ni njia ya kuonyesha msisitizo. Timotheo akajakuwa mshiriki mkuu wa huduma ya Paulo.

▣ **"Mwana wa mwanamke aliyeamini, lakini babaye alikuwa Myunani"** Kutokana na 2 Tim. 1 :5 tunajifunza kuwa bibi pia alikuwa ni mwamini wa Kiyahudi au Myahudi aliyebobea kwenye imani. Bibi yake aliitwa Loisi na mama yake aliitwa Eunike. Mama yake, na huenda bibi yake, akawa muumini kwenye safari ya kwanza ya Paulo.



**16:2 "mtu huyu alishuhudiwa vema"** Hii ni kauli isiotimilifu tendwa yenye hali ya kuelekeza. Watu walimsema vizuri Timotheo tena na tena. Moja ya sifa ya kiongozi wa kanisa ilikuwa ni "kujiepusha na shutuma," ndani ya jamii inayoamini na isiyoamini (kama vile 1 Tim. 3:2, 7, 10).

▣ **"walioko Listra"** Mji alioishi Timotheo ulikuwa ni Listra. hata hivyo, baadhi ya machapisho ya Kiyunani ya Mdo. 20:4 (na maandiko ya Origen) yanadokeza kuwa Derbe ulikuwa ni mahali alipokuwa akiishi.

**16:3 "Paulo akamtaka wafuatane naye"** Tambua kuwa Paulo alimwita Timotheo. Hili halikuwa chaguo pekee la Timotheo (kama vile 1 Tim. 3:1). Kwa maana Timotheo akajakuwa mwakilishi wa Kitume wa Paulo.

▣ **"akamtwaa, akamtahiri"** Paulo alimtaka yeye aweze kufanya kazi na Wayahudi (kama vile 1 Kor. 9:20; Mdo. 1 5:27-29). Haya hayakuwa malalamiko na wafuasi wa dini ya Kiyahudi kwa sababu

1. Matokeo ya baraza la Yerusalemi (kama vile Mdo. 1 6:15)
2. Alikataa kumtahiri Tito (kama vile Gal. 2:3)

Hata hivyo, matendo ya Paulo kwa uhakika yaliwachanganya! Namna ya Paulo ya kuvileta vitu vyote kwa watu wote ili kuwavuta baadhi (kama vile 1 Kor. 9:19-23) kuliwafanya watu na wokovu wao kuwa kipaumbele!

▣ **"babaye alikuwa Myunani"** Njeo ya wakati usiotimilifu inadokeza kuwa alikuwa amekufa.

**16:4** Paulo na Sila walitoa taarifa (yaani, kauli isiotimilifu tendaji elekezi) juu ya matokeo ya baraza la Yerusalemi (kama vile Mdo. 1 5:22-29). Kumbuka haya "mambo ya msingi" yalikuwa kwa ajili ya makusudi mawili:

1. kuwepo na ushirika ndani ya makanisa
2. Kuwahubiri Wayahudi (kama vile ilivyokuwa tohara ya Timotheo)

**16:5** Haya ni moja ya maelezo mafupi ya Luka (kama vile Mdo. 6:7; 9:31; 12:24; 16:5; 19:20; 28:31). Paulo alikuwa na moyo wa kuwafanya watu kuwa wanafunzi (kama vile Mdo. 1 4:22; 1 5:36; 1 5:5). Uinjilisti pasipo kuwanya watu kuwa wanafunzi unakiuka agizo kuu (cf. Matt. 28:18-20) na unapelekea katika "kuanguka kiroho!"

▣ **"makanisa"** Angalia Mada Maalum katika Mdo. 5:11.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 16:6-10**

<sup>6</sup> Wakapita katika nchi ya Frigia na Galatia, wakikatazwa na Roho Mtakatifu, wasilihubiri lile neno katika Asia. <sup>7</sup> Walipofika kukabili Misia wakajaribu kuenda Bithinia, lakini Roho wa Yesu hakuwapa ruhusa, <sup>8</sup> wakapita Misia wakatelemkia Troa. <sup>9</sup> Paulo akatokewa na maono usiku; alimwona mtu wa Makedonia amesimama, akimsihi, na kumwambia, Vuka, uje Makedonia utusaidie. <sup>10</sup> Basi alipokwisha kuyaona yale maono, mara tukataka kutoka kwenda Makedonia, kwa kuwa tuliona hakika ya kwamba Mungu ametuita tuwahubiri Habari Njema.

**16:6 "Wakapita katika nchi ya Frigia na Galatia"** Katika andiko hili Luka anaongelea zaidi juu ya jamii, makundi yanayokubaliana kuliko kutengeneza majimbo au mgawanyiko wa kisiasa. Hii nahau ingaliweza kurejelea kwenye mipaka isio rasmi kati ya makundi haya ya kikabila.

▣ **"Wakikatazwa na Roho"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu. Ni neno la kawaida katika maandiko ya kale ya Kiyunani na katika agano jipya. Roho kwa undani kabisa alijihusisha na matendo na maamuzi ya kanisa la mwanzo (kama vile 2:4; 8:29,39; 1 0:19; 1 1 :12,28; 1 5:28; 1 6:6,7; 21 :4; Rum. 1 :13). Makanisa ya leo yamepoteza nguvu ya kanisa la mwanzo.

▣ **"katika Asia"** Hili linarejelea kwenye jimbo la Kirumi la Asia Ndogo, ambalo lilikuwa upande wa mwisho wa

Magharibi mwa Uturuki ya leo.

**16:6,7 "na Roho Mtakatifu. . .Roho wa Yesu"** Kwa ajili ya tabia ya Roho, angalia Mada Maalum katika Mdo. 1:2.

Angalia mada ifuatayo.

### **MADA MAALUM: YESU NA ROHO**

Kuna bubujiko kati ya kazi ya Roho na Mwana. G. Campbell Morgan alisema jina zuri la Roho Mtakatifu ni "Yesu mwingine" (hata hivyo, tofauti yao, utu wa milele). Ufuatao ni mlinganisho wa mhusari wa kazi na wadhifa wa Mwana na Roho.

1. Roho aitwaye "Roho wa Yesu" au maelezo yanayofanana (kama vile Rum. 8:9; 2 Kor. 3:17; Gal. 4:6; 1 Pet. 1:11).
2. Wote wanaitwa kwa maneno sawa
  - a. "kweli"
    - 1) Yesu (Yohana 14:6)
    - 2) Roho (Yohana 14:17; 16:13)
  - b. "mwombezi"
    - 1) Yesu (1 Yohana 2:1)
    - 2) Roho (Yohana 14:16,26; 15:26; 16:7)
  - c. "Mtakatifu"
    - 1) Yesu (Marko 1:24; Luka 1:35; Matendo 3:14; 4:27,30)
    - 2) Roho (Luka 1:35)
3. Wote hukaa ndani ya waamini
  - a. Yesu (Mt. 28:20; Yohana 14:20,23; 15:4-5; Rum. 8:10; 2 Kor. 13:5; Gal. 2:20; Efe. 3:17; Kol. 1:27)
  - b. Roho (Yohana 14:16-17; Rum. 8:9,11; 1 Kor. 3:16; 6:19; 2 Tim. 1:14)
  - c. Baba (Yohana 14:23; 2 Kor. 6:16)
4. Kazi ya Roho ni kutoa ushuhuda juu ya Yesu(kama vile Yohana 15:29; 16:13-15)

**16:7 "Misia"** Hili lilikuwa ni eneo la kikabila sehemu za Kaskazini mwa jimbo la Kirumi huko Asia Ndogo. Lilizungukwa na mabarabara makuu ya Kirumi. Miji mikuu yake ulikuwa Troa, Assos, and Pergamo.

▣ **"Bethania"** Hii mji pia ulikuwa Magharibi mwa Asia Ndogo, Kaskazini mwa Masia. Hili halikuwa jimbo la Kirumi katika siku za Luka, lakini liliunganishwa na Ponto kuwa moja ya sehemu ya kisiasa. Baadaye Petro alilitembelea eneo hili (kama vile 1 Pet. 1:1). Tunajifunza toka kwa Filo kuwa palikuwepo makoloni mengi ya Kiyahudi.

**16:8 "wakapita Misia"** Katika muktadha huu, lazima imaanishe "kupita katikakati" au "eneo la" (kama vile BAGD 625). Kumbuka, mazingira yanaamua maana na sio misamiati/kamusi.

▣ **"Troa"** Hii mji ulikuwa yapata maili nne toka Troa ya kale. Ulipatikana yapata miaka 400 mapema na kubakia kuwa mji huru wa Kiyunani mpaka ulipokuja kuwa koloni la Kirumi. Ulikuwa ni mji wenye bandari meli zilipoondokea toka Masia hadi Makedonia.

**16:9 "Paulo akatokewa na maono"** Mungu alimwongoza Paulo mara nyingi kwa namna ya nguvu ya ajabu.

1. Kwa nuru na sauti ya Yesu, Mdo 9:3-4
2. Maono, Mdo. 9:10
3. Maono, Mdo. 16:9,10
4. Maono, Mdo. 18:9
5. Ndoto, Mdo. 22:17
6. Malaika wa Mungu Mdo. 27:23

▣ **"mtu wa Makedonia"** Ni namna gani Paulo alimutambua kuwa ni mtu toka Makedonia haijulikani. Yumkini ni kwa sababu ya matamshi, nguo, marashi, au alithibitishiwa katika maono. Baadhi ya watoa maoni wanafikiri kuwa yule mtu alikuwa ni Luka (kama vile 1 6:1 0).

Haya yalikuwa ni maamuzi ya kijiografia. Injili ikageuka kuelekea Ulaya!

▣ **"uje. . .utusaidie"** Ya kwanza iko katika kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu, ikitumika kama shurutishi, ya pili ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Maono yalikuwa dhahiri na yenye kutia mkazo.

**16:10 "sisi"** Huu ni uonekanaji wa mara ya kwanza wa kipengere "sisi" katika kitabu cha Matendo. Hili linamrejelea Luka alipoongezwa kwenye kundi la Paulo, Sila na Timotheo katika safari umisheni (kama vile Mdo. 1 6:1 0-1 7; 20:5-1 5; 21 :1 -1 8; 27:1 -28:1 6). Baadhi ya watoa maoni wamefikiri kuwa Paulo aliyeonekana katika Mdo. 16:9 alikuwa Luka, tabibu mtu wa mataifa na mwandishi wa injili ya Matendo.

▣ **"Makedonia"** Ugiriki ya sasa ilikuwa imegawanyika katika majimbo mawili ya Kirumi.

1. Achaia upande wa kusini (Athene, Corinto, Sparta)
2. Makedonia upande wa Kaskazini (Filippi, Thessalonike, Berea)

▣ **"tuliona hakika ya kwamba"** Hili ni neno *sumbibazō*, kiuhalisia lenye kumaanisha kukusanya pamoja au kuunganisha . hapa linaainisha kuwa yote yale yaliyotokea yalikuwa ni maongozi ya Mungu kwenda Makedonia.

1. Roho hakuwaruhusu wao kuhubiri huko Asia, kama vile Mdo. 16:6
2. Roho aliwashikilia huko Bathinia, kama vile mst 7
3. Na maono ya Mdo. 16:9

▣ **"Mungu ametuita"** Hii ni kauli timilifu tendwa yenye kuarifu. Uongozi wa Roho ulikuwa sio kwa ajili ya usalama, bali kwa ajili ya uinjilisti. Siku zote haya ndiyo mapenzi ya Mungu.

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 16:11-15

<sup>11</sup> Basi tukang'oa nanga kutoka Troa, tukafika Samothrake kwa tanga moja, na siku ya pili tukafika Neapoli; <sup>12</sup> na kutoka hapo tukafika Filipi, mji wa Makedonia, mji ulio mkuu katika jimbo lile, mahali walipohamia Warumi; tukawa katika mji huu, tukikaa siku kadha wa kadha. <sup>13</sup> Hata siku ya sabato tukatoka nje ya lango, tukaenda kando ya mto, ambapo tukadhani ya kuwa pana mahali pa kusali; tukaketi, tukasema na wanawake waliokutana pale. <sup>14</sup> Mwanamke mmoja, jina lake Lidia, mwenye kuuza rangi ya zambarau, mwenyeji wa Thiatira, mcha Mungu, akatusikiliza, ambaye moyo wake ulifunguliwa na Bwana, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo. <sup>15</sup> Hata alipokwisha kubatizwa, yeye na nyumba yake, akatusihi, akisema, Kama mmeniona kuwa mwaminifu kwa Bwana, ingieni nyumbani mwangu mkakae. Akatushurutisha.

**16:11 "Tukafika"** Haya ni moja ya maneno ya kibaharia yaliyotumiwa na Luka (kama vile sura ya. 27). Walichukua meli na kukwea njia ya moja kwa moja, na sio meli za pwani. Luka aliyafahamu maneno ya kibaharia vizuri au aliwahoji mabaharia.

▣ **"Samothrake"** Hiki ni kisiwa kidogo chenye miamba kilichoinuka juu ya bahari yapata futi 5,000. Ilikuwa ni kati kati ya Troa na Filipi.

▣ **"Neapoli"** Kiuhalisia huu ni "mji mpya." Palikuwepo na miji mingine huko Mediterrania yenye majina haya. Huu mmoja ulikuwa ni bandari kwa ajili ya Filipi, ambao ulikuwa umbali wa maili 10. Barabara kuu ya Kirumi iliyotoka Mashariki hadi Magharibi ikimalizikia safari ngumu na ndefu upande wa Mashariki.

**16:12 "Filipi"** Katika lugha ya Kiyunani ni wingi, yumkini likidokeza muunganikano wa makazi mengi kufanya kuwa mji mmoja. Ulikuwa kwenye njia kuu maarufu ya Kirumi, njia ya Ignatia. Huu mji kiasili uliitwa Krenidesi (yaani visima). Filipo II huko Makedonia aliuteka kwa sababu ya kuwepo kwa dhahabu nyingi .

**NASB,NRSV "mji uliokuwa mkuu katika jimbo la Makedonia"**

**NKJV "mji mkuu katika sehemu ya Makedonia"**

**TEV "mji wa jimbo la kwanza la Makedonia"**

**NJB "mji mkuu wea jimbo"**

Hiki kifungu hakijulikani. Amphipolis ulikuwa ni "mji unaoongoza huko Makedonia." Kile Luka alimaanisha juu ya hili hakijulikani. Yaweza kuwa ni cheo cha heshima kwa sababu ya umuhimu wake.

▣ **"koloni la Kirumi"** Katika mwaka wa 42 k.k., Octavian na Marko aitwaye Antoni alimshinda Cassius na Bruto karibia na mji huu. Katika hali ya kukumbuka ushindi huu, Octavian aliutengeneza mji wa Filipi kuwa koloni la Kirumi na makao ya wanajeshi wake waliostaafu. Katika mwaka wa 31 k.k, baada ya kumshinda Antoni na Kreopatra huko Attium, Octavian aliweka vikosi vyake huko.

Makoloni mengine ya Kirumi yaliyotajwa katika Agano Jipya ni Pisidia Antiokia, Listra, Troa, Corinto, na Ptolema. Yote ilikuwa na haki ya kuwa miji huko Italia yenye:

1. serikali yao binafsi
2. Isiyo na kodi
3. marupurupu maalum ya kisheria

Mara nyingi Paulo alihubiri na kuanzisha makanisa katika makoloni haya ya Kirumi.

**16:13 "hata siku ya Sabato"** Inavyoonekana hapakuwepo na Sinagogi huko Filipi. Hili lilikuwa ni kolono la Kirumi, yawezekana hata hapakuwepo na wanaume 10 wa Kiyahudi katika mji, ambayo ilikuwa ni hesabu ndogo iliyohitajika ili pawepo na Sinagogi. Inavyoonekana palikuwepo na watu baadhi waliomwogopa Mungu au walio badili dini (kama vile Mdo. 1 6:1 4; 1 3:43; 1 7:4,1 7; 1 8:7). Wengi wa wanawake walivutiwa na maadili ya dini ya Kiyahudi.

▣ **"kando ya Mto"** Hapa panaonekana kuwa sehemu iliyozoneleka kwa ajili ya ibada ya kidini (kama vile Josephus' *Antiquities of the Jews* 1 4.1 0.23).

▣ **"tukaketi"** Hii inaonekana kuwa sehemu yenyewe ya mafundisho ya sheria ya dini ya Kiyahudi, lakini ulikuwa ni mji wa Kirumi na, kwa hiyo, yawezekana haukuwa na umuhimu wowote. Huu ni ushahidi wa macho mwingine wa Luka.

**16:14 "Mwanamke mmoja, jina lake Lidia, mwenyeji waThiatira"** Jimbo la Kirumi huko Makedonia lilikuwa na fursa nyingi kwa ajili ya wanawake kuliko sehemu nyingine yeyote katika karne ya kwanza ya ulimwengu wa kimediterania. Lidia ulikuwa ni mji huko Asia Ndogo (kama vile Ufu. 2:1 7ff). Ulijulikana kwa rangi zake za hudhurungi, iliyotengenezwa kutokana na magamba ya kombe/konokono, iliyokuwa maarufu kwa Warumi. Palikuwepo na Sinagogi mjini kwao. Jina lake lilitokea huko Lidia, jimbo la mji wa kale, ambapo mji ulikuwa. Hakutajwa katika barua za Paulo kwa hiyo, yawezekana alikuwa ameshakwisha fariki.

▣ **"Mcha Mungu"** Hii inarejelea juu ya walewacha Mungu waliopendezwa na dini ya Kiyahudi lakini walikuwa bado kubadili itikadi.

▣ **"moyo wake ulifunguliwa na Bwana"** Biblia inaelezea uhusiano uliopo kati ya Mungu na Mwanadamu kama Agano. Mungu mara zote huchukua fursa ya kuanzisha mahusiano na kuunda namna ya agano (angalia mada maalum katika Mdo. 2:47). Wokovu ni agano la kimahusiano. Hakuna awezae kuokolewa isipokuwa Mungu ameanzisha (kama vile Yn 6:44,65). Hata hivyo, shauku ya Mungu ni kuwa wanadamu wote wapate kuokolewa (kama vile Yn 3:1 6; 4:42; Tito 2:1 1 ; 1 Tim. 2:4; 4:1 0; 2 Pet. 3:9; 1 Yn 2:1 ; 4:1 4); kwa hiyo, dokezo ni kwamba

Mungu, kwa viwango Fulani (mafunuo ya kiasili, kama vile Zab. 19:1-6 au mafunuo maalum, kama vile Zab. 19:7-14), yanakabiliana na kila mwanadamu na dhambi zake (kama vile Warumi 1 -3) na tabia zake. Swali lililopo ni kuwa kwa nini wewngine wanakubali wengine hawakubali! Mimi mwenyewe siwezi kukubaliana kuwa jibu ni uchaguzi wa Mungu mwenyewe kuwachagua baadhi, na sio wengine. Watu wote wameumbwa kwa sura ya Mungu (kama vile Mwa.1:26-27) na Mungu ameahidi kuwakomboa wote Mwa.3:15.

Huenda sio muhimu kuelewa kwa nini, lakini ndio namna tunaipeleka injili kwa wote na ipate kutenda kazi kwenye mioyo na fikra za wasikiaji (kama vile Mt. 1 3:1 -23). Paulo alihubiri Lidia mkewe na nyumba nzima wakaikubali injili.

**16:15 "hata alipokwisha kubatizwa, yeye na nyumba yake"** Hii inavyoonekana inarejelea familia yake, watumwa na watenda kazi (kama vile Kornelio, Mdo. 10:2; 1 1 :1 4; na wafungwa wa kifilipi, Mdo. 1 6:33). Pia, tambua kuwa yeye mke, kama ilivyo kwa wengine katika Agano Jipya, walibatizwa haraka. Halikuwa suala la uchaguzi! Angalia Mada Maalum: Ubatizo katika Mdo. 2:38. Swali la kithiolojia lililojitokeza kwenye mstari huu ni kuwa, "watoto pia walihusisha katika mfano huu wa mazungumzo ya kifamilia katika kitabu cha Matendo? Kama ndivyo, kwa hiyo kuna mwongozo wa kibiblia kwa ajili ya ubatizo wa watoto wadogo katika "familia za waliookoka."wale wote wanaodai hili kama ushahidi pia wanaelekeza kwenye taratibu za Agano la Kale la kuwajumuisha watoto wadogo katika taifa la Israel kama watoto wadogo (yaani., watahiriwe siku ya nane baada ya kuzaliwa, angalia James D. G. Dunn, kur. 1 75-1 76).

Ingawa inawezekana kuwa imani katika Kristo mara moja iliathiri familia nzima (kama vile Kumb. 5:9 na 7:9) katika muundo huu wa kijamii, swali linabaki kuwa "je hii ni imani ya wote kuifuata katika kila tamaduni?" ningalitetea kuwa Agano Jipya ni ufunuo kuhusu uchaguzi binafsi wa hiari uhusiano na maana ya kulitambua kosa. Mtu lazima atambue hitaji lake kwa ajili ya mwokozi. Hili linatupelekea maswali zaidi, "je watu wanazaliwa wadhambi kwa ajili ya Adamu, au wanakuwa wadhambi wakati wakichagua kutomtii Mungu?"sheria ya dini ya Kiyahudi inaruhusu kipindi cha utoto kutokuwa na hatia mpaka apate maarifa ya kisheria na awe na uwezo wa kuitunza hiyo sheria; kwa wavulana, miaka 13, kwa wasichana, miaka 12. Walimu wa dini ya Kiyahudi hawasisitizi Mwanzo 3 kwa nguvu kama kanisa. Agano Jipya ni vitabu kwa ajili ya watu wazima. Linadai upendo wa Mungu kwa watoto, lakini ujumbe wake umeelekezwa kwa watu wazima! Hata hivyo, tunaishi kwenye jamii ya watu wenye kujitawala kibinafsi, lakini huko Mashariki ya karibu inaongozwa na jamii ya kikabila, ukoo, familia!

▣ **"kama"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza, inayofikiliwa kuwa kweli kwa mwamini kutokana na mtazamo wa mwandishi au kusudi lake la kifasihi.

▣ **"mmeniona kuwa mwaminifu kwa Bwana"** Maneno ya kwanza ni kauli timilifu tendaji elekezi. Lidia anadai kuwa yeye sasa ni mwamini. Alikuwa akiwakaribisha hawa wamisionari kuitumia nyumba yake na mali zake kwa ajili ya injili. Hii ni kutokana na ujumbe wa Yesu kwa wale sabini alipowatuma kwa ajili ya huduma (kama vile Luka 1 0:5-7).

▣ **"ingieni nyumbani mwangu mkakae"** Lidia alikuwa mtu wa tabia ya utetezi, mwanamke mfanya biashara! Hiki kitenzi cha kwanza ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu, iliyotumika kama yenye kushurutisha; ya pili ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO 16:16-18**

<sup>16</sup> Ikawa tulipokuwa tukienda mahali pale pa kusali, kijakazi mmoja aliyekuwa na pepo wa uaguzi akatukuta, aliyewapatia bwana zake faida nyingi kwa kuagua. <sup>17</sup> Akamfuata Paulo na sisi akipiga kelele, akisema, Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenye kuwahubiria njia ya wokovu. <sup>18</sup> Akafanya hayo siku nyingi. Lakini Paulo akasikitika, akageuka akamwambia yule pepo, Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu. Akamtoka saa ile ile.

**16:16 ikawa"** Inavyoonekana hili lilitokea siku iliyofuata, yumkini siku ya sabato iliyofuata. Hii ilikuwa ni nafasi ya kukabiliana nayo, lakini Mungu aliingilia kati kwa ajili ya kusudi lake, kama alivyo katika kila tukio, kila siku, kila mkabiliano binafsi!

▣ **"aliyekuwa na pepo la uaguzi"** Kuna sentensi mbili zilizotumika kumwelezea huyu binti mtumwa. "Ubashiri" wa kwanza (unaopatikana hapa tu katika Agano Jipya) una mazingira ya Agano la Kale, lakini unatumia maneno tofauti ya Kiyunani katika tafasiri ya maandiko ya agano la kale la Kiyunani (kama vile Law. 1 9:31 ; 20:6,27; Kumb. 1 8:1 1 ; 1 Sam. 28:3,7; 2 Fal. 21 :6; 1 Nya. 1 0:1 3). Huyu alikuwa ni mtu aliyepagawa na mapepo ambaye, kwa nyimbo, manuizo, au kutafasili tabia za kiasili (yaani., mruko wa ndege, mawingu, mabaki kwenye kikombe cha kunywea, ini la mnyama) lingaliweza kutabiri na, kwa kiwango Fulani, kuathiri mambo ya mbele.

Katika muundo wa kitamaduni wa Kiyunani neno ni *puthōn*, ambalo linatokana na mithiolojia ya Kiyunani pale nyoka mkubwa alipouwawa na Apollo. Na hadithi hizi za kubuni zikaja kuwa ibada za mafunuo (yaani., Delphi), ambapo mwanadamu anaweza kuwasiliana na miungu. Eneo hili lilijulikana kwa sababu ya uwepo wake wa kuwa na nyoka wengi (yaani., nyoka wenye sumu) ambao wangaliweza kumtambalia mtu aliyelala hekaluni na kumruhusu nyoka kumtembelea kwa ajili ya kusudi la kujua na kuathiri mambo ya mbele.

▣ **"kwa kuwaagua"** Neno hili (kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo, jinsi ya kike, ikiwa katika umoja) imetumika hapa tu katika Agano Jipya. Mzizi wa neno ni la kawaida katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani kwa ajili ya "mwaguzi, mwonaji, nabii,"mara zote katika mazingira hasi. Inamaanisha mtu anayepayuka, kwa maana hiyo inadokeza ndoto ya mchana kweupe yenye kuambatana na utabiri. Hapa inadokeza yule atabiriye mambo ya mbele kwa ajili ya masilahi. Maana ya kimuktadha na kimsamiati ni kuwa binti alikuwa amepagawa na mapepo.

**16:17 "akamfuata Paulo. . . akipiga kelele"** Hii ni kauli tendaji endelvu ya wakati uliopo na kauli isiotimilifu tendaji yenye kuarifu. Aliendelea kumfuata na akapiga kilele (kama vile Mdo. 1 6:1 8).

▣ **"watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu"** Yesu asingekubaliana na ushuhuda wa kimapopo (kama vile Luka 8:28; Marko 1 :24; 3:1 1 ; Mt. 8:29) na wala Paulo kwa sababu ingaliwapelekea kumaanisha wanakubaliana na mambo ya kimapopo. Neno : Mungu aliye juu"(kama vile Marko 5:7; Luka 8:28) lilitumika kwa YHWH (yaani., *El, Elyon*) katika Mwa. 1 4:1 8-1 9; Hii roho haikutoa ushuhuda wa kumtukuza Mungu, bali ni kishirikisha injili na mapepo.

▣ **"wenye kuwahubiri njia ya wokovu"** Hakuna andiko lolote lenye neno "njia" (kama vile toleo la NRSV). Yumkini alikuwa akisema kuwa ilikuwa ni njia mojawapo ya Mungu aliye juu. Hili pepo sio kwamba linajaribu kuisadia huduma ya Paulo.

Kusudi la maelezo haya ni

1. Kumtambua Paulo na utabiri
2. Kuleta suluhisho, sio njia ya wokovu (yaani., imani katika Kristo)

Biblia ya NET (uk. 2022 #1 6) ina mjadala mzuri juu ya suala la kisarufi linalohusiana na mambo ya ufasiri wa neno "namna" dhidi ya "njia." Suala lenyewe hapa ni kuwa kile wasikiaji katika karne kwanza huko Filipi wangaliweza kutambua. Katika muundo wao wa kitamaduni, "Mungu aliye juu" angaliweza kurejelewa *Zeus*, kwa hiyo uwepo wa kukosekana kiambishi cha awali kikiwa na neno "njia" sio suala la kiufafanuzi.

**16:18 "lakini Paulo akasikitika"** Kwa mfano huu Paulo alitenda, sio nje ya upendo, bali nje ya maumivu. Alikuwa naye ni mtu tu! Hiki kitenzi chenye nguvu kinapatikana katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani katika Mhu. 1 0:9, ambapo inamaanisha kazi ngumu. Katika Agano Jipya linatumika hapa tu na katika Matendo 4:2. Linadokeza mtu ambaye aliyechakaa.

▣ **"yule pepo"** Tambua Paulo hamzungumzii yule binti mtumwa, bali yule pepo amumilikie na kumwendesha. Upungaji pepo wa Paulo alifundishwa kwa namna ile ile kama wengine wapunga pepo walivyofundishwa katika

Agano Jipya (yaani., kwa jina la Yesu). angalia Mada Maalum: Kupagawa na mapepo na Upungaji Pepo katika Mdo. 5:1 6.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 16:19-24**

<sup>19</sup> Basi bwana zake walipoona ya kuwa tumaini la faida yao limewapotea, wakawakamata Paulo na Sila, wakawakokota mpaka sokoni mbele ya wakuu wa mji; <sup>20</sup> wakawachukua kwa makadhi, wakasema, Watu hawa wanachafua sana mji wetu, nao ni Wayahudi; <sup>21</sup> tena wanatangaza habari ya desturi zisizokuwa halali kwetu kuzipokea wala kuzifuata, kwa kuwa sisi tu Warumi. <sup>22</sup> Makutano wote wakaondoka wakawaendea, makadhi wakawavua nguo zao kwa nguvu, wakatoa amri wapigwe kwa bakora. <sup>23</sup> Na walipokwisha kuwapiga mapigo mengi, wakawatupa gerezani, wakamwamuru mlinzi wa gereza awalinde sana. <sup>24</sup> Naye akiisha kupata amri hii akawatupa katika chumba cha ndani, akawafunga miguu kwa mkatale.

**16:19 "walipoona ya kuwa tumaini la faida yao limepotea"** Hawa "mabwana" hawakujali hata kidogo kuwa mwanadamu ametolewa toka kwenye ukandamizwaji kwenda kwenye uovu. Walijaa hofu na kupotelewa na mali (kama vile Mdo. 1 6:1 6), zaidi kama watu walioonekana katika Luka 8:26-39.

▣ **"wakawakamata Paulo and Sila"** Sababu ya Luka na Timotheo kutokukamatwa haijulikani.

**16:20 "Makadhi"** Hili ni neno *praetors*. Rasmi vyeo vyao vilikuwa *duumvirs*, lakini tunajifunza toka kwa Kikero kuwa wengi walipendwa kuitwa *Praetors*. Luka yuko sahihi katika matumizi yake vyeo rasmi vya kiserikali ya Kirumi. Hii ni moja ya ushahidi wa historia yake.

**16: 20, 21 "nao ni Wayahudi. . .sisi ni Warumi"** Hii inaonyesha majivuno yao ya kijamii na dhuluma. Muda wa Paulo huko Filipi yawezekana ulikuwa karibu na tamko la Klaudio la kuwaondoa Wayahudi toka Rumi, mwaka wa 49-50 b.k (kiukweli alikataa taratibu za ibada za Kiyahudi). Mrumi asiye Msemitiki anaweza onekana katika Cicero's *Pro Fiasco* 28 and *Javenal* 1 4.96-1 06.

▣ **" tena wanatangaza habari ya desturi zisizokuwa halali kwetu kuzipokea wala kuzifuata"** Tambua shutuma hizi hazikumwathiri binti mtumwa aliyekuwa akipunga pepo. Inavyoonekana inarejelea kwenye mahubiri yao ya injili ya Yesu Kristo. Dini ya Kiyahudi ilikuwa ni dini ilikuwa imerasimishwa kisheria katika himaya ya Kirumi, lakini kama ilivyokuja julikana dhahili kuwa Ukristo ulikusudiwa kuonekana kama dini tofauti na, kwa hiyo, ni dini isiyofaa. Ilikuwa ni kosa kwa Wayahudi kujaribu kuwabadilisha dini Warumi, na ilikuwa kosa kwa Paulo pia.

**16:22 " wakawavua nguo zao kwa nguvu, "** Muundo wa maneno unadokeza kuwa makadhi wawili yaani *Praetors*, waliondolewa kwa makelele ya umati wa watu, wakawavua nguo zao Paulo na Sila (kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu, wingi). Hii ingalikuwa kwao ni hali isio ya kawaida kuwa watendaji wenye nguvu katika tukio la kimahakama

1. Wakawavua nguo (kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu)
2. Wakaamuru wapigwe bakora (yaani., kauli isio timilifu tendaji yenye kuarifu ikifuatiwa na kauli tendaji isio na ukomo ya wakati uliopo)

▣ **" wapigwe kwa bakora"** Aina hii ya adhabu (yaani., *verberatio*, ambayo ilitolewa na mamlaka ya baraza la mji) haikuwa kali kama ile ya Kirumi ya kuchapwa na mjeledi. Hapakuwepo na idadi ya viboko. Paulo alipigwa namna hii mara tatu (kama vile 2 Kor. 1 1 :25). Hii ni ile tu iliyowekwa kwenye kumbukumbu (kama vile 1 The. 2:2).

**16:24 " akawatupa katika chumba cha ndani, "** Hii inamaanisha kuwepo na ulinzi wa hali ya juu. Palikuwepo na sababu ya kuwepo na hofu (kama vile 1 6:29). Upungaji pepo wa Paulo ulikamata usikivu wao.

▣ " **akawafunga miguu kwa mkatale**" Magereza mengi katika siku hizo yalikuwa yakifungwa minyororo kwenye kuta ambapo mfungwa alifungwa hapo. Kwa hiyo, milango ilitiwa komeo, na sio kufungwa tu. Huu mlundikano ungaliongeza upana wa kipimo na kusababisha hofu kubwa na kuongeza ulinzi.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA): MATENDO 16:25-34**

<sup>25</sup> Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwambia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza. <sup>26</sup> Ghafula pakawa tetemeko kuu la nchi, hata misingi ya gereza ikatikisika, na mara hiyo milango ikafunguka, vifungo vya wote vikalegezwa. <sup>27</sup> Yule mlinzi wa gereza akaamka, naye alipoona ya kuwa milango ya gereza imefunguka, alifuta upanga, akataka kujiua, akidhani ya kuwa wafungwa wamekimbia. <sup>28</sup> Ila Paulo akapaza sauti yake kwa nguvu, akisema, Usijidhuru, kwa maana sisi sote tupo hapa. <sup>29</sup> Akataka taa ziletwe, akarukia ndani, akitetemeka kwa hofu, akawaangukia Paulo na Sila; <sup>30</sup> kisha akawaleta nje akasema, Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka? <sup>31</sup> Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako. <sup>32</sup> Wakamwambia neno la Bwana, yeye na watu wote waliomo nyumbani mwake. <sup>33</sup> Akawakaribisha saa ile ile ya usiku, akawaosha mapigo yao, kisha akabatizwa, yeye na watu wake wote wakati uo huo. <sup>34</sup> Akawaleta juu nyumbani kwake, akawaandalia chakula, akafurahi sana, yeye na nyumba yake yote, maana amekwisha kumwamini Mungu.

**16:25 "panapo usiku wa manane"** Yumkini walishindwa kulala kwa sababu ya maumivu ya viboko na mlundikano wa watu.

▣ "**wakimwomba Mungu na kumwambia nyimbo za kumsifu**" Inawezekana kuwa dhima ya kithiolojia ya maombi haya na nyimbo za sifa zilisababisha wafungwa wamwamini Kristo (yaani, "wafungwa walikuwa wakiwasikiliza wao") kwa sababu hapana hata mfungwa mmoja aliyetoroka pindi tetemeko lilipo fungua milango (kama vile Mdo. 1 6:26,28, "sote tuko hapa").

▣ "**na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza**" Hii ni kauli isiyotimilifu ya kati (shahidi) yenye kuarifu, ikidokeza wafungwa kuendelea kuwasikiliza Paulo na Sila. Kitenzi *epakroaomai* ni neno adimu katika Agano Jipya na tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani. Matumizi yake katika 1 Sam. 1 5:22 yanadokeza usikivu wa ndani wenye furaha. Hawa wafungwa wa mtaani wasio na makazi waliusikiliza kwa makini na kuupokea ujumbe wa pendo la Mungu, uangalizi na ukubarifu!

**16:26 "ghafila pakawa tetemeko kuu la nchi"** Hili lilikuwa ni tukio la kiasili, lakini likiwa na madhara ya ajabu (kama vile Mt. 27:51 ,54; 28:2). Mungu alimwokoza Petro toka gerezani kwa namna ya malaika (kama vile Mdo. 4:31 ), lakini hapa tukio lilichaguliwa kumpa Paulo nafasi ya kuihubiri injili kwa wote wafungwa na walinzi.

**16:27 "alifuta upanga"** Huu ulikuwa ni upanga mdogo, wenye makali pande mbili uliokuwa na kutu ndani ya ala, ukiwa umetengenezwa mfano wa ulimi. Hiki kilikuwa kifaa kwa ajili ya adhabu kubwa kwa ajili ya raia wa kirumi. Ikiwa mlinzi atampoteza mfungwa, basi huyo mlinzi atasitahili kupewa adhabu ya huyo mfungwa (kama vile Mdo. 1 2:1 9).

**16:28** Imani ya Paulo na Sila na dhima ya maombi yao na nyimbo zilileta hamasa kubwa kwa wafungwa wengine (nafikiri, wao pia waliokolewa)!

**16:29 "akataka taa ziletwe"** Tambua huu ni wingi. Palikuwepo na walinzi wengine.

**16:30 "Bwana zangu, yanipasa nini ili nipate kuokoka?"** Hii inaaksi (1 ) hofu ya mwanadamu ya ajabu na (2) kutafuta amani na Mungu! Aliitaka amani na furaha walioionyesha Paulo na Sila, hata katika hali hii isio haki na ya maumivu. Mtambue mtu huyu, kama ilivyo kwa wengi, elewa lazima pawepo aina ya mwitikio wa mwanadamu



(kama vile Luka 3:1 0,1 2,1 4; Mdo. 2:37; 22:1 0).

**16:31 "mwaminini Bwana Yesu"** Kitenzi ni (kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu) *pisteuō* chaweza kutafasiliwa “sadiki” “imani” au “amini.” angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:40, 3:1 6, na 6:5. Huu kimsingi ni mwitikio wa kuamini (kama vile Mdo. 1 0:43). Pia tambua kuwa ni imani ndani ya mtu, na sio mafundisho, au utaratibu wa kithiolojia. Huyu mtu hakuyajua mazingira ya Kiyahudi (yaani., Yona huko Ninawi). Bado mahitaji kwa ajili ya wokovu kamili ni marahisi na ni yale yale! Huu ni muhtasari fasaha wa injili katika Agano Jipya (kama vile Mdo. 1 0:43). Toba yake (kama vile Marko 1 :1 5; Mdo. 3:1 6,1 9; 20:21 ) alithibitika kwa matendo yake.

▣ **"utaokoka, wewe na nyumba yako"** Katika ulimwengu wa kale dini ya mzee wa kaya ndiyo ilikuwa dini ya familia nzima (kama vile Mdo. 1 0:2; 1 1 :1 4; 1 6:1 5; 1 8:8). Ni kwa namna gani hili lilitendeka kwa kiwango cha mtu binafsi haijulikani, lakini inavyoonekana ilihusisha baadhi ya hatua ya imani binafsi kwa ile sehemu ya mtu mwenyewe. Hatimaye Paulo alihubiri ujumbe mzima wa injili kwa walinzi na nyumba zao (kama vile Mdo. 1 6:32). Kwa mfano huu, sio tu wanyumbani kwao pia gerezani!

**16:32 "neni la Bwana"** Kuna utofauti unaohusiana na kifungu hiki.

1. "Neni la Bwana" lipo katika maandishi ya MSS P<sup>45,74</sup>,  $\kappa^2$ , A, C, D, E. UBS<sup>4</sup> inatoa alama "B".
2. "Neni la Mungu" lipo katika MSS  $\kappa^*$ , B

Katika muktadha ni kwa nani neni hili “Bwana” linarejelea?

1. Yesu, Mdo. 1 6:31
2. YHWH (kama vile Mdo. 1 6:25,34; 1 3:44,48; ni kifungu cha agano la kale, kama vile Mwa. 1 5:1 4; 1 Sam. 1 5:1 0; Isa. 1 :1 0; Yona 1 :1 )

**16:33 "kisha akabatizwa, yeye na nyumba yake yote"** Hii inaonyesha umuhimu wa ubatizo. Matendo ya Mitume kinataja tena na tena. angalia **MADA MAALUM: UBATIZO** katika Mdo.2:38. Yesu aliuifanya (kama vile Luka 3:21 ) na akaamuru ufanyike (kama vile Mt. 28:1 9) na hilo likakaa (kama vile Mdo. 2:38). Pia likaendelea kwa mifano mingine katika Matendo ya Mitume kuwa ubatizo ulitendeka mara moja baada ya mtu kukiri imani (kama vile Mdo. 1 0:47-48). kwa maana hiyo kwao ilikuwa ni ukiri wa imani wa wazi na maneno katika Kristo. (yaani., Rum. 1 0:9-1 3).

**16:34 "akafurahi sana, yeye na nyumba yake yote"** Vitenzi viwili viko katika umoja vikiwarejelea walinzi. Hata hivyo, kifungu cha kielezi kinadokeza ujumuishaji familia mlandano. Kitenzi “sadiki” ni kauli timilifu tendaji endelevu, inayodokeza hali ya kutulia. Tambua badiliko katika njeo toka katika Mdo. 16:31.

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 16:35-40

<sup>35</sup> Kulipopambauka makadhi wakawatuma wakubwa wa askari wakisema, Waacheni watu wale waende zao.

<sup>36</sup> Yule mlinzi wa gereza akamwarifu Paulo maneno haya akisema, Makadhi wametuma watu ili mfunguliwe; basi, sasa tokeni nje, enendeni zenu kwa amani. <sup>37</sup> Paulo akawaambia, Wametupiga mbele ya watu wote bila kutuhukumu, na sisi tu Warumi, tena wametutupa gerezani; na sasa wanataka kututoa kwa siri? Sivyo, lakini na waje wenyewe wakatutoe. <sup>38</sup> Wakubwa wa askari wakawapasha makadhi habari za maneno haya; nao wakaogopa, waliposikia ya kwamba hao ni Warumi. <sup>39</sup> Wakaja wakawasihi; na walipokwisha kuwatoa nje, wakawaomba watoke katika mji ule. <sup>40</sup> Nao wakatoka gerezani wakaingia nyumbani mwa Lidia; na walipokwisha kuonana na ndugu wakawafaraji, wakaenda zao.

**16:35 "Makadhi"** Kiuhalisia walikuwa "watoa adhabu" (*hrabdouchosta lictor*). Hili linarejelea kwa wale waliohusika katika kufundisha nidhamu (kama vile Mdo. 1 6:20). Chama cha “kifashisti” huko Italia kilipata jina lake kutokana na neni hili. Rundo la hizi bakora (toka Latin *fasces*) zilikuwa ni alama ya mamlaka ya kisiasa.

**16:37 "na sisi tu Warumi"** Filipi lilikuwa ni koloni la Kirumi likiwa na marupurupu mengi ya kisheria ambao ungaliweza kuwa kwenye hatari kama tabia za kuwanyanyasa raia wa Kirumi zingalitaarifiwa. Kuwapiga raia wa Kirumi lilikuwa kosa kubwa kwenye hali yao ya kisheria ya kikoloni (kama vile 1 6:39; see Livy, "History" 1 0.9.4 au Kikero, "Pro Rabirio 4.1 2-1 3).

**16:39** kusudi la Paulo kupinga yawezekana ilikuwa ni kulinda hali Fulani iliyotambulika kwao. Viongozi, kwa matendo yao, wanadokeza kuwa kuhubiri injili halikuwa kosa! Mlango ulifunguka kwa ajili bidii ya kuihubiri injili huko mbeleni katika Filipi.

**16:40 "nao wakatoka"** Luka inavyoonekana alikaa pembeni. Bado tunamwona hapa katika Mdo.20:5-6.

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa mfasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki.

Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana..

1. kwa nini Roho Mtakatifu anaitwa Roho wa Kristo?
2. Kwa nini Mungu aliruhusu wamisionari kukabiliana na upinzani mzito wa namna hiyo na majaribu?
3. Kwa nini Paulo hakukubaliana na ushuhuda wa yule binti wa kitumwa?
4. Orodhesha watu waliookolewa huko Filipi.
5. Kwanini ni Paulo na Sila tu waliwekwa gerezani?
6. Kwa nini wafungwa wengine hawakuweza kukimbia?
7. Orodhesha vipengere vya wokovu katika sura hii. Je viko tofauti na na vya sura zingine katika Matendo ya Mitume?
8. je walenzi hawa wana taarifa zozote za nyuma kuhusu dini ya Kiyahudi au Ukristo?
9. Ina maana gani kusema "na nyumba yake yote ikaokolewa?"
10. Kwa nini Paulo aliwataka maafisa wa mji kuomba radhi mtu binafsi?

## MATENDO YA MITUME 17

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFASIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Ghasia huko Thesalonike 17:1-9	Kumhubiri Kristo huko Thesalonike 17:1-4 Shambulio kwenye Nyumba ya Yasoni 17:5-9 Kuhudumu huko Berea	Toka thesalonike hadi Ethene 17:1-9	Huko Thesalonike 17:1-4 17:5-9 Huko Berea	Thesalonike: ugumu alioupata kwa Wayahudi 17:1-4 17:5-9 Matatizo mapya huko Berea 17:10-12 17:13-15 Paulo huko Ethene
Mitume huko Berea 17:10-15	17:10-15	17:10-15	17:10-15	17:10-12 17:13-15
Paulo huko Ethene 17:16-21	Mwana falsafa huko Ethene 17:16-21	Paulo huko Ethene 17:16-21	Akiwa Ethene 17:16-21	Paulo huko Ethene 17:16-18
17:22-28a	Akihutubia Aeropagus 17:22-34	17:22-31	17:22-31	17:19-21 17:22a Hotuba ya Paulo Mbele ya baraza La Aeropagus 17:22b-23 17:24-28
17:28b-31				17:29 17:30-31
17:32-34		17:32-34	17:32-34	17:32-34

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("[A Guide to Good Bible Reading](#)")

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

Maelezo mafupi ya ujumbe wa Paulo kwa wasomi wa Kiyunani huko (1 7:1 5-34). Yanafanana na yale ya Matendo 1 4:1 5-1 8.

- A. kuna Mungu mmoja, muumba wa mbingu (roho) na nchi (maada)
  - 1. Ambaye ndani mwao hawamjui
  - 2. Asiye ishi katika hekalu la binadamu au ibada ya sanamu
  - 3. Asiye hitaji kitu chochote toka kwa mwanadamu
  - 4. Yeye ndiye chanzo cha maisha ya kweli
- B. yuko na mamlaka juu ya historia ya mwanadamu
  - 1. akayafanya mataifa yote toka kwa mtu mmoja
  - 2. Akaweka mipaka ya mataifa
- C. ameweka shauku ndani ya mwanadamu kumjua Yeye, na si mgumu kupatikana
  - 1. alijifanya kama hazioni dhambi zile nyakati za ujinga
  - 2. Lazima tutubu
- D. ataihukumu misingi yake
  - 1. ameweka siku ya hukumu
  - 2. hukumu itatolewa na Masihi
  - 3. huyu Masihi aliinuliwa toka katika wafu kuithibitisha nafsi na kazi yake

## Mji wa Thesolanike

- A. Historia fupi ya Thesalonike
  - 1. Thesalonike ulikuwa ni mji ulioko katika Ghuba ya Termaiki. Thesalonike ulikuwa ni mji wa Pwani kupitia Ignatia (njia kuu ya mataifa) barabara kuu ya Kirumi, ikitokea Mashariki wa Rumi. Ulikuwa ni mji wa bandari, pia ulikuwa karibu sana na uwanda wa Pwani, wenye utajiri na wenye kustawi vizuri. Hizi faida tatu ziliufanya mji wa Thesalonike kuwa mji mkubwa, kituo kikubwa cha kibiashara na siasa huko Makedonia..
  - 2. Thesalonike mwanzoni kabisa ulijulikana kam Terma, jina hili lilitokana na chemichemi zilizotoa maji ya moto katika eneo hili. Mwanahistoria wa kale, Pliny wa umri mkubwa, anairejea miji ya Terma na Thesalonike kama ilikuwa pamoja. Kama hii ndiyo sababu, hivyo basi mji wa Thesolanike uliuzunguka mji wa Terma na kuumiliki (Leon Morris, *The First and Second Epistles to the Thessalonians*, Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1 991 , p. 1 1 ). Bado wana historia wanaamini kuwa Cassanda, mkubwa mmoja wa Iskanda Mkuu, aliitwa jina la Terma katika Mwaka wa 315 k.k. baada ya binti wa Filipo aliyeshi Makedonia na dadaye Iskanda na mkewe, Wathesalonike (Strabo VII Fragment 21 ). Wakati mwingine kipindi cha mwanzo cha kuueneza Ukristo, Thesalonike ilikuja kujulikana kwa jina “mji wenye imani halisi” kwa sababu ya tabia zake za Kikristo (Dean Farrar, *The Life and Work of St. Paul*, New York: Cassell and Company, Limited, 1 904, p. 364). Leo hii Thesalonike unajulikana kama Salonika na bado ni mji maarufu huko Ugiriki.
  - 3. Thesalonike ulikuwa ni mji wa kimataifa kama ulivyo Korinto, wenye wakazi toka pande zote za Dunia.
    - a. Watu washenzi wa Kijerumani toka Kaskazini waliishi huko, wakiendesha dini zao za kipagani na tamaduni.
    - b. Wayunani waliishi huko, wakitokea Akaia kuelekea Kusini na toka kwenye visiwa vya bahari ya Aegea, waliporudi wakaleta mabadiliko na falsafa.
    - c. Warumi toka Magharibi pia walikaa huko. Kwa kiasi kikubwa walikuwa ni wale wanajeshi waliostaafu na kuleta nguvu zao za utashi, mali, na siasa.
    - d. Mwishowe, Wayahudi wakaja kwa wingi toka Mashariki; baadaye moja ya tatu wa ya idadi ya watu walikuwa ni Wayahudi. Wakaleta imani yao ya kimaadili ya uwepo wa Mungu mmoja na madhara yao ya kitaifa.
  - 4. Thesalonike, ukiwa na idadi ya watu wapatao 200,000, kweli ulikuwa mji wa kimataifa. Ulikuwa ni kituo cha uchaguzi na kituo cha afya kwa sababu ya chemichemi zake za maji ya moto. Ulikuwa mji na kibiashara kwa sababu ya bandari yake, ukiwa na uwanda wenye rutuba na ukaribu wa njia ya Ignatia

5. Kama mji mkuu na wenye ukubwa, Thesalonike ulikuwa ni mji wa makao makuu ya kisiasa huko Makedonia. Ukiwa ni mji mkuu wa jimbo la Warumi na makao ya raia wengi wa Kirumi (hasa wanajeshi waliostaafu), ukaja kuwa mji huru. Wathesolanike hawakulipa ushuru na mji uliendeshwa na sheria za Kirumi, kwa vile wengi wa Wathesolanike walikuwa ni raia wa Kirumi. Kwa hiyo watawala wa kithesolanike waliitwa "politarchs." Cheo hiki hakikuweza kutokea mahali popote katika fasihi, lakini kimehifadhiwa kwa maneno ya kale ya kiushindi juu yake huko Thesalonike yajulikanyo kama Vardar Gate (Farrar, uk.371 n.).
- B. Matukio muhimu ya ujio wa Paulo huko Thesalonike
1. Matukio mengi yalimwongoza Paulo kwenda Thesalonike, tofauti na hayo matukio ya kimwili ndio aliyalenga, wito maalum wa ki-Mungu. Mwanzoni kabisa Paulo hakupanga kulitembelea bara la Ulaya. Shauku yake juu ya safari ya pili ya umisioanari ilikuwa ni kuyatembelea makanisa ya Asia Ndogo ambayo aliyaanzisha kwenye safari yake ya kwanza baadaye na kurudi sehemu za Mashariki. Muda ulipowadia wa kwenda kasikazini, Mungu akaanza kufunga milango. Matokeo ya hili ni wakati Paulo akiona maono huko Makedonia (kama vile Mdo. 1 6:6-1 0). Hii ilisababisha vitu viwili vitokee: kwanza, bara la Ulaya lilihubiriwa kwa injili na pili, Paulo, kwa sababu ya matukioa Fulani Fulani huko Makedonia, akaanza kuandika nyaraka zake (Thomas Carter, *Life and Letters of Paul*, Nashville: Cokesbury Press, 1 921 , p. 1 1 2).
  2. Sababu ya vitu vilivyo msababisha aende huko Thesalonike
    - a. Paulo alikwenda Filipi, mji mdogo usio na Sinagogi. Kazi yake huko ilizuiwa na mmiliki wa binti mtumwa wa "kinabii" mwenye mapepo na baraza la mji. Paulo alipigwa na kudhalilishwa, lakini bado kanisa lilianzishwa. Kwa sababu ya upinzani uliokuwepo na adhabu za kimwili, Paulo alilazimishwa kuondoka, yumkini mapema kuliko vile alivyokusudia.
    - b. Alikwenda wapi baada ya kutoka hapa? Alipitia Amfipoli na Afolonia, ambapo pia hapakuwepo na Sinagogi
    - c. Akafika kwenye mji mkubwa wa eneo, Thesalonike, ambao ulikuwa na Sinagogi. Paulo alikuwa amekwisha kuweka mkakati wa kuwafikia Wayahudi wa mahala kwanza. Alilifanya hili kwa sababu
      - 1) maarifa yao juu ya Agano la Kale;
      - 2) muda wa kuwafundisha na kuwahubiri kile Sinagogi walikwisha kukipokea;
      - 3) nafasi yao kama watu waliochaguliwa, watu wa agano la Mungu (kama vile Mt. 1 0:6; 1 5:24; Rum. 1 :1 6-1 7; 9-1 1 );
      - 4) Yesu alivyojitolea mwenyewe kwanza kwao, baadaye ulimwenguni—pia sisi, Paulo angalifuata mfano wa Kristo.

## Wenzake na Paulo

- A. Paulo aliambatana na Sila na Timotheo huko Thesalonike. Luka alikuwa na Paulo huko Filipi na akabaki huko. Tunajifunza haya kwa maneno "sisi" na "wao" katika Matendo ya mitume 16 na 17. Luka anazungumzia neno "sisi" huko Filipi, lakini "wao" kama walivyosafiri kwenda Thesoalnikie.
- B. Sila, au Silvanus, alikuwa ni mtu Paulo alimchagua kwenda nae katika safari ya pili ya umisionari baada ya Barnaba na Yohana aitwaye Marko aliporudi huko Kilikia.
  1. ni wa kwanza kutajwa katika Biblia kwenye Mdo. 1 5:22, ambapo aliitwa mtu mkubwa kati ya ndugu katika kanisa la Yerusalem.
  2. Pia alikuwa ni nabii (kama vile Mdo. 1 5:32).
  3. Alikuwa raia wa Kirumi kama Paulo (kama vile Mdo. 1 6:37).
  4. Yeye na Yuda Barsaba walitumwa Antiokia na kanisa la Yerusalem kupeleleza mazingira (kamavile Mdo. 1 5:22,30-35).
  5. Paulo alimsifia katika 2 Kor. 1 :1 9 na kumtaja katika barua zake mbali mbali.
  6. baadaye anatambuliwa na Petro katika maandiko ya 1 Petro (kama vile 1Petro 5:12)
  7. Wote Paulo na Petro walimwita Silvanus wakati Luka alimwita Sila.
- C. Timotheo alikuwa mwenziwe na mtenda kazi mwenza na Paulo
  1. Paulo alikutana naye Listra, mahali alipoongoka kwenye safari yake ya kwanza ya umisionari.

2. Timotheo alikuwa nusu Myunani (baba) na nusu Myahudi(mama). Paulo alihitaji kumtumia ili kuwahubiri watu wa mataifa.
  3. Paulo alimtahiri ili kwamba aweze kutenda kazi na Wayahudi.
  4. Timotheo ametajwa kwenye salamu katika 2 Wakorinto, Wakolosai, 1 na 2 Wathesolanike na Filemoni.
  5. Paulo alimtaja Yeye kama ni“mwana katika huduma” (kama vile 1 Tim. 1 :2; 2 Tim. 1 :2; Tito 1 :4).
  6. Asili ya Paulo kote katika nyaraka zake alidokeza kuhusu Timotheo kuwa mdogo na mtu mwenye aibu. Lakini bado Paulo alikuwa na imani naye na kumwamini (kama vile Mdo. 1 9:27; 1 Kor. 4:1 7; Fil. 2:1 9).
- D. Hili linafaa kwenye kipengere juu ya wenzake na Paulo waliotajwa wakaandaliwa watu walioingia Thesalonike na wakaambatana na Paulo kwenye safari yake ya umisheni. Walikuwa ni Aristarko (Mdo. 1 9:29; 20:4;27:2) na Sekundo (Mdo. 20:4). Pia, Dema inawezekana naye alikuwa wa Thesalonike (Filemon 24; 2Tim. 4:1 0).

## Huduma ya Paulo ndani ya Mji

- A. Huduma ya Paulo huko Thesalonike ilifuata mwongozo wake wa kawaida wa kwenda kwanza kwa Wayahudi na baadaye kurudi kwa mataifa. Paulo alihubiri katika masinagogi juu ya Sabato tatu. Ujumbe wake ulikuwa ni juu ya “Yesu ni Masihi.” alitumia maadiko ya Agano la Kale kuonyesha kuwa Masihi ilimpasa kuteseka (kama vile Mwa. 3:1 5; Isa. 53), na sio Masihi wa muda wa kisiasa. Pia Paulo alisisitiza ufufuko na kutoa wokovu kwa wote. Yesu kwa uwazi mkubwa aliletwa kama Masihi aliyeahidiwa toka zamani atakaye waokoa watu wote
- B. Jawabu la ujumbe huu ulikuwa kwamba baadhi ya Wayahudi, wale wa mataifa wenye kumcha Mungu, na wanawake wengi muhimu walimkubali Yesu kama Bwana na Mwokozi wao. Uchunguzi wa haya makundi ya wale walioongoka ni ya maana katika kuzielewa nyaraka zilizoletwa baadaye katika kanisa hili.
- C. Watu wa mataifa walijuisa wengi wa washirika wa kanisa, kama ilivyoonekana kukosekana kwa vidokezo kwenye Agano la Kale katika mojawapo ya zile nyaraka mbili. Mataifa tayari walikuwa wamekwisha kumkubali Yesu kama mwokozi na Bwana kwa sababu mbali mbali.
  1. Dini zao za kitamaduni hazikuwa na miiko ya nguvu. Mji wa Thesalonike upo chini ya Mlima Olimpasi na wote walijua haukuwa mrefu.
  2. Injili ilikuwa ya bure kwa wote.
  3. Ukristo haukuwajumuisha wale wote waliokuwa na utaifa wa Kiyahudi. Dini ya Kiyahudi iliwavutia wengi kwa sababu ya imani yao ya Mungu mmoja na maadili yao, lakini ilipingana na wengi kwa sababu ya sherehe zao zilizokuwa na migongano (kama vile tohara), na asili ya kijamii na athari za kitaifa.
- D. Wengi wa "wanawake wenye vyeo" waliukubali Ukristo kwa sababu ya ya uwezo wa wanawake hawa kuchukua uwamuzi wao wa kuchagua dini waipendayo. Wanawake zaidi walikuwa huru huko Makedonia na Asia Ndogo kuliko wale waliobaki kwenye ulimwengu wa dola ya Wagiriki-Warumi (Sir Wm. M. Ramsay, *St. Paul the Traveler and Roman Citizen*, New York: G.P. Putnam's Sons, 1 896, uk. 227). Bado wale wanawake wasio na uwezo, ingawa walikuwa huru, lakini bado walikuwa chini ya udhibiti wa mila na imani ya kuabudu miungu wengi (Ramsay, uk. 229).
- E. wengi wamepatikana na matatizo ya muda mrefu yaliyomfanya Paulo asalie Thesalonike:
  1. Mdo. 1 7:2 inamwongelea Paulo akihojiana nao ndani ya Sinagogi juu ya Sabato tatu akiwa huko Thesalonike.
  2. 1 The. 2:7-1 1 inatambua kuhusu biashara ya Paulo, alikuwa mtengeneza mahema au kama wengine walivyodai kuwa alikuwa akichakata ngozi
  3. Fil. 4:1 6 inakubaliana na ukazi wa muda mrefu, pele Paulo alipopokea msaada wa kifedha toka kanisa kanisa la Filipi pindi akiwa Thesalonike. Umbali kati ya miji hii miwili yapata miili 100. Wengine wanadai kuwa Paulo alikaa huko kwa muda wa miezi miwili au mitatu na kwamba ile Sabato tatu inarejelea tu kwenye huduma ya Wayahudi (Shepard, uk. 1 65).
  4. Maelezo tofauti juu ya wale walioongoka katika Mdo. 17:4 na 1 The. 1 :9 na 2:4 yanakubaliana na maoni haya, tofauti muhimu katika maelezo ni kule kukataliwa kwa ibada ya sanamu na wale wa

mataifa. Wale watu wa Mataifa wa Matendo walikuwa ni Wayahudi waliobadili itikadi na tayari walikuwa wamekwisha ondoka kwenye ibada ya sanamu. Mukadha unamdokeza Paulo kuwa angaliweza kuwa na huduma kubwa kati ya Wamatifa wapagani kuliko Wayahudi.

5. Ni lini huduma kubwa iliweza kuwepo haijulikani kwa vile Paulo mara zote alikwenda kwa Wayahudi kwanza. Baada ya kuukataa ujumbe wake, akawageukia watu wa mataifa. Walipoitikia injili kwa wingi, Wayahudi wakaona wivu na kuanzisha ghasia ndani ya makundi ya mji.
- F. kwa sababu ya ghasia Paulo alitoka nyumbani mwa Yasoni na kujificha pamoja na Timotheo na Sila, ingawa hawakuwepo wakati kundi la watu walipoichoma nyumba ya Yasoni wakiwatafuta wao. Gavana wa mji alisababisha Yasoni kuweka mdhamana wa ulinzi kuhakikisha kunakuwepo na amani. Hii ilimsababisha Paulo kuondoka kwenye mji wakati wa usiku na kwenda huko Berea. Ingawa, kanisa liliendelea kumshuhudia Kristo machoni pa upinzani mkubwa.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 17:1-9

<sup>1</sup> Wakiisha kupita kati ya Amfipoli na Apolonia wakafika Thesalonike, ambapo palikuwa na sinagogi la Wayahudi. <sup>2</sup> Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa maneno ya maandiko sabato tatu, <sup>3</sup> akiyafunua na kuwaeleza ya kwamba ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu; na ya kwamba, Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari zake ndiye Kristo. <sup>4</sup> Wengine miongoni mwao wakaamini, wakashikamana na Paulo na Sila; na Wayunani waliomcha Mungu, wengi sana, na wanawake wenye cheo si wachache. <sup>5</sup> Na Wayahudi wakaona wivu, wakajitwalia watu kadha wa kadha katika watu ovyo wasio na sifa njema, nao wakakutanisha mkutano, wakafanya ghasia mjini, wakawaenda watu wa nyumba ya Yasoni, wakataka kuwapeleka mbele ya watu wa mji; <sup>6</sup> na walipowakosa, wakamkokota Yasoni na baadhi ya ndugu mbele ya wakubwa wa mji, wakipiga kelele, wakisema, Watu hawa walioupindua ulimwengu wamefika huku nako, <sup>7</sup> na Yasoni amewakaribisha; na hawa wote wanatenda mambo yaliyo kinyume cha amri za Kaisari, wakisema na kwamba yupo mfalme mwingine, aitwaye Yesu. <sup>8</sup> Wakafadhaisha ule mkutano na wakubwa wa mji walipoyasikia hayo. <sup>9</sup> Nao walipokwisha kumtoa dhamana Yasoni na wenziwe wakawaacha waende zao.

**17:1 "Wakiisha kupita Amfipoli na Apolonia"** Miji hii miwili ilikuwa kwenye njia kuu iendayo Rumi, njia ya Ignatia (yaani., njia ya mataifa), barabara kuu Magharibi mwa Mashariki yapata maili 500. Inayounganisha sehemu za Mashariki na Magharibi mwa himaya na ambayo inatengeneza mtaa mkubwa wa Thesalonike.

▣ **"Thesalonike"** Angalia utangulizi kwenye sura hii.

▣ **"Ambapo palikuwa na Sinagogi"** Haya yalikuwa ni maelezo ya Paulo na mwendelezo wa tangazo (kama vile Mdo.1 7:2; 3:26; 1 3:46; Rum. 1 :1 6; 2:9,1 0; Mdo. 9:20; 1 3:5,1 4; 1 4:1 ; 1 7:2,1 0,1 7; 1 8:4,1 9; 1 9:8), yumkini kwa sababu alifikiri injili ilikuwa kwanza kwa ajili ya Wayahudi (kama vile Rum. 1 :1 6) kwa sababu ya unabii wa Agano la Kale. Pia, wengi wa wacha Mungu walihudhulia, wakalifahamu, na kuliheshimu Agano la Kale.

**17:2 " sabato tatu, "** Kwa maana hiyo aliongea ndani ya Sinagogi tu kuhusu Sabato tatu. Yumkini alikuwa ndani ya mji zadi ya wiki tatu (kama vile Fil. 4:1 6), lakini sio kwa kipindi kilichotarajiwa.

▣ **"akahojiana nao kwa maneno ya maandiko "** Paulo alilinganisha nabii za ki-Masihi na mafundisho ya maisha ya Yesu, kifo, na ufufuo. Aliyachukua maelezo haya toka kwa Stefano (Matendo 7) na toka kwenye mafunzo yake ya sheria za Kiyahudi.

**17:3**

**NASB" akiwaelezea na kuwapa ushahidi"**

**NKJV"akiwaelezea na kuyafunua"**

## NRSV,NJB"akiwaelezea na kuwathibitishia"

### TEV"akiwaelezea maandiko, na kuyathibitisha kwao"

Neno la kwanza ni *dianoigō*, lililotumia na Yesu alipowafungua maandiko wale wawili waliokuwa wakienda Emau (kama vile Luka 24:32,45). Pia lilitumiwa na Yesu alipowafungua macho ili kwamba wapate kumtambua Yeye (kama vile Luka 24:31 ). Neno hili hili lilitumiwa katika Mdo.1 6:1 4 kwa ajili ya Mungu alipoufungua moyo wa Lidia apate kuelewa injili. Neno la pili , *paratithēmi*, limetumika mara nyingi kwenye maandiko ya Luka kwa ajili ya kumwekea mtu chakula, lakini hapo panamaanisha “kuuweka ukweli wazi” au “kumsifu (kama vile Mdo. 1 4:23; 20:32). Mara mbili katika Luka (kama vile Luka 1 2:48; 23:46) limetumika kwa ajili ya kuwaaminisha watu kitu. Paulo kwa uangarifu mkubwa aliwapa injili wale waliosikia (yaani., kuwekeza, *parathēkē*, 1 Tim. 6:20; 2 Tim. 1 :1 2,1 4). Baadhi walikubali (baadhi Wayahudi, baadhi wacha Mungu, na wengi walikuwa wanawake wenye vyeo).

▣ **"ilimpasa Kristo kuteswa"** Neno "ilimpasa" (*dei*) ni kauli isiotimilifu tendaji elekezi, inayodokeza uhitaji (angalia maelezo kamili katika Mdo. 1 :1 6). Masihi mwenye kuteswa alitabiriwa katika Agano la Kale (kama vile Mwa. 3:1 5; Zab. 22; Isa. 52:1 3-53:1 2; Zak. 1 2:1 0), lakini hakuwahi kuonwa na walimu wa dini. Kwa nguvu neno hili lilitetewa na wahubiri wa kitume (kama vile Luka 24:46; Mdo. 3:1 8; 26:23; 1 Pet. 1 :1 0-1 2). Ukweli huu ulikuwa ni kikwazo kwa Wayahudi (kama vile 1 Kor. 1 :22-23). Angalia maelezo katika Mdo. 3:1 8.

▣ **"na kufufuka toka katika wafu"** Hiki ni kigezo kinachojulikna kwenye hotuba zote za Petro, Stefano, na Paulo katika Matendo (sehemu ya *kerygma* (mafundisho), angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:1 4). Ni nguzo muhimu ya injili (kama vile 1 Wakorinto 15).

▣ **"Huyu Yesu ninayemtangaza kwenu ndiye Kristo"** Kuna tofauti nyingi katika machapisho ya Kiyunani kwenye maneno ya mwisho ya sentensi hii.

1. "Kristo, Yesu" – MS B
2. "Kristo, Yesu" – baadhi ya tafasiri za Kilatini na Coptic
3. " Kristo Yesu" – MSS P<sup>74</sup>, A, D
4. "Yesu Kristo" – MS  $\kappa$
5. "Yesu ambaye ni Kristo" –toleo la MS E na Bohairic Coptic
6. "ambaye ni Kristo" –toleo la Georgian

Wasomi wengi wanachagua mstari wa #1 (Vaticanus)kwa sababu sio wa kawaida (toleo la UBS4 linatupatia alama "C" katika kuipima). katika muundo huu wa Sinagogi neno “ambaye ni Kristo” lingalimaanisha yule mpakwa mafuta aliyeahidiwa katika Agano la Kale:wafalme, manabii, wachungaji. Yesu anatimiliza kazi zote tatu (kama vile Ebr. 1 :1 -3). Huu utiwaji mafuta ilikuwa ni alama ya uchguzi wa Mungu na uwezeshaji kazi ya huduma. Angalia **MADA MAALUM: KUTIWA MAFUTA KATIKA BIBLIA (BDB 603)** katika Biblia kwenye Mdo. 4:27. Kanisa la mwanzo linakubaliana tena na tena kuwa Yesu wa Nazareti alikuwa Masihi aliyeahidiwa (kama vile Mdo. 2:31 -32; 3:1 8; 5:42; 8:5; 9:22; 1 7:3; 1 8:5,28), kufuatana na uthibitizo uliojirudia na wa wazi wa Yesu mwaneyewe.

**17:4 "Wakashikamana"** Kitenzi cha Kiyunani (kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu) kinapatikana hapa tu katika Agano Jipya. Kiuhalisia kinamaanisha "kuteuwa kwa kupiga kura." Katika muktadha huu kinadokeza "kuwafuata" au "kuambatana nao." "upigaji kura" ilikuwa ni njia ya Agano la Kale ya kujua mapenzi ya Mungu.

Ni maana ya

1. kivumishi (*pros*)
2. Mzizi (*klēpoō*)
3. Irabu sauti tendwa inadokeza kitendo cha Uungu

Mungu akaifungua mioyo yao kama alivyofanya kwa Lidia (kama vile Mdo. 1 6:24; pia tambua mawazo mfanano katika 1 Pet. 5:3).

▣ **"Wayunani waliomcha Mungu"** Palikuwepo na wafuasi wa dini ya Kiyahudi ambao walikuwa bado hawajaongoka kikamilifu, kulikohusiana na

1. Kutahiriwa
2. Ubatizo wa mtu



### 3. Kutoa dhabihu hekaluni ikiwezekana huko Yerusalem

▣ **"wengi sana"** Huu ni mfano mwingine wa matumizi ya Luka ya neno *litotes* (kutoa maelezo yasiyo kamili ya kimakusudi, kama vile Mdo.1 2:1 8; 1 5:2; 1 9:1 1 ,23,24; 20:1 2; 26:1 9,26; 27:20; 28:2), mara nyingi katika mtindo wa kukanusha . hapa kiuhalisia kifungu ni "hawakuwa wachache," kilichowekwa mwishoni mwa sentensi kwa ajili ya msisitizo.

▣ **"wanawake si wachache"** Wanawake walikuwa na uhuri mkubwa huko Makedonia (Lidia) kuliko sehemu nyingine yeyote ile ya ulimwengu wa Mediterania. Maelezo yanaonyesha huko Pisidia Antiokia palikuwa pakijirudia (kama vile Mdo. 1 3:43,45,50). Machapisho ya Kiyuani ya familia za ki-Magharibi yanaongeza kifungu katika Mdo. 17:4 kinachodai kuwa hawa wanawake walikuwa na wake wa viongozi.

**17:5 "Wayahudi wakaona wivu"** Wayahudi wasioamini wananisikitisha (kama vile Mdo. 1 4:2), lakini kuwa na wivu (kama vile Mdo.5:1 7) ni sikitiko! Hawa hawakuwa wamevutiwa na ari ya kidini kama Sauli, lakini wakaona wivu! Idadi ya wale walioongoka (kama vile Mdo. 1 3:45), na sio maudhui ya mahubiri, ndicho kilicho waudhi. Luka aliwatumia "Wayahudi" mara nyingi kinyume, kwa maana ya kukashifu (kama vile Mdo. 1 2:3; 1 3:45; 1 4:2; 1 7:1 3), kama alivyofanya Paulo (kama vile 1 The. 2:1 5-1 6). Wakafanana na wale waliopinga na kuikataa injili!

**NSB" watu wasio na sifa njema"**

**NKJV" watu waovu wasio na sifa njema"**

**NRSV" watu wagomvi ndani ya mji"**

**TEV" wahuni toka mitaani"**

**NJB" majambazi ndani ya mji"**

Neno hili linaelezea yule azururaye mtaani pasipo kufanya kazi, mvivu asiyejibidisha.

▣ **"watu kadha wakadha"** Neno hili linapatikana hapa tu katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania. "kundi la watu" ni maana iliyotumika kimuktadha. Luka alikuwa ni mtu msomi mwenye maneno mengi (yaani., kitabibu, kibaharia, etc.).

**17:6 "wakamkokota Yasoni"**Baadhi wanabashiri kuwa Yasoni aliyetjwa katika Rum. 16:21 ni yule yule , lakini haijulikani.

▣ **"na baadhi ya ndugu"** Muundo huu unaonyesha kuwa Yasoni bado hakuwa mwamini. Haswa ni namna gani Yasoni alikuwakaribisha wale Wamisionari haijulikani. Yawezekana kuwa

1. Paulo au Sila walifanya kazi kwa ajili yake
2. walikodi nafasi kwa ajili yake
3. Walikaa nyumbani kwake

kitenzi "karibu" katika Mdo. 1 7:7 kinamaanisha "kumpokea mgeni" (kama vile Luka 1 0:38; 1 9:6; Yakobo 2:25).

▣ **"wakubwa wa mji"** Neno hili "wakubwa wa mji" lilimaanisha viongozi wa muda. Hili lilikuwa jina maalum kwa ajili viongozi wa serikali ya mtaa huko Makedonia. Ni neno adimu, lililotumika hapa tu na katika Mdo.17:8 katika Agano la Kale, au katika fasihi ya Kiyunani na matumizi yake yanaonyesha maarifa ya Luka ya eneo husika na kuunga mkono wanahistoria wa Matendo ya Mitume (NASB Study Bible, uk. 1 607, lakini neno limepatikana katika maneno ya Kiyunani juu ya tao kwenye njia ya Ignatia huko Thesalonike ) . Luka alikuwa ni mwana historia sahihi wa umri pindi wakati hili likiwa adimu. Alikuwa na agenda ya imani, ambayo waamini walithibitisha kuwa kama

**NASB" waliousumbua ulimwengu"**

**NKJV, NRSV**

**NJB" walioupindua ulimwengu"**

**TEV" waliosababisha machafuko kila mahali"**

Hili linadokeza hukumu juu ya uhaini (kama vile Mdo. 21 :38; pia tambua 1 6:20; 24:5). Hili ni neno lenye nguvu. Tambua Paulo analitumia katika Gal. 5:1 2. Tunajua toka katika 1 The. 2:1 4-1 6 kuwa kanisa lilipata misukosuko mingi. Walitambua juu ya kuenea kwa huu mgawanyiko mpya wa dini ya Kiyahudi.

**17:7 "amri za Kaisari"** Baadhi wanafikiri hili linahusiana na Klaudio' (mwaka 41 -54 b.k) tamko la mwaka 49-50 b.k, ambapo ilikatata ibada za dini za Kiyahidi huko Rumi. Tamko hili, matokeo yake, lilisababisha idadi ya Wayahudi huko Rumi kuondoka. Hata hivyo, nafikiri muktadha uko wazi kwamba unarejelea kwenye mahubiri ya injili. Ilikuwa ni kosa kwa mtu yeyote kumbadili dini Mrumi.

▣ **"wakisema kwamba yupo mfalme mwingine aitwaye Yesu"** Hukumu hii ni kwa sababu ya

1. msisitizo mzito wa Paulo juu ya matukio ya siku ya hukumu kwenye mahubiri yake huko Thesalonike
2. Maneno yaliyotumiwa na Wakristo kwa ajili ya Yesu yanafanana nay ale yaliyotumiwa na Warumi kwa Kaisari (mfalme, bwana, na mwokozi)

**17:8**

**NASB, TEV "wakubwa wa mji"**

**NKJV "watawala wa mji"**

**NRSV "wakuu wa mji"**

**NJB "washauri wa mji"**

Hili ni neno la Kiyunani *politarchs*, ambalo ni ajili ya wale waliochaguliwa kila mwaka kwenye mji wa Makedonia. Hawakuwa Warumi bali ni viongozi wa maeneo (AB, juzuu ya. 5, kur. 384-389).

**17:9 "wakamtoza"** Yumkini hii ilikuwa dhamana kubwa ya kifedha iliyowekwa na wale walioongoka karibuni (kama vile Mdo. 1 7:4,6,1 0), kuhakikisha kuwa Paulo hakuendelea kuhubiri ndani ya mji. Wengine wanalihusianisha hili na 1 The. 2:1 8.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 17:10-15**

<sup>10</sup> Mara hao ndugu wakawapeleka Paulo na Sila usiku hata Beroya. Nao walipofika huko wakaingia katika sinagogi la Wayahudi. <sup>11</sup> Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo. <sup>12</sup> Basi watu wengi miongoni mwao wakaamini, na wanawake wa Kiyunani wenye cheo, na wanaume si wachache. <sup>13</sup> Lakini Wayahudi wa Thesalonike walipopata habari ya kwamba neno la Mungu linahubiriwa na Paulo hata katika Beroya, wakaenda huko nako wakawachafua na kuwafadhaisha makutano. <sup>14</sup> Mara hiyo wale ndugu wakampeleka Paulo aende zake mpaka pwani; bali Sila na Timotheo wakasalia huko. <sup>15</sup> Lakini wale waliomsindikiza Paulo wakampeleka mpaka Athene; nao wakiisha kupokea maagizo kuwapeleka Sila na Timotheo, ya kwamba wasikawie kumfuata, wakaenda zao.

**17:10 "Beroya"** Huu ulikuwa ni mji mkubwa katika siku za Paulo yapata maili 60 Magharibi, karibia na njia kuu ya Ignatia. Pia ulikuwa na jamii ya Wayahudi, mmoja aliyekubali kumsikiliza Paulo na kuithibitisha thiolojia toka kwenye maandiko aliyo yarejea toka Agano la Kale.

▣ **"wakaingia katika Sinagogi la Wayahudi"** Andiko linadokeza kuwa mara tu walipoingia, hata baada ya safari ndefu, mara moja wakaenda ndani ya Sinagogi. Yawezekana ilitokea kuwa siku ya Sabato au yawezekana walifahamu wangelifuatwa na wale waliopinga. Muda ulikuwa ni wa muhimu. Waamini wa leo wa kimagharibi tayari wamekwisha kupoteza uwakala na kipaumbele cha uinjilisti!

**17:11 "walikuwa waungwana"** Hili neno lilitumika kwa watu wenye mali, wenye elimu, watu wa daraja la juu (kama vile LXX Ayubu 1 :3; Luka 1 9:1 2). Haya maelezo ya wazi hayakuweza kuwafaa Wayahudi wa Berea; kwa hiyo, ni kwa namna ya kiistiari kwa ajili ya mtu anayependa kusikia mawazo mapya na kuyapima. Mawazo haya mapya yangewamaanisha wale wakazi walioongoza ndani ya mji waliokuwa wakiabudu ndani ya Sinagogi (kama

vile Mdo. 1 7:1 2).

▣ "**wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo**" Hii ndiyi njia ya kuupima ukweli. Mbinu za mahubiri ya Paulo zilikuwa ni za kurejea Agano la Kale na kuonyesha ni kwa namna gani lilitumika kwa Yesu. Kifungu ("ikiwa mambo haya yalikuwa hivyo") yanajumuisha sentensi yenye masharti daraja la nne ikiwa na dhamira ya uchaguzi, kama vile Mdo. 1 7:27; 20:1 6; 24:1 9; 27:1 2), inayodokeza kutengwa mbali na ukweli .

baadhi waliitikia; wengine walikataa (ajabu ya injili).

**17:12 "wengi wao wakaamini"** Hii inamaanisha kuwa wengi wa Wayahudi wa Sinagogi na wengi wa wale wacha Mungu, waliitikia. Angalia Mada Maalum katika Mdo. 3:1 6 na 2:40.

▣ "**wenye cheo**" Huu ni muunganiko toka kwa neno "ya kufaa" na "umbo" au "mwonekano." Lilitumika kwa watu wenye heshima, wenye sifa njema, na watu maarufu (kama vile Mdo. 1 3:50 na Yusufu wa Armataya, Marko 1 5:43).

**17:13** Hii inaonyesha ushindani wa kimakusudi wa wapinzani wa Kiyahudi wa Paulo. Wengi wao walikuwa Wayahudi waaminifu wakitenda nje ya sababu za kidini (kama Sauli aliyokuwa nayo). Hata hivyo, mbinu zao zinadhilisha aina ya kiroho chao kilivyo

**17:14 "mpaka Pwani"** Hili laweza kumaanisha

1. Paulo alisafiri kwenda Ethene kwa kutumia boti
2. Paulo alienenda na njia ya ya Pwani mpaka Ethene

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO 17:16-21**

<sup>16</sup> Paulo alipokuwa akiwangojea huko Athene na kuona jinsi mji ule ulivyojaa sanamu, roho yake ilichukizwa sana ndani yake. <sup>17</sup> Basi katika sinagogi akahojiana na Wayahudi na waliomcha Mungu, na wale waliokutana naye sokoni kila siku. <sup>18</sup> Na baadhi ya Waepikureo na Wastoiko, wenye ujuzi, wakakutana naye. Wengine wakasema, Mpuzi huyu anataka kusema nini? Wengine walisema, Anaonekana kuwa mtangaza habari za miungu migeni, kwa maana alikuwa akihubiri habari za Yesu na ufufuo. <sup>19</sup> Wakamshika, wakamchukua Areopago, wakisema, Je! Twaweza kujua maana ya elimu hii mpya unayoinena? <sup>20</sup> Kwa maana unaleta mambo mageni masikioni mwetu, tutapenda kujua, basi, maana ya mambo haya. <sup>21</sup> Kwa maana Waathene na wageni waliokaa huko walikuwa hawana nafasi kwa neno lo lote ila kutoa habari na kusikiliza habari za jambo jipya.

**17:16 "Athene"** Huu ulikuwa ni mji mkubwa wa Ugiriki wenye urithi wa kitamaduni na bado ni kituo cha wasomi wa ulimwengu wa Kirumi. Ni mji uliosifika katika utamaduni, ushirikina, na uchafu wa kila aina.

▣ "**roho yake**" Machapisho ya herufi kubwa ya Kiyunani ya Agano Jipya hayana

1. nafasi kati ya neno na neno
2. Alama za kutenga maneno
3. Herufi kubwa (herufi zote ni kubwa)
4. Mstari na mugawanyo wa vifungu

Kwa hiyo, muktadha tu ndio unaweza kuamua hitaji kwa ajili ya herufi kubwa. Mara nyingi herufi zinatumiwa kwa ajili ya

1. majina ya Uungu
2. majina ya mahali
3. Majina ya watu

Neno "roho" laweza kurejelea

1. Roho Mtakatifu (kama vile Marko 1 :5)
2. Nafsi hai ya mwanadamu (kama vile Marko 8:1 2; 1 4:38)
3. Baadhi ya viumbe katika ulimwengu wa roho (yaani., mapepo, kama vile Marko 1 :23)

Katika muktadha huu inarejelea kwa Paulo kama mtu. kuna sehemu nyingi katika maandiko ya Paulo ambapo muundo wa kisarufi unatumika kuelezea kile ambacho Roho Mtakatifu anakiweka ndani ya mwamini mwenyewe

1. "sio roho wa utumwa," "roho ya uasilishaji, Rum. 8:1 5
2. "roho ya upole," 1 Kor. 4:21
3. "roho ya imani (uaminifu), 2 Kor. 4:1 3
4. "roho ya hekima na ufunuo," Efe. 1 :1 7

Ni wazi toka kwenye muktadha kuwa Paulo anatumia "roho" kama njia ya kujirejelea mwenyewe au watu wengine (1 Kor.2:1 1 ; 5:4; 2 Cor. 2:1 3; 7:1 3; Rum. 1 :9; 8:1 6; Fil. 4:23).

**NASB"ilichukizwa sana ndani yake"**

**NKJV"ilichukizwa ndani yake"**

**NRSV"ilihuzunika sana"**

**TEV"ilifadhaika sana"**

**NJB"ilichukizwa"**

Hii ni kauli tendwa elekezi isio kamilifu ya neno *paroxunō*, ambayo kimsingi inamaanisha "kuamusha," lakini hapa limetumika kitamathari "kuchochea." Hili ni neno (katika muundo wake wa jina) ambalo limetumika kuelezea ugomvi wa Paulo na Barnaba juu ya Marko, nduguye Yohana katika Mdo.15:39. Limetumika kwa namna chanya katika Ebr. 1 0:24.

**17:17** Paulo alihusika kwa wote Wayahudi ("wakihojiana ndani ya Sinagogi") na Watu wa mataifa, wale wote waliovutiwa na dini ya Kiyahudi (wacha Mungu) na wale wote waliokuwa wapagani wakiabudu sanamu ("wale wote waliokuwa maeneo ya sokoni"). Paulo aliyahutubia haya makundi mbali mbali katika njia tofauti: kwa watu wa mataifa na Wayahudi alitumia Agano la Kale, lakini kwa wapagani alijaribu kutafuta mazingira yanayofaa (kama vile Mdo. 17:22-31 ).

**17:18 "Wapekureo"** Kundi hili liliamini kuwa misukosuko au furaha ndio lilikuwa lengo la maisha. Waliamini hakuna mwili baada ya kufa. "yafurahiye maisha sasa" ulikuwa ndio wito wao (muundo wa kuweka imani katika anasa). Walishikilia kuwa miungu haihusiki na wanadamu. Walipata majina yao toka kwa mwanafalsafa Epicurus, wa huko Ethene, mwaka 341 -270 k.k, lakini walikuza hitimisho lao la msingi. Epicurus aliiona misukosuko kwa maana pana kuliko misukosuko ya kimwili (yaani., mwili wenye afya na fikra tulivu). "Epicurus anatajwa kuyasema haya, 'hata ukimfanya mtu akawa na furaha, usimwongeze chochote katika ustawi wake, bali mwondolee shauku yake'" (*The NewSchaff-Herzog Encyclopedia ofReligious Knowledge*, juzuu ya. IV, uk. 1 53).

▣ **"Wastoiko"** Kundi hili liliamini kuwa mungu alikuwa (1 ) nafsi ya ulimwengu au (2) kuwepo ndani ya uumbaji wote (kuabudu miungu wengi). Walidai kuwa mwanadamu lazima aishi kwa amani na asili iliyopo ( yaani., miungu). Sababu ilikuwa ni kuwa na ubora wa juu. Udhhibiti, utosherevu, na utulivu wa kimihemko katika kila hali lilikuwa ndilo lengo. Hawakuamini kuna maisha baada ya kufa. Mwasisi wao alikuwa Zeno, mwanafalsafa toka Kilikia, aliyehamia Ethene yapata miaka 300 k.k. walilipata jina lake kutokana na ukweli kwamba alifundisha michoro *stoa* huko Ethene.

▣ **"Mropokaji"** Neno hili lilitumika kwa ndege aina ya shorewanda wanaokula nafaka shambani. Lilikuja kuanza tumika ki-sitiari kwa walimu wanao zunguka huku na kule wakichukua kipande cha habari hapa na pale na kujaribu kukiiza. . The *R.S.V. Interlinear* by Alfred Marshall analitafasiri kama "wizi wa mawazo." Toleo la NJB lina neno "kuiga."

▣ **"mtangaza habari za miungu migeni"** Kiuhalisia hili neno "foreign *daimōn* " lililotumika kwa maana ya nguvu ya kiroho au miungu (kama vile 1 Kor. 1 0:20-21 ). Hawa wanafalsafa wa ki-Ethene walikuwa wabadili itikadi za kidini (waabudu miungu wengi wa kimabara).

1. Yawezekana hawa wanafalsafa wa Ethene walichukua maneno ya Paulo kama rejeo la miungu wawili (*Jerome Biblical Commentary*, juzuu ya. 2, uk. 1 99).
  - a. miungu ya afya
  - b. miungu ya ufufuo (yaani., Anastasia)
2. Yawezekana waliona mmoja kama
  - a. mwanaume (Yesu)
  - b. mwanamke (neni ufufuo ni nomino jinsi ya kike)
3. Msamiati wa injili wa Paulo (kama vile NET Bible) wenyewe wawezakuwa ni chanzo cha mkanganyiko wa uhusiano na Mungu mmoja katika nafsi tatu (yaani., Utatu, angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:32).
  - a. Baba
  - b. Mwana
  - c. Roho

▣ **"kwa maana alikuwa anahubiri habari za Yesu na ufufuo"** Kikwazo cha injili kwa Wayahudi kilikuwa "Masihi mwenye kuteseka" na kwa Wayunani ilikuwa ni "ufufuo" (kama vile 1 Kor. 1 :1 8-25). Maisha baada ya kifo cha nafsi, na mwili havikustahili ndani ya uelewa wa Wayunani kuhusu miungu au mwanadamu. Walidai nuru ya ki-Ungu kwa kila mtu, au iliyokamatwa ndani ya mwili wa asili. Wokovu ulikuwa ni ukombozi toka kwa mwili na kuingiza ndani ya nafsi isiyo na Uungu.

**17:19 "wakamshika, wakamchukua Areopago"** Neno *areopages* linamaanisha kilima cha Ares (mungu wa vita). Katika utaratibu wa Kirumi wa kuabudu miungu wengi, mungu wa vita alitwa Mars. Katika siku maridhawa za Waethene, ulikuwa ni mjadala wa kifalsafa wa mji wa wasomi uliojulikana. Hapakuwepo na kesi za kimahakama, bali ni mjadala wa wazi mbele ya baraza la viongozi wa mji. Huu ni mfano wa mahubiri ya Paulo kwa wapagani, kama ilivyokuwa 13:16 na kuendelea ilikuwa ni kwa wacha Mungu wa mataifa. Namshukuru Mungu kwa ajili ya mihtasari ya ujumbe

▣ **"je, twaweza kujuamaana yah ii elimu mpya unayoinena"** Hapa kuna tofauti kati ya udadisi wa kisomi (kama vile Mdo. 17:20-21 ) na ufunuo. Mungu ametuumba ili kuwa wadadisi (kama vile Mhubiri 1 :8-9,1 8; 3:1 0-1 1 ), lakini usomi wa mwanadamu hauwezi kuleta amani kati ya hekima za mwanadamu na ufunuo wa Mungu katika 1 Wakorinto 1-4.

**17:19-20** Maneno haya yana lugha ya upole kijamii. hili lilikuwa, katika maana muundo wa chuo kikuu.

**17:21** Huu mstari unaonekana kuwa ni maoni ya kiuandishi. Inaonyesha kuwa heshima ya Mdo. 1 7:1 9-20 hayakuwa ni maulizo ya kweli ya kisomi, bali ni mtindo wa kitamaduni wa sasa. Walifurahia kusikiliza na kujadili. Walikuwa wanajaribu kuamusha utukufu wa nyuma wa Ethene. Sikitiko hawakuweza kutofautisha kati hekima ya mwanadamu na ufunuo wa ki-Ungu.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):MATENDO 17:22-31**

<sup>22</sup> Paulo akasimama katikati ya Areopago, akasema, Enyi watu wa Athene, katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini. <sup>23</sup> Kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko na kuyaona mambo ya ibada yenu, naliona madhabahu iliyoandikwa maneno haya, KWA MUNGU ASIYEJULIKANA. Basi mimi nawahubirini habari zake yeye ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua. <sup>24</sup> Mungu aliyefanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono; <sup>25</sup> wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu cho chote; kwa maana ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote. <sup>26</sup> Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao; <sup>27</sup> ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone, ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu. <sup>28</sup> Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu. Kama vile mmoja wenu, mtunga mashairi alivyosema, Maana sisi sote tu

wazao wake.<sup>29</sup> Basi, kwa kuwa sisi tu wazao wa Mungu, haitupasi kudhani ya kuwa Uungu ni mfano wa dhahabu au fedha au jiwe, vitu vilivyochongwa kwa ustadi na akili za wanadamu.<sup>30</sup> Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu.<sup>31</sup> Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu.

**17:22 "watu wa kutafakari mambo ya dini"** Hii kiuhalisia ni "kuiogopa miungu (*daimōn*).\" Hili laweza kumaanisha (1 ) katika maana hasi, "miiko,\" kama ilivyo katika toleo la King James, au (2) kwa maana chanya, "dhahiri sana katika utendaji wa kweli ya kidini \" (NKJV, NJB kama vile Mdo. 25:1 9). Watu hawa walikuwa na udadisi wa kisomi na kuyaheshimu mambo ya kidini, lakini kwa kiwango fulani (desturi zao).

▣ **"nyote"** Tambua idadi ya hesabu katika hotuba hii kuwa Paulo alitumia neno "wote" lililojumuishwa au kifungu kinachofanana nacho

1. "heshima zote,\" Mdo. 1 7:22
2. "vitu vyote,\" Mdo. 1 7:24
3. "maisha yote na pumzi,\" Mdo. 1 7:25
4. "vitu vyote,\" Mdo. 1 7:25
5. "kila taifa,\" Mdo. 1 7:26
6. "vyote katika uso wa dunia,\" Mdo. 1 7:26
7. "kila mmoja wetu,\" Mdo. 1 7:27
8. "sisi\" (mara mbili\", Mdo. 1 7:28
9. Kila mahali,\" Mdo. 1 7:30
10. "ulimwengu\" (hasa dunia wanaoishi watu), Mdo. 1 7:31
11. "watu wote,\" Mdo. 1 7:31

habari njema za Paulo zilikuwa kwamba Mungu aliwapenda wanadamu wote (yaani., akawaumba kwa sura yake, kama vile Mwa. 1 :26-27) na ametoa njia kwao wapate kumjua (yaani., kusudi la asili la uumbaji lilikuwa kufanya ushirika na Mungu, kama vile Mwa. 3:8 na kusamehewa (yaani., toka matokeo ya anguko, kama vile. Mwanzo 3).

**17:23 "iliyoandikwa, 'kwa mungu asiyejulikana'"** Wayunani waliogopa wangaliweza kumsahau au wangeliweza kuiacha miungu yao muhimu ambayo ingaliwasababishia matatizo kama wangeliacha, kwa hiyo waliweka sanamu ya ukumbusho (kama vile Pausanias, *Description of Greece* 1 :1 :4 na Philostratus, *Life of Apollonius* 6:3:5). Inaonyesha hofu yao katika ulimwengu wa roho na ibada yao ya kuabudu miungu wengi.

▣ **" mnayemwabudu bila kumjua"** Kuna mchezo wa maneno hapa kati ya "asiyejulikana" (*agnōētō*) na "ujinga" (*agnoountes*). Tunapata neno la Kiingereza "mwenye kusadiki kuwa hatuna habari za Mungu" kutoka katika neno hili la Kiyunani . Paulo alikuwa anarekebisha uwasilishaji wa injili kwa wapani waliokuwa wakiamini katika ulimwengu usio rafiki wa nafsi.

▣ **"Ninayehubiri habari zake"** Paulo kwa wazi anadai kuwa yeye siyo "mtu wa kubwabwaja" (Mdo. 1 7:1 8) na kuwa anamjua Mungu wasiye mfahamu wao.

**17:24 "Mungu aliumba ulimwengu na vitu vyote vilivyomo"** Hoja ya kwanza ya Paulo kithiolojia ni kuwa Mungu ndiye muumbaji (kama vile Mwa. 1 -2; Zab. 1 04; 1 46:6; Isa. 42:5). Wayunani waliamini kuwa roho (Mungu) na maada (atomu) vyote ni vya milele. Paulo anadai dhana ya Mwanzo 1 ya uumbaji ilikuwa ni ya kibinafsi, kwa makusudi Mungu akaumba vyote mbingu na nchi (sayari na vyote vilivyomo).

▣ **"hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono "** Hii ni nukuu toka (1 ) Agano la Kale (kama vile 1 Fal. 8:27; Isa.66:1 -2) au (2) mwanafalsafa wa Kiyunani, Euripides, kipengere cha 968. Kuna rejeo mbali mbali katika

muktadha huu toka kwa waandishi wa Kiyunani (kama vile Mdo. 1 7:25; 28). Paulo pia alijifunza kwa wasomi wa Kiyunani.

**17:25 "kana kwamba anahitaji kitu chochote"** Mawazo ya kufanana kama haya yanapatikana (1 ) Euripides' *Heracles* 1 345f; (2) Plato's *Euthyphro* 1 4c; (3) Aristobula, kipengere cha 4; or (4) Zaburi 50:9-1 2. Mahekalu ya Kiyunani mara zote yalionekana kama sehemu ambazo miungu ililishwa na kuangaliwa.

▣ **"kwa maana ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote"** Hili linaweza kuwa dokezo kwa Isa.42:5. Hii ni namna ya Paulo kithiolojia kudai kuwa (1 ) pendo la Mungu ni kwa ajili ya wanadamu (rehema, neema) na (2) utoaji wa Mungu wa neema kwa mwanadamu. Ukweli mfanano ulitolewa na Zeno, mwanzilishi wa shule za ukakamavu, uliorekodiwa katika Clement of Alexandria, *Stromateis* 5:76:1 . Tambua neno "*autos*," ni yeye mwenyewe! Ni ajabu na ukweli namna gani kwa watu wa mataifa kusikia na kupokea.

**17:26 "alifanya kutoka katika mmoja"** Familia za kimagharibi za machapisho ya Kiyunani zinaongeza neno "damu moja." Hata hivyo, machapisho ya Kiyunani P<sup>74</sup>, x, A, na B yanaliondoa neno (toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa alama "B" ya uondoaji[kiwastani inajulikana]). Kama vile mwanzo ilikuwa inarejelea kwa Adamu. Ikiwa ni kidokezo kwenye falsafa ya Kiyunani inaaksi umoja wa wanadamu toka kwenye kusanyiko moja. Kifungu hiki na kile kinachofuata kwa wazi kinachodai mshikamano kwa wanadamu wote (yamkini ni dokezo toka Mal. 2:1 0, au hata tafasiri ya maandiko ya kale ya kiebrania(LXX) ya Kumb. 32:8), na kithiolojia inadaiwa kuwa wanadamu waliumbwa kwa sura ya Mungu (kama vile Mwa. 1 :26-27). Yale yaliyobaki katika mstari huu pia yaweza kudokeza habari za kitabu cha Mwanzo. Mwanadamu anaamriwa kuwa mwenye kuzaa matunda na kuijaza nchi (kama vile Mdo. 1 :28; 9:1 ,7). Wanadamu walikuwa wakaidi kugawanyika na kuijaza nchi. Mnara wa Babel (kama vile Mwa. 1 0-1 1 ) unaonyesha kuwa ilikuwa ni mbinu ya Mungu kuyakamilisha haya.

▣ **"akisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani na mipaka ya makazi yao"** Paulo anadai kuwa sio kwamba Mungu aliumba kila kitu, lakini aliviongoza vitu vyote. Hili laweza kuwa dokezo la Kumb.32:8 (LXX). Hata hivyo, ukweli huu unatetewa kila mahali katika Agano la Kale (kama vile Ayubu 12:23; Z.ab. 47:7-9; 66:7).

**17:27** Kifungu cha kwanza chaweza kuwa ni rejeo lingine toka kwa mwana ushairi wa Kiyunani, Aratus.

▣ **"ingawa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la nne inayoamaanisha kuondolewa mbali toka kwenye ukweli. Wanadamu lazima watambue hitaji lao. Vitenzi vyote ni kauli tendaji yenye uchaguzi ya wakati uliopita usiotimilifu

**NASB, NKJV**

**NRSV**"wamtafute hata kwa kupapasa-papasa"

**TEV**"hata kwa kutomasa"

**NJB**"hata wakigusa njia zao kwa ajili yake"

Neno hili linamaanisha "kugusa" au "kuhisi" (kama vile Luka 24:39). Muktadha huu unadokeza hali ya kiuchunguzi kutokana na giza au mkanganyiko. Wanajaribu kumtafuta Mungu, lakini sio rahisi. Upagani ni nguvu ipotoshayo yenye kuainisha anguko, kama ifanyavyo ibada ya sanamu na (kama vile Warumi 1 -2), lakini Mungu yupo!

▣ **"ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu"** Ni ukweli namna gani wa kushangaza. Mungu alitumba sisi, Mungu yuko kwa ajili yetu, Mungu yuko na sisi (kama vile Zaburi 139)! Paulo kwa nguvu zote anatetea pendo la Mungu, uangalizi, na uwepo kwa wanadamu wote. Hii ndiyo kweli ya injili (kama vile Efe. 2:1 1 -3:1 3). Paulo yawezekana alikuwa akidokeza kwenye Kumb. 4:7 au Yer. 23:23-24, lakini akiyatabiria kwa wanadamu wote. Hii ni siri iliyofichika kwa Agano Jipya!

**17:28 "kama vile mmoja wetu mtunga mashairi alivyosema"** Kifungu kilichopita, "katika Yeye tunaishi na kutembea na kuwepo," ni nukuu toka

1. Cleanthes' *Hymn to Zeus*. Alikuwa ndiye mkuu wa shule ya uvumilivu toka mwaka 263-232 k.k. au

2. Aratus's (toka Soli, mji ulioko karibu na Tarso) *Phainomena*, mstari wa 5. Aratus alikuwa mtu wa Kilikia na aliishi toka mwaka 31 5-240 k.k. Rejeo hili linasisitiza
  - a. uwepo wa Mungu kila mahali (kama vile Mdo. 1 7:27) au
  - b. uumbaji wa Mungu wa wanadamu wote (kama vile Mdo. 1 7:26). Paulo pia anawanukuu mahayawani katika 1 Kor. 15:32 na msanii ya Kiyunani Menander, *Thais*, katika 1 Kor. 1 5:33. Paulo alifundishwa katika fasihi za Kiyunani na ufasaha wa kusema, yumkini huko Tarso, kwenye chuo kikubwa cha mji.

▣ "**maana, sisi sote tu wazao wake**" Hii ni nukuu nyingine, yumkini toka Epimenides, mkazi wa Krete, iliyonukuliwa na Diogenes Laertius katika *Lives of the Philosophers* 1 :1 1 2.

**17:29** Hili ni hitimisho la Pulo na ukanushaji wa ibada ya sanamu (kama vile Zab. 1 1 5:1 -1 8; Isa. 40:1 8-20; 44:9-20; 46:1 -7; Yer. 1 0:6-1 1 ; Ebr. 2:1 8-1 9). Sikitiko kwa mwanadamu aliyeanguka ni kuwa wanatafuta ukweli wa kiroho na ushirika wa vitu vilivyotengenezwa na watu ambavyo havisikii, kujibu, au kusaidia!

**17:30 "zamani zile za ujinga alijifanya kama hazioni"** Hii nidhana ya kushangaza ya neema ya Mungu (kama vile Rum.3:20,25; 4:1 5; 5:1 3,20; 7:5,7-8; 1 Kor. 1 5:56). Wamekwisha kuisikia injili na wanawajibika kiroho!

▣ "**Mungu anawaagiza watu wote wa kila mahali**" Maelezo haya yanadai kuwa

1. kuna Mungu mmoja tu
2. Anawataka watu wote watubu

Inaonyesha ujumuishwaji wa neema na upendo wa Mungu (kama vile Yohana 3:1 6; 4:42; 1 Tim. 2:4; Tit. 2:1 1 ; 2 Pet. 3:9; 1Yn 2:1 ; 4:1 4). Huu sio ujumuishaji wa pamoja katika maana kuwa wote wataokolewa (kama vile Mdo. 1 7:32-33), lakini kwa maana kuwa Mungu ana shauku kuona ya kuona watu wote wakitubu na kumwamini Yesu kwa ajili ya wokovu. Yesu alikufa kwa ajili ya wote! Wote wanaweza okolewa! Muujiza wa uovu ni kuwa sio wote wataokolewa.

▣ "**watubu**" Neno la Kiebrania limaanisha "kubadilika kwa kitendo," wakati neno la Kiyunani linarejea kwenye "badiliko la fikra" angalia [MADA MAALUM: TOBA KATIKA AGANO LA KALE](#) katika Mdo. 2:38.

**17:31 "kwa maana ameweka siku ambayo atauhukumu ulimwengu"** Ujumbe wa Paulo kwa wazi na kwa kujirudia unatetea rehema ya Mungu na utoaji. Lakini hii ni nusu ya ujumbe. Mungu wa upendo na rehema pia Yeye ni Mungu asiye na upendeleo mwenye shauku ya haki. Wanadamu walioumbwa kwa mfano wake watatoa hesabu ya utumishi wa zawadi ya uzima (yaani., Zab. 96:1 3; 98:9). Dhamira ya Agano Jipya ni kuwa Mungu atauhukumu ulimwengu (ukosoaji juu ya ulimwengu unaojulikana) ni wa kujirudia (mf. Mt. 1 0:1 5; 1 1 :22,24; 1 6:27; 22:36; 25:31 -46; Ufu.20:1 1 -1 5).

▣ "**kwa mtu aliyemchagua**" Dhana hii ya hukumu ya siku ya mwisho unaosimamia juu ya uhusiano wa imani kwa yule mtu aliyefufuka, Yesu wa Nazareti (wakala wa YHWH kwenye hukumu), hakuwa na thamani na wa kutoaminika kwa hawa wasomi wa Kiyunani (kama vile 1 Kor. 1 :23), lakini moyo wa ushuhuda wa injili (kama vile Mdo. 1 0:42; Mt. 25:31 -33).

▣ "**akimfufua kutoka katika wafu**" Mada hii inajirudia mara nyingi katika kitabu cha Matendo (kama vile Mdo. 2:24,32; 3:1 5,26; 4:1 0; 5:30; 1 0:40; 1 3:30,33, 34,37; 1 7:31 ). Ni kiini cha uthibitisho wa injili kwamba Mungu Baba aliukubali uzima, mafundisho na kifo mbadala cha Yesu. Mafundisho kamili ya neno juu ya somo la (1) ufufuko wa Yesu na (2) ufufuko wa waamini ni 1 Wakorinto 15

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MATENDO 17:32-34**

<sup>32</sup> Basi waliposikia habari za ufufuo wa wafu wengine walifanya dhahaka; wengine wakasema, Tutakusikiliza tena katika habari hiyo. <sup>33</sup> Basi hivi Paulo akaondoka akawaacha. <sup>34</sup> Baadhi ya watu wakashikamana naye,



**wakaamini; katika hao alikuwamo Dionisio, Mwareopago, na mwanamke mmoja jina lake Damari, na watu wengine pamoja na hao.**

**17:32 "waliposikia habari za ufufuo wa wafu"** Wayunani, isipokuwa wafuasi wa mwanafalsafa Epicure, wanaamini katika nafsi iishiyo milele, na sio mwili. Ufufuo ulikuwa kikwazo kikubwa kwao (kama vile Mdo. 1 7:1 8; 1 Kor. 1 :23).

▣ **"walifanya dhahaka"** Neno hili linatumika hapa tu katika agano Jipya, lakini muundo uliothibitika unaonekana katika Mdo. 5:30 na 26:21 . Mzizi wa neno (*chleusma* au *chleusmos*) unatumika katika maandiko ya kale ya Kiyunani mara nyingi kwa ajili ya "kejeli" au "dhahaka" (kama vile Ayubu 1 2:4; Zab. 79:4; Yer. 20:8).

▣ **"wengine wakasema, tutakusikiliza tena katika habari hiyo"** Ujumbe wa Paulo juu ya upendo wa Mungu na uangalizi kwa ajili ya watu wote ulikuwa mpya kiasi kwamba hawa wasikiaji walivutiwa nao, lakini sio wote walishawishika.

**17:34 "baadhi ya watu wakashikamana naye, kati ya hawa alikuwemo Dionisio"** Kuna uwezekano wa kuwepo mititiko mitatu kwenye injili:

1. kukataa, "baadhi wanaanza kudhahaki" (Mdo. 1 7:32)
2. Kuchelewa kufanya maamuzi, "tutakuona siku nyingine kutokana na hili(Mdo. 1 7:32)
3. kuamini, "wengine wakaungana na Paulo na kuamini" (Mdo. 17:34; 1 The. 1 :9-1 0)

Hii inafanana na hadithi ya mafumbo ya mpanzi (kama vile Mathayo 1 3).

▣ **"Dionisio, Mwareopago"** Anaonekana kuwa mhudhuliaji wa haya majadiliano ya kifalsfa kwenye kilima cha Mars. Angalau msomi mmoja aliamini. Eusebius, *Eccl. His.* 3:4:6-7 na 4:23:6 anasema akajakuwa Askofu wa kwanza wa Ethene au Korinto. Kama hili ni kweli, ni ajabu ilioje ya mageuzi! Injili ni biashara ya mageuzi!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa mfasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki.

Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. kwa nini Paulo alikwepa miji Fulani mikubwa kama Amfopolia and Apollonia?
2. Kwa nini maumivu ya Kristo yanawafadhaisha sana Wayahudi?
3. Kwa nini mwitikio wa Berea kwenye injili ni wa muhimu na wa kutia moyo?
4. Kwa nini Paulo alisikia kuchochewa na hali ya kiroho wa watu wa Ethene?
5. Kwa nini hotuba ya Paulo juu ya kilima cha Mars ilikuwa ya muhimu? (dhidi ya. 22-24)

## MATENDO YA MITUME 18

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFASIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Paulo huko Korintho	Akihudumu huko Korintho	Uanzishaji wa kanisa huko Korintho	Huko Korintho	Msingi wa kanisa la Korintho
18:1-4	18:1-17	18:1-4	18:1-4	18:1-4
18:5-11		18:5-11	18:5-8	18:5-11
			18:9-11	Wayahudi wampeleka Paulo mahakamani
18:12-17		18:12-17	18:12-13	18:12-17
			18:14-17	
Paulo arejea Antiokia	Paulo arejea Antiokia	Mwisho wa safari ya pili ya umisionari na Mwanzo wa safari ya Tatu	Kurejea huko Antiokia	kurudi Antiokia na kuanza safari ya tatu
18:18-23	18:18-23	18:18-21	18:18-21	18:18
				18:19-21
		18:22-23	18:22-23	18:22-23
Apolo ahubiri huko Efeso	Huduma ya Apolo	Apolo huko Efeso	Apolo huko Efeso na Korintho	Apolo
8:24-28	18:24-28	18:24-28	18:24-28	18:24-26
				18:27-28

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("A Guide to Good Bible Reading"))

### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembele katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuwiwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHA): MATENDO 18:1-4

<sup>1</sup> Baada ya mambo hayo, Paulo akatoka Athene akafika Korintho. <sup>2</sup> Akamwona Myahudi mmoja, jina lake Akila, mzalia wa Ponto; naye amekuja kutoka nchi ya Italia siku za karibu, pamoja na Prisila mkewe, kwa sababu Klaudio amewaamuru Wayahudi wote watoke Rumi, naye akafikilia kwao; <sup>3</sup> na kwa kuwa kazi yao ya ufundi ilikuwa moja, akakaa kwao, wakafanya kazi pamoja, kwa maana walikuwa mafundi wa kushona hema. <sup>4</sup> Akatoa hoja zake katika sinagogi kila sabato, akajaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani.

**18:1 "akatoka Athene akafika Korintho"** Mji wa Korintho ulikuwa maili 50 Magharibi mwa Ethene kwenye shingo ya nchi. Paulo alikuwa mpweke huko Ethene na hata kwa kipindi kifupi akiwa Korintho (kama vile Mdo. 1 8:5). Paulo alikuwa na matatizo ya macho (miiba ndani ya mwili, kama vile 2 Kor. 1 2). Ilikuwa ni vigumu kwake yeye kuwa mpweke.

### MADA MAALUM: MJI WA KORINTHO

- A. Njia ya usafiri kipindi cha majira ya baridi maeneo ya sehemu muhimu za kusini mwa Uyunani (yaani, Cape Malea) zilikuwa za hatari mno kwa hiyo njia za ardhini zilikuwa za muhimu sana. Kijografia kitongoji cha Korintho kilikuwa maili nne ndani ya shingo ya nchi kati ya Ghuba ya Korintho (yaani, Ziwa ionia) na Ghuba ya Saranic (yaani, Ziwa Aegea) na kuufanya mji kuwa mji mkubwa wa kibiashara (ulibobea kwenye aina ya vyungu na aina maalumu ya shaba nyeupe), na kituo cha kijeshi. Katika siku za Paulo, hii kiuhalisia ulikuwa ni utamaduni wa Mashariki na Magharibi kukutana.
- B. Korintho pia ulikuwa ni kitovu kikubwa cha tamaduni za ulimwengu wa Kiyunani na Kirumi kwa sababu ulikuwa ni mwenyeji wa michuano ya Mabara ya mwaka 581 K.K (kwenye Hekalu la Poseidon). Michezo ya Olympic huko Anthens, Uturuki, kila baada ya miaka minne, zilishindanishwa katika saizi na uwezo (Thucydides, *Hist*, 1.13.5)
- C. Katika mwaka wa 146 K.K Korintho ilijihusisha na mapinduzi (yaani, Shirikisho la Achani) dhidi ya Rumi na uliharibiwa na mtawala wa Kirumi Lucius Mummius na kundi kubwa la Kiyunani liligawanyika kwenye utumwa. Kwa sababu ya umuhimu wake wa kibiashara na kijeshi ulijengwa upya huenda mwaka wa 46 au 48 K.K na Julius Kaisari. Na ukajakuwa koloni kubwa la Rumi pale wanajeshi wa Kirumi walipostaafu. Ulikuwa ni mji ulioingizwa kama mji wa kumi kwa usanifu wa majengo na utamaduni na ulikuwa ni kitovu cha utawala wa Rumi (yaani, Maseneta) jimbo la Achani katika mwaka 27 K.K. lilikuja kuwa jimbo la kifalme mwaka 15 B.K.
- D. Mji wa zamani wa Korinto ni mji uliokuwa umeimarishwa na kujengwa juu ya vilima, ukiinuka yapata futi 1880 toka usawa wa bahari, ulikuwa ni eneo la Hekalu la Aphrodito. Hekalu hili lilihusishwa kuwa na makahaba 1000 (Strabo, Geograpy, 8.6.20-22). Kuitwa "Wakorintho" (yaani, *Korinthiazesthai*, ukiwa na sarafu ya Aristophanes [450-385 K.K]) kwanza ulistahili kuacha maisha mfanano ya vurugu. Hekalu hili, kama lilivyojulikana kwenye mji, liliharibiwa na tetemeko yapata miaka 150 kabla ya Paulo kuwasili pale, kama ilivyokuwa tena katika mwaka wa 77 B.K, haijulikani kama makundi ya dini yaliendelea kustawi katika siku za Paulo. Kwa vile Warumi katika mwaka wa 146 K.K waliuharibu mji na kuuwa au kuwafanya watumwa wenyeji wote wa pale. Uzuri wa mji wa Kiyunani ulichukuwa nafasi na hadhi ya kikoloni ya Warumi (Pausani II 3.7). Utamaduni huu wa Kirumi badala ya utamaduni wa Kiyahudi, ulitengeneza tofauti muhimu katika kuitafasiri 1 Wakorintho.

**18:2 "Myahudi mmoja,aitwaye Akila. . .Prisila"** Mke wake, Prisila, pia aliitwa Priska, mara nyingi anatajwa kwanza (kama vile Mdo. 1 8:1 8,26; 1 Kor. 1 6:1 9; 2 Tim. 4:1 9), ambacho sio kitu cha kawaida katika tamaduni za ukuu wa

kaya (angalia [MADA MAALUM: WANAWAKE KATIKA BIBLIA](#) katika Mdo.2:1 7). Jina lake linaendana na familia tajiri ya Kirumi (gens Prisca). Hakuwahi kusema kuwa yeye si Myahudi. Ni habari gani kubwa ya upendo ingalikuwa kama ingalikuwa mtoto tajiri wa kike toka Rumi kuolewa na mtembezi wa Kiyahudi mtengeneza mahema au mchakata ngozi ! walitengeneza urafiki na kufanya kazi ya biashara pamoja na Paulo. Walimsaidia mwanafunzi Apolo.

▣ **"siku za karibu"** katika *A Translator's Handbook on the Acts of the Apostles*, uk. 347, Newman and Nida walitengeneza habari ya kulisimua kuhusu hiki kielezi, *prosphatōs*. Mwanzoni kilimaanisha "mauaji mapya," lakini kilikuja kutumika kiisitari kama "siku za karibuni." Huu ni mfano mzuri wa namna gani kuwa asili ya neno sio kila mara ni kiashirio kizuri cha maana. Maneno lazima yaelezwe katika muundo wake wa kisasa na kimuktadha. Wingi wa ushindwaji wa kutafasiri Biblia umekuja toka kwa watafasiri wa leo walioshindwa kutambua utumiaji wa kiisitari au nahau.

▣ **"naye amekuja kutoka nchi ya Italia akiwa na mkewe Prisila, kwa sababu Klaudio ameamuru Wayahudi wote waondoke toka Rumi"** katika *Historia Contra Paganus* 7.6.1 5, Orosius anasema tarehe ya hili tangazo ilikuwa mwaka wa 49 b.k. Suetonius, katika *Life of Claudius* 25.4, anatumia kuwa ilikuwa kupitia maaandamano katika mitaa wanapokaa Wayahudi mahali pa uanzishaji wa *Chrestus*. Warumi walichanganya kati ya Christus na Chrestus (kama vile Tacitus, *Annals* 25:44:3). Dio Cassius katika *Histories* 60.6, anasema Wayahudi hawakuondolewa , lakini walikatazwa kuendesha mila zao za kale. Badiliko la kitenzi lenye hali ya kuendelea, "naye amekuja," ni wakati timilifu tendaji wenye hali ya kuendelea, ukidokeza kuwa kitendo cha kuendelea kilikuwa ni cha kudumu au muda mrefu. Tangazo la Klaudio (amri) ni kauli timilifu tendwa isio na ukomo.

**18:3 "kwa kuwa kazi yao ya ufundi ilikuwa moja"** Hili mara nyingi lilifikiliwa kuwa utengenezaji wa mahema, lakini neno linaweza kurejea kwenye uchakataji wa ngozi. Mazingira ya nyuma ya Paulo katika sheria za Kiyahudi zilihitiwa kwamba awe na kazi au biashara ya kiulimwengu. Ili pasiwepo na mwalimu wa dini ya Kiyahudi ambaye angeweza kuchukua pesa kwa ajili ya ufundishaji. Kilikia, nyumbani kwa Paulo, palitambulika kwa ajili ya kuwa na ngozi na mbuzi wenye manyoya mengi.

**18:4 "akatoa hoja zake katika Sinagogi kila Sabato"** Paulo alihudhulia kila Sabato kwa ajili ya "kuhojiana" na "kujaribu kuwashawishi" (hizi zote ni njeo zisizo kamilifu). Paulo alikwenda kwa Wayahudi kwanza kwa sababu

1. ulikuwa ni mfano wa Yesu (kama vile Mt. 1 0:5-6)
2. Walilifahamu Agano la Kale
3. Wacha Mungu wa Kiyunani kwa pamoja walihusika kwenye ujumbe (kama vile Rum. 1 :1 6)

Sinagogi lilianza kipindi cha kwenda uhamishoni Babeli kama sehemu ya kuabudu, elimu, na maombi. Ilikusudiwa kuanzisha na kuendeleza tamaduni za Kiyahudi.

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA):MATENDO 18:5-11

<sup>5</sup> Hata Sila na Timotheo walipotelemka kutoka Makedonia, Paulo akasongwa sana na lile neno, akiwashuhudia Wayahudi ya kwamba Yesu ni Kristo. <sup>6</sup> Walipopingamana naye na kumtukana Mungu, akakung'uta mavazi yake, akawaambia, Damu yenu na iwe juu ya vichwa vyenu; mimi ni safi; tangu sasa nitakwenda kwa watu wa Mataifa. <sup>7</sup> Akaondoka huko akaingia katika nyumba ya mtu mmoja jina lake Tito Yusto, mcha Mungu, ambaye nyumba yake ilikuwa mpaka mmoja na sinagogi. <sup>8</sup> Na Krispo, mkuu wa sinagogi, akamwamini Bwana pamoja na nyumba yake yote. Wakorintho wengi waliposikia, waliamini, wakabatizwa. <sup>9</sup> Bwana akamwambia Paulo kwa maono usiku, Usiogope, bali nena, wala usinyamaze, <sup>10</sup> kwa kuwa mimi ni pamoja nawe, wala hapana mtu atakayekushambulia ili kukudhuru; kwa maana mimi nina watu wengi katika mji huu. <sup>11</sup> Akakaa huko muda wa mwaka mmoja na miezi sita akifundisha kati yao neno la Mungu.

**18:5 "Sila and Timotheo walipotelemka toka Makedonia"** Inavyoonekana walileta sadaka ya upendo toka kwa waumini wa huko Filipi, iliyomsababisha Paulo kuhubiri muda wote (kama vile 2 Cor. 1 1 :9; Fil. 4:1 5). Timotheo pia alileta habari kuhusu kanisa la Thesalonike katika kujibu kile ambacho Paulo kilimsababisha kuandika 1 na 2

Wathesalonike (kama vile Mdo. 1 7:1 4). Inaonekana kuwa, mara tu Luka alipokwenda Filipi kuwafanya waamini wapya kuwa wanafunzi, Timotheo alikwenda Thesalonike na Sila Berea. Paulo aliwajibika na mafunzo ya Wakristo wapya (yaani., agizo kuu la kuwafanya na kuwafundisha kuwa wanafunzi, sio tu maamuzi). Alitaka kuacha kanisa lililo hai, lenye kukua na kuzaa katika kila mji alioutembelea.

**NASB"Paulo akasongwa sana na lile neno"**

**NKJV"Paulo akashurutishwa na Roho"**

**NRSV"Paulo akasongwa kulinena neno"**

**TEV"Paulo akatoa muda wake wote kuhubiri ujumbe"**

**NJB"Paulo akatoa muda wake kulihubiri neno"**

Kuna tofauti ya maandiko ya Kiyunani katika kifungu hiki. Maandiko mazuri na ya awali yana kihusishi cha wakati cha neno *Logos* (kama vile MSS P<sup>74</sup>,  $\kappa$ , A, B, D, E, pamoja na tafasiri za Vulgate, Peshitta, na Coptic). Toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa alama "B". Upokeaji wa maandiko ya agano jipya kwa Kiyunani yana neno "roho" (*pneumati*), yaliyopatikana zaidi mwanzoni mwa machapisho ya Kiyunani ya herufi ndogo (matatu kati yake ni ya kale kwenye karne ya kumi)

▣ **"kwa upole akiwashuhudia kwamba Yesu ni Bwana"** Linganisha kati ya 9:22 na 17:3 kuhusu njia za Paulo za ushawishi (kauli isiotimilifu tendwa elekezi ya neno *sunechō*, inayomaanisha kubana), ambayo kwa kiasi kikubwa ilifanana na njia ya Stefano (kama vile Matendo 7). Angalia maelezo katika Mdo. 2:40. Mara nyingi hili linarudia madai ya kithiolojia (yaani., Yesu ni Masihi, angalia maelezo katika Mdo.17:3) ambayo ndiyo ufunguo kwa wengine!

**18:6 "wakapingana naye na kumtukana"** Hizi zote ni kauli za kati endelevu za wakati uliopo, zinazosisitiza kuendelea kuhusika binafsi. Kwa bahati mbaya yote yakawa majibu ya kawaida toka kwa Wayahudi waliotawanyika miongoni mwa mataifa.

▣ **"akakung'uta mavazi yake"** Hii ilikuwa alama ya Kiyahudi kwa ajili ya kukataliwa (kama vile Neh. 5:1 3; Mdo. 1 3:51 ; Luka 9:5; 1 0:1 1 ). Angalia maelezo kamili katika Mdo.13:51 .

▣ **"Damu yenu na iwe juu ya vichwa vyenu"** Hii nahau ya Agano la Kale ina vidokezo mbali mbali.

1. wajibu wa waangalizi, wote mmoja mmoja na wote pamoja, Ezek. 3:1 6ff; 33:1 -6
2. Wajibu binafsi, Yos. 2:19; 2 Sam. 1 :16; Ezek. 18:1 3; Mdo. 18:6; 20:26
3. Wajibu wa pamoja wa wahenga au taifa, 2 Sam. 3:28-29; 2 Fal. 2:33
4. Muunganiko wa agano jipya # 2 na #3, Mt. 27:25

Uzima ulikuwa katika damu (cf. Lev. 1 7:1 1 ,1 4). Umwagaji wa damu ulimfanya mtu awajibike kwa Mungu kwa ajili ya kifo hicho (kama vile Mwa. 4:1 0; 9:4-6).

▣ **"Mimi ni safi"** Hii ni sitiari ya kidhabihu ya Agano la Kale ya uwajibikaji wa mtu binafsi. Paulo hakuwajibika kiroho (kama vile Ezekiel 33) kwa ajili ya Wayahudi kuisikia injili katika mji. Aliwashirikisha ujumbe lakini wasingalipokea. Sisi tu safi?

▣ **"tangu sasa nitakwenda kwa watu wa Mataifa"** Hii njia ya kiinjistiki na laana vikawa vya kawaida kwa Paulo (kama vile Mdo. 1 3:46; 1 8:6; 26:20; 28:28). Paulo aliijisikia kulazimika kuhubiri kwenye nyumba za Waisrael kwanza, akimfuatisha Yesu (kama vile Mt. 1 0:6; 1 5:24; Marko 7:27). Aliyaelezea haya kithiolojia katika Rum. 1 :3,5,9-11 na kimsukumo katika Mdo. 9;1 5; 22:21 ; 26:1 7 (kama vile Rum. 1 1 :1 3; 1 5:1 6; Gal. 1 :1 6; 2:7-9; Efe. 3:2,8; 1 Tim. 2:7; 2 Tim. 4:1 7).

**18:7 "Tito Yusto"** Kuna uwezekano mbali mbali wa kumtambua huyu "mcha Mungu" aliyeishi mbele ya Sinagogi huko Korintho.

1. jina lake kamili ni Gayo Tito Yusto na kanisa la Korintho lilikutana nyumbani kwake(kama vile Rum. 1 6:23)

2. Anaweza kuwa ni Gayo aliyetajwa katika 1 Kor. 1 :1 4 ambaye alibatizwa na Paulo
3. Kuna suluhisho la maandiko ya Kiyunani linalohusiana na jina hili.
  - a. *Titou loustou*, MSS B, D<sup>2</sup> (toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa alama "C" )
  - b. *Titou loustou*, MSS  $\kappa$ , E, P
  - c. *loustou*, MSS A, B<sup>2</sup>, D\*
  - d. *Titou*, tafasiri za Peshitta na Coptic

▣ **"mcha Mungu"** Ujumbe toka kwa Aprofodito (karne ya 3rd ), anatumia kifungu, "wamwabuduo Mungu" kwa wale wa mataifa walioshikamana na kuhudhuria ndani ya Sinagogi. Kwa hiyo "wacha Mungu" (1 0:1 -2,22; 1 3:1 6,26) lina maana sawa na "wamwabuduo Mungu" (kama vile 1 3:50; 1 6:1 4; 1 8:6-7). Kifungu hiki ni kigumu kukielezea. Kifungu mfanano kimetumia kwa Lidia katika Mdo.1 6:1 4 na Wayunani mbali mbali huko Thesalonike katika Mdo. 17:4 na huko Berea katika Mdo.1 7:1 7. Walionekana kuwa Wayunani waliovutiwa na dini ya Kiyahudi, wakahudhuria katika Sinagogi ikiwezekana, lakini hawakuwa wabadili dini kamili. hata hivyo, kifungu "wale wababili dini waliomcha Mungu" linatumika kuelezea wabadili dini waliokuwepo ndani ya Sinagogi huko Perga Pamfilia katika Mdo. 13:43.

**18:8 "Krispo"** Huyu mtu alikuwqa mwangalizi na msimamizi wa masinagogi ya nyumbani (kama vile 1 Kor. 1 :1 4).

▣ **"akamwamini Bwana yeye pamoja na nyumba yake yote"** Kitabu cha Matendo kinaweka kumbu kumbu za mifano mbali mbali ambapo mkuu ya kaya aliongoa na familia nzima ikabatizwa (kama vile 1 1 :1 4; 1 6:1 5,31 -34; 1 8:8, angalia **MADA MAALUM: UBATIZO** katika Mdo. 2:38). Familia ilikuwa ndio kipaumbele. Ubinafsi haukusisitizwa. ingawa hii ni tofauti na uelewa binafsi wetu wa uinjilisti, hii haisababishi kutokuufanya sasa au kutokuufanya ukweli. Hata hivyo, pia inatakiwa kutambulika kuwa sio wote washirika wa familia zilizo okolewa waliohudhulia kanisani walikuwa wameokoka. Onesmo alikuwa mtumwa kwenye nyumba ya Filemoni mahali kanisa lilipokutana, lakini hakuwa ameokoka mpaka pale alipokutana na Paulo ndani ya gereza. Kwa wale "waliookolewa "angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:40 and 3:1 6.

▣ **"Wakorintho wengi waliposikia, wakaamini, na kubatizwa"** Wengi wao huko Korintho walikuwa tayari wameupokea ujumbe wa Paulo, lakini Paulo alikwisha katishwa tamaa na alihitaji kutiwa nguvu kwa maono maalum ya ki-Mungu (kama vile Mdo. 18:10b). Makanisa ya huko Korintho (makanisa ya nyumbani) yalikuwa ni makusanyiko magumu yenye kuwa na matatizo. Aliwapenda, lakini walimsababishia maumivu makali (kama vile I na 2 Wakorintho). kuna ufanano ulio muhimu katika muktadha huu katika 1 Kor. 1 :1 4-1 7. Nimejumuisha moja ya maelezo yangu toka kwenye fasiri yangu juu ya 1 Wakorintho. Angalia kwenye mtandao [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org)

**"1 Kor. 1:17 "kwa vile Kristo hakunituma kubatiza, bali kuhubiri"** Hii haimaanisha kuudharau ubatizo, lakini ni kuzijibu roho za mgawanyiko ndani ya kanisa la Korintho ambalo lilikuwa likiwainua viongozi fulani. Hata hivyo, maelezo haya yanaonyesha kuwa ubatizo haukuonekana kama nguvu ya neema ya "kisakramenti."

Inashangaza kuona kuwa baadhi ya wale wanaotafasiri maandiko ya Paulo kwa maana ya kisakramenti wakati katika maandiko yake yote hasa alitaja karamu ya Bwana mara moja tu katika 1Korintho 11 na ubatizo mara mbili, katika Rum. 6:1-11 na Kol. 2:12. Hata hivyo, ubatizo ni mapenzi ya Mungu kwa kila mwamini.

1. Ni mfano wa Yesu
2. Ni amri ya Yesu
3. Ni utaratibu wa kawaida, uliotegemewa kwa waamini wote

Siwezi amini kama ndio mwongozo kwa ajili ya kupokea neema ya Mungu au Roho. Ilikuwa ni fursa ya wazi kwa waamini wapya kuitamka imani yao mbele ya umati na maamuzi thabiti. Hakuna mwamini wa Agano Jipya angeweza kuuliza, "lazima nibatizwe ili nipate kuokoka?" Yesu alifanya! Yesu analiamuru kanisa kutenda! Tendeni! "ubatizo bado ni tamko kuu la wazi lenye ushawishi wa imani ya mtu, hasa katika tamaduni za wasio Wakristo.

**18:9 "usiogope"** Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo ikiwa na kiambata hasi, ambayo mara nyingi inamaanisha kuzuia kitendo ambacho tayari kiko katika mchakato. hili linaweza kuwa ni dokezo kwenye Mwa. 26:24 au Kumb.

1 :29-33;20:1 , wakati Isaka alikuwa na hofu. Paulo alikuwa na hofu na akahitaji kutiwa moyo na Kristo. Luka anaweka kumbu kumbu ya maono haya maalum ya utiwaji moyo katika Mdo. 22:1 7-1 8; 23:1 1 ; 27:23-24. Ikiwa mtu kama Paulo alichoka kuyatenda mema, inakushangaza wewe kufanya hivyo? Yesu yu pamoja nasi (kama vile Mdo. 1 8:1 0; Mt. 28:20)! Agizo kuu bado linabaki kuwa mwongozo wa lengo, ambalo ndilo jambo kuu (kama vile Mt. 28:1 8-20; Luka 24:47; Mdo. 1 :8).

▣ **"bali nena, wala usinyamaze"** Hizi zote ni kauli shurutishi (kauli tendaji ya wakati uliopo na kauli tendaji ya wakati uliopita usiotimilifu). Hofu lazima isiwanyamazishe wapiga mbiu ya injili! Misukumo yetu inapanda na kushuka, lakini Mdo.1:8 bado inabaki kama nuru ituongozayo (kama vile 2 Tim. 4:2-5).

**18:10 "Mimi nipo pamoja nawe"** Hakuna ahadi kubwa (kama vile Mwa. 26:24; Kut. 3:1 2; 33:4; Zab. 23:4; Mt.28:20; Ebr. 1 3:5). Tambua kuwa yu pamoja nasi, sio kwa faraja yetu binafsi au ulinzi, bali kwa ujasiri wa uinjilisti (sisi pia, kusudi la kujazwa na Roho katika kitabu cha Matendo). Uwepo wa Roho ni kwa ajili ya kupiga mbiu, wala si wa amani binafsi.

▣ **"kwa maana Mimi nina watu wengi katika mji huu"** Kifungu "ninao watu wengi" ni dokezo katika matumizi ya Agano la Kale ya neno hili kwa Waisrael (yaani., watu wa Mungu), lakini sasa katika Agano Jipya inawarejerea wale walioko Korintho (Wayahudi na watu wa Mataifa) ambao wangaliitikia ujumbe wa injili. Kwa maana hapana tena Myahudi waka Myunani (kama vile Rum. 3:22; 1 Kor. 1 2:1 3; Gal. 3:28; Kol. 3:1 1 ). Kanisa sasa linaitwa kwa vyeo vya agano la kale (kama vile Gal. 6:1 6; 1 Pet. 2:5,9; Ufu.1 :6). Huu ni msisitizo wa maamuzi ya Mungu ya kabla na maarifa yajayo (kama vile Warumi 9; Waefeso 1 ). Ah!, kama tungalionga kitabu cha uzima sasa hivi! Ushuhuda wa kanisa ungekuwa thabiti (kama vile Ufu. 13:8). Uhakika binafsi ni kwa ajili ya ujasiri wa uinjilisti, na sio uthibitisho wa tiketi ya kwenda mbinguni pindi mwamini anapokufa!

**18:11** Mstari huu unasaidia kuanzisha utaratibu wa kupanga taratibu za matukio kwa ajili ya safari ya kimisionari ya Paulo. Ingawa kifungu ni kigumu kuelezeka, lakini kinadokeza kazi ya kuhubiri ya miezi kumi na minane huko Korintho.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIOBORSHWA): MATENDO 18:12-17**

<sup>12</sup> Hata Galio alipokuwa liwali wa Akaya, Wayahudi wakamwinukia Paulo kwa nia moja, wakamleta mbele ya kiti cha hukumu, <sup>13</sup> wakisema Mtu huyu huwavuta watu ili wamwabudu Mungu kinyume cha sheria. <sup>14</sup> Na Paulo alipotaka kufunua kinywa chake, Galio akawaambia Wayahudi, Kama lingekuwa jambo la dhuluma au la hila mbaya, enyi Wayahudi, ingekuwa haki mimi kuchukuliana nanyi; <sup>15</sup> bali ikiwa ni hoja juu ya maneno na majina na sheria yenu, liangalieni ninyi wenyewe, maana mimi sitaki kuwa mwamuzi wa mambo hayo. <sup>16</sup> Akawafukuza waondoke mbele ya kiti cha hukumu. <sup>17</sup> Nao wote wakamshika Sosthene, mkuu wa sinagogi, wakampiga mbele ya kiti cha hukumu. Wala Galio hakuyaona mambo hayo kuwa ni kitu.

**18:12 "Galio"** kutoka kwenye vyanzo vya kibiblia na vyanzo zaidi vya kibiblia tunajifunza kuwa huyu alikuwa kiongozi mwenye maarifa alipenda haki. Nduguye, Seneka, akamwambia, "hata wale wanaompenda ndugu yangu Galio kwa nguvu zao zote hawampendi ipasavyo" na "hakuna mtu kamwe alikuwa mzuri kwa yeyeto kama alivyo kuwa Galio kwa wote." Hawa wagombea wa kisiasa walitusaidia kupanga safari ya Paulo. Alikuwa ni gavana wa jimbo la Kirumi yapata miaka miwili na nusu akitawala kuanzia mwaka 51 b.k

▣ **"Hata Galio alipokuwa liwali wa Akaya"** Luka alikuwa mwanahistoria sahihi. Majina ya maofisa wa Kirumi katika eneo hili yalibalika tangu mwaka 44 b.k; "gavana wa jumbo" (kama vile Mdo. 13:7;19:38) lilikuwa sahihi kwa sababu Mfalme mkuu Klaudio alilitoa jimbo hili kwa seneti.

▣ **"Wayahudi kwa nia moja"** Luka anakitumia kifungu hiki mara nyingi kuelezea umoja wa waumini (kama vile Mdo.1 :1 4; 2:1 ,46; 4:24; 5:1 2; 8:6; 1 5:25), lakini hapa inadokeza umoja wa Wayahudi huko Korintho wenye wivu na wapinga injili (kama vile Mdo. 1 8:6). Mifano mingine ya matumizi ya kifungu hiki kwa maana hasi ni 7:57; 1 2:20; na 19:29. Neno "wayahudi" mara nyingi lina maana hasi katika mandiko ya Luka.

▣ **"wakamleta mbele ya kiti cha hukumu"** Hili ni neno *bēma* (kiuhalisia ni, "hatua "). Kilikuwa ni kiti au jukwaa la Kirumi lililowekwa kwa ajili ya kutoa haki (kama vile Mt. 27:1 9; Yohana 1 9:1 3; Mdo. 25:6,1 0,1 7; 2 Kor. 5:1 0).

**18:13 "ili wamwabudu Mungu kinyume cha sheria"** Madai ya Wayahudi kuwa Ukristo ulikuwa ni ukiukaji wa wa sheria zao, kwa hiyo, hapana sehemu ya dini ya Kiyahudi, iliyokuwa muhimu katika masuala ya kisheria. Ikiwa Galio angetawala kwa kuangalia mashitaka haya, Ukristo ungalikuwa dini isioruhusiwa kisheria. Lakini, kama ilivyokuwa, Ukristo ulifurahia utetezi wa kisiasa (ulionekana kama mgawanyiko wa dini ya Kiyahudi, ambayo ilikuwa dini iliyotambulika kisheria) chini ya sheria za Kirumi mpaka kwenye unyanyasaji wa mtawala nero, miaka 10-12 baadaye. Hata inawezekana kuwa moja ya kusudi la Paulo katika kukiandika kitabu cha Matendo ilikuwa ni kuonyesha kwa maandishi kuwa Ukristo haukuwa na athari yeyote katika utawala wa Kirumi, kila afisa wa Kirumi aliandikwa kama mwenye kuutambua ukweli huu.

**18:14 "ingekuwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la pili. Ni muundo adimu unatengeneza maelezo ya uongo ili kutengeneza hoja au kuendeleza mjadala. Mara nyingi unaitwa hali yenye "kinyume na ukweli." Hii ingelipaswa kutafasiliwa "kama lilikuwa ni suala kukosea au kosa lisilo la kibinadamu, ambavyo sivyo, hivyo ingalistahili kwangu kuchukuliana na wewe, ambavyo sivyo."

**18:15 "ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza. Suala la kisheria lilikuwa, kiukweli, ni suala la kidini. Galio kihakima alitambua mwenendo halisi wa Wayahudi. Hangeweza na asingtenda kama mwamuzi kwenye suala hili.

**18:16 "akawafukuza waondoke"** Hii ni moja ya uonekanaji wa kitenzi hiki katika Agano Jipya, lakini kilikuwa kikitumika mara nyingi katika maandiko ya kale ya Kiyunani (kama vile 1 Sam. 6:8; Ezek. 34:1 2).ni muundo ulioimarika wa neno *elaunō*, linalomaanisha kufukuzwa kwa nguvu.

**18:17 "nao wote wakamshika Sosthene"** "Nao wote" linarejea kwa Wayahudi wa Mdo.1 8:1 2 au yumkini kwa Wayunani, kimsingi kunakoonyesha wale wasio kabila la kisemiti kwenye miji ya Kiyunani. Sosthene alichukua nafasi ya Krespo kama kiongozi wa Sinagogi. Kwa nini Wayahudi walimpiga haijulikani. Huenda alimruhusu Paulo kuzungumza ndani ya Sinagogi.

▣ **"wala Galio hakuyaona mambo hayo kuwa ni kitu"** Huyu kiongozi wa kisiasa, tofauti na Pilato, asingaliyumbishwa na umati wa watu.

#### ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA): MATENDO 18:18-21

<sup>18</sup> Baada ya hayo Paulo akazidi kukaa huko siku nyingi, kisha akaagana na ndugu akaabiri kwenda Shamu; na Prisila na Akila wakaenda pamoja naye, alipokwisha kunyoa kichwa chake huko Kenkrea; maana alikuwa ana nadhiri. <sup>19</sup> Wakafika Efeso, akawaacha huko. Yeye mwenyewe akaingia katika sinagogi, akahojiana na Wayahudi. <sup>20</sup> Walipomtaka akae wakati mwingi zaidi, hakukubali; <sup>21</sup> bali aliagana nao, akisema, Nitarejea kwenu tena, Mungu akinijalia. Akatweka, akatoka Efeso,

**18:18 "Kenkrea"** Hii ilikuwa moja ya bandari huko Korintho. Ilikuwa imekalia kwenye bahari ya Aegea. Upande wa mashariki mwa mkono wa nchi kule Korintho ilikokuwa. Inatajwa tena kama mahali pa kanisa katika Rumi 16:1.

▣ **"alikuwa ana nadhiri"** Kiutaratibu wa kupanga matukio, hii inarejelea nadhiri isio kamili ya Mnazareti katika kitabu cha Hes.6:1-21 (cf. F.F. Bruce, *Answers to Questions*, uk. 52). Paulo analifanya hili tena katika Mdo. 21 :24



(angalia maelezo hapo). Kunyoea kichwa ingalitambulisha mwisho wa nadhiri. wote A. T. Robertson na M. R. Vincent wanalifikilia hili kuwa haikuwa nadhiri ya Mnazareti kwa sababu ingaliweza kusitishwa huko Yerusalem kutokana na mila za Kiyahudi. Paulo alifanya kila kitu kwa watu ili aweze kuwapata baadhi ili kuwaaminisha kuwa alikuwa ni Akila aliyekuwa amenyoea kichwa chake

**18:19 "Efeso"** Huu ulikuwa ni mji wa kibiashara Magharibi mwa Asia Ndogo. Baada ya bandari ya Mileto kuharibiwa na maporomoko ya udongo toka kwenye mifereji ya Mto, masuala ya kibiashara yakahamia pwani ya Efeso, ambao pia ulikuwa na bandari ya asili. Wakati wa kipindi cha agano Jipya baada ya kupita siku njema za watu wa Efeso zilikuwa zimekwisha pia. Bado ulikuwa ni mji mkubwa na maarufu, lakini si kama ulivyokuwa mwanzo kwa sababu

1. ulikuwa ni mji mkubwa wa jimbo la Kirumi huko Asia Ndogo. Haukuwa mji mkuu, ingawa gavana wa Kirumi aliishi huko. Ulikuwa mji mkuu wa kibiashara kwa sababu ya kuwa na bandari nzuri ya asili.
2. Ulikuwa ni mji huru, ulioruhusu kuwa na serikali za mitaa na uhuru mwingi, pamoja na kutokuwepo na kikosi cha kijeshi cha Warumi.
3. Ulikuwa ni mji pekee ulioruhusiwa kuendesha mashindano ya nchi za Asia yaliyoendeshwa mara mbili kila mwaka.
4. Ni mahali palipokuwa na hekalu la miungu ya Atemi (Diana huko Latini), lililokuwa ni moja ya maajabu saba ya kidunia kwenye siku zake. Lilikuwa na ukubwa wa 425 x 220 likiwa na nguzo 127, zikiwa na urefu wa 60ft; nguzo 86 kati yake zilikuwa zimefunikwa kwa (angalia Pliny's *Hist. Nat.* 36:95ff). Sura ya mungu Artemi kuwa na sura ya mwanamke anayenyonyesha. Inamaanisha kuwa palikuwepo na makahaba wengi wenye kupenda anasa ndani ya mji (kama vile Matendo 19). Ulikuwa ni mji usio na maadili, wenye tamaduni nyingi.
5. Paulo alikaa katika mji huu yapata miaka mitatu (kama vile Mdo. 18:18na kuendelea; 20:13).
6. Inadaiwa kuwa palikuja kuwa makao ya Yohana baada ya kifo cha Maria huko Palestina.

▣ **"Yeye mwenyewe akaingia katika Sinagogi akahojiana na Wayahudi"** Paulo aliwapenda watu wake (kama vile Rum.9:1-5). alijaribu pasipo kushindwa ili kuwafikia kwa ajili ya injili.

**18:20** Hawa Wayahudi walikuwqa kama watu wa Berea. Walikuwa tayari kusikiliza. Kwa nini Paulo hakupenda kubaki mahali hapa haikuelezewa katika maandiko, lakini katika Mdo. 18:21 inaonyesha alikuwa tayari kurudi kwa maelekezo ya Mungu tarehe za baadaye.

**18:21 "nitarejea kwenu tena, Mungu akinijalia"** Paulo aliamini maisha yake yako mikononi mwa Mungu, na sio mikononi mwake (kama vile Rum. 1:10; 15:32; 1 Kor. 4:19; 16:7). Huu ni mtazamo wa ulimwengu kibiblia (kama vile Ebr. 6:3; Yakobo 4:15; 1 Pet. 3:17). Paulo atarudi na Efeso kuwa ndio mtizamo wake mkuu wakati wa safari yake ya tatu ya umisionari.

**ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA): MATENDO 18:22-23**

<sup>22</sup> na alipokwisha kushuka Kaisaria, akapanda juu, akawasalimu kanisa, kisha akatelemkia Antiokia. <sup>23</sup> Hata akiisha kukaa huko siku kadha wa kadha akaondoka, akapita kati ya nchi ya Galatia na Frigia, mji kwa mji, akiwathibitisha wanafunzi.

**18:22** Mstari wa 21 unamalizia na safari ya Paulo akiondoka kutoka Efeso. Mstari wa 22 unaonyesha akitua Palestina (Kaisaria) na kutembelea kanisa huko Yerusalem ("aliendelea, kithiolojia kuongea) na baadaye tena (akateremka) Antiokia ya huko Shamu. Ikumbukwe kuwa Luka haweki kumbu kumbu za mpango kamili wa safari, bali anarukia kwenye tukio muhimu la kithiolojia hadi lingine. Kitabu cha Matendo sio historia ya leo, lakini ni historia nzuri, na iliyo sahihi! Mstari wa 22 unamalizia na safari ya pili ya umisionari na mstari wa 23 wenyewe unanza na safari ya tatu ya umisionari.

▣ **"Kanisa"** angalia Mada Maalu katika Mdo. 5:1 1 .

▣ **"nchi ya Galatia na Frigia"** Kifungu hiki "nchi ya Garatia" bado ni chanzo za mkanganyiko kati ya wasomi ikiwa inarejelea ni mgawanyiko wa kijamii au wa kisiasa ndani ya Uturuki ya sasa. Nchi ya Frigia kwanza inatajwa katika Matendo 2:10. Baadhi waliokuwa kwenye tukio la Pentekoste walitoka katika eneo hili. Paulo alikatazwa kuhubiri katika eneo hili katika Mdo. 16:6. Mtu anashangaa ikiwa kifungu hiki "kuwaimarishwa wanafunzi wote" katika sehemu ya waraka wa Mdo. 18:23 inarejea kwa wale walioongoka siku ya Pentekoste huko Frigia au wale waliokolewa na Paulo huko Derbe, Listra, na Ikonja, uliokuwa Pidisia sehemu ya kusini mwa jimbo la Kirumi Garatia. Huu ni mwanzo wa safari ya tatu ya umisionari (kama vile Mdo. 18:23-21 :1 6).

▣ **"akiwathibitisha wanafunzi"** Paulo alilishika agizo kuu la Mt. 28:1 9-20 kwa kumaanisha. Huduma yake ilijumuisha mambo yote uinjilisti (kama vile Mt. 28:1 9) na kuwafanya kuwa wanafunzi (kama vile Mdo. 1 5:36; Mt. 28:20).

#### **ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA): MATENDO 18:24-28**

<sup>24</sup> Basi Myahudi mmoja, jina lake Apolo, mzalia wa Iskandaria, mtu wa elimu, akafika Efeso; naye alikuwa hodari katika maandiko. <sup>25</sup> Mtu huyo alikuwa amefundishwa njia ya Bwana; na kwa kuwa roho yake ilikuwa ikimwaka, alianza kunena na kufundisha kwa usahihi habari za Yesu; naye alijua ubatizo wa Yohana tu. <sup>26</sup> Akaanza kunena kwa ujasiri katika sinagogi; hata Prisila na Akila walipomsikia wakamchukua kwao, wakamweleza njia ya Bwana kwa usahihi zaidi. <sup>27</sup> Na alipotaka kuvuka bahari aende mpaka Akaya, ndugu wakamhimiza, wakawaandikia wale wanafunzi wamkaribishe, naye alipofika akawasaidia sana wale waliokwisha kuamini kwa neema ya Mungu. <sup>28</sup> Kwa maana aliwashinda Wayahudi kabisa kabisa mbele ya watu wote, akionyesha kwa maneno ya maandiko ya kuwa Yesu ni Kristo.

**18:24-28** Haya yanaonekana kuwa kama maelezo yanayohusiana huenda na

1. Prisila and Akila
2. Wafuasi wa Yohana mbatizaji (hawapo katika mtiririko wa uwandishi wa matukio)
3. Yanasimama kama waraka wa Paulo wa kumhakiki Apolo

**18:24 "Myahudi mmoja, jina lake Apolo"** Sio hali ya kawaida kwa Wayahudi kutajwa kabla ya mungu wa Kiyunani. Alikuwa amesoma sana na mhubiri mwenye ushawishi mzuri (kama vile Mdo. 1 8:24-1 9:1 ). Huduma yake huko Korintho ilikuwa ya msaada, lakini ikajakuwa ya matatizo pale kikundi kimoja kati ya vile vikundi vidogo vitatu (vilivyomshabikia Paulo, Petro, Apolo, kama vile 1 Kor. 1 -4) kilipomchukua kama mshindi wao. Alikataa kurudi Korintho (kama vile 1 Kor 1 6:1 2).

▣ **"mzaliwa wa Iskandaria"** Huu ulikuwa ni mji wa pili kwa ukubwa katika himaya ya Rumi, uliojulikana kwa kuwa na maktaba kubwa na wenye chachu ya kitaaluma. Ulikuwa ni mji wenyekuwa na idadi kubwa ya Wayahudi (ambapo Biblia ya Kiebrania ilitafasiriwa kwa Kiyunani, maandiko ya kale ya Kiyunani) na palikuwa nyumbani kwake Filo, Myahudi maarufu, mwanafalsafa mwenye kufuata mawazo ya Pilato, msomi mwenye kuweza kutafasiri maana zilizofichika.

▣ **"akafika Efeso"** Kitabu cha Matendo sio kitabu chenye maelezo ya ndani, na utaratibu mzuri wa kuandika matukio. Tayari Paulo alikuwa amekwisha ondoka (kama vile Mdo. 1 8:23).

▣ **"Mtu hodari kwa kunena"** Hili neno katika lugha ya Koine ya huko Uyunani laweza kuamaanisha mtu msomi au mwenye ushawishi. Katika maandiko ya kale ya Kiyunani neno *logios* linatumika juu ya maono ya Mungu. Apolo dhahili alikuwa amekilimiwa kwenye kuongea mbele za watu. (Myunani mwenye elimu ya usemaji) kuliko Paulo

(linganisha 1 Kor. 1 :1 7; 2:1 ; 2 Kor. 1 0:1 0; na 1 1 :6). Alikuwa mhubiri wa nguvu!

▣ **"na alikuwa hodari wa maandiko"** Neno "maandiko" linarejea kwenye Agano la Kale (kama vile 1 The. 2:1 3; 2 Tim. 3:1 6; 1 Pet. 1 :23-25; 2 Pet. 1 :20-21 ), pasipo kujumuisha 2 Pet. 3:1 5-16, ambapo maandiko ya Paulo (kwa mfuanano) yanafikiriwa kuwa yenye hali ya kuvuviwa. Apolo alilifahamu Agano la Kale vizuri. Neno "mwenye uwezo" ni *dunatos*, linalotumika kuonyesha uwezo wa Yesu katika maneno na matendo katika Luka 24:19 na kwa Musa katika Matendo 7:22.

**18:25 "mtu huyu alikuwa amekwisha kufundishwa"** Hii ni kauli tendwa yenye mafumbo ya wakati uliopita ainishi (kama vile Luka 1:4). Amekuwa akijifunza katika mafundisho ya Yesu, lakini ni kwa kiwango Fulani au muda Fulani. Curtis Vaughan, *Acts*, uk. 118, tanbihi #2, inaorodhesha vitu vile Apolo angelivijua na kuvihubiri.

1. Yohana alikuwa mtangulizi wa Masihi.
2. Alimzungumzia Masihi kama Mwanakondoo wa Mungu aziondoaye dhambi za dunia.
3. Yesu wa Nazareti alikuwa Masihi.

Pia nafikiri kuwa toba ilikuwa yamkini ikisisitizwa kote katika mahubiri ya Yohana na Yesu

▣ **"njia ya Bwana"** "Njia" kilikuwa cheo cha kwanza kuwaelezea wafuasi wa Yesu katika Mdo. (kama vile Mdo. 9:2; 1 9:9,23; 22:4; 24:1 4,22; Yohana 14:6). Mara nyingi lilitumika katika Agano la Kale (kama vile Kumb. 5:32-33; 31 :29; Zab.27:1 1 ; Isa. 35:8), ambapo inaongelea kuhusu imani katika mfumo wa maisha. Haijulikani ikiwa lina maana hiyo katika andiko hili (kama vile Mdo. 1 8:26). Apolo alifahamu kitu Fulani kumhusu Yesu, lakini inavyoonekana ilikuwa huduma yake ya kwanza hapa duniani na sio injili kabla ya kwenda kalvari, au kabla ya ufufuko.

▣ **"roho yake ilikuwa ikimwaka"** Hii kiuhalisia ni "kuwakwa rohani." Kifungu hiki kinamaanisha kuelezea shauku ya Apolo kwa kile alichofahamu na kutambua kuhusu maisha na mafundisho ya Yesu.

▣ **"naye alikuwa akijua ubatizo wa Yohana tu"** Kifungu hiki kuhusu Apolo chaweza kuwa ni mbinu ya kifasihi iliyotumiwa na Luka kuwatambulisha wafuasi wake katika Mdo. 19:1-7. Paliokuwepo na upotoshaji mbali mbali uliotokea katika karne ya kwanza huko Palestina uliohusianishwa na mafundisho ya Yohana Mbatizaji na mahubiri. Yohana alikuwa ndiye nabii wa mwisho wa Agano la Kale aliyeandaa mapito kwa ajili ya ujio wa Masihi (kama vile Isa. 40:3; Mt. 3:3), lakini hakuwa ndiye mhubiri wa kwanza wa injili. Ikiwa mahubiri ya Apolo yalilenga sana kwa Yohana, hivyo alipoteza umuhimu kamili wa Yesu. wote Yohana na Yesu walisisitiza "toba," "imani," na "maisha ya ki-Ungu." Mwanzoni wote waliwaita Wayahudi kwenye ahadi mpya ya imani na utendaji (agano la uaminifu na imani binafsi katika YHWH). Hata hivyo, ujumbe wa Yesu ulianza kwenye ujasiri wa kutetea mahali pake muhimu. (mf. Yohana 10 na 14), yumkini hili ndilo lilikosekana kwa Apolo.

**18:26 "akaanza kusema kwa ujasiri katika Sinagogi"** Hiki kitenzi ni kile Paulo alichotumia wakati akiongea na Wayahudi ndani ya Sinagogi katika Mdo.13:46; 1 4:3; 1 9:8 na mbele ya Festo katika Mdo.26:26. Apolo alikuwa mhubiri mwenye nguvu na thabiti.

▣ **"akiwa ndani ya Sinagogi"** Tambua Priska na Akila pia alikuwepo. Huu ulikuwa ni utamaduni wa kawaida wa Paulo.

▣ **"Prisila na Akila"** Ametajwa kwanza mara kadhaa, katika Matendo 1 8:1 8,26; Rum. 1 6:3; 2 Tim. 4:1 9.hii ni hali ya juu isiyo ya kawaida. Yumkini alikuwa ni mwenye hadhi ya juu au Mrumi mtu mwenye cheo. Katika Mdo. 18:2, Akila anasemekana kuwa Myahudi, lakini sio Prisila. Walifukuzwa toka Rumi chini ya tamko la mtawala mkuuu Klaudio katika mwaka 49 b.k. walikutana na kumfanya Paulo kuwa rafiki huko Korintho na kuambatana naye huko Efeso. Watatu kati yao walikuwa ni watengeneza mahema.

▣ **"wakamchukua kwao"** Neno hili lintumika kuelezea mtu aliyekubalika au kupokelewa kama rafiki. Haijulikani ni vipi au wapi Prisila na Akila walilifanya hili kwa Apolo. Wangeliweza kuongea nae kibinafsi au wangekwenda naye

nyumbani kwao. Tambua hawakumnyanyasa au kumkabiri wazi wazi!

▣ "**wakamwelezea njia ya Bwana kwa usahihi**" Alikuwa mtu wa kufundishika, ambacho ni kitu adimu kwa watu welevu waliokilimiwa! Dhahili aliitikia habari zao kamili kumhusu Yesu.

**18:27 "alipotaka kuvuka Bahari aende Akaya"** Machapisho ya Kiyunani ya herufi kubwa D yanaongeza maneno "kwenye mahojiano wa Wakristo huko Korintho." kwao alikuwa ni mhubiri wa aina yake.

▣ "**ndugu. . wakawaandikia**" Barua za uthibitisho toka kanisa moja hadi lingine zinarejelea kwa Rumi.16:1 ; 2 Kor. 3:1 ; na 2 Yohana. Hii ilikuwa ni njia ya kanisa la mwanzo ya kuepuka wahubiri waongo waliokuwa wakisafiri.

▣ "**akawasaidia sana wale waliokwisha kuamini kwa neema ya Bwana**" Kuna njia mbili ya kukielewa kifungu hiki.

1. Hiki kinarejelea waumini ambao tayari walikuwa wameokolewa kwa neema (NASB, NKJV, NRSV, TEV)

2. Hii inarejea kwenye neema ya Mungu ya kumwezesha Apolo (NJB)

Kitenzi kikuu, kilichosaidia ni kauli ya kati tendwa elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Apolo alikuwa wa Baraka! Kiambata "kuamini" ni kauli timilifu tendaji, yenye kumaanisha tayari walikuwa wamekwisha amini. Apolo alikuwa akitenda kama mwanafunzi, na sio kama mwinjilisti, huko Korintho.

**18:28** Apolo alitumia Agano la Kale katika njia ile ile kama Petro, Stefano, na Paulo. Akionyesha toka Agano la Kale kuwa Yesu Masihi alikuwa mfano endelevu katika hotuba kwa Wayahudi katika Matendo (angalia maelezo katika Mdo. 17:3).

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni kuhusu mwongozo wa kusoma, ambao una maana kuwa, unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Biblia. Kila moja wetu sharti atembe katika nuru tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni kipaumbele katika tafasiri. Usiachie kazi hii kwa mtoa maoni.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio ya mwisho.

1. kwa nini Prisila aliorodheshwa kwanza mara kwa mara katika agano jipya?
2. Paulo alipataje kuwatambua Prisila na Akila? Kwa nini?
3. Je, Prisila and Akila walirudi tena Rumi? tutajuaje?
4. Linganisha aina ya mafundisho ya Paulo na Apolo.
5. Je Apolo alikuwa Mkristo kabla ya kutembelewa na Akila na Prisila?

## MATENDO YA MITUME 19

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Paulo katika Efeso Yohana	Paulo katika Efeso	Huduma ndefu ya Paulo ktk Efeso	Paulo katika Efeso	Wanafunzi wa katika Efeso
19:1-7	19:1-10	19:1-7	19:1-2a 19:2b 19:3a 19:3b 19:4	19:1-7  msingi wa kanisa la Efeso
19-8-10 Wana wa Skewa	Miujiza ya kumtukua Kristo	19:8-10	19:5-7 19:8-10	19:8-10
19:11-20	19:11-20	19:11-20	wana wa Skewa 19:11-14  19:15 19:16-20	Wayahudi wapunga pepo 19:11-12 19:13-17  19:18-19 19:20
Ghasia Efeso Paulo	vurugu Efeso		Vurugu katika Efeso	Mipango ya
19:21-27	19:21-41	19:21-22	19:21-22	19:21-22 Efeso: vurugu
za		19:23-27	19:23-27	Wafua fedha 19:23-27
19:28-41		19:28-41	19:28-34	19:32-41
			19:35-41	

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("[A Guide to Good Bible Reading](#)")

### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 19:1-7

<sup>1</sup> Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, akiisha kupita kati ya nchi za juu, akafika Efeso; akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko; <sup>2</sup> akawauliza, Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini? Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia. <sup>3</sup> Akawauliza, Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema, Kwa ubatizo wa Yohana. <sup>4</sup> Paulo akasema, Yohana alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia watu wamwamini yeye atakayekuja nyuma yake, yaani, Yesu. <sup>5</sup> Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu. <sup>6</sup> Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri. <sup>7</sup> Na jumla yao walipata wanaume kumi na wawili.

**19:1 "nchi za juu"** Hii inamaanisha njia mbadala ya kupitia nchi zilizoko uwanda wa juu (yaani., kwenye mwinuko) na kwenye makanisa yaliyoanzishwa na Paulo kipindi cha nyuma kwenye shughuli za umishionari huko Galatia ya kusini

▣ **"Efeso"** Michael Magill, *NT TransLine*, ukurasa wa 413, #25, una kidokezo cha taarifa. Huu ilikuwa ni mji mkuu wa Asia ambapo Paulo alikuwa amekatazwa kwenda katika Mdo. 16:6. Alipita hapo kwa muda kidogo katika Mdo. 18:19-21, akipanga kurudi. Sasa amechukua zaidi ya miaka miwili, 19:10."

▣ **"wanafunzi"** Neno linamaanisha kuwa walikuwa waamini (kama vile Mdo. 19:2, "mlipoamini," angalia Mada Maalumu katika Mdo. 3:16 na 6:5) katika Yesu kama Masihi kupitia ujumbe wa Yohana au yawezekana kupitia mahubiri ya Apollo. Roho inavyoonekana alimtuma Paulo kwa njia hii ya juu kwa kusudi la kuwasaidia hawa "wanafunzi" kujua na kuzoea kweli kamili ya injili.

**19:2 "Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?"** Ule ukweli kwamba wanaitwa "wanafunzi" (Mdo. 19:1) na kauli "mlipoamini" inamaanisha hawa walikuwa waaminio. Swali hili linaunganisha (1) ukaribishaji binafsi wa Roho wakati wa mtu kuamini (kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu na kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu) na (2) vitendo vya maandalizi ya Roho ambavyo bila hivyo hakuna ambaye angeamini (kama vile Yohana 6:44,65; Rum. 8:9). Kuna viwango na hatua za kazi za Roho (kama vile Mdo. 8:11, 15-17). Kitabu cha Matendo ya Mitume chenyewe kinatakiwa kiwape onyo wakarimani wa kisasa kutokuwa imani za dini "muhimu" viashiria na utaratibu wa wokovu. Matendo ya Mitume inaandika na kuweka kumbukumbu juu ya yale yaliyotokea. Wokovu ni uhusiano binafsi ambao unajumuisha mtu mzima, lakini mara kwa mara huu ni uzoefu unaoendelea kama uhusiano unaokua ndani na taarifa zaidi za kimaandiko zianeleweka. Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:40.

▣ **"La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia"** Mahubiri ya Yohana yasingeweza kuwa yameleta athari za kiroho bila Roho (kama vile Rum. 8:6-11; 1 Kor. 12:3; 1 Yohana 4:2). Yohana alimtaja Roho katika mahubiri yake (kama vile Mt. 3:11; Marko 1:8; Luka 3:16; Yohana 1:32-33), Lakini lazima ikumbukwe ujumbe wake ulikuwa ni wa maandalizi, sio utimilifu (kama vile Isa. 40:3; Mt. 3:3). Yohana alikuwa nabii wa mwisho wa Agano la Kale na muhubiri wa mpito na mwandalizi wa kuja kwa Masihi. Aliwaelekeza watu kwa Yesu (kama vile Yohana 1:19-42).

**19:3 "Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani?"** Walikuwa wafuasi wa Yohana Mbatizaji inavyoonekana walikuwa waminifu kwa nuru waliyokuwa nayo lakini walihitaji ufafanuzi zaidi kuhusu maisha, kifo, ufufuo na kupaa, (Yaani Injili) ya Yesu, just kama Apollo (kama vile Mdo. 18:24-28).

**19:3-4 "Kwa ubatizo wa Yohana"** Ubatizo wa Yohana ulijumuisha toba na matarajio (kama vile Mt. 3:11; Marko 1:15). Hata hivyo inatakiwa imalizike kwa imani katika Yesu. Kutoka katika Historia tunajua kwamba kulikuwa na vikundi vya uvumi kadhaa ambavyo viliundwa katika karne ya kwanza wakidai kuwa wafuasi wa Yoahana Mbatizaji (*Recognitions of Clement*, chapter 60). Utunzaji wa taarifa hizi unawezekana kuwa ulikuwa njia ya Luka ya kukana na kukataa athari za makundi haya (kama vile Yohana 1:19-42).

**19:4 "wamwamini yeye"** Angalia Mada Maalum: Amini katika Mdo. 3:16 and 6:5.

**19:5 "wakabatizwa"** Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:38.

▣**"kwa jina la Bwana Yesu"** Luka anafunua ubatizo kama "katika Jina la Yesu" (kama vile Mdo. 2:38; 8:12,16; 10:48). Angalia **MADA MAALUM: JINA LA BWANA** katika Mdo. 2:21. Mathayo anafunua kama "Katika jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu" (kama vile Mt. 28:19). Kanuni ya ubatizo sio msingi wa wokovu lakini sehemu ya muhimu sana kwa mtu kubatizwa. Kuiona kanuni kama ufunguo ni kuweka msisitizo katika sehemu isiyosahihi. Wokovu sio usahihi wa kisakramenti wa ibada lakini lango kuingia katika toba/uhusiano wa kiimani na Yesu. Angalia Kidokezo katika Mdo. 2:38. Kama tunavyojua, Apollo, ambaye naye pia alijua ubatizo wa Yohana tu, yeye hakubatizwa upya! Roho alikuwa dhahiri katika mahubiri yenye nguvu na mafundisho.

**19:6 "Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao"** kuwekea mikono mara kwa mara kunatajwa kwa kuunganisha na Roho (kama vile Mdo. 8:16-17; 9:17), lakini sio siku zote (kama vile Mdo. 10:44, angalia Mada Maalum katika Mdo. 6:6). Biblia inaunganisha Roho na mwamini katika namna tatu tofauti:

1. wakati wa imani
2. wakati wa ubatizo
3. wakati wa kuwekea mikono

Mgawanyiko huu unatakiwa utuonye dhidi ya elimu ya imani za dini kwa mfumo huo. Matendo ya Mitume haikukusudiwa kufundisha utaratibu fulani wa kinjozi. Lazima nikiri kwamba wanafunzi hawa kumi na mbili wa Yohana kunena kwa lugha kunanishangaza sana hata mimi. Siku zote katika Matendo ya Mitume kunena kwa lugha ni ushahidi wa kuamini watangazaji wa Kiyahudi kwamba Mungu

1. amelikubali kundi jipya au
2. amevunja kizuizi cha kijiografia (angalia dokezo kamili katika Mdo. 2:4b)

Ni kundi gani jipya watu hawa walikuwa wakiwakilisha? Walikuwa tayari wanafunzi (kama vile Mdo. 19:1). Kwanini Luka alichagua kuweka kumbukumbu ya tukio hili? Alichagua kulitambulisha pamoja na Apollo katika Mdo. 18. Hii haishabihiani na utaratibu, ambao yawezekana unamaanisha kwamba wafasiri wa kisasa wanajaribu kufitisha ajenda au vipimo vya ufasiri juu ya maandiko ya Luka ambayo hayarandani! Labda tukio hili la kunena kwa Lugha ni zaidi ya yale katika Korintho! Hii ni aina yake ya kushangaza katika njia ya Agano Jipya inayoelezea kuja kwa Roho kwa watu binafsi.

1. kuja juu ya (*erchomai plus epi*), kama vile Mt. 3:16; Luka 19:6 [kama *epi*, 2:25]
2. kubatizwa kwa, kama vile Mt. 3:11; Marko 1:8; Luka 3:16; 11:16; Yohana 1:33; Mdo. 1:5
3. kushuka juu ya, kama vile Mt. 3:16; Marko 1:10; Luka 3:22
4. kuja juu ya (*eperchomai ukiongeza epi*), kama vile Luka 1:35; Mdo. 1:8
5. kujazwa na, kama vile Luka 1:15,41,67; Mdo. 2:4; 4:8,31; 9:17; 13:9,52
6. kumiminiwa na (*ekcheō*), kama vile Mdo. 2:17-18,33; 10:45; Tito 3:6
7. kupokea, kama vile Mdo. 2:33,38; 8:15,17,19; 10:47; 19:2
8. kutoa, Mdo. 5:32; 10:45; 15:8

9. kuanguka juu ya (*epiπτῶ*), kama vile Mdo. 8:16; 10:44; 11:15

▣ **"na kutabiri"** Neno hili lina visawe vya tabia ya kishauku (kama vile 1 Sam. 10:10-12; 19:23-24). Muktaadha unaweza ukasaidia fasiri hii. Hata hivyo neno hili katika 1 & 2 Wakorintho (kama vile 1 Kor. 11:4,5,9;14:1,3,4,5,24,31,39) linamaanisha kutangaza injili kwa injili. Ni ngumu kutoa maana ya unabii katika Agano Jipya. Tokea kujazwa kwa Roho mara kwa mara kunaunganishwa kutangaza injili kwa ujasiri, Hili ni kusudio la muktaadha huu pia. Angalia [MADA MAALUM: UNABII WA AGANO JIPYA](#) katika Mdo. 11:27.

**19:7 "Na jumla yao walipata wanaume kumi na wawili"** Kumi na mbili ni moja ya namba kadhaa ambazo zinatumiwa mara kwa mara kiishara katika Biblia, lakini hapa inaonekana kuwa kihistoria. Angalia Mada Maalum: Kumi na Mbili katika Mdo. 1:22 na Hesabu za kiishara katika Maandiko katika Mdo 1:3

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 19:8-10**

<sup>8</sup> Akaingia ndani ya sinagogi, akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu, na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu. <sup>9</sup> Lakini wengine walikaidi, wakakataa kuamini, wakiitukana ile Njia mbele ya mkutano; basi, akaondoka akawaacha, akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina lake Tirano. <sup>10</sup> Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote

**19:8 "Akaingia ndani ya sinagogi "** Huu ulikuwa ni utaratibu wa kawaida (kama vile Mdo. 9:20; 13:5,14; 14:1; 17:2, 10; 18:4,19,26).

▣ **"akanena kwa ushujaa"** Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati timilifu. Ilikuwa ni moja ya matokeo ya "kujazwa na Roho" (kama vile Mdo. 4:13,29,31; 9:28,29; 14:3; 18:26). Paulo aliomba jambo hili katika Waefeso. 6:19.

▣ **"miezi mitatu"** Sinagogi hili katika Efeso inavyoonekana ilimruhusu Paulo kuhubiri, kufundisha na kufikiri pamoja nao kwa Sabato nyingi. Hii yenyewe inaonesha kiwango cha kufunguka kwa injili ni heshima kwa uwezo wa ki-Mungu aliyopewa Paulo.

▣ **"ufalme wa Mungu"** Haya yalikuwa ni maudhui makuu ya mahubiri ya Yesu. Inamaanisha utawala wa Mungu katika maisha ya binadamu sasa na kwamba siku moja yatahitimishwa duniani kote kama ilivyo mbinguni (kama vile Mt. 6:10). Angalia Mada Maalum katika Mdo.1:3.

**19:9 "baadhi walikuwa wenyu ugumu na wenye kuasi"** Wote wanaosiki injili wana uchaguzi (kama vile Mdo.17:32, 34). Hii inaaksi fumbo la mpanzi (kama vile Mathayo 13; Marko 4). Hii ni siri ya uovu (kama vile Mdo. 2 Kor. 4:4). Neno "kuwa na shingo ngumu" (*sklērunō*) ni kauli tendwa elekezi wa wakati usiotimilifu (kuasi ni kauli tendali elekezi ya wakati usiotimilifu), ambayo inamaanisha mwanzo wa kitendo au kurudiwa rudiwa kwa kitendo kwa wakati uliopita. Hili ni neno lenyewe linalotumiwa katika Rum. 9:18 kuelezea kufanywa mioyo migumu kwa wana wa Israeli kulikofanywa na Mungu na pia kurudiwa kwa kitenzi katika Waebrania 3 na 4 (kama vile Mdo. 3:8,13,15; 4:7) Kushughulika na ugumu wa mioyo ya wana wa Israeli wakati wa kutapakaa jangwani. Mungu hajishughulishi kiuntendaji kufanya migumu mioyo ya wanadamu ambao anawapenda na wamefanywa kwa sura yake, lakini haruhusu uasi wa mwanadamu kujidhihirisha wenyewe (kama vile Rum. 1:24,26,28) na uovu binafsi kushawishi wale aliowaumba (kama vile Efe. 2:1-3; 4:14; 6:10-18).

▣ **"kuongea uovu juu ya Njia ile mbele ya watu"** Injili kimsingi inatofautiana kutokana na kutojitenga na kujikita katika jozi za akili ya utenda kazi wa dini ya Kiyahudi kwamba kulikuwa na msingi wa pamoja unaofanana uliowezekana ikiwa nguzo za injili zilikataliwa. Utaratibu unaojirudia rudia wa Luka wa upinzani mkali wa Kiyahudi kwa injili unaendelea (kama vile Mdo. 13:46-48; 18:5-7; 19:8-10; 28:23-28).



▣ **"Njia ile"** Angalia vidokezo katika Mdo. 18:25 na 19:23.

▣ **"shule ya Tirano"** Mswaada wa Agano Jipya (The codex Bezae), D, kutoka karne ya tano, anaongeza kwamba Paulo alikuwa akifundisha kutokea saa 5 za asubuhi mpaka sa 10 jioni, wakati sehemu kubwa ya mji walikuwa na kipindi cha mapumziko na majengo yalikuwa yakipatikana. Hili laweza kuwa jambo la desturi za kinywa. Paulo angeweza kufanya biashara yake wakati ule ule wa masaa ya biashara na alafu afundishe wakati wa kipindi kinachobaki (kama vile Mdo. 20:34).

Kumekuwa na nadharia kadhaa kama utambulisho wa Tirano.

1. Alikuwa mpotoshaji anayetajwa na Suidas. Suidas aliandika katika karne ya kumi, lakini alitumia vyanzo vya kuaminika vilivyoandikwa nyakati za kiuandishi na ualimu. Kazi yake ya kifasihi ni kama kamusi ya kisiasa, na watu wa kiuandishi.
2. Alikuwa mwalimu wa kiyahudi (Meya) aliyeendesha shule binafsi kwa kufundisha sheria ya Musa lakini hakuna ushahidi wa kimaandiko kwa nafasi hii.
3. Jengo hili kwa asili lilikuwa uwanja wa michezo lakini baadaye ukumbi wa masomo uliomilikiwa au kuitwa kwa jina la Tirano

Paulo alitakiwa kuondoka katika Sinagogi na inavyoonekana kulikuwa na waongofu wengi wakutumia nyumba, hivyo alikodi ukumbi wa kuendesha masomo. Hii ilimruhusu yeye kupata mawasiliano na watu wa Efeso.

**19:10 "miaka miwili"** Katika Mdo. 20:31 Paulo anataja muda aliochukua wote katika jimbo (miaka mitatu).

▣ **"waliokaa katika Asia waliisikia sauti"** Huku ni kutia chumvi kwa wazi kabisa. Yesu mara nyingi alizungumza kwa kuweka chumvi. Hii ni sehemu ya asili na mtindo wa fasihi ya mashariki ipendayo nahau.

### **MADA MAALUM: FASIHI YA KIMASHARIKI (mafumbo ya kibiblia)**

1. Utambzi huu wa ndani (yaani, kwamba Biblia ni kitabu cha mashariki, si kitabu cha magharibi) umekuwa msaada zaidi kwangu binafsi kama mtu anayependa na kuiamini Biblia kama Neno la Mungu. Katika kujaribu kuichukulia Biblia kwa umakini inakuwa dhahiri kwamba maandiko tofauti tofauti yanaifunua kweli katika uteuzi, si katika namna za kinfumo. Andiko moja lililovuviwa haliwezi kufuta ama kushusha andiko lingine lililovuviwa! Kweli huja katika kuyafahamu Maandiko (Maandiko yote, si sehemu tu, iliyovuviwa, kama vile 2 Tim. 3:16-17), si kunukuu kifungu kimoja (kuhakiki maandiko)!
2. Kweli nyingi za kibiblia (fasihi ya mashariki) zinawasilishwa katika are presented in mtindo wa lahaja ufanano wa kimaafumbo (kumbuka waandishi wa Agano Jipya, isipokuwa Luka, ni wanafikra wa Kiebrania, walioandika katika Kiebrania cha kawaida. Fasihi ya Hekima na Fasihi ya Ushahiri inawasilisha kweli katika mfuatano. Huu ufanano kinzani hutenda kazi kama fumbo. Huu uigaji wa ufanano hutenda kazi kama ufanano wa vifungu). Kwa kiasi fulani yote kwa ni ya kweli kwa usawa! Mafumbo haya ni ya kimaumivu kwa mapokeo ya kimadhehebu yaliyotunzwa kwa upendo mkubwa!
  - a. Maamuzi ya kabla dhidi ya utashi huru wa mwanadamu
  - b. Ulinzi wa mwamini dhidi ya hitaji la ustahimilivu(angalia Mada Maalum: Uatahimilivu)
  - c. Dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari
  - d. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama Mwanadamu
  - e. Yesu kuwa sawa na Baba dhidi ya Yesu aliyekuwa mtii kwa Baba
  - f. Biblia kama neno la Mungu dhidi ya uandishi wa kibinadamu
  - g. Kutotenda dhambi (ukamilifu, kama vile Warumi 6) dhidi ya kutenda dhambi kidogo
  - h. Kuhesabiwa haki kwa mwanzo moja kwa moja dhidi ya utakaso endelevu (angalia Mada Maalum: Utakaso)
  - i. Kuhesabiwa haki kwa imani (Warumi 4) dhidi ya kuhesabiwa haki kwa njia ya matendo (kama vile

Yakobo 2:14-26)

- j. Uhuru wa Mkristo (kama vile Rum. 14:1-23; 1 Kor. 8:1-13; 10:23-33) dhidi ya wajibu wa Mkristo (kama vile Gal. 5:16-21; Efe. 4:1)
- k. Mungu apitaye uwezo wa kibinadamu dhidi ya uwepo wake wa kila mahali
- l. Hatimaye Mungu asiyejulikana dhidi ya Mungu ajulikanaye katika maandiko na ndani ya Kristo.
  
- m. Sitiari nyingi za Paulo kwa ajili ya wokovu
  - 1) Uasilishaji (kupanga mtoto/kumtwaa)
  - 2) Utakaso
  - 3) kuhesabiwa haki
  - 4) Kukombolewa
  - 5) Kutukuza
  - 6) Majaaliwa
  - 7) Upatanisho
- n. Ufalme wa Mungu uliopo dhidi ya ule utakaotimia mbeleni
- o. Toba kama zawadi ya Mungu (kama vile Mdo.11:18; Rum. 2:4; 2 Tim. 2:25) dhidi ya toba kama mwitikio wa lazima kwa ajili ya wokovu (kama vile Marko 1:15; Mdo. 20:21)
- p. Agano la Kale ni la kudumu dhidi ya Agano la Kale limekwisha kupita na ni batili na utupu (kama vile Mt. 3:17-19 dhidi ya Mt. 5:21-48; Warumi 7 dhidi ya Wagalatia 3)
- q. Waamini ni watumishi/watumwa au wana/warithi

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 19:11-20**

<sup>11</sup> Mungu akafanya kwa mikono ya Paulo miujiza ya kupita kawaida; <sup>12</sup> hata wagonjwa wakaletewa lesu na nguo zilizotoka mwilini mwake, magonjwa yao yakawaondokea, pepo wachafu wakawatoka. <sup>13</sup> Baadhi ya Wayahudi wenye kutanga-tanga, nao ni wapunga pepo, wakajaribu kutaja jina la Bwana Yesu juu yao waliopagawa na pepo wachafu, wakisema, Nawaapisha kwa Yesu, yule anayehubiriwa na Paulo. <sup>14</sup> Walikuwako wana saba wa mtu mmoja Skewa, Myahudi, kuhani mkuu, waliofanya hivyo. <sup>15</sup> Yule pepo mchafu akawajibu, akawaambia, Yesu namjua na Paulo namfahamu, lakini ninyi ni nani? <sup>16</sup> Na yule mtu aliyepagawa na pepo mchafu akawarukia wawili, akawaweza, akawashinda, hata wakatoka mbio katika nyumba ile hali wa uchi na kujeruhiwa. <sup>17</sup> Habari hii ikajulikana na Wayahudi wote na Wayunani waliokaa Efeso, hofu ikawaingia wote, na jina la Bwana Yesu likatukuzwa. <sup>18</sup> Na wengi wa wale walioamini wakaja wakaungama, wakidhihirisha matendo yao. <sup>19</sup> Na watu wengi katika wale waliotumia mambo ya uganga wakakusanya vitabu vyao, wakavichoma moto mbele ya watu wote; wakafanya hesabu ya thamani yake, wakaona ya kwamba yapata fedha hamsini elfu. <sup>20</sup> Hivyo ndivyo neno la Bwana lilivyozidi na kushinda kwa nguvu.

**19:11** Hii sio mara ya kwanza Mungu anatumia miujiza ya kupita kawaida kuthibitisha kweli yake na Mzungumzaji wake (kama vile Mdo. 3:1-10; 5:15; 8:6,13; 9:40-42; 13:11-12; 14:8-11). Ushirikina na matendo ya kiibada za shetani walikuwa wametawanyika na kijidhabiti katika Efeso. Mungu aliye mwingi wa rehema aliruhusu nguvu yake ya kupita kawaida na mamlaka kukaa katika Masihi kuelezea mwenyewe kupitia Paulo kwa watu hawa waliofungwa na shetani. Oh, rehema za Mungu!

**19:12 "leso"** Hii yawezekana ilikuwa lesu zilizofungwa kuzunguka kichwani wakati wa kazi.

▣ **"nguvu"** Hii inamaanisha mavazi ya kazi kama vile wawaayo maseremala. Uponyaji huu ulionesha huruma ya Mungu, nguvu na kuthibitisha injili na huduma ya Paulo.

▣ **"pepo wachafu wakawatoka"** Mapepo haya (kama vile Luka 10:17) yanaitwa "roho wachafu" (kama vile Mt. 12:45; Luka 7:21; 8:2; 11:26; Mdo. 19:12,13,15,16). Lakini pia Luka anawaita "roho wachafu" (kama vile Mdo. 5:16; 8:7; angalia Mada Maalum katika Mdo. 5:3 na 5:16). Katika Mdo. 16:16 pepo linaitwa "roho ya nyoka (miungu)." Tungo hizi zote zinaonekana kuwa visawe.

Paulo mara kwa mara anazungumzia vipengele vya mapepo kama "utawala wote na mamlaka na nguvu na utawala" (Efe. 1:21), "watawala na mamlaka katika ulimwengu wa roho" (Efe. 3:10), au "dhidi ya watawala, dhidi ya nguvu, dhidi ya nguvu za giza za ulimwengu huu, dhidi ya nguvu za roho za ubaya katika maeneo ya ulimwengu wa mbingu" (Efe. 6:12). Hii lazima ilimaanisha baadhi ya viwango vya roho za kipepo zenye kujipanga. Lakini kwa namna gani na kwa nini na wapi na nani yanadhaniwa kwasababu Biblia haichagui kufunua maelezo ya ulimwengu wa roho. Haifunui kwa usahihi nguvu ya Kristo (na ya Mitume) juu ya shetani na ufalme wake wa giza na mauti. "Jina" la Yesu liko juu ya majina yote! Kumjua yeye kunaleta wokovu, amani, ukamilifu, urejesho, na afya.

### **MADA MAALUM: MALAIKA KATIKA MAANDIKO YA PAULO**

Walimu wa sheria za Kiyahudi walifikiri kwamba malaika waliona kijicho juu ya upendo na utulivu wa Mungu (yaani, utoaji wa amri zake juu ya Mt. Sinai) kwa mwanadamu aliyeanguka na, hivyo, hawa walikuwa na vita juu yao. Walimu wa Uongo waliodai kuwa na ujuzi wa kipekee walidai kwamba wokovu ulipatikana tu kwa maneno ya siri kupitia maeneo ya vita vya kimalaika (kama vile Wakolosai na Waefeso), ambayo yaliwaongoza mungu mwema, aliyeinuliwa.

George Eldon Ladd ana muhutasari mzuri wa maneno yaliyotumiwa na Paulo kuwazungumzia malaika katika kitabu chake cha *A Theology of the New Testament*:

"Paulo harejelei juu ya malaika wema na wabaya tu, juu ya Shetani na pepo; analitumia kundi lingine la maneno kuonyesha viwango vya roho za kimalaika. Istilahi hii ni kama ifuatavyo:

'Utawala' [*archē*], I Kor. 15:24; Efe. 1:21; Kol. 2:10

'Mamlaka' [*archai*; RSV, "wana wa mfalme"], Efe. 3:10; 6:12; Kol. 1:16; 2:15; Rum. 8:38

'Mamlaka' [*exousia*], I Kor. 15:24; Efe. 1:21; Kol. 2:10

'Ufalme' [*exousiai*; RSV, "mamlaka"], Efe. 1:21

'Nguvu' [*dynamis*], I Kor. 15:24; Efe. 1:21

'uwezo' [*dynameis*], Rum. 8:38

'Enzi' [*thronoi*], Kol. 1:16

'Usultani' [*kyriotēs*; RSV, "ufalme"], Efe. 1:21

'Vitu vya enzi' [*kyriotētes*], Kol. 1:16

'Wakuu wa giza hili,' Efe. 6:12

'Ulimwengu wa roho (majeshi) wa uovu katika ufalme huu,' Efe. 6:12

'Nguvu za giza,' Kol. 1:13

'Kila jina liitwalo,' Efe. 1:21

'Vya mbinguni, vya duniani, na vya chini ya nchi,' Flp. 2:10 " (uk. 401).

**"Wayahudi wenye kutanga-tanga, nao ni wapunga pepo"** Wapunga pepo wa Kiyahudi walikuwa ni wa kawaida waliozoeleka (kama vile Luka 11:19). Mukadha huu kwa usahihi unaonesha kwamba upungaji pepo sio jambo la kanuni ya muujiza (majina), lakini kwa uhusiano wa kibinafsi na Yesu. Ikiwa kifungu hiki cha habari kisingekuwa cha huzuni basi kingekuwa cha kuchekesha! Josephus anatwambia juu ya upungaji pepo wa Kiyahudi katika *Antiq.* 8.2.5 kwa Eleaza, ukitumia nuio la Sulemani.

**19:13 "pepo wachafu"** Hii inamaanisha kipepo. Agano Jipya mara kwa mara juu ya ukweli huu wa kiroho, lakini haijadili asili yake au maelezo kuhusu utaratibu wake au shughuli. Udadisi, hofu, na utendaji wa huduma unahitaji kusababisha makisio mengi. Huna karama ya upungaji pepo inayoorodheshwa katika Agano Jipya, lakini hitaji lake liko wazi. Baadhi ya vitabu vya msaada ni

1. *Christian Counseling and the Occult* by Kouch

2. *Biblical Demonology and Demons in the World Today* by Unger
3. *Principalities and Powers* by Montgomery
4. *Christ and the Powers* by Hendrik Berkhof
5. *Three Crucial Questions About Spiritual Warfare* by Clinton E. Arnold

Angalia Mada Maalum: Kipepo katika Mdo. 5:16.

**19:14 "Skewa, Myahudi, kuhani mkuu"** Wana taaluma wa kisasa hawawezi kutafuta jina hili katika maandiko mengine. Ni tatizo kwa kuhani mkuu wa Kiyahudi (*archiereus*) kuwa katika Efeso. Kulikuwa na Sinagogi la eneo fulani, lakini hekalu pekee la kiyahudi lilikuwa Yerusalemu tu. Luka analitumia neno hilihili mara kwa mara katika injili yake na Matendo ya Mitume kwa Kuhani Mkuu na familia yake katika Yerusalemu. Wengine wanadhania kwamba mtu huyu alikuwa kwa namna fulani ameunganishwa na familia ya Kuhani Mkuu, au yawezekana kiongozi wa moja ya (Kama vile 1 Nyakati 24:7-19). Ikiwa mtu huyu na wanawe walikuwa makuhani, inashangaza kwamba hawakutumia YHWH kama jina lenye nguvu kushughulikia roho kama wafanyavyo kwa uchavi na ibada za kishetani.

**19:15 "Yesu namjua na Paulo namfahamu"** kitenzi cha kwanza ni *ginōskō*; cha pili ni *epistamai*. Kwa namna fulani ni visawe. Yote yanatumika lakini kwa muktadha huu ni wazi utofauti uliotengenezwa kati ya maarifa ya Yesu kama Kristo ya pepo hili na Paulo kama msemaji wake,

**19:17** Luka anaweka kumbukumbu wa jambo hili kuonesha kwa namna gani Roho alikuwa anamkuza Yesu (kauli tendwa elekezi ya wakati usiotimilifu) Yesu (kama vile Yohana 14:25; 16:13-14).

**19:18 "wa wale walioamini"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Swali ni, Je waamini walikuwa katika ibada za siri au tungo hii inamaanisha imani yao mpya katika Injili? Pia inawezekana kwamba waamini wapya wa injili walikuwa kwa mwanzo wakishawishika na uchawi wao wa kwanza. Angalia Mada Maalum: Vitenzi vya njeo za Kiyunani vilivyotumika kwa ajili ya wokovu katika Mdo.2:40. Waabuduo wa siri wa kwanza labda walikuwa wameshawishika na kile kilichotokea kwa wapunga pepo wa Kiyahudi katika Mdo. 19:13-16. Ujumbe wa tukio hili ulionesha nguvu ya mtu, jina la Yesu, likienea kwa kasi (kama vile Mdo. 19:17). Watu hawa walikuwa wwanajua nguvu ya "jina"

▣ **"wakaja"** Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati usiotimilifu.

▣ **"wakaungama, wakidhihirisha matendo yao"** Shamu ya kale ilikuwa imejaa ibada za siri ilikuwa iani iliyozoeleka kwamba kufunua kanuni ya kimiujiza ya mtu ilisababisha isiwe fanisi. Hii ilikuwa njia ya kukataa shughuli zao za siri zilizopita. Kuna aina ya fasihi ya kimiujiza inayojulikana katika ulimwengu wa kale "Maandiko ya Kiefeso"! Tukio hili linaonesha uweza wa injilii juu ya ibada za siri (kama vile Mdo. 19:20).

## MADA MAALUMU: KUTUBU (AGANO JIPYA)

Toba (sambamba na imani) ni hitaji la pande zote mbili yaani Agano la Kale (Nacham, BDB 636, KB 688, mf., Kut. 13:17; 32:12,14; Shuv, BDB 996, KB 1427, m.f. 1 Flm. 8:47; Eze. 14:6; 18:30; tazama [Mada Maalum: Toba](#) [Agano la Kale]) na Agano Jipya.

1. Yohana Mbatizaji (Mt. 3:2; Marko 1:4; Luka 3:3,8)
2. Yesu (Mt. 4:17; Marko 1:15; Luka 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3)
3. Petro (Matendo 2:38; 3:19; 8:22; 11:18; 2 Petro. 3:9)
4. Paulo (Matendo 13:24; 17:30; 20:21; 26:20; Rum. 2:4; 2 Kor. 2:9-10)

Lakini Toba ni nini? Ni huzuni ya kiroho? Ni kumaanisha kuacha dhambi? Eneo zuri katika Agano la Jipya katika kuelewa maana tofauti ya dhana hii ni 2 Wakorintho 7:8-11, ambapo hizo tatu zinanahusiana, lakini ni tofauti, maneno ya Kiyunani yanatumiika.

1. "huzuni" (*lupeō*, kama vile. mst. 8 [mara mbili], 9 [mara tatu], 10 [mara mbili], 11). Inamaanisha kupata maumivu au kutambua na ina maana ya kitheolojia isiyofungamana na upande wo wote.
2. "toba" (*metanoēō*, kama vile mst. 9,10). Ni muunganiko wa neno "baada ya" na "kumbukumbu," ambayo inadokeza akili mpya, njia mpya ya kufikiri, mtazamo mpya kuhusu maisha na Mungu. Hii ni toba ya kweli.
3. "majuto" (*metamelomai*, kama vile mst. 8 [mara mbili], 10). Ni muungano wa "baada ya" na "uangalifu." Linatumika juu ya Yuda katika Mt. 27:3 and Esau katika Ebr. 12:16-17. Linadokeza sikitiko juu ya matokeo, si juu ya matendo. Toba na imani ni matendo ya kimaagano yanayohitajika (kama vile Marko 1:15; Matendo 2:38,41; 3:16,19; 20:21). Kuna baadhi ya maandiko ambayo yanadokeza kwamba Mungu hutoa toba (kama vile Matendo 5:31; 11:18; 2 Tim. 2:25). Lakini maandiko mengi yanalitazama hili kama mwitikio muhimu wa agano la mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu ya wokovu huru.

Maelezo ya maneno yote ya Kiebrania na Kiyunani yanahitajika ili kuelewa maana kamili ya toba. Neno la Kiebrania linadai "mabadiliko ya tendo," ambapo neno la Kiyunani linadai "mabadiliko ya akili." Mtu aliyeokolewa anapokea akili na moyo mpya (kama vile Eze. 36:26-27). Anafikiri tofauti na kuishi tofauti. Badala ya "Kilicho ndani ni kwa ajili yangu?" sasa swali ni "Mapenzi ya Mungu ni nini?" Toba si hisia ambazo hufifia au dhambi ya moja kwa moja, bali uhusiano mpya na Aliye Mtakatifu ambaye humbadilisha mwamini kwa uendelevu na kuwa ndani ya utakatifu. Si rahisi mtu akasitisha kufanya kitu au kuachana nacho, bali ni kwa mtazamo na uelekeo mpya katika maisha. Anguko linatusabisha sisi kujitazama wenyewe lakini injili inaturuhusu sisi kumtazama Mungu. Toba ni tendo la kugeuka na imani ni tendo la kugeuka kitu/kifikra!

"**muujiza**" Angalia Mada Maalum katika Mdo. 8:9. Vinavyoitwa "vitabu" (*biblos*) vilimaanisha vitabu vikubwa au magombo madogo palipoandikwa viapo au laana. Hivi vilikuwa vikivaliwa kama hirizi. Gharama kubwa inaonesha (1) kwa namna gani watu hawa walikuwa wachawi na (2) kwa nama gani injili ili wafungua huru!

▣ "**wakavichoma moto mbele ya watu wote**" Hizi zilikuwa ni karatasi zilizotengezwa kwa ngozi na vitabu vilivyotafutwa vilivyokuwa aghali. Kuvichoma kwao kulikuwa ni toba ya wazi ya waumini na kukiri kwao kwa imani ndani ya Kristo "nguvu"!

**19:20** Ujumbe wa injili unabinafsishwa (yaani neno la Bwana) na kufanywa kimutahsari. Muhtasari wa Luka unatusaidia kugawa Matendo ya Mitume katika vipengele sita (kama vile Mdo 6:7; 9:31; 12:24; 16:5; 19:20; 28:31).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 19:21-22**

<sup>21</sup> Mambo hayo yalipokwisha kumalizika, Paulo akaazimu rohoni mwake, akiisha kupita katika Makedonia na Akaya, aende Yerusalemu, akisema, Baada ya kuwako huko, yanipasa kuuona na Rumi pia. <sup>22</sup> Akatuma watu wawili miongoni mwa wale waliomtumikia kwenda Makedonia, nao ni Timotheo na Erasto, yeye mwenyewe akakaa katika Asia kitambo.

**19:21**

**NASB** "Paulo alidhamiria rohoni mwake"  
**NKJV** "Paulo alikusudia katika roho"  
**NRSV** "Paulo aliamua katika roho yake"  
**TEV, NJB** "Paulo aliamua akilini mwake"  
**TEV (DOKEZO)** "Paulo akiongozwa na Roho, aliamua"

Hapa ni muunganiko wa ukuu wa Mungu na utashi huru wa kibinadamu. Hajajulikana ikiwa matumizi ya neno hili "spiritroho" refers tolinamaanisha:

1. Roho Mtakatifu au
2. roho ya binadamu (kama vile Mdo. 7:59; 17:16; 18:25; Rum. 1:9; 8:16; 1 Kor. 2:11; 5:4; 16:18; 2 Kor. 2:11; 7:13; 12:18; Gal. 6:18; Flp. 4:23). Ikiwa ni Roho Mtakatifu, huu ni mfano mwingine wa uongozi wa kiungu unaounganishwa na mwikitio sahihi wa kibinadamu.

Luka mara kwa mara anatoa maoni mafupi kutambulisha tukio ambalo linatokea baadaye. Hii ni hakika kuwa inawezekana Luka anamfanya Paulo aamue kwenda Yerusalemu kama matokeo ya uongozi wa Mungu (yaani *kufa*, Mdo. 19:21; Angalia kidokezo kamili katika Mdo. 1:16), na sio matokeo ya vurugu zilizosababishwa na Demetrio na wafua fedha wa Efeso (kama vile Mdo. 19:23-41).

▣ **"yanipasa kuuona na Rumi pia"** Paulo alihitaji (*dei*) kutembele kanisa la Rumi (kama vile Mdo. 9:15; Rum. 1:10) akiwa anaelekea Uhispania (kama vile Rum. 15:24, 28). Alitaka wao wamjue yeye na kusaidia kazi yake ya umisheni. Yeye pia alitaka kuongeza Baraka zake. Karama kwa hali zao.

**19:22 "Erasto"** Kuna mtu anatajwa kwa jina la huyu bwana katika Rum. 16:23. Anaitwa mwazini wa mji wa Korintho. Jina hili linatokea tena katika 2 Tim. 4:20. Ikiwa inamzungumzia mtu huyuhuyu, hiyo haijaleweka bado.

▣ **"yeye mwenyewe akakaa katika Asia kitambo"** Injili ilienea kwa utukufu, ikiathiri na kugeuza jimbo (kama vile 1 Kor. 16:9).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 19:23-27**

<sup>23</sup> Wakati huo kukatukia ghasia si haba katika habari ya Njia ile. <sup>24</sup> Kwa maana mtu mmoja, jina lake Demetrio, mfua fedha, aliyekuwa akifanya vihekalu vya fedha vya Artemi, alikuwa akiwapatia mafundi faida nyingi. <sup>25</sup> Akawakusanya hao, pamoja na wengine wenye kazi ile ile, akasema, Enyi wanaume, mnajua ya kuwa utajiri wetu hutoka katika kazi hii. <sup>26</sup> Tena mnaona na kusikia ya kwamba si katika Efeso tu, bali katika Asia yote pia Paulo huyo ameshawishi watu wengi na kuwageuza nia zao, akisema ya kwamba hiyo inayofanywa kwa mikono siyo miungu. <sup>27</sup> Si kwamba kazi hii yetu ina hatari ya kudharauliwa tu; bali na hekalu la mungu mke aliye mkuu, Artemi, kuhesabiwa si kitu, na kuondolewa utukufu wake, ambaye Asia yote pia na walimwengu wote humwabudu.

**19:23 "Njia ile"** Haya yalikuwa maelezo ya awali kabisa kwa Ukristo. Inazungumzia dhana ya Agano la Kale (mfano Zaburi 1:1,6; 5:8; 25:4,8,9,12; 27:11; 37:5,7,23,34; 119:101, 105) ya mtindo wa maisha ya imani (kama vile Mdo. 9:2; 19:9,23; 22:4; 24:14,22; pia yawezekana 18:25-26).

**19:24 "vihekalu vya fedha"** Hii inamaanisha taswira ndogo za fedha (1) ya Hekalu la Artemi au (2) kimondo kilichokuwa na mwonekano kama mwanamke. Watafiti wa mambo ya kale wamepata taswira nyingi za fedha za mungu huyu, lakini sio sehemu za ibada (hekalu) lenyewe lilikuwa ni moja ya maajabu saba ya dunia. Angalia kidokezo katika Mdo. 18:19, #4.

▣ **"Artemi"** Hekalu la miungu ya Artemi aliyekuwa akiabudiwa Efeso hatambulikani na Diana wa Rumi. Huyu mungu yuko karibu na Cybele, mungu mwanamke. Desturi hizi za kiibada zilikuwa na mfanano na ibada za uzao za Kanaani (angalia M. R. Vincent, *Word Studies*, vol. 1, ukurasa wa 271).

▣ **"faida nyingi"** mateso yalikuwa na au chimbuko la kiuchumi (kama vile Mdo. 19:25,27). Angalia kidokezo kamili kwenye makusudi ya Luka ya urahisishaji bila kutoa maelezo kikamilifu (yaani *litotes*) katika Mdo. 12:18.

▣ **"wafua vyuma"** Kutoka katika neno hili la Kiyunani tunapata neno la kiingereza "fundi sanifu." katika ulimwengu wa kale wa ulimwengu wa Kishamu wa wafuaji au ushirika wa mafundi walikuwa maarufu sana na wenye nguvu. Paulo alikuwa sehemu ya fundi wa mahema.

**19:26-27** Hii inatupatia maarifa kwenye mafanikio na kupenyeza kwa huduma ya Paulo katika Asia.

▣ **"akisema ya kwamba hiyo inayofanywa kwa mikono siyo miungu"** Hii inaaksi dhana ya Agano la Kale ya ubatili wa ibada ya sanamu (kama vile Kumbu. 4:28; Zab. 115:4-8; 135:15-18; Isa. 44:9-17; Yer. 10:3-11).

**19:27** Kuna vifungu vya habari kadhaa katika fasihi ya Kiyunani ya karne ya kwanza ambayo inataja Artemi wa Efeso. Inavyoonekana kulikuwa na miji tofauti tofauti thelathini na tisa ya ulimwengu wa shamu ambao ulikuwa unajumuisha katika ibada ya uzao wa mama huyu wa miungu.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MTUME 19:28-41**

<sup>28</sup> Waliposikia haya wakajaa ghadhabu, wakapiga kelele, wakisema, Artemi wa Waefeso ni mkuu. <sup>29</sup> Mji wote ukajaa ghasia, wakaenda mbio wakaingia mahali pa michezo kwa nia moja, wakiisha kuwakamata Gayo na Aristarko, watu wa Makedonia waliosafiri pamoja na Paulo. <sup>30</sup> Na Paulo alipotaka kuingia kati ya watu, wanafunzi hawakumwacha aingie. <sup>31</sup> Na baadhi ya wakuu wa Asia, walio rafiki zake, wakatuma watu kwake, wakimsihi asijihudhulishe nafsi yake ndani ya mahali pa michezo. <sup>32</sup> Basi wengine walikuwa wakilia hivi na wengine hivi; kwa maana ule mkutano ulikuwa umechafuka-chafuka, na wengi wao hawakuijua sababu ya kukusanyika kwao pamoja. <sup>33</sup> Wakamtoa Iskanda katika mkutano, Wayahudi wakimweka mbele ya watu. Iskanda akawapungia mkono, akitaka kujitetea mbele ya wale watu. <sup>34</sup> Lakini walipotambua ya kuwa yeye ni Myahudi, wakapiga kelele wote pia kwa sauti moja kwa muda wa kama saa mbili, wakisema, Artemi wa Waefeso ni mkuu. <sup>35</sup> Na karani wa mji alipokwisha kuwatuliza watu, akasema, Enyi wanaume wa Efeso, ni mtu gani asiyejua ya kuwa mji wa Efeso ni mtunzaji wa hekalu la Artemi, aliye mkuu, na wa kitu kile kilichoanguka kutoka mbinguni? <sup>36</sup> Basi kwa kuwa mambo haya hayawezi kukanushwa, imewapasa kutulia; msifanye neno la haraka haraka. <sup>37</sup> Kwa maana mmewaleta watu hawa, wasioiba vitu vya hekalu wala kumtukana mungu mke wetu. <sup>38</sup> Basi ikiwa Demetrio na mafundi walio pamoja naye wana neno juu ya mtu, baraza ziko, na maliwali wako; na washitakiane. <sup>39</sup> Bali mkitafuta neno lo lote katika mambo mengine, yatatengenezwa katika kusanyiko lililo halali. <sup>40</sup> Kwa maana tuna hatari ya kushitakiwa kwa ajili ya matata haya ya leo, ambayo hayana sababu; na katika neno hilo, hatutaweza kujiudhuru kwa mkutano huu. <sup>41</sup> Alipokwisha kusema haya akauvunja mkutano.

**19:28** Mstari huu unaonesha kwa namna gani ulimwengu wa kale ulikuwa umeshikilia dini na desturi zao za kimaeneo. Watu wengi walipata maisha yao ya kila siku katika njia zinazounganishwa na mahekalu ya maeneo ya kipagani.

▣ **"Artemi wa Waefeso ni mkuu"** Huyu mungu wa uzao mara kwa mara alikuwa akiitwa "Mkuu." Hii inawezekana ilikuwa wito wa hekalu la kuabudia.

**19:29 "wakaenda mbio..... mahali pa michezo"** Uharibifu na mabaki yake ya ukumbi huu mkubwa wa Kirumi bado upo mpaka leo. Ulikuwa unaweza kupokea watu elfu 25 na 56 (makisio yanatofautiana).

▣ **"kwa nia moja"** Matendo ya Mitume mara kwa mara inatumia tungo hii "kwa nia moja" kuelezea umoja na ushirika wa waaminio (kama vile Mdo. 1:14; 2:1,46; 4:24; 5:12; 8:6; 15:25), lakini pia namna gani uovu unavyoweza kungana (kama vile Mdo. 7:57; 12:20; 18:12). Umoja wenyewe sio lengo. Ni kusudi la umoja ambao ni wa msingi!

▣ **"Gayo"** Alikuwa akitokea Derbe (kama vile Mdo. 20:4). Hili lilikuwa ni jina lililozoeleka, hivyo utambulisho wenye mpaka ni mgumu (kama vile 1 Kor. 1:14; 3 Yohana 3).

▣ **"Aristarko "** Alikuwa anatokeaThessalonike (kama vile Mdo. 20:4; 27:2; Kol. 4:10-11; Flp. 2:4).

**19:30 "wanafunzi hawakumwacha aingie"** Paulo alikuwa mtu mwenye nia yenye nguvu sana! Hata hivyo, aliwaruhusu waaminio wengine kushawishi baadhi ya uchaguzi wake (kama vile Mdo. 19:31).

**19:31 "Na baadhi ya wakuu wa Asia"** Neno hili linamaanisha "viongozi wa eneo waliochaguliwa," lakini lilitumika katika namna kadhaa. Hili ni neno lingine la kiufundi kwa ajili ya viongozi wa eneo wa kisiasa. Inavyoonekana walikuwa wamekwisha kuwa waaminio pia, au angalau marafiki wa Paulo. Tena Luka anaonesha kwamba Ukristo haukuwa tishio kwa mamlaka za maeneo za kiserikali. Ni mistari kama huu hapa ambayo inasababisha baadhi ya wafasiri kudhania kuwa Matendo ya Mitume iliandikwa ili kisomwe katika mashtaka ya Paulo huko Rumi. Tena na tena kanisa lilikuja katika mgogoro na Wayahudi lakini sio na serikali!

**19:32 "kusanyiko"** Neno lilelile la kiyunani (*ekklesia*) lilitumika kwa ajili ya kanisa. Katika Mdo. 19:32,39, na 41 lilimaanisha kusanyiko la watu wa mjini. Kanisa la kwanza lilichagua neno hili kwasababu ya matumizi yake katika Tafsiri ya Agano la Kale "kusanyiko la Israeli." Angalia Mada Maalum: Kanisa (*ekklesia*) katika Mdo. 5:11.

▣ **"na wengi wao hawakuijua sababu ya kukusanyika kwao pamoja"** Lilikuwa ni tukio la watu wenye kufanya ghasia hakika.

**19:33 "Iskanda"** Wayahudi wa eneo walitaka ieleweke kwamba walikuwa kundi lililojitenga kutoka kwa hawa wamishonari wafanyabiashara wa Kikristo, lakini liliwalipukia wenyewe. Kama huyu ni mtu yuleyule anayetajwa katika 2 Tim. 4:14 haijulikani, lakini 1 Tim. 1:20 inatengeneza hofu.

▣ **"akawapungia mkono"** Hii ilikuwa njia ya kimila ya kutafuta ukimya ili mtu aweze kuzungumza (kama vile Mdo. 12:17; 13:16; 19:33; 21:40).

▣ **"kujitetea"** Tunapata neno la Kiingereza "kuomba msamaha" kutoka katika neno hili ambalo linamaanisha utetezi wa kisheria. Luka alitumia kitenzi hiki mara kwa mara (kama vile Luka 12:11; 21:14; Mdo. 19:32; 24:10; 25:8; 26:1,2,24) na nomino katika Mdo. 22:1 na 25:16.

**19:34** Hii inaonesha aidha (1) hakuwa mwana nadhalia ya Kisemiti wa ulimwengu wa Wayunani-Warumi au (2) hasira ya umati huu katika huduma ya Paulo.

**19:35 "Na karani wa mji"** Huyu alikuwa mfanyakazi wa umma, aliyekuwa kama kiungo wa serikali ya Kirumi katika miji hii ikiwa na mahekalu yake maarufu. Neno *grammateus*. Linatumika mara kwa mara katika Matendo ya Mitume kwa jili ya waandishi wa Kiyahudi (kama vile Mdo. 4:5; 6:12; 23:9). Katika Tafsiri ya Agano la Kale ilimaanisha viongozi wa Misri waliokabidhi kumbukumbu kwa mamlaka ya juu (kama vile Kutoka 5:6) na kwa maofisa wa kiyahudi (kama vile Kumbukumbu la Torati 20:5).

▣ **"mji wa Efeso ni mtunzaji wa hekalu la Artemi"** Neno kwa mlinzi kidhahiri "mfagiaji wa hekalu" (*neōkos*, mwangalizi wa hekalu). Hii ilikuwa imefanyika kuwa cheo cha heshima, ngawa kiasili ilimaanisha watumwa wa chini wa hekalu.

▣ **"na wa kitu kile kilichoanguka kutoka mbinguni"** inavyoonekana ni kimondo kilichochongwa kama mwanamke mwenye matiti. Hii ilikuwa ni sanamu kamilifu ya ibada ya uzao. Neno "mbinguni" kidhahiri ni iliyoanguka kutoka kwa Zeus (*dios*).

**19:37** Sababu ya vurugu haikuwa na msingi wa kweli na hivyo walikuwa wanawajibika kisheria kwa kuadabishwa kinidhamu na mahakama (kama vile Mdo. 19:40).

**19:38-39 "na washitakiane"**..Waache wafuate njia na utaratibu sahihi uliowekwa kwa ajili ya mashitaka yao. Hii mistari miwili ina sentensi mbili zenye masharti daraja la kwanza

**19:38 "maliwali"** Kulikuwa na majimbo ya Kirumi ya aina mbili, wale waliondeshwa na mfalme na wale waliongozwa na Baraza (*Augustus, Acts of Settlement, 27 b.c.*). Majimbo ya Kirumi yalikuwa yalitawaliwa na

1. Majimbo ya kibaraza yanayotawaliwa na maliwali au waendesha mashitaka
2. majimbo ya kifalme yanayotawaliwa na waendesha mashitaka wa kisheria



3. majimbo yenye matatizo mengine madogomadogo yalikuwa yakitawaliwa na viongozi wa maeneo
4. majiji huru yalitawaliwa na viongozi wa eneo husika laini chini ya mwongozo wa Kirumi
5. miji wateja kama Palestina ilitawaliwa na viongozi wa eneo lile lakini kukiwa na mipaka na usimamiaji wa kodi

Efeso ilikuwa ni jimbo la Kibaraza "maliwali." Maliwali wanatajwa mara tatu:

1. Sergius Paulus, Kipro, Mdo. 13:7-8,12
2. Annaeus Gallio, Akaya, Mdo. 18:12
3. hakuna jina kamili, lakini kipengele, Efeso, Mdo. 19:38

**19:39-41 "kusanyiko"** Hili ni neno *ekklesia*, ambalo lilitumika na miji ya Kiyunani kwa makusanyiko ya mji. Ilikuwa kutumiwa kwa ajili ya kanisa lililokusanyana kwasababu katika Tafsiri ya Agano la Kale neno la Kiebrania kwa "kusanyiko" (*Qahal*).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je tunatakiwa kuangalia Mdo. 19:2-6 as kama andiko la kuthibitisha
  - a. kubatizwa upya kwa baadhi ya waaminio
  - b. kuwekea mikono kupokea Baraka ya kunena kwa lugha?
2. Toa maana ya unabii (Mdo. 19:6).
3. Kwa nini Matendo ya Mitume inaweka kumbukumbu ya matukio ya Paulo kwa wote Apollo na hawa kumi na mbili wa Yohana Mbatizaji?
4. Je Mdo. 19:11-12 ni usanifishaji kwa kanisa katika vizazi vyote na desturi? Kwanini/kwanini sio??
5. Kwanini kupunga pepo hakujumuishwi katika orodha ya karama za rohoni?
6. Kwanini Waaminio hawapewi taarifa zaidi za kibiblia kuhusu somo hili?
7. Nini ilikuwa kusudi la matukio haya ya miujiza? (kama vile Mdo. 19:17)

## MATENDO YA MITUME 20

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Safari ya Paulo Kwenda Makedonia	Safari huko Ugiriki	safari ya mwisho Ugiriki	kwenda Makedonia na Akaya	Paulo anaondoka Efeso
20:1-6	20:1-6	20:1-6	20:1-6	20:1-6
Salamu za kuaga Za Paulo kwenda Troa	hyduma huko Troa	Kurudi kwa Paulo Troa	safari ya mwisho ya Paulo kwenda Troa	Troa:Paulo anafufua mfu kuwa hai
Safari kutoka Troa Kwenda Mileto	kutoka Troa kwenda Mileto		kutoka Troa kwenda Mileto	kutoka Troa kwenda Mileto
20:13-16	20:13-16	20:13-16	20:13-16	20:13-16
Paulo anazungumza Na wazee wa Efeso	wazee wa Efeso wanaonywa		hotuba ya kuaga ya Paulo kwa wazee wa Efeso	kuagwa kwa Wazee wa Efeso
20:17-24	20:17-38	20:17-18a  20:18b-24	20:17-24	20:17-18a  20:18b-21  20:22-24
20:22-35		20:25-35	20:25-31  20:32-35	20:25-27  20:28 20:29-32
20:36-38		20:36-38	20:36-38	20:33-35 20:36-38

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia" \("A Guide to Good Bible Reading"\)](#))

### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu

4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MSTARI WA 1-6

- A. Hii ni kwa kifupi na hivyo kwa namna fulani muhtasari wa huduma ya Paulo unachanganya huko Makedonia na Ugiriki katika safari yake ya tatu ya umishenari.
- B. Njia bora ya kuainisha huduma ya Paulo katika eneo hili ni kupitia barua zake na haswa Wakorintho wa 1 & 2.
- C. Luka anajaribu kuelezea mienendo ya Paulo kwa kutumia alama na majina ya maeneo lakini uchache wake wa maneno unasababisha mkanganyiko.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 20:1-6

<sup>1</sup> Kishindo kile kilipokoma, Paulo akatuma kuwaita wanafunzi akawaonya, akaagana nao, kisha akaondoka aende zake mpaka Makedonia. <sup>2</sup> Naye akiisha kupita pande zile na kuwafaraji kwa maneno mengi, akafika Uyunani. <sup>3</sup> Alipokwisha kukaa huko miezi mitatu, na Wayahudi kumfanyia vitimvi, alipotaka kwenda Shamu kwa njia ya bahari; basi akaazimu kurejea kwa njia ya Makedonia. <sup>4</sup> Watu hawa wakafuatana naye, Sopatro Mberoya, mwana wa Piro, na Aristarko na Sekundo, watu wa Thesalonike; na Gayo mtu wa Derbe, na Timotheo; na Tikiko na Trofimo watu wa Asia. <sup>5</sup> Ila watu hao wamekwisha kutangulia wakamngojea Troa. <sup>6</sup> Sisi tukatweka baada ya siku za mikate isiyotiwa chachu, tukatoka Filipi, tukawafikia Troa, safari ya siku tano, tukakaa huko siku saba.

**20:1 "Kishindo kile kilipokoma"** Tungo hii ni tata. Haimaanishi kutaka kumaanisha kwamba Paulo aliacha Efeso kwa mara moja kwasababu vurugu ilianza na Demetrio . Paulo hakuondoka kwasababu ya vurugu, lakini kwasababu kazi yake ya kiinjalisti ilimalizika, kama kauli yake mwenyewe Demetrio iliweka dhahiri (kama vile Mdo. 19:26).

▣ **"Paulo akatuma kuwaita wanafunzi akawaonya"** Paulo alikuwa anajali sana juu ya uinjilisti na kufanya wanafunzi (kama vile Mdo. 20:2; Mt. 28:18-20). Injili ingawa inapokelewa ka mtu mmoja mmoja tunafanyika familia ambayo huduma inafanyika (kama vile 1 Kor. 12:7). Lengo la waamini wa mahali lilikuwa ni kanisa!

**20:2 "Naye akiisha kupita pande zile "** Hii yawezekana inamaanisha (1) kwenda Illyricum (kama vile Rum. 15:19) au (2) kuelekea miji ya Filipi, Thesalonike, na Beroya.

▣ **"akafika Uyunani."** Uyunani (*Hellas*) inamaanisha jimbo la Kirumi la Akaya (kama vile Mdo. 19:21). Hii inamaanisha hasa mji wa Korintho. Paulo alipanua huduma yake katika eneo hili. Wakati huu aliandika Warumi. Alikuwa na wasiwasi juu ya kanisa la Korintho, kama ilivyo katika 1 Kor. 16:5-9 na 2 Kor. 2:12-13 inaonesha kwa usahihi.

**20:3** Mstari huu unahusiana na mipango ya safari ya Paulo. Mara kwa mara alikuwa akiibadilisha kwasababu ya mazingira. Kwa maana hii Paulo alifikiri ilikuwa sio busara (yaani mbinu za Wayahudi) kuchukua meli ya kihujaji kuelekea Yerusalemu, hivyo alisafiri kwa njia ya nchi kavu.

▣ **"Wayahudi kumfanyia vitimvi, alipotaka kwenda Shamu kwa njia ya bahar"** Yawezekana alikuwa alipanga kusafiri kwenye meli ya kihujaji ambayo ilikuwa ikisimama katika bandari zote njiani kuchukua mahujaji wa Kiyahudi kwenye sherehe huko Yerusalemu.

▣ **"Sopatro, Aristarko na Sekundo,; na Gayo, na Timotheo; na Tikiko na Trofimo."** Hawa yawezekana ni wanaume kutoka katika makanisa mbalimblai waliotumwa kumsindikiza zawadi ya kifedha maalumu kwenda katika kanisa la Yerusalemu (kama vile 1 Kor. 16:1-3; 2 Kor. 8-9).

1. Sopatro yawezekana ni Sosipater wa Rum. 16:21.
2. Aristarko anatajwa 19:29; 27:2 na Kol. 4:10.
3. Tikiko ametajwa katika Efe. 6:21-22; Kol. 4:7-8; 2 Tim. 4:12 na Tito 3:12.
4. Gayo anatajwa katika Mdo.19:29.
5. Trofimo anatajwa katika Mdo. 21:29 na 2 Tim. 4:20.

Ifuatayo inachukuliwa kutoka katika fasiri yangu kwenye 1 Wakorintho (Angalia [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org) ).

**"makusanyo"** *Logia* ni neno ambalo limepatikana katika mafunjo ya Kiyunani katika Misri kama zawadi ya fedha kwa makusudi ya kidini, lakini haihusiana na kodi iliyozoeleka (kama vile Moulton, Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament*, ukurasa 377). Haijulikana ikiwa katika muktadha huu inamaanisha kwa kujali zawadi zilizo zoeleka au zawadi za ziada. Paulo alianza kujali huklu kwa maskini katika Yudea kulikotokana na mazungumzo na Yakobo, Petro, Yohana na Barnababa katika Gal. 2:10; 6:10. Matoleo haya maalum yalianza na kanisa huko Antiokia ambapo Paulo na Barnaba walitumikia, Mdo. 11:27-30. Matoleo haya yanatajwa katika vitabu kladhaa vya Agano Jipya (kama vile Rum. 15:26; 2 Kor. 8-9; 1 Kor. 16:1). Lilikuwa ni jaribio la kuimarisha mahusiano kati ya kanisa mama la Kiebrania na makanisa ya mataifa.

Paulo anatoa wito huu kwa michango hii kwa majina kadhaa.

1. kusaidia maskini, Mdo. 24:17
2. ushirika, Rum. 15:26,27; 2 Kor. 8:4; 9:13
3. kutodaiwa, Rum. 15:27
4. huduma, Rum. 15:27; 2 Kor. 9:12"

Kutoka 2 Kor. 8:6,16 inaonekana kwamba Tito yawezekana alikuwa mwakilishi wa kanisa. Inashangaza sana kwamba Luka hakuwahi kumtaja Tito katika Matendo ya Mitume. Nadharia imekuwa kwamba Tito alikuwa nduguye Luka na kwa kulinda heshima hiyo akaamua kuliondoa jina lake. Hii inaweza pia kuelezea ndugu asiyetajwa jina katika 2 Wakorintho 8:18, ambaye wengi wanadhani kuwa alikuwa ni Luka (Origen inaliandika kwa kumbukumbu katika kitabu cha Eusebius' *His. Eccl.* 6.25.6; A. T. Robertson's, *Word Pictures in the New Testament*, ukurasa 245).

F. F. Bruce, *Paul: Apostle of the Heart Set Free*, anatoa maoni yake juu ya ito na Luka kuwa ndugu

Maelezo mafupi ya ukimya wa Luka ambaye alikuwa jemedari anayeaminiwa na Paulo ni kwamba Tito alikuwa nduguye Luka; kama vile W. M. Ramsay, *St. Paul the Traveler and the Roman Citizen* (London, 1895), p. 390; *Luke the Physician and Other Studies* (London, 1908), ukurasa 17 f.; A. Souter, 'A Suggested Relationship between Titus and Luke', *Expository Times* 18 (1906-7), ukurasa 285, na "The Relationship between Titus and Luke', *ibid.*, kurasa wa 335 f. Lakini ikiwa uhusiano huu unadumishwa, hivyo inawezekana kwamba Luka ni 'ndugu' katika 2 Wakorintho 8:18. (angalia ukurasa wa 320) umeondolewa: Kusudi la Paulo kumtuma huyu 'ndugu' akiambatana na Tito ilikuwa kwamba awe mdhamini wa kujitegemea kwa ajili ya usimamizi wa uadilifu wa utawala kwa ajili ya misaada ya kupunguza makali ya njaa, na kusudi hili lingeleta mkanganyiko ikiwa wabezaji wangekuwa wamepewa fursa kuwavuta hisia kwenda kwenye uhusiano wa damu kati ya hawa wawili. Hakuna kitu ambacho kingekuwa bora zaidi kupigiwa hesabu ili kuendeleza makisio yale ambayo yameendelea yaliyokuwepo" (ukurasa 339 kidokezo #5).

**20:5 "sisi"** Luka anaanza tena na ripoti yake ya ushuhuda wa macho ambao ulikatishwa akiwa Filipi (kama vile Mdo. 16). Hiki kipengele cha "sisi" kinatambulishwa kama 16:10-17; 20:5-15; 21:1-18; na 27:1-28:1b.

**20:6 "Siku za mikate isiyochacha"** Karamu ya siku saba katikati ya mwezi wa pili ilikuwa imeunganishwa na siku moja ya kalamu ya Pasaka (kama vile Kutoka 13). Usuli wa kiyahudi wa Paulo ulishawishi namna alivyo ona kalenda. Hatufahamu chochote kuhusu, hivyo pia Paulo hakuitunza kalamu hii kwa ajili ya kusudi la ushuhuda (kama vile 1 Kor. 9:19-23). Yawezekana inatajwa kwasababu alikuwa anapanga safari yake kuwa katika Yerusalemu ifikapo Pentekoste (kama vile Mdo. 20:16)

**ANDIKO LA NASB(LILILOBRESHWA) MATENDO YA MITUME 20:7-12**

<sup>7</sup> Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane. <sup>8</sup> Palikuwa na taa nyingi katika orofa ile tulipokuwa tumekusanyika. <sup>9</sup> Kijana mmoja, jina lake Eutiko, alikuwa ameketi dirishani, akalemewa na usingizi sana; hata Paulo alipoendelea sana kuhubiri, akazidiwa na usingizi wake akaanguka toka orofa ya tatu; akainuliwa amekwisha kufa. <sup>10</sup> Paulo akashuka, akamwangukia, akamkumbatia, akasema, Msifanye ghasia, maana uzima wake ungalimo ndani yake. <sup>11</sup> Akapanda juu tena, akamega mkate, akala, akazidi kuongea nao hata alfajiri, ndipo akaenda zake. <sup>12</sup> Wakamleta yule kijana, yu mzima, wakafarijika faraja kubwa sana.

**20:7 "Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate"** Hii inaonesha taratibu za kanisa la kwanza la kukutana siku za jumapili (siku ya kwanza ya kazi ya juma) kuwa na mlo mmoja wa ushirika (Mdo. 20:11) na kalamu ya ukumbusho ("kuvunja mkate" ni nahau ya Agano Jipya kwa ajili ya Kalamu ya Bwana). Yesu mwenyewe aliweka tukio la kuabudu la jumapili kwa kuonekana kwake mara tatu baada ya kufufuka (kama vile Yohana 20:19,26; 21:1; Luka 24:36; 1 Kor. 16:2).

Toleo la *The Helps for Translator series (The Acts of the Apostles* na Newman na Nida, ukurasa wa 384) inasema kwamba Luka anamaanisha muda wa kiyahudi na kwamba hii ilikuwa Jumamosi jioni (kama vile toleo la TEV), lakini nyingi za fasiri ni dhahiri, "siku ya kwanza ya juma." Haya ni matumizi ya tungo hii tu katika Matendo ya Mitume. Paulo anatumia tungo "siku ya kwanza ya wiki" katika 1 Kor. 16:2 tu, ambapo inamaanisha Jumapili.

▣ **"akafuliza maneno yake"** Paulo alitaka kuwafundisha na kuwatia moyo kwa kadri inavyowezena (kama vile Mdo. 20:2,31).

▣ **"hata usiku wa manane"** Wayahudi walianza siku katika mapambazuko au jioni kwasababu ya Mwanzo 1, wakati Warumi walianza siku wakati wa usiku wa manane.

**20:8 "Palikuwa na taa nyingi"** Hii ilikuwa lazima ni sehemu yenye joto, iliyojaa na hata hali ya kujaa moshi. Ni kama inavyoonekana Luka anajaribu kusema.

**20:9 "Kijana mmoja"** Neno hapa linamaanisha mtu ambaye yuko katika mwanzo wa maisha yake. Neno tofauti linatumika katika Matendo ya Mitume 20:12. Linamaanisha mtoto. Eutiko ni kijana wa makamo.

▣ **"Eutiko. . . hata Paulo alipoendelea sana kuhubiri, akazidiwa na usingizi wake"** Hii kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo inaonesha ushahidi wa kibiblia kwa vyote mahubiri ya muda mrefu na wasikilizaji wanaosinzia!

▣ **"akainuliwa amekwisha kufa"** Inavyoonekana alikuwa amekufa! Angalia mstari wa 12.

**20:10 "Paulo akashuka, akamwangukia akamkumbatia"** Paulo alitenda kama Eliya na Elisha katika Agano la Kale ambao walifufua waliokufa katika namna hiyohiyo (kama vile. 1 Wafalme 17:21; 2 Wafalme 4:34). Anawaambia wasikilizaji wake wasifadhaike, lakini kwa kusema ukweli nahisi kwamba Paulo alikuwa amefadhaishwa na tukio hili!

▣ **"Msifadhaike"** Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi ambacho mara nyingi kinamaana ya kuacha kitendo kilichoko tayari katika mchakato.

**2:12**

**NASB, TEV** "na tulitiwa moyo sana"

**NKJV, NRSV** "hawakuweza kutiwa moyo hata kidogo"

**NJB** "na walitiwa moyo sana"

Matoleo ya NKJV na NRSV ni dhahiri na yanaonesha hali ya nahau hasi zilizozungumzwa kwa kutokuzwa (kama vile Mdo. 12:18; 15:2; 19:11,23,24; 20:12; 26:19,26; 27:20; 28:2).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 20:13-16**

<sup>13</sup> Lakini sisi tukatangulia kwenda merikebuni, tukaabiri kwenda Aso, tukikusudia kumpakia Paulo huko; kwa maana ndivyo alivyoagiza, yeye mwenyewe aliazimu kwenda kwa miguu. <sup>14</sup> Alipotufikia huko Aso, tukampakia, kisha tukafika Mitilene. <sup>15</sup> Tukatweka kutoka huko, na siku ya pili tukafika mahali panapokabili Kio; siku ya tatu tukawasili Samo, tukakaa Trogilio, siku ya nne tukafika Mileto. <sup>16</sup> Kwa sababu Paulo amekusudia kupita Efeso merikebuni, asije akakawia katika Asia; kwa maana alikuwa na haraka, akitaka kuwahi Yerusalemu siku ya Pentekoste, kama ikiwezekana.

**20:13 "merikebuni"** Mipango ya Paulo ya safari ilitakiwa ibadilishwe kwasababu ya njama zilizokuwa zimepangwa dhidi ya maisha yake ambazo zilikuwa zimekusudiwa zifanyikie baharini (kama vile Mdo. 20:3). Yawezekana Paulo alitaka kujua wakina nani walikuwa merikebuni kabla yeye kupanda. Paulo ilimbidi afanye safari nchi kavu kutokea Troa mpaka Aso ambapo angeweza kuchukuliwa na meli kutokea Troa. Watu wote ambao wanatajwa katika Matendo ya Mitumes 20:4 walikuwa tayari ndani ya meli hii.

**20:14 "tukafika Mitilene"** Huu ni mji mkuu wa kisiwa cha Lesbos. Ni kisiwa kikubwa kuliko vyote kilichojitenga na pwani ya Asia ndogo (Uturuki Magharibi).

**20:15-16** Inashangaza kwa namna gani Luka alijua kuhusu safari za majini. Anatumia maneno mengi ya kitaalamu yahasuyo safari za majini wakati atoapo taarifa yake hii (vipengele vya "sisi") ya Matendo ya Mitume. Kadhaa ya vipendgele vya "sisi vinajumuisha safari za majini Inavyoonekana alikuwa ni mtu aliye msomi na aliyesafiri sana maeneo mbalimbali.

**20:15 "Kio"** Hiki ni kisiwa kingine cha bahari ya Aegean. Ni sheumu ndefu, kisiwa chembamba ambacho kipo karibu sana na pwani.

▣ **"Samo"** Hii nacho bado ni kisiwa mbali ya pwani magharibi mwa Asia Ndogo iliyo karibu na Efeso.

▣ **"Mileto"** Uliwahi kuwa mji mkubwa na muhimu wa mambo ya usafiri wa majini kusini mwa Efeso na Mwanzoni mwa mkondo wa Mto. Paulo alifika mahali hapa na kuagiza viongozi wa kanisa katika Efeso Ilikuwa ni safari ya maili thelathini.

**20:16 "Paulo amekusudia kupita Efeso"** Hii inaonekana kumaanisha kwamba Paulo alikuwa na baadhi ya maamuzi huru juu ya meli. Ikiwa sio hivyo itakuwa (1) walikuwa wamekodi meli wote kwa pamoja (2) walikodi meli ambayo haikusimama Efeso.

▣ **"kama"** ni sentensi yenye masharti daraja la nne (*ei* pamoja na hali ya kuamriwa), ambayo inaelezea matamano.

▣ **"Pentekoste"** Hii ilikuwa sherehe ya kiyahudi ya siku hamsini baada ya Pasaka. Paulo aliikosa sherehe ya Pasaka kwasababu ya mstari wa 3.

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MATENDO YA MITUME 20:17-21:16

- A. Hiki ni kipengele cha ulinzi binafsi katika kifungu hiki cha habari, kama vile wengine walikuwa wanaendelea kumvamia Paulo binafsi (kama vile Mdo. 20:33).
- B. Huu ni mfano pekee tu katika Matendo ya Mitume ya Paulo kuwahubiria waumini. Katika Mdo. 13:16 anawahutubia Wayahudi, wakati katika Matendo ya Mitume 14:15 na 17:22 anawahutubia wapagani wa Kiyunani.
- C. Ujumbe huu una usambamba mwingi kwenye barua za Paulo kwa namna mtu angetegemea. Upekee wa misamiati ya Paulo inaaksiwa kwa uzuri katika kuagwa huku. Hii inaonesha uaminifu wa Luka katika kuweka kumbukumbu ya shuhuda za wengine

### ANDIKO LA NASB(LILILOBRESHWA) MATENDO YA MITUME 20:17-18a

<sup>17</sup> Toka Mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa. <sup>18</sup> Walipofika kwake, akawaambia,

**20:17 "Mileto"** Bandari hii ilikuwa kama Maili 30 kusini mwa Efeso

▣ **"wazee"** Kutoka katika hili neno (*presbuteros*) tunapata neno "Mzee wa kanisa" au "Wazee wa kanisa wenye cheo sawa." Kwasababu ya Matendo ya Mitume 20:17,28 na Tito 1:5,7 maneno "wazee" (*presbuteroi*) na "Maaskofu" (*episcopoi*) ni visawe vya maneno "mchungaji" (*poimenos*, kama vile Efe. 4:11). Neno "Mzee" lilikuwa na usuli wa kiyahudi (viongozi wa kiyahudi wa kikabila) na "askofu" au "mwangalizi" lilikuwa na mazingira ya kiutawala wa siasa za kiyunani.

Kuna makundi mawili tu ya viongozi wa makanisa ya nyumbani wanaotajwa katika Agano Jipya yaani wachungaji na mashemasi (kama vile Flp. 1:1). Kunaweza kukawa na makundi matatu yaliyotajwa katika 1 Timotheo 3, ambayo yanajumuisha kazi za wajane au mashemasi wa kike (kama vile Rum. 16:1). Tazama kwamba neno liko katika wingi. Hii yawezekana inamaanisha viongozi wa makanisa ya nyumbani (kama vile Mdo. 11:30; 14:23; 15:2, 4,6,22-23; 16:4; 21:18; 1 Tim. 5:17, 19; Tito 1:5; Yakobo 5:14; 1 Pet. 5:1).

▣ **"Kanisa"** Neno la Kiyunani (*ekklesia*) ni neno linalotumika kwa ajili ya kusanyiko la mji (kama vile 19:39). Hata hivyo lilitumika kufasiri tungo za Agano la Kale "kusanyiko (*qahal*) la Israeli" katika Tafsiri ya Agano la Kale. Kanisa la kwanza lilichagua kuelezea mwili mpya wa waaminio kwasababu liliwatambulisha wao na watu wa Mungu wa Agano la Kale. Kanisa la Agano Jipya walijiona wenyewe kama wakamilishaji wa kweli wa ahadi za Agano la Kale kwasababu ya kuwa Yesu wa Nazareti alikuwa Masihi wa kweli. Angalia Mada Maalum katika Mdo. 5:11.

### ANDIKO LA NASB (LILILOBRESHWA) MATENDO YA MITUME 20:18b-24

Ninyi wenyewe mnajua tangu siku ya kwanza nilipokanyaga hapa Asia, jinsi nilivyokuwa kwenu wakati wote, <sup>19</sup> nikimtumikia Bwana kwa unyenyekevu wote, na kwa machozi, na majaribu yaliyonipata kwa hila za Wayahudi; <sup>20</sup> ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia neno lo lote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba, <sup>21</sup> nikiwashuhudia Wayahudi na Wayunani wamtubie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo. <sup>22</sup> Basi sasa, angalieni, nashika njia kwenda Yerusalemu hali

nimefungwa rohoni, nisyajue mambo yatakayonikuta huko; <sup>23</sup> isipokuwa Roho Mtakatifu mji kwa mji hunishuhudia akisema, ya kwamba vifungo na dhiki vyaningoja. <sup>24</sup> Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu, kuishuhudia Habari Njema ya neema ya Mungu.

**20:18 "Ninyi wenyewe mnajua .....jinsi nilivyokuwa kwenu wakati wote,"** Kutembea kwa Paulo na kuzungumza kulithibitisha uhusiano wake na Kristo. Ukweli kwamba Paulo analisema hili kwa nguvu katika Mdo. 20:18-19 inaonesha uwepo wa wakosoaji.

**20:19 "nikimtumikia Bwana kwa unyenyekevu wote"** Neno linaanza na orodha ya vigezo vya Kikristo ambavyo vinazalisha umoja (kama vile Efe. 4:2-3). "Unyenyekevu" ni maadili ya kipekee ya Mkristo ambayo hayakujumuishwa katika wanamaadili wa Kiyunani (wastoiki) orodha yao ya maadili. Wote Musa (kama vile Hesabu 12:3) na Yesu (kama vile Mt. 11:29) yanaelezewa na neno hili. Paulo analitumia mara kadhaa (Kama vile Efe 4:2; Flp. 2:3; Kol. 2:18,23; 3:12).

### **MADA MAALUM: MAOVU NA MAADILI KATIKA AGANO JIPYA**

Orodha ya vipengele vyote yaani maovu na maadili ni vinaendana kwa pamoja katika Agano Jipya. Mara nyingi hivi huakisi maeneo yote yaani katika Sheria za Kiyahudi na orodha ya tamaduni. Orodha za Agano Jipya za kuzilinganisha sifa pambanuzi zinaweza kuonekana katika:

	<b>Maovu</b>	<b>Maadili</b>
1. Paulo	Rum. 1:28-32 Rum. 13:13 1 Kor. 5:9-11 1 Kor. 6:10 2 Kor. 12:20 Gal. 5:19-21 Efe. 4:25-32 Efe. 5:3-5 --- Kol. 3:5,8 1 Tim. 1:9-10 1 Tim. 6:4-5 2 Tim. 2:22a, 23 Tito 1:7, 3:3	--- Rum. 12:9-21 --- 1 Kor. 6:6-9 2 Kor. 6:4-10 Gal. 5:22-23 --- --- Flp. 4:8-9 Kol. 3:12-14 --- --- 2 Tim. 2:22b,24 Tito 1:8-9; 3:1-2
2. Yakobo	Yakobo 3:15-16	Yakobo 3:17-18
3. Petro	1 Pet. 4:3 2 Pet. 1:9	1 Pet. 4:7-11 2 Pet. 1:5-8
4. Yohana	Ufu. 21:8; 22:15	---

▣ **"kwa machozi, na majaribu"** Paulo anaorodhesha vitu vya kimwili na kihisia ambavyo alikabiliana navyo kama Mtume kwa Mataifa katika 2 Kor. 4:7-12; 6:3-10; 11:24-28. Gharama za huduma!

▣ **"kwa hila za Wayahudi"** Kuna mifano kadhaa ya hizi "hila" katika Mdo. (kama vile Mdo. 9:24; 13:45,50; 14:2,4,5,19; 17:5,13; 18:12; 20:3; 21:27; 23:12,27,30; 24:5-9,18-19).



**20:20 "sikujiepusha"** Hili ni neno la kibaharia (kama vile Mdo. 20:27, kauli ya kati elekezi ya wakati uliopita usio timilifu) kwa ajili ya kupiga kibaharia wakati meli inapokabili bandari.

▣ **"neno lo lote liwezalo kuwafaa"** Paulo aliwafundisha wao kila kitu kinachohusiana na injili: namna ya kuipokea, namna ya kuishi na namna ya kulinda, namna ya kuendeleza.

▣ **"bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba"** Paulo yawezekana alifundisha tu katika mikutano ya makundi ya wazi (sio mikutano ya siri), lakini pia ndani ya nyumba za watu binafsi (au yawezekana makanisa ya nyumbani). Jambo kubwa ni kwamba walijua sawasawa namna gani Paulo alifanya kazi miongoni mwao na pia nini kile Paulo alisema. Paulo lazima alivamiwa na kundi la watu wa mahali pamoja. Hii ilikuwa ni njia yake ya kukengeusha ukosoaji.

**20:21 "nikiwashuhudia Wayahudi na Wayunani "** Kuna ujumbe mmoja kwa makundi yote mawili. Mara kwa mara uwasilishaji unatofautiana lakini maudhui ni yale yale kama mahubiri katika Mdo. (*kerygma*, angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:14) inaonesha. Paulo alilifanya kama kipaumbele kuwasilisha injili kwa Wayahudi kwanza (kama vile Warumi 1:16; 1 Kor. 1:18,24).

▣ **"wamtubie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo"** Toba ni kubadili ufahamu (neno la Kiyunani), ikifuatiwa na kubadili kwa matendo (neno la Kiebrania). Angalau ni moja ya vigezo vya wokovu. Nyingine ni imani katika Bwana wetu Yesu (kama vile Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; angalia Mada Maalum katika Mdo. 3:16). Moja ni hasi (kugeuka kutoka katika ubinafsi na dhambi). Nyingine ni chanya (kugeuka kumkumbatia Yesu na upatanisho wake kwa niaba yetu). Vyote vinatajikana. Nimekuja kuamini kwamba kuna vigezo kadhaa vya Agano Jipya: hii hakika ni toba ya mwanzo na imani na toba endelevu na imani, lakini pia utii na ustahimilivu.

Kuna utofautiano kadhaa katika maandiko ya kale ya Kiyunani kuhusu "Bwana wetu Yesu Kristo." Cheo cha "Kristo" kinaondolewa katika maandiko B (Vaticanus), lakini yanakuwepo katika P<sup>74</sup>, X, A, na C. Kama ilivyo katika wingi wa utofautiano huu, haubadillishi maana ya andiko. Andiko la Kiyunani toleo la UBS<sup>4</sup> linaamini kusoma kwa kifupisho ni "karibia na hakika" kwasababu hakuna sababu kwani mwandishi yoyote angelifuta lakini kuna ushahidi wao wa kupanuka kwa usambamba wa tungo kuelekea katika tungo kamili inayotegemewa (angalia kiambatisho cha pili: Uhakiki wa kimaandiko).

**20:22**

**NASB** "fungwa rohani"

**NKJV** "fungwa katika roho"

**NRSV** "matelka wa Roho"

**TEV** "katika utii wa Roho Mtakatifu"

**NJB** "utekaji wa Roho"

Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliotimilifu. Inaonesha maana ya Paulo ya uongozi wa ki-Ungu (kama vile Mdo. 18:21; 19:21; 20:23; 1 Kor. 4:19; 7:40; 16:7). Angalia [MADA MAALUM: ROHO \(PNEUMA\) KATIKA AGANO JIPYA](#) katika Mdo. 2:2 na kidokezo katika Mdo. 19:21. Roho Mtakatifu anatajwa katika Mdo. 20:23.

**20:23 "isipokuwa Roho Mtakatifu mji kwa mji hunishuhudia akisema, ya kwamba vifungo na dhiki vyaningoja "**

Hii yawezekana ilifanyika kupitia manabii tofauti tofauti waliokuwa wakitumiwa na Roho Mtakatifu kumuonya Paulo (kama vile Mdo. 9:16; 21:4, 10-12). Mara kwa mara Roho mtakatifu hutuma na hutumia kile kinachoonekana hakifai, kwa ajili ya kusudi la njia chanya (kama vile Isa. 55:8-11). Paulo hakukubali kurudishwa nyuma na magumu binafsi kadiri ya alivyoamini, ilimsaidia kufikia kusudi la Mungu.

**20:24 "Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu"** Aina hii ya kufikiri ni kinyume na fikra ya kibinafsi ya mwanadamu aliyeanguka. Wakristo wana mtazamo wa kiulimwengu tofauti tofauti. Wamekufa kwa

nafsi na dhambi na wako hai kwa Mungu (kama vile Warumi 6; 2 Kor. 5:14-15; Gal. 2:20; 1 Yohana 3:16). Kifo cha uonevu na dhuluma wa nafsi kunaleta uhuru wa huduma ya kujikana nafsi.

▣ **"kuumaliza mwendo wangu"** Hili ni neno la kimichezo kwa ajili ya wakimbia mbio. Paulo anapenda kutumia sitiari za kimichezo. Mara kwa mara anazungumza juu ya maisha yake kama tukio la kimichezo (kama vile 1 Kor. 9:24-27; Gal. 2:2; 5:7; Flp. 2:16; 3:14; 2 Tim. 2:5; 4:7). Paulo aliamini kuwa Mungu alikuwa na mapenzi maalum, mpango, kusudi kwa ajili ya maisha yake.

▣ **"huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu"** Paulo alipokea wito wake akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9). Waaminio wote wanaitwa na kupewa karama kama wahudumu (kama vile Efe. 4:11-12). Huku ni kutimilizwa, mtizamo huu wa kiulimwengu utabadilisha namna tunavyoishi (kama vile 2 Kor. 5:18-20). Tu wanaume na wanawake tulio kazini katika kutimiza kusudi! Tumeokolewa ili kutumika. Wote sisi tu wajumbe wa injili na karama!

▣ **"Habari Njema ya neema ya Mungu"** Tumaini pekee la mwanadamu ni rehema na neema ya Mungu isiyobadilika. Utatu wa Mungu umetupatia kila kitu tunachokihitaji kwa ajili ya maisha ya utele. Tumaini letu liko katika yeye alivyo na kile alichofanya. Inashangaza namna Luka anavyotumia nomino kwa nadra neno "injili" (sio kila sehemu zote katika Luka na ni mara mbili tu katika Matendo ya Mitume 15:7; 20:24), lakini anatumia kitenzi cha wingi, mara nyingi katika vitabu vyote viwili.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 20:25-35**

<sup>25</sup> Na sasa, tazameni, mimi najua ya kuwa ninyi nyote niliowahubiria ufalme wa Mungu, nikienda huko na huko, hamtaniona uso tena. <sup>26</sup> Kwa hiyo nawashuhudia wote siku hii ya leo, ya kuwa mimi sina hatia kwa damu ya mtu awaye yote. <sup>27</sup> Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu. <sup>28</sup> Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe. <sup>29</sup> Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi;<sup>30</sup> tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao. <sup>31</sup> Kwa hiyo kesheni, mkikumbuka ya kwamba miaka mitatu, usiku na mchana, sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi. <sup>32</sup> Basi, sasa nawaweka katika mikono ya Mungu, na kwa neno la neema yake, ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa. <sup>33</sup> Sikutamani fedha wala dhahabu, wala mavazi ya mtu. <sup>34</sup> Ninyi wenyewe mnajua ya kuwa mikono yangu hii imetumika kwa mahitaji yangu na ya wale waliokuwa pamoja nami. <sup>35</sup> Katika mambo yote nimewaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi imewapasa kuwasaidia wanyonge, na kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema mwenyewe, Ni heri kutoa kuliko kupokea.

**20:25 "mimi najua ya kuwa ninyi nyote. . . hamtaniona uso tena"** Alikuwa anapanga kwenda Uhispania (kama vile Rum. 15:24,28), lakini hii yawezekana kimuktadha ikamaanisha kukua kwake, kufungwa kulikotabiriwa na yawezekana kifo huko Yerusalemu. Ikiwa nyaraka za kichungaji zinafunua safari ya nne ya kimishonari ya Paulo hivyo alirudi katika hili eneo tena.

1. Efeso, 1 Tim. 1:3; 3:14; 4:13
2. Mileto, 2 Tim. 4:20
3. Yawezekana hata Troa, 2 Tim. 4:13.

Paulo aliishi kwa imani katika uongozi wa Mungu. Hakujua hasa hatima yake

▣ **"niliowahubiria ufalme wa Mungu"** angalia Kidokezo katika Mdo. 2:34.

**20:26 "sina hatia kwa damu ya mtu awaye yote"** Hii ni nahau ya Kiyahudi, kama Mdo.18:6, au kwa udhahiri zaidi, Ezek. 3:16 na 33:1. Paulo kwa uaminifu alikuwa amewasilisha injili (kama vile 2 Kor. 2:17). Sasa wale waliokuwa

wameitikia na wale waliokataa wanabeba mzigo wa maamuzi yao wenyewe. Huduma moja, uharibifu mwingine (kama vile 2 Kor. 2:15-16).

**20:27 "sikujiepusha"** Angalia kidokezo katika Matendo ya Mitume 20:20.

▣ **"kusudi lote la Mungu"** Lazima sisi siku zote tutangaze injili kamili na sio sehemu tu zinazopendeza! Haya yanaweza yakawa maelezo kwa Wayahudi waliodai kwamba Paulo aliacha sehemu ya ujumbe (yaani Sheria ya Musa-Dini ya Kiyahudi) au kwa wenye vipaji wa 2 Wakorintho 12 waliofikiri kwamba Paulo hakuwa na uzoefu wa kiroho. Kusudio la Mungu ni kwamba wanadamu warejeshwe kwenye ushirika kamili pamoja na yeye Mwenyewe ambalo lilikuwa kusudio la uumbaji (kama vile Mwanzo 1:26,27; 3:8;12:3).

**20:28 "itunzeni nafsi zenu "** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Haya maonyo yako katika 1 Kor. 16:13; Kol. 4:2; 1The. 5:6,10. Maisha ya Mkristo yana vyote sehemu ya Mungu na mwanadamu. Mungu siku zote anachukua hatua na kuanzisha mambo, lakini waaminio lazima waitikie. Kwa namna moja tunawajibika kwa maisha yetu ya kiroho (kama vile Flp. 2:12-13). Kile ambacho ni kweli kwa waamini binafsi, ni kweli kwa viongozi wa kanisa (kama vile 1 Wakorintho 3).

▣ **"na lile kundi lote nalo "** Hii ni sitiari kwa ajili ya watu wa Mungu (kama vile Zaburi 23; Luka 12:32; Yohana 21:15-17). Pia ni neno la asili kwa "mchungaji." Angalia Dokezo katika Mdo. 20:17. Viongozi wa Kanisa wanawajibika kwa Mungu kwa ajili yao wenyewe na makanisa yao (kama vile 1 Wakorintho 3).

▣ **"Roho Mtakatifu amewaweka ninyi"** Hii inaonyesha wito wa ki-Ungu wa Mungu katika kuchagua viongozi wa kanisa.

▣ **"waangalizi"** Angalia dokezo katika Mdo. 20:17.

▣ **"kanisa lake Mungu"** Neno "Mungu" linapatikana katika maandiko ya kale ya kiyunani P<sup>74</sup>, A, C, D, na E, wakati "Bwana" linapatikana katika MSS  $\kappa$  na B. Paulo anatumia tungo "kanisa la Mungu" mara kwa mara, lakini kamwe sio tungo "kanisa la Bwana." Mukstadha unasaidia "Kanisa la Bwana" kwasababu tungo inayofuata, "kwa damu yake mwenyewe," ambayo kwa hakika inamaanisha Kristo. Hata hivyo jii ni aina ya kihariri ya mabadiliko ya maandishi ambayo yangetarajiwa (angalia Bruce M. Metzger, *A Textual Commentary*, ukurasa 480-482). Hivyo toleo la maandiko ya Kiyunani la UBS<sup>4</sup> linaendelea kushikilia "Mungu," lakini linaipa alama ya "C" . "Bwana" ingekuwa aina ya usomaji usio wa kawaida na mgumu (Angalia Kiambatisho mbili: Uhakiki wa kimaandiko).

Andiko hili linahudumu kama mfano mzuri wa namna maandishi wanavyobadilisha maandiko kwa ajili ya sababu za kithiolojia. Mjadala mzuri unapatikana katika Bart D. Ehrman's *The Orthodox Corruption of Scripture*, ukurasa wa 87-89. Waandishi walibadili maandiko kuyafanya yawe yenye nguvu kimafundisho dhidi ya uvumi wa elimu ya Kristo ya siku hizo. Mdo. 20:28 unatoa aina mbalimbali za mabadiliko yawezekana yanayohusiana na mivutano ya ndani ya kihistoria au kithiolojia.

Kabla ya kutupa mikono yetu katika kupoteza tumaini lazima tukumbuke kuwa Agano Jipya lina desturi za kimaandiko kubwa, zilizo nzuri zaidi kuliko maandiko yote ya kale. Ingawa hatuwezi kuwa na uhakika wote wa maandiko yaliyomo kamili katika uandishi wa asili, bado tunalo tumaini na maandiko sawia! Maandiko ya asili yako katika utofauti utofauti. Utofauti huu hauathiri maandiko yoyote makubwa! Angalia *Rethinking New Testament Textual Criticism* ed. David Alan Black.

▣ **"alilolinunua kwa damu yake mwenyewe0"** Hii inaaksi dhana ya Agano la Kale ya mbadala wa kidhabihu (kama vile Mambo ya Walawi 1-7; Isaya 53). Msisitizo huu unashangaza kwamba hautajwi sana katika *kerygma* ya Matendo ya Mitume (Angalia James D. G. Dunn, *Unity and Diversity in the NT*, ukurasa wa 17-18). Lakini pia inawezekana ni rejea yenye nguvu kuhusu uungu wa Yesu (yaani "Kanisa la Mungu"). Paulo mara kwa mara anatumia tungo inayoonesha kwenye kweli hii (kama vile Rum. 9:5; Kol. 2:9; Tito 2:13).

Pia inawezekana kufasiri tungo ya kiyunani kama "Kupitia Aliye wake," ikimaanisha uhusiano wa karibu (yaani Mwanawe Yesu). F. F. Bruce, *Commentary on the book of the Acts*, ukurasa 416 #59, inasema tungo hii inatakiwa ifasiriwe "kwa namna ya damu ya Wake mwenyewe," ambayo inaelezea inashuhudiwa vizuri katika Mafunjo ya fasihi ya Koine ya Kimisri.

**20:29 "mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu"** Hii ni sitiari inayojikita kwenye sitiari iliyokwisha tumika hapo kabla ya "kundi" na "mchungaji." Hii inapelekea tatizo la walimu wa uongo, wote kutoka nje (Mdo. 20:29) na ndani (Mdo. 20:30). Wote walikuja katika mavazi ya kondoo (kama vile Mt. 7:15-23; Luka 10:3; Yohana 10:12, pia katika maandiko ya siku za mwisho ya vipindi vya kati vya fasihi ya Biblia, I Enoch 89:10-27; IV Ezra 5:18). Waaminio lazima wajaribu wale wanaodai kuhubiri neno la Mungu (kama vile 1 Yohana 4:1 Kuwajaribu kwa uaminifu wao kwa injili, vyote katika maneno na matendo (kama vile Mdo. 20:18-24; Mathayo 7; Rum. 16:17-18).

**20:30 "wakizungumza mapotovu"** "wakizungumza" ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo, wakati "mambo mapotovu" ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliotimilifu, ikitumika kiuthibitisho (shamirisho la moja kwa moja). Maana yake ya msingi ni "kugeuza." Inatumika kuelezea jamii ya binadamu (kama vile Luka 9:41; Flp.2:15). Tendo hili linaelezewa (neni tofauti) in katika 2 Petro 3:15- 16.

▣ **"kuwatoa wanafunzi wawaandame"** Swali la kithiolojia ni "Je wale wanaoondolewa wanakuwa wamepotea au kuchanganyikiwa?" (kama vile Mt. 24:24). Haiwezekani kukaa kimfumo wa imani lakini imani ya kweli huendelea! (kama vile 1 Yohana 2:18).

## **MADA MAALUMU: UASI (APHISTĒMI)**

Neno la Kiyunani *aphistēmi* lina uwanja mpana wa elimu-maana. Hata hivyo, Neno la Kiingereza "uasi" limetokana na neno hili na athari za matumizi yake kwa wasomaji wa sasa. Muktadha, kama iliyo kawaida, ndio ufunguo, sio maelezo ya wakati uliopo.

Hili ni neno lililounganishwa kutokana na KIHUSISHI *apo*, ambacho kinamaanisha "kutokana na" au "mbali na" and *histēmi*, "kukaa," "kusimama," au "kupachika." Angalia matumizi yafuatayo (yasiyo ya kitheolojia):

1. kuondoa kimwili
  - a. kutoka Hekaluni, Luka 2:37
  - b. kutoka katika nyumba, Marko 13:34
  - c. kutoka kwa mtu, Marko 12:12; 14:50; Matendo 5:38
  - d. kutoka katika vitu vyote, Mat. 19:27,29
2. kuondoa kisiasa, Matendo 5:37
3. kuondoa kimahusiano, Matendo 5:38; 15:38; 19:9; 22:29
4. kuondoa kisheria (tarakisha), Kumb. 24:1,3 (LXX) na Agano Jipya, Mat. 5:31; 19:7; Marko 10:4; 1 Cor. 7:11
5. kuondao deni, Mat. 18:7
6. kuonyesha kutokuhusika kwa kuondoka, Mat. 4:20; Yohana 4:28; 16:32
7. kuonyesha kutokuhusika kwa kutoondoka, Yohana 8:29; 14:18
8. kuruhsu au kutoa kibali, Mat. 13:30; 19:14; Marko 14:6; Luka 13:8

Katika maana ya kitheolojia KITENZI pia kina matumizi mapana:

1. kufuta, kusamehe, kuifuta hatia ya dhambi, Kut.32:32 (70) (LXX); Hes. 14:19; Yak. 42:10 na Agano Jipya, Mat. 6:12,14-15; Marko 11:25-26
2. kujiondoa toka dhambini, 2 Tim. 2:1
3. kukataa kwa kujiondoa toka kwenye
  - a. Sheria, Mat. 23:23; Matendo 21:21
  - b. imani, Ezek. 20:8 (LXX); Luka 8:13; 2 The. 2:3; 1 Tim. 4:1; Ebr. 3:12

Waamini wa sasa wanauliza maswali mengi ya kitheolojia ambayo waandishi wengi wa Agano Jipya wasingalifikiri kuyahusu. Moja ya haya yangeliweza kuhusiana na uelekeo wa sasa wa kuitenga imani (uthibitisho) kutoka

kwenye imani (utakaso).

Kuna watu katika Biblia walihusishwa miongoni mwa watu wa Mungu na jambo lililotokea na kusababisha wao kuondoka.

- I. Agano la Kale
  - A. Wale walioisikia taarifa ya wale wapelelezi kumi na wawili (kumi), Namba 14 (kama vile Heb. 3:16-19)
  - B. Kora, Namba 16
  - C. Wana wa Eli, 1 Samueli 2, 4
  - D. Sauli, 1 Samueli 11-31
  - E. Manabii wa uongo (mifano)
    1. Kumb. 13:1-5 18:19-22 (nji za kumtambau nabii wa uongo)
    2. Jeremia 28
    3. . Ezeieli 13:1-7
  - F. Manabii wa uongo
    1. Ezeieli 13:17
    2. Nehemia 6:14
  - G. Uovu wa viongozi wa Israeli (mifano)
    1. Yeremia 5:30-31; 8:1-2; 23:1-4
    2. Ezeieli 22:23-31
    3. Mika 3:5-12
- II. Agano Jipya
  - A. Hili neno la Kiyunani kifasihi linamaanisha "kuasi." Vitabu vyote vya Agano la Kale na Agano Jipya vinathibitisha uchochezi wa uovu na mafundisho ya uongo kabla ya Ujio wa Pili (kama vile Mat. 24:24; Marko 13:22; Matendo 20:29,30; 2 The. 2:9-12; 2 Tim. 4:4). Neno hili la Kiyunani linaweza kuyaaakisi maneno ya Yesu katika Mfano wa Udongo unaopatikana katika Mathayo 13; Marko 4; na Luka 8. Kwa kudhaniwa walimu hawa wa uongo si Wakristo, bali waamini wachanga (kama vile Ebr. 3:12).

Swali la kitheolojia ni hili walimu wa uongo wanawapeleka wapi waamini? Hili ni vigumu kulijibu kwa kuwa kulikuwa na walimu wa uongo katika makanisa anzilishi (kama vile 1 Yohana 2:18-19). Mara nyingi tamaduni au madhehebu yetu yanajibu swali hili pasipokuwa na marejeo ya maandiko ya Biblia mahususi (isipokuwa njia ya kuhakiki kwa nukuu mstari ulio nje ya muktadha ili kwa uangalifu kuhakiki madhara yaliyomo).
  - B. Imani Thabiti
    1. Yuda, Yohana 17:1
    2. Simoni mchawi, Matendo 8
    3. Wale waliozungumziwa katika Mat. 7:13-2
    4. Wale waliozungumziwa katika Mathayo 13; Marko 4; Luka
    5. Wayahudi wa Yohana 8:31-59
    6. Alexanda na Himenayo, 1 Tim. 1:19-20
    7. Wale wa 1 Tim. 6:21
    8. Himanayo na Fileto, 2 Tim. 2:16-18
    9. Dema, 2 Tim. 4:10
    10. Walimu wa uongo, 2 Peter 2:19-22; Yuda 1:12-19
    11. wapinga Kristo, 1 Yohana 2:18-19
  - C. mani isiyo kuwa na matunda
    1. 1 Wakorintho 3:10-15
    2. 2 Petro 1:8-11

Mara chache tunafikiri juu ya haya maandiko kwa kuwa mfumo wa injili yetu (Ufuatao mtazamo wa Calvin, Arminian, n.k.) unaamuru mwikio wa kimamlaka. Tafadhari usinihukumu kabla kwa kuwa nafundisha somo langu. Shauku yangu ni hatua ya kiufasiri. Tunapaswa kuipa nafasi Biblia ili izungumze nasi na si kuiumba katika mpangilio wa thiolojia iliyopita. Mara nyingi hii inaumiza na kushtua kwa kuwa thiolojia zetu zilizo nyingi ni za

kimadhehebu, kitamaduni, kimahusiano (mzazi, rafiki, mchungaji), si za kibiblia (tazama [Mada Maalumu: Nini maana ya neno "Kupokea," "Kuamini," "Kiri/Ungama," na "Call Upon"?](#)). Wengine walio miongoni mwa watu wa Mungu wanarudi nyuma na kutokuwa miongoni mwa watu wa Mungu (m.f. Rum. 9:6).

**20:31 "kuweni macho"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo (kama vile Marko 13:35), ambayo ni sambamba na Mdo. 20:28, "jilindeni nyie wenyewe" (kauli tendaji shurutishi). Viongozi wa Mungu na kanisa la Mungu sharti likeshe wakijilinda dhidi ya walimu wa uongo—sio wale wasiotaka kufuata yale tuyapendayo, lakini wale wasiojai injili na mtindo wake wa maisha.

▣ **"kwa miaka mitatu"** Hii inamaanisha muda wa Paulo wa kukaa katika Efeso. Muda huu unaashiria kujumuishwa kwa shughuli za Paulo katika eneo hili. Alikaa kwa muda mrefu na waaminio hawa kuliko mji mwingine wowote, kanisa, au eneo. Walifahamu injili, Sasa lazima wailinde na kuisambaza!

**20:32 "nawaweka katika mikono ya Mungu"** Hii inamaanisha "kuwakabidhi kwa" (kama vile Mdo. 14:23). Tunawajibika kwa Mungu kwa Injili tuliyokabidhiwa (kama vile 1 Tim. 1:18). Tunawajibika kuwarithisha na wengine ambao nao watairithisha kwa watakaofuata (kama vile 2 Tim. 2:2). Jina "Mungu" linapatikana katika MSS P<sup>74</sup>,  $\alpha$ , A, C, D, na E. Neno "Bwana" linapatikana katika MS B. Toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa *Theos* alama ya "B" (karibia na hakika).

▣ **"na kwa neno la Neema"** Hiki ni kisawe cha tungo kwa "injili." Angalia dokezo katika Mdo. 20:24.

▣ **"iwezayo kuwajenga"** Tambua kwamba hii ni nafsi na kweli ya Mungu (Injili) inayopelekea makuzi (kama vile Mdo. 9:31). Paulo anatumia hii sitiari mara kwa mara. Hili ni neno la Kiyunani linaloweza kufasiriwa kwa vyote "kujenga" au "kuonya" (kama vile 1 Wakorintho 14). Hili ndilo lengo la Injili, sio tu makuzi ya mwamini mmoja mmoja, lakini kanisa zima.

## MADA MAALUM: KUADILISHA

Neno hili oikodomeō na muundo wa maneno yake mengine yanatumiwa mara kwa mara na Paulo. Kidhahiri lilimaanisha "kujenga nyumba" (kama vile Mt. 7:24), lakini lilikuja kutumika kisitiari kwa:

1. Mwili wa Kristo, kanisa, 1 Kor. 3:9; Efe. 2:21; 4:16
2. Kujenga
  - a. ndugu wadhaifu, Rum. 15:1
  - b. majirani, Rum. 15:2
  - c. ninyi kwa ninyi, Efe. 4:29; 1 Wathesalonike 5:11
  - d. watakatifu kwa ajili ya huduma, Efe. 4:11
3. tunajenga au kuonya kwa
  - a. upendo, 1 Kor. 8:1; Efe. 4:16
  - b. kuweka mipaka juu ya uhuru binafsi, 1 Kor. 10:23-24
  - c. kukwepa kudhaniwa, 1 Tim. 1:4
  - d. kuweka mipaka ya wazungumzaji katika huduma za kuabudu (waimbaji, walimu, manabii, wanenaji kwa lugha, na wakalimani), 1 Kor. 14:3-4,12
4. vitu vyote sharti vionywe
  - a. mamlaka ya Paulo, 2 Kor. 10:8; 12:19; 13:10
  - b. kauli za kimutahsari katika Rum. 14:19 na 1 Kor. 14:26

▣ **"na kuwapeni ninyi urithi"** Katika Agano la Kale Mungu alikuwa Urithi wa Walawi na makuhani. Katika Agano Jipya Mungu ni urithi wa waaminio wote kwasababu waaminio ni watoto wa Mungu kupitia mtu na kazi ya Kristo (kama vile Rum. 8:15,17; Gal. 4:1-7; Kol. 1:12). Waaminio wa Agano Jipya, kama Waisraeli wa Agano la Kale, ni makuhani (kama vile 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6). Tumekusudiwa kuhudumia ulimwengu uliopotea.

▣ **"kati ya wale waliotakaswa"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliotimilifu. Angalia [MADA MAALUM: UTAKATIFU WA AGANO JIPYA/UTAKASO](#) katika Mdo. 9:32.

**20:33 "mavazi ya shaba au dhahabu"** Hivi vilikuwa vitu vya thamani. Paulo anatetea dhamira zake na matendo yake. Katika Agano Jipya tamaa na maonyo ya kingono mara kwa mara ni sifa bainifu ya walimu wa uongo (kama vile 1 Kor. 3:10-17).

**20:34 "nilihudumia mahitaji yangu mwenyewe"** Paulo alikataa kuchukua msaada kutoka katika makanisa ambayo alikuwa akiyahudumia kwasababu ya kushutumiwa mara kwa mara na walimu wa uongo juu ya dhamira yake. Paulo alijihudumia mwenyewe katika mahitaji (kama vile 1 Kor. 4:12; 9:3-7; 2 Kor. 11:7-12; 12:13; 1 The. 2:9; 2 The. 3:6-13). Pia Paulo kama mwalimu aliye na mafunzo alikuwa na wasiwasi binafsi kuhusu kupokea pesa kwa ajili ya mafundisho yake. Hata hivyo anaelezea kwamba wahudumu wa Injili wanatakiwa walipwe (kama vile 1 Kor. 9:3-18; 1 Tim. 5:17-18). Kuna hadithi ya kimuhtasari fupi nzuri ya ulimwengu wa shamu wa karne ya kwanza iliyoandikwa na James S. Jeffers, *The Greco-Roman World of the New Testament Era*. Inataja kwamba Paulo anaelezea kufanya kazi kwa mikono yangu mwenyewe ili kukidhi mahitaji ya mwili katika safari zote tatu za kimishonari (kama vile ukurasa wa 28).

1. Safari ya kwanza, 1 Kor. 4:12; 9:6; 1 The. 2:9
2. Safari ya Pili, Mdo. 18:3
3. Safari ya tatu, Mdo. 19:11-12; 20:34; 2 Kor. 12:14

**20:35** Tazama kwamba kazi ngumu za waaminio sio kwa ajili ya kujipatia faida binafsi au raha bali kwa ajili ya wengine walio katika uhitaji katika jina la Kristo (kama vile 2 Kor. 9:8-11). Nukuu ya Paulo kutoka kwa Yesu haipatikani katika kitabu cha Injili chochote. Hivyo lazima iwe desturi ya kinywa. Huu "udhaifu" hautumiki hapa katika namna ya kumpa umbile mkristo (kama vile Rum. 14:1; 15:1; 1 Kor. 8:9-13; 9:22), Lakini uhitaji wa kimwili. Paulo alifanya kazi kujisaidia mwenyewe na waamini wengine walio katika mahitaji.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 20:36-38**

<sup>36</sup> Alipokwisha kunena haya akapiga magoti, akaomba pamoja nao wote. <sup>37</sup> Wakalia sana wote, wakamwangukia Paulo shingoni, wakambusu-busu, <sup>38</sup> wakihuzunika zaidi kwa sababu ya neno lile alilosema, ya kwamba hawatamwona uso tena. Wakamsindikiza hata merikebuni.

**20:36 "akapiga magoti"** Huu haukuwa mkao wa kawaida wa kimaombi kutoka katika historia ya kiyahudi ya Paulo. Hii yawezekana ilikuwa kujitoa kiibada maalum (kama vile Mdo. 20:32; 21:5).

**20:37 "wakamwangukia Paulo shingoni"** The Toleo la NKJV liko dhahiri sana, "alianguka katika shingo ya Paulo." Shukrani kwa viongozi wa kanisa wanaokuja kutusaidia!

**20:38 "wakihuzunika zaidi kwa sababu ya neno lile alilosema"** Hii inamaanisha Mdo.20:25.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Paulo alikuwa akisafiri na watu wengi kutok akatika miji tofauti tofauti katika Matendo ya Mitume 20:4?
2. Nini kusudio la kithiolojia la Mdo. 20:7-10?
3. Kwanini Mdo. 20:13 inachanganya sana?
  
4. Kwanini Paulo anajilinda mwenyewe kwa wazee wa Kiefeso?
5. Kwa nini Paulo alikuwa bado anakwenda Yerusalemu ikiwa manabii walikuwa wakimuonya kuhusu madhara makubwa ya kuutembelea mji (Mdo. 20:22-23)
6. Kwanini Manabii wa uongo wamekuwepo katika kila kizazi na zama? Je wamekombolewa? Je wale wanaowafuata wao wamekombolewa? Nabii wa uongo ni yupi?
7. Kwanini Matendo ya Mitume 20:36-38 inasababisha sisi kupenda na kuombea viongozi wetu wa maeneo?



## MATENDO YA MITUME 21

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Safari ya Paulo Kuelekea Yerusalemu	Tahadhari dhidi ya Safari ya kuelekea Yerusalemu	Paulo Arudi Palestina	Paulo Aenda Yerusalemu  (20:7:21:14)	Safari ya Kuelekea Yerusalemu
21:1-6	21:1-14	21:1-6	21:1-6	21:1-6
21:7-14		21:7-14	21:7-11	21:7-14
	Paulo asistiza Juu ya amani	Usawa wa Paulo na Dini ya Kiyahudi	21: 12-13  21:14	Kuwasili kwa Paulo huko Yerusalemu
21:15-16	21:15-26	21:15-16	21:15-16	21:15-16
Paulo Amtembelea Yakobo			Paulo amtembelea Yakobo	
21:17-26	Akamatwa ndani ya Hekalu	21:17-26	21:17:25	21:17-25
	21:26-36		21:26	21:26
Paulo Akamatwa Hekaluni		Paulo akamatwa na Kuwekewa Ulinzi	Paulo akamatwa Hekaluni	Kukamatwa kwa Paulo
21:27-36		(21:27-22:9)  21:27-36	21:27-29  21:30-36	21:27-29  21:36
Paulo Akijitetea	Akihutubia Makutano ya Yerusalemu		Paulo Ajitetea	
21:37-22:5	(21:37-22:21)	21:37-40	(21:37-22:5) 21:37a  21:37b-38  21:39  21:40-22:2	21:37-40

## **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["MwongozowausomajiMzuriwaBiblia"](#) ("A Guide to Good Bible Reading"))

### **KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Ayaya kwanza
2. Ayayapili
3. Ayatatu
4. N.k

### **TAMBUZI ZA KIMUKTADHA**

Sura hii inashangaza katika kile ambacho hakizungumzwi! Hakuna msistizo wa Paulo kuhusiana na changizo kutoka makanisa ya Mataifa hadi makanisa ya Yerusalemu. James D. G. Dunn, *Unity and Diversity in the NT*, kr. 272-278, analifanya hili katika ubunifu wenye kuvutia kwamba kuna mvutano kati ya Yakobo (anayejulikana kwa uaminifu wake kwa desturi za Dini ya Kiyahudi) na Paulo kuhusu nafasi ya Masimulizi katika maisha ya Myahudi aminiye.

### **USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO**

#### **ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 21:1-6**

<sup>1</sup> Ikawa tulipokwisha kujitenga nao na kuabiri, tukafika Kosi kwa tanga moja, na siku ya pili yake tukafika Rodo na kutoka huko tukafika Patara, <sup>2</sup> tukapata merikebu itakayovuka mpaka Foinike tukapanda tukatweka. <sup>3</sup> Na tulipoona Kipro tukaiacha upande wa kushoto; tukasafiri mpaka Shamu tukashuka Tiro. Kwa maana huko ndiko merikebu yetu itakakoshusha shehena yake. <sup>4</sup> Tukiisha kuwaona wanafunzi tukakaa huko siku saba, nao wakamwambia Paulo kwa uweza wa Roho asipande kwenda Yerusalemu. <sup>5</sup> Hata tulipotimiza siku zile tukaondoka tukaenda zetu, na watu wote, pamoja na wake zao na watoto wao, wakatusindikiza mpake nje ya mji, tukapiga magoti pwani tukaomba; <sup>6</sup> na baada ya kuagana tukapanda merikebuni, nao wakarudi kwao.

**21:1"tukasafiri"** Hili ni neno la kibaharia linalomaanisha kusafiri moja kwa moja kwa kutumia ngarawa (kama vile Matendo ya Mitume 16:11). Luka alikuwa na ujuzi sana wa maneno ya kusafiri kwa matanga (kama vile Matendo ya Mitume 21:3). Vipengele vya kitabu cha Matendo ya Mitume vilivyo vingi vya kiwakilishi "tu/sisi" vilihusisha kusafiri kwa matanga.

▣ **"Kosi"** Hili neno linamaanisha "kutaniko." Hili ni jina lenye kujumuisha kisiwa na mji wake mkubwa. Kisiwa hiki ndipo palipokuwa nyumbani kwa Hippocrates (karne ya tano b.k.) na kilikuwa kituo kikubwa cha shule ya tiba. Huu ulikuwa utawala huru uliofikiriwa kuwa sehemu ya jimbo la Kirumi huko Asia. Eneo hili lilikuwa umbali wa maili arobaini kusini mwa Miletus.

▣ **"Rodo"** Hili pia ni jina la kisiwa na mji wake mkuu. Hiki kisiwa cha kibiashara kilikuwa maarufu kwa (1) kukua kwake (2) chuo kiku chake, ambacho kilikuwa kimebobeza elimu ya ufasaha wa kusema na kuhutubu. Katika kipindi kilichopita (29 b.k.) kisiwa hiki kilikuwa maarufu sana kwa ajili ya shaba zilizopatikana humo, sanamu ndefu 104' za watu ambazo zilizokuwa zimesimishwa bandarini. Hiyo sanamu ilifanyakazi kama kitu cha kuleta nuru ndani ya nyumba.

▣ **"Patara"** Familia ya Kimagharibi ya machapisho ya Kiyunani (kama vile P<sup>41</sup>, D) na baadhi ya matoleo ya kale ya Kilatini yanaongeza neno "na Myra" (yaliyo mengi ni nyongeza kutoka 27:5), ambayo ilikuwa bandari kuu ya

merikebu za kuelekea Siria. Toleo la UBS<sup>4</sup> linatoa andiko fupi sana lenye daraja "A"(yumkini). Patara ulikuwa mji wa pwani katika Likia. Mji huu ulikuwa maarufu kwa sababu ya ubashiri wa Apollo, ambao kwa wakati huo huo ulikuwa wa kushindana na Delphi pia.

**21:2" tukapata merikebu itakayovuka mpaka Foinike"** Hii lazima ilikuwa meribu kubwa. Merikebu zilizokuwa ndogo zilikishikiriwa pwani. Merikebu hii iliokoa muda wao mwingi kwa kuwasafirisha moja kwa moja.

**21:3"tulipoona Kipro"** Lazima hili lilileta wazo juu ya Barnaba na safari ya kwanza ya kimisionari.

▣**"Tiro"** Haya yalikuwa makazi ya pwani ya Foinike.

**21:4"wanfunzi"** Katika mji huu kulikuwa na kanisa ambalo lilianzishwa baada ya mateso ya Stefano (kama vile Matendo ya Mitume 8:4; 11:19). Katika kipindi hiki waamini walikuwa wakiwatafuta waamini wengine wa kuishi nao (kama vile Matendo ya Mitume 21:7,16).

▣**"wakamwambia Paulo kwa uweza wa Roho asipande kwenda Yerusalemu"** Hili linarejelea juu ya kuwepo kwa manabii katika kusanyiko hili la wenyeji (kama vile Matendo ya Mitume 20:23; 21:10-12). Ujumbe wao uliohusu mateso ulikuwa wa kweli na bado kwa hakika ziara ya Paulo ilikuwa ni mapenzi ya Mungu (kama vile Matendo ya Mitume 21:14). Yesu, kupitia Anania, alimwambia Paulo juu ya kazi ya maisha yake (kama vile Matendo ya Mitume 9:15-16). Kuteswa kulikuwa sehemu ya hili, lakini pia aliendelea kuwashuhudia Wafalme.

**21:5" tukapigamagotipwanitukaomba"** Hii ni sura nzuri sana ya upendo wa Mkristo na mahusiano. Hii inaweza kuwa huduma ya kipekee, kama Matendo ya Mitume 20:32,36.

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 21:7-14**

<sup>7</sup> Hata tulipomaliza safari yetu kutoka Tiro tukafika Tolemai, tukawaamkia ndugu tukakaa kwao siku moja.<sup>8</sup> Asubuhi yake tukaondoka, tukafika Kaisaria, tukaingia nyumbani mwa Filipo, mhubiri wa Injili, aliyekuwa mmoja wa wale saba, tukakaa kwake.<sup>9</sup> Mtu huyu alikuwa na binti wanne, mabikira, waliokuwa wakitabiri.<sup>10</sup> Basi tulipokuwa tukikaa huko siku nyingi, nabii mmoja jina lake Agabo akashuka kutoka Uyahudi.<sup>11</sup> Alipotufikia akautwaa mshipi wa Paulo, akajifunga miguu na mikono, akasema, Roho Mtakatifu asema hivi, Hivyo ndivyo Wayahudi wa Yerusalemu watakavyomfunga mtu mwenye mshipi huu, nao watamtia katika mikono ya watu wa Mataifa.<sup>12</sup> Basi tuliposikia haya, sisi na watu wa mahali pale, tukamsihi asipande kwenda Yerusalemu.<sup>13</sup> Ndipo Paulo alipojibu, Mnafanya nini, kulia na kunivunja moyo? Kwa maana mimi, licha ya kufungwa, ni tayari hata kuuawa katika Yerusalemu kwa ajili ya jina lake Bwana Yesu.<sup>14</sup> Alipokataa shauri letu, tukanyamaza tukisema, Mapenzi ya Bwana na yatendeke.

**21:7 "Tolemai"** Mji huu uliitwa jina hili baada ya Iskanda Mkuu ambaye alitawala katika Misri na alikuwa babu wa Ptolemy II ambaye aliujiunga mji huu mnamo 26 k.k. Hii ndiyo Bandari pekee ya asili katika pwani ya Palestina. Katika Agano la Kale mji huu uliitwa Aka (kama vile Waamuzi 1:31). Siku hizi huu mji unaitwa kwa jina lake la vita takatifu, Akre.

▣**"ndugu"** Katika Matendo ya Mitume hiki ni kisawe cha neno "wanafunzi" (kama vile Matendo ya Mitume 21:4,16). Hili liliwadhihirisha waamini katika Kristo.

▣**"tukakaa kwao"** Tazama maelezo katika Matendo ya Mitume 21:4.

**21:8"tukaondoka"** Kwa vyo vyote haijulikani kama waliondoka kupitia nchi kavu ama baharini.

▣**"Kaizaria"** Haya ni makao makuu ya Kirumi ya huko Palestina. Huu ulikuwa mji wa pwani wenye bandari ndogo iliyotengenezwa na watu. Filipo Mhubiri wa Injili aliishi hapa (kama vile Matendo ya Mitume 8:40).

▣“**mhububiri wa injili**” Kwa mshangao hili neno linatumika mara tatu pekee katika Agano Jipya (kama vile Efe. 4:11 na 2 Tim. 4:5). Hatufahamu kwa usahihi karama hii ya kihuduma imehusisha nini. Neno lenyewe linamaanisha "aliyehubiri injili."

▣“**aliyekuwa mmoja wa wale saba**” Aya hii inarejelea juu ya tatizo la kanisa la Yerusalemu kulalamika juu ya mgawo wa chakula usio sawa kwa wajane waliozungumza Kiyahudi. Kanisa liliwachagua watu saba wa kumhudumia mhitaji huyu. Wote walikuwa na majina ya Kiyumnani. Hawa saba walikuwa wahubiri wenye nguvu. Hawa walikuwa wa kwanza kuyakamata maono ya injili ulimwenguni kote (kama vile Matendo ya Mitume 6).

**21:9 " Mtu huyu alikuwa na binti wanne, mabikira . . .waliokuwa wakitabiri"** Kumbuka Luka alikuwa na ufuatiliaji wa kipekee juu ya wanawake. Tunahitaji kufikiria upya juu ya nafasi zetu kwa wanawake katika nafasi za uongozi (kama vile Yoeli 2:28-32; Matendo ya Mitume 2:16-21) katika kanisa uliojikita juu ya ushahidi wote wa Agano la Kale. Tazama Mada Maalum: Wamnamwake katika Biblia katika Matendo ya Mitjume 2:17. Kitabu kilicho nisaidia ni kile cha Gordon Fee, *Gospel and Spirit*. Mapokeo ya Kanisa yanafafanua kwamba hawa waliendelea na safari hadi Asia Ndogo (Filigia) na kwamba mabinti zake waliishi muda mrefu na kumtumikia Mungu kwa muda mrefu. Tunajifunza mapokeo haya kutoka nukuu za Eusebius kutoka pande zote Polycrates na Papias (kama vile *Eccl. Hist.* 3:31:2-5).

**21:10 abniimmojajina lake Agabo**"Kuna njia kama mbili za kulielewa neno hili.

1. katika barua za Korintho hili linarejelea kushiriki au kuihubiri injili (kama vile 1 Kor. 14:1)
2. kitabu cha Matendo ya Mitume kinawataja manabii (kama vile Matendo ya Mitume 11:27-28; 13:1; 15:32; 21:10, hata kutoa unabii, 21:9)
3. Tatizo la neno hili ni, namna karama ya unabii wa Agano Jipya zinavyohusiana na ule unabii wa Agano la Kale? Katika Agano la Kale manabii ndiyo waandishi wa Maandiko.

Katika Agano Jipya kazi hii wanapewa wale Mitume kumi na wawili asilia na wasaidiza wao. Kama lilivyo neno "mtume" linashikiriwa kama karama endelevu (kama vile Efe. 4:11), lakini kazi ilibadilika baada ya kifo cha wale kumi na Wawili, hivyo, ni utawala wa nabii. Uvivio (tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 13:1) umefikia kikomo; hakuna Andiko lililovuviwa zaidi (kama vile Yuda Matendo ya Mitume 21:20). Kazi ya msingi wa unabii wa Agano Jipya ni kuhubiri injili, lakini pia unaonyesha namna ya kutumia kweli za Agano Jipya kwa hali ya sasa na uhitaji. Tazama Mada Maalum: Unabii wa Agano Jipya katika Matendo ya Mitume 11:27.

**21:11** Agabo, kama manabii wa Agano la Kale Yeremia na Ezekieli, walitenda nje ya ufunuo wake.

**21:12 "tukamsihi" Hii kauli tendaji elekezi ya wakati usiotimilifu.** Hii inaweza kumaanisha (1) kuanza tendo au (2) kurudiarudia tendo katika wakati uliopita.

**21:13** Ni vigumu kulinganisha tendo la kinabii pamoja na maana ya Paulo kwamba kwenda Yerusalemu yalikuwa mapenzi ya Mungu (kama vile mst.4).

▣"**jina lake Bwana Yesu**" tazama Mada Maalum: [JINA LA BWANA](#) katika Matendo ya Mitume 2:21.

**21:14 " Mapenzi ya Bwana nayatendeke"** ya Hii ni kauli ya kati shurutishi wakati uliopo, inayotumika katika maombi. Mungu alikuwa na mpango na makusudi ya maisha ya Paulo. Paulo ajihisi kwamba aliyafahamu mapenzi ya Mungu hata katika uso wa upekee na unabii wa mara kwa mara kuhusu matatizo ambayo yaliibuka. Lazima Paulo alikuwa amefikiri kwamba unabii huu ulikuwa kwa ajili ya maandalizi ya kiroho na kiakili na na si zuiu.

## **MADA MAALUM: MAPENZI (*thelēma*) YA MUNGU**

“Mapenzi” ya Mungu yamejikita katika namna mbalimbali.

## INJILI YA YOHANA

- Yesu alikuja kuyatenda mapenzi ya Baba yake (kama vile Yohana 4:34; 5:30; 6:38)
- Kuwafufua siku ya mwisho wale wote Baba aliowampa Mwana (kama vile Yohana 6:39)
- Kwamba wote waamini katika Mwana (kama vile Yn. 6:29; 40)
- Maombi yaliyojibiwa kuhusiana na kuyatenda mapenzi ya Mungu (kama vile Yn 9:31 na Yn 5:14)

## VODOKEZO VYA INJILI

- Kuyatenda mapenzi ya Mungu ni jambo la muhimu (kama vile. Mt. 7:21)
- Kuyatenda mapenzi ya Mungu hutufanya kuwa kaka na dada pamoja na Yesu (kama vile Mt. 12:50; Marko 3:35)
- Sio mapenzi ya Mungu kwa yeyote kuangamia (kama vile Mt.18:14; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9)
- Kalvari ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa Yesu (kama vile Mt. 26:42; Luka 22:42)

## NYARAKA ZA PAULO

- ukomavu na huduma ya waamini wote (kama vile Rum. 12:1-2)
- waamini waliondolewa kutoka katika enzi hii ya maovu (kama vile Gal. 1:4)
- mapenzi ya mungu ulikuwa ni mpango wake wa ukombozi (kama vile. Efe.1:5, 9,15)
- waamini wanapitia na kuishi maisha yaliyojazwa na Roho (kama vile 5:17-18)
- waamini wamejazwa na maarifa ya Mungu (kama vile Kol. 1:9)
- waamini wanafanywa kuwa imara na wakamilifu (Kol. 4:12)
- waamini wanatakaswa (kama vile 1The. 4:3)
- waamini watoa shukrani katika vitu vyote (kama vile The.5:18)

## NYARAKA ZA PETRO

- Waamini wanatenda haki (yaani, kunyenyekea kwenye mamlaka ya chini) na, kwa hiyo wanawanyamazisha watu wajinga, hivyo kuwapa fursa kwa kuijua injili/matendo mema (cf. 1Pet. 2:15)
- Mateso ya waamini (kama vile 1 Pet. 3:17; 4:19)
- Waamini hawapaswi kuishi maisha ya ubinafsi (kama vile 1 Pet. 4:2)

## NYARAKA ZA YOHANA

- waamini kuendelea kudumu milele (kama vile Yohana 2:17)
- waamini ni kielelezo kwa maombi yaliyojibiwa (kama vile 1 Yohana 5:14)

## ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 21:15-16

<sup>15</sup> Baada ya siku zile tukachukua vyombo vyetu tukapanda kwenda Yerusalemu. <sup>16</sup> Baadhi ya wanafunzi wa Kaisaria wakafuatana na sisi, wakamchukua na Mnasoni, mtu wa Kipro, mwanafunzi wa zamani ambaye ndiye tutakayekaa kwake.

**21:15 "tukachukua vyombo vyetu"** Toleo la King James Version lina neno "tukachukua mizigo yetu" (NKJV lia "tukapakia"). Hili ni neno halisi lililotaka kuzungumzia juu ya maandalizi ya safari na linapatikana hapa tu katika Agano Jipya.

▣"Yusalemu" Mji huu ulikuwa yapata umbali wa maili 64.

**21:16 "Mnasoni"** Huyu alikuwa Kristo wa Kiyahudi kutoka Kipro (kama Barnaba). Huyu angeweza kuwa mmojawapo wa wale Wayahudi wa Kiyunani, kama wale saba wa Matendo ya Mitume 6. Kwa uwazi kabisa huyu alikuwa mwamini kutoka siku za awali; bila shaka Luka alimhoji kwa ajili ya Injili yake wakati alipokuwa katika Palestina kipindi cha kutiwa gerezani kwa Paulo huko Kaizaria.

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KATIKA MATENDO YA MITUME 21:17-23:30

A. MAELEZO MAFUPI YA MATENDO YA MITUME 21:17-26:32 (Kutiwa gerezani kwa Paulo na ulinzi katika Yerusalemu na Kaizaria.)

1. Maandamano na kukamatwa kwake katika Hekalu Matendo ya Mitume 1:17-40
2. Kujitetea kwa Paulo mbele ya makutano Matendo ya Mitume 22:1-22
3. Mahojiano ya Warumi Matendo ya Mitume 22:23-30
4. Mahojiano ya Wakuu wa Sinagogi Matendo ya Mitume 23:1-10
5. Mpango wa kumuua Paulo Matendo ya Mitume 23:11-35
6. Paulo akiwa mbele ya Feliki Matendo ya Mitume 24:1-23
7. Paulo akiwa mbele ya Feliki na Drusilla kwa maelezo binafsi Matendo ya Mitume 24:24-27
8. Paulo akiwa mbele ya Festo Matendo ya Mitume 25:1-12
9. Paulo akiwa mbele ya Agripa II na Bernike Matendo ya Mitume 25:13-26:32

### B. MAMBO YA KAWAIDA YA KUJITETEWA KWA PAULO

Mambo ya Kawaida	Paulo akiwa mbele Ya Makutano	Paulo Akiwa Mbele ya wakuu wa sinagogi	Paulo Akiwa Mbele ya Feliki	Paulo Akiwa mbele ya Festusi	Paulo Akiwa mbele ya Agripa II
1. Historia ya awali ya Kiyahudi	22:3		24:14,17-18		26:4
2. Mafunzo yake ya Kifarisayo na kundi Lake la wauaji		23:6-9	24:15,21		26:5-8
3. Mateso yake ya "Njiani"	22:4-5				26:9-11
4. Ushuhuda wake Binafsi wa kuongoka kwake	22:6-16				26:12-16
5. Kuitwa na Mungu kwa ajili ya huduma ya kipekee	22:17-22				26:17-23

### C. ULINGANIFU WA MASADUKAYO NA MAFARISAYO

	<u>MASADUKAYO</u>	<u>MAFARISAYO</u>
Chimbuko	Kipindi cha Makabayo	Kipindi cha Makabayo
Jina linalomaanisha	"Wafuasi wa Zadoki"	"Aliyetengwa"
Wadhifa wa Kijamii	Mtawala wa Kikuhani	Mtu wa kawaida asiye mweledi
Suala la Kiroho	Torati iliyoandikwa tu (hasa Kitabu cha Mwanzo kupitia Kumbukumbu la Torati )	Torati ya masimulizi & ile iliyoandikwa pamoja na Chuo cha Manabii na vipengele vya Maandiko ya sheria za Agano la Kale.

Theolojia

Isiyobadilika  
-ni kinyume cha  
Mafarisayo, ambao  
Walishtakiwa kwa  
kushawishiwa wafuasi  
wa Zoloster (kama vile 23:8)

Endelevu  
-nadharia ya umalaika  
liyokuzwa sana  
-kuamini katika maisha baada  
ya kifo na ufufuo  
- sheria zilizowekwa kwa  
maisha ya kila siku

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 21:17-26**

<sup>17</sup> Tulipofika Yerusalemu wale ndugu wakatukaribisha kwa furaha. <sup>18</sup> Hata siku ya pili yake Paulo akaingia kwa Yakobo pamoja nasi, na wazee wote walikuwako. <sup>19</sup> Na baada ya kuwaamkia, akawaeleza mambo yote moja moja Mungu aliyoyatenda katika Mataifa kwa huduma yake. <sup>20</sup> Nao waliposikia wakamtukuza Mungu, wakamwambia, Ndugu yetu, unaona jinsi Wayahudi walioamini walivyo elfu nyingi, nao wote wana wivu sana kwa ajili ya torati. <sup>21</sup> Nao wameambiwa habari zako, ya kwamba unawafundisha Wayahudi wote wakaa katika Mataifa kumwacha Musa, ukiwaambia wasiwatahiri watoto wao, wala wasizifuate desturi. <sup>22</sup> Basi, ni nini? Bila shaka watasikia kwamba umekuja. <sup>23</sup> Basi fanya neno hili tunalokuambia. Wako kwetu watu wanne waliofungwa na nadhiri. <sup>24</sup> Wachukue watu hao, ujitakase pamoja nao, na kuwagharimia ili wanyoe vichwa vyao, watu wote wapate kujua ya kuwa habari zile walizoambiwa juu yako si kitu, bali wewe mwenyewe unaenenda vizuri na kuishika torati. <sup>25</sup> Lakini kwa habari za watu wa Mataifa walioamini, tuliandika na kutoa hukumu yetu ya wao kujilinda nafsi zao na vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na damu, na kitu kilichosongolewa, na uasherati. <sup>26</sup> Ndipo Paulo akawatwaa wanaume wale, na siku ya pili yake akajitakasa nafsi yake pamoja nao, akaingia ndani ya hekalu, akitangaza habari ya kutimiza siku za utakaso, hata sadaka itolewe kwa ajili ya kila mmoja wao.

**21:17** Hiii ilikuwa ishara nzuri kwamba waamini wa Yerusalemu walimwonyesha Paulo pamoja na hawa watu wa Mataifa walioongoka moyo wa ukarimu (kama vile Luka 8:40; 9:11; Matendo ya Mitume 2:41; 18:27; 21:17; 24:3; 28:30), lakini pia kulikuwa na chuki katika kanisa la Yerusalemu (kama vile Matendo ya Mitume 21:20-21).

**21:18-19 "Paulo akaingia kwa Yakobo pamoja nasi"** Hapa hakuna tajo maalum la karama kutoka Mkanisa ya Mataifa (kama vile Matendo ya Mitume 24:17). Paulo alitengeneza taarifa yenye kufanana na ile ya Yakobo katika Matendo ya Mitume 15:12. Yakobo ni ndugu wa Yesu na kiongozi aliyeheshimiwa katika kanisa la Yerusalemu (kama vile Matendo ya Mitume 12:17; 15:13).

**21:18 "na wazee wolte walikuwako"** Tambaua kwamba hapa hakuna tajo la Mitume. Kwa uhakika kabisa hapakuwa na ziara za kimisionari nje ya nchi, au labda walikufa. Haya matumizi ya neno "wazee" linaaksi matumizi yake ya Kiyahudi (kama vile Matendo ya Mitume 4:5,8,23; 6:12; 11:30; 15:2,4,6,22,23; 16:4; 23:14; 24:1,25; 25:15; Ebr. 11:2; Yakobo 5:14), si matumizi yake ya baadaye ya kutumiwa na kanisa juu ya wachungaji (kama vile Matendo ya Mitume 14:23; 20:17,18,23; 1 Tim. 5:17,19; Tito 1:5; 1 Pet. 5:1; 2 Yohana 1; 3 Yohana 1).

**21:19** Baadhi ya watoa maoni wengine wanafikiri kwamba Paulo alipokelewa kwa mapokezi yaliyopoa na faedha zilizotoka makanisa ya Mataifa hazikubaliwa. Hapa kuna mwelekeo wa kufikiria kwao.

1. Paulo aliendelea kukaa nyumbani mwa Wayahudi wa Kiyunani, si mmoja wa viongozi wa kanisa la Yerusalemu.
2. Hakuna mwonekano wa kufurahisha juu ya karama. Hii hata haitajwi.
3. Uongozi ulimweleza Paulo muda mfupi namna alivyokuwa atakiwa katika kati ya maelfu katika kanisa la Yerusalemu.
4. Kamwe kanisa halikuzungumzia juu ya kumwezesha Paulo alipokuwa gerezani ama katika mashtaka yake.

Yapaswa kunenwa kwamba kulikuwa na mgogoro na machafuko kuhusu ujumbe wa na umisionari wa Paulo. Hata hivyo, Matendo ya Mitume 21:19 inaonekana kuwa chanya kwangu!

**21:20 "Wayahudi walioamini walivyo elfunyingi"** Ni ushahidi wenyewe wa injili na upendo wa Mungu wenye kushangaza kwa watu wa Kiyahudi katika Yerusalemu. Kulikuwa na mabaki ya Kiyahudi ya wale waliamini. Huenda Zek. 12:10 imetimia!

▣**"waliani"** Hii ni kauli tendaji timilifu ya wakati unaoendele (tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 3:16 na 6:5). Kwa hakika linamaanisha imani ya kweli iokoayo. Mtu aweza kuokolewa pasipokuwa na uelewa kamili na hata ijapokuwa haelewi mambo yote ya Kithiolojia, (kama vile Matendo ya Mitume 1:6; Luka 19:11). Paulo angewaelezea kama Wakristo "wadhaifu" (kama vile Rum. 14:1-15:13; 1 Kor. 8; 10:23-33). Angeliinama kifudufudi kuwatia moyo, ilimradi "udhaifu" hauithiri injili (waligbadilishwa kuwa Wayahudi wa Wagalatia).

▣**"wana wivu sana kwa ajili ya torati"** Kifungu hiki kinaonyesha idadi kubwa ya Mafarisayo walioongoka, wakereketwa, au Waessene. Hata hivyo, mabadiliko hayo hayakuondoa chuki zao za kidini. Hawa walikuwa sawa na wale waliofanywa kuwa Wayahudi wa huko Galatia. inastajibisha sana kuona namna Paulo alivyowapenda na kuwaunga mkono waaamini waliokuwa "dhaifu" lakini asingeweza kuwavumilia "waalimu wa uongo" au wale walioifasiri injili katika namna isiyotakiwa.

**21:21" wameambiwa habari zako, yakwamba unawafundisha Wayahudi wote wakao katika Mataifa"**Hiki kifungu "kuambiwa" kinaaksi nahau ya Kiebrania "kuiga tena ," ambayo inamaanisha mafundisho ya mdomo. Hili linaunganishwa na kitenzi cha wakati uliopo (kufundisha) kuonyesha kwamba Wayahudi waliokuwa ndani ya Yerusalemu kwa kurudia rudia walikuwa wameambiwa kazi ya Paulo katika maana ya chuki. Mashtaka haya yalikuwa mazito sana kuliko kuwahubiri Mataifa, ambao walisababisha vurugu kubwa (kama vile Matendo ya Mitume 15). Hili neno "kuambiwa" ni neno lenye nguvu ambalo linaingia katika lugha ya Kiingereza kama "uasi" (kama vile 2 The. 2:3). Jambo la kitheolojia lililohusiana na namna Wayahudi wanaoamini wanavyopaswa kuhusiana na Agano la Kale halikusuluhishwa! Katika maana nyingine hili ni jambo la "masinagoga ya Kimasihi"!

**21:23" Wako kwetu watu wane waliofungwa nanadhiri"** Kwa uwazi kabisa hawa walikuwa mojawapo ya waamini wa kanisa. Hili linarejelea ile nadhiri ya Nazarethi iliyokuwa imefungwa (kama vile Hes. 6:1-8). Paulo alikuwa imefungwa nadhiri hiyo hiyo hapo awali (kama vile Matendo ya Mitume 18:18). Hatufahamu hata kidogo kuhusu undani wa hii nadhiri yenye mipaka (kama vile *Nazir*1:3).

**21:23-25** Kifungu hiki kinatupa utambuzi wa kuutambua mtazamo wa Paulo kuhusu uhusiano wa Wakristo wa Kiyahudi juu ya Torati ya Musa. Paulo angeendelea kuzichunguza desturi za Kiyahudi (kama vile Matendo ya Mitume 18:18; 20:6), hasa hasa wakati alipokuwa akijaribu kuwahubiria Wayahudi (kama vile 1 Kor. 9:19-23). Bila shaka huu ilikuwa ukubalifu wa ushirika wa Masihi wa Kiyahudi katika siku zetu.

**21:24"kuwagharimia"** Inawezekana Paulo hakuweka nadhiri ya Nazarethi yeye mwenyewe kwa kwa kiwango hiki, lakini aliilipa dhabihu iliyohitajika kwa ajili ya wengine. Walimu wa sheria za dini ya Kiyahudi walifundisha kwamba hii ilikuwa heshima kubwa kukipa gharama hii kwa ajili ya nadhiri ya Nazarethi (*Ned.* 10a).

## **MADA MAALUM : NADHIRI YA MNAZARETI**

- A. Hii ilikuwa njia ya kila mtu, mume au mke (kama vile Hes. 6:1), ambaye hakuwa wa kabila la Lawi, kujitoa yeye mwenyewe kwa ajili ya kazi ya Mungu (yaani, "mtakatifu kwa Bwana"). Jina Nazareti inamaanisha "aliyetengwa" (BDB 634, KB 684), ambalo ni wazo la mzizi wa neno la Kiebrania takatifu (tazama Mada Maalum: Takatifu).
- B. Katika Agano la Kale hii ilikuwa nadhiri ya kudumu



1. Samsoni (Amu. 13:7)
  2. Samueli ( 1 Sam. 1:21)
  3. Yohana Mbatizaji
- C. Dini ya Kiyahudi iliboresha neno fupi la nadhiri ya Mnazarethi (bila shaka iliboreshwa kutokana na maneno yalio katika Hes. 6:5). Urefu mfupi sana zilikuwa siku thelathini. Hili neno fupi nadhiri lilihitimishwa kwa kunyoa nywele na kuchoma nywele sambamba na dhabihu hekaluni.
- D. Mahitaji ya kipekee (kama vile Hes. 6:1-8)
1. Aajitenge na divai na vileo, wala asile zabibu (kama vile Hes. 6:3-4).
  2. Asinyoe nywele za mtu ye yote.
  3. Asinguse mtu aliyekufa. Hili la kutoshiriki katika taratibu zo zote za mazishi ya Kiyahudi lisingewezekana.
  4. Kujitia unajisi kwa kumkaribia yule aliyekufa ghafla katika Hes. 6:9. Kwa uwazi kabisa hali ya Paulo katika Matendo ya Mitume 21:23-25 ilihusisha suala hili. Kulikuwa na kipindi cha utakaso na dhabihu kilichokubaliwa (kama vile Hes. 6:9-12).

▣ **"wanyoe vichwa vyao"** Nadhiri ya Nazarethi inajadiliwa katika Namba 6. Wale walioweka nadhiri za kudumu hawakuruhusu kunyoa nywele zao. Hata hivyo, nadhiri za muda mfupi zilitambuliwa kwa sifa ya kunyoa nywele mwishoni mwa kipindi cha wakati. Mstari huu unaonyesha namna Paulo alivyojaribu kufuata utamaduni pale alipojaribu kuhubiri (kama vile 1 Kor. 9:19-23; 10:23-33).

**21:25 "tuliandika"** Aya hii inarejelea juu ya usemi wa kiutawala wa Baraza la Yerusalemu (kama vile Matendo ya Mitume 15:19-20, 28-29). Kumbukumbu hii iliondoa nadharia ya desturi na miiko ya vyakula kati ya waamini wa Kiyahudi na waamini wa makundi ya Mataifa katika mchanganyiko wa makanisa ya Wayahudi waliotawanyika katika mataifa mbalimbali (nje ya Palestina). Hili, hata hivyo, halikuwa na uhusiano wa Wayahudi waaminio na Agano la Musa.

**21:26 "tukaingia ndani ya hekalu"** Hili ndilo lililosababisha ghasia, si kulitatua!

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 21:27-36

<sup>27</sup> Basi zile siku saba zilipokuwa karibu kutimia, Wayahudi waliotoka Asia wakamwona ndani ya hekalu, wakawataharakisha watu wote, wakamkamata, <sup>28</sup> wakapiga kelele, na kusema, Enyi wanaume wa Israeli, tusaidieni. Huyu ndiye mtu yule afundishaye watu wote kila mahali kinyume cha taifa letu na torati na mahali hapa. Tena, zaidi ya haya, amewaingiza Wayunani katika hekalu, akapatia unajisi mahali hapa patakatifu. <sup>29</sup> Kwa maana walikuwa wamemwona Trofimo, Mwefeso, pamoja naye mjini, ambaye walidhanja ya kuwa Paulo amemwingiza katika hekalu. <sup>30</sup> Mji wote ukataharuki, watu wakakutanika mbio mbio, wakamkamata Paulo, wakamkokota, wakamtoa hekaluni; mara milango ikafungwa. <sup>31</sup> Na walipokuwa wakitafuta njia ya kumwua, habari zikamfikilia jemadari wa kikosi ya kwamba Yerusalemu imechafuka, mji mzima. <sup>32</sup> Mara akatwaa askari na maakida, akawashukia mbio. Nao walipomwona jemadari na askari wakaacha kumpiga Paulo. <sup>33</sup> Kisha jemadari akakaribia, akamshika, akaamuru afungwe kwa minyororo miwili; akauliza, Nani huyu? Tena, amefanya nini? <sup>34</sup> Wengine katika makutano wakapiga kelele wakisema hivi, na wengine hivi. Basi alipokuwa hawezi kupata hakika ya habari kwa sababu ya zile kelele, akatoa amri aletwe ndani ya ngome. <sup>35</sup> Basi Paulo alipofika darajani ilikuwa kuchukuliwa na askari kwa sababu ya nguvu ya makutano. <sup>36</sup> Maana kundi kubwa la watu wakamfuata, wakipiga kelele, na kusema, Mwondoe huyu.

**21:27 "Wayahudi waliotoka Asia"** Maadui wa kale wa Paulo iliwapasa kuja Yerusalemu kwa ajili ya sikukuu pia. Sasa Paulo alikuwa nje ya dini ya Kiyahudi.

**21:28 "Huyu ndiye mtu yule afundishaye"** Hawa Wayahudi wa ki-Asia waliyafasiri mahubiri ya Paulo kama yaliyo kinyume na dini ya Kiyahudi badala ya kukamilisha ahadi za Agano la Kale. Haya mashtaka ni sawa na yale yaliyofanyika dhidi ya Stefano (kama vile Matendo ya Mitume 6:13). Paulo mwenyewe amelielezea hili; hakika alikubaliana na nafasi hii ya theolojia ya Kiyahudi (kama vile Matendo ya Mitume 22:20) kabla ya kukabilina kwake na Kristo huko Dameski. Huu ujumbe wa Kristo ulidhohofisha nadharia ya sheria na nadharia ya taratibu za dini maarufu ya Kiyahudi ya karne ya kwanza! Hili halikuonekana kama wazo la Paulo kuhusu wokovu wa kiulimwengu uliopatikana kwa "watu wote tu"—bali pia dai la kitheolojia la wokovu tengefu ndani tu na kupitia imani katika Kristo.

▣**"zaidi ya haya, amewaingiza Wayunani katika hekalu"** Hili tukio la kudhahaniwa lingalipaswa kufanyika katika ua wa ndani wa Israeli, ambapo nadhiri za Wanazareti zilifanyika kwenye kingo za kusini mashariki. Hili lilikuwa la kisheria kwa Mataifa kuingia ua wa nje wa Hekalu pekee. Hili lilikuwa shtaka la uongo (kama vile Matendo ya Mitume 21:29).

**21:29 "Trofimo, Mwefeso"** Hawa Wayahudi kutoka Asia (Efeso) waliwafahamu wote Paulo na Trofimo na walipanga kifo cha Paulo tokea mwanzo (kama vile Matendo ya Mitume 20:3). Na sasa waliiona nafasi yao kuendelea na chuki za ubaguzi wa rangi ya Kiyahudi na Paulo kuuawa (kama vile Matendo ya Mitume 21:31,36).

**21:30 "milango ikafungwa"** Inavyoonekana hili lilikuwa lango la Ua wa Israeli na Ua wa Wanawake. Hekalu lilikuwa na nguvu yake ya dola ya Walawi walioshikilia maagizo. Tendo hili lilikuwa kwa ajili ya

1. kulitunza Hekalu lisinajisiwe
2. kumlinda Paulo kwa kujaribu kumrudisha Hekaluni kwa ajili ya usalama

Wayahudi hawa walitenda katika namna ile ile kama ulivyofanya umati huko Efeso (kama vile Matendo ya Mitume 19).

**21:31 "jemadari wa kikosi"** Kiuhalisia huyu ni kiongozi wa maelfu. Huyu anaweza kuwa mtawala wa ngazi ya juu katika jeshi la Kirumi (mpanda farasi) aliyepewa cheo humo Yerusalemu wakati umati ulipofurika mara tatu kutoka idadi yake ya kawaida. Kazi yeke ilikuwa kushikiria maagizo.

▣**"kikosi maaskari"** Waliishi katika Ngome ya Antonia, ambayo ilikuwa imetazamana sana na Ua wa Hekalu. Hii ilijengwa na Herode Mkuu kama mahali, lakini sehemu hii ilitumiwa na Warumi kama makao makuu ya jeshi (kama vile Josephus, *Wars* 5.5.8).

**21:32 "askari na maakida"** Kiuhalisia akida alikuwa kiongozi wa mamia. Ngome ya Antonia ilikuwa imetazamana sana na eneo la Hekalu. Eneo hili lilikuwa limeimarishwa sana kwa ulinzi, hasa wakati wa kipindi cha siku za sikukuu.

**21:33 "afungwe kwa minyororo miwili"** Hili lingemaanisha (1) mikono na miguu ama (2) miongoni mwa askari wa Kirumi. Kwa uwazi kabisa askari walifikiri huyu alikuwa mfitinishaji (kama vile Matendo ya Mitume 21:38).

**21:34-35** Hili linaonyesha ghasia na taharuki ya makutano (kama vile Matendo ya Mitume 21:30).

**21:35 "madaraja"** Haya madaraja yalitanda toka Ngome ya Antonia kuelekea eneo la hekalu ambalo limedokezwa katika Matendo ya Mitume 21:32, "kuwashukia mbio." Kulikuwa na sehemu mbili za mapitio haya ya madalaja, kila moja likielekea katika sehemu mbalimbali za hekalu. Warumi walitaka kumwondosha kwa haraka yeyote aliyekonekana kuandamana. Siku za sikukuu mara nyingi zilikuwa siku za machafuko ya kitaifa.

**21:36 "Mwondoe huyu"** Haya ni maneno sawa na yale yaliyozungumzwa juu ya Yesu (kama vile Matendo ya Mitume 22:22; Luka 23:18; Yohana 19:15). Kuna ufanano mwingi kati ya Wayahudi na Warumi namna walivyowaenda Paulo na Yesu.

## ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 21:37-40

<sup>37</sup> Naye alipokuwa analetwa ndani ya ngome, Paulo akamwambia jemadari, Nina ruhusa nikuambie neno? Naye akasema, Je! Unajua Kiyunani? <sup>38</sup> Wewe si yule Mmisri ambaye kabla ya siku hizi aliwafitinisha wale watu elfu nne, walioitwa Wauaji, akawaongoza jangwani? <sup>39</sup> Paulo akasema, Mimi ni mtu wa Kiyahudi, mtu wa Tarso, mji wa Kilikia, mwenyeji wa mji usiokuwa mnyonge. Nakuomba, nipe ruhusa niseme na wenyeji hawa. <sup>40</sup> Basi, alipompa ruhusa, Paulo akasimama madarajani, akawapungia mkono wale wenyeji; na ilipokuwa kimya kabisa, akanena nao kwa lugha ya Kiebrania, akisema,

**21:37 "Unajua Kiyunani"** Koloneli alistaajabishwa na Paulo kuzungumza lugha ya Koine ya huko Uyunani kwa sababu kwa hakika alifikiri kwamba Paulo alikuwa mfitinishaji wa Kimisri kama alivyosikia kumhusu (kama vile Matendo ya Mitume 21:38 na *Antiq.* 2.1 3.5;20.8.6 Josephus). Uasi huu wa Kimisri ulitokea kati ya 52-57 b.k.

**21:38"yule Mmisri" Hili ni neno *sicarii*,** ambalo ni neno Kilatini lenye maana ya muuaji au mchinjaji. Katika Kitabu cha Agano Jipya mara nyingi hawa waliitwa "wakereketwa" katika (kama vile Luka 6:15; Matendo ya Mitume 1:13). Hili lilikuwa kundi la Wayahudi lililojitolea kwa ajili ya mashambulizi ya kimachafuko kwa Warumi. A. T. Robertson, *Word Pictures in the New Testament*, juzuu. 3, uk. 382, anataja kwamba hili neno la pekee lilitumiwa na Josephus kueleza juu haya wafitishaji wa Kiyahudi (kama vile Josephus, *Wars* 2.13.5; *Antiq.* 20.8.6,10).

**21:39"mwenyeji wa mji usiokua wa mnyonge"** Hii ni nahau (*litotes*, tazama katika Matendo ya Mitume 12:18), ambayo Paulo alitumia kuelezea juu ya uenyeji wake katika wa mji wenye chuo kikuu chenye hadhi ya kulimwengu. Maelezo mengine yanayofuatia hayaelezi kama mtawala wa Kirumi alijawa na hofu.

**21:40 "alipompa ruhusa"** Huyu jemedari bado alitaka kujua hili lilihusu nini!

▣**"akawapungia mkono"** Kwa uwazi hili lilijulikana vema kuwa kupunga mkono ni ishara ya kunyamazisha watu ili mtu aweze kuzungumza (kama vile Matendo ya Mitume 12:17; 13:16; 19:33; 21:40; 26:1). Hii inaweza kuwa ishara ya mazungumzo ambayo Paulo alijifunza wakati alipokuwa akichukua mafunzo ya ufasaha wa maneno huko Tarso.

▣**"akanena nao kwa lugha ya Kiebrania"** Paulo alinena na makutato katika lugha ya Kiaramu (Wayahudi walikuwa wamejifunza kuzungumza Kiaramu katika miaka yao ya utawala wa Kiajemi). Ishara hii iliwanyamazisha makutano kwa muda fulani (kama vile Matendo ya Mitume 22:2)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki.

Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ikiwa nmanabii wa kila walimwambia Paulo kutokwenda huko Yerusalemu, kwani nini alienda?
2. Ni kwa jinsi gani/wahayahudi waaminio walihusiana na Agano la Musa?
3. Je! Mashtaka ya Wayahudi wa Kiasia dhidi ya Paulo katika Matendo ya Mitume 21:28a yalikuwa ya kweli?
4. Je! maoni ya jemedari (Matendo ya Mitume 21:38) yana maanisha kwama Wayahudi wachache walifahamu Kiyunani au kwamba yeye alifikiri Paulo alikuwa Mmisri?

## MATENDO YA MITUME 22

MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA				
UBS <sup>4</sup>	NKJV	NRSV	TEV	NJB
Paulo anajitetea Mwenyewe 21:37-22-5	Anahutubia umati wa Yerusalemu 21:37-22:21	kukamatwa kwa Paulo na kujitetea (21:27-22:29) 21:37-22:1	Paulo anajitetea Wayahudi wa Yerusalemu (21:37-22:5)	Paulo anahutubia 22:1-5
Paulo anaelezea Uongofu wake 22:6-11 22:12-16		22:2 22:3-5	22:3-5 Paulo anaelezea uongofu wake	
Paulo anatumwa Kwa Mataifa 22:17-21		22:17-21	Paulo anaitwa kuhubiri kwa Mataifa 22:17-21	22:17-21
Paulo na kiongozi Wa Kirumi 22:22-29	Uraia wa Kirumi wa Paulo 22:22-29	22:22-29	22:22-25 22:26 22:27a 22:27b 22:28a 22:28b 22:29	Paulo mwenye uraia wa Kirumi 22:22-29
Paulo mbele ya Baraza (22:30-23:11) 22:30-23:5	Wakuu wa baraza la Sinagogi wagawanyika 22:30-23:10	22:30	Paulo mbele ya baraza (22:30-23:11) 22:30	Uwepo wake mbele ya wakuu wa baraza la Sinagogi (22:30-23:11) 22:30

### KUSOMA MZUNGUKO WA TATU (kutoka “[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)

#### *KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza

2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 22:1

<sup>1</sup>Enyi wanaume, ndugu zangu na baba zangu, nisikilizeni, nikijitetea mbele yenu sasa.

22:1

NASB "Ndugu zangu na Baba zangu"

NKJV "Wanaume, ndugu zangu na Baba zangu"

NRSV "ndugu zangu na Baba zangu"

TEV "Wayahudi wenzangu"

NJB "ndugu zangu, Baba zangu"

*A Translator's Handbook on the Acts of the Apostles*, kilichoandikwa na Newman na Nida kinasema hii inamaanisha watu wa kizazi cha Paulo na wale ambao ni wakubwa zaidi yake (kama vile ukurasa wa 419). Hata hivyo, nafikiri hii lazima ni nahau (Stephano alitumia kauli ya utangulizi hii katika Mdo. 7:2) kwa kuwa Paulo alikuwa na umri zaidi ya miaka 60 wakati huu na hii haishabihiani na umri wa wafanya ghasia. Kulikuwa na baadhi ya waamini katika umati huu. Yawezekana neno hili "ndugu" kipekee linawamaanisha wao. Hata hivyo, Paulo siku zote alitambulikana kwa uraia wake na utaifa (kama vile Rum 9:1-5; Flp. 3:5).

▣"nikijitetea" Tunapata neno la Kiingereza "apology (msamaha)" kutoka katika neno hili la Kiyunani (*apologia*). Ilimaanisha ulinzi/kujitetea kwa kisheria kwa njia ya mdomo. Neno hili lilitumika mara kadhaa katika Matendo ya Mitume likihusianishwa na mashtaka ya Paulo (kama vile Mdo. 25:16; 2 Tim. 4:16).

### ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA): MATENDO YA MITUME 22:2

<sup>2</sup>WaliposikiakwambaanasemanaokwalughayaKiebraniawakazidikunyamaza; akasema,

22:2 "lughu ya Kiebrania" Hii inamaanisha kiaramaiki. Maeneo yote katika Injili ambapo maneno halisi ya Yesu yameandikwa yapo katika lugha ya Kiaramaiki. Hii ilikuwa ni lugha kwa kiebrania cha kale. Ilikuwa ni lugha ya ufalme wa Kiajemi. Wayahudi walijifunza walipokuwa chini ya utawala wao. Kwa mfano katika Nehemia 8, ambapo Ezra anasoma sheria ya Musa katika Kiebrania, Walawi walitakiwa kuifasiri kwenda katika lugha ya Kiaramaiki kwa ajili ya watu (kama vile Neh. 8:7).

▣"wakazidi kunyamaza" Utangulizi wa Paulo wa kipole ukiunganishwa na weredi wake wa Kiaramaiki na ukweli kwamba wengi wa watu hawa wafanya ghasia walimfahamu kunasababisha utulivu wa ghafla na wa kushangaza. Walitaka kusikia kile ambacho alitaka kusema- fursa nzuri na kamilifu ya kuhubiri kwa viongozi wa dini ya Kiyahudi.

### ANDIKO LA NASB (LILLOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 22:3-5

<sup>3</sup>Mimi ni mtu wa Kiyahudi, nalizaliwa Tarso, mji wa Kilikia, ila nililelewa katika mji huu, miguuni pa Gamalieli, nikafundishwa sheria ya baba zetu kwa usahihi, nikawa mtu wa jitihadi kwa Mungu kama ninyi nyote mlivyo leo hivi; <sup>4</sup>nikawaudhi watu wa Njia hii hata kuwaua, nikawafunga, nikiwatia gerezani, wanaume na wanawake.

<sup>5</sup>Kama Kuhani Mkuu naye anishuhudiavyo, na wazee wa baraza wote pia, ambao nalipokea barua kwao kuwapelekea ndugu wale, nikaenda Dameski, ili niwalete wale waliokuwa huko hata Yerusalemu, hali

## wamefungwa, ili waadhibiwe.

**22:3 "Mimi ni mtu wa Kiyahudi, nalizaliwa Tarso"** Paulo anajaribu kujitambulisha mwenyewe na umati huu wa Kiyahudi. Anaelezea Uyahudi wake (kama vile 2 Kor. 12:22; Flp. 3:5-6). Alikuwa akichukuliwa kama Myahudi anayezungumza Kiyahudi aliyeko ughaibuni. Tungo "lakini nimelelewa katika mji huu" kisarufi kunaweza kumaanisha aidha (1) Tarso au (2) Yerusalemu. Kimuktadha, Yerusalemu ilimaanisha. Ikiwa hivyo ndivyo, mafunzo ya Paulo katika sitiari lazima yalitokea/kufanyika sehemu fulani pembeni.

▣ **"nikafundishwa chini ya Gamalieli"** Huyu alikuwa mwalimu aliyeheshimiwa sana (kama vile Mdo. 5:34-40). Ananukuliwa katika *Mishnah* mara kadhaa. Paulo alikuwa mwalimu huru wa shule ya Hillel. Umati huu ungekuwa umefurahishwa na kauli hii. Angalia [MADA MAALUM: GAMALIELI](#) katika Mdo. 5:34.

▣ **"kwa usahihi sawa na sheria za baba zetu"** Hii ingemaanisha kwamba alikuwa Mfarisayo (kama vile Mdo. 23:6; 26:5) na mwenye shauku na hicho (kama vile Mdo. 22:4; Gal. 1:14; Flp. 3:6). Mfarisayo walikuwa wamejitoa katika utii wa kuongea (yaani Talmud), ambayo inatafsiriwa kuwa Agano Jipya.

▣ **"kama ninyi nyote mlivyo leo hivi"** Paulo anatambua ari zao na uthabiti wao. Hapo kabla alikuwa mmoja wao!

**22:4 "Nililiudhi"** Wakati wote wa huduma ya Paulo aliziangalia siku zilizopita kwa majuto makubwa. Analitaja hili mara kwa mara (kama vile Mdo. 9:1,13,21; 22:4,19; 26:10-11; Gal. 1:13,23; Flp. 3:6; 1 Tim. 1:13). Paulo mara kwa mara anamaanisha kwake yeye mwenyewe kama mdogo wa watakatifu kwasababu ya matendo yake (kama vile 1 Kor. 15:9; 2 Kor. 12:11; Efe. 3:8; 1 Tim. 1:15).

▣ **"Njia hii"** Hili lilikuwa jina la mwanzoni kabisa la kanisa la Kikristo (kama vile Mdo. 9:2; 19:9,23; 22:4; 28:14,22). Inarejerea

1. Yesu kama "Njia" (kama vile Yohana 14:6)
2. imani ya kibiblia kama mtindo wa maisha (kama vile Kumbukumbu la Torati 5:32-33; 31:29; Zaburi 27:11; Isa. 35:8)

▣ **"kwa kifo"** Paulo alikuwa nao baadhi ya Wakristo waliouawa (kama vile Mdo. 8:1,3; 26:10)! Kweli alihusika katika kifo cha Stephano (kama vile Mdo. 7:58, 8:1).

▣ **"kuwafunga na kuwaweka gerezeni waume kwa wake"** Ukweli kwamba Paulo alifanya hivi kwa wanawake hakika inaonesha uzito wa mateso yake.

**22:5** Paulo anashirikisha mazingira yake yaliyompelekea kuongoka kwake kiimani kwa Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9).

▣ **"Baraza la Wazee"** Hii kidhahiri ni "wazee wote." Luka anatumia neno hilo kwa ajili ya Baraza la Wazee wa Sinagogi katika Luka 22:66. Hili sio jina la kawaida linalotumika katika mwili huu wa viongozi wa Kiyahudi (SBaraza la wazee wa Sinagogi). Inaweza kumaanisha kamati ndogo ya kiutawala.

▣ **"Mimi pia nalipokea nyaraka"** F. F. Bruce, *Paul: Apostle of the Heart Set Free*, ana mjadala mzuri na kumbukumbu ya kimaandiko ya haki utendaji kazi za baraza la wazee wa Sinagogi kutoka katika nchi zinazozunguka (ukurasa wa 72). Kwa taarifa zaidi za kihistoria angalia I Macc. 15:21 na Falvius Josephus.

▣ **"wale waliokuwepo pale"** Tungo hii inamaanisha kwamba hawa walikuwa Wayahudi waaminio waliokuwa wamekimbia mateso katika Yerusalemu.

## ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 22:6-11

6Ikawa nilipokuwa nikisafiri, nikikaribia Dameski, wakati wa aduhuri,ghafula nuru kuu ilitoka

mbinguni, ikanimulikia pande zote. 7Nikaanguka chini, nikasikia sauti ikiniambia, Sauli, Sauli, mbona unaniudhi? 8Nikajibu, Wewe u nani, Bwana? Akaniambia, Mimi ni Yesu Mnazareti, ambaye wewe unaniudhi. 9Na wale waliokuwa pamoja nami waliiona ile nuru, lakini hawakuisikia ile sauti ya yule aliyesemanami. 10Nikasema, Nifanye nini, Bwana? Bwana akaniambia, Simama, uingie Dameski, na huko utaambiwa habari za mambo yote yaliyoamriwa uyafanye. 11Na nilipokuwa sioni kwa sababu ya fahari ya nuru ile, nikaongozwa na mikono ya owaliokuwa pamoja nami, nikaingia Dameski.

**22:6 "wakati wa aduhuri"** Haya ni maelezo ya nyongeza yasiyopatikana katika kitabu cha Matendo ya Mitume 9:3.

**22:7** Haya ni marudio ya Mdo. 9:4.

**22:8**

**NASB, NJB "Yesu Mnazareti"**

**NKJV, NRSV**

**TEV "Yesu wa Nazareti"**

Paulo anashirikisha ushuhuda wake binafsi mara tatu katika Matendo ya Mitume 9:1-31; 26:4-18, lakini hapa na 26:9 hapa ni mahali pekee ambapo anatumia maelezo. Kidhahiri anayeongelewa hapa ni "Yesu mnazareti." Hili ni neno la matengenezo katika Mdo. 24:5, lakini ni neno la unabii katika Mt. 2:23. Inawezekana kuwa sio maelezo ya kijiografia, lakini cheo/jina la Kimasihi kutoka "tawi" (kama vile Isa. 11:1; 53:2) kutoka katika neno la Kiebrania *nēser* (kama vile Yer. 23:5; 33:15; Zeka.3:8; 6:12). Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:22.

▣ **"Ni Mimi unayeniudhi"** Angalia dokezo kamili katika Mdo. 9:4.

**22:9 "lakini hawakuielewa sauti"** Hakuna mgongano katika ya habari za uongofu wa Paulo katika Mdo. 9:7 na 22:9. Sarufi ya Kiyunani inamaanisha kwamba wenzake walisikia sauti lakini hawakuyaelewa maneno. Angalia 9:7 kwa ajili ya mjadala kamili.

**22:10 "Wote kwamba waliteuliwa kwa ajili yako"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati timilifu. Inaaksi maneno ya Yesu kwa Anania katika Mdo. 9:15-16. Paulo alikuwa mpango maalum na mgumu kuutekeleza. Katika namna kadhaa Maono ya Paulo na agizo yanafuata manabii wa Agano la Kale (kama vile Isa. 6; Yer. 1; Ezek. 2-3). 22:11 Nafikiri hii ilikuwa ni sababu ya Paulo kusema "mwiba katika mwili." Baadhi ya nadharia zihusuzo mwiba wa Paulo katika Mwili ni:

1. Mababa wa kanisa la kwanza, Luther, na Calvin, wanasema ilikuwa ni matatizo yake ya kiroho na asili yake iliyoanguka (yaani "katika mwili")
2. Krisostom anasema ilikuwa ni matatizo na watu (kama vile Hesabu 33:55; Waamuzi 2:3)
3. wengine wanasema ilikuwa ni kifafa
4. Mheshimiwa William Ramsay anasema ilikuwa ni Maralia
5. Nafikiria kuwa ilikuwa ni ugonjwa wa macho, tatizo la macho lililozoeleka na linalojulikana (linganisha na Gal. 4:13-15 na 6:11) lililochochea au kusababishwa na upofu wake wa awali njiani akielekea Dameski (kama vile Mdo. 9, Yawezekana ni maelezo ya Agano la Kale katika Yohua23:13)

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 22:12-16**

<sup>12</sup> Basi mtu mmoja, Anania, mtauwa kwa kuifuata sheria, aliyeshuhudiwa wema na Wayahudi wote waliokaa huko, <sup>13</sup> Akanijia, akasimama karibu nami, akaniambia, Ndugu yangu Sauli, uone. Nikamwinulia macho yangu saa ile ile. <sup>14</sup> Akasema, Mungu wa baba zetu amekuchagua wewe upate kujua mapenzi yake, na kumwona yule Mwenye haki, na kuisikia sauti itokayo katika kinywa chake. <sup>15</sup> Kwa maana utakuwa shahidi wake kwa watu wote, wa mambo hayo uliyoyaona na kuyasikia. <sup>16</sup> Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake.

**22:12** Haya ni maelezo kamili ya Anania kuliko 9:10. Inavyoonekana alikuwa mtu asiyekuwa na elimu, kama Paulo alikuwa mcha Mungu kulingana na sheria ya Musa. Inawezekana ilimaanisha kuwa pia alikuwa Farisayo.

1. Luka kwa mfanano huohuo anamuelezea Simeoni, mtu aliyemuona Yesu hekaluni wakati akiwa mdogo sana (kama vile Luka 2:25).
2. Luka pia analitumia juu ya Wayahudi wa ughaibuni waliokuja Yeusalemu siku ya Pentekoste wakati Roho alipokuja kwa nguvu (kama vile Mdo. 2:5).
3. Luka analitumia mara ya tatu juu ya watu waliomzika Stephano baada ya kupigwa mawe (kama vile Mdo. 8:2).

Hivyo neno hili halishabihiani na mwamini katika Kristo kama mfuasi wa dhati wa dini ya kiyahudi. Anaitwa "mwanafunzi" katika Mdo. 9:10; Hivyo alikuwa amefanyika mwamini. Na bado hata kama alikuwa Mkristo, alikuwa bado na heshima kwa jamii ya kiyahudi katika Dameski.

**22:13** Huduma ya Anania kwa Paulo inatuonesha sisi kwamba hakuna mgawanyo wa wazi wa waamini wa Agano Jipya kati ya makasisi (kundi maalum lililowekwa wakfu) na wahudumu. Maneno ya Yesu yalikuwa mamlaka kwa:

1. kuwekea mikono (kama vile Mdo. 9:12,17) juu ya Paulo na kuamuru uponyaji (kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu, Mdo. 22:13, Angalia Mada Maalum katika Mdo. 6:6)
2. kufunua mapenzi ya Yesu kwa huduma ya Paulo (Mdo. 22:15)
3. kumwambia Paulo abatizwe (Paulo yawezekana alikuwa amebatizwa mwenyewe kama matakwa ya mwongofu ya Wayahudi, kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu, Mdo. 22:16)
4. Kuwa chombo cha Paulo kujazwa na Roho (kama vile Mdo. 9:17)

Unaweza kuona moyo wa Anania anapomuita huyu mtesi wa wazi na muuaji (kama vile Mdo. 9:13-14) "Ndugu Sauli."

**22:14 "Mungu wa baba zetu"** Tungo hii ilitumika kuelezea Uungu wa ibada za kiyahudi. Paulo anataka kuweka wazi kuwa ilikuwa ni YHWH (angalia Mada Maalum katika 1:68) aliyewasiliana naye na kumpa agizo yeye kupitia Mwanawe Yesu. Paulo hakuitwa na mungu mwingine zaidi ya Mungu wa Uyahudi!

▣ **"kuyajua mapenzi yake"** Mapenzi ya awali na ya msingi ya YHWH ni kwa wanadamu kumjua Yesu (kama vile Yohana 6:29,40). Mapenzi zaidi ya Mungu kwa Paulo ilikuwa kuwa Mtume wa umishionari kwa Mataifa (kama vile Mdo. 9:15; 22:15; 26:16).

▣ **"kumuona Yule Mwenye Haki"** Hiki ni cheo au wadhifa wa kimasihani (kama vile Zaburi 45; 72; Mdo. 3:14; 7:52; 1 Yohana 2:1). Paulo angekuwa na fursa na upendeleo wa ufunuo binafsi wa Yesu mtukuzwa (kama ilivyokuwa kwa Stephano, kama vile Mdo. 7:55-56). Angalia [MADA MAALUM: HAKI](#) katika Mdo. 3:14.

▣ **"na kusikia usemi kutoka katika kinywa chake"** Hii inaonekana kumaanisha sauti kutoka mbinguni katika Mdo. 22:7-8 (yaani *Bat Kol*, kama vile Kumb. 4:12; 1 Wafalme 19:12-13; Ayubu 4:16; Yer. 25:30; Ezek. 1:25,28; Yoeli 3:16; Amosi 1:2; Luka 3:22; 9:35; Mdo. 10:13,15), Lakini ilikuwa kama ikimaanisha zaidi kwa Mdo. 22:17-21. Pia inawezekana kwamba inamaanisha maono maalum kadhaa ambayo Paulo alikuwa nayo wakati wote wa huduma yake. Angalia orodha katika Mdo. 22:17-21.

**22:15 "ushuhuda . .kwa watu wote"** Huu ni ukweli wa kushangaza kwamba Injili ya Yesu Kristo kwa wanadamu wote (kama vile Yohana 3:16; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:1; 4:14). Sio wote watakaopokea, sio wote wanaweza kuelewa kirahisi lakini wote wanajumuishwa katika upendo wa Mungu na dhabihu ya Yesu na mahubiri ya Paulo! Huu ni ukweli kwamba ghasia hizi zilikataliwa (kama vile Mdo. 22:22). Paulo kwa makusudi hatumii neno "Mataifa" kwamba Anania alimrithisha yeye kutoka kwa Yesu (kama vile Mdo. 9:15). Paulo alijua mlipuko wa namna gani neno hili la kushusha hadhi *go'im* (nchi au Mataifa) ingekuwa kwa



wayahudi hawa washika dini. Ubaguzi wake na majivuno yao ya kimakabila yalikuwa hata yamesababisha kuminywa kwa unabii jumuishi wa manabii wa Agano la Kale!

▣"**Mliyoyasikia na kuona**" Hiki kitenzi cha kwanza ni kauli tendaji elekezi ya wakati ulio timilifu; cha pili ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Kwanini njeo mbali mbali hazina uhakika. Zinaonekana kuwa sambamba. Paulo atabeba kumbukumbu ya kukutana kwake binafsi na Kristo mfufuka katika nyakati zote za maisha yake. Anataja hili mara tatu katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Yawezekana alitoa ushuhuda wake binafsi katika kila Sinagogi.

**22:16 "mbatizwe na kuoshwa dhambi zenu"** Zote ni kauli za kati shurutishi za wakati uliopita usiotimilifu. Haya ni maelezo ya Agano la Kale kwa matukio ya kisherehe (kama vile Law. 11:25,28,40; 13:6,34,56; 14:8-9; 15:5-13,21-22,27; 16:26,28; 17:15-16; Hesabu 8:7,21; 19:19; Kumb. 23:11). Inatumika hapa kama kiwakilishi cha kuoshwa kiroho katika Kristo (kama vile 1 Kor. 6:11; Efe. 5:26; Tito 3:5; Ebr. 10:22). Ubatizo ulikuwa ukiri wa wazi wa kanisa la kwanza. Angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:38 kwa ajili ya mjadala kamili wa kithiolojia. Tazama irabu sauti ya kati ikimaanisha ubatizo wa aina zote mbili (kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu) na kusafishwa (kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu). Paulo asingeliweza kuosha dhambi zake, lakini angeliweza kujibatiza mwenyewe (desturi za kiyahudi kwa waongofu). Mara kwa mara inasemekana kwamba kuzamishwa ni utaratibu pekee wa Agano Jipya (kama vile Warumi 6 na Wakolosai 2), lakini hapa Ubatizo unaunganishwa na sitiari ya kuoshwa (kama vile Mdo. 2:38; 1 Kor. 6:11; Efe. 5:26; Tito 3:5; Ebr. 10:22). Kithiolojia 1 Pet. 3:21 inaonesha kwamba ni kiwakilishi na sio Sakramenti! Wafasiri wa kisasa lazima wawe waangalifu juu ya kujikita sana kwenye sauti irabu ya kati au tendwa kwasababu haya yalikuwa yanaunganishwa kwenye muundo wa kauli tendwaji. Paulo inasemekana alibatizwa (KAULI TENDWAJI) katika Mdo. 9:18. Namna ya ubatizo wa Paulo sio jambo kubwa sana lakini ubatizo wake yeye mwenyewe!

▣"**kuliitia jina lake**" Hili "jina" sio kanuni ya kimiujiza, lakini kutambuliwa kwa wazi juu ya umiliki wa Yesu na mwanzo wa uhusiano wa kibinafsi pamoja naye (kauli ya kati endelevu ya wakati uliopita usio timilifu ikitumika kama kauli shurutishi), ambalo ni jambo la mtazamo wa kufanana na Kristo na mtindo wa maisha. Kanuni ya ubatizo wa kanisa la mwanzo ilisema wazi kwa njia yam domo na mwanafunzi "Yesu ni Bwana" (kama vile Rum. 10:9-13; 1 Kor. 1:2; 2 Tim. 2:22). Maneno halisi au kanuni sio ya msingi (ya Usakramenti), lakini moyo wa uanafunzi (amini, pokea). Angalia dokezo katika Mdo. 2:38 na Mada Maalum katika Mdo. 2:21.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 22:17-21**

<sup>17</sup> Ikawa nilipokwisha kurudi Yerusalemu, nilipokuwa nikisali ndani ya hekalu, nikawa hali ya kuzimia roho, <sup>18</sup> nikamwona, naye akiniambia, Hima, utoke Yerusalemu upesi, kwa sababu hawatakubali ushuhuda wako katika habari zangu. <sup>19</sup> Nami nikasema, Bwana, wanajua hao ya kuwa mimi nalikuwa nikiwafunga gerezani wale wanaokuamini na kuwapiga katika kila sinagogi. <sup>20</sup> Na damu ya Stefano shahidi wako ilipomwagwa, mimi nami nilikuwa nikisimama karibu, nikikubali, na kuzitunza nguo zao waliomwua. <sup>21</sup> Naye akaniambia, Enenda zako; kwa kuwa mimi nitakutuma uende mbali kwa watu wa Mataifa.

**22:17-21** Huu ni mmoja wa mfano mwingine wa maono maalum ya Paulo (kama vile Mdo. 18:9-10; 23:11; 27:23-24). Katika muktadha huu inashabihiana na unabii wa Mdo. 22:14.

**22:17 "Nilipokwisha kurudi Yerusalemu"** Katika shuhuda wa Paulo katika Mdo. zote 9 na hapa, kunavyoonekana inavyoamaanisha kwamba alirudi Yerusalemu punde tu baada ya kurudi kwake, lakini Gal. 1:11-24 inafunua kipindi

kirefu (mpaka miaka miaka mitatu) kabla ya Paulo kurudi.

▣"**nikaanguka katika jaribu**" Angalia dokezo katika Mdo. 10:10.

**22:18** Yesu anazungumza Kauli tendaji shurutishi za wakati uliopita usio timilifu kwa Paulo: "Fanya hima" na "ondoka." Maonyo ya Yesu yanaelezwa katika njama/hila za walimu wa ungu wa kiyahudi za mauaji, zilizoandikwa katika Mdo. 9:29.

**22:19 "Bwana"** Sarufi ya jambo hili inaweza kuwa aidha "Mungu wa Baba zetu" (Mdo. 22:14) au "Mwenye haki" (Mdo. 22:14). Kikundi cha ghasia cha Kiyahudi kingeweza kuwa kimeelewa YHWH, lakini mwamini yoyote aliyekuwapo angeweza kujua kuwa ni Yesu. Kugeuzwa ni kawaida katika nukuu za Agano la Kale zinapotumika juu ya Yesu katika Agano Jipya. Ni tungo tata ya "imani juu ya Mungu mmoja katika Utatu" (Angalia Mada Maaluma katika Mdo. 2:32 na 2:39)!

▣ **"Nikiwafunga na kuwapiga"** Hizi ni kauli tendaji za wakati usiotimilifi zenye mafumbo, ambazo zinaashiria kitendo kinachoendelea katika wakati uliopita. Angalia dokezo kamili katika Mdo. 22:4.

▣ **"Wale waliokuamini wewe"** Angalia Mada Maalum zinazohusiana katika Mdo. 2:40, 3:16, na 6:5.

**22:20** Angalia dokezo katika Mdo. 7:58-59 na 8:1. Paulo anaelezea tamaa yake ya kwanza ya matendo yake kwa kutumia kauli endelevu za wakati usiotimilifu zenye mafumbo tatu.

1. Alikuwa amasimama pale na kikundi cha wafanya ghasia.
2. Alikuwa anakubaliana na upigwaji wa mawe.
3. Alikuwa anawalinda wale waliokuwa wakimpiga mawe Stephano.

Mahubiri ya Stephano na kifo chake vilikuwa na ushawishi mkubwa kwa Paulo.

**22:21 "Nitakutuma wewe mbali kwa Mataifa"** Hii ni rejea ya wazi kwa safari za kimishonari za Paulo na kilele cha ushuhuda mbele ya viongozi wa kiserikali ya Kirumi katika Palestina na pia Rumi mbele ya Kaisari (kama vile Mdo 23:11). Alijua kauli hii ingeweza kuamsha umati!

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 22:22-29**

<sup>22</sup> Wakamsikiliza mpaka neno lile, wakapaza sauti zao, wakisema, Mwondoe huyu katika nchi, kwa maana haifai aishi. <sup>23</sup> Walipokuwa wakipiga kelele na kutupa mavazi yao na kurusha-rusha mavumbi juu, <sup>24</sup> yule jemadari akaamuru aletwe ndani ya ngome, akisema aulizwe habari zake kwa kupigwa mijeledi, ili ajue sababu hata wakampigia kelele namna hii. <sup>25</sup> Hata walipokwisha kumfunga kwa kamba, Paulo akamwambia yule akida aliyesimama karibu, Je! Ni halali ninyi kumpiga mtu aliye Mrumi naye hajakuhumiwa bado? <sup>26</sup> Yule akida aliposikia, akaenda akamwarifu yule jemadari, akisema, Unataka kufanya nini? Kwa maana mtu huyu ni Mrumi. <sup>27</sup> Jemadari akaja, akamwuliza, Niambie, u Mrumi? Akasema, Ndiyo. <sup>28</sup> Jemadari akajibu, Mimi nalipata wenyeji huu kwa mali nyingi. Paulo akasema, Na mimi ni Mrumi wa kuzaliwa. <sup>29</sup> Basi wale waliokuwa tayari kumwuliza wakaondoka wakamwacha. Na yule jemadari naye akaogopa, alipojua ya kuwa ni Mrumi, na kwa sababu amemfunga.

**22:22** Kauli zao ni za kinahau na zilikuwa na sehemu mbili.

1. "kuondoa (kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo) kutoka duniani kama mwanadamu" (kama vile Luka 23:18; Mdo. 21:36)
2. "hafai (kauli tendaji ya wakati usiotimilifu) kwa yeye kufa" (kama vile Mdo. 25:24)

Upendeleo wake wa kikabila na kidini vinafunuliwa. Wanadamu wote wanawekewa mazingira Fulani kihistoria na kiutamaduni.

**22:23**

**NASB** "wakiyatupa mavazi yao"

**NKJV** "wakizichana nguo zao"

**NRSV** "wakizitupa joho zao"

**TEV** "wakipunga mavazi yao"

## NJB "wakipunga joho zao"

Huku kuvua na kupunga nguo au kuyatupa angani kulikuwa ishara za Agano la Kale za kuomboleza juu ya kufuru (*Greek-English Lexicon*, Louw na Nida, vol. 1, ukurasa 213, kama vile Mdo. 14:14).

▣"**kuyarusha mavumbi angani**" Paulo ana bahati kuwa hakukuwa na mawe. Kujiwekea mavumbi juu ya kichwa kulikuwa ni ishara ya maombolezo (kama vile Yoshua 7:6; 1 Sam. 4:12; 2 Sam. 1:2; Ayubu 2:12), hapa maombolezo juu ya kufuru (kama vile Isa. 47; Maombolezo 2; Mika 1:10).

### MADA MAALUMU: I BADA KWA WALIO KATIKA HUZUNI

Waisraeli walieleza huzuni kwa mpendwa wao aliyefariki na toba binafsi, pamoja na makosa ya jinai yaliyofanyika kwa ujumla kwa njia kadhaa:

1. Kurarua mavazi, Mwa. 37:29,34; 44:13; Waamuzi. 11:35; 2 Sam. 1:11; 3:31; 1 Fal. 21:27; Ayubu 1:20
2. Kuvaa gunia, Mwa. 37:34; 2 Sam. 3:31; 1 Fal. 21:27; Yer. 48:37
3. Kuvua viatu, 2 Sam. 15:30; Isa. 20:3
4. Kuweka mikono kichwani, 2 Sam. 13:19; Yer. 2:37
5. Kuweka vumbi kichwani, Yos. 7:6; 1 Sam. 4:12; Neh. 9:1
6. Kuketi sakafuni, Omb. 2:10; Ezek. 26:16 (kulala chini, 2 Sam. 12:16); Isa. 47:1
7. Kupiga kifua, 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26; Nah. 2:7
8. Omboleza, 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26
9. Kata mwili, Kumb. 14:1; Yer. 16:6; 48:37
10. Kufunga, 2 Sam. 1:12; 12:16,21; 1 Fal. 21:27; 1 Nya. 10:12; Neh. 1:4
11. Kuimba na kusifu katika maombolezo, 2 Sam. 1:17; 3:31; 2 Nya. 35:25
12. Upara (nywele zilikatwa), Yer. 48:37
13. Kunyoa ndevu, Yer. 48:37
14. funika kichwa au uso, 2 Sam. 15:30; 19:4

Hizi zilikuwa ishara za nje kutokana na hisia za ndani

**22:24 "Jemedari"** Hili ni neno *chiliarch* (kama vile Mdo 22:27-29), ambalo linamaanisha kiongozi wa 1000, kama neno *akida* (kama vile Mdo 22:25,26) ikimaanisha kiongozi wa 100. Hata hivyo hesabu zinakaribiana. Alikuwa ni Afisa aliyesimamia jeshi la kirumi katika Yerusalemu.

▣"**Vikosi**" Hii inamaanisha ngome ya Antonia, ambayo ilionekana kuunganishwa na eneo la Hekalu. Ilikuwa imejengwa katika kipindi cha Waajemi siku za Nehemia (kama vile Neh. 2:8; 7:2). Herode Mkuu aliita upya jina la Marco Antonia. Wakati wa nyakati za karamu Yerusalemu ilijaa mara tatu zaidi ya idadi yake ya watu iliyozeleka Warumi walipeleka idadi kubwa ya vikosi kutoka Kaisaria kwenda kwenye ngome ya Antonia kwa ajili ya makusudi ya kiusalama.

▣"**kuhoji kwa kupiga**" Hii inamaanisha "kupiga ili kupata taarifa kutoka kwake." Kupiga kulikuwa ni aina ya ukatili wenye mateso. Wengi walikufa kutokana na hili. Ilikuwa ni ya kutisha na kuumiza zaidi kuliko ile ya kuburuzwa ya kiyahudi au ya kupigwa na fimbo ya Kirumi. Mapigo ya kutumia kifimbo cha ngozi kikiwa na sehemu ya chuma, jiwe au mfupa ulioшонewa kama vinyuzi nyuzi ilitumika kupiga wafungwa.

**22:25 "kumnyoosha nje"** Mara nyingi waliokutwa na haya waliinamishwa na kufungwa katika mbao ya chini ili mateso yaweze kufanyika.

▣"**Je ni sheria**" Wanajeshi hawa walikuwa wanakaribia kuasi sheria zao wenyewe kutokana na vipengele kadhaa:

1. raia wa Kirumi asingeweza kufungwa (kama vile Mdo. 21:33 na 22:29)

2. raia wa Kirumi asingeweza kubezwa na kufedheheshwa (kama vile, Livy, *History* 10:9:4; Cicero, *Pro Rabirio* 4:12-13)
3. Paulo hakuwa ameshtakiwa na kukutwa na hatia (kama vile Mdo. 16:37)

**22:27 "Wewe u Mrumi"** Hii "wewe" inawekewa mkazo. Afisa huyu wa Kirumi hakuwa anaamini kuwa Paulo ni Mrumi.

**22:28 "Nalipata Uraia huu kwa fedha nyingi sana"** Kulikuwa na njia tatu za kuwa raia wa Kirumi:

1. kwa kuzaliwa
2. kupata kutokana na huduma au kazi maalumu ya kiserikali kwa taifa
3. kwa kununua (Dio Cassius, *Rom. Hist.* 60:17:5-6)

Jina hili la Askari lilimaanisha kwamba alipata uraia wake kwa kuununua chini ya Klaudio na kwamba alikuwa Myunani (Claudius Lysias, kama vile Mdo. 23:26). Mkewe Claudio, Messaline, mara kwa mara aliuzua uraia wa Kirumi kwa fedha nyingi sana.

#### **ANDIKO LA NASB(LILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 22:30**

<sup>30</sup>Sikuyapiliyakeakitakakujuahakika, nikwasababuganiameshitakiwanaWayahudi, akamfungua, akawaamuru wakuu wa makuhani na baraza yote wakutane. Akamleta Paulo chini, akamwekambeleyao.

**22:30 "akawaamuru wakuu wa makuhani na baraza yote wakutane"** Hii inaonesha nguvu ya Kirumi. Wazee wa Baraza la Sinagogi lililazimishwa kukutana, yawezekana katika ngome Antonio. Hii inaonekana kuwa haikuwa rasmi, bali mkutano wa kirejareja. Paulo alitakiwa kukabiliana na mashtaka haya lakini katika mazingira ya Kirumi.

#### **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Paulo hata alithibutu kujitetea mwenyewe mbele ya umati huu wenye ghasia?
2. Kwanini Luka anaaandika zaidi ya mara tatu ushuhuda wa Paulo wa kuongoka kwake yeye mwenyewe akiwa njiani kuelekea Dameski?
3. Ni kwa namna gani matumizi ya Anania kwa Roho kunapinga mwendelezo wa tume?
4. Orodhesha maono ya Paulo. Kwanini alihitaji aina hii ya kukutana kwa kiungu?
5. Ni kwa namna gani matokeo ya kujitete kwa Paulo mbele ya makundi yenye ghasia katika hekalu yanashabihiana vipi na mpango wa Mungu?

## MATENDO YA MITUME 23

<b>MGAWANYO WA AYA ZA TAFSRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Paulo akiwa mbele ya Baraza	Wakuu wa Sinagogi Wadawanyika	Paulo akiwa mbele ya Wakuu wa Sinagogi	Paulo akiwa mbele ya Baraza	Kuonekana mbele ya Wakuu wa Sinagogi
22:30-23:5	22:30-23:10	(22:30-23:10 22:30-23:5	(22:30-23:11)  23:1-3 23:4 23:5 23:6	(22:30-23:11)  23:1-5  23:6-10
23:6-10	Njama Dhidi ya Paulo	23:6-10 Paulo Anatumwa Kaizaria	23:6 23:7-9 23:10	23:6-11
23:11	23:11-22	23:11	23:11	23:11
Njama Dhidi ya Maisha ya Paulo			Njama Dhidi ya Maisha ya Paulo	Mpango wa Siri wa Wayahudi Dhidi ya Paulo
23:12-22		23:12-15 23:16-22	23:12-15 23:16-18 23:19 23:20-21 23:22	23:12-15 23:16-22
Paulo Anatumwa kwa Feliki Liwali	Anatumwa kwa Feliki		Paulo Anatumwa kwa Liwali Feliki	Paulo Anasafirishwa hadi Kaizaria
23:23-30	23:23-35	23:23-25 23:26-30	23:23-25 23:26-30	23:23-25 23:26-30
23:31-35		23:31-35	23:31-35	23:31-35

### **KUSOMA MZUNGUKO WA TATU (kutoka “[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)”)**

#### ***KUFUATIA KUSUDI ASILIA LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kil mmoja wetu sharti atembeee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia n aRoho Mtakatifu ni vipaumbele

atika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsir tan hapo juu.

Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya inasomo moja tu.

1. Ayaya kwanza
2. Ayayapili
3. Ayatatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA KUSOMA

### ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 23:15

<sup>1</sup>Paulo BB V watu wa baraza, akasema, Ndugu zangu, mimi kwa dhamiri safi kabisa nimeishi mbele za Mungu hata leo hivi. <sup>2</sup>Kuhani Mkuu Anania akawaamuru wale waliosimama karibu naye wampige kinywa chake. <sup>3</sup>Ndipo Paulo akamwambia, Mungu atakupiga wewe, ukuta uliopakwa chokaa. Wewe umeketi kunihukumu sawasawa na sheria, nawe unaamuru nipigwe kinyume cha sheria? <sup>4</sup>Wale waliosimama karibu wakasema, Je! Unamtukana Kuhani Mkuu wa Mungu? <sup>5</sup>Paulo akasema, Sikujua, ndugu zangu, ya kuwa yeye ni Kuhani Mkuu; maana imeandikwa, Usimnene mabaya mkuu wa watu wako.

23:1

NASB, NRSV "akawakazia macho"

NKJV "akawatazama kwa makini"

TEV "akawakadolea macho"

NJB "akawatazama kwa upole"

Tazama maelezo katika Matendo ya Mitume 1:10. Luka analitumia neno hili mara nyingi. Hapa analitumia kumhusu Paulo. Paulo analitumia katika 2 Kor.3:7,13 pekee..

▣ "baraza" Tazama Mada Maalum: Wakuu wa Sinagogi katika Matendo ya Mitume 4:5.

▣ "Ndugu" Paulo anawaita Wayahudi "ndugu" mara kadhaa (Matendo ya Mitume 13:26,38; 22:1,5; 23:1,5,6). Wayahudi wanamuita Paulo ndugu katika Matendo ya Mitume 13:15. Anania anamuita ndugu katika Matendo ya Mitume 9:17, kama linavyofanya kanisa huko Yerusalem katika Matendo ya Mitume 21:20. Hata hivyo, wayahudi wa Kiyahudi pia wanaitwa kwa jina hili (mf. Matendo ya Mitume 9:30; 10:23; 11:1,12; 12:17; 15:3,7,13,22). Hili neno linaunganishwa na "mwanafunzi" katika Matendo ya Mitume 11:29; 18:27. Pia hili linatumika kwa waamini wa Kiyunani katika Matendo ya Mitume 16:2,40. Hivyo neno hili lina utata na lazima liunganishwe na andiko na kundi maalum.

▣ "nimeishi . . . mbele za Mungu" Hii ni kauli elekezi (yenye ushahidi) ya wakati timilifu wa nenopoliteuō ambapo tunalipata neno la Kiingereza lenye maana ya siasa au sera. Neno hili lilitumika kwa maana nyingine ya raia (kama vile Flp.1:27). Paulo anaeleza kwamba kwa imani ametimiza majukumu ya kuwa mmoja wa Dini ya Kiyahudi mbele za Mungu.

NASB "kwa dhamiri safi kabisa"

NKJV "katika dhamira yote iliyo safi"

NRSSV "dhamira safi"

TEV "dhamira yangu kwa safi kwa ukamilifu"

NJB "kwa ukamilifu ni dhamira safi"

Paulo analitumia neno "dhamiri" mara kwa mara katika barua za Wakolintho (kama vile Matendo ya Mitume 4:4; 8:7,10,12; 10:25,27,28,29; 2Kor. 1:12; 4:2; 5:11). Hili linarejelea ile maana ya ndani ya kimaadili ya kile kinachokubaliwa au kisichokubaliwa (kama vile Matendo ya Mitume 23:1). Dhamira inaweza kuathiriwa na maisha ya wakati uliopita, chaguzi zetu zilizo duni, au kupitia Roho wa Mungu. Si mwongozo wenye dosari, bali hutambulisha mipaka binafsi ya imani. Kwa hiyo, kuzichafua dhamiri yetu, hata kama i katika uharibifu au udhaifu, ni tatizo kubwa la kimani.

Dhamira ya muumini inahitaji kuumbwa na neno la Mungu zaidi na zaidi na Roho wa Mungu (kama vile 1 Tim. 3:9). Mungu atawahukumu waamini (yaani, walio wanyonge au wenye nguvu, kama vile Rum. 14:1-15:13) kwa nuru walionao, lakini sisi sote yatupasa kuwa wazi kwa ajili ya Biblia na Roho kwa nuru zaidi na kukua katika maarifa ya Bwana Yesu Kristo.

▣ **"mbele za Mungu hata leo hivi"** Paulo analiumba dai hilihili katika 2 Kor. 1:12; 2 Tim. 1:3. Yeye anakiri kuwa anapigana vita (kama vile Rum. 7:23, hasa Matendo ya Mitume 23:7). Hoja zake za kithiolojia katika Warumi 1-8 zinajikita katika vita ya sheria ya kila mtu na dhamiri (kama vile Matendo ya Mitume 3:9-23; 4:15; 5:20).

**23:2 "Kuhani Mkuu Anania"** Katika Kiebrania jina lake lingepaswa kuwa Hanania. Hili si sawa na Anania wa Luka 3:2, Yohana 18:13, au Matendo ya Mitumes 4:6, bali mwingine (Anania, mwana wa Nebedaeus au Nedebacus) ambaye aliteuliwa na Herode Chalcis, ambaye alitawala kuanzia 48-59 b.k (Josephus, *Antiq.* 20.9.2). Maandiko ya Josephus yanatwambia mengi kuhusu huyu Kuhani Mkuu.

1. alipokuwa Kuhani Mkuu, *Antiq.* 20.5.2; *Wars*, 2.12.6.
2. alipokuwa yeye na mtoto wake (Ananus) walipopelekwa utumwani huko Roma, *Antiq.* 20.6.2
3. alipouawa na waandamanaji karibia na ndugu yake, *Wars* 2.17.9 Josephus ndiye mara zote chanzo hai cha kale cha matukio ya Kiyahudi na watu walioko Palestina.

▣ **"wampige kinywa chake"** Hii ilikuwa alama ya makufuru (kama vile Yohana 18:22).

**23:3 "Mungu atakupiga wewe"** Hili limenukuliwa katika kwa maelezo ya undani katika Josephus, *Wars* 2.17.9.

▣ **"ukuta uliopakwa chokaa"** Haikujulikana ni nini hasa alichokuwa akikinena Paulo.

Wayahudi wanaitumia stia hii kumaanisha unafiki (kama vile Mt. 23:27)

hili linaweza kuwa dokezo la Eze. 13:10-15

▣ **"kinyume cha sheria"** Hili linaweza kuwa dokezo la Law. 19:15. Pia tazama Yohana 7:51.

**23:5 "Sikujua, ndugu zangu, ya kuwa yeye ni Kuhani Mkuu"** Nadaharia za Paulo kutojua si kutokana na

1. udhaifu wake wa kutokuona
2. kutokumjua kwa sababu Paulo alikuwa amekwenda Yerusalemu kwa miaka kadhaa
3. kutomtambua Kuhani Mkuu kwa sababu ykutokuvaa vazi lake rasmi
4. hakujua nani aliyekuwa akizungumza
5. kukosa ukubalifu wa matendo yake yaani, kejeli)

▣ **"maana imeandikwa"** Paulo alionyesha kuifahamu na kuiheshimu Sheria kwa kuinukuu Kut. 22:28.

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME :23:6-10**

<sup>6</sup>Paulo alipotambua ya kuwa sehemu moja ni Masadukayo, na sehemu ya pili ni Mafarisayo, akapaza sauti yake katika ile baraza, Ndugu zangu, mimi ni Farisayo mwana wa Farisayo; mimi ninahukumiwa kwa ajili ya tumaini la ufufuo wa wafu. <sup>7</sup>Alipokwisha kunena hayo palikuwa na mashindano baina ya Mafarisayo na Masadukayo, mkutano ukafarakana. <sup>8</sup>Kwa maana Masadukayo husema ya kwamba hakuna kiyama wala malaika wala roho; bali Mafarisayo hukiri yote. <sup>9</sup>Pakawa na makelele mengi. Waandishi wengine wa upande wa Mafarisayo

wakasimama, wakateta, wakisema, Hatuoni uovu wo wote katika mtu huyu; bali ikiwa roho au malaika amesema naye, ni nini? <sup>10</sup>Ugomvi mkubwa ulipotokea, yule jemadari akachelea Paulo asije akararuliwa nao, akaamuru askari washuke na kumwondoa kwa nguvu mikononi mwao, na kumleta ndani ya ngome.

**23:6 "alipotambua"** Paulo anaweza kuwa alitambua ya kuwa hakisikia kwa usahihi kutoka kwa kuhani mkuu wa ki-Sadukayo.

▣ **"Masadukayo"** Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 4:1.

▣ **"Mafarisayo"** Paulo alikuwa Mfarisayo (kama vile Matendo ya Mitume 26:5; Flpl. 3:5-6) kutoka familia ya Mafarisayo. Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 5:34.

▣ **"mimi ninahukumiwa kwa ajili ya tumaini la ufufuo wa wafu"** Paulo alilitupilia mbali lile suala la kitheolojia ambalo Mafarisayo na Masadukayo walikuwa wakilipinga. Masadukayo hawakukubali juu ya kuwepo maisha baada ya kifo, ambapo Mafarisayo walikuwa wakilikiri (kama vile Ayubu 14:14; 19:23-27; Isa. 25:8; 26:19; Dan. 12:2). Hili lilisababisha kuwepo kwa makundi mawili ya baraza yaliyokuwa yakipingana (kama vile Matendo ya Mitume 23:7-10).

**23:7 "mkutano ukafarakana"** Maanaya msingi ya neno hili ni "kuwa na woga" (kama vile Luka 5:36; 23:45). Hili lilikuja kutumika kistiari kumaanisha mafarakano ndani ya makundi (kama vile Matendo ya Mitume 14:4; 23:7). Mafarakano kati ya madhehebu haya mawili ya Kiyahudi mara nyingi yalikuwa ya wazi. Paulo alitengeneza sura za mafundisho yen yekuvutia.

**23:8 "hakuna kiyama wala malaika"** Mstari wa 8 ni maoni ya Luka yatokanayo na chimbuko lake. Je! Kifungu hiki kinamaanisha kuwa kuna vipengele viwili vya viumbe viwili vya kiroho au kimoja? Chimbuko la vyote kibiblia ni la kiutata, lakini Ebr.1:5,13, na 14 zinamaanisha kwamba hivi ni vyote ni sawa. Kile walichokikataa Masadukayo kilikuwa ni ule uwili wa viumbe vya kiroho vya mema na mabaya (Zoroastrian dualism). Mafarisayo wameieleza kwa undani dhana ya Agano la Kale katika ugumu wa uwili wa Kiajemi na hata kuiendeleza kwa mtiririko wa kimalaika na kimapepo (viongozi kadhaa wa kila kundi). Chanzo bora nilichokipata kuhusu karne ya kwanza ya ni Alfred Edersheim, *The Life and Times of Jesus the Messiah*, Kiambata XIII.

**23:9**

**NASB** "Pakawa na makelele mengi"

**NKJV** "kukatokea mmayowe mengi"

**NRSV** "kisha kukazuka mayowe"

**NJB** "makelele yakazidi kuwa mengi"

Kifungu hiki hiki kinapatikana katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani ya Kut.12:30 pia nukuu Kut. 3:7; 11:6; Esth. 4:3; Isa.58:4; 65:19). Hili neno "makelele" (*kraugē*) pia katika Mt. 25:6; Luka 1:42; Efe. 4:31; Ebr. 5:7; Ufu. 21:4. Andiko pekee ndilo liwezalo kubainisha aina ya mayowe "makelele" (yaani, yaliyo chanya au hasi).

Neno lingine linaloonyesha hisia za ndani "kuteta" (*diamachomai*) ambalo pia linatumika katika maandiko ya kale ya Kiyunani LXX katika Dan. 10:20. Maoni ya Paulo yalisababisha makelele, hisa za ghadhabu, ambazo hasa hasa ndizol tulizozihitaji!



▣"waandishi" Hawa walikuwa wataalamu wa kisheria katika vyote mazungumzo (Buku la sheria za Kiyahudi) na sheria iliyoandikwa (Agano la Kale).Wengi wao walikuwa Mafarisayo.

## **MADA MAALUM: WATAKATIFU (*hagios*)**

Huu ni usawa wa Kiyunani wa neno la Kiebrania *kadosh* (NOUN, BDB 871; VERB, BDB 872, KB 1066-1067; tazama Mada Maalum: Takatifu), lililo na maana ya msingi ya kumweka mtu katia usawa, kitu fulani, au baadhi ya sehemu tofauti na matumizi ya YHWH yaliyojitenga. Hili linadokeza dhana ya Kiingereza ya "wekwa wakfu." Israeli lilikuwa "taifa takatifu" la YHWH (kama vile 1 Pet. 2:9, ambayo inanukuu Kut. 19:6). YHWH anaweka mbali na ubinadamu kwa kutumia asili Yake (milele, Utakatifu usiombwa) na sifa Yake (ukamilifu wa maadili). Yeye ni kipimo ambapo vitu vyote vinapimwa na kuhukumiwa. Yeye yu kila mahali, Mtakatifu, Mtakatifu wa Watakatifu.

Mungu aliwaumba wanadamu kwa ushirika, lakini anguko (Mwanzo 3) lilisababisha kikwazo cha mahusiano na maadili kati ya Mungu Mtakatifu na mwanadamu mdhambi. Mungu alichagua kuurejesha ufahamu Wake wa uumbaji; hivyo, Anawaita watu Wake kuwa "watakatifu" (kama vile Law. 11:44; 19:2; 20:7,26; 21:8). Kwa imani uhusiano wa YHWH na watu Wake ukawa mtakatifu kwa nafasi zao za kiagano ndani Yake, lakini pia wanaitwa kuishi maisha matakatifu (tazama Mada Maalum: Utakaso, kama vile Mt. 5:48; Efe. 4:1,17; 5:2-3,15; 1 Pet. 1:15).

Huku kuishi kitakatifu kunawezekana kwa sababu waamini wamekubaliwa kwa utimilifu na kusamehewa kupitia (1) Maisha ya Yesu na (2) kazi na uwepo wa Roho Mtakatifu ndani ya fikra na mioyo yao. Hili linahimarisha hali ya ukinzani kwa waamini:

1. kuwa watakatifu kwa sababu ya haki ya Kristo iliyowekwa ndani yao (kama vile Warumi 4)
2. walioitwa kuishi kitakatifu kwa sababu ya uwepo wa Roho (tazama Mada Maalum: Utakaso)

Waamini ni "watakatifu" (*hagioi*) kwa sababu ya

3. mapenzi ya yule Aliye Mtakatifu (Baba, kama vile Yohana 6:29,40; 1 Pet. 1:15-16)
4. kazi ya Mwana aliye Mtakatifu (Yesu, kama vile 2 Kor. 5:21; 1 Pet. 1:18-21)

uwepo wa Roho Mtakatifu akaaye ndani (kama vile Rum. 8:9-11,27)

Mara nyingi katabu cha Agano Jipya kinawarejelea watakatifu kama WINGI (isipokuwa mara moja katika Flp. 4:21, lajkini muktadha unalifanya neno hili kuwa WINGI). Kuokolewa ni kuwa sehemu ya familia, mwili, ujenzi! Imani ya kibiblia huanza na mapokezi binafsi, bali suala li ndani ya ushirika wa pamoja. Kila mmoja wetu amekirimiwa kama vile 1 Kor. 12:11) kwa ajili ya afaya, ukuaji, na manufaa ya Mwili wa Kristo—kanisa (kama vile 1 Kor. 12:7). Tumeokolewa ili kutumika! Utakatifu ni sifa ya familia!

Hili linakuwa adimu kwa waamini (kama vile Matendo ya Mitume 9:13,32,41; 26:10; Rum. 1:7; 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Efe. 1:1; Flp. 1:1; Kol. 1:2) na njia ya kuonyesha huduma kwa wengine (kama vile Rum. 12:13; 16:2; Efe. 1:15; Kol. 1:4; 1 Tim. 5:10; Ebr. 6:10). Paulo alichukua wakati wa kipekee wa kujitoa kwa makanisa Mataifa kwa watu wahitaji waliokuwa ndani ya Kanisa Mama ndani ya Yerusalemu (kama vile Rum. 15:25-26; 1 Kor. 16:1; 2 Kor. 8:4; 9:1).

▣"mtu huyu" Matumizi ya hiki kifungu nomino katika muktadha huu yanaonyesha kwamba hiki si kifungu kanushi moja kwa moja.

▣ **"ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti dalaja la kwanza partialau isiyotimilifu. Hawa waandishi walidai kuwa Paulo alikuwa na jambo fulani kutoka katika ulimwengu wa kiroho, lakini kwa hakika hawakuwa sawa. Uharaka wao kutumia nguvu juu ya Paulo kulionyesha namna walivyokuwa kinyume kwa kundi lao wenyewe. Kwa uhakika kabisa hawakuwataka Masadukayo zaidi ya kuwasaliti Mafarisayo. Kwa kuwa huu ni muundo wa kisarufi usio timilifu, upokeaji wa maandiko, ukifuatiwa na machapisho ya Kiyunani ya herufi kubwa H, L, na P, na linaongeza, kifungu "na tusipambane dhidi ya Mungu," ambachokinachukuliwa kutoka Matendo ya Mitume 5:39.

**23:10 "akaamuru askari washuke na kumwondoa kwa nguvu"** Selikali ya Kirumi imeyaokoa maisha ya Paulo kwa mara ya pili sasa. Paulo hakuona mshangao kwa serikali kama ni yenye kumtumika Mungu (kama vile Warumi 13). Hili linaweza kuhusiana na "yule azuiaye" katika 2 The. 2:6-7.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 23:11**

<sup>11</sup>**Usiku ule Bwana akasimama karibu naye, akasema, Uwe na moyo mkuu; kwa sababu, kama ulivyonishuhudia habari zangu Yerusalemu, imekupasa kunishuhudia vivyo hivyo Rumi nako.**

**23:11 "Bwana akasimama karibu naye"** Hapa kuna maono binafsi ya kumtia moyo Paulo (kama vile Matendo ya Mitume 18:9-10; 22:17-19; 27:23-24). Paulo hakuwa mtu bila kuwepo hali ya kukatishwa tama na mashaka.

▣ **"Uwe na moyo mkuu"** Hii ni kauli tendaji yenye masharti ya wakati uliopo. Haya ndiyo matumizi pekee ya neno hili katika maandiko ya Luka. Lazima Paulo atakuwa alishiriki hili pamoja na Luka. Yesu analitumia neno hili mara kadhaa (kama vile Mt. 9:2,22; 14:27; Yohana 16:33).

▣ **"imekupasa kunishuhudia vivyo hivyo Rumi nako"** Haya yaklikuwa mapenzi ya Mungu kwa Paulo kutiwa gerezani kwamba angeonekana kwa mbele ya Kaizari. Injili itahubiriwa katika Rumikama vile Matendo ya Mitume 19:21; 22:21)! Hivyo "yakupasa" tazama maelezo kamili katika Matendo ya Mitume 1:16.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) :MATENDO YA MITUME 12-15**

<sup>12</sup>**Kulipopambauka, Wayahudi wakafanya mapatano, wakajifunga kwa kiapo kwamba hawatakula wala hawatakunywa hata wamwue Paulo.** <sup>13</sup>**Na hao walioapiana hivyo walipata zaidi ya watu arobaini.** <sup>14</sup>**Nao wakaenda kwa wakuu wa makuhani na wazee, wakasema, Tumejifunga kwa kiapo tusionje kitu hata tumwue Paulo.** <sup>15</sup>**Basi sasa ninyi pamoja na wazee wa baraza mwambieni jemadari amlete chini kwenu, kana kwamba mnataka kujua habari zake vizuri zaidi; na sisi tu tayari kumwua kabla hajakaribia.**

**23:12-15** Aya hii inatuharifu juu ya mpango wa mauaji wa baadhi ya Wayahudi. Haya ni makusudi mengine ya mauaji (kama vile Matendo ya Mitume 23:21) kama wale Wayahudi waliofanya mpango wa mauaji kumhusu Yesu.

**23:13 "aidi ya watu arobaini"** Arobaini ni nahau ya Kiyahudi iliyomaanisha umbali, kipindi cha wakati kisichokuwa na mwisho, lakini hapa kinatumika kwa watu, hivyo bila shaka ni sahihi. Tazama Mada Maalum: Hesabu katika Maandiko katika Matendo ya Mitume 1:3.

**23:14 "wakuu wa makuhani na wazee"** Hii ni njia iliyofupishwa ya kuwarejelea Wakuu wa Masinagogi. Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 4:5.

**NASB "Tumejifunga kwa kiapo"**

**NKJV "tumejiwekea mipaka kwakiapo kukuu"**

**NRSV "tumejifunga wenywe kwa kiapo kikali"**

**TEV "tumehadi kwa ahadi kali"**

**NJB "tehaidi kwa ahadi kali"**

Hizi tafasiri za Kiingereza ni zinajaribu kutafsiri kifungu cha nahau ya kiutambuzi, "Tumejifunga kwa kiapo" Wale waliokula kiapo hawakumuua Paulo. Nashangaa ikiwa walikikosa kifo? Kwa uwazi masimulizi yaliruhusu njia ya viapo hivi vya damu. Tazama Mada Maalum ifuatayo.

## **MADA MAALUM: LAANA (ANATHEMA)**

### **I. AGALA KALE**

Kuna maneno kadhaa katika Kiebrania yenye kuzungumzia neno "laana." Neno *Herem* (BDB 356, KB 353) lilitumika kumaanisha jambo fulani lilitolewa kwa Mungu (kama vile Agano la kale la Kiebrania - LXX linalitafsiri neno hili kama *anathema*, BAGD 54, Lev. 27:28). Mara nyingi neno hili limehusishwa katika uharibifu wa vitu kwa sababu lilikuwa takatifu sana kwa matumizi ya mwanadamu (kama vile Kumb. 7:26; Yos. 6:17-18; 17:12). Hili lilikuwa neno lililotumika katika dhana ya "vita takatifu." Mungu alimwambia Yoshua kuwaaharibu Wakanaani. Yeriko ilikuwa nafasi ya kwanza, "matunda ya kwanza" ya uharibifu huu mtakatifu/ utakaso.

### **II. AGANO JIPYA**

Katika Agano Jipya neno *anathema* na miundo yake inayohusiana ilitumika katika maana kadhaa na tofauti:

- A. kama uzuri au sadaka kwa Mungu (kama vile Lukea 21:5)
- B. kama kiapo cha kifo (kama vile Matendo ya Mitume 23:14)
- C. kulaani na kuapa (kama vile Marko 14:71)
- D. Kanuni ya laana iliyohusiana na Yesu (kama vile 1 Kor. 12:3)
- E. Mungu kumtia mtu au kitu fulani katika hukumu au uharibifu (kama vile Rum. 9:3; 1 Kor. 16:22; Gal. 1:8-9)

Namba D hapo juu inakanganya sana. Nimehusisha maelezo yangu kutoka 1 Kor. 12:3:

"Yesu amelaaniwa" ni usemi unaleta mshtuko. Kwa nini mtu ye yote (isipokuwa mapokeo ya Kiyahudi) adai azungumzie Mungu kuwa alinene hili? Hili neno (yaani, *anathema*) lenyewe lilikuwa na maelezo ya nyuma ya Agano la Kale (yaani, Kiebrania, herem). Hili lilihusiana na dhana ya Vita Takatifu, ambapo mji ulitengwa kwa ajili ya Mungu na, hivyo, ilikuwa mtakatifu. Hili lilimaanisha kwamba kila kitu kina pumzi ndani yake, mwanadamu au mnyama, yampasa kufa (kama vile Yos. 6:17; 7:12). Nadharia zinazohusu namana neno hili lilivyotumia katika Wakorintho ni:

1. kwamba hili lina muundo wa Kiyahudi uliohusu viapo vya sinagogi (kama vile Matendo ya Mitume 26:11, yaani, baadaye, kanuni za laana ya kisheria zilitumika kuwaondoa Wakristo katika sinagogi). Kubaki mmojawapo ilimpasa mtu kumkataa au kumlaani Yesu wa Nazarethi.
2. kwamba hili lina muundo wa Kirumi unaohusiana na kumwabudu Mfalme ambapo Kaizari pekee

ndiye angeitwa "Bwana"

3. kwamba hili lina muundo wa ibada ya kipani ambapo laana zilitamkwa juu ya watu kwa kuliitia jina la mungu. Hili pia linaweza kutafsiriwa, "Yesu Anaweza kulaani —" (kama vile 1 Kor. 16:22).
4. kwamba alihusianisha kifungu hiki na dhana ya Yesu kitheolojia ya tabia za laana za Agano la Kale kwetu sisi (kama vile Kumb. 21:23; Gal. 3:13).
5. Mafunzo ya sasa kutoka Korintho (kama viletambihi #1 uk. 164 katika Bruce Winter's *After Paul Left Corinth*) inanukuu marekebisho neno laana linalopatikana katika makumbusho a zaamani huko Korintho. Wasomi wa ki-Biblia wamekuwa wakidhani kwamba KITENZI unganishi "ni" lazima kiwekwe ndani ya kifungu, "Yesu anashtakiwa," lakini ushahidi huu wa elimu kale kwa usahihi kabisa unaonyesha kwamba laana hizi za kipindi cha karne ya kwanza ya Kirumi kutoka Korintho zinapungukiwa KITENZI (kama zilivyo baadhi ya laana katika Agano la Kale la Kiebrania- LXX la Kumb. 22:15-20), kama ifanyavyo 1 Kor. 12:3. Kuna ushahidi mwingine zaidi wa elimu kale kwamba Wakristo wa karne ya kwanza ya Korintho ya Kirumi walitumia kanuni za laana katika utaratibu wa mazishi (yaani, kipindi cha Byzantine, unaopatikana katika makaburi ya ki-Kristo (J. H. Kent, *The Inscriptions*, 1926-50. Princeton: American School of Classical Studies, 1966, juzuu. 8:3, na. 644).

Sehemu zingine za kanisa la huko Korintho zilikuwa zikirejea kwa laana za kipagani kwa jina la Yesu dhidi ya washirika wengine wa kanisa. Hii si njia pekee ya tatizo, bali pia sababu ya chukizo. Huu ni mfano mwingine wa mvutano ndani ya kanisa hili. Paulo aliwataka kujenga kanisa, kuliadilisha kanisa; hawa walitaka kuilaani sehemu ya kanisa!

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 23:16-25**

<sup>16</sup>Mjomba wake Paulo akasikia habari za kuotea kwao, akaenda akaingia ndani ya ngome akampasha Paulo habari. <sup>17</sup>Paulo akamwita akida mmoja, akasema, Mchukue kijana huyu kwa jemadari; maana ana neno la kumwarifu. <sup>18</sup>Basi akamchukua, akampeleka kwa jemadari, akamwambia, Paulo, yule mfungwa, aliniita akataka nikuletee kijana huyu kwa kuwa ana neno la kukuambia. <sup>19</sup>Yule jemadari akamshika mkono akajitenga pamoja naye kando, akamwuliza kwa faragha, Una neno gani utakalo kuniarifu? <sup>20</sup>Akasema Wayahudi wamepatana kukuomba umlete Paulo chini kesho, ukamweke mbele ya baraza, kana kwamba wanataka kupata habari zake kwa usahihi zaidi. <sup>21</sup>Basi wewe usikubali; kwa maana watu zaidi ya arobaini wanamwotea, wamejifunga kwa kiapo wasile wala wasinywe hata watakapomwua; nao sasa wako tayari, wakiitazamia ahadi kwako. <sup>22</sup>Basi yule jemadari akamwacha kijana aende zake, akimwagiza, Usimwambie mtu awaye yote ya kwamba umeniarifu haya. <sup>23</sup>Akawaita maakida wawili, akasema, Wekeni tayari askari mia mbili kwenda Kaisaria, na askari wapanda farasi sabini, na wenye mikuki mia mbili, kwa saa tatu ya usiku. <sup>24</sup>Akawaambia kuweka wanyama tayari wampandishe Paulo, na kumchukua salama kwa Feliki liwali. <sup>25</sup>Akaandika barua, kwa namna hii,

**23:16**"Mjomba wake Paulo" Tunayo maswali mengi kuhusu familia ya Paulo, lakini hili limewekwa sirini. Ni kwa namna gani aliufahamu mpango huu pia haijulini. Huenda huyu pia alikuwa Mfarisayo.

**23:21** Shambulio hili pia lingehusisha mauaji ya walinzi wa kirumi!

**23:23** Majeshi ya kubahatisha yaliyomsindikiza Paulo hakika yalikuwa (1) wapiga upinde 200, wapanda farasi 70, na askari 200 au (2) askari wa farasi 200 nawapiga upinde 70. Familia ya magharibi ya machapisho ya Kiyunani ina yongeza ya maelezo marefu (kama vile NKJV).

▣"saa tatu" Huu ni muda wa kawaida wa Kirumi.Walianza kuuhesabu usiku mnamo saa 12 jioni.Hii ingeweza kuwa saa tatu 3 usiku.

▣"Kaizaria" Haya yalikuwa makao makuu ya utawala wa Kiriumi katika Palestina.

**NASB, NKJV**

**NRSV, TEV** "askari wa mikuki"

**NJB** "wasaidizi"

**REB** "majeshi ya upande wa kulia"

**NASB**

**(tanbihi)** "wapanda milima wa ziada" au "wanyama wa kusindkwa"

**NEB** "wapiga upinde"

Maana ya *nenodexiolaboshajulikani*.Kiuhalisia "aliyetumwa au sehemu sahihi" (*dexios*).Hili linarejelea juu ya

1. baadhi ya askari wenye ujuzi (wapiga upinde au mkuki)
2. yule aliyekuwa ameshikilia farasi wa pili
3. yule aliyekuwa mpakani

Hivyo chaguzi nyingi zinaonyesha kwamba hawa wa sasa hawajui maana kamili.

**23:24"Feliki"** Mwana historia wa Kirumi Tacitus (*Histories* 5:9, *Annals* 12:54) anamuita Antonius Felix mkatili na asiye mwenye tamaa. Huyu aliipata nafasi yake kupitia ndugu yake, Pala (wote waliwekwa huru kutoka utumwani), ambaye alikuwa rafiki wa karibu wa Mfalme Claudius. Huyu alitumika kama wakili wa Palestina kutoka 52-59 b.k.

**23:25 "namna"** Tazama Mada Maalum: Namna (*tupos*) katika Matendo ya Mitume 7:43.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 23:26-30**

<sup>26</sup>Klaudio Lisia kwa liwali mtukufu Feliki, Salamu! <sup>27</sup>Mtu huyu alikamatwa na Wayahudi, wakawa karibu kumwua, ndipo nikaenda pamoja na kikosi cha askari nikamwoko, nilipopata habari ya kuwa yeye ni Mrumi. <sup>28</sup>Nami nikitaka kulijua lile neno walilomshitakia, nikamtelemsha nikamweka mbele ya baraza; <sup>29</sup>nikaona kwamba ameshitakiwa kwa ajili ya maswali ya sheria yao, wala hakushitakiwa neno lo lote la kustahili kuuawa wala kufungwa. <sup>30</sup>Hata nilipopewa habari kwamba patakuwa na vitimvi juu ya mtu huyu, mara nikampeleka kwako, nikawaagiza na wale waliomshitaki, wanene habari zake mbele yako. Wasalamu.

**23:26-30** Hii ni barua iliyohitajika kwa mwendesha mashtaka kuhusu maelezo ya kesi ya Paulo (kama vile Matendo ya Mitume 25:12 na kuendelea). Hii iknaeleza mtiririko wa matukio, lakini inakuwa katika namna hiyo kama Lysias anavyoonekana mwema.

**23:26** Huu ni mstari ambao unatwambia jina la Chiliarch.

**23:29** Mstari huu unaendana na mtiririko wa Luka unaoonyesha Ukristo na viongozi wake, wakati walipokamatwa mbele ya maafisa wa kiserikali, mara nyingi walikutwa bila hatia na kufikiriwa kama watu sahihi. Rumi haikuogopa cho chote "Njia"!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 23:31-35**

<sup>31</sup>Basi, wale askari wakamchukua Paulo kama walivyoamriwa, wakampeleka hata Antipatri usiku; <sup>32</sup>hata asubuhi wakawaacha wale wapanda farasi waende pamoja naye, nao wakarudi zao ngomeni. <sup>33</sup>Na wale walipofika Kaisaria, na kumpa liwali ile barua, wakamweka Paulo mbele yake. <sup>34</sup>Naye alipokwisha kuisoma, akawauliza, Mtu huyu ni wa jimbo gani? Alipoarifiwa ya kuwa ni mtu wa Kilikia, <sup>35</sup>akasema, Nitakusikia wewe watakapokuja wale waliokushitaki; akaamuru alindwe katika nyumba ya uliwali ya Herode.

**23:31 "wakampeleka hata Antipatri usiku"** Mji huu ulijengwa na Herode Mkuu na kuuita jina la baba yake, Antipata II. Hili lilichukua muda upatao maili 30-40. Sehemu sahihi ya mji haijulikani. Sababu iliyowafanya askari waendao kwa miguu kurudi (kama vile Matendo ya Mitume 23:32) katika eneo hili ni

1. hili lilikuwa eneo la mwanzo la Mataifa
2. mandhari ya nchi ilikuwa wazi na tambarare, hivyo kulikuwa na hatari kidogo ya mashambulizi ya ghafla

**23:33 "liwali "Kiuhalisia huyu ni" wakili."** Lukayuko sahihi sana katika nyadhifa zake na maafisa wa Kirumi.

**23:34 "akawauliza, Mtu huyu ni wa jimbo gani"** Hii ilikuwa ni kwa ajili ya utawala uliyokuwa umehimarishwa. Kwa kuwa Paulo alitoka katika Jimbo la Kifalme la Feliki angejaribu kuishinda kesi hiyo. Kulikuwa na mgawanyiko wa utawala wa aina tatu katika Dora ya Kirumi:

1. ya Kifalme (Kaizari)
2. wa kiseneti
3. wa mahali (kama Maherode)

**23:35 "watakapokuja wale waliokushitaki"** Hawa wangepaswa kuwa wayahudi waliotoka Asia ambao walimshtaki Paulo katika Hekalu kwa ajili ya kuwaleta watu wa Mataifa katika eneo la Kiyahudi lililozuiliwa. Ukweli ni kwamba hawa kutotakiwa kuonekana kuleta matokeo ya mashtaka ya kutawanyika. Lakini, kadri ilivyotokea mara kwa mara, siasa za mahali ziliathiri haki!

▣ **"alindwe katika nyumba ya uliwali ya Herode"** Warumi walikuwa wema kwa Paulo wakati alipokuwa mikononi mwao (kama vile Matendo ya Mitume 24:23). Paulo alizidi kukaa katika nyumba iliyojengwa na Herode Mkuu, ambayo hapo awali ilikuwa ikitumika kwa makazi yake biafsi, lakini sasa ikawa imekuwa makao Makuu ya Kirumi.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wafasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri. Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Linganisha ulinzi wa Paulo na orodhesha mambo ya kawaida.
2. Je! Paulo alijiona kama Myahudi mwnye imani?
3. Je! kuna lo lote tunalolifahamu kumhusu jamaa wengine za Paulo Kutokana na Matendo ya Mitume?

## MATENDO YA MITUME 24

MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA				
UBS <sup>4</sup>	NKJV	NRSV	TEV	NJB
Mashtaka Dhidi ya Paulo	Kushtakiwa Dhidi ya Uchochezi	Paulo Akiwa Mbele ya Feliki	Mashtaka Dhidi ya Paulo	Mashataka Mbele ya Feliki
24:1-9	24:1-9	25:1-2a 24:2b-8 24:9	24:1-2a 24:2b-9	24:1-9
Paulo Akijitetea Mbele ya Feliki	Kujitetea Mbele ya Feliki		Kujitetea kwa Paulo Mbele ya Feliki	
24:10-21	24:10-21	24:10a 24:10b-21 Feliki Achelewesha	24:10a 24:10b-16 24:17-21	24:10a Usemi wa Paulo Mbele ya Liwali wa Kirumi 24:10b-13 24:14-16 24:17-21 Kukamatwa kwa Paulo huko Kaizaria
24:22-23	24:22-27	24:22-23	24:22-23	24:22-23
Paulo Akiwa katika Uangalizi			Paulo Akiwa Mbele ya Feliki na Dursila	
24:24-26		24:24-26	24:24-26	24:24-26
24:27		24:27	24:27	24:27

### KUSOMA MZUNGUKO WA TATU (kutoka "[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)")

#### *KUFUATIA KUSUDI ASILIA LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili

7. Aya tatu
8. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 24:1-2a

<sup>1</sup>Baada ya siku tano, Anania, Kuhani Mkuu, akatelemka na baadhi ya wazee pamoja naye, na msemi mmoja, Tertulo, nao wakamweleza liwali habari za Paulo.

<sup>2</sup>Naye alipoitwa, Tertulo akaanza kumshitaki, akisema

**24:1** "Anania, Kuhani Mkuu" Tazama maelezo kamili katika Matendo ya Mitume 23:2. Vema! Kuhani mkuu alikuja mwenyewe kutoka Yerusalemu hadi Kaisaria. Kwa hakika Paulo alikuwa mwiba katika miili yao!

▣ "akatelemka " Kwa Yesu, Yerusalemu mara nyingi iko "juu" na maeneo mengine yote ya kijiografia yako "chini."

▣ "wazee " Katika Agano la Kale neno hili lilirejea juu ya wale viongozi wazee wa kikabila. Katika kipindi cha kukimbilia Babel. Neno hili lilitumika kumaanisha utajiri, watu wa Yerusalemu walikuwa wa muhimu. Mara nyingi katika Agano Jipya Wakuu wa Sinagogi wanaelezwa kama "Makuhani Wakuu, waandishi, na wazee." Huenda hawa walikuwa mojawapo ya Wakuu wa Sinagogi ambao walikuwa wafuasi wa Mafarisayo. Uongozi wa Hekalu uliona tatizo kubwa pale Mafarisayo walipokuwepo (kama vile Matendo ya Mitume 23:6-10).

▣ "Tertulo" Huyu alikuwa mwanasheria wa kukodiwa (wakili) au mzungumzaji (kama vile NKJV). Huu ni muundo wa neno la Kiyunani *rēma* au "neno lililozungumzwa." Kwa uhakika kabisa huyu aliwakilisha mashtaka ya Wakuu wa Masinagogi katika muundo wa sheria za Kirumi uliokubaliwa, bila shaka katika lugha ya Kilatini.

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 24:2b-9

<sup>2b</sup>Kwa kuwa mnapata amani nyingi chini yako, Feliki mtukufu, na kwa maangalizi yako mambo mabaya yanatengenezwa kwa ajili ya taifa hili, <sup>3</sup> basi tunayapokea kila wakati na kila mahali, kwa shukrani yote.

<sup>4</sup> Lakini nisikuudhi zaidi, nakusihi utusikilize maneno machache kwa fadhili zako. <sup>5</sup> Kwa maana tumemwona mtu huyu mkorofi, mwanzilishi wa fitina katika Wayahudi wote duniani, tena ni kichwa cha madhehebu ya Wanazorayo. <sup>6</sup> Na tena alijaribu kulitia hekalu unajisi; tukamkamata; [tukataka kumhukumu kwa sheria yetu.

<sup>7</sup> Lakini Lisia jemadari akafika akamwondoa mikononi mwetu kwa nguvu, <sup>8</sup> Akawaamuru wale waliomshitaki waje kwako.] Wewe mwenyewe kwa kumwuliza-uliza utaweza kupata habari ya mambo yale yote tunayomshitaki sisi. <sup>9</sup> Wayahudi nao wakamshitaki, wakisema ya kuwa ndivyo yalivyo.

**24:2b-4** Utangulizi huu haukuwa jaribio la kujipendekeza (huenda ulitarajiwa), bali katika maana isiyokuwa na msingi. Feliki alikuwa mtu katili (kama vile Tacitus, *Histories* 5.9 na *Annals* 12.2). Feliki alikuwa katika nafasi yake ya pekee kwa sababu ya ndugu yake, Pala, ambaye, karibu na Feliki, alikuwa huru aliyetoka Antonia (binti yake Marc Antony), Claudius, mama wa Mfalme. Baadaye aliondolewa na Nero kutokanana madai ya watu (kama vile Josephus, *Wars* 2.12.8- 13.7 na *Antiq.* 20.7.7-8.9).

**24:2b** "mnapata amani nyingi" Baadhi wanafikiri kwamba usemi huu unarejelea jaribu lake la kukomesha waandamanaji wa Kiyahudi wenye msimamo mkali walioitwa *sicarii* (watu wenye upanga/wachinjaji). Tazama *Wars* 2.13.2.



**24:5 "tumemwona mtu huyu"** Hili ni kusudi la Luka katika kitabu chote cha Matendo ya Mitume kuuonyesha ulimwengu wote wa Kirumi kwamba mashtaka yaliyouhusu Ukristo ni ya uongo. Ndiyo sababu ya Luka kunukuu uthibitisho mbalimbali mbele ya Mahakama za Kirumi na tawala mbalimbali. Paulo alishtakiwa kwa mambo matatu:

1. mwenye kusababisha fadhaa
2. kuwa kiongizi wa dhehebu jipya
3. mvurugaji wa hekalu

**NASB** " mkorofi"  
**NKJV** "mlaaniwa"  
**NRSV** "mmoja wa wale waliolaaniwa"  
**TEV** "mvurugaji hatarishi"  
**NJB** "msumbufu kamili"

Hili linatokana na neno linalomaanisha tauni (kama vile Luka 21:11). Katika Agano la Kale (LXX) pia neno hili lilikuwana maana ya tauni, lakini kistiari lingeweza kutumika kumaanisha mtu (kama vile Mit. 19:25).

▣ "**wote duniani**" Hakika huu ni usemi uliochochewa kwa makusudi na bado ni ukamilifu wa utendaji mzuri wa huduma ya Paulo katika mataifa mbalimbali waliko Wayahudi.

▣ "**kichwa**" Hili ni neno ambatani la Kiyunani linalotokana na neno "tayari" na "kusimama." Hili lilitumika katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani ya Ayubu 15:24, "mfalme aliye tayari kwa vita." Hili linapatikana hapa tu katika Agano Jipya na si katika mafunjo yote ya lugha ya Koine liyopatikana katika Misri.

▣ "**madhehebu**" Hili neno *haires* lilimaanisha tu "mgawanyiko" au "kundi dogo" (kiuhalisia, "kufanya uchaguzi"). Hili lilikuja kuwa na maana nyingine hasi, kama liwezavyo kuonekana katika neno letu la Kiingereza "apostasy-uasi," ambalo linatokana na neno la Kiyunani. Wakuu wa Sinagogi wanaelezwa kwa neno hili lililo katika Matendo ya Mitume 5:17 na Mafarisayo katika Matendo ya Mitume 15:5. Katika muktadha huu ulio katika Matendo ya Mitume, Paulo anauchukulia Ukristo kama sehemu ya msingi ya historia ya imani ya Kiyahudi na tumaini (kama vile Matendo ya Mitume 24:14).

▣ "**Wanazorayo**" Hili neno linarejea juu ya wafuasi wa Yesu wa Nazarethi. Baadhi wanadia kwamba hili neno linatokana na mji wa Nazarethi lakini wengine wanalihusianisha neno hili na neno *nezer* (BDB 666) au "tawi," wadhifa wa yule Masihi (kama vile Isa. 11:1; 53:2). Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:22.

**24:6** Tambua mashtaka yaliyoundwa dhidi ya Paulo katika Matendo ya Mitume 21:28 ya kwamba alikuwa akilinajisi hekalu, sasa yamebadilika na kuwa "alijaribu kulinajisi hekalu." Hakikia walikuwa na mashtaka duni. Mahubiri ya Paulo yaliyosababisha matokeo mema hakika yalikuwa tatizo kwao.

**24:7** Yale mabano yaliyo katika toleo la NASB yanaonyesha nyongeza ya kimaandiko inayopatikana katika herufi kubwa MS E (karne ya 8) na mengine madogo madogo kadhaa yaliyoanza karne ya 9. Usomaji mrefu unapatikana katika NKJV. Haya yanaonekana kubadilisha kutaka kwake/kwao kwa ajili ya kumjeruhi Paulo kutoka uongozi wa Kiyahudi hadi Lisia. Toleo la UBS<sup>4</sup> linaitenga nyongeza hii na kukadiria toleo fupi sana (MSS P74,  $\aleph$ , A, D, Baadhi ya Matoleo ya kale ya Kilatini, Maandiko ya Kiyunani, Coptic, na matoleo ya Georgia) kama vile alama "B" (ni hakia). Toleo la UBS<sup>3</sup> lilijumuisha usomaji mrefu lakini liliupa daraja "D" (kiwango cha juu cha kushuku).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 24:10-21**

**10**Na liwali alipompungia mkono ili anene, Paulo akajibu, Kwa kuwa ninajua ya kwamba wewe umekuwa mwamuzi wa taifa hili kwa muda wa miaka mingi, najitetea mwenyewe kwa moyo wa furaha. **11**Maana waweza kujua ya kuwa hazijapita siku zaidi ya kumi na mbili tangu nilipopanda kwenda Yerusalemu ili

kuabudu. 12 Watu hawa hawakuniona ndani ya hekalu, nikihojiana na mtu, au kufanya fujo katika mkutano, wala katika masinagogi wala ndani ya mji. 13 Wala hawawezi kuyahakikisha mambo haya wanayonishitaki sasa. 14 Ila neno hili naungama kwako ya kwamba kwa Njia ile ambayo waiita uzushi, ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu, nikiyaamini yote yanayopatana na torati na yaliyoandikwa katika vyyo vya manabii. 15 Nina tumaini kwa Mungu, ambalo hata hao nao wanalitazamia, ya kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia. 16 Nami ninajiozea katika neno hili niwe na dhamiri isiyo na hatia mbele za Mungu na mbele ya watu siku zote. 17 Baada ya miaka mingi nalifika niwalettee watu wa taifa langu sadaka na matoleo. 18 Wakaniona ndani ya hekalu nikishughulika na mambo haya, hali nimetakaswa, wala sikuwa na mkutano wala ghasia; lakini walikuwako baadhi ya Wayahudi waliotoka Asia, 19 ambao imewapasa hao kuwapo hapa mbele yako na kunishitaki, kama wana neno lo lote juu yangu. 20 Au watu hawa wenyewe na waseme, ni kosa gani waliloliona kwangu niliposimama mbele ya baraza, 21 isipokuwa kwa ajili ya sauti hii moja, nilipolia nikisimama katikati yao, na kusema, Kwa ajili ya ufufuo wa wafu ninahukumiwa mbele yenu hivi leo.

**24:10** Kama wanadsheri wa Wakuu wa Sinagogi alitumia utangulizi maalum (huenda alitarajiwa kiutamaduni), vivyo hivyo, ndivyo Paulo alivyofanya.

▣ "**najitetea**" Hapa tunalipata neno la Kiingereza lenye maana ya "radhi" au "watetezi" kutokana na neno hili la Kiyunani. Kiuhalisia hili lilimaanisha utetezi wa sheria ya mazungumzo ndani ya mahakama.

**24:11-12** Paulo anadai kwamba mambo haya yaliyokuwa yakitendka hadharani humo Yerusalemu hayakuwa ya halali na yalikuwa ya fedheha. Huyu alishtakiwa kwa kosa la kulinajisi hekalu, lakini katika hali halisi, alikuwa akikamilishaibu zilizokubaliwa.

**24:14 " Njia ile"** Hili lilikuwa jina la awali kwa Wakristo ambalo lilisistiza kwamba Yesu ni njia iendayo kwa Mungu (Yohana 14:6) na ushirika wa maisha (kama vile Matendo ya Mitume 9:2; 19:9,23; 22:4; 24:22 na huenda 18:25-26).

▣ "**ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu**" Paulo kwa usahihi anadai katika mstari wake kwamba anamhubiri Yesu katika njia isiyoweza kulikiuka Agano la Kale. Yesu ni utimilifu wa matumaini ya Israeli na ahadi. Yeye hauoni Ukristo kama kitu kipya na cha tofauti bali utimilifu (kama vile Yesu katika Mt. 5:17-19).

▣ "**torati. . . manabii**" Hii ni migawanyo miwili miongoni mwa migawanyo mitatu misingi ya Agano la Kale iliyofungamana:

1. Torati (Sheria) — Mwanzo – Kumbukumbu la Torati
2. Manabii
  - a. manabii wa kale — Yoshua - Wafalme (isipokuwa Ruthu)
  - b. manabii waliofuatia — Isaya - Malaki (isipokuwa kitabu cha Maombolezo na Danieli)
3. Maandiko
  - a. Gombo la kitabu— Ruthu, Esta, Mhubiri, Wimbo Ulio Bora, na Maombolezo
  - b. fasihi ya hekima — Ayubu, Zaburi, Mithali
  - c. historia ya kukimbilia Babel— Nyakati I & 2, Ezra, na Nehemia

**24:15 " Nina tumaini kwa Mungu, ambalo hata hao nao wanalitazamia"** Paulo anadai kwamba kubobea kwake katika imani ni sawa na washtaki hawa (kama vile Matendo ya Mitume 24:16), isipokuwa katika mtazamo wake wa ufufuo. Paulo anajaribu kujitetea kwa kuonyesha kwamba mgogoro unahusu jambo la kitheolojia ndani ya Dini ya Kiyahudi, ambayo Rumi haikutaka ihusishwe. Kwa kulijua zaidi neno "tumaini" tazama [MADA MAALUM: TUMAINI](#) katika Matendo ya Mitume 2:25.

▣ **"kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia"** Kifungu hiki kinarejelea juu ya ile theolojia ya Mafarisayo, si si uongozi wa hekalu la Wakuu wa Sinagogi. Josephus, *Antiq.* 18.1.3, pia anadai kwamba baadhi ya Mafarisayo waliukanusha ufufuo wa wasio haki (kwa mtazamo wa sasa uhusuo maangamizi tazama Edward Fudge, *The Fire That Consumes*). Biblia imejaa dhana hii ya ufufuo wa jumla (kama vile Isa. 25:8; Dan. 12:2; Mt. 25:46; Yohana 5:29; Rum. 2:6-11; Ufu. 20:11-15). Paulo aliuona Ukristo kama utimilifu wa asili wa Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-19). Haukuwa jambo jipya!

**24:16 "Nami ninajizoeza katika neno hili niwe na dhamiri isiyo na hatia"** Kifungu hiki hiki ndicho kilichumuudhi sana Kuhani Mkuu katika Matendo ya Mitume 23:1-2. Paulo anakirudia tena kifungu hiki katika kuwepo kwake. Hiki ni sawa na mjadala wake unaohusu juhudi binafsi katika 1 Kor. 9:24-27. Kuvumilia katika kumhubiri Feliki (kama vile Matendo ya Mitume 24:25) halikuwa jambo rahisi la kukamilisha na kulitunza. Uvumilivu ni moja ya matunda ya Roho katika Gal. 5:22 na huenda ni kifuniko cha orodha ya matunda!

**24:17 "nalifika niwaletee watu wa taifa langu sadaka "** Kwa neno "sadaka" tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 3:2. Huenda neno hili likarejelea juu ya makanisa ya Mataifa hadi kanisa lililoko Yerusalemu (kama vile Rum. 15:25-27; 1 Kor. 16:1-4; 2 Wakorintho 8-9). Inashangaza kuwa hili halikutajwa katika Matendo ya Mitume 21:15 na kuendelea. Hii inaweza kuonyesha kwamba hili halikupokelewa vema na watu wote wa kanisa la Yerusalemu (tazama James D. G. Dunn, *Unity and Diversity in the New Testament*). Ubaguzi wa rangi ulikuwa umekwisha kuimarishwa na ilikuwa vigumu kuushughulikia hata kwa waamini.

▣ **" matoleo"** Hili linazungumzia

1. hitimisho la Paulo la ahadi za Mnazarethi lililozuiliwa (kama vile Matendo ya Mitume 21:24)
2. kuomba kwake kwa ajili ya wengine waliozuiliwa kuziona ahadi za Mnazarethi (kama vile Matendo ya Mitume 21:24)

Kwa sababu kifungu hiki kinaonekana kuunganishwa kisarufi "kutoa sadaka," inawezekana kwamba yote mawili yanarejelea juu ya desturi za Kiyahudi, si matoleo yalitotoka makanisani.

**24:18 " Wakaniona ndani ya hekalu nikishughulika na mambo haya, hali nimetakaswa"** Hii hatua ya desturi za Kiyahudi ilikuwa ya uchochezi kwa Yakobo na wazee wa kanisa (kama vile Matendo ya Mitume 21:17-26). Hili lilimaanisha waumini wa sheria za Kiyahudi ndani ya kanisa, lakini katika ukweli, hili liliwaghadhabisha wazungumzaji Wayahudi wa Kiyunani toka Asia.

**24:18-19 " Wayahudi waliotoka Asia, <sup>19</sup> ambao imewapasa hao "** Hii ilikuwa hoja muhimu ya kisheria katika kujitetea kwa Paulo (kama vile Matendo ya Mitume 24:19). Mashuhuda wa macho walioleta mashtaka hawakuwepo! Wale waliomshataki Paulo juu ya kupotosha ulimwengu mzima hawakuwana na uthibitisho wa unaoonekana (kama vile Matendo ya Mitume 24:20)! Asia ndiyo rejeo la kijiografia kwa watu wa Kiyahudi kutoka kusikni hadi Uturuki magharibi, kasha ikaitwa Asia Ndogo.

**24:19b "kama"** Hii ni kauli yenye masharti dalaja la nne, namna ya kueleza umuhimu ambao baadaye unaondolewa kutoka katika uwezekano. A. T. Robertson, *Word Pictures in the New Testament*, uk. 420, anaiita hali mchanganyiko yenye hitimisho lililo katika dalaja la pili (yaani, lakini zisizokuwepo, Matendo ya Mitume 24:19a). Ie *Sarufi* yake (uk. 1022) inaorodhesha sentensi shurutishi zingine lilizo katika mchanganyiko katika maandiko ya Luka (kama vile Luka 17:6 na Matendo ya Mitume 8:31).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME : 24:22-23**

<sup>22</sup> Basi Feliki aliwaahirisha, kwa sababu alijua habari za Njia ile kwa usahihi zaidi, akasema, Lisia jemadari atakapotelemka nitakata maneno yenu. <sup>23</sup> Akamwamuru yule akida kwamba Paulo alindwe; ila awe na nafasi, wala asimkataze mmojawapo wa rafiki zake kumtumikia.

**24:22** Ni wazi kuwa Feliki alikuwa amekwisha sikia habari za Yesu na Ukristo. Bila shaka kama mtawala wa Kirumi alikwa amearifiwa kwa ufupi kuhusu hali ya mahali eneo hilo ambapo angepewa. Mke wa Feliki alikuwa Myahudi (kama vile Matendo ya Mitume 24:24), ambapo ilimaanisha kuwa na upenyo wa nafasi ya kuyafahamu mafundisho ya Dini ya Kiyahudi. Ie Njia ilifikiriwa kuwa dhehebu lililokuwa ndani ya Dini ya Kiyahudi na ilikuwa hivyo, hivyo, dini ya "kisheria" katika Dora ya Kirumi.

**24:23** Hili linaonyesha kwamba Feliki hakumuona Paulo kama mtu hatarishi na aliruhusu awe huru na upenyo. Huyu tena ni mtawala wa Kirumi ambaye hakuuchukulia Ukristo kama tatizo la kisiasa. Kwa hakika hii ilikuwa moja ya sababu ya Luka katika kuandika Injili yake!

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 24: 24-27**

<sup>24</sup> Baada ya siku kadha wa kadha, Feliki akafika pamoja na Drusila mkewe aliyekuwa Myahudi, akatuma kumwita Paulo akamsikiliza habari za imani iliyo kwa Kristo Yesu. <sup>25</sup> Na Paulo alipokuwa akitoa hoja zake katika habari ya haki, na kuwa na kiasi, na hukumu itakayokuja, Feliki akafanya hofu akajibu, Sasa enenda zako, nami nikipata nafasi nitakuita. <sup>26</sup> Pamoja na hayo alitaraji kwamba atapewa fedha na Paulo; kwa hiyo alimwita mara nyingi akaongea naye. <sup>27</sup> Na miaka miwili ilipotimia, Feliki akampokea Porkio Festo atawale badala yake. Na Feliki, akitaka kuwafanyia Wayahudi fadhili, akamwacha Paulo amefungwa.

**24:24** "Drusila" Huyu alikuwa mdogo sana, na kwa uwazi kabisa alikuwa mzuri wa sura, binti wa Herode Agripa I na dada wa Bernice na Agripa II. Alikuwa mke wa tatu wa Feliki, ambaye alimchukuwa kutoka kwa Azizus, Mfalme wa Emesa (kama vile Josephus, *Antiq.* 20.7.2).

**NASB, NRSV,**

**TEV, NJB** "Kristo Yesu"  
**NKJV** "Kristo"

Uchaguzi #1 unapatikana katika MSS P<sup>74</sup>,  $\aleph^*$ , B, E, na Kilatini cha Kale, Matoleo ya Kilatini. Andiko fupi sana unapatikana katika MSS  $\aleph$ , A, C, na matoleo ya Peshitta na Coptic. Tafsiri ya UBS<sup>4</sup> inatoa toleo lililo refu lenye daraja "B" (pana uhakika). Mtu anashangaa ikiwa katika mukatadha huu jina "Kristo" lazima litafsiriwe "Masih" (toleo la MS 044 lina jina Masih).

▣ " **imani** " Hili ni neno la kithiolojia lililo muhimu. Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:40; 3:16; na 6:5. Kumbuka hizi kweli za kithiolojia katika lugha ya Koine ya Kiyunani hazijajikita katika matumizi ya Kiyunani, bali katika Tafsiri ya Agano la Kale la Kiebrania. Hili lilikuwa Agano la Kale kwa ajili ya kanisa.

**24:24-25** Paulo alihubiri injili mara kwa mara (kama vile Matendo ya Mitume 24:26b) kwa Feliki na Drusila. Hili ndilo jambo halisi ambalo Yesu alimtaka alifanye (kama vile Matendo ya Mitume 9:15). Alijiona mwenye hatia, lakini pia alijiona mchoyo (yaani, alimtaka Paulo kumpa rushwa) na kuyatupilia mbali maamuzi yake (kama vile Matendo ya Mitume 24:26).

**24:26** Kwa hakika Paulo alikuwa na kiasi fulani cha faedha wakati wa kipindi hiki cha kutiwa gerezani. Huenda kutoka (1) urithi binafsi au (2) msaada uliotoka makanisani (yaani, Filipi au Thesalonika). Feliki alikuwa akimuita Paulo mara kwa mara, si kumsikia tu akizungumza, bali katika matumaini ya kupokea rushwa.

**24:27** " **Na miaka miwili ilipotimia** " Wengi waliamini kuwa ni katika kipindi kipindi hiki ambacho Luka akizikusanya taarifa za ushahidi kutoka kwa wale waliokuwa Palestina kwa ajili ya Injili (kama vile Luka 1:1-4). Lazima hiki kitakuwa ni kipindi cha kukatisha tamaa kwa mtu jeuri kama Paulo! Hata hivyo, hakuutafuta uhuru kwa njia ya rushwa. Yeye akjifahamu kuwa yu ndani ya mapenzi ya Mungu.

▣ " **Porkio Festo** " Kuna kutokukubaliana kati ya wanahistoria wa Kirumi, Suetonius na Tacitus, kuhusiana na muda kamili wa kuanza kwa ofisi yake. Feliki aliwekwa katika majaribio katika mwaka wa 55 b.k.lakini hili halina uhakika kama aliwekwa hatiani na kuondolewa baadaye au katika mwaka wa 59. Festus alifariki mnamo mwaka wa 62 b.k. akiwa katika utawala (kama vile Josephus, *Antiq.* 20.9.1). Yapo mambo machache yanayojulikana kumhusu (kama vile Josephus, *Antiq.* 20.8.9-10; *Wars* 2.14.1).

▣ "**akamwacha Paulo amefungwa**" Ilikuwa desturi ya kuwaachilia wafungwa wote katika kipindi cha mabadiliko ya tawala. Mstari huu unaonyesha hali ya kisiasa na udhaifu wa vingozi wa Kirumi, pamoljia na nguvu ya Wakuu wa Sinagogi.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wafasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! Neno "Mnazarethi " linamaanisha nini ?
2. Nini maana ya jina la kwanza la kanisa katia Matendo ya Mitume kuwa "Njia"
3. Eleza umuhimu wa Matendo ya Mitume 24:15

## MATENDO YA MITUME 25

MGAWANYO WA AYA WA TAFSRI ZA KISASA				
UBS <sup>4</sup>	NKJV	NRSV	TEV	NJB
Paulo anaomba Rufani kwa Kaizari	Paulo anaomba Rufani kwa Kaizari	Paulo anaomba Rufani kwa Mfalme	Paulo anaomba Rufani kwa Mfalme	Paulo anaomba Rufani kwa Kaizari
25:1-5	25:1-12	25:1-5	25:1-5	25:1-5
25:6-12		25:6-12	25:6-8 25:9 25:10-11 25:12	25:6-12
Paulo aletwa Mbele ya Agripa na Bernike	Paulo akiwa mbele ya Agripa	Kujitetea kwa Paulo mbele ya Agripa  (25:13-26:32	Paulo akiwa Mbele ya Agripa na Bernike	Paulo Ajihudhulisha Mbele ya Mfalme Agripa
25:13-22	25:13-27	25:13-22	25:13-21 25:22a 25:22b	25:13-22
25:23-27		25:23-27	25:23-27	25:23-26:1

### KUSOMA MZUNGUKO WA TATU (kutoka “Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia”)

#### KUFUATIA KUSUDIO ASILIA LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Ayaya kwanza
6. Ayayapili
7. Ayatatu
8. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA): MATENDO YA MITUME 25:1-5

1 Hata Festo alipokwisha kuingia katika uliwali, baada ya siku tatu akapanda kwenda Yerusalemu kutoka Kaisaria. 2 Kuhani Mkuu na wakuu wa Wayahudi wakampasha habari za Paulo, wakamsihi, 3 na kumwomba fadhili juu yake, kwamba atoe amri aletwe Yerusalemu, njiani wapate kumwotea na kumwua. 4 Lakini Festo akajibu ya kwamba Paulo analindwa Kaisaria; naye mwenyewe yu tayari kwenda huko karibu. 5 Akasema, Wale walio na mamlaka kwenu na watelemke pamoja nami wakamshitaki, ikiwa liko neno baya katika mtu huyu.

**25:1 "Festo"** Huyu alikuwa mrithi wa Feliki. Huyu alikuwa na roho ya uungwana, lakini kwa hakika huyu alikuwa chini ya nguvu ya utawala ule ule na fikra hizo hizo. Huyu alitawala kwa miaka miwaili na kufariki mnamo mwaka 62 b.k. akiwa madarakani (kama vile Josephus, *Antiq.* 20.8.9).

▣ "**baada ya siku tatu**" Hii inaonyesha namna mfadhaiko na ung'ang'anizi wa uongozi wa Kiyahudi kumhusu Paulo. Pia Festo pia alitaka kuunda wazo zuri la mwanzo.

**25:2 " Kuhani Mkuu na wakuu wa Wayahudi "** Hili linaweza kuwarejelea Wakuu wa Sinagogi, kundi ambalo likilikuwa limeundwa na viongozi 70 wa Kiyahudi kutoka Yerusalemu. Hawa waliunda kiungo cha juu cha kisheria za Kiyahudi katika vipengele vyote vya kiutawala na kidini. Tazama Mada Maalum katika 4:5. Hata hivyo, hiki kingeweza kurejelea juu ya matajiri wengine na wenyeji waliokuwa wasomi waliokuwa Yerusalemu ambao walikuwa na hofu ya kukutana na mawakili wapya wa Kirumi na kuanza kuimarisha uhusiano mwema pamoja naye. Kwa hakika ni dhahili kwamba hili linarejelea juu ya makundi yote mawili. Baada ya miaka miwili kulikuwa na kuhani mkuu mwingine mpya, Ishmael mwana wa Fabus (56-62 b.k). Yeye , pia, alitaka kujiimarisha mwenyewe na njia nzuri ya kulifanya hili ilikuwa ni kumvamia Mfarisayo aliyekwisha kuvunja sheria, Paulo.

▣ "**wakampasha habari**" Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati usiotimilifu. Walimuuliza tena na tena.

**25:3** Hili linaonyesha hali ya chuki dhidi ya Paulo kwa upande wa viongozi hawa wa kidini .Hawa walimuona Paulo kama adui aliyotoka miongoni mwao!

▣ "**( njiani wapate kumwotea na kumwua)**" Mbinu za uongozi wa Kiyahudi halizikubadilika (kama vile Matendo ya Mitume 23:12-15).

**25:5 "ikiwa"** Hii ni sentensi shurutishi dalaja la tatu ambayo inadhaaniwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au makusudi yake (kama vile A. T. Robertson, *Word Pictures in the New Testament*, juzuu 3, uk. 429). Dr. Bruce Tankersley, katika kitabu chake cha the Koine Greek specialist at East Texas Baptist University, anasema hili linaweza kuwa dalaja la tatu kwa sababu hakuna kitenzi katika sentensi shurutishi. Festo alidhani kuwa Paulo alikuwa mwenye hatia. Kwa nini viongozi wa Kiyahudi walikuwa ving'ang'anizi sana, na kuwa wasumbufu sana?

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 25:6-12

6 Alipokwisha kukaa kwao siku nane au kumi si zaidi, akatelemkia Kaisaria; hata siku ya pili akaketi katika kiti cha hukumu akaamuru Paulo aletwe. 7 Alipokuja, wale Wayahudi walioshuka kutoka Yerusalemu wakasimama karibu yake wakaleta mashitaka mengi mazito juu yake, wasiyoweza kuyayakinisha. 8 Paulo akasema akijitetea, Mimi sikukosa neno juu ya sheria ya Wayahudi, wala juu ya hekalu, wala juu ya Kaisari. 9 Lakini Festo akitaka kujipendekeza kwa Wayahudi akamjibu Paulo, akisema, Je! Wataka kwenda Yerusalemu, ukahukumiwe huko mbele yangu kwa ajili ya mambo hayo? 10 Paulo akasema, Mimi ninasimama hapa mbele ya kiti cha hukumu cha Kaisari, ndipo panipasapo kuhukumiwa; sikuwakosa Wayahudi neno, kama wewe ujuavyo sana. 11 Basi ikiwa ni mkosa au nimetenda neno la kustahili kufa, sikatai kufa; bali, kama si kweli

**neni hili wanalonishitaki, hapana awezaye kunitia mikononi mwao. Nataka rufani kwa Kaisari. 12 Basi Festo alipokwisha kusema na watu wa baraza, akajibu, Umetaka rufani kwa Kaisari! Basi, utakwenda kwa Kaisari.**

**25:6-9** Kuwepo kwa matukio haya kulimwonyesha Paulo kwamba hapakuwa na tumaini la kweli kuhusu haki kwa Festo. Yeye alikitambua alichokuwa akingojea katika Yerusalemu (kama vile Matendo ya Mitume 25:3). Yeye pia alimfahamu kuwa Yesu alimtaka kwenda Roma (kama vile Matendo ya Mitume 9:15).

**25:6 " Alipokwisha kukaa kwao siku nane au kumi si zaidi"** Ningefikiri kwamba viongozi wa Kiyahudi walimshinda na kumwekea utaratibu Festo. Hawa waliwatawala watawala wote wa Kirumi.

**25:8** Paulo anadai kutokuwa hatia ya mashtaka yote dhidi ya

1. Sheria ya Musa (kama vile Matendo ya Mitume 21:21,28)
2. hekalu (kama vile Matendo ya Mitume 21:28; 24:6)
3. Kaizari (kama vile Matendo ya Mitume 16:21; 17:7)

Numba na 2 ndiyo aina ya mashtaka ambayo Stefano alidaiwa kukiuka katika Matendo ya Mitume 6:13-14.

**25:10-11** Paulo anadai kwamba alikuwa tayari machoni pa utawala wa kweli na katika nafasi sahihi. Luka ananukuu katika Matendo ya Mitume 25:11 rufani ya kiutawala kwa Kaizari. Haki ya rufani kwa Kaizari kwa mara ya kwanza ilianza na Octavian mnamo 30 k.k. (kama vile Dio Cassius, *History*, 51.19). Uanzishwaji huu wa kujitetea uliimarishwa kwa ajili ya kuzuia uzushi, kujisafisha, na utesaji wa raia ye yote wa Kirumi ambaye aliomba rufani kwa Kaizari (kama vile Paulus, *Sententiae* 5.26.1). Kuna mjadala mzuri wa Sheria ya Kiyunani ya karne ya kwanza katika A. N. Sherwin-White's *Roman Society and Roman Law in the New Testament*, "hotuba ya nne: Paulo mbele ya Felix na Festus," kr. 48-70.

**25:11 " ikiwa. . . kama"** Hizi ni sentensi mbili shurutishi dalaja la kwanza ambazo zinadhaniwa kuwa za kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kusudi lake. Matumizi haya mawili katika muktadha yanaonyesha namna utungaji huu wa kisafrufi ulivyotumika kuunda hoja. Ya kwanza inakinzana na ukweli (lakini kwa uhalisia namna hiyo hiyo ilitumiwa na Feliki katika Matendo ya Mitume 25:5); ya pili inaenda sambamba na ukweli.

▣ **" sikatai kufa"** Paulo alitambua nguvu ya utawala (kama vile Rum. 13:4). Mtazamo wa Agano la Kale kuhusu adhabu unaweza kupatikana katika Mwa. 9:6. Tazama mjadala wa kuvutia katika *Hard Sayings of the Bible*, kr. 114-116.

**NASB, TEV " hapana awezaye kunitia mikononi mwao"**

**NKJV "hapana awezaye kunishikilia mikonono mwao"**

**NRSV "hapana awezaye kunirejesha mikononi mwao"**

**NJB "hana mwenye haki ya kunisalimisha mikononi mwao"**

Hili neno *charizoma* kimsingi linamaanisha "kutoshereza" au "kujitolea kama mwokozi." Paulo alitambua kwamba Festo alikuwa akijaribu kuufurahisha uongozi wa Kiyahudi kwa kujitolea yeye mwenyewe! Hata hivyo, inawezekana kwamba Festo anajaribu kudumisha agizo lililotolewa na Julius Kaizari (kama vile Josephus, *Antiq.* 14.10.2), ambayo ilisistiza utawala wa Kirumi kuruhusu matakwa ya makuhani wakuu.

▣ **"Nataka rufani kwa Kaisari"** Hii ilikuwa haki ya kisheria ya kila raia wa Kirumi katika kesi za adhabu za makazi (Pliny the Younger, Letters 10.96). kutokana na hoja hii katika historia, basi Nero alikuwa Kaizari (a.d. 54-68).

**25:12 " baraza"** Neno hili linarejelea ju ya wataalam wa Festo wa sheria za Kirumi, si viongozi wa Kiyahudi.



## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MATENDO YA MITUME 25:13-26:32

### MAZINGIRA YA NYUMA

#### A. Herode Agrippa II (Marcus Julius Agrippa)

Huyu ni mwana wa Herode Agrippa I (kama vile Matendo ya Mitume 12), ambaye alikuwa mtawala wa kisiasa wa Yudea na ambaye alikuwa akilitawala Hekalu na Ukuhani (a.d. 41-44) na mjukuu wa Herode Mkuu

1. Huyu alipata elimu yake humo Rumi na alikuwa Mkatoriki. Huyu alirudi Rumi baada ya vita ya Kiyahudi ya 70 b.k. na kufia pale pale mnamo 100 b.k.
2. Akiwa na umri wa miaka 17 baba yake alipofariki, lakini alikuwa kijana mdogo sana kuchukua maamuzi ya ufalme wake
3. Katika mwaka wa 50 b.k. Herode Chalcis, mjomba wa Agrippa II, Mfalme wa Chalcis (himaya ndogo iliyo upande wa Kaskazini wa Palestina), alifariki na Agrippa II akapewa himaya yake na Mfalme Claudio. Pia, alipewa madaraka juu ya Hekalu na Kuhani Mkuu.
4. Katika mwaka wa 53 b.k. alibadilisha himaya hii ndogo kwa ajili ya maliwali wa Herode Filipi (Ituraea na Trakonite) na Lysanius (Abilene).
5. Baadaye, Mfalme Nero aliongeza miji na vijiji kadhaa kandokando ya Bahari ya Galilaya kwa mamlaka yake. Makao yake makuu yalikuwa Kaizaria ya Filipi, ambayo aliita kwa jina jipya Neronias.
6. Kwa marejeleo zaidi ya Kihistoria kama vile:
  - a. Josephus *Jewish Wars* 2.12.1,7-8; 15.1; 16.4; 7.5.1
  - b. Josephus' *Antiquities of the Jews* 19.9.2; 20.5.2; 6.5; 7.1; 8.4; 9.6.

#### B. Bernike

1. Huyu alikuwa binti mkubwa wa Herode Agrippa I.
2. Huyu alikuwa dada wa Agrippa II, na kwa kipindi cha wakati fulani aliweza kuwa na uhusiano wa kimapenzi na ndugu wa mbali (hakuna ushahidi wa hili, ni uzushi tu). Baadaye alikuwa mtawala wa Mfalme Tito ambapo alikuwa mtawala mkuu. Huyu alikuwa Mrumi mkuu ambaye aliiharibu Yerusalemu na lile Hekalu mnamo 70 b.k.
3. Huyu alikuwa dada wa Drusila (kama vile Matendo ya Mitume 24:24).
4. Huyu aliolewa na Herode Chalcis (kaka wa Herode Agrippa I, mjomba wake), lakini alipofariki aliolewa na kaka yake.
5. Baadaye aliolewana Polemon, Mfalme wa Kilikia, lakini alimuachana kurudi kwa kaka yake ambaye ambaye alikuwa amepewa cheo cha "Mfalme."
6. Huyu alikuwa mtawala wa Mfalme Vespasian.
7. Marejereo ya kihistoria
  - a. Josephus *Jewish Wars* 2.1.6; 15.1; 17.1.
  - b. Josephus' *Antiquities of the Jew* 19.9.1; 15.1; 20.1.3
  - c. Tacitus' *History* 2.2
  - d. Seutonius' *Life of Titus* 7
  - e. Dio Cassius' *Histories* 65.15; 66.18
  - f. Juvenal's *Satire* 61.156-157

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 25:13-22**

**13 Siku kadha wa kadha zilipokwisha kupita, Agripa mfalme na Bernike wakafika Kaisaria, wakimwamkia Festo. 14 Na walipokuwa wakikaa huko siku nyingi, Festo akamweleza mfalme habari za Paulo, akisema,**

Yupo hapa mtu mmoja aliyeachwa na Feliki kifungoni; 15 ambaye nilipokuwa Yerusalemu wakuu wa makuhani na wazee wa Wayahudi wakaniarifu habari zake, wakinitaka hukumu juu yake. 16 Nikawajibu kwamba si desturi ya Warumi kumtoa mtu awaye yote, kabla mtu yule aliyeshitakiwa hajaonana na washitaki wake uso kwa uso, na kupewa nafasi ya kujitetea katika mashitaka yake. 17 Basi walipokutanika hapa sikukawia; bali siku ya pili nikaketi katika kiti cha hukumu nikaamuru mtu huyo aletwe. 18 Na wale waliomshitaki waliposimama hawakuleta neno lo lote baya, kama nilivyodhani, 19 bali walikuwa na maswali mengine mengine juu yake katika dini yao wenyewe, na katika habari ya mtu mmoja Yesu, aliyekuwa amekwisha kufa, ambaye Paulo alikaza kusema kwamba yu hai. 20 Nami nikaona shaka jinsi ya kutafuta hakika ya habari hii, nikamwuliza kama anataka kwenda Yerusalemu ahukumiwe huko katika mambo haya. 21 Lakini Paulo alipodai kuwekwa ahukumiwe na Kaisari, nikaamuru alindwe hata nitakapompeleka kwa Kaisari. 22 Agripa akamwambia Festo, Mimi nami nalikuwa nikitaka kumsikia mtu huyu. Akasema, Utamsikia kesho.

**25:13 "Agripa mfalme"** Aya hii inamrejelea Agrippa II. Huyu alikuwa ndugu wa Drusila na Bernike. Hutu alipata elimu yake humo Roma na alikuwa mwaminifu sana kwa sera na taratibu za Kirumi.

### MADA MAALUM: BERNIKE

1. Huyu alikuwa binti mkubwa wa Herode Agripa I (alizaliwa mnamo 28 B.K).
2. Alikuwa dada wa Agripa II, kwa kipindi cha wakati akawa na mahusiano ya kipanzi naye. Baadaye alikuwa mkuu kwa Tito ambapo alikuwa mpenzi mkuu .
3. Pia alikuwa mke wa tatu wa Feliki, dada wa Drusila.
4. Aliolewa kwa Herode Chalcis (kaka wa Herode Agripa, mjomba wake), lakini alipokufa alisogea kwa kaka yake.
5. Baadaye aliolewa na Polemon, Mfalme wa Cilikia, lakini alimuacha na kurudi kwa kaka yake ambaye alikuwa amepewa cheo cha "Ufalme."
6. Huyu alikuwa mpenzi wa wote Vespasian na Tito.
7. Kwa marejeleo zaidi ya kihistoria tazama
  - a. Josephus' *Jewish Wars* 2.11.6; 15.1; 17.1.
  - b. Josephus' *Antiquities of the Jews* 19.9.1; 15.1; 20.1:3
  - c. Tactius' *History* 2:2
  - d. Seutonius' *Life of Titus* 7
  - e. Dio Cassius' *Histories* 65.15; 66.18
  - f. Juvenal's *Satire* 61.156-157

**25:13-19** Tena hili linafunua moja ya maandiko ya Luka na sababu za kitheolojia, ambazo zinaonyesha kwamba Ukristo haukuwa na athari za kisiasa huko Rumi (kama vile Matendo ya Mitume 25:25). Katika miongo ya kale ya karne ya kwanza Ukristo ulifikiriwa kama dhehebu la Kiyahudi, ambalo lilitambuliwa na Rumi kama dini ya kisheria. Rumi haikutaka hata sehemu ya mabishano miongoni mwa madhehebu ya dini za Kiyahudi!

**25:18 "hawakuleta neno lo lote baya, kama nilivyodhani"** Hili linaonyesha nguvu na asili ya upinzani wa Kiyahudi. Huu haukuwa wa kisiasa, bali wa kidini.

**NASB, NRSV**

**NJB, NIV** "kosa"

**NKJV** "mambo hayo"

**TEV** "makosa ya uovu"

**REB** "mashtaka"

**NET Bible** "matendo ya uovu"

## ASV "mambo yaliyo maovu"

Kuna utofauti kadhaa.

1. *ponērōn* – kimilikishi wingi katika MSS 2, B, E, yenye maana ya "mambo yaliyo maovu" (kama vile Matendo ya Mitume 28:21)
2. *ponērau* –kimilikishi cha umoja kisicho na jinsi chenye mashitaka katika MSS P74, A, C\*
3. *ponēra* – kimilikishi wingi chenye mashitaka katika MSS 2, C<sup>2</sup>
4. *ondoa* – MSS L, P, na baadhi ya mafungu ya Biblia yaliyokusudiwa kusomwa (kama vile NKJV)

Toleo la UBS<sup>4</sup> linaweza uchaguzi #1 katika maandiko pamoja na darlaja "C" (ngumu katika kuchukua maamuzi). Feliki alistaajabu kwamba mashtaka haya hayakuwa na maana yo yote ilimpasa kutatenda mambo yahasuyo dini za Kiyahudi, si mambo ya kisheria.

**25:19 " dini "** Kiuhalisia neno ambatani linatokana na neno "woga" na "miungu." Neno hili linaweza kumaanisha "ushirikina," ambalo kwa hakika ndilo viongozi wa Kiyahudi walilolifikiria kuhusiana na dini ya Kiyahudi. Hata hivyo, Festo hakutaka kuwakashifu wenye mamlaka wa Kiyahudi, hivyo alitumia neno lenye utata (hivyo hivyo, Paulo, Matendo ya Mitume 17:22). Mistari ya 18-19 tena inaonyesha kwamba haki ya Kirumi ilimkuta Paulo pasipokuwa na hatia au Ukristo.

▣ **"habari ya mtu mmoja Yesu, aliyekuwa amekwisha kufa, ambaye Paulo alikaza kusema kwamba yu hai"** Ufufuo ulikuwa moja ya kitovu cha nguzo ya hotuba (*kerygma*, tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:14) katika Matendo ya Mitume (kama vile Matendo ya Mitume 26:8). Ukristo unasimama au unaangukia katika dai hili la kitheolojia (kama vile 1 Wakorintho 15).

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 25:23-27

**23**Hata asubuhi Agripa akaja pamoja na Bernike kwa fahari nyingi, wakaingia mahali pa kusikia maneno, pamoja na maakida wakuu na watu wakuu wa mji; Festo akatoa amri, Paulo akaletwa. **24** Festo akasema, Mfalme Agripa, na ninyi nyote mliopo hapa pamoja nasi, mnamwona mtu huyu, ambaye jamii yote ya Wayahudi huko Yerusalemu na hapa pia wamenitaka niwasaidie, wakipiga kelele kwamba haimpasi kuishi zaidi. **25** Lakini mimi naliona kwamba hakutenda neno la kustahili kuuawa, na yeye mwenyewe alipotaka kuhukumiwa na Kaisari, nalikusudia kumpeleka kwake. **26** Nami katika habari yake sina neno la hakika la kumwandikia bwana. Kwa hiyo nimemleta hapa mbele yenu, hasa mbele yako wewe, mfalme Agripa, ili akiisha kuulizwa-ulizwa nipate neno la kuandika. **27** Kwa maana naona ni neno lisilo maana kumpeleka mfungwa, bila kuonyesha mashitaka yale aliyoshitakiwa.

**25:23** Ni nafasi gani ya kustaajabisha tuliyonayo ya kuihubiri injili!

▣ **" maakida"** Hili neno *chiliarch*, limaanisha kiongozi wa maelfu, kama aliyeishi karne nyingi linavyomaanisha kiongozi wa mamia. Tunajifunza kutokana na Josephus' *Antiq.* 19.19.2, kwamba washirika wasaidizi watano katika Kaizaria katika kipindi hiki. Hivyo, huenda watu wa kijeshi wanarejelewa hapa.

▣ **"wakuu wa mji"** Aya hii ingeweza kurejelea viongozi wa mji wa Kaizaria.

Yatambue makundi yaliyokuwa katika baraza.

1. wakili wa Kirumi
2. mfalme wa dini ya Idumean
3. viongozi wa jeshi la kirumi
4. viongozi wakuu wa kiraia wa huko Kaizaria

▣ **25:26 "wakuu"** Hili neno ni *sebastos*, ambalo lilikuwa na usawa wa Kiyunani wa neno la Kilatini *augustus*. Asili yake ya msingi ni "kuhesimu," "kutukuza," "kusifu," au "kuabudu." Kwa mara ya kwanza neno hili lilitumika kwa Octavian mnamo 27 k.k. na Senata. Hapa, linatumika kwa Nero (. 54-68 b.k). Nero anaonekana kupanua heshima

ya Mkuu wa madhehebu.

**25:26 " sina neno la hakika la kumwandikia "** Festo alikuwa na tatizo hilo hilo kama alililokuwa nalo Lisia, akida kutoka Yerusalemu. Huyu alizuiliwa na sheria ya Kirumi kuandika mashtaka dhidi ya Paulo kwa makubaliano ya ushahidi wo wote au maoni ya kisheria. Paulo alikuwa mtata kwa hawa viongozi wa Kiyunani.

▣ **"bwana" Hili ni neno la Kiyunani kurios**, ambalo linamaanisha mmiliki, mkuu, mtawala. Haya ni matumizi ya kwanza ya ushahidi wa neno *kurios* kama wadhifa unaojitegemea kwa Nero. Wadhifa huu ulipingwa na Wakuu kama Octavian/Augustus na Tiberia kwa sababu walidhani kwamba wadhifa huu ulikaribiana na wadhifa wa mtawala wa Kilatini (mfalme), ambao ulisababisha wasiwasi kwa umati wa Kirumi na Senata. Hata hivyo, hili linaonekana mara nyingi wakati na baada ya siku za Nero. Vespasian na and Tituo walitumia neno "mwokozi" na Domitian alitumia neno "mungu" kutoa maelezo yao (kama vile James S. Jeffers, *The Greco-Roman World* uk. 101). Hili neno *kurios* linakuwa mateso dhidi ya Wakristo, ambaye angetumia neno hili tu kwa Yesu Kristo.

Walikaidi kulitumia katika sadaka ya uvumba na uaminifu wa kiapo kwa Rumi.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wafasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini viongozi wa Kiyahudi walimhofu na kumchukia Paulo?
2. Ni kwa jinsi gani sura hii inakisi moja ya sababu za Luka za kuandika kitabu cha Matendo ya Mitume?
3. Nini sababu ya Paulo katika kujitetea mbele ya Agripa na Bernike?

## MATENDO YA MITUME 26

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Paulo Anajitetea Mbele ya Agripa	Maisha ya Awali ya Paulo	Kujitetea kwa Paulo Mbele ya Agripa  (25:13-26:32)	Paulo Ajitetea Mbele ya Agripa	Paulo atokea mbele ya Agripa  (25:13-26:1)
26:1-11	26:1-11	(26:1)	26:1	Usemi wa Paulo Mbele ya Mfalme Agripa
		26:2-3 26:4-8 26:9-11	26:2-3 26:4-8 26:9-11	26:4-8 26:4-8 26:11
Paulo Akizungumza Kuhusu Kubadilika Kwake	Paulo Akirudia Maelezo ya Kubadilika Kwake		Paulo Akizungumzia juu ya Kubadilika Kwake	
26:12-18	26:12-18	26:12-18	26:12-18	26:12-18
Ushuhuda wa Paulo kwa Wayahudi na Mataifa	Maisha ya Paulo Baada ya Kubadilika		Paulo Akiizungumzia Kazi Yake	
26:19-23	26:19-23	26:19-23	26:19-23	26:19-23
Paulo Amuomba Rufani Aripa Akubali				Muitikio wa Wasikilizaji Wake
26:24-29	26:24-32	26:24-29	26:24-26:24-29  26:25-27  26:28 26:29	
26:30-32		26:30-32	26:30-32	26:30-32

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("[A Guide to Good Bible Reading](#)")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 26: 1

<sup>1</sup>Agripa akamwambia Paulo, Una ruhusa kusema maneno yako. Ndipo Paulo akanyosha mkono wake, akajitetea,

**26:1 "akaunyosha mkono wake"** Hii ilikuwa ishara ya kusalimiana na utangulizi wa hotuba (kama vile Matendo ya Mitume 12:17; 13:16 na 21:40, ambapo ishara za mikono zinatumiwa kwa ajili ya utulivu na ukimya).

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 26:2-3

<sup>2</sup> Najiona nafsi yangu kuwa na heri, Ee mfalme Agripa, kwa kuwa nitajitetea mbele yako leo, katika mambo yale yote niliyoshitakiwa na Wayahudi. <sup>3</sup> Hasa kwa sababu wewe unajua sana desturi na maswali yote waliyo nayo Wayahudi; kwa sababu hiyo nakuomba unisikilize kwa uvumilivu.

**26:2-3** Paulo anatanguliza kujitetea kwake katika muundo ule ule na kwa namna ya kufurahisha, kama alivyofanya katika mashtaka yake mbele ya Feliki (kama vile Matendo ya Mitume 24:10), ishara ambayo huenda ilikuwa ni tarajio muhimu kiutamaduni.

**26:2 "katika mambo yale yote niliyoshitakiwa na Wayahudi "** Rumi ilimwingiza Agripa II katika kushughulikia mashtaka ya Hekalu na Ukuhani. Japokuwa huyu alikuwa mfuasi wa Kirumi na kupata elimu yake katika Rumi, alifahamu vema undani wa imani ya Kiyahudi (kama vile Matendo ya Mitume 26:3).

▣ **"heri"** Hili ni neno lile lile ambalo linatoa maelezo ya awali kwa kila Heri za Mt. 5:3-12; Luka 6:20-22; na Zab. 1:1 katika Agano la Kale la Kiebrania.

**26:3**

**NASB, NKJV** "desturi na maswali yote"

**NRSV** "desturi na mabishano yote"

**TEV** "desturi za Kiyahudi na migogoro yote"

**NJB** "desturi na mabishano"

Neno la kwanza *niethōn*, ambapo tunalipata neno la Kiingereza "mbari," au kipengele cha kitamaduni cha kundi fulani la watu. Neno la pili *dzētēmatōn* linatumika mara kwa mara katika Matendo ya Mitume kudokeza majadiliano na mabishano juu ya kipengele cha sheria za Dini ya Kiyahudi (kama vile Matendo ya Mitume 15:2; 18:15; 23:19; 25:19; 26:3). Maneno haya hayakuwa ya kawaida kwa sababu ya kuwepo kwa makundi kadhaa ndani ya dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza: Masadukayo, Mafarisayo (pia makundi ya kitheolojia ya Shammai na Hillel), na wafuasi wa Zerosta.

### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 26:4-8

<sup>4</sup>Kwa maana Wayahudi wote wanajua maisha yangu tangu ujana, yaliyokuwa tangu mwanzo katika taifa langu huko Yerusalemu, <sup>5</sup>wakinijua sana tangu mwanzo, kama wakipenda kushuhudia, ya kwamba nalikuwa

**Farisayo kwa kuifuata madhehebu ya dini yetu iliyo sahihi kabisa.** <sup>6</sup>Na sasa ninasimama hapa nihukumiwe kwa ajili ya tumaini la ahadi baba zetu waliyopewa na Mungu, <sup>7</sup>ambayo kabila zetu kumi na mbili wanataraji kuifikia, wakimwabudu Mungu kwa bidii mchana na usiku. Nami ninashitakiwa na Wayahudi kwa ajili ya tumaini hilo, Ee Mfalme. <sup>8</sup>Kwa nini limedhaniwa kwenu kuwa ni neno lisilosadikika, kwamba Mungu awafufua wafu?

**26:4" Wayahudi wote wanajua maisha yangu** "Paulo amelirudia hili mara kwa mara (kama vile Matendo ya Mitume 22:3-5; 23:1;24:16; 25:8). Paulo ameishi maisha ya mfano miongoni mwa Wayahudi katika Yerusalemu (kama vile Matendo ya Mitume 26:5).

▣**"taifa langu mwenyewe"** Haijulikani ni wapi Paulo alikulia. Hili lingeweza kurejelea juu ya (1) Tarso huko Kilikia au (2) Yerusalemu.

**26:5 "ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la tatu ambayo inamaanisha tendo lenye umuhimu. Katika andiko hili Paulo alifahamu kwamba wangeshuhudia kuhusu maisha yake ya nyuma, lakini wasingeweza.

▣**" Farisayo kwa kuifuata madhehebu ya dini yetu"** Hili lilikuwa dhehebu la kitheolojia la dini ya Kiyahudi ambalo lilishamiri Kipindi cha Wamakabayo. Hili lilikuwa katika utendaji wa tamaduni za masimulizi na zilizoandikwa. Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 5:34.

**26:6" tumaini la ahadi baba zetu waliyopewa na Mungu"** Hili linarejelea juu ya uanabii wa Agano la Kale juu ya (1) ujio wa Masihi ama (2) ufufuo wa wafu (kama vile Matendo ya Mitume 23:6; 24:15; Ayubu14:14-15; 19:25-27; Dan. 12:2). Paulo aliona "Njia" kama utimilifu wa Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-19; Wagalatia 3). Kwa neno "tumaini" tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:25 na Mada Maalum: *Kerygma* katika Matendo ya Mitume 2:14.

**26:7" kabila zetu kumi na mbili** "Unasaba wa kimakabila (wana wa Yakobo) bado ulikuwa wa muhimu sana kwa Wayahudi. Makabila mengi kati ya kumi yaliyotawanyika huko kaskazini hawakurudi kutoka uhamishoni Ashuru (722 b.k.).Tunafahamu taarifa zingine zilitoka katika Agano Jipya.

1. Mariamu, Yusufu, na Yesu walitoka katika kabila la Yuda (kama vile Mt. 1:2-16; Luka 3:23-33; Ufu. 5:5)
2. Kabila la analinaelezwa kama kabila la Asheri (kama vile Luka 2:36)
3. kabila la Paulo linaelezwa kama kabila la Benjamini (kama vile Rum. 11:1; Flp. 3:5)  
Herode Mkuu alikuwa na wivu juu ya hili na alikuwa na kumbukumbu za Hekalu, ambazo zilionyesha vizazi, vilivyozuiliwa. Kwa wale "kumi na wawili" tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 1:22.

▣**"tumaini"** Mtu anashanga haswa ni tumaini gani linalozungumziwa na Paulo. Kutokana na muktadha mpana mtu angeliweza kudhani ni lile lile la ufufuo (kama vile Matendo ya Mitume 26:8).Tazama [MADA MAALUM: TUMAINI](#) katika Matendo ya Mitume2:25.

▣**"wakimwabudu Mungu kwa bidii mchana na usiku"** Paulo alilipenda kundi lake (kama vile Rum. 9:1-3). Alifahamu vyema namna kundi hili lilivyomtumikia YHWH katika mazingira magumu. Pia kwa upekee alifahamu hatari ya sheria, ung'ang'aniaji, na nadharia ihusuyo utawala wa tabaka la juu. "Usiku na mchana" ilikuwa nahau ya nguvu na kanuni (kama vile Matendo ya Mitume 20:31; Luka 2:37).

**26:8 "Kwa nini limedhaniwa kwenu kuwa ni neno lisilosadikika"** Paulo anazungumzia makundi mawili:

1. Agripa na Wayahudi wengine waliokuwepo
2. Watu wa Mataifa waliopo, kama vile Festo

▣ **"kwamba"** Hii ni sentensishurutishi darajala kwanza ambayo inadhaniwa kuwa ya kweli kutokana na matazamo wa mwandishi ama kwa ajili ya makusudi yake ya kuiandishi.

▣ **"Mungu anafufua wafu"** Kifungu hiki kinazungumzia tumaini la Kiyahudi la ufuo wa jumla (tazama Ayubu 14:14-15; 19:25-27; Isa. 25:8; 26:19; Dan. 12:2-3), lakini Paulo alikuwa na ufufuo wa Kristo hasa akilini mwake (kama vile 1 Kor. 15:1-28). Hawa washtaki wa Kisadukayo wangejawa na hofu kwa wakati huo (kama vile Matendo ya Mitume 23:1-10).

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 26: 9-11**

<sup>9</sup> Kweli, mimi mwenyewe naliona ndani ya nafsi yangu kwamba yanipasa kutenda mambo mengi yaliyopingamana na jina lake Yesu Mnazareti; <sup>10</sup> nami nikayafanya hayo Yerusalemu; niliwafunga wengi miongoni mwa watakatifu ndani ya magereza, nikiisha kupewa amri na wakuu wa makuhani; na walipouawa nalitoa idhini yangu. <sup>11</sup> Na mara nyingi katika masinagogi yote naliwaadhibu, nikawashurutisha kukufuru; nikawaonea hasira kama mwenye wazimu, nikawaudhi hata katika miji ya ugenini.

**26:9** Paulo (*egō*, "Mimi" *naemautō*, "mimi mwenyewe") alikiri kuongozwa vibaya na shauku ya dini yake, ambapo

▣ **"jina"** Hii nahau ya kisemitiki inamaanisha "mtu wa" (kama vile Matendo ya Mitume 3:6,16). Hii si kanuni ya kishirikina, bali uhusiano binafsi!

▣ **"Yesu wa Nazarethi"** Tazama Mada Maalum katika Matendio ya Mitume 2:22.

**26:10 "watakatifu"** Kiuhalisia neno hili ni "waliotengwa." Sasa Paulo alikuwa amekwisha tambua ni nani aliyokuwa akiwatesa na kuwaua, Watu wa Mungu! Ni mshtuko wa namna gani, uchungu, na uongofu wa maono ya Paulo kuelekea Dameski ambao angekuwa nao, kubobea kwa mawazo na maisha kwa ujumla! Kwa "watakatifu" tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 9:13.

▣ **"nikiisha kupewa amri"** Paulo alikuwa mtesaji mwenye "mamlaka" kwa Wakuu wa Makuhani.

▣ **"na walipokwisha kuuawa"** Aya hii inaonyesha nguvu ya mateso. "Njia" halikuwa jambo kubwa; lilikuwa ni suala la uzima na kifo na bado ni lile lile!

▣ **"nalitoa idhini yangu"** Hili ni neno la kiufundi lililo katika lugha ya Kiyunani la kutoa idhini ya kiutawala katika Wakuu wa makuhani ama sinagogi. Lakini kwa kuwa hakuna sinagogi la mahali ambalo lingetoa idhini kuhusu mambo yahasuyo kifo, bila shaka hawa walikuwa wakuu wa makuhani. Ikiwa ilikuwa ni wakuu wa makuhani, kisha Paulo angekuwa amekwisha oa. Kiuhalisia neno lilimaanisha "jiwe jeupe," ambalo lilitumika kuchora—kwa vyo vyote ni jeusi au jeupe (kama vile Ufu. 2:17)

**26:11 "nikawashurutisha"** Hii ni kauli isiyotimilifu ya neno la Kiyunani lenye kumaanisha kulazimisha ama kutoa amri (kama vile Matendo ya Mitume 28:19), lakini hapa linatumika katika maana ya kujaribu. Neno hili linarejelea tendo lililorudiwarudiwa katika wakati uliopita.

▣ **"kukufuru"** Sauli alijaribu kuwashurutisha wakiri wazi imani yao katika Yesu kama Masihi na kisha kuwashtumu. Katika mateso yaliyofuatia, waamini walishurutishwa kukana imani katika Kristo, lakini muktadha huu ni hali tofauti ya kiutamaduni.

**NASB** "nikawaonea hasira"

**NKJV** "nikawaonea ghadhabu sana"

**RSV** "nikawaonea hasira kuliko kawaida"



TEV "nilighadhabika sana"  
NJB "hasira yangu kali ilikuwa dhidi yao"

Hiki ni kielezi chenye nguvu ("nyingi zaidi") na chenye hali endelevu (kauli yakati [yenye ushahidi]). Festo alitumia ushabiki huo huokwa Paulo (yaani, neno wazimu katika Matendo ya Mitume 26:24)

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME : 12-18**

<sup>12</sup>Basi katika kazi hiyo nilipokuwa nikienda Dameski, mwenye mamlaka na maagizo ya wakuu wa makuhani; <sup>13</sup>Ee Mfalme, ndipo wakati wa aduhuri njiani naliona nuru inatoka mbinguni ipitayo mwangaza wa jua, ikinimulikia mimi, na wale waliofuatana nami pande zote. <sup>14</sup>Tukaanguka nchi sote, nikasikia sauti ikisema nami kwa lugha ya kiebrania, Sauli! Sauli! Mbona waniudhi? Ni vigumu kwako kuupiga mateke mchokoo. <sup>15</sup>Nami nikasema, Wewe u nani, Bwana? Bwana akaniambia, Mimi ni Yesu, ambaye wewe unaniudhi. <sup>16</sup>Lakini inuka, usimame kwa miguu yako, maana nimekutokea kwa sababu hii, nikuweke wewe uwe mtumishi na shahidi wa mambo haya uliyoyaona, na wa mambo ambayo katika hayo nitajidhihirisha kwako; <sup>17</sup> nikikuokoa na watu wako, na watu wa Mataifa, ambao nakutuma kwao; <sup>18</sup>uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuelekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.

**26:12** Luka ananukuu ushuhuda binafsi wa Paulo mara tatu katika Matendo ya Mitume, 9:1-31; 22:3-21, na hapa. Huruma na uchaguzi wa Mungu kwa Sauli u-wazi. Ikiwa Mungu kupitia Kristo aliweza kumsamehe na kumtumia mtu huyu, anaweza kusamehe na kumtumia mtu ye yote yule!

**26:13** Tazama maelezo kamili katika Matendo ya Mitume 9:3. Ile dhana ya kwamba kuna tofauti katika undani wa sehemu zote tatu ambapo Paulo anashirikisha mjadala wake kwa kuzungumzia kwa usahihi juu ya Luka kuchukua kumbukumbu ya kujitetea kwake kisheria (na, ambapo, pia hotuba hizi) katika Matendo ya Mitume!

**26:14** Tazama maelezo kamili katika Matendo ya Mitume 9:4. Frank Stagg, *New Testament Theology*, ameandika aya ndefu inayozungumzia uhusiano muhimu kati ya Yesu na kanisa lake.

"Ukweli ulio muhimu zaidi kuhusu hukumu ni kwamba tunahukumiwa katika uhusiano na Kristo. Katika kugeuka, hii ni hukumu katika uhusiano na watu wake. Uhusiano wetu wa kweli kwake unaakisiwa katika uhusiano wetu na watu wake. Kuwatumikia watu wake ni kumtumikia yeye na kuwakana ni kumkana yeye (Mt. 25:31-46). Kamwe Agano Jipya halimruhusu mtu kuutenganisha uhusiano wake na Kristo, kutoka huo hadi kwa watu wengine. Kuwatesa ni kumtesa yeye (Matendo ya Mitume 9:1-2,4-5; 22:4,7-8; 26:10-11,14-15). Kumtenda dhambi ndugu ni kumtenda dhambi Kristo (1 Kor. 8:12). Japo hatuokolewi kwa kazi zetu, tunaokolewa kwayo; kupitia hayo tunaakisi uhusiano wetu wa kweli na neema yake. Hukumu ni huruma kwao ambayo husababisha wao kuikubali hukumu, na hukumu ni huruma kwao waliohurumiwa (Mt. 5:7)" (uk. 333).

▣ **"lugha ya kiebrania"** Ndani ya shuhuda tatu binafsi za Paulo katika Matendo ya Mitume, hii ndiyo sehemu pekee ambapo undani wa Yesu kunena kwa lugha ya Kiaramu unatajwa. Tazama maelezo kamili katika Matendo ya Mitume 22:2.

▣ **"Sauli, Sauli"** Hii ni nusu ya sehemu iliyopita ya Matendo ya Mitume 26:14 na sehemu iliyopita ya Matendo ya Matendo ya Mitume 26:15, pamoja na Matendo ya Mitume 26:16-18, ni eneo linalonukuu kuanzia kwa Yesu hadi kwa Paulo katika barabara ya kuelekea Dameski.

▣ **"Ni vigumu kwako kuupiga mateke mchokoo"** Kifungu hiki ni cha kipekee katika muktadha huu, huenda ni kwa sababu hii ni methali ya Kiyunani/Kilatini, si ya Kiyahudi. Mara nyingi Paulo alikuwa na utambuzi ni watu wa namna gani aliyokuwa akizungumza nao na namna ya kuwasiliana nao! Hili linarejelea juu ya

1. Fimbo ilichaguliwa inayotumiwa na wale wanaoswaga ng'ombe aina ya maksai akokotaye mikokoteni na plau
2. Makisio mbele ya farasi wavutao mkokoteni wa kigari au kigari kusaidia wanyama wasije wakapiga miguu yao nyuma. Mithali hii ilitumika kuonesha kwa kuashiria ujinga wa kibinadamu wa kupinga kazi za kiungu.

**26:15** Tazama maelezo kamili katika Matendo ya Mitume 9:5.

▣"**Mimi ni Yesu, ambaye wewe unaniudhi**" Hili linaonyesha uhusiano wa karibu kati ya Yesu na kanisa lake, (kama vile Mt. 10:40; 25:40,45). Kuwaumiza ni kumuumiza yeye!

**26:16 "Lakini inuka, usimame kwa miguu yako"** Hizi zote ni kauli tendaji zenye masharti za wakati uliopita usiotimilifu. Sauti hii inatambuliwa kwa wito wa kinabii wa Yeremia1:7-8 na Ezekieli 2:1,3.

▣"**nimekutokea kwa sababu hii**" Mungu alikuwa na uteuzi mahususi kwa Paulo. Kubadilika kwa Paulo na wito wake haufanani, bali ni wa ajabu! Huruma ya Mungu imedhihirishwa kwa nguvu pamoja na uchaguzi wa Mungu kwa ajili ya huduma ya Ufalme na ukuaji wa ufalme.

▣"**nimekutokea. . . nitajidhihirisha kwako**" Yote hii ni miundo ya neno *horaō*. Sentensi ya kwanza ni kauli tendewa elekezi ya wakati uliopita usio timilifu na hii ya pili ni kauli tendewa elekezi ya wakati ujao. Katika maana hii Yesu anamuahidi Paulo kukutana naye kwa upekee. Paulo alikuwa na maono kadhaa ya ki-Ungu katika kipindi cha huduma yake (kama vile Matendo ya Mitume 18:9-10; 22:17-21; 23:11; 27:23-24). Pia Paulo anakitaja kipindi hiki cha mafunzo katika Arabia ambayo alifunzwa na Yesu (kama vile Gal. 1:12,17,18).

▣"**nikuweke**" Kiuhalisia neno hili linamaanisha "kuchukua mkononi" Hii ilikuwa nahau ya kumtakia mtu mambo mema (kama vile Matendo ya Mitume 22:14; 26:16).

▣"**mtumishi na shahidi**" Kiuhalisia neno hili lilirejelea juu ya "mpiga kasia" ndani ya melikebu. Neno hili baadaye lilikuja kutumika katika mtindo wa nahau likimaanisha mtumishi. Kutokana na neno la pili, *martus*, tunalipata neno la Kiingereza "shahidi." Neno hili lilikuwa na maana mbili:

1. shahidi (kama vile Luka 11:48; 24:48; Matendo ya Mitume 1:8,22; 5:32; 10:39,41; 22:15)
2. shujaa wa kidini (kama vile Matendo ya Mitume 22:20)

Maana zote hizi zilikuwa na uzoefu binafsi wa Mitume wengi na wengine wengi, na waamini wengi katika zama kipindi chote!

**26:17 "nikikuokoa"** Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo. Katika sauti irabu ya kati neno hili mara nyingi linamaanisha kuchagua ama kuamua. Mara kwa mara neno hili linatafsriwa "kumboa ama okoa" (kama vile Matendo ya Mitume 7:10,34; 12:11; 23:27). Mahusiano ya Mungu ya karibu yako dhahiri hapa. Paulo aliyapokea maono kadhaa kati ya haya wakati wa kuhudumu kwake kwa ajili ya kumtia moyo. Bila shaka hili linadokeza juu ya andiko la Agano la Kale la Kiebrania la Isa. 48:10 ama Yer. 1:7-8,19 pasipo shaka.

▣"**nikikuokoa na watu wako, na watu wa Mataifa**" Paulo alikumbana na upinzani kutoka katika makundi yote (kama vile 2Kor. 11:23-27).

▣"**ambao nakutuma kwao**" Neno "Mimi" ni la kimkazo (*egō*) kama ilivyo katika Matendo ya Mitume 26:15. Hiki ni kitenzi *apostellō* (kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo), ambapo tunalipata neno "Mtume." Kama Baba alivyomtuma Yesu, ndivyo Yesu alivyowatuma mashahidi wake, mitume (kama vile Yohana 20:21).

## MADA MAALUM: MAMLAKA (exousia)

- I. Matumizi ya Luka – Inatia shauku kuyachunguza matumizi ya Luka ya neno exousia (mamlaka, uweza, au haki ya kisheria).
  1. Katika Luka 4:6 Shetani anadai kuwa na uwezo wa kumpa Yesu mamlaka.
  2. Katika Luka 4:32,36 watu wa Kiyahudi walistaajabishwa namna Yesu alivyofundisha, kwa kutumia mamlaka yake binafsi.
  3. Katika Luka 9:1 Aliwapa uweza na mamlaka Mitume Wamke.
  4. Katika Luka 10:19 Aliwapa mamlaka wamisionari wake sabini.
  5. Katika Luka 20:2,8 kiini cha swali la mamlaka ya Yesu kinaulizwa.
  6. Katika Luka 22:53 uovu umeruhusu mamlaka ya kushtumu na kumuua Yesu.

Ijapokuwa si katika Luka, utangulizi wa injili ya Mathayo kuhusu Agizo Kuu (Mt. 28:18), "nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani," huu ni usemi wa mamlaka ya Yesu unaoshangaza.

Yesu alidai kuwa na mamlaka kwa sababu

1. maneno ya Mungu yaliyonenwa kwake katika
    - a. ubatizo wake (Luka 3:21-22)
    - b. kubadilika kwake (Luka 9:35)
  2. utimilifu wa unabii wa Agano la Kale
    - a. kabila la Yuda (kama vile Mwa. 49:10)
    - b. uzao wa Yese (kama vile 2 Samueli 7)
    - c. kuzaliwa kwake katika Bethlehemu (kama vile Mika 5:2)
    - d. kuzaliwa kwake wakati wa dora ya nne (Rumi) ya Danieli 2
    - e. alivyowasaidia maskini, vipofu, wahitaji (Isaya)
  3. kupunga kwake pepo kulifunua uweza wake na mamlaka juu ya Shetani na ufalme wake.
  4. kuwaansa waliolala mauti kulionyesha uweza wake juu ya maisha ya kimwili na mauti.
  5. miujiza yake yote aliufunua uweza wake na mamlaka mpangilio, utofauti, na muonekano.
    - a. Asili
    - b. Ulishaji
    - c. Uponyaji
    - d. kumbukumbu za kiakili
    - e. uvuaji wa samaki
- II. Matumizi ya Paulo ya neno "mamlaka" yalikusiana na wanawake wa ki-Kristo. Suala hili la mamlaka pia limejadilikwa katika 1 Wakorintho 11 katika uhusiano wa wanawake kufunika vichwa. Ufuatao ni muundo wa maelezo yangu yalioyopo hapa.

**1 Kor. 11:10 "Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani"** Matumizi ya mamlaka katika 1 Wakorintho yanaweza kueleweka katika njia kadhaa. Jambo la msingi (katika muktadha huu) ni "mamlaka" (exousia) gani yanayozungumziwa.

Kwanza, lazima ieleweke kwamba neno *exousia* mara nyingi lilihusiana na neno *dunamis* (uweza). Otto Betz ina makala yenye kuvutia kuhusu neno *exousia* katika *New International Dictionary of New Testament Theology*, juzuu 2, kr. 606-611. Hapa kuna mifano mitano.

"Sifa zake za Agano la Kale kwamba maneno *exousia* na *dunamis* yote yalikusikana na kazi ya Kristo, matukio ya mpangilio mpya wa nguvu ya umbile la kiulimwengu na kuwawezesha waamini" (uk. 609).

"Hili neno *exousia* kwa waamini. Mamlaka ya muumini wa ki-Kristo inapatikana katika utawala wa Kristo na kuvunja nguvu zote. Hili linamaanisha vyote uhuru na huduma" (uk. 611).

"Huyu yuko huru kwa kila kitu (1 Kor. 6:12; 10:23 *exestin*); dai hili, ambalo lilikuwepo tangu awali kupitia kwa wanaushawishi wa kimathehebu huko Korintho, lilipendelewa na Paulo ambaye alilithibitisha kwa usahii kabisat" (uk. 611).

"Katika utendaji, hata hiovyo, uhuru huu usiozuiliwa kinadharia unaongozwa kwa kwa fikra za kile chenye kuwasaidia Wakristo wengine na kusanyiko kama kama kitu kamili cha mtazamo wa ukweli kwamba ukombozi kamili bado unakuja (1 Kor. 6:12; 10:23)" (uk. 611).

"'Mambo yote ni ya kisheria [*exestin*] kwangu mimi,' lakini si mambo yote yenye kusaidia. 'Mambo yote ni ya kisheria [*exestin*],' lakini si mambo yote yenye kujenga. Mtu asiyatafute yaliyo mema tu, bali mema kwa ajili ya jirani yake" (1 Kor. 10:23 na kuendelea). Nukuu iliyo ndani ya nukuu hizi bila shaka ndio wito wa wa wanasheria huko Korintho. Paulo anawakabili kwa kuukubali ukweli wao, lakini kwa kuonyesha kwamba si ukweli kamili" (uk. 611).

Mara nyingi Paulo anatumia maneno haya mawili ndani ya barua zake kwa kanisa la Korintho.

1. *exousia*, 1 Kor. 7:37; 9:4,5,6,12 (mara mbili),18; 11:10; 2 Kor. 13:10
2. *dunamis*, 1 Kor. 1:18; 2:4,5; 4:19,20; 5:4; 15:24,43; 2 Kor. 4:7; 6:7; 8:3 (mara mbili); 12:9; 13:4 (mara mbili)

Haki na uweza yalikuwa mambo makuu kwa wate wanasheria na wanahaki. Paulo anajaribu kutembea katika mstari uliyonyooka katika ya kingo zote. Katika muktadha huu wanawake wa ki-Kristo wanasisitizwa kuyakubali maagizo ya Mungu ya uumbaji yaliyotolewa (yaani, Kristo-mwanadamu-mwanamke) kwa makusudi ya ufalme wa baadaye. Paulo anaeleza juu ya makubaliano halisi (kama vile Mwa. 1:26-27; 2:18) katika mistari ya 1 Kor. 11:11-12. Hili ni la hatari kithiolojia

1. kutenga mstari mmoja katika muktadha huu
2. kutumia mabadiliko ya mawasiliano ya madhehebu ya kifumo katika suala hili la mahusiano ya wanaume na wanawake/waume kwa wake wa karne ya kwanza kwa kila utamaduni katika kila karne
3. kuukosa ulinganifu wa Paulo baina ya uhuru wa Mkristo na agano la wajibu wa ushirika wa Mkristo.

Wanawake wa ki-Kristo walipata wapi uhuru wa kushiriki kama viongozi katika ibada za kusanyiko (yaani, kanisa la nyumbani)? Hakika si kutoka katika sinagogi. Ni mwelekeo gani wa kiutamaduni utokanao na jamii ya Kirumi ya karne ya kwanza? kwa hakika hilinawezekana na katika mtazamo wangu hili linasaidia kueleza juu ya mitazamo yangu ya sura hii. Hata hivyo, pia inawezwekamna kwamba nguvu ya injili, ujurejesho wa "sura na mfano wa Mungu" halisi uliopotea katika Anguko, hiki ndicho chanzo. Kuna kiwango cha ubora mpya wenye kuogopesha katika maeneo yote ya maisha ya mwanadamu na jamii. Lakini usawa huu unaweza kurudishwa ndani ya bima kwa ajili ya matumizi mabaya binafsi. Upanuzi huu usiofaa ndiyo Paulo anaoujelezae.

F. F. Bruce, *Answers to Questions*, kwa ujkweli amenisaidia kufikiri kupitia mambo mbalimbali ya kimkanganyiko yalijumuisha mapokeo ya kanisa la Ukristo wa sasa wa magharibi. Kama ulivyo ufafanuzi wa maandiko matakatifu mara nyingi nimekuwa nikifikiria kwamba wanawake kujifunika ilimaanisha kuonyesha karama ya Mungu (au usawa wa pade mbili wa Mwa. 1:26,27), si mamlaka wa mume wake. Hata hivyo, Nisingepata tafsiri hii miongoni wa vyanzo vya kibiblia nivitumiavyo, hivyo, Nilisita kuliweka hili katika maoni au kulihubiri/kulifundisha. Bado nakumbuka msisimko na uhuru niliokuwa nikiusikia wakati F. F. Bruce alipofikiria kitu kile kile (tazama *Answers to Questions*, uk. 95). Nafikiri waamini wote wanaitwa, kwa wakati wote, wamekirimwa kuwa watumishi wa Kristo (kama vile Efe. 4:11-12)!

**26:18 "uwafumbue. . .wageuke"** Zote ni kauli zisizo na ukomo za wakati uliopita usio timilifu. Haya yanaweza kuwa maelezo ya Isa. 42:7. Masihi atafungua macho yaliyopofuka kama sitiari ya kufungua macho ya kiroho (kama vile Yohana 9). Maarifa ya injili na uelewa lazima utangulie wito wa muitikio wa kujitolea (toba na imani). Shetani

anajaribu kufunga ufahamu na mioyo (kama vile 2 Kor. 4:4) na Roho anajaribu kuwafungua (kama vile Yohana 6:44,65; 16:8-11).

▣"**waiache giza. . . nguvu za Shetani**" Tazama usambamba. "utawala" ni neno la Kiyunani *exousia*, siku zote linafasiriwa kama mamlaka na nguvu (kama vile matoleo ya NKJV, NRSV, TEV). Ulimwengu upo chini ya ushawishi wa uovu binafsi (kama vile Efe. 2:2; 4:14; 6:10-18; 2 Kor. 4:4; Kol. 1:12-13, angalia Mada Maalum katika Mdo. 5:3). Katika Agano la Kale na hasa nabii za Isaya, Masihi (angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:31) alitakiwa kuleta uono kwa wasioona (vipofu). Ilikuwa vyote utabiri wa kimwili na pia sitiari za ukweli (kama vile. Isa. 29:18; 32:3; 35:5; 42:7,16)

▣"**kwa nuru . . . kwa Mungu**" Tazama usambamba. Wanadamu wa Kale waliogopa giza. Ilikuwa ni sitiari ya uovu. Nuru katika namna nyingine ilikuwa ni sitiari ya kweli, uponyaji na usafi. Kifungu cha habari chenye usambamba mzuri juu ya nuru ya injili ni Yohana 3:17-21.

▣"**kwamba waweze kupokea**" Kitenzi katika tungo hii ni kauli isiyo na ukomo ya wakati uliopita usiotimilifu. Hakuna "labda" katika maandiko ya Kiyunani (kama vile matoleo ya TEV, NJB). Sharti pekee katika muktadha huu ni tungo "kwa imani katika Mimi", ambayo inawekwa mwisho katika sentensi ya Kiyunani kwa ajili ya msisitizo. Baraka zote za Mungu zinategemeana na mwikio katika imani (yaani kupokea, kama vile Yohana 1:12) Kwa neema yake (kama vile Efe. 2:8-9). Hii ni jambo linaloletwa la masharti ya kiagano katika Agano la Kale.

▣"**msamaha wa dhambi**" Luka anatomia neno hili (*aphesis*) mara kwa mara. Katika Luka 4:18 linatumika katika nukuu kutoka Isa. 61:1, ambapo linamaanisha kuachilia LXX matumizi ya Kutoka. 18:2 na Mambo ya Walawi. 16:26.2. Katika Luka 1:77; 3:3; 24:47; Mdo. 2:38; 5:31; 10:43; 13:38; 26:18, inamaanisha "uondoaji wa hukumu ya dhambi," ambayo inaaksi LXX matumizi ya Kumb. 15:3, ambapo linatumika kuhusu kuondolewa kwa deni. Matumizi ya Luka yanaaksi ahadi ya Agano Jipya ya Yer. 31:34.

▣"**na urithi**" Hili ni neno la Kiyunani *klēros*, ambalo linamaanisha kupiga kura (kama vile Law. 16:8; Yonah 1:7; Mdo 1:26) kuamua urithi, kama katika Mwanzo 48:6; Kutoka 6:8; na Yoshua 13:7-8. Katika Agano la Kale Walawi hawakuwa na ardhi ya kurithi isipokuwa katika miji ya kilawi 48 (kama vile Kumb. 10:9; 12:12), lakini Bwana mwenyewe alikuwa urithi wao (kama vile Hesabu 18:20). Sasa katika Agano Jipya Waamini wote ni makuhani (kama vile 1 Petro 2:5,9; Ufu. 1:6). Bwana (YHWH) ndiye urithi wetu; sisi tu watoto wake (kama vile Rum. 8:15-17).

▣"**wale waliotakaswa**" Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati ulio timilifu. Waaminio (Watu walioshikilia imani) wamekuwa wakiendelea na kuendelea kutakaswa kwa imani katika Kristo (kama vile Mdo. 20:21). Angalia Mada Maalum katika Mdo.9:32. Sio shetani wala mapepo yawezayo kuchukua hili mbali nasi au kutunyang'anya (kama vile Rum. 8:31-39).

#### **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 26:19-23**

<sup>19</sup> Kwa hiyo, Ee Mfalme Agrippa, sikuyaasi yale maono ya mbinguni, <sup>20</sup> bali kwanza niliwahubiri wale wa Dameski na Yerusalemu, na katika nchi yote ya Uyahudi, na watu wa Mataifa, kwamba watubu na kumwelekea Mungu, wakiyatenda matendo yanayopata na kutubu kwao. <sup>21</sup> Kwa sababu ya hayo Wayahudi wakanikamata ndani ya hekalu wakajaribu kuniua. <sup>22</sup> Basi kwa kuwa nimeupata msaada utokao kwa Mungu nimesimama hata leo hivi nikiwashuhudia wadogo kwa wakubwa, wala sisemi neno ila yale ambayo manabii na Musa waliyasema, kwamba yatakuwa; <sup>23</sup> ya kwamba Kristo hana budi kuteswa na ya kwamba yeye kwanza kwa kufufuliwa katika wafu atatangaza habari za nuru kwa watu wake na kwa watu wa Mataifa.

**26:19 "Hivyo Mfalme Agrippa"** Angalia dokezo katika Mdo 25:13, utangulizi. Paulo alikuwa anajaribu kumfikia mtu huyu kwa injili (kama vile 26:26-29).

▣ **"sikuacha kutii"** Neno la Kiyunani *peithō* linatoka katika jina la kutafuta miungu ya ushawishi. Katika muktadha huu wa kiambishi awali hasi, ambacho kinahasisha, kwa kuashiria "kutotii" (kama vile Luka 1:17; Rum. 1:30; 2 Tim. 3:2; Tito 1:16; 3:3). Hivyo, katika nmna ya nji ya ulazimishaji wa lugha ya Koine ya Kiyunani kukanusha kitu, lakini katika muktadha huu ni njia ya kifasihi ya kukiri utii wa Paulo!

▣ **"maono ya kimbingu"** Hii inamaanisha kukutana kwa Paulo na Kristo aliyetukuzwa mfufuka akiwa njiani Dameski.

**26:20 "Dameski. . Yerusalemu"** Angalia Mdo. 9:19-25,27 kwa ajili ya hududuma ya Paulo katika Dameski; 9:26-30 kwa ajili ya huduma ya Paulo katika Yerusalemu na yawezekana 9:31 kwa huduma ya Paulo Yudea.

▣ **"tubuni na kumgeukia Mungu"** Ujumbe wa Paulo (kama vile Mdo. 20:21) ilikuwa sawa na

1. Yohana Mbatizaji (kama vile Mt. 3:1-12; Marko 1:4-8)
2. Ujumbe wa kale wa Yesu (kama vile Marko. 1:15)
3. Petro (kama vile Mdo. 3:16,19)

Neno la Kiyunani linamaanisha kubadili ufahamu. Neno la Kiebrania linamaanisha kubadili matendo. Yote yanajumuisha toba ya kweli. Angalia Mada ya kweli katika Mdo. 2:38. Mahitaji mawili ya Agano Jipya (ambayo pia ni mahitaji ya Agano la Kale) kwa ajili ya wokovu ni toba (kugeuka kutoka katika ubinafsi na dhambi) na imani (kumgeukia Mungu na Kristo).

▣ **"Kuenenda kupasavyo toba"** Mtindo wa maisha ya mwamini (kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo) yanathibitisha/imani yake ya kujitoka ya mwanzo (kama vile Mt. 3:8; Luka 3:8; Efe. 2:8-10, Yakobo na 1 Yohana). Mungu anawataka watu wake ambao wanaaksi tabia yake. Waaminio ambao wameitwa kuja kufanana na Kristo (kama vile Rum. 8:28-29; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 2:10). Injili ni

1. mtu wa kumwalika
2. ukweli kuhusu mtu huyo kuamini
3. aina ya maisha ambayo mtu huyo anapaswa aishi

**26:21** Hayakuwa maoni yap Paulo ya kithiolojia , lakini mahubiri yake kwa na ujumuishi wa "mataifa" (kama vile Mdo. 26:20) ambayo ilisababisha ghasia katika hekalu.

▣ **"walijaribu kuniua"** Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati usio timilifu (yenye ushahidi) (iliyojaribiwa tena na tena) ikiwa na kauli isiyo na ukoo ya wakati uliopita usio timilifu (kuua). Wayahudi (kama vile Mdo. 9:24) kutoka Asia (kama vile Mdo. 20:3,19; 21:27,30) wakijaribu kumuua Paulo mara kadhaa.

**26:22 "kuwashuhudia wote wakubwa na wadogo"** Hii ni nahau jumuishi ya. Ni ukiri wa Paulo (kama wa Petro, kama vile Mdo. 10:38) kwamba yeye kama Mungu sio mwenye upendeleo (kama vile Kumb. 10:17; 2 Nyakati 19:7, angalia dokezo kamili katika Mdo. 10:34). Anahubiri kwa wanadamu wote.

▣ **"sikusema kitu lakini kile ambacho manabii na Musa walisema"** Paulo anaelezea kuwa ujumbe wake na hadhira (yaani mataifa) sio wa kubuni, lakini unabii wa Agano la Kale. Anachofanya ni kufuata mwongozo wa Agano la Kale (angalia Mada Maalum katika Mdo. 1:8), ahadi na kweli.

**26:23** Tazama kwamba ujumbe wa Paulo ulijumuisha sehemu tatu:

1. Masihi aliteseka kwa ajili ya msamaha wa wanadamu
2. ufufuo wa Masihi ulikuwa matunda ya kwanza ya ufufuo wa waaminio
3. Habari hii njema ilikuwa kwa ajili ya Wayahudi na mataifa

Hizi sehemu tatu za kithiolojia ikiunganishwa na mstari wa 20 ambayo inaonesha kwa namna gani sisi binafsi tunampokea Kristo (toba, kugeuka kutoka katika ubinafsi na dhambi; imani, kumgeukia Mungu katika Kristo).

▣ **"kwamba Kristo alipaswa kuteseka"** Kwa ajili ya msingi wa hoja za kithiolojia za mahubiri ya kitume katika Matendo ya Mitume angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:14. Ilikuwa kizuizi kwa Wayahudi (kama vile Kor. 1:23), lakini ilikuwa ni utabiri wa Agano la Kale (kama vile Mwanzo 3:15; Zaburi 22; Isaya 53). Kweli hii inapatikana katika Luka 24:7,26,44-47. Kiyunani "Kristo" inaaksi cheo cha Kiebrania "Masihi." Paulo anaelezea kwamba Yesu aliyesulubiwa alikuwa kweli Kristo, Aliyehaidiwa, mpakwa Mafuta (kama vile Mdo. 2:36; 3:6,18,20; 4:10,26; 13:33; 17:3; 26:23, angalia Mada Maalum: Masihi katika Mdo. 2:31).

▣ **"kwamba kwa sababu ya ufufuo wake kutoka katika wafu"** Kwasababu ya andiko hili na Rum.1:4, pale pakaibuka uvumi wa kwanza "nadharia ya kuchukuliana" (angalia dibaji), ambayo ilielezea kwamba Yesu wa kibinadamu alitunukiwakwa ajili ya maisha mazuri kwa kufufuliwa kutoka katika awafu. Hata hivyo elimu na nadharia hii ilipuuza maandiko yote kuhusu kuwepo kwake hapo kabla kama vile Yohana 1:1; Flp. 2:6-11; Kol. 1:15-17; na Ebr. 1:2-3. Yesu amekuwepo siku zote; Amekuwepo Mungu siku zote; Yeye alifanyika mwili kwa muda ufaao.

▣ **"nuru"** Nuru ni sitiari ya kale ya kweli na usafi (kama vile Mdo. 26:18; Isa. 9:2; 42:6-7).

▣ **"kwa Wayahudi na kwa Mataifa"** Kuna injili moja kwa makundi yote (kama vile Efe. 2:11- 3:13). Hii ilikuwa ni maajabu ambayo yalikuwa yamefichwa kutoka katika vizazi. Wanadamu wote wamefanywa kwa sura ya Muumbaji mmoja Mungu (kama vile Mwanzo 1:26-27). Mwanzo 3:15 ahadi kwamba Mungu atatoa wokovu kwa wanadamu walioanguka. Isaya anakiri U-Masihi wa kiulimwengu (mfano Isa. 2:2-4; 42:4,6,10-12; 45:20-25; 49:6; 51:4; 52:10; 60:1-3; na pia Mika. 5:4-5).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 26: 24-29**

<sup>24</sup> Alipokuwa akijitetea hivi, Festo akasema kwa sauti kuu, Paulo, una wazimu, kusoma kwako kwingi kumekugeuza akili. <sup>25</sup> Lakini Paulo akasema, Sina wazimu, Ee Festo mtukufu, bali nanena maneno ya kweli na ya akili kamili. <sup>26</sup> Kwa maana mfalme anajua habari za mambo haya, nami naweza kusema naye kwa ujasiri, kwa sababu najua sana ya kuwa hapana neno moja katika hayo asilolijua; kwa maana jambo hilo halikutendeka pembeni. <sup>27</sup> Mfalme Agripa, je! Wawaamini manabii? Najua ya kuwa wawaamini. <sup>28</sup> Agripa akamwambia Paulo, Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo. <sup>29</sup> Paulo akamjibu, Namwomba Mungu kwamba, ikiwa kwa machache au ikiwa kwa mengi, si wewe tu ila na hao wote wanaonisikia leo wawe kama mimi, isipokuwa vifungo hivi.

**26:24 "Festo akasema kwa sauti kuu "** Ujumbe wa Paulo haukuwa wa kuaminika kwake. Mtazamo wake na tamaduni, elimu na nafasi iliyobagua uwezo wake wa kuelewa.

▣ **"kusoma kwako kwingi kumekugeuza akili"** Kwa namna ya mzunguko hii inaonesha, uwazi na ushawishi wa utetezi wa Paulo.

**26:25 "ya akili kamili"** Neno la Kiyunani *sōphrosunē* inatoka katika maneno mawili ya kiyunani, "yenye afya" na "ufahamu." Inamaanisha mkabiliano wa mizani kwa maisha na kufikiri. Ni kinyume "nje ya ufahamu" na "iliyochanganyikiwa" (kama vile Mdo. 26:24).

▣ **"kweli"** Angalia Mada Maalum hapa chini.

#### **MADA MAALUM: "KWELI" KATIKA MAANDIKO YA PAULO**

Matumizi ya Paulo ya neno hili na muundo wake wenye uhusiano yanatokana na usawa wake wa Agano la Kale, neno *emet*, linamaanisha uaminifu au mwaminifu (BDB 53; tazama Mada Maalum: Amini, Sadiki, Imani, na Uaminifu katika Agano la Kale). Katika maandiko ya Kiyahudi ya Kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya

neni hili lilitumika kuzungumzia ukweli katika kutofautisha uongo. Labda ufanano wa karibu wa "Nyimbo za Shukrani" ilikuwa katika Magombo ya Kale ya Bahari ya Chumvi ambapo ufanano huu unatumika katika mafundisho yaliyofunuliwa". Wana Jumuiya ya Essene wakawa "maishahidi wa ukweli huu. "

Paulo anatumia neno hili kama njia ya kuirejelea injili ya Yesu Kristo.

1. Warumi 1:18,25; 2:8,20; 3:7; 15:8
2. 1 Wakorintho 13:6
3. 2 Wakorintho 4:2; 6:7; 11:10; 13:8
4. Wagalatia 2:5,14; 5:7
5. Waefeso 1:13; 6:14
6. Wakolosai 1:5,6
7. 2 Wakolosai 2:10,12,13
8. 1 Timotheo 2:4; 3:15; 4:3; 6:5
9. 2 Timotheo 2:15,18,25; 3:7,8; 4:4
10. Tito 1:1,14

Pia Paulo analitumia neno hili kama njia ya kueleza kunena kwake kwa usahihi/uaminifu

1. Matendo ya Mitume 26:25
2. Warumi 9:1
3. 2 Wakorinto 7:14; 12:6
4. Waefeso 4:25
5. Wafilipi 1:18
6. 1 Timotheo 2:7

Huyu pia analitumia neno hili kueleza shauku yake katika 1 Kor. 5:8 na maisha (pia kwa Wakristo wote) katika Efe. 4:24; 5:9; Flp. 4:8. Wakati mwingine analitumia neno hili kuzungumzia watu.

1. Mungu, Rum. 3:4 (kama vile Yohana 3:33; 17:17)
2. Yesu, Efe. 4:21 (sawa sawa na Yohana 14:6)
3. Ushahidi wa ki-Utume, Tito 1:13
4. Paulo, 2 Kor. 6:8

Paulo anatumia muundo pekee wa KITENZI (yaani, *alētheuō*) katika Gal. 4:16 na Efe. 4:15, ambapo linairejelea injili. Kwa usomaji zaidi fuatilia Colin Brown (ed.), *The New International Dictionary of New Testament Theology*, juzuu 3, kr. 784-902.

**26:26-28 "Kwa maana mfalme anajua habari za mambo haya"** Kume kuwa na mjadala kubwa kuhusu mistari hii. Inavyoonekana Paulo alitaka kumtumia Agrippa II kuthibitisha ushuhuda wake na ikiwezekana amlete kwenye kukubali ukweli wake. Mstari wa 28 inaweza kufasiriwa, "Je unataka kunifanya shuhuda wa Ukristo?"

**26:26 "nami naweza kusema naye kwa ujasiri"** Luka mara kwa mara anatumia neno hili, siku zote linaunganishwa na Paulo (kama vile Mdo. 9:27,28; 13:46; 14:3; 18:26; 19:8). Siku zote inafasiriwa "kuzungumza kwa ujasiri" (kama vile 1 The. 2:2). Hii ni moja ya udhihirisho wa ujazo wa Roho Mtakatifu. Ilikuwa ni moja ya makusudi ya maombi ya Paulo katika Efe. 6:20. Tangazo la Injili kwa ujasiri ni lengo la Roho kwa kila mwamini.

▣ **"kwa maana jambo hilo halikutendeka pembeni"** Petro alitengeneza maelezo haya haya tena na tena kwa wasikiaji wake katika Yerusalemu (kama vile Mdo. 2:22,33). Kweli ya injili zilihakikiwa na historia.

**26:27** Paulo alifahamu kwamba Agrippa alikuwa akilikubali Agano la Kale. Paulo anaweka madai kwamba ujumbe wake wa injili ilikuwa wazi inatambuliwa kutoka katika maandiko ya Agano la Kale. Haikuwa ujumbe "moya" au "kubuni"! Ilikuwa ni unabii unaotimizwa.

**26:28**

**NASB** "Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo "

**NKJV** "Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo "

**NRSV** "Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo "



TEV "Kwa muda huu machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo "  
NJB "kwa muda mchache, hoja zako wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo"

Huu ulikuwa ni mbadala wa kimsamiati *oligō* (maana yake ndogo au ndogo zaidi), "kwa muda mfupi" (toleo la NASB, NRSV, TEV), au "kwa nguvu kidogo" (NKJV, NJB). Mchanganyiko huu pia unaonekana katika Mdo. 26:29. Ipo pia utofauti wa kimaandiko unaohusiana na tungo hii: "kufanya" au "kufanya" (*poieō*) katika maandiko P<sup>74</sup>, x, A (UBS<sup>4</sup> inatoa alama ya "A"), au "kufanyika" katika MS E na fasiri za Vulgate za Peshitta. Maana katika Muktaadha kubwa ni wazi. Paulo alitaka kuwasilisha injili kwa namna ya kwamba wale wote waliojua na kikiri Agano la Kale (Agrippa) angeweza kuletwa katika usawishi au katika uangalau, kukiri umuhimu wa nabii hizi za Agano la Kale.

▣ **"Wakristo"** Watu wa "Njia" (wafuasiwa Kristo) waliitwa Wakristo hapo kwanza Antiokia huko Siria (kama vile Mdo. 11:26). Eneo lingine ambapo jina hili linatokea katika Matendo ya Mitume ni katika midomo ya Agrippa II, ambalo linamaanisha kuwa jina lilikuwa limekua sana kwa kujulikana.

**26:29 "Namwomba Mungu kwamba"** Mstari wa 29 ni sentensi yenye masharti daraja la nne (*an* pamoja na hali ya kimbadala), ambayo inaelezea shauku ambayo inaweza kuja kwenye kweli. Mara nyingi ni maombi au matamano. Paulo alitamani wasikilizaji wake, wa Kirumi na Kiyahudi wangukuwa wa imani katika Kristo kama yeye mwenyewe.

#### ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 26:30-32

<sup>30</sup> Mfalme na liwali na Bernike na wale walioketi pamoja nao wakasimama; <sup>31</sup> hata walipoondoka wakasemezana, wakisema, Mtu huyu hatendi neno linalostahili kifo wala kufungwa. <sup>32</sup> Agripa akamwambia Festo, Mtu huyo angeweza kufunguliwa, kama asingalitaka rufani kwa Kaisari

**26:30** Ni kwa namna gani Luka alipata taarifa hizi? Yalikuwa ni maongezi ya binafsi baina ya viongozi wa kiserikali (na familia zao).

1. mfanyakazi alisikia haya na kumtaarifu Luka?
2. Luka anadhanika kile walichokisema kwa kauli iliyotokea kufanana na mazungumzo yao
3. Luka anatumia fursa hii kuimarisha kimakusudi yake ya kifasihi kwa kuonesha kwamba sio Paulo au Ukristo ulio tishio kwa Rumi

**26:31-32 "Mtu huyo angeweza kufunguliwa, kama asingalitaka rufani kwa Kaisari"** Hii inaonesha moja ya kusudiu kubwa la kuandikwa kwa Matendo ya Mitume, ambalo lilikuwa ni kuonesha kwamba Ukristo haukuwa jambo lenye uelekeo wa uhaini kwa Rumi. Hii ni sentensi yenye masharti daraja la pili inayotoa maelezo ya uongo kuendeleza ukweli. Mtu huyu inawezekana aliwekwa huru (jambo ambalo halikuwa hivyo) kama asingeweza kukata rufani kwa Kaisari (jambo ambalo hakulifanya).

#### MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri. Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa jinsi gani kujitetea huku kunatofautiana na kule kujitetea mbele ya Festo na Feliki?
2. Ni kwa jinsi gani ushuhuda binafsi wa Paulo unaendana na utetezi wake wote?
3. Kwa nini Masihi ateswaye haeleweki kwa Wayahudi?
4. Kwa nini mstari wa 28 ni mgumu sana kuutafsiri?
5. Ni kwa jinsi gani mjadala wa Festo, Agripa na Bernike (Matendo ya Mitume 26:30-31) unaendana na muundo wa kimaandishi wa makusudi ya Luka katika Matendo ya Mitume?

## MATENDO YA MITUME 27

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Paulo anatabiri	safari ya Rumi	safari kwenda Malta	Paulo kwenda Rumi	safari kuelekea Rumi
Kwenda Rumi				
27:1-8	27:1-8	27:1-8	27:1-6	27:1-3 27:4-6
	Onyo la Paulo Linapuuzwa		27:7-8	27:7-8
27:9-12	27:9-12	27:9-12	27:9-12	27:9-12
Dhoruba baharini	katika dhoruba		dhoruba baharini	dhoruba na kupinduka Kwa melikebu
27:13-20	27:13-38	27:13-20	27:13-20	27:13-20
27:21-26		27:21-26	27:21-26	27:21-26
27:27-32		27:27-32	27:27-32	27:27-32
27:33-38		27:33-38	27:33-38	27:33-38
Kuangamia kwa melikebu	kuangamia kwa melikebu huko Malta		kuangamia kwa melikebu	
27:39-44	27:39-44	27:39-44	27:39-41 27:42-44	27:39-41 27:42-44

### **MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka ["Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"](#) ("[A Guide to Good Bible Reading](#)")

#### ***KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembeke katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

- A. Luka alikuwa na maarifa makubwa yaliyohusu ubaharia (A. T. Robertson, *Word Pictures in the New Testament*, vol. 3, ukurasa wa 456, anasema Luka anatumia ambatani tisa pamoja na *pleō*, kusafiri majini) pia pamoja na fasihi, dawa, historia na thiolojia. Hii hapa ni orodha ya maneno na tungo za kiufundi na kibaharia
1. Kug'oa (kama vile Mdo. 13:4; 14:26; 20:15;27:1)
  2. chini ya (kama vile Mdo. 27:4,7)
  3. kug'oa nanga (kama vile Mdo. 27:13)
  4. *eurquilo* (kama vile Mdo. 27:14)
  5. kushindana na upepo (kama vile Mdo. 27:15)
  6. tukipita chini (kama vile Mdo. 27:16)
  7. kuikaza chini (kama vile Mdo. 27:17)
  8. nanga ya bahari (*skeuos*) (kama vile Mdo. 27: 17)
  9. vyombo vya merikebu (*skeuēn*) (kama vile Mdo. 27:19)
  10. bildi (kama vile Mdo. 27:28[mara mbili])
  11. pima(kama vile Mdo. 27:28[mara mbili])
  12. nanga nne kutoka katika pande za nyuma (kama vile Mdo. 27:29,40)
  13. kamba za usukani (kama vile Mdo. 27:40)
  14. kutweka nanga kabla ya safari kuelekea katika upepo (kama vile Mdo. 27:40)
  15. kubisha/kwenda zigizaga (MSS P<sup>74</sup>, X, A, kama vile Mdo. 28:13)
- B. Kitabu kimoja cha kale ambacho kimekuwa msaada mkubwa kwa Wafasiri ni kile cha James Smith's *The Voyage and Shipwreck of St. Paul*, 1848.
- C. Safari hii ya Rumi ilikuwa ikifanywa wakati wa hatari wa kusafiri katika mwaka (kama vile Mdo. 27:1,4,7,9,10,14). Mara nyingi Novemba-Februari ulikuwa muda hatari kusafiri, pamoja na ukingoni mwa kipindi cha wiki mbili mpaka tatu za kabla na baada. Kusafirishwa kwa melikwa nafaka kawaida kuelekea Rumi kulichukua siku kumi mpaka kumi na nne, lakini kwasababu ya uelekeo wa upepo kurudi kungechukua siku sitini.
- D. Kuna aina za meli tatu tofauti yawezekana hata nne zinazotajwa katika kifung hiki cha habari
1. Meli ya pwani ambayo iligoa kila bandari na kupita ukingoni sambamba na pwani.
  2. Meli mbili za nafaka za Kimisri ambazo zilichukua nafaka kutoka Misri kupeleka Italia
  3. Yawezekana meli kubwa kati ya Naples na kugoa nchi kavu maili 43 kusini mwa Rumi

Inashangaza kufuatilia hadithi ya Luka ya safari hii kwenye ramani ya Shamu.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 27:1-8

<sup>1</sup> Basi ilipoamriwa tuabiri hata Italia, wakamtia Paulo na wafungwa wengine katika mikono ya akida mmoja, jina lake Yulio, wa kikosi cha Augusto. <sup>2</sup> Tukapanda katika merikebu ya Adramitio iliyokuwa tayari kusafiri mpaka miji ya pwani za Asia, tukatweka; Aristarko, Mmakedonia wa Thesalonike, akiwa pamoja nasi. <sup>3</sup> Siku ya pili tukawasili Sidoni; Yulio akamfadhili sana Paulo akampa ruhusa kwenda kwa rafiki zake, apate kutunzwa. <sup>4</sup> Kutoka huko tukatweka, tukasafiri chini ya Kipro ili kuukinga upepo, kwa maana pepo zilikuwa za mbisho. <sup>5</sup> Tulipopita bahari ya upande wa Kilikia na Pamfilia, tukafika Mira, mji wa Likia. <sup>6</sup> Na huko yule akida akakuta merikebu ya Iskanderia, tayari kusafiri kwenda Italia, akatupandisha humo. <sup>7</sup> Tukasafiri polepole kwa muda

**wa siku nyingi, tukafika mpaka Nido kwa shida; na kwa sababu upepo ulikuwa ukituzua tukapita chini ya Krete, tukaikabili Salmone. <sup>8</sup> Tukaipita kwa shida, pwani kwa pwani, tukafika mahali paitwapo Bandari Nzuri. Karibu na hapo pana mji uitwao Lasea.**

**27:1 "Basi ilipoamriwa tuabiri hata Italia"** Festo aliwatuma wakati wa hatari wa mwaka kwa ajili ya kugoa. Hii neno "sisi" inamaanisha Paulo na Luka (yawezekana na wengine). Wengi wa "sisi" vipengele vya Matendo ya Mitume vina sehemu ya safari za kibaharia (kama vile Mdo. 16:10-17; 20:5-15; 21:1-18; 27:1-28:16).

▣ **"Wafungwa wengine"** Hatujui chochote kuhusu wao isipokuwa walikuwa wafungwa wa kifalme waliokuwa wakielekea Rumi.

▣ **"akida"** Watu hawa siku zote wanawasilishwa na maneno hasi katiuka Agano Jipya (kama vile Mt. 8; Luka 7; 23:47; Mdo. 10; shutuma za Paulo, 21-28).

▣ **"wa kikosi cha Augusto"** Walidhaniwa kuwa wajumbe wa kiofisi kati ya Rumi na majimbo (kama vile W. M Ramsay, *St. Paul the Traveler and Roman Citizen*, ukurasa 315, 348), lakini hili ni kisio ambalo halijaandikwa tu kabla ya Mfalme Hadrian (117-138 b.k.).

**27:2 "merikebu ya Adramitio"** Hii ilikuwa ni meli ya pwani ambayo ilisimama katika kila bandari. Bandari ya nyumbani ya meli hii ilikuwa ni bandari bahari ya Asia Ndogo. Hii ni hatua ya kwanza ya safari ndefu na hatari kwa Rumi.

▣ **"Aristarko"** Nyumbani kwake palikuwa ni Thessalonika; yawezekana alikuwa anarudi nyumbani (kama vile Mdo. 19:29; 20:4; Kol. 4:10; Filemoni 24). Labda alikuwa anasindikizwa na Sekunda (kama vile Mdo. 20:4 na baadhi ya baadhi ya maandiko ya Kiyunani ya mstari huu).

**27:3 "Sidoni"** Huu ni Mji wa ambao upo maili sitini na saba kaskazini mwa Kaisaria. Ulikuwa mji wa kale wa Foenike, lakini kwa siku nyingi ulikuwa umekwisha pitwa na Tiro.

NASB	"kwa kujali"
NKJV, NRSV	"kwa upole"
TEV	"alikuwa mpole"
NJB	"alikuwa anajali"

Hili ni neno ambatani kutoka "upendo" (*philos*) na "ubinadamu" (*anthrōpos*). Neno linatumika mara mbili katika Matendo ya Mitume, nomino katika Mdo. 28:2 (kama vile Tito 3:4) na kihisishi hapa katika Mdo. 27:3. Yulio alikuwa mtu anayejali na mwenye huruma (kwa namna fulani wa kushangaza kwa wanajeshi walioko kazini). Yeye yumkini alikuwa amesikia kuhusu kesi ya Paulo.

▣ **"rafiki zake"** Hii yawezekana inamaanisha Wakristo wa kule. Yulio alimwamini Paulo lakini yawezekana mlinzi wa Kirumi alikwenda pamoja naye.

▣ **"akamfadhili"** Maandiko hayasemi kibayana ni fadhila za namna gani (kihisia, kimwili, kifedha).

**27:4 "chini ya Kipro"** Hii ni tungo inayochanganya kwasababu inafanya wasomaji wa lugha ya kiingereza wafikirie "kusini mwa Kipro," lakini kiukweli, ilimaanisha Kaskazini. Majina mengina yanayotajwa yapo kusini na pwani ya magharibi mwa Uturuki ya sasa.

**27:6 "merikebu ya Iskanderia, tayari kusafiri kwenda Italia"** Hii ilikuwa ni meli kubwa (ilikuwa na uwezo wa kubeba watu 276 pamoja na kiwango kikubwa cha nafaka) kutoka Misri kuelekea Rumi. Wakisasa wanajua meli

hizi kutokana na picha katika kuta za Pompeii na kutoka katika maandiko ya Lucia, karibia miaka ya 150 b.k. Mira ilikuwa bandari kubwa kwa ajili ya meli hizi kubwa za nafaka.

**27:7 "Kilikia"** Huu ulikuwa mji huru wa ubaharia kusini magharibi mwa pwani ya jimbo la Kirumi la Asia. Meli nyingi zilizokuwa zinashikiliwa na Rumi zilitumia bandari hii (kama vile Thucydides, *Hist.* 8.35). Ulikuwa na bandari mbili kwasababu ulikuwa umewekwa mahali pa rasi.

▣**"Salmone"** Huu ulikuwa ni mji mashariki mwa ncha ya kisiwa cha Krete. Kwasababu ya muda wa mwaka walijaribu kufanya kazi katika magharibi yao kwa kutia naga karibu na kisiwa.

**27:8 "Bandari Nzuri"** Hii ni ghuba karibu na Kusini mwa mji wa Lasea huko Krete. Haikuwa bandari lakini ghuba. Ingeweza kuwa vigumu sana kukaa hapa wakati wote wa baridi.

**ANDIKO LA NASB(LILILOBRESHWA) MATENDO YA MITUME 27:9-12**

<sup>9</sup> Na wakati mwingi ulipokwisha kupita, na safari ikiwa ina hatari sasa, kwa sababu siku za kufunga zilikuwa zimekwisha kupita, Paulo akawaonya, <sup>10</sup> akawaambia, Wanaume, naona kwamba safari hii itakuwa na madhara na hasara nyingi, si ya shehena na merikebu tu, ila na ya maisha yetu pia. <sup>11</sup> Lakini yule akida akawasikiliza nahodha na mwenye merikebu zaidi ya yale aliyoyasema Paulo. <sup>12</sup> Na kwa sababu bandari ile ilikuwa haifai kukaa wakati wa baridi, wengi wao wakatoa shauri la kutweka kutoka huko ili wapate kufika Foinike, kama ikiwezekana, na kukaa huko wakati wa baridi; nayo ni bandari ya Krete, inaelekea kaskazini-mashariki na kusini-mashariki.

**27:9** Kuna nyakati Fulani za mwaka (miezi ya baridi) wakati wa maporomoko ya upesi ya dhoruba za barafu na uelekeo wa upepo ulifanya kusafiri baharini kuwe hari sana katika Shamu.

▣**"kufunga"** Hii inamaanisha Siku za Upatanisho (kama vile Law. 16). Hii ilikuwa siku pekee ya kufunga inayotajwa katika maandiko ya Musa. Hii ingesababisha safari wakati mwingine iwe kati ya Septemba na Oktoba. Oktoba kilikuwa kipindi cha ukingo kwa safari za baharini.

▣**"Paulo alianza"** Hii ni njeo ya wakati usio timilifu (1) kitendo kinachoendelea katika wakati uliopita au (2) mwanzo wa kitendo. Katika mbadala wa kimuktadha #2 ni bora.

**27:10** Paulo anatoa onyo kali na dhahiri. Hata hivyo, kiukweli jambo hili halikutokea. Je Paulo alikuwa natoa mawazo yake mwenyewe ("natambua"), au je Mungu alibadilisha awazo yake na kuamua kuwaacha watu waliokuwa wakisafiri (kama vile Mdo. 27:24)?

**27:11**

<b>NASB</b>	"nahodha na kiongozi"
<b>NKJV</b>	"nahodha na mmiliki"
<b>NRSV</b>	"nahodha na mmiliki"
<b>TEV, NJB</b>	"kapteni na mmiliki"

Tungo hii inaashiria watu wawili tofauti.

1. nahodha (*kubernētēs*), ambalo linamaanisha mwendesha usukani wa meli, ambaye anaongoza usukani wa meli (kama vile Ufu. 18:17)
2. kapteni (*nauklēros*, ambatani ya "meli" [*naus*] na "kurithi" au "vingi" [*klēros*]), ingawa neno laweza kumaanisha "wamiliki wa meli" (kama vile F. F. Bruce, *The Book of Acts*, ukurasa wa 507, ananukuu Ramsay, *St. Paul the Traveler*, ukurasa wa 324, ambaye ananukuu *Inscriptiones Graecae*, 14.918). Matumizi yake katika mafunjo ya Koine "kapteni." Tofauti hasa kati ya haya maneno mawili haijulikani (kama vile Louw na Nida, *Greek English Lexicon*, vol. 1, ukurasa wa 548 dhidi ya Harold Moulton, *The Analytical Greek*

*Lexicon Revised*, ukurasa 275), lakini yawezekana kwenye meli ya ukubwa huu (Meli ya nafaka ya Alexandria) kulikuwa na viongozi wa vyeo tofauti kadhaa, pamoja na mabaharia wa kila siku.

**27:12 "ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la nne. Wale ambao walifanya maamuzi ya kugoa nanga walijua kuwa ingekuwa hatari lakini walifikiri watapita na kufanikiwa tu.

▣**"Foinike"** Hii ni bandari kusini mwa pwani mwa Krete, magharibi mwa Bandari Nzuri. Bado kuna mashaka kutoka katika vyanzo vya kale kuhusu wapi ilipo hasa (Strabo, *Geography*, 10.4.3 dhidi ya Ptolemy, *An Egyptian Geography* 3.17.3). Walikuwa bado wanagoo nanga karibu na pwani kando ya pwani ya kusini mwa Krete.

▣**"kukabili kusini magharibi na kaskazini magharibi"** Inavyoonekana katika Foinike kulikuwa na miji miwili iliyoachanishwa na kipande cha ardhi kilichojitokeza na kuacha alama. Bandari moja ingeweza kuhusianishwa na upepo kutoka katika mwelekeo mwingine. Wakati wa mwaka uliamua bandari gani itakuwa bora.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 27:13-20**

<sup>13</sup> Na upepo wa kusi ulipoanza kuvuma kidogo, wakidhani ya kuwa wamepata waliyoazimu kupata, wakang'oa nanga, wakasafiri karibu na Krete pwani kwa pwani. <sup>14</sup> Baada ya muda mchache ukavuma upepo wa nguvu wa namna ya tufani, uitwao Eurakilo, <sup>15</sup> merikebu iliposhikwa, na kutoweza kushindana na upepo, tukaiacha tukachukuliwa. <sup>16</sup> Na tukipita upepo karibu na kisiwa kidogo kiitwacho Kauda tukadiriki kuikweza mashua; lakini kwa shida. <sup>17</sup> Walipokwisha kuikweza wakatumia misaada, wakaikaza merikebu kwa kupitisha kamba chini yake, nao wakiogopa wasije wakakwama katika fungu liitwalo Sirti, wakatua matanga wakachukuliwa vivi hivi. <sup>18</sup> Na kwa maana tulikuwa tukipigwa sana na ile tufani, siku ya pili yake wakaanza kuitupa shehena baharini. <sup>19</sup> Siku ya tatu wakatupa vyombo vya merikebu kwa mikono yao wenyewe. <sup>20</sup> Jua wala nyota hazikuonekana kwa muda wa siku nyingi, na tufani kuu ikatushika, basi tukakata tamaa ya kuokoka.

**27:14**

NASB, NRSV	"upepo mkali"
NKJV	"upepo mkali "
TEV	"upepo wenye nguvu sana"
NJB	"upepo wa mbisho"

Neno la Kiyunani ni *tuphōn* (dhoruba) + *ikos* (kama). Huu ulikuwa ni upepo wa ghafla wenye nguvu. Ilikuwa yawezekana inachagizwa na kufanya kubwa na milima ya Krete yenye urefu wa futi 7,000.

NASB	"Eurakilo"
NKJV	"Eurakilo"
NRSV, TEV	"tufani ya kaskazini mashariki"
NJB	"tufani ya kaskazini mashariki"

Hili lilikuwa ni jina maalumu ambalo mabaharia walitoa kwa aina hii ya upepo wakati wa msimu huu. Linaundwa na (1) neno la Kiyunani, "upepo wa mashariki" (*euros*) na (2) neno la Kilatini "upepo wa kaskazini" (*aquilo*). ulikuwa ni upepo wa ghafla, wenye nguvu uelekeo kaskazini mashariki.

Kwasababu hili lilikuwa neno la kiufundi la kibaharia (*eukakulōn*), lilikuja kueleweka vibaya baadaye na waandishi ambao walilirekebisha katika njia kadhaa ili kujaribu kutengeneza maana.

**27:15 "kutoweza kushindana na upepo"** Meli za kale zilikuwa na macho yaliyopakwa rangi katika pande mbili za kuta upinde. Baadaye michoro ya wanyama au binadamu iliwekwa kwenye kuta pinde (kama vile 28:11). Hata leo tunazipa meli sifa za kike za kibinadamu (sitiari). Tungo hii kidhahiri ina "dhidi" (*anti*) pamoja na "jicho" (*ophthalmos*). Wasingeweza kuielekeza meli katika upepo.

**27:16 "Kauda"** Hiki kisiwa kidogo kiko maili hamsini nje ya pwani ya kusini mwa Krete. Sasa wakati huu walikuwa hawana msaada katika kukabiliana na upepo wenye nguvu wa kaskazini mashariki. Walitumia hifadhi ndogo kutoka katika upepo kufanya kile ambacho wasingeweza kuandaa meli kwa ajili ya mchafuko wa bahari. Kuna maandiko kadhaa tofauti kama ilivyo jina la kisiwa hiki.

1. *Kauda*, MSS P<sup>74</sup>,  $\kappa^2$ , B
2. *Klauda*, MSS  $\kappa^*$ , A
3. *Klaudēn*, MSS H, L, P, na maandiko mengi madogo kabisa ya baadaye
4. *Gaudēn*, maandiko ya Kiyunani yanayotumiwa na Jerome
5. *Klaudion*, baadhi ya maandiko madogo madogo sana

Matoleo ya UBS<sup>3</sup> na UBS<sup>4</sup> yanatoa #1 alama ya "B" (karibu na hakika). Mbadala mbili za kwanza zinaweza kuwa muundo wa Kiyunani na muundo wa Kilatini wa jina.

▣ **"kuiongoza mashua"** Hii ilimaanisha tanga ndogo katika kupigwa na mawimbi (kama vile Mdo. 27:30, 32). Tanga hili linalotembea lilitengeneza jarife ambalo lilifanya ugumu kuendelea kuiongoza meli kubwa.

**27:17 "wakatumia misaada, wakaikaza merikebu kwa kupitisha kamba chini yake"** Hii inamaanisha kukusanya kamba maalumu kuzunguka ganda ili kusaidia kulishikilia kwa pamoja wakati wa dhoruba (kama vile Aristotle, *Rhetoric* 2.5.18).

▣ **"fungu liitwalo Sirti"** Huu ni upepo utembeao katika pwani ya Afrika Kaskazini. Zilikuwa zikiitwa Sirti Kuu na Sirti Ndogo (kama vile Pliny, *Nat. Hist.* 5.4, 27). Yalikuwa makaburi mengi ya merikebu. Kuepuka Sirti kubwa mabaharia waliongoza meli kiupandeupande ili kuelekea kusini polepole.

▣ **"nanga ya baharini"** Msingi wa utafsiri sahihi wa muktadha wa neno "kushushwa." Walishusha nini: (1) nanga ya majini au (2) sehemu ya kutweka nanga? Kusudi lilikuwa kushusha meli chini, lakini wakati huo huo kuruhusu baadhi ya maongozi.

Nanga ya baharini sio nanga ambayo ilitua chini, lakini shuka kama la mwavuli wa parachuti ambalo lililotumia uzito wa maji lililomo likipungua meli kutoka (kama vile maandiko ya Kilatini na matoleo ya NASB, NRSV, na NJB).

Kuna fasiri kadhaa za kiingereza ambazo zinafasiri hii kama "kushusha nanga" (kama vile matoleo ya NKJV, TEV, NJB, na Peshitta katika Kingereza). Neno la Kiyunani kidhahiri linamaanisha "kitu" (kama vile Louw & Nida, *Greek-English Lexicon*, vol. 2, ukurasa wa 223) na lazima ifasiriwe katika ufahamu wa muktadha husika. Kuna maandiko ya mavunjo hasa ambayo yanatumia kwa ajili ya nanga (kama vile Moulton & Milligan, *The Vocabulary of the Greek Testament*, ukurasa wa 577). Ikiwa hivyo wanashusha sehemu ya nanga lakini sio sehemu zote. Walitakiwa kubakiza sehemu ya uongozaji na kujaribu kusafiri upandeupande polepole inavyoiwezekana.

**27:18-19** Hii inaonesha ni kwa machafuko namna gani na hatari dhoruba hii ilionekana kuwa hawa walikuwa mabaharia wa msimu (kama vile Mdo. 20).

**27:18 "kuitupa shehena baharini"** This act shows that these sailors were truly afraid for their lives. Kitendo hiki kinaonesha kwamba hawa mabaharia kwa hakika walikuwa wanahofu ya maisha yao.

**27:19 "vyombo vya merikebu"** Hakika nini jambo hili linamaanisha haijulikani. Yawezekana nanga kuu na mfumo wa makamba yake. Neno hili ni tata. Neno hili hili linamaanisha nanga ya baharini, au sehemu ya nanga katika Mdo. 27:17.

**27:20 "Jua wala nyota hazikuonekana kwa muda wa siku nyingi"** Tungo hii inavyoonekana inafunua kwamba hawakuwa na maarifa mahali walipokuwepo. Walikuwa na woga wa pwani ya Afrika kaskazini, lakini hawakuweza kusema ni kwa karibu kiasi gani walikuwa wamekaribia (kama vile Mdo. 27:29). Bila nyota au jua wasingeweza kusafiri au kutambua walipo na wanapoelekea.

▣ **"basi tukakata tamaa ya kuokoka"** Hii jozi ya hatua kwa kutia moyo kwa Paulo yakijita katika maono ya mwanzo (kama vile Mdo 27:21-26). Mali zao zilikuwa zimeondoka!

## ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) MATENDO YA MITUME 27:21-26

<sup>21</sup> Na walipokuwa wamekaa wakati mwingi bila kula chakula, Paulo akasimama katikati yao, akasema, Wanaume, iliwapasa kunisikiliza mimi na kutokung'oa nanga huko Krete, na kupata madhara haya na hasara hii. <sup>22</sup> Sasa nawapeni shauri, iweni na moyo mkuu, kwa maana hapana hata nafsi mmoja miongoni mwenu atakayepotea, ila merikebu tu. <sup>23</sup> Kwa maana usiku huu wa leo malaika wa Mungu yule ambaye mimi ni wake, naye ndiye nimwabuduye, alisimama karibu nami, <sup>24</sup> akaniambia, Usiogope, Paulo, huna budi kusimama mbele ya Kaisari; tena, tazama, Mungu amekupa watu wote wanaosafiri pamoja nawe. <sup>25</sup> Basi, wanaume, changamkeni; kwa sababu namwamini Mungu, ya kwamba yatakuwa vile vile kama nilivyoambiwa. <sup>26</sup> Lakini hatuna budi kupwelewa katika kisiwa kimoja.

**27:21 "walipokuwa wamekaa wakati mwingi bila kula chakula"** Kuna angalau uwezekano wa aina tatu yenye maana za kuhusiana kwa Mdo. 27:33:

1. Yawezekana walikuwa wakiogopa bahari kutokana na misukosuko iliyosababishwa na dhoruba
2. Walikuwa wakiomba na kufunga kwa sababu za kidini za kusazwa (yaani ibada za kipagani, kama vile Mdo. 27:29)
3. walikuwa wakijishughulisha wakijaribu kuokoa meli, kula kulikuwa jambo dogo sana

▣ **"iliwapasa kunisikiliza mimi "** Hii ilikuwa kauli ya Paulo "naliwaambia!" Ilimpatia Paulo fursa ya kuwa msemaji wa Roho.

**27:22 "ila merikebu tu"** Tazama matumizi ya *dei* katika Mdo. 27:26. Tazama dokezo kamili *dei* katika Mdo. 1:16. Inatumika mara tatu katika sura hii (Mdo.27:21,24,26).

**27:23 "malaika wa Bwana"** Mara kadhaa Yesu au malaika kwa Paulo kumtia moyo (kama vile Mdo. 18:9-10; 22:17-19; 23:11; 27:23-24). Mungu alikuwa na mpango wa kiinjalisti na Kusudi kwa maisha ya Paulo (kama vile Mdo. 27:26; 9:15) na dhoruba haikuwa inaenda kukoma.

**27:24 "Usiogope, Paulo"** Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopo (yenye ushahidi) yenye kauli hasi endelevu ambayo mara kwa mara inamaanisha kitendo ambacho tayari kilicho katika mchakato (kama vile Mdo. 23:11; Mithali. 3:5-6).

▣ **"Mungu amekupa watu wote wanaosafiri pamoja nawe"** Kitenzi cha kwanza ni kauli ya kati elekezi ya wakati mkamilifu (yenye ushahidi). Mungu alikuwa na mpango na kusudi katika huduma ya Paulo (kama vile Mdo. 9:15; 19:21; 23:11). Yeye lazima (*dei*) atoe ushuhuda katika Rumi kabla ya viongozi wake wa kiserikali na kijeshi.

Maisha ya Paulo na imani yalikuwa na athari katika hatika ya watenda kazi wenzake. Huu upanuzi wa neema unaweza kuonekana katika Kumb. 5:10; 7:9; 1 Kor. 7:14. Hii haiondoi majukumu binafsi, lakini yanaendeleza ushawishi mkuu wa familia inayoamini, marafiki na watendakazi wenza.

**27:25** Maonyo ya Paulo kama vile Mdo. 27:22, "kuendeleza ujasiri wako," ni kauli isiyo na ukomo ya wakati uliopo, inarudiwa, "endeleza ujasiri wako," ambayo ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo.

▣ **"Kwa kuwa namwamini Mungu"** Kukutana kwa Paulo na Kristo anayeishi inamsababishia kuamini neno la Mungu ("itafanyika sawasawa na namna nilivyoambiwa" kauli tendwa elekezi ya wakati timilifu). Imani ni mkono ambao unapokea zawadi za Mungu —na sio wokovu, ila ubanifu wa hali.

Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament* ana kauli kubwa na nukuu kutoka Romaine, *Life of Faith*.

"Sasa tunakabili Agano Jipya kwa utofauti wa wazi kati ya imani sehemu moja, na tumaini na tegemeo upande mwingine. Imani ni kumwamini Mungu kwa Neno lake, wakati tumaini na uvumilivu ba pia tegemeo ni matunda sahihi ya imani, udhihirisho katika miundo mabalimbali ujasiri ambao mwamini anajiskia. Ujumbe unatoka kwangu kutoka kwa Mwandishi wa uwepo wangu; inaweza kuwa tishio, ahadi



au amri. Ikiwa nitaichukulia kuwa 'ni kweli na amina,' hiyo ni imani; na tendo ambalo linasababisha ni kitendo cha **amunah** au uaminifu wa Mungu. Imani kulingana na Maandiko inaonekana kumaanisha neno, ujumbe au ufunuo. Hivyo msomi Romaine asema katika andiko lake *Life of Faith*:—'Imani inaashiria kuamini kweli ya Neno la Mungu; inahusiana na baadhi ya neno lililonenwa au na baadhi ya ahadi zilizofanywa nae, na inaelezea imani ambayo mtu anayelisikia analichukua kuwa kweli: anakubaliana nalo, analitegemea, kulifanyia kazi sawasawa: hii imani.' Matunda yake yatatofautiana kutokana na asili ya ujumbe unaopokelewa na kulingana na mazingira ya kupokea. Ilimsababisha Nuhu kujenga Safina, Ibrahimu kumtoa mwanawe, Musa alikataa kuitwa mwana wa mtoto wa binti Farao, Waisraeli walitembea wakiuzunguka ukuta wa Yeriko. Namwamini Mungu kwamba itakuwa kama ambavyo nimeambiwa—hii ndiyo picha ya mchakato ambao Biblia inaita imani" (kurasa104-105).

Kwa "amini angalia Mada Maalum katika Mdo. 2:40; 3:16; na 6:5.

#### **ANDIKO LA NASB(LILILOBRESHWA) MATENDO YA MITUME 27:27-32**

**27** Hata usiku wa kumi na nne ulipofika, tulipokuwa tukichukuliwa huko na huko katika bahari ya Adria, kama usiku wa manane baharia wakadhani ya kuwa wanaikaribia nchi kavu. **28** Wakatupa bildi wakapata pima ishirini, wakaendelea kidogo wakatupa bildi tena, wakapata pima kumi na tano. **29** Wakachelea tusije tukapwelewa mahali penye miamba, wakatupa nanga nne za tezi, wakaomba kuche. **30** Na baharia walipotaka kukimbia na kuiacha merikebu, wakiishusha mashua baharini kana kwamba wanataka kutupa nanga za omo, **31** Paulo akawaambia akida na askari, Hawa wasipokaa ndani ya merikebu hamtaweza kuokoka. **32** Basi askari wakazikata kamba za mashua, wakaiacha ianguke.

**27:27 "siku ya kumi na nne"** Wakati huu unashabihiana sana kabisa na umbali uliofikiwa na kutoka katika ukanda (yaani nanga ya baharini). Walisafiri maili 476 katika maili 36 kwa muda wa kipindi cha saa 24.

▣ **"bahari ya Adria"** Hii inamaanisha kusini mwa Shamu ya kati (Adria). Haimaanishi Bahari ya Adria ya siku zetu.

▣ **"wakadhani ya kuwa wanaikaribia nchi kavu"** Walikuwa yawezekana kwamba walisikia viziuzi au waliona ndege Fulani au samaki.

**27:28 "bildi"** Hii inatoka katika kitenzi kinachomaanisha "kuondoka bila kutua," ambayo inamaanisha kushusha kamba iliyojaa uzito, iliyowekewa alama ya kuashiria urefu wa Maji.

▣ **"pima"** Huu ulikuwa umbali kati ya mikono iliyonyooshwa. Iliashiria kipimo kilichotumika na mabaharia kuelezea urefu wa maji.

**27:29** Ilikuwa bado giza. Hawakujua kule ambako walikuwa hasa. Walitaka kupunguza mwendo au kusimamisha meli kukabili nchi kavu mpaka waone ambapo meli ilipokuwa ikielekea .

**27:30** Mabaharia hawa walikuwa watu wa imani. Walikuwa tayari kufanya chochote ambacho wangeweza kufanya ili kujiokoa wenyewe.

**27:31** Kulikuwa na masharti (sentensi yenye masharti daraja la tatu) yaliyounganishwa na maono ya Paulo yaliyoreshwa bna ahadi ya Mungu.

▣ **"kuokolewa"** Hii ni nmna ya Agano la Kale ya kuokolewa kimwili (kama vile Yakobo 5:15). Kumfahamu Paulo, mabaharia hawa, wanajeshi na wasafiri wenzake pia walisikia injili ambayo inaleta namna ya Agano Jipya ya neno ya wokovu wa kirohoNi muujiza mkuu namna gani kuokolewa kutoka katika mauti ya mwilini kufa kifo cha milele!

#### **ANDIKO LA NASB(LILILOBRESHWA) MATENDO YA MITUME 27:33-38**

**33** Na kulipokuwa kukipambauka Paulo akawasihi wote wale chakula, akisema, Leo ni siku ya kumi na nne

kungoja na kufunga, hamkula kitu cho chote.<sup>34</sup> Basi nawasihi mle chakula, maana itakuwa kwa wokovu wenu; kwa maana hapana hata unywele wa kichwa cha mmoja wenu utakaopotea.<sup>35</sup> Alipokwisha kusema hayo akatwaa mkate, akamshukuru Mungu mbele yao wote akaumega akaanza kula.<sup>36</sup> Ndipo wakachangamka wote, wakala chakula wenyewe.<sup>37</sup> Na sisi tuliokuwa ndani ya merikebu tulipata watu mia mbili na sabini na sita.<sup>38</sup> Walipokwisha kushiba wakaipunguza shehena ya merikebu, wakiitupa ngano baharini.

**27:34** "hapana hata unywele wa kichwa cha mmoja wenu utakaopotea " Paulo anatumia maneno yanayofanana nay a Yesu (kama vile Luka 12:7; 21:18). Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya ulinzi (kama vile 1 Sam. 14:45; 2 Sam. 14:11; 1 Wafalme. 1:52).

**27:35** Hii haimaanishi Meza ya Bwana lakini inaonesha imani ya Paulo hakta katikati ya misukosuko. Imani ya Paulo inashawishiwa na wengine (kama vile Mdo. 27:36).

**27:37** "mia mbili na sabini na sita" Hii inajumuisha wafanyakazi wa meli na abiria.

1. Maandiko B (karne ya nne) yana "76"
2. MSS x (karne ya nne) na C (karne ya tano) ina "276"
3. Maandiko A (karne ya tano) ina "275"
4. Fasiri zote za kingereza za kisasa zina 276

UBS<sup>4</sup> inatoa alama ya "B" (karibu na hakika).

**27:38** Hii ilikuwa ni meli ya ngano kubwa kutoka Misri. Walikuwa tayari wamekwishatupa mizigo yao kilindini kweny maji (kama vile Mdo. 27:18).

#### ANDIKO LA NASB( LILILOBORESHWA) MATENDO YA MITUME 27: 39-44

<sup>39</sup> Kulipokucha hawakuitambua ile nchi, ila waliona hori yenye ufuo, wakashauriana kuiegsha merikebu huko, kama ikiwezekana. <sup>40</sup> Wakazitupilia mbali zile nanga, na kuziacha baharini, pamoja na kuzilegeza kamba za sukani, wakalitweka tanga dogo ili liushike upepo, wakauendea ule ufuo. <sup>41</sup> Lakini wakafikia mahali palipokutana bahari mbili, wakaiegsha merikebu, omo ikakwama ikakaa isitikiswe, bali tezi ilikuwa imefumuliwa kwa nguvu za mawimbi. <sup>42</sup> Shauri la askari lilikuwa kuwaua wafungwa, mtu asiogele na kukimbia. <sup>43</sup> Bali akida, akitaka kumponya Paulo, akawazuia, wasifanye kama walivyokusudia, akawaamuru wale wawezao kuogelea wajitupe kwanza baharini, wafike nchi kavu; <sup>44</sup> nao waliosalia, hawa juu ya mbao na hawa juu ya vitu vingine vya merikebu. Na hivyo watu wote wakapata kuifikilia nchi kavu salama.

**27:39** Walikuwa bado wanaweza kuongoza meli yao kwa namna fulani (kama vile Mdo. 27:40). Kuna maandiko ya Kiyunani tofauti yanayohusiana na "kuendesha meli kuelekea kwenye" (kama vile MSS x, A, B<sup>2</sup>) na "kuwasili nchi kavu salama" (kama vile MSS B\* na C). Haya maneno mawili yanaonekana kuwa na mfanano (*exōsaivs. eksōsai*). Maandiko ya kale ya Kiyunani ya kale mara kwa mara yalisomeka kwa mmoja na kunakiliwa na wengi. kufanana kwa sauti kwa maneno kulikuwa mara kwa mara kunachanganya.

**27:40** Miamba hii kandokando ya ufukwe ilisababisha kuvunjika kwa merikebu nyingi. Kwa namna hii mwamba ulikua mahali ambapo mawimbi ya bahari na maji ya ghuba yalikutana.

NASB, NKJV

NJV "washika usukani"

NRSV, TEV "washika usukani"

Hii inamaanisha waendesha usukani miwili, ambayo ilikuwa hasa ya meli kubwa. Yakobo 3:4 Inatumia neno hili hili "waendesha usukani."

▣"**kuiegsha**" Hili ni neno nadra, akini lazima limaanishe kugoa nanga katika gubeti (kama vile Juvenal, *Sat.* 12.69).

**27:42 "Shauri la askari lilikuwa kuwaua wafungwa"** Ikiwa wangetoroka wanajeshi wangetakiwa kuwajibika kwa kupewa adhabu!

**27:43** Maneno ya Paulo, imani na matendo yalikuwa yamewashawishi viongozi wa Kirumi ikiwezekana wawaamini na kumlinda yeye.

## **MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeke katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Taaarifa ya Luka kuhusu safari ya Paulo ya Rumi ina maneno mengi ya kibaharia. Huku kunamaanisha nini?
2. Kwanini Mdo. 27:20 ni muhimu sana kithiolojia?

## MATENDO YA MITUME 28

<b>MGAWANYO WA AYA WA TAFASRI ZA KISASA</b>				
<b>UBS<sup>4</sup></b>	<b>NKJV</b>	<b>NRSV</b>	<b>TEV</b>	<b>NJB</b>
Paulo katika Kisiwa cha Malita	Huduma ya Paulo huko Mlita	Paulo katika Malita	Katika Malita	Kusubiri katika Malita
28:1-10	28:1-10	28:1-6 28:7-10	28:1-6 28:7-10	28:1-6 28:7-10
Paulo Awasili Huko Rumi	Kuwasili huko Rumi	Safari yakuelekea Rumi	Kutoka Malita hadi Rumi	Kutoka Malita hadi Rumi
28:11-15	28:11-15	28:11-15	28:11-15	28:11-15
28:16    28:26	Huko Rumi	28:15-16 28:26		
Paulo Ahubiri Katika Rumi	Huduma ya Paulo huko Rumi	Paulo na Wayahudi wa Rumi		Paulo Afanya Afanya Mawasiliano na Wayahudi wa Kirumi
28:17-22	28:17-31	28:17-22	28:17-20 28:21-22	28:17-20 28:21-22
				Maazimio ya Paulo kwa Warumi wa Kiyahudi
28:23-29		28:23-29	28:23-27 28:28	28:23-27 28:28
28:30-31		Hitimisho 28:30-31	28:29 28:30-31	Mwisho 28:30-31

### **KUSOMA MZUNGUKO WA TATU** (kutoka "[Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia](#)")

#### ***KUFUATIA KUSUDI ASILIA YA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA***

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

9. Ayaya kwanza
10. Ayayapili

11. Ayatatu
12. N.k

## USOMAJI WA NENO NAKIFUNGU CHA NENO

### ANDIKO LA NASB (LILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 28:1-6

<sup>1</sup>Tulipokwisha kuokoka, ndipo tulipojua ya kuwa kisiwa kile chaitwa Melita. <sup>2</sup>Wenyeji wakatufanyia fadhili zisizokuwa za kawaida. Kwa maana waliwasha moto, wakatukaribisha sote, kwa sababu ya mvua iliyonyesha na kwa sababu ya baridi. <sup>3</sup>Paulo alipokuwa amekusanya mzigo wa kuni, na kuuweka motoni, nyoka akatoka kwa ajili ya ule moto akamzonga-zonga mkononi. <sup>4</sup>Wenyeji walipomwona yule nyoka akilewa-lewa mkononi, wakaambiana, Hakosi mtu huyu ni mwaaji; ambaye ijapokuwa ameokoka katika bahari haki haimwachi kuishi. <sup>5</sup>Lakini yeye akamtukusia motoni asipate madhara. <sup>6</sup>Wao wakadhani ya kuwa atavimba au kuanguka chini kwa kufa ghafula; na wakiisha kumwalia sana, na kuona kwamba halimpatu dhara lo lote, wakageuka, wakasema kwamba yeye ni mungu.

**28:1**"Tulipokwisha kuokoka" Neno hili *sōzō* (kama vile Matendo ya Mitume 27:31) pamoja na neno *dia* linaambishwa mwanzoni. Kwa hali ya kawaida neno hili lilitumika kwa mtu aliyewasili mahali fulani kwa katika hali ya usalama (kama vile Matendo ya Mitume 23:24; 27:44; 28:1,4). Hata Luka analitumia neno hili kuzungumzia uponyaji wa kimwili katika Luka 7:3. Hii kauli tendwa endelevu ya wakati uliopita usio timilifu inaonyesha kwamba Luka aliongeza hali ya kuonyesha usalama kama iliyotolewa na Mungu (sauti irabu tendewa) kulingana na neno Lake (kama vile Matendo ya Mitume 27:21-26).

▣ **"Malita"** Watu wa Kisemitiki waliosafiri kwa kutumia matanga pia walikiita kisiwa hiki Melita, ambapo hili lilikuwa neno la Kikaanani lililomaanisha "mkimbizi." Eneo hili kwa asili yake lilikuwa koloni la Foenike. Eneo hili lilikuwa katika kati ya Sikili na Afrika ya Kaskazini. Huu ni urefu wa maili kumi na nane tu na upana wa maili, lakini eneo lilitoshereza thamani ya bahari ya kibiashara. Eneo hili lilikuwa na bandari kadhaa zilizokuwa nzuri.

**28:2** **Wenyeji** "chimbuko la neno hili ni "washenzi." Jina hili halimaanishi kushusha heshima, kwa uhalisia linarejelea mtu ye yote asiyezungumza Kiyunani au Kilatini.

**NASB** "fadhili zisizokuwa za kawaida"

**NKJV, NRSV**

**NJB** "wema usiokuwa wa kawaida"

**TEV** "walikuwa wema sana"

Kifungu hiki kinalo neno *philanthrōpo* lililoongezewa sifa, ambacho kwa uhalisia wake ni "mwenye fadhili" kama ilivyo katika Matendo ya Mitume 27:3. Utunzaji na utoaji wa kipekee ulifanywa na wenyeji hawa ulikuwa ni kwa sababu waliiona miujiza wa Paulo kupambana na nyoka ufukweni mwa bahari. Muujiza huu, na matendo mengine ya kimujiza (kama vile Matendo ya Mitume 28:7-10), ilifungua mlango wa unjilisti! Mara nyigi Paulo alikuwa akiwaza kuihubiri injili (kama vile 1 Kor. 9:19-23).

**28:3**"Paulo alipokuwa amekusanya mzigo wa kuni" Kwa hakika hili linaonyesha unyenyekevu wa Paulo. Yeye alikuwa akifanya kazi sambamba na wengine wote. Hakuwa na tabia ya kujibagua kwa sababu za kielimu tangu siku ile ya barabara ya kwenda Dameski!

▣ **"nyoka. . . akamzonga-zonga mkononi"** Maana ya msingi ya neno hili ni "kuambatanisha" Hili linamaanisha "kamata" au "kuzungusha karibu."

**28:4 "yule nyoka"** Neno hili "nyoka" linakuwa neno la kitabibu linalomaanisha sumu ya nyoka (kama vile Matendo ya Mitume 10:12).

▣ **"haki haimwachi kuishi"** "Haki" au "miungu mitatu ya Kiyunani" lilkuwa na jina la miungu yao. Hawa walielezwa kwa kutumia chuma kulingana na mazigira, sawasawa na Amosi 5:19. Mstari wa 6 unaonyesha kwamba wenyeji wa kisiwa hiki walikuwa waabudu miungu ya kishirikina.

**28:6** Hawa wakazi wa kisiwa walikuwa na uzoefu wa kipekee kuhusu nyoka waliokuwa kisiwani. Mabadiliko ya muhimu ya kimtazamo ni sawa na mapambano ya wapagani kuhusu miujiza katika Matendo ya Mitume 14:11-13.

▣ **" kufa ghafula"** Hii ni moja kati maneno ya kitabibu yaliyotumiwa na Luka (kama vile Matendo ya Mitume 28:8). Hili linapatikana katika Agano Jipya pekee.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 28:7-10**

<sup>7</sup> Karibu na mahali pale palikuwa na mashamba ya mkuu wa kisiwa, jina lake Publio; mtu huyu akatukaribisha kwa moyo wa urafiki, akatufanya wageni wake kwa muda wa siku tatu. <sup>8</sup> Ikawa babaake Publio alikuwa hawezi homa na kuhara damu. Paulo akaingia kwake, akaomba, akaweka mikono yake juu yake, na kumpoza. <sup>9</sup> Yalipokwisha kutendeka hayo wengine waliokuwa na magonjwa katika kisiwa wakaja wakapozwa; <sup>10</sup> nao wakatuheshimu kwa heshima nyingi; basi tulipoabiri wakatupakilia vitu vile tulivyokuwa na haja navyo.

**28:7 " mkuu "** Neno hili linamaanisha baadhi ya madaraka ya kiserikali, kiuhalisia, "watu wa kwanza katika ukuu" (kama vile Matendo ya Mitume 13:50; Luka 19:47, "wa watu"; 16:12, "wa mji"). Hili limepatikana katika minara miwili ya kisiwa hiki, moja ni la Kiyunani na lingine ni la Kilatini. Rumi imekiruhusu kisiwa hiki kujiongoza chenyewe na kwa kiasi fulani, uraia kamili wa Kirumi.

**28:8 " alikuwa hawezi homa na kuhara damu"** Malita ni kisiwa kilichojulikana kwa homa zilizotokana na bacteria waliokuwa ndani ya maziwa ya mbuzi waliowafuga.

▣ **" akaweka mikono yake juu yake, na kumpoza"** Tazama Mada Maalum: Kuwekea Mikono katika Matendo ya Mitume 6:6.

**28:9** Vitenzi vyote hivi si timilifu, ambavyo vinamaanisha tendo lenye kurudiwa rudiwa au endelevu katika wakati uliopita (dhamira elekezi). Walizidi kuja. Mungu aliendelea kuwaponya kupitia Paulo. Kitenzi cha Kiyunani katika tafsiri zaidi ya Kiingereza "kupata tiba" ni *therapeuō*, ambapo tunalipata neno la Kiingereza "matibabu." Neneo hili linaweza kutumika kama "huduma" pamoja na "uonyaji." Ni muktadha pekee uwezao kutambulisha lilpi lililo sahihi.

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 28:11-15**

<sup>11</sup> Baada ya miezi mitatu tukasafiri katika merikebu ya Iskanderia iliyokuwa imekaa pale kisiwani wakati wa baridi; na alama yake ni Ndugu Pacha. <sup>12</sup> Tukafika Sirakusa, tukakaa siku tatu. <sup>13</sup> Kutoka huko tukazunguka tukafikia Regio; baada ya siku moja upepo wa kusi ukavuma, na siku ya pili tukawasili Puteoli. <sup>14</sup> Huko tukakuta ndugu, wakatusihi tukae nao siku saba; na hivi tukafika Rumi. <sup>15</sup> Na kutoka huko ndugu, waliposikia habari zetu, wakaja Mikahawa Mitatu.kutulaki mpaka Soko la Apio na Mikahawa Mitatu. Paulo alipowaona alimshukuru Mungu, akachangamka.

**28:11" merikebu ya Iskanderia"** Bila shaka hii ilikuwa meli kubwa nyingine ya nafaka ambayo ilikuwa ikielekea katika Ghuba ya Nepali kutoka Misri (kama vile Matendo ya Mitume 27:6,38).

▣ **"merikebu ya Iskanderia iliyokuwa imekaa pale kisiwan"** Bahari ya Mediteranea ilikuwa imechafuka sana kiasi cha kutoweza kusafiri wakati wa miezi ya baridi. Njia za merikebu ziliziba kuanzia Februari au Marchi.

▣ **"na alama yake ni Ndugu Pacha"** Aya hii inarejelea kwa wale wana mapacha wa Zeus, Caster na Pollox. Hawa walikuwa wawezeshaji wa wasafiri kwa matanga katika katika mahekalu ya miungu ya Kirumi. Poseidon aliwapa alijitoa kwa ajili ya kuthibiti upepo, mawimbi, na vimbunga. Kusanyiko lao maalumlilikuwa Gemini. Inavyoonekana kulikuwepo na alama yao iliyoinamia, viumbe viwili vyenye mfano wa watu.

**28:12" Sirakusa"** Huu ulikuwa mji mkuu wa Sikili eneo la pwani ya mashariki. Hii bandari ilikuwa umbali wa maili themanini kaskazini mwa Malita.

**28:13" tukazunguka** "machapisho ya kale ya herufi kubwa  $\kappa$  (Siniaticus), na B (Vaticanus) yana kifungu "nanga nzito," ambapo lilikuwa neno la kiufundi la kuzunguka (hii ni sifa kuu ya Luka), lakini machapisho mengine ya kale P<sup>74</sup>,  $\kappa^c$ , na A yana "upitaji," kama 16:8.

▣ **"Regio"** Huu ni mji ulioko kusini magharibi pembezoni mwa Italia.

▣ **"Puteoli"** Hiki kilikuwa kituo kidogo cha uagizaji wa nafaka humo Rumi katika Ghuba ya Nepali. Hawa walisafiri umbali upatao maili 180 kwa siku mbili.

**28:14"Huko tukakuta ndugu"** Walikuwepo Wakristo waliokuwa katika mikusanyiko humo Italia (kama vile Matendo ya Mitume 28:15) na Rumi waliomlaka Paulo.

**28:15" Soko la Apio"** Hili lilikuwa eneo la mwisho la safari za kuingia kutoka kusini mwa Italia na mwanzoni mwa njia kuu ya Kirumi iliyoitwa Njia ya Appian. Hii ilikuwa umbali upatao maili arobaini na tatu hadi Rumi.

▣ **" Mikahawa Mitatu"** Hii ilikuwa sehemu ya mapumziko iliyokuwa umbali upatao maili therathini na tatu kutoka Roma.

▣ **"Paulo. . . Mikahawa Mitatu"** Hakika Paulo kwa mara nyingine alivunjika moyo. Huyu anaonekana kulegea katika hili. Yesu alimtokea kwa upekee mara kadhaa ili kumtia moyo.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 28:16**

<sup>16</sup>Tulipoingia Rumi Paulo alipewa ruhusa kukaa kwake mwenyewe pamoja na askari aliyemlinda.

**28:16 " Tulipoingia Rumi "** Hivi sivyo namna alivyotarajia Paulo kuingia Rumi. Bali, hii ilikuwa namna ya Mungu aliyoiipanga kwa Paulo kwa ajili ya kuzungumza na serikali ya Kirumi, jeshi, na viongozi wa kidini.

▣ **" Paulo alipewa ruhusa kukaa kwake mwenyewe pamoja na askari aliyemlinda"** Paulo aliyashinda mashtaka yaliyokuwa nyumbani mwake. Ushuhuda wa afisa ambaye alimleta ulikuwa chombo katika maamuzi yake.

**ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 28:17-22**

<sup>17</sup>Ikawa baada ya siku tatu akawaita wakuu wa Wayahudi wakutane, hata walipokutanika akawaambia, Ndugu zangu, ningawa sikufanya neno kinyume cha watu wetu wala neno lililopingamana na

desturi za baba zetu, nalitiwa katika mikono ya Warumi, hali nimefungwa, tokea Yerusalemu. <sup>18</sup> Na hao walipokwisha kuniuliza-uliza walitaka kunifungua, kwa maana hapakuwa na sababu yo yote kwangu ya kuuawa. <sup>19</sup> Lakini Wayahudi walipotoa hoja juu ya shauri hili nalishurutishwa kutaka rufani kwa Kaisari. Si kwamba nalikuwa na neno la kuwashitaki watu wa taifa langu. <sup>20</sup> Basi kwa ajili ya hayo, nimewaita mje kunitazama na kusema nami; kwa maana nimefungwa kwa mnyororo huu kwa ajili ya tumaini la Israeli. <sup>21</sup> Wale wakamwambia, Sisi hatukupata nyaraka zenye habari zako kutoka Uyahudi, wala hapana ndugu hata mmoja aliyefika hapa na kutupasha habari, au kunena neno baya juu yako. <sup>22</sup> Lakini tunataka kusikia kwako uonavyo wewe; kwa maana katika habari za madhehebu hiyo imejulikana kwetu kwamba inanenwa vibaya kila mahali.

**28:17 " akawaita wakuu wa Wayahudi wakutane"** Hiki kilikuwa kiwango cha msistizo (kama vile Matendo ya Mitume Rum. 1:16; 2:9). Yeye anaeleza mambo yake ya sasa na kufungua mlango wa kuiwasilisha injili.

**28:18-19** Tena hapa makusudi ya Luka kuomba radhi yanaweza kuwa yameonekana hapo awali! Ukristo haukuleta athari kwa serikali ya Kirumi.

**28:19" Wayahudi walipotoa hoja juu ya shauri hili"** Uchaguzi huu wa maneno unaonekana kuwa na mwelekeo wa kuwazungumzia viongozi wa Kiyahudi katika Rumi. Luka analitumia neno *loudaios* (Wayahudi) katika maana mbili.

1. utaifa – Matendo ya Mitume 2:5,11; 9:22; 10:22,28; 11:19; 13:56; 14:1; 16:1,3,20; 17:1; 17:10,17; 18:2,4,5,19; 19:10,17,34; 20:21; 21:21,39; 22:3,12; 24:5,9; 24:24,27; 25:8,9,24; 20:7; 28:17
2. wale waliyoyashuhudia kwa macho mambo yaliyofanyika katika juma la mwisho la maisha ya Yesu – Matendo ya Mitume 2:15; 10:39

Huyu pia alilitumia neno hili katika tambuzi tofauti.

1. Katika maana hasi – Matendo ya Mitume 9:23; 12:3,11; 13:45,50; 14:2,4,5,19; 17:5,13; 18:12,14,28; 19:13,14,33; 20:3,19; 21:11,27; 22:30; 23:12,20,27; 24:19; 25:2,7,10,15; 26:2,21; 28:19
2. Katika maana chanya – Matendo ya Mitume 13:43; 14:1; 18:2,24; 21:20 Bila shaka andiko bora zaidi katika Matendo ya Mitume ambalo linaonyesha maana nyingine mbalimbali za neno hili ni Matendo ya Mitume 14:1-2.

**28:20" kwa ajili ya tumaini la Israeli"** Paulo anawahutubia hawa viongozi wa Kiyahudi katika njia hii ili kuhimarisha uhusianowake pamoja na wasikilizaji wake. Anajaribu kuitafuta misingi ya kanuni za viongozi wa Kiyahudi katika "tumaini la Israeli." Kwa Paulo, ambayo ilimrejelea Yesu, kwao, ahadi ya Yule Ajaye Aliyehaidiwa, Masihi au yawezekana ni yule wa ufufuo!

**28:21** Uhaba huu wa habari zinazomhusu Paulo ni wa kushangaza kwa upande wa huduma ya Paulo ya ziara tatu za umisheni na matukio na tetesi za humo Yerusalemu.

**28:22** Ni dhahiri kwamba habari zilizo Yesu zilienea na zilizo nyingi zilikuwa za mwitikio wa injili. Katika maeneo ya Kiyunani hizi hazikuwa habari njema! Hata hivyo, hawa viongozi wa Kiyunani walikuwa tayari kumpa Paulo usikivu wao.

▣ **"madhehebu hiyo" Tazama Mada Maalum:** Yesu Mnazareti katika Matendo ya Mitume 2:22.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 28:23-29**

<sup>23</sup> Wakiisha kuagana naye siku, wakamjia katika nyumba aliyokaa, watu wengi sana, akawaeleza kwa taratibu na kuushuhudia ufalme wa Mungu, akiwaonya mambo yake Yesu, kwa maneno ya sheria ya Musa na ya manabii, tangu asubuhi hata jioni. <sup>24</sup> Wengine waliamini yale yaliyonenwa, wengine hawakuyaamini. <sup>25</sup> Na walipokuwa hawapatani wao kwa wao, wakaenda zao, Paulo alipokwisha kusema neno hili moja, ya



**kwamba, Roho Mtakatifu alinena vema na baba zetu, kwa kinywa cha nabii Isaya,<sup>26</sup> akisema, Enenda kwa watu hawa, ukawaambie, Kusikia, mtasikia wala hamtafahamu; Na kuona, mtaona wala hamtatambua;<sup>27</sup> Kwa maana mioyo ya watu hawa imepumbaa, Na masikio yao ni mazito ya kusikia, Na macho yao wameyafumba; Wasije wakaona kwa macho yao, Na kusikia kwa masikio yao, Na kufahamu kwa mioyo yao, Na kubadili nia zao, nikawaponya.<sup>28</sup> Basi ijulikane kwenu ya kwamba wokovu huu wa Mungu umepelekwa kwa Mataifa, nao watasikia!<sup>29</sup> Alipokwisha kusema hayo, Wayahudi wakaenda zao, wakiulizana mengi wao kwa wao.]**

**28:23 "t wakamjia. . . watu wengi sana. . . tangu asubuhi hata jioni"** Paulo alieleza juu ya imani ya ki-Kristo kwa Wayahudi hawa siku nzima! Ni fursa iliyoje.

▣ **"ufalme wa Mungu"** Hiki ndicho kitovu cha mahubiri na mafundisho ya Yesu (mifano). Huu ni ukweli uliopo katika maisha ya waamini na ukamilifu wa baadaye wa utawala wa Mungu juu ya dunia yote iliyoanguka (kama vile Matendo ya Mitume. 6:10). Kwa uwazi kifungu hiki hakikhusiana na Israeli pekee, bali kilikuwa sehemu muhimu ya tumaini la Israeli (kama vile Matendo ya Mitume 28:20). Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 1:3.

▣ **"sheria ya Musa na ya manabii"** Hili ni la pili kati ya migawanyo mitatu ya kanuni za Kiebarania (tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 13:15 na angalia katika Matendo ya Mitume 24:14) ambalo linasimama kwa ajili ya Agano la Kale zima (kama vile Matendo ya Mitume. 5:17; 7:12; 22:40; Luka 16:16; 24:44; Matendo ya Mitume 13:15; 28:23). Mbinu ya Paulo (uanishi wa ki- Kristo na unabii uliotabiriwa) ilikuwa ni kuyaweka sawa maandiko ya Agano la Kale kandokando ya maisha ya Yesu.

**28:24** Hili linaaksi ile siri ya injili. Kwa nini wengine waliamini na wengine hawakuamini ile siri ya ukuu wa Mungu na mapenzi huru wa mwanadamu. Katika maana iliyo moja huduma ya Paulo kwa viongozi wa Kiyahudi humo Rumi ni mfano wa huduma ya Paulo. Kwanza alishirikiana wa Wayahudi. Alishiriki utimilifu wa Maandiko ya Agano la Kale. Wengine waliamini wengine hawakuamini. Hili pia, lilitabiriwa katika Agano la Kale (kama vile Isa. 6:9-10).

**28:25-27 " Roho Mtakatifu alinena vema na baba zetu, kwa kinywa cha nabii Isaya"** Aya hii inafunua mtazamo wa Paulo wa siri ya kujtoamini kwa taifa la Israeli! Hii nukuu iliyo katika mistariya 26-27 inatokana na Isa. 6:9-10. Yesu alikutumia mstari huu mara kwa mara kwa mwanadamu asiye amini (kama vile Mt. 13:14-15; Marko 4:12; Luka 8:10; Yohana 12:39-40). Kwa wakati huu Paulo alikuwa amekwisha andika kitabu cha Warumi 9-11 (kwa nini Israeli ilimkataa Masihi wake?). Israeli ya Agano la Kale isingeliweza/haikuamini kwa ukamilifu pia. Kulikuwa na makaki ya imani, lakini kulikuwa na umati wa wasioamini.

**28:28 "wokovu huu wa Mungu umepelekwa kwa Mataifa"** Hili linaweza kuwa dokezi la Zaburi 67, hasa Matendo ya Mitume 28:2. Hiki kipengele cha kiulimwengu cha Ukristo ndicho kilichosababisha ghasia katika Yerusalemu na matatizo endelevu kwa Wayahudi. Hili ni la kimatiki na linatokana na Mwa. 1:na Paulo kama mpango wa Mungu wa ukombozi wa milele katika Efe. 2:11-3:13! Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 1:8.

## **MADA MAALUM: MABAKI (BDB 984, KB 1375), NAMNA TATU**

Dhana ya Agano la Kale ya kifungu cha "mabaki matakatifu" ni kigezo cha sasacha Manabii (hasa manabii wa karne ya nane na Yeremia). Neno hili linatumika katika maana tatu:

1. wale waliomudu kuishi ndani ya uhamisho (yaani Ezra 9:8,14-15; Neh. 1:2-3; Isa. 10:20-23; 17:4-6; 37:4,31-32; 46:3; Yer. 23:3; 31:7-8; 42:15,19; 44:12,14,28; Mika 2:12; 5:7-8; 7:18; Hag. 1:12-14; 2:2; Zak. 8:6,11-12)
2. wale waliobaki kuwa waaminifu kwa YHWH (yaani, Isa. 4:1-5; 11:11,16; 28:5; Yoeli 2:32; Amosi 5:14-15)
3. wale walio sehemu ya matengenezo mapya ya siku za mwisho na uumbaji mpya (yaani, Amosi 9:11-15;

Zek. 8:6)

Ule mfano wa udongo katika Marko 4:1-20 na Mt. 13:1-23, ambao unanukuu Isa. 6:9-10, ni mfano mzuri wa namna Agano Jipya linavyolielewa neno hili (pia nukuu Rum. 9:6 katika kuirejelea Israeli ya siku za Paulo).

Haya "mabaki" ya Agano Jipya yameundwa na Wayahudi waliomwamini Kristo (kama vile Rum. 9:27-29) na Mataifa waliomwamini Kristo (kama vile Rum. 9:24-26). Makundi yote yanazungumziwa katika Rum. 9:30-35; 11:11-24,25-32. Kuamini juu ya Israeli si suala la rangi (yaani, Rum. 9:6; 2:18-19), bali kuliadini kundi la wafuasi waaminifu wa mambo mapya wa Mungu, ufunuo kamili katika Yesu. Kulizungumza hili kunaonekana kuwa ni kuyakataa maandiko ya Agano la Kale (yaani, Yer. 31:7-9; Mika 5:7-8) kuhusu taifa la Israeli kuwa mabaki. Tafadhari tazama katika Mada Maalumu yangu: Kwa nini Ahadi za Agano la Kale Zinaonekana kuwa Tofauti Sana na Ahadi za Agano Jipya? Injili hubadilisha kila kitu!

▣ **"nao watasikia"** Huu ni ukweli wa Warumi 9-11. Wayahudi walimkataa Masihi kwa sababu Yeye hakwendana na matarajio yao na kwa sababu hii injili ilifungua mlango wa imani kwa watu wote. Suala la Agano Jipya hakika si Wayahudi dhidi ya Mataifa, bali waamini dhidi ya wasioamini. Jambao hili si kuuliza mama yako ni nani, bali ni kuuliza kama moyo wako u wazi kwa ajili ya Roho wa Mungu na Mwana wa Mungu?!

**28:29** Mstari huu uliondolewa katika machapisho ya kale ya Kiyunani P<sup>74</sup>, ,~~κ~~,A, B, na E. Huu haunekani katika machapisho yo yote ya Kiyunani kabla ya P, ambayo inaangukia karne ya sita b.k. Toleo la UBS<sup>4</sup> inatoa daraja tengefu kama daraja "A" (lenye uhakika).

#### **ANDIKO LA NASB (LILIBORESHWA) : MATENDO YA MITUME 28:30-31**

<sup>30</sup>Akaka muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliyokuwa ameipanga, akawakaribisha watu wote waliokuwa wakimwendea, <sup>31</sup> akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu.

**28:30 "miaka miwili mizima "** Bila shaka kipindi hiki kilikuwa

1. kipindi cha kawaida cha wakati kilichihitajika kumuona Kaizari
2. wakati uliohitajika kupata magazeti toka kwa Festo
3. kipindi cha kusubiri kwa lazima kwa ajili ya ushahidi toka Asia au Yerusalemu
4. kukaribia na amri ya kisheria ya mipaka

Ni katika kipindi hiki Paulo alipoandika barua yake akiwa kifungoni (Wakolosai, Waefeso, Filimoni, na Wafilipi).

▣ **"katika nyumba yake aliyokuwa ameipanga"** Paulo alikuwa na vyanzo vya mapato.

1. Alikuwa akitengeneza mahema au kufanya kazi
2. Alisaidiwa na makanisa (Tesalonika na Filipi)
3. Alikuwa na baadhi za fedha za kurithi

▣ **"akawakaribisha "** Luka alilitumia neno hili mara kwa mara kwa maana nyingine ya "kuwakaribisha kwa moyo" (kama vile Matendo ya Mitume 18:27; 28:30 na *paradechōmai* katika Matendo ya Mitume 15:4). Neno hili lilitumiwa na umati wa watu kumkaribisha Yesu katika Luka 8:40 na 9:11. Neno hili lilitumika kuikaribisha injili kama ilivyohubiriwa na Petro katika Matendo ya Mitume 2:41.

▣ **"wote waliokuwa wakimwendea"** Hili lilikuwa tatizo. Injili ya Paulo imefika ulimwenguni kote. Hii ilikuwa "habari njema" kwa watu wote, si Wayahudi pekee!

**28:31 "akihubiri . . . kuyafundisha"** Wale wa mwanzo, kanisa lililofuatia baada ya Mitume lilitengeneza tofauti kati ya njia hizi mbili za kuuwasilisha ukweli. Jumla ya hotuba iliyonukuliwa katika Matendo ya Mitume (Petro, Stefano, Paulo) kinaitwa *Kerygma* (uenezaji, kama vile Matendo ya Mitume 20:25; 28:31; Rum. 10:8; Gal. 2:2; 1 Kor. 9:27; 2 Tim. 4:2), ambapo mafundisho ya Yesu yaliyofasiriwa katika Nyaraka yanaitwa *Didache* (mafundisho, kama vile Matendo ya Mitume 2:42; 5:28; 13:12; Rum. 16:17; 1 Kor. 14:20).

▣ **" ufalme wa Mungu"** Hili lilikuwa jambo la mahubiri ya Yesu. Aya hii inarejelea juu ya utawala wa Mungu ndani ya moyo wa mwanadamu wa sasa kwamba siku moja utatimizwa duniani kama ilivyo mbinguni. Pia kifungu hiki si kwa Wayahudi pekee. Tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 1:3.

▣ **"bwana"** Neno "Bwana" ni tafsiri ya neno la Kiebrania *adon*, ambalo lilimaanisha "mmiliki, mume, mtawala, au bwana" (tazama [MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU](#) katika Matendo ya Mitume 1:6). Wayahudi walikuwa na woga wa kulitaja jina takatifu la YHWH badala yake walilitumia visivyo na kuvunja mojawapo ya Amri Kumi za Mungu. Kila waliposoma Maandiko, waliondoa jina la *Adon* lenye maana ya YHWH. Hii ndiyo maana tafsiri zetu za Kiingereza zinatimia herufi kubwa zote kwa majina Bwana kwa maana ya YHWH katika Agano la Kale. Kwa kubadilisha jina hili (*kurios* katika Kiyunani) kwa Yesu, waandishi wa kitabu cha Agano Jipya wanaueleza Uungu na ubora Wake pamoja na Baba.

▣ **" Yesu"** Jina "Yesu" ni jina alililopewa na malaika akiwa mtoto Bethlehemu (kama vile Mt. 1:21). Hili limeundwa na nomino mbili za Kiebrani : "YHWH," jina maagano ya Uungu, na "wokovu" (iyaani, Hosea). Hili ni sawa na jina la Kiebrania lililo sawa na jina Yoshua. Hili linapotumika peke yake mara nyingi linamtambulisha mtu, Yesu wa Nazarethi, mwana wa Mariamu (mf. Mt. 1:16, 25; 2:1; 3:13,15,16).

▣ **"Kristo"** Jina "Kristo" ni tafsiri ya Kiyunani ya neno la Kiebrania *Messiah* (yaani, Alitepakwa Mafuta, tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 2:31). Jina hili linaeleza juu ya jina la Yesu la Agano la Kale kama YHWH Aliyehaidiwa kuweka sawa zama mpya za haki.

**NASB** "kwa ujasiri mwing, asikatazwe na mtu "

**NKJV** "kwa ujasiri wote, hapana awezaye kumzuia"

**NRSV** "kwa ushupavu wote na bila kuzuiliwa"

**TEV** "kuzungumza kwa ushupavu wote na uhuru"

**NJB** "kwa ukamilifu usio na woga na pasipo kizuizi cho chote kutoka kwa mtu ye yote"

Mstari huu unaonyesha kwamba mamlaka za Kirumi hazikuufikiria kama ni uasi au hatari. Andiko la Kiyunani linaishia na kielezi "huru" au "isiyozuiliwa." Hili linaonekana kusistiza juu ya asili endelevu ya kazi ya kutangaza na uweza wa Roho. Wengi wamedhani, wamejikita katika Matendo ya Mitume 1:1 matumizi ya neno "kwanza," ambalo linamaanisha zaidi ya mbili, kwamba Luka alikuwa na mpango wa kuandika toleo la tatu. Wengine pia hufikiri kwamba hili toleo la tatu linaweza kuwa Barua za Kichungaji (1 Timotheo, 2 Timotheo na Tito). Kwa neno la Kiyunani (*parrhēsia*), hili linatafsiriwa kama "uwazi" na NASB, tazama Mada Maalum katika Matendo ya Mitume 4:29.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wafasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini kitabu cha Matendo ya Mitume kinahitisha kwa kumuonyesha Paulo akiwa bado gerezani? Kwa nini kinahitimisho la ghafla?
2. Kwa nini Luka anachukua muda murefu akielezea ziara ya Paulo na kubaki kwake Roma?
3. Kwa nini Paulo anajaribu mara nyingi kuwashuhudia Wayahudi kwanza?
4. Eleza tofauti kati ya *Kerygma* na *Didache*.

# TAFASIRI SAHIHI ZA ISTILAHU ZA VISARUFI VYA KIYUNANI

Lugha ya kawaida ya Koine mara nyingi inafahamika kama Kiyunani kilichoboea, ilikuwa ni lugha ya kawaida ya ulimwengu wa Mediterania ilianzishwa na Alexandra mkuu (336-323 B.C) na ikadumu mpaka miaka ya (300 B.C-A.D 500). Haikuwa rahisi, Kiyunani kuwa cha daraja la juu, lakini kwa njia nyingi ni dhana ya Kiyunani ambayo ilikuja kuwa lugha ya pili karibu na mashariki ya kale na ulimwengu wa Mediterania.

Kiyunani cha Agano Jipya kilikuwa ni cha kipekee kwa njia kadhaa kwa watumiaji wake, isipokuwa Luka mwandishi wa kitabu cha Waebrania, yamkini alitumia lugha ya Kiarama kama lugha ya msingi. Kwa hiyo, uandishi wao uliathiliwa na dhana ya muundo wa Kiarama. Pia, walisoma na kunukuu wandishi wa maandiko ya kale (tafasiri ya Kiyunani ya maandiko ya kale) ambayo pia yaliandikwa kwa lugha ya Koine. Lakini maandiko ya kale pia yaliandikwa kwa wasomi wa Kiyahudi ambao lugha yao ya asili ilikuwa sio ya Kiyunani.

Hii ilisaidia kuwa kama kumbukumbu ambayo haiwezi kulipeleka Agano Jipya kwenye muundo mgumu wa kisarufi. Ni wa kipekee na bado una mambo mengi yaliyo pamoja na (1) maandiko ya kale (2) maandiko ya kale kama yale ya Yusufu na (3) mafunjo yaliyopatikana Misri. Kwa hiyo tunakabilianaje na uchambuzi wa visarufi vya Agano Jipya.

Muundo wa kisarufi wa lugha ya Koine na Agano Jipya la lugha ya Koine ulibadilika. Kwa njia tofauti ulikuwa ni urahisishaji wa sarufi. Mazingira ndio yatakuwa mwongozo wetu mkuu. Maneno pekee yana maana katika upanuzi wa mazingira, kwa hiyo, muundo wa kisarufi unaweza tu kueleweka katika mwanga wa (1) aina mahsusi ya mwandishi, na (2) mazingira mahsusi

Hapana hitimisho la fasiri ya dhana na muundo wa Kiyunani unaowezekana. Kimsingi lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ya maneno tu. Mara nyingi msingi wa utafasiri ni aina na dhana ya maneno. Mara nyingi vishazi vikuu hutokea kwanza, vikionyesha kushinda vingine vyote. Katika kueleza kitenzi cha Kiyunani, vipande vitatu vya habari lazima vizingatiwe (1) kiini cha msisitizo wa njeo, sauti na dhamira (tukio au umbo); (2) kiini cha maana husika ya kitenzi (usawidi kamusi); na (3) mtiririko wa mazingira yenyewe (isimu ya mpangilio wa maneno)

## I. NJEO

- A. NJEO au sura inajumuisha uhusiano wa VITENZI ili kukamilisha kitendo au kutokamilisha kitendo. Mara nyingi huitwa “utimilifu” au “utoutimilifu”
  - 1. Njeo timilifu zinaangazia juu ya utoaji wa kitendo. Hakuna taarifa nyingine zilizotolewa isipokuwa ya kile kilichotokea! Kuanza kwake, mwendelezo au ukomo wake haukuelezwa.
  - 2. Njeo zisizo timilifu zinaangazia juu ya mchakato endelevu wa kitendo. Zinaweza kuelezewa dhidi ya unasaba wa kitendo, kudumu kwa kitendo, mwendelezo wa kitendo, n.k.
- B. Njeo zaweza kugawanywa kwa jinsi mwandishi anavyoona kitendo kinavyoendelea.
  - 1. Kimetokea-KITENZI TIMILIFU
  - 2. Kilivyotokea au matokeo yake-KITENZI CHA WAKATI ULIOPIA
  - 3. Kilivyokuwa kikitokea nyuma na matokeo yake yakastahimili, lakini sio sasa-KITENZI CHA WAKATI ULIOPIA TIMILIFU
  - 4. Kinatokea –WAKATI ULIOPO
  - 5. Kilikuwa kikitokea- WAKATI USIOTIMILIFU
  - 6. Kitatokea –WAKATI UJAO

Mfano thabiti wa jinsi njeo hizi zinasaidia katika utafasiri ungalikuwa wa neno “okoa.” Lilitumika katika NJEO nyingi tofauti kuonyesha kwa pamoja mchakato na ukomo.

- 1. KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU- “okolewa” (Rum 8:24)

2. KITENZI CHA WAKATI ULIOPIA- “ameokolewa na matokeo yake yanaendelea” (Efe 2:5,8)
  3. KITENZI CHA WAKATI ULIOPO- “anaokolewa” (cf. 1Kor 1:18; 15:2)
  4. KITENZI CHA WAKATI UJAO- “ataokolewa” (cf. Rum 5:9,10; 10:9)
- C. Katika kuzingatia juu ya VITENZI VYA NJEO, mfasiri huangalia sababu za mwandishi wa kwanza alichagua kuelezea yeye binafsi NJEO fulani. Tarajio la NJEO “hakuna madoido” lilikuwa ni la KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU. Kilikuwa ni muundo wa KITENZI cha kawaida “kisichoainishwa” “kisichotambulika” “kisichochoka.” Chaweza tumika katika Nyanja pana ambamo mazingira lazima yaelezee. Kwa kawaida kilikuwa kinaelezea kuwa kitu fulani kimetendeka. Sura ya muda uliopita ulikusudia tu katika DHAMIRA ELEKEZI. Kama pana NJEO nyingine zilizotumika, uainishaji wa kitu fulani ulikuwa unasisitizwa. Lakini ni nini?
1. NJEO YA WAKATI ULIOPIA. Hii inaongelea juu ya tendo lililokwisha tendeka na matokeo yakiendelea kuwepo. Katika namna fulani ilikuwa ni muunganikano wa NJEO ZA WAKATI TIMILIFU na ZA WAKATI ULIOPIA. Mara kwa mara mlengo ulikuwa juu ya matokeo yalioendelea kuwepo au kumalizika kwa kitendo. Mfano: Efe 2:5 & 8, “umekuwa na unaendelea kuokolewa.”
  2. NJEO YA WAKATI ULIOPIA AINISHI. Hii ilikuwa kama njeo ya WAKATI ULIOPIA isipokuwa matokeo yalishakoma. Mfano: “Petro alikuwa akisimama nje mlangoni” (Yoh 18:16)
  3. NJEO YA WAKATI ULIOPO. Hii inazungumzia juu ya kitendo kisichokiwisha au kisichotimilifu. Mtizamo mara nyingi ni juu ya uendelezaji wa tukio. Mfano: “kila mmoja ashikamanae ndani yake haendelei kutenda dhambi”, “kila mmoja aliyesamehewa na Mungu haendelei kutenda dhambi” (1Yoh 3:6 & 9).
  4. NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU. Katika njee hii uhusiano na NJEO YA WAKATI ULIOPO ni mwendelezo wa uhusiano kati ya WAKATI ULIOPIA na WAKATI ULIOPIA AINISHI. WAKATI USIOTIMILIFU unaongelea juu ya kitendo ambacho hakijaisha kutendeka ambacho kilikuwa kinatokea lakini sasa kimekoma au mwanzo wa kitendo awali. Mfano: “kwa hiyo Yerusalemu yote waliendelea kumwacha” au “ Yerusalemu yote wakaanza kumwacha”(Mt3:5)
  5. NJEO YA WAKATI UJAO. Hii inaongelea juu ya kitendo ambacho kawaida kilijitokeza ndani ya muda mwafaka. Inaangazia juu ya umuhimu wa jambo kutokea kuliko utokeaji wa uhalisia. Mara nyingi unazungumzia juu ya ualakini wa tukio. Mfano: “Heri wale....wata...”(Mt 5:4-9).

## II IRABU

- A. Irabu inaelezea mahusiano kati ya kitendo cha KITENZI na KIIMA
- B. IRABU TENDAJI ilikuwa ni njia ya kawaida, tarajiwa, isiosisitiza utetezi wa kwamba kiima kilikuwa kikitenda kitendo cha KITENZI.
- C. IRABU TENDEWA ina maana kuwa KIIMA kilikuwa kikipokea kitendo cha KITENZI kilichotolewa na mtu wan je. Mtu wa nje anayetoa kitendo alionyeshwa katika Agano Jipya la Kiyunani kwa mambo na VIHUSISHI vifuatavyo:
  1. Mtu binafsi wa moja kwa moja wa *hupo* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22; Mdo 22:30)
  2. Mtu binafsi wa kati na *dia* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22)
  3. Mtu wa kawaida asiyehusika na *en* kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO
  4. Wakati mwingine ni mtu binafsi au asiyehusika kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO pekee.
- D. IRABU YA KATI inamaanisha kuwa KIIMA kinatoa tendo la KITENZI na pia moja kwa moja kinahusishwa katika kitendo cha KITENZI. Mara nyingi huitwa irabu ya kurefusha matakwa binafsi. Muundo huu unasisitiza KIIMA cha kishazi au sentesi kwa namna nyingine. Muunganikano huu haupatikani katika Kiingereza. Una uwezekano mpana wa maana na ufasiri katika Kiyunani. Baadhi ya mifano ya dhana hizi ni;

1. YENYE KUJIREJEA – kitendo cha moja kwa moja cha kiima chenyewe. Mfano: “kajiangika mwenyewe” (Mt 27:5)
2. YENYE KUTIA MKAZO- kiima kinazaa kitendo chake chenyewe. Mfano: “shetani mwenyewe anajifanya kama malaika wa nuru” ( 2Kor 11:14)
3. Kukubaliana – mwingiliano wa viima viwili. Mfano: “walishauliana wao kwa wao” (Mt 26:4)

### III. DHAMIRA (au “NAMNA”)

- A. Kuna namna nne za DHAMIRA katika lugha ya Koine. Zinaashiria uhusiano wa KITENZI kuwa kweli, haswa ndani ya wazo la mwandishi mwenyewe. DHAMIRA hizi zinagawanyika katika namna pana mbili: ile inayoonyesha ukweli (ELEKEZI) na ile inayoonyesha umuhimu (UTEHEMEZI, KUAMURU/KUSHURUTISHA na HALI YA UCHAGUZI).
- B. DHAMIRA ELEKEZI ilikuwa ni NAMNA ya kawaida ya kuelekeza kitendo ambacho kimekwisha tokea au kilikuwa kinatokea, haswa kwenye wazo la mwandishi. Ilikuwa namna pekee ya Kiyunani ya kueleza ukomo wa muda na hata hapa sura hii ilikuwa daraja la pili.
- C. DHAMIRA TEGEMEZI kinaelekeza yumkini kitendo kitakachotokea mbeleni. Kitu fulani ambacho hakijawahi tokea lakini nafasi ya kutokea ingaliwezekana. Ina vitu vingi vinavyofanana na KITENZI CHA WAKATI UJAO ELEKEZI. Utofauti ni kuwa UTEHEMEZI unaelezea kiwango fulani cha mashaka. Katika Kiingereza hii mara nyingi inaelezewa na neno “ingalikuwa”, “ingaliweza”, “yawezekana” au “yenye uwezo”.
- D. DHAMIRA YA UCHAGUZI inaelezea utashi ambao kinadharia unawezekana. Ilifikiliwa ni hatua moja mbele kutoka katika ukweli kuliko HALI YA UTEHEMEZI. HALI YA UCHAGUZI inaelezea uwezekano chini ya hali fulani. HALI YA UCHAGUZI ilikuwa ni nadra katika Agano Jipya. Utumikaji wake mara nyingi kilikuwa ni kifungu maarufu cha Paulo. “yawezekana isiwe” (KJV, Mungu anakataza), kimetumika mara kumi na tano ( cf. Rum 3:4,6,31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14; 11:1,11; 1Kor 6:15; Gal 2:17; 3:21; 6:14) mfano mwingine unapatikana katika Thes 1:38, 20:16, Mdo 8:20 na 1Thes 3:11
- E. DHAMIRA SHURUTISHI inasisitizia juu ya amri ambayo iliwezekana, lakini msisitizo ulikuwa juu ya dhamira ya mnenaji. Inatetea juu ya uwezekano wa hiari na ilishurutishwa juu ya chaguzi za wengine. Kulikuwa na matumizi ya kipekee ya HALI YA KUSHURUTISHA katika maombi na hitaji la mtu wa tatu. Amri hizi zinapatikana tu katika WAKATI ULIOPO na njeo ya WAKATI TIMILIFU katika Agano Jipya.
- F. Baadhi ya visarufi vinabainisha VIAMBATA kama moja aina ya NAMNA. Ni vya kawaida katika Agano Jipya la Kiyunani, mara nyingi vikielezwa kama KIVUMISHI CHA TENDO. Vinatafasiriwa kama muunganiko wa VITENZI vikuu ambavyo vinafanana. Tofauti pana iliwezekana katika utafasiri wa viambata. Ni vizuri kuzirejea tafasiri nyingi za Kiingereza. *The Bible in Twenty Six Translation* kilichochapishwa na Baker ni msaada mkubwa hapa.
- G. KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni njia ya kawaida au “kisichotambulika” cha Kuingiza matokeo. Njeo nyingine, irabu au zilikuwa na ufasiri mahususi ambao mwandishi wa kwanza alihitaji kuwasilisha.

### IV. Kwa mtu ambaye hayuko na uzoefu na lugha ya kiyunani, msaada wa usomaji unaofuata utatoa taarifa inayohitajika;

- A. Friberg, Barbara na Timothy. Analytical Greek New Testament. Grand Rapids: Baker 1988
- B. Marshall, Alfred. Interlinear Greek-English New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1976
- C. Mounce, William D. The Analytical Lexicon to the Greek New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1993
- D. Summer Ray. Essential of the New Testament Greek Nashville: Broadman 1950

- E. Kitaaluma mtangamano wa kozi ya lugha ya Koine unapatikana kupitia taasisi ya Moody Bible iliyoko Chikago II

## V. NOMINO

- A. Ki-isimu, NOMINO zinaainishwa kwa jambo. Jambo ni lile lililoshurutisha dhana ya NOMINO ambayo ilionyesha kuwa na uhusiano na KITENZI na sehemu nyingine ya sentesi. Katika lugha ya Koine kazi nyingi za uhusika zilionyesha na VIHUSISHI. Tangu dhana ya uhusika iliweza kutambua tofauti ya mahusiano mbali mbali, VIHUSISHI vilitokea kutoa utengano mzuri wa kazi hizo.
- B. Uhusika wa Kiyunani uliainishwa kwa njia nane zifuatazo;
1. UHUSIKA WA KIIMA ulitumika kwa ajili ya kutaja na kawaida kilikuwa ni kiima cha sentesi au kishazi. Pia ilitumika kwa NOMINO ARIFU na VIVUMISHI vikiunganishwa na VITENZI “kuwa” au “kufaa”
  2. UHUSIKA MILIKISHI ulitumika kwa ajili ya kuelezea na kawaida ulitoa kivumishi au thamani ya nenolililofanana nalo. Ulijibu swali, “aina gani?” mara nyingi ulielezewa na utumiaji wa KIHUSISHI cha Kiingereza “ya/za”
  3. UHUSIKA WA KUONDOA ulitumia dhana ile ile ya kushurutisha kama ya UMILIKISHI, lakini ulitumika kuelezea utenganifu. Kawaida ulidokeza utengano wa alama kwenye muda, nafasi, kiini, chanzo au degrii. Mara nyingi ulielezewa na matumizi ya KIHUSISHI cha Kiingereza “kutoka”.
  4. UHUSIKA WA WAKATI ulitumika kuelezea matwaka ya mtu binafsi. Hii ingalidokeza mtizamo chanya au hasi. Mara nyingi hiki kilikuwa si kitu cha moja kwa moja. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ya”.
  5. UHUSIKA WA MAHALI ilikuwa dhana shurutishi ya WAKATI, lakini ilielezea mahali au eneo kwenye nafasi, muda au ukomo. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ndani, juu, ni, kati, kwa, juu ya na mbali na”
  6. UHUSIKA WA KUTUMIKA ilikuwa ni dhana shurutishi kama uhusika wa WAKATI na MAHALI. Unaelezea namna au uhusiano. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza cha neno “kwa” au “enye”
  7. UHUSIKA WA KUSHUTUMU ulihusika kuelezea hitimisho la kitendo. Unaelwzea ukomo. Haswa utumikaji wake ulikuwa kwenye dhana ya moja kwa moja. Ulijibu maswali “kwa umbali gani” au “kwa namna gani”
  8. UHUSIKA WA KAULI ulitumika kuelezea moja kwa moja.

## VI. VIUNGO NA VIUNGANISHO

- A. Kiyunani ni lugha sahihi kwa sababu ina viunganishi vingi. Viunganisho fikra ( vishazi, sentesi na aya). Ni vya kawaida kwamba utouwepo wao mara nyingi unakuzwa. Kama jambo la uhakika, viunganisho na viungo hivi vinaonyesha muelekeo wa fikra za mwandishi. Mara nyingi ni vya maana kupima ni kipi haswa anajaribu kukiwakilisha.
- B. Hapa pan orodha ya baadhi ya viunganishi na viungo na maana zake (taarifa hizi zimekusanywa haswa toka kwa H.E Dana na Julius K. Mantery. A Manual Grammar of the Greek New Testament
1. Viunganishi vya wakati
    - (a) *epei, epedē, hopote, hōs, hote, hotan* (TEGEMEZI)- “lini”
    - (b) *heōs*- “wakati”
    - (c) *hotan, epan* (TEGEMEZI)- “kila, wakati wowote”
    - (d) *heōs, achri, mechri* (Tegemezi)- “mpaka”
      - a. *priv* (kitenzijina)- “kabla”
      - b. *hōs*- “tangu”, “lini”, “kama”.



2. Viunganishi venye mantiki

a. Kusudi/dhumuni

- 1) *hina* (TEGEMEZI) *hopōs* (TEGEMEZI) *hōs*- “ya kwamba”, “kuwa”
- 2) *hōste*(KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
- 3) *pros*(KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO) au *eis* (KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”

b. Tokeo (kuna uhusiano wa karibu kati ya kusudio la dhana ya kisarufi na tokeo)

- (1) *hōste*(ISIYO NA KIKOMO, hasa hiki ni cha kawaida)- “ili kwamba”, “hivyo”
- (2) *hiva*(TEGEMEZI)- “ya kwamba”
- (3) *ara*- “kwa kiasi hicho”

c. Chanzo au sababu

- 1) *gar*(chanzo/athari au sababu/hitimisho)- “kwa”, “kwa sababu ya”
- 2) *dio*, *hotiy*- “kwa sababu ya”
- 3) *epei*, *epeidē*, *hōs*- “tangu”
- 4) *dia*(ikiwa na SHUTUMA) na (ikiwa na KIUNGO KISICHO NA UKOMO)- “kwa sababu ya”

d. Maamuzi

- (1) *ara*, *poinun*, *hōste*- “kwa hiyo”
- (2) *dio*(KIUNGO HITIMISHO chenye nguvu)- “kwa sababu ipi”, “kwa nini”, “kwa hiyo basi”
- (3) *oun*- “kwa hiyo basi”, “kwa kiasi hicho”, “hatimaye”, “hivyo basi”
- (4) *tinoun*- “kufuatana na”

e. –a kinyume au tofauti

- (1) *alla*( yenye KINYUME thabiti)- “lakini”, “isipokuwa”
- (2) *de*- “lakini”, “ingawa”, “bado”, “kwa upande mwingine”
- (3) *kai*- “lakini”
- (4) *mentoi*, *oun*- “ingawa”
- (5) *plēn*- “hata hivyo” (haswa katika Luka)
- (6) *oun*- “ingawa”

f. Ulinganifu

- (1) *hōs*, *kathōs* (ingiza vishazi linganifu)
- (2) *kata*(kwa muunganiko, *katho*, *kathoti*, *kathōsper*, *kathaper*)
- (3) *hasos*(katika Kiebrania)
- (4) *ē*- “kuliko”

g. Enye mlolongo au mtiririko

- (1) *de*- “na”, “sasa”
- (2) *kai*- “na”
- (3) *tei*- “na”
- (4) *hina*, *oun*- “kile”
- (5) *oun*- “kasha”(katika Yohana)

3. Matumizi yenye mkazo

- a. *alla*- “kwa hakika”, “naam”, “kwa kweli”
- b. *ara*- “hakika”, agharabu”, “kweli”
- c. *gar*- “lakini kweli”, “agharabu”, “hakika”
- d. *de*- “hakika”
- e. *ean*- “hata”
- f. *kai*- “hata”, “hakika”, “kweli”

- g. *mentoi*- “hakika”
- h. *oun*- “kweli”, “kwa hali zote”

## VII.

- A. SENTESI SHURUTISHI ni ile iliyo na kishazi kimoja au zaidi. Muundo huu wa kisarufi unaongeza utafasiri kwa sababu unatoa amri, sababu au chanzo kwa nini kitendo cha KITENZI kikuu kimetokea au hakikutokea. Palikuwa na aina nne za sentesi shurutishi. Zilitoka kwa zile zilizofikiriwa kuwa kweli toka kwa mtizamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kwa lile alilokuwa na utashi nalo.
- B. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ilielezea kitendo au kile kilichofikiliwa kuwa kweli toka kwa mtimamo wa mwandishi au kusudio lake. Ingawa ilielezwa kwa neno “kama.” Katika mazingira tofauti lingeweza kutafasiriwa “tangu”(cf. Mt 4:3, Rum 8:31). Ingawa hii haimaanishi kudokeza kuwa MADARAJA YA KWANZA yote ni ya kweli. Mara nyingi yalitumika kuweka alama kwenye hoja au kuangazia kosa(cf. Mt 12:27)
- C. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA PILI mara nyingi huitwa “inayopingana na ukweli”. Inaelezea kitu ambacho kilikuwa ni cha uongo kwenye ukweli wa kufanya jambo. Mfano:
  1. “kama kweli alikuwa nabii, ambapo sio, alikuwa sasa nani na mwanamke wa tabia gani anaye mng’ang’ania yeye, lakini hawezi (Thess 7:39)
  2. Kama kweli Musa, lakini hamkumwamini, mngaliniamini na mimi lakini hamkuniamini (Yoh 5:46)
  3. Kama ningalitaka kuwapendezesha wanadamu lakini sivyo, nisingalikuwa mtumwa wa Christo hata sasa(Gal 1:10)
- D. DARAJA LA TATU linaongelea juu ya tukio lijalo ambalo laweza kutokea. Mara nyingi unafikirika uwezekanao wa kitendo kutokea. Kawaida inaashiria tahadhari. Kitendo cha KITENZI kikuu ni tahadhari juu ya tendo la kishazi “hiki”. Mfano toka 1Yoh 1:6-10; 2:4,6,9,15,20,21,24,29; 4:20; 5:14,16
- E. DARAJA LA NNE ni daraja la mbali lililoondolewa kwenye uhakika. Ni adimu katika Agano Jipya. Kama jambo la kweli, hakuna SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA NNE lililokamilika ambamo pande zote za jambo zinastahili maelezo. Mfano wa DARAJA LA NNE ni ufunguzi wa kishazi katika 1Pet 3:14. Mfano wa sehemu DARAJA LA NNE ni katika kuhitimisha kishazi katika Mdo 8:31.

## VIII. VIZUIZI

- A. KITENZI CHA KUAMURU CHA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIAMBATA MĒ mara nyingi (lakini hakitengwi) kina msisitizo wa kusimamisha tendo ambalo liko kwenye mchakato. Baadhi ya mifano: “msijiwekee hazina yenu duniani.....”(Mt 6:19); “msisumbukie maisha yenu.....” ( Mt 6:25); “wala msiendeele kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi.....”(Rum 6:13); “wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu wa Mungu (Efe 4:30) na “tena msilewe kwa mvinyo.....”(Ef 5:18)
- B. KITENZI TEGEMEZI TIMILIFU kina mkazo wa “udhahanifu au mwanzo wa kutenda kitendo” baadhi ya mifano: “msidhani ya kuwa.....”(Mt 5:17); “msisumbuke.....”(Mt 6:31); “msiuonee haya.....”(2Tim 1:8)
- C. KITENZI HASI CHENYE JOZI kikiwa na DHAMIRA TEGEMEZI ni chenye msisitizo hasi. “kamwe, katu” au “kwa hali yeyote ile”. Baadhi ya mifano: “kamwe, hataonja mauti.....”(Yoh 8:51); “hakika, kamwe.....”(1Kor 8:13)

## XI

- A. Katika lugha ya Koine, KIBAINISHI CHA WAZI cha neno “wale, Yule,ile” kina matumizi mfanano na kwenye Kiingereza. Kazi yake kuu ilikuwa ni ya “muonyeshwaji”, ni njia ya kukamata hisia ya neno, jina au kirai.

Utumiaji unatofautiana kati ya mwandishi na mwandishi kwenye Agano Jipya. KIBAINISHI CHA WAZI pia chaweza kutenda

1. Kama chombo cha kutofautisha mfano cha kuonyesha
2. Kama alama ya kurejea KIIMA kilichowekwa awali au mtu
3. Kama njia ya kutambua kiima kwenye sentesi kikiwa na KITENZI kinchounganisha. Mfano: “Mungu ni Roho” Yoh 4:24, “Mungu ni nuru” 1Yoh 1:5; “Mungu ni upendo” 4:8,16

B. Lugha ya Koine haina KIBAINISHI KISICHO CHA WAZI kama ilivyo kwenye Kiingereza cha neno “a” herufi ya kwanza ya alfabeti au “an” mbadala wa “a” kwenye irabu zinazoanza na herufi kama “e”, “h”. Kutokuwepo na KIBAINISHI CHA WAZI chaweza kumaanisha;

1. Mlengo juu ya tabia au thamani ya kitu
2. Mlengo juu ya aina ya kitu

C. Waandishi wa Agano Jipya walitofautiana sana kwa jinsi KIBAINISHI kilivyotumiwa.

#### X NJIA ZA KUONYESHA MKAZO KWENYE AGANO JIPYA LA KIYUNANI

A. Mbinu za kuonyesha msisitizo zinatofautiana toka kwa mwandishi mmoja hadi mwingine kwenye Agano Jipya. Waandishi waendelezaji na warasimishaji walikuwa ni Luka na mwandishi wa Waebrania.

B. Mwanzo kabisa tumesema ya kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni kipimo na kisichoangaliwa kwenye msisitizo, lakini njeo nyingine, irabu au dhamira zina umuhimu wa ufasiri. Hii sio kumaanisha kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI mara nyingi hakikutumika kwenye umakinishaji wa kisarufi. Mfano: Rum 6:10 (mara mbili)

C. Upangiliaji wa neno kwenye lugha ya Koine.

1. Lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ngumu isiyo tegemezi, kama vile Kiingereza, kwenye mpangilio wa maneno. Kwa hiyo mwandishi angaliweza kutofautiana kwenye mpangilio wa kawaida aliotegemea kuonyesha.

- a. Kile mwandishi alihitaji kusisitiza kwa viongozi
- b. Kile mwandishi angalikishangaza kwa viongozi
- c. Kile mwandishi alichosikia toka ndani

2. Mpangilio wa kawaida wa neno kwenye Kiyunani bado ni jambo ambalo halijatulia ingawa mpangilio wa kawaida unaokusudiwa ni

a. Kiunganishi cha VITENZI/Vitenzi unganishi

- (1) KITENZI
- (2) KIIMA
- (3) SIFA

b. VITENZI elekezi

- (1) KITENZI
- (2) KIIMA
- (3) KISHAMILISHI
- (4) KISHAMILISHI KISICHO DHAHIRI
- (5) KIRAI HUSISHI

c. Virai vya NOMINO

- (1) NOMINO
- (2) KIVUMISHI
- (3) KIRAI HUSISHI

3. Mpangilio wa neno waweza kuwa muhimu mno kwenye upangiliaji wake. Mfano:

- a. “walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika” (Gal 2:9) kirai “mkono wa kuume wa shirika” imegawanyika na kuwekwa mbele kuonyesha umuhimu wake.
  - b. Pamoja na Kristo (Gal 2:20), iliwekwa kwanza kifo chake kilikuwa kiini.
  - c. “ni sehemu nyingi na kwa njia nyingi” (Ebr 1:1), iliwekwa kwanza. Ilikuwa ni kwa namna Mungu alivyojidhihilisha mwenyewe kwa tofauti na sio ukweli wa mafunuo.
- D. Kawaida kwa kiasi fulani cha degrii ya msisitizo ulionyeshwa na
1. Urudiaji wa KIWAKILISHI ambacho tayari kilikuwepo katika KITENZI kilichonyambulika. Mfano: “mimi mwenyewe, hakika nitakuwa nawe.....”(Mt 28:20)
  2. Ukosekanaji wa KIUNGO tarajiwa, au kitu kingine cha kuunganisha maneno, virai, vishazi au sentesi. Hii inaitwa (isiofungamana). Kitu unganishi kilikuwa ni
    - a. Ibada ya kubarikiwa kwa Kristo, Mt 5:3 ff(ikisisitizia orodha)
    - b. Yohana 14:1 (maada mpya)
    - c. Rumi 9:1 (kifungu kipya)
    - d. 2Kor 12:20 ( inasisitizia orodha)
  3. Urudiaji wa maneno au virai vilivyomo katika mazingira tajwa. Mfano: “usifwiwe utukufu wa neema yake” (Efe 1:6, 12 & 14). Kirai hiki kilitumika kuonyesha kazi ya kila mtu wa utatu.
  4. Utumiaji wa nahau au neno (sauti) unakaa kati ya istilahi.
    - a. Tasifida- maneno mbadala kwa viima vyenye miiko kama “lala” kwa kifo (Yoh 11:11-14) au “nyayo” kwa viungo vya uzazi vya kiume (Ruth 3:7-8; 1Sam 24:3)
    - b. Maneno ya kuzunguka- mbadala wa maneno kwa jina la Mungu, kama “ufalme wa mbingu” (Mt 3:21) au “sauti toka mbinguni” (Mt 3:17)
    - c. Maumbo ya hotuba
      - (1) Kutowezekana kuyakuza (Mt 3:9; 5:29-30; 19:24)
      - (2) Upole wa maelezo (Mt 3:5; Mdo 2:36)
      - (3) Mfano halisi wa (1Kor 15:55)
      - (4) Kejeli (Gal 5:12)
      - (5) Dondoo za kishairi (Flp 2:6-11)
      - (6) Mvumo unaokaa kati ya maneno
        - (a) “kanisa”
          - i. “kanisa” (Efe 3:21)
          - ii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)
          - iii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)
        - (b) “huru “
          - i. “Mwanamke huru” (Gal 4:31)
          - ii. “uhuru” (Gal 5:1)
          - iii. “huru” (Gal 5:1)
    - d. Lugha ya kinahau- ni lugha ambayo mara nyingi ni ya kitamaduni na lugha bayana
      - (1) Hii ilikuwa ni matumizi ya kistiari ya neno “chakula” (Yoh 4:31-34)
      - (2) Hii ilikuwa ni matumizi ya kiistiari ya neno “hekalu” (Yoh 2:19; Mt 26:61)
      - (3) Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya kuonyesha huruma, ya neno “chukia” (Mwa. 29:31; Kumb.21:15; Thess 14:36; Yoh 12:25; Rum 9:13)
      - (4) “wote” dhidi ya “wengi”. Linganisha Isa. 53:6 (“wote”) na 53:11 & 12 (“wengi”). Istilahi hizi zina maneno sawa kama Rum 5:18 na 19 kama inavyoonyesha.
  5. Utumiaji wa kifungu cha isimu moja kwa moja badala ya neno moja. Mfano: “Bwana Yesu Kristo”.
  6. Utumiaji maalumu wa neno *autos*

- a. Wakati likiwa na KIFUNGU (nafasi ya kivumishi angama) kilichofasiliwa “sawa”
  - b. Wakati bila KIFUNGU (nafasi ya kuarifu) kilitafasiliwa kama KIWAKILISHI CHENYE MKAZO CHA KUJIREJEA- “mwenyewe jinsia ya ME” “mwenyewe jinsia ya KE” au “yenyewe/chenyewe”
- E. Wanafunzi wa Biblia wasio weza soma Kiyunani waweza kutambua mkazo katika Nyanja tofauti:
1. Utumiaji wa misamiati ya kichambuzi na andiko nasaba la Kiyunani/ Kiingereza.
  2. Mlinganyo wa fasili za Kiingereza, hasa toka kwa nadharia za fasiri zinazotofautiana. Mfano: ufasiri mlinganyo wa “neni kwa neno” (KJV, NKJV, ASV, NASB, RSV, NRSV) na “mfanano wa karibu” (William, NIV, NEB, REB, JB, NJB, TEV)  
Msaada mzuri hapa ungalikuwa ni ule toka *The Bible in Twenty-Six Translation* kilichochapishwa na Baker.
  3. Utumiaji wa *The Emphasized Bible* cha Joseph Bryant Rotherham (Kregel, 1994).
  4. Utumiaji wa tafasiri yenyewe.
    - a. *The American Standard Version* ya mwaka 1901
    - b. Young’s Lateral Translation of the Bible cha Robert Young (Guardian Press, 1976)

Usofaji wa kisarufi unachosha lakini unafaa kwa ufasiri mzuri. Maelezo hasa sahihi, maoni na mifano inahamasisha na kuwaamusha watu wasiojua Kiyunani kutumia mihitasari ya kisarufi iliyotumiwa kwenye juzuu hii. Hakika maana hizi zimerahisishwa zaidi. Zisingaliweza kutumika katika hali madhubuti na a kulazimisha, lakini kama ngazi ya kupandia kwenda kwenye uelewa mkubwa wa isimu za Agano Jipya. Kimatumaini maana hizi zitawawezesha wasofaji kuelewa maoni ya msaada mwingine wa usofaji kama vile maoni ya kiufundi juu ya Agano Jipya.

Ni lazima tuweze kuthibitisha ufasiri wetu uliolenga kwenye habari iliyopatikana kwenye maandishi ya Biblia. Sarufi ni moja ya msaada mkubwa wa vipengere hivi, vipengere vingine vingalijumuisha muundo wa kihistoria, maandishi ya kifasihi, utumiaji wa neno la wakati ule ule na dondoo zinazorandana.

# Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi

Somo hili litajikita kwa namna moja kutoa maelezo yanayopatikana katika maoni haya.

Mhutasari ufuatao utahusika

- I. Vyanzo vya maelezo ya Biblia zetu za Kiingereza
    - A. Agano la Kale
    - B. Agano Jipya
  - II. Maelezo mafupi ya matatizo na nadharia ya “maoni dhaifu” pia yanaitwa “uhakiki wa maandiko”
  - III. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya usomaji wa badaye
- I. Vyanzo vya maandiko ya Biblia yetu ya Kiingereza

A. Agano la Kale

1. Machapisho ya kale ya Kiebrania ya karne ya kumi na tisa (MT)-maandiko ya konsonanti za Kiebrania yalipangwa na Rabbi Aquiba miaka 100 Baada ya Kristo. Nukta za irabu na lafudhinukuu za pembeni, vituo vya uandishi na alama za nukta zilizoongezwa katika karne ya sita Baada ya Kristo na vilihitimishwa katika karne ya tisa Baada ya Kristo. Yalifanywa na familia ya wasomi wa Kiyahudi wajulikanao kama Wana-maandiko ya Kale ya Kiebrania. Muundo wa maandiko walioutumia ulikuwa sawa na ule katika Mishnah, Talmud, Targums, Peshitta, na Vulgate.
2. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania (LXX) –Utamaduni unasema Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania ilitengenezwa na wasomi wa Kiyahudi 70 katika siku 70 katika maktaba ya Alexandria chini ya ufadhili wa Mfalme Ptolemy wa II (285-246 K.K). Tafsiri ilidhaniwa kuwa matakwa ya kiongozi wa Kiyahudi aliyeishi katika Alexandria. Utamaduni huu unatokana na “Herufi Aristeas.” Mara kwa mara Tafsiri ya Agano Kale(LXX) ilijikita katika kutofautiana kwa utamaduni wa maandishi ya Kiebrania kutoka katika maandishi ya Rabbi Aquiba (MT).
3. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (MBC)-Michoro ya Bahari ya Chumvi -iliandikwa huko Ruma kipindi cha K.K(200 Kabla ya Kristo hadi Baada ya Kristo 70) na madhehebu ya Kiyahudi waliojitenga waitwao “ Esene”. Machapisho ya Kiebrania, yalikutwa katika sehemu nyingi kandokando ya Bahari ya Chumvi yakionyesha baadhi ya zile tofauti za machapisho ya familia za Kiebrania nyuma ya Machapisho ya Kale ya Kiebrania (MKK)na Tafsiri za Kale za Kiebrania (70).
4. Baadhi ya mifano ya mahususi ni kwa namna gani ulinganifu wa maandishi haya imewasaidia wakalimani kulielewa Agano la Kale.
  - a. Tafsiri za Kale za Kiebrania zimewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa maandishi ya Kale ya Kiebrania.
    - (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania za Isa. 52:14, “Kama vile wengi watakavyo shangazwa Naye.”
    - (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania ya Isa. 52:14, “Bado kama vile wengi walivyo staajabishwa Nawe.”
    - (3) Katika Isa. 52:15 tofauti ya kiwakilishi cha Tafsiri za Kale za Kiebrania imehakikishwa
      - (a) Tafsiri za Kale za Kiebrania, “hivyo mataifa mengi yatashangazwa naye”
      - (b) Maandishi ya Kale ya Kiebrania, “hivyo yeye ameyatapakaza mataifa mengi”
  - b. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) yamewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa Maandishi ya Kale ya Kiebrania
    - (1) Mafunjo ya Bahari ya Chumvi ya Isa. 21:8, “ndipo akalia Karibu na mlinzi wa mnara nilipo simama.”
    - (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania (MT) ya Isa. 21:8, “ndipo akalia kama simba, Ee Bwana, mimi nasimama daima juu ya mnara wakati wa mchana.....”
  - c. Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) zote zilisaidia kuichuja Isa. 53:11
    - (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari Chumvi (DSS), “Baada ya kutaabika sana, mtumishi wangu atafurahi. Kwa kuwajibika kwake kikimilifu, atatosheka na matokeo hayo.”

- (2) Maandishi ya Kale ya Kale ya Kiebrania (MT), “Ataona —ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki Atawafanya wengi kuwa wenye haki.”

B. Agano Jipya

1. Maandishi yapatayo 5,300 yote au sehemu za Agano Jipya la Kiyunani yapo hadi leo. Yapatayo 85 yameandikwa katika karatasi za mafunjo na 268 ni maandishi yaliyoandikwa yote kwa herufi kubwa (maandiko adimu) Baadaye, mnamo karne ya tisa B.K., maandishi yaliyo somwa (madogo sana) yalikuwika. Maandishi ya Kiyunani yaliandikwa kutoka namba zipatazo 2,700. Pia tunazo nakala zipatazo 2,100 za orodha ya Machapisho ya maandiko Matakatifu yalitumika katika kuabudu ambayo tunaita misale ya waumini.
2. Machapisho ya Kiyunani yapatayo 85 yaliyokuwa na sehemu za Agano Jipya zilizoandikwa katika karatasi za mafunjo yamejengewa katika makumbusho. Baadhi yao yamewekwa katika kipindi maalumu kutoka karne ya pili A.D., yaliyo mengi ni kuanzia karne za tatu na nne A.D. Hakuna kati ya machapisho ya kale. Hizi zilizo na Agano Jipya Kamili. Hii ni kwa sababu hizi ni nakala za kale za Agano Jipya hazimaanishi kuwa sio ya kujiendesha yenyewe zina tofauti chache. Zilizo nyingizilinkuliwa kwa kasi kwa matumizi ya kawaida. Utunzaji haukuzingatiwa katika utendaji. Hivyo, zina utofauti mwingi.
3. Kitabu cha miswada ya kale chenye maandishi ya Kale ya Kiyunani ya karne ya nne B.K. kinachojulikana kwa herufi ya Kiebrania  $\aleph$  (aleph) au (01), iliyokutwa katika nyumba ya Mt. Katarina juu ya Mlima Sinai na Tischendorf. Tarehe yake imeandikwa kuanzia karne ya nne B.K. iliyokuwa na zote Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na za Agano Jipya la Kiyunani. Ni aina ya “Maandishi ya Kialekzandria.”
4. Kitabu cha miswada ya Kale cha Alexandrianus, kijulikanacho kama “A” au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayo ilipatikana katika Alexandria, Misri.
5. Kitabu cha miswada ya Kale cha Machapisho ya Kiyunani cha karne ya nne, kijulikanacho kama “B” au (03), iliyopatikana katika maktaba ya Vatikani katika Roma na imeandikiwa tarehe kuanzia katikati ya karne ya nne B.K. Ina zote Tafsiri za Kale za Kiebrania za Agano la Kale na Agano Jipya la Kiyunani. Yalikuwa aina ya “Maandishi ya Kialekzandria.”
6. Kitabu cha miswada ya kale cha Ephraemi, kijulikanacho kama “C” au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayokwa makusudi yaliaribiwa.
7. Kitabu cha miswada ya Kale cha Bazae, kijulikanacho kama “D” au (05), machapisho ya Kiyunani ya karne ya kwanza ya tano au sita. Ni mwakilishi mkuu wa kile kinachojulikana kama “Maandishi ya Magharibi.” Ina maongezeko mengi ulikuwa ushahidi mkuu wa tafsiri ya Mfalme James.
8. Agano Jipya la machapisho ya kale yanaweza kuwekwa katika makundi matatu, kadria nne, familia ambazo zimeshiriki sifa fulani.
  - a. Maandishi ya Kialekzandria kutoka Misri
    - (1) P<sup>75</sup>, P<sup>76</sup> ( yapata 200 B. K.), ambayo inachukua kumbukumbu ya Injili.
    - (2) P<sup>46</sup> (yapata 225 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya barua za Paulo
    - (3) P<sup>72</sup> (yapata 225-250 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya Petro na Yuda
    - (4) Kitabu cha miswada ya Kale B, kiitwacho Viticanus (mnamo 325 B. K), ambacho kimebeba Agano la Kale zima na Agano Jipya
    - (5) Origen alinukuu kutoka aina hii ya maandiko
    - (6) Machapisho ya kale mengine ambayo yanaonyesha aina hii ya maandishi ni  $\aleph$ , C, L, W, 33
  - b. Maandishi ya Magharibi kutoka Afrika ya Kaskazini
    - (1) alinukuu kutoka wakuu wa kanisa wa Afrika ya Kaskazini, Tertullian, Cyprian, na tafsiri za Kale za Kilatini
    - (2) yalinukuliwa kutoka Irenaeus
    - (3) ilinukuliwa kutoka Kilatini na tafsiri za kale za Kisiria
    - (4) Andiko D la Machapisho ya kale “Bazae” ilifuata aina ya maandishi haya
  - c. Byzantine Mashariki kutoka Constantinople
    - (1) aina ya maandishi inaakisiwa katika 80% ya 5,300 MSS

- (2) ilinukuliwa na kanisa la mapadre wa Antiokia ya Silia, Cappadoceans, Chrisostom, natherodoret
- (3) Andiko A la machapisho ya kale, katika Injili tu
- (4) Andiko E la machapisho ya kale, (karne ya nane) ya Agano Jipya
- d. aina ya nne iwezekanayo ni ya “Kikaizari” kutoka Palestina
  - (1) kwanza inaonekana katika Mrko tu
  - (2) baadhi ya shuhuda zake ni P<sup>45</sup> na W

## II. Matatizo na nadharia ya “ukosoaji dhaifu.”

### A. Ni kwa namna gani tofauti zilitokea

- 1. isio angalifu au bila kukusudia (matukio mengi mno)
  - a. makosa madogo madogo ya macho katika kunakili kwa mkono ambapo ulisomwa mfano wa pili wa maneno yanayofanana na pale ambapo yanaondoa maneno yote katikati (mfanano wa maneno)
    - (1) makosa madogo madogo ya macho katika kuondoa maneno ya herufi jozi au vifungu (urudiaji wa maneno)
    - (2) makosa madogo madogo ya kumbukumbu katika kurudia kifungu au msitari wa maandishi ya Kiyunani (mshabaha ule ule)
  - b. makosa madogo madogo ya masikio katika kunakili maneno ya imla ambapo makosa ya kiuandishi hutokea (itacism). Mara nyingi makosa ya kiuandishi hudokeza au kutaja herufizenye mfananowa sauti za maneno ya Kiyunani.
  - c. maandishi ya Kiyunani ya kale hayakuwa na sura au mgawanyo wa mistari, chache au alama za uandishi na hakuna mgawanyo kati ya maneno. Inawezekana kuzigawa herufi katika nafasi kuunda maneno tofauti.
- 2. makusudi
  - a. mabadiliko yalifanywa ili kufanikisha muundo wa kisarufi wa maandishi yaliyo nakiliwa
  - b. mabadiliko yalifanywa ili kuyaleta maandiko katika ulinganifu na maandiko mengine ya kibiblia (mlinganyosambamba)
  - c. mabadiliko yalifanywa kwa kuuunganisha masomo mawili au zaidi yaliyokuwa tofauti katika muungano mmoja wa maandishi marefu (conflation)
  - d. mabadiliko yalifanywa kusahihisha makosa yaliyotambuliwa katika maandishi ( cf. I Kor. 11-27 na I Yohana 5:7-8)
  - e. baadhi ya taarifa za nyongeza kama mpangilio wa kihistoria au ufafanuzi sahihi wa maandishi uliwekwa pembezoni kwa nakala moja lakini zilihamishiwa katika maandishi kwa kuzinakili mara ya pili ( Yohana 5:4)

### B. Mafundisho muhimu ya ukosoaji wa maandiko (mwongozo wa kimantiki ili kubainisha usomaji halisi wa maandishi wakati tofauti inapojitokeza)

- 1. maandishi ambayo hayakuwa na ustadi zaidi au ambayo hayakuwa muhimu kisarufi yamkini ni halisi
- 2. maandishi mafupi zaidi yamkini ni halisi
- 3. maandishi ya kale yamepewa uzito zaidi kwa sababu ya ukaribu wake kihistoria katika uhalisia, kila kitu kuwa sawa zaidi
- 4. Machapisho ya kale ni namna mbali mbali ya kijiografia mara nyingi yana usomaji halisi
- 5. Kimafundisho maandishi ya wanyonge, hasa yale yanayohusiana na majadiliano makuu ya kitheolojia ya kipindi cha mabadiliko ya machapisho kama Utatu katika Yohana 5:7-8, yanapaswa kupendelewa.
- 6. maandishi ambayo yanaweza kuelezea zaidiasili ya tofauti zingine
- 7. nukuu mbili ambazozinzsaidia kuonyesha usawa katika tofauti zinazotaabisha
  - a. kitabu cha J. Harold Greenless, *Introduction to New Testament Textual Criticism*, “Hakuna mafundisho ya Kikristo yanayoning’inia juu ya maandishi yenye kujadiliwa; na



mwanafunzi wa Agano wa Jipya anapaswa kuyatambua maandiko yake anayoyataka kuwa mwenye imani zaidi au kuwa mwenye nguvu kimapundisho kuliko msukumo asilia” (uk. 68).

- b. W. A. Criswell alimwambia Greg Garrison ya *The Birmingham News ambayo yeye (Criswell)* haamini kila neno katika Biblia ni la kutia moyo “angalau si kila neno ambalo limekwisha kutolewa kwa alaiki ya kisasa kwa karne za watafsiri.” Criswell alisema “Mimi ni mwamini sana katika ukosoaji wa maandishi. Kama vile, Nafikiri, nusu ya sura ya 16 ya Marko ni uasi: haitii moyo, imebuniwa...Unapolinganisha machapisho hayo kwa kurudi huko nyuma, hakukuwa na kitu kama hicho kama lilehitimisho la Kitabu cha Marko. Mtu fulani alikiongeza...” Mababa wa uzao wa SBC wasio wakoaji walidai kuwa “kutia maneno yasiokuwepo katika kitabu” pia ni dhahiri katika Yohana, uwajibikaji wa Yesu katika bwawa la Bethesda. Na alijadili tofauti mbili za uwajibikaji wa kujinyonga kwa Yuda ( Mt. 27 na Matendo 1): “Ni maoni tofauti ya kujinyonga,” Criswell alisema “Kama iko katika Biblia, kuna maelezo yake. Na hatia mbili za kujinyonga kwa Yuda ziko katika Biblia.”Criswell aliongeza, “Ukosoaji wa Maandishi nisayansi ya ajabu ndani yake yenyewe. Si ya muda mfupi kupita, si isiyo husiana.Ni yenye nguvu na kuu...”

### III. Matatizo ya machapisho (ukosoaji wa maandishi)

#### A. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya kusoma zaidi

1. *Biblical Criticism, Historical, Literary and Textual*, na R. H. Harrison
2. *The Textual of the New Testment: Its Transmission, Corruption and Restoration*, na Bruce M. Metzger
3. *Introduction to New Testament Textual Criticism*, na J. H Greenlee

# SIMULIZI ZA AGANO LA KALE

## I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Uhusiano kati ya Agano la Kale na namna nyingin za upangaji wa matukio
  1. Fasihi nyingine ya Mashariki ya Karibu ni ya kubuni
    - a. ni ya kimiungu (mara nyingi miungu ya kibinadamu inaaksi nguvu za asili lakini kwa kutumia vipengele vya mgogoro binafsi miongoni mwao) iliegemea juu ya asili ya mkusanyiko wa matukio (kufa na kufufuka kwa miungu)
  2. Greco-Roman ni kwa ajili ya kufurahisha na kutia moyo kuliko kuchukua kumbukumbu ya matukio ya kihistoria pekee (Homer katika namna nyingi huakisi vile vipengele vya ki-Mesopotamia vinavyojirudia mara kwa mara)
- B. Yumkini matumizi ya maneno matatu ya Kijerumani yanaeleza utofauti katika aina ama ufafanuzi wa historia
  1. "Historie," uchukuaji kumbukumbu ya matukio (ufafanuzi wa kuidani)
  2. "Geschichte," kufasiri matukio yanayoonyesha umuhimu wake kwa mwanadamu
  3. Heilsgeschichte" neno linalorejelea kwa upekee juu ya mpango wa Mungu wa ukombozi na kazi iliyo ndani ya matendo ya kihistoria
- C. Simulizi ya Agano la Kale na Agano Jipya ni "Geschichte" ambayo yanapelekea kulielewa vema neno Heilsgeschichte; haya ni masimulizi ya matukio ya kihistoria yaliyobobea katika uchambuzi wa kthiolojia
  1. matukio yaliyochambuliwa tu
  2. mpangilio si muhimu kama theolojia
  3. matukio yaliyowekwa katika mafungu mafungu ili kuuufunua ukweli

Simulizi ni namna ya kawaida katika Agano la Kale. Imekuwa ikidhaniwa kwamba 40% ya Agano la Kale ni simulizi. Hivyo, aina hii inatumiwa na Roho katika kuwasilisha ujumbe wa Mungu na sifa yake kwa mwanadamu aliyeanguka. Lakini, hili linafanyika, si kwa kudhahania (kama Nyaraka za Agano Jipya), bali kwa vidokezo, muhtasari, au majibizano yaliyochambuliwa /mazungumzo ya aina moja. Yampasa mtu kuendelea kujiuliza kwa nini hili limechukuliwa kumbukumbu. Hili linajaribu kusistiza nini? Ni kusudi gani la kithiolojia? Hili haliwezi kuwa na maana ya kushusha thamani ya historia. Lakini, hii ni historia kama alivyo mtumishi na ulivyo mwelekeo wa ufunuo.

## II. Simulizi za Kibiblia

- A. Mungu yu hai katika neno lake. Waandishi wa Biblia waliovuviwa wanachagua matukio Fulani kumdhilisha Mungu. Mungu ndiye mhusika mkuu wa Agano la Kale.
- B. Kila simulizi inatenda kwa njia mbali mbali:
  1. Mungu ni nani na anafanya nini katika dunia
  2. Mwanadamu anadhihilishwa kupitia pale Mungu anaposhughulika na watu pekee na utambulisho wa kitaifa
  3. Kama mfano mahususi ulioutambua ushindi wa kijeshi wa Yoshua uliohusianishwa na utekelezaji wa agano (kama vile 1 :7-8; 8:30-35)
- C. Mara nyingi simulizi zinajiweka pamoja kufanya sehemu kubwa ya fasihi ambayo inadhihirisha ukweli.

## III. Kanuni za ufasiri wa simulizi za Agano la kale

- A. Majadiliano mazuri niliyoyaona kuhusu kutafasiri simulizi za agano la kale ni kutoka kwa Douglas Stuart *in How to Read the Bible For All Its Worth*, kur. 83-84
  1. simulizi za agano la kale mara nyingi hazifundishi moja kwa moja maandiko

2. simulizi za agano la kale zinaelezea mafundisho yaliyofundishwa sawia mahali popote
  3. simulizi zinaweka kumbukumbu kile kilichotokea-sio lazima kuwika kile kingaliweza kutokea au kingetokea kila wakati. Kwa hiyo, sio kila simulizi zina uadilifu wa kipekee wenye kutambulika wa habari.
  4. Kile watu wanakifanya katika simulizi sio mfano mzuri wa muhimu kwetu. Mara nyingi, huwa tofauti.
  5. Wengi wa wahusika katika simulizi za Agano la Kale wako mbali na ukweli, na matendo yao pia.
  6. Mara zote hatuambia mwisho wa masimulizi ikiwa kile kilichotokea kilikuwa ni chema au kibaya. Tunatarajia kuweza kuhukumu kuwa katika msingi wa kile Mungu alichotufundisha moja kwa moja pasipo shaka sehemu yeyote katika maandiko
  7. Simulizi zote ni za kiuchaguzi na zisizo kamilika. Sio kwamba maelezo yote muhimu mara zote hutolewa (kama vile Yn. 21:25). Kile kinachotokea katika simulizi ni chote kile mwandishi aliyevuviwa anafikiri kuwa muhimu kwetu kukielewa.
  8. Simulizi hazikuandikwa kujibu maswali yote ya kithiolojia. Haswa yamewekewa makusudi maalum yaliyo na mipaka na kushughulika na masuala Fulani, na kuyaacha mengine kushughulikiwa kwa namna nyingine
  9. Simulizi zaweza kufundisha huenda kwa uwazi (kwa kuanzisha kitu Fulani) au kwa kutokuwa wazi (kwa wazi yakidokeza kitu Fulani bila kukianzisha).
  10. Mwishoni mwa utafiti, Mungu anabaki kuwa mshindi wa simulizi za Kibiblia.
- B. Majadiliano mengine mazuri juu ya kuzitafasili simulizi yanapatikana katika Walter Kaiser dhidi ya uafafanuzi wa maandiko ya kithiolojia.

Dhana pekee ya usimuliaji wa sehemu ya maandiko ni kuwa mwandishi mara zote anaruhusu maneno na vitendo vya watu katika simulizi yake kuelezea kiini cha msukumo wa ujumbe wake. Hivyo basi, badala ya kutuelezea sisi kwa maelezo ya moja kwa moja, kama yale yanayopatikana kwenye madhehebu au sehemu ya mafundisho ya maandiko, mwandishi anajaribu kubaki kwa kiasi Fulani katika mazingira kwa namna ya mafundisho au maelezo ya kitathimini yanavyohusika. Kwa matokeo hayo, ikajakuwa muhimu kabisa kutambua muktadha mpana ambao simulizi zitaingiliana na kujiuliza kwa nini mwandishi ulitumia uchaguzi maalum wa matukio katika utaratibu maalum aliouweka. Mfanano wa ushahidi kumaanisha sasa utakuwa ni mpangilio wa matukio na uchaguzi wa maelezo toka kwenye mkanganyiko wa wahubiri, watu, au matukio. Zaidi, uitikiaji wa ki-Mungu na ukadiriaji wa watu hawa na matukio lazima mara zote yapimwe kwa namna mwandishi anavyomruhusu mtu mmoja au kikundi cha watu kuitikia kwa kiwango cha juu cha utaratibu uliochaguliwa wa matukio; yaani, kama hakuingilia kati simulizi kutoa yak wake(kwa mfano, tathimini ya Mungu kwa kile kilichochukua nafasi”(uk.205)

- C. Katika simulizi ukweli hupatikana katika sehemu yote ya fasihi na sio katika maelezo. Uwe mwangalifu kwenye uhakiki wa maandiko au utumiaji wa simulizi za Agano la Kale kama ulivyowasilishwa kwa ajili ya maisha yako.
- IV. Madaraja mawili ya utafasiri
- A. Matendo ya ukombozi wa YHWH, na mafunuo kwa ajili ya uzao wa Abraham
  - B. Mapenzi ya YHWH kwa ajili ya maisha ya kila mwamini(kwa kila rika)
  - C. Wa kwanza unatazamisha juu ya “kumjua Mungu(wokovu); wa pili ni namna ya kumtumikia Yeye(imani ya maisha ya Mkristo, kama vile Rum.1 5:4; I Kor. 1 0:6,1 1

## UFAFANUZI/FAHARASA

**Uasilishaji.** Hili ni moja kati ya maoni ya kale ya uhusiano wa Yesu na Uungu. Kimsingi inadai kwamba Yesu alikuwa mwanadamu wa kawaida kwa kila namna na alichukuliwa na Mungu kwa kazi maalumu katika ubatizo wake (Mt. 3:17; Marko 1:11) au katika ufufuo Wake (cf. Rum.1:4). Yesu aliyaishi maisha haya kama mfano ambao Mungu, kwa kiasi chake, (ubatizo, ufufuo) uliyomuasilisha Yeye kama “mwana” Wake (Rum.1:4 Flp. 2:9). Hili lilikuwa kanisa la mwanzo na maoni ya watu wa karne ya nane. Badala ya Mungu kuwa mwanadamu (umbo la kibinadamu) akalirejeresha hili na sasa mwanadamu anakuwa Mungu!

Ni vigumu kusema namna gani Yesu, Mungu Mwana, Uungu uliokuwepo kabla alivyo zawadiwa au kuwa mbadala kwa ajili ya maisha yenye mfano. Kama Yeye alikuwa tayari ni Mungu, ni kwa namna gani Yeye alitolewa kama zadiwa? Kama Yeye alikuwa na utukufu wa Kiungu wa awali ni kwa namna gani Yeye angeliheshimiwa zaidi? Ingawa ni vigumu kwetu sisi kutambua, kwa namna Baba alivyomuheshimu Yesu katika dhana maalumu ya ukamilifu Wake wa kuyatimiza mapenzi ya Baba.

**Shule ya Alexandria.** Njia hii ya ukalimani wa kibiblia ilikuzwa katika Alexandria, Misri katika karne ya pili B.K. Inatumia misingi ya kanuni za ukalimani ya Philo, ambaye alikuwa mfuasi wa Pilato, mara nyingi inaitwa njia ya kiistiari. Ilitawaliwa katika kanisa hadi wakati wa Marekebicho. Watetezi wake zaidi walikuwa Origen na Augustine. Tazama Moisea Silva, *Has The church Misred The Bible?* (Academic, 1987)

**Ufuasi wa Alexandria.** Haya ni machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano kutoka mji wa Alexandria, Misri ikijumuisha Agano la Kale, lililothibitishwa, pamoja na Agano Jipya. Ni moja ya ushahidi wetu mkubwa katika Agano Jipya zima la Kiyunani (isipokuwa sehemu za kitabu cha Mathayo, Yohana, na II Wakorintho). Wakati ambapo machapisho haya, ambayo yanapewa alama “A, na machapisho ya alama “B” (ya Vatican) yanaafiki juu ya usomaji unaofikiwa kuwa ya mwanzo na baadhi ya wasomi.

**Istiari.** Hii ni aina ya ukalimani wa kibiblia ambayo kiasili ulianzishwa ndani ya dini ya Kiyahudi huko Alexandria. Ilienezwa na Philo wa Alexandria. Msukumo wake wa msingi ni shauku ya kufanya uhusiano wa Maandiko na utamaduni wa mtu au mfumo wa kifalsafa kwa mpangilio wa historia ya Biblia na/ au muktadha wa maandishi. Inatafuta uficho au kweli ya kiroho nyuma ya kila kifungu cha maandiko. Inapaswa kukubaliwa kwamba Yesu, katika Mathayo 13, na Paulo, katika Wagalatia 4, alitumia istiari kuiwasilisha kweli. Kwa hali yoyote, hii, ilikua katika muundo wa taipolojia (uanishi), na si istiari halisi.

**Uchanganuzi wa misamiati.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti ambacho kinamruhusu mtu kutambua kila muundo wa Kiyunani katika Agano Jipya. Ni mkusanyiko, katika mpangilio wa alfabeti za Kiyunani, wa kimuundo na maelezo ya msingi. Katika muunganiko kwa tafsiri mbalimbali, unaruhusu usomaji wa wasio Wayunani kuchambua visarufi vya Agano la Kale la Kiyunani kimsamiati na kimuundo.

**Ushabihiano wa Maandiko.** Hiki ni kifungu kinachotumika kueleza wazo kwamba Biblia nzima imefunuliwa na Mungu, na ni, kwa hiyo sio mkanganyiko bali ukamilifu. Ukubalifu wa dhanio hili ni msingi kwa matumizi yanayo fanana na vifungu vya maneno katika kufasiri maandiko ya biblia.

**Utata.** Hii inarejea juu ya mashaka ambayo yanaleta matokeo katika nyaraka zilizoandikwa ambapo kuna maana mbili ziwazekana au zaidi au wakati vitu viwili au zaidi vinakuwa vikirejewa kwa wakati mmoja. Inawezekana kwamba Yohana anatumia utata huu kwa makusudi.

**Elimu ihusuyo tabia ya mwanadamu.** Inamaanisha kuwa na “tabia zinazohusiana na wanadamu.” neno hili linatumika kueleza lugha zetu za kidini kumuhusu Mungu. Linatokana na neno la Kiyunani kumuhusu mwanadamu. Inamaanisha kwamba tunazungumza kuhusiana na Mungu kana kwamba Yeye alikuwa mwanadamu. Mungu anaelezwa katika umbo la mwili lionekano, kijamii, maneno ya kisaikolojia ambayo

yanahusiana na wanadamu (cf. Mwa. 3:8; II Wafalme 22: 19-23). Hii, hakika ni mshabihiano pekee. Hata hivyo maarifa yetu kumhusu Mungu, ingawa ni kweli, lakini yamewekewa mipaka.

**Shule ya Antiokia.**Hii njia ya ufasiri wa kibiblia ilianza huko Antiokia, Syria katika karne ya tatu B.K. kama kuonyesha hisia juu ya utaratibu wa kiistiari wa Alexandria, huko Misri. Msingi wa msukumo wake uliangalia maana ya kihistoria ya Biblia. Ilitafasiri Biblia kama fasihi ya kawaida ya mwaadamu. Shule hii ilikuwa imejumuishwa katika ubishi kumhusu Kristo kama alikuwa na asili mbili (mafundisho kuhusu uwili wa Yesu) au asili moja (Mungu kamili na mwanadamu kamili). Ilitambuliwa kama maoni ya kupinga Ukristo kwa Kanisa Katoriki la Rumi na kuhamishiwa Uajemi lakini shule ilikuwa na umuhimu mdogo. Misingi ya kanuni zake za ufasili wa kibiblia baadaye ikawa kanuni za ufasili wa watu walioleta mageuzi kwenye dini ya Kiprostanti (Luther and Calvin).

**Kutabaini.** Hii ni moja miongoni mwa njia tatu za uwasilishaji wa neno uliotumika kudokeza uhusiano kati ya misitari ya ushairi wa Waebrania. Unahusiana na misitari ya ushairi yenye kukinzana kimaana (cf. Mit. 10:1; 15:1).

**Fasihi ya mafunuo.** Hii ilikuwa ni namna tanzu ya Wayahudi wenye nguvu, hata kuonekana ya kipekee. Ilikuwa ni aina ya uandishi wenye mafumbo uliotumika nyakati za uvamizi na umiliki dola yenye nguvu ya Kiyahudi. Inafikiriwa kwamba mtu, muumbwaji aliyekombolewa na Mungu na kuyatawala matukio ya ulimwengu, na kwamba Israeli ina upendeleo maalumu na uangalizi kutoka Kwake. Fasihi hii inahaidi ushindi mkuu na kupitia juhudi pekee za Mungu.

Ni ishara kuu na ya ubunifu sana yenye maneno ya mafumbo. Mara nyingi ilieleza ukweli katika rangi, tarakimu, maono, ndoto, upatanishi wa kimalaika, alama za siri za maneno, mara nyingi uwili wa vitu kati ya mema na mabaya.

Baadhi ya mifano tanzu hapa ni (1)katika Agano la Kale, Ezekieli (sura ya 36-48), Danieli (sura ya 7-12), Zekaria; na (2) Katika Agano Jipya, Mathayo 24;Marko 13; II Wathesalonike 2 na Ufunuo.

**Mtetezi.**Hili linatoka katika mzizi wa neno la Kiyahudi “ulinzi wa kisheria.” Haya ni mafundisho ndani ya theolojia ambayo yanatafuta kutoa ushahidi na uwiano wa hoja za kifikra kwa imani za Kikristo.

**Haki ya kutangulia.**Kimsingi huu ni ukaribu wa maana ya neno “dhanio.” Inahusisha ufikiliaji wa wa maana za awali zilizokubalika, kanuni au nafasi iliyosadikika kuwa kweli paspo uchambuzi au uchunguzi.

**Ufuasi wa Arius.**Arius alikuwa mhudumu ndani ya kanisa huko Aexandria, Misri katika karne ya tatu na mwanzoni mwa karne ya nne. Alikubali kwamba Yesu alikuwepo hapo kabla lakini si kwa Uungu (si sawa na asili ya Baba), huenda kwa kufuata Mithali8:22-31. Alipingwa na askofu wa Alexandria, ambaye alianza (B.K. 318) mabishano yalidumu kwa miaka mingi. Ufuasi wa Arius ulikuja kuwa kanuni rasmi katika Kanisa la huko Mashariki. Baraza la Nicaea katika 325 B.K.walimshtumu Arius na kuutetea usawa na Uungu kamili wa Mwana.

**Jamii ya watu wakuu.** Alikuwa mmoja wa wanafalsafa wa kale wa Ugiriki, mwanafunzi wa Pilato na mwalimu wa Iskanda Mkuu.Ushawishi wake, hata sasa, umefika maeneo mengi yanayofundisha mafunzo ya kisasa. Hii ni kwa sababu alisistiza maarifa ni kupitia uchunguzi na upambanuzi. Hii ni moja ya itikadi ya njia za kisayansi.

**Miandiko binafsi.** Hili ni jina lililotolewa kwa maandishi ya mwanzo ya Biblia. Maandiko haya asilia yaliyoandikwa kwa mkono yote yamepotea. Baadhi tu ya nakala zimesalia. Hiki ndio chanzo cha utofauti wa maandishi mbalimbali katika machapisho ya Kiebrania na Kiyunani.

**Maandiko ya asili ya karne ya sita.** Haya ni machapisho ya Kiyunani na Kiratini ya karne ya sita B.K. Yanasanifiwa na alama “D.” Imejumuisha Injili na Matendo na baadhi ya Nyalaka za Jumla. Inabainishwa na nyongeza nyingi za maandishi yenye ueledi. Inaunda msingi wa “uundaji wa maandiko”ambayo ni tamaduni za machapisho makuu ya Kiyunani nyuma ya toleo la King James Version.

**Upendeleo.** Hili ni neno linalotumika kueleza maelezo yenye nguvu kuhusiana na jambo au mtazamo fulani. Ni mtizamo ambao uadilifu ndani yake hauwezekani kungalia kitu au maoni Fulani. Ni madhara ya kieneo.

**Mamlaka ya Kibiblia.** Ni neno lililotumika katika maana maana ya kipekee. Linaelezwa kama uelewa wa kile alichokisema mwandishi asilia katika siku zile zake na kutumia ukweli huu katika siku zetu. Mamlaka za Kibiblia mara nyingi zinaelezwa kuitazama Biblia yenyewe kama kiongozi chetu chenye mamlaka. Hata hivyo, katika hali ya sasa, utafasiri sio sahihi. Nimeweka mipaka juu a dhana ya Biblia kama ilivyotafasiriwa na kanuni za njia ya historia ya kisarufi.

**Orodha ya vitabu vya Agano Jipya.** Hili ni neno linalotumika kuelezea maandishi yanayosadikiwa kuvuviwa kipekee. Limetumika kuangalia maandiko yote ya Agano la kale na Agano jipya.

**Kristo kama kitovu.** Ni neno lililotumika kuonyesha Kristo kama kitovu cha mambo yote. Na lilitumiwa kuunganisha dhana ya kwamba Yesu ni Bwana wa Biblia zote, Mawazo ya Agano la Kale dhidi yake na utimilifu wa malengo yake.

**Fasiri.** Hii ni aina pekee ya utafiti wa kitabu. Inatoa kwa pamoja usuli wa kitabu cha Biblia. Pia inajaribu kuelezea maana ya kila kipengele cha kitabu. Baadhi inatazamisha matumizi, wakati mwiingine zinahusiana na andiko katika hali ya kiufundi. Vitabu hivi ni vya manufaa, lakini lazima vitumike baada ya mtu kufanya uchunguzi wake wa awali. Tafasiri za watoa maoni lazima zisikubalike kuhakiki. Ukilinganisha fasiri nyingi toka kwa mitizamo ya wanathiolojia tofauti utaona inasaidia.

**Itifaki.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti kwa usomaji wa Biblia. Inaorodhesha kila utokeaji wa neno katika Agano Jipya na la Kale. Inasaidia katika njia tofauti: (1) kubainisha maneno ya Kiebrania au Kiyunani yaliyoko nyuma ya maneno ya kiingereza: (2) kulinganisha kurasa ambapo neno lile lile la Kiebrania au Kiyunani limetumika: (3) kuonyesha mahali ambapo maneno mawili tofauti ya Kiebrania au Kiyunani yametafasiriwa kwa neno lie lile la kiingereza: (4) kuonyesha mwendelezo wa kutumia maneno fulani katika vitabu fulani au maandishi: (5) inasaidia mtu kupata somo katika Biblia (cf. Walter Clark's *How to use New Testament Greek Study Aids*. kurasa za 54-55).

**Magombo ya Bahari ya Chumvi.** Inarejerea mlolongo wa maandiko ya kale yaliyoandikwa katika Kiebrania na Kiarama ambayo yalipatikana karibu na Bahari ya Chumvi mwaka 1947. Palikuwepo na maktaba za kidini ya Kiyunani ya karne ya kwanza. Msukumo wa umilikaji toka Rumi na vita ya kinazi vya miaka ya sitini viliwasababisha wao kuficha magombo yaliyokuwa yamefungashwa ndani ya vyungu kwenye mapango au mashimo. Inatusaidia sisi kuelewa muundo wa kihistoria wa palestina ya karne ya kwanza na kuthibitisha maandiko ya mossorettes kuwa yako sahihi kwa kiasi fulani enzi ya awali kabla ya Yesu B.C.

**Mambo yaliyofasiliwa.** Njia hii ya kimantiki au ufikiliaji inatokana na kanuni ya pamoja ya matumizi maalumu kwa njia ya wazo. Hii ni kinyume toka ufikiliaji wa mambo yaliyofasiriwa, ambayo yanaangazia njia ya kisayansi toka kwenye uchunguzi maalumu kwenda hitimisho la pamoja (nadharia)

**Mbinu pembuzi.** Hii ni njia ya kufikilisha ambapo kile kinachoonekana kuleta mkanganyiko au mafumbo huwekwa pamoja katika hali ya mkazo, ikitafuta jibu la pamoja ambalo linajumuisha pande zote za fumbo. Mafundisho mengi ya Biblia yana upembuzi unaofanana, kuamuliwa kabla-mapenzi huru, ulinzi-ustahimilivu, imani-kazi; uwamuzi-ufuasi; uhuru wa Mkristo-uwajibikaji wa Mkristo

**Wayahudi waliotawanyika katika mataifa mengine.** Hili ni neno la kiufundi la Kiyunani lililotumiwa na wapalestina wa Kiyahudi kuelezea wayahudi wengine walioishi nje ya mipaka ya kijiografia ya nchi ya ahadi.

**Mlinganyo wa nguvu.** Hii ni nadhalia ya ufasili wa Biblia. Tafasili ya Biblia inaweza kuangaliwa kama mwendelezo toka ushirika wa "neno kwa neno", mahali ambapo neno la Kiingereza lazima liwekwe kwa kila neno la Kiyunani au Kiebrania, kwenye "ufasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa angalizo la chini ya neno au kifungu cha awali.

Katika nadharia hizi mbili ndipo pana “mlinganyo wa nguvu” unaojaribu kuchukua neno la mwanzo kwa umakini wake, lakini limefasiliwa katika miundo ya visarufi vya kisasa na nahau. Majadiliano mazuri ya kweli ya hizi nadharia mbali mbali za fasili zinapatikana katika makala ya Fee na Stuart *How to Read the Bible For Its Worth*, uk. 35 na katika Robert Bratcher’s utangulizi katika Biblia ya TEV.

**Kutofuata mfumo.** Neno hili linatumika katika mahusiano ya uhakiki wa maandiko. Unarejerea kitendo cha kuchagua usomaji toka machapisho tofauti tofauti ya Kiyunani ili kufika kwenye neno linalotakiwa kuwa karibu na maandiko ya mwanzo.

**Kupotosha maana.** Hili neno ni kinyume cha neno fasili ya maandiko. Kama fasili ya maandiko ni “kuondoa” kulingana na kusudio la mwandishi wa awali, basi neno hili litamaanisha “kuingiza” wazo la kigeni.

**Elimu ya asili na historia ya neno.** Hii ni dhana ya usomaji wa neno unaojaribu kuyakinisha maana ya awali ya neno. Kutokana na chanzo cha maana hii, utumiaji wa kipekee unaotambulika kirahisi katika ufasili, elimu ya asili na historia ya neno sio kiini cha mtizamo, mbali na maana ya wakati ule ule na utumiaji wa neno.

**Fasili ya maandiko.** Hili ni neno la kiufundi kwa utendaji wa kutafasili kifungu maalumu. Inamaanisha “uondoaji nje” (wa neno) ukidokeza kwamba dhumuni letu ni kuelewa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika uelewa wa muundo wa kihistoria, mazingira ya kifasihi, sintaksi na maana ile ile ya neno.

**Namna ya Uwasilishaji.** Hili ni neno la Kifaransa ambalo limedokeza aina mbali mbali ya fasihi. Msukumo wa neno hili ni mgawanyiko wa miundo ya fasihi katika namna mbali mbali ambazo zinashirikishana tabia za aina moja. Usimuliaji wa kihistoria, mashairi, mithali, ufunuo na uandikishaji.

**Maarifa ya utambuzi/mafunuo.** Zaidi ya maarifa tulionayo kuhusu imani potofu yameletwa toka maarifa ya utambuzi wa maandiko katika karne ya pili. Ingawa mawazo ya awali yalikuwepo katika karne ya kwanza (na kabla). Baadhi ya maelezo ya mafunuo ya kinazi ya Valentino na Cerinthin ni (1) mwili na roho vyote vilikuwepo kabla. mwili ni mwovu, na Roho ni nzuri. Mungu, ambaye ni Roho hawezi kuhusishwa moja kwa moja na mwili mwovu (2) kuna asili (*eons au* daraja la kimalaika) kati ya Mungu na mwili. Wa mwisho au wa chini alikuwa YAHWE wa Agano la kale, ambaye aliuumba ulimwengu (*kosmos*); (3) Yesu alikuwa mwanzilishi kama YAHWE lakini akiwa juu ya viwango, karibu na Mungu wa kweli. Wengine walimweka juu zaidi lakini bado yu chini kuliko Mungu na hakika asiye na mwili wa Kiungu (cf. 1:14). Kwa vile mwili ni mwovu, Yesu asingelikuwa na mwili wa kibinadamu na bado akawa na hali ya Kiungu. Alikuwa ni nafsi ya kufikirika (cf. 1Yoh 1:1-3; 4:1-6); na (4) wokovu ulipatikana kupitia imani katika Yesu pamoja na maarifa maalumu, yaliyojulikana na watu maalumu. Maarifa (maneno ya siri) yalihitaji kupitia ulimwengu wa kimbingu. Washikiliaji sana wa kisheria za Kiyahudi nao pia walihitaji kumfikia Mungu. Walimu wa uongo wenye maarifa ya utambuzi walitetea miundo miwili kinzani ya kimaadili (1) baadhi ya stadi za maisha hazikuhusiana na wokovu. Kwao wokovu na utakaso ulifumbwa kwenye maarifa ya siri (neno la siri) kupitia ulimwengu wa kimalaika (*eons*); au (2) kwa wengine stadi ya maisha ilikuwa muhimu katika wokovu. Walisisitiza miundo ya maisha kama kielelezo cha utakaso wa kweli.

**Kanuni za ufasili.** Hili ni neno la kiufundi kwa kanuni zinazoongoza ufasili wa maandiko. Ni seti ya mwongozo maalumu na sanaa/kipawa. Kibiblia, au takatifu, kanuni za ufasili zimegawanyika kwa namna mbili; kanuni za ujumla na kanuni maalumu. Hizi zinahusiana na aina tofauti za fasihi zinazopatikana katika Biblia. Kila aina tofauti (tanzu)zina mwongozo wake wa kipekee lakini zinashirikiana na baadhi ya dhana na namna ya utafasili.

**Uhakiki juu ya maandiko.** Hii ni namna ya utafasili wa kibiblia ambao unatazamisha kwenye muundo wa kihistoria na umbo la fasihi hasa hasa katika kitabu cha Biblia.

**Nahau.** Neno hili linatumika kwenye vifungu vinavyopatikana katika tamaduni tofauti zenye maana maalumu na sio vilivyohusiana na maana ya kawaida ya maneno binafsi. Maana ya mifano ya kisasa ni: “ilikuwa ni vizuri sana” au “umeniua”. Biblia pia inajumuisha aina hizi za vifungu.

**Nuru.**Hili ni jina lililotolewa kwenye dhana kuwa Mungu aliongea na mwanadamu. Dhana nzima kwa kawaida imeelezwa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda kwenye historia ya binadamu: (2) uvuvio-ametoa utafasili sahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) nuru –ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Kudukiza.** Hii ni njia ya kimantiki au kufikiria inayotoka sehemu Fulani na kuenea sehemu yote. Ni njia ya kutegemea majaribio ya kisasa. Kimsingi, huu ni mjongeo wa watu wenye hadhi ya juu.

**Unasaba.** Hii ni aina ya chombo cha uchunguzi kinachoruhusu wale wasiojua lugha za kibiblia kuchunguza maana yake na muundo. Inaweka tafasili ya kiingereza kwenye ngazi ya neno kwa neno chini ya lugha ya awali ya kibiblia. Chombo hiki kinajumuishwa na “misamiati ya kiuchunguzi” ambayi inatoa miundo na maelezo ya msingi ya Kiebrania na Kiyunani.

**Uvuvio.**Hii ni dhana ya kwamba mungu aliongea na mwanadamu kwa kuwalinda waaandishi wa kibiblia kwa usahihi na uwazi ili kuweka kumbukumbu ya mafunuo yake. Dhana nzima imeelezwa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) uvuvio-ametoa utafasiri wasahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu Fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) Nuru-ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Lugha ya maelezo.** Hii inatumika pamoja na nahau pale Agano la Kale lilipoandikwa. Inaongelewa juu ya dunia kwa namna jinsi vitu vinavyotokea kwenye milango mitanmo ya fahamu. Sio maelezo ya kisayansi hata yakamaanisha kuwepo.

**Ushikiliaji sana wa sheria.** Mwenendo huu umeainishwa kwa msisitizo zaidi juu ya sheria au matambiko. Unajaribu kutegemea juu ya utendaji wa mwanadamu kama njia ya ukubalifu kwa Mungu. Unajaribu kushusha uhusiano na kuinua utendaji, mwote ambamo dhana muhimu ya mahusiano ya kimaagano kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu mtenda dhambi.

**Tafasili sisisi.** Hili ni jina jingine la mlengo wa kimaandiko na njia za kihistoria za za kanuni za ufasili toka Antiokia. Ina maana kwamba utafasili unahusika katika maana dhahili za lugha ya mwanadamu, ingawa inaendelea kutambua uwepo wa lugha za kitamathali.

**Fasihi tanzu.** Hii inarejerea kwenye miundo ya utofauti ili kwamba mawasiliano ya uwanadamu yanaweza kuchukuliwa kama vile ushairi au simulizi za kihistoria. Kila aina ya fasihi ina nji/namna yake maalumu ya kanuni ya ufasili kwa kuongezea kwenye kanuni za pamoja kwa fasihi zote zilizoandikwa.

**Sehemu ya fasihi.** Hii inarejerea mgawanyo wa lengo kuu la kitabu cha Kibiblia. Inaweza kuundwa na misitari, aya, au ibara chache. Ni kijumuishi pekee chenye kiini cha somo.

#### **Lower criticism- Uhakiki wa kawaida wa maandiko.**

**Maandiko ya asili.** Neno hili linahusiana na nakala mbali mbali za Agano jipya la Kiyunani. mara nyingi limegawanyika katika aina tofauti kwa (1) nyenzo iliyotumika kuandikiwa kwayo (mafunjo, ngozi) au (2) muundo wenyewe wa uandishi. Limefupishwa kwa neno “MS” (umoja) au “MSS” (wingi).



**Andishi la kidesturi la Kiebrania la Biblia ya Kiyahudi.** Hii inarejerea karne ya nane A.D. maandiko ya asili ya Kiebrania ya Agano la kale yalitolewa na vizazi vya wasomi wa Kiyahudi ambayo yalijumuisha alama za irabu na mihtasari mingine ya maandiko. Yanatengeneza msingi wa neno kwa Agano letu la kale la Kiingereza.

**Mshabihiano wa neno.** Huu ni namna ya msembo ambao jina la kitu linatumika mbadala wa kitu kingine kinachofanana nacho. Kwa mfano “ birika linachemka” ki uhalisia inamaanisha “maji yaliyeko kwenye birika yanachemka”.

**Orodha ya vitabu vya Agano jipya.** Hii ni orodha ya vitabu vya sheria za kanisa la Agano jipya. Iliandikwa huko Rumi kabla ya mwaka 200 A.D. Inatoa vitabu ishirini na saba kama vile vile vya Agano Jipya la Waporostanti. Hii wazi kabisa inaonyesha makanisa madogo madogo ya mahali katika sehemu mbali mbali za milki ya Rumi kulikuwa “kiutendaji” pamewekwa sheria za kanisa kabla ya baraza kuu la kanisa la karne ya Nne.

**Ufunuo wa asili.** Hii ni namna ya Mungu mwenyewe kujifunua kwa mwanadamu. Unajumuisha utaratibu wa kiasili (Rum 1:19-20) na dhamila adilifu (Rum 2:14-15). Umeongelewa katika Zaburi 19:1-6 na Warumi 1-2. Umatofautishwa toka kwenye mafunuo maalumu, ambayo kwa mungu mwenyewe ni muhimu kujifunua katika Biblia na mwanae pekee Yesu wa Nazareti. Uangaliaji huu wa kithiolijia unasisitizwa tena na mwenendo wa “dunia ya zamani” kati ya wanasayansi wa Kikristo (cf. maandishi ya Hagh Ross) wanatumia uangaliaji huu kwa kuthibitisha kuwa kweli yote ni kweli ya Mungu. Ulimwengu ni mlango ulio wazi wa maarifa ya kumjua Mungu; ni tofauti toka kwa ufunuo maalumu (Biblia); unawapa wanasayansi uhuru wa kufanya uchunguzi juu ya utaratibu wa kiasili. Kwa maoni yangu , hii ni fursa mpya ya ajabu kushuhudiwa juu ya wanasayansi wa ulimwengu wa magharibi.

**Ufuasi wa Nestory.** Nestory alikuwa ni mkuu wa familia ya Constantino kwenye karne ya tano. Alifundishwa huko Antiokia ya Syria na kuthibitisha kwamba Yesu ana asili mbili, moja ni mwanadamu kamili na nyingine ni Mungu kamili. Maoni haya yalichepushwa toka kwenye mtazamo wa asili wa mtu mmoja wa Orthodox kutoka Alexandria. Kusudio kubwa la Nestory lilikuwa ni cheo cha “mama wa Mungu” alichopewa Maria Magdalena. Nestory alipingwa na Cylil wa Alexandria na, kwa kuwekwa matatani juu ya mafundisho yake huko Antiokia. Antiokia yalikuwa makao makuu ya mtazamo wa kihistoria wa visarufi vya maandiko kwa utafasili wa Kibiblia, wakati Alexandria yalikuwa makao makuu ya shule Nne zilizotengwa kwa ajili ya utafasili. Nestory hatimaye aliondolewa toka ofisini na kukimbilia mafichoni.

**Mwandishi wa awali.** Hii inarejerea wandishi halisi wa maandiko

**Mafunjo/Magombo.** Haya yalikuwa aina mojawapo ya nyenzo toka Misri zilizotumika kuandikiapo maandiko. Yalitengenezwa kwa majani au magome ya miti. Ni nyenzo ambazo nakala za zamani Agano la Kale la Kiyunani zilihifaziwapo.

**Vifungu Mlinganyo.** Ni sehemu ya mtazamo kuwa yote yaliyomo kwenye Biblia yametoka kwa Mungu na, kwa hiyo, ni ufafili wake mahsusi na mlinganyo wa kweli wa kimafumbo. Hili pia ni la msaada pale mtu anapojaribu kutafasili kifungu kisicho wazi au kigumu. Pia inamsaidia mtu kupata kifungu kilicho wazi juu ya somo husika vile vile mtazamo wote wa kimaandiko juu ya somo husika.

**Ufafanuzi/fasili.** Hili ni jina la nadhalia ya utafali wa Biblia. Utafasili wa Biblia unaweza kuangaliwa kama mwendelezo wa mahusiano wa “neon kwa neon” ambapo neon la Kiingereza laweza kuweka kwa kila neon la Kiebrania au Kiyunani kwenye “fasili” ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa mtazamo wa kawaida wa neon au kifungu cha awali. Kati ya nadhalia mbili hizi “mlinganyo wa nguvu” ambao unajaribu kuchukuawa kwa umakini andiko la awali lakini likatafasiliwa katika muundo wa kisasa wa kisarufi na nahau. Kweli kabisa mjadara mzuri wa nadhalia hizi mbali mbali za utafasili zinapatikana katika chapisho la Fee na Stuart *How to Read the Bible For All Its Worth, Uk. 35.*

**Aya.** Huu ni msingi wa ufasili wa fasihi moja kinadhania. Unajumuisha wazo moja kuu na mwendelezo wake. Tukibaki na musukumo wake mkuu hatutatazama juu ya udogo wake au uzuri wa kusudi la mwandishi wa awali.

**Uparokia.** Hii inahusiana na mapendeleo yaliyofungiwa kwenye muundo wa tamaduni/ thiolojia ya kawaida. Haitambui asili ya mapokeo ya kweli yaliyobadilika ya Kibiblia au matumizi yake.

**Fumbo.** Hii inarejerea kweli zile zinazoonekana kuleta mkanganyiko, nab ado zote zikabaki kuwa kweli, ingawa bado zinakinzana. Zinaunda kweli kwa kuwakilisha toka pande zilizo kinyume. Kweli nyingi za Kibiblia zinawakilishwa kimafumbo (au kiupembuzi). Kweli za Kibiblia sio kama nyota zilizotengana, zimetengenezwa kwa ukilimio wa sehemu za nyota.

**Pilato.** Alikuwa ni mmoja ya wanafalsafa wa Ugiriki ya kale. Falsafa yake kwa kiasi kikubwa ulisababisha kanisa la mwanzo kupitia wasomi wa Alexandria, Misri na baadaye, Augustino. Alituma ujumbe kuwa kila kitu duniani ni kiini macho na ni mfano tu wa kielelezo asili wa vitu vya rohani. Baadaye wanathiolojia wakasawazisha “mtizamo/mawazo” ya Pilato na ulimwengu wa kiroho.

**Dhanio.** Hili linarejerea uelewa wa jambo tulilowaza kabla. Mara nyingi tunaunda wazo au hukumu kuhusu mambo hata kabla hatujatazamisha maandiko yenyewe. Uelekezaji huu vile vile hujulikana kama upendeleo, kujitanguliza mbele, kudhania au kuelewa kabla.

**Uhakiki wa maandishi.** Hiki ni kitendo cha kutafasili maandiko kwa nukuu za kifungu bila kuangalia mazingira ya haraka au ukubwa wa mazingira katika fahisi moja. Hii inaondoa vifungu toka kwa kusudio la mwandishi wa awali na mara nyingi unahusha jaribio la kuhakiki maoni binafsi wakati huo likithibitisha mamlaka ya Kibiblia.

**Ualimu wa dini ya Kiyahudi.** Ngazi hii ya maisha ya watu wa Uyahudi yalianza walipokimbilia Babel (586-538 B.C). kama ushawishi wa makuhani na hekalu ulivyoondolewa, masinagogi ya kawaida yakawa mtizamo wa maisha ya Kiyahudi. Hivi vitovu vya kawaida vya tamaduni za Kiyahudi, ushirika, kuabudu na elimu ya Biblia ikawa mtizamo wa maisha ya kidini kitaifa. Katika siku za Yesu, hii “dini ya wandishi” ilikuwa sambamba na ile ya makuhani. Katika kuanguka kwa Yerusalemu mwaka wa 70 A.D muundo wa kiandishi, ukitawaliwa na mafalisayo, walidhibiti mwelekeo wa maisha ya kidini ya Kiyahudi. Inachagizwa na utafasili wa kiutendaji, na wa kisheria wa Torah kama ulivyoielezwa katika tamaduni za Talmud.

**Ufunuo.** Hili ni jina lililopewa kwenye dhana ya kwamba Mungu amesemazana na mwanadamu. Wazo zima mara nyingi limeelezewa katika maneno matatu- (1) Ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) Uuvio-Ametoa tafasili sahihi ya matendo yake na maana yake kwa mtu Fulani aliyemchagua kuweka kumbukumbu ya mwanadamu (3)Nuru-Amempa Roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa ukaribu wake.

**Elimu-maana.** Hii imerejerea kipimo halisi cha maana kinachohusiana na neno. Kimsingi ina vidokezo mbali mbali vya neno katika mazingira tofauti.

**Maandiko ya kale ya Kiyunani.** hili ni jina lililopewa tafasili ya Kiyunani ya Agano la kale la Kiebrania. Mafundisho ya zamani yanasema kuwa yaliandikwa kwa siku 70 na wasomi sabini wa Kiyahudi kwa ajili ya maktaba ya Alexandria, Misri. Tarehe ya kimapokeo ilikuwa 250 B.C (kiukweli yawezekana ilichukua zaidi ya miaka Mia kumaliza kuandika). Tafasili hii ni muhimu kwa sababu (1)inatupatia andiko la kale kulinganisha na andiko la Kiebrania (2) inatuonyesha sisi hali ya utafasili wa Kiyahudi katika karne ya pili na tatu B.C (3) inatupatia uelewa wa umasihi wa Kiyahudi kabla ya kumkataa Yesu. Kifupi chake ni “LXX”.

**Machapisho ya asili.** Haya ni machapisho ya asili ya Kigiriki ya karne ya Nne A.D. Yalivumbuliwa na msomi wa Kijerumani, Tischendorf, katika nyumba ya mtawa Catheline, kwenye eneo la kimila la mlima Sinai. Maandishi haya yameundwa na herufi ya kwanza ya Kiebrania ya alfabeti inayoitwa “*eleph*” (Ϝ). Yanajumuisha Agano la Kale na Agano Jipya kwa pamoja.

**Kujitakasa.** Hili neno ni kisawe chenye istiari katika maana kuwa linakwenda mpaka kwenye historian a mazingira ya fasihi ya kifungu na kulifasili katika msingi wa jambo lingine.

**Visawe.** Hii inarejerea maana yenye kariba au mfano wa maana moja (ingawa kiukweli hakuna maneno mawili yenye elimu-maana kamili iliyopishana). Kwa karibu sana yanahusiana kiasi kwamba moja linaweza kuwa mbadala wa lingine katika sentesi bila kupoteza maana. Pia yanatumika kuunda moja kati ya miundo mitatu ya mlinganyo wa ushairi wa Kiebrania. Kwa maana hii inarejeshwa mistari miwili ya ushairi ambayo inaelezea kweli ile ile (cf. Zab 103:3).

**Sintaksi.** Hili ni neno la Kiyunani linalirejeresha muundo wa sentesi. Inahusiana na namna ya sehemu ya sentesi zinaweza wekwa pamoja kuleta maana kamili.

**Usanisi.** Hii ni moja ya maneno matatu yanayohusiana na aina ya ushairi wa Kiebrania. Neon hili linaongelea juu ya mistari ya ushairi uluojengwa juu ya mwingine katika maana moja, wakati mwingine huitwa “taaluma ya mabadiliko ya hali” (k.v. Zab 19:7-9).

**Thiolojia mpangilio.** Hii ni hatua ya utafasili ambayo inajaribu kuhusisha ukweli wa Biblia katika hali ya pamoja na mlingano. Ina mantiki zaidi kuliko historia tupu, ni uwasilishaji wa thiolojia ya Kikristo kwa namna ( Mungu, mtu, dhambi,wokovu).

**Buku la taratibu na kanuni za Kiyahudi.** Ni wadhifa uliokuwapo kwa ajili ya upangaji wa simulizi za kanuni na taratibu za Kiyahudi. Wayahudi wanaamini ulitolewa kwa Musa kwa kusimuliwa na Mungu kwenye mlima Sinai. Ki-ukweli inaelekea kuwa ni mkusanyiko wa hekima za walimu wa Kiyahudi kwa miaka mingi. Kuna matoleo mawili tofauti yaliyo andikwa juu ya Talmud: ya Babel na fupi la kiparestina ambalo halikwisha.

**Uhakiki wa tofauti za kiuandishi.** Huu ni usomaji wa maandiko wa Biblia. uhakiki wa maandiko ni muhimu kwa sababu hakuna maandiko ya mwanzo yaliyopo na nakala zilizopo zinatofautiana toka moja hadi nyingine. Unajaribu kuelezea utofauti na kufika (karibu iwezekanavyo) na maneno ya awali kabisa ya miandiko ya Agano la kale na jipya. Mara nyingi unaitwa “uhakiki wa asili ya neno”.

**Upokeaji wa Maandiko.** Usanifishaji huu ulianza kwenye toleo la Elzevir la Agano jipya la Kiyunani katika mwaka wa 1633 A.D. Kimsingi ni muundo wa Agano jipya la Kiyunani lililozalishwa toka kwenye maandiko machache ya asili ya Kiyunani na matoleo machache ya Erasmo ya Kilatini (1510-1535), Stephano (1546-1559) na Elzevir (1624-1678). Katika *An Introduction to the Textual Criticism of The New Testament uk. 27 cha A.T Robertson* anasema “andiko la Byzantine kiutendaji ni aina ile ile ya uundaji wa maandiko. Andiko la Byzantine ni la thamani ya chini kati ya familia tatu ya maandiko ya awali ya Kiyunani (Kimagharibi, Alexandria na Byzantine). Inajumuisha mkusanyiko wa makosa ya karne nyingi za maandiko na nakala za mkono. Hata hivyo, A.T Robertson alisema uundaji wa maandiko umetunza kwa ajili yetu andiko sahihi kimalidhawa (uk.21). Mapokeo haya ya maandiko ya asili ya Kiyunani (hasa Erasmo, toleo la tatu la 1522) yanatengeneza msingi wa toleo la King James la mwaka 1611 A.D.

**Sheria za Musa.** Hili ni neno la Kiebrania lenye maana ya “ufundishaji”. Lilitokea kuwa wadhifa rasmi wa maandishi ya Musa (Mwanzo mpaka Kumbu kumbu la Torati). Kwa Wayahudi ulikuwa ni mgawanyo wa kimamlaka wa kanuni za kanisa la Kiebrania.

**Uanishaji.** Hii ni aina ya urasimishaji wa wa utafasili. Mara nyingi unahusisha kweli ya Agano jipya inayopatikana katika vifungu vya kale kwa njia ya analojia. Namna hii ya kanuni za ufasili ilikuwa ni dalili kubwa ya njia za Alexandria. Kwa sababu ya matukano ya aina hii ya utafasili, mtu lazima aweke ukomo wa matumizi yake kwa mfano mahsusi ulioandikwa katika Agano jipya.

**Maandiko ya Vatican.** Haya ni maandiko ya asili ya Kiyunani ya karne ya Nne A.D . Yalipatikana kwenye maktaba ya Vatican. Uwasili wake unajumuisha vitabu vyote vya Agano la kale, ufunuo na Agano jipya. Hata hivyo, sehemu

zingine zilipotea( Mwanzo, Zaburi, Waebrania, Filemon na Ufunuo). Inasaidia maandiko ya asili kubadilisha miandiko ya maneno ya awali. Tena yameundwa kwa herufi kubwa “B”.

**Tafasili ya Biblia ya Kilatini.** Ni jina la tafasili ya Biblia ya Kilatini ya Jerome. Ilikuwa ndio msingi au utafasili wa “kawaida” wa kanisa Katoriki la Rumi. Lilifanyika mwaka 380 A.D.

**Hekima ya Fasihi.** Hii ni fasihi tanzu iliyozoeleka enzi za kale karibu na pande za Mashariki (na ulimwengu wa kisasa). Kimsingi lilikuwa ni jaribio la kuelekeza kizazi kipya juu ya mwongozo wa maisha ya ushindi kupitia ushairi, mithali, au insha. Ilielezwa zaidi kwa watu binafsi kuliko kwenye jumuiya iliyongana. Haikutumia viini macho kuweka historia, lakini ilisimamia uzoefu na uchunguzi wa maisha katika Biblia, Ayubu kupita Wimbo ulio Bora, anasadiki uwepo na ibada ya YAHWE, lakini mtizamo huu wa ulimwengu wa kidini sio wa wazi kwa uzoefu wa kila mtu kila wakati.

**Picha ya ulimwengu na Mtizamo wa Kidunia.** Haya ni maneno mwandani. Yote yana dhana ya kifalsafa kuhusiana na uumbaji. Neno “picha ya ulimwengu” inarejerea “kwa namna gani” juu ya uumbaji wakati “mtizamo wa kidunia” unahusiana na “nani.” Maneno haya yote ni muhimu kwenye utafasili pale mwanzo 1-2 inaposhughulika hasa hasa na nani, na sio kwa namna gani juu ya ulimwengu.

**YAHWE/YEHOVA.** Hili ni jina la Agano la Mungu katika Agano la kale. Linaelezwa katika kitabu cha Kutoka 3:14. Ni muundo wa KISABABISHAJI wa neno la Kiebrania “kuwa” ambalo Wayahudi waliogopa kulitamka jina hili ili wasilitamke bure; kwa hiyo, walitumia jina lingine badala yake yaani “Adonai” likimaanisha “Bwana”. Hivi ndivyo jina la Agano limetafasiliwa katika Kiingereza.

## MAELEZO YA KIMAFUNDISHO YA BOB

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtasari mfupi wa thiolojia yangu kama ufuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neon la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu (Angalia [MADA MAALUM: UVUVIO\[SPECIAL TOPIC: INSPIRATION\]](#)). Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake (Angalia [Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukombozi \(Special Topic: YHWH's Eternal Redemptive Plan\)](#)). Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, uumbaji na ukombozi (Angalia [MADA MAALUM: UWEPO WA MUNGU MMOJA \(SPECIAL TOPIC: MONOTHEISM\)](#)). Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhahilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendelea. Amejidhahilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja (Angalia [MADA MAALUM: UTATU\(SPECIAL TOPIC: TRINITY\)](#)).
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa ndani wa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo (Angalia [Majaaliwa \(Calvinism\) Dhidi Ya Mapenzi Huru Ya Kibinadamu \(Arminianism\) Predestination \(Calvinism\) vs Human Free Will \(Arminianism\)](#)).
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada (Angalia [MADA MAALUM: UOVU BINAFSI \(SPECIAL TOPIC: PERSONAL EVIL\)](#)). Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana Tazama [Mada Maalum:Ina Maana Gani "Kupokea" "Kusadiki" "Kukiri/Kutubu" na "Kusihi"? \(Special Topic: What Does It Mean to "Receive," "Believe," "Confess/Profess," and "Call Upon"?\)](#)
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini([Mada Maalum: "Kuamini" Katika Agano Jipya\(Special Topic: "Believe" in the NT\)](#))katika Kristo na toba toka dhambini ([MADA MAALUM: TOBA\[AGANO JIPYA\] SPECIAL TOPIC: REPENTANCE \(NT\)](#)) Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.

8. Roho Mtakatifu ni “Yesu mwingine”(Mada Maalum: Yesu na Roho(Special Topic: Jesus and the Spirit) Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.
9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa kweli ya Mungu wataatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake. Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

“Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo.